طبقات ورثة الأنبياء

الجزء الاول

تجميع وانتاج

المستكشف أبومنال دانا

TABAQAT WARATHAT AL ANBIYAI

JUZU'U AL AWWAL

MATABAKA YA WARITHI WA MITUME

JUZUU YA KWANZA

المستكشف ابو منال دانا

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

KIMETAYARISHWA NA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Muharram 1444 A.H - 2022 C.E

المستكشف ابو منال دانا

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

طبقات ورثة الأنبيـاء

الجزء الاول

تجمع وانتج
المستكشف ابو منال دان

TABAQAT WARATHAT AL ANBIYAI - JUZUU AL AWWAL.

MATABAKA YA WARITHI WA MITUME - JUZUU YA KWANZA.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kimetayarishwa Na Kukusanywa Na Al Mustakshif Abu Manal Danah.
1444 A.H – 2022 C.E

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُواْ فِى ٱلْمَجَٰلِسِ فَٱفْسَحُواْ يَفْسَحِ ٱللَّهُ لَكُمْ وَإِذَا قِيلَ ٱنشُزُواْ فَٱنشُزُواْ يَرْفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ مِنكُمْ وَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْعِلْمَ دَرَجَٰتٍ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo idha qeela lakum tafassahoo fee almajalisi faifsahoo yafsahi Allahu lakum wa-idha qeela onshuzoo faonshuzoo yarfaAAi Allahu alladheena amanoo minkum waalladheena ootoo alAAilma darajatin waAllahu bima taAAmaloona khabeerun *(Surat Al Mujaddila 58:11)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini pale mnapoambiwa kua muache nafasi kwenye mikusanyiko yenu basi acheni nafasi, kwani Allah atakupeni Nafasi kubwa (kutoka kwenye rehma zake) na mnapoambiwa kua mnyanyuke (kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala kiibada) basi Nyanyukeni, kwani Allah atawapandisha Walioamini miongoni mwenu na (atawapandisha darja) wale ambao wamepewa Ilm, na Allah ni mwenye habari juu ya kila mnachokifanya.***

Na akasema tena *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿ثُمَّ أَوْرَثْنَا ٱلْكِتَٰبَ ٱلَّذِينَ ٱصْطَفَيْنَا مِنْ عِبَادِنَا فَمِنْهُمْ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهِۦ وَمِنْهُم مُّقْتَصِدٌ وَمِنْهُمْ سَابِقٌۢ بِٱلْخَيْرَٰتِ بِإِذْنِ ٱللَّهِ ذَٰلِكَ هُوَ ٱلْفَضْلُ ٱلْكَبِيرُ﴾

Thumma awrathna alkitaba alladheena istafayna min AAibadina faminhum *dha*limun linafsihi waminhum muqtasidun waminhum sabiqun bialkhayrati bi-idhni Allahi dhalika huwa alfadhlu alkabeeru *(Surat Fatir 35:32)*

Tafsir: **Na kisha tukawarithisha Kitabu (Qur'an) wale ambao tuliowachagua miongoni mwa waja wetu (katika *Ummah wa Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam*). Na kisha kuna waliojidhulumu nafsi zao, na kuna wanaofuata msimamo wa kati na kuna wale ambao kwa idhini ya Allah ni wenye kukimbilia kufanya mema. Hio ni fadhila kubwa sana**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na kama alivyosema Imam At Tirmidhii katika Hadith kua:

عن أبي الدرداء رضي الله عنه عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: «مَنْ سَلَكَ طَرِيقا يَبْتَغي فيه عِلْما سَهَّل الله له طريقا إلى الجنة، وإنَّ الملائكة لَتَضَعُ أَجْنِحَتها لطالب العلم رضًا بما يَصنَع، وإنَ العالم لَيَسْتَغْفِرُ له مَنْ في السماوات ومَنْ في الأرض حتى الحيتَانُ في الماء، وفضْلُ العالم على العَابِدِ كَفَضْلِ القمر على سائِرِ الكواكب، وإنَّ العلماء وَرَثَة الأنبياء، وإنَّ الأنبياء لم يَوَرِّثُوا دينارا ولا دِرْهَماً وإنما وَرَّثُوا العلم، فَمَنْ أَخَذَهُ أَخَذَ بحَظٍّ وَافِرٍ

Amesema Abu Darda *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **‘Mtu mwenye kufuata njia ya kutafuta Ilm ya Dini, basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* atamrahisishia njia ya Peponi, na Malaika nao wanamtanulia mbawa zao chini ya Miguu ya wenye kutafuta Ilm ya Dini kuonesha furaha kutokana na njia aliyoifuata. Viumbe wote Mbinguni na Ardhini, hata Samaki Baharini hua ni wenye kumuombea Maghfira mwenye kutafuta Ilm. Kwani utukufu wa Mwanazuoni dhidi ya mwenye kufanya Ibada hua ni sawa na Ukubwa wa Mwezi dhidi ya Nyota zote. Na bila ya shaka Wanazuoni ni warithi wa Mitume. Kwani Mitume hawakuacha kitu kama Dhahabu au Fedha bali wamewacha Ilm, Hivyo atakaeipata basi hua amepata sehemu ya kitu kikubwa sana.’**
(Imam At Tirmidhii, Imam Ibn Majah)

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

UTANGULIZI

Alhamd Lillahi Rabbi Al Alamiin, wa salatu wa salamu Aala Ashrafi Al Anbiyai wa Al Mursalin Sayyidna Muhamamd Salallahu Alayhi wa Salam wa Aala Alihi wa As-habihi ajmaAin, wa Al Awliyaa wa Al Salihiin wa aAla Jamii Aibadi Al Muuminin... Aama baad!

عَنْ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ أَبِي حَفْصٍ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يَقُولُ:

" إنَّمَا الْأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ، وَإِنَّمَا لِكُلِّ امْرِئٍ مَا نَوَى، فَمَنْ كَانَتْ هِجْرَتُهُ إلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ فَهِجْرَتُهُ إلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ، وَمَنْ كَانَتْ هِجْرَتُهُ لِدُنْيَا يُصِيبُهَا أَوْ امْرَأَةٍ يَنْكِحُهَا فَهِجْرَتُهُ إلَى مَا هَاجَرَ إلَيْهِ"

Amir Ul Muuminin Abu Hafs Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* Amesema kua: **'Nimemsikia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi* akisema kua: 'Amali hua zinategemeana na Nia hivyo kila Mtu atalipwa kulingana na alivyonuia. Hivyo wale waliohama kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake, basi kuhama kwake ni kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake, lakini kwa wale waliohama kwa ajili ya manufaa ya Kidunia, au kwa ajili ya Mwanamke wa kuoa basi kuhama kwake hua ni kulingana na kile alichokihamia'***(Bukhari na Muslim)*

Namshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kumtakia Rehma na Amani Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kuniwezesha kwa mara nyengine tena kutimiza nia yangu ya kutayarisha Vitabu vitakavyowanufaisha kwa kuwafumbua macho Waislam kwa Ujumla, wasiojua kuhusiana na Dini yao, angalau wawe ni wenye kunufaika kutokana navyo.

Hiki ni moja kati ya vitabu vitabu ambavyo ni vyenye kuzungumzia kuhusiana na historia za miongoni mwa Wanazuoni waliotangulia kabla yetu, kulingana na Darja zao na jitihada zao na matunda ya jitihada zao hizo ambazo zinaendelea kuunufaisha Ummah wa Kiislam kwa Ujumla, na hivyo namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* awalipe Wanazuoni kwa jitihada zao kwa malipo ya kuwaingiza kwenye rehma zake na kuwajaalia Pepo zenye darja ya juu Miongoni mwa Pepo zake.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kwani ni kutokana na Jitihada zao Wanazuoni hawa ndio sisi Waislam wa leo tumefikiwa na neema ya manufaiko ya Ilm zao hapa tulipo katika wakati wa Uhai wetu..*Alhamd Lillah*. Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* pia atuwezeshe kua ni miongoni mwa watakaokua ni wenye kunufaika na Ilm zao na kua ni wenye kufuata nyayo zao, kwani kutokana na kufuata hatua za Nyayo zao Wanazuoni hao basi ndio kwenye kupatikana Uongofu, kwani wao ni miongoni mwa walioongozwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo sisi hatuna budi isipokua kufuata Nyayo zao na hii ni kutokana na kama tulivyoona kulingana na hadith kua Wanazuoni ni Warithi wa Mitume.

Na kutokana na kua Wanazuoni ndio Warithi wa Mitume basi pia inatubidi tujue historia za Maisha yao, ili tupate kujua namna walivyokua wakiishi katika nyakati zao, na jitihada zao kwa ajili ya Uislam, kwa ajili ya Akhera yao na kwa ajili ya Mola wao, ili angalau nasi tupate kuona mifano hai ya kuiiga kutokana na mafunzo ya kusoma historia za Maisha yao kulingana na *Tabaqat* zao.

Neno *Tabaqat* linatokana na neno *Tabaqah* ambalo hua linamaanisha Tabaka, Kufunika Kitu, Kupangilia au kuweka kitu kimoja juu ya chengine, na pia hua linamaanisha Hadith au Kisa ambapo neno *Tabaqat* hua liko katika hali ya Wingi, na hivyo kwa upande wa kiuandishi hua linatumika kumaanisha Mpangilio wa Matabaka ya historia za watu wenye Darja maalum katika jamii kulingana na wakati walioishi katika Uhai wao na Uzuri wa athari zao njema walizoziacha hapa Duniani kwa ajili ya kuipigania Akhera yao.

Kwani Wanazuoni hawa kamwe hawakua ni wenye kuipigania Dunia yao kwani walikua ni wenye kujua maana ya maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo kua:

﴿مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلْحَيَاةَ ٱلدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ إِلَيْهِمْ أَعْمَالَهُمْ فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ ۝ أُوْلَٰئِكَ ٱلَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ فِي ٱلْآخِرَةِ إِلَّا ٱلنَّارُ وَحَبِطَ مَا صَنَعُواْ فِيهَا وَبَاطِلٌ مَّا كَانُواْ يَعْمَلُونَ﴾

Man kana yureedu alhayata alddunya wazeenataha nuwaffi ilayhim aAAmalahum feeha wahum feeha la yubkhasoona; Ola-ika alladheena laysa lahum fee al-akhirati illa alnnaru wahabita ma sanaAAoo feeha wabatilun ma kanoo yaAAmaloona *(Surat Hud 11:15-16)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: ***Yeyote yule anaetaka Maisha ya Kidunia na mapambo yake, basi tutawalipa kikamilifu kutokana na amali zao ndani yake na hawatopunguziwa malipo yao; Hao ndio wale ambao hawana Chao katika Akhera isipokua Moto na ni bure waliyoyafanya Ndani yake, ni Batili yale yote waliyokua wakiyafanya.***

Ambapo tunapozungumzia Wanazuoni basi anasema Imam Al Shibli kua: '**Mimi Nimemsikia Abu Al Zawawi akisema kua: 'Alisema miongoni mwa watu wenye Hikma kua: 'Hakuna Mwanazuoni ambae anaewezekana kweli kuitwa Mwanazuoni hadi pole atakapokua ni mwenye kua ni mwenye kutimiza hali nne zifuatazo:**

-Lazima awe ni Mtu ambae amebobea katika Fani ya Ilm aliyokua nayo.

-Lazima awe na Uwezo wa kuzungumzia na kuandika juu ya fani ya Ilm aliyokua nayo.

-Lazima awe ni mwenye kujua jukumu lake juu ya Ilm aliyokua nayo.

-Lazima awe na uwezo wa kutatua matatizo yatakayotokana na fani ya Ilm aliyokua nayo.'''

Na tunapozungumzia kuhusiana na Ilm ya Wanazuoni basi hua tunazungumzia juu ya ile I'lm yenye Manufaa ambayo hua ni ile I'lm ambayo ni yenye kumpelekea Mtu kua ni mwenye Kumjua, Kumuamini na Kumpenda zaidi Mola wake kama zinavyoelezea aya kuhusiana na wenye kumjua, kumuamini na kumpenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ ٱللَّهِ أَندَاداً يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ ٱللَّهِ وَٱلَّذِينَ آمَنُواْ أَشَدُّ حُبّاً لِلَّهِ وَلَوْ يَرَى ٱلَّذِينَ ظَلَمُوۤاْ إِذْ يَرَوْنَ ٱلْعَذَابَ أَنَّ ٱلْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعاً وَأَنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعَذَابِ﴾

Wamina alnnasi man yattakhidhu min dooni Allahi andadan yuhibboonahum kahubbi Allahi waalladheena amanoo ashaddu hubban lillahi walaw yara alladheena *dh*alamoo idh yarawna alAAadhaba anna alquwwata lillahi jameeAAan waanna Allaha shadeedu alAAadhabi *(Surat Al Baqara 2: 165)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: **Na miongoni mwa watu kuna wale wanaowachukua Miungu wengine, zaidi ya Allah, na hivyo huwapenda wao kama wanavyompenda Allah. Lakini wale wenye Kuamini hua ni wenye kumpenda Allah kwa mapenzi makubwa zaidi, na ya laiti kama wale wafanyao maovu wangeona, wakati watakapoona adhabu kua kila kitu kipo chini ya umiliki wa Allah na Allah ni mkali wa kuadhibu.**

Na pia amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua ndani ya Visa na Hadith vya Mitume, Manabii na Waja wema hua mna Mafunzo ya Kiroho, muongozo wa namna tunavyotakiwa kuishi maisha yetu na vile vile kutuamsha kihisia na kutuzidishia Imani ndani ya Nyoyo zetu kama zinavyosema aya:

﴿وَكُلاًّ نَّقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبَاءِ ٱلرُّسُلِ مَا نُثَبِّتُ بِهِ فُؤَادَكَ وَجَآءَكَ فِى هَٰذِهِ ٱلْحَقُّ وَمَوْعِظَةٌ وَذِكْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ﴾

Wakullan naqussu AAalayka min anba-i alrrusuli ma nuthabbitu bihi fu-adaka wajaaka fee hadhihi alhaqqu wamawAAi*dh*atun wadhikra lilmu/mineena *(Surat Hud 11:120)*

Tafsir: ***Na tunakuelezea Visa juu yako (Ewe Muhammad Salallahu A'layhi wa Salam) kutoka katika habari za Mitume ili kuuzidisha nguvu Moyo wako, na kutokana na haya umekuja kwako ukweli na mawaidha na ukumbusho kwa wenye kuamini.***

Ambapo ndani yake aya hii basi inatuonesha kua ndani ya visa vya Mitume na watu wema waliotangulia kuna manufaa mengi sana yanayozidisha Imani za wenye kuamini na ndio maana akasema Imaam Al Junayd kua: '**Katika Visa hua mna Majeshi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo kutokana nayo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kuwapa nguvu ya Kiimani ndani ya nyoyo zao wale awapendao**'

Hivyo kutokana na mifano ya Historia za Wanazuoni hua kuna Uthibitisho wa Imani ndani ya Vifua vya Waumini kutokana na mafunzo yaliyo ndani yake ya Maisha ya Wanazuoni ambao hata hivyo hatuwezi kuwazungumzia wote, bali inabidi tuwazungumzie baadhi yao muhimu tu na tutakao wakumbuka kutokana na kutajwa kwao kwenye vitabu mbali mbali vya Ilm tofauti za Dini ya Kiislam kwani wako wengi sana.

Na bila ya shaka wengi wao ni Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii na hii ni kwa sababu Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii ndio waliokua wako mbele zaidi

katika jitihada za kufuatilia na kuandika vitabu vya *Tabaqat* za Historia za Wanazuoni wao tofauti na Wanazuoni wa Madhhab mengine kama vile kwa mfano Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambao wao walianza kuandika vitabu vya *Tabaqat* za Wanazuoni wao kupitia kwa Imam Al Qurashi alieishi katika karne ya 7 Al Hijra karne 2 baada ya kuanza kuandikwa kwa *Tabaqat* za Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambao wao walianza kuandika vitabu vy*a Tabaqat* kwenye karne ya 5 Al Hijra.

Na kwa upande wengine ni kutokana na Umaarufu wa Wanazuoni wa *Madhhab* ya Imam Al-Shafi'i ambao ni wenye kunatokana na uthabiti na jitihada za kweli za Imam Al Shafi'i mwenyewe na wa Wanazuoni wanaofuata *Madhhab* hayo, vile vile Maimamu wengi wa *Hadith* ni aidha wafuasi wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i au wanaegemea upande wa Imam Al Shafi'i.

Mwanazuoni mkubwa *Qutb ud Din* Ahmad Ibn Abdul Rahim maarufu kama *Shah Waliyu Allah* Ad Dahlawi, ambae ni mfuasi wa *Madhhab* ya Imam Abu Hanifa anasema '***Madhhab* ya Imam Al Shafi'i ni *Madhhab* pekee ambayo yametoa Wanazuoni bora zaid katika fani zote za Dini ya Kiislam katika historia ya *Madhhab* ya *Ahlu Sunna Wal Jammah*.**'

Ambapo hata historia ya chuo kikuu cha Kiislamu cha Al Azhar cha Misri, chuo ambacho ni kikubwa kuliko vyote duniani kwa umri na kwa darja ya juu ya utolewaji wa *I'lm* ya Dini ya Kiislam, inaonesha kua Mufti Mkuu wa chuo kikuu cha Kiislamu cha Misri Al Azhar, ilikua ni lazima atokee katika *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i hadi mwaka 1287 *Al Hijr*. Hii inathibitisha ule usemi maarufu katika somo la *Fiqh* usemao kua '**Mashafi'i ndio nguzo ya *I'lm* ya dini ya Kiislam**'.

Hivyo Ingawa wengi wao ni Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafi lakini pia nimejaribu kukusanya na kujumuisha ndani yake Kitabu hiki *Tabaqat* za Wanazuoni wa Madhhab tofauti wa Kiume na wa Kike ambao wamefanya mema na mazuri yenye manufaa yanayofaa kuigwa mengi sana angalau na sisi tupate kujifunza kutokana yaliyotokea ndani ya maisha yao.

Na hivyo kua ni mwenye kujaribu kubainisha kua Dini ya Kiislam ni Dini ya Ibn Adam wote kwa ujumla bila ya kubagua baina ya Wanaume au Wanawake, kwani kinachoangaliwa ndani yake kua ni kigezo bora na kua mfano wa kuigwa hua si Maumbile ya Ibn Adam husika kama Mwanamme au Mwanammke bali ni Ucha Mungu unaotokana na Imani na Ilm ya Mtu husika ndani ya Moyo na ufahamu wake juu ya Mola wake kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿يٰأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَـٰكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَـٰكُمْ شُعُوباً وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوۤاْ
إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عَندَ اللَّهِ أَتْقَـٰكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ﴾

Ya ayyuha alnnasu inna khalaqnakum min dhakarin wauntha wajaAAalnakum shuAAooban waqaba-ila litaAAarafoo inna akramakum AAinda Allahi atqakum inna Allaha AAaleemun khabeerun *(Surat Al Hujarat 49:13)*

Tafsir: ***Enyi watu! Hakika sisi tumekuumbeni nyinyi kutokana na Mwanamme Mmoja na Mwanamke mmoja, na tukakufanyeni kua katika mataifa na makabila mbali mbali ili mpate kujuana (na msichukiane). Kwa hakika m-bora wenu mbele ya Allah ni mwenye Taqwa zaid miongoni mwenu. Na Allah ni mjuzi wa kila kitu na ni mwenye habari ya kila mnachokifanya.***

Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atunufaishe nayo kwa kutuzidishia Imani ya Dini ya Kiislam zaidi na atujaalie kua ni wenye kumpenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kwa mapenzi Makubwa zaidi na pia kua ni wenye kuwapenda Wanazuoni ambao ni *Warathatu Al Anbiyai wa Al Mursalin.*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

YALIYOMO:

UTANGULIZI **..........5**
YALIYOMO: **..........11**
VITABU VILIVYOTANGULIA VYA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH: **..........18**
ABU MUSLIM AL KHAWLANI NA FAYRUZ AL DAYLAMI **..........19**
QADHI SHURYAKH AL YAMANI **..........33**
ZAYNAB BINT JARIRI AL HANZALI AL TAMIMI **..........37**
UWEYS AL QARNI **..........40**
AHNAF IBN QAYS **..........46**
IMAM KAAB AL AHBAR **..........51**
IMAM ALQAMAH IBN QAYS AL QUFI **..........54**
IMAM ABU RAJA'A AL UTARID **..........57**
IMAM SHAQIQ IBN SALAMAH **..........60**
IMAM AL RABII IBN KHUTHAYM ATH THAWRY **..........63**
IMAM MASRUQ AL QUFI 1 AH **..........75**
IMAM QABISAH IBN DHUAYB 8 AH **..........78**
IMAM AL QARI ABD ALLAH AL DIMASHQ 8 AH **..........80**
IMAM YUNUS IBN MAYSARA 12 AH **..........81**
IMAM AL QARI YAZID AL QA'QA **..........82**
IMAM SAID IBN MUSAYYIB 15 AH **..........83**
IMAM UBAYD ALLAH IBN ABD ALLAH 16 AH **..........88**
IMAM ABU BAKR IBN ABD RAHMAN 16 AH **..........90**
IMAM MUJAHID IBN JABR 21 AH **..........91**
IMAM AMR ASH SHABI 21 AH **..........95**
IMAM HASAN AL BASR 21 AH **..........103**
IMAM ABD RAHMAN IBN ABI LAILA 21 AH. **..........115**
IMAM JABIR IBN ZAID 22 AH **..........119**

IMAM URWA IBN AZ ZUBAYR 23 AH 123
IMAM ATAA IBN ABI RABAH 25 AH..126
IMAM AD DAHHAK IBN MUZAHIM 25 AH 132
IMAM IKRIMAH MAWLA IBN ABBAS 25 AH 136
IMAM ABD ALLAH IBN MUHAYRIZ..138
IMAM ABU BISHR AL MURRI..141
IMAM AL MUTARRIF IBN ABD ALLAH..144
IMAM ATAA IBN SULAYMAN 147
IMAM KHARIJA IBN ZAYD IBN THABIT 30 AH..................................148
IMAM HABIB AL AJAMI 31 AH..150
SHAYKHA HAFSAH BINT SIRIN 31 AH...157
IMAM SALAMAH IBN DINAR..159
IMAM HAMMAM IBN MUNABIH 167
IMAM WUHAYB IBN WARD...170
IMAM MUHAMMAD IBN AL MUNKADIR 32 AH 174
IMAM MUHAMMAD IBN SIRIN 33 AH 179
IMAM WAHB IBN MUHABIH 34 AH 185
IMAM TAWUS IBN KAYSAN 35 AH..191
IMAM SALIM IBN ABD ALLAH IBN UMAR 36 AH.............................198
IMAM ZAYN AL ABIDIN 38 AH 200
IMAM QASIM IBN MUHAMMAD 38 AH 204
IMAM ATAA IBN YASIR 39 AH..206
IMAM BAKR IBN ABD ALLAH AL MUZANI 208
IMAM AMR IBN QAYS AL-MULAI 210
IMAM RABIAH AL RAY...212
IMAM ABU ZUR BILAL BIN SA'D...215
IMAM MAYMUN IBN MIHRAN 40 AH 219
IMAM MALIK IBN DINAR 41 AH 223

IMAM THABIT AL BUNANI 41 AH 227
IMAM SAID IBN JUBAYR 45 AH 231
IMAM AL QARI IBN KATHIR AL MAKKI 45 AH....................................241
IMAM NAAFI MAWLA IBN UMAR...242
IMAM IBN ABI MULAIKAH 245
IMAM SAFWAN IBN SULAYMI 246
IMAM TALHA IBN MUTARRIF 249
IMAM AL QARI NAAFI IBN NUAYM..251
IMAM AMR IBN DINAR 46 AH 252
IMAM IYAS IBN MUAWWIYAH 46 AH...254
IMAM IBRAHIM AN NAKHAI 46 AH 257
IMAM ABD RAHMAN AL SUDDI 49 AH...259
IMAM ATAA AL KHURASAN 50 AH..260
IMAM DAUD AT TAI 50 AH..265
IMAM MAKHUL AL SHAMI 50 AH 267
IMAM YAZID IBN ABI HABIB 53 AH 270
IMAM YAHYA IBN YAMAR 272
IMAM AL ZUHRI 58 AH. 274
IMAM ABU MUNDHIR HISHAM IBN URWA 61 AH 278
SHAYKHA FATIMA BINT AL MUNDHIRI...281
IMAM SULAYMAN AL AMASH 62 AH..282
IMAM QATADAH AL SADUSI 62 AH 286
UMAR IBN ABD AL 'AZIZ 63 AH...291
IMAM ABU ZINAD 65 AH 299
IMAM AL QARI ABU AMR AL BASR 68 AH..300
IMAM HASAN IBN SINAN 68 AH 301
IMAM ABD ALLAH IBN AWN 68 AH 302
IMAM AYUB AL SAKHTIYANI 68 AH 305

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM AL QARI ABU AMR IBN A'ALA A L BASR 70 AH......................309
IMAM ABU ABD RAHMAN IBN LAILA 76 AH......................................311
IMAM MANSUR AL MU'TAMIR...315
IMAM HAYWA IBN SHURAIH...317
IMAM ABU BASR AL BASR..320
IMAM YUNUS IBN UBAYD...330
IMAM YAHYA IBN ABI KATHIR..334
IMAM IBRAHIM IBN ABI ABLA...337
IMAM ZAYD IBN ZAYN AL AABIDIIN 79 AH.....................................339
IMAM SHAQIQ AL BALKHI..340
IMAM IBN SHABRAMA...342
IMAM AL QARI HAMZA AL KUFI 80 AH..344
IMAM MUHAMAMD IBN IS-HAQ 80 AH..344
IMAM SHU'BAH IBN HAJJAJ 80 AH..346
IMAM JAFAR AS SIDDIQ 80 AH...349
IMAM ABU HANIFA 80 AH...353
IMAM MUQATIL IBN SULAYMAN 80 AH...363
IMAM ABD UL MALIK IBN UMAR 82 AH...365
IMAM HAMMAD IBN SALAMAH 82 A.H...367
IMAM KHALAF IBN HAWSHAB..369
IMAM MISAR IBN KIDAM...370
IMAM ABD AL AZIZ IBN ABI RAWWAD..375
IMAM YAHYA IBN MUADH AL RAZI...377
IMAM AL-AWZAI 88 AH...381
IMAM AL QARI ASIM AL QUFI 90 AH...385
IMAM MALIK 93 AH..386
IMAM AL LAYTH IBN SAAD 94 AH...392
IMAM AL AYYASH 95 AH...395

IMAM WAHB IBN WAHB....398
IMAM SUFYAN ATH THAWRY 97 AH....399
IMAM HAMMAD IBN ZAYD 98 AH....409
SHAYKHA RABIA AL ADAWWIYAH 98 AH....412
IMAM YUSUF AL ASBATI 100 AH....417
IMAM KHALIL IBN AHMAD 100 AH....420
IMAM HASAN IBN SALIH 100 AH....422
IMAM AL YAMAN AL ASWAD....424
IMAM IBRAHIM IBN ADHAM 101 AH....426
IMAM ABU MUAWWIYAH HUSHAYM IBN BISHR 104 AH....432
IMAM SUFYAN IBN UYAYNAH 107 AH....434
IMAM ZUFAYR IBN HUZAYL....439
IMAM AL FUDAYL IBN IYADH 110 AH....441
IMAM ABD ALLAH IBN ABDI LAILA....448
SHAYKHA SHA'WANA....449
IMAM DAIGHAM IBN MALIK....452
IMAM ABD ALLAH IBN MUBARAK 117 AH....461
IMAM AL QARI YAQUB IBN IS-HAQ 117 AH....472
IMAM AL QARI AL KISAI AL KUFI 119 AH....473
IMAM AL MUAFI IBN IMRAN 120 AH....475
IMAM ABD ALLAH IBN HUBEYK....478
IMAM ABD ALLAH IBN WAHB 125 A.H....480
IMAM IBN ABD RAZZAQ AL SANAANI 126 AH....483
IMAM WAKI IBN JARRAH 127 AH....484
IMAM MUSA AL KADHIM 128 A.H....488
IMAM MIMSAD AD DINAWARI 130 AH....491
IMAM ABU YA'LA....496
IMAM AL WAQIDH 130 AH....497

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM MA`RUF AL-KARKHI 132 AH *516*
IMAM IBN QASIM..*522*
IMAM ABD RAHMAN IBN MAHDI 135 AH *522*
IMAM BISHR AL-HAFI...*530*
IMAM ABU SULYAMAN AD DARANI AL ANSI *534*
IMAM AHMAD IBN ASIM AL-ANTAKI *538*
IMAM AL SIBAWAYH AL NAHWI 143 A.H *541*
SAYYIDA NAFISA 145 AH...*546*
IMAM AHMAD IBN ABI AL-HAWARI *549*
IMAM AHMAD IBN HADRAWAYHH 145 AH *551*
SHAYKHA RABIA BINT ISMAIL AL DIMASHQ *554*
SHAYKHA HALIMA AL DIMASHQ *555*
SHAYKHA AL LUBABA AL MUTA AL A'ABBIDA *556*
IMAM MANSUR IBN `AMMAR *557*
IMAM ABU DHIB *558*
IMAM AL SHAFI'I 150 AH..*560*
IMAM ABU AL HASAN ALI RIDHA 153 AH..*609*
IMAM YAHYA IBN MAIN 158 AH..*612*
IMAM AL ZAHID AL ISFAHANI 158 AH..*614*
IMAM SARI AL-SAQATI 160 AH..*618*
IMAM IBN SAHNUN 160 AH *621*
IMAM IS-HAQ IBN RAHAWAYH 161 AH *623*
IMAM ALI IBN AL MADINI 161 AH *633*
IMAM AHMAD IBN HANBAL 164 AH..*637*
IMAM MANSUR IBN AMMAR...*643*
IMAM IBN KULLAB..*646*
IMAM AL MUHASIBI 165 AH...*649*
IMAM AL HARMALA AL SHAFII 166 AH *665*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM IBN SAD 168 AH 668
IMAM ABU AL HASAN AL TUSI...670
IMAM ABU UBAYD AL BUSRI...678
IMAM AL BUWAYTI 680
IMAM ABU THAWR 170 AH 683
IMAM AL HUMAIDI 170 AH...684
IMAM AL ANMATI...686
IMAM IBN SIBGHI AL ZAFARANI 170 AH...687
IMAM AL KARABISI 689
IMAM AL RABII IBN AL MURADI 174 AH 690
IMAM AL MUZANI 175 AH..693
IMAM AD DARIMI 181 AH..700
SHAYKHA FATIMA AL NISHAPURI...702
IMAM DHU NUN AL MISRI 181 AH...705
IMAM AL KIRMANI 190 AH 712
IMAM BUKHARI 194 AH..714
IMAM ABU ZURAH AL RAZI 194 AH...719
IMAM ABU HATIM AL RAZI 195 AH 724
IMAM ABU HAFS AL HADDAD...727
IMAM HATIM AL ISAM 733
IMAM ABU BAKR IBN WARRAQ...744
IMAM ABU UTHMAN AL HIRI 749
VYANZO VYA VITABU VILIVYOTUMIKA KWENYE KITABU............759
VYANZO VYA MTANDAONI VILIVYOTUMIKA KWENYE KITABU ...759

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

VITABU VILIVYOTANGULIA VYA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH:

1-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA KWANZA - MWAKA - *1435 AL HIJRA* (2014).

2-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA PILI - MWAKA - *1437 AL HIJRA* (2016).

3-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA TATU - MWAKA *1439 AL HIJRA* (2018).

4-TAFSIR SURAT YUSUF – AHSAN AL QASAS - MWAKA *1441 AL HIJRA* (2020).

5-ULU UL AZMI MINNA RUSULUN JUZUU AL AWWAL – WENYE AZMA THABIT MIONGONI MWA MITUME JUZUU YA KWANZA – MWAKA 1442 AL HIJRA (2021).

6-ULU UL AZMI MINNA RUSULUN JUZUU AL THANI – WENYE AZMA THABIT MIONGONI MWA MITUME JUZUU YA PILI – MWAKA 1443 AL HIJRA (2022).

ABU MUSLIM AL KHAWLANI NA FAYRUZ AL DAYLAMI

Mnamo mwaka wa 632 kabla ya kufariki *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kulitokea uasi katika ardhi ya Yemen wa kuwapotosha baadhi ya watu waliokua wameongoka baada ya kutoka kwenye kiza cha ukafiri na kuingia kwenye Nuru ya Imani ya Dini ya Kiislam kwa kuibuka kwa watu wenye kujinadia kua na wao pia wamekua ni Mitume akiwemo Aswad Al Ansi wa Yemen.

Aswad Al Ansi alikua ni mtu ambae mweye mwili mkubwa, Mnafiq, Mshirikina na pia alikua ni mwenye nguvu ya kutumia ulimi wake kwa kumkufuru Mola wake kwa hoja za maneno yenye uwezo wa kuwapotosha wengi miongoni mwa wale wanaomsikiliza mbele yake. *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimjaalia Aswad Al Ansi pia mali na mamlaka na kua ni mwenye Wafuasi wengi sana kiasi ya kua baadhi ya Makabila makubwa yakaanza kuungana nae ikiwemo kabila la Bani Madh-haj ambalo lilikua ni Kabila la Watu wengi miongoni mwa watu wa Yemen na hivyo ikawa kila anaepingana nae basi hua ni adui yake na huamua kumuangamiza wa ajili ya Maslahi ya Dunia yake.

Miongoni mwa waliowahi kukutana na mtihani wa Al Aswad Al Ansi kabla ya kufariki kwake, basi alikuwepo kijana moja aitwae Abd Allah Ibn Tsuwab ambae alikua ni maarufu kwa jina la Abu Muslim Al Khawlani ambae alikua ni mwenye Imani kubwa sana, kwani alikua ni mwenye kujitolea kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* peke yake na ni mwenye kuapa kua ataitumikia Dini ya Kiislam na kueneza ujumbe wake kwa nguvu na uwezo wake wote.

Habari ya kijana huyu Abu Muslim Al Khawlani ilipomfikia Al Aswad basi akaamua kumtafuta kwa udi na uvumba hadi akampata na kumkamata na kuamua kua atampa adhabu ya mfano wake ili watu wasiweze kumfuata na kupingana na upotovu wake Al Aswad. Hivyo baada ya Abu Muslim Al Khawlani kukamatwa basi Al Aswad akaamrisha kua zikusanywe kuni nyingi sana uwanjani kisha uwashwe moto kwa ajili ya kumuadhibu Abu Muslim Al Khawlani wa kumchoma moto Abu Muslim Al Khawlani.

Baada ya moto kukolea basi akawasili Al Aswad Al Ansi huku akiwa na walinzi wake waliokua wamemzunguka, na kisha baada ya dakika kadhaa akaingizwa uwanjani Abu Muslim Al Khawlani huku akiwa taabani kwa adhabu alizokabiliana nazo baada ya kukamatwa kwake na alipofikishwa mbele yake basi Al Aswad akamuuliza Abu Muslim Al Khawlani : '**Jee unashuhudia kua Muhammad Ndie Mtume wa Allah?**'

Abu Muslim Al Khawlani akajibu: **‘Naam Nashuhudia kua Muhammad ni Mja na ni Mtume wake *Allah Subhanah wa Ta’ala* na ndie *Sayyid Al Mursalin* na ndie Mtume wa Mwisho.’**

Al Aswad akauliza huku akiwa amejawa na hasira: ‘**Na Jee unashuhudia kua mimi ni Mtume wa Allah?’**

Abu Muslim Al Khawlani akasema: ‘**Sijakufaham, sikusikii kwani masikio yangu yameziba.**’ Al Aswad akasema: ‘**Basi nitakutumbukiza ndani ya moto sasa hivi yatazibuka.’**

Abu Muslim Al Khawlani akasema: ‘**Kama ukinitumbukiza mimi ndani ya Moto huu wenye kuni za miti basi nawe utalipwa na *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa kutumbukizwa ndani ya moto ambao kuni zake ni Watu na Mawe, chini ya usimamizi wa Malaika wenye nguvu kubwa sana ambao kamwe hawamuasi Mola wao.**’

Al Aswad akasema: **‘Hakika mimi sina haraka, nakusubiri na kukupa mda ili upate kubadilisha mtizamo wako nakupa nafasi nyengine ya kufikria juu ya hilo, hivyo jee bado unaendelea kukubali kua Muhamamd ni Mtume wa Allah?’**

Abu Muslim Al Khawlani akajibu: ‘**Naam, hakika mimi nnashuhudia kua Muhammad ni Mja na ni Mtume wa *Allah Subhanah wa Ta’ala*, ambae ametumwa kwa ajili ya kutuongoza kwenye Dini ya uongofu, *Allah Subhanah wa Ta’ala* amejumuisha ujumbe wake wote ndani ya ujumbe aliokuja nao Muhammad.**’

Al Aswad akauliza tena kwa sauti kubwa huku subira yake juu ya upinzani wa Abu Muslim Al Khawlani dhidi yake ikiwa inamalizika: ‘**Na Jee unashuhudia kua mimi ni Mtume wa Allah?’**

Abu Muslim Al Khawlani akajibu huku akiwa ni mwenye kuonekana kua amejawa na utulivu kwa kusema: ‘**Sijakufaham, sikusikii kwani masikio yangu yameziba.**’ Jambo ambalo lilimzidisha hasira Al Aswad na hivyo akaamrisha kua Abu Muslim Al Khawlani aingizwe ndani ya moto unaowaka mbele yake uwanjani hapo.

Lakini kabla ya kutekelezwa amri hio basi mmoja kati ya washauri wa Abu Aswad akamnongo'neza Abu Aswad kwa kumwambia kua: ‘**Hivi jee unajua kua, huyu mtu ni miongoni mwa wenye Nyoyo zilizokua na Ikhlasi ndani yake? Hivyo Dua zake hua ni zenye kujibwa, kwani *Allah Subhanah wa Ta’ala* kamwe hua hawaachi mkono Waja wake wacha Mungu katika nyakati za Mitihani yao wanapomhitaji,**

hivyo kama ukimtumbukiza Motoni na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akimuokoa, basi ujue kua kila kitu ulichokisimamia hadi kufikia hapa ulipo kitaangamia na kitakua ndio mwisho wake hapo hapo kwani watu wote wataukataa Utume wako.'

'Na inabidi ufahamu pia kua kama ukimchoma moto na matokeo yake akawa ni mwenye kufariki kutokana nao, basi watu watamchukulia huyu kua ni Shahidi kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na watu watamtukuza na kumpandisha darja kubwa sana, hivyo jambo bora la kufanya kwako basi ni kumuwachia na kumfukuza asionekane kwenye ardhi ya nchi yako, na hapo utapata utulivu mkubwa sana.'

Al Aswad akatafakkari na kuona kua huo aliopewa ni ushauri mzuri sana, hivyo akaamua kumuwachia huru Abu Muslim Al Khawlani na kumfukuza kutoka kwenye ardhi ya Yemen asionekane tena, kwani akionekana na kukamatwa tena basi atauliwa, ambapo tukio hili la kufukuzwa kutoka kwenye ardhi ya Yemen lilimfurahisha sana Abu Muslim Al Khawlani kwani alikua na hamu sana ya kutekeleza mipango yake ya kueleeka kwenye Mji wa Madina kukutana na Mtu anaempenda sana ambae ni *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na miongoni mwa Watu waliokua na athari kubwa pia katika Ardhi ya Yemen na wenye kuheshimika walikuwemo pia watu wa kabila la Abna ambao walikua ni wenye asili ya Uajemi ambao walioana na watu wa Yemen na walikua wakitawala baadhi ya sehemu ya Ardhi ya Yemen ikiwemo mji wa Sanaa kwa kumuwakilisha mfalme Kisra Anushiravan wa Uajemi na kuuondoa Utawala wa Uhabeshi kutoka kwenye ardhi ya Yemen.

Ambapo baadae watu hawa ambao kiongozi wao alikua akitwa Shahr Ibn Badhar walipopata habari kuhusiana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi wakasilimu na kua Waislam na hivyo wakawa ni wenye kupingana na Utawala wa Aswad Al Ansi kama alivyokua Abu Muslim Al Khawlani ambae yeye alipata nusra ya kuondoka kutoka nchini Yemen.

Lakini kwa upande wa watu wa Abna walipata pigo kwani Aswad Al Ansi alipigana nao watu wa Abna, na akafanikiwa kumuua kiongozi wao aliekua akiitwa Shahr Ibn Badhar na kisha akamteka mke wa Shahr Ibn Badhar ambae alikua ni Mwanamke mzuri sana aliekua akiitwa Dadha na kumfanya kua ni Mke wake, baada ya tukio hili basi akauteka mji wa Sanaa, Mji wa Hadhramawt, Taif, Ahsa na Aden pia.

Baada ya kupata habari hii basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akatuma ujumbe wake kwa baadhi ya watu wa Yemen anaowaamini na kuwahakikishia kua wasivunjike

Moyo bali wanatakiwa wapingane nae kwa vyovyote vile itakavyokua ambapo mmoja kati ya waliochaguliwa kufikishiwa ujumbe huo wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutokana na Imani yao alikuwemo pia Fayruz Al Daylami ambae alikua ni miongoni mwa watu wenye misimamo miongoni mwa watu wa Abna baada Shahr Al Badhar na alikua ni Binamu yake Dadha aliekua mke wa Shahr Badhar.

Anasema Fayruz Al Daylam kua: '**Hakika mimi na watu wa Abna waliokua pamoja nami hatukua na shaka hata kidogo juu ya *Rasul Allah Slallahu Alayhi wa Salam* kua ndio Mtume wa Mwisho, na hatukua tukimuamini Al Aswad ambae ni adui wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hata kidogo ndani ya nyoyo zetu na tulikua tunasubiri tupate nafasi ya kumuondoa katika cheo chake kwa njia yeyote iwezekanavyo'**

'Tulipopata ujumbe wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, basi kila mmoja wetu aliingia ari zaidi na kugawana majukumu juu ya nini cha kufanya baina yetu dhidi yake Al Aswad Al Ansi, kwani *Rasul Allah Salallahu Alayh wa Salam* alituambia kuhusiana nae na namna anavyotumia nguvu zake na uwezo wake na uhusianao wake na kiongozi wake ambae ni Qays Ibn Yaghuth kua hana usalama chini yake kutokana na dhulma zake.

Hivyo mimi na Ibn Ami yangu Dadhawayh tukaenda kwa Qays na kumwambia kuhusiana na maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na tukamkaribisha kufanya Al Aswad kua chakula cha Mchana kabla ya yeye Al Aswad hakuwahi kumfanya Qays kua ni chakula cha Usiku, ambapo nae akakubaliana na mtizamo wetu na kuuona kua ni msaada kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake, hivyo akatuwekea wazi siri zake na mipango yake yote, na kwa pamoja sisi watatu tukaamua kumshambulia Al Aswad Kutoka ndani ya Kasri lake huku ndugu zetu wengine wakisubiri kumshambulia kwa nje yake.'

Hivyo ikabakia kumtafuta Ibn Ami yetu Dadha ambae Al Aswad alimuoa baada ya kumuua Mume wake, kwani ilikua kuna ulazima wa Dadha kushirikiana nasi, hivyo tukaenda kwenye Kasri la Al Aswad na kusalimiana nae na kisha nikamwabia Dadha: 'Ewe Ibn Ami hivi jee unajua wewe kuhusiana na Ubaya wa ambao ametufanyia sisi na pamoja nawe? Kwani amemuua Mume wako na ametudhalilishia Wanawake wetu, amewaua Waume zao na kuwanyang'anya Mamlaka yao, angali hii ni Barua kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwetu sisi na kwa wAtu wote wa Yemen kwa ujumla, ambao unatutaka kumalizana na huu mtihani mkubwa uliopo mbele yetu, hivyo jee utakubali kushirikiana nasi?'

Dhada akauliza: ‘**Unataka niskusaidie vipi?**’ nami nikasema: ‘**Katika kumuondoa kwake..**’ nae akasema: ‘**Yaani kumuondoa Duniani Wa Allahi, sina mwengine wa kushirikiana nae zaidi juu ya hili**’ nami nikasema: ‘**Mimi nilikua naogopa kukushauri juu ya hili**’ nae akasema: ‘**Naapa kwa yule ambae ndie aliemtuma *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama muonyaji na mbashiriaji habari njema kua mimi sikuwahi kua na shaka na Dini yangu hata kidogo, *Allah Subhanah wa Ta’ala* hakujaalia Mtu kuchukiwa nami kama ninavyomchukia Al Aswad, kwani mara ya kwanza tu nilipomuona nilimjua kua ni mtu Fasiq na mpotovu na asiemaliza kufanya mambo maovu sana yasiyosemeka.**’ Nami nikamuuliza: ‘**Hivyo jee tutamuondoaje?**’

Dadha akasema: ‘Ukweli ni kua analindwa sana na ana ulinzi mkubwa, kwani hakuna sehemu ndani ya Kasri lake ambayo haiko chini ya ulinzi, ila kuna sehemu ambayo iko upande wa vyumba vya kushoto ambao kuna uhuru kidogo katika wakati wa usiku wa manane, hivyo nitakuwekeeni silaha na utaingia ndani na utanikuta mie nakusubiri mlangoni, ila kua makini kwani hili si jambo rahisi hivyo kama mtu akisikia na kuwapa habari walinzi basi hu ndio utakua mwisho wetu.’ Nami nikasema: ‘Bila ya shaka uko sahih.’

Dadha akasema: ‘Ila nna ushauri mwengine’ nami nikauliza: ‘Upi?’ nae akasema: ‘Kesho nitumie mtu ambae unamuamini miongoni mwa wafanyakazi wako, nitamfahamisha kutengeneza njia ya kuingilia ndani kirahisi kwa kutokea ndani kwa ndani’ nami nikasema: ‘Hili ni Jambo bora zaidi’ baada ya hapo nikaagana nae na kuenda kuwataarifu wengine juu ya mpango huo nao wakakubaliana nami na kisha tukaagana kwa ajili ya matayarisho ya kila mmoja wetu kuwepo katika wakati husika katika sehemu husika.

Wakati ulipowadia wa siku ya kuvamia, basi tukavamia katika sehemu tuliyokubaliana pamoja na wenzangu na kuingia ndani tukawasha taa na kukuta silaha zimewekwa tukazichukua na kuelekea kwenye chumba cha Adui wa Allah, na tukamkuta Ibn Ami yangu Dadha akiwa amesimama mlangoni kwake, akatuonesha alipokuwepo nasi tukaingia ndani chumbani mwake, alikua amelala anakoroma, nikamvamia na kumkata kwenye shingo yake na akaanza kulia kama Nyati anaechinjwa, na mara wakaja Walinzi wake kwa haraka sana na kuuliza: ‘Kuna nini?’

Dadha akawajibu: ‘Miswe na Khofu kwani Mtume anapokea Wahyi wake’ na hivyo Walinzi hao wakaondoka, nasi tukasubiri hadi ulipowadia wakati wa Alfajir nami nikasimama kwenye ukuta wa Ngome hio, na kuadhini kwa kusema: ‘*Allahu Akbar Allahu Akbar!*’ na kuendelea na Adhana hadi nilipofikia katika maneno yasemayo ‘*Ashhadu anna Muhammad ur Rasulullah*! basi nikamalizia kwa kusema: '*Wa ashhadu anna al Aswad al-Ansi Al kadh-dhab!*’

Hili ndio lililokua neno ambalo wanalisubiri Waislam, kwani ndio uliokua ufunguo wa Ujumbe wa kukamilika kwa jambo letu, hivyo Waislam wakavamia Ngome kutoka katika kila upande huku wakinadia: 'Allahu Akbar!' Walinzi wa Al Aswad walichanganyikiwa na kuzidiwa kiasi ya kua hadi lilipochomoza Jua basi kila kitu kilikua kimeshamalizika, na kisha tukatuma ujumbe kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumtaarifu yaliyotokea.

Hivyo wajumbe wa Ujumbe huo walipowasili katika Mji wa Madina wakapata habari kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amefariki katika usiku huo walipowasili na kuambiwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alishusiwa Wahyi kuhusiana na kifo cha Aswad Al Ansi katika usiku aliofariki.

Tunaporudi kwa upande Abu Muslim Al Khawlani katika kuhama kwake kutoka katika ardhi ya Yemen na kukimbilia katika ardhi ya Mji wa Madina basi nae kwa bahati mbaya kabla ya kuwasili katika Mji wa Madina akapata habari kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amefariki dunia na Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* amechaguliwa kua ni Khalifa wa kwanza wa Umma wa Kiislam, hizi zilikua ni habari ambazo zilimvunja moyo sana Abu Muslim Al Khawlani, kwani zinambainishia kua hakuwa ni mwenye kuwahi kukutana nae yule mtu anaempenda kuliko wote ambae yeye amejitolea kwa ajili yake na pia kwa ajili ya Mola wake.

Lakini hata hivyo Abu Muslim Al Khawlani hakukatisha safari yake kwani ingawa hatoweza kufanikisha lengo kuu la safari yake lakini kwa upande mwengine basi alikua anajua kua atafankiwa kutekeleza lengo jengine la safari yake, ambalo ni kutafuta Ilm zaidi ya Dini yake kueneza ujumbe wa Mola wake na kuendelea kuipigania Dini yake kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, hivyo akaendela na safari yake hadi katika Mji wa Madina na kisha akaingia katka Msikiti wa Madina na jambo la kwanza kwake lilikua ni kumsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika kaburi lake.

Na kisha akasali Sala ya Sunna na kukaa pembeni na kuegemea kwenye moja kati ya Nguzo za Msikitini hapo na kupumzika, mara akatokezea Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na kumsalimia Abu Muslim Al Khawlani na kumuuliza: '**Hivi wewe unatokea kwenye ardhi ya Nchi gani?**'

Abu Muslim Al Khawlani akasema: **'Mimi natokea kwenye Ardhi ya Yemen**'

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema kumuuliza Abu Muslim Al Khawlani: '**Hebu niambie vipi kuhusiana na yule ndugu yetu alietaka kuchomwa moto akiwa hai na Adui wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*? Na kisha akaokolewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*?**'

Abu Muslim Al Khawlani akajibu: ‘**Mzima Alhamd lillah!’** ambapo jibu hili lilimshangaza Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambae hapo hapo akataka kujua zaidi kwa kuuliza: ‘**Hivyo unavyojibu kama yeye ndie wewe, *Subhanah Allah*, sio wewe lakini?**’

Abu Muslim Al Khawlani akajibu: ‘**Naam bila ya shaka ndie mimi**’, na hivyo hapo hapo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamkumbatia Abu Muslim Al Khawlani kwa hisia kubwa sana na kisha akambusu kwenye paji lake la uso, kisha akamuuliza Abu Muslim Al Khawlani: ‘**Hivi jee umesikia habari za namna *Allah Subhanah wa Ta’ala* alivyomfanyia Adui yake na adui yako?’**

Ambapo Abu Muslim Al Khawlani akajibu: ‘**La, hakika mimi sina habari yeyote kutoka Yemen tangu nilipohama kutoka kwenye ardhi ya nchi hio.’**

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: ‘***Allah Subhanah wa Ta’ala* amemjaalia Al Ansi kuua kupitia kwenye mikono ya Waumini waliokuwepo nchini Yemen na kuwarudisha wafuasi wake kwenye njia iliyonyooka ya *Allah Subhanah wa Ta’ala.’***

Abu Muslim Al Khawlani akajibu: **‘Shukrani na sifa njema zote anastahiki *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa kunijaalia mimi kutoondoka Duniani kabla ya kusikia habari za kifo za Fasiq na kurudi kwa watu wa Yemen kwenye njia ya muongozo wa Uislam.’**

Umar Ibn Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: **‘Shukrani na sifa njema zote anastahiki *Allah Subhanah wa Ta’ala* alienipa mimi nafasi ya kukutana na mmoja kati ya watu wa Umma wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alietaka kufanyiwa kama alivyofanyiwa *Khalilu Allah Ibrahim Alayhi Salam*.’**

Kisha Umar Ibn Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamchukua Abu Muslim Al Khawlani na kumtambulisha kwa *Amir ul Muuminin* Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* ambae nae akakubaliana na kua ni miongoni mwa waliokua chini ya *Amir ul Muuminin* Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* na kisha *Umar Radhi Allahu Anhu* akamuomba Abu Muslim Al Khawlani awaelezee kisa chake.

Baada ya hapo Abu Muslim Al Khawlan akaamua kubakia kwenye Mji wa Madina na kujitafutia Ilm kutoka kwa Muadh Ibn Jabal, Awf Ibn Malik, Abu Ubaidah Ibn Jarrah, Abu Dhar Al Ghifari, Ubaydah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhum* na wengineo.

Abu Muslim Al Khawlani alikua ni Mtu ambae anaewajali sana wale wasiokua na uwezo zaidi yake kiasi ya kua siku moja Abu Muslim Al Khawlani aliporudi nyumbani kwake

na alimkuta mke wake akiwa analalamika kua hamna Chakula Nyumbani, hivyo akamuuliza mke wake kama kuna pesa yeyote ndani ambapo nae akajibu kua kuna Dinar moja. Hivyo Abu Muslim Al Khawlani akaichukua Dinar hio na kisha akachukua mfuko na kuelekea sokoni na alipofika njiani akakutana na masikini ambae alimlalamikia na kumuomba msaada Abu Muslim Al Khawlani hivyo Abu Muslim Al Khawlani akachakua Dinari yake moja na kumpa Masikini huyo, na kisha akaujaza Mkoba wake kwa unga wa mbao, na kisha akarudi nyumbani na kuuweka mkoba huo ndani na kutoka haraka sana.

Siku hio hakurudi nyumbani hadi usiku baada ya *Salat al Isha* na alipoingia ndani basi Mke wake akamletea Mikate na kumuwekea juu ya Meza. Hivyo Abu Muslim Al Khawlani akashangaa na kuuliza: '**Huu Unga umepata wapi uliopikia mikate?**' mke wake akajibu: '**Ndio ule ulioneletea wewe kwenye mkoba.**' Abu Muslim Al Khawlani akala mikate hio huku akilia kutokana na Miujiza ya Rehma na Neema za Mola wake juu yake.

Abu Muslim Al Khawlani alikua ni Mtu ambae mwenye Imani kubwa sana na Ucha Mungu kiasi ya kua alikua hapendi kukaa na watu Wanaozungumzia kuhusiana na mambo ya Kidunia. Lakini hata hivyo siku moja aliingia Msikitini na kisha akakutana watu ambao walikua wanazungumzia mambo ya kidunia ndani yake, hivyo akawaangalia kwa mshangao na kisha akasema kuwaambia watu hao:

'***Subhanah Allah!* Mfano wangu mie na wenu nyie ni sawa na mtu ambae alikumbana na mvua kubwa sana, na kisha akaona mbele yake kua kuna ukuta na Mlango, hivyo akakimbilia na kuufungua Mlango huo na kuharakisha kuingia ndani akitarajia kua atapata sehemu ya kujificha Mvua ndani yake, lakini alipoingia baada yake akagundua kua kumbe hakuna paa ndani yake ukuta huo hivyo kukimbilia kwake kumekua bure. Kwani mimi nimekimbilia Msikitini humu nikitarajia kukutana na watu waliozama kwenye *Dhikr Allah* lakini badala yake nakutana na watu waliozama kwenye Dunia yao.'**

Kwa upande wa Fayruz Al Daylami aliishia katika ardhi ya Yemen hadi pale alipofariki *Amir ul Muuminin* Abu Bakr AS Siddiq *Radhi Allahu Anhu* na hivyo mamlaka ya Ukhalifa yakabebwa na *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambae aliamua kumuandikia barua Fayruz Al Daylami ambayo ilikua inasema:

'Hakika mimi nimeona kua wewe unakazi kubwa sana ya kula Mikate na Asali tu, hivyo barua hii ikikufikia basi njoo haraka kwangu kwenye Mji wa Madina kwa ajili ya kuungana nami katika kuipigania njia ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'

Na baada ya kupata barua hio basi Fayruz Al Daylami akafunga safari kutoka Yemen na kuelekea kwenye Mji wa wa Madina na alipofika katika mji huo akaelekea moja kwa moja kwenye nyumba ya *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*, na kukutana na Umati wa watu ukiwa unasubiri kuonana nae. Hivyo nae akaomba ruhusa kuona nae, na akaruhusiwa na kusogea na kusubiri mlangoni, lakini mara akatokea kijana wa Quraysh ambae alikua anataka kuingia ndani na akampiga kikumbo Fayruz Al Daylami ambapo nae akampiga kibao kijana huyo.

Kijana huyo akaingia moja kwa moja kwa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kulalamikia juu ya tukio hilo la kupigwa na Fayruz, hivyo *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*, akamwita Fayruz na kumuuliza: '**Imekuaje Ewe Fayruz?**' Fayruz akasema: '**Ewe *Amir ul Muuminin* hakika wewe umenialika mimi, lakini huyu kijana hukumualika, umeniruhusu mimi kuingia lakini huyu kijana kumruhusu, na aliamua kuingia ndani kabla yangu mie hivyo nami nikafanya kama ulivyoambiwa**'

Amir ul Muuminin Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: '***Al Qisas!***' kumaanisha kua Fayruz inabidi alipizwe kwa kupigwa kibao na kijana huyo. Fayruz akauliza: **'Kisasi lazima kilipizwe juu ya hili?'** *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* **: 'Lazima'** Hivyo Fayruz Al Daylami akapiga magoti kwa ajili ya kupokea adhabu ya dharuba ya kibao kutoka kwa kijana husika ambae alikua amesimama kwa ajili ya kulipiza kisasi hicho.

Ambapo wakati kijana huyo alipokua anajitayarisha mkono wake kumpiga kibao Fayruz Al Daylami, basi *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema kumwambia kijana huyo: '**Subiri ewe Kijana, kwani kwanza nataka nikuambie kuhusiana na alivyoniambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Usiku mmoja ambapo aliniambia kua: 'Katika usiku huu, Al Aswad Al Ansi ameuliwa na Mcha Mungu aitwae Fayruz Al Daylami kwa kumkata kichwa chake**''

Kisha *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamwangalia kijana huyo na kumuliza kwa kusema: '**Hivyo ewe Kijana jee unafikiria kua kumlipizia Kisasi kunastahiki baada ya kusikia haya aliyoyasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam?***' ambapo kijana huyo akasema: '**La hakika mimi nimemsamehe baada ya kuniambia juu ya yale yaliyoonekana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana nae.**'

Na ingawa Fayruz Al Daylami alikua amesha samehewa na kijana huyo lakini hata hivyo nae akawa hakuridhika kutokana na kua na khofu ya Mola wake na hivyo akauliza kwa kusema: '**Hivi jee Ewe A*miru Muuminin* unadhani kua kuepukana na kisasi kutokana na nilichokifanya baada ya kupata uthibitisho wake kauli yake kunisamehe, hufikriii wewe kua kunisamehe kwake hakukutokana na ushawishi**

wa uliyoyasema?’ *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: **‘La!’**

Na baada ya thibitisho hilo basi Fayruz Al Daylami akasema kumwambia *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*: **‘Hakika mimi nnatangazia hapa kua nnashuhudia kua Upanga wangu, Farasi wangu na Dinari 30000 zangu nilizokua nazo nazitoa kwa ajili ya huyu kijana kua kama malipo ya fidia kwake kutoka kwangu.**’

Na hivyo *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamwambia kijana huyo kua: ‘**Hakika usamehevu wako umelipwa ewe Kijana na bila ya shaka sasa hivi wewe ni miongoni mwa watu walio Matajiri.’** Naam huyo ndio Fayruz Al Daylami.

Hivyo tunarudi kwa Abu Muslim Al Khawlani ambae kama tulivyosema kua yeye baadae alihamia katika Ardhi ya Sham ambapo kabla ya kufariki kwake katika vita vya Jihad basi alikutana na Muawwiyah Ibn Abu Sufyan kutokana na mara kwa mara kua ni mwenye kuhudhuria vikao vyake.

Safari moja Abu Muslim Al Khawlani aliwasili katika kikao hicho na kumkuta Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* akiwa amezungukwa na Magavana wake, Washauri wake wa Kivita na kiuchumi n.k, na Abu Muslim Al Khawlani akaona na kuhisi namna watu wanavyomheshimu na kumnyenyekea, hivyo akaona kua hili ni jambo ambalo linaweza likamharibia Imani yake Muawwiyah Ibn Abu Sufyan *Radhi Allahu Anhu* labda ikawa anajiona n.k

Hivyo Abu Muslim Al Khawlani akasalimia kwa kusema: ‘***Assalam Alayk ya Ajiral Al Mu’uminin***’ ambapo neno *Ajira* hua linamaanisha Muajiriwa. Na baada ya kusikia salamu hio basi watu wote waliomzunguka Muawwiyah wakaja juu na kumwambia Abu Muslim Al Khawlani kua: ‘**La hutakiwi kumwita hivyo, bali sema *Amir Ul Muumini.*’** Lakini hata hivyo *Abu Muslim Al Khawlani* akaendelea kusema: ‘***Assalam Alayk ya Ajiral Al Mu’uminin***’ ’

Na watu hao walipokuja juu basi Abu Muslim Al Khawlani akamwambia Muawwiyah Ibn Abi Sufyan *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘**Hakika wewe ni mtu ambae umechaguliwa na *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua ni Msimamizi wa Watu, kama vile ambavyo Mtu anavyoteua na kumuajiri Mtu kwa ajili ya kusimamia mifugo yake, ambae atalipwa ujira mkubwa kutokana na kazi yake hio kama atawasimamia vizuri Wanyama hao, kiasi ya kua waliokonda watanenepa na waliokua wadogo watakua wakubwa na wenye kuumwa watakua na afya.**

Ambapo kama Mtu huyo atakua ni mweye kudharau mifugo yake hio aliyoajiriwa aisimamie basi na hivyo Wanyama wakawa ni wenye kukonda na kufariki na maziwa yao na ngozi zao kua hazifai hata kutumika, basi hatoweza kulipwa malipo yeyote kama hali itakua hivyo na bado atabada adhabu kutokana na kutowasimamia Wanyama wake hao, hivyo ewe Muawwiyah chagua lililokua bora kwako wewe na sahau kuhusiana na kile unachokitaka.'

Baada ya kusikia maneno hayo basi Muawwiyah Ibn Abi Sufyan *Radhi Allahu Anhu* akakaa kimya kisha akasema: 'Namuomba Allah, akulipe wewe kwa malipo bora zaidi kutokana na kutujali kwako sisi na watu wengine, kwani kwa hakika sisi tunajua kua wewe daima ni mwenye kutoa ushauri kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* na kwa ajili ya manufaa ya Waislam.'

Hivyo Mwishoni mwa uhai wake Abu Muslim Al Khawlani aliumalizia katika Ardhi ya Sham ambapo aliamua kuishi kwa sababu ya kua karibu na mipaka ya ardhi za Waislam kwa ajili ya kupigana na Maadui wa Uislam na katika jitihada zake hizo alipokua na wenzake safari moja wakikabiliana na Maadui zao wa Utawala wa Roman Empire basi iliwabidi kuvuka mto wenye maji mengi sana, kiasi ya kua ilibidi lazima lipatikane daraja kama wanataka kuvuka kwa usalama wao, lakini Abu Muslim Al Khawlani akawaambia wenzake kua: '**Hapa tutavuka kwa *Biismi Allahi Al Rahmani Al Rahim* hivyo nifuateni mimi huku kila mmoja akiwa ni mwenye kusema *Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahim***'

Hivyo Abu Muslim Al Khawlani akatangulia mbele huku jeshi likimfuata na akasema *Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahim* na kisha wakaingia kwenye Mto ambao waliuvuka, huku Maji ya mto yakiwa hayajazamisha hata kwato za Farasi wao yaani ilikua kama wanatembea na Farasi wao juu ya kioo kilicowekwa juu ya Maji.

Abu Muslim Al Khawlani alifarki mnamo mwaka 62 Al Hijra Mjini Dimashq.

Naam, mfano huu wa kisa cha Abu Muslim Al Khawlani na Fayruz Al Daylami unatuthibitishia Ukweli wa Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yaliyomo ndani ya kitabu chake cha Qur'an na kudhihirisha kua maneno yaliyomo ndani ya kitabu hicho kitukufu ni ya haki na ni kutoka kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliyomshushia Mtume wake *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* pale aliposema katika aya ifuatayo:

﴿كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَلَوْ آمَنَ أَهْلُ ٱلْكِتَابِ لَكَانَ خَيْراً لَّهُمْ مِّنْهُمُ ٱلْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ ٱلْفَاسِقُونَ﴾

Kuntum khayra ommatin okhrijat lilnnasi ta/muroona bialmaAAroofi watanhawna AAani almunkari watu/minoona biAllahi walaw amana ahlu alkitabi lakana khayran lahum minhumu almu/minoona waaktharuhumu alfasiqoona *(Surat Al Imran 3:110)*

Tafsir: ***Hakika Nyinyi (Waislam) ni Ummah Bora uliowahi kuja kutokana na Watu, kwani mnaamrishana Mema na kukatazana Maovu na mnamuamini Allah, na kama watu wa Ahl ul Kitab wangeamini ingekua bora wao kwani ingawa miongoni mwao kuna watu walioamini lakini wengi wao ni waasi.***

Ambapo anasema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn `Abbas *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na aya hii kua: '**Aya hii inawahusu wale waliokua kwenye kizazi cha mwanzo cha Waumini wa Dini ya Kiislam yaani Masahaba na waliofuatia baada yao na watakaofuatia ambao watakua ni wenye hali ya kua kama ilivyoelezewa kwenye aya hii na wakaishi maisha yao kama ilivyoainishwa kwenye aya hii.'**

Ambapo *Mujaddid Ad Din Sultan al Mutakkalimin* Imam Fakhr Ad Din Al Razi basi yeye anasema kua: **'Amesema Imam Al Qaffal kua ingawa Ummah nyenginezo pia zilikua zikiamrishana Mema na kukatazana Mabaya na pia walikua ni wenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala*, lakini Ummah huu umepandishwa Darja ya kua ni Ummah Bora zaidi kwa sababu mbali ya kua unaamrishana Mema na Kukatazana maovu lakini pia unafanya Jitihada kupigania kuamrishana Mema na Kukatazana Maovu'** ambao huu pia ndio mtizamo wa Imam Al Suddi.

Ambapo kwa upande wa Imam Hasan Al Basr basi yeye anasema kua: '**Ummah wote wa Kiislam ni wenye kujumuishwa ndani ya maneno ya aya hii na hii ni kutokana na hadithi isemayo kua:**

Amesema Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Hakika mimi nimepewa mambo maalum ambayo hakuwahi kupewa Mtume yeyote abla yangu kwani mimi nimesaidiwa na Khofu,

nimepewa Funguo za Ardhini, nimeitwa jina la Ahmad na Mchanga umetagaziwa kua ni tohara kwangu na Ummah wangu umetangaziwa kua ni Ummah Bora.''

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Ummah wangu ni kama Maji ya Mvua yaani haiwezekani kusema ni matone yepi yenye manufaa zaidi yaliyotangulia au yanayofuatia.**'

Ambapo amesema pia Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Sisi tulikua tumekaa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo akatuuliza: 'Hivi jee nyinyi mnafikiria kua ni nani miongoni mwa viumbe ni wa bora zaidi Kiimani?**' Masahaba wakasema: '**Ni Malaika**'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: '**Itakuaje wasiwe na Imani wakati wao wako na Mola wao?**' hivyo Masahaba wakasema: **'Basi ni Mitume.**'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: '**Itakuaje wasiwe na Imani wakati wao wanapokea ujumbe kutoka kwa Mola wao?**' Masahaba wakasema: **'Basi ni Sisi'** *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: '**Itakuaje msiwe na Imani wakati mimi niko pamoja nanyi? Bali ni wale watakaokuja baada yenu ambao watayaona maandiko na kuyaamini.**''

Hivyo Alhamd lillah Masahaba Walimuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wakamuamini Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha wakafanya jitihada ya kubeba jukumu la kuusiana Mema na kukatazana Mabaya na kuendeleza Ilm ya Dini ya Kiislam kutokana na Imani kubwa waliyokua nayo ambapo miongoni mwao walikuwemo Masahaba Wanazuoni wakiwemo kina Ubay Ibn Qaab, Zayd Ibn Thabit, Abd Allah Ibn Abbas, Abd Allah Ibn Zubayr, Abd Allah Ibn Masud, Zayd Ibn Abd Allah Ibn Umar na Abd Allah Ibn Amr Al As *Radhi Allahu Anhum*, n.k

Ambao walitoa Wanafunzi wengi sana na hivyo Ilm yao ikatapakaa na kuenea katika kila sehemu ya Ardhi iliyokua na Waislam, na kuenezewa na Wanazuoni wa maeneo mbali mbali na wenye asili mbali mbali wakiwemo Waarabu, Waajemi, Waafrika, Wakurdi, Waturuki, Warusi, Warumi, Waliokua huru na pia waliokua Watumwa hapo kabla.

Kama anavyosema Imam Abu Abd Rahman Muhamamd Ibn Abd Rahman Ibn Abi Layla kua: **'Takriban Wanazuoni wote walikua hawana asili ya Uarabu' hivyo Isa Ibn Musa (Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Abd Allah Ibn Al Abbas *Radhi Allahu Anhu)* akaniuliza: 'Hivi Jee ni Nani Mufti wa Basra?' Nami nikasema: 'Al Hasan Ibn Hasan Al Basr na Muhamamd Ibn Sirrin' nae akauliza: 'Jee ni nani watu wawili hawa?' nami nikasema: 'Wote hawa walikua ni Watumwa walioachiwa**

huru.' nae akasema: 'Na ni nani Qadhi wa Makkah?' nami nikasema: 'Ataa Ibn Rabah, Mujahid na Said Ibn Jubayr' nae akauliza: 'Na ni nani watu hao?' nami nikasema: 'Watumwa walioachiwa Huru.'

Nae akauliza: 'Jee ni Nani Qadhi wa Mji wa Madina?' nami nikasema: 'Ni Zayd Ibn Aslam, Muhammad Ibn Al Munkadir na Nafi'i Ibn Abi Junayh' nae akauliza: 'Ni nani hao?' nami nikasema: 'Ni Watumwa walioachiwa huru' hivyo hapa muonekano wa Uso wake ukabadilika, na kisha akasema: 'Jee ni nani Qadhi wa Quba?' nami nikasema: 'Ni Rabia Ar Rai na Ibn Abi Zinad' nae akauliza: 'Ni Nani hao?' nami nikasema: 'Ni miongoni mwa Watumwa walioachiwa huru.'

Hapa muonekano wa uso wa Isa Ibn Musa ukawa ni wenye kuingia kiza, na kisha akasema: 'Jee ni nani Qadhi wa Yaman?' nami nikasema: 'Tawus, Watoto wake na Wahb Ibn Munabih' Isa Ibn Musa akasimama kutoka kwenye kiti chake huku akiwa ametokwa na mishipa ya uso na kuuliza: 'Na ni Nani Qadhi wa Khurasan?' nami nikasema: 'Ataa Ibn Abd Allah Al Khurasan' nae akaniuliza : 'Na ni nani huyo?' nami nikajibu: 'Ni Mtumwa alieachiwa Huru'

Uso wa Isa Ibn Musa ukawa mwekundu lakini akaamua kua mtulivu na hivyo akauliza: 'Jee ni nani Qadhi wa Syria?' Nami nikasema: 'Ni Makhul' nae akauliza: 'Jee Ndio nani huyo?' nami nikasema: 'Ni Mtumwa alieachiwa huru' hivyo akauliza: 'Ni Nani Qadhi wa Kufah?' nami nikataka kujibu kua ni Al Hakim Ibn Utbah na Amar Ibn Abi Salman, lakini nikawa na khofu juu ya kitakaochotokea nikisema hivyo, hivyo nikajibu: 'Ibrahim An Nakhai na Ash Shabi' nae akasema: 'Ndio nani hao?' nami nikasema: 'Ni Waarabu' nae akasema: 'Allahu Akbar' kisha akakaa kitako chini. *(Al-'Iqd Al-Farīd)*

Na Amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua : ***'Allah Subhanah wa Ta'ala* humjaalia Ilm yule amtakae, kwani kama Ilm ingekua imejaaliwa kwa ajili ya watu maalum basi kutokana na koo bora ndio wangekua wanaostahiki kua nayo zaidi, lakini hata hivyo Ata'a Ibn Rabah alikua ni Mtumwa wa Abyssinia, Yazid Ibn Habib alikua ni Mnubi na Hasan Al Basr na Muhamamd Ibn Sirin wote walikua ni Watumwa.**'

Hivyo Basi Wanazuoni hawakua ni wenye asili ya Makkah na Madina tu, Wala hawakua ni Waarabu na Watu waliokua huru tu, bali walikua ni watu wenye kutokana na asili ya hali ya mazingira tofauti na kutoka katika maeneo mbali mbali kama tutakavyoona katika Historia za maisha yao na ni kutokana na Taqwa na Imani waliyokua nayo, hivyo jitihada zao ilikua ni sehemu ya kuonesha shukrani kwa Mola wao kutokana na neema ya Ilm aliyowajaalia kua nayo, hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawazidishia juu ya neema aliyowajaalia na hivyo wakafanikiwa kutufikishia na sisi yale waliyofikishiwa wao, ambapo wachache miongoni mwao Wanazuoni hao ni pamoja na wafuatao:

QADHI SHURYAKH AL YAMANI

Qadhi Shuraykh Ibn Al Harith Ibn Qays Ibn Al Jahm Al Kindi Al Qadhi *Al Yamani* alikua ni *Mukhadram* yaani Muislam ambae aliishi katika kipindi cha Ujahiliyyah na pia akaishi katika kipindi cha Uislam na kusilimu lakini hakuwahi kuonana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Shurayh Ibn Al Harith Ibn Qays Ibn Al Jahm Al Kindi Al Qadhi *Al Yamani* ambae alikua ni Mwanafunzi wa Sahaba Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* na hivyo baadae akahamia katika mji wa Madina na kutoa hukmu katika tukio lililotokea katika kipindi cha Utawala wa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*

Hivyo katika kipindi hicho basi *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alinunua Farasi kutoka kwa Bedui mmoja, kisha akamlipia Farasi huyo na kisha akampandia na kuondoka nae. Lakini baada ya kusafiri kwa mda, basi *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akagundua kasoro iliyopo kwenye farasi huyo na hivyo akamrudisha Farasi huyo kwa Bedui aliemuuzia kutokana na kasoro hio. Na hapo Bedui huyo akagoma na kusema kua Farasi huyo aliponunuliwa alikua mzima.

Hivyo *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu akamwambia Bedui* huyo kua achague Qadhi ambae atahukumu kesi yao hio ya *Al Kharaj bi Al Dhamana,* hivyo Bedui huyo akamchagua Shuraykh Ibn Harith Ibn Qays Ibn Jahm Al Kindi Al Yamani kua ndio awe Qadhi wa kuamua madai hayo, ambapo *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akakubaliana shauri hilo.

Na baada ya kesi hio kufikishwa kwa Shuraykh Ibn Harith Al Kindi Al Yamani na kusikiliza basi akamwambia *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu:* ‘***Ya Amir ul Muuminin*** **hivi ulipomchukua farasi huyu alikua ni mzima na hana kasoro?**’ *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu akajibu:* ‘**Naam!**’.

Hivyo Shuraykh Ibn Harith Al Kindi Al Yamani akasema: ‘***Al Kharaj bi Al Dhamana.*** **Hivyo kaa nacho ulichokinunua au kirudishe kwa mwenyewe kama kilivyokua wakati ulipokinunua.**’

Kutokana na Hukmu hio basi *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamwangalia Shuraykh Ibn Harith Al Kindi Al Yamani huku akitabasam kwa kumhusudisha kutokana na Uadilifu wake. Halafu akamwambia: ‘**Ya Shuraykh hakika mimi nimekuchagua wewe kua uwe *Qadhi* Mkuu wa Mji wa Kufah.**’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ama kwa upande mwengine basi katika kuagalia ushahidi katika amana na dhamana basi tunarudi tena kwa Shuraykh Ibn Harith Ibn Qays Ibn Jahm Al Kindi Al Yamani ambae nae katika kipindi cha Utawala wa *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* ambapo *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alipoteza ngao yake ambayo alikua anaipenda sana, na kisha kwa bahati nzuri akaja akaikuta Ngao hio inauzwa katika Soko la katikati ya Mji wa Kufah, na mmoja kati ya wauzaji ambao hakua Muislam.

Amir ul Muuminin Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alipoiona tu ngao hio akaijua na kusema kua hio ni ngao yake na akamwambia Muuzaji duka huyo sokoni hapo kua: '**Hii ni ngao yangu na ilinianguka katika sehemu fulani na katika siku fulani.'**

Yule muuzaji akasema: '**Laa! Hii ni ngao yangu ambayo imo ndani ya mikono yangu.**' *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akajibu: '**La hii ni ngao yangu kwa sababu mimi sijawahi kuiuza ngao hii kwa mtu yeyote yule na wala sijawahi kumpa mtu yeyote**.'

Hivyo ikawa kuna ugomvi ambapo *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akamwambia yule Muuzaji duka kua bora atafutwe mtu atoe hukmu ya kesi hio. Yule Muuzaji akakubali na kusema kua hakimu anaemtaka yeye kuhukumu kesi hio inabidi awe ni *Qadhi Al* Shuraykh Ibn Harith Ibn Qays Ibn Jahm Al Kindi Al Yamani.

Na walipofika kwa *Qadhi* Shuraykh Ibn Harith Ibn Qays Ibn Jahm Al Kindi Al Yamani basi *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akaelezea kua Ngao hio ni yake lakini ilipotoea na kwa kua hakuiuza wala hakumpa mtu yeyote kwa kumgaia basi ngao hio ni yake. Ama kwa upande wa yule Muuzaji ambae alikua si Muislam basi hakusema kama *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* anasema uongo ama la bali alisema tu kua: '**Ngao hii ni yangu kwani imo mikononi mwangu.**'

Hivyo *Qadhi* Shuraykh Ibn Harith Ibn Qays Ibn Jahm Al Kindi Al Yamani akamwambia *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Kwa hakika mimi ninakuamini wewe kua usemayo kua ni kweli. Lakini sasa ili niamue kwa haki kama ninavyoamini basi inabidi wapatikane mashahidi wako wawili.'**

Amir ul Muuminin Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema kua: '**Kwa hapa katika mji huu mimi ninao watu mashahidi wawili tu ambapo wa kwanza ni Qanbar ambae ni Msaidizi wangu na wa pili ni Mtoto wangu Al Hasan.**'

Al *Qadhi* Shuraykh Ibn Harith Ibn Qays Ibn Jahm Al Kindi Al Yamani akasema kua: '***Ya Amir ul Muumin* hakika wewe unajua kua Mtoto hawezi kua shahidi kwa ajili ya manufaa ya Baba yake.**'

Amir ul Muuminin Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema kua : '**Ya Shuraykh ! Inakuaje kua mtu alietabiriwa Pepo hawezi kua Shahidi? Hivi jee wewe hukuwahi kusikia aliyoyasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Hasan na Husayn kua ni mabwana wa Vijana wa Peponi?**'

Hapo *Qadhi* Shuraykh Ibn Harith Ibn Qays Ibn Jahm Al Kindi Al Yamani akasema: '**Naam! Nimesikia. Lakini sasa tunarudi pale pale kua Mtoto hawezi kua shahidi kwa ajili ya manufaa ya Baba yake.**'

Hivyo *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akamgeukia yule muuzaji Duka na kusema: '**Basi chukua hio Ngao kwani kwa hakika mimi sina Shahidi mwengine'** yule Muuza Duka nae akajibu: '**Ya Ali! Chukua wewe hii Ngao! Ama kwa hakika hii Dini yenu ni Dini ya Haki kweli, kwani mimi nnao uwezo wa kumshitaki *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib na kisha nnaweza kumfanya *Qadhi* atoe hukmu kulingana na Madai yangu. Hakika nami najitangazia kua kuanzia sasa hivi Mimi ni Muislam.'**

Na kisha baada ya hapo akamwambia *Qadhi* Shuraykh Ibn Harith Ibn Qays Ibn Jahm Al Kindi Al Yamani kua anaenda kujiunga na Jeshi la *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* ambapo *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akampa jamaa huyo Ngao hio na pia akampa na Farasi, baadae muuza Duka huyo akawa ni miongoni mwa Wanajeshi waliokua upande wa *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* katika vita vya *Siffin.*

Katika tukio jengine linalo onesha uadilifu wake Qadhi Shuraykh basi tunaona kua aliamua kumfunga Jela Mtoto wake kutokana na kosa la kuzia utekelezwaji wa haki na kumwambia: '**Hakika wewe Mtoto wangu ni bora kwangu mie kuliko kitu chengine chochote kile Ulimwenguni, lakini hata hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni bora kwangu mie na nampenda zaidi kuliko nnavyokupenda wewe**.'

Ambapo tunapoangalia matukio haya basi tunaona kua Qadhi Al Shuraykh alikua ni mwenye uadilifu wa hali ya juu ambao unatakiwa kua nao kila Muislam kama zinavyoamrisha aya pale ziliposema:

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ كُونُواْ قَوَّامِينَ بِٱلْقِسْطِ شُهَدَآءَ لِلَّهِ وَلَوْ عَلَىٰ أَنْفُسِكُمْ أَوِ ٱلْوَالِدَيْنِ وَٱلأَقْرَبِينَ إِن يَكُنْ غَنِيّاً أَوْ فَقِيراً فَٱللَّهُ أَوْلَىٰ بِهِمَا فَلاَ تَتَّبِعُواْ ٱلْهَوَىٰ أَن تَعْدِلُواْ وَإِن تَلْوُواْ أَوْ تُعْرِضُواْ فَإِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيراً﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ya **ayyuha alladheena amanoo koonoo qawwameena bialqisti shuhadaa lillahi walaw AAala anfusikum awi alwalidayni waal-aqrabeena in yakun ghaniyyan aw faqeeran faAllahu awla bihima fala tattabiAAoo alhawa an taAAdiloo wa-in talwoo aw tuAAridoo fa-inna Allaha kana bima taAAmaloona khabeeran** *(Surat An Nisaa 4:135)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini kuweni wenye kusimamia haki wenye kushuhudia kwa ajili ya Allah, hata kama itakua ni dhidi ya Nafsi zenu: Au Wazee wenu au Watu wa Karibu yenu iwe mtu huyo ni tajiri au ni masikini, kwani Allah ni m-bora wa usimamizi kwa wote, hivyo msifuate Matamanio yenu, hivyo msiuepuke Uadilifu, kwani mkiepuka au mkizuia Uadilifu basi kwa hakika Allah ni mwenye kua na habari juu ya kila mnachokifanya.***

Ambapo anasema Imam Adh Dhahabi kua: '***Qadhi*** **Shuraykh alikua na Nyumba ambayo alikua akiingia ndani yake katika siku ya Ijumaa tu na kukaa peke yake na hakuna hata mtu mmoja aliekua akijua alikua akifaya nini ndani yake.**'

Ambapo alisema Qadhi Shuraykh kua: '**Hakika mimi ama nikipatwa na Mitihani basi hua ni mwenye kumshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* mara 4:**

Kwanza kwa kunijaalia mtihani ambao si mbaya zaidi ya huo alionipa.

Pili hua namshukuru pale anaponipa Subra ya kuustahmilia Mtihani huo.

Tatu Hua namshukuru kwa kunijaalia mimi kua ni mwenye kusema *Istijara* yaani '*Inna lillahi wa inna Ilayhi Rajiuun*' kwa ajili ya kupata Malipo bora zaid.

Nne hua namshukuru kwa kutoufanya Mtihani huo kua katika Mitihani ya Dini yangu.'

Ama kwa upande mwengine basi Qadhi Shuraykh alikua ni Miongoni mwa Wanazuoni wanaowapenda Sana Wake zao na kubainisha wazi Mapenzi yao hayo, kwani alisema Qadhi Shuraykh kuhusiana na Mkewe aitwae Zaynab kua: '**Hakika mimi nimewaona watu wakiwapiga wake zao, hivyo namuomba Allah aupoozeshe Mkono wangu kama mimi nikimpiga Mke wangu, kwani Zaynab ni kama Jua na Wanawake wengine ni kama Nyota, hivyo Jua linapochomoza basi Nyota hutoweka.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ZAYNAB BINT JARIRI AL HANZALI AL TAMIMI

Zaynab Bint Jariri alikua ni Mwanamke Mcha Mungu na ni mfano wa kuigwa miongoni mwa Wanawake wema kwani alikua ni mke wa Qadhi Al Shuraykh Al Yamani.

Ambapo anasema Imam Ash Ashabi kua: '**Siku moja Shuraikh aliniambia mimi kua: 'Ewe Ash Shabi unajua kua wewe unatakiwa uowe Mwanamke wa Banu Tamim? Kwani wana ufaham mzuri sana.'**

Hivyo nami nikamuliza: **'Ufahamu wao ukoje?'**

Shuraykh akasema: **'Siku moja mimi nilikua narudi Mazikoni katika kipindi cha wakati wa mchana, nikapita kwenye makazi ya watu wa Banu Tamim, na nikamuona Mwanamke mzee ambae alikua amesimama kwenye mlango wa Nyumba yao na Binti ambae uzuri wake sijawahi kuuona hapo kabla, hivyo nami nikakaribia Nyumba hio na kisha nikaomba kinywaji, japo kua sikua ni mwenye kua na kiu, ambapo Bibi huyo akaniuliza: 'Jee unataka kunywa nini?' nami nikasema: 'Chochote kile'**

Hivyo yule Bibi akamwambia yule Binti: 'Haraka sana kamletee Maziwa kwani huyu ni mgeni muhimu kwetu.'

Hivyo nami nikamuuliza yule Bibi: 'Huyu binti ni nani?'

Nae akasema: 'Ni Zainab Bint Jariri Al Hanzala'

Nami nikauliza: 'Jee kaolewa ama bado.'

Bibi huyo nae akanijibu kua hajaolewa, hivyo nikaomba kua nilete posa ili nimuoe na Bibi huyo akaniambia kwa kutumia lafdhi ya watu wa Banu Tamim kua: 'Sawa In-shaa Allah kama atakukubali''

Na kisha nikarudi Nyumbani nikapumzika lakini akili yangu yote ilikua kwa Binti yule, hivyo nikasali na kisha nikaelekea kwa ndugu zangu kina Al Alqamah, Al Aswad, Al Musayib na Musa Ibn Arfat, na kisha tukatoka hadi kwa Ami yake yule Bint, na aliponiona akasema: 'Ya Abu Umayah, Jee ulikua unataka nini?'

Nami nikasema: 'Nataka kumuoa Zaynab ambae ni Bint wa Kaka yako.'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo nae akasema: ‘Hata yeye pia amesema kua anataka kuolewa nawe’ na hivyo tukaoana.

Baada ya kumuoa ndio nikakumbuka ugumu wa nyoyo za Wanawake wa watu wa Tamim na kuanza kujuta kwanini nikamuoa, lakini nikasema: ‘Nitafanyaje mimi? Bora nimuache au, lakini Sina la kufanya kwani ndio nimeshamuoa, hivyo bora nimuangalie labda nitaridhika nae, na kama sikuridhika nae basi nitafanya nitakavyoridhika’

Ewe Ash Shabi kama ungewaona, namna Wanawake wao walivyokua wakimuusia Mwanamke huyo wakati walipomleta kwangu, na kwa kua najua kua kama Mke akienda kwa Mume wake basi Mume na asali Rakaa 2 na kisha amuombe *Allah Subhanah wa Ta’ala* amjaalie kile kilichokua na kheri kutoka kwa Mke wake na amlinde kutokana na shari iliyomo ndani yake, basi nami nikasali na kisha nikatoa Salamu, nami nikaona kua nae amesali na kua ananiombea mimi Dua, na kisha baada ya kuomba dua akaja mfanyakazi akachukua nguo zangu na kisha akanipa Kanzu ya rangi ya njano ya kiza na kunivisha.

Na kisha nyumba ilipokua haina watu, tupo mimi na yeye tu, basi nikamkaribia na kutaka kumshika kiuno chake, lakini nae akasema: ‘Subiri ewe Abu Ummayah simama hapo hapo ulipokuwepo’ kisha akasema: ‘*Alhamd Lillah Rabbi Al Alamin Iyyaka NaaAbudu wa Iyyaka NastaA’in, wa Salallahu ala Muhammad wa alihi,* hakika mimi sikujui wewe na wala sizijuia tabia zako, hivyo kwanza niambie mie ni kipi unachokipenda kuhusiana nami ili nishikamane nacho na kipi hukipendi ili niachane nacho, kwani tumeshaoana na haya ndio majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* juu yetu, na kuanzia sasa hivi mimi ni wako na hivyo fanya kama alivyoamrisha *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua ‘Kaa nae au achana nae kwa usalama’, hayo ndio niliyokua nataka kukuambia, nami naomba msahama kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa ajili yangu mie na kwa ajili yako wewe.’

Shuraykh akaendelea kusema kua: ‘Ya Ash Shabi, Zaynab alinipelekea mimi kusema bila ya kutoka maneno yafuatayo: ‘‘*Alhamd Lillah Rabbi Al Alamin Iyyaka NaaAbudu wa Iyyaka NastaA’in, wa Salallahu ala Muhammad wa alihi,* Hakika wewe umesema Maneno mazuri sana, hivyo kama utashikamana nayo basi basi utafaidika sana na kama ukiachana nayo basi utakula hasara kubwa sana, hakika mimi nakipenda hiki na hiki na sikipendi hiki na hiki, na hivyo sasa hivi tumeshaoana na tuko pamoja na hatutotengana, ukiona jambo jema basi lizungumzie na ukiona baya basi achana nalo.’

Halafu Zaynab akasema kitu ambacho nimekisahau sikikumbuki tena, na kisha akaniuliza: ‘Hivi jee unasemaje kuhusiana na kutembeleana kifamilia’ nami

nikasema: ‘Hakika mimi sipendi wakati watu wanapokua wanakuja na kunishughulisha shughulisha sana.’

Hivyo nae akauliza: ‘Hivi Jee unataka nimruhusu nani na nani miongoni mwa Majirani zako kua wanaweza kuja nyumbani kwako? Kwani utakaowaruhusu basi nami nitawaruhusu na utakaokataa wasije nami nitakataa’ Nami nikamwambia: ‘Familia fulani ni nzuri na waadilifu na Fulani sio waadilifu.’’

Ewe Ash Shabi hakika katika usiku wa siku hio mimi nililala nikiwa na furaha kubwa sana, Zaynab aliishi na mie kwa mda wa Mwaka mzima nami sikuwahi kuona jambo lolote lile baya kuhusiana nae, ambapo baada ya mwaka siku moja nilirudi safarini kwenye vikao vya Mahkama ya Qadhi, nami nikamuona Bibi mzee akiwa anasimamia nyumbani kwetu.

Hivyo nikauliza: ‘Huyu ndio nani’ na nikaambiwa kua: ‘Huyu ndio Mama mkwe wako’ hapo nami nikasahau kila kitu, na hivyo nikakaa kitako na kumuangalia yule Bibi, ambae sijawahi kumuona hapo kabla, ambapo nae akasema: ‘*Salaam Alayk* ya Abu Umayah’ nami nikaitikia: ‘*Wa Alaykum Salaam*, wewe ni nani?’ nae akasema: ‘Mimi ni Mama mkwe wako’

Nami nikasema: ‘Namuomba Allah akukaribishe karibu yake’ nae akaniuliza: ‘Vipi kuhusiana na hali ya mke wako?’ nami nikajibu: ‘Mke wangu ni mzuri sana *Ma-shaa Allah*’

Nae akasema: ‘Ewe Abu Umayah, Mwanamke hua si mbaya pale inapokua kuna sababu 2; Akijifungua Mtoto wa Kiume na akikubalika kwa Mume wake, hivyo kama unashaka nae, basi chukua bakora, Wa Allahi hakuna kitu kibaya ndani ya Nyumba ya Mume kama Mke alieharibika.’

Nami nikasema: ‘Wa Allahi Hakika wewe una Malezi mazuri sana.’

Nae akasema: ‘Hivi Jee unataka Mama mkwe wako awe anakutembelea.’

Nami nikajibu: ‘Naam wakati wowote.’

Hivyo Mama Mkwe wangu akawa anakuja katika kila mwanzoni mwa mwaka kwa ajili ya kunipa wasia mzuri zaidi ya uliopita, nami nikaishi na mke wangu kwa miaka 20 bila ya kugombana nae wala kumgombeza hata mara moja, isipokua mara moja tu, tena kwa sababu ya kumuonea, kwani sikuwa ni mwenye kufanya uadilifu juu ya jambo hilo ambalo ni kua, Muadhini aliadhini baada ya sisi kusali Sunna Rakaa 2, wakati mimi nikiwa ndie Imam wa Kijiji kizima. Nilimuona N’ge

akiwa anakaribia, hivyo nami nikachukua sufuria kisha nikamfunika Nge huyo na kusema: 'Zaynab usiondoke mpaka nirudi.'

'Ya laiti kama ungemuona ewe Ash Shabi wakati niliporudi kusali kwani nilikuta kua tayari ameshatafunwa na Nge, na Zaynab amekaa pale pale akiwa na maumivu makali sana tangu nilipomuacha kabla ya kuenda Msikitini, hivyo nikachukua Chumvi, na kisha nikaanza kumsugulia kidole chake alichotafunwa na kumsomea *Surat Al Fatiha, Al Falaq na Al Nas.'* *(Tabai' an-Nisaa cha Ibn 'Abd Rabbih al-Andalusi)*

UWEYS AL QARNI

Uweys Ibn Amir Al Qarni alizaliwa katika ardhi ya Mji wa Qarn nchini Yemen katika kipindi cha kabla ya Uislam, na hivyo alikua ni Muislam baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kupata Utume ingawa hakuwahi kuonana nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hakuwahi kutembelea kwenye Mji wa Madina hadi katika kipindi cha Utawala wa *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*

Uweys Al Qarni alikua ni mwenye kazi ya kufuga wanyama katika ardhi ya Yemen ambapo miongoni mwa Wanyama aina ya Ngamia, ambao hata hivyo hawakua wake bali walikua wenye kumilikiwa na watu wengine, na hivyo hakua ni mwenye kupatana na wamiliki wa Wanyama hao kuhusiana na malipo ya uchungaji huo, kwani yeye alikua ni mwenye kuridhika na kila akipatacho kutokana na kua ni mwenye kujua kua ndio majaaliwa yake kutoka kwa *Allah Subahanh wa Ta'ala.*

Uweys Al Qarni alikua ni mwenye kuhisi yeye na Mama yake tu kwenye Kibanda chake na hivyo kila akipatacho alikua akikitumia kwa ajili yake na mama yake na kwa ajili ya kuwasaidia masikini kwa kuwapa kama sadaka. Baada ya kupata habari za kuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* basi Uweys Al Qarn alikua ni mwenye kuingia kwenye Uislam moja kwa moja na kua na hamu sana ya kutaka kuonana nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kutokana na kua na mapenzi nae zaidi ya anavyompenda mtu yoyote yule, lakini ilikua ni vigumu kwake kumuacha Mama yake ambae nimtu mzima kwa ajili ya kufunga safari ya miezi kutoka nchini Yemen kuelekea kwenye Mji wa Madina kwa ajili ya kukutana nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na hivyo kutokana na mapenzi yake hayo makubwa basi Uweys Al Qarni kamwe hakua ni mwenye kumsahau Mola wake, kwani alikua ni mwenye kua kila wakati ni wenye kumfikiria *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam,* na

hivyo pia kua ni mwenye kuwausia wengine juu ya Mola wake na kuwaamrisha kufanya mema na kuwakataza kufanya maovu.

Kwani alikua anasema *Uways Al Qarni* kua: **‘Ogopeni Adhabu ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kama vile ambavyo mnavyoogopa kua na kosa la kuua watu wote.’**

Na amesema Asbagh Ibn Zayd kua: **‘Uways Al Qarni alikua akisema kila siku inapoingia jioni kua: ‘Usiku wa leo ni kwa ajili ya Kurukuu na hivyo hua ni wenye kurukuu usiku huo kucha hadi Alfajir, na inapofika jioni ya siku ya pili basi hua ni mwenye kusema: ‘Usiku huu ni kwa ajili ya Kusujudu’ na hivyo usiku wa siku hio ndani yake hua ni mwenye kusjudu kucha. Na jioni nyengine inapowadia basi husema kua Usiku huu ni wa Sadaqa tu, na hivyo Usiku huo kucha hua ni mwenye kutoa Sadaqa tu kutokana na kila kitu chake cha ziada alichokua nacho, na kisha hua ni mwenye kusema: ‘Ya Allah yeyote yule atakaefariki kutokana na njaa basi usinibebeshe mie jukumu kutokana na njaa yake, na yeyote atakaefariki kutokana na baridi kwa kukosa nguo basi usinibebeshe mie jukumu kutokana kutomvisha nguo mtu huyo.’’’**

Ambapo mbali ya kua hawajawahi kuonana lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua ni mwenye kua na habari juu ya Uweys Al Qarni na namna anavyompenda yeye na *Allah Subhanah wa Ta’ala,* na pia namna anavyomheshimu na kumhudumia Mama yake, kwani alikua akisema: **‘Uweys Al Qarni ni mtu mwenye mfano bora wa Ihsan na kufanya wema.’**

Na baadhi ya wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisimama na kuangalia katika upande wa kusini wa Mji wa Madina kuelekea katika ardhi ya Yemen na kusema: **‘Hakika mimi nnasikia Upepo wa Rehma unaopepea kutoka katika ardhi ya Yemen.’**

Alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **‘Katika siku ya Malipo *Allah Subhanah wa Ta’ala* atajaaliwa kuwemo Malaika 70,000 ambao watakua katika Maumbile ya sura ya Uways Al Qarni na kisha atamuweka Uways Al Qarn pamoja nao miongoni mwao, na wataingizwa Peponi bila ya kujua ni yupi ndie Uways Al Qarni miongoni mwao.’**

Na akasema pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘**Kuna mtu katika Ummah wangu ambae ataruhusiwa kuwaombea watu katika siku ya Malipo, watu ambao idadi yao ni sawa na idadi ya Kondoo na Manyoya yao Kondoo wa Bani Rabia na Bani Mudar.’**

Kwani katika kipindi hicho ilikua hakuna Kabila lenye Kondoo wengi kama Makabila mawili hayo katika ardhi nzima ya Hijaz, hivyo Masahaba wakauliza: **'Jee Mtu huyo ndio nani huyo Ya Rasul Allah?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua: **'Kuna Mja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Masahaba wakasema: **'*Ya Rasul Allah* Sisi sote pia ni Waja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema kua: **'Ni Uways'**

Masahaba wakauliza: '**Yuko wapi Mtu huyo?**' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: **'Yupo katika maeneo ya *Al Qarn.*'**

Masahaba wakauliza: **'*Ya Rasul Allah,* hivi jee amewahi kukuona wewe?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **'Hajaniona kwa Macho ya Uso wake.'**

Masahaba wakasema: **'Inakuaje hadi ikawa anakupenda Sana lakini hawezi kuja kuonana nawe.'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema kua: **'Hawezi, na hii ni kutokana na sababu mbili, kwanza amezuilika, na pili ni kutokana na kujitolea kwake Kiimani, kwani Mama yake ni Mzee sana, halafu kipofu na hawezi kutembea, hivyo Uways hua ni mwenye kujichumia kipato chake kutokana na uchungaji wake wa Ngamia wakati wa mchana na usiku humhudumia Mama yake kutokana na malipo yake aliyoyachuma.'**

Masahaba wakauliza: 'Hivi Jee sisi tutaonana nae?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema kumwambia Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Wewe hutowahi kumuona katika wakati wako**' na kisha akawaambia Umar Ibn Al Khattab na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhum* kua: '**Nyinyi mtamuona, mwili wake una Nywele nyingi na ana weupe kidogo kwenye upande wa ubavu kushoto na kwenye kiganja chake, sio kama weupe wa ugonjwa, mkikutana nae mpeni salam zangu na mwambieni auombee Ummah wangu.'**

Hivyo Uways Al Qarni aliishi na Mama yake katika ardhi ya Al Qarni hadi pale alipofariki Mama yake huyo basi akahama katika Mji huo na kuelekea katika Mji wa Kufah nchini Iraq.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Wakati *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* alipokua anakaribia kufariki Dunia aliwaambia Masahaba zake kua anataka Shati lake apewe Uways Al Qarni, hivyo mda baada ya kufariki kwake basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu na* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* wakaelekea katika ardhi ya Kufah na wakamuulizia Uways Al Qarni ambapo nao wakaambiwa kua: **'Ni mtu ambae kama mwenda wazimu kwani ni mwenye kupenda kuishi peke yake peke yake na hua ni mwenye kuwakimbia watu, kwani akikaa nao basi hua ni mwenye kulia pale watu wanapocheka, na mda wote hua ni mwenye kua na huzuni'**

Hivyo nao wakamuulizia anapatikana wapi, na akasema kua alionekana kwenye maeneo ya bonde la Arni Hivyo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu na* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* wakaelekea kwenye eneo hilo na wakamkuta akiwa anasali. Hivyo wakamsubiri na baada ya kusali wakamsalimia na kujitambulisha na kisha nao wakamuuliza jina lake ambapo nae akasema kua ni Abd Allah.

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema kua: **'Sisi sote ni waja wa *Allah Subahanh wa Ta'ala,* hivyo jee jina lako halisi ni nani?'** nae akasema: **'Uways'.**

Hivyo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: **'Tunaomba utuoneshe mikono yako'** ambapo nae akawapa na wakaiangalia, na kisha Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: **'Mtume wetu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anakutumia Salaam zake na ametupa sisi hili shati lake kua tukupe kama zawadi kutoka kwake na kusema kua ulivae na kisha uuombee Ummah wake.'**

Uways Al Qarni akasema: **'Ewe Umar, hivi huoni kua mimi ni mtu dhaifu, nisiekua na uwezo wa kujiombea hata dua kutokana na dhambi zangu, hivi kweli hamjakosea nyinyi? Yaani kua mmetumwa mumpe hili shati na kisha kuombewa dua na Mtu mwengine badala yangu?'**

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: **'La, hatujakosea, kwani sisi tumeambiwa kua ujumbe tumfikishie Uways Al Qarni, na bila ya shaka kwa namna tulivyoeleezewa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya sifa zako na muonekano wako kulingana na vithibitisho tulivyoviona basi mtu huyo ni wewe.'**

Hivyo Uways Al Qarni akalipokea Shati hilo na kisha akalibusu akalinusa na kisha kujipangusia usoni mwake na kisha akasema: **'Nisubirini hapa hapa'** na kisha akaondoka akapinga hatua mbili tatu na akalivaa Shati hilo kwa unyenyekevu mkubwa sana na kisha akasjudu huku akiwa ni mwenye kusema ndani yake sijida hio kua: **'Ewe Mola wangu, hakika Mtume wako *Salallahu Alayhi wa Salam*, amemtuma Umar Ibn Al Khattab na Ali Ibn Abi Talib kuleta Shati lake tukufu kwangu mimi mja wako masikini nisiekua na uwezo wa kitu chochote, hivyo nakuomba kwa ukubwa**

wako na uwezo wako na usamehemvu wako uusamehe Ummah wa Mtume wako Muhamamd kutokana na makosa yao, kwani wewe ni mwenye wingi wa huruma na usamehevu'

Na hivyo shati hilo la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, alilozawadiwa Uways Al Qarni ndio lile shati ambalo alipewa zawadi Sultan Abd Al Hamid wa Dola la Kiislam la Ottoman mnamo mwaka 1618, nae akalijengea katika Msikiti wa Hirkai Sharif uliopo Instabul Uturuki.

Ambapo alisema Imam Sufyan Ath Thawry kua: **'Uways Al Qarni alikua ana Joho ambalo alikua akilivaa hua linaburura Ardhini wakati anapokaa kitako, na hivyo alikua akisema: 'Ya Allah nnaomba samahani juu yako kwa Tumbo lenye njaa, na mwili uliokua haujavishwa nguo, lakini mimi similiki chochote Duniani hapa isipokua hiki nilichokua nacho mgongoni na nilichokua nacho ndani ya tumbo langu''***(Mustadrak Al Hakim)*

Ambapo kwa upande wa Imam Amr Ash Shabi basi amesema kua: **'Kuna mtu kutoka katika ukoo wa Murad alipishana na Uways Al Qarni na kumuuliza: 'Vipi hali yako asubuhi hii ya leo?' ambapo Uways Al Qarni akajibu: '*Alhamd lillah*' akaulizwa: 'Vipi maisha yako?'**

Nae akajibu: **'Maisha yangu ni ya mtu ambae sasa hivi sifikirii kua nitaishi hadi Jioni na inapofika jioni hua sifikirii kua kama nitakua ni mwenye kufika kua hai hadi asubuhi' na hivyo sijui kama nitaingia Peponi au Motoni : 'Ewe Mtu wa Bani Murad, hakika Kifo na kukikumbuka Kifo hua hakumpi furaha wala utulivu Mtu anaemuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani Ilm yake juu ya Haki za Mola wake hua haimpi nafasi juu ya usimamizi wa Mali zake, na kusimamia kwake haki hua hakumruhusu kua na rafiki yeyote''**

Katika kipindi ambacho Uways Al Qarni alipokua anaishi katika maeneo ya Mji wa Kufah basi mbali ya kua alikua akaijaribu kukaa mbali na watu na kutochanganyika nao, lakini kuna wale waliokua wakimjua, ilikua ni wenye kumfuatilia kwa ajili ya kunufaika kutokana nae, ambapo mmoja wapo watu hao alikua ni Harim Ibn Hayyan ambae alimjua habari zake baada ya kusikia kupitia katika Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu yake.

Hivyo anasema Harim Ibn Hayyan kua: **'Mimi nilitaka kuonana na Uways Al Qarn, kutokana na kusikia Hadith inayomzungumzia kuhusiana na uwezekano wa uombezi wake, na hivyo nikafunga safari hadi katika mji wa Kufah, na kuanza kumtafuta na mwisho wake nikamkuta ukingoni mwa Mto wa Euphrate akiwa anatia Udhu, na moja kwa moja nikamjua kwa sababu hapo zamani pia mimi nilikua namjua.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

'Na nilipofika karibu yake nikamsalimia, nae akajibu salamu yangu, nikataka kumpa mkono lakini akanitizama na kisha hakuupokea mkono wangu huo. Nami nikasema: 'Allah akuingize kwenye Rehma zake ewe Uways na akusamehe dhambi zako pia, vipi hali yako?'

Kwa sababu alikua anatia huruma alikua amekonda sana tofauti na ninavyomjua mimi hapo kabla, kiasi ya kua muonekano wake ulinifanya nianze kutokwa na machozi, ambapo nae akaanza kulia pia huku akisema: 'Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akupe maisha mazuri na marefu ewe Harim Ibn Hayyan, vipi nawe hali yako?''

Nami nikasema: **'*Alhamd lillah,* hebu Niambie kuhusiana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*'**

Nae akasema: **'Hakika mimi sijawahi kuonana nae, bali nilikua ni mwenye kusikia habari zake kutoka kwa watu wengine, na wala mimi sina Ilm ya hadith, na sitaki kua Muhadith wala Mufti, bali nna mambo mengine ya shughuli zangu ambayo siyawezi.'**

Hivyo nikamwambia niusie basi japo kidogo, ambapo nae akauchukua mkono wangu akautizama na kisha akasema : ***'Audhu Bi Allahi Minna Al Shaytani Al Rajim'* na kisha akaanza kulia, huku akiwa ni mwenye kusema kua: 'Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:**

﴿وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلإِنسَ إِلاَّ لِيَعْبُدُونِ﴾

Wam<u>a</u> khalaqtu aljinna waal-insa ill<u>a</u> liyaAAbudooni *(Surat Adh Dhariyat 51:56)*

Tafsir: ***Na sikuwaumba Majini na Ibn Adam isipokua kwa ajili ya kuniabudu mimi.***

Na kisha akasema tena katika aya nyengine kua:

﴿وَمَا خَلَقْنَا ٱلسَّمَآءَ وَٱلأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لاَعِبِينَ﴾

Wam<u>a</u> khalaqn<u>a</u> alssam<u>a</u>a waal-ar<u>dh</u>a wam<u>a</u> baynahum<u>a</u> l<u>a</u>AAibeena *(Surat Al Anbiyah 21:16)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

*Tafsir: **Na sikuziumba Mbingu na Ardhi na kila kilichomo baina yake kwa ajili ya mchezo.***

Na kisha baada ya kusoma aya mbili hizo basi akapiga ukele mkubwa sana kama wa mtu mwenye maumivu makali sana hadi nikadhania kua labda ameingia wazimu, kisha akaniuliza: '**Ewe Harin Ibn Hayyan, hivi kwanini ukanifuata mimi?'** nami nikamwambia: **'Kwa sababu nilikua na hamu ya kukuona na pia kutaka kuzungumza nawe'** hivyo nae akasema: **'Hakika mimi siwezi kumpa ushauri mtu yeyote anaetaka kua na ukaribu nami, hivyo ushauri wangu kwako ni kua: Unapoingia Usiku nawe ukaenda kulala, basi fahamu kua kifo hua kipo chini ya Mto wako, na unapoamka asubuhi basi fahamu kua Kifo kipo mbele yako.**

Usiangalie udogo wa Dhambi, bali angalia ukubwa wa yule unaemuasi, kwani ukiichukulia Dhambi kua ndogo basi nawe hua unakua unamfanya Mola wako kua Mdogo, na ukiichukulia kua ni kubwa basi hua unamfanya Mola wako mkubwa zaidi aliekukataza dhambi hio.'

Nami nikamuuliza: **'Hivi jee unanishauri nielekee wapi kuishi kimaisha?'** nae akasema: **'Dimashq'** nami nikamuuliza: **'Kwani huko Dimashq, Maisha yana hali gani?'** nae akasema: **'Ole wako na Moyo wako, Kwani unapokua na shaka basi Moyo hua haukubali ushauri'**

Aliulizwa Uways Al Qarn : '**Hivi Khusuu ndio nini'** ambapo nae akajibu: **'*Khushuu* hua ni hali anayokua nayo mtu anapokua mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kiasi ya kua hata kama akichomwa na kitu chenye ncha kali hua si mwenye kuhisi maumivu yatokanayo na kitu hicho, kutokana na kujihisi kua yuko mbele ya Mola wake.'**

AHNAF IBN QAYS

Abu Bahr Ahnaf Dahhak Ibn Qays Ibn Husayn Al Tamimi Al Sadi alizaliwa katika ardhi ya nchini Iraq Mjini Basra katika kipindi cha wakati wa uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini hata hivyo hakua ni mwenye kujaaliwa kukutana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ingawa alisilimu katika kipindi hicho hicho pia.

Ahnaf Ibn Qays alikua ni mkuu wa Kabila la watu wake na ndie aliewaongoza watu wake wote katika kabila lake kuingia kwenye Uislam kutokana na kuheshimika kwake na pia kutokana na Ucha Mungu wake, kwani anasema Imam Hasan Al Basr: '**Ahnaf**

Ibn Qays alikua ni Mtu mwenye kuheshimika nami sijawahi kuona Mtu mcha Mungu kama yeye miongoni mwa watu wa Kabila lake.'

Ahnaf Ibn Qays alisoma kwa Umar Ibn Al Khattab, Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu*, Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*, Abu Dhar Al Ghifari *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* na wengineo.

Baada ya kufariki *Rasul Allahu Salallahu Alayhi wa Salam* na baada ya kufariki *Amir ul Muuminin* Abu Bakr Al Sadiq *Radhi Allahu Anhu* na hivyo Mamlaka ya Khalifa kua chini ya *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*, basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimjaalia Ahnaf Ibn Qays kua ni mwenye kutembelea Mji wa Makkah yeye na baadhi ya watu wa Kabila lake, ambapo ujumbe huo ulipofika katika mji wa Madina mbele ya Umar Ibn Al Khattab R*adhi Allahu Anhu* basi Ahnaf Ibn Qays akakaa pembeni anasikiliza kila mtu anavyozungumzia kuhusiana na hali yake.

Hivyo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akawauliza watu hao: '**Jee mnahitaji kitu chochote kile?**'

Hivyo Ahnaf Ibn Qays akasogea karibu na kisha akasema: '**Naam *Ya Amir Ul Muumini,* unajua kua ufunguo wa Sadaqa na Neema zaidi ni *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na ndugu zetu katika sehemu nyengine za ardhi wao wanaishi katika ardhi yenye upatikanaji wa Maji na ardhi yeye rutba, ambapo sisi kwa upande wetu tunaishia kwenye sehemu ya ardhi ambayo ni kame na iliyozungukwa na maji ya chumvi kwa upande mmoja na kwa upande wa pili kuna Jangwa.**

Nasi hatuna Wanyama wa Mifugo wala mashamba, hivyo upatikanaji wa chakula chetu sisi hua ni mgumu sana, kiasi ya kua mtu aliekua dhaifu miongoni mwetu humbidi kusafiri kilomita mbili kwa ajili ya kutafuta maji. Hivyo kama hukutusaidia kutimiza mahitaji yetu madogo madogo kama haya na kuondoa umasikini wetu basi sisi tutakua ni Kabila lililoangamia.'

Baada ya kusikia maneno hayo yaliyojaa hikma na busara ndani yake kutokana na ufahamu wa msemaji wa maneno hayo, basi *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akawapa watu hao wa Basra sehemu ya hazina kutoka katika *Bayt ul Maal* na kisha akamuandikia Gavana wake aliekua akiishi Basra ambae ni Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* kwa kumwambia kua awajengee watu wa Basra njia za mifereji ya Maji kwa ajili ya kumwagilia ardhi yao, na kisha kumwambia kua: '**Kaa nae karibu sana Ahnaf Ibn Qays ili uwe unashauriana nae katika mambo mbali mbali ya Jamii ya Kiislam na kua ni mwenye kusikiliza kauli zake.**'

Ulipowadia mda wa Ahnaf Ibn Qays kua ni mwenye kutaka kurudi nyumbani na watu wake basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamzuia na kumuomba akae nae

pamoja kidogo katika mji wa Madina ili apate kunufaika na Hikma na Busara zake, hivyo Ahnaf Ibn Qays akakaa kwenye Mji wa Madina kwa mda wa Mwaka mmoja huku nae akiwa ni mwenye kujichumia Ilm kutoka kwa Masahaba Wanazuoni wa Mji wa Madina.

Ahnaf Ibn Qays alikua ni kiongozi wa jeshi la *Amir ul Muuminin Umar Ibn Al Khattab Radhi Allahu Anhu* lililouingiza Uislam katika maeneo ya Iran na Khurasan, ambapo Ahnaf Ibn Qays na jeshi lake la Waislam alimshinda Mfalme Yazdijud ambae nae alikimbilia kuomba masaada kwa Wafalme wenzake akiwemo kiongozi wa ardhi ya Uturuki na China.

Hivyo Mjumbe wake alipofika kwa mtawala wa China basi akampa barua kutoka kwa Yazdijud ambapo mtawala huyo wa China akasema: **'Ni jukumu letu Wafalme kusaidiana, lakini kwanza niambie kuhusiana hali ya hawa watu walio kufukuzeni kutoka kwenye Ardhi yenu, kwani naona mnasema kua ni watu ambao wako kidogo kiidadi na nyie mko wengi, lakini ukweli wa kua nyinyi mko wengi na wao wako kidogo na bado wao wakapata ushindi, hii kidogo inanitia wasi wasi, kwani unaonesha kua wao wana sifa nzuri zaidi yenu.'**

Hivyo Mjumbe huyo akasema: **'Niulizie masuali unayotaka kuniuliza juu yao nami nitakujibu'**

Mtawala wa China akauliza: **'Jee hawa watu hua wanaweka Masharti ya kuaminika kabla ya kupigana na nyinyi?'** Mjumbe huyo akasema: **'Naam, hua wanatutaka kufanya moja kati ya vitu vitatu na kisha hutuachia sisi kuamua kutokana navyo vitu vyenyewe ni: Kukubaliana na Imani ya Dini yao, Kuwalipa Jizya au kukabiliana na Vita'**

Mtawala wa China akauliza: **'Jee ni wa namna gani utiifu wao kwa viongozi wao?'** ambapo mjumbe akajibu: **'Wako makini sana juu ya utiifu wa Viongozi wao kwani wanawatii ipasavyo'** Mtawala wa China akauliza: **'Hivi jee kuhusiana na wanachokifaya kua ni chenye kukubalika kwao na kipi kisichokubalika? Jee wanakifanya haramu kilicho Halali na kukihalalisha kilicho haramu?'** Mjumbe akajibu; **'La'**

Mtawala wa China akajibu: '**Kama ni hivyo basi hakuna kitakachowashinda watu hawa hadi pale watakapokiharamisha kile kilicho Hali na kukihalalisha kile kilicho haramu'** na kisha baada ya hapo akajibu barua aliyoletewa kwa kusema: **'Kama sikuwa ni mwenye kuata maelezo kutoka kwa mjumbe wao basi ningekutumia Jeshi kubwa sana linaloanzia kutoka katika ardhi ya Khurasan hadi China, lakini kama tatizo ni kua kutokana na hali yao basi kama watu hawa wakiambiwa na Mtume wao kua wauvamie Mlima basi watauangusha Mlima huo,**

kwani hakuna atakaeweza kuishinda Nguvu ya Imani iliyojaa ndani ya Nyoyo zao, na hawatoshindwa, hivyo hata ama wakija kwangu mimi basi kutokana na Imani yao wanaweza wakaniangamiza na mimi pia. Hivyo ushauri wangu kubaliana nao watu hao kutafuta usalama kwa kukaa kwenye ardhi yenu bila ya matatizo'

Ahnaf Ibn Qays aliendelea kua miongoni mwa viongozi wa jeshi la Khurasan katika kipindi cha *Amir Ul Muuminin Uthman Ibn Affan Radhi Allahu Anhu.* Ambapo katika kipindi hicho alipoenda katika Ibada ya Hija basi kulitokea tukio ambalo Ahnaf Ibn Qays mwenyewe analielezea kwa kusema kua: '**Katika kipindi cha Utawala wa Khalifa Uthman, mimi nilikua nikifanya *Tawwaf* mara akanifuata mmoja kati ya watu wa kabila la Quraysh na kuuchukua mkono wangu na kisha kuniuliza; 'Jee nikupe habari njema?' nami nikasema: 'Naam.''**

Nae akasema: **'Jee unakumbuka pale *Rasul Allahu Salallahu Alayhi wa Salam* aliponituma mimi kwenye Kabila lako ili nikuusieni kuingia kwenye Uislam? Nami nikakuusieni' na kisha wewe ukaniambia kwa kusema kua: 'Hakika wewe unausia juu ya kitu kizuri sana, tabia nzuri, na kuwaepusha watu na mambo mabaya ambayo sijawahi kuyasikia, na ukasema kua wewe ulikua Muislam tangu ulipobaleghe na hivyo Kabila lako liliukubali Uislam kutokana na ushauri wako?'**

'Hivyo niliporudi Madina na kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na yaliyotokea basi nae akasema: 'Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* Amsamehe Dhambi zake Ahnaf' na hivyo baada ya hapo basi mimi sikuwa na kitu nilichokua nikikitegemea kuhusiana na Akhera yangu isipokua uombezi huo wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*'

Ahnaf Ibn Qays alifariki mnamo mwaka 67 Al Hijra katika mji wa Kufah ambapo anasema Abd Rahman Ibn Uqba aliehudhuria maziko yake hayo kua: '**Mimi nilihudhuria maziko ya Ahnaf Ibn Qays, na niliingia Kaburini na nilipokua nikilirekebisha Kaburi basi nililiona likiwa linazidi kutanuka, na nilipowaambia wenzangu juu ya tukio hilo basi wao walisema kua hawakuona tukio hilo.'**

Ambapo aliusia Ahnaf Ibn Qays kwa kusema kua: '**Hakika mimi hua nna umakini sana katika mambo yafuatayo ambayo yatawanufaisha watakayoyatumia: Kwanza sijishirikishi na wale ambao hawataki kunishirikisha katika jambo lao, Siendi kwenye Milango ya wenye Mamlaka bila ya kua na wito wao, Naona kua si sahihi kwa watu kunisaidia mimi kwa kile ambacho wao wenyewe hua wanakihitaji.'**

Ahnaf Ibn Qays alisema kua: **'Kuweni na Tabia njema na mtasifiwa na kutokua na matatizo, kwani maradhi mabaya zaidi ni Tabia mbaya na Ulimi mchafu.'**

‘Mtu mwenye heshima hua ni yule mwenye kusimamia maneno yake, mwenye busara ni yule asiesema uongo, na mwenye Imani hua hasengenyi.’

‘Kulingana na Mtu mwenye Busara na Tabia njema, basi ni kua Wazee hua hawawaachii kitu chochote watoto wao, na waliokufa kwa walio hai isipokua matayarisho kufanya Amali njema na mambo yenye Manufaa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala.*’

‘Ibn Adam hujulikana kutokana na kile alichokua nacho, kwa mfano kama mtu atakua ni mwenye kucheka kufanya matani basi huonekana kua ni mtu wa kati na kati.’

‘Unapokua nasi usizungumzie kuhusiana na Wanawake, Chakula wala Kinywaji, kwa sababu wale tusiowapenda sisi ni wenye kuzungumzia kuhusiana na sehemu zao za siri na wanachokula na kunywa.’

‘Uwezo wa mtu kuachana na chakula anachokipenda hua unategemeana na ukubwa wa heshima yake na maumbile yake.’

‘Kua Mnyenyekevu na Mwenye Subra.’

‘Kama mtu akifanya uadui dhidi yangu basi mimi huhusiana nae kulingana na hali tatu zifuatazo: Kama yeye akiwa ni Mkubwa zaidi yangu basi humheshimu na sifanyi chochote, kama yeye ni mwenye Umri mdogo zaidi yangu basi hua simfanyii ubaya wowote, na kama akiwa sawa na umri wangu basi hua namsamehe na kumkirimu.’

‘Hua hakuna utulivu kwa yule mwenye kuona wivu.’

‘Inanishangaza inakuaje mtu mwenye kutokea kwenye sehemu inayopitia pia mkojo anakua ni mwenye kiburi na kujiona sana.’

‘Hakuna Utajiri mzuri bila ya kua na ukarimu na hakuna urafiki bila ya kuaminiana.’

‘Usimlalamikie mtu yeyote kuhusiana na mitihani yako kwani huenda unaemwambia akawa ni rafiki yako kisha ukamhuzunisha au akawa ni adui yako na hivyo ukamfurahisha.’

‘Ewe Mola wangu kama ukinisamehe basi hakika wewe ni msamehevu na ukiniadhibu basi mimi ni mwenye kustahiki adhabu zako.’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Alisifiwa kwa kuambiwa Ahnaf Ibn Qays kua: **'Hakika wewe ni Mtu mtaratibu katika kila kitu'** ambapo nae akasema: **'Naam, kwani kuharakisha kwangu mimi hua ni katika wakati inapoingia Sala, hunibidi kuisali kwa wakati wake, Katika maziko huhitajika kuzika kwa wakati na Katika Ndoa kwa kuozesha kwa wakati.'**

'Urafiki ni kitu laini sana, kiasi ya kua kama hukukilinda basi kitavunjika, hivyo kilinde katika wakati unapokua na hasira kwa kua na uadilifu kiasi ya kua yule aliekukosea atakuja kukuomba msamaha, kubali kumsamehe na wala usimlaumu.'

Muawwiyah Ibn Abu Sufyan Radhi Allahu Anhu alimuuliza Ahnaf Ibn Qays: **'Ya Abu Al Bahr Jee unausiaje kuhusiana na Watoto?'** Ahnaf Ibn Qays akasema: **'Watoto ni Matunda ya Nyoyo zetu hivyo waonesheni Mapenzi na urahisi katika mambo, furahieni juu ya matendo yao mema, na wala msiwafanyie ugumu na hivyo kuwafanya kua ni wenye kuyachoka maisha yao.'**

IMAM KAAB AL AHBAR

Imam Abu Is-haq Kaab Al Ahbar alikua ni Mwanazuoni mkubwa sana wa Dini ya Kiyahudi aliekua akiishi katika ardhi ya Yemen, na alitaka kuingia katika Dini ya Uislam katika kipindi cha Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na aliamua kuenda katika Mji wa Madina kwa ajili ya kuingia kwenye Uislam kupitia kwenye mikono ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mwenyewe lakini kwa bahati mbaya au nzuri alipokua njiani akapata habari ya kifo cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha pia akasikia kuhusiana na Mitume walioibuka baada ya kufariki kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, hivyo nae akaamua kurudi katika ardhi ya Yemen.

Hivyo Imam Kaab Al Ahbar alikaa kwa mda hadi pale ulipoingia madarakani utawala wa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akaamua kuelekea tena katika ardhi ya Madina kwa ajili ya kusilimu na akahamia katika ardhi ya Humus baada ya kusilimu kwake ambapo aliishi hadi kufariki kwake mnamo mwaka 32 Al Hijra.

Anasema Imam Kaab Al Ahbar kua: ***'Allah Subhanah wa Ta'ala*** **anapokua anampenda Mja wake alieamini basi hua ni mwenye kuichukua Dunia yake na kuiweka mbali na Mja wake huyo kwa ajili ya kumpandisha Daraja yake Peponi na anapomchukia Mja wake basi humfanya kua ni mwenye kujisikia huru hapa Duniani na kua na furaha tele na hivyo kua ni mwenye kumzamisha na kumshusha kwenye kina cha Moto wa Jahannam.'**

Imam Kaab Al Ahbar alisema tena kua: **'Yeyote yule anaejisalimisha kwenye Mali na Utajiri basi na Dini yake pia hujisalimisha na hivyo nae hua ni mwenye kudhurika.**'

'Moto wa Jahannam hautomugusa yule ambae ni mwenye kutokwa na machozi kwa ajili ya Mola wake.'

'Naapa mimi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua nnapenda kuona Machozi yakinitiririka kwenye macho yangu zaidi kuliko kua ni mwenye Umiliki wa Mlima wa Dhahabu na kuutoa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*.'

'Zing'arisheni nyumba zenu kwa Nuru ya *Dhikr Allah*, zitieni Baraka Nyumba zenu kwa Kusali ndani yake, kwani nnaapa kwa jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua wale wenye kufanya hivyo ni wenye kujulikana na Watu wa Mbinguni ambao hua ni wenye kusema kua: 'Fulani na fulani wamezipamba nyumba zao kwa kumkumbuka *Allah Subahanh wa Ta'ala* ndani yake.''

'Kukaa kimya ni miongoni mwa Tabia njema kwa sababu ni sehemu nzuri ya kufanya mema na kuepukwa na wenye shaka na hapo hao Mtu hua ni mwenye kujipunguzia Dhambi.'

'*Allah Subhanah wa Taala* hua hampendi yule anaetabasam bila ya kuwepo kwa haki na pia yule ambae hana malengo katika maisha yake.'

'Naapa kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: 'Kama mmoja wenu angekua yuko katika upande wa Mashariki ya Dunia na kisha Moto wa Jahannam ukawa kwenye upande wa Magharibi ya Dunia na kisha Moto huo ukaoneshwa kwa Mtu huyo basi Mtu huyo hatoweza kulistahmilia joto la Moto huo, hivyo Enyi Ibn Adam ni rahisi kufanya aliyoyaamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala*, msijiingize kwenye Moto huo kwani hamuwezi kuustahmilia juu yake.''

'Kuna madaraja manne juu ya Moto ambapo la kwanza ni kwa wale wenye kuuvunja udugu, la pili kwa wale wenye Madeni, la tatu ni kwa wale wenye kutumia nguvu kwa kukosa subra na la nne kwa wale ambao ni makatilii.'

'Anapotaka mmoja wenu kupata heshima katika siku ya Malipo basi na atafakkari ukubwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwani akifanya hivyo basi lazima atakua Mwanazuoni. Na akitosheka na riziki yake basi hatomhitaji mwengine yeyote zaidi ya Mola wake, na anapokumbuka kasoro zake na makosa yake basi hulia na hivyo kua ni mwenye kuizima bahari ya moto wa Jahannam.'

‘Wasiokua na Ilm hua ni wenye kujisifu kwa Ilm yao, kwani sehemu ya Ilm yao ni kujisifu kwao.’

‘Wamebarikiwa wale ambao ni wenye kuyafanya Majumba yao kua ni Miskiti, kwani Miskiti ni nyumba za wenye Taqwa, na *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni mwenye kujivunia wale waja wake wenye kuzificha Amali zao.’

‘Peponi kuna watuwanaolia, wakiulizwa kwanini wanalia basi hua ni wenye kusema: ‘Hakika mimi nimeuliwa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala*, na ni mwenye kuupata ushahidi ambao ni kitu kitamu sana, hivyo natamani kua nirudishwe tena Duniani ili niupate kwa mara tatu tena zaidi, lakini nnalia kwa sababu siwezi tena kua shahidi.’’

‘Watakuja Wanazuoni katika wakati wa mwisho wa Dunia ambao watawausia watu katika kuachana na Dunia, lakini wao watakua ni wenye kuikumbatia Dunia, Watawatia Khofu kwa ajili ya Mola wao watu lakini wao watakua hawana hata dalili ya Khofu kwa Mola wao, watawataka watu wakae mbali na wenye Madaraka lakini wao hawatoachana nao, wataipakaza tope Dunia lakini wao watakaa na Matajiri na kua mbali na Masikini, watakua wanapingana na wanachokijua kama vile wanavyopingana Wanawake mbele ya Wanaume wao. Wanazuoni hawa hua hawafai na ni wenye kuchukiwa na *Allah Subhanah wa Ta’ala.’*

‘Unapolala basi lala kwa ubavu wa kulia na uso wako uelekeze Kibla, kwani kulala ni kama kufa.’

‘Kuna Manufaa mengi sana katika mikusanyiko ya Ilm, ila watu hawajui thamani ya kuhudhuria kwake, ya laiti kama wangekua wanajua malipo yake basi wangeuana kwa ajili ya kukimbilia mikusanyiko yake, na kuacha kila kitu chao kwa ajili ya Mikusanyiko hio.’

‘Mja mwema anapofariki na kuingizwa Kaburini basi mema yake humzunguka Kaburini humo kama Sala, Zakkat, Hijja n.k Hivyo wanapokuja Munkar na Nakir kwa mtu huyo basi Sala huwaambia Malaika hao kua: ‘Mtu huyu alikua akisimama mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa miguu yake, hivyo hamuwezi kumuadhibu miguu yake’ na wanapokuja kichwani basi Funga huwasimamia Malaika hao na kuwaambia: ‘Kichwa hiki kilifunga kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* hivyo hamuwezi kukiadhibu.’

Kisha Malaika hao wataenda kwenye sehemu nyengine za Mwili na watakutana na Amali za Ibada nyengine ikiwemo Hija, Jihad n,k ambazo nazo zitakataa mwili huo kuadhibiwa, na kisha wataenda kwenye mikono na mikono hio itasema: ‘Kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi mikono hii ilitoa Sadaka na Zakkah hivyo

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

haiwezekani kua mumuadhibu' na hivyo Malaika hao watashindwa kumuadhibu Mtu huyo na hivyo watasema: 'Kwa kua uliishi Duniani ukiwa kama Mja mwema na msafi na umekufa kirahisi basi kua Salama kwa Usalama' kisha Malaika hao watamletea mtu huyo Mavazi ya Peponi na kumtanulia Kaburi lake na kulijaza Nuru ambayo itabakia hadi siku ya Malipo.'

IMAM ALQAMAH IBN QAYS AL QUFI

Imam Abu Shibl Alqamah Ibn Qays Ibn Abd Allah Ibn Malik An Nakhai Al Kufi alizaliwa katika ardhi ya nchini Iraq miaka takriban 20 kabla ya mwaka wa kwanza Al Hijra, ambapo ingawa ilikua ni katika kipindi ambacho *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam yuko* hai, lakini yeye hakuwahi kuonana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.

Na ingawa hakuwahi kumuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini hata hivyo aliwahi kuonana na Masahaba wengi sana ambao nao walimnufaisha sana kwa Ilm ya Dini ya Kiislam akiwemo Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ambae ndie Mwalimu wake mkuu, kiasi ya kua Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* mwenyewe alikua akisema kuhusiana na Imam Alqamah kua: '**Hakika hakuna kitu ninachokijua mimi bila ya Alqamah kua ni mwenye kukijua na kukifundisha.**'

Na pia baadi ya wakati alikua anapoulizwa suali basi hua ni mwenye kusema: '**Mfuateni Alqamah mmuulize juu ya hili.**'

Mbali ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* lakini Imam Alqamah pia alisoma kwa Masahaba wengi sana wakiwemo Umar Ibn Khattab,Uthman Ibn Affan, Ali Ibn Abi Talib, Salman Al Farsi, Abu Darda, Khalid Ibn Walid, Hudhayfah Ibn Al Yaman, Aisha Bint Abu Bakr, Sa'd Ibn Abu Waqqas, Ammar Ibn Yasir, Abu Mas'ud Badri, Abu Musa Al Ashari, Maqal Ibn Sinan, Salama Ibn Yazid, Shuraykh Ibn Artat, Qays Ibn Marwan *Radhi Allahu Anhum* na wengineo

Hivyo bila ya shaka haishangazi kuona kua hata baadhi ya Masahaba walikua wakimfuata Imam Alqamah palae wanapotaka kujua kuhusiana na Dini yao kutokana na ukubwa wa Ilm yake na hivyo kua ni kiongozi wa Wanazuoni wa Fiqh ya Mji wa Kufah baada ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu.*

Imam Alqamah alikua ni mwenye kufuata nyayo za Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* katika kila kitu kuanzia cha Maisha yake ya Kidunia na ya kiakhera pia, kiasi ya

kua wakati Imam Amr Ash Shabi na Imam Ibrahim An Nakhai walipokua wakitafuta Ilm basi walikua wakiambiana kwa kusema kua: '**Leo Twendeni tukasome kwa yule ambae ni mwenye kufanana na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kwa kimaumbile na kitabia.**'

Kwani Imam Alqamah alikua ni Mjomba wake Imam Ibrahim An Nakhai na hivyo alikua akimfundisha pia na hivyo haishangazi kua tunapoiangalia Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa na miongoni mwa Hadith zake basi tunaona kua Sanad yake inatoka kwa *Rasul Allah Salallahu Aalyhi wa Salam* kupitia kwa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kupitia kwa Ilam Alqamah kupitia kwa Imam Ibrahim An Nakhai kupitia kwa Imam Hammad kufikia kwa Imam Abu Hanifah.

Kwani Imam Abu Hanifa mwenyewe alikua akimkubali sana Imam Alqamah na hivyo alikua akisema kua: '**Ni Jambo lililowazi kua Alqamah ni mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith na Fiqh kuliko hata baadhi ya Masahaba**.'

Na ingawa Imam Alqamah alikua na Ilm kubwa sana lakini alikua ni Imam ambae ana mtizamo wa kua inakirihisha kuandika vitabu vya Ilm kwani huenda vikaangukia kwenye mikono sio, ambapo mtizamo huu alidumu nao hadi pale alipomuona Imam Masruq Ibn Ajda akiandika na kusema kua baada ya kuhifadhi basi hua ni mwenye kufuta hayo aliyoyaandika.

Imam Ahmad Ibn Hanbal anasema kua Imam Alqamah alikua ni mwenye kuaminika katika Hadith na ni Thiqah.

Imam Alqamah alikua ni muungaji mkono mkubwa sana wa Mamlaka ya utawala wa *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na hivyo alikua si mtu mwenye mtizamo mzuri kuhusiana na Mamlaka ya Muawwiyah Ibn Abi Sufyan *Radhi Allahu Anhu* kwani Imam Alqamah alipigana vita vya Siffin pamoja na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*

Imam Alqamah alikua pia ni mwenye sifa ya kua msomaji mzuri sana wa Qur'an na alikua ni mwenye kujaaliwa sauti nzuri katika *Qiraa* chake, ambapo wasikilizaji wake walikua wanafikia hadi kuzimia kutokana na usomaji wake na anasema Imam Ibrahim An Nakhai kua: '**Alqamah Ibn Qays alikua akisoma Qur'an mbele ya Abd Allah Ibn Masud ambae alikua akimsikiliza huku akisema: 'Soma, Soma, Wazazi wangu watolewe kafara kwa ajili yako, ya Alqamah!''**

Na yeye mwenyewe Imam Alqamah alikua anasema kua: **'Abd Allah Ibn Masud alikua akiniita na kunitaka nimsomee Qur'an, hivyo hua nnamsomea na nnaposita basi hua ni mwenye kusema, endelea, endelea ya Alqamah'**

Abd Allah Ibn Masud alikua akimwambia Imam Alqamah kua: '**Kwa hakika kama *Rasul Allah Salallahu Aalyhi wa Salam* angekuona wewe ewe Alqamah basi bila ya shaka angekua na furaha kubwa sana, na angepata utulivu mkubwa sana**.'

Imam Abu Is-haq anasema kua: **'Amesema Aswad Ibn Yazid kua:** '**Mimi nilimuona Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akimsomesha Ilm Alqamah Ibn Qays ambapo alikua akimsomesha *Tashahhud* kama vile ambavyo anavyomsomesha kisomo cha Qur'an.**''

Imam Alqamah anasema kua: '**Amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua; 'Iliposhuka aya ya 82 ya *Surat Al An'aam,* isemayo:**

﴿ٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَلَمْ يَلْبِسُوٓاْ إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُوْلَٰئِكَ لَهُمُ ٱلأَمْنُ وَهُمْ مُّهْتَدُونَ﴾

Alladheena amanoo walam yalbisoo eemanahum bi*dh*ulmin ola-ika lahumu al-amnu wahum muhtadoona *(Surat Al An'aam 6:82)*

Tafsir: ***Ni wale ambao ni wenye kuamini na kutochanganya Imani yao na Dhulma basi kwa ajili yao kuna amani na wao ndio walioongozwa.***

Basi Masahaba wakasema: **'Hivi Jee ni yupi miongoni mwetu tumewadhulumu?' Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Aya hii haihusiani na nyinyi, kwani hamjaona nyinyi kua Luqman alimwambia Mtoto wake kua:**

﴿وَإِذْ قَالَ لُقْمَانُ لاِبْنِهِ وَهُوَ يَعِظُهُ يٰبُنَيَّ لاَ تُشْرِكْ بِٱللَّهِ إِنَّ ٱلشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ﴾

Wa-idh qala luqmanu liibnihi wahuwa yaAAi*dh*uhu ya bunayya la tushrik biAllahi inna alshshirka la*dh*ulmun AAadheemun *(Surat Luqman 31:13)*

Tafsir: ***Na kumbuka wakati Luqman alipomwambia Mtoto wake kwa kumuuisa kua: 'Ewe Mtoto wangu usimshirikishe Allah, kwani kwa hakika Shirk ni dhambi kubwa sana.'***

Hivyo Dhulma iliyozungumziwa kwenye aya ya 82 ya *Surat Al An'aam* ni ya kumshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala.'*

Imam Alqamah alikua si mwenye kuhifadhi Qur'an tu bali pia alihifadhi Hadith 100,000 kwenye Moyo wake, na alikua akisema kua: '**Hakika mimi nikihifadhi kitu ndani ya**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Moyo wangu basi ninapokisoma hua kama nakisoma kwenye kartasi iliyopo mbele yangu.'

Imam Alqamah alifariki mnamo mwaka 62 Al Hijra akiwa na umri wa miaka 90 baada ya kuwacha wasia usemao kua: '**Nitakapokufa basi niamrisheni nitoe shahada kwenye Kichwa changu na kisha wala msitangazie kifo changu bali nizikeni haraka sana.'**

Imam Abd Ul Malik alifariki mnamo mwaka 101 Al Hijra.

IMAM ABU RAJA'A AL UTARID

Imam Abu Rajaa Al Utarid Imran Ibn Milhan Al Basr alizaliwa takriban miaka 22 kabla ya Uislam, na alisilimu katika mwaka wa 8 wa Uislam lakini hata hivyo hakuwahi kuonana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Imam Abu Rajaa anaendelea kusema kua: **'Sisi zamani tulikua tukitengeneza Chungu ya Mchanga katika wakati wa Ujahilliyah, na kisha tunatoboa shimo katikati yake na kisha hua tunamimina Maziwa ndani yake na kuanza kuabudu kwa kuuzunguka chungu hio ya mchanga, na kisha hua tunarudi Nyumbani, katika wakati huo tulikua tunaviheshimu vile vitu ambavyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameviharamisha, na tulikua tukisema kua: 'Ewe Mmiliki ambae huna Mungu isipokua yeye Mola wetu'**

Mimi niliuwahi wakati wa Mtume *Salallahu Alayhi wa Salam* lakini sikuwahi kuonana nae, nilikua kijana katika wakati huo, na sikuwahi kuona watu wasiokua na akili na waovu kama walivyokua Waarabu, kwani walikua wanaweza wakawachukua Mbuzi mweupe na kisha wakasema kua ndio Mungu wao na kisha wakamuabudu.'

Imam Abu Rajaa anaendelea kusema kua: **'Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipopewa Utume sisi tulikua tunaabudu Sanamu la Jiwe, ambalo tulikua tukilibeba na kuliweka juu ya Ngamia na kisha kuenda nalo kila sehemu tunayoenda. Safari moja tulifika kwenye sehemu ambayo ilikua ina kilima cha Mchanga na hivyo tukaliweka juu yake Sanam hilo.**

Na kisha tukaondoka kwa ajili kuenda kutafuta Maji, na tuliporudi basi tukakuta Sanam hilo limeanguka, na kuzama kwenye chungu ya Mchanga huo, hivyo nami nikalinyanyua na kisha nikasema: 'Mungu gani wewe, ambae huwezi hata kujizuia

kutokana na kuanguka na kuzama kwenye Mchanga? Huyu hawezi kua ni Mungu, kwani anaweza kuuliwa hata na Mbuzi kwa kutumia mkia wake, Hivyo hawezi kua ni Mungu.' Na hapo ndio nikaanza kua Muislam, na hivyo baadae nikaelekea katika Mji wa Madina, lakini nilipofika na kumuulizia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa salam* basi nikaambiwa kua ameshafariki.'

Baada ya kusilimu basi Imam Abu Rajaa alikua ni Mcha Mungu na mwenye Ilm Kubwa na Ufahamu mpana sana kwani alisoma kwa Masahaba wakiwemo Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Umm ul Muuminin Aisha *Radhi Allahu Anha*, Abu Musa Al Ashari, na wengineo *Radhi Allahu Anhum* na hivyo alipohamia katika Mji wa Basra alikua akiaminika sana.

Imam Abu Rajaa ni miongoni mwa Maimamu ambao waliishi kwa umri mkubwa sana, kwani aliishi kwa umri wa zaidi ya miaka 140 na hivyo alikua ni mwenye kusomesha Wanafunzi wengi sana na alifariki mnamo mwaka 117 Al Hijra.

Ambapo anasema Imam Ibn Saad kua: '**Imam Abu Rajaa alikua ni *Thiqah* na ni mwenye llm kubwa ya Qur'an al Karim**'

Kutokana na ukubwa wa Ilm na Ufahmu wake basi siku moja kuna mtu alienda kwa Imam Muhamamd Ibn Sirrin na kumwambia: '**Nimekuja kukuuliza suali fulani**' hivyo Imam Muhammad Ibn Sirrin akasema: **'Naam, Uliza.'** Mtu huyo akasema: **'Hivi Jee kuna Kiumbe Jini yeyote yule ambae yuko hai aliefunga Makubaliano na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*?'**

Hivyo Imam Muhamamd Ibn Sirrin akasema: **'Ama kusema ukweli, sifikirii kama mimi nnastahiki kuulizwa suali kama hili, kwani kuhusiana na suali hili basi mfuate Abu Rajaa, na kisha kamuulize yeye kwani ndie mwenye kujua zaidi juu ya hili.'**

Ambapo anasema Kathir Ibn Abd Rahman kua; '**Sisi tulienda kwa Abu Rajaa na tukamuuliza:** '**Ya Abu Rajaa, hivi jee kuna Kiumbe Jini yeyote yule ambae yuko hai aliefunga Makubaliano na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*?**' **ambapo nae akasema: 'Wacha nikuambieni mimi kuhusiana na Jambo hili, kwani siku moja mimi nilienda kwenye Nyumba moja nami nikagonga Mlango wa Nyumba hio taratibu, na mlango ulipofunguka ghafla nikaona Kuna Nyoka ambae alikua anajibiringitisha na kujisokota na hapo hapo akafariki ghafla.'**

Hivyo nikamchukua na kumchimbia shimo na kumzika. Na wakati nafanya hivyo basi nikasikia sauti za watu wengi sana ambao nilikua siwaoni lakini walikua wakisema: '*Assalaam Alaykum*' hivyo nilipoangalia na kutoona yeyote basi

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

nikaitikia na kisha nikauliza: 'Jee nyie ndio Nani?' ambapo sauti hizo zikasema: Sisi ni Viumbe Majini, na tunamuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akuingize kwenye Rehma zake, kwani wewe unayo Darja kubwa sana mbele yetu.'

Nami nikauliza: 'Kwanini?' ambapo nao wakasema: 'Kwa sababu huyu Nyoka uliemzika alikua ndie Kiumbe Jini wa Mwisho ambae alifunga mkataba wa makubalino na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*'. Katika wakati huo mimi nilikua na umri wa miaka 135'

Imam Abu Rajaa alikua ni mtu mcha Mungu na mwenye kufanya Ibada sana, na alikua akisema; '**Baada ya kufariki kwangu, basi mimi sitokua na kitu chengine cha kukitegemea ambacho kitanisaidia zaidi ya Sala 5 ambazo nnamuabudia Mola wangu kwa kuusugulia uso wangu juu ya uso wa Ardhi**'

Ambapo anasema Abu Al Ashshab kua: '**Abu Rajaa alikua akisoma Qur'an na Kusalisha katika kila siku 10 za mwisho za Mwezi wa Ramadhani**'

Imam Abu Rajaa aliulizwa: **'Hivi Jee kuna Sahaba yeyote yule wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alikua anauogopa Unafiq?' ambapo nae akasema: 'Hakika mimi nimewaona Masahaba wote wakiwa ni wenye nyoyo zenye kuwaka Moto wa Mapenzi kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na walikua ni wenye kujitolea kila kitu chao kikamilifu kwa ajili ya Mola wao.'**

Imam Abu Rajaa alikua akisema: **'Mimi nimewaona watu ambao wanawaelezea watu kuhusiana na Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kile wanachotakiwa kukifanya, hii haiwafanyi watu wawe ni wenye kupenda maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* bali itawafanya wawe ni wenye kuyachukia, kwani hua hawawabashirii habari njema bali hua wanawatisha. Msifanye hivyo, msiyafanye mambo yakawa magumu, kwa sababu watu hua ni wenye haki juu yao na pia juu ya familia zao. Enyi Waislam, Uko wapi Uislam? Hakika nyinyi mmeuwacha Nyuma ya Ukuta.'**

Alisema Imam Abu Rajaa kua **: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Hakika Mola wenu ni mwingi wa Rehma, hivyo yeyote yule anaekusudia kufanya jema kisha akawa hajalifanya basi Mtu huyo huandikiwa kua ni mwenye kulifanya jambo hilo. Hivyo kama akilifaya Jambo hilo basi hua ni mwenye kuandikiwa kua ni sawa na aliefanya mambo mema 700 au zaidi, na kama mtu akikusudia kufanya jambo ovu na kisha akawa hakulifanya basi Mtu huyo hua ni mwenye kuandikiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua amefanya jambo jema, na kama akilifanya basi hua ni mwenye kuandikiwa kua amefanya Ovu moja, au humfutia jema lake moja.''**

IMAM SHAQIQ IBN SALAMAH

Imam Abu Wael Shaqiq Ibn Salama Al Asad Ibn Kuzaymah Al Kufi alizaliwa katika ardhi ya Kufah, miaka 10 kabla ya Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na ingawa alizaliwa katika kipindi hicho lakini hakuwa ni Sahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* mbali ya kua aliwahi kuonana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwani alisilimu baada ya kufariki *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kwani anasema Abu Bishr kua: '**Amesema Zabarqan Al Siraj kua:** '**Alisema Abu Wael kua: 'Nakumbuka mimi nilipokua na umri wa miaka 10, katika kipindi kisichokua cha Uislam nilikua nachunga Kondoo kwa ajili ya familia yangu wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliposhushiwa Utume**''

Ambapo anasema Imam Waki Ibn Jarrah kua: '**Amesema Abu Al Abbas kua: 'Mimi nilimuuliza Abu Wael: 'Hivi Jee uliwahi kukutana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam'*** ambapo nae akasema: '**Naam, ila nilikua ni kijana Muasi, na sikumuona kua alikua ni Mtume.'**''

Anasema tena Abu Wael kua: '**Tulikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nami nikamkabidhi Kondoo na kumwambia: 'Chukua hii kama Sadaqa' ambapo nae akasema: 'Hakuna Sadaqa katika Kondoo huyu''** ambapo hii inaonesha kua Imam Shaqiq analielezea tukio wakati akiwa bado hajasilimu na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuweza kupokea Sadaqa hio kutoka kwake, na kisha baada ya tukio hili, basi akatokezea Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu* na walipomuona wakaanza kumkimbia kwa khofu.

Imam Al Amash anasema kua: **'Shaqiq Ibn Salamah aliniambia kua: 'Ewe Sulayman, hakika kama ungetuona sisi wewe wakati tulipokua tukimkimbia Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu* katika siku ya Bizakhah na kisha mimi nikaanguka kutoka kwenye Ngamia wangu, bado kidogo tu anivunje Shingo yangu nilikua na umri wa miaka 21, hakika kama ningefariki katika siku hio basi ningekua ni mwenye kuingia Motoni.''**

Ambapo anasema Muhammad Ibn Hamid Al Razi anasema kua amesema Abu Wael kua: **'Mimi nilikua nimepanda Ngamia wa familia yangu na mara Ghafla akanipita Mtu ambae alikua amepanda Farasi, na hivyo Ngamia wangu akakimbia na kisha kuna mtu ambae alisema: 'Mpandishe huyo mtoto kwenye Ngamia wake' nami nikauliza: 'Ndio nani huyu aliesema hivi?' na mtu huyo akaniambia: 'Huyo ndie *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*'''**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Hicho kilikua ni kipindi cha Ujahiliyah ambapo baadae Imam Shaqiq Ibn Salamah akasilimu na kuanza kujitafutia Ilm ya Dini ya Kiislam na kua ni mwenye kusoma kutoka kwa Masahaba wakiwemo *Amir ul Muuminin Abu Bakr As Siddiq, Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab, *Amir ul Muuminin* Uthman Ibn Affan, *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib, Ammar Ibn Yasar, Muadh, Abd Allah Ibn Masud, Abu Al Darda, Abu Musa Al Ashari, Hudhayfah Ibn Al Yamman, *Umm Ul Muuminin* Aisha, Usama Ibn Zaid Abu Hurayrah na wengineo *Radhi Allahu Anhum.*

Amesema Imam Abu Zurra kua: '**Hadith za Imam Shaqiq Ibn Salama kutoka kwa Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu ni Mursal.* Shaqiq ni mtu mwenye kuaminika na ni mwenye kupenda kuzungumza sana'**

Na anasema Muhammad Ibn Fadhil kua: '**Amesema Baba yangu kua amesema Shaqiq Ibn Salamah kua: 'Hakika mimi nilisoma Qur'an kwa mda wa miezi miwili.**''

Imam Shaqiq Ibn Salamah alikua ana Ilm kubwa sana na Ucha Mungu Mkubwa sana kiasi ya kua baada ya kusoma kwake basi alikua ni Imam mwenye kutegemewa katika maeneo ya Kufah kwani aliwahi kuulizwa Amr Ibn Murra: '**Hivi Jee ni nani mwenye Ilm kubwa zaidi katika Mji wa Kufah kupitia kwenye Hadith za Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu?*'** ambapo nae akajibu: '**Abu Wael.**'

Ambapo anasema Asim Ibn Abi Al Nujud kua: '**Hakika mimi sijawahi kumsikia Abu Wael akiwa ni mwenye Kutukana au kulaani Ibn Adam mwenzake au Mnyama'**

Anasema Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Jafar kua: '**Amesema Abu Yahya Al Razi kua amesema Hammad kua, amesema Abda kua amesema Zabarqan kua: 'Mimi nilikua na Abu Wael, hivyo nikaanza kumtukana na kumlaani Hajjaj Ibn Yusuf na kuanza kuelezea kasoro zake ambapo Abu Wael akaniambia: 'Usimlaani wala kumtukana kwani huwezi kujua huenda akawa ni mwenye kusema Ya Allah Nisamehe Makosa yangu' na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamsamehe.'**

Na anasema Imam Al Amash kua: '**Ewe Sulayman, hawa Watoto wa Kifalme wetu hawako huku wala kule kwani hawana Ucha Mungu wa watu wa Dini ya Kiislam na wala hawana akili za Kijahiliya.**'

Anasema Imam Ibn Sad kua: '**Imam Shaqiq Ibn Salamah ni *Thiqah* na ni mwenye Ilm Kubwa sana ya Hadith.**'

Na Imam Yahya Ibn Main anasema kua: '**Imam Shaqiq Ibn Salamah alikua ni mfano wa kipekee miongoni mwa wenye Ilm.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Shaqiq Ibn Salamah aliwasomesha kina Imam Masruq, Imam Alqamah, Imam Hamran Ibn Aban, Imam Yahya Ibn Main, Imam Al Amash, Imam Amr Ash Shabi, Imam Al Subai, Imam Manssur Ibn Mutammar n.k.

Anasema Imam Al Amash kua: '**Mimi nilimuona Abu Wael akiwa amevaa Suruali yake ikiwa iko nusu ya sehemu ya chini ya magoti yake, juu yake akiwa amevaa shati lake na juu yake akiwa amevaa kilemba chake.'**

Amesema Imam Sulayman Ibn Mihran kua: '**Amesema Shaqiq Ibn Salamah kua Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Pepo iko karibu sana kwenu kama vile ilivyokua ukaribu wa Mtu na Kamba ya kiatu chake, na Jahannam iko katika ukaribu kama huo.'**

Anasema Marif Ibn Wasil kua: **'Sisi tulikua tumekaa na Abu Wael, na watu wakazugumzia kuhusiana na Ukaribu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Waja wake ambapo Abu Wael akasema: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kua: 'Kama Ibn Adam akinikaribia mimi kwa pima moja, basi mimi namkaribia kwa ukaribu wa Mkono mmoja, ukinikaribia kwa mkono moja mimi nakukaribia wewe kwa nyanda moja, ukija kwa kutembea mimi nakuja kwa kukukimbilia.'''**

Anasema Affan Ibn Muslim kua: '**Amesema Abu Wael kua: 'Mimi nilivamia pamoja Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* katika ardhi ya Sham na kisha akasema: 'Msivae nguo za Hariri na wala msinywe kutoka katika vyombo vya Dhahabu wala Fedha, kwani ni kwa ajili yao hapa Duniani na ni kwa ajili yetu kesho Akhera.'''**

Yazid bin Abi Ziyad anasema kua: **'Mimi nilimuuza Abu Wael: 'Hivi Jee ni nani mkubwa baina yenu wewe na Masruq?' ambapo nae akasema: 'Mimi ni mkubwa kuliko Masruq' na kisha akasema: 'Mimi niliulizwa hivi jee ni nani mkubwa baina yako na Rabii Ibn Khuthaym? Nami nikasema mimi ni mkubwa zaidi yake kiumri ila yeye ni mkubwa zaidi yangu kiufaham''**

Ibn Aun anasema kua: '**Kuna mtu alikuja kwa Abu Wael wakati tukiwa katika Ibada ya Hija ambapo nae akauliza: 'Abu Wael, hivi Jee unaonaje kuhusiana na Mahujai?' Abu Wael akajibu: 'Hivi Jee inakuaje hadi wewe unataka mimi nitoe hukumu kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala?*''**

Asim Ibn Bahdala anasema kua: '**Mimi nilimsikia Abu Wael akisema wakati wa Kusjudu kua: 'Ya Allah nakuomba unisamehe kwani ukinisamehe basi utakua ni mwenye kunisamehe Milele, na kama ukiamua kuniadhibu basi utakua unaniadhibu bila ya kua na mwisho wa adhabu''**

Amesema Imam Al A’mash kua: ‘**Shaqiq Ibn Salamah alisema: ‘*Ya Allah* kama umetuandikia sisi kua ni miongoni mwa watu walioangamia basi tufutie na utuandikie kua ni miongoni mwa watu walioingizwa kwenye Rehma zako, na kama umetuandikia kua tuwe ni miongoni mwa walioingizwa kwenye Rehma zako basi tupe Msimamo Thabit kwani kwa hakika:**

﴿يَمۡحُوا۟ ٱللَّهُ مَا يَشَآءُ وَيُثۡبِتُ وَعِندَهُۥٓ أُمُّ ٱلۡكِتَٰبِ﴾

Yamhoo Allahu ma yashao wayuthbitu waAAindahu ommu alkitabi *(Surat Ar Rad 13:39)*

Tafsir: ***Ni Allah mwenye kufuta akitakacho na kukithibitisha akitakacho, na kwake yeye ndio wkenye Umm ul Kitab’***

Amesema Imam Shaqiq Ibn Salamah kua: ‘**Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* alikua ni mwenye kupenda kutuusia sisi katika kila siku ya Alkhamis, hivyo kuna mtu akasema: ‘Ewe Abu Abd Rahman sisi tunapenda kua wewe utuusie katika kila siku.’ Ambapo nae akasema: ‘Hakuna kinachonizuia mimi bali sifanyi hivyo kwa sababu ya kua naogopa kukuchosheni, kwani mimi nafuata njia ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliyoitumia katika kutuusia sisi kwa kua na khofu ya kutotuchosha’’***(Imam Muslim)*

Amesema Asim kua: **‘Dhir Ibn Hubaysh alikua ni mkubwa kiumri kuliko Abu Wail Shaqiq Ibn Hubaysh, hivyo walikua kila wanapokaa pamoja basi Abu Wael hua ni mwenye kukaa kimyaa kwa sababu ya kumheshimu Ibn Hubaysh.’**

Imam Shaqiq Ibn Salamah alifariki mnamo mwaka 82 Al Hijra.

Anasema Asim Ibn Bahdala kua: ‘**Wakati Abu Wael alipofariki, basi Abu Burda alimbusu paji lake la uso.**’

IMAM AL RABII IBN KHUTHAYM ATH THAWRY

Imam Abu Yazid Al Rabii Ibn Khuthaym Al Thawry Bani Mudar alizaliwa katika maeneo ya Al Thawry ambae baadae alihamia katika maeneo ya ardhi ya Kufah ambapo ndiko alikofariki mnamo mwaka 65 Al Hijra.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym alikulia katika mazingira ambayo yalimpelekea kua ni miongoni mwa watu 10 wenye Ucha Mungu zaidi katika karne yake, na alianza kusoma tangu akiwa mdogo kiasi ya kua baada ya kupata ufahamu kwani mara moja Usiku wakati akiwa bado mtoto basi mama yake aliamka kutoka usingizini na kumkuta Mtoto wake huyo akiwa mwenye Mihrab akiwa ni mwenye kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Na hivyo mama yae huyo akamuuliza: '**Vipi imekuaje? Huna usingizi au?'**

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **'Ewe Mama yangu itakuaje kwa yule mtu ambae ni mwenye kujua kua kuna uvamizi kutoka kwa Adui yake awe ni mwenye kuweza kulala usingizi ndani ya usiku wake?**' Ambapo maneno haya yalimfanya Mama yake huyo kua ni mwenye kutokwa na machozi.

Na wakati alipokua mkubwa basi Mama yake aliamka usiku na kumkuta Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akiwa analia, hivyo akamuuliza: **'Mbona unalia kumetokea nini?'** Imam Al Rabii akasema: **'Nalia kwa sababu mimi ni mwenye khofu inayotokana na kua ni mwenye kuua'** Mama yake akashtuka na kisha akamuuliza: ***'Subhanah Allah!*** **Ilikuaje? Umemuua nani?'** Imam Al Rabii akasema: **'Ewe Mama yangu hakika mim inimekiua mimi mwenye, kwani nimeiua Nafsi yangu kutokana na Dhambi zangu.**'

Imam Al Rabi Ibn Khuthaym alisoma kwa Sahaba Abd Allah Ibn Masud R*adhi Allahu Anhu* na alikua ni Mwanafunzi mwenye Ilm kubwa snaa miongoni mwa Wanafunzi wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* na alikua ni mcha Mungu mkubwa sana pia na mwenye kuachana kabisa na Dunia kiasi ya kua alikua akifanana na Masahaba na hivyo alisema Abd Allah Ibn Masud R*adhi Allahu Anhu* kumwambia Imam Al Rabi Ibn Khuthaym kua*:* **'Ewe Abu Yazid kwa hakika kama *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angekuona wewe basi bila ya shaka angekupenda sana'**

Na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akamwambia tena Imam Al Rabi Ibn Khuthaym kua: **'Ama kwa hakika kila nikikuona wewe basi mimi hua ni mwenye kuwakumbuka waja wema'**

Na kutokana na kua Ilm kubwa na Ucha Mungu sana basi Imam Al Rabii alikua ni Mwanafunzi pekee wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ambae anaruhusika kumuona Mwalimu wake katika wakati wowote ule autakao, kwani Wanafunzi wengine wote wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* walikua hawaruhusiki kuonana nae bila ya kumtaarifu.

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym alikua ni mwenye kuuzuia na kuulinda Ulimi wake kwa zaidi ya miaka 30, kwani alikua ni mwenye kujiandikia katika kartasi kila neno analolizungumza katika kila siku ya uhai wake, na kisha unapofika wakati wa kuenda

kulala hu ni mwenye kuyahesabu na kuyaangalia yale yote aliyoyasema ndani ya siku hio, na kisha hua mwenye kusema: '**Ole wangu mie, kwani kwa hakika wale waliokaa kimya na kutosema kitu ndio tu waliokoka.'**

Ambapo anasema Imam Muhamamd Ibn Sirin kua: **'Sisi tulienda kwenye Nyumba ya Alqamah Ibn Qays, ambapo mara akaja Al Rabii Ibn Khuthaym akakaa pembeni ya nyumba na kisha akasema: 'Mnatakiwa msitamke kitu chochote isipokua maneno yaliyomo katika hali 9 ambayo ni: *Subhana Allah, Alhamd Lillah, La Ilaha Illa Allah, Allahu Akbar,* Kusoma Quran, Kuamrishana Mema, Kukatazana Mabaya, Kumuomba Mema *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Kumuomba Nusra yake na mambo maovu.''**

Ambapo siku moja aliulizwa Imam Al Rabii Ibn Khuthaym: **'Hivi kwanini wewe si mwenye kukaa barazani pamoja na watu wengine?'** ambapo nae akajibu: **'Kwa sababu ya kuogopa kua sitoweza mimi kutorudisha salaam au kutoinamisha chini macho yangu.'**

Kuna mtu mmoja alienda kwa Imam Al Rabii Ibn Khuthaym na kisha akaanza kumzungumzia mtu mwengine hivyo Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akamuuliza Mtu huyo : **'Hivi Jee umeshawahi kupigana na Warumi?'** Mtu huyo akasema: **'La'** Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akamuuliza tena: **'Jee umeshawahi kupigana na Waajemi?'** Mtu huyo akasema : **'La'** Hivyo Imam Al Rabii Ibn Khuthaym kasema: **'Hivyo hii inamaanisha kua Warumi na Waajemi watakua Salama kutokana nawe lakini Muislam mwenzako hawezi kua salama kutokana nawe, hivyo jee hebu niambie inakuaje?'**

Safari moja Imam Al Rabii Ibn Khuthaym aliulizwa: **'Mbona hujaonekana ukiwa ni mwenye kumkosoa Mtu yeyote yule?' ambapo nae akasema: 'Mimi mwenyewe sijaridhika na nafsi yangu hiyo jee nitaikosoaje nafsi ya mwenzangu?'**

Anasema Imam Bakr Ibn Maiz kua: **'Sisi hatukuwahi kumuona Al Rabii Ibn Khuthaym akiwa ni mwenye kusali Sala ya Sunnah kwenye Msikiti isipokua mara moja tu, kwani yeye alikua ni mwenye kupendelea kufuata Sunnah ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ya Kusali Nyumbani bila ya kuonekana na watu.**'

Anasema Imam Sufyan Ath Thawry kua: '**Amesema Mke wa Al Rabii Ibn Khuthaym kua: 'Kila kitendo cha Ibada kilichokua kikifanywa na Khuthaym kilikua ni cha Siri kubwa sana, kiasi ya kua hata kama akiwa ni mwenye kusoma Qur'an na kisha akaja Mgeni basi Qur'an hiyo hua ni yenye kufichwa kwanza kwa nguo zake'**'

na Imam Abd Rahman Ibn Yazid anasema kua: '**Al Rabii Ibn Khuthaym alikua akimtembelea Alqamah katika siku za Ijumaa na kisha hua wanakaa na**

kuzungumza, nami pia hua wananiita na hivyo hua nakaa nazungumza nao, ambapo Ijumaa moja waliniita nami nikaenda. Na kisha Alqamah akaniambia: ‘Hivi umesikia Al Rabii Ibn Khuthaym amekuja kutuambia nini?’

Nami nikasema: ‘La sijui amekuja kutuambia nini?’ Alqamah akasema: ‘Al Rabii anasema kua, watu wa *Ahl Al Kitabi* mara moja waliniambia mimi kua, hivi hamuona mara ngapi watu wanaomba Dua lakini hawajibiwi?’ hii ni kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua hakubali kupokea kitu isipokua kile kitakachokua ni cha kwake yeye alichopewa kwa Ikhlas.’

Nami nikasema: ‘**Lakini Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* amesema hivyo hivyo pia’ ambapo nae akaniuliza: ‘Amesema?’ nami nikasema: ‘Hivi Jee kwani wewe hukumsikia akisema kua: ‘Naapa kwa yule ambae hakuna mwengine anaestahiki kuabudiwa kua: ‘Allah hapokei jambo lolote kutoka kwa yeyote yule ambae ni mwenye kutaka kusikika au kuonekana au anaecheza cheza, kwani hua ni mwenye kuitikia na kukubali kutoka kwa yule mwenye kusema kutoka ndani ya kina cha Moyo wake’ ambapo nae akasema: ‘Naam, kwa hakika mimi nimesikia akisema hivyo pia.’’’**

Imam Rabia Al Khuthaym alikua ni mwenye kusali na kubakia kwenye rukuu moja ya mwisho usiku kucha na ikiingia Alfajir humalizia Sala yake hio, na kisha alikua akisema: **‘Kwa Hakika wale wenye Ikhlasi wameshatangulia kabla yetu na sisi tumebakia peke yetu huku tukiwa hatuna kitu’** na alikua ni mwenye kuusia kwa kusema kua: **‘Ulinde Moyo wako dhidi ya Mnong’onezo wa Shaytan, ulaghai wake na mitego yake, kwani *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni mwenye kumnyanyua Mja wake kutokana na Unyenyekevu na humuongoza katika kanuni za unyenyekevu na kujisalmisha kwake kutokana na ukubwa wake na kuzijua siri za kila kiumbe wake.’**

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym alisema kua: **‘Kama ukiwa na uwezo wa kua katika sehemu ambayo hutojulikana na mtu yeyote katika wakati huu basi utumie uwezo huo’**

Anasema Imam Al Rabii Ibn Khuthaym kua: **‘Amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alichora umbo la kiboksi cha pembe nne kwenye ardhi, na kisha akachora mstari mmoja kati kati ndani yake hadi nje yake, kisha akachora mistari myengine midogo midogo inayoielekea Mstari huo mkubwa ndani ya kiboksi hicho na kisha akasema kuuoneshea mstari huo wa kati kati kua:**

Huyu ndio Ibn Adam na hiki (kiboksi) kilichomzunguka ndio mipaka ya uhai wake, na hiki (kilichozidi) hua ni Matumaini yake na mategemeo yake, na hii

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

mistari midogo midogo, ni yale mambo yatakayomtokea kwenye Maisha yake, hivyo kikimkosa kimoja basi hua ni mwenye kupatikana na chengine na hicho chengine kikimkosa basi chengine chake hukutana nae’’

Imam Rabii Ibn Khaytham alisema kua: **‘Kila Kitu ambacho hakitofanywa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua ni si chenye manufaa yeyote.’**

Ambapo anasema mmoja kati ya Wanafunzi wake kua: ‘**Mimi nilikua na urafiki na Al Rabii Ibn Khuthaym, lakini sikuwahi kumsikia akizungumza isipokua kwa kutumia maneno mazuri juu ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwani alikua akipenda kusema kua:**

﴿مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلْعِزَّةَ فَلِلَّهِ ٱلْعِزَّةُ جَمِيعاً إِلَيْهِ يَصْعَدُ ٱلْكَلِمُ ٱلطَّيِّبُ وَٱلْعَمَلُ ٱلصَّالِحُ يَرْفَعُهُ وَٱلَّذِينَ يَمْكُرُونَ ٱلسَّيِّئَاتِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَكْرُ أُوْلَٰئِكَ هُوَ يَبُورُ﴾

Man kana yureedu alAAizzata falillahi alAAizzatu jameeAAan ilayhi yasAAadu alkalimu alttayyibu waalAAamalu alssalihu yarfaAAuhu waalladheena yamkuroona alssayyi-ati lahum AAadhabun shadeedun wamakru ola-ika huwa yabooru *(Surat Fatir 35:10)*

Tafsir: ***Mwenye kutaka utukufu basi utukufu ni wa Allah Subhanah wa Ta’ala pekee, kwake yeye ndiko kwenye kupanda maneno mazuri na amali njema lakini kwa wale ambao ni wenye kupanga maovu basi ni juu yao Adhabu kali sana na mipango yao itaangamia.***

Ambapo kwa upande wa Imam Abd Rahman Ibn Ajli basi yeye anasema kua : **‘Siku moja mimi nililala pamoja na Al Rabii, na aliponiona kua nimelala basi alinyanyuka na kuanza kusali na katika kusoma kwake basi akasoma aya isemayo:**

﴿أَمْ حَسِبَ ٱلَّذِينَ ٱجْتَرَحُواْ ٱلسَّيِّئَاتِ أَن نَّجْعَلَهُمْ كَٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّالِحَاتِ سَوَآءً مَّحْيَاهُمْ وَمَمَاتُهُمْ سَآءَ مَا يَحْكُمُونَ﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Am hasiba alladheena ijtarahoo alssayyi-ati an najAAalahum kaalladheena amanoo waAAamiloo alssalihati sawaan mahyahum wamamatuhum saa ma yahkumoona*(Surat Al Jathiya 45:21)*

Tafsir: ***Hivi wanajihesabu wale ambao ni wenye kufanya Maovu kua tutawajaalia malipo sawia kama wale walioamini na wakafanya Mema wakati wakiwa hai na wanakufa? Ni kubaya sana kuhukumu kwao huko.***

Katika Usiku kucha na hivyo akasali kwa kusoma na kuirudia aya hii tuu hadi Alfajir huku akiwa na macho meupee yasiyokua na usingizi hata chembe.'

Na akasema mmoja kati ya Marafiki yake Imam Al Rabii Ibn Khuthaym kua: **'Siku moja mimi nilikua pamoja na Abd Allah Ibn Masud** ***Radhi Allahu Anhu*** **na Al Rabii Ibn Khuthaym, na tulipofika kwenye ukingo wa mto Euphrate basi tukakutana na Tanuri kubwa sana la kuokea Matofali ambalo dani yake mlikua na Moto mkubwa sana na Mvuke mkubwa ni wenye kutoka ndani yake, na kisha Matofali yakawekwa ndani yake. Ambapo Al Rabii alipouona Moto huo basi alisimama akajawa na khofu huku akiwa ni mwenye kusoma aya isemayo:**

﴿إِذَا رَأَتْهُم مِّن مَّكَانٍ بَعِيدٍ سَمِعُواْ لَهَا تَغَيُّظاً وَزَفِيراً۝وَإِذَآ أُلْقُواْ مِنْهَا مَكَاناً ضَيِّقاً مُّقَرَّنِينَ دَعَوْاْ هُنَالِكَ ثُبُوراً﴾

Idha raat-hum min makanin baAAeedin samiAAoo laha taghayyu*dh*an wazafeeran; Wa-idha olqoo minha makanan dhayyiqan muqarraneena daAAaw hunalika thubooran*(Surat Al Firqaan 25)*

Tafsir: ***Wakati Moto utakapowaona wao kutoka sehemu ya mbali, watausikia mvumo wake na mlio wake wa kutisha, na watakapotiwa ndani ya Uchochoro wake wakiwa wamefungwa minyororo watalia kwa sauti kali sana kwa Muangamizo wake.***

Na kisha Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akazimia hapo hapo, ambapo nasi tukamsubiri kwa mda hadi akazindukana na kisha tukampeleka Nyumbani kwake.

Safari moja Imam Al Rabii Ibn Khuthaym alinunua Farasi kwa malipo ya Dirham 30000, ambae alikua akimtumia kwa ajili ya kupigani vita vya Jihad, hivyo siku moja aliporudi Nyumbani basi mfanyakazi wake aitwae Yassir alimchukua Farasi huyo na kuenda kumfunga, na baada ya mda alipoenda kumuangalia basi akatuka kua Farasi

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

huyo hayupo, hivyo akarudi kwa Imam Al Rabii Ibn Khuthaym na kumlalamikia kwa kusema: **‘Ewe Al Rabii Farasi hayupo, kaenda wapi?**’

Imam Al Rabii akajibu: **‘Farasi wangu ameibiwa ewe Yasir’** Yasir akashangaa na kuuliza: **‘Jee uliona wewe wakati alipokua akiibiwa?’**

Ambapo Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **‘Naam, aliibiwa wakati mimi nilipokua kwenye Dhikr Allah, hivyo sikuweza kuachana na Dhikr Allah kwa ajili Farasi wangu, kwani hakuna chenye Umuhimu kwangu mimi zaidi ya Mola wangu.’**

Na kisha Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akaomba dua kwa kusema: **‘Ya Allah hakika alieiba ameniibia mimi na wala simimi niliemuibia yeye, hivyo ya Allah kama yeye ni Tajiri basi muongoze na kama ni masikini basi mpe utajiri.’**

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym amesema kua: **‘Yeyote yule atakaesema *La Ilaha Illa Allah Wahdahu la Sharika La, Lahu al Mulk wa Lahu Al Hamd wa Huwa aAla Kulli Shayin Qadir* mara 10 hua ni sawa na aliewaachia huru Watumwa wanne kutoka katika kizazi cha Nabii Ismail.’**

Ambapo anasema Imam Amr Ash Shabi kua: **‘Mimi nilimuliza Al Rabii Ibn Khuthaym: ‘Jee umeyasikia wapi maneno haya?’ ambapo nae akasema: ‘Kutoka kwa Amr Ibn Maimun’ hivyo nami nikamfuata Amr Ibn Maimun na kumuuliza; ‘Jee umeyasikia wapi maneno haya?’ ambapo nae akasema kua: ‘Nimeyasikia kutoka kwa Ibn Abi Laila’ hiivyo nikamfuata Ibn Abi Laila na kumuuliza: ‘Jee umeyasikia wapi maneno haya?’ ambae nae akasema kua: ‘Amesema Abu Ayub Al Ansari ambae yeye ameyasikia kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.’’***

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym alikua ni miongoni mwa wenye kuitafsiri ile aya isemayo:

﴿وَسَارِعُوٓاْ إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا ٱلسَّمَاوَاتُ وَٱلْأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ۞ٱلَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِى السَّرَّآءِ وَٱلضَّرَّآءِ وَٱلْكَاظِمِينَ ٱلْغَيْظَ وَٱلْعَافِينَ عَنِ ٱلنَّاسِ وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلْمُحْسِنِينَ﴾

WasariAAoo ila maghfiratin min rabbikum wajannatin AAardhuha alssamawatu waal-ardhu oAAiddat lilmuttaqeena; Alladheena yunfiqoona fee alssarra-i

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

waaldhdharra-i waalkadhimeena alghaydha waalAAafeena AAani alnnasi waAllahu yuhibbu almuhsineena *(Surat Al Imran 3:133-134)*

Tafsir: ***Na Kimbilieni njia inayoeleeka kwenye usamehevu wa Mola wenu, na Pepo ambayo upana wa ardhi yake ni kama upana wa Mbingu na ardhi zilizotayarishwa kwa ajili ya wenye Taqwa. Wale Ambao ni wenye kutoa (Kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala) kile walichoruzukiwa iwe kwenye wakati wa neema na wakati wa shida na wakazizuia hasira zao na wakawasamehe watu basi Allah huwapenda wenye kufanya Mema.***

Kua wenye kuzizuia hasira zao hua ni wale ambao ni wenye kuzivua Nafsi zao kutokana na kutokua na Kisasi.

Imam Ibn Abi Duniyah anasema kua: **'Pale Imam Al Rabii Ibn Khuthaym alipokua akihisi ugumu ndani ya Moyo wake basi alikua Usiku ni mwenye kuenda kwenye Kaburi la rafiki yake aliefariki na kisha hua ni mwenye kunadia kwa kusema: 'Ewe Fulani Ibn Fulani, hakika mimi natamani kama ningekua ni mwenye kujua kilichokufika wewe ulipofika mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*' na kisha huanza kulia hadi machozi yakamtiririka kwa wingi sana.'**

Ambapo kwa upade mwengine kuna wasemao kua: **'Imam Al Rabi Ibn Khaytham alikua ni mwenye kuchimba Kaburi Nyumbani kwake, na hivyo anapokua ni mwenye kuhisi ugumu wa Moyo wake, basi hua ni mwenye kuingia ndani ya Kaburi hilo na kulala kwa muda wa saa moja na kisha hua ni mwenye kutoka huku akisema: 'Umerudi, tena Duniani hivyo basi fanya mema kabla haijafika ile siku ambayo ni yenye kuelezewa na aya zisemazo:**

﴿حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءَ أَحَدَهُمُ ٱلْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ٱرْجِعُونِ۝لَعَلِّيٓ أَعْمَلُ صَالِحاً فِيمَا تَرَكْتُ كَلاَّ إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَآئِلُهَا وَمِن وَرَآئِهِمْ بَرْزَخٌ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ﴾

Hatta idha jaa ahadahumu almawtu qala rabbi irjiAAooni; LaAAallee aAAmalu salihan feema taraktu kalla innaha kalimatun huwa qa-iluha wamin wara-ihim barzakhun ila yawmi yubAAathoona *(Al Mu'minun: 23:99-100)*

Tafsir: ***Hadi pale yatakapomjia mmoja wao Mauti na hivyo atakua ni mwenye kusema: 'Ewe Mola wangu nirudishe. Ili nipate kufanya mema niliyoacha Nyuma' la hayo si chochote bali ni maneno tu na nyuma yao kuna Barzakh hadi katika siku watakayofufuliwa.***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Mnamo mwishoni wa Uhai wake Imam Al Rabii Ibn Khuthaym alipatwa na Mtihani wa maradhi ya kupooza na hivyo alikua si mwenye kua na uwezo kutoka nje lakini hata hivyo Wanafunzi wake walikua wakimfuata kwa ajili ya kunufaika na Ilm yake kama anavyosema Hilal Ibn Isa pale alipomwambia Mundhir Al Thawry kua: **'Hivi jee nikupeleke kwa Shaykh, ambae atatupelekea sisi kutuzidishia Imani zaid?'**

Ambapo Mundhir Al Thawry akasema: **'Naam bila ya shaka kwani Malengo ya kuja kwangu katika Mji wa Kufah hasa ni kukutana na Shaykh wenu Mkuu Al Rabi Ibn Khuthaym, kwani mimi nna hamu sana kuishi katika mazingira yaliyojaa Imani, ila jee ataturuhusu sisi kuonana nae? Kwani nimesikia kua naumwa na amepooza katika baadhi ya sehemu ya Mwili wake na hatoki nje, na hivyo ni mwenye kutumia mda wake na Mungu wake tu na haonani na watu.'**

Ambapo Hilal akasema: **'Naam ingawa yuko katika hali hio kwa mda mrefu sasa, lakini hata hivyo maradhi hayo hayajambadilishia tabia zake'**

Ambapo Mundhir Al Thawry akasema: **'Kwa unavyonjua wewe Shaykh kutokana na ukarimu na upole wake, jee nnaweza kumuuliza masuali au itanibidi nikae kimya tu huku nikimsikiliza atakachosema?'**

Hilal akasema: **'Hata kama ukikaa kimya mbele yake kwa uda wa mwaka mzima basi kamwe Al Rabii Ibn Khuthaym hatosema kitu, hatozungumza nawe hadi pale utakapomuuliza kwani yeye hua ni mwenye kuhesabu kila neno lake kua linatakiwa liwe ni Dhikr na kimya chake kua ni Tafakkur'**

Hivyo Mundhir akasema: **'Kama ni hivyo basi wacha twende tukamuangalie'**, hivyo wakatoka na walipofika kwenye nyumba ya Imam Al Rabii Ibn Khuthaym wakagonga mlango na kujitambulisha na kisha wakaomba kuingia ndani, na wakaruhusiwa, na kukutana nae Imam Al Rabii Ibn Khuthaymah na kumuuliza hali yake.

Ambapo Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akajibu: **'Hakika mimi nnajisikia dhaifu mwili wangu, lakini hata hivyo bado nnaendelea kunufaika na Rehma za Mola wangu juu yangu.'**

Ambapo Hilal akasema: **'Kuna Daktari mzuri sana amewasili katika Mji wa Kufah. Hivi jee unataka nimlete aje kukuangalia?'**

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **'Ewe Hilal hakika mim ini mwenye kujua kua Dawa hua ni zenye kusaidia, lakini hapo hapo nimewaona watu wa Ad, Thamud na makabila ya watu wengine pia, nimeona ari yao katika kuifuatilia Dunia na kutafuta mapambo ya Dunia, na wao walikua ni wenye nguvu na imara miili yao zaidi yetu, na mbali ya kua nao pia walikua na madaktari na wagonjwa**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

lakini hakuna hata Daktari mmoja aliekua bingwa aliebakia hai na wala Mgonjwa alietibiwa nae ambae aliishi milele.'

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **'Lakini kwa hakika mimi kama haya ni maradhi basi ningeyatibu'** hivyo Mundhir akauliza: **'Kwani unadhani ni maradhi gani?'**

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **'Dhambi na dawa yake ni Istighfar na kutubu kwa kutorudia kuyafanya tena.'**

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akaendelea kusema: '**Haya ni mambo yaliyofichikana, yasiyooneana na macho ya mtu wa kawaida, ijapokua hua hayafichikani mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Hivyo umuhimu nikufanya mema tu kila siku ndio Dawa yake.'**

Kisha Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akaanza kulia, hivyo Mundhir akauliza: **'Basi inatosha mbona unalia sana hivyo? Kwani kutokana na hali yako hua haifai'**

Ambapo Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akauliza kwa kusema: **'Na kwanini mimi nisilie hivi wakati mimi nimekutana na Masahaba wengi sana ambapo kama tukijifananisha nao basi mbele yao sisi hua ni kama Majambazi.'**

Wakati Imam Al Rabii Ibn Khuthaym anasema hivyo basi mlango wake ukawa unagongwa, na Imam Al Rabi Ibn Khuthaym akasema: **'Ingia'** na hapo akaingia mtoto wa Imam Al Rabii Ibn Khuthaym ambae alisema: '**Ewe Baba Mama amekutayarishia Vileja uvipendavyo kwa ajili yako jee nikuletee?'** Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **'Naam'** hivyo mtoto huyo akatoka na kisha mlango ukagongwa tena na Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **'Ingia.'**

Na hivyo akaingia mtu mzee ambae alikua ni mwenye muonekano kama wa mtu asiekua na akili na ni mwenye kuchuruzikwa na madenda mdomoni ambae alipoingia basi akakaa kwenye kiti ambacho mbele yake kuna meza, na mara akaingia mtoto wa Imam Al Rabii Ibn Khuthaym na kuamirshwa na Imam Al Rabii kuweka sahani ya Vileja juu ya meza, na mzee huyo akaanza kula vileja hivyo vyote hadi akavimaliza.

Na baada ya hapo mtoto huyo akasema: '**Allah amuingize kwenye rehma zake Baba yangu, kwani Mama yangu amefanya kazi kubwa kwa ajili ya kupika Vileja hivi kwa ajili ya Baba yangu ambae anavipenda sana, lakini hata hivyo baba yangu hata hakuvionja mbali ya kua anavipenda na akavitoa kwa wale wasiojua hata ni nini kile walichopewa kula.'**

Imam Al Rabi Ibn Khuthaym akasema:

﴿لَنْ تَنَالُواْ ٱلْبِرَّ حَتَّىٰ تُنْفِقُواْ مِمَّا تُحِبُّونَ وَمَا تُنْفِقُواْ مِنْ شَيْءٍ فَإِنَّ ٱللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ﴾

Lan tanaloo albirra hatta tunfiqoo mimma tuhibboona wama tunfiqoo min shay-in fa-inna Allaha bihi AAaleemun *(Surat Al Imran 3:92)*

Tafsir: ***Na hamtoweza kuufikia Ucha Mungu hadi pale mtakapotoa miongoni mwa vile mnavyovipenda, na juu ya kila mnachokitoa basi Allah ni mwenye kujua juu yake.***

Wakati anamalizia kusoma aya hio basi mara akaingia mtu ambae akasema kumwambia Imam Al Rabii Ibn Khuthaym kua: **'Ewe Abu Yazid, Al Husayn ameuliwa.'**

Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **'Inna lillahi wa inna ilaihi rajiun'** na kisha akasoma aya ifuatayo:

﴿قُلِ ٱللَّهُمَّ فَاطِرَ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلْأَرْضِ عَالِمَ ٱلْغَيْبِ وَٱلشَّهَادَةِ أَنتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِي مَا كَانُواْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ﴾

Quli allahumma fatira alssamawati waal-ardhi AAalima alghaybi waalshshahadati anta tahkumu bayna AAibadika fee ma kanoo feehi yakhtalifoona. *(Surat Az Zumar 39:46)*

Tafsir: ***'Sema (Ewe Muhammad) Ewe Allah muanzilishi wa Mbingu na Ardhi, mwenye kujua yanayoonekana na yasiyoonekana, wewe ni ndie mwenye kutoa hukmu baina ya Waja wako kuhusiana na yale waliyo tofautiana.'***

Hivyo mtu huyo akauliza: **'Hivi Jee una mtizamo gani juu ya mauaji haya ewe Al Rabii?'** Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: '**Wote hao watakutana kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ndiko watakapo hukumiwa'**

Ambapo Hilal Ibn Isa akasema: **'Naam hebu tuusie kidogo'** na hivyo Imam Al Rabi Ibn Khuthaym akasema: '**Ewe Hilal usiridhike na sifa za Ibn Adam juu yako kwani wao ni wenye kujua juu ya muonekano wa nje wa Mwili wako, hivyo jua kua utahesabiwa kila kitu chao, hivyo kila kisichofanywa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kitakua ni chenye kuyeyuka.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na Mundhir akasema: **'Na mimi niusie tafadhali'** Imam Al Rabi Ibn Khuthaym akasema: '**Ewe Mundhir Muogope *Allah Subhanah wa Ta'ala* huku ukiwa ni mwenye kujua juu ya kile ulichokua nacho na kile usichokua nacho, na kisha muachie kila kitu chako *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Ewe Mundhir usiseme kumwambia Mola wako kua unatubu wakati wewe si mwenye kutubu bali ni mwenye kudanganya kwani baadae unafanya makosa hayo hayo, hivyo sema kumuomba Mola wako kwa kusema : 'Ya Allah nipokelee Toba yangu'

Ewe Mundhir fahamu kua hakuna haja ya kuzugumza chochote isipokua kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na kumsabih na kumpwekesha, na kukatazana yale aliyoyakataza na kuamrishana mema na kusoma Qur'an.

Kumbukeni Kifo katika kila wakati wa uhai wenu kwani kinakupelelezeni bila ya nyinyi kujijua, kwani kitu chochote kile kilichopotea kwa mda mrefu hua ni chenye kuibuka tena baadae hivyo jee tutafanyeje sisi kesho Akhera?

Na kisha baada ya hapo Imam Al Rabi Ibn Khuthaymah akaanza kulia na kisha akasoma aya ifuatayo:

﴿ كَلَّآ إِذَا دُكَّتِ ٱلْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا ۝ وَجَآءَ رَبُّكَ وَٱلْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا ۝ وَجِاْيٓءَ
يَوْمَئِذٍۭ بِجَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ ٱلْإِنسَٰنُ وَأَنَّىٰ لَهُ ٱلذِّكْرَىٰ ۝ ﴾

Kall<u>a</u> i<u>dh</u>a dukkati al-ar<u>dh</u>u dakkan dakk<u>a</u>n; Waj<u>a</u>a rabbuka waalmalaku <u>s</u>affan <u>s</u>aff<u>a</u>n; Wajee-a yawma-i<u>dh</u>in bijahannama yawma-i<u>dh</u>in yata<u>dh</u>akkaru al-ins<u>a</u>nu waann<u>a</u> lahu al<u>dhdh</u>ikr<u>a</u>*(Surat Al Fajr 89:21-23)*

Tafsir: ***'La pale Ardhi itakaposagwa na kua unga Na Mola wako atakapokuja na Malaika kwa safu na safu na kuletwa Jahannam karibu katika siku hio ndio Mtu atakapokumbuka, lakini kukumbuka kwake huko hakutomfaa kitu'***

Na baada ya kusoma aya hio basi Adhana ikaadhaniwa, na hivyo Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema kuwambia Mtoto wake: '**Twende zetu Msikitini ewe Mtoto wangu'** na hivyo nasi tukamsaidia kwa kila mmoja wetu kwa kumbeba bega moja huku na moja huku, huku miguu yake ikiwa ni yenye kujiburura kidogo kidogo, huku Mundhir akiwambia Imam Al Rabii Ibn Khuthaym kua: **'Ewe Abu Yazid *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekusamehe na kukupa afueni ya kuweza kusali nyumbani'**

Lakini Imam Al Rabii Ibn Khuthaym akasema: **‘Uko sahih usemavyo ewe Mundhir lakini sasa mimi nimemsikia Muadhini akisema Njooni kwenye Mafanikio, hivyo yeyote yule miongoni mwetu atakaesikia wito wa kuenda kwenye mafanikio basi inambidi kuitikia wito huo kuelekea kwenye Mafanikio hata kama kwa kutambaa kama ikimbidi’**

Imam Al Rabii Ibn Khaytham alifariki mnamo mwaka 65 Al Hijra, ambapo wakati anakaribia kufariki basi Binti yake alikua akilia na hivyo Imam Al Rabi Ibn Khuthaym akasema kumwambia Binti yake huyo kua: **‘Usilie ewe Binti yangu kwani kwa hakika Baba yako anaelekea kwenye sehemu njema’**

IMAM MASRUQ AL QUFI 1 AH

Masruq Ibn Ajda Ibn Malik Ibn Umayyah Ibn Abd Allah Ibn Murri Ibn Salman Al Hamadani Al Wadii Al Kufi alizaliwa mnamo mwaka wa kwanza Al Hijra. Ambapo wanasema Wanazuoni kua jina lake la umaarufu la Masruq lililotoka na neno *Masruq* ambalo hua limaanisha Mtu alieibiwa au alietekwa Nyara na hii ni kutokana na kua Imam Masruq alipokua mtoto mdogo aliwahi kuibiwa akawa haonekani lakini baadae akapatikana.

Imam Masruq alikua ni mwananfuzi aliejipatia Ilm yake ya Dini kutokana na kusoma kwa Masahaba wakiwemo *Umm Ul Muuminin* Aisha, *Sayyidna* Ali Ibn Abi Talib na Abd Allah Ibn Masur *Radhi Allahu Anhum* na pia alisoma kwa Qadhi Al Shuraykh. Na hivyo miongoni mwa Wanafunzi wake wamo kina Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Anas Ibn Sirin, Shaqiq Ibn Salama, Imam Amr Ash Shabi, Imam Abd Rahman Ibn Abd Allah Masud n.k

Ambapo anasema Ibrahim Ibn Muntasir kua: ‘**Masruq alikua ni mwenye kufunga pazia baina yake na familia yake na kisha hua ni mwenye kuingia kwenye Ibada zake na kuwaacha wao na Dunia yao.**’

Na anasema Imam Ash Shabi kua: ‘**Siku Moja katika wakati wa Kiangazi Masruq alizimia kutokana na kua ni mwenye kufunga, kwa kawaida alikua si mwenye kulalamika juu ya chochote kwa Binti yake. Ambapo baada ya tukio hilo basi Binti huyo akamwambia Baba yake: ‘Ewe Baba yangu bora fungua tu unywe maji.’’**

Imam Masruq akauliza: ‘Hivi unataka nini kutoka kwangu ewe Binti yangu?’. Binti huyo akasema: ‘Mimi nilikua nataka ujihurumie nafsi yako’ ambapo Imam

Masruq akajibu: 'Yaani Ewe Binti yangu unataka kua mimi nijihurumie kwa siku moja dhidi ya siku ambayo umri wake ni miaka elfu 50?'

Ambapo kwa upande wa Imam Amr Ash Shabi basi anasema kua: **'Wakati Ubayd Allah Ibn Ziyad alipokuja katika Mji wa Kufah aliliza, hivi jee ni nani Mtu bora miongoni mwenu?' na watu nao wakajibu Masruq.'**

Na akasema tena Imam Amr Ash Shabi kuhusiana nae kua: **'Masruq ndie anaestahiki hasa kutoa Fatwa kuliko Qadhi Shuraykh , kwani Qadhi Shuraykh alikua akiuliza zaidi kuhusiana na mitizamo ya Masruq.'**

Ambao alisema Imam Ibn Madini alisema kua: **'Hakika mimi siwezi kumruhusu yeyote yule kusali nyuma ya Abu Baqr katika sala ya Jamaa isipokua Masruq.'**

Na Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema kua amesema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: **'Hakuna Mtu muhimu baada Al Qamah kama Masruq.'**

Imam Yahya Ibn Main nae akasema kuhusiana na Imam Masruq kua: **'Masruq alikua ni mtu ambae anaaminika na hakuna aliekua na mfano wake, Uthman Ibn Saad alimuuliza Yahya kuhusiana na Masruq na Urwa kuhusiana na *Umm ul Muuminin* Aisha, na hakua ni mwenye kusita katika kujibu kwake kwani alisema: 'Yeye Masruq ni Mtu ambae anaaminika na ana hadithi nyingi sana zinazostahiki kunukuliwa.''**

Ambapo kwa upande wa Imam Al Ajali basi yeye anasema kua: **'Imam Masruq alikua ni *Tabiina* Muaminifu na ni miongoni mwa watu wa karibu wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua ameruhusika kutoa Fatwa hadharani, na alikua akisali hadi miguu inavimba.'**

Imam Abu Naim amesema kuhusiana na Imam Masruq kua: **'Miongoni mwa Marafiki wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* alikuwepo mmoja ambae alikua akimuogopa sana Mola wake na kumpenda sana pia Mola wake, hivyo ilikua kila siku anazikumbuka Dhambi zake alizozifanya.'**

Na Imam Said Ibn Jubayr anasema kua: '**Masruq alikutana na mie na akasema: 'Ewe Said hakuna cha kutufanya sisi tupendezwe isipokua kuzisugua Nyuso zetu na Mchanga.'**'

Ibrahim Ibn Muhamamd Ibn Al Muntasir anasema kua: '**Khalid Ibn Abd Allah Ibn As ambae alikua ni Gavana wa Basrah alimpa zawadi Mjomba wangu Masruq Dirham 30000 katika wakati ambao alikua akizihitaji sana, lakini hata hivyo hakuzichukua.**'

Ibrahim Ibn Muhamamd Ibn Al Muntasir anaendelea kusema kua: '**Masruq hakua ni mwenye kuchukua malipo wakati anapofanya kazi ya Qadhi kwani alikua ni mwenye kuongozwa na ile aya isemayo:**'

﴿إِنَّ ٱللَّهَ ٱشْتَرَىٰ مِنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ ٱلْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعْداً عَلَيْهِ حَقّاً فِى ٱلتَّوْرَاةِ وَٱلإِنْجِيلِ وَٱلْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ مِنَ ٱللَّهِ فَٱسْتَبْشِرُواْ بِبَيْعِكُمُ ٱلَّذِى بَايَعْتُمْ بِهِ وَذٰلِكَ هُوَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ﴾

Inna Allaha ishtara mina almu/mineena anfusahum waamwalahum bi-anna lahumu aljannata yuqatiloona fee sabeeli Allahi fayaqtuloona wayuqtaloona waAAdan AAalayhi haqqan fee alttawrati waal-injeeli waalqur-ani waman awfa biAAahdihi mina Allahi faistabshiroo bibayAAikumu alladhee bayaAAtum bihi wadhalika huwa alfawzu alAAadheemu *(Surat At Tawbah 9:111)*

Tafsir: ***Kwa Hakika Allah amenunua Maisha ya Waumini na Mali zao kwa bei ambayo malipo yake ni Pepo. Wanapigana kwa ajili ya njia ya Allah hivyo wanaua wengine na wao wanauliwa. Na amewaahidi Allah kwa haki ambayo ameihakikisha ndani ya Tawrati na Injil na Qur'an na jee ni nani Mkweli katika kutimiza Ahadi zaidi ya Allah? Hivyo furahieni Makubaliano ambayo mmekubaliana kwani huko ndio kwenye kufuzu kukubwa sana.***

Ibrahim Ibn Muhamamd Ibn Al Muntasir anaendelea kusema kua: '**Amesema Masruq kua hakuna kitu bora kwa Muumini zaidi ya Kaburi kwani hua ni mwenye kua mbali na matatizo na mazonge ya kidunia, na hua yuko salama kutokana na Adhabu za Allah.**'

Amesema Abu Dhuha kua: '**Siku moja Masruq alimsaidia mtu kwa kumuombea Msamaha, na kisha mtu huyo akampa Masruq zawadi ya Mtumwa wa kike, ambapo Masruq akakasirika na kusema: 'Na kama ningejua kua haya ndio yaliyokuwemo ndani ya ufahamu wako basi nisingezungumzia juu yake na wala nisingemalizia kukuombea, kwani mimi nimesikia Abd Allah Ibn Masud akisema kua: 'Yeyote yule anaetoa Msaada kumuombea Mtu kwa nia ya kupata haki yake au ya kudharau dhulma, halafu akawa ni mwenye kulipwa kutokana nao msamaha huo na kisha akapokea basi hicho alichokifanya hua ni Haram.'**''

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo anasema Imam Amr Ash Shabi kua amesema Imam Masruq kua: '***Umm ul Muuminin* Aisha *Radhi Allahu Anha* alimwambia Masruq kua: 'Ewe Masruq hakika mimi ninakuchukulia wewe kua kama Mtoto wangu wa kumzaa na wewe ni miongoni mwa watu nnaowapenda zaidi, hivyo jee unayo Ilm ya kuijua kasoro ya Nafsi yako?**''

Anasema Imam Amr Ash Shabi kua: '**Masruq alisafiri kutoka Kufah kuelekea Basra kwa ajili ya kuifuata maana ya aya moja tu kwa mtu fulani, na alipofika katika Mji wa Basra akaambiwa na mtu huyo kua yeye haijui maana ya aya hio lakini anaeijua anaishi Dimashq nchini Syria, hivyo Masruq akafunga safari kueleka kwenye ardhi ya nchi ya Syria**.'

Alipochaguliwa kua Qadhi wa Mji wa Kufah basi hakua ni mwenye kuchukua mshahara wowote kutokana nayo kazi hio kwani alikua akisema kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala* amenunua maisha yangu na mali kutoka kwa Waislam dhidi ya Pepo, na kusema kua:** '**Hakika mimi nna mtizamo mzuri juu ya Mja wangu pale anaposema kua hakuna unga wala dirham kwenye nyumba yake'**'

Siku moja Imam Masruq alikua amepanda Punda wake akiwa amefuatana na Mtoto wa Dada yake ambae alimuuliza kwa kumwambia: '**Jee unataka nikuoneshe Dunia?**' na Mtoto huyo wa Dada yake akaitikia :**'Naam**' hivyo Imam Masruq akaenda nae hadi kwenye mahame ya Hira na kisha alipofika akamuonesha na kumwambia: '**Hii ndio Dunia, watu wake wamekula na kuibadilisha kua ni uchafu na wamevaa nguo na kuzibadilisha kua ni matambara.**'

Katika siku ambayo alikua anafariki Imam Masruq basi alikua akilia huku akisema: '**Hakika mimi niko baina ya njia mbili na siji nitapelekwa wapi, nitapelekwa Peponi au Motoni.**' Imam Masruq alifariki huku akiwa hana hata ndururu ndani ya nyumba yake kiasi ya kua iliwabidi watu wachangishane ili wamnunulie Sanda ya kumvisha.

Imam Sufyan Ibn Uyayna anasema kua: '**Masruq alifariki mnamo mwaka 63 Al Hijra.**'

IMAM QABISAH IBN DHUAYB 8 AH

Imam Abu Said Qabisah Ibn Dhuayb Al Khuzai Amr Ibn Kulaib Ibn Asram Ibn Abd Allah Ibn Qamir Ibn Habashiah Ibn Salul Ibn Kaab Ibn Amr Ibn Rabi'ah alizaliwa mnamo mwaka wa 8 Al Hijra katika Mji wa Madina ambapo baba yake alikua ni *Sahaba*

wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam. Na hivyo Imam Qabisah alikua ni mwenye kujipatia Ilm yake kutoka kwa Masahaba wakiwemo Abu Baqr As Siddiq, Umar Al Khattab, Abu Al Dardaa, Zayd Ibn Thabit, Bilal Ibn Rabah, Abd Rahman Ibn Awf, Ubaydah Ibn Samit, Tamim Ad Dari na wengine *Radhi Allahu Anhum.*

Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hjar Al Asqalani amesema kuhusiana na Imam Qabisah kua: '**Qabisah Ibn Dhuayb alikua ni mmoja kati ya Watoto wa Masahaba na alizaliwa katika kipindi cha uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini hakuwahi kunukuu kutoka kwake.**'

Na hivyo tangu utotoni Imam Qabisah alikua ni mwenye kua na Ilm kubwa sana kutokana na Walimu aliokua nao na pia kutokana na jitihada zake na majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake. Na akawa pia ni Mwalimu wa watoto wenzake katika Mji wa Madina na alipokua mkubwa basi ikawa anahesabika kua ni mmoja kati ya Wanazuoni wa juu wa Mji wa Madina.

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Az Zuhri, Imam Is-haq Ibn Qabisah, Imam Makhul, Imam Abu Shatta Jabir Ibn Zayd, Imam Uthman Ibn Ubayd Allah, Imam Rajaa Ibn Haywa na wengineo.

Amesema Abu Zinad kua: '**Abd Al Malik Ibn Marwan alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni wanne Wacha Mungu, ambao ni yeye mwenyewe, Said Ibn Al Musayyib, Urwa Ibn Az Zubayr na Qabisah Ibn Dhuayb.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Makhul basi yeye amesema kua: **'Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu mwenye Ilm kubwa kama Qabisah.'**

Na kwa upande wa Imam Ash Shabi basi yeye anasema kua: **'Qabisah alikua ni mwenye Ilm kubwa zaidi kuliko wote kulingana na mtizamo wa Zayd Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu.*'**

Na akasema Imam Ibn Shihab kua: **'Qabisah ni mmoja kati ya Wanazuoni wa Ummah huu.'**

Imam Adh Dhahabi amesema kua: **'Qabisah ni Thiqah mwenye kuaminika na ni mwenye Hadith nyingi sana.'**

Imam Qabisah aliishi katika Mji wa Madina na kisha baadae akahamia katika Mji wa Dimashq na akawa ni Waziri wa Khalifa Abd ul Malik Ibn Marwan baada ya kujeruhiwa katika vita vya Hara na kupofuka Jicho Moja na alifariki mnamo mwaka 88 Al Hijra.

IMAM AL QARI ABD ALLAH AL DIMASHQ 8 AH

Imam Abd Allah Ibn Amr Al Dimashq alizaliwa mnamo mwaka wa 8 Al Hijra katika Mji wa Dimashq nchini Syria.

Imam Abd Allah Al Dimashq alikua akijulikana pia kwa jina la Imam Abu Imran Al Yahsabi na alikua ni Mtaalamu mkubwa sana wa Ilm ya kisomo cha Qur'an kwani ni mmoja kati ya Maimamu ambao *Qiraa* chake kinahesabika kua ni moja kati ya aina 7 za Qiraa cha Qur'an.

Imam Abd Allah Ibn Amr alisoma kwa Imam Al Mughira Ibn Abi Shihab. Na ingawa Imam Abd Allah Ibn Amr mwenyewe anasema kua: '**Hajui ni nani aliemsomesha aina ya Qiraa chake'** lakini kwa upande wa Imam Al Jazari basi yeye anasema kua: **'Kuna nukuu za aina nane tofauti ambazo zimetokana nae na iliyosahihi kabisa ni ile inayosema kua alisoma Qura'n kwa Al Mughira.'**

Ambapo anasema Al Haytham Ibn Imran kua: '**Abd Allah Ibn Amr alikua ni Imam wa katika Msikiti katika kipindi cha Utawala wa Al Walid Ibn Abd ul Malik, na alikua ni mwenye kusema kua ametokana na asili ya watu wa Himyar lakini kuna watu waliokua wakipingana nae juu ya asili yake hio.**'

Imam Abd Allah Ibn Amr alikua pia ni mtaalamu wa Ilm ya Hadith na Fiqh na hivyo baada ya kufariki Imam Bilal Ibn Abi Darda aliekua Qadhi wa Syria basi Imam Abd Allah Ibn Amr Ad Dimashq akachaguliwa kua ni Qadhi wa Mji wa Dimashq, na hivyo Imam Abd Allah Ibn Amr alikua akikubalika sana na watu wa Syria na aina ya Qiraa chake kua ni chenye kupendwa sana na watu wa Syria.

Imam Al Qari Abd Allah Ibn Amr Al Dimashq aliishi kwa mda wa miaka 110 kwani alifariki mmo mwaka 118 Al Hijra katika Mji wa Dimashq na kuwaacha Wanafunzi wake wakuu wawili ambao ni Hisham Ibn Ammar Ibn Nuayr Ibn Maysara ambae alizaliwa mnamo mwaka 153 Al Hijra na kufariki mnamo mwaka 245 Al Hijra.

Hisham Ibn Ammar Ibn Nuayr Ibn Maysara alikua ni mtaalamu wa Ilm ya Qiraa cha Qur'an, Hadithi na Fiqh na alikua ni mwenye kunukuu Hadith 400 kutoka kwa Mwalimu wake.

Mwanafunzi wa pili wa Imam Abd Allah Al Dimashq alikua ni Imam Abd Allah Ibn Ahmad Ibn Bashir Ibn Dakwan ambae pia alisoma kwa Imam Al Qari Al Kisai. Imam Al Dakwan alizaliwa mnamo mwaka 173 Al Hijra na alifariki mnamo mwaka 242 Al Hijra.

IMAM YUNUS IBN MAYSARA 12 AH

Imam Abu Ubaydah Yunus Ibn Abd Allah Ibn Maysara Al Hamiri alizaliwa katika maeneo ya Dimashq mnamo mwaka 12 Al Hijra na hivyo alijipatia Ilm yake kutoka kwa Masahaba na Wanazuoni waliokua wakiishi katika ardhi ya Sham wakiwemo Muawwiyah Ibn Abu Sufyan *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*, Ummu Ad Dardaa *Radhi Allahu Anha*, *Abu Said Az Zuraqi Radhi Allahu Anhu* Abd Allah Ibn Bishr, Abu Muslim Al Khawlani, Amr Ibn Waqid na wengineo.

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Daud, Imam Darqutni na Imam Ibn Saad basi wanasema kua: **'Imam Yunus Ibn Maysara ni Thiqah na anaeaminika.'**

Imam Yunus Ibn Maysara alikua ndie pia msomaji wa Qur'an wa Masjib Ayub wa Dimashq ambapo anasema Haytham Ibn Imran kua: **'Yunus Ibn Maysara alikua akiomba Dua siku moja wakati Jua lilipokua likitua na alikua akisema: 'Ya Allah, nijaalie mie kua ni mwenye kuupata Ushahidi, hivyo nikashangaa mimi kwa nini anomba Dua awe Shahidi wakati yeye ni mwenyewe ni kipofu?'lakini hata hivyo Abd Allah Ibn Ali alipoingia katika Mji wa Dimashq basi Ibn Maysara aliupata ushahidi huku akiwa na mri wa miaka 120'**

Ambapo anasema Abd Rahaman Ibn Walid kua**: 'Yunus Ibn Maysara wakati alipokua anakribia kifo chake basi alikua akisema: Wacha Mungu wameshamalizika, na kilichobakia ni watu wenye kunuka harufu ya maovu ya wakati huu tu.'''**

Alisema Imam Yunus Ibn Maysara kua: **'Jambo Jema hua ni lenye kuupa Moyo Utulivu, na Jambo ovu hua ni lenye kuyaongeza Kasi Mapigo ya Moyo''**

Amesema pia Imam Yunus Ibn Maysara kua: **'Wasil aliomba Dua kwa kusema kua: 'Ewe Mola wangu, kwa hakika fulani Ibn fulani yupo ndani ya Usimamizi wako, na anakabiliana na Adhabu ya Kaburi na Mitihani yake, na wewe ni Muadilifu na mwenye uwezo juu ya kila kitu, hivyo msamehe na muingize kwenye rehma zako, kwani wewe ni mwingi wa Rehma na Huruma.''**

Na akasema tena kua amesema: **'Abu Idris Al Hawlani kua amesema Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Wakati Mtu anapotoka kwenye nyumba yake na kuelekea kwa ndugu yake mgonjwa kwa ajili ya kumtizama, basi hua ni mwenye kuingia kwenye Rehma ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na anapokaa pembeni yake ndugu yake huyo anaeumwa, basi Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* humfunika'**

Amesema pia Imam Yunus Ibn Maysara kua: ‘**Amesema Muadh Ibn Jabal kua: ‘Baada ya Mola wangu *Allah Subhanah wa Ta’ala* kukataza kuabudia Masanamu basi pia alikataza kunywa Pombe na kubishana na watu.’**

Amesema pia Imam Yunus Ibn Maysara kua: **‘Imeandikwa katika Lawh Al Mahfudh kua; ‘Kwa hakika mimi ndie Allah, hakuna Allah zaidi yangu mwingi wa Rehma na Mwingi wa Huruma, Huurma yangu inaizidi Hasira yangu na Usamehevu wangu unaizidi Adhabu zangu’**

IMAM AL QARI YAZID AL QA’QA

Imam Al Qari Yazid Ibn Al Qa’qa alikua pia akijulikana kama Imam Abu Jafar Al Makhzumi Al Madani Al Qari, Imam Al Madani alikua ni Mwanafunzi wa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* na pia Imam Abd Allah Ab Allah Al Ayyash Ibn Ab Rabiah.

Ambapo anasema Imam Al Jazari kua: **‘Imam Al Madani alikua ni mmoja kati ya Wasomaji 10 wa Qur’an wa kipindi cha Tabiina, yaani kipindi cha kizazi cha pili cha Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na alikua ni mwenye kukubalika sana na mwenye ari kubwa sana.’**

Na Imam Yahya Ibn Muin anasema kua: **‘Abu Jafar Al Madani alikua ni mmoja kati ya wenye Mamlaka ya kisomo cha Qur’an miongoni mwa watu wa Madina kwani kutokana na sababu hii basi ndio akawa anaitwa Al Qari’**

Imam Al Madani alikua pia si mwenye Ilm kubwa ya Hadith ingawa alisoma kwa Abu Hurayrah kwani alikua akivutiwa zaidi na Qur’an, lakini hata hivyo hadith zake zilikua ni sahih. Imam Al Madani alifariki mnamo mwaka 130 Al Hijra na kuacha Wanafunzi ambao waliendeleza Qiraa chake ambao ni Imam Isa Ibn Wardan Al Madani Al Hadhdha ambae alikua ni mtaalamu mkubwa sana wa Ilm ya Qiraa na alifariki mnamo mwaka 160 Al Hijra.

Mwanafunzi wake wa pili alikua ni Imam Sulayman Ibn Muslim Ibn Jammaz Abu Al Rabiah Al Zuhr ambae ni mwenye kutokana na uko wa Banu Zuhra wa Madina. Imam Ibn Jammaz alikua pia mtaalamu mkubwa wa Qiraa cha Qur’an ambapo nae alifariki mnamo mwaka 170 Al Hijra.

IMAM SAID IBN MUSAYYIB 15 AH

Imam Abu Muhamamd Said Ibn Al Musayyib Ibn Hazn Ibn Abi Wahb Ibn Amr Ibn Idd Ibn Imran Ibn Makhzum alizaliwa katika Mji wa Madina mnamo mwaka 15 Al Hijra, hiki kilikua ni kipindi cha mwanzoni mwa Utawala wa *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*

Imam Said Ibn Musayyib alikua ni Mwanazuoni mwenye Ilm kubwa sana kiasi ya kua alikua akijulikana pia kama *Imam At Tabiina* yaani Imamu wa Kizazi cha Tabiina, na bila ya shaka aliipata darja hii kutokana na kua alikua ni Mwanafunzi wa Sahaba Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* ambapo kutokana na kuelewana nae na kupendana nae Mwanafunzi wake huyo basi Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* alikua na binti yake ambae alikua ni Mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith na hivyo aliamua kumuozesha binti yake huyo kwa Said Ibn Musayyib.

Imam Said Ibn Musayyib alisoma pia kwa Masahaba kadhaa akiwemo Baba yake ambae ni Mzee Musaayib, Umar Ibn Al Khattab, Uthman Ibn Affan, Ali Ibn Abi Talib, Sa'd Bin Abi Waqqas, Hakeem Ibn Hizaam, Abd Allah Ibn 'Abbas, Abd Allah Ibn 'Umar, Abda Allah Ibn 'Amr Ibn Al 'Aas, Mu'ammar Ibn'Abdillah, Abu Dhar, Abu Darda, Hassan Ibn Thaabit, Zayd Ibn Thaabit, 'Abd Allah Ibn Zayd Al Mazani, 'Ataa Ibn Usayd, 'Uthman Ibn Abil 'Aas, Abu Tha'labah Al Khushany, Abu Qatadah, Abu Musa Al Ashari, Abu Sa'id, 'Aishah, Asma Bint 'Umays, Khawla Bint Hakim, Fatimah Bint Qais, Umm Sulaym, Umm Shurayk, *Radhi Allahu Anhum* na wengineo.

Ambapo anasema Imam Said Ibn Musayyib kua: '***Rasul Allah Salallahu Allahu Alayhi wa Salam* alimuuliza Babu yangu jina lake, ambapo Babu yangu akasema: 'Mimi naitwa Hazn' ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia Hazn kua: 'La wewe bora uwe Sahl' Lakini Babu yangu akasema: 'La, hakika mimi siwezi kubadilisha Jina nililopewa na Baba yangu, kwani kila mtu ananifahamu kutokana nalo'. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakaa kimya. Imam Said Ibn Musayyib anaendelea kusema kua 'Tangu siku hio Hazn haikuachana nasi.'***(Imam Bukhari)*

Tukio hili linatuonesha Umuhimu wa kuwachagulia Majina mazuri watoto wetu, kwani kwa njia moja au nyengine hua ni yenye kuwaathiri sana katika maisha yao. Kwani neno *Hazn* hua linamaanisha Ugumu au Huzuni na neno *Sahl* hua linamaanisha Wepesi.

Kwani amesema Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Katika siku ya Malipo Mtaitwa kwa Majina yenu na ya Mababa zenu hivyo Jipeni Majina Mazuri'***(Sunan Abu Daud)*

Naam..hapa kidogo nataka tufahamiane, ilitusije tukachanganya na ile hadith inayozungumzia kuhusiana na Talqini ya Abu Ummamah *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua, Mmoja wenu anapofariki basi wekeni sawa Udongo (baada ya Kumzika) na kisha mmoja wenu asimame kwenye upande wa Kichwani kwake na aseme: 'Ewe Fulani Bnu Fulani'' (Kwa kutumia Jina la Mtu kisha Jina la Mama yake badala ya Jina la Baba yake)** *(Imam At Tabrani)*

Ambapo Hadith hizi mbili zinaonesha kua Kaburini hua ni kwa Jina la Mama lakini tukifufuliwa hua kwa Jina la Baba na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Bendera Itawekwa Katika siku ya Malipo kwa Kila Msaliti na kisha Itatangaziwa mbele ya kila mtu kua: Huu ni Usaliti wa Fulani Ibn Fulani Ibn Fulani** *(Sahih Bukhari)*

Ambapo Mtu atakaeitwa Katika siku ya Kiama akiwa na Jina baya basi atakua ni mwenye kujisikia vibaya sana kwani amenyimwa haki yake na hivyo atamtafuta Baba yake na kisha atamuuliza Baba yake: **'Ewe Baba yangu, hakika mimi *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliniumba nikiwa Muislam, hivyo kwanini wewe Ukanichagulia mimi Jina Baya?'**

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Moja kati ya Haki ya Mtoto kwa Mzee wake ni Kupewa Jina Zuri na Ilm.'**

Na akasema Imam Malik Ibn Anas katika Kitabu chake cha Al Muwwata kua: **'Umar Ubn Al Khattab R*adhi Allahu Anhu* alimwita Mtu mmoja na kisha akamuuliza Jina lake ambapo mtu huyo akasema kua anaitwa Jamara yaani Mwenge wa Moto**

Akamuuliza Jina la Baba yake nae akasema Shihab (yaani Nyota Inayotembea Angani na kuunguza kila kitu ikutanayo) Na kisha akamuuliza Ukoo wake ambapo nae akasema Hurqah yaani Moto Unaowaka Ripu ripu, Na kisha akamuuliza Unatoka maeneo gani ambapo nae akasema Hutamah yaani Moto wa Jahannam

Hivyo Umar akasema Kimbilia Nyumbani kwani Watu wako wanaungua Moto, hivyo Mtu huyo akakimbilia Nyumbani kwao na alipofika akakuta kama alivyosema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* yaani Familia yake yote imeteketea kwa Moto.'

Ambapo kwa upande wa Imam An Nawawi basi nae pia anasema katika Riyadh Al Salihina kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anatafuta watu wa Kumkamua Ngamia Maziwa kwa ajili ya kutoa Sadaqah, hivyo akaomba Mtu wa kujitolea kwa ajili ya kumkamua Maziwa Ngamia huyo.'**

Hivyo katika watu waliokuwepo mbele yake Miongoni mwa Masahaba basi akanyanyuka Mmoja kwa ajili ya kujitolea kumkamua Ngamia na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: 'Jina lako nani?' Mtu huyo akasema Murrah (Ladha Chungu) hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia: 'Kaa Kitako'

Akanyanyuka wa pili na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: 'Jina Lako Nani?' Nae akasema : 'Harb (Vita)'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kaa Chini'**

Akanyanyuka Mtu wa tatu ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: 'Jina lako nani?' Nae akasema: 'Yaish(Anaeishi Maisha Marefu)'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Nenda Kamkame Maziwa Ngamia'

Naam..hivi ni baadhi tu ya Vithibitisho ambavyo vinatuonesha umuhimu wa kupeana Majina Mazuri, kutokana na yanavyokua na uwezo wa Kutuathiri kimaisha, kiasi ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akichagua watu kulingana na Majina yao hadi katika utekelezwaji wa Mambo maalum.

Hivyo tunarudi kwa Imam Sayid Ibn Musayyib ambapo tunaona kua alikua ni kijana aliekua akipenda kutafuta Ilm kiasi ya kua alikua anatembea kwa masiku na masiku kwa miguu kwa ajili ya kutafuta I'lm ya hadith moja tu, ambapo baada ya kuipata basi alikua ni mwenye kutoa Fatwa wakati wa Masahaba, na Imam Makhul anasema kuhusiana na Said Ibn Musayyib kua: '**Imam Said Ibn Musayyib alikua ni Mwanazuoni wa Wanazuoni.**'

Ambapo anasema Maymun Ibn Mihran kua: '**Baada ya kukutana na Abd Allah Ibn Abbas, Abu Hurayrah, basi Umar Ibn Abd Al Aziz hakuwa ni mwenye kutatua kesi yeyote bila ya kuwasiliana na Said Ibn Musayyib.**'

Ama kuhusiana na Sala ya Jamaa basi ilikua haiwahi kutokea kua itaadhiniwa Adhana ya Sala kabla ya Imam Said Ibn Musayyib kuwepo Msikitini na hii si kwa sababu labda Muadhini alikua anamsubiri Imam Said Ibn Musayyib ndio aadhini la, bali Imam Said Ibn Musayyib alikua na kawaida ya kufika Msikitini mapema sana hata mda wa Adhana bado haujaingia. Na kila siku alikua akisali katika Safu ya Mwanzo.

Alisema Imam Said Ibn Musayyib kua: '**Hakika mimi sijawahi kukosa Takbir ya mwanzo ya Sala ya Jamaa hata mara moja kwa mda wa miaka 50, na sijawahi**

kusali nikaona nyayo za Mtu mbele yangu kwa miaka 50’ Imam Said Ibn Musayyib aliwahi kufanya Ibada ya Hija kwa mda wa miaka 40 mfululizo.

Ambapo anasema Kathir Ibn Mutallib kua: ‘**Mimi nilikua nikihudhuria darsa ya Said Ibn Musayyib kwa mda mrefu, na hivyo ikatoea kuna kipindi ikawa nimesita kuhudhuria darsa zake. Hivyo niliporudi basi akaniuliza: ‘Ulikuwepo wapi?’ nami nikamwambia: ‘Mke wangu alifarikia Dunia hivyo nilikua nimeshughulika katika kushughulikia maziko yake’ hivyo nae akaniuliza: ‘Kwanini hukututaarifu? Tungehudhuria maziko yake’’**

Kisha Said Ibn Musayib akaniuliza: ‘Hivi Jee umetambulishwa na Mwanamke mwengine?’ nami nikasema: ‘*Yarhamak* (Allah akuingize kwenye Rehma zake) jee ni nani atakaekubali kuniozesha wakati mimi sina ninachokimiliki isipokua Dirham 2 au 3 tu.’ Said Ibn Musayyib akasema: ‘Mimi.’ Nami nikamuuliza: ‘Kweli wewe utakubali hivyo?’ nae akasema : ‘Naam.’ Kisha baada ya hapo akamshukuru *Allah Subhanah wa Ta’ala* na Kumtukuza na akamsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kuniozesha Binti yake kwa Dirham 2 au 3.’

Baada ya hapo mimi nikasali Sala ya Maghrib na nikaondoka kueleeka Nyumbani kwangu, kwani nilikua nimefunga, nikatayarisha Iftar yangu ambayo ilikua ni Mkate na Samli., na mara nikasikia Mlango unagongwa, nami nikauliza: ‘Nani?’ na nikajibiwa: ‘Said’ nikaanza kujiuliza ni Said gani? Kwani kwa miaka 40 Said Ibn Musayyib alikua si Mtu wa kutoka Nyumbani kwake kuenda sehemu nyengine yeyote isipokua Msikitini.

Hivyo nikafungua Mlango na nikamuona Said Ibn Musayyib nami nikamuuliza: ‘Kwanini hukumtuma Mtu akanifuata ili mimi nije kukufuata wewe?’ nae akasema: ‘Kwa sababu wewe una haki zaid ya kua mimi nikifuate wewe’ hivyo nami nikamuuliza: ‘Kwani kuna nini?’ nae akajibu: ‘Wewe Ulikua ni mjane, nami nikakuozesha (kwa binti yangu) hivyo sipendi kua uutumie usiku huu huku ukiwa uko peke yako. Nimekuletea huyu hapa mke wako.’

Binti yake alikua amesimama nyuma yake nami sikumuona kutokana na urefu wa Said Ibn Musayyib, hivyo akamkamata na kumuingiza ndani ya Mlango wa Nyumba yangu, ambapo nae alikua amekaa kimya kutokana na heshima na kuona haya.

Hivyo mimi nikaweka bakuli la Samli na Mkate pembeni ya Taa ili aweze kuona, na kisha nikapanda juu ya paa na nikawaita Majirani na kuwataarifu kuhusiana na Ndoa yangu, habari ambayo ilimfikia Mama yangu ambapo nae akaja kutokana nayo, na kuniambia kua: ‘uso wangu ni haramu kwa uso wako (yaani sitozungumza na wewe) kwa mda wa siku 3’ ili amtayarishe bi harusi kwa ajili

kusherekea harusi ndani ya siku hizo 3, kabla ya mimi kua nae, hivyo nikasubiri zikapita siku 3 kisha nikaenda kwa Mama yangu. Kwa hakika Binti yake Said Ibn Musayyib alikua Mwanamke mzuri sana kuliko wote, alikua ni mwenye kukijua vizuri sana Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na haki za Mume.'

Imam Said Ibn Al Musayyib alikua pia ni mwenye Ilm ya kutafsiri Ndoto na ni mwenye busara na hikma nyingi sana, kwani alisema kua: '**Hakuna Wema kwa Mtu ambae asietaka kukusanya Mali kutokana na kipato chake cha halali, na akatimiza haki zake mali hio na hivyo kua ni mwenye kujizuia kutokana na kuomba.'**

Anasema Ibn Hurmullah kua: **'Nilimuuliza mimi Mfanyakazi wa Said: 'Hivi Jee Said alikua kisali vipi Nyumbani kwake?' ambapo nae akajibu kwa kusema: 'Sijui ila alikua akisali sana na alikua akisoma *Surat Sad* mara nyingi sana.'**

Wanasema Wanazuoni kua mwenye kusoma *Surat Sad* hua ni mwenye kupata Malipo sawia na uzito wa malipo ya Mlima ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliudhalilisha kwa Nabii Musa. Na atakaesoma katika usiku wa siku ya Ijumaa basi atapata malipo Mema ya kwake yeye na familia yake ndani ya nyumba yake hapa Duniani na kesho Akhera kua ni mwenye Kasri kubwa sana kama malipo yake na familia yake kutokana nayo.

Ama kuhusiana na Ilm ya Imam Said Ibn Musayyib basi anasema Imam Makhul kua: **'Hakika mimi ilisafiri sana kwa ajili ya kutafuta Ilm lakini kamwe sijawahi kuonana na mtu mwenye kua na Ilm kubwa kama Said Ibn Musayyib.'**

Na akasema pia Ali Ibn Al Madani kua: **'Hakika mimi sijawahi kuona Mtu mwenye Ilm miongoni mwa Tabiina kama Said Ibn Musayyib, kwani yeye yuko juu sana miongoni mwa Tabiina.'**

Imam Abu Hatim nae amesema kua: **'Hakuna miongoni mwa Tabiina mwenye hikma kama Sadi Ibn Musayyib na mwenye msingi imara wa Sanad kutoka kwa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kama yeye.'**

Na anasema Imam Maymun Ibn Mihran kua: '**Mimi nilienda kwenye Mji wa Madina na kuuliza kuna mtu gani ambae ni mwenye Ilm kubwa zaidi ya Fiqh nami nikaelekezwa kwa Said Ibn Musayyib, hivyo nikaelekea kwake na kumuuliza niliyotaka kumuuliza.'**

Ambapo anasema Imam At Tabari kua: **'Alisema Yazid Ibn Abi Yazid: 'Sisi tulikua tukimuuliza Said Ibn Musayyib kuhusiana na vilivyo Halali na Haramu, na alikua ni mwenye Ilm kubwa zaid kuhusiana navyo miongoni mwa watu, na tulipokua**

tukimuuliza kuhusiana na tafsiri ya aya za Qur'an basi alikua akisema: 'Msiniulize mimi kuhusiana na aya za Quran, bali muulizeni yule anaedai kua hakuna kilichofichikana kwake kutokana nayo' yaani akimaanisha Ikrimah ambae ni Mwanafunzi wa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allau Anhu''*

Ambapo kwa upande wa Imam Az Zuhri basi anasema kua: '**Hakika mimi nilikua nikitafuta Ilm kutoka kwa watu watatu: Kwa Said Ibn Musayyib ambae ni mwenye Ilm kubwa zaidi ya Fiqh, Urwa Ibn Az Zubayr ambae ni mwenye kina kisichokua na Mwisho wa Ilm na kama utataka kupata Ilm ambayo hakuna aliekua nayo basi utaipata kwa Ubaydullah.**'

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Nuaym basi anasema kuhusiana na Said Ibn Musayyib kua: '**Said Ibn Musayyib alikua ni Sahib wa kufanya Ibadah na wa Sala ya Jamaah, alikua ni mcha Mungu na ni mwenye Kukinai Nafsi yake na alikua ni mwenye kushikamana na Jina lake katika kufanya Ibada zake kwani alikua ni mwenye *Ibada Saiid* yaani mwenye kufanya Ibada Inayofurahisha na alikua ni mwenye kukaa mbali na Maovu.'**

Alisema Imam Said Ibn Musayyib kua: **'Kwangu mimi kutoka na kuenda Msikitini kwa ajili ya Sala ya Ijumaa ni bora kuliko Kuenda katika Ibada ya Hija.'**

Imam Said Ibn Musayyib alifariki mnamo mwaka 94 Al Hijra.

IMAM UBAYD ALLAH IBN ABD ALLAH 16 AH

Ubaydullah Ibn Abd Allah Ibn Utba Ibn Masud alizaliwa katika kipindi cha Utawala wa *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* katika mji wa Madina na bila ya shaka alitoka katika familia ya watu wenye Ilm na kukulia kwenye mazingira yaliyojaa Nuru ya Ilm ya Dini ya Kislam kwani hata kaka yake nae alikua ni Mwanazuoni wa Hadith ambae alikua akiitwa Awn Ibn Abd Allah Ibn Utba ambae alikua pia ni Mjukuu wa Utbah Ibn Masud R*adhi Allahu Anhu* ambae pia ni kaka wa Sahaba Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*.

Imam Ubaydullah Ibn Abd Allah Ibn Utba alikua ni Mwanafunzi wa Masahaba wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam ambapo miongoni mwao ni Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Aisha *Radhi Allahu Anha*, Umm Salamah *Radhi Allahu Anha*, Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*, n.k hivyo alikua ni Mtu ambae ni mwenye Ilm kubwa sana ya Qur'an, Hadith, Fiqh, na Lugha pia, na pia alikua ni Mwalimu wa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Aziz *Radhi Allahu Anhu.*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ubayd Allah alikua ni Imam ambae ni mtulivu katika kila jambo lake hata ndani ya Ibada zake kiasi ya kua siku moja Imam Zayn Al Abidin alimfuata wakati akiwa anasali na hivyo akakaa kwa mda mrefu akiwa anamsubiri amalize kusali.

Ambapo anasema Imam Ubayd Allah kuhusiana na Ilm ya Hadith kua: **'Mimi sijawahi kufuatili kuisikia Hadith isipokua kwa ajili ya kutaka kuifaham Undani wake.'**

Na akasema Imam Ibn Malik kua: **'Mimi nilidhani kua tayari nimeshakua na Ilm hadi pale nilipokaa na Ubayd Allah Ibn Abd Allah Ibn Utbah Ibn Masud.'**

Imam Ibn Hibban anasema kua: **'Imam Ubayd Allah Ibn Abd Allah Ibn Masud alikua ni Bwana wa Tabiina.'**

Imam Abu Jafar Al Tabari anasema kuhusiana na Imam Ubayd Allah kua: **'Alikua ni mwenye kujitolea kuhusiana na Ilm, ni mtaalamu mahiri kuhusiana Hukmu, kuhusiana na yaliyo halali na haram na alikua ni mtaalamu kubwa wa Mashairi.'**

Imam Ibn Abd Al Barr anasema kua: **'Imam Ubayd Allah alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni 10 kati ya Wanazuoni 7 ambao Fatwa zao zinakubalika na kutumika sana, alikua ni Imam Mcha Mungu, Mwenye Ilm kubwa ya Fiqh na Lugha na mwenye kunufaisha.'**

Amir ul Muuminin Umar Ibn Abd Al Aziz alisema: **'Hakika kwangu mimi kua kwenye mkusanyiko wa Wanazuoni ni vizuri zaidi kuliko kua na Umiliki wa Dunia nzima. Na Wallahi kama ningekua na uwezo ningenunua usiku mmoja wa Ubayd Allah Ibn Abd Allah kwa Dinar 1000 kutoka kwenye *Bayt ul Maal.'***

Imam Al Waqidhi amesema kua: **'Imam Ubayd Allah Ibn Abd Allah ni Mwanazuoni Muaminifu, Mwanafiqh mwenye Ilm ya Hadith kubwa sana na Lugha na alikua si mwenye kuona vizuri mwishoni mwa Uhai wake.'**

Na Imam Al Zuhri akasema: **'Hakika mimi sijawahi kukaa na Mwanazuoni kutokana na kutaka kujua kile alichokua nacho bila ya kubishana nae, na nilikua nikibishana na Urwa Ibn Az Zubayr hadi pale nilipokutana na Ubayd Allah ambae sikuwahi kubishana nae kwa sababu alikua ana Ilm kubwa sana, kwani yeye ni Bahari ya Ilm.'**

Imam Ubad Allah Ibn Abd Allah alifariki mnamo mwaka 98 Al Hijra.

IMAM ABU BAKR IBN ABD RAHMAN 16 AH

Imam Abu Bakr Ibn Abd Rahman Ibn Harith Ibn Hisham Ibn Mughirah Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Makhzum alizaliwa mnamo mwaka 16 Al Hijra na alikua ni Imam mwenye Ilm kubwa sana ya Qur'an, Fiqh na Hadith na alikua ni mcha Mungu sana kiasi ya kua alikua akijulikana pia kwa jina la Mtawa wa Quraysh kutoka na kudumu kwake sana kwenye Ibada, kwa upande wa Ilm yake basi alisoma kutoka kwa Masahaba wakiwemo *Umm ul Muuminin* Aisha na *Umm ul Muuminin Umm* Salamah, Amar Ibn Yasir, Abu Hurayrah, Asma Bint Umays, Marwan Ibn Al Hakam na wengineo *Radhi Allahu Anhum.*

Babu yake Imam Abu Bakr Ibn Abd Rahman alikua ni Sahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alisilimu katika siku ya Ufunguzi wa Mji wa Makkah, na kisha baada ya hapo akaelekea katika ardhi ya Syria na kupigana chini ya Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu* na akapata ushahidi katika vita vya Yarmouk.

Miongoni mwa Wanafunzi wake ni watoto wake wawili Abd Allah, Abd Al Malik, Mujahid, Umar Ibn Abd Al Aziz, Amr Ash Sha`bi, Irak Ibn Malik, Amr Ibn Dinar, Imam Al Zuhri, Abd Rabb Ibn Said, Ikrimah Ibn Khalid, na wengine.

Ambapo anasema Imam Al Waqidhi kua: '**Jina lake Abu Bakr, na alikua ni Kipofu, alikua ni *Thiqah*, Mwanafiqh na Mwanazuoni mwenye ukarimu mkubwa sana na mwenye ilm kubwa ya Hadith.**'

Na amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: '**Mimi nilikua natamani kua ningekua na Watoto 10 kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wote wakiwa kama Abu Bakr Ibn Abd Al Rahman.**'

Kwa upande wa Imam Ibn Kharash basi yeye anasema kua: '**Imam Abu Bakr Ibn Abd Rahman ni Imam wa Waislam na ni ndugu wa Waislam pia.'**

Imam Adh Dhahabi amesema kua: '**Imam Abu Bakr ni Mkusanyiko wa Ilm, Heshima na Jitihada na alikua ni miongoni mwa waliomrithi Baba yake kwa kuheshimika.**'

Imam Abu Bakr Ibn Abd Rahman alikua ni miongoni mwa Wanazuoni 7 waliokua juu katika kizazi cha Tabiina cha watu wa Madina na alifariki mnamo mwaka 94 Al Hijr.

IMAM MUJAHID IBN JABR 21 AH

Imam Mujahid Ibn Jabar Al Makki alizaliwa mnamo mwaka wa 21 Al Hijr katika Mji wa Makkah alikua ni Mwanafunzi wa *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na alikua ni Mtumwa wa Abd Allah Ibn Saib Ibn Abi Saib Al Makhzumi.

Imam Mujahid Ibn Jabar alikua ni mtaalamu mkubwa wa Tafsir ya Qur'an na Hadith na alikua ni Mwanazuoni wa mwazo miongoni mwa Tabiina kua ni mwenye kuandika Tafsir ya Qur'an, ambapo alisema kua: '**Hairuhusiki kwa mtu mwenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* na siku ya Malipo kuzungumzia kuhusiana na Qur'an bila ya kua na ufahamu wa Lugha ya Kiarabu cha asili.**'

Imam Mujahid Ibn Jabr hakusoma tu kwa Sahabah Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* lakini pia alisoma kwa *Baab Al Ilm Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Saad Ibn Abi Waqqas Radhi Allahu Anhu, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu, Umm ul Muuminin* Aisha Radhi Allahu Anha n.k na bila ya shaka alikua ni Mwanafunzi ambae ni mwenye uchu na hamu kubwa ya kutaka kujua kwani alikua yuko tayari kufanya kila kitu kwa ajili tu ya kutaka kujua hata kwa ajili ya kupata maana halisi ya Aya moja tu ya Qur'an na hivyo alikua ni mtu mwenye kufunga safari kwa ajili ya kufuatilia Ilm hio.

Ambapo anasema Imam Ibn Saad katika Tabaqat yake kua: **'Mujahid alirudia Tafsir ya Qur'an kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* mara 30'** na ndio maana akasema Imam Sufyan Ath Thawry kua: **'Kama Ukipata Tafsir ya Mujahid basi itakutosheleza kabisa.'**

Kwani Tafsir ya Imam Mujahid ni yenye kuzunguka kwenye kumjumuisho wa Kanuni nne zifuatazo:

Tafsir ya aya kwa kutumia aya nyengine - kama kwenye mfano ufuatao:

﴿وَلَيَحْمِلُنَّ أَثْقَالَهُمْ وَأَثْقَالاً مَّعَ أَثْقَالِهِمْ وَلَيُسْأَلُنَّ يَوْمَ ٱلْقِيَامَةِ عَمَّا كَانُواْ يَفْتَرُونَ﴾

Walayahmilunna athqalahum waathqalan maAAa athqalihim walayus-alunna yawma alqiyamati AAamma kanoo yaftaroona *(Surat Al Anqabut 29:13)*

Tafsir: ***Na kwa hakika watabeba uzito wa Mizigo yao wenyewe na uzito wa mizigo ya myengine baada ya uzito wa mizigo yao, na bila ya shaka wataulizwa katika siku ya Malipo kuhusiana na kile walichokua wakikizusha.***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambayo ni aya iliyotafsiriwa na Imam Mujahid kwa aya isemayo:

﴿لِيَحۡمِلُوٓاْ أَوۡزَارَهُمۡ كَامِلَةٗ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ وَمِنۡ أَوۡزَارِ ٱلَّذِينَ يُضِلُّونَهُم بِغَيۡرِ عِلۡمٍۗ أَلَا سَآءَ مَا يَزِرُونَ﴾

Liyahmiloo awzarahum kamilatan yawma alqiyamati wamin awzari alladheena yudhilloonahum bighayri AAilmin ala saa ma yaziroona *(Surat An Nahl 16:25)*

Tafsir: ***Watabeba uzito wa Mizigo yao katika siku ya Malipo na Uzito wa Mizigo ya wale waliowapotosha kwa kutojua kwao, kwa hakika huu ni uzito Mzito sana watakaobeba.***

Tafsir kulingana na Sunnah na Hadith.
Tafsir kwa kutumia Ufahamu.
Tafsir kwa kutumia Ilm ya Kusoma.

Ambapo anasema Imam Ibn Is-haq kua: '**Amesema Mujahid kua: 'Mimi nilimpa Ibn Abbas Msahafu mara tatu kuanzia mwanzo hadi mwisho, na nikamuomba kusimama katika kila aya kwa ajili ya ufafanuzi juu yake.'**'

Ambapo Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal ni wenye kuitegemea sana Tafsir ya Imam Mujahid katika vitabu vyake na Imam Bukhari pia, ambapo kwa upande wa Imam Adh Dhahabi basi yeye anasema kua: **'Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na Uongozi wa Mujahid na Wanazuoni wote wa Hadith wamemnukuu Hadithi zake.'**

Imam Qatadah Al Sadusi amesema kuhusiana na Imam Mujahid kua: **'Katika watu waliokua hai basi mwenye Ilm kubwa ya Qur'an ni Mujahid.' Ambapo Imam Ibn Jurayj amesema kua: 'Kusoma na kujifunza Hadith kutoka kwa Mujahid ni bora kwangu mimi kuliko Familia yangu yote na kua na Utajiri'**

Na Imam Al Amash akasema: **'Mimi nilikua nikifikiria kua Mujahid ni mtu asiejua kitu pale nilipomuona namna alivyoovyaa nguo za kawaida, nilidhani kua ni mchunga Punda aliepoteza Punda wake na hivyo amechanganyikiwa kutokana na jambo hilo, lakini anapozungumza kuhusiana na Mitizamo ya I'lm basi alikua ni kama mwenye kutema Almasi kutoka mdomoni mwake.'**

Hamid Ibn Araja amesema kua: **'Mujahid alikua ni mwenye kusema *Allahu Akbar* kila baada ya kumaliza kusoma Sura kuanzia *Surat Al Dhuha* hadi mwisho wa Qur'an'**

Miongoni mwa Wanafunzi wake Imam Mujahid Ibn Jabr ni pamoja na Imam Qatadah Al Sadusi, Imam Amash, Imam Amr Ibn Dinar, Mansur Ibn Ayyub n.k.

Ambapo ingawa hakuna Tafsir ya Asili ya Imam Mujahid Ibn Jabr sasa hivi lakini kuna Tafsir yenye jina lake ambayo ni Tafsir yenye Kauli na Mitizamo yake ndani yake.

Amesema Imam Adh Dhahabi kua: **'Mujahid ni Shaykh wa Wasomaji Qur'an na Wafasiri.'**

Amesema Imam Mujahid kua:

'Sisi tulikua tukitafuta Ilm ambayo hata hivyo tulikua hatuna nia yeyote ndani yake, kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akatutilia Nia ndani yake.'

'Na sijui ni ipi neema bora zaidi aliyonijaalia mie *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua kama ni kuniongoza mimi na kuingia kwenye Uislam au kuniokoa mimi kutokana na Matamanio ya Nafsi yangu.'

'Hakuna hata Muumini mmoja anaefariki bila ya kua ni mwenye kuliliwa na ardhi kwa siku 40'

'Hata kama mtu atatumia Mali yake yenye ukubwa kama wa Mlima wa Uhud kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi bado mtu huyo hawezekani kua ni miongoni mwa wenye kufanya Israfu.'

'Hakuna mtu hata mmoja anaefariki bila ya kuwasilishwa Roho yake mbele ya watu wake, hivyo kama yeye alikua ni mtu *Dhikr Allah* basi atawasilishwa mbele ya watu wa *Dhikr Allah* na kama alikua ni mtu wa Matamanio ya Kidunia basi huwasilishwa mbele ya watu wa Matamanio ya Kidunia.'

'Ibilis alisema kua: 'Kama Ibn Adam hatoweza kunisaidia mie basi hatoweza kunisaidia katika mambo matatu: Kuchukua Mali isiyokua yake; Kufanya Israfu juu ya kile kisichokua chake; Na Kumzuilia Mwenzake kutokana na kupata haki yake.''

'Kama Mja atamgeukia Mola wake kwa Moyo wake wote, basi Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* nae atamgeuzia Nyoyo za Waumini zote katika upande wake Mja wake huyo.'

‘Ardhi imejaaliwa kwa ajili ya Malaika wa Mauti kua kama ni Bakuli, na hivyo hutoa ndani yake chochocte kile akitakacho, na imejaaliwa hivyo kwa ajili ya kumsaidia Malaika wa mauti kukamata akitakacho.’

‘Yeyote yule asiekua na haya kuhusiana na uhalali wa riziki yake basi riziki yake itakua na urahisi sana kupatikana.’

‘Mwanazuoni ni yule ambae ni mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa wingi hata kama ilm yake ni ndogo na Mjinga ni yule asiemuogopa A*llah Subhanah wa Ta’ala* hata kama Ilm yake ni kubwa.’

‘Bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta’ala* hurahisishia mtoto na mtoto wa mtoto wa Mja mwema kutoka na Uja wema mwema wa Mja wake.’

‘Mimi nilifuatana na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kwa Khirbet, nae akaniambia: ‘Ewe Mujahid familia yako imefanya yepi? Na wako wapi wazee wako?’ Nami nikaitikia kwa kusema: ‘Wazee wangu wametangulia kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala*’, ambapo nae akajibu: ‘Wazee wametangulia, na amali zao zimebakia.’’’

‘Mimi nilifuatana na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* ambapo nilitaka kumtumikia Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* lakini yeye akanitumikia mimi.’

‘Mwenye Busara miongoni mwa watu ni yule ambae ni mwenye kukumbuka madhambi yake anapokua peke yake na kisha akaomba msamaha kwa Mola wake.’

Imam Sufyan Ath Thawry amesema kua: **‘Soma Tafsir kutoka kwa watu wanne: ‘Mujahid, Said Ibn Jubayr, Ikrimah na Ad Dahaq.’’** ambapo Imam Qatadah amesema kua: **‘M-bora mwenye kujua zaidi kuhusiana na Tafsir ya Quran miongoni mwa waliobakia ni Mujahid.’**

Imam Mujahid amesema kua: **‘Kuna mambo mawili ambayo kama Mtu atajizuia nayo basi funga yake itakua Salama, ambayo ni Kusengenya na kusema uongo’**

Alisema Imam Mujahid kua: **‘Inakirihisha kwa Mtu kumuangalia mwenzake kwa kumtolea Macho wakati anaposimama baada ya kukaa kwake au kumuuliza wapi alipokua hapo kabla baada ya kuwasili kwake.’**

Imam Mujahid Ibn Jabr alifariki mnamo mwaka 104 Al Hijr katika Mji wa Makkah huku akiwa katika Sala katika hali ya Kusjudu akiwa na Umri wa miaka 83.

IMAM AMR ASH SHABI 21 AH

Imam Amr Ibn Abd Allah Ibn Sharahil Ibn Abd Allah Al Shabi alizaliwa mnamo mwaka 21 Al Hijra katika Mji wa Kufah nchini Iraq. Imam Amr Ash Shabi alizaliwa akiwa na pacha wake aitwae Al Layth Ash Shabi. Ambapo Imam Amr Ash Shabi alikua ni kijana alietofautiana na pacha wake kwa kua na ndevu nyingi sana, alikua mwenye mwili mwembamba na mwenye ngozi ya rangi inayokaribia kwenye wekundu kuliko weupe.

Tunapozungumzia kuhusiana na Ilm yake basi Imam Amr Ash Shabi alikua ni Mwanafunzi ambae ni mwenye ufahamu wa kuhifadhi mzuri sana kiasi ya kua yeye mwenyewe alikua ni mwenye kusema kua: '**Sikuwahi mimi kuandika kitu kwenye Kartasi hadi hii hii leo na wala haikuwahi kutokea kua kuna mtu ambae amenihadithia Hadith bila ya mimi kua si mwenye kuihifadhi hadithi hio na wala si mwenye kutaka kua irudiwe tena kwa ajili yangu mie.**'

Ambapo anasema Ahmad Ibn Abd Allah Al Ajly kua: '**Ash Shabi amenukuu Hadith kutoka kwa Masahaba 48 wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na Hadith zake ni Sahih, kwani hakunukuu isipokua Hadith Sahih.**'

Kutokana na kua na aina hio ya Ufahamu huo na jitihada zake basi Imam Amr Ash Shabi alijaaliwa kua na I'lm kubwa sana kwani alisoma kwa Masahaba wakubwa Wanazuoni akiwemo Amir ul Muuminin Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu, Umm Ul Muuminin* Aisha *Radhi Allahu Anha,*Saad Ibn Abi Waqqas *Radhi Allahu Anhu,* Zayd Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu,* Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu,* Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu,* Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu,* Zayd Ibn Arqam *Radhi Allahu Anhu,* Mughira Ibn Shubah *Radhi Allahu Anhu, n.k.*

Na hivyo haishangazi kuona kua anasema Asim Ibn Sulayman kua: '**Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu mwenye Ilm kubwa ya Hadith miongoni mwa watu wa Kufa, Basra, Hijaz na kwengineko kama Ash Shabi.**'

Na Imam Az Zuhri alisema: '**Wanazuoni wako wanne, Said Ibn Musayyib wa Madina, Amr Ash Shabi wa Kufah, Hasan Al Basr wa Basra na Makhul wa Sham.'**

Na Ash'as Ibn Siwar alisema: **'Hasan Al Basr alisema na kutubainishia sisi kuhusiana na Ash Shabi pale aliposema: 'Wa Allahi Ash Shabi ana Ilm kubwa sana.''**

Abi Usama alisema pia kua: '**Umar Ibn Al Khattab alikua ni kiongozi wa watu katika Wakati wake, kisha baada yake akafuatia Abd Allah Ibn Abbas, kisha akafuatia Amr Ash Shabi na kisha Sufyan At Thawry.**'

Na akasema Imam Sulayman At Taymi: **'Amesema Abu Miljaz kua: 'Hakika mimi sijawahi kuona Mtu mwenye Ilm zaidi kuliko Ash Shabi, kwani si Said Ibn Musayyib, si Tawus, si Ataa, si Hasan Al Basr na wala si Muhammad Ibn Sirin anaemkuta, kwani mimi nimekutana na wote hao.''**

Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi anatuelezea kuhusiana na Mwanafunzi wa Imam Malik ambae alikua mwanazuoni kutokana na kukutana kwake na Imam Ash Shabi katika eneo ambalo linaelezewa kwa kusema kua: '**Katika kipindi cha wakati wa Imam Ash Shabi kulikua kuna Mlevi mmoja ambae alikua hawezi kuacha Ulevi kabisa na alikua akiitwa Abd Allah Ibn Masalamah Al Qanabi**.

Safari moja Al Qanabi alikua amekaa na marafiki zake akinywa ulevi na mara mbele yake akaona zogo na tafrani, linalotokana na watu wengi kua ni wenye kumzonga mtu mmoja ambae alikua amepanda juu ya Punda wake, hivyo Al Qanabi akataka kujua imekuaje? Na huyo mtu ndie nani hivyo akajiuliza Moyoni mwake kwa kusema: 'Kwanini watu wote wale wanamzonga yule mtu mmoja'.

Hivyo akachukua chupa yake ya ulevi na kuelekea kwenye zogo hilo la watu na kuuliza : 'Huyu Mtu ndie nani?' ambapo nae akajibiwa kua: 'Huyu ni Imam Maarufu' nae akauliza: 'Anaitwa nani?' Akaambiwa kua: 'Anaitwa Imam Ashabi' Al Qanabi akauliza: 'Jee anafanya Jambo gani?' na akajibiwa kua : 'Ni Mwanazuoni wa Hadithi.'

Al Qanabi akauliza: 'Mwanazuoni wa Hadithi ndio anafanya nini?' akajibiwa kua: 'Mwanazuoni wa Hadithi hua ni mtu mwenye Ilm ya Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae hua amezihifadhi, anazisomesha na pia anazifanyia kazi kwa vitendo.'

Hivyo baadae Al Qanabi akamfuata Imam Ash Shabi ambae alikua amekaa juu ya Punda wake na kumwambia: 'Kama wewe kweli ni Mwanahadith basi nihadithie japo hadithi Moja.'

Kutokana na Hikma na Busara zake basi Imam Ash Shabi akamuangalia Al Qanabi ambae alikua na chupa yake ya Ulevi Mkononi, akatafakkari na akajua kua atumie hadithi gani kulingana na hali aliyokua nayo Al Qanabi, hivyo akamwambia Al Qanabi: 'Amesema Abda Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Alla Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua: 'Miongoni mwa Kauli za

Mitume waliotangulia ambayo inatumika ni ule usemao 'Kama huna Haya basi fanya unalotaka.'

Baada ya kusikia Hadith hio basi vidole vya Al Qanabi vikaangusha chini Chupa ya Ulevi aliyokua nayo mkononi, kutokana na kujiuliza: 'Hivi Jee mimi ni mtu nisie ona Haya?' kwani hadithi hio ilikua ni yenye kumgusa sana Moyoni mwake, na hivyo akaondoka na kuenda nyumbani kwake na kujifungia chumbani mwake akaanza kulia huku akajiuliza tena: 'Hivi nnafanya nini mimi hadi sasa na maisha yangu haya? Kwanini nnaendelea Kunywa Ulevi na kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala*?'

Hivyo Al Qanabi akaamua kurudi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kufanya toba. Akatoka chumbani mwake na kumwambia mama yake kua: '**Hakika mimi nnahama kutoka katika ardhi ya nchi hii, nnaenda kuwaambia Wanazuoni na Maulamaa kua nataka kutafuta Ilm ya Dini ya Uislam, na mimi nataka niwe kama Imam Ash Shabi, ambae ni Mwanazuoni wa Hadith, hivi kwanini mimi si Mwanahadithi? Kama Imam Ash Shabi, kama Imam Ash Shabi anaweza kua Mwanazuoni basi na mimi pia nnaweza kua Mwanazuoni**.'

Hivyo Al Qanabi akawauliza Wanazuoni wa eneo lake na akaambiwa kua: '**Nenda kartika Darsa ya Imam Malik, kwani yeye ndie Imam mkubwa miongoni mwetu, hivyo ukiwa Mwanafunzi wake basi utakua na uwezo wa kua Mwanazuoni wa Hadith.**'

Hivyo Al Qanabi akafunga safari kutoka Basra akaelekea kwenye Mji wa Madina kwa Imam Malik na akaanza kusoma chini yake hadi akafanikiwa kua ni miongoni mwa Wanafunzi wakubwa wa Imam Malik, na alisoma kwake kwake kwa mda wa miaka 20 na hivyo tunapomzungumzia Imam Al Qanabi basi hua tunamzungumzia Mwalimu wa Wanazuoni wa Hadith akiwemo Imam Bukhari na pia Imam Muslim.

Imam Amr Ash Shabi alikua ni mwenye kuheshimika sana na ni mwenye hikma na busara kama tulivyoona kwenye kisa cha Imam Al Qanabi na pia kama anavyotuelezea mwenyewe kwenye kisa kifuatacho pale aliposema kua: '**Hajjaj Ibn Yusuf aliniita mie na nilipofika Mlangoni mwa Jumba lake, nikakutana na Yazid Ibn Abi Muslim ambae aliniambia: 'Inna Lillah, Ash Shabi mbali ya kua na Ilm yako yote hio inakuaje unataka kubeba jukumu kwa Amiri wa Shirk na Nifaq katika Siku ya Malipo? Ama mimi naona bora ujiokoe'**

Na kisha Muhammad Ibn Hajjaj akakutana na mie na pia Yazid, na nilipoingia kwa Al Hajjaj basi Al Hajjaj akasema: 'Ah wewe pia Ash Shabi unakua ni miongoni mwa wanaopigana nasi?' nami nikasema: 'Allah akuongozee mambo yako ewe Amir, kwani sisi tumehamanika Majumbani mwetu, viongozi

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

wamesababisha uharibifu na kutufungia njia zetu, mimi siwezi kulala wala kukimbia kwa sababu ya khofu, nasi hua tunaangamia pale tunapokua si Wacha Mungu na tunapokua hatuna utulivu wa akili'

Al Hajjaj Ibn Yusuf akasema: 'Wa Allahi amesema Ukweli Ash Shabi kwani hawakua Wacha Mungu walipokua wakipingana nasi na wala hawakua na Uwezo zaidi yetu walipokua hawana utulivu wa akili hivyo waachieni.'

Kisha Al Hajjaj Ibn Yusuf akaniuliza suali kuhusiana na Mirathi kulingana na Dada. Mama na Babu nami nikajibu: 'Hakika juu ya hili kuna tofauti ya Mitizamo baina ya Masahaba watano wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na jambo hili, ambao ni Uthman, Zayd Ibn Thabit, Abd Allah Ibn Masud, Ali Ibn Abi Talib na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhum*.'

Hajjaj Ibn Yusuf akaniuliza: 'Jee Abd Allah Ibn Abbas amesemaje juu yake?' Nami nikasema: 'Amesema kua Babu hua ni sawa na Baba na kisha akampa Mama sehemu ya Tatu na Dada hakumpa kitu chochote.''

Hajjaj Ibn Yusuf akauliza: 'Na Jee Amir *Ul Muuminin* amesemaje kuhusiana nalo?' Nami nikasema: '*Amir ul Muuminin* Uthman Ibn Affan amegawa hapa katika makundi matatu.'

Hajjaj Ibn Yusuf akauliza: 'Na Zayd Ibn Thabit?' nami nikasema: 'Ameugawa katika sehemu 9 ambapo Mama atapata sehemu 3, Babu sehemu 4 na Dada sehemu 2.'

Hajjaj Ibn Yusuf akauliza: 'Na kuhusiana na Ibn Masud nae?' nami nikasema: 'Ameigawa katika sehemu 6 ambapo Dada amema 3 Mama amempa 2 na Babu amempa sehemu 1' hivyo Hajjj Ibn Yusuf akachagua Mtizamo wa Uthman Ibn Affan.

Katika historia ya Uislam basi Khalifa Abd Ul Malik Ibn Marwan ndie mtu wa mwanzo katika Waislam kua ni mwenye kuanza kutumia jina la Abd Ul Malik, anasema Imam Amr Ash Shabi kua: '**Mara moja Khalifa Abd Malik Ibn Marwan alinituma na Mjumbe wake kwa Mfalme wa Rumi, na Mjumbe huyo alipofika kwa mfalme wa Rumi basi Mfalme wa Rumi akaniuliza mimi masuali kadhaa na nikayajibu yote.**'

Na ni kawaida wajumbe wote kua hua hawakai kwa Mfalme wa Rumi kwa mda mrefu, lakini hali ilikua tofauti kwa upande wa Amr Ash Shabi kwani Mfalme wa Rumi alimzuia kwa siku kadhaa hadi pale Imam Ash Shabi alipoomba ruhusa kuondoka, Imam Ash Shabi anaendelea kusema kua: '**Nilipokua najitayarisha kuondoka basi Mfalme**

wa Rumi akaniuliza: 'Hivi wewe ni miongoni mwa Washauri wa Khalifa wanaokaa ndani ya Jumba la Khalifa?' nami nikajibu: 'La, mimi ni mtu wa kawaida tu Miongoni mwa Waislam''

Hivyo Mfalme wa Rumi akamnong'oneza mlinzi wake na kisha mimi nikapewa kadi na kuambiwa: '**Ukishampa Khalifa wako barua ulizokua nazo basi mpe na kadi hii pia.**' Hivyo Imam Al Shabi akapokea Kadi hio na kisha akaanza safari ya kurudi katika mji wa Dimashq na alipofika akakabidhi mizigo yote aliyopewa na Mfalme wa Rumi kwa Khalifa Abd |Ul Malik Ibn Marwan lakini akasahahu kumpa na ile ile kadi, hadi hapo baadae ambapo Imam Amr Ash Shabi ndio akakumbuka kuhusiana na kadi hio na akamkabidhi Khalifa Abd Malika Ibn Marwan Kadi hio.

Baada ya kupewa Kadi hio basi Khalifa Abd Malik Ibn Marwan akamuuliza Imam Amr Ash Shabi: '**Hivi jee Mfalme wa Rumi alikuambia chochote kabla ya kukupa kadi hii?'**

Imam Amr Ash Shabi akajibu: **'Naam, Mfalme wa Rumi aliuliza kama mimi ni miongoni mwa Washauri wa Khalifa wanaokaa ndani ya Jumba la Khalifa ama la? Nami nikamwambia kua mimi ni mtu wa kawaida tu miongoni mwa Waislam.**'

Kisha Imam Amr Ash Shabi akasimama na kuondoka, lakini alipofika kwenye Mlango wa Kasri la Khalifa Abd ul Malik Ibn Marwan basi akaambiwa kua anaitwa na Khalifa Abd Ul Malik Ibn Marwan na aliporudi na kufika mbele yake basi Khalifa Abd Ul Malik Al Marwan akamuuliza Imam Amr Ash Shabi: '**Jee unajua hii kadi imeandikwa nini?**' Imam Amr Asha Shabi akajibu: '**La**'.

Khalifa Abd Ul Malik Ibn Marwan akamwambia Imam Amr Ash Shabi: **'Isome'** na alipoisoma basi akaona kua imeandiwa kua: '**Inashangaza kuona kua katika jamii ya watu wenye Mtu kama huyu miongoni mwao, wamemchagua Mtu mwengine kua ni Khalifa wao**', baada ya kuisoma basi Imam Amr Ash Shabi akasema kumwambia Khalifa Abd Ul Malik Ibn Marwan kua: '**Wallahi, kama ningejua kua imeandikwa hivi basi mimi nisingeichukua na wala nisingeikabidhi kwako Kadi hii, kwani amesema maneno haya kwa sababu hajakuona wewe mwenyewe**'

Kalifa Abd ul Malik Ibn Marwan akasema: '**Hivi jee unajua kwanini akaandika ujumbe wa Kadi hii**' Imam Amr Ash Shabi akasema: **'La sijui' Khalifa Abdul Malik Ibn Marwan akasema: 'Mfalme wa Rumi ameandika ujumbe wa Kadi hii kwa sababu ananionea Wivu mimi kua nawe, hivyo amejaribu kuubadilisha mtizamo wa Moyo wangu dhidi yake huku akitegema kua mimi nitakuua wewe na hivyo Waislam wote wasifanikiwe kunufaika na Ilm yako**' na kisha Khalifa Abd Ul Malik Ibn Marwan akamwachia Imam Amr Ash Shabi, na habari hii ilipofika Rumi basi Mfalme wa Rumi akasema kweli hilo ndio lililokua kusudio langu.

Siku moja Imam Amr Ash Shabi aliulizwa: ‘**Hebu tuambie hivi jee wewe ni Mwanazuoni au ni Mwanafiqh?**’ Imam Amr Ash Shabi akasema: ‘**Ole wenu! Haiwezakani kuwajumisha watu na kile ambacho wako mbali nacho, kwani Faqih ni yule anaejidhibiti Nafsi yake kutokana na kumuasi *Allah Subhanah wa Ta’ala* na Mwanazuoni ni yule ambae anaemuogopa *Allah Subhanah wa Ta’ala,* na kwa hakika sisi tuko mbali sana na hao.**’

Kuna mtu alimuuliza Imam Ash Shabi kwa kusema kua: **‘Hebu niambie eti ni kweli Mtoto wa nje ya Ndoa hua ni mbaya zaidi kati ya watu watatu hawa ambao ni Baba, Mama na yeye mwenyewe?’** Imam Ash Shabi akasema: **‘Kama ni hivyo basi Mama yake angekua anastahiki ya kupata adhabu ya kupigwa Mawe wakati yeye akiwa ndani ya tumbo la Mama yake, na asingepewa nafasi ya kusubiriwa kuzaliwa kwake kisha ndio Mama apewe adhabu hio.’**

Na ingawa alikua ni mwenye Ilm kubwa sana lakini Imam Ash Shabi alikua ni mtu asiependa kujibu kila analoulizwa kwani amesema Salt Ibn Ibrahim kua: **‘Sijawahi kuona mimi mtu ambae anasema sana: ‘Sijui’ kama Ash Shabi’**

Alisema Imam Ash Shabi kua: ‘**Kuna watu wa aina nne, wa kwanza ni wale wanaompenda Ali na kumchukia Uthman, wa pili ni wale wanaompenda Uthman na kumchukia Ali, wa tatu ni wale wanaowapenda wote na wa nne ni wale wanaowachukia wote’** hivyo akaulizwa: **‘Hivyo wewe upo kwenye kundi gani?’** Imam Ash Ashabi akasema: **‘Mimi nnawachukia wote wanaowachukia wawili hawa.’**

Na akasema tena Imam Ash Shabi kua: **‘Kumpenda Abu Bakr na Umar na kukubali ukubwa wa darja yao hua ni sehemu ya Sunnah’**

Amesema Imam Amr Ashabi kua: **‘*Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alisikia sauti ya kijana wa kiume ambae alikua ni mwenye kulia na kunadia kwa kusema: ‘Ewe Mwenye Uadilifu katika kuhukumu toa hukumu baina yangu mie na Mama yangu Mzazi kwa haki.**’

Hivyo *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamfuatilia Kijana huyo na alipompata akamuuliza: ‘Kwanini wewe unaomba Dua dhidi ya Mama yako?’

Ambapo kijana huyo akasema: ‘Kwa sababu amenibeba mimi tumboni mwake kwa mda wa miezi 9, ameninyonyesha kwa mda wa miaka miwili, lakini nilipokua mkubwa wa kuweza kutofautisha baina ya jema na ovu basi Mama yangu huyu amenikataa, na kunifunkuza kutoka nyumbani mwake’

***Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu akauliza:* 'Wewe unatoka katika Kabila gani na Mama yako ndio nani?'**

Yule kijana akasema kua: 'Mimi natoka katika kabila fulani na mama yangu ni fulani bint fulani'

***Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu akaamrisha* Mama huyo akaitwe iliaje kujibu shutuma zake, na hivyo mama huyo akaja na Kaka zake wanne wa kiume na Mashahidi 40 ambao wote walitoa ushahidi wa kua Mwanamke huyo ni Mwari, Bikira, hajawahi kuolewa na wala hamjui Kijana huyo na wao pia hawamjui kijana huyo ambae anataka kuutia aibu ukoo wao'**

***Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema kumuuliza kijana huyo: 'Jee ewe Kijana unasemaje kuhusiana na Ushahidi wa Mashahidi hawa'**

Kijana akasema: 'Wa Allahi mimi naapa kua huyu ni Mama yangu, ni Mama yangu, ni Mama yangu.'

***Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema kumwambia Mwanamke huyo: 'Ewe Mwanamke jee umemesikia Mtoto wako anavyosema?'**

Ambapo Mwanamke huyo akasema: 'Wa Allahi nnaapa mimi kwa yule ambae asieonekana na kwa Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kua Mimi simjui huyu kijana bali ni mwenye kutaka kunipa Jina baya mie tu katika kabila langu, kwani mimi ni Bikira na sijawahi kuolewa'

***Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akawaamrisha Askari wake kwa kusema: 'Mchukueni kamuwekeni Jela kwanza'**

Hivyo kijana huyo akachukuliwa na askari hao na kupelekwa Ndani, wakati anapelekwa ndani basi njiani akakutana na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na hivyo Kijana huyo akasema: 'Ewe Ibn Ami wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* hakika mimi nimedhulumiwa na Umar ameamrisha kua nipelekwe Jela.'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akawasimamisha Askari hao na kuwaambia: 'Subirini kwanza msimpeleke ndani bali mpelekeni kwangu mie.' Na kisha akamfuata Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ili nae awepo pamoja nae.

Hivyo kijana huyo akachukuliwa hadi kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na alipofika basi Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akamuuliza kilichotokea na hivyo kijana huyo akaelezea tangu mwanzo hadi mwisho, kama alivyoelezea mbele

ya *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambae nae pia alikuwepo hapo pamoja na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na kijana huyo.

Hivyo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akamuita yule Mwanamke ambae nae akaja na Mashahidi wake wote Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akamwambia Kijana aseme madai yake, na kisha akamhoji Mwanamke ambae nae pamoja na Mashahidi wake wakakataa kua si Mama wa Kijana huyo. Hivyo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Mimi nitaihukumu kesi hii kama vile alivyonifundisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na *Allah Subhanah wa Ta'ala* alie juu ya Arshi yake ataridhika na hukumu yangu hio. Hivyo ewe Mwanamke jee unae Walii wako?'

Yule Mwanamke akasema: 'Naam, hawa hapa Kaka zangu ndio Mawalii wangu'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Jee mtakubaliana na Hukmu yangu nitakayoitoa?' ambapo watu hao wakasema: 'Naam Ewe Ibn Ami wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* tutakubaliana nayo, vyovyote vile itakavyokua'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* aakumuuliza *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema: 'Umar Jee unaniruhusu niendelee?' ambapo *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Naam endelea'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Nnashuhudia mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kua nimemmuozesha huyu Mwanamke kwa kijana huyu kwa malipo ya Mahari ya Dirham 40 ambazo nitalipa mimi mwenyewe kutoka mfukoni mwangu.'

Na kisha baada ya hapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema kumwambia mfanyakazi wake kua: 'Nenda Nyumbani kachukue Dirham 40 kisha niletee hapa sasa hivi' ambapo mfanyakazi huyo akaenda Nyumbani nakisha akarudi na Dirham 40 akamkabidhi Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* Ambae nae akazichukua na kumpa kijana huyo na kumwambia: 'Mpe mke wako Dirham hizi na kisha ondokeni kisha mrudi mkiwa tayari mna ushahidi kua mmeshaona kweli'

Kijana akazichukua Dirham hizo na kisha akafanya kama alivyoamrishwa na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na akasema kumwambia yule Mwanamke: 'Twende zetu nikakuoe'

Ambapo yule Mwanamke akaanza kulia kwa kusema: 'Nisaidie ewe Ibn Ami wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* Nisaidie, kwani haifai kuniozesha kwa

Mtoto wangu niliemzaa mwenyewe. Kwani kwa Hakika mimi nnaapa kua huyu ni mtoto wangu, Kaka zangu waliniozesha mimi hapo kabla na nikajifungua Mtoto huyo lakini baadae alipokua mkubwa wakamkataa na kunitaka nimtenge na nikatae kua sio wangu, hivyo mimi nilifanya hivyo kwa ajili ya kuwaridhisha wao ingawa nampenda sana Mtoto wangu huyu.'

Hivyo Mwanamke huyo akamchukua Mtoto wake huyo na kurudi nae nyumbani kwake.

Imam Amr Ash Shabi alifariki mnamo mwaka 105 Al Hijra.

IMAM HASAN AL BASR 21 AH

Mnamo mwaka wa 21 Al Hijra ambacho kilikua ni kipindi cha Utawala wa *Amir ul Muuminina* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* katika Nyumba ya aliekua Mtumwa wa Zayd Ibn Harith *Radhi Allahu Anhu* aitwae Yasir alizaliwa mtoto wa kiume ambae alikua akijulikana kama Abu Sa'id Ibn Abi Al Hasan Yasar Al Basri, maarufu kama Hasan Al Basr ambae baada ya kuzaliwa tu basi alichukuliwa na kupelekwa moja kwa moja kwa *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambae alimuombea Dua kwa kusema: **'Ya Allah nakuomba mjaalie awe na Hikma na Imani na awe ni mwenye kupendwa na watu wote.'**

Hasan Al Basr aliitwa Al Hasan kwa sababu alipozaliwa alikua na muonekano mzuri na wenye kuvutia *Ma-shaa Allah*, na alikulia ndani ya Nyumba ya *Umm Ul Muuminin* Ummu Salama *Radhi Allahu Anha* na kusomeshwa na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na hivyo Hasan Al Basr alikua ni mtoto ambae alikulia katika malezi bora kabisa na katika wakati wa uhai wake alikua ni mwenye kuwaona Masabaha 120 ambapo 70 kati yao walikua ni Masahaba waliopigana vita vya Badr.

Ambapo miaka 16 baada ya kuzaliwa kwake basi familia yake ilihama kutoka katika mji wa Madina na kuelekea katika Mji wa Basra nchini Iraq ambapo aliishi maisha yake yote yaliyobakia katika uhai wake na ndio maana akawa anajulikana kama Hasan Al Basr yaani Hasan wa Mji wa Basra.

Hivyo haishangazi kuona kua Imam Hasan Al Basr alikua ni kijana mwenye ufahamu mkubwa sana na uwezo wa hali ya juu tofauti na watoto wengine waliokulia katika umri wa rika lake. Kiasi ya kua Imam Hasan Al Basr alikua yuko juu sana na mwenye kutisha tunapozungumzia Ilm ya Dini ya Kiislam ikiwemo Qur'an, Hadith na pia alikua ni mwingi wa Hikma, na aliwapita hata wengi miongoni mwa Watu wazima waliokua

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

wakiishi katika wakati wake, na bila ya shaka kutokana na kujua kwake na hikma zake na kipindi alichoishi basi wengi sana walimnasibisha na Masahaba.

Mwanzoni mwa wakati wa Ujana wake Imam Hasan Al Basr alikua ni Mujahid ambae alipigana katika vita vya kadhaa na pia aliwahi kua mfanyabiashara wa vito vya mapambo ya thamani na kisha baada ya hapo akahama moja kwa moja kwenye kutoka kwenye fani hizo na kuzama zaidi kwenye Ilm ya Dini kwa ajili ya kumtumikia Mola wake kikamilifu.

Tunapomzungumzia Imam Hasan Al Basr basi hua tunamzungumzia Imam ambae alikua akihesabiwa kua ni miongoni mwa Mawalii wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na Ucha Mungu wake ambao ndio wale waliotajwa kwenye hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema juu yao kua:

'Kamwe Ardhi haitokosa watu 40 ambao ni wenye kufanana na *Khalillu Allah* na kutokana nao, basi watu watapat Mvua na Msaada (wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*), na haitokei kua mmoja wao kua ni mwenye kufariki isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* humteua mwengine kuchukua nafasi yake badala yake' ambapo amesema Imam Qatadah Al Sadusi kua: **'Hakika sisi hatukua na shaka kua Al Hasan Al Basr alikua ni miongoni mwao watu hao.'**

Kwa upande wa Ilm ya Hadith basi Imam Hasan Al Basr amenukuu hadith 1400 ambazo nyingi miongoni mwao ni zenye kutoka kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* moja kwa moja kutoka kwake. Na ingawa Imam Hasan Al Basr alikua na Wanafunzi wengi sana lakini mmoja miongoni mwa Wanafunzi wake Imam Hasan Al Basr alikua na ukaribu nae sana na huyu alikua akijulikana kama Imam Habib Al Ajami.

Imam Hasan Al Basr alikua ni mwenye sifa ya kua anapoizungumzia Akhera basi watu hua ni wenye kutokwa na machozi, na anapowazungumzia Masahaba na jitihada zao katika Uislam basi alikua ni mwenye kuwaacha watu wakiwa ni wenye kulia pia ambapo miongoni mwa Kauli zake ni kua: '**Hakika mimi nimewaona Masahaba waliopigana vita vya Badr walivyokua wakiishi, na nakuoneni mnavyoishi nyie, na leo hii kama Masahaba hao watafufuka basi nyinyi mtawaona wao kua ni Waliochanganyikiwa kwa namna wanavyoishi na wanavyomuamini na kumuogopa Allah *Subhanah wa Ta'ala* na wao watakuoneni nyinyi kua hamkumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na mnavyoishi.**'

Imam Hasan Al Basr anaendelea kuusia kwa kusema kua: '**Masahaba walikua wana upekee wanapokua na Marafiki zao, na ni wenye kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* wanapokua peke yao, ni wenye kuridhika na cha halali walichokipata na ni wenye shukrani wanapokua na urahisi katika kila jambo lao, Watulivu wanapokua na Matatizo kwani walikua wakimkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* wanapokua hawana kazi na ni wenye kutamani rehma zake.**

Miongoni mwao Masahaba basi wale wenye Ilm walikua wanapewa Darja mbele ya Masahaba wenzao na kuheshimiwa bila kuangaliwa anafanya kazi gani au kipato chake, na wanapofariki basi Roho zao hua ni zenye kusheherekewa Mbinguni, Enyi Waislam hivyo ndivyo walivyokua Watu wema waliotangulia kabla yenu, hivyo kama nyinyi mkipotoka basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakuzilieni rehma zake juu yenu'

Kutokana na ukubwa wa Ilm yake basi anasema Rabi Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Hakika mimi nilipata bahati ya kua pamoja na Hasan Al Basr kwa miaka 10 takriban kila siku nilikua nikisikia jambo jipya kutoka kwake na sijawahi hata mara moja kusikia kutoka kwake kitu ambacho amekirudia katika kusomesha kwake**'

Imam Hasan Al Basr alisema kuhusiana na wasomaji wa Qur'an kua: **'Kuna wasomaji wa Qur'an wa aina tatu: Aina ya kwanza ni ya wale ambao hua wanaitumia Qur'an kua ni kama Biashara ya kujipatia Mkate wao.**

Aina ya pili ni ya wale ambao wanashikamana na herufi zake na kuachana na Sharia zake na hivyo kua ni wenye kujiona mbele ya Watu wao kutokana nayo na hua ni wenye kutafuta manufaa yake kutoka kwa Watawala, na kuna wengi miongoni mwa Waliohifadhi Qur'an waliomo kwenye kundi hili, na Allah asiwaongeze idadi yake.

Aina ya tatu ni ya wale ambao ni wenye kutafuta shifaa kutokana nayo na hivyo kua ni wenye kuiweka Qur'an kwenye maradhi ya Nafsi zao. Na hukimbilia nayo kwenye maeneo ya Ibada na kuikumbatia. Hawa ni wale ambao ni wenye Taqwa na ni wenye kulivaa guo la Huzuni na unyenyekevu. Hawa ndio wale ambao kutokana nao basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kushusha Mvua kwa ajili yao na kuwapa ushindi dhidi ya maaduia zao. Wa Allahi aina hii ya wenye kuhifadhi Qur'ani hua ni adimu sana zaidi ya *Kibrit Al Ahmar*'

Ambapo *Kibrit Al Ahmar* hua ni Red Sulpher au Salfa Nyekundu, na ukweli ni kua hakuna Sulpher yenye rangi Nyekundu, kwani Sulpher hua ni yenye rangi manjano, hivyo hii *Kibrit Al Ahmar* hua ni mchanganyiko wa Madini ya Salfa na Zebaki. Ambayo Salfa hua ni yenye rangi ya Manjano na yenye sifa ya kua ni Yenye kuruhusu mchanganyiko wenye kuweza kutoa Nguvu ya Mripuko wenye kuunguza.

Zebaki yaani Mercury hua na rangi Nyeupe na Kijivu na ni yenye sifa ya Kutiririka na kufuata mkondo, ni baridi na tulivu na yenye kukubali kupokea hali ya mabadiliko.

Ambapo Salfa na Zebaki zinapochanganyishwa pamoja basi matokeo yake hupatikana kitu kinachojuliana kama Salfa Nyekundu ambayo hua na sifa ya upekee yenye uwezo wa kupokea na kutoa nguvu za kipekee zisizokua za kawaida.

Hivyo kifalsafa basi *Kibrit Ahmar* hua aina ya Kanuni ambazo hua zinatumika na kuweza kukipelekea kitu kua ni chenye mabadiliko ya hali ya juu kabisa kutoka katika

hali ya Kawaida na kuingia katika hali ya Upekee na Uadimu ambao hua unaweza hata kutumika kuyabadilisha Madini ya Chuma cha kawaida kua ni Dhahabu,

Ama kwa upande wa Ilm ya Dini ya Kiislam basi sifa ya *Kibrit Al Ahmar* hua inamaanisha maumbile ya Ibn Adam wa kawaida mwenye uadimu wa Darja ya hali ya juu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* iliyoofichikana ndani ya Moyo wake mja huyo kutokana na kua ni mwenye kujisalimisha kikamilifu katika kutekeleza Maamrisho ya Mola wake. Kwani Salfa hua ni Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Taa'ala* na Zebaki hua ni Usalimisho wa Mja kwa Mola wake juu ya maamrisho yake.

Sifa zake Imam Hasan Al Basr zilikua ni zenye kuonekana katika Darsa zake na Ucha Mungu wake, Ustahmilivu wake, Subra yake, Ukweli na uaminifu wake, kua na Moyo mkubwa kwake kwa ukarimu na kutoa Hukmu basi alikua ni mwenye kufanana na Nyota kubwa sana.

Imam Hasan Al Basr alikua kila wakati amezungukwa na Wanafunzi ambao ni wenye kuhitaji maelezo kutoka kwake katika fani tofauti za Ilm, alikua akiwasomesha baadhi *Tafsir*, wengine Hadith na wengine Fiqh na pia alikua akifafanua kuhusiana na Fatwa kwa wengine na kwa wengine alikua akiwafundisha Kanuni za Fiqh n.k kwani kila akifundishacho na akisemacho Imam Hasan Al Basr kilikua ni chenye kutokana na kwenye kina cha Moyo wake ambao ulikua ni wenye kujaa Ikhlasi ndani yake.

kwani Imam Hasan Al Basr alikua ni mwenye kuikimbia kwa kasi kubwa sana sifa ya kutokua na Ikhlasi ambayo kinyume chake hua ni kua na sifa ya unafiq alikua akisema kua: '**Hakuna anaeuogopa Unafiq isipokua yule Mtu ambae ni Alieamini kweli, na hakuna anaejihisi kua amesalimika na Unafiq isipokua yule ambae ni Mnafiq na Hakuna asieuogopa Unafiq isipokua Mtu huyo hua ni Mnafiq**.'

Na amesema tena Imam Hasan Al Basr kua: '**Muislam hubakia kua ni Muislam pale anapokua anajiusia Nafsi yake na kuendelea kujichunga kwa kujihesabia Kasoro zilizomo ndani ya Nafsi yake'**

Imam Hasan Al Basr aliusia kwa kusema: '**Tafuteni Utamu unaopatikana katika Mambo matatu. Jambo la kwanza ni utamu wa ndani ya Sala, Utamu wa Kufanya *Dhikr Allah* na Utamu wa Kusoma Qur'an, kwani Utamu wake vitu hivi hupatikana ndani yake, na ukiupata ndani yake basi fahamu kua Mlango wa Peponi uko wazi kwa ajili yako, na kama ukiukosa basi Mlango wa Peponi umefungwa kwa ajili yako.**'

Imam Hasan Al Basr alikua ndie mtu wa mwanzo kushauri utumiwaji wa Tasbih za mkononi kwa ajli ya kufanya *Dhikr Allah*, kwani alikua ni mwenye kusema kua: '**Kile tulichokitumia mwanzoni mwa njia yetu hatutamani kuachana nacho tunapofika mwishoni mwa njia yetu, kwani mimi hua napenda kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Moyo wangu, Kwa Mikono yangu na kwa Ulimi wangu**'

Ambapo anasema Imam Ibn Muflih kua: '**Hasan Al Basr amekiingiza kitendo cha kuubusu Mkono wa Mwanazuoni kua ni sehemu ya Kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala***'

Ambapo amesema Imam Al Suyuti kuhusiana na kauli hii ya Imam Hasan Al Basr kua: '**Na vipi iwe vyenginevyo, wakati *Tasbih* hua ni zenye kumkumbusha Mtu kuhusiana na Mola wake, na na mara chache kwa mtu kua na Tasbih bila ya kumkumbuka *Allah Subhnaha wa Ta'ala* a****mbapo jambo hili ni moja kati ya manufaa makubwa ya Tasbih'**

Ama kuhusiana na unyenyekevu ndani ya Sala basi alisema Imam Hasan Al Basr kua: '**Kama itakua huijali Sala yako, basi utakua unajali nini zaidi yake? Kwa sababu kila unapokua unaijali Sala yako basi ndio unavyojaaliwa kuyarekebisha maisha yako, hivi jee hamjasikia kua Sala imeambatanishwa na Mafanikio? Pale inaponadiwa *'Hayya aAala Al Salah Hayya Aala al Falah!' yaani 'Njooni katika Sala, Njooni katika Mafanikio'* hivi jee Utamuombaje *Allah Subhanah wa Ta'ala* akupe Mafanikio wakati hutimizi wajibu wako kwake?'**

Imam Hasan Al Basr alikua ni mtu mwenye kutafakkar sana kuhusiana na Akhera yake kuliko Dunia yake kiasi ya kua alikua si mtu mwenye kucheka sana kwani bali alikua ni mwenye Kulia zaidi kwa ajili ya Mola Akhera yake kwani alikua akisema kua: '**Saa moja ya Kutafakkar ni bora kuliko Mwaka mzima wa *Qiyam Al Layl.***'

Na anasema Imam Al Qushayri kua: **'Kamwe haitokei kwa mtu kukutana na Hasan Al Basr bila ya kudhania kua Hasan Al Basr amefikwa na Mtihani Mkubwa Sana.**'

Na bila ya shaka mbali ya kua Imam Hasan Al Basr alikua ni mtu kwenye kua na huzuni kwa kufikiria juu ya Akhera yake lakini kwa upande mwengine alikua ni mtu mwenye kujua kuutumia mda wake kulingana na matukio maalum, kwa mfano katika siku za sikukuu za Idd basi Imam Hasan Al Basr alikua ni mtu ambae mwenye furaha na kuvaa nguo zenye kupendeza zaidi, kiasi ya kua hata watu walikua wakimuona basi hua hawawezi kumjua kua ndio yeye, kwani katika sikukuu moja kuna Wanawake walitoka nje na kisha waliporudi ndani wakaulizwa: '**Hivi Jee mmemuona Mtu gani aliependeza zaidi katika siku ya leo?' Wanawake hao wakajibu:** '**Ni yule Imam alievaa Kilemba Cheusi**' wakimaanisha kua ni Imam Hasan Al Basr.

Siku moja Imam Hasan Al Basr alisikia kua katika Mji wa Basra kuna mtu ambae alikua anapenda kuishi peke yake kivyake vyake, hivyo akaamua kumtembelea mtu huyo ili amjue na apokutana nae baada ya kumsalimia basi Imam Hasan Al Basr akamuuliza mtu huyo: '**Unaonekana kua ni mtu anaependa kukaa peke yake, hivyo jee ni kwa sababu gani hupendi kujumuika na watu?**'

Mtu huyo akajibu: **'Majukumu yangu hayaniruhusu mimi kujumuika na Watu.'**

Imam Hasan Al Basr akasema: **'Jee unajua kua katika mji huu kuna Mtu anaitwa Hasan Al Basr? Hivi hutaki kumtembelea hata mara moja?'**

Mtu huyo akajibu : **'Majukumu yangu hayaniruhusu hata kukutana na huyo Hasan Al Basr'**

Hivyo Imam Hasan Al Basr akauliza kwa kusema: **'Hivi jee hayo Majukumu uliyokua nayo ni Majukumu gani?'**

Mtu huyo akajibu: **'Wakati nnapokaa na kutafakkari kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala*, basi hua ni mwenye kuona neema za *Allah Subhanah wa Ta'ala* na dhambi zangu, hivyo hua ni mwenye kubakia kuonesha shukrani kwa neema hizo na kuomba maghfira kwa dhambi zangu.'**

Hivyo Imam Hasan Al Basr akasema: **'Kama ni hivyo basi bila ya shaka wewe ni mwenye kua na Busara sana kuliko hata Hasan Al Basr, na hivyo haina haja kwako kujumuika na watu hivyo endelea kusimamia majukumu yako.'**

Imam Hasan Al Basr amesema kua: **'Muumini hua ni mwenye kufanya Amali njema kwa wingi hukua kiwa ni mwenye kua na khofu kubwa kua hata kama ikiwa atatumia mali yake yenye wingi wa Mlima Uhud basi katika kutoa sadaka basi hua hana uhakika kua atauona mbele ya Mola wake na kutokana na kua na hali hio basi ndivyo huzidi ucha Mungu wake, wakati Mnafiq hua ni mwenye kusema: 'Kuna watu wengi sana hivyo mimi nitasamehewa tu' na hivyo hua ni mwenye kuendelea na kufanya maovu.'**

Imam Hasan Al Basr akasema pia kua: **'Imenifikia mie kua pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* anapowaneemesha watu kwa jambo jema basi hua anawataka wawe na shukrani. Na kama wakiwa na shukrani basi huwazidishia, na kama wakiwa hawana shukrani basi anao uwezo wa kuifanya neema hio ikawa ni adhabu kwa watu hao'**

Imam Hasan Al Basr aliusia baada ya kuzika Makaburini kwa kusema kua: **'Namuomba Allah amrehemu yule ambae ni mwenye kuishi maisha yake kwa ajili ya siku kama ya leo, kwani ni katika siku kama ya leo ndio mnaweza kufanya yale ambayo hayawezekani kufanywa na ndugu zenu waliomo humu ndani Makaburini, hivyo tumieni afya yenu na mda wenu vizuri kabla haijafika siku ya matatizo ya kuhesabiwa'**

Akasema Imam Hasan Al Basr tena kua **'Wallahi, hakika mimi sijawahi kumuona Mtu ambae amepewa Neema nyingi za Kidunia na kisha akawa hana Khofu kua neema hio inaweza ikawa Mtihani kwake, isipokua kwa yule mtu ambae ni mwenye asiekua na ufahamu, na kamwe Allah hajawahi kuzuia Neema za kidunia bila ya mtu huyo kufikiria kua hilo ni jambo zuri kwake isipokua kwa yule ambae ni mwenye ufaham mdogo. '**

Imam Hasan Al Basr alisema kua: **'Kujifunza mada moja tu ya sehemu ya Ilm na kisha kuifundisha mada hio kwa Muislam ni bora kwangu mie kuliko kua na**

umiliki wa Dunia nzima na kila kitu kilichomo ndani yake na kisha kuutoa kwa ajili ya Allah.’

Imam Hasan Al Basr akasema: **‘Kutoka na kuenda kumsaidia Muislam Mwenzako mwenye Matatizo ni bora kuliko kuenda Hajj na kurudi na Kuenda tena.’**

Amesema Hasan Al Basr kua: **‘Enyi Vijana, Itafuteni Akhera yenu kwani kwa hakika sisi tumeona watu ambao walikua wakiikimbilia Akhera yao na kuikuta ndani ya Dunia yao, lakini kamwe hatukuwahi kuona yeyote yule ambae aliikimbilia Dunia na kisha akaikuta Akhera yake ndani yake.’**

Wanafunzi wake Imam Hasan Al Basr Walimuuliza Imam Hasan Al Basr kwa kusema: **‘Ewe Abu Said hivi jee unaweza kutuusia sisi juu ya lile ambalo litatunufaisha?’**

Imam Hasan Al Basr akasema: **‘Nakuusieni mambo matatu, ambapo Kwanza kaeni mbali na yale mambo ambayo mmeheramishiwa.**

Pili, kuweni ni wenye kukimbilia katika Kufanya Mema mliyoamrishwa kuyafanya;

Tatu, Fahamuni kua katika Uhai wenu kuna Hatua mbili ambazo kila mmoja hua ni mwenye kuchukua, ambapo hatua ya kwanza hua ni kwa ajili yake na hatua ya pili ni dhidi yake, hivyo kuweni makini na hatua mnayoichukua ili muwe ni wenye kujua mnatoka wapi na mnaelekea wapi.’

Na akasema tena Imam Hasan Al Basr: **‘Ulimi wa Mtu mwenye Ufahamu hua uko nyuma ya Moyo wake, hivyo anapotaka kusema basi hua ni mwenye kutafakkari kwanza, kua kama maneno yake yatakua kwa ajili ya manufaa yake basi atayasema na kama yatakua ni dhidi yake basi hatoyasema. Na Ulimi wa Mtu asiekua na Ufahamu, hua uko nyuma ya Ulimi wake hivyo pale anapokifikiria tu kitu basi hua ni mwenye kukisema bila ya kujali kua kitu hicho kitakua dhidi yake au kwa manufaa yake.’**

Akasema tena Imam Hasan Al Basr: **‘Mambo manne hua ni yenye kuainisha maangamizo ya Mtu: ‘Kua na Moyo Mgumu; Kua na Macho Makavu yasiyotoka Machozi’; Kua na Matumaini ya Uhai wa Kidunia na Kua na Uchu wa kukumbatia na kukusanya mapambo ya Dunia.’**

Kuna mtu alienda kwa Imam Hasan Al Basr na kumwambia: **‘Ewe Hasan Al Basr hakika mimi nimekuja kwako kwa ajili ya kubishana kuhusiana na imani ya dini’** ambapo Imam Hasan Al Basr akasema: **‘Hakika mimi naijua Imani ya Dini yangu, hivyo kama wewe umeipoteza yako basi nenda kaitafute sehemu ulikoipotezea.’**

Imam Hasan Al Basr alikua ni mtu ambae asiependa kuusia kile ambacho asichokifanya, kutokana na kua amehoji *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ لِمَ تَقُولُونَ مَا لاَ تَفْعَلُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo lima taqooloona ma la tafAAaloona *(Surat As Saff 61:2)*

Tafsir: ***Enyi wale ambao Mlioamini Kwanini mnasema yale ambayo hamuyafanyi?***

Hivyo Imam Hasan Al Basr katika Khutba zake hakuwahi kuzungumzia kuhusiana na kuwaachia huru Watumwa, kiasi ya kua aliulizwa: **'Hivi Kwanini wewe Hujawahi kuzungumzia kuhusiana na kuwaachia Huru Watumwa?**' ambapo nae akasema: **'*Inshaa Allah* nitazungumzia Ijumaa Ijayo'**

Lakini hata hivyo zilipita Ijumaa tatu bila ya kuzungumzia jambo hilo, alipolizwa tena akasema: **'Ili nizungumzie kuhusiana na kuwaachia Huru Watumwa basi inabidi kua mimi niwe nao Watumwa kisha niwaachie Huru. Na ili niwe na Watumwa inabidi niwe na pesa za kuwanunulia kwanza kisha ndio niwaachie Huru, na kwa hakika mimi sitaki kua miongoni mwa wale walioambiwa:**

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ لِمَ تَقُولُونَ مَا لاَ تَفْعَلُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo lima taqooloona ma la tafAAaloona' *(Surat As Saf 61:2)*

Tafsir: ***Enyi Wale ambao Mlioamini kwanini Mnasema (Kuhusiana na) kile ambacho msichokifanya?***

Miongoni mwa Wanawake Wacha Mungu wa Mji wa Basra aliekua akiishi katika wakati wa Imam Hasan Al Basr basi alikua yule aitwae Burda Sarimmiyah ambae alikua anapenda kulia sana, kwa ajili ya kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, Hivyo Imam Hasan Al Basr akawambia Mwanamke huyo kwa kusema kua: **'Ewe Burda hakika ya Mwili wako una haki yake juu yako na Macho yako yana haki juu yako,'** ambapo Burda akasema: **'Ewe Abu Said, hakika kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* atanijaalia mimi kua ni Mtu wa Peponi basi atanipa Macho Mazuri zaidi ya haya na kama atanijaalia kua Mtu wa Motoni basi atanipa Mabaya zaidi ya haya'**

Na miongoni mwa kauli zake Imam Hasan Al Basr ni kua:

'Tamaa humuangamiza Mwenye Il'm.'

‘Mtihani wa Matamanio ya tumbo ndio yaliyompelekea Adam kumuasi Mola wake, na Mtihani wa matamanio haya hua Daima unamuandama Ibn Adam.’

‘Hakika ya Dunia ni kipando chako, hivyo kama ukikiendesha basi kitakufikisha unapotaka kuenda, lakini kama kikikuendesha basi kitakuangamiza.’

‘Dunia ni sehemu ya kuchuma Amali, hivyo yeyote yule atakaeishi ndani yake huku akiwa ni mwenye kuichukia basi atakua ni mwenye kufuzu na ni mwenye kuiheshimu Dunia. Ama kwa yule atakaeishi ndani yake akiwa amejawa na Mapenzi ya Dunia na akazama ndani yake basi atakua ni mwenye kuiangamiza Nafsi yake na hatokua na manufaa na Dunia.’

‘Uhai wa Dunia hii umeumbwa kwa siku tatu: Jana ambayo imeshapita na kila kitu chake kilichofanywa ndani yake; Kesho ambayo haijafika na haitofika; Leo ambayo ndio uliyokua nayo kufanya unayotakiwa kufanya.’

‘Ilikua ikisemwa kua ni sehmeu ya Unafiq kua na hali ya utofauti wa ndani ya Nafsi yako na Muonekano wako, kusema jambo moja na kufanya jengine na kua tofauti katika kuingia kwako na katika kutoka kwako, na Asili ya Unafiq ni Kusema Uongo.’

‘Atakua ni mwenye kua na maumivu makali sana yule mtu ambae amejaaliwa neema na *Allah Subhanah wa Ta’ala* kisha akazitumia neema hizo kwa ajili ya kumuasi *Allah Subhanah wa Ta’ala.*’

‘Hakuna kusengenya kwa yule mtu ambae ni mwenye kuzusha au kwa mtu mwenye kufanya dhambi hadharani.’

‘Imani hua ni si kwa kujipamba wala si kwa kufikiria mema, bali hua ni kile kitu kinachokaa ndani ya kina cha Moyo na kuthibitishwa na Mateno yako, hivyo yeyote yule atakaeamrisha Mema bila ya kufanya Mema basi maneno yake yatalinganishwa na vitendo vyake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala*. Hivyo yeyote yule atakaeamrisha Mema nae akafanya Mema basi maneno yake yatapandishwa Daraja na Amali zake na hii ni kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta’ala* amesema:

﴿مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلْعِزَّةَ فَلِلَّهِ ٱلْعِزَّةُ جَمِيعاً إِلَيْهِ يَصْعَدُ ٱلْكَلِمُ ٱلطَّيِّبُ وَٱلْعَمَلُ ٱلصَّالِحُ
يَرْفَعُهُ وَٱلَّذِينَ يَمْكُرُونَ ٱلسَّيِّئَاتِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَكْرُ أُوْلَٰئِكَ هُوَ يَبُورُ﴾

Man kana yureedu alAAizzata falillahi alAAizzatu jameeAAan ilayhi yasAAadu alkalimu alttayyibu waalAAamalu alssalihu yarfaAAuhu waalladheena yamkuroona alssayyi-ati lahum AAadhabun shadeedun wamakru ola-ika huwa yabooru *(Surat Fatir 35:10)*

Tafsir: ***Mwenye kutaka Utukufu basi kwa Allah uko Utukufu wa kila kitu, kwani kwake yeye ndio kwenye kupanda kauli njema na Amali njema huzipandisha Darja (Kauli hizo kutokana na mema hayo) ama kwa wale wenye kupanga maovu basi ni juu yao adhabu kali na mipango yao itaangamia.'***

Ama kuhusiana na ile Dua ya aya isemayo:

﴿وَمِنْهُم مَّن يَقُولُ رَبَّنَآ آتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ﴾

Waminhum man yaqoolu rabbana atina fee alddunya hasanatan wafee al-akhirati hasanatan waqina AAadhaba alnnari *(Surat Al Baqara 2:201)*

Tafsir: ***Na wale wenye kusema: 'Ewe Mola wetu tupe sisi mema ya Dunia hii na Mema ya Akhera na utuepushe na Adhabu ya Moto'***

Basi Imam Hasan Al Basr anasema kua: '**Mema ya Dunia hii ni hua ni Ilm na Kufanya Ibada na Mema ya Akhera hua ni Pepo**'

Imam Hasan Al Basr alisema: **'Pale mtu anapotafuta Ilm basi hua haichukui mda isipokua Ilm hio itaonekana kwenye nyenyekevu wake, katika mtizamo wa Macho yake, Katika Ulimi wake na Mikono yake na Sala yake, na Kauli zake na kujitenga kwake na Mapambo ya Dunia. Na mtu anaepata sehemu ndogo ya Ilm na kisha akaifanyia kazi basi itakua ni bora kwake kuliko hata kua na umiliki wa Dunia nzima na kisha kuitoa kwa ajili ya akhera yake '**

Imam Hasan Al Basr alisema: **'*Allah Subhanah wa Ta'ala* ameamrisha matendo mema na kisha akamrahisishia Ibn Adam kuyafanya matendo hayo, na amekataza matendo maovu na kisha na kisha akamsaidia Ibn Adam kuachana nayo matendo hayo. Hivyo fanyeni kwa kadri mtakavyoweza kuustahamilia Moto wa Jahannam, kwani hamtokua na kisingizio kama mwisho wenu mtaishia kuingia ndani yake.'**

Ama kuhusiana na wenye Il'm basi amesema Imam Hasan Al Basr kua: **'Wanafiqh hua ni wale ambao hawavutiwi na maisha ya Dunia, wenye kuikimbilia Akhera yao,**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

wenye Ilm ya Dini ya Kiislam, wenye kumuabudu Mola wao na hua ni wenye kujizuia kutokana na kuwavunjia heshima Waislam wenzao, na kuwadhulumu Mali zao na hua ni wenye kuwausia Mema juu yao.'

Imam Hasan Al Basr alisema: **'Miongoni mwa watu ambao watahesabiwa kiwepesi katika siku ya Malipo basi ni wale ambao, ni wenye kujihesabia Nafsi zao hapa Duniani kwa Ajili ya Mola wao. Wale ambao ni wenye kutafakkar matendo yao, kiasi ya kua kama nia yake ni kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni mwenye kudumu katika kulifanya Jambo hilo, vyenginevyo hua ni mwenye kuachana na jambo hilo. Kwani kwa hakika Siku ya Malipo hua ni nzito kwa wale wenye pupa katika maisha haya na hivyo hawakuweza kujidhibiti Nafsi zao. Kwani hawa watamkuta *Allah Subhanah wa Ta'ala* amewahesabia kila kitu chao hadi kile kidogo kabisa.'**

Imam Hasan Al Basr alisema: **'Yule ambae ni mwenye kuzidishiwa Mali, basi na Dhambi zake huongezeka, na yule mwenye kuongezeka kwa Maneno yake basi Uongo wake huongezeka. Mwenye kua na Matendo maovu basi hua ni mwenye kujiadhibu Nafsi yake'**

Imam Hasan Al Basr alisema: **'*Allah Subhanah wa Ta'ala* amuingize kwenye rehma zake yule Mtu ambae ametumia uhai wake hapa Duniani kwa kuufanya kua ni Amanah, na kisha akairudisha Amanah hio kwa mwenyewe huku yeye akibakia kua ni mwepesi kabisa'**

Imam Hasan Al-Basri aliulizwa: **'Hivi Jee sisi hatutakiwi kua ni wenye kuona haya kumuomba msamaha *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na kisha kufanya dhambi tena na kisha kuomba msamaha tena na kisha kufanya dhambi tena?'**

Imam Hasan Al Basr akajibu: **'Shaytan ni mwenye kupenda kua nyinyi muwe na hali hio, ya kuona haya hivyo dumuni katika kufanya Istighfar.'**

Imam Hasan Al Basr aliulizwa : **'Hivi Jee Ibilisi anakua analala?'** ambapo nae akajibu kwa kusema kua: **'*Wallahi* kama angekua analala basi na sisi tungepata afueni kubwa sana.'**

Ambapo alisema Imam Hasan Al Basr: '**Kuna wakati ambao hua inatokea mtu ambae ni mwenye kutafuta Ilm basi hua ni mwenye kuweza kuonekana kwa athari ya Ilm yake hio ndani ya maisha ya mtu huyo katika Ucha Mungu wake, tabia zake, mtizamo wa macho yake, kauli zake na kusikia kwake.**'

Imam Hasan Al Basr alisema: '**Zawadi kwa Ajili ya Malipo ya Akhera ni Salat, Saum, Sadaqah na Kutokwa na Machozi kwa ajili ya Allah, ambapo Sala hua ni Ibada pekee bora inayohitaji Umakini kwani Hukukaribisha kwa *Allah Subhanah***

***wa Ta'ala*, *Funga ni Muhimu* kwani huuboresha Mwili wa Ibn Adam na pia huiboresha Nafsi yake, *Sadaqa* hua ni ngao inayomlinda Mja kutokana na Hasira za *Allah Subhanah wa Ta'ala* dhidi yake, na Machozi hua ni njia bora ya kupata ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na usamehevu wake**

Anasema Imam Abu Talib Al Makki kua: **'Hasan Al Basr ni Imam wetu katika Aqida tunayoiwakilisha, sisi tanafuata hatua zake na kutokana na taa yake ndio tunapata Nuru yetu'**

Anasema Abu Ubaidah Ibn Naji kua: **'Sisi tulimtembelea Hasan Al Basr katika siku ambayo alikua anataka kufariki na akatuambia kua: 'Karibuni, Salama na Amani ya Allah ziwe juu yenu na kisha atukaribishe sote kwenye makazi mema. Kwani hii hua ni dalili nzuri kwa kila mkweli na mwenye subra, ambapo sehemu yenu ya Dini hii haitakiwi iwe ni katika kusikia kwa masikio yenu na kusema mnayoyasikia kwa midomo yenu.**

***Allah Subhanah wa Ta'ala* amuingize kwenye rehma zake yule ambae anaekula mkate wa bei rahisi, anaevaa nguo kuukuu, anaekaa kitako ardhini na kufanya kazi ngumu na kulia kwa ajili ya Dhambi zake, na kujitahidi kuzikimbia adhabu za Allah na kua ni mwenye kudumu katika kuomba rehma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* hadi kifo kitakapomkuta wakati akiwa katika hali kama hii''**

Mnamo mwezi 5 Rajabu ya siku ya Ijumaa ya mwaka wa 110 Al Hijra Imam Hasan Al Basr alifariki Dunia akiwa na umri wa miaka 89. Hii ilikua ni siku ya huzuni kubwa kiasi ya kua mji wote wa Basra ulihuzunika na kuhudhuria kwenye maziko ya Imam Hasan Al Basr na hivyo katika siku hio kwa mara ya kwanza hakukua na Mtu hata mmoja katika wakati wa Sala ya Al Asr kwenye Msikiti wa Mkuu wa Basra kwani wote walikua wako mazikoni.

Na amesema Imam Hasan Al Basr kua: **'Ibn Adam anapofariki basi Ibn Adam wenzake huulizana juu ya Ibn Adam huyo aliefariki kwa kusema: 'Jee amewacha Nini?' ambapo kwa upande wa Malaika basi wao hua ni wenye kuulizana juu ya Ibn Adam huyo aliefariki kwa kusema kua: 'Jee ametanguliza nini''**

Alisema Imam Hasan Al Basr kua : **'*Allah Subhanah wa Ta'ala* hakumuwekea Mja wake Mipaka ya Kufanya Wema zaid ya Kifo kama alivyosema kwenye Qur'an:**

﴿وَٱعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ ٱلْيَقِينُ﴾

WaoAAbud rabbaka <u>h</u>att<u>a</u> ya/tiyaka alyaqeenu *(Surat Al Hijr 15:99)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: **Na Muabudu Mola wako Hadi itakapokufikia Yaqini (Kifo).**

Moja kati ya Hadith yenye upekee ambayo imo kwenye Sahih Bukhari ni ile ya Imam Hasan Al Basr ambayo amesema kua: **Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: *'Allah Subhanah wa Ta'ala* atamruhusu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuwaombea watu wa Motoni, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Kutokana na uwezo wangu, Na Ufalme wangu, Na Utukufu wangu na ukubwa wangu, basi mimi nitamtoa nje ya Moto kila Mtu aliesema *La Ilaha Illa Allah.''***

IMAM ABD RAHMAN IBN ABI LAILA 21 AH.

Imam Abu Isa Abd Rahman Ibn Abi Laila Yasar Ibn Bilal Ibn Uhaiha Ibn Al Jullah Al Ansari alizaliwa mnamo mwaka 21 Al Hijra mjini Kufa katika ardhi ya Iraq, miaka miwili kabla ya kufariki *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na kuna wasema kua alizaliwa mnamo mwaka 17 Al Hijra na pia wasemao kua mwaka 19 Al Hijra.

Imam Ibn Abi Laila alikua ni Mtoto wa Sahaba Ansar wa Madina ambae alikua akijulikana kwa jina la Yasar Abi Laila *Radhi Allahu Anhu* ambae ndie aliekua mbebaji wa Bendera ya *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* katika vita vya Ngamia.

Imam Abd Rahman Ibn Abi Laila alisoma kwa Mashaba 120 ambapo miongoni mwao ni pamoja na *Amir ul Muuminin* Uthmani Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu*, *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*, Abu Ayub Al Ansari *Radhi Allahu Anhu.* Abu Dhar Al Ghifari *Radhi Allahu Anhu.* Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu.nk*

Imam Ibn Abi Laila alisoma pia kutoka kwa Imam Abd Rahman Ash Shabi, Imam Mujahid Ibn Jabar. Imam Abd Al Malik Ibn Umar na wengineo. Hivyo Imam Ibn Abi Laila alikua ni mwenye Ilm kubwa ya Hadith Kiraa cha Qur'an na Fiqh, na alikua akiaminika sana na hivyo nae pia alisomesha Wanazuoni wengi akiwemo Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Hakam Ibn Utayba, Imam Yazid Ibn Abi Ziyad, Imam Husayn Ibn Abd Rahman na wengineo katika fani mbali mbali za Ilm ya Dini ya Kiislam.

Anasema Imam Muhamamd Ibn Sirrin kua: '**Mimi nilikua nimekaa na Abd Rahman Ibn Abi Laila, ambapo nikaona kua Wenzake wanavyomtukuza kwani alikua akichukuliwa kama mtoto wa Mfalme.'**

Anasema Imam Thabit Al Bunani kua: '**Tulipokua tukikaa pamoja na Abd Rahman Ibn Abi Laila kwa ajili ya kusoma kwake basi alikua akimwambia mmoja wetu: 'Soma Qur'an' na kisha baada hapo alikua akifafanua na kusema kua aya hii imeshushwa kwa sababu hii na hii, na aya hii imeshushwa kwa sababu hii na hii''**

Amesema Imam Abd Rahman Ibn Abi Layla kua: '**Siku moja kuna Yahudi ambae alikutana na Umari Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na kisha akasema: 'Yule Jibril ambae rafiki yenu *(Muhamamd Salallahu Alayhi wa Salam)* anamzungumzia mara kwa mara, basi sisi ni adui yetu: 'Hivyo Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Yeyote yule ambae ni Adui wa Allah na Malaika wake na Mitume wake, na Jibril na Mikail, basi kwa hakika Allah ni Adui wa Waliokufuru.' Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha aya inayodhibitisha maneno ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* isemayo:**

﴿قُلْ مَن كَانَ عَدُوّاً لِّجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَىٰ قَلْبِكَ بِإِذْنِ ٱللَّهِ مُصَدِّقاً لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَهُدًى وَبُشْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ۞مَن كَانَ عَدُوّاً لِّلَّهِ وَمَلآئِكَتِهِ وَرُسُلِهِ وَجِبْرِيلَ وَمِيكَالَ فَإِنَّ ٱللَّهَ عَدُوٌّ لِّلْكَافِرِينَ﴾

Qul man kana AAaduwwan lijibreela fa-innahu nazzalahu AAala qalbika bi-idhni Allahi musaddiqan lima bayna yadayhi wahudan wabushra lilmu/mineena; Man kana AAaduwwan lillahi wamala-ikatihi warusulihi wajibreela wameekala fa-inna Allaha AAaduwwun lilkafireena *(Surat Al Baqara 2:97-98)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad) Yeyote yule atakaekua Adui wa Jibril (Basi wacha afe kwa hasira zake) kwani kwa hakika yeye ndie alieishusha (Qur'an) Ndani ya Moyo wako kwa Idhini ya Allah, kuthibitisha vile vilivyokuja kabla yake (Zabur, Tawrat na Injil) na Uongofu na ubashirio mwema kwa Waumini. Hivyo yeyote yule atakaekua ni Adui wa Allah, na Malaika wake na Mitume wake, Jibril na Mikail basi kwa hakika Allah ni Adui wa Wasioamini.''''*** *(Al Ittiqan - Imam Al Suyuti)*

Ambapo anasema Imam Mujahid Ibn Jabr kua: '**Amesema Imam Abd Rahman Ibn Abi Laila kua: 'Amesema Ubayy Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* alikua yuko karibu na hodhi la Banu Ghifar pale Jibril**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

alipokuja kumwambia kua: ‘Allah anakuamrisha wewe kua watu wako wasome Qur’an kwa kisomo cha (ahruf) matamshi ya aina moja. Na baada ya hapo basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Namuomba mimi Allah anisamehe lakini watu wangu hawatoweza kufanya hivyo.

Hivyo Jibril akaja tena kwa mara ya pili, na akasema: ‘Allah anakuamrisha wewe kua watu wako wasome Qur’an kwa kisomo cha (ahruf) matamshi ya aina mbili. Na baada ya hapo basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Namuomba mimi Allah anisamehe lakini watu wangu hawatoweza kufanya hivyo.

Hivyo Jibril akaja tena kwa mara ya tatu, na akasema: ‘Allah anakuamrisha wewe kua watu wako wasome Qur’an kwa kisomo cha (ahruf) matamshi ya aina tatu. Na baada ya hapo basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Namuomba mimi Allah anisamehe lakini watu wangu hawatoweza kufanya hivyo.

Hivyo Jibril akaja tena kwa mara ya pili, na akasema: ‘Allah anakuamrisha wewe kua watu wako wasome Qur’an kwa kisomo cha (ahruf) matamshi ya aina nne. Na baada ya hapo basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Namuomba mimi Allah anisamehe lakini watu wangu hawatoweza kufanya hivyo.

Hivyo Jibril akaja tena kwa mara ya pili, na akasema: ‘Allah anakuamrisha wewe kua watu wako wasome Qur’an kwa kisomo cha (ahruf) matamshi ya aina saba, na katika kila kisomo cha harf watakachotamka watakua wako sahih. *(Sahih Muslim, Musannaf Ibn Abi Shaiba)*

Anasema Imam Abd Rahman Ibn Abi Layla kua: ‘Siku moja Masahaba walikua safarini pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na mmoja wao kati ya Masahaba akalala, na Sahaba mmoja akachukua kamba ya Sahaba alielala, na kumsababishia mwenzake huyo alielala usumbufu kwa kumkosesha utulivu pale alipoamka. Na hivyo akasema R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Haikubaliki kwa Muislam kumkosesha Utulivu Muislam mwenzake (hata kama ni kwa kumtania).’’*(Imam Abu Daud)*

Imam Abd Rahman Ibn Abi Laila amesema tena kua: **‘Aliniambia mimi Kaab Ibn Ujrah *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Jee unataka nikuzawadie kitu? Kwani sisi tulikua tukisema kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Ya Rasul Allah, sisi tunajua kuhusiana na kukusalimia wewe, lakini jee tunatakiwa tukutumie vipi sala zetu?’ Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: *‘Semeni Allahumma Salli 'ala Muhammad wa 'ala ali Muhammad, kama Sallaita 'ala Ibrahima wa barik 'ala Muhammad kama barakta 'ala ali Ibrahim fil-'alamin, innaka hamidun majid’’’(Imam An Nasai)***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na akasema Imam Thabit Al Bunani kua: '**Abd Rahman Ibn Abi Laila alikua akishamaliza kusali Sala ya Alfajir basi hua ni mwenye kuchukua Msahafu na kusoma hadi pale Jua linapochomoza'**

Zaid Ibn Qudamah amesema kua: **'Abd Rahman Ibn Abi Laila alikua ni mtu mwenye Ilm kubwa zaidi ya watu wote wa wakati wake.**'

Ambapo anasema Imam Abu Nuyam Al Isfahani kua: **'Wanafunzi wa Ilm ya Kisomo cha Qur'an walikua wakikusanyika kwenye Nyumba ya Ibn Abi Laila kwa ajili ya kujifunza Qur'an kutoka kwake.**'

Ambapo tunapozungumzia kuhusiana na Maktaba za Mwanzo katika historia ya Uislam basi ni Nyumba ya Imam Abd Rahman Ibn Laila, ambayo baadae ilifanywa kua ni Maktaba rasmin ya Mji wa Madina mnamo mwaka 85 Al Hijra.

Amesema Imam Mujahid Ibn Jabr kua: '**Abd Rahman Ibn Abi Laila alikua na nyumba ambayo ndani yake mlikua mna kopi za Qur'an ambazo zilikua zikisomwa na watu wanaotaka kusoma Qur'an, watu walikua wakiingia na kusoma Qur'an na walikua hawatoki ndani yake isipokua kwa ajili ya kuenda kula'**

Imam Abd Rahman Ibn Abi Laila alikua Anapenda kava za nje Misahafu hio siziwe kavu sana na wala zisiwe ngumu sana bali ziwe laini ili ziwavutie watu kua ni zenye kuwatia hamu ya kuishika na kuisoma Qur'an.

Na anasema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: '**Amesema Imam Abd Rahman Ibn Abi Laila kua: 'Mimi nimekutana na Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* 120, na hakuna hata mmoja miongoni mwao aliekua anataka kusomesha Hadith bila ya kutaka kua bora mwenzake awe ndie mwenye kuisomesha Hadithi husika.'**

Anasema Imam Abd Rahman Ibn Abi Laila kua: **'*Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alitutembelea sisi katika wakati wa Joto huku akiwa amevaa nguo za Baridi, na akatutemebelea katika siku za Baridi huku akiwa amevaa nguo za Joto. Akaomba maji ya kunywa kisha akanywa na kisha akajifuta jasho kutoka kwenye paji lake la uso.'**

Hivyo niliporudi nyumbani mimi nikamwambia Baba: 'Baba, Hivi hukumuona wewe *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alipotutembelea sisi katika wakati wa Joto huku akiwa amevaa nguo za Baridi, na akatutemebelea katika siku za Baridi huku akiwa amevaa nguo za Joto.' Ambapo Baba yagu

akasema: 'Kumbe hujafahamu twende zetu' na hivyo akanishika mkono hadi kwa *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na tulipofika basi Baba yangu akamwambia *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na niliyoyasema.

Ambapo *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akamuuliza Baba yangu: 'Jee hukuwepo wewe kwenye Vita vya Khaybar?'

Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu akasema: 'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua: 'Nitampa Bendera Mtu ambae anampenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake wanampenda yeye.*'

Na kisha akaniita mimi wakati nikiwa nnaumwa na Macho, hivyo nami nikasema kua: 'Macho yananiuma' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanitemea mate machoni na kisha akaniambia niyafumbue macho yangu. Nami nikayafungua na tangu sikuhio mimi sijaumwa na macho tena wala kua na matatizo yeyote nayo. Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaniombea dua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema: 'Ya Allah Mlinde Ali kutokana na madhara ya Joto na Baridi' na hivyo tangu siku hio basi mimi sikuwahi kuhisi Joto wala baridi.*'*

Na anasema Abdullah Ibn Al-Harith kua: **'Mimi nilikutana na Abd Rahman Ibn Abi Laila na sikudhania kua Wanawake watazaa mtu kama yeye'**

Imam Ibn Abi Laila alifariki mnamo mwaka 83 Al Hijra katika vita vya Jihad vya Dair Al Jamajim.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM JABIR IBN ZAID 22 AH

Ingawa Imam Jabir Ibn Zayd Al Azd alizaliwa mwaka 22 *Al Hijr* katika kijiji cha Farq, kilichopo baina ya mji wa Manna na mji wa Nizwa uliopo nchini Oman lakini asili ya Imam Jabir Ibn Zayd Al Azd, inatokana na katika kabila la watu wenye asili ya Yemen linalojulikana kama Al Azd. Katika karne ya 4 baada ya Nabii Isa *A'layhi Salaam* kabila hilo lilikua likiongozwa na Malik Ibn Fahm ambae aliliongoza kuelekea Mashariki katika maeneo ya mwambao wa *Bandar Sahar.*

Walipofika huko wakatawala maeneo hayo, na baadae wakutanua eneo la Mamlaka yao, na kuamua kulipa jina la '*Oman*'. Jina la Oman linatokana na eneo la ardhi

lililonyanyuka juu tofauti na maeneo mengine yaliyolizunguka eneo ambalo walikua wakiishi watu wa Al Azd wa *Ma'rib.*

Wakati bado Jabir akiwa mtoto mdogo wazee wake walihama kutoka Oman na kuhamia Iraq katika mji wa Basrah. Na hivyo Jabir Ibn Zayd alihifadhi *Qur'an* akiwa bado na umri mdogo kabla hata ya kujipatia elimu yake ya dini katika mji wa huo. Imam Jabir Ibn Zayd alikua katika Tabi'in, hivyo aliwahi kukutana na Masahaba zaidi ya 70 wakiwemo Masahaba wa mwanzo waliopigana katika vita vya Badr waliokua wakiishi Basra, Makkah na Madinah.

Imam Jabir Ibn Zayd alisoma *Hadith* na *I'lm* ya dini kutoka kwa Masahaba hao na alikua akipenda sana kuenda Makka na Madinah wakati wa Hija, inasemekana alienda kuhiji zaid ya mara 40. Huko alikutana na mke wa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* mama Aishah *Umm ul Mu'minin Radhi Allahu A'nha* ambae alimpa *I'lm* ya mambo mengi yanayohusu maisha ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, kuhusiana na Dini na mambo uongozi wa Kiiislam pia.

Imam Jabir Ibn Zayd alisomeshwa pia na Masahaba wenye *I'lm* zaid ya Uislam akiwemo A'bd Allah Ibn Masoud, A'bd Allah Ibn Umar, Anas Ibn Malik na Abd Allah Ibn 'Abbas *Radhi Allahu A'nhu* ambae ndie aliekua Mwalimu wake mkuu. Abd Allah Ibn 'Abbas *Radhi Allahu A'nhu* ambae alikua '*Bahr ul Ilm* ' Bahari ya *I'lm* aliridhika na *I'lm* aliyokua nayo Mwanafunzi wake Jabir Ibn Zayd na aliwahi kusema, **'Kama watu wa Basrah watamsikiliza Jabir Ibn Zayd pekee, basi atawapa *I'lm* kubwa iliyomo katika kitabu cha Allah *Subhanahu wa Ta'ala'*.**

Siku moja, anasema Al Rabí kua alipokua anaishi Basrah, alimuuliza Abd Allah Ibn 'Abbas *Radhi Allahu A'nhu* kuhusiana na mas-ála fulani ambapo, Abd Allah Ibn 'Abbas *Radhi Allahu A'nhu* akamjibu '**Kwa nini unaniuliza mie wakati unaishi pamoja na Jabir Ibn Zaid**'.

Imam Jabir Ibn Zayd alikua Mwanazuoni mkubwa sana, Maimamu wote wa *Hadith*, wanamuamini Imam Jabir Ibn Zayd kua ni mtu ambae *Hadith* zake ni sahihi, wanaomjua wanasema kua alikua mwingi wa *I'lm* kuliko hata Mwanazuoni Hasan Al Basr. Imam Jabir Ibn Zayd alikua Mufti Mkuu wa Basrah na alikua akitoa Fatwa katika mambo mbali mbali magumu na mepesi yanayohusu dini, kwani alikua ni mmoja kati ya wenye *I'lm* kubwa ya kutoa Fatwa.

Alijitolea maisha yake yote kusomesha dini na alikua na Wanafunzi wengi na pia alikua mcha mungu mkubwa alieishi maisha ya kawaida, kwani alikua akisema kua '**Nimemuomba Allah mambo matatu na amenineemesha yote: Mke mzuri na mcha Mungu, kipando kizuri (Farasi) na kipato halali na kitakacho nitosheleza kila siku**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

katika maisha yangu' na pia alikua akisema **'Hamna tajiri kuliko mie, kwani sina hata dirham moja mfukoni, lakini pia sina hata mtu mmoja ambae ananidai**'. Mwanachuoni Muhammad Ibn Sirrin alisema, '**Abu Shatha (Jabir Ibn Zayd) alikua ni mtu mwenye Taqwa.**'

Imam Jabir Ibn Zayd alikua haandiki Fatwa zake, lakini Wanafunzi wake walikua wakiziandika, na hivyo mwenyewe alikua akisema '***Inna lilah*, wanaandika ushauri ambao inawezekana kesho nikaubadilisha**'. Lakini hata hivyo baadhi ya Wanazuoni wa Ibadhi wanasema kua Imam Jabir Ibn Zayd aliandika kitabu kikubwa cha *Hadithi* na Fatwa ambacho kilikua kinaitwa '*Diwan Jabir Ibn Zayd*'.

Baadhi ya Wanazuoni wa Sunni wanasema kua Imam Jabir Ibn Zayd hakuwa na uhusiano na Maibadhi. Anasema Qatadah na Daud Hind kua amesema Azrah '**Nilimwambia Jabir kua Maibadhi wanasema wewe ni miongoni mwao**' naye akasema '**Nnajitangazia mbele ya Allah kua sio miongoni mwao**''.

Vilevile inasemekana kua Hind bin Al Muhallab amesema kua ijapokua Jabir alikua ni rafiki yake wa karibu na wa mama yake, alikua akiwaamrisha wafanye kila kitu ambacho kitawakaribisha kwa Allah lakini hakuwakaribisha katika Uibadhi.

Imam Ibn Hajar Asqalani ambae ni mfuasi wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i anasema kua amepokea kutoka kwa Al Dhuafa wa Al Salji ambae amesema kua Jabir Ibn Zayd alikua ni Ibadhi.

Imam Abu Hasan Al Ashari katika kuzungumzia Imani ya Khawarij anasema '**Ibadhi wanasema kua Imam Jabir Ibn Zayd ni kati ya Salafi (Watu wema waliotangulia)'** maneno ambayo Imam Al Hadid ameyasema pia.

Imam Al Rabi' Ibn Habib wa *Madhhab* ya Ibadhi (Mwanafunzi wa Imam Jabir Ibn Zayd), Al Salimi na Maimamu wa *Hadith* wa *Ahlu Sunnah wal Jamaa* akiwemo Imam Bukhari, Imam Ahmad Ibn Hanbal na Ibn Hibban wanasema kua Imam Jabir Ibn Zayd alifariki katika mwaka 93 *Al Hijr*.

Haijulikani nani alimtangulia mwenzie kufariki baina ya Imam Jabir Ibn Zayd na A'bd Allah Ibn Ibadh, kwani baada ya Imam Jabir Ibn Zayd kufariki alirithiwa na Mwanafunzi wake aliekua akiitwa Abu Ubaidah Muslim Ibn Abi Karimah Al Tamimi. Abu Ubaidah alisomeshwa pia na Masahaba kama Anas Ibn Malik, Abd Allah Ibn 'Abbas *Radhi Allahu A'nhu* na Abu Hurayra pia ingawa si kwa muda mrefu sana. Abu 'Ubaidah Muslim Ibn Abi Karimah alisema, '**Amepotea kila Mwanahadith ambaye hana Imam wa *Fiqh*, kwani kama Allah *Subhanahu wa Ta'ala* asingelitupendelea kwa kutupa Jabir Ibn Zayd basi nasi pia tungelipotea.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Abu Ubaidah alifanya jitihada kubwa ya kuwasomesha watu wengi kisirisiri ambao baadae walieneza misimamo ya Kiibadhi katika sehemu za Yemen ambapo Imam wa kwanza wa Hadhramawt alikua ni Imam Abd Allah Yahya Al Kindi ambae alichaguliwa kutoka Basra kwa Abu Ubaidah Muslim Ibn Abi Karimah na ilikua ni katika mwaka 129 A.H, na miaka mitano baadae katika mwaka 134 A.H akachaguliwa Imam wa pili ambae alikua ni Imam wa mwanzo wa Oman aliekua akiitwa Imam Julanda Ibn Masoud Al Ma'awaly na mnamo mwaka 140 A.H Imam Abu Al Khattab Abd A'la al Ma'afiri aliekua Mwanafunzi wa Abu Ubaidah mwenye asili ya Yemen ambae alikua ni Imam wa tatu kuchaguliwa na kua Imam wa kwanza wa Afrika Kaskazini. Miongoni mwa Wanafunzi wa Abu Ubaidah waliokua na *I'lm* ya juu alikuwa ni Al Rabi Ibn Habib Al Farahid mwenye asili ya Oman ambae alikua ndie kiongozi wa Jumuiya ya Ibadhi katika mji wa Basra.

Al Rabi' Ibn Habib alizikusanya *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ambazo zinatumiwa na *Madhhab* ya Ibadhi katika kitabu kinachoitwa *Al-Jami'i Al Sahih* ambacho pia hujulikana kama *Musnad Rabi' Ibn Habib* ambacho ndani yake mna *Hadith*i zilizopokelewa na Maimamu wa Ibadhi tu, ingawa kitabu cha Musnad Rabi' Ibn Habib cha asili hakitumiki sana siku hizi kwani badala yake kinatumika kitabu cha Abu Yaqub Yusuf Ibrahim Al-Warijlani kinachoitwa *Tartib Al Musnad* chenye *Hadith* 1005 ambazo ni mkusanyiko wa *Hadith* zilizokusanywa na Al Rabi' Ibn Habib na Abu Yaqub Yusuf.

Wafuasi wa *Madhhab* ya Ibadhi wanategemea sana *Hadith* zilizotoka kwa Imam Jabir Ibn Zayd ambae amenukuu *Hadith* kutoka kwa Masahaba wengi wakiwemo pia wale ambao alikua hakubaliani nao katika mitizamo ya kisiasa. Anasema Dr. Amr Khalfan Al Nami aliezaliwa katika eneo la *Nalut* liliopo Magharibi mwa nchi ya Libya ambae pia ni Mwanazuoni wa *Madhhab* ya Ibadhi na Mtafiti na Muuandishi kua,'**Kujitenga kwa Maibadhi, dhidi ya baadhi ya Masahaba kunahusiana na mambo ya Uongozi wa Kisiasa tu na hakukuhusiana juu ya *I'lm* yao ya Dini. Kwani hili linaonekana wazi pale tunapoona kua kuna kukubalika kwa Hukmu na Mitizamo ya Ali Ibn Abi Talib, Uthman Ibn Affan na wengineo wengi na hata huyo Muawwiyah ambae Maibadhi hawakukubaliana nae, basi alikua ni miongoni mwa Masahaba ambao Jabir ibn Zayd alizinukuu *Hadith* za *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* kutoka kwake.**'.*(Studies in Ibadhism)*

Hadith nyingi zilizokusanywa na Al Rabi' Ibn Habib pia zinapatikana katika vitabu vya *Hadith* vya *Madhhab* vya Ahl *Sunnah* wal Jamaah. Lakini hata hivyo kuna baadhi ya *Hadith* za *Madhhab* ya Ibadhi ambazo wafuasi wa Ahlu Sunna wal Jamaah au Sunni hua hawakubaliani nazo na wanasema ni za kutungwa (*mawdhu*'), kama ilivyokua kua kuna *Hadith* za Ahl *Sunnah* wa Jamaah ambazo wafuasi wa *Madhhab* ya Ibadhi hawakubaliani nazo kwa kusema kua ni za kuzusha (*bida'a*).

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ingawa wafuasi wa *Madhhab* ya Ibadhi wana msimamo wa kua wao ndio Waislamu halisi na *Fiqh* yao ndio *Fiqh* halisi inayowakilisha dini ya Kiislam na *Sunnah* zao ndio *Sunnah* sahihi kuliko za *Madhhab* mengine ya Kiislam kama vile alivyosema Imam Muhammad Yusuf Atfayyesh kua: '***Madhhab* yetu ni ukweli wenye uwezekano wa kukosea, na *Madhhab* ya wenzetu ni kukosea kwenye uwezekano wa kua kweli**'.

Lakini hata hivyo mtizamo huu hua ni moja kati ya sifa kuu inayochangiwa na wafuasi wa kila Madhhab yaliyomo katika Dini ya Kiislam – Kwani kila Wafuasi wa Madhhab husika iwe Ibadhi, Shia, Hanafi, Maliki, Shafi na Hanbal basi hua na mtizamo huo huo kua wao wana asilimia kubwa ya kua sahih na asilimia ndogo ya kutokua sahih, na wafuasi wa Madhhab mengineyo hua na asilimia kubwa ya kukosea na asilimia ndogo ya kua sahih.

IMAM URWA IBN AZ ZUBAYR 23 AH

Miongoni mwa Wanazuoni wakubwa wakuu wa Mji Wa Madina alikuwemo pia Imam Urwa Ibn Az Zubayr Ibn Awwam ambae alizaliwa mnamo mwaka 23 Al Hijra ambae ingawa alikulia katika kipindi cha Mvutano miongoni mwa Waislam uliopelekea kuuliwa kwa Amir Muuminin Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* na kupelekea kukosekana kwa utulivu katika Mji wa Madina.

Lakini hata hivyo mazingira hayakumzuia Urwa Ibn Az Zubayr kua ni mwenye kukosa kutafuta Ilm, kwani alijitahid na kua ni mwenye kusoma Qur'an, Hadith na Fiqh kiiasi ya kua alikua akisifika kutokana na kua na hali ya Bahari ya Ilm isiyokwisha Ndoo za maji mbali ya kuchotwa kwake kwa wingi.

Ambapo anasema Imam Said Ibn Musayyib kua: '**Urwa ni mtu mwenye Ilm kubwa ya Hadith**' na hii ni kwa sababu alisoma kutoka kwa Masahaba wakiwemo *Aisha Radhi Allahu Anha* ambae alikua ni mtoto wa Dada yake yaani Asma. Hivyo Imam Urwah Ibn Az Zubayr alikua pia ni mtaalamu mkubwa wa Fiqh na Mirathi.

Ambapo anasema Imam Urwa Ibn Az Zubayr mwenyewe kua: **'Kabla ya kufariki Aisha *Radhi Allahu Anha*, basi nilijiona kua mimi ni miongoni mwa watu wanne ambao ni wenye kuhifadhi hadithi kutoka kwake, hivyo nikasema kua: 'Kama akifariki basi hakutokua na Hadith itakayopotea kwani kwa hakika mimi nimezihifadhi hadith zake zote''**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Urwa Ibn Az Zubayr aliandika vitabu lakini baadae akaamua kuvichoma Moto kwa kukhofia kua huenda vikatumika sivyo, na kisha baadae akajuta na kusema: **'Bora ningekua na vitabu vyangu kuliko hata kua na Familia yangu na Mali maradufu niliyokua nayo.'**

Imam Urwah Ibn Az Zubayr alikua ni mtu ambae mwenye kuifanyia kazi Ilm yake kwa vitendo, kwani alikua ni mwenye kufunga katika siku za joto kali na ni mwenye kudumisha Qiyam Al Layl na kuudumisha Ulimi wake katika *Dhikr Allah.* Alikua ni mwenye kusoma Qur'an katika wakati wa mchana kutwa.

Safari moja Imam Urwa Ibn Az Zubayr alialikwa na Khalifa Al Walid Ibn Abd Malik wa Banu Umayyad kwenye Mji wa Dimashq na hivyo akafunga safari yeye na mtoto wake mkubwa wa kiume aitwae Muhammad, ambae alikua ni mwenye muonekano wa kuvutia na ni mwenye kupenda kuvaa kwa kupendeza.

Walipofika katika Mji wa Dimashq basi wakapokewa kwa Khalifa Al Walid ambae nae akasema alipomuona Muhamamd Ibn Urwah kwa namna anavyovutia muonekano wake wa utanashati kua: **'Naam hivi ndivyo anavyotakiwa kuonekana Kijana wa Quraysh.'**

Na hivyo jioni yake siku hio Imam Urwa akawa anaumwa na mguu ambao ulikua umevimba sana. Khalifa Al Walid akamletea Madaktari tofauti wa kumtibu lakini hata hivyo walishindwa na kusema kua tiba yake ni kua Mguu huo ukatwe kabisa kwani tatizo lake likiachiwa basi litaenea mwili mzima.

Imam Urwa Ibn Az Zubayr akakubaliana na rai hio, na Madaktari wakataka kua kabla ya kumkata basi wampe Imam Urwa dawa yenye kilevi kitakachomkatia Maumivu wakati wa ukatwaji wa mguu huo, lakini Imam Urwa akakataa na kusema: **'La siwezi kuruhusu hilo, kwani hua ni sawa na kuomba msaada kwa kutumia kitu cha Haram ambacho kitanipelekea kua ni mwenye kuomba msamaha wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Hivyo Madaktari hao wakamwambia Imam Urwa kua watampa dawa ya kuondoa Maumivu, lakini Imam Urwa akasema: **'Hakika mimi sitaki kuondolewa sehemu ya kiungo cha mwili wangu bila ya kuhisi maumivu ambayo yatanipelekea kua ni mwenye kulipwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana nayo.'**

Hivyo Madaktari wakakubaliana kua watamkata mguu bila dawa ya ganzi, na wakawaita watu ili waje kumzuia Imam Urwa Ibn Az Zubary ili asije akaleta fujo kwa maumivu, lakini Imam Urwa Ibn Az Zubayr alipowaona watu hao basi akauliza kwa kusema: **'Watu wote hawa ni wa nini?'** na alipoambiwa sababu ya kuwepo kwao basi akajibu: **'La warudisheni, kwani mimi sina haja ya kuzuiliwa kwa sababu namtemegea**

***Allah Subhanah wa Ta'ala* na kutokana na kumkumbuka kwangu kwake basi nategemea kua Dhikr Allah zangu zitanisaidia katika tukio hili'**

Hivyo watu hao wakaondolewa na kisha kazi ya kukatwa mguu wa Imam Urwa Ibn Az Zubayr ikaanza kwa kukatwa Nyama ya mguu huo kwa kisu cha upasuaji na kisha kuchukuliwa msumeno kwa ajili ya kuukata Mfupa wa mguu huo, ambapo kwa upande wa anaefanyiwa upasuaji huo yaani Imam Urwa Ibn Az Zubayr alikua katulia na hakuna sauti inayosikika kutoka kwenye Mdomo wake isipokua maneno yasemayo: ***'La Ilaha Illa Allah w Allahu Akbar.'***

Na kisha baada ya kumalizwa kukatwa kwa mguu huo basi yakachukuliwa mafuta yamoto na kumwagiwa kwenye jeraha la mguu wake huo kwa ajili ya kusitisha umwagikaji wa damu wa mguu huo, ambapo tukio hili lilimpelekea Imam Urwa Ibn Az Zubayr kupoteza fahamu na kisha kuja kuzindukana masaa baadae.

Ambapo baada ya kuzindukana kwake basi akaomba aletewe sehemu ya mguu wake uliokatwa, na alipopewa basi akaubusu na kisha akautizama na kusema: **'Naapa kwa alienipa kiungo wewe, kua mimi sikukutumia kwa kutembelea kuelekea kwenye sehemu ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakutaka niende hata mara moja.'** Na kisha akaamrisha kua mguu huo ukoshwe, utiwe manukato na kuvishwa sanda na kisha ukazikwe Makaburini, na baada ya hapo ikaanza safari ya kurudi kwake katika Mji wa Madina kwa kubebwa.

Imam Urwa Ibn Az Zubayr alipofika katika Mji wa Madina akawaambia watu waliokuja kumpokea kwa kusema kua: **'Msishtuke kwa mnachokiona kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amenijaaliwa watoto wanne wa Kiume na amemchukua mmoja na kunibakishia watatu, hivyo utukufu na shukrani zote ni zake, kwani pia amenipa viungo vinne na amechukua kimoja na kuniruhusu kubwakiwa na vitavu hivyo pia shukrani zote ni zake *Allah Subhanah wa Ta'ala, Wa Allahi* naapa kua kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* amechukua kidogo kwangu mie basi bado ameniwachia na kingi na kama amenijaribu kwa mara moja basi amenisamehe mara nyingi'**

Watu wakampa pole Imam Urwa Ibn Az Zubayr, na miongoni mwao ni Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Talha ambae alimwambia kwa kusema: '**Pokea habari njema ewe Abu Abd Allah, kwani mmoja kati ya Mtoto wako na mmoja kati ya miguu yako imeshatangulia Peponi, na nyuma ya hivyo vilivyotangulia basi vitafuata vile vilivyobakia *In-shaa Allah.* Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameruhusu kubakia kutoka kwako vile ambavyo tunavihitaji na kile ambacho hatuwezi bila kua nacho, ambayo ni Ilm yako na mitizamo ya ufahamu wako basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutunufaisha nacho.**'

IMAM ATAA IBN ABI RABAH 25 AH

Imam Abu Muhammad 'Ata' Ibn Abi Rabah Al Makki Al Qurayshi alizaliwa katika mwaka 25 Al Hijra katika ardhi ya Yemen na kisha familia yake ikahamia katika Mji wa Makkah wakati yeye akiwa bado mdogo. Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua ni Mtu mweusi ambae ni Mtumwa wa Ibn Khaytham Al Qurashi ambae baadae aliemuachia huru na alikua ni mwenye kujipatia Ilm yake kutoka kwa Masahaba wakiwemo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu, Umm ul Muuminin* Aisha Radhi *Allahu Anha* na wengineo.

Hivyo Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua ni miongoni mwa Ataa wanazuoni wakubwa wa kipindi cha Tabiina ambapo wiongoni mwao alikuwemo pia Imam Ataa Al Khurasani, Imam Ataa Ibn Yasir, Imam Ataa Ibn Sulayman na Imam Ataa Ibn Saib, ambapo tunapozungumzia kuhusiana na Imam Ataa Ibn Abi Rabah basi hua tunazungumzia Imam ambae yuko juu zaidi kwa Ilm miongoni mwa Ataa Wanazuoni.

Anasema Imam Muhammad Ibn Abd Allah Ad Dibaj kua: '**Hakika mimi sijawahi kuona Mufti aliekua ni bora zaid ya Ataa Ibn Abi Rabah**' kwani Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua anaposomesha Darsa basi Darsa yake ilikua ni yenye kua na Nuru ya Dhikr Allah na anapoulizwa suali na akatoa Fatwa basi hua anatoa kwa ufafanuzi wa kina kwani alikua na Ilm kubwa ya Fiqh, Quran, Tafsir na Hadith.

Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Ibada ya Hija, kiasi ya kua katika wakati wa Uhai wake ambao ulikua ni wakati wa Utawala wa Banu Ummayah, basi kila inapofika Ibada ya Hija mji wa Makkah hua ni wenye kutangaziwa kua: **'Hairuhusiki kwa Mtu yeyote kutoa Fatwa kuhusiana na Ibada ya Hija isipokua Imam Ataa Ibn Abi Rabah, na kama sio yeye basi anaeruhusika baada yake ni Abd Ibn Abi Najih**'

Safari moja Imam Nu'man Ibn Thabit Abu Hanifa alienda katika Mji wa Makkah katika kipindi cha Ibada ya Hija na kisha akaingia kwa mmoja kati ya Vinyozi wa Mji huo, ambapo baada ya kusalimia na kabla ya kukaa kwenye kiti basi akataka kupatana bei kabla ya kukatwa Nywele zake, lakini Kinyozi akamwambia Imam Abu Hanifa: '**Katika Ibada hua hamna Masharti ya Mapatano**'

Baada ya hapo Imam Abu Hanifa akakaa kwenye kiti kilichokua kinaipa mgongo Al Kaabah, hivyo Kinyozi huyo akamgeuzia Imam Abu Hanifa katika Upande wa Kibla, na kisha Kinyozi huyo akaanza kumkata kwa kuanzia kwenye upande wa kulia wa kichwa chake, na huku Kinyozi akamwambia Imam Abu Hanifa kua anatakiwa awe anafanya Takbir katika kukaa kwake huku akinyolewa Nywele zake, baada ya kumaliza

kunyolewa basi Kinyozi akamwambia Imam Abu Hanifa kua asali rakaa mbili kisha za Sunna na kisha ndio aondoke, hivyo Imam Abu Hanifa ikambidi aulize: ‘**Umeipata wapi Ilm hii ewe Kinyozi?’** Kinyozi akajibu: ‘**Hakika mimi nilimuona Imam Ataa Ibn Abi Rabah akifanya hivyo nilivyokuambia**.’

Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua ni Mcha Mungu sana, ambapo anasema Imam Ibn Jurayj kua: ‘**Imam Ataa Ibn Abi Rabah aliigeuza sakafu ya Msikitini kua ni kitanda chake kwa muda wa miaka 20’**

Na akasema Imam Nu’man Ibn Thabit Abu Hanifa kua: **‘Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu aliekua juu Kiilm kama Ataa Ibn Abi Rabah.’**

Ingawa Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua ni Mwanafunzi wa Masahaba lakini hakua ni miongoni mwa waliosoma moja kwa moja kutoka kwa baadhi yao mbali ya kua anazo hadithi kutoka kwa Masahaba hao ambazo hua ni *Mursal Hadith* yaani Hadithi ambayo imeharakishwa na kukosekana kwa kiunganishi baina ya Tabiina na Sahaba kwa mfano hadith zake kutoka kwa Abu Sa’īd al-Khudrī, Zayd Ibn Khālid, Umm Salamah, Umm Hāni, Umm Kurz, Rāfi’Ibn Khadīj, Usāmah, Jubayr Ibn Mu’tam, Abu Ad Darda na Fadhal Ibn ‘Abbās *Radhi Allahu Anhum.* Na hivyo basi Imam Ahmad Ibn Hanbal hakua ni mwenye kuzipa kipaumbele sana *Mursal Hadith* za Imam Ataa Ibn Abi Rabah kwa sababu alikua hadharau hadith yeyote.

Ambapo Umar Ibn Said amesema kua: ‘**Mama yangu alilala kisha akamuota *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* usingizini akimwambia kua: ‘Ataa Ibn Abi Rabah ni *Sayyid Ul Muslimin***’’

Anasema Muhammad Ibn Abd Allah kua: ‘**Sikuwahi mimi kuona Mtu anaetafuta radhi za *Allah Subhanah wa Ta’ala* kupitia katika njia ya kutafuta Ilm’**

Ambapo anasema Mtoto wa Imam Ataa Al Khurasan aitwae Uthman Ibn Ata Al Khurasani kua: ‘**Mimi na Baba yangu tulikua tunaelekea kwa Khalifa Hisham Ibn Abd Ul Malik, na tulipokaribia mji wa Dimashq basi tukamuona Mtu Mzee Mweusi akiwa juu ya Punda wake huku akiwa amevaa nguo zilizochakaa na Joho lililochoka huku akiwa amevaa Kofia ambayo imetoboka pia, kiasi ya kua kwangu mie ilikua ni vichekesho, hivyo nikacheka, na Baba yangu akanigombeza kwa kusema: ‘Unamjua nani huyu? Huyu ni Ataa Ibn Abi Rabah ndie Qadhi Mkuu wa Hijaz’**

Kisha baba yangu akashuka kutoka kwenye Punda wake na Imam Ataa akashuka kutoka kwenye Punda wake na wakasalimiana kwa kukumbatiana, na kisha wakapanda Punda wao na kuelekea kwenye Mlango wa Khalifa Hisham’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kisha Imam Ataa Al Khurasani akamuelezea Mtoto wake yaliyotokea walipofika mbele ya Khalifa Hisham kwa kusema: '**Mara tu baada ya Hisham kujua kuhusiana na kuwasili kwa Ataa Ibn Abi Rabah basi akaturuhusu sisi kuingia na kukutana nae, na Wa Allahi mimi nimepata bahati ya kukutana nae kwa sababu ya Ataa, hivyo Khalifa Hisham akampokea na kumruhusu kukaa pembeni yake kwenye kiti chake na kisha akamuuliza: 'Nikusaidie nini ya Abu Muhammad?'**

Ambapo Ataa akataka kua Mishahara ya Watu wa Haram, Madina na maeneo ya baina yake yanayojulikana kama Thaghar, walipwe kwa wakati na hapo hapo Khalifa Hisham akaamrisha wafanyakazi wake walipwe na waonewe huruma. Na kisha baada ya hapo akainama na kumuuliza Ataa: 'Kuna zaidi ewe Abu Muhammad?'

Imam Ataa Ibn Abi Rabah akasema: 'Ewe *Amir Ul Muuminin* Muogope Mola wako kwa ajili ya Nafsi yako, fahamu kua ulizaliwa peke yako na utafariki peke yako na isha utafufuliwa peke yako na utahesabiwa peke yako kwani wote hawa unaowaona karibu yako hawatokua pamoja nawe' na hapo hapo Khalifa Hisham akaanguka chini huku akiwa analia, ambapo Ataa akaondoka bila ya hata kumuangalia, nami nikafuatana nae, na tulipofika Mlangoni basi mmoja kati ya Watu wake wakatuletea bahasha kutoka kwa Khalifa Hisham lakini hata hivyo Ataa akakataa kuipokea na kusema:

﴿وَمَآ أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِنْ أَجْرِىَ إِلاَّ عَلَىٰ رَبِّ ٱلْعَالَمِينَ﴾

Wam<u>a</u> as-alukum AAalayhi min ajrin in ajriya ill<u>a</u> AAal<u>a</u> rabbi alAA<u>a</u>lameena *(Surat Ash Shuara 26:109)*

Tafsir: ***Nami Sikudaini juu yake kutokana nao Ujira kwani malipo yangu ni kutoka kwa Mola wa Ulimwengu tu.***

Wa Allahi nnaapa mimi kua aliingia ndani na kutoka, lakini hakuchukua kitu chochote hata tone la Maji'

Kutokana na ukubwa Ilm yake basi Mitazamo yake Imam Ataa Ibn Abi Rabah ilikua ikifuatwa na watu wote katika eneo lake lakini yeye mwenyewe alikua ni mwenye kusema kua: '**Hakika mimi nnaona haya mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'al*a kua Mitizamo yangu iwe ni yenye kufuatwa kwenye Ardhi yake**'

Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua ni mwenye kusoma aya 200 na zaidi katika kila wakati anapokua anasali *Salat Tahajjud*, na alikua akipenda kukaa kimya sana pale anapokua

amekaa pamoja na watu na anapozungumza basi wale waliomzunguka hua kama walioshushiwa mwamko juu yao.

Anasema Imam Ataa Ibn Abi Rabah kua: '**Mtu anaponihadithia Hadith mimi hua ni mwenye kusikiliza kama kwamba sijawahi kuisikia Hadith hio, ingawa nimeshawahi kuisikia hadith hio kabla ya kuzaliwa kwake mtu huyo.**'

Imam Ataa Ibn Abi Rabah alimuusia Mtoto wa Kaka yake kwa kumwambia: **'Ewe Mtoto wa Kaka yangu, wale waliotangulia kabla yako hawakua ni wenye kupenda maneno matupu yasiyonufaisha hapa Duniani wala Akhera, bali walikua wakisoma Qur'an, wakiamrishana mema, wakikatazana mabaya walikua wakisoma Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kuzifanyia kazi kwa vitendo na huzungumza pale inapostahiki tu.'**

Imam Ataa Ibn Abi Rabah alisema: **'Yeyote yule anaehudhuria baraza anayotajwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hujaalia kuhudhuria kwake hapo kua ni mwenye kumfutia madhambi ya baraza 10 za mambo maovu alizohudhuria, na kama mtu huyo atakua ni mwenye kuomba dua katika baraza hio, basi tendo hilo litampelekea kua ni mwenye kufutiwa madhambi ya vikao 100 alivyokua amekaa hapo kabla vya madhambi'**

Khalifa Abd Al Malik Ibn Marwan alipoedna katika Mjiwa Makkah kwa ajili ya Ibada ya Hija basi aliomba kukutana na Imam Ataa Ibn Abi Rabah, na hivyo Imam Ataa Ibn Abi Rabah akaingia kwenye Majlis ya Khalifa Abd Ul Malik ambae nae ingawa alikua emkaa pamoja na watu wake, lakin baada ya kumuona tu Imam Ataa Ibn Abi Rabah basi akanyanyuka na kumsalimia Imam Ataa Ibn Abi Rabah na kisha akauchukua mkono wake na kumuashiria kua akae kitako pembeni yake, ambapo baada ya kukaa Khalifa Abd Al Malik akamuomba Imam Ataa Ibbn Abi Rabah amuusie.

Hivyo Imam Ataa Ibn Abi Rabah akasema: '**Ewe *Amir ul Muuminin*, Muongope *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kuusimamia na kuyafanyia matengenezo majengo ya Masjid Haram na Masjid An Nabawi, na yape umuhimu mkubwa sana mambo mawili haya'**

Khalifa Abd Al Malik akasema: '**Shukrani nitajitahid kuyapa kipaumbele haya uliyoniambia.**'

Ambapo Imam Ataa Ibn Abi Rabah akaendelea kwa kusema: '**Vile vile wasimamie watoto wa Jamaa zako pia, usiwadhuru kwani wewe umeingia Madarakani kupitia kwao wao, simamia haki za wale waliokua chini yako, *Muogope Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na Waislam waliokua mipakani mwa ardhi yako wakilinda**

usalama dhidi ya maadui zako, kwani wao ndio ngao ya Waislam dhidi ya maadui zao, wasimamie mahitaji yao na usiwasahau'

'Halafu vile vile fuatilia matatizo ya Waislam waliokua chini yako, kwa sababu hilo ndio jukumu lako, Muogope *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na wale waliokua chini ya usimamizi wako ambao wako kwenye milango yako, bila ya kujali hali zao, ifunge milango yako lakini usiwafungie milango na kuwaacha peke yao'

Kisha Imam Ataa Ibn Abi Rabah akanyanyuka na kutaka kuondoka, hivyo Khalif Abd Ul Malik akasema: **'Shukran nitasimamia hayo pia, lakini mbona unataka kuondoka huku ukiwa umezungumzia kuhusiana na wenzako bila ya kuzungumzia kuhusiana na Nafsi yako? Jee huhitaji kitu chochote?'**

Imam Ataa Ibn Abi Rabah akasema: **'Usiwe na wasi wasi kwani mimi ninapokua na mahitaji hua namuomba yule ambae ni mwenye Mamlaka ya umiliki wa kila kitu, hivyo hapa mimi nimekukumbusha kuhusiana na Mahitaji ya Waislam waliokua chini yako tu'**

Khalifa Abd Al Malik Ibn Marwan akasema: **'*Ma-shaa Allah* hii ndio Heshima na Utukufu, kwani hii ndio hali ambayo inakupandisha wewe darja.'**

Alisema Abu Asim Ath Thaqafi kua : **'Abu Jafar kua alisema: 'Shikamaneni na Ataa Ibn Abi Rabah vizuri sana ili mpate kunufaika nae.'**

Imam Ataa Ibn Abi Rabah alisema: **'Amesema Zayd Ibn Khalid *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua: 'Mtu yeyote yule atakaemsaidia kimahitaji *Mujahid* anaeenda vitani *fi Sabili Allah* au akaisaidia Familia yake na kuisimamia hadi *Mujahid* huyo akarudi basi Mtu huyo hua ni mwenye kulipwa malipo sawa na *Mujahid* huyo, na wala si chini ya malipo ya *Mujahid* huyo, na Mtu atakae msaidia kimahitaji Hujaji anaeenda kuhiji Makkah au akasimamia familia ya Hujaji huyo kimahitaji hadi akarudi basi hua ni mwenye kulipwa malipo sawia ya Hujaj huyo na si chini ya malipo yake, na mtu atakaempa Iftar Mtu aliefunga basi nae atalipwa malipo sawa na Mtu huyo aliefunga.'''**

Alisema Imam Ataa Ibn Rabbah kua: **'Amesema Abu Darda *Radhi Allahu Anhu*, kua 'Mimi nilikua natembea mbele ya Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* ambapo *Rasul Alah Salallahu Alayhi wa Salam* akaniona na hivyo akasema: 'Unatembea mbele ya Abu Bakr? Hakika Jua halijawahi kuchomoza wala kutua juu ya Mtu kama Abu Bakr baada ya Mitume na Manabii.'''**

Amesema Ataa Ibn Abi Rabah kua: **'Amesema Abd Allah Ibn Umar: 'Alikuja mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mtu mwenye asili ya Uhabeshi na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Uliza unalotaka kuuliza' ambapo nae akasema: 'Ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, hakika wewe umefadhilishwa juu yetu kwa uzuri wa maumbile yako na rangi yako na kua na Utume wako. Hivyo jee kama mimi nikikuamini wewe na kisha nikafanya uliyoniamrisha nitaingia Peponi pamoja nawe?'**

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, akasema: 'Naam' kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, akasema: 'Kwa yeyote yule atakaesema *La Ilaha Illa Allah*, basi kuna Ahadi mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na maneno hayo matukufu. Na yeyote yule atakaesema *Subhanah Allah wa Bihamdihi* basi hua ni mwenye kuandikiwa malipo ya kua ni mwenye kufanya Mema 124000, kwa ajili yake''

Imam Ataa Ibn Abi Rabbah anasema tena kua: '**Amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, katika siku ya Malipo, kutakua kuna watu wa aina tatu ambao watakua juu kwenye Milima ya Miski, watatu hawa hawatokua na Khofu pale watu watakapokua na Khofu, ambapo wa Kwanza ni yule ambae atakua ni Imam kutokana na kuismoa Qur'an Al Karim huku akiwa ni mwenye kufikiria Ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Malipo atakayoyapata kutoka kwake. Wa Pili ni yule ambae Atakaekua ni Muadhini na kuwaita Watu kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'al*a mara Tano kwa Siku, na wa Tatu ni yule ambae alikua ni Mtumwa, lakini Utumwa wake huo haukumzuia yeye kutokana na Kumuabudu Mola wake.''**

Akasema tena Imam Ataa Ibn Abi Rabah kua: **'Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Sisi tulimuuliza *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam*: 'Hivi Jee ni kipi kisomo cha Qur'an kilichokua Bora zaidi?' *Rasul Allah Salallahu Aalyhi wa Salam* akasema: 'Ni Kile Kisomo cha Mtu ambae anaposoma basi unamhisi kua ni mtu mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'''**

Imam Ataa Ibn Abi Rabah alisema kua: **'Muislam yeyote yule anaehudhuria mhadhara ambao *Allah Subhnah wa Ta'ala* anatajwa basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hujaalia mhudhurio wake huo kua ni wenye kumfutia madhambi ya mihudhurio yake 10 ya Maovu, na kama Muislam huyo ataomba ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kuwepo kwake kwenye mhadhara huo basi kitendo hicho kitakua ni chenye kujaaliwa kumfutia yeye mtu huyo madhambi ya mihadhara 700 ya maovu aliyohudhuria hapo kabla'**

Ambapo anasema Imam Al Awzai kua: **'Imam Ataa Ibn Abi Rabah alifariki mnamo mwaka 114 Al Hijra katika ardhi ya Makkah na alikua akipendwa sana na Watu.'**

IMAM AD DAHHAK IBN MUZAHIM 25 AH

Imam Abu Qasim Dahhak Ibn Muzahim Al Hilali alizaliwa katika Mji wa Balkh katika ardhi ya Samarqand akiwa na ndugu zake wawili ambao ni Muhamad na Muslim, Imam Ad Dahhak aliishi katika Mji wa Balkh na kujipatia Ilm yake kutoka kwa Wanazuoni wa Mji huo ambapo baadae akaamua kufunga safari kujiongezea Ilm katika maeneo ya Mji wa Bukhara.

Alisema Ibn Habib kua: '**Ad Dahhak Ibn Muzahim ni Mwenye kuheshimika kwa Ilm kubwa sana na ni Mwalimu wa Wanafiqh.'**

Ingawa Imam Ad Dahhak alikua pia na Ilm ya Hadith ambazo nyingi miongoni mwao zimo kwenye kitabu cha Sunan Abu Daud na Jamii At Tirmidhii na ingawa kuna Maimamu waliosema kua hadith za Imam Ad Dahhak ni Munkar na Dhaif akiwemo Imam Yahya Ibn Said na hii ni kutokana na kua Hadith zake zina kasoro ya Irsaal yaani ya kutomtaja Sahaba ndani yake aliepokea Hadithi husika na pia kasoro ya Tadlis ambayo hua ni ya kukiuka au kuwaruka walionukuu Hadith, jambo ambalo hua halikubaliki na baadhi katika fani ya Ilm ya Hadith.

Ambapo hii ni sifa ambayo pia wanayo baadhi ya Wanazuoni katika baadhi ya Hadith kwa mfano akiwemo Imam Al Amash, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Malik, Imam Ibn Is-haq, Imam Ibn Jurayj, Imam Al Ghazali, Imam Al Wasiti n.k

Na hivyo basi hii haiwezi kumfanya Imam husika kutoaminika kutokana na kasoro hio, na ndio maana kwa upande mwengine basi tunaona kua Imam Ad Dahhak ametajwa pia kua ni Imam mwenye kuaminika wa Hadith na Wanazuoni wakiwemo Imam Yahya Ibn Main, Imam Abu Zura Al Razi, Imam Daraqutni, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Bukhari na pia na Imam Ibn Hajar Al Asqalani.

Na ndio maana akasema Imam Adh Dhahabi kua: '**Abu Qasim ni Muandishi wa Tafsir ya Qur'an ambae ni chombo kilichoshehena Ilm, na ingawa alikua hana sifa bora ya Ilm ya Hadith lakini yeye mwenyewe ni mwenye kuaminika.'**

Katika Hadith zake basi Imam Ad Dahhak amenukuu hadith za Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas, Abu Sa'id Al Khudry, Abd Allah Ibn Umar, Anas Ibn Malik, Sa'id Ibn Jubayr, 'Ata' Ibn Abi Rabah, Tawwus *Radhi Allahu Anhum.*

Tukiachana na Ilm ya Hadith basi tunapomuangalia Imam Ad Dahhak kwa upande mwengine basi tunaona kua alikua ni Imam ambae amezama zaidi katika Ilm ya Tafsir

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ya Qur'an na ni mwenye Ilm kubwa zaidi ya Tafsir, kwani hio ndio fani ya Ilm iliyokua ikimvutia zaidi kiasi ya kua alikua ni mwenye kua na Wanafunzi wa kiume wafikao 3000 na wa kike walikua 700 ambao wote alikua akiwasomesha Qur'an, na hata Tafsir za Imam At Tabari na Imam Al Baghawi zimetokana na Tafsir ya Imam Ad Dahhak.

Kwani Imam Ad Dahhak alisoma katika ardhi ya Ray wakati Imam Said Ibn Jubayr alipotembelea maeneo hayo na hivyo kujipatia Ilm ya Tafsir ya Qur'an kutoka kwa *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kupitia kwa kwa Imam Said Ibn Jubayr. Na ndio maana hata Imam Sufyan Ath Thawry aliusia kwa kusema kua: '**Fuata Tafsir kutoka kwa watu wanne ambao ni Said Ibn Jubayr, Mujahid Ibn Jabr, Ikrimah Mawla Ibn Abbas na Ad Dahhak Ibn Muzahim.'**

Ambapo ni Imam Ad Dahhak ni miongoni mwa watu wa mwanzo kubainisha kua: '**Aya zilizoanzia na *Ya Ayyuha Nnasu* ni aya zilizoshuka Katika Mji wa Makkah na aya zilizoanza na *Ya Ayyuha Aladhina Amanuu* ni Aya zilizoshuka katika Mji wa Madina**'

Ama kwa upande mwengine basi kuna Maimamu wasemao kua Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim aliwahi pia kuishi jirani na *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akiwemo Imam Ibn Hajar Al Asqalani katika *Tahdhiib Al-Tahdhiib* na pia Imam Al Janabi Al Kalbi.

Ambapo anasema Imam Al Ajlah kua: **'Imam Ad Dahhak alikua akipenda kusema kua: 'Tafuta Ilm wakati unaweza kuitafuta Ilm''** kwani Imam Ad Dahhak ilikua kila siku ni mwenye kujihesabia na hivyo siku yake inapomalizika basi alikua ni mwenye kulia kwa kusema: **'Sijui mema yangu mangapi kati ya yaliyopanda juu leo yamekubaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**

Usiku mmoja wa siku ya Ijumaa, Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim aliondoka nyumbani kwake na kuelekea Msikitini na alipofika akakutana na kijana ambae alikua akisali na katika kusjudu kwake, basi kijana huyo alikua akiomba Dua kwa kusema:

'Ya Allah Hakika wewe ni mwenye Ufalme juu ya kila kitu nami nakuamini, ama kwa hakika amefarajika yule ambae ni mwenye kukutegemea wewe, na ni mwenye kukuogopa, na hivyo anawakilisha matatizo yake kwako, kwani ameshughulishwa na mapenzi yako, anapokua kizani hua yuko peke yake hivyo hua anakubaliwa katika kukuomba kwake, ewe Mola wangu hakika mimi nakuamini sana.'

Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim aliposikia Dua hio akaanza kulia na kisha akamuuliza kijana huyo baada ya kusali kwa kusema: **'Allah akuingize kwenye Rehma zake, hivi unaitwa nani mwenzangu?' kijana kajibu: 'Mimi naitwa Rashid Ibn Sulayman'**

Imam Ad Dahhak: **'Hivi jee unaweza kubakia nasi kwa mda kidogo?'** ambapo Rashid akasema: **'Ni vigumu sana kuwezekana hivyo kutokana na raha inayopatikana pale unapokua karibu na Mola wa Ulimwengu na Viumbe wote, hivyo jee inawezekana kua karibu na viumbe huku ukiwa ni mwenye karibu na Muumba?'** kisha kijana huyo akaondoka.

Imam Ad Dahhak akatoka kumfuata kijana huyo lakini hakumuona tena, hivyo akamuomba ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** kua amjaalie kukutana nae tena kijana huyo kabla ya kufariki kwake. Na baada ya mda mrefu kupita safari moja Imam Ad Dahhak alipokua kwenye Ibada ya Hija katika maeneo ya pembeni ya Al Kaabah akamkuta Rashid Ibn Sulayman akiwa amekaa kitako huku kuna watu wanasoma *Surat al Anaam* wakiwa wamemzunguka mbele yake.

Imam Ad Dahhak akakaribia karibu na Rashid Ibn Sulayman alipomuona basi akasimama na kumsalimia Imam Ad Dahhak na kisha akamkumbatia, na kisha Rashid Ibn Sulayman akamuuliza Imam Ad Dahhak: **'Hivi Jee hukumuomba wewe *Allah Subhana wa Ta'ala* kua atukutanishe kabla ya kufariki kwako?'** Imam Ad Dahhak akajibu: **'Naam! Ila niambie ilikuaje mpaka ukajua kuhusiana na Dua yangu hio niliyoiomba?'**

Na baada ya kuulizwa suali hilo basi Rashid Ibn Sulayman akatokezewa na hali ambayo ilikua si ya kawaida na kisha akaanguka na kupoteza fahamu, na kisha alipozindukana basi akasema: '**Ya Akhi, *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakukutanisha pamoja Peponi, na hakutokua na kutengana wala huzuni baina yetu' na kisha kijana huyo akatoweka tena, na Imam Ad Dahhak hakuweza kumuona tena kijana huyo.**

Alisema Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim kua: **'Hakika mimi nimeonana na Wanazuoni wa Akhera, ambapo wao walikua ni wenye kufunza kua na Taqwa, Wara, Halal na Haram na vitu vyenye kushabihiana walikua wakiachana navyo, ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa leo basi wao hua ni wenye kujishughulisha na *Ilm al Kalam.*'**

Ambapo Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim amesema kuhusiana na aya ifuatayo:

﴿أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ ٱلْقُرْآنَ تَرْتِيلاً﴾

Aw zid AAalayhi warattili alqur-a̲na tarteela̲n *(Surat Al Muzamil 73:4)*

Tafsir: ***Au zidisha juu yake kidogo na Usome Qur'ani kwa Mtiririko wake.***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kua inamaanisha Soma Qur'an kwa taratibu kwa mtiririko wa herufi moja baada ya moja kua ni yenye kusikikana wazi wazi.

Kwani Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim alikua akisoma Qur'an na kurudia mara aya moja mara kadhaa hadi kua ni mwenye kufahamu ipasavyo, kwa sababu alikua akisema kua: **'Motoni kuna matabaka tofauti moja juu ya jengine, na hivyo ndivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anavyowatia khofu Waja wake kuwaambia Enyi waja wangu niogopeni, niogopeni.'**

Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim alisema kua: **'Kama mtu akifariki huku akiwa katika hali ya kua ni mwenye kuendelea kunywa Ulevi atafufuliwa akiwa katika hali ya kua na Ulevi wake.'**

Na akasema tena kua: **'Salama na Amani za *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni Rehma na Usamehevu kwa Mja'**

Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim alisema kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua: 'Wanazuoni wa Umaah wangu wako wa aina Mbili. Ambapo wa Kwanza ni wale ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* amempa Ilm na kisha nae akawasomesha wenzake bila ya kutaka malipo kutoka kwao wala kusifiwa. Hawa ndio wale ambao wenye kuombwa Dua na Ndege wa Angani na Samaki wa Majini na Wanyama wa Ardhini na Malaika Wanawaombea. Hawa ndio wale ambao watakua ni Marafiki wa Manabii na Mitume katika Siku ya Malipo, na watakua mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* wenye Darja ya juu.'**

Wa aina ya Pili ni ya yule Mwanazuoni ambao ni Wabakhili juu ya Ilm yao ambayo wamejaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na hivyo hua ni wenye kuisomesha Ilm hio kwa waja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa malipo, hawa ndio wale ambao wataletwa katika siku ya Malipo wakiwa wanawaka Moto midomoni mwao, na watu watasema: 'Hivi si huyu si ndio yule mtoto wa Fulani Ibn Fulani ambae alikua ni Mbakhili juu ya Ilm yake ambayo alijaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipokua Duniani na hivyo akawa ni mwenye kuitoa kwa Malipo na Mshahara.''

Imam Ad Dahhak Ibn Muzahim alifariki katika ardhi ya Balkh katika mwaka 105 Al Hijra

IMAM IKRIMAH MAWLA IBN ABBAS 25 AH

Imam Abu Abd Allah Ikrimah Mawla Abd Alla Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alikua ni mtu mwenye asili ya Barbar ambao ni wa maeneno ya Afrika Kaskazini na yeye alikua ni mwenye kutoka katika Ardhi ya nchi ya Morroco.

Ikrimah alikua ni mtumwa alienunuliwa na Husayn Ibn Abi Hurr Al Anbari ambae alimzawadia Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alipochaguliwa kua Gavana wa Basra na *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na ndio maana Ikrimah akawa anajulikana kwa jina Ikrimah Mawla Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu.*

Mbali ya kua ni Mtumwa lakini Ikrimah alisoma kwa Masahaba wengi sana wakiwemo Abd Allah Ibn Abbas, Aisha, Abu Hurairah, Abd Allah Ibn Umar, Abd Allah Ibn Amr, Uqbah Ibn Amer, Ali Ibn Abi Talib, Safwan Ibn Umayyah, Al Hajjaj Ibn Amr Al Ansari, Jaber Ibn bin Abd Allah, Hamna Bint Jahsh na Abu Said Al-Khudri *Radhi Allahu Anhum*.

Hivyo Imam Ikrimah alikua ni mtu mwenye Ilm kubwa sana ya Qur'an, Hadith na Fiqh kwani alitembea ardhini kwa ajili ya kuitafuta katika maeneo mbali mbali ikiwemo Basra, Makkah, Madina, Sham, Misri na Khurasan, ambapo anasema mwenyewe kuhusiana naMji wa Madina alipokua katika Masjid An Nabawi kua: '**Mimi nimekutana na Masahaba 200 ndani ya miskiti huu**'

Ambapo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alikua akisema: '**Chochote kile alichokinukuu Ikrimah kutoka kwangu kikubalini kwa sababu hajawahi kusema uongo mbele yangu**'

Imam Ikrimah alikua ni mwenye kukubalika kiasi ya kua alikua anaruhusika kutoa Fatwa kwenye Mlango wa Nyumba ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* wakati Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* mwenyewe yuko ndani ya nyumba yake, Kwani Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* mwenyewe alikua akimwambia: '**Nenda katoe Fatwa, nami nitashukuru kwa msaada wako**.'

Miongoni mwa Wanafunzi wa Imam Ikrimah ni pamoja na Imam Ibrahim An Nakhai, Amr Al Shabi, Khalid Al Hazza, Imam Al Amash, Imam Said Ibn Masruq, Imam Az Zuhri Abu Al-Zubair Al Makki, Ayoub Al Sakhtiyani, Jaber Al Jaafi, Hamid Al Tawil, Khalid Al-Hudhaa, Daud Ibn Al Husain, Said bin Masrouq, Al-Amash, Sammak Ibn Harb, Asim Ibn Bahdala, Asim Al Ahwal, Ibn Tawus, Abd Allah Ibn Kisan, Ibn Laith Ibn Abi Salim, Shehab, Mughirah Ibn Muqsim, Muqatil Ibn Hayyan, Musa Ibn Ayyub, n.k

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Allah Subhanah wa Ta'ala alimjaalia Imam Ikrimah kua na ufahamu mkubwa sana kiasi ya kua alikua na uwezo wa kufafanua aya moja kwa kupitia katika milango takriban 50 ya kimaana, ambapo Imam Jabir Ibn Zayd alikua akisema kuhusiana na Imam Ikrimah kua: '**Huyu ndio Ikrimah *Mawla* wa Abd Allah Ibn Abbas na yeye ni Mtu ambae ni mwenye bahari ya Ilm kubwa sana.**'

Ambapo anasema Habibi Ibn Thabit kua: '**Mara moja katika mara ambazo ni nadra sana kutokea walikutana Wanazuoni watano Nyumbani kwangu ambao ni Ata'a, Tawus, Mujahid, Said Ibn Jubayr na Ikrimah. Ambapo Mujahid na Said Ibn Jubayr walikua wakimuuliza Ikrimah na kujifunza kutoka kwake *Tafsir*, na ilikua hawamuulizi kuhusiana na aya yeyote ya Qur'an isipokua walikua wakipata ufafanuzi mkubwa juu yake.**'

Ambapo anasema Ayoub Al Sakhtiyani kua: '**Mimi nilitaka kusafiri kuelekea kwa Ikrimah ambae nilikua najua kua yuko mbali sana, ambapo mara ghafla nikamuona mtu akiwa amepanda Punda katika Mji wa Basra huku akiwa amezungukwa na watu na nilipomuulizia nikaambiwa kua ni Ikrimah, nami nikajaribu kumkimbilia lakini sikufanikiwa kutokana na kuzongwa kwake na watu hivyo sikuweza kumuuliza kitu chochote, na hivyo ikanibidi niridhike na kujifunza kutoka kwake kutokana na masuali anayojibu baada ya kuulizwa na watu waliomzonga**'

Akasema pia Ibn Manda kua: '**Uaminifu na kukubalika kwa Ikrimah kumethibitishwa na wengi miongoni mwa Tabiina ambao ni 70 miongoni mwao na wamo Wanazuoni wakubwa sana, ambapo hua ni vigumu kukutikana kwa uthibitisho kama huo kwa Wanazuoni wengine, kwani hata wale waliokua wakimsema Ikrimah basi nao pia walikua wakiminukuu.**'

Na Imam Bukhari amesema pia kua: '**Hakuna miongoni mwa wenzangu ambae hakumtegema Ikrimah katika kutafuta muongozo.**'

Imam Yahya Ibn Muin amesema pia kua: '**Ukimuona mtu anamsingizia Ikrimah basi fahamu kua anaemsingizia hua si mwenye kua na ukweli katika Uislam wake.'**

Imam Amr Ash Shabi alisema kua: **'Hakuna mtu aliebakia mwenye Ilm kubwa ya Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama Ikrimah.'**

Anasema Mughira Ibn Muqsim kua: **'Aliulizwa Said Ibn Jubayr: 'Hivi jee kuna mtu unaemjua ambae ana Ilm kubwa zaidi yako?' ambapo nae akasema: 'Naam, ni Ikrimah''**

Yahya Ibn Ayub anasema kua: **'Ibn Jurayj aliniuliza mimi: 'Hivi jee wewe umenukuu kutoka kwa Ikrima?' nami nikasema la, nae akaniambia: 'Basi hakika wewe umekosa sehemu 3 kati ya 4 za Ilm''**

Imam Sufyan Ath Thawri aliusia kwa kusema kua: **'Chukueni Tafsiri kutoka kwa watu wanneambao ni Said Ibn Jubayr, Mujahid, Ikrimah na Ad Dahhak'**

Al Farazdaq Ibn Jaws anasema kua: **'Mimi nilikua nimekaa na Shahr Ibn Hawshab katika maeneo ya Jurjan, mara akatokea Ikrimah hivyo tukamuuliza Shahr: 'Vipi tumwite?' nae akasema: 'Mwiteni kwani hakuna taifa lisilokua na kiongozi wake, na kama ikiwa tutachagua kiongozi wetu basi Ikrimah anastahiki kua kiongozi wetu''**

Amesema Imam Ikrimah kua: **'Kila kitu kina Msingi wake na msingi wa Uislam ni Tabia njema'**

Amesema Imam Ikrimah kua: **'Ilm hua ina bei yake'** hivyo nae akaulizwa: **'Jee ni bei gani hio?'** Imam Ikrimah akasema: **'Kuiweka kwa Mtu atakaeihifadhi vyema na kutoipoteza.'**

Imam Ikrimah akasema tena kua: **'Ibilisi hujihisi vibaya sana pale Mja anaporudi kwa Mola wake na kumuomba huku akilia, hadi *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamsamehe juu ya kosa lake hilo na mengineyo.'**

Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Nasr Al Marwazi alisema: **'Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na kukubalika kwa Hadith za Ikrimah kuanzia kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal, Is-haq Ibn Rahwayh, Abu Thawr na Yahya Ibn Main, Ikrimah ni Imam wa watu Dunia hii.'**

Imam Ikrimah alifariki katika mji wa Madina mnamo mwaka 105 Al Hijra huku akiwa na umri wa miaka 80 ambapo watu wa Mji wa Madina walisema: **'Mwenye Ilm zaidi miongoni mwa watu na mtu mwenye kujulikana zaidi amefariki.'**

IMAM ABD ALLAH IBN MUHAYRIZ

Imam Abu Muhayr Abd Allah Ibn Muhayriz Al Makki alizaliwa katika Mji wa Makkah ndani ya miaka 100 ya mwanzoni ya Al Hijra kwani alifariki mnamo mwaka 99 Al Hijra. Imam Ibn Muhayriz, alihamia katika ardhi ya Jerusalem na hivyo kua ni Mwanazuoni wa Dimashq baada ya kua ni mwenye kusoma kutoka kwa Masahaba wakiwemo Abu

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu,* Muawwiyah Ibn Abu Sufyan *Radhi Allahu Anhu,* Abu Sharma Al Ansari *Radhi Allahu Anhu,* Ubaydah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu,* Ummu Dardaa *Radhi Allahu Anha* na wengineo *Radhi Allahu Anhum.*

Ambapo wa upande wa Imam Al Awzai basi yeye anasema kuhusiana na Imam Ibn Muhayriz kua: **'Imam Ibn Muhayriz ni mmoja kati ya Wanazuoni Watano Wakubwa wa Tabiina**' na kasema tena kua: '**Kama Mtu anataka Mwanazuoni wa kumfuata basi na amfuate Imam Ibn Muhayriz.**'

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Makhul Ash Shami, Imam Khalid Ibn Durayk, Imam Abu Bakr Ibn Hafs, Imam Muhammad Ibn Yahya, Imam Abd Al Azizi Ibn Abd Al Malik, n.k

Kwani kama ilivyokua vile amaavyo Watu wa Madina walivyokua wakijisifia kuhusiana na ukubwa wa ilm ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* basi kwa upande wa watu wa Dimashq wao walikua wakijisifia kutokana na na na Imam Abd Allah Ibn Muhayriz

Imam Abd Allah Ibn Muhayriz alikua ni *Thiqah* na mwenye kuaminika sana ambapo hadithi zake zinapatika katika Vitabu 6 vikuu vya Hadith. Na alikua ni mtu Mcha Mungu sana, Mnyenyekevu na mwenye Subra na mwenye kuishi kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam,* kwani ilikua kama akienda katika sehemu fulani yenye watu ambao wakimjua basi hua ni mwenye kuondoka ili asije kusifiwa mbele ya watu hao.

Ambapo anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Amesema Ismail Ibn Ibrahim kua amesema Ibn Abi Salamah kua: 'Ibn Muhayriz aliingia kwenye Duka la Vitambaa kwa ajili ya kununua baadhi ya Vitambaa, ambao mmoja kati ya watu walikuwepo Dukani hapo basi akamuuliza Muuzaji Duka huyo kwa kusema: 'Jee unamjua ni nani huyu alieingia?' ambapo Imam Ibn Muhayriz akageuka na kusema: 'Hakika sisi tumekuja Dukani kununua bidhaa kwa Dirham zetu na wala si kwa Dini yetu' na kisha akatoka Dukani hapo na kuenda zake.**''

Imam Ibn Muhayriz alikua ni mtu ambae anaependa kuvaa nguo anazoshonewa na mke wake kwani alikua hapendi kuvaa nguo zinazouzwa Madukani, kiasi ya kua mmoja kati ya marafiki zake alikua akimwambia: '**Hakika wewe una Sifa Mbili ambazo ni kwanza Mcha mUngu halafu pili ni mwenye Ubakhili wa kutotaka kununua Nguo Madukani**' na Hivyo Imam Ibn Muhayriz alikua akisema: '**Baada ya kufanya Dhambi kwa kuvaa nguo za Hariri, basi ni bora kwangu mie kuvaa nguo hizi nilizoshonewa hata kama itakua ni zenye kunisababishia kuchunika Ngozi yangu.**'

Baada ya kuzongwa sana na rafiki yake huyo basi Imam Ibn Muhayriz akanunua nguo mbili kutoka Misri na akawa ni mwenye kuanza kuvaa nguo hizo tu. Imam Ibn Muhayriz

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

alikua kila wakati ni mwenye kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo basi alikua kila wakati ni mwenye kuonekana kua na rangi yenye kusawijika kutokana na khofu hio, hivyo alikua akiomba kwa kusema: '**Ya Allah nakuomba unijaalie kua ni mwenye kukuogopa wewe hata kama Mwili wangu utabadilika rangi yake na kua wa Manjano na kukonda kutoka na kua na khofu juu yako.**'

Na alipoulizwa kwanini akawa anaomba hivyo basi akasema kua: '**Ukiwa unaonekana na kujionesha mbele za watu unapokua na neema, na kujisifia na watu wakaonesheeana vidole juu yako basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakuingiza Motoni katika siku ya Malipo.**'

Anasema Imam Ibn Muhayriz kua: '**Mimi nilizungumza na Fudayl Ibn Iyadh ambae nilimuomba anipe wasia hivyo nae akasema: 'Kama ukiwa na sifa tatu zifuatazo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakuneemesha kwa Neema zaidi kutokana na Sifa hizo ambazo ni: 'Kujifunza kile usichokijua, Kujua namna ya Kusikiliza na Kuwatembelea wale wasiokutembelea wewe.'**''

Ambapo anasema Imam Ibn Muhayriz kua; '**Yeyote yule anaetembea mbele ya Mzee wake basi hua ni mwenye kumvunjia haki yake Mzee wake huyo, ingawa inakubalika kutembea mbele kwa ajili ya kuwaondolea maudhi njiani mwao, na yeyote yule anaemwita Mzee wake kwa jina lake la utani basi hua si mwenye Adabu ingawa inaruhusika kusema huyu ni Baba yangu au huyu ni Mama yangu.**'

Anasema Musa Ibn Uqba kua: '**Mimi nilikuwepo mazikoni pamoja na Ibn Muhayriz katika maeneo ya Ramla, ambapo nae akasema: 'Nafahamu kua Muislam anapofariki basi Waislam husema: 'Sifa zote anastahiki *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie alietujaalia sisi kufariki wakati tukiwa kwenye Dini ya Kiislam' halafu Waislam hao hua ni wenye kusahau juu ya Kifo, na wala hua hawakumbuki, kuhusiana na maneno yasemayo kua: 'Hairuhusiki, kuzungumza jambo lolote lile ndani ya Msikiti isipokua mambo matatu: 'Maneno ya wale watu wanaosali ndani yake, Maneno ya wale wanaomkubuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake na maneno ya wale wanaoelimisha Ilm ya Dini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake.'**''

Na akasema tena Imam Ibn Muhayriz kua: '**Unapoona vitu vizuri basi mtukuze *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na unapoona mambo mabaya basi Muombe *Allah Subhanah wa Ta'ala* auepushe Umma wa *Muhamamd Salallahu Alayhi wa Salam'*** na akasema kua: '**Sisi tulikua tunahesabu kua amali ni bora kuliko Ilm lakini leo hii tunahitaji Ilm zaidi kuliko Amali, kwani Ilm imesahaulika.**'

Imam Ibn Muhayriz alikua ni mwenye kusoma Qur'an kila siku, ingawa alikua ni mwenye kukifanya kila kitu chake kuhusiana na Ibada zake kua ni siri kama vile

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ambavyo alivyokua yeye mwenyewe hapendi kujulikana mbele za watu, ingawa alikua ni mwenye kupenda sana kuwasaidia marafiki zake pale wanapokua na shida.

IMAM ABU BISHR AL MURRI

Imam Abu Bishr Salih Ibn Bishr Ibn Wahd Ibn Muhayriz Al Basr Al Muri alizaliwa mjini Basra katika kipindi cha miaka 100 ya mwanzoni ya Uislam na alikua ni Mwanazuoni wa Ilm ya Hadith, Fiqh, na Ilm ya Qiraa, kwani alisoma kutoka kwa Imam Muhammad Ibn Sirrin, Imam Hasan Al Basr, Imam Qatadah Ibn Diamah, Imam Hisham Ibn Hasan na Wanazuoni wengineo.

Ingawa alizaliwa na kua ni mwenye kuishi katika Mji wa Basra lakini Imam Muhayriz Al Murri baadae alihamia katika Mji wa Baghdad baada ya kuhitajika katika mji huo kutokana na mualiko wa Khalifa Mahdi, ambae alikua ni kiongozi mwenye kuwaheshima sana na kuwapenda Wanazuoni, ambapo Watu wa Baghdad walinufaika sana kutokana na Ilm aliyokua nayo Imam Muhayriz Al Murri.

Ambapo baada ya kuokea Mualiko huo basi Imam Muhayriz Al Murri akaelekea katika Mji wa Baghdad ambapo alipokelewa na Khalifa mwenyewe kwa pamoja na watoto wake wawili ambao ni Musa na Harun, ambao walipofika mbele ya Imam Muhayriz Al Murri basi wakaamrishwa kushuka ili wamsaidie Imam Muhayriz Al Murri kushuka kutoka kwenye Farasi wake, jambo ambalo lilimtia haya kubwa sana Imam Muhayriz Al Murri ambae alikua si mtu wa kujiona wala kujionesha.

Baada ya kufika kwenye baraza ya Khalifa Al Mahdi basi Imam Muhayriz Al Murri akamuusia Khalifa Al Mahdi kwa kumwambia: ‘**Ewe *Amir Ul Muuminin* nakupa Wasia kua unatakiwa uwe na Subra na Ustahmilivu, kwa sababu aliekaribu miongoni mwa Waja wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni yule aliekua na Subra na ustahmilivu na hivyo kua ni mwenye kuustahmilia Ushauri hata kama ukiwa ni mchungu kwake, kwani hata wale waliokua wakitaka kua na ukaribu pia na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua ni wenye kushikamana na mafundisho yake na Sunnah zake.**’

‘**Ewe *Amir ul Muuminin,* kua makini na majukumu yako na kua ni mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta’ala* ambae ndie aliekupa I’lm na ufaham, ambapo kutokana na hayo basi kwako wewe kamwe hakutokua na jibu litakalokubalika utakalojibu kwa kusema ‘sijui.’’**

‘*Ewe Amir ul Muuminin, Rasul Allah Salallah Alayhi Wa Salam* hua ni adui kwa kila mwenye kuwadhulumu watu wa Umma wake, na hivyo kila mtu mwenye uadui na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi hua pia ni mwenye Uadui na *Allah Subhanah wa Ta’ala.* Ambapo kutokana na kupingana kwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi mtu huyo hua ni mwenye kutayarishiwa vikwazo kwa ajili yake.

Hivyo kama unataka kua na msimamo Thabit na sehemu nzuri ya kuuweka Mguu wako ili usiteleze kesho katika siku ya Malipo basi shikamana na Kitabu Cha *Allah Subhanah wa Ta’ala* na *Sunnah za Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Hivyo haifai kwako wewe kua ni mwenye kupingana na *Allah Subhanah wa Ta’ala* na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Nami nimekuusia haya kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* nawe umeyasikiliza na hivyo yakumbatie na kisha shikamana nayo’

Ambapo baada ya Wasia huo basi Khalifa Al Mahdi akavutiwa zaidi na Imam Ibn Muhayriz Al Murri, na akamzawadia zawadi lakini Imam Ibn Muhayriz Al Murri akakataa kupokea zawadi hizo.

Imam Muhayriz Al Murri hakua ni mwenye kumpa wasia Khalifa Al Mahdi tu bali pia alikua ni mwenye kumuusia kila mtu anaehitaji wasia wake kwa maneno yake na kwa namna anavyoishi maisha yake, ambayo ndani yake alikua ni mwenye kusoma sana Qur’an, kufanya *Dhikr Allah* na kutokwa na machozi mengi sana kwa ajili ya Mola wake, si kutokana na kukumbuka Dhambi zake tu bali pia kutokana na kua na Taqwa na kufaham maneno ya Mola wake ndani ya Kitabu chake kitukufu cha Qur’an, kwa mfano alikua lazima atokwe na machozi pale anapoisoma ile aya isemayo:

﴿يَوْمَ تُقَلَّبُ وُجُوهُهُمْ فِى ٱلنَّارِ يَقُولُونَ يَٰلَيْتَنَآ أَطَعْنَا ٱللَّهَ وَأَطَعْنَا ٱلرَّسُولَا۠﴾

Yawma tuqallabu wujoohuhum fee alnnari yaqooloona ya laytana ataAAna Allaha waataAAna alrrasoola *(Surat al-Ahzab 33:66)*

Tafsir: ***Siku ambayo Nyuso zao zitakapogeuzwa kwenye Moto nao watasema: ‘Ole wetu, sisi, kama tungekua ni wenye kumtii Allah na kumtii Mtume wake.’***

Ambapo mbali ya kua ni mwenye kulia lakini Imam Ibn Muhayriz Al Murri alikua ni mwenye sauti nzuri sana katika kusoma kwake, kwani alikua ndie msomaji bora wa Mji wa Basra na Baghdad kiasi ya kua watu walikua ni wenye kupenda kumsikiliza na kua ni wenye kukihisi kwa hisia zao kisomo chake, ambapo baadhi ya watu walikua wakianguka na kuzimia.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo alisema Sufyan Ath Thawry kuhusiana na Qiraa chake Imam Ibn Muhayriz Al Murri kua: '**Ibn Muhayriz yuko kama Mtume ambae ametumwa kwa watu wake.'**

Amapo anasema Imam Ibn Hibban kua: '**Ibn Muhayriz alikua ni Mcha Mungu Sana miongoni mwa Wacha Mungu wa Basra, na ndie msomaji wao bora wa Qur'an, alikua skisoma Qur'an katika Mji wa Basra kwa kutumia sauti nzuri sana laini na nyororo, alikua ni mfanyaji mema ambayo hata yeye mwenyewe alikua hajui kua ni mwenye kufanya mema hayo.'**

Alisema Imam Salih Ibn Bishr Muhayriz Al Murri kua: '**Hikma humuongezea heshima mwenye heshima na humnyanyua kidarja Mtumwa na kumuweka kwenye Baraza la Sultan'**

'Kama mtu anataka kujua ni kitu gani ametayarishiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi na aangalie kile alichotayarisha kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

'Wa chini kabisa miongoni mwa Watu wa Peponi atakua na Meza mbili zilizotegnezwa kwa Dhahabu na Fedha ikiwa na rangi tofauti zilizozungukwa na Hur Layn 10, 000, na hua ni mwenye kula akitakacho miongoni mwa vya mwisho alivyovitamani kwa ladha wa hamu ya mwanzo.'

Siku moja mke wake Imam Muhayriz Al Murri alipata ugonjwa wa kupooza, ambapo akaamua kumsomea Qur'an na akapona, watu wakaulizana imekuaje? Ambapo Imam Muhayriz akasema: '**Wa Allahi, nnaapa mimi kua siwezi kushangaaa pale nitakapoona Maiti itakaposomewa Qur'an kisha ikawa ni yenye kufufuka.'**

Akasema Imam Muhayriz Ibn Murra kua: '**Muislam anatakiwa atafute Ladha ya mambo matatu katika Dunia yake, ambayo Utakapoyapata kile unapoyatafuta basi furahia ladha yake na ukiyakosa basi fahamu kua mlango wake umefungwa kwa ajili yako, hivyo inabidi ulie kwa ajili yake mambo hayo ni: 'Ladha ya Ibada ya Sala, Ladha ya Utamu wa kusoma Qur'an na Ladha ya Dhikr Allah kwa wingi sana.' '**

'Kama unataka *Allah Subhanah wa Ta'ala* akuneemeshe na Rehma zake kama unavyotaka basi Wajali waja wake kama anavyotaka.'

'Safari ya Akhera ni ndefu sana hivyo tayarisha Chakula chako kwa ajili ya Safari hio na fahamu kua chakula bora ni kile cha Halali.'

'Dunia ni salio la wale waliotangulia kabla yetu, yaliyopita yameshatuacha na sio yetu, hivyo achana na Dunia kabla haijakuacha na chukulia kua kama kwamba kifo kipo pembeni ya kitanda chako.'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

'Nashangaa namna watu wanavyodharau Akhera yao mbali kuamrishwa kujitayarisha nayo, tena bado wanaghafilishana kutokana nayo'

Imam Abu Bishr Al Murri alifariki mnamo mwaka 172 Al Hijra mjini Baghdad.

IMAM AL MUTARRIF IBN ABD ALLAH

Imam Immad Ad Din Abu Abd Allah Mutarrif Ibn Abd Allah Ibn As Sihhir Ibn Awf Ibn Kaab Ibn Wikdan Ibn Quraysh alizaliwa katika Mji wa Makkah katika familia ya Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wenye Ilm kubwa ya Dini na Taqwa.

Hivyo Imam Al Mutarrif Ibn Abd Allah alisoma kwa Baba yake mzani na pia akasoma kwa Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu,* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Ubay Ibn Ka'b *Radhi Allahu Anhu,* Abu Dharr Al Ghifari *Radhi Allahu Anhu*, Imran Ibn Hussein *Radhi Allahu Anhu, Umm Ul Muuminin* Aisha *Radhi Allahu Anha*, Muawwiyah Ibn Abu Sufyan *Radhi Allahu Anhu,* Imam Hasan Al Basr, Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi, Imam Muhammad Ibn Wasi n.k

Imam Al Mutarrif Ibn Abd Allah alikua ni mtu mcha Mungu, mwenye Ilm na ni mwenye kuaminika, alikua ni mwenye kupenda kuvaa nguo pana na mwenye kupenda kupanda Farasi na ni mwenye kumuusia kila mtu wakiwemo Watawala na wenye Mamlaka na kuwarudisha kwenye njia ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani alisema Imam Al Mutarrif kua: '***Kama Allah Subhanah wa Ta'ala* angenipa nafasi ya kuchagua sasa hivi baina ya kuenda Peponi, au kuenda Motoni au Kua Vumbi basi mimi ningechagua kua Vumbi'** na akasema pia kuhusiana na wale wanaosengenya kua: **'Hakika mimi siwezi kua na urafiki na Mtu anaesengenya.'**

Imam Al Mutarrif alikua ni mtu mwenye Subra kubwa sana kiasi ya kua hata Mtoto wake mdogo wa Kiume alipofariki basi hakua ni mwenye kua na huzuni kabisa kwani kwake iliua ni kawaida tu ya kua hayo ni majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo katika siku ya Maziko alivaa vizuri sana kama kawaida yake, na alipoulizwa mbona yuko katika hali hio basi akasema: **'Hivi jee nyinyi mnanitegemea mimi kua ni mwenye kulia na kutoridhika na kifo? Wallahi mimi nnaapa kua kama Dunia nzima na kila kilichomo ndani yake kiko chini ya Umiliki wangu mie, na kisha vikatakiwa kutumiwa kwa ajili ya kununulia funda moja tu la Maji ya Mto wa Al Kawthar wa Peponi basi mimi ningeitoa Dunia na vitu vyote hivyo bila ya kusita.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na ingawa wengi kati ya Wacha Mungu walikua ni wenye kukesha Usiku kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini kwa upande wake yeye Imam Al Mutarrif alikua ni mtu mwenye kulala vizuri sana katika usiku wake bila ya kuamka kwa ajili ya sala za usiku isipokua katika wakati wa Sala ya Al Fajir na alipoulizwa kwa nini anapenda kufanya hivyo basi alisema: '**Natumia Usiku wangu kwa ajili ya Kulala na kisha naitumia Siku yangu huku nikiwa nimejawa na Majuto, kwani kwangu mimi ni bora kuamka asubuhi huku nikiwa na Majuto kuliko kuamka asubuhi huku nikiwa nimeridhika kutokana na Ibada za Usiku'**

Imam Al Mutarrif aliakua ni mtu ambae kama alivyo muonekano wa nje wake kua ni mwenye usafi na kupendeza basi ndivyo namna alivyokua ndani ya Moyo wake, kwani alikua akisema kua: **'Wakati Mja anapokua yuko sawia ndani ya Mwili wake na nje yake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kusema: 'Naam..Huyu ndie Mja Wangu wa Kweli.''**

Imam Al Mutarrif alikua ni mtu ambae hapendi watu wanaosoma Qur'an mbele za watu kisha wakawa wanasifiwa na watu hao, kwani alikua akisema**: 'Ama kwa hakika hakuna Waliohifadhi Qur'an katika wakati wetu kwani wasomaji wote wanasoma kwa ajili ya kujipatia neema za Kidunia kutokana na kisomo chao'**

Na pia alikua hapendi wanaoandika vitabu kwa ajili ya Dunia yao kwani anasema kua: '**Kutakua na watu katika siku ya Malipo ambao walikua wakiandika mambo siyo katika Dunia, na hivyo watasema katika siku hio, ya laiti Kalamu zetu bora zingekua ni za moto na hivyo tusingezigusa na wala tusingeweza kuandikia.**'

Aliusia Imam Al Mutarrif kwa kusema: **'Mimi sishangai kuona namna mtu anaeangamia namna anavyoangamia, bali nashangaa kuona mtu anaefurahia kuokolewa namna anavyoweza kuokolewa. Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* kamwe hajawahi kutoa neema kubwa zaidi kwa mja wake kuliko kuisalimisha nafsi yake mja huyo kwenye Imani na kufariki huku akiwa kwenye Iman**.'

Na akasema tena kua**: 'Uadilifu wa Moyo ndio Uadilifu wa Amali, na Usahihi wa Amali ndio Usahih wa Nia.'**

'Hakuna kitu chenye thamani kwa Ibn Adam kama Ufahamu wa Akili, miongoni mwa vitu alivyopewa Ibn Adam.'

'Kuachana na Mambo yenye shubha hua ni sifa ya wale tu ambao ni wenye kujichunga kua kwenye hali hio.'

‘Kama matamanio hayakuingia kwenye Nyoyo za Wacha Mungu basi kamwe wasingeweza kua na mafanikiko mbele ya udhihirisho wa *Allah Subhanah wa Ta’ala.’*

‘Kwa yeyote yule asiekua na huruma na wafanyao dhambi basi anatakiwa japo kidogo kuwaombea kua watubu na wasamehewe kwani ni tabia za Malaika kua ni wenye kuwaombea maghfira kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* wale watu waliomo Duniani.’

‘Ubora wa kila kitu hua ni katika kua na hali ya kati na kati.’

‘Fitna haiji kwa ajili ya kuwaongoza njia Watu, bali kwa ajili ya wale ambao ni wenye kupigana na Nafsi zao kuachana na Mtamanio ya Nafsi zao.’

‘Hakika mimi hua nnapenda kua na Afya na mwenye shukrani, kuliko kua ni mwenye kua na Subra katika wakati wa Mitihani.’

‘Yeyote yule mwenye kunisifu mimi hua ni mwenye kuniadhirisha mimi na nafsi yangu.’

Yazid Ibn Abd Allah aliulizwa: **‘Hivi Jee Al Mutarrif hua anafanya nini pale inapokua kuna mgogoro baina ya Waislam?’ ambapo nae akajibu: ‘Hua ni mwenye kukaa ndani ya Nyumba yake kimyaa na wala hatoki nje wala hazungumzi na yeyote hadi migogoro huo itatuliwe’**

Imam Al Mutarrif alikua ni mwenye kukaa nje kidogo ya Mji wa Basra kwa sababu ya kutopenda kujichanganya na Watu kwani alikua akisema: **‘Ili uwe ni mwenye kuheshimika basi inabidi uwe si mwenye kuwategemea watu, na hivyo hapo ndio utaweza kudumisha heshima yako na uzuri wako’**

Na hivyo siku moja wakati anaenda kwenye Sala ya Al Fajir pamoja na mtoto wake basi mara ghafla zikatokea nuru mbili ambazo zilikua zikimurika juu na chini kwenye fimbo yake ya kutembelea, hivyo akamwambia Mtoto wake: **‘Ewe Abd Allah hebu angalia kwani kama ningewaambiwa watu juu ya hili basi kila mtu angeona kua mimi nnasema uongo.’**

Na anasema Hasan Ibn Amr Al Fazari kua: **‘Thabit Al Yaman na rafiki yake waliingia nyumbani kwa Mutarrif, na kumkuta Imam Mutarrif akiwa anang’ara kwa nuru tatu ambapo moja ikiwa kwenye Paji lake la Uso, ya pili kwenye upande wa kushoto wa Kifua chake kwenye Moyo wake na ya tatu miguuni mwake, hivyo wakashangaa na wakamuuliza Imam Al Mutarrif: ‘Vipi mbona umekua na hali hio?’ Imam Al Mutarrif akauliza: ‘Hali gani mnayoizungumzia nyie?’ nao**

wakasema: 'Umejaa Nuru.' Ambapo Imam Al Mutarrifu akasema: 'Hii Nuru ni kulingana na kusjudu kwangu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'* '

Na kila siku ya Ijumaa Imam Al Mutarrif alikua ni mwenye kutoka na Punda wake hadi Msikitini na kisha baada ya hapo huelekea makaburini ambapo hua ni mwenye kulala kwa dakika kadhaa, na hua ni mwenye kusikia na kujua hali ya ila mmoja wapo aliepo makaburini hapo, na Ijumaa moja alikua pamoja na watu basi mara akapita Ndege aliekua akilia hivyo nae akawauliza watu hao: '**Jee mnajua kasema nini ndege huyo?**' watu wakasema; **'La'** Imam Al Mutarrif akasema: **'Wanasema: 'Imani iwe Juu yenu, na Sala na Salam ziwe juu ya Wacha Mungu.''**

Imam Al Mutarrif alikua ni mwenye kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema: **'Ya Allah, hakika mimi nakuomba msamaha wako na msamaha wa kila amali yangu njema niliyoifanya kwa Ikhlasi, kwa sababu mimi ni mwenye kutaka Ridhaa yako tu.'**

'Ya Allah nakuomba utusamehe hata kama hukufurahishwa nasi kwani Mmiliki hua ni mwenye kuwasamehe Watumwa wake hata kama hakuridhika nao'

'Ya Allah usizikatae Dua za walikuwepo pamoja nami kwa kwa sababu yangu, nauomba wakubalie Dua zao.'

'Ibn Adam anatakiwa amuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Ikhlasi na ridhaa na kisha anatakiwa afanye Istighfar katika kila baada ya Ibada husika.'

Yeyote yule aliekua akiinga kwenye Nyumba ya Imam Al Mutarrif huku akiwa na huzuni basi alikua akitoka na furaha na tabasam kwani Imam Al Mutarrif alikua hazugumzii kuhusiana na Dunia, bali kuhusiana na Akhera na Jahannam tu.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM ATAA IBN SULAYMAN

Imam Ataa Ibn Sulayman Al Basri alikua ni Mwanafunzi wa Sahaba Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* na pia Imam Hasan Al Basr na alikua mcha Mungu lakini asiependa kujionesha. Kwani Ucha Mungu wake na khofu ya kumuogopa Mola wake ilimpelekea kua hata hamu ya kula kua hana wachia mbali hamu ya kusomesha.

Imam Ataa Ibn Sulayman Al Basr alikua ni mtu ambae kamwe hakua ni mwenye kuomba ajaaliwe aingie Peponi, bali alikua ni mwenye kuomba ajaalie kuupata usamehevu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani alikua anajihesabu kua ana dhambi

nyingi sana hadi ikafikia hawezi kutoka hata ndani na hata udhu alikua akiutilia kitandani mwake.

Ambapo anasema Nuaym Ibn Muwarri kua: '**Sisi tulimtembelea Ataa na tulipofika kwake tulimkuta akiwa anarudia kwa majuto makubwa kwa kusema: 'Ya Laiti Mimi bora Mama yangu asingenizaa' na alikua akiomba: 'Ya Allah niingize kwenye Rehma zako mimi kutokana na ugeni wangu hapa Ulimwenguni, niingize kwenye Rehma zako mimi katika kuingia kwangu Kaburini, niingize kwenye Rehma zako mimi katika siku ya kusimamishwa mbele yako.**''

Khofu ya kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ilimfanya Imam Ataa Ibn Sulayman asahau hata kusoma Qur'an, kwani ufahamu wake yeye wote unamfikiria Mola Wake na adhabu zake na hivyo akawaomba wenzake kua wamtafutie Dawa ya kuondokana na matatizo hayo kwa kusema: '**Nitafutieni mimi hadithi itakayo niwezesha kuepukana na usahaulivu huu niliokua nao**.'

Na wakati alipokua akitia Udhu kwa ajili ya kusali basi alikua akilia sana kabla ya hata kua ni mwenye kuingia kwenye hio Ibada ya Sala yenyewe, siku moja akaulizwa imekuaje ikawa na hali hio ambapo nae akasema: '**Wa Allahi nnaomba mimi kua bora nihesabiwe amali zangu kabla ya kuwasili siku ya Malipo ili nisiwe ni mwenye kusimamishwa mbele ya Mola wangu.**'

Siku moja Sarrar Ibn Ubayda alimtembelea nyumbani kwake Imam Ataa Ibn Sulayman na hivyo Mke wa Imam Ataa Ibn Sulayman akamuomba Sarrar amshauri kuhusiana na kulia sana kwake kwani kutamuathiri afya yake, ambapo Imam Ataa Ibn Sulayman alipousiwa juu ya hilo basi akasema:

'**Hakika mimi kila ninapofikiria namna watu watakavyoadhibiwa ndani ya Moto basi nami hua najiona nimo ndani ya Moto huku mikono yangu ikiwa imefungwa nyuma ya shingo yangu na kisha nauona ukali wa moto wa Jahannam, namuomba Allah akuingize kwenye rehma zake, Ewe Sarrar**'

Imam Ataa Ibn Sulayman alifariki mnamo mwaka 140 Al Hijra.

IMAM KHARIJA IBN ZAYD IBN THABIT 30 AH

Imam Kharijah Ibn Zayd Ibn Thabit alikua ni Mwanafiqh mkubwa wa Madina ambae Ilm yake ilitokana na kusomeshwa kwake na baba yake ambae alikua ni Mwanafiqh Sahaba wa Madina aitwae Zayd Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu.*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Kharijah Ibn Zayd alisoma pia kwa mama yake ambae ni Umm Saad *Radhi Allahu Anha*, kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu, Abd Allah Ibn Umar Radhi Allah Anhu, Uthman Ibn Affan Radhi Allahu Anhu, Usama Ibn Zayd Radhi Allahu Anhu na* Masahaba wengineo Allah awaridhie.

Imam Kharijah Ibn Zayd Ibn Thabit alizaliwa mnamo mwaka wa 30 Al Hijra na alikua na Ilm kubwa ya Hadith na Mirathi, na alikua ni Mcha Mungu sana miongoni mwa wacha Mungu wa Mji wa Madina na ni mwenye kuachana na Dunia na kujitenga na watu na kutokana na kua na hali hio basi Ilm yake haikua ni yenye kuenea kwa watu wengi sana.

Anasema Mus'ab Ibn Az-Zubairi kua: '**Kharijah na Talha Ibn Abd Allah Ibn Awf walikua ni wenye Ilm ya kugawa mirathi na waliandika vitabu na watu walikua ni wenye kupendelea mitizamo yao**'

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Sad basi anasema kua: '**Kharija alikua ni *Thiqah* anaeaminika na Hadithi zake ni nyingi sana**' na huo pia ni mtizamo wa Ahmad Ibn Abd Allah Al Ijli.

Na kwa upande wa Ubaid Allah Ibn Umar basi alisema kua: '**Wale ambao walioendeleza Ilm ya Fiqh baada ya kufariki kwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Mji wa Madina walikua ni Kharija Ibn Zayd Ibn Thabit, Said Ibn Musayyib, Urwa Ibn Az Zubayr, Al Qasim Ibn Muhamamd, Qabisah Ibn Dhuayb, Abd Malik Ibn Marwan, Sulayman Ibn Yasir Mawla Maimunah.**'

Imam Kharija Ibn Zayd Ibn Thabit alikua ni miongoni mwa wenye Ilm kubwa sana ya Fiqh, ambapo anasema Al Darawardi kua: **'Amesema Ubayd Allah Ibn Umar kua Ilm ya Fiqh baada ya Masahaba wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam wa Madina ni Kharija Ibn Zayd Ibn Thabit, Said Ibn Al Musayyib, Urwa, Al Qasim Ibn Muhammad, Qabisah Ibn Dhuayb, Abd Al Malik Ibn Marwan na Sulayman Ibn Yasar.'**

Kabla ya kufariki kwake Kharijah Ibn Zayd Ibn Harith alilala akaota kua amejenga jengo lenye ngazi 70 na alipomaliza kujenga basi jengo hilo lote likaporomoka, hivyo alipoamka akasema: **'Huu ni mwaka wangu wa 70 kuishi hapa Duniani unaonesha ndio mwaka wangu wa mwisho wa uhai wangu.'**

Hivyo mnamo mwaka huo aliyoota ndoto hio ambao ulikua ni mwaka wa 100 Al Hijra Imam Kharijah Ibn Zayd Ibn Harith alifariki Dunia akiwa na umri wa miaka 70.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM HABIB AL AJAMI 31 AH

Imam Habib Ibn Muhammad Al Ajami Al Basr alizaliwa katika ardhi ya Uajemi mnamo mwaka 31 Al Hijra na alijaaliwa kua ni mtu mwenye mali nyingi sana. Na hivyo kua ni mwenye kujulikana kama Papa wa Riba katika Mji wake kutokana na kua ni mwenye kukopesha watu wenye shida kwa Riba, na pia alikua akijulikana kama Ruba wa Ardhini kutokana na kuwanyonya watu baada ya kuwakopesha, kiasi ya kua ingawa alikua anawasaidia wengei kwa kuwakopesha lakini watu wengi walikua hawampendi katika mji wake kutokana na kupenda kula riba katika kila anachokopesha.

Hali hii ya mazigira aliyokua akiishi Imam Habib Al Ajami iliwapelekea hadi watoto wa mji wake kua ni wenye kumnadia kutokana na kupenda kwake Riba, hivyo nae akaamua kuachana na kazi hio na kuomba msamaha wa Mola wake kutokana na minadio hio na kutopendwa na watu wake, hivyo akauza Mali zake na kisha akatoa sadaka kwa ajili ya Mola wake huku akisema: '**Ewe Mola wangu hakika mimi nanunua Msamaha wako kutokana na Mali niliyokua nayo hivyo nakuomba niwachie huru kutokana na makosa yangu niliyoyafanya hapo kabla.**'

Baada ya kufanya Hijra ya kuachana na mambo maovu basi Imam Habib Al Ajami akaamua kufanya Hijra ya kuhama katika Mji wake aliokua akiishi na kuhamia katika mji wa Basra ambako alikutana na Imam Hasan Al Basr, na hivyo ingawa hapo kabla yake alikua ni mtu asiekua mcha Mungu lakini *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimuonesha njia sahih kupitia kwa Imam Hasan Al Basr na hivyo Imam Habib Al Ajami akarudi kwa Mola wake na kua ni Mcha Mungu mwenye kufanya *Istighfar* sana.

Neno *Istighfar* linatokana na neno *Ghafara* ambalo hua linamaanisha Kufunika, Kuficha, Kukipa Kitu Ulinzi, Kurekebisha Mambo au hali ya kitu kutoka katika hasi isiyokubalika na kukiweka katika hali inayokubalika, Kudharau au kutotilia maanani kasoro aukosa la kitu au mtu Fulani. Neno *Ghafara* ndio lililotoa neno *Istighfar* na pia likatoa neno *Ghafur*.

Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na *Istighfar* basi hua tunazungumzia kuhusiana na kumuomba yule ambae ndie mwenye Jina na Sifa Tukufu ya *Al Ghafur* ambae ni *Allah Subahanh wa Ta'ala* ambapo sifa hio maana yake hua Mwenye utukufu wa kutuzuia na kutulinda sisi Ibn Adam kutokana na huruma zake na ukarimu wake na Rehma zake juu yetu kutokana na kufanya Madhambi na Makosa kutokana na Udhaifu wetu sisi ambao ni Viumbe wake.

Na Ulinzi huo *Al Ghafur* wa *Allah Subahanh wa Ta'ala* hua unajumuisha hali mbili ndani yake ambazo ni:

Kutuzuia na kutulinda Ibn Adam kutokana na kufanya Makosa au Dhambi kutokana na kasoro na udhaifu wetu Ibn Adam.

Kutuzuia na kutulinda sisi Ibn Adam kutokana na Adhabu zinazotokana na makosa hayo yaliyofanyika kutokana na kasoro za kimaumbile za Kibinadamu.

wani kabla ya kua Imam basi Habib al Ajemi alikua ni Mtu ambae Tajiri sana anaishi katika maeneo ya Mji wa Balkh. Na mbali ya kua na Utajiri lakini Habib alikua akijulikana katika Mji wake kama Papa wa Riba kwani alikua anakopesha watu kwa malipo ya Riba, na kwa kua watu wa Mji wake walikua Masikini basi walikua wanakopa kwake huku wakilia kwani anawaumiza na wao hawana la kufanya.

Ambapo hali hii iliwapelekea watu hao kumchukia Habib kiasi ya kua hata Watoto wakawa wanamnadia hadharani akitokea tu kwa kusema kua Anakuja Papa wa Riba, na bila ya shaka *Allah Subhanah wa Taala* akitaka kukuongoza basi hakuna atakaekupotosha. Hivyo ulipowadia mda wa kuongoka basi Habib Al Ajami akatafakkari na kisha akaona kua kumbe alikua amepotea, na akawa ni mwenye kujuta kwa aliyoyafanya.

Hivyo akaamua kuuza Mali zake zote, na kisha malipo yake yote akayatoa Sadaka zote huku akisema: **'Ya Allah hakika mimi nimefanya Makosa mengi sana, Hivyo nimeamua kuachana na makosa yangu hayo, na nakuomba unipokelee Sadaka yangu yote hii ninayoitoa ili niweze kupata Usamehevu wako.'**

Kisha baada ya kufanya Hijra ya Kivitendo kwa kuacahana na Mambo maovu basi Habib Al Ajami akaamua kufanya Hijra nyengine ambayo ni ya Kuhama kutoka katika Mji wake na kuelekea katika Mji wa Nchi nyengine kabisa. Na hivyo akatoka Afghanistan akaelekea Iraq katika Mji wa Basra.

Hivyo baada ya Habib Al Ajami kutubu kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kufanya Hijra kutoka katika Maisha yake ya Uasi kwa Mola wake na kuhamia kwenye Utiifu mbele ya Mola wake na hivyo kua ni mwenye kudumu na Istighfar ya Dhati na Iliyojaa Ikhlasi ndani yake basi kama tulivyosema akaamua pia kuhama katika Mji wake na kuhamia katika Mji wa Basra.

Na alipowasili katika Mji wa Basra basi akaulizia kuhusiana na Mwanazuoni bora kuliko wote, na akaambiwa kua ni Imam Hasan Al Basr na Imam Muhammad Ibn Sirrin. Hivyo

akaamua kusoma kwa Imam Hasan Al Basr lakini hapo hapo akawa anaenda kwa Imam Muhammad Ibn Sirrin pia.

Na kwa sababu Habib Al Ajami alikua ni Mtu wa Afghanistan basi alikua si mtu anaeweza kutamka Lugha ya Kiarabu kwa ufasaha.Hivyo ingawa alikua anahudhuria Darsa lakini alikua si mtu mwenye kusema sana. Kwani Lugha inamtatiza katika kutamka, hivyo siku Moja Imam Hasan Al Basr aliingia Msikitini akamkuta Habib Al Ajami anasali Sala ya Maghribi. Na kwa kua Lugha ya Kiarabu kwake ni shida kutamkika basi katika kusoma kwake *Surat At Fatiha* basi Habib Al Ajami alikua hawezi kutamka vizuri neno *Alhamd Lillah* na alikua anasema *Alhemd Lillah.*

Hivyo Imam Hasan Al Basr aliposikia namna anavyotamka basi akaona kua haifai kusali nyuma ya Habib Al Ajami na hivyo akasali peke yake. Ambapo katika Usiku wa siku hio Imam Hasan Al Basr alipolala akaota anaambiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: ‘**Katika Sala zako zote ulizosali basi nimezikubali isipokua hizi ya leo ya Magharibi uliyokataa kusali Nyuma ya Habib Al Ajami. Na hii ni kwa sababu wewe ulikua ni mwenye kuyaangalia Matamshi ya anaesali na huku akiwa ni mwenye kuona Ikhlasi iliyomo ndani ya Moyo wa anaesali’**

‘**Kwani mimi hua siangalii matamshi ya anaefanya Ibada bali hua nnaangalia ndani ya Moyo wa anaefanya Ibada husika, kua Moyo wake uko na nani? Kama Moyo wake uko pamoja nami basi nami hua pamoja nae, hivyo hata kama mtu anaefanya atakua na kisomo kizuri lakini kama Moyo wake hauko pamoja nami basi hua ni Malaika ndio weye kuiwakilisha Ibada hio mbele yangu na kisha mimi hua nna hiari ya kuikubali ama la. Ambapo kwa yule ambae Moyo wake hua upo pamoja nami katika Ibada basi mimi hua ni mwenye kuipokea Ibada hio mimi mwenyewe moja kwa moja na kuikubali**.’

Kwani hapa inabidi tufahamu kua tunamzungumzia Imam Hasan Al Basr ambae ni Imam wa Kizazi cha Tabiina ambapo nao watu wa kizazi hicho walikua wanamhesabu Imam Hasan Al Basr kua ni miongoni mwa Masahaba kutokana na Ucha Mungu na Ilm yake. Lakini hapo hapo Imam Hasan Al Basr kakutana na Mwanafunzi wake

Asiejua kitu, Habib Al Ajami anaesoma kwake na asiejua hata kutamka maneno ya lugha ya Kiarabu kwa ufasaha na hivyo hua na kasoro katika usomaji wake wa Qur'an. Ambae kutokana Istighfar anayoifanya Habib Al Ajami kuelekea kwa mwenye sifa ya Al Ghaffur basi Habib Al Ajami akapandishwa Darja na kunufaika kutokana na Ikhlasi katika Istighfar na katika kila Ibada yake. Na tunaona mfano wa Imam Habib Al Ajami ambae ingawa awali alikua ni Mtu muovu lakini Ikhlasi yake mbele ya Mola wake katika kuomba Msamaha unatuonesha umuhimu wa Ikhlasi katika kufanya Istighfar kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwa upande mwengine kuna tukio ambalo lilitokea katika kipindi hiki cha uhai wa Imam Habib Al Ajami na Imam Hasan Al Basr baada Hajjaj Ibn Yusuf alituma Askari wake wakamkamate Imam Hasan Al Basr, hivyo Imam Hasan Al Basr nae akakimbilia kwenye Nyumba ya Mwanafunzi wake yaani Imam wetu tunaemuangalia ambae ni Imam Habib Al Ajami.

Na bila ya shaka, Imam Habib Al Ajami ni Mtu alikua ametubu kwa Mola wake na hivyo ni mwenye kudumu katika kufanya Istighfar ya ukweli na kwa maana hio basi si Mtu ambae ni mwenye kusema Uongo. Kwani kwake yeye ni tofauti na mimi nawe, kwani kwake yeye Uongo ni Uongo hata uwe wa kumnusuru Mtu.

Hivyo baada ya Imam Hasan Al Basr kuingia ndani ya Nyumba ya Imam Habib Al Ajami, basi askari wakapata habari kua Imam Hasan Al Basr amejificha ndani ya Nyumba ya Imam Habib Al Ajami. Hivyo nao wakaenda na kumuuliza Imam Habib Al Ajami kwa kusema: **'Hakika sisi tumesikia na tunajua kua Hasan Al Basr amejificha Ndani ya Nyumba yako.'**

Imam Habib Al Ajami akasema: **'Naam, Bila ya Shaka kaingia sasa hivi ingieni Mtamkuta'**

Hivyo Askari hao wa Hajjaj Ibn Yusuf wakaingia ndani ya Nyumba hio na kutafuta kote kote Juu chini ndani nje, lakini hawakukiona hata kivuli cha Imam Hasan Al Basr mbali aya kua kweli alikua yumo ndani amekaa kitako anawaangalia.

Hivyo wakatoka wakamuuliza tena Imam Habib Al Ajami: '**Hivi wewe umesema Ukweli ama anatutania**?'

Imam Habib Al Ajami akasema: '**Kwa hakika mimi nimesema Ukweli na siwezi kukutanieni**' hapo Askari hao wakarudi tena ndani na kutafuta tena, lakini hawakuona Mtu.

Na baada ya kuchoka kutafuta basi askari hao wakajithibitishia kua Imam Hasan Al Basr hayumo ndani ya Nyumba hio nao wakaondoka.

Na mara walipoondoka basi Imam Hasan Al Basr akatoka ndani yake nyumba hio huku akisema kumwambia Imam Habib Al Ajami: '**Nnajua Kweli kua ni kutokana na Dua zako *Alhamd lillah* ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakuniweka wazi mbele ya Macho ya waliokua wakinitafuta, Lakini suali langu mimi kwake wewe Habib hivi jee ni kwanini wewe ukawaambia kua mimi nimo ndani**?'

Kwani Imam Habib Al Ajami akajibu: '**Ewe Mwalimu wangu, bila ya shaka kutokukuona kwao hakukutokana na Dua zangu bali kutokukuona kwao kumetokana na mimi kusema Ukweli, kwani huko ndiko kulikopelekea mimi na wewe kutoadhirika mbele yao'**

Imam Hasan Al Basr akamuuliza Habib Al Ajami: **'Hivi Jee ulisoma nini mpaka wakawa hawajaniona?'**

Imam Habib Al Ajami Akasema: **'Nilisoma *Ayat ul Kursy* mara 10, nikasoma *Amana Rasul mara* 10 na nikasoma *Qul Huwa Allahu Ahad* mara kumi kisha nikasema: 'Ya Allah hakika mimi ninakukabidhi Al Hasan kwenye Hifadhi yako hivyo mhifadhi.''**

Hapa kidogo tukumbushane kuhusiana na Umuhimu wa *Ayat Ul Kursiyu* kwani:

Mwenye kudumu kusoma Ayat Al Kursiyu mara kwa mara basi mbali ya kua hua na ulinzi wa Malaika wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini pia Darja yake ya Kidunia na Kiakhera Hua inapanda.

Kwani Mtu Mwenye Kudumu na *Ayat Ul Kursiyu* basi katika kuisoma kwake hua ni mwenye Kudumu na Adhkar, Kisomo cha Quran, Dua, na kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake.

Mwenye kusoma *Ayat Ul Kursiyu* 313 kwenye Mbegu za Mazao yake anayotaka kupanda Shambani basi Mazao hayo huzidi katika Uzalishwaji wake na kua na Barka zaid.

Mwenye Kudumu na kusoma *Ayat Ul Kursiyu* basi hua ni mwenye kujiamini, mwenye kukinai mwenye kua na uwezo wa kuepukana na matatizo na hatari na mwenye kua na utulivu ndani ya Moyo wake.

Mwenye kudumu na kusoma *Ayat Ul Kursiyu* na *Surat Ikhlas* si chini ya mara 10 kwa kila siku basi hua ni mwenye kupata ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ni mwenye kua mbali na ushawishi wa Ibilisi.

Mwenye kuyasomea Maji ya Mvua au Maji ya Zamzam *Ayat Ul Kursiyu* 50 na kisha akanywa basi Ufahamu wake hutanuka na hua na uwezo wa kuhifadhi zaid.

Mbali ya kua *Ayat Ul Kursiyu* ukiisoma Baada ya Sala basi huipandisha Sala yako Moja kwa Moja kwa Mola wako na kukutayarishia wewe ulie hai Mazingira ya Peponi lakini pia ukiwasomea waliokufa basi nao hunufaika na kupata Nuru ndani

ya Makaburi yao nawe pia hupata Malipo kutokana na kuwatumia wao kisomo hicho.

Hivyo *Ayat Ul Kursiyu* hufungua Milango ya Rehma, Hifadhi na Nusra kwa anaesoma na kwa anaesomewa na katika sehemu inayosomewa.

Ambapo ukisoma *Ayat Ul Kursiyu* na huku ukipulizia katika sehemu 6 nje ya mwili wako (Kulia, Kushoto, Mbele, Nyuma Juu na Chini) na kisha mara 1 ukajivutia hewa ndani ya Mwili wako basi hua tayari umeshajiingiza Ndani ya Ngome ya Ulinzi wa kutoonekana na Maadui zako katika sehemu uliyokuwepo.

Naam, katika kuishi wake basi siku moja Imam Habib Al Ajami alimualika Imam Hasan Al Basr nyumbani kwake kwa ajili ya Chakula cha Mchana. Wakati wamekaa wanakula mara mlango ukagongwa, na ulipofunguliwa basi Imam Habib Al Ajami akagundua kua aliegonga Mlango alikua ni Maskini ambae anaomba chakula.

Hivyo Imam Habib Al Ajami akasogea kwenye meza ya chakula na kisha akachota takriban Chakula chote kutoka kwenye Sahani iliyopo mbele ya Imam Hasan Al Basr na kisha akampelekea Muombaji aliepo Mlangoni. Imam Hasan Al Basr akashangaa, na kisha akasema: '**Habib, Hakika wewe ni Mtu mwenye Thamani kubwa sana, lakini kama ungekua una Ilm kubwa zaid basi ingekua bora kwako. Kwani inakuaje unachukua chakula chote ulichomualika Mgeni wako Nyumbani kwako na kisha unampa Mtu anaeomba, badala ya kwanza kukigawa Chakula hicho nusu ukamwachia Mgeni wako na nusi ukampa Muombaji?'**

Imam Habib Al Ajami akakaa kimya bila ya Kujibu, na mara akaingia Mfanyakazi, ambae alikua na Sinia iliyojaa Nyama ya Kondoo ya kuchoma na Mkate na Dirham 500 zimewekwa pembeni yake, Sinia hio akakabidhiwa Imam Habib Al Ajami huku akiambiwa kua ni zawadi ameletewa. Imam Habib Al Ajami akaiweka Sinia hio mbele ya Imam Hasan Al Basr, na kisha akachukua Dirham 500 hizo na kumpa Mfanyakazi huyo na kumwambia kua na yeye achukue hio ni zawadi yake. Na kisha akamkaribisha tena Imam Hasan Al Basr kula huku na yeye akianza kula Nyama ya Kondoo huyo huku akisema:

'Ewe Imam Wangu Wewe pia ni Mtu mwenye thamani kubwa sana, lakini kama ungekua na Imani Zaidi basi bila ya shaka ungekua Mtu bora zaidi, kwani Ilm yako inatakiwa lazima iwe ni yenye kuenda sambamba na Imani ndani ya Moyo wako'

Na vile vile kuna siku Imam Habib Al Ajami alimkuta Imam Hasan Al Basr akiwa amekaa kwenye ukingo wa Mto Euphrate akisubiri Mashua avuke. Kuelekea upande wa

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

pili. Hivyo Imam Habib Al Ajami akamuuliza baada ya kumsalimia Imam Hasan Al Basr: **‘Ewe Imam vipi mbona umesimama hapa?**’

Imam Hasan Al Basr akasema: **‘Nasubiri Mashua nivuke.’**

Imam Habib Al Ajami akauliza kwa kusema: **‘Ewe Imam, Hakika wewe ni Mwalimu wangu, lakini imekuaje? Kwani umenifundisha mengi na nimejifunza mengi kutoka kwako Ikiwemo Kuachana na kutokua na Ubaya na Ibn Adam wenzangu ndani ya Moyo wangu, Kuufunga Moyo wangu na kuachana na Dunia, Kupatwa na Mitihani kuna malipo makubwa ukiwa na Subra, Kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kila kitu changu ikiwemo kuweka Mguu wangu juu ya maji na kutembea juu yake baada ya kusema *Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahim.*’**

Na kisha Imam Habib Al Ajami akaweka Mguu wake ndani ya Maji ya Mto Euphrate na akavuka kwa kutembea bila ya kuzama wala kuroa maji. Huku akimwacha Imam Hasan Al Basr akiwa ameshangaa na hapo hapo kisha akazimia.

Alipozindukana Imam Hasan al Basr akajikuta amezungukwa na Watu na alipoulizwa kimetokea nini? Basi Imam Hasan Al Basr akasema: ‘**Mwanafunzi wangu amenikosoa na kisha akaondoka kwa kutembea juu ya maji, Nikazimia kwa sababu ya Kujiuliza Kama kesho Akhera tukiambiwa Tuvuke kwenye Sirat na mimi nikawa katika hali kama niliyokua nayo leo, Jee itakuaje hali yangu?**’

Imam Habib Al Ajami alikua na Joho la Sufi zuri sana ambalo alikua akivaa katika nyakati mbali mbali, hivyo safari moja alielekea kwenye ukingo wa mto na kisha akalivua Joho hilo na kuliweka chini Ardhini, na kuingia ndani ya Mto na kukoga ndani yake, kwa bahati akatokea Imam Hasan Al Basr ambae alishangaa kuona Joho la Imam Habib Al Ajami likiwa Ardhini, huku Imam Habib Al Ajami akiwa mbali ndani ya maji, hivyo akalichukua Joho hilo na kusema: ‘**Huyu Muajemi hajui hata thamani ya Joho hili, kwani halitakiwi kuachwa kwenye sehemu kama hii, linaweza likatoweka**’

Baada ya mda Imam Habib Al Ajami akatoka nje ya Mto na moja kwa moja kuelekea kwenye Joho lake na kumkuta Imam Hasan Al Basr akiwa anamsubiri na Joho hilo mkononi, hivyo akamuuliza Imam Hasan Al Basr: **‘Vipi imekuaje mbona umesimama hapa?’**

Imam Hasan Al Basr akasema: **‘Hivi wewe hujui kua Joho kama hili haliwezi kuachwa katika sehemu kama hii bila ya uangalifu? Kwani linaweza likapotea.’**

Imam Habib Al Ajami akasema: **‘Hili Joho mimi nililiwacha chini ya Usimamizi wa yule ambae ndie aliekuchagua wewe kua ni mwenye kulisimamia.’**

Imam Habib Al Ajami alifariki mnamo mwaka 120 Al Hijra katika mwezi 3 Rabi Al Thani ambayo ni sawa na mwaka 738 mnamo mwezi March.

SHAYKHA HAFSAH BINT SIRIN 31 AH

Katika kipindi cha Utawala wa *Amir ul Muuminin* Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu*, Jeshi la Waislam likiongozwa na *Sayf Allah* Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu* lilifanikiwa kuuingiza Uislam katika maeneo ya Ardhi ya Iraq, kwa njia ya mapigano na Waislam walishinda na wakateka baadhi ya Mateka ambapo miongoni mwao alikuwemo Mzee Sirin.

Mzee Sirin alichukuliwa na kupelekewa katika Mji wa Madina na akawa ni Mtumwa wa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambapo baadae Sirin akasilimu na kujipatia Ilm kubwa sana kutoka kwa Sahaba huyo Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* na akajikomboa kutoka kwenye Utumwa na kisha akamuoa mwanamke ambae ni Mtumwa aitwae Safiyyah ambae alikua ni Mtumwa alieachiwa huru na *Amir Ul Muuminin* Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* harusi ambayo ilihudhuriwa na Masahaba ambao miongoni mwao 18 walikua ni waliopigana katika vita vya Badr akiwemo Sahaba Ubbay Ibn Qaab *Radhi Allahu Anhu* ambae ndie alieikusanya Qur’an yote na kuiweka kwenye Mas-haf moja kutokana na amrisho la *Amir Ul Muuminin* Abu Baqr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* kuutokana na ushauri wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*

Matunda ya Ndoa hii baina ya Siriin na Safiyyah yaliyotoa watoto kadhaa akiwemo Fatma aliezaliwa mnamo mwaka 31 AH na Muhammad Ibn Sirin alizealiwa miaka miwili baadae na wengineo wengi ambao walikua ni Wanazuoni wa Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwemo Hafsa Bint Sirin, Karima Bint Sirin n.k

Ambapo inasemekana kua Karimah Bint Sirin alikua anakaa bila ya kuondoka kwenye Msala wake kwa muda wa miaka 15, kwani alikua akiondoka anapokua na haja ya kuondoka lakini mda wote alikua anautumia kwenye Msala wake.

Ama kuhusiana na Hafsah Bint Sirin basi anasema Imam Al Mizzi kua: ‘**Amesema Ilyas Ibn Muawiyyah kua: ‘Hakika mimi sijawahi kukutana na Mtu yeyote ambae nnaweza kumkubali zaidi ya Hafsah Ibn Sirin’ na akaulizwa: ‘Vipi kuhusiana na na Hasan Al Basr na Muhammad Ibn Sirrin?’ Ilyas Ibn Muawwiyah akasema: ‘Bila ya shaka siwezi kumkukubali yeyote zaidi yake kwani yeye aliihifadhi Qur’an yote wakati akiwa na umri wa miaka 12.’’**

Ambapo anasema Hisham Ibn Hassan kua: **‘Kila wakati ilipotokea kua Muhammad Ibn Sirin anakutana na jambo au kitu kinachomtatiza yeye baada ya kuulizwa kuhusiana na Qiraa cha Qur’an basi alikua akisema: ‘Nenda kamuulize Hafsa’’**

Hafsa Bint Sirin alikua pia ni Mwanzuoni mkubwa wa Ilm ya Hadith na pia ni Mwanazuoni mkubwa wa Ilm ya Fiqh kwani alikua amesoma kutoka kwa Sahaba Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* na ndio maana Hadith zake nyingi kutoka kwa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* zinapatikana kwenye Sahih Bukhari na pia katika vitabu vyengine sita vya Hadith zimo hadith kupita kwake.

Hisham Ibn Hasan anasema kua: **‘Hafsa alikua akiingia katika sehemu yake ya Kusali basi anasali Adhuhuri, Al Asr Maghrib, Isha na Fajr na kisha hubakia kwenye Msala hadi jua linapochomoza, kisha hurukuu na kuondoka, kisha anaenda kutia udhu upya na kulala hadi wakati wa Adhuhuri na kisha anarudi kwenye chumba chake cha Kusalia’**

Hishaam Ibn Hasan anaendelea kusema kua: ‘**Moyo wake Hafsa ulikua Laini na Macho yake yalikua ni yenye kutiririkwa na machozi usiku kucha, kiasi ya kua siku moja aliulizwa mfanyakazi wake: ‘Hivi jee inamuonaje Bibie wako?’ Mfanyakazi nae akajibu: ‘Ni Mcha Mungu sana isipokua anaonekana kua kama ni Mtu aliefanya Dhambi kubwa sana kwani Usiku kucha hua ni mwenye kulia na kusali**’

Hisham Ibn Hasan anaendela kusema kua: ‘**Hudhayl mtoto wa Hafsah alikua akikusanya kuni katika wakati wa Joto, kisha huzichanja na Hafsa alisema: ‘Nilikua nahisi Ubaridi na ulipowadia wakati wa Kipupwe Hudhayl alikua akija na jiko na kuliweka nyuma yangu wakati mimi nikiwa kwenye Msala nae hukaa na kuniwashia jiko kwa kuni alizozichanja ambalo hunipa ujoto joto na hua tunabakia katika hali hio hadi pale *Allah Subhanah wa Ta’ala* anapopenda**’

Na nnapotaka kumuondoa basi kwa kumwambia: ‘**Ewe Mtoto wangu nenda Nyumbani kwako’ basi hua ni mwenye kukumbuka kwanini hua ananifanyia hivyo, hivyo hua nnamuachia’ na alipofariki Dunia baada ya kuumwa na kifua basi nilikua nikihisi maumivu ndani ya kifua changu ambayo yalikua hayaondoki, hadi pale nilipokutana na aya isemayo:**

﴿وَلَا تَشْتَرُواْ بِعَهْدِ ٱللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا إِنَّمَا عِندَ ٱللَّهِ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ۝مَا عِندَكُمْ يَنفَدُ وَمَا عِندَ ٱللَّهِ بَاقٍ وَلَنَجْزِيَنَّ ٱلَّذِينَ صَبَرُوٓاْ أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Wala tashtaroo biAAahdi Allahi thamanan qaleelan innama AAinda Allahi huwa khayrun lakum in kuntum taAAlamoona; Ma AAindakum yanfadu wama AAinda Allahi baqin walanajziyanna alladheena sabaroo ajrahum bi-ahsani ma kanoo yaAAmaloona *(Surat An Nahl 16:95-96)*

Tafsir: ***Na wala Msinunue kwa thamani ndogo Makubaliano ya Allah kwani kile kilichopo mbele ya Allah ni bora kwenu nyinyi kama mngejua. Hakikua kile mlichokua nacho isipokua kitakwisha na kile kilichokuwepo kwa Allah kitabakia. Na kwa wale wenye Subra bila ya shaka watalipwa kwa ubora kulingana na yale mema waliyokua wakiyafanya.***

Alisema Hafsa Bint Sirin kua: **'Funga ni Ngao isiyovunjika hadi pale mtu atakapoivunja kwa Kusengenya.'**

Hafsah Bint Sirin alifariki mnamo mwaka 101 Al Hijra na maziko yake yalihudhuriwa na Wanazuoni wakubwa wakiwemo Hasan Al Basr na Muhammad Ibn Sirin.

IMAM SALAMAH IBN DINAR

Imam Salamah Ibn Dinar alikua ni Tabiina ambae alizaliwa katika Kipindi cha Masahabah katika Ardhi ya Uajemi na Mama yake alikua ni Mwanamke kutoka katika familia za watu wa Roman Empire.

Kwani tunapomzungumzia Imam Salamah Ibn Dinar basi hua tunamzungumzia Imam ambae alikua ni Mcha Mungu sana na mwenye Ilm kubwa sana, na hii ni kutokana na kua alikua ni mwenye kupenda kutumia mda wake kutafuta Ilm na pia kukaa na watu wenye kumkumbusha kuhusiana na Mola wake.

Imam Salamah Ibn Dinar Al Makhzumi alikua ni Mtu ambae haithamini kabisa Dunia na kila kitu kilichomo ndani yake.

Ambapo anasema Imam Abd Rahman Ibn Zayd kua: '**Imam Salamah Ibn Dinar alikua ni mwenye Hikma nyingi sana kuliko Mtu yeyote yule, na hakuna Mtu ambae aliidharau Dunia kama yeye**'

Kwani kila mara ilikua inapotokea kua Imam Salamah Ibn Dinar anaona Matunda ya chakula basi alikua ni Mwenye kusema kwa kuyaambia Matunda hayo:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

‘Hakika Matunda nyie nakuahidini kua nitakuleni Peponi na wala si hapa Duniani.’

Illikua ni kawaida ya Imam Salamah Ibn Dinar kuwausia watu kwa kusema kua: ‘**Enyi Watu Uficheni Ucha Mungu wenu kama vile mnavyojificha katika kufanya Madhambi yenu.’**
‘**Enyi Watu achaneni na kila kitu ambacho kitakupelekeeni kua ni wenye kutokipenda Kifo, ili msije mkawa na Khofu baada ya kufariki kwenu.’**

Kwani Imam Salamah Ibn Dinar alikua akipenda kusema kua: ‘**Hakika katika Dunia kuna sehemu 2 za Vitu. Ambapo sehemu ya kwanza ni kwa ajili yangu na Sehemu ya Pili ni kwa ajili ya Watu wengine.’**

‘**Ama kuhusiana na kile ambacho ni kwa ajili ya wengine basi nitafanya kila njia ili nisikichukue kilicho chao, Ili riziki yangu isizuiliwe kwa ajili yangu na riziki ya wengine isizuiliwe kutokana nami.’**

Imam Salamah Ibn Dinar alisema: **‘Kila kilichopita katika Dunia hii hua ni sawa na Ndoto na kila kilichobaki hua ni sawa na matumaini.’**

‘Natamani kua nyinyi mngekua mnailinda Dini yenu kama vile ambavyo mnavyojilinda kutokana na uchafu wa viatu vyenu.’

‘Kama ingekua njia ya kuingilia Peponi inatokana na kuachana na unavyovipenda katika maisha haya basi bado Pepo ingekua inastahiki zaidi ya hivyo, kwani itakuaje mtu ataingia Peponi huku akiwa ni mwenye kuachana na sehemu moja kati ya sehemu 1000 anazozipenda Ulimwenguni? Kwani jee itakuaje kama ikiwa mtu ataokoka na moto ambao maumivu yake hua ni sawa na maumivu ya sehemu moja kati ya sehemu 1000 ya yale anayoyachukia Ulimwenguni?’

Imam Salamah Ibn Dinar ambae alisema: **‘Ni Nani Kama Ibilisi, Kwani kama hukumtii basi hawezi kukudhuru, lakini kama ukimtii basi hakunufaishi bali hukufilisi.’**

Na pia akahoji kwa kusema: **‘Ewe Ibn Adam hivi huoni wewe kua Mola wako anakunufaisha kwa Neema na Rehma bila ya kusita? Hivyo kwanini Unamuasi Mola wako? Na hutaki kumtii Mola wako?’**

Siku moja Khalifa wa Utawala wa Banu Ummayah wa Damascus aitwae Sulayman Ibn Abd Ul Malik alipotembelea Mji wa Madina baada ya Ibada ya Hija, basi aliomba kukutana na Watu waliokutana na Masahaba katika Maisha yao.

Hivyo akaambiwa kua mmoja wapo ni Imam Salamah Ibn Dinar, kwa hivyo Khalifa Sulayman Ibn Abd Ul Malik akaomba Imam Salamah Ibn Dinar aitwe mbele yake na alipofika basi akaanza kumhoji: **'Ewe Abu Hazim kwanini wewe si Muaminifu kwangu mie?'**

Hivyo Imam Salamah Ibn Dinar akasema: **'Ewe *Amir ul Muuminin* hivi ukisema kua mimi si Muaminifu hua unamaanisha nini?'**

Khalifa Sulayman akajibu: **'Naam..Kuna Watu wakubwa wakubwa waliposikia kua nimekuja Madina basi nao wamekuja kwangu lakini wewe hujaja.'**

Imam Salamah Ibn Dinar akasema: ***'Ewe Amir ul Muuminin,* Hakika mimi wewe sikujui na wala wewe hunijui, na ndio kwanza tumejuana hivyo utasemaje kua mimi sio Muaminifu?'**

Hapo Khalifa Sulayman Ibn Abdul Malik akaangalia chini kwa kutahayari, kisha akawaambia waliopo mbele yake: **'Naam Hakika Imam Yuko Sahih na mimi nimekosea.'**

Khalifa Sulayman akasema: **'Niambie Ewe Abu Hazim kwanini sisi Ibn Adam hua tunaogopa Kifo?'**

Imam Salamah akasema: **'Kwa sababu sisi hua tunastawisha Dunia yetu na kuiangamiza Akhera yetu, na hivyo bila ya shaka hua tunachukia kurudi kwenye maangamizo.'**

Khalifa Sulayman akasema: **'Uko sahih, hivyo Ewe Abu Hazim, sisi tuna sehemu gani kesho mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hapo baadae?'**

Imam Salamah akasema: **'Linganisha matendo yako na Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha baada ya hapo ndio utaweza kujua.'**

Khalifa Sulayman akasema: **'Naweza kuyaona haya kwenye aya gani?'**

Imam Salamah akasema: **'Katika aya zisemazo**

﴿إِنَّ ٱلْأَبْرَارَ لَفِى نَعِيمٍ۝وَإِنَّ ٱلْفُجَّارَ لَفِى جَحِيمٍ۝﴾

Inna al-abrara lafee naAAeemin; Wa-inna alfujjara lafee jaheemin *(Surat Al Infitar 82: 13-14)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: ***Hakika wale waliokua wasafi wako kwenye Neema, na wale waliokua wachafu wako kwenye Moto.***

Khalifa Sulayman akauliza: **'Kama ni hivyo basi ziko wapi Rehma za Allah?'**
Imam Salamah akasema:

﴿وَلاَ تُفْسِدُواْ فِى ٱلأَرْضِ بَعْدَ إِصْلاَحِهَا وَٱدْعُوهُ خَوْفاً وَطَمَعاً إِنَّ رَحْمَةَ ٱللَّهِ
قَرِيبٌ مِّنَ ٱلْمُحْسِنِينَ﴾

Wala tufsidoo fee al-ardhi baAAda islahiha waodAAoohu khawfan watamaAAan inna rahmata Allahi qareebun mina almuhsineena *(Surat Al Araf 7: 56)*

Tafsir: ***Na wala msifanye Israfu juu ya Ardhi baada ya kuwekwa sawa na muombeni yeye (Allah Subhanah wa Ta'ala) kwa khofu na Matumaini, kwani bila ya shaka Rehma ya Allah iko karibu na wenye kufanya Mema.***

Imam Salamah akasema: '**Wenye kufanya Mema watarudi kwa Mola wao kama msafiri anaerudi Nyumbani kwake, wakati watu waovu watarudi kama watumwa waliokimbia na kisha wakakamatwa na kurudishwa kwa nguvu kwa Mmiliki wao.'**

Khalifa Sulayman akaanza kutokwa na machozi huku akisema: '**Hivi Jee nitawezaje kujirekebisha ewe Abu Hazim?'**

Imam Salamah akasema: '**Kwa kuachana na mapambo ya Dunia na kua na heshima.'**

Khalifa Sulayman akasema: '**Hivi jee nitawezaje kutumia mali yangu ili nipate kuhesabiwa kua ni msafi mbele ya** ***Allah Subhanah wa Ta'ala*****?'**

Imam Salamah akasema: **'Kama utaikusanya kwa njia sahih na kuiweka kwenye njia sahih na ukaigawa sawia ki haki kwa watu.'**

Khalifa Sulayman akauliza: '**Hivi jee ni kitu gani chenye manufaa zaidi?'**

Imam Salamah akasema: **'Maneno ya Ukweli yanayosemwa mbele za watu wanaoogopwa na wanaotegemewa kutoa msaada.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Khalifa Sulayman akauliza: **‘Ewe Abu Hazim hivi jee ni Dua gani ambayo ni Mustajaba zaid?’**

Imam Salamah akajibu: **‘Dua ya Mja mwema kwa ajili ya Mja mwema.’**

Khalifa Sulayman akauliza: **‘Jee Sadaqah ii ndio bora zaidi.’**

Imam Salamah akasema: ‘**Sadaqah ya kutoka kwa mwenye shida kuelekea kwa mwenye shida bila ya masimbulio wala maneno mabaya.’**

Khalifa Sulayman akauliza: **‘Jee ni nani mtu mwenye ukarimu na heshima zaidi mbele ya watu?**’

Imam Salamah akajibu: **‘Wale watu wenye kuuona Utiifu kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kisha wakaufanyia kazi na kisha wakausomesha kwa wengine.’**

Khalifa Sulayman akauliza: **‘Jee ni nani Mtu mjinga zaidi?’**

Imam Salamah akajibu: ‘**Ni yule mtu ambae ameathiriwa na matamanio ya marafiki zake hata kama marafiki hao wakiwa ni Madhalim, na hivyo hua ni mwenye kuiuza Akhera yake kutokana na manfuaa ya Dunia ya wengine.’**

Khalifa Sulayman akauliza: ‘**Jee unaweza kuungana nasi na hivyo tukajifunza vitu kutoka kwako?**’

Imam Salamah akajibu: **‘La Haiwezekani.’**

Khalifa Sulayman akauliza: **‘Kwa nini?’**

Imam Salamah akajibu: **‘Kwa sababu mimi nna khofu ya kua nitakua ni mwenye kuelemea upande wako kisha *Allah Subhanah wa Ta’ala* ataniadhibu kwa kunipa mitihani hapa Duniani na kesho Akhera.’**

Khalifa Sulayman akasema: ‘**Niambie shida yako basi nipate kukusaidia.’**

Imam Salamah akanyamaza kimyaa, hadi pale Khalifa Sulayman alipolirudia tena suali hilo ambapo nae akajibu: **‘Shida yangu ni kuachiwa huru na Moto na kua na hamu ya kuingizwa Peponi.’**

Khalifa Sulayman akajibu: **‘Ama kuhusiana na hila basi liko nje ya uwezo wangu.’**

Imam Salamah akajibu: **'Basi na mimi sina shida wala haja nawe.'**

Khalifa Sulayman akasema : '**Basi nakuomba uniombee Dua.'**

Imam Salamah akanyanyua mikono juu na kusema: '**Ya Allah! Kama Sulayman ni mja wako umpendae, basi mrahisishie kwa ajili yake njia ya kufanya mema hapa Duniani na kesho Akhera, na kama akiwa ni mmoja kati ya maadui zako, basi muongoze kama utakavyo..Aaamiin.**'

Ambapo mmoja kati ya watu wa Khalifa Sulayman waliowazunguka akamuuliza Imam Salamah: '**Hivi kwanini umemuombea Dua kama hio? Yenye kuhoji kuhusiana na hali yake Amir ul Muuminin kama mzuri au muovu?'**

Imam Salamah akasema: '**Inavyotakiwa ni kudhihirisha kuhusiana na kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wala sio kuyaficha yaliyomo ndani yake.**'

Kisha Imam Salamah akamwangalia Khalifa Sulayman na kumwambia: '***Ya Amir Ul Muuminin*, watu waliotangulia kabla yetu walikua wakiishi katika wema na furaha pale ilipokua viongozi wao walipokua wanaenda kwa Wanazuoni kwa ajili ya kujihesabia nafsi zao. Na kisha wakafuata watu ambao waliokua na hali ya chini ambao wana Ilm ya mambo mengi sana na kuhudhuria kwa Viongozi kwa ajili ya kujitafutia Dunia yao'.**

Na hivyo Viongozi wamekua hawaangalii wala hawawajali Wanazuoni wao, hivyo nao wakawa ni watu dhaifu na wanyonge sana mbele ya macho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, hivyo kama sehemu ya Wanazuoni watakua hawana hamu na kile kilichopo kwa Viongozi wao basi bila ya shaka Viongozi watawafuata Wanazuoni hao kwa ajili ya kujitafutia Ilm kutoka kwao. Lakini kutokana na kua Wanazuoni wanataka kile kilichopo kwa Viongozi, basi Viongozi hao hawajali kile kilichopo kwa Wanazuoni.'

Hivyo Khalifah Sulayman akasema: '**Naam uko sahih, hivyo niongezee ushauri wako, kwani sijaona mimi mtu ambae hikma zake ziko karibu na ulimi wake zaidi yako.'**

Imam Salamah akasema: **'Kama wewe ni Mtu ambae ni mwenye kutaka ushauri basi kile nilichokisema mwanzo kinakutosheleza, lakini kama si miongoni mwao watu hao basi haina haja kwangu mie kutia mshale wa upinde kwenye Upinde ambao hata hivyo hauna Kamba ya kuvutia.'**

Khalifa Sulayman akasema: **'Ewe Abu Hazim, nategemea kua unataka kuniusia zaid.'** ambapo Imam Salamah akasema: **'Sawa, nitakuusia kwa kifupi kabisa kua**

Mtukuze *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hakikisha kua hakuoni katika hali ambayo hataki kukuona na kukuweka wewe kwenye sehemu aliyokuweka.'

Khalifa Sulayman akaaga kwa kusema: **'Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akulipe kila la kheri ewe Mcha Mungu anaependa kuusia.'**

Imam Salamah Ibn Dinar aliporudi Nyumbani basi akakutana na mfuko uliojaa Dinar ambao ameletewa kua kama ni zawadi yake, na ndani yake mlikua mna ujumbe usemao kua: **'Tumia zawadi hii kwa ajili yako, na bado kuna nyengine kama pale itakapomalizika'** hivyo Imam Salamah akaandika barua ambayo inasema:

'Ewe Amir Ul Muuminin hakika mimi nnatafuta ulinzi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hivyo kama masuali yako kwangu yalikua hayana maana na na majibu yangu kwako yalikua siyo, basi Wa Allahi sitaki hili kua ni lenye kutokea kwako wewe, na wala lisitokee kwangu mie, kwani kama hizi Dinari ni malipo kwa ajili ya yale niliyokuambia, basi kwangu mie bora ni kula mzoga wa Nguruwe pale inapokua hakuna njia nyengine kwani utakua ni halali kuliko Dinari hizi.'

'Na kama itakua hizi Dinari ni halali yangu kutoka kwenye *Bayt ul Maal* basi suali langu mie ni kua: Hivi jee unawalipa na Waislam wengine kama hivi unavyonilipa mie?'

Na kisha Imam Salamah Ibn Dinar akaichukua Barua hio na kuitumbukiza kwenye mfuko wa Dinari kutoka kwa *Amir Ul Muumini* na kumrudisha na Dinari zake.

Nyumba ya Imam Salamah Ibn Dinar ilikua ni Madrasa ambayo ilikua inatumiwa na kila mtu mwenye kutaka kutafuta Ilm, ambapo safari moja ndani yake Nyumba hio ilitembelewa na Imam Abd Rahman Ibn Jarrir na mtoto wake ambapo Imam Abd Rahman Ibn Jarrir akamuuliza Imam Salamah kwa kusema: **'Ewe Abu Hazim hebu nielezee kuhusiana na kua na Moyo uliokua hai.'**

Imam Salamah akasema: **'Hupatikana kwa kujisafisha kutokana na makosa makubwa makubwa, kwani ni pale tu Ibn Adam anapoamua kuachana na Dhambi kubwa basi Moyo wake hua ni wenye kufunguka kwa ajili yake. Usisahau ewe Abd Rahman kua: 'Kile kidogo unachokidharau katika Dunia hii hua ni chenye uzito mkubwa katika Akhera yetu, hivyo kila fadhila utakayoifanya ambayo itakua haikukaribishi karibu na Mola wako, basi bila ya shaka itakua ni yenye kugeuka kua ni Adhabu kubwa kwako''**

Hivyo mtoto wake Imam Abd Rahman akauliza kwa kusema: **'Walimu wetu ni wengi hivyo jee ni nani tuwafanye kua ndio mfano wa kuigwa kwetu?'**

Imam Abd Rahman akasema: **'Ewe Mtoto wangu fuata mfano wa wale wenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* wanapokua katika sehemu ya faragha na wale wanaojikinga na maovu, na kujiboresha kutoka katika ujana wao na kuendelea hadi uzeeni mwao. Fahamu ewe mtoto wangu kua: 'Hakuna siku hata moja inayochomoza Jua bila ya kua ni yenye kumjia yule Mwanafunzi mwenye kutafuta Ilm mwenye Matamanio, na hivyo hua ni mwenye kukimbizana nayo hadi kufikia mwisho wake mtu huyo, hivyo kama Ilm yake itayashinda matamanio yake basi siku hio hua ni ya mafanikio kwake mtu huyo, lakini kama matamanio yake yakiizidi Ilm yake basi Mtu huyo hua amekula hasara kwa siku hio.''**

Imam Abd Rahman akamgeukia Imam Salamah na kumuuliza: **'Ewe Abu Hazim, mara nyingi sisi Ibn Adam hua ni wenye kupata vile ambavyo tunastahiki kuonesha shukrani kutokana navyo, hivyo jee ni ipi hali stahiki ya kuonesha shukran?'**

Imam Salamah akasema**: 'Kwa kila sehemu ya kiungo cha Mwili wetu hua kina njia yake ya kuonesha Shukrani.'**

Imam Abd Rahman akauliza: **'Kwa hivyo Jee tutaonesha vipi shukrani kwa kutumia macho yetu?'**

Imam Salamah akasema: **'Pale unapoona kitu kizuri basi litanue jicho lako na unapokiona kitu kibaya basi lifunge.'**

Imam Abd Rahman akauliza: **'Jee ni vipi tunaweza kuonesha shukrani kwa kutumia masikio yetu?'**

Imam Salamah akasema: **'Unaposikia Jema basi unalidhihirisha na unaposikia ovu basi unalificha.'**

Imam Abd Rahman akauliza: **'Jee ni vipi tunaweza kuonesha shukrani kwa kutumia mikono yetu?'**

Imam Salamah akajibu: **'Usiitumie kwa kuchukua kile ambacho kisichokua chako, na wala usiitumie kuzuia haki ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwani usisahau wewe Abd Rahman kua: 'Yeyote yule anaejibania kwa kuonesha shukrani zake kwa kutumia Ulimi tu bila ya kutumia viungo vyengine, basi hua ni sawa na mtu ambae anazo nguo lakini amezitundika kwenye henga.''**

Imam Salamah Ibn Dinar alikua ni Mtu ambae mwenye Taqwa na asiependa Kujionesha kwani alikua ni mwenye kujifunika Pazia la Unyeyekevu na alikua ni mwenye kukesha katika *Qiyam Al Layl* kwani alikua ni mwenye Kuiona Dunia ni sehemu yenye Mapambo ya Mpito na Kifo kua sio Kitu kikubwa sana chenye kuhitaji kuogopewa.

Kwani kutokana na Ucha Mungu wake basi alikua tayari katika wakati wowote kuingia ndani ya eneo la kukutana na Mola wake. Huyu alikua ni Imam ambae Jina lake ni miongoni mwa majina ya watu ambao yako hai na yanakumbukwa mpaka leo kutokana na wema Wake.

Ambapo kama tunavyoona pale baada ya kufariki Khalifa wa Banu Ummayad aitwae Sulayman Ibn Abd Ul Malik basi mamlaka ya Utawala wake yakachukuliwa na Khalifah Hisham Ibn Abd Ul Malik, hivyo alipotembelea katika Mji wa Madina akaomba kukutana na Imam Salamah Ibn Dinar na hivyo Imam Salamah Ibn Dinar akakubali Mualiko huo.

Na alipofika Mbele yake basi Khalifa Hisham Ibn Abdul Malik akamwambia Imam Salamah Ibn Dinar kua anaomba amuusie kwa kumpa wasia kutoka kwake hivyo Imam Salamah Ibn Dinar akamwambia Khalifa Hisham Ibn Abd Ul Malik kua: **‘Muogope Allah na Jitenge na Mapambo ya Dunia kwani Utakuja kuulizwa na Mola wako juu ya kila Ulilolifanya, Utaulizwa Ulikichumaje kile cha Halali yako na Utaadhibiwa Kutokana na kile kilichokua Haram kwako.’**

Imam Salamah Ibn Dinar akaendelea kusema kua: **Fahamu ewe *Amir ul Muuminin* kua: ‘Viongozi bora zaidi ni wale ambao wanaowapenda Wanazuoni na Wanazuoni Wabaya zaidi ni wale ambao Wanaowapenda zaidi Viongozi.**’

Khalifa Hisham Ibn Abdul Malik akataka kumpa zawadi Imam Salamah Ibn Dinar lakini hata hivyo Imam Salamah Ibn Dinar akakataa zawadi hio huku akisema: **‘La, ewe *Amir Ul Muuminin*, kwani kabla ya kuja kwako mimi niliahidi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: Kama atanipa atakachonipa basi Nitamshukuru na Kama akinipokonya kitu basi Nimeridhika juu yake.’**

Subhanah Allah!

Huyo ndie Imam Salamah Ibn Dinar ambae alifariki katika Mji wa Madina mnamo mwaka 140 Al Hijra.

IMAM HAMMAM IBN MUNABIH

Imam Abu Uqbah Hammam Ibn Munabih Ibn Kamil Ibn Shaykh Al Yamani Al Sanai Al Abnai alikua ni Mwanazuoni wa Ilm ya hadithi aliezaliwa katika Mji wa Sanaa nchini Yemen na alikua ni Kaka yake Imam Wahb Ibn Munabih. Alikua akiitwa Al Abnai kwa

sababu asili yao ilikua ni watu wa Irani waliohamia katika ardhi ya Yemen kabla ya kuingia Uislam katika ardhi ya Yemen.

Imam Hammam Ibn Munabih alikua ni Thiqah kwani alisoma kutoka kwa Masahaba kadhaa wakiwemo Abu *Hurayrah Radhi Allahu Anhu*, Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah IbnZubayr *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* n.k

Imam Hammam Ibn Munabih alikua ni mwenye kupenda sana kusoma, kuandika vitabu kupigana vita vya jihadi kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na alikua ni mfanya biashara, hivyo alikua ni mwenye kumletea vitabu pia ndugu yake ambae Imam Wahb Ibn Munabih ambae pia kwa upande mwengine alikua ni miongoni mwa Wanafunzi wake ambapo pamoja nae miongoni mwa Wanafunzi hao ni pamoja na Imam Aqil Ibn Malik Ibn Munabih, Imam Ali Ibn Hasan, Imam Ma'mar Ibn Rashid ambae ndie Mwalimu wa Imam Abd Razak Al Sanani, na wengineo. Imam Hammam Ibn Munabih alifariki mnamo mwaka 131 Al Hijra.

Imam Hammam Ibn Munabih na alikua ni muandishi pia ambae aliaziandika Hadith 140 alizozisoma kutoka kwa Abu Hurayrah, ambapo kitabu hicho kilikua kikiitwa *Sahifat Sahih* hizi ni hadith pia zilizoandikwa na Imam Ma'mar Ibn Rashid ambapo kutoka kwake zikanukuliwa na Imam Abd Razak Al Sanani na kisha zinanukuliwa na Imam Ahmad Ibn Hanbal katika kitabu chake cha *Musnad Imam Ahmad,* na pia hadith zake zimo kwenye kitabu cha Imam Bukhari.

Imam Yahya Ibn Maina asema kua: '**Imam Hammam Ibn Munabih ni Thiqah'** ambapo huo pia ndio mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Hanbal, na kwa upande wa Imam Al Ijli basi yeye akasema kua: '**Al Hammam ni mwenye kutoka katika kizazi cha Tabiina na ni Thiqah wa ardhi ya Yemen.'**

Imam Sufyan Ibn Uyaynah akasema kua: **'Mimi nilimuona Al Hammam kwa mda wa miaka 10 na alikua ni mwenye kunufaisha sana'**

Ambapo anasema Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Hakika nyinyi mnakuwa vilema kutokana na Unafiq, hivyo jihadharini kutokana na unafiq, kwani kusema bila ya uthibitisho hua ni kusema Uongo katika Dunia na unapokua hutaki kununua bidhaa basi usimsababishie mnunuzi mwengine madhara ya kutotaka kununua, msioneane wivu na wala msishindane kuhusiana na kukimbilia mambo ya Kidunia na wala msizidishe chumvi katika maneno yenu, msichukiane na wala msiachane, enyi waja wa Allah kuweni Ndugu.'**

Na akasema Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kuna saa katika siku ya Ijumaa ambapo kama Muislam ataomba ndani yake kutoka kwa Mola wake, basi bila ya shaka *Allah Subhana wa Ta'ala* atampa kile anachokiomba.'**

Amesema tena Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Malaika hua wanakuja kwenu nyie na kubadilishana Usiku na mchana, na hupishana katika Nyakati za Sala ya Alfajir na Al Asr, ambapo Malaika anaetumia mda wake pamoja nawe anapofika mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ingawa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kujua hali yako, lakini hua ni mwenye kuuliza: 'Vipi kuhusiana na Mja wangu mmemuwacha akiwa vipi? Ambapo Malaika hao hua ni wenye kusema: 'Tumemuwacha akiwa anasali''**

Na akasema tena Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* alipoviumba viumbe basi aliandika kwenye *Lawh Al Mahfudh* ambayo ilikua mbele yake juu ya Arshi yake kua: 'Rehma zangu zimeipita Ghadhabu zangu.''**

Na akasema Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kila Mtume hua ni mwenye kua na Dua Maalum ambayo hua inapokewa, ambapo mimi kwa upande wangu nimependa kua niiwache dua yangu hio nisiiombe hadi katika siku ya Malipo kwa ajili ya kuuombe Umma wangu.'**

Na akasema pia Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaenitii mimi hua ni mwenye kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala* na mwenye kuniasi mimi basi hua ni mwenye kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na yeyote atakae mtii mwenye amri juu yake, basi atakua amenitii mimi na yule atakaemuasi mwenye amri juu yake basi atakua ameniasi mimi.'**

Na akasema tena Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Siku ya Kiama kitakuja pale Jua litakapochomoza kutoka katika upande linapotua, ambapo watu wote watakaozaliwa katika sehemu itakayozama jua hilo basi watakua ni Wenye Kuamini, lakini hata hivyo Imani hio haitowafaa kitu watu hao ambao hawakuamini hapo kabla au hawajachuma chochote kutokana na Imani yao'**

Na akasema tena Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Usimuangalie Mtu yeyote aliekua yuko chini yako Kiimani katika Dini kwani Utakua ni mwenye kujiona na kujiangamiza, bali waangalie wale walio juu yako katika Dini, kwani hivyo ni heri kwako. Usiwaangalie wale**

wenye Mali zaidi yako, kwani utahuzunikia na Majaaliwa ya Allah juu yako, kisha akasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Muangalie yule ambae anahangaika kutafuta riziki yake kwa tabu na kisha hapo ndio utakua na shukrani kwa neema alizokujaalia Mola wako.'

Na akasema tena Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: 'Wasaidie wenzako ili nami nipate kukusaida wewe'**

Na akasema tena Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Imam anatakiwa kufuatwa, Unapomfuata Imam kwenye Sala basi usipingane nae, Imam Anaposema Takbir, basi nawe sema Takbir, anaporukuu basi nawe rukuu, anaposujudu basi nawe sujudu na Imam anapokaa kitako basi nawe kaa kitako.'**

Na akasema tena Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Amesema *Allah Subahan wa Ta'ala* kua: 'Mja wangu anapopanga kufanya Jema, na kisha akashindwa kulifanya kutoka na jambo lolote basi mimi humuandikia kua ni mwenye kulifanya mara moja jambo hilo, kwenye kitabu chake, na akilifanya basi humuanidkia kua amefanya mara 10 zaidi yake. Na pia Mja wangu anapokua anakusudia kufanya Jambo ovu, basi mimi hua nnamsamehe kama hakulifanya ovuhilo, na kama akilifanya basi hua nnamuandikia kua amefanya ovu moja.'**

Na akasema tena Imam Hammam Ibn Munabih kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Utajiri si kua na Mali nyingi wala Afya Nzuri bali Utajiri hua ni wa kua na Moyo Msafi'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM WUHAYB IBN WARD

Imam Abu Uthman Abd Al Wahab Wuhayb Ibn Ward alizaliwa katika Mji wa Makkah na kua ni mwenye kukulia katika mazingira mazuri ya kujitafutia Ilm yake kutoka kwa baadhi ya Masahaba wa *Rasual Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* na kutokana na kua ni mwenye kupenda kutafuta Ilm na kufanya Ibada basi alikua ni mwenye kupata, Ilm kubwa sana na ni mwenye kuaminika sana kutokana na Ucha Mungu wake pia.

Imam Wuhayb Ibn Ward alikua ni kuishi katika wakati wa kipindi cha kina Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Ibrahim Ibn Adham, Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Fudayl Ibn Iyad na wengineo ambapo katika wakati ambao Imam Sufyan Ath Thawry

alipokua akija katika Ibada ya Hija baada ya kutoa Darsa basi hua ni mwenye kuwaambia Wanafunzi wake kua: '**Nyanyukeni sasa hivi tuende kwa Daktari wa Nafsi zetu Wuhayb Ibn Ward tukapate maneno ya hekima kutoka kwake.**'

Imam Wuhayb Ibn Ward alikua ni Mtu ambae asiecheka, kwani mda mwingi alikua ni mwenye kulia kwa ajili ya Mola wake na alikua akisema: '**Mimi sifahamu inakuaje Nyoyo za wale ambao ni wenye kujua kuhusiana na kukusanywa katika siku ya Malipo na kuhojiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* zinaweza kua ni zenye kucheka**'

Na ilikua kila inapoingia katika wakati wa Usiku basi Imam Wuhayb Ibn Ward alikua si mwenye kulala kwani alikua ni mwenye kuhuisha Usiku wake na hivyo alikua ni mwenye kusali Sala ya Al Fajir kwa Udhu wa Salat Isha, alipoulizwa hivi ni kwanini akawa halali usiku basi alisema; '**Nimekua katika hali hii kwa mda mrefu kwa sababu ya Aya za Qur'an zinazozungumzia Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua zinanikosesha usingizi'**

Ambapo kila baada ya Sala basi Imam Wuhayb Ibn Ward alikua akiomba Dua kwa kusema: '**Ya Rabbi kama ikiwa kuna kasoro katika Sala yangu basi nakuomba unisamehe, na kama nimefanya kosa kubwa au dogo basi pia nisamehe kutokana nayo'**

Safari moja Imam Muhamamd Ibn Al Munkadir alikua anaumwa, hivyo Imam Wuhayb Ibn Ward akamtembelea kwa ajili ya kumtizama na alipofika akamuuliza anaumwa na nini na wapi panamuuma, hivyo Imam Muhammad Ibn Al Munkadir akamuonesha sehemu iliyokua ina maumivu na hapo hapo Imam Wuhayb Ibn Ward akauchukua mkono wake na kuuweka kwenye sehemu hio na kisha akasema: '***Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahim,* kama hii *Biismi Allahi Rahmani Rahim* ikisomewa kwa unyenyekevu na ihklasi kwenye Mlima basi Mlima huo utamomonyoka'** na hapo hapo maumivu ya Imam Muhammad Ibn Al Munkadir yakatoweka na akapona.

Imam Wuhayb Ibn Ward aliulizwa na Wanazuoni wenzake: '**Utajibu nini kama ukiulizwa Hivi jee unatamani kufariki haraka ili uonane na *Allah Subhanah wa Ta'ala*? Au unataka Uishi zaidi kwa ajili ya kupata kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* zaidi? Au bora uwe ulietosheka na Majaaliwa ya Allah *Subhanah wa Ta'ala* juu yako na hivyo kukaa kimya bila ya kusema chochote?'**

Imam Wuhayb Ibn Ward akasema: 'Hakika mimi nitanyamaza kimya kwani chochote kile atakachonijalia *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi nitakubaliana nacho kwani mimi nampenda yeye na nimeridhika nae' hapo Imam Sufyan At Thawyr ambae alikuwepo pamoja nao Wanazuoni hao waliouliza basi kasema**: 'Ama kwa hakika Umetoa Jibu lililobora kabisa.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Anasema Imam Wuhayb Ibn Ward kua: **‘Kuna siku nilikua ninasali kwenye Hatim Sharif, mara baada ya kumaliza kusali nikasikia sauti inatoka ndani ya Al Kaabah ikisema: ‘Ewe Jibirl hakika mimi nililalamika kwanza kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kisha kwkao wewe, kua mimi nimechoka na maneno yasiyoka na maana na mawazo ya wale wanaonizunguka, hivyo kama hali ikiendelea kama hivi basi mimi huenda nikachanika vipande vipande na kila kipande kikaenda upande wake kilikotoka.’**’

Imam Wuhayb Ibn Ward anasema pia kua: ‘**Siku moja nilikua nimejinyoosha kitandani mwangu na mara nikasikia sauti ikisema: ‘Mmiliki Mtu ambae ni mwenye kumtii *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kusimamia maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta’ala’* nami nikauliza kwa kusema: ‘Allah akuingize kwenye Rehma zake, hivi unazungumzia nini?’**

Hivyo mtu huyo akanionesha mimi Muhuri wake, na nilipouangalia nikaona kua umeandikwa *Ayn Mim Ra,* na kisha haukuchukua mda isipokua Umar Ibn Abd Al Azizi akawa Khalifa na kuongoza kwa kutumia Kitabu cha Allah na kumtii.’

Na siku moja nilikua nimekaa kwenye ukingo wa Mto mara akatokea mtu na akanishika mkono na kuniambia kua: **‘Ewe Wuhayb! Hakika uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni mkubwa kuliko wako, hivyo kila unavyozidi kumuogopa basi ndio unavyokua na ukaribu zaid kwake na ndio unavyozidi kua ni mwenye kuona haya mbele yake.’**

Imam Wuhayb Ibn Ward alisema: **‘Hakuna kitu kinachoburudisha Moyo, na pia kumfanya mtu kua ni mwenye huzuni na mwenye huzuni zaidi kuliko kusoma Qur’an huku ukiwa ni mwenye kufaham na mwenye kutafakkar.’**

‘Chochote kile utakachofanya basi hutoweza kua huru kutokana nacho isipokua utakapokua na umakini juu ya uhalali wa kile unachokitia mdomoni mwako.’

‘Siku moja Nabii Yahya alimuona Ibilis na kumwambia: ‘Hebu niambie vipi hua unakua unawasaka watu?’ Hivyo Ibilisi akasema: ‘Kwetu sisi, Ibn Adam hua ni wa aina 3, wa kwanza hua ni Mitume, hua hatuna uwezo dhidi yenu, kisha hufuata watu wa kudni la pili ambao hua wanatupa taabu sana kuwalaghai, lakini mwisho wake hua tunafanikiwa na hata hivyo baadae hua wanafanya Istighfar, na hivyo jithada zetu hua ni za bure.

Lakini na sisi hua hatuvunjiki moyo dhidi ya watu hawa kwani tunajaribu kuwalaghai tena, na tunafanikiwa lakini nao wanafanya istighfar tena na hivyo jitihada zetu hua ni za bure tena, hivyo nasi hua tunajaribu tena na tukifanikiwa

nao hufanya Istighfar tena, hivyo nasi hua hatuvunjiki moyo nao juu yao, ama watu wa kundi la tatu ni wale ambao wako kwenye mikono yetu na hua tunao uwezo wa kuwafanya tutakavyo.''

'Hata kama nikiona Ardhi kua imekua Bati na Mbingu kua ni Shaba basi kamwe sitovunjika moyo na wala kuwa na khofu na riziki yangu, kwani nikiwa na khofu basi itakua tayari najihesabu kua mimi si miongoni mwa wenye kuamini kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie Mtoaji riziki kwa viumbe wake wote.'

'Zuhd hua ni kutohuzunika na kupoteza umiliki wa mapambo ya Dunia na kutoharibika kutokana na kle unachomiliki katika mapambo hayo.'

'Unapomshauri Mtu basi muelezee umuhimu wa kufanya Ibada, kwani Ibada ni muhimu kwa Mtu kama vile ambavyo inavyokua Bahari ni Muhimu kwa ajili ya Meli.'

Imam Wuhayb Ibn Ward aliulizwa kuhusiana na Malipo ya Amali njema kwa mfano kama Tawwaf, n,k ambapo nae akajibu: **'Usiulize kuhusiana na Malipo ya Amali njema, bali uliza ni njia gani muhimu ya kuonesha shukrani kwa Mola wake yule mtu ambae amefadhiliwa kufaya Amali njema hio'**

Siku moja Imam Sufyan At Thawry, Imam Abd Allah Ibn Mubarak na Imam Fudayl Ibn Iyad walienda kwa Imam Wuhayb Ibn Ward, na wakawa wanazungumzia kuhusiana na Tende hivyo Imam Wuhayb Ibn Ward akasema kua: **'Tende ilikua ni chakula changu ninachokipenda sana, lakini siku hizi sili tena kwa sababu Tende zinazouzwa hapa hua zinachanganyika na Tende za Shamba la Zubaydah na mitende myengine' hivyo Imam Abd Allah Ibn Mubarak akasema:**

'Hutakiwi kufikiria sana juu ya hayo kwani kama ukifuatilia sana basi itakubidi hata mkate hutoweza kuula kwani ardhi ya Mji wa Makkah imechanganyika na mashamba ya watu ambao hawapo hivyo Mkate pia hua una mashaka ndani yake kama zilivyo Tende.'

Baada ya kusikia maneno hayo basi Imam Wuhayb Ibn Ward hapo hapo akaanguka chini na kuzimia, ambapo baada ya kuona tukio hilo basi Imam Sufyan Ath Thawry akasema: **'Ewe Ibn Mubarak umeshamuua Wuhayb'** ambapo Imam Abd Allah Ibn Mubarak nae akasema: **'Nimemwambia ili apate kujua ukweli ulivyo'** baada ya tukio hilo basi Imam Wuhayb Ibn Ward akazindukana na kusema: '**Kuanzia sasa hivi sitokula tena Mikate**' na hivyo tangu siku hio Imam Wuhayb akawa ni mwenye kula Maziwa tu kama chakula chake.

Hivyo siku moja mama yake alimletea Maziwa na hivyo Imam Wuhayb Ibn Ward akamuuliza Mama yake huyo: **‘Jee Maziwa haya yametokana na Kondoo gani? Na Kondo huu anachungwa wapi? Na alinunuliwa kwa pesa gani?’ hivyo Mama yake huyo akashindwa kujibumasuali hayo na Imam Wuhayb Ibn Ward akagoma kunywa Maziwa hayo, ambapo Mama yake akasema: ‘Ewe Mtoto wangu Kunywa kwani *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni msamehevu atakusamehe.’ Na Imam Wuhayb Ibn Ward akasema: ‘Itakuaje mimi niwe ni mwenye kufanya uasi kama huu huku nikijua na kisha nitegemee kusamehewa, na itakuaje nitake kusamehewa? Itakuaje**?’

Imam Wuhayb Ibn Ward alifariki mnamo mwaka 153 Al Hijra.

IMAM MUHAMMAD IBN AL MUNKADIR 32 AH

Imam Muhammad Ibn Al Munkadir Ibn Abd Allah Ibn Al Hadir Ibn Abd Al Uzza Ibn Ameir Ibn Al Harith Ibn Haritha Ibn Saad Ibn Taym Ibn Murrah Ibn Ka`b Ibn Luay ambae ni maarufu kama Imam Al Hafiz Al Qidwa.

Imam Al Munkadir alikua na Ilm kubwa sana kwani alisoma kwa *Umm Ul Muuminin* Aisha, Abu Hurayrah, Abd Allah Ibn Umar, Jabir Ibn Abd Allah, Abd Allah Ibn Abbas, Abd Allah Ibn Umar, Anas Ibn Malik, Abu Umammah na Masahaba wengine *Radhi Allahu Anhum,* na pia alisoma kwa Said Ibn Al Musayyib, Urwa Ibn Al Zubayr na Abu Salih Dakhwan Al Sammam.

Ambapo wingi wa Ilm yake pia unaonekana pale tunapoangalia na kuona kua miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Amr Ibn Dinar, Imam Al Zuhri, Imam Hisham Ibn Urwa, Imam Ibn Jurayj, Imam Ibn Abu Dhib, Imam Jafar As Sadiq, Imam Sufyanain yaani Sufyan Ath Thawry na Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Al Awzai, Imam Abu Hanifa Imam Malik, Umar Ibn Abd Ul Aziz, n,k.

Ambapo anasema Imam Ibn Rahwayh kua: ‘**Amesema Imam Sufyan Ath Thawry kua: ‘Muhammad Al Munkadir ni *Thiqah* na na Wacha Mungu walikua wakimzunguka na alikua akijihisi kua hastahiki kukubalika kama anavyokubalika’’**

Imam Al Humaidi alisema kua: **‘Muhammad Al Munkadir ni Al Hafidh’**

Ambapo kwa upande wa Imam Al Tirmidhii basi yeye amesema kua: ‘**Mimi nilimuuliza Muhammad (Imam Bukhari) hivi jee Al Munkadir amenukuu kutoka**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kwa Aisha?' 'Nae akasema : 'Naam, kwani anasema katika Hadith zake kua: 'Nimemsikia Aisha akisema kua..' nami nikasema: 'Kama *Sanad* ya Ibn Munkadir inathibitishika kama hivi, basi ni *Sanad* bora, na hii ni kwa sababu yeye amehusiana nae na ametofautishwa kwake kwani alikua pamoja nae kwa zaidi ya miaka 20'''

Kwani Imam Muhammad Ibn Al Munkadir alikua na uhusiano wa damu na Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu,* ambao umetokana kwa mmoja kati ya Mababu ambae alikua akiitwa Saad Ibn Tamim, na hivyo alikua akienda kwa Aisha *Radhi Allahu Anha* kutokana na ukaribu wa udugu huo na alikua akamsaidia katika mambo mbali mbali.

Ambapo safari moja kabla ya Imam Ibn Al Munkadir kuoa basi Aisha *Radhi Allahu Anha* alisema kumwambia Imam Ibn Al Munkadir: '**Kama ningekua na pesa kiasi ya Dirham 10,000 basi bila ya shaka ningekupa.**' Na hivyo katika siku hio hio akatokea Muawwiyah Ibn Abu Sufyan akampa Aisha *Radhi Allahu Anha* Dirham 10,000, hivyo Aisha *Radhi Allahu Anha* akasema kuiambia nafsi yake kua: '***Ma-shaa Allah* Aisha kwa haraka sana yanakua yale unayoyaota.**'

Na kisha akamtuma Mtu akamwite Muhamamd Ibn Al Munkadir na alipokuja basi akampa zile Dirham 10,000 ambazo Imam Muhamamd Ibn Al Munkadir akazitumia kwa ajili ya Harusi yake ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimjaalia kupata watoto watatu aliowapa majina ya Muhammad, Abu Bakr na Umar.

Imam Abu Hatim Al Busti kua: '**Imam Al Munkadir alikua ni Imam wa Wasomaji, na alikua hawezi kuacha kulia pale anaposoma Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Ndevu zake zilikua ni zenye rangi ya njano ya Hina.**'

Na anasema Imam Ibn Zayd kua: '**Kuna watu ambao walikua wakisafiri pamoja na Muhammad Ibn Al Munkadir katika wakati wa kiangazi na njiani mmoja wao akasema: 'Hakika mimi nna hamu ya Jibini mbichi' na hivyo akaomba Dua, na wakaendelea na safari yao kisha njiani wakakuta Jibini Mbichi, na kisha mmoja wao akasema: 'Kama ingepatikana na Asali'**

Muhammad Ibn Al Munkadir akasema: 'Yule aliekujaalieni jibini anao uwezo huo.' Na kisha wakaendelea na safari yao kidogo na mbele wakakutana na Sega la Asali hivyo wakakaa chini na kisha wakaanza kula.'

Khalid Ibn Abd Allah Al Yamami amesema kua: '**Muhammad Al Munkadir alikabidhiwa amana na kisha mwenye Amana hio akamfuata baada ya kua ni mwenye kuihitaji, hivyo Muhamamd Al Munkadir akaitafuta na akawa haioni hivyo akasali Rakaa mbili na kisha akaomba dua kwa kusema: 'Ewe Mola wa Hewa Mbinguni, Ewe ulieifunika Ardhi kwa Maji, na Ewe ambae upo kabla ya**

kuchomoza Jua na baada ya kuchomoza Jua, Nikabidhie Amanah yangu kwa ajili yangu.’’

Na hapo hapo akaona kua amana hio ipo chini ya miguu yake na akaikabidhi kwa mwenyewe. Ambapo Imam Ibn Abi Al Duniyah anasema kuhusiana na tukio hili kua hii amana ilikua ni Dinar 100.

Imam Sufyan Ath Thawry amesema kua: ‘**Muhammad Ibn Al Munkadir alikua akisema: ‘Hivi Jee ni macho mangapi yanayoiangalia riziki yangu kwenye kiza cha Ardhi na cha Bahari.’ na alipokua akilia basi alikua akijipaka machozi yake kwenye uso wake na ndevu zake huku akisema: ‘Hakika mimi nimesikia kua Moto wa Jahannam hauwezi kula katika sehemu ambayo imeguswa na machozi.**’’

Imam Ibn Al Munkadir alisema: ‘**Hakika mimi nimepigana na Nafsi yangu kwa miaka 40 hadi nikawa ni mwenye kuchoka kabisa.**’

Imam Ibn Al Munkadir aliusia kwa kusema pia kua: ‘***Allah Subhanah wa Ta’ala* humhifadhi Mja wake hadi kwa kupitia kwa Mtoto wake na kwa Mtoto wa Mtoto wake, na humhifadhi katika mzunguko huo na hivyo huhifadhika kwa kila wema baina yao**’

Anasema Umar Ibn Muhammad Ibn Al Munkadir kua: ‘**Mimi nilikua nimechukua Msahafu wa Baba yangu ambapo nae akasema: ‘Alipita Mtumwa wake na kisha akazungumza nae na akacheka nae’ na kisha akasema: ‘*Inna Lillahi wa Inna Ilayhi Rajiun*’ hadi nikadhani kua kuna jambo baya limetokea, hivyo nikamuuliza: ‘Kuna nini?’ ambapo nae akasema: ‘Sikuwa ni mwenye kusoma Qur’an wakati nilipokua nikizungumza nae**’’

Imam Ibn Al Munkadir alisema: ‘**Utakuja wakati ambapo wale watu watakao kua wanaomba Dua tu ndio watakao okoka, kama vile Dua ya mtu anaezama.**’

Imam Ibn Al Munkadir alikua akiitwa *Al Bakkah* yaani mwenye Kulia Sana na hii ni kwa sababu ya kua ni mwenye kumuogopa sana *Allah Subhanah wa Ta’ala* na ni mwenye kua na khofu sana na Dhambi zake, hivyo siku moja aliulizwa na Mama yake ambae alisema: ‘**Ewe Mtoto wangu, hakika mimi kama ingekua sikujui tangu utotoni mwako, basi ningekua nnafikiria kua wewe unalia kwa sababu ya kutokana na Dhambi kubwa ambayo umeifanya, hivyo kwanini unalia sana?**’ ambapo Imam Al Munkadir akasema: ‘**Hakika Mimi nnalia kutokana na kuujua Ukubwa wa Ufalme wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kitakachotokea katika siku ya Malipo.**’

Imam Muhammad Ibn Munkadir alisema kua: ‘**Siku moja nilikua nimekaa Msikitini pembeni ya Kibla nikiwa nnaomba Dua katika katika ya Usiku, na kulikua kuna**

Mtu ambae amesimama katika moja kati ya Nguzo za Msikitini humo huku uso wake ukiwa ameufunika, na nikamsikia akiwa anaomba Dua huku akisema: 'Ya Allah, Ukame umetuathiri vibaya sana sisi waja wako, hivyo nakuomba ijaalie Mvua iwe ni yenye kutunyeshea' na haukuchukua mda isipokua kikaja kiwingu na Mvua ikanyesha'

Imam Muhammad Ibn Al Munkadir alikua na hamu kubwa sana ya kuwajua Wacha Mungu waliokaribu yake hivyo akajaribu kutaka kumjua huyo ni nani, na hivyo akasema: '**Kumbe katika Mji huu kuna Mcha Mungu ambae mimi simjui**' **hivyo baada ya kumaliza Sala zake basi miminikamfuata hadi akafika kwenye Nyumba ya Anas, na kisha akaingia ndani yake. Nami nikarudi Msikitini na kusubiri hadi baada ya kusali *Salat Al Fajr*.**

Kisha nikaenda kwenye ile Nyumba na kugonga Mlango, na alipofungua Mlango nikamsalimia na kisha nikamwambia kua: 'Nilikusikia Jana Ukiomba Dua na nimeona matokeo ya Dua yako, hivyo jee utaniruhusu mimi kukusaidi riziki yako ili wewe upate kua ni mwenye kua ni mwenye kushughulikia Ibada zako?'

Ambapo nae akajibu: 'La, lakini nilikua nakuomba kua Tafadhali usimwambie mtu yeyote kuhusiana naim hadi nitakapofariki, na wala usinifuate tena kwa sababu watu watagundua hali yangu na hivyo kila kitu kitakua hadharani' hivyo nami nikamuuliza: 'Hivyo tutaonana wapi?'nae akajibu: 'Msikitini'.

Imam Ibn Al Munkadir hakuwahi kumwambia Mtu yeyote kuhusiana na tukio hilo hadi alipofariki Mtu huyo, ambapo kuna wanaosema kua Mtu huyu alikua ni Muafrika mshona viatu wa Mji wa Madina.

Ama kwa upande wa Imam Ibn Wahb basi yeye anasema kua: '**Mimi niliambiwa kua Mtu huyo alihama kwenye nyumba hio na kuhamia katika sehemu ambayo hajulikani, hivyo mmiliki wa nyumba aliyokua akikaa alikua akisema kua: 'Allah Amsamehe Ibn Al Munkadir ambae alimlazimisha Mja mwema kuhama katika nyumba yetu.''**

Hujjat Ul Islami Imam Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali anasema kua: '**Muhammad Ibn Al Munkadir alikua anauza vitambaa ambapo baadhi vilikua ni vya Dirham 5, na baadhi vya Dirham 10, hivyo alipokua hayupo basi mfanyakazi wake akauza vitambaa vya Dirham 5 kwa bei ya Dirham 10, na baada ya kujua tukio hilo basi Muhammad Ibn Al Munkadir akatumia siku nzima kumtafuta mnunuzi huyo hadi aampata na kisha akamwambia:**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

‘Samahani lakini, Mfanyakazi wangu amekosea kwani alikuuzia Vitambaa vya Dirham 5 kwa bei ya Dirham 10’ lakini yule mnunuzi akasema: ‘**Hamna tatizo kwa sababu mimi nimekubaliana nae**’

Lakini Muhamamd Ibn Al Munkadir akasema: ‘**Hata kama umekubaliana nae lakini mimi siko tayari kukutia hasara wewe, isipokua kwa sharti la kua ukubaliane nasi katika moja kati ya mambo matatu yafuatayo: Aidha tukubadilishie uchukue vitambaa vya Dirham 10 badala yake, au tukurudishie Dirham zilizozidi au uturudishie Vitambaa vyetu nasi tukupe Dirham zako’ baada ya kusikia Masharti hayo, basi yule Mnunuzi akasema: ‘Basi bora nirudishie Dirham zilizodi**’

Baada ya Mnunuzi huyo kurudishiwa Dirham zake na Muhammad Ibn Al Munkadir kuondoka, basi yule mnunuzi akauliza: ‘**Yule Muuzaji ndio nani?’ ambapo akajibiwa kua: ‘Yule ndio Muhammad Ibn Al Munkadir’** Hivyo yule mnunuzi akasema: ***‘La Ilaha Illa Allah!*** **Ndio maana akawa ni mwenye kuvijaza maji visima wakati sisi tunapokua tumekauka.**’

Imam Muhammad Ibn Al Munkadir amesema kua: ‘**Kumlisha Masikini Muislam hua kunamhakikishia Mtu kusamehewa Dhambi zake.**’

Imam Muhammad Ibn Al Munkadir alifariki mnamo mwaka 129 Al Hijra na alipokua anaumwa na kukaribia kifo chake basi alikua akilia pia na alipoulizwa kwanini analia basi alisema : ‘**Hakika mimi naogopa kua nisije nikaunganishwa na wale waliotajwa kwenye ile aya isemayo:**’

﴿وَلَوْ أَنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُواْ مَا فِى ٱلأَرْضِ جَمِيعاً وَمِثْلَهُ مَعَهُ لاَفْتَدَوْاْ بِهِ مِن سُوۤءِ ٱلْعَذَابِ يَوْمَ ٱلْقِيَامَةِ وَبَدَا لَهُمْ مِّنَ ٱللَّهِ مَا لَمْ يَكُونُواْ يَحْتَسِبُونَ﴾

Walaw anna lilladheena *dh*alamoo ma fee al-ardhi jameeAAan wamithlahu maAAahu laiftadaw bihi min soo-i alAAadhabi yawma alqiyamati wabada lahum mina Allahi ma lam yakoonoo yahtasiboona *(Surat Az Zumar 39:47)*

Tafsir: ***Ama na wale waliojidhulumu, hata kama wangekua wana kila kitu kilichopo ardhini na mithili yake, basi kwa hakika wangevitoa kwa ajili ya kujiokoa kutokana na adhabu ya siku ya Malipo, na kisha baada yake kitakua wazi kutoka kwa Allah juu ya kile walichokua hawakihesabu.***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Sufyan Ath Thawry alimuuliza Imam Ibn Al Munkadir: **'Hivi jee ni kitu gani kinachokufurahisha wewe zaidi?'** ambapo Imam Ibn Al Munkadir akajibu: **'Ni Kukutana na ndugu yangu wa Kiimani na kisha nikamfurahisha.'**

IMAM MUHAMMAD IBN SIRIN 33 AH

Imam Muhammad Ibn Sirin alizaliwa katika Mji wa Basra mnamo mwaka 33 Al Hijra na hivyo kua ni miongoni mwa Wanazuoni waliosomeshwa na Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* miongoni mwa waliokua pamoja nae ni Sahaba Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*, ambapo walioishi pamoja nae katika wakati wake ni pamoja na Hasan Al Basr, Al Fudayl Ibn Iyadh na wengineo.

Imam Muhamamd Ibn Sirin alikua ni Imam mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith, Qura'n, Fiqh na ni mwenye kujua vizuri sana kuhusiana na Utabiri wa ndoto, na alikua ni mwenye kufunga saum kila baada ya siku moja, na hio katika siku moja asiofunga basi alikua hali kitu isipokua chakula cha asubuhi tu, na alikua ni mwenye kukesha usiku kucha kufanya Ibada katika mwezi mzima wa Ramadhani kwani alikua akisema kua: '**Mtu hua anatakiwa kusali Usiku ndani ya Mwezi wa Ramadhani japo kwa wakati ambao hua ni sawa na wa kumkama Mbuzi Maziwa**'

Ambapo anasema Hisham Ibn Hasan kua: '**Hakika mimi nilikua nikisikia Kilio cha Muhamamd Ibn Sirin nyumbani kwake katika wakati wa Usiku, ijapokua wakati wa Mchana alikua ni mtu Mcheshi sana unapomtembelea Nyumbani kwake.**'

Na anasema Muriq Ibn Ujali kua: '**Hakika mimi sijawahi kuona Mtu mwenye Ucha Mungu kama na mwenye Uwezo mkubwa Kiilm kama Muhammad Ibn Sirin**'

Anasema Shaykha Fatma Bint Sirin ambae ni Dada yake Imam Muhammd Ibn Sirin kua: '**Wakati Muhammad Ibn Sirin anapokua mbele ya Mama yetu basi alikua ni mwenye kusimama kwa heshima na kuona haya na inapombidi kusema basi alikua akijizuia kusema kwa maneno yake yote**'

Imam Muhammad Ibn Sirin alikua ni mwenye kusema: '**Pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* anapomuingiza Mja wake kwenye Rehma zake basi humuelekeza Mja huyo kwa mtu mwema kwa ajili ya kumuusia**'

Na akasema tena kua: '**Kama Mtu anataka awe ni mwenye kunufaika katika Ulimwengu wa Dunia hii na Akhera yake pia, basi ni bora kwake kua ni mwenye**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kushikamana na yule mtu ambae atakua ni mwenye kumuamrisha kufanya mema na kumkimbiza kutokana na kufanya maovu'

Kuhusiana na Ilm yake ya utabiri wa ndoto basi aliulizwa Imam Muhammad Ibn Sirin ambapo nae akasema: '**Muogope Mola wako wakati unapokua Macho na kisha usiwe na khofu juu ya utakachokiona ndani ya ndoto zako**'

Na Imam Muhammd Ibn Sirin alipokua akiulizwa kuhusiana na kutoa tafsiri ya baina ya mambo mawili yanayofanana basi alikua ni mwenye kuchukua Mtizamo uliokua karibu zaidi na Qur'an, kwani alikua akisema kua '**Ilm hii ni yenye kutokana na Dini yetu, hivyo kua muagalifu inajifunza kutoka kwa nani**'

Ambapo anasema Misa Ibn Al Mughirah kua: '**Mimi nilimuona Muhammad Ibn Sirin akiingia Sokoni katika wakati wa Mchana, huku akiwa amezama kwenye dhikr Allah, hivyo kuna Mtu akasema: 'Aah! Ibn Sirin! katika wakati kama huu basi ndio unafanya Dhikri hizo?' Imam Muhammad Ibn Sirin akasema: 'Hakika ni katika Soko ndio mtu unaweza ukavutiwa na mapambo yake na hivyo kujisahau kutokana na kumkumbuka Mola wako'**'

Siku moja Imam Muhammad Ibn Sirin alikua amekaa katika mkusanyiko wa watu na ilipofika wakati wa Sala ikaadhiniwa Adhana, na kisha watu wakasimama kwa ajili ya kusali Sala ya Jamaa ambapo ingawa Imam Ibn Sirin alikuwa anatakiwa kusalisha lakini akakataa na kusema: '**Wacha mwenye Ilm zaidi ya Kusoma Qur'an na asalishe kwani wamo miongoni mwetu walioihifadhi ndani ya Nyoyo zao**' hivyo Sala ikasalishwa na mtu mwengine na baada ya kumalizika kusaliwa Sala hio basi Imam Muhamamd Ibn Sirin akaulizwa: '**Hivi kwa nini hukutaka kusalisha Sala hii leo?**' ambapo nae akajibu: '**Kwa hakika mimi sikutaka kua watu wawe ni wenye kusema kua Leo tumesalishwa Sala ya Jamaa na Muhammad Ibn Sirin**'

Kutokana na ucha Mungu wake basi Imam Muhammad Ibn Sirin alikua ni mwenye kujizuia kula visivyokua halali yake kiasi ya kua kuna siku alialikwa kwenye harusi na hivyo kabla ya kutoka Nyumbani kwake basi akawataka watu wa Nyumbani kwake wampe chakula kitamu ili ale. Lakini hata hivyo watu wa Nyumbani kwake wakamwambia kua ya nini? Wakati anaenda Harusini? Ambapo nae akajibu: '**Hakika mimi nnachukia kula hadi nikashiba kutokana na vyakula vya watu wengine**'

Ambapo anasema Hisham Ibn Hasan kua: '**Kila mara ilipokua Hind Bint Al Muhallabi anamualika Hasan Al Basr na Muhammad Ibn Sirin katika chakula basi Muhammad Ibn Siri alikua akijizuia kuenda na Hasan Al Basr alikua ni mwenye kuwajibika kuenda**' kwani Imam Muhamamd Ibn Sirin alikua akisema kua: '**Usimbebeshe rafiki yako mzigo zaidi ya atakaoweza kuubeba.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Safari moja Imam Muhamamd Ibn Sirin alileteva zawadi ya Dirham 40,000 lakini hata hivyo aligoma kuipokea kutokana na kua na shaka ya kua sehemu ya pesa hio haina uhalali ndani yake ambapo anasema Imam Sulayman Al Taymi kua: '**Imam Muhammad Ibn Sirin aliigomea zawadi hio kwa sababu alikua akijua kua hakuna Maimamu wawili watakaoweza kukubaliana kua pesa hio haina uharamu ndani yake**.'

Wakati Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* alipofariki, basi aliwacha wasia kua mwili wake ukoshwe na Imam Muhammad Ibn Sirrin ambae katika wakati huo alipofariki alikua yupo ndani kifungoni, hivyo watu wa Mji wa Basra wakaomba ruhusa kwa Gavana wa Basra kua Imam Muhammad Ibn Sirrin atolewe ili akamkoshe Sahaba huyo, na hivyo Gavana akatoa amrisho la kutolewa nje kwa Imam Muhammad Ibn Sirrin.

Lakini hata hivyo Imam Muhamamd Ibn Sirrin alikataa kutoka nje na kusema kua hawezi kutoka hadi pale yule Mtu aliemuingiza ndani aje kumtoa, na hivyo watu wakamfuata Mtu huyo pia ambapo nae akatoa ruhusa hio, na baada ya hapo ndio Imam Muhammad Ibn Sirrin akatoka nje na kuenda kuukosha mwili wa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu.*

Siku Moja kuna mtu alidai kua anamdai Imam Muhammad Ibn Sirrin Dirham 2, lakini hapo hapo akasema kua hakuna ulazima wa yeye kulipwa na Imam Ibn Sirrin, hivyo mtu huyo akamwambia Imam Ibn Sirrin kua ale kiapo kwa ajili ya kukataa kulipa Dirham 2 hizo, na Imam Ibn Sirrin akala kiapo hicho, hivyo watu wakamuuliza Imam Muhammad Ibn Sirrin wa kusema: **'Inakuaje unakula kiapo kwa ajili ya Dirham mbili tu?' ambapo Imam Muhammad Ibn Sirin akasema: 'Naam kwa sababu sitaki mtu huyu awe ni mwenye kula kisichokua halali yake.'**

Anasema Imam Qatadah Al Sadusi kua: **'Imam Muhamamd Ibn Sirin aliitaja Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa mtu, ambapo mtu huyo akasema: 'Lakini mbona fulani na fulani wanasema kadha w kadha?' Imam Muhammad Ibn Sirin akasema: 'Mimi nakwambia wewe yaliyosemwa kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha wewe unaniambia kuhusiana na waliyosema fulani na fulani? Hivyo mimi sitozungumza tena nawe.''**

Wakati Imam Muhammad Ibn Sirin alipokua kitandani anakaribia kifo chake basi alisema kumwambia Mtoto wake: **'Ewe Mtoto wangu nilipie Madeni yangu, lipa yale tu ambayo nnadaiwa na watu' hivyo mtoto wake huyo akasema: 'Jee nimuachie huru Mtumwa wako kwa ajili yako?' ambapo Imam Muhammd Ibn Sirin akasema: 'Bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye uwezo wa kunilipa mimi na wewe kwa kila utakalonifanyia kwa ajili yangu.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo anasema Muamar kua: ‘**Kuna mtu alikuja kwa Ibn Sirrin na kusema kua: ‘Mimi nimeota kua kuna Njiwa aliimeza Lulu na na akaitema na alipoitema ilikua ni kubwa zaidi ya hali yake ya awali, na kisha nikamuona Njiwa ambae alimeza Lulu ambayo alipoitema na kuitoa ikawa ndogo zaidi na kisha nikamuona Njiwa ambae amemeza Lulu akaimeza na kuitema huku ikiwa kama ilivyokua hapo awali**’

Ambapo Imam Ibn Sirin akasema: ‘**Ama kuhusiana na Njiwa wa Kwanza basi n Hasan Al Basr ambae husikiliza Hadith na kisha huihifadhi na kufanyaia kazi na kuifundisha, ama kwa yule wa pili basi hua ni Mtu ambae husikiliza Mawaidha hanufaiki nayo na wa tatu hua ni yule mtu ambae anasikiliza na kisha anaifikisha kama ilivyo’**’

Ambapo amesema Imam Bakr Ibn Abd Allah Al Muzni kua: ‘**Yeyote yule anaetaka kumuangalia Mcha Mungu wa wakati wetu basi na amuangalie Muhamamd Ibn Sirrin**’

Na akasema Muwaraq Al Ajli kua: ‘**Hakika mimi sijawahi kuona Mtu mwenye Ilm na Ucha Mungu wake na msafi kwenye Fiqh kama Muhammad Ibn Sirin**’

Kua mtu alikuja kwa Imam Muhammad Ibn Sirin na kumwambia kua: **‘Hakika mimi nimeona kwenye Ndoto yangu kua kuna Ndege Mkubwa ambae alitua kwenye Muasumini na kisha akazila Asumini zake zote’** na baada ya kusikia ndoto hio basi Imam Muhammad Ibn Sirin akabadilika muonekano wa Uso wake kisha akasema: ‘**Ndoto yako inamaanisha Vifo vya Wanazuoni’** ambapo ndio katika mwaka huo akafariki Imam Hasan Al Basr na kisha akafariki Imam Muhammad Ibn Sirin.

Ndani ya mwaka huo huo wiki moja kabla ya kufariki kwake Imam Muhammad Ibn Sirin basi alikua amekaa anakula chakula cha asubuhi na mara akaja Mwanamke Nyumbani mwake, na baada ya kusalimiana nae basi Mwanamke huyo akasema: ‘**Nimeota Ndoto**’.

Imam Muhammad Ibn Sirin akasema: ‘**Jee utaniacha kwanza nile au unataka niwache kula kisha nikusikilize?**’ yule Mwanamke akasema: ‘**Kula tu**’ hivyo Imam Muhamamd Ibn Sirin akawa anakula huku Mwanamke huyo akiendelea kumhadithia kuhusiana na ndoto yake kwa kusema: ‘**Nimeona Mwezi ukifungamana na Nyota ya Thuraya (Taurus), halafu nikasikia Sauti ikisema kua: ‘Nenda kwa Ibn Sirin na mwambie kuhusiana na hii ndoto yako.**’’

Imam Muhammad Ibn Sirin akashtuka akawacha kula na kusema: ‘**Niambie tena namna ulivyoiona hii ndoto**’ yule Mwanamke akarudia tena kuelezea namna alivyoiona ndoto yake hio, huku muonekano wa uso wa Imam Muhammad Ibn Sirin

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ukiwa unazidi kuonekana kua ni wenye kushtuka zaidi, ambapo Shaykha Fatma Bint Sirin akamuuliza Imam Muhammad Ibn Sirin: ‘**Mbona muonekano wa Uso wako umebadilika hivyo?**’

Imam Muhamamd Ibn Sirin akasema: ‘**Huyu Mwanamke ananiambia kua mimi nitafariki baada ya wiki moja**’ na bila ya shaka Imam Muhammad Ibn Sirin akafariki wiki moja baada ya siku 7 ndani ya mwaka 110 Al Hijra katika Mji wa Basra huku akiwa na umri wa miaka 76 na ilikua ni siku 100 baada ya kufariki Imam Hasan Al Basr.

IMAM SULAYMAN IBN YASSAR 34 AH

Imam Abu Abd Rahman Sulayman Ibn Yasir alikua ni miongoni mwa Wanafiqh wakubwa wa kizazi cha Tabiina katika Mji wa Madina aliezaliwa mnamo mwaka 34 Al Hijra, na alikua ni mwenye Ilm kutoka kwa *Umm Ul Muuminin* Maimuna Bit Harith *Radhi Allahu Anha* ambae alikua kimilikiwa nae na pia alikua ni Mwanafunzi wa *Umm Ul Muuminin* Umm Salamah *Radhi Allahu Anha, Umm Ul Muuminin* Aisha *Radhi Allahu Anha* Zaid Ibn Thabit, Abd Allah Ibn Abbas, Abu Hurairah, Hassan Ibn Thabet, Jaber bin Abd Allah, Rafi’ Ibn Khadij na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum.*

Sulayman Ibn Yasir alikua ni mwenye Ilm kubwa sana kiasi ya kua Immam Said Ibn Mussayib alikua akiulizwa suali basi hua ni mwenye kusema: ‘**Nenda kwa Sulayman Ibn Yasir kwani yeye ni m-bora miongoni mwa wanaojua na wakawa hai hadi hii leo’** ambapo na kwa upande wa Imam Malik basi alikua ni mwenye kusema kua: ‘**Sulayman Ibn Yasir ni miongoni mwa Wanazuoni waliobakia baada ya Said Ibn Musayyib.**’

Ambapo kwa upande wa Abu Al Zinad basi yeye anasema kua: ‘**Sulayman Ibn Yasir alikua ni Mtu mwenye kufunga daima na kaka yake Ata alikua akifunga baadhi ya siku na baadhi ya siku akiwacha.**’

Ambapo kwa upande wa Qatadah basi anasema kua: ‘**Mimi nilifika kwenye Mji wa Madina na kuuliza jee ni nani mwenye Ilm kubwa zaidi ya Talaka katika mji huu? Na nikaambiwa kua ni Sulayman Ibn Yasir**’

Imam Ibn Saad amesema kuhusiana nae kua: ‘**Sulayman Ibn Yasir ni Mwanazuoni mwenye Hikma, anaeaminika, ni Mwanafiqh na Mwanahadith mwenye Ilm kubwa ya Hadith**’ ambapo kwa upande wa Imam Al Zuhri basi anasema kua: ‘**Sulayman Ibn Yasir ni M-bora miongoni mwa Wanazuoni bora.**’

Abu Al-Zinad amesema kua: ‘**Miongoni mwa Wanazuoni na Wanafiqh wa Madina ambao nimekutana nao na ni wenye kutosheleza kutokana na Ilm yao ni Said Ibn Musayyib, Urwah, Al Qasim, Abu Bakr Ibn Abdul Rahman, Kharija Ibn Zaid, Ubaid Allah Ibn Abd Allah Ibn Utbah na Sulayman Ibn Yasir.**’

Anasema Musab Ibn Uthmani kua: ‘**Sulayman Ibn Yasir alikua ni mtu mwenye Sura nzuri sana ya kuvutia.**’

Safari moja Sulayman Ibn Yasir aliondoka kutoka katika mji wa Madina na rafiki yake hadi walipofika kwenye eneo la *Al Abwa*, hivyo rafiki yake huyo akaondoka na kuenda kununua vitu sokoni na Sulayman Ibn Yasir akabakia katika hema walilopiga kambi kwa siku hio.

Mara akatokea Mwanamke mmoja mzuri sana ambae kutoka kwenye moja kati ya hema la watu wa Abwa na kuja kwenye hema la Sulayman Ibn Yasir na alipofika basi Sulayman Ibn Yasir akadhani kua Mwanamke huyo anataka chakula, hivyo akamkaribisha chakula ambapo Mwanamke huyo akasema akajifunua uso wake na kusema: ‘**La, hakika mimi sitaki chakula bali nataka nipate kutoka katika familia yako.**’

Imam Sulayman Ibn Yasir akasema: ‘**Hakika Ibilis amekutayarisha wewe kwa ajili yangu**’ na kisha akaanza kuweka kichwa chake kwenye mikono yake na kuanza kulia kwa sauti, kutokana na kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta’ala.*

Yule Mwanamke alipoona tukio hilo basi akajifunika uso wake na kuondoka na kurudi kwenye hema lake, alipokuja rafiki yake na kumkuta katika hali hio akamuuliza kilichotokea ambapo nae akaelezea kilichotokea. Ambapo na rafiki yake huyo nae akaanza kulia zaid, na alipoulizwa kwa nini nae analia basi akasema: ‘**Kwa Sababu mimi naogopa kua kama nigekua wewe basi nisingekua na Subra ya kujizuia juu yake Mwanamke huyo.’**

Baada ya tukio hilo Imam Sulayman Ibn Yasir akaelekea katika Mji wa Makkah, akafanya Tawwaf na Ibada nyenginezo na kisha na akalala pembeni ya Al Kaabah, mara usingizi akatokea Mtu Mzuri sana ambapo Imam Sulayman Ibn Yasir akasalimiana nae kisha akamuuliza: ‘**Wewe ndio Nani?**’ yule mtu akasema: ‘**Mimi ni Yusuf Ibn Yaqub**’ Imam Sulayman Ibn Yasir akasema: **‘Yusuf As Siddiq?’** nae akasema: **‘Naam’** Imam Sulayman Ibn Yasir akasema: **‘Kuna jambo geni sana kwenye Kisa chako na Imraat Al Aziz’** Nabii Yusuf akasema: **‘Hakika mna jambo bora zaidi katika kisa chako wewe na Mwanamke wa Al Abwa.’**

Baada ya Amir Muuminin Umar Ibn Abd ul Aziz kupewa Madaraka ya Uongozi na Waislam basi alimchagua Sulayman Ibn Yasir kua Msimamizi wa Soko La Madina, na alifariki mnamo mwaka 100 Al Hijra.

IMAM WAHB IBN MUHABIH 34 AH

Imam Wahb Ibn Munabih Ibn Kamil Ibn Siij Ibn Dhi Kibar Abu Abd Allah Al Yamani As Sanaani, alizaliwa mnamo mwaka 34 Al Hijra, Baba yake alikua ni mwenye asili ya Yemen aliehamia katika maeneo ya Khurasan kutokea kwenye mji wa Herat.

Imam Wahb Ibn Munabih alisoma kutoka kwa sahaba Anas Ibn Malik, Abd Allah Ibn Abbas, Jabir Ibn Abd Allah, Abd Allah Ibn Umar, Abu Hurayrah na Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhum.*

Na pia alisoma kutoka kwa Tabiina kama kina Imam Tawus Ibn Qaysan, Amr Ibn Dinar, Amr Ibn Shuayb na pia kutoka wa kaka yake ambae ni Hamam Ibn Munabih ambapo alisema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Wahb Ibn Munabih alikua ni Mtu wa Uajemi mwenye asili ya Yemen ambae ni mwenye Nasaba ya jina lenye neno *Dhi* na kutokana na jina hio kuna Usharifu ndani yake**'

Ambapo kwa upande wa Al Ijaali basi yeye alisema kua: '**Wahb Ibn Munabih alikua ni Tabiina mwenye kuaminika na alikua ni Qadhi wa Mji wa Sanaa, Yemen.**'

Kwani Wahb Ibn Munabih alikua ni Qadhi wa Mji wa Sanaa Yemen aliechaguliwa na Imam Umar Ibn Ad Al Aziz na alikua ni miongoni mwa watu wenye kujitenga sana na Dunia, ambae mwenye Ilm kubwa sana hususan ya Hadith, Fiqh na ya *Ahl ul Kitab,* na ingawa alikua si mwenye kulala sana Usiku lakini alikua akiota kwenye ndoto basi hua kinakua kama kinavyokua mchana.

Ambapo alisema Imam Wahb Ibn Munabih kua: '**Kama ikiwa Mtu utayaangamiza Matamanio ya nafsi yako basi Ibilis hua ni mwenye kukukimbia kwa kuogopa hata kivuli chako.**'

Na akasema pia kua: '**Kama kuna mtu ambae atakusifu kutokana na sifa ambayo huna basi jua kua atalaumu kutokana na kile ambacho pia huna**' hivyo alikua kama akisifiwa sana mbele za Watu basi alikua akisema: '**Hakika mimi nimejitizama na sijajiona kua nnazo sifa hizo msemazo.**'

Na aliusia Imam Wahb Ibn Munabih kwa kusema kua: '**Kueni Waangalifu na mambo matatu ambayo ni: Kufuata Mkumbo; Kufuata Matamanio ya Nafsi na Kua ni wenye kupenda kujionesha.**'

Mbali ya kua ni mwenye Ilm kubwa sana lakini Imam Wahb Ibn Munabih alikua ni Mtu asiechoka wala kukinai kuhusiana na kitu kinachoitwa Ilm kwani alikua ni mwenye kupenda sana kusoma vitabu na kufanya Ibada ambapo siku moja alimtembelea rafiki yake katika maeneo ya Saada na akatumia Usiku wake katika nyumba hio ya rafiki yake, ambapo usiku huo rafiki yake huyo alipotoka usiku akamkuta akiwa amekaa anasoma huku mguu wake mmoja ukiwa unaonekana ngozi yake na weupe wake ilikua kama mwangaza wa Jua.

Hivyo siku ya pili yake asubuhi rafiki yake huyo akamwambia: '***Subhanah* Allah jana nilikuona usiku ukiwa unasoma huku mguu wako ukiwa unang'ara kama Jua**' ambapo Imam Wahb Ibn Munabih akasema: '**Fanya uliyoyaona kua ni siri yako.**'

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kumwambia Imam Ataa Al Khurasani kua: '**Wanazuoni waliotangulia kabla yetu walikua wakiachana na Dunia yao kutokana na Ilm yao na hivyo hawakua ni wenye kujali kuhusiana na Dunia ya Watu wengine. Kiasi ya kua walikua ni wenye kuona ubaya wake. Hivyo jitahidi kukaa mbali na milango ya makasri ya Sultan kwa sababu kwenye Milango yao kuna Mitihani kama ilivyokua kuna Mitihani kwenye Ngamia bora walio wazuri**.'

Kwani hawawezi kukudhuru kwa chochote kutokana na Dunia yao isipokua kukuharibia kuhusiana na Dini yako na Akhera yako. Ewe Ataa kama ikiwa utakinai na ulichokua nacho basi utaukinai uhai wako wote, na kama hukukinai na ulichokua nacho basi hakuna utakacho kikinai juu yake ndani ya uhai wako, na faham kua Tumbo lako ni Bahari na Bahari ndani yake hua haina chochote isipokua bonde lililojaa Uchafu.'

Kuna mtu alimfuata Imam Wahb Ibn Munabih na kumwambia: '**Ewe Wahb Ibn Munabih hakika mimi nimeamua kuachana na kujumuika pamoja na Watu'**

Imam Wahb Ibn Munabih akasema: **'La haifai kuachana na kujumuika na watu kwani wao wanakuhitaji wewe na wewe unawahitaji wao, hivyo jumuika pamoja nao isipokua unapokua nao basi kua miongoni mwa Viziwa, Vipofu na Mabubu, Mwenye kutafakkar na kufaham na kisha mwenye kukaa kimya.**'

Na akasema Imam Wahb Ibn Munabih kua: '**Ilm ni Rafiki wa Muumini, Ustahmilivu ndio Waziri wake, Ufahamu wake ndio Muongozo wake, Kufanya kazi kwake ndio Thamani yake, Subra ndio Kiongozi wa Jeshi lake, Ukarimu ndio Baba yake na Ukarimu ndio ndugu yake.**'

Imam Wahb Ibn Munabih akasema tena pia kua: ‘**Muumini hua ni mwenye kuangalia ili ajue, huzungumza ili afahamu, hukaa kimya ili kufikisha na hukaa peke yake ili kujiongezea zaidi**.’

Muthanna Ibn As Sabbaah amesema kua: ‘**Mimi nilikua pamoja na Wahb Ibn Munabih kwa mda wa miaka 40 na sikuwahi kumuona akilaumu hata mara moja kiumbe chochote kile.**’

Ambapo kwa upande wa Al Fadhl Ibn Abi Iyash basi amesema kua: ‘**Nilikua nimekaa na Wahb Ibn Munabih na mara akaja mtu na kumwambia, nimekutana na fulani na fulani ambao wamekusema vibaya**’ hivyo Wahb Ibn Munabih akakasirika na kusema: ‘**Hivi Ibilisi hakumuona mjumbe mwengine yeyote wa kuniletea ujumbe huu zaidi yako?**’

Hivyo Mtu huyo hakukaa na akaondoka na mda baada ya kuondoka mtu huyo basi wakatokea wale ambao walisemwa kua wamemsema vibaya Imam Wahb Ibn Munabih na wakamsalimia Imam Wahb Ibn Munabih ambapo nae akawasalimia na kuwanyooshea mkono na wakakaa pamoja na kuzungumza nao.

Miongoni mwa kauli za wasia za Imam Wahb Ibn Munabih ni pamoja na:

‘Iman hua ni yenye kuchakaa na hua ni yenye kupambwa upya kwa Taqwa, Uzuri wake hua ni Haya na Mali yake hua ni Fiqh’

‘Mtu yeyote yule mwenye mambo matatu hua tayari ni mwenye kupambwa na pambo la Uadilifu: Mwenye Ukarimu; Mwenye Subra katika wakati wa Mitihani na mwenye Kauli njema.’

‘Ongeza wingi wa Urafiki kindugu kwa kadiri utakavyoweza, kwani ukiwa huna haja nao basi hawawezi kukudhuru na ukiwahitaji watakunufaisha.’

Muumini hua ni mwenye kuangalia ili ajifunze, mwenye kusema ili afahamu, hukaa kimya ili awe salama, na hua ni mwenye kua na mda wa kukaa peke yake ili aweze kuzitumia nafasi zinazoangukia katika upande wake.

Ambapo Imam Ibn Hibban amesema kuhusiana na Imam Wahb Ibn Munabih kua: ‘**Wahb Ibn Munabih alikua akipenda sana kusoma vitabu na alikua mda wote akifanya Ibada na kuifanyia kazi Ilm yake. Alikua ni mtu mwenye kujitolea katika Ucha Mungu na alikua ni mwenye kusali Sala ya Al Fajir kwa udhu wa Sala ya Isha kwa mda wa miaka 40’**

Imam Muslim Ibn Khalid Al Zanji amesema pia kua: **‘Wahb Ibn Munabih alikaa kwa muda wa miaka 20 bila ya ubavu wake kugusa kitanda ndani ya miaka 40 hivyo hakutia udhu baina ya Isha na Alfajir.’**

Abd Samad Ibn Miqal alisema kua: ‘**Mimi nilikaa na Mjomba wangu Wahb Ibn Munabih kwa miezi na alikua akisali Sala ya Alfajir kwa Udhu wa Isha’**.

Kwani Imam Wahb Ibn Munabih mwenyewe alikua akisema: ‘**Kwa Hakika ni wakati wa usiku ambapo Muumini hua ni mwenye kupata utulivu anapokua pekee yake na Mola wake** ’.

Amesema Imam Wahb Ibn Munabih kua: **‘Hakuna Ibn Adam anaependwa zaidi na Ibilisi zaidi ya yule anaependa kula zaidi na kulala zaidi.’**

Kwa upande wa *Mujaddid Ad Din* Imam Ibn Hajar Asqalani amesema kuhusiana na Imam Wahb bn Munabih kua: ‘**Ni Mtu Muaminifu**’ Imam Adh Dhahabi anasema pia kua alikua ni Mwenye Ilm ya Utabiri lakini baadae akaachana nayo. Ambapo kwa upande wa Hadithi zake basi Imam Wahb Ibn Munabih amenukuliwa kwenye vitabu vya Imam Bukhari, Imam Muslim, Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhi, Imam An Nasai na Imam Ibn Majah.

Na kwa upande wa *Shaykh ul Islami* Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi basi yeye amesema kua: ‘**Imam Wahb Ibn Munabih ni Tabiina maarufu kwa ilm yake ya *Ahl Al Kitab* na Wanakubaliana kuhusiana na kuaminika kwake katika Kunukuu Hadith.**’

Na Imam Adh Dhahabi anasema kua: ‘**Wahb Ibn Munabih anaaminika, Maarufu, Mwenye Hadithi nyingi na ni Mchangamfu.**’

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **‘Ewe Ibn Adam hakuna mwenye Nguvu na Uwezo kama Muumba na hakuna asiekua na Uwezo na Dhaifu kama Kiumbe alieumbwa.’**
‘Nimesoma mimi kwenye vitabu kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* amesema kua: ‘Hakika mimi nnamtosheleza Mja wangu, pale anapokua ni mwenye hua na utiifu kwangu, hivyo mwache nifanye anavyotaka na humpa bila yakutaka, kile anachokihitaji kwani mimi ni mwenye kujua kile ambacho anakihitaji’’

‘Ibilisi anao uwezo wa kuwadhibiti maelfu ya watu wajinga, kiurahisi kokote kule anakotaka na vyovyote vile atakavyo lakini, hawezi kumfanyia hivyo Mwanazuoni kwani atakua na mda mgumu kweli kufanikisha hilo.’

‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* alimwambia Nabii Daud: ‘Ewe Daud hivi jee unajua ni wepi miongoni mwa Waja wangu ambao mimi hua nnapenda kuwasamehe?’ Nabii Daud akasema : ‘La, Jee ndio Waja wepi hao ya Allah?’ *Allah Subhanah wa Ta’ala* akasema: ‘Ni wale ambae wanapokumbuka Dhambi zao basi hua ni wenye kutetemeka kwa khofu.’’
‘**Tabia Njema kabisa yenye manufaa kwenye Dini ya Mja ni kutovutika na Mapambo ya Dunia, na jambo baya kabisa ni kufuata Matamanio ya Nafsi yake, ambapo sehemu ya kuednekeza Matamanio ya Nafsi hua ni Kupenda Mali, Cheo na kupenda kusifiwa mbele ya watu, kwani mtu anaependa Mali na Darja hua ni mwenye kuanguia kwenye Haram.**

Na yeyote yule ameangukia kwenye haramu basi hua ni mwenye kumkasirisha *Allah Subhanah wa Ta’ala,* na mwenye kumkasirisha *Allah Subhanah wa Ta’ala* bila ya shaka hua ni mwenye kuangamia.’

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: ‘ **Mambao matatu yafuatayo hua ni sehemu ya Dhulma Kupingana na wale waliokua juu yako Kiamri, Kuwadhulumu wale waliokau chini yako kwa kutumia nguvu na Kumsaidia mwenye kufanya Dhulma.’**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: ‘Sifa tatu zifuatazo ni za Mtu Mnafiq, hua mvivu katika amali zake anapokua peke yake, hua hodari katika amali zake anapokua mbele za watu na hua ni mwenye kupenda kusifiwa kutokana na Amali zake.’

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **‘Kuna dalili tatu za Watu wenye wivu na kijicho: ‘Kutokua na uwezo wa kuwavutia na kuwaathiri watu, humsengenya yule anaemuonea wivu anapokua yuko mbali yake, na humsifu anapokua mbele yake. Hufurahia anapopatwa na matatizo yule anaemuonea wivu.’**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: ‘**Wale wasioomba Ushauri hua ni wenye kujuta baadae, na wale wanaoojona kua wanajitosheleza basi hufanya kama wanayotaka.’**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: ‘**Mcha Mungu ni yule mtu ambae ni mwenye kuachana na mengi kati ya mambo yaliyoruhusika kutokana na kua na khofu ya kua kushabihiana na uharamu ndani yake, na hivyo hua ni mwenye kutafuta kile kilichokua ni halali yake, mtu huyu hubakia na ucha Mungu wake hata kama atakua ni mwenye kufatilia mambo ya kidunia.’**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **‘Yeyote yule ambae si mwenye kujali yaliyo haramu na yaliyo halali, basi hata kama ataonekana kua ni mwenye kuachana na**

Dunia yake lakini kutojali kwake juu ya kipi ni kilicho halali yake na kipi ni haramu yake huonesha kua ni mwenye maradhi ya Matamanio ya Kidunia.'

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **'Mtu mkarimu zaidi ni ambae ni mwenye kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuachana na makatazo yake. Na mtu mbakhili zaidi ni yule ambae ni mwenye kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hata kama akiwa ana mali nyingi sana.'**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **'Moja kati ya Dhmabi kubwa sana mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* mbali ya Ushirikina basi ni kumdhihaki Mtu.'**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **'Kama mtu akiingia kwenye mitihani basi inabidi ajue kua ameingia kwenye hali ya Mitume na Wacha Mungu, kwa sababu wote hao walikutwa na Mitihani mikubwa sana katika Dunia hii.'**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **'Kila kitu mwanzo huanza kuonekana kua ni kidogo lakini halafu hukua katika hali ya ukubwa zaidi isipokua Mitihani, kwani Mitihani huanza na uzito mkubwa sana lakini baadae hupungua uzito wake na kutoweka kabisa mitihani hio'**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **'Ushauri wa yule ambae ni mwenye sifa ya usengenyaji hua hauwezi kuaminika'**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **'Yeyote yule anaejisifia sana hua ni mwenye kuyakataa maumbile yake'**

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: '**Mwanzo wa kila Neema hua nikatika mambo matatu, Jambo la kwanza nikatika Uislam, kwani neema zote hua hazikamiliki na hazina manufaa bila ya kua na neema ya Uislam, kwanihua ni aliekoseshwa Neema ya Kuishi katika Raha ya Milele hapo baadae.**

Jambo la pili ni Afya kwani bila ya kua na neema hii basi Maisha hua hayana maana, kwani Dunia hua ni kama Chumba kidogo kwa Mtu asiekua na Afya.

Jambo la tatu ni neema ya Mali ambayo kama ikitumiwa ipasavyo basi itmapelekea aliekua nao kupata thawabu nyinyi nyingi zaidi'

Imam Wahb Ibn Munabih alisema kua: **'Muumini anatakiwa ajumuike pamoja na watu, kisha akae kimya kwa ajili ya kujifunza asiyoyajua kutokana nao, kujikinga na mazungumzo yasiyokua na maana na kuwausia wengine mambo ya kheri '**

Katika kipindi cha uhai wa Khalifa Sulayman Ibn Abd Malik wa Utawala wa Banu Umayyad, wakati alipokua katika mji wa Makkah, liliokotwa Jiwe ambalo lilikua lina maandishi yasiyojulikana maana yake, hivyo ikabidi atafutwe mtu ambae anaweza kuyasoma maandishi hayo na hivyo akaitwa Imam Wahb Ibn Munabih ambae alipopewa jiwe hilo basi akalisoma kwa kusema kua linasema kua:

'Ewe Ibn Adam, kama kweli unajua namna wakati wako unavyokukaribia basi ungeachana na tamaa zako za mda mrefu, na kuzidisha kufanya mambo mema zaidi badala yake nakujaribu kuachana na Dunia yako, kwanikesho itakua ni siku ya Majuto dhidi yako pale ndugu zako na watoto wako watakapokuingiza Ardhini, na kisha kukuacha huku ukiwa huna uwezo wa kurudi tena Duniani, lakini kama umefanya mema na ukaingia Kaburini basi ni hongera kwako na kama ukiwa umeingia kaburni na mzigo wa dhambi basi ni aibu yako, hivyo jitauyarishe na siku ya Malipo kabla haijawa ni ya majuto kwako. Tahadhari'

Imam Wahb Ibn Munabih alimwambia Imam Ataa Al Khurasan kua**: 'Wanazuoni waliotangulia kabla yetu sisi hawakua ni wenye kuitilia maanani Dunia kwa kushikama na llm ya Dini yao, na hivyo watu wa wakati huo walikua wanaisheshimu Ilm ya Dini yao na hivyo wakawa wanawaheshimu Wanazuoni pia, lakini sasa hivi wale wenye Ilm wanaieneza Ilm yao kwa watu wenye kuendekeza Matamanio ya Kidunia, kwa sababu ya kua macho yao yanatizama mali zao, labda wanadhani kua wanaweza kuipata Dunia yao kutokana nazo. Na hivyo sasa hivi watu wanaoiendekeza Dunia hawaiheshimu wala hawaithamini hata Ilm yao Wanazuoni hao.'**

'Ewe Ataa kaa mbali na wageni wa Sultan, kwani kuna kilevi kwenye milango yao, hivyo huenda ukaipata Dunia kutoka kwao lakini utakua ni mwenye kuitolea Kafara Dini yako na kuipoteza kabisa. Fahamu kua yeyote yule asietosheka na riziki yake hapa Duniani hatokina kitu chochote na mwisho wake atabakia kutoshelezwa na gao la mchanga katika kuzikwa kwake.'

Imam Wahb Ibn Munabih alifariki mnamo mwaka 114 Al Hijra katika Mji wa Sanaa Yemen.

IMAM TAWUS IBN KAYSAN 35 AH

Ingawa Imam Tawus Dakhwan Ibn Kaysan alikua ni mtu mwenye asili ya Yemen, lakini alizaliwa katika ardhi ya Uajemi baada ya wazazi wake kuhamia katika maeneo hayo, na aliitwa Tawus kwa sababu ya Ukubwa na Uzuri wa Ilm yake mbele ya Wanazuoni

wengine na Ucha Mungu wake na hii ni kutokana na jitihada zake katika kutafuta kwake Ilm katika maeneo mbali mbali na kwa Wanazuoni mbali mbali.

Kwani Imam Tawus alisoma kwa *Bahr ul Ilm* Abdallah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na bila ya shaka alikua ni mmoja kati ya Wanafunzi wake bora na hivyo akawa ni mwenye Ilm kubwa sana ya Qur'an, Hadith na Fiqh.

Imam Tawus alikua ni mtu ambae aliamua kuachana kabisa na Dunia yake na alikua ni mwenye kudumu na Idhkar, wenye kumjua walikua wanasema kua Imam Tawus alikua ni **'Kitabu kilichojaa manukato ya Taqwa'** Kwani Imam Tawus alikua ni Mcha Mungu na Mwenye unyenyekevu mkubwa sana na alikua ni mtu ambae ni mwenye kuwakimbia watu wenye Mamlaka mbali ya kua alikua si mwenye kuwaogopa bali alikua ni mwenye kutokua na ukaribu nao.

Kwani Imam Tawus alikua ni mtu mwenye uthubutu wa kusema lolote mbele ya yeyote na alisema Imam Tawus kua: **'Chochote kile Ibn Adam atakachokisema kwa Ulimi wake basi hua kinaandikwa, hata kilio chake katika wakati wa maumivu anapokua anaumwa ndani ya mwili wake'**

Katika wakati wa uhai wake alikua akiishi pamoja na Imam Wahb Ibn Munabih na hivyo siku moja wote wawili waliamua kuelekea kwa Gavana wa Yemen aitwae Muhammad Ibn Yussuf ambae alikua ni ndugu yake Hajjaj Ibn Yusuf kwa ajili ya kuumuusia, na baada ya kuwasili mbele ya baraza lake Gavana huyo basi Imam Tawus akatoa wasia mrefu sana uliojaa matumaini na khofu ndani yake.

Wakati anaendelea kutoa Mawaidha hayo basi Gavana huyo akamwambia mfanyakazi wake kua: **'Chukua vitambaa vyenye thamani kubwa sana kisha viweke kwenye bega la Tawus'** na hivyo Mfanyakazi huyo akondoka na aliporudia akarudi akarudi na Vitabaa vya rangi ya Kija na kuviweka keney bega la Imam Tawus, ambapo Imam Tawus aliendelea kutoa mawaidha yake huku akichezesha mabega yake hadi vile vitambaa vikaanguka chini vyote, na kisha akanyanyuka yeye na Imam Wahb Ibn Munabih wakaondoka.

Tukio hili lilimkera Gavaa huyo, lakini akajizuia na kutofanya lolote mbele za watu, na hivyo walipofika nje ya Kasri la Gavana basi Imam Wahab Ibn Munabih akamwambia Imam Tawus: **'Tawus, Wallahi umefanya sivyo, kwa sababu hatutakiwi kumkasirisha, wewe ungevipokea tu vile vitambaa kisha tukaja tukaviuza na pesa zake tukatoa Sadaqa kwa masikini'**

Imam Tawus akasema: **'Uko sahih kama ikiwa sijali kuhusiana na Wanazuoni watakaosema kua na sisi tutafanya kama alivyovyanya Tawus kua tutapokea**

zawadi kutoka kwa wenye Mamlaka, na kisha hawatofanya kama ulivyosema yaani kuviuza na kutoa Sadaqa.'

Baada ya tukio hilo basi Gavana Muhamamd Ibn Yusuf akachukua kifuko cha Dinari 700 za Dhahabu na akampa mfanyakazi wake na kumwambia: '**Chukua hizi nenda kwa Tawus kafanye kila njia mpaka azipokee, na kama akizipokea basi mimi nitakuzawadia wewe zawadi nzuri sana.**'

Hivyo mfanyakazi huyo akatoka hadi Nyumbani kwa Imam tawus na alipofika akamwambia Imam Tawus kua: '**Kuna mzigo wako nimepewa na Gavana'** ambapo Imam Tawus akasema: **'Samahani lakini mimi sina haja na kitu kutoka kwake'** hivyo mfanyakazo huyo akajaribu kumshawishi Imam Tawus apokee zawadi hio lakini wapi, kazi yake ilikua bure, hivyo akaamua kua mfuko huo lazima auche na wakati anatoka akaona kua kuna tundu kwenye moja kati ya ukuta wa nyumba ya Imam Tawus na hivyo akauchomeka mfuko huo kweye tundu hio na kisha akaondoka. Na kisha akamtaarifu Gavana kua Tawus amepokea zawadi hio.

Muhamamd Ibn Yusuf alifurahi sana alipopata habari hio, lakini hakusema kitu chochote juu yake, baada ya kupita siku mbili Muhamamd Ibn Yusuf akawatuma watu wawilikwa Imam Tawus pamoja na mfanyakazi aliempelekea Imam Tawus Mfuko wa Dinari zile, huku akiwambia kua wakifika basi wamwambie Imam Tawus kua Ule mfuko ulipelekewa kwake kimakosa hivyo anatakiwa auarudishe ili upelekewe unakostahiki.

Hivyo watu hao wakaenda hadi kwa Imam Tawus na walipofika wakafikisha ujumbe huo, ambapo Imam Tawsu akasema: **'La, mimi sikupokea wala sikuchukua kitu chohote kutoka kwa Gavana, hivyo sina cha kukirudisha'** watu hao wakasisitiza kua Imam Tawusa amepokea Mfuko wa Dinar 700, Imam Tawus akamuuliza yule mfanyakazi: '**Hebu sema ukweli, jee mimi nilipokea kitu chochote kile kutoka kwako?**' yule mfanyakazi akaanza kutetemeka kwa khofu na hivyo akasema: **'La, bali mimi niliuweka ule kwenye ukuta wa nyumba yako bila wewe mwenyewe kujua'**

Imam Tawus akasema: '**Nendeni kaangalieni katika sehemu ambaayo anasemakua aliuweka mfuko huo kisha muuchukue mfuko wenu'** watu hao wakaenda kwenye sehemu hio iliyokua na tundu na wakakuta ule mfuko ukiwa uko kama ulivyokua katika siku uliyowekwa na kisha wakarudisha Mfuko huo kwa Gavana.

Mda baada ya kutokea tukio hilo basi ndani ya mwaka huo huo Imam Tawus akaelekea kwenye Mji wa Makkah kwa ajili ya Ibada ya Hijja ambapo nako likatokea tukioa ambalo Imam Tawus analiezea kwa kusema: '**Wakati nikiwa katika Mji wa Makkah nikifanya Ibada ya Hijja, niliitwa mimi na Hajjaj Ibn Yusuf, ambae alinipokea**

kwa vizuri sana na kisha akaniuliza kuhusiana na Manasik ya Hija ambayo alikua hayajui vizuri sana na kuhusiana na mambo mengineo pia.'

Wakati tunazungumza mara Hajjaj Ibn Yusuf akasikia sauti ya mtu ambae alikua akisome *Talbiyah* kwa sauti ya juu, na hivyo akaamrisha kua mtu huyo aletwe mbele yake na alipoletwa basi akamuuliza: 'Wewe unatoka katika kundi la watu gani?' yule Mtu akasema: 'Katika Kundi la Waislam' Hajjaj Ibn Yusuf akasema: 'La hivyo sivyo nilivyouliza, mimi nimekusudia unatoka katika kundi la watu wa ardhi gani?'

Mtu huyo akasema: 'Kutoka kundi la watu wanaoishi Yemen' Hajjaj akauliza: 'Jee vipi Gavana wenu anaendeleaje?' yule mtu akasema: 'Mimi nilipoondoka alikua Mnene, Mzima na yuko salama' Hajjaj Ibn Yusuf akasema: 'La mimi sikukusudia hivyo bali nimekusudia anaendeleaje na nyinyi?' yule mtu akasema kua: 'Anatujali tunapokua hatupo.'

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: 'Inakuaje unasema maneno haya wakati wewe unajua kua yule ni ndugu yangu?' yule mtu akasema: 'Hivi jee unafikiria kua darja yake mbele yako ni kubwa kuliko darja yangu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*? Wakati mimi nikiwa natembelea nyumba yake tukufu kama Hujjaji huku nikiwa nnamuamini Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* na nafuata Dini yake?' hapo Hajjaj IbnYusuf akakaa kimyaa.

Kisha yule mtu akaondoka bila ya hata kuomba ruhusa, hivyo nami nikanyanyuka na kumfuata huku ikisema: '**Huyu atakua ni mcha Mungu, hivyo wacha nimfuate kabla hajatoweka katika zogo la watu' na nilipomtafuta nikamkuta analikaribia guo la Al Kaabah na kuligusisha na shavu lake huku akisema: 'Ya Allah Nakuomba ulinzi wako kwani ni kwako wewe tu mimi ndiko ninakokutegema, Ewe Allah nijaalie kua na maamuzi katika Ukarimu wako na niwe ni mwenye kukubali Uhakika wako ambao ni mkubwa zaidi kuliko tabia za Wabaya, nijaalie niwe na utajiri unaotokana na mikono ya Mabakhili wanaojitanguliza Nafsi zao kwanza. Ewe Allah nakuomba muongozo kutokana na matatizo kwa kutumia wingi wa hikma zako na wema wako wa milele ya *Rabbi Al Alamin*'**

Na baada ya kumaliza hapo akatoweka pamoja na watu wengine waliokuwepo hapo hivyo sikumuona tena hadi katika siku ya Arafah, ambapo nilimuona akijumuika na watu, nami nikamkaribia nikamsikia anaomba dua kwa kusema: 'Ya Allah kama hukuikubali Hija iliyojaa uchovu na jitihada zangu basi nakuomba usinizuie kutokana na malipo ya msiba wa kutojijali nafsi yangu' na kisha akataoweka tena kwenye kundi la watu.

Nami nikapoteza matumaini ya kumuona tena, hivyo nikaomba Dua kwa kusema: 'Ya Allah Mkubaie Dua zake na Dua zangu, Mtekelezee matumainio yake na matumainio yangu, mthibitishie hatua zake na hatua zangu akatika siku ambayo hatua zitatelea, na utukutanishe katika ***Al Kawthar ya Akramah Al Akramin*'**

Safari moja katika Utawala wa Khalifa Sulayma Ibn Abd ul Malik Ibn Marwan kuweka vitu vyake katika *Bayt ul Atiq* na kisha kupumzika kwenye Al Kaabah basi aliwaambia watu wake: '**Hebu tafuteni Mwanazuoni ambae anaweza kutupa Mawaidha kidogo katika masiku haya.** '

Watu hao wakamtafuta Mwanazuoni aliekuwepo katika wakati huo na wakampata Imam Tawus na hivyo wakaambiana kua: '**Huyu hapa Imam Tawus ni Mwanazuoni ambae maneno yake ni ya Haki katika kuusia kuhusiana na** ***Allah Subhanah wa Ta'ala*'** hivvyo wakamfuata na baada ya kumsalimia wakamwambia Imam Tawus: '**Twende zetu kuna mualiko wako kutoka kwa Khalifa Sulayman Ibn Abdul Malik'**

Hivyo Tawus baada ya kuambiwa maneno hayo basi akakubaliana na Mualiko huo kwani anajua kua anatakiwa akausie kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambako kunawatiwa khofu Watawala na kuwafanya wawe ni wenye kujua ukubwa na uzito wa jukumu lao mbele ya Mola wao.

Imam Tawus alipofika mbele ya Khalifa Sulayman Ibn Abdul Malik akasalimia na kisha akaongozwa kwenye baraza la ujumbe wa Khalifa Sulyaman Ibn Abd Ul Malik na akaulizwa kuhusiana na Manasik ya Hijja nae akajibu na kufafanua kama inavyotakiwa na kisha baada ya hapo akakumbuka katika Nafsi yake kua atakuja kuulizwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na Mkutano huo, hivyo akamgeukia Khalifa Sulayman na kumwambia: '**Hivi jee ewe Khalifa Sulayman kuna Jabali kuwa sana ndani ya Moto wa Jahannam linaning'inia juu kiasi ya kua kama likiachiwa basi katika kuanguka kwake hadi kufika chini hua linachukua miaka 70, hivyo jee unajua kua Jabali hilo limewekwa kwa ajili ya watu gani?'**

Khalifa Sulayman akasema: **'La Sijui mimi kuhusiana na Jabali hilo, hivi jee limewekwa kwa ajili ya nani?'** Imam Tawus akasema: **'Limewekwa kwa ajili ya kuwaangukia wale ambao wamejaaliwa kua ni wenye kusimamia Sheria za** ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **hapa Ulimwenguni na kisha watu hao wakawa ni wenye kuzidharau sharia hizo'**

Khalifa Sulayman akashtuka hapo hapo na akaanza kutokwa na machozi, na Imam Tawus nae akanyanyuka kuondoka kwenye Baraza hilo na kuelekea nyumbani kwake alipokua anakaa katika Mji Wa Makkah.

Imam Wahb Ibn Munabih alikutana na Tafiya ambae alikua ni Mwanamke Mcha Mungu sana anaeishi Mjini Jerusalem, hivyo Imam Wahb Ibn Munabih akamuuliza Tafiya: '**Ewe Tafiya, hivi Jee ni jambo gani kwako wewe ni ngumu zaidi?'** ambapo Tafiya akasema '**Ukweli ni kua kwangu mie Tafakkur ni hambo gumu zaid'** Imam Wahb Ibn Munabih akauliza : '**Kwanini?'**

Tafiya akasema: '**Katika kutafakkar kwangu hua nnamfikiria *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Ukubwa wake na yatakayotokea katika siku ya Malipo, na hapo Ufahamu wangu hua ni wenye kuchoka, Machoyangu hupetoza Nuru yake na viungo vyangu vya mwili hua ni vyenye kupoteza nguvu zake'** hivyo Imam Wahb Ibn Munabih akasema: '**Kama ni hivyo basi bora kwako wewe uwe ni mwenye kukimbilia kwenye kisomo cha Qur'an'.**

Katika wakati wa Utawala wa Khalifa Hisham Ibn Abd Ul Malik basi nae pia aliomba ushauri kutoka kwa Imam Tawus ambae alipofika mbele yake basi Imam Tawus akavua viatu vyake na kisha akamsalimia Khalifa Abdul Malik bila ya kutumia jina la *Amir ul Muuminin* na kisha akakaa kitako mbele yake kabla ya hata kupewa ruhusa ya kukaa, jambo ambalo halikumridhisha Khalifa Hisham na hivyo akasema: '**Hivi kwanini ukafanya ulivyofanya Ewe Tawus?**'

Imam Tawus akauliza: **'Kwani nimefanya nini?'**

Khalifa Hisham akasema: '**Umevua viatu vyako mwanzoni mwa Zulia langu, Hukunisalimia kwa cheo changu, Umeniita kwa jina langu moja kwa moja na umekaa kitako bila ya kuamrishwa.**'

Imam Tawus akajibu: '**Ama kuhusiana na kuvua viatu basi mimi kila siku hua nnavua viatu vyangu mara 5 mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hivyo wewe hutakiwi kukasirika juu ya hilo. Ama kuhusiana na kukusalimia bila ya kutaja cheo chako basi hii ni kwa sababu si Waislam wote wanakuunga mkono, na hivyo mimi naogopa kukupa wewe cheo ambacho kitakua ni cha uongo, ama kuhusiana na kukuita kwa jina lako mja kwa moja basi ingawa *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliwaita Mitume wake kwa Majina kwa mfano kama Ewe Daud, Ewe Yahya, Ewe Musa, Ewe Isa, lakini aliwaita maadui zake kwa vyeo vyao kwa mfano Imeangamia mikono ya Abu Lahab na bila ya shaka yeye pia ataangamia'**

Ama kuhusiana na kukaa kitako mbele yako bila ya kuamrishwa nawe basi kwa hakika mimi nimemsikia *Amiru ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akisema kua: 'Ukitaka kumuona Mtu wa Motoni basi angalia yule aliekaa wakati wengine waliomzunguka wakiwa wamesimama' na hivyo mimi sipendi kukuangalia wewe na kisha nikakuona kua ni mtu wa Motoni'

Baada ya kusikia ujumbe huo basi Khalifa Hisham akasema: **‘Nimekufaham ewe Tawus sasa hebu niusie’** Imam Tawus akasema: **‘Mimi nilimsikia Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akisema kua: ‘Motoni kuna Nyoka ambao ni wakubwa kama Nguzo na Nge wenye ukubwa kama wa Farasi, ambao ni maalum kwa Viongozi wasiokua waadilifu kwa watu wao’’** kisha baada ya hapo Imam Tawus akanyanyuka na kuondoka.

Anasema Imam Ataa Ibn Ab Rabah kua: ‘**Siku moja Tawus aliniona mimi katika hali ambayo hakuipenda hivyo akaniambia: ‘Ewe Ata hivi kwanini wewe unaelezea shida zako kwa yule mtu ambae ni mwenye kuufunga mlango mbele yako na kuweka walinzi nje yake?’ muombe yule ambae ni mwenye kuacha wazi mlango wake na kukuita ndani yake na mwenye kuahidi kutekeleza ahadi zake’**

Imam Tawus alimuusia mtoto wake kwa kumwambia: **‘Ewe Mtoto wangu jumuika na watu wema kwani nawe utajumuishwa nao katika kundi lao, na wala usijumuike na watu wajinga kwani nawe utajumuishwa nao pamoja nao hata kama ukiwa si kama wao, fahamu kua kila kitu kina kilele chake na kilele cha Mtu hua kinategemea na ukamilifu wa Dini yake na Tabia zake.’**

Anasema Abd Allah Ash Shami kua: ‘**Mimi nilienda kwenye Nyumba ya Tawus Ibn Kaysan kutaka kujifunza kitu kutoka kwake na nilikua simjui, hivyo basi nilipogonga na kufunguliwa mlango nikakutana na Mzee Fulani ambae nilimsalimia na kisha nikamuuliza: ‘Jee wewe ndie Tawus Ibn Kaysan’ Mzee huyo akasema : ‘La mimi ni Mtoto wake’ hivyo nami nikasema: ‘Kama wewe ni mtoto wake basi bila ya shaka Shaykh atakua Mtu mzima sana, nami nimetoka mbali kwa ajili ya kuja kusoma kwake’’**

Mtoto wa Tawus akasema: ‘Usiwe Mjinga, kwani watu wanaosomesha Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua hawawi wazee wenye kusahau, ingia ndani’ nami nikaingia ndani na nikamsalimia Tawus na kumwambia: ‘Hakika mimi nimekuja kwako kwa sababu nataka kujifunza kutokana na ushauri wako’

Tawus akasema: ‘Nitakua mchache wa maneno, hivi jee unataka kujua kuhusiana na ujumbe wa Taurat, Zabur, Injil na Quran?’ nami nikasema : ‘Naam’ Tawus akasema: ‘Muogope Allah kwa kadiri utakavyoweza kwa kutolinganisha Khofu yako juu yake na khofu za aina nyengine, Muombe maombi makubwa kuliko namna unavyomuogopa na wafurahishe wengine kama unavyojifurahisha nafsi yako’

Kuna mtu alimwambia Imam Tawus kua anamuomba amuombee Dua ambapo nae akasema: **‘Hakika mimi sioni unyenyekevu tosha wa kumuogopa *Allah Subhanah***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

***wa Ta'al*a kwenye Moyo wangu wa kukuombea wewe mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*.'**

Mnamo mwaka 106 Al Hijra Imam Tawus alifariki Dunia wakati akiwa katika ibada ya Hija yake ya 40 katika maeneo ya Muzdalifa baada kusali Sala ya Isha na kupumzika kwake, hakuamka tena.

IMAM SALIM IBN ABD ALLAH IBN UMAR 36 AH

Wengi wetu ni wenye kuwajua Masahaba wawili maarufu sana wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambao ni *Umar ibn Al Khattab Radhi Allahu Anhu* na mtoto wake ambae ni Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab Radhi *Allahu Anhu*. Kwani baada ya watu wawili hawa ambao ni watu ambao wamebashiriwa Pepo, basi kuna mtu wa tatu ambae ametokana na Watu wawili hawa muhimu katika Uislam.

Na mtu huyo si mwengine isipokua ni Mjukuu wa *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kupitia kwa mtoto wake huyu Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*, ambae alikua na Mtoto wake aitwae Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*.

Kwani tunapomzungumzia Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* basi hua hatumzungumzii mtu yeyote yule isipokua tunamzungumzia Mmoja kati ya Wanazuoni 7 Wakuu wa Mji wa Madina baada ya kufariki Masahaba. Kwani hawa walikua ni Wanazuoni waliozaliwa katika kipindi cha Masahaba na hivyo hawakuwahi kumuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.

Na hivyo hua wanajulikana kama Tabiin yaani waliofuatia baada ya Masahaba. Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua ni kijana aliejipatia Ilm yake kutoka moja kwa moja kwa Masahaba. Na bila ya shaka Mwalimu wake wa kwanza ambae ni Sahaba alikua ni Baba yake. Na katika Masahaba hakuna anaemuweza Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kwa Kufuata Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kwani mpaka sehemu aliyosimama *Rasul Allah Salallahu* na kujisaidia haja ndogo basi Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua lazima akajisaidie hapo hapo.

Kwa sababu kwake yeye hio ni Sunnah sasa fikiria wewe kua Baba mtu anakua kama hivi, halafu na mtoto anafuata Nyayo zake, jee hali yake itakuaje? Naam hio ndio hali aliyokua nayo Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*.

Na si hivyo tu, kwani ingawa hio ni hali yake katika Ibada lakini kwa upande mwengine basi Salim ibn Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua ni Kijana Mwenye Imani, Tabia na Misimamo kama ya Babu yake. Yaani alikua pia kama Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*

Hivyo Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar alikua ni kijana anaependwa sana na Baba yake. Na bila ya shaka Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua ni kijana Mcha Mungu sana, kiasi ya kua anasema *Mujtahid* Imam Malik Ibn Anas ambae ndie muanzilishi wa Madhhab ya Maliki kua: '**Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akifanana zaid na Wacha Mungu waliotangulia kabla yake kuliko wale aliokua nao katika Wakati wake'**

Kwani siku Moja Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alikua amekaa ndani ya Jengo Tukufu la *Al Kaabah* akifanya *Dhikr Allah*, mara akatokea Khalifa wa Banu Ummayad aitwae Hisham Ibn Abd Ul Malik ambae ni mwenye kumjua vizuri Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na hivyo akamsalimia na kisha akamwambia: '**Ewe Salim! Kama itatokea kua Una Shida basi usiwache kunijuulisha**'

Ambapo Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akanyanyua uso wake na kusitisha Dhikr zake na kisha akasema: '**Hakika Mimi nnaona Haya kua Nimekaa ndani ya Nyumba ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha, niwe ni mwenye Kumuomba kitu Mwengine zaid yake**.'

Kwani Khalifa Hisham akatahayari, lakini hapo hapo akavutiwa na Jibu la Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kwani lilikua linatokana na Ucha Mungu wake. Hivyo Khalifa Hisham akatoka nje ya *Al Kaabah*. Akakaa na kumsubiri Imam Salim atoke nje ya Al Kaabah, hadi pale Imam huyo alipotoka nje yake.

Na alipotoka basi akamsogelea na kumwambia Imam Salim kua: '**Ewe Salim, Hakika sasa hivi Umetoka nje ya Al Kaabah na huko Ndani yake, hivyo nakuomba kua kama utakua na Shida basi usiwache kuniambia nami niko tayari kukusaidia'**

Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: '**Unataka nikujuulishe kuhusiana na Jambo la Kidunia au la Kiakhera?**

Khalifa Hisham akajibu: '**Jambo lolote lile la Kidunia ukiwa na haja nalo niambie**'

Hivyo Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: '**Ewe Hisham! Hakika mimi Sijawahi Kumuomba kuhusiana Jambo la**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kidunia kutoka kwa yule ambae ndie alieiumba Hii Dunia. Hivyo Itakuaje leo hii Mimi Niwe ni mwenye kumuomba yule asiekua Mmiliki wa Dunia hii?'

Naam..Baada ya Khalifa Umar Ibn Abd Ul Aziz kuingia Madarakani basi aliomba Wasia kutoka kwa Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambae nae alimuusia kwa kumwambia: '**Ewe Umar Ibn Abd Al Aziz kama unataka usiwe na mzigo mzito mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika siku ya Malipo basi basi jichunge na Dunia hii kama vile Mtu anavyojichunga katika Ibada ya kufunga na hivyo Iftar yake hua ni katika wakati wa kifo chake.'**

Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Radhi Allahu Anhu alifariki mnammo mwaka 106 Al Hijra na alisaliwa na Khalifa Hisham Ibn Abd Ul Malik baada ya ibada ya Hija ya mwaka huo katika Mji wa Madina.

IMAM ZAYN AL ABIDIN 38 AH

Imam Zayn Al Abidin alizaliwa katika siku ya Alkhamis ya tarehe 5 mwezi wa Shaaban ya mwaka 38 Al Hijr katika mji wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yaani Mji wa Madina, katika familia ya *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kupitia kwa Husein ambae ni mjukuu wa *Rasul Allah Salallahu Allahu Alayhi wa Salam* na alipewa jina la Ali Ibn Husein Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*, na akawa pia anajulikana kama Zayn Al Abidin.

Mama yake Imam Zayn Al Abidin alikua ni Shahrbanu ambae alikua ni Mtoto wa Mfalme wa Yazdigard wa tatu wa Uajemi, ambae alitekwa baada ya Waislam kuiteka ardhi ya Khurasan katika kipindi cha Utawala *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*, ambapo neno Shahrbano maana yake hua ni Mwanamke Mzuri wa Ardhi fulani.

Ambapo anasema Imam Az Zuhri kua: '**Hakika mimi sikuwahi kuona mtu yeyote wa kabila la Quraysh alie bora kama alivyokua Imam Zayn Al Abidin.**'

Kwani Imam Zayn Al Abidin alilelewa na babu yake yaani *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kwa mda wa miaka 10 na akalelewa na ami yake yaani Hasan Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na akalelewa kwa mda wa miaka 11 na baba yake yaani Imam Husein Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu.*

Imam Zayn Al Abidin alikua ni mwenye kufanana sana kimaumbile na Babu yake yaani

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kwani hakua mweupe pepee bali alikua ni mweupe mwenye wekundu na hakua mrefu sana ila alikua ni mwenye ndevu nyingi sana.

Ambapo anasema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Mimi nilikua nimekaa ukumbini kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, huku *Husein Radhi Allahu Anhu* akiwa kweye mikono ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nae akasema kuniambia: 'Ewe Jabir, kuna mtoto atakaezaliwa kutokana nae (Husein) ambae atakua anaitwa Ali ambae nae atakua na mtoto ambae atakua anaitwa Muhammad, hivyo ukikutana nae basi nisalimie''**

Imam Zayn Al Abidin alikua ni kijana mwenye tabia nzuri sana, mwenye Ilm kubwa sana, heshima, ukarimu na huruma nyingi sana kwa wenye kuhitaji msaada, hata kama ni watu wenye mtizamo mbaya juu yake, kwani kua aliwahi kusikia kua kuna mtu anamsema vibaya kwa mda mrefu, hivyo nae akafunga safari kumfuata mtu huyo na alipofika akamsalimia kwa ukarimu na ucheshi kiasi ya kua mtu huyo alibadilisha mtizamo wake juu yake Imam Zayn Al Abidin na kumuomba msamaha na kuanza kutafuta kua na ukaribu nae.

Ambapo anasema Imam Malik kua: **'Imam Zayn Al Abidin ni Mtu mwenye kutokana na Watu bora.**'

Imam Abu Hazim anasema kua: **'Mimi sijaona Mwanafiqh aliekua juu zaidi yake.'**

Na kwa upande wa Imam Ibn Shaibah basi yeye anasema kua: **'Sanad bora zaidi ni zile zilizonukuliwa na Imam Zayn Al Abidin ambazo amenukuu kutoka kwa Husein *Radhi Allahu Anhu.*'**

Imam Zayn Al Abidin Ali Ibn Husayn Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alikua anapenda sana kusali, kiasi ya kua anaweza akababakia katika kusjudu kwa saa nzima. Hivyo siku moja alikua Nyumbani kwake, Nyumba yake ikawa inawaka Moto, na yeye alikua kwenye Sijda. Watu wakatoka ndani ya Nyumba hio huku wakinadia Moto! Moto!

Wakatoka watu wote na vitu vyao, na walipofika nje wakajiona kua wako peke yao bila ya kuwepo Imam Zayn al Abidin *Radhi Allahu Anhu.* Watu hao wakanza kuulizana yuko wapi na wakajawa na khofu, wasiwasi na huzuni kubwa sana.

Lakini baada ya mda Moto ukaisha na kuzimika, watu wakaingia ndani na kumkuta Imam Zayn Al Abidin bado akiwa kwenye Sijda huku akiwa hajadhurika hata kidogo kutokana na Moto huo hivyo wakamsubiri mpaka alipomaliza Kusali na alipomaliza basi wakamuuliza: '**Ya Zain Al Abidin hivi hukusikia wewe watu walipokua wakinadia Moto Moto!?'**

Imam Zayn Al Abidin akasema: '**Bila ya shaka nilisikia lakini sasa akili yangu yote ikakimbilia kufikiria kwenye Moto wa Jahannam badala ya kukimbilia kufikiria Moto wa Duniani, hivyo khofu yangu ikazama kwenye moto wa Akhera kwani ndio mkali zaidi, ikanibidi nibakie kwenye Sijda kumuomba Mola wangu aniepushe na Moto wa Jahannam**.'

Imam Zayn Ibn Abidiin alikua ni mtu mwenye kujitolea kila kitu chake kwa ajili ya Uislam, na alikua akiwatumia misaada Masikini kwa siri bila ya kua ni mwenye kujlikana kua ni mwenye kufanya hivyo, mbali ya hivyo liakini pia Imam Zayn Al Abidin alikua ni mtu mwenye Subra kubwa sana kwani baada ya vita vya Karbala basi alikamatwa na kuongozwa kwa miguu huku akiwa amefungwa minyororo hadi katika Mji wa Dimashq.

Na katika kipindi cha utawala wa Khalifa Abdul Malik Ibn Marwan basi alikamatwa na kutembezwa kwa miguu kutoka Madina hadi Syria huku akiwa amefungwa minyororo. Ambapo katika mtukio yote haya basi hakuwahi kulalamika hata mara moja kwa watu wala kwa Mola wake bali alikua ni mwenye kumshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa mitihani yake. Hili ni jambo ambalo lilimtia huzuni sana Imam Az Zuhri ambae alikua ni Mwanafunzi wake, hivyo akaenda moja kwa moja kwa Khalifa Abd Ul Malik Al marwan kumuombea Imam Zayn Al Abidin ili aachiwe huru na Khalifa Abd Ul Malik Ibn Marwan alipomuachia Huru basi Imam Al Zuhri akarudi nae Imam Zay Al Abidin katika Mji wa Madina.

Siku Moja Imam Zayn Al Abidin alikua akipita katika mitaa ya Mji wa Madina na mara akagongana bega na mmoja kati ya watu ambao ni wageni katika Mji wa Madina. Hivyo mtu huyo akaanza kugombana nae Imam Zayn Al Abidin ambae hata hivyo wafanyakazi wa Imam Zayn Al Abidin wakaingilia kati na kutaka kupigana na Mtu huyo, lakini Imam Zayn Ibn Abidiin akawazuia na kisha akaumuuliza kwa ukarimu Mtu huyo kama ana tatizo lolote lile basi atamsaidia kutatua tatizo hilo.

Ambapo suali hilo lilimfanya mtu huyo kupungukiwa na hasira na hivyo akainamisha kichwa chini kwa kuona haya. Hivyo Imam Zayn Ibn Abidiin akavua Joho lake na kisha akamvisha Mtu huyo, na kisha akaamrisha kua apewe Dirham 1000, jambo hili nalo pia likamzidisha mtu huyo kunyong'onyea na hivyo akaanza kulia huku akionesha shukrani kwa kusema: '**Wallahi nnadhani mimi kua wewe ni miongoni mwa watu watokanao na ukoo wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.**'

Imam Zayn Al Abidin akasema: '**Unayoyasema ni maneno mazuri sana kutokana na unachokijua lakini kile kisichojulikana kwako juu yangu ni bora zaidi**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Siku moja Imam Zayn Al Abidin alimtembelea Muhammad Ibn Usamah na akamkuta akiwa analia kwa sababu ya deni asiloweza kulipa hivyo Imam Zayn Al Abidin akamlipia deni hilo.

Kuna mtu alimzulia Imam Zayn Al Abidin, hivyo Imam Zayn Al Abidin akamwambia Mtu huyo kua: '**Kama ikiwa hayo unayosema juu yangu ni ya kweli basi mimi naomba msamaha kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kama si ya kweli basi bila ya shaka pia nitakuombea wewe msamaha kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala***' hivyo mtu huyo akajisikia vibaya sana na akamwambia Imam Zayn Al Abidin kua: '**Kwa hakika mimi ndie niliekukosea hivyo naomba msamaha wako na pia nnaomba uniombee msamaha wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* anikubalie msamaha wangu**'

Ambapo anasema Imam Talha Al Shafii: '**Siku moja wakati Imam Zayn Al Abidin anasali basi mara Ibilisi akatokea katika maumbile ya Nyoka mkubwa sana, na kisha akakiingiza mdomoni mwake kidole gumba cha mguu wa Imam Zayn Al Abidin, lakini Imam Zayn Al Abidin akatulia tulii hata hakushtuka, na kisha baada ya hapo Nyoka huyo akakiwacha kidole hivyo na akakaa pembeni, na mara ikasikika sauti ikisema: 'Hakika wewe ni Lulu ya wenye kufanya Ibada, wewe ndie Chifu wa wenye kusjudu.'**

Anasema Imam Jafar As Sadiq kua: '**Babu yangu Imam Zayn Al Abidin alipokua akisoma Qur'an basi uzuri wa kisomo chake ulikua unawavutia wengi sana kiasi ya kua watu wote waliokua wakimsikiliza walikua wanajawa na khofu juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kutojuana hali zao baina yao miongoni mwao.**'

Aliulizwa Imam Zayn Al Abidin: **'Hivi jee ni mtu gani ambae ataangaliwa na kuonekana kua ni mwema katika siku ya Malipo?'** ambapo nae akasema: **'Ni yule mtu ambae furaha yake haimpelekei kufanya madhambi na hasira zake hazimzuii kufanya yale yaliyokua sahih.'**

Alisema Imam Zayn Al Abidin kua: '**Pale Muislam anapotoa Sadaqah na mpokeaji wa Sadaqah hio akomba Dua kumuombea alietoa basi Dua hio hua ni yenye kukubaliwa.'**

Imam Zayn Al Abidin alifariki mnamo siku ya mwezi 18 wa Muharram wa 96 Al Hijra baada ya kuumwa kutokana na kudhurika na sumu na alizikwa kwenye Mji Wa Madina, ambapo kuna wasemao kua alifariki nchini Misri na kuzikwa Mjini Al Qahira.

Ambapo katika siku aliyozikwa basi watu waliona kua maiti yake ina alama mgongoni, hivyo wakaulizana juu ya alama hio, na Imam Muhamamd Al Baqir akasema: '**Baba yangu alikua ni mwenye kuwanufaisha Masikini, Wajane, Wazee, na Mayatima**

hivyo kila siku usiku alikua akitoka huku akiwa na gunia lake la tende mgongoni kwa ajili ya kuwagaiwa watu wasiokua na uwezo wa mji wa Madina.'

IMAM QASIM IBN MUHAMMAD 38 AH

Imam Al Qasim Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* alikua ni mjukuu wa *Amir Ul Muuminin* Abu Bakr As Siddiq *Radhu Allahu Anhu* na hivyo shngazi yake alikua ni *Ummu Ul Muuminin* Aisha *Radhu Allahu Anha*, ambapo mama yake Al Qasim alikua ni Mehrbanu bint Yazdigard wa tatu ambae alikua pia ni Dada yake Sharhbanu Bint Yazdigard ambae ni Mama yae Imam Zayn Al Abidin.

Imam Al Qasim alikua ni mmoja kati ya Wanafiqh wakubwa sana wa mji wa Madina na hii ni kwa sababu alikua ni mwenye kusoma kutoka kwa Shangazi yake *Ummu Ul Muuminin* Aisha *Radhu Allahu Anha*, na hivyo alikua na ilm kubwa sana ya Quran, Hadith na Fiqh.

Kwani Imam Al Qasim alikua akisema kua: '**Aisha alikua ni Mufti mwanamke katika kipindi cha Abu Bakr, Umar na Uthman *Radhi Allahu Anhum* hadi alipofariki na mimi nilikua najitahidi kusoma kutoka kwake na pia kwa Abd Allah Ibn Abbas, Abu Hurayrah na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum***'

Ambapo anasema Imam Abu Zannad kua: '**Hakika mimi sijawahi kuona mtu aliekua bora zaidi ya Al Qasim katika wakati wetu kwani ilikua mtu hahesabiki kua na Ilm miongoni mwa watu hadi pale anapokua ni mahiri katika Ilm ya Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Al Qasim alikua mkamilifu katika hilo'**

Imam Al Qasim alikua ni mwenye kuchukia kukosa kuenda kwenye Masjid Nabii hivyo kila siku alikua anapenda kua kila anapoenda hua ni mwenye kusali Rakaa mbili na kisha hua ni mwenye kukaa katika sehemu ambayo ilikua ikipendwa kukaliwa na *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* katika maeneo ya *Rawdhah* baina ya Kaburi la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Minmbar yake, na kisha baada ya hapo Wanafunzi wake hua ni wenye kumzunguka kwa ajili ya kujipatia Ilm yake.

Imam Al Qasim Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* na Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* walikua ni Maimamu wawili wa Mji wa Madina ambao walikua wakaiminiwa na kusikilizwa kutokana na Taqwa na Ilm yao ingawa walikua hawana Mamlaka yeyote ya kisiasa kwenye Mji wa Madina lakini walikua wakisikilizwa sana na Makhalifa wa Utawala wa Banu Umayyad wa Dimashq.

Ambapo alisema Khalifa Umar Ibn Abd Ul Aziz kua: '**Kama ingekua yamo ndani ya mikono yangu maamuzi ya Ukhalifa basi mimi ningemteua Al Qasim kua ni Khalifa katika wakati wangu.**'

Ambapo alisema Imam Sufyan kua: '**Kuna baadhi ya watu walienda kwa Al Qasim wakiwa na Sadaqa ambayo aliigawa na kisha akenda kusali, na wakati alipokua anasali basi watu hao wakaanza kumsengenya Al Qasim. Hivyo mtoto wake akawaambia watu hao, nyinyi mnamzungumzia vibaya mtu ambae aligawa Sadaqa zenu bila ya yeye kuchukua hata sehemu ya Sadaqa hio**?'

Hivyo baada ya kumaliza kusali Imam Al Qasim akamwambia Mtoto wake huyo: '**Mara nyengine kaa kimya usiseme kitu**' na hii ni kutokana na kua Imam Al Qasim hakua mtu mwenye kupenda kuwafurahisha watu kutokana na ayafanyayo bali alikua ni mwenye kutafuta ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na ayafanyayo.

Ambapo anasema Yahyah Ibn Said kua: '**Hakika sisi hatujawahi kuona mtu aliekua bora katika wakati wetu kama Al Qasim'** na akasema Ayub As Sakhtiyani kua**: 'Hakika mimi sijawahi kuona mtu bora kama Al Qasim, kiasi ya kua baada ya kufariki kwake aliacha Dinar 100,000 kwa ajili ya Masikini ambazo zote zilikua ni kutokana na kipato chake cha halali.**'

Na alisema Imam Al Qasim kua: **'Mtu anaeishi kwenye ujinga baada ya kujua haki za Allah hua ni bora kuliko yule anaetoa Fatwa bila ya kua na Ilm.'** Kwani mbali ya kua ni mwenye kujua sana lakini Imam Al Qasim hakua ni mtu mwenye kupenda kutoa Fatwa kutokana na Ucha Mungu wake, na hata alipokua akiulizwa ni nani mwenye Ilm zaid? : '**Al Qasim au Salim?**' basi alikua ni mwenye kujibu: '***Ya Allah! Subhanah Allah! Subhanah Allah, Subhanah Allah*..ni Salim, bora Muulizeni yeye.**'

Ambapo anasema Imam Ibn Is-haq kua: '**Al Qasim alikua hapendi kusema kua Mimi nna Ilm zaid ya Salim kwa sababu hiyo hua ni Kujionesha, na alikua hasemi kua ni Salim kwani kusema hivyo hua ni kusema uongo. Kwani Bila ya shaka Al Qasim alikua yuko juu kuliko Salim.**'

Amesema Imam Abu Az Zinad kua: '**Sikuwahi mimi kuona mtu mwenye kujua kuhusiana na Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* zaid ya Al Qasim, na sikuona mwenye ufaham kama wake**.'

Imam Sufyan Ibn Uyaynah anasema kua: '**Watu wanaojua Hadith kutoka kwa Aisha *Radhi Allahu Anha* ni Al Qasim Ibn Muhammad, Urwah Ibn Az Zubayr na Amarah Bint Abd Rahman.**'

Imam Al Qasim aliishi kwa mda katika Mji wa Madina na kisha baadae akaondoka na kuhamia katika maeneo ya ardhi ya baina ya Makkah na Madina mnamo mwaka 109 Al Hijra ambao alifariki katika sehemu hio huku akiwa na umri wa miaka 70.

IMAM ATAA IBN YASIR 39 AH

Imam Abu Muhammad Ata Ibn Yasir Al Madani alizaliwa katika Mji wa Madina mnamo mwaka wa 39 A Hijra, na alikua ni mtumwa alieachiwa huru wa *Ummu ul Muuminin* Maymuna Bint Harith *Radhi Allahu Anha* ambapo kutokana nae ndipo alipoanzia kujipatia Ilm yake.

Imam Ataa Ibn Yasir alisoma kwa Masahaba kadha ambao walikua ni Wanazuoni akiwemo Zayd Ibn Thabit, Abd Allah Ibn Masud, Abd Allah Ibn Abbas, Abd Allah Ibn Umar, Aisha *Umm ul Muuminin,* Abu Dardaa, Abu Dhar Al Ghifari, Muadh Ibn Jabal, Ubaydah Ibn Samit, Muawwiyah Ibn Hakam, Abu Qatadah, Abu Hurayrah na wengineo *Radhi Allahu Anhum.*

Imam Ataa Ibn Yasir alikua ni miongoni mwa Wasomaji wazuri sana wa Qur'an, kwani yeye alikua ni miongoni mwa mabingwa wenye jukumu la kuihifadhi Qur'an kwa watu wa Mji wa Madina, ambapo katika wakati wa kipindi chake ilikua kuna Wanazuoni wenye jukumu hili katika Miji mitano ambayo ni Madina, Makkah, Kufah, Basra na Dimashq.

Imam Ataa Ibn Yasir ni Mwanazuoni anaeaminika sana katika Ilm ya Qiraa na Hadith, hivyo alikua ni Hazina kubwa ya Ilm ya Dini ya Kiislam, ambapo Imam Ibn Hibban amesema kua: '**Ataa Ibn Yasir ni Mmoja kati ya Wanazuoni wa Hadith ambao wako makini sana na wasiotaka maskhara katika kunukuu Hadith**' na Imam Ibn Saad amesema kua: **'Ataa Ibn Yasar ni Thiqah'**

Ambapo miongoni mwa Hadith alizozinukuu Imam Ataa Ibn Yasir ni ile isemayo kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Mtu mwenye Dirham 40 au kitu chenye thamani hio na kisha akawa ni mwenye kuomba, basi hua ni mwenye kufanya Dhambi kutokana na kuendelea kuomba kwake**.'' na pia ile isemayo kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Watu walio bora ni wale wenye kulipa madeni yao kwa haraka sana.**''

Na anasema Imam Ataa Ibn Yasr kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuuliza kwa kumwambia Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Ewe Umar, hivi jee ewe Umar utajisikiaje pale utakapofariki, na kisha watu wako watatayarisha Kaburi lako, na kisha wakakutia ndani yake na kukufunika udongo juu yako, na kisha Munkar na Nakir wakaanza kukuuliza masuali, huku Sauti zao zikiwa kama Radi na Macho yao kama mwangaza wa Radi, na Nywele zao zikiwa hazikuchanwa. Na Meno yao yakiwa na ncha kali na kuugeuza udongo wa kaburi lako Juu chini, na kukuweka katika hali ngumu tofauti na kukutisha, Utakuaje hali yako ewe Umar?'**

Ambapo Umar akauliza: ‘Hivi Jee itakua na akili zangu kama ilivyo sasa hivi?’ ambapo *Rasul Allah Salallahu A’layhi wa Salam* akasema: ‘Naam.’ Ambapo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: ‘Nitashughulika nao na kuwajibu masuali yao wayaulizayo.’’

Amesema Imam Ataa Ibn Yasar kua: **‘Listi ya wale watakaofariki katika siku ya mwezi 15 Sha’ban hua anakabidhiwa Malaika Izrail, ambapo katika siku hio basi kuna watu wanaojenga Majumba, wanafanya kazi, wanapanda Miti, Wanaoa n.k ambao wote wamo kwenye listi hio lakini hawajijui.’**

Imam Imam Ataa Ibn Yasar amesema kuhusiana na aya ifuatayo kua:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِنَّمَا ٱلْخَمْرُ وَٱلْمَيْسِرُ وَٱلْأَنصَابُ وَٱلْأَزْلَٰمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ

ٱلشَّيْطَٰنِ فَٱجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo innama alkhamru waalmaysiru waal-ansabu waal-azlamu rijsun min AAamali alshshaytani faijtaniboohu laAAallakum tuflihoona *(Surat Al Maidah 5:90)*

Tafsir: ***Enyi wale ambao Mlioamini hakika ya Ulevi, na Kamari na Masanamu na Kuangalia kwa kutumia Mipinde ni Uchavu miongoni mwa amali za Shaytani, hivyo jiepusheni nazo ili mptae kua ni wenye kufaulu.***

Maana ya Aya hii tukufu katika kitabu cha *Tawrat* inasema kua: ‘Achaneni na michezo isiyokua na maana na angamizeni ala zenu za Miziki, hivyo tukatuma ukweli na kusema Aibu iliyoje kwa mwenye kunywa Kilevi, yaani hapa *Allah Subhanah wa Ta’ala* anaapa kwa Utukufu wake na kusema kua: ‘Kama mtu akiwa atakunywa Ulevi na wakati anajua kua ni Haram basi nitamjaalia kua na kiu kubwa sana katika siku ya Malipo, na kama ataachana nao kutokana na kujua kua ni haramu basi nimjaalia kua ni mwenye kunywa kutokana na Mito ya Peponi’’

Imam Ataa Ibn Yasir alifariki nchini Misri mnamo mwaka 102 Al Hijra.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM BAKR IBN ABD ALLAH AL MUZANI

Imam Bakr Ibn Abd Allah Al Muzani alizaliwa ndani ya miaka 100 ya Mwanzo ya Uislam na alisoma kwa Masahaba wakiwemo kina Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas R*adhi Allahu Anhu* na pia alisoma kwa Wanazuoni wa Tabiina wakiwemo kina Imam Mughira Ibn Shuba, Imam Hasan Al Basr, na wengineo.

Imam Bar Ibn Abd Allah aliwasomesha Wanazuoni wenge sana pia wakiwemo kina Imam Qatadah, Imam Thabit Al Bunani, Imam Sulayman At Taymi, Imam Ibn Al Madini, Imam Abu Zura, Imam Yahya Ibn Main n.k

Imam Bakr Ibn Abad Allah alikua ni Mcha Mungu na mwenye kuaminika sana, na alikua ni mtu mwenye kuachana na Dunia kabisa na ni mwenye kukaa mbali na kila jambo la haramu na lisilokua na uwazi kuhusiana na uhalali wake ndani yake.
Kutokana na Ucha Mungu wake basi Imam Bakr alikua akijiona ana Dhambi nyingi sana, kiasi ya kua huenda Ibada zake anazofanya na wenzake zisije zikakataliwa kutokana nae, hivyo Imam Bakr alipoenda kwenye Ibada ya Hija basi alisema baada ya Ibada yake hio kua: '**Kama mimi nisingekua miongoni mwao basi huenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* angewasamehe Mahujaji wote.'**

Ambapo alisema Imam Bakr kua: **'Miongoni mwa mambo nnayoyapenda mimi zaidi ni kuwapenda watu wema'**

Imam Bakr Ibn Abd Allah alisema kua: **'Kama ukiwa unahisi kua unapata kero na adha kutoka kwa Waumini wenzako basi fahamu kua hii ni kutokana na Dhambi ambayo uliifanya hapo kabla, hivyo rudi kwa Mola wako haraka sana na fanya Istighfar, na ukiona kua unapata mapenzi kutoka kwa Waislam wenzako basi jua hio ni kutokana na kua na Utiifu wako kwa Mola wako na hivyo Mshukuru Mola wako.'**

Na akasema tena kua: '**Ukimuona mtu ni mwenye kudumu katika kusambaza aibu za wenzake huku na kule kama kwamba hio ndio kazi yake peke yake basi fahamua kua mtuhuyo amenasa kwenye Mtihani wa kuadhibiwa na Mola wake.**'

Na akasema tena kua: '**Jihadhari na nua ni mwenye kusema maneno yasiyokua na maana ambayo yatakupelekea kua ni mwenye kupata dhambi kutokana nayo unapokosea na kusema uongo, kwani hii hua inamaanisha kua una mtizamo usiokua mzuri juu ya Muislam mwenzako.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Amesema Imam Bakr Ibn Abd Allah kua: **‘Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Amesema *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua: ‘Enyi Ibn Adam, hata kama Dhambi zenu zitakua ni zenye kujaa hadi kufikia kuzigusa Mbingu, basi kama mkiomba msamaha kwangu mimi, basi mimi nitakusameheni, na Enyi Ibn Adam hata kama mkija kwangu huku mkiwa na Dunia nzima ya Madhambi, na kisha mkakutana na mimi bila ya kua ni wenye kunishirikisha mimi basi mimi nitakusameheni dhambi zote.’’’**

Imam Bakr Ibn Abd amesema kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa kuhusiana na vitu viwili ambavyoni lazima kuingia Ndani yake, yaani Pepo na Moto ambapo nae akasema: ‘Pepo ni Wajibu kwa Mtu ambae atakutana nae *Allah Subhanah wa Ta’ala* bila ya kua ni mwenye kumshirikisha, kwani yeyote yule atakaekutana na *Allah Subhanah wa Ta’ala* baada ya kua ni mwenye kumshirikisha basi Moto hua ni wajibu kwake.’’

Anasema Imam Bakr Ibn Abd Allah kua: ‘**Unapokua pamoja na rafiki yako, hua unatakiwa uwe ni mwenye kutimiza wajibu wako juu yao, kiasi ya kua hata kama itafunguka kamba ya kiatu chake nawe ukawa hujamsubiri wakati akiwa anaifunga kamba yake hio basi unakua hujasimamia haki ya urafiki wenu huo juu yake.’**

Imam Bakr Ibn Abd Allah alikua akiomba Dua kwa kusema: **‘Ewe Mola wangu, hakika bila ya msaada wako basi mimi siwezi kufikia malengo yangu, na wala siwezi kujilinda kutokana na madhara dhidi yangu, kwani kila kitu changu kiko chini ya Mamlaka yako, Nakuhitajia kwa kila changu ewe Mola wangu.’**

Na alikua akipenda kuomba kwa kusema: **‘Ewe Allah tujaalie sisi Riziki ambayo itatupelekea kua ni wenye kukukumbuka na kuonesha shkuran juu yako.’**

Na pia alikua akiomba kwa kusema: ‘Ya Allah tufungulie Milango ya Hazina ya Rehma, na wala usituadhibu leo hapa Duniani wala kesho Akhera baada ya Rehma zako hizo. Ya Allah tujaalie vya halali na vilivyosafi katika riziki zako na rehma zako, na usitujaalie kua ni wenye kumhitaji yeyote yule zaidi yako ili tuweze kuonesha shukuran juu yako, Ya Allah tuongezee tuwe na Shukran kwa Rehma zako na chakula cha Halali ulichotujaalia, kwani kutokana na msaada wako tu ndio tunaweza kua huru kutokana na kuwategemea wengine zaidi yako.’

Imam Bakr Ibn Abd Allah anatuusia kwa kusema kua: **‘Enyi Ibn Adam, kuweni na matumaini juu ya Rehma za Mola wenu, ila matumaini hayo yasikupelekeeni kua ni wenye kua na uhakika juu yake, kwani uhakika huo unaweza kukupelekeeni kua ni wenye kumuasi Mola wenu na mkapata Adhabu zake juu yenu. Na muogopeni sana Mola wenu ila khofu hio isiwe ni yenye kukupelekeeni kupoteza**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

matumaini yenu juu yake, kwani vyovyote vile itakavyokua kuhusiana na dhambi zenu basi tumainieni usamehevu wa Mola wenu, na hivyo rudini kwake atakusameheni.'

Ibn Adam hawezi kua Mcha Mungu hadi pale atakapokua ni mwenye kuachana na Dunia yake na ni mwenye kuzidhibiti hasira zake.

'Bila ya kukinai ndani ya Dunia hii basi hakuna kitakachokutosheleza, iwe ni gao la Tende, Gilasi ya Maji, Kivuli cha Hema Jangwani na kadhalika, kwani Nafsi yako Daima hua ni yenye kutaka zaidi.'

'Mtu hua ni mwenye kupata heshima pale anapokua mnyenyekevu.'

'Fanyeni sana Istighfar kwa sababu katika siku ya Kiama Mtu hua na Furaha pale atakapoona Istighfar baada ya kila jambo kwenye kitabu chake.'

Imam Bakr Ibn Abd Allah: **'Kama mtu akialikwa kwenye sherehe, na kisha nae akaalika mtu mwengine kwenye sherehe hio, basi mtu huyo anastahiki kibao kimoja cha Uso. Kama mtu akialikwa nyumbani kwa mtu kisha akaambiwa kaa hapa nae akasema la, nitakaa hapa hapa basi mtu huyo aliealikwa anastahiki kupigwa vibao viwili vya uso. Na kama mtu amealikwa na kisha akakaribishwa Chakula kisha nae akamualika mwenyeji wake kua nae ale pamoja nae basi mtu huyo anastahiki vibao vitatu vya uso, kwa sababu katika matukio yote haya matatu, vitendo vyake mtu husika na maneno yake hua ni vya kijinga.'**

IMAM AMR IBN QAYS AL-MULAI

Imam Abu Abd Allah Amr Ibn Qays alikua ni mmoja kati ya Wanafiqh wakubwa watano wa Mji wa Kufa ambae pia alikua ni mfumaji na muuzaji vitambaa mzuri sana kama vile ambavyo alivyokua ni mwenye bidii kubwa sana wa kutafuta Ilm ya Dini yake na bila ya shaka aliipata kutokana na Jitihada zake.

Imam Amr Ibn Qays alisoma kwa Imam Abu Is-haq, Imam Ataa Ibn Abi Rabah, Imam Ikrimah, Imam Sufyan Ath Thawry na wengineo. Ambapo Wanazuoni wa Ilm ya Hadith wanasema kua Imam Amr Ibn Qays ni Imam anaeaminika na ni mwenye Ilm kubwa na hadith zake zinapatia kwenye *Sahih Muslim na Adab Al Mufrad.*

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake pia ni Mwalimu wake ambae ni Imam Sufyan Ath Thawry ambae anasema kua: '**Mwalimu wangu Imam Amr Ibn Qays**

alinifundisha na kunisomesha mie, Ilm ya Hadith, Ilm ya Qiraa, Ilm ya Faraidh, Ilm ya Mirathi na Ilm nyenginezo. Baadhi ya wakati nilikua nikienda Dukani kwake na kama sikumkuta hua naenda Nyumbani kwake ambapo hua namkuta anasali au anasoma Qur'an'.

Ilikua ni mtu alieachana na Dunia yake na kazi zake. Kwani kama ikiwa sikumkuta Nyumbani kwake basi ilikua naweza kumkuta msikitini huku akiwa analia, na nikimkosa Msikitini basi nampata Makaburini ambako ndio analia kwa sauti kubwa zaid.'

Hivyo Imam Amr Ibn Qays alikua pia na ilm kubwa ya Qiraa cha Qur'an ambacho alijifunza kutoka kwa Imam Asim. Imam Amr Ibn Qays alikua ni mtu mwenye Ucha Mungu, huruma na ukarimu mkubwa sana na alikua ni mwenye kuishi kama namna walivyokua wakiishi Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kufuata mfano bora wa maisha ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mwenyewe, kwani alikua ni mwenye kutoa sadaqa mali yake yote kwa masikini. Na alikua akiwaonea huruma zaidi wale walioghafilika na Akhera yao kwa kusema: '**Inasikitisha sana maisha ya watu hawa namna wanavyoishi kwani hawajui kile kinachowasubiri katika siku ya Malipo.**'

Imam Amr Ibn Qays alikua ni mtu mwenye kuifikiria sana Akhera yake na kumuogopa Mola wake kiasi ya kua alikua anaonekana kua na huzuni kwa mda mrefu zaidi, hivyo Siku moja mmoja kati ya Wanafunzi wake alimuona Imam Amr Ibn Qays akiwa analia hivyo akamuuliza: '**Ewe Imam Mbona unalia? Wakati umri wako wote umekua ukiutumia kutokana na kua na huzuni kubwa sana?**'

Imam Amr Ibn Qays akasema: '**La mimi siulilii umri wangu bali nalia kwa sababu ya kua na khofu ya kuja kunyimwa Rehma za Mola wangu katika siku ya Malipo.**'

Na kutokana na Unyenyekevu wake basi mbali ya kua ni Imam mwenye Ilm lakini ilikua anapokua mbele ya Mwenye Ilm zaidi yake basi hua ni mwenye kupiga magoti huku akisema: '**Nifundishe kile ambacho alichokufundisha *Allah Subhanah wa Ta'ala***'

Imam Amr Ibn Qays alisema kuwaambia Wanafunzi wake kua: **'Mnapokua mnajishughulisha na Nafsi zenu, basi hua mnasahau kuhusiana na Nafsi za wengine na mnapokua mnajishughulisha juu ya Nafsi za wengine basi hua mnasahau juu ya Nafsi zenu.'**

Na akasema tena kua: **'Msingi wa Unyenyekevu hua unasimamia kwenye mambo matatu. Kuwasalimia watu unaokutana nao kabla hawajakusalimia wao, kukubali kukaa katika sehemu isiyokua ya Darja ya Juu mnapokutana mbele za Watu na**

Kutopenda kusifiwa kutokana na mambo mema yaliyofanywa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'*

Imam Amr Ibn Qays aliusia kwa kusema pia kua: **'Unaposikia kuhusiana na Jambo jema basi litekeleze haraka sana'** na **'Kamwe usijichanganye na Watu waovu kwani uovu wao hukuathiri ndani ya Moyo wako.'**

Imam Amr Ibn Qays akasema kua: **'Yeyote yule anaepata faida kwa kuwasaidia chakula masikini kwa siku 20 na kisha akawa ni mwenye kufanya biashara ya magendo, basi hua hawezi kulipa fidia badala yake hata kam ataitoa mali yake yote kwa kuwapa masikini.'**

Imam Amr Ibn Qays alisema pia kua: **'Halali iko wazi na Haramu iko wazi na chenye kushabihiana kipo baina ya pande mbili hizo hivyo yeyote yule atakaeachana na vyenye kushabihiana basi atakua ameisalimisha Dini yake, hivyo anaeingia kwenye yenye kushabihiana hua ni mwenye kuingia kwenye Haram kirahisi. Kwani Mnyama mwenye kula majani Karibu na shimo basi hua ni mwenye kujihatarisha kutumbukia shimoni humo.'**

Imam Amr Ibn Qays alifariki mnamo mwaka wa 146 Al Hijra ambapo mji wa Kufa wote ulihuzunika na kuhudhuria maziko yake, na sala yake ya Jeneza ilisalishwa na Imam Abu Hayyan Al Tamimi ambapo wakati sala hio inaendelea basi ikasikika sauti ya mngurumo mkubwa uliosababishwa na kushuka kwa ndege weupe watupu waliokua hawakuwahi kuonekan hapo kabla kwenye eneo wakiwa wamejaa kwenye eneo hilo, hivyo watu wakashangazwa na tukio hilo na Imam Abu Hayyan Al Tamimi akasema: '**Mbona mnashangaa? Hao ni Malaika wamekuja kwa ajili ya kushuhudia wema wa Amr Ibn Qays**.'

Ambapo kwa upande mwengine basi kuna watu walioona pia watu waliokua wamevalinga nguo nyeupe tupu kwenye maziko hayo kama anavyosema Abd Allah Ibn Said Al Hafi kua: '**Mimi nilikuwepo kwenye maziko ya Amr Ibn Qays, na kulikua na watu wengi sana ambayo walikua wamevalia nguo nyeupe mazikoni hapo, na waliondoka baada ya Sala hio ya Maiti.**'

IMAM RABIAH AL RAY

Imam Rabiah Ibn Farrukh At Taimi Al Madani Al Ray alikua akijulikana pia kwa jina la Abu Sulayman na pia Rabiah Al Ray alikua ni mzaliwa wa Mji wa Madina na alisoma kwa Masahaba wakiwemo Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* na pia kwa Wanazuoni

waliofuatia baada ya Masahaba wakiwemo Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar, Imam Kharijah Ibn Zaid Ibn Thabit, Imam Sulaiman Ibn Yasar, Imam Qasim Ibn Muhammad Ibn Abi Bakr, Imam Urwah Ibn Zubayr, Imam Abd Allah Ibn Abd Allah Ibn Mas'ud, Imam Said Ibn Musayyab, Imam Ubaid Allah Ibn Abd Allah, Imam Al Qasim Ibn Muhammad, Salamah Ibn Dinar, Imam Hanzalah Ibn Qays na Imam Makhul Ash Shami.

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake wamo pia Imam Malik, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Al Awzai, Imam Sulayman Ibn Bilal, Imam Ismail Ibn Jafar n.k

Imam Rabiah Al Ray aliishi kipindi kimoja na Imam Abu Zinad, na Imam Rabiah Al Rai alipewa jina la Al Ray kwa sababu alikua ni Imam ambae alikua akipenda kutumia Rai na makisio katika Fiqh yake pale anapokua ni mwenye kukosa uthibitisho katika Vyanzo Vikuu vya Fiqh ambavyo ni Qura'n na Sunah.

Ambapo Ubayd Allah Ibn Umar anasema kua: **'Imam Rabiah Al Ray alikua ni mwenye uwezo mkubwa wa kutatua matatizo yetu yote tofauti kwani alikua ni Imam mwenye hikma zaid miongoni mwetu.**'

Ambapo anasema Majisun kua: '**Mimi sikuwahi kuona Mtu mwenye Ilm kubwa ya kuhifadhi Hadith kama Rabiah.'**

Anasema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua siku moja Imam Rabiah Al Ray alionekana akiwa analia, na alipoulizwa kwa nini analia basi alisema: **'Unafiq uliowazi wa wakati wetu na Matamanio ya Nafsi yaliyofichikana ndani yake, na watu kwa wanazuoni wao wamekua kama watoto kwenye mapaja ya Mama zao, yaani kama wakiwaamrisha basi hua ni wenye kutii na wakiwakataza basi hua ni wenye kuachana na waliyokatazwa.'**

Ambapo anasema Al Uwaisi kua: '**Rabiah alikua akimwambia Ibn Shihab kua: 'Hali yangu sio sawa na yako'** ambapo nae akauliza : **'Kwanini unasema hivyo?' Imam Rabiah akasema : 'Kwa sababu mimi hua ni mwenye kudhihirisha mtizamo kwa yeyote yule mwenye kuutaka na pia kwa yule anaetaka kuachana nao, na wewe hua unazungumzia kuhusiana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tu.'**

Abu Damra nae anasema kua: **'Rabiah alikutana na watu ambao walikua wanazungumzia kuhusiana na Qadar, na hivyo akasema: 'Kama kweli nyinyi ni wenye kuamini basi kua Qadar maana yake ni kua kile kilichomo ndani ya mikono yenu ni kikubwa zaidi kuliko kile kilichomo kwenye mikono ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* yaani kama wema na uovu vimo chini ya mikono yenu'.**

Ambapo Ahmad Ibn Abd Allah Al Ajli basi yeye anasema kua: **'Baba yangu alisema kua: 'Rabiah amesema kua, aliulizwa yeye kuhusiana na namna anavyotumia Qiyas katika hali tofauti ambapo nae akasema: 'Qiyas hua hakina maana bila ya kumgusia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na bila ya sisi kua ni wenye kuamini.''**

Imam Rabiah Al Ray alisema kua: **'Ilm ndio njia ya kupitia katika kila Jambo'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Malik basi anasema kua: **'Rabiah alienda kwa *Amir ul Muuminin* na kisha akapewa Mtumwa wa kike, lakini nae akamkataa, na hivyo *Amirul Muuminin* akampa Rabiah 50000 Dinar ili akanunue mwenyewe Mtumwa mwengine, na pia akampa Mtumwa huyo lakini pia alikataa'**

Imam Al Layth anasema kua: '**Amesema Yahya Ibn Said kua: 'Hakika mimi sijawahi kuona mtu mwenye ufahamu zaidi kama Rabiah''**

Muadh Ibn Muadh alisema kua: '**Alisema Siwar Ibn Abd Allah Ibn Anbari kua: 'Hakika mimi sijawahi kumuona mtu mwenye Ilm zaidi ya Rabiah' hivyo mimi nikamuuliza: 'Hata Hasan Al Basr na Muhamamd Ibn Sirrin?' nae akasema: 'Naam, hata Al Hasan na Ibn Sirrin''**
Anasema Abdu al Azizi Ibn Salamah kua: '**Mimi nilienda Iraq, na watu wa Iraq wakanifuata na kuniuliza: 'Hebu tuelezee kuhusiana na Rabiah Al Rai' nami nikasema: 'Enyi watu wa Iraq, hakika nyinyi mnamuulizia Rabia Al Rai lakini *Wallahi* mimi sijawahi kumuona mtu yeyote yule aliehifadhi Ilm kubwa kama yeye kwa mbele ya mwaka zaidi''**

Abd Al Aziz Ibn Al Majshon akasema kua: '***Wa Allahi* mimi sijawahi kumuona Mtu ambae yuko mbele kimtizamo zaidi ya mwaka kama Rabiah.**' Ambapo na Malik alisema kua: '**Rabia alikua ni mwenye kua na Majibu ya hapo kwa hapo katika kutoa Fatwa'**

Ambapo Ibn Wahb anasema kua: '**Amesema Abd Rahman Ibn Zayd kua: 'Rabiah alikua ni Mwanazuoni wa Fiqh anaeaminika na hakukua na Mtu aliekua Mkarimu katika Mji wa Madina kama yeye kutokana na kile kilichomo mikono mwake, alikua akifuatwa na watu, japokua yeye alikua hawafuati watu isipokua kwa yule ambae ni mwenye kupenda kujumuika pamoja nae.''**

Kwani Imam Rabiah Al Ray mwenyewe alikua akisema kua: **'Mtu mwenye kutoa sehemu ndogo ya Msaada hua ni bora kuliko yule mwenye kuiuza Ilm yake.'**

Anasema Ahmad Ibn Amran kua: **'Nimemsikia Abu Bakr Ibn Ayyash akisema kua: 'Mimi niliingia Msikitini na nikamuona Rabia akiwa amekaa kitako, na kuna**

vijana wamekaa mbele yake wakimuangalia na kumsikiliza, hivyo mimi nikamuuliza: 'Jee umenukuu kutoka kwa Anas?' nae akasema: 'Hadith mbili tu' Abu Bakr Al Khatib akasema: 'Yule alikua ni Rabia Al Faqih, Mwanazuoni, Al Hafidh na Mwanahadith.''

Anasema Imam Malik kua: '**Az Zuhri alikuja kwa Rabiah na akauchukua mkono wake kisha wakaingia ndani na hawakutoka tena hadi mchana wake, na kisha Ibn Shihab Az Zuhri akatoka na kusema: 'Sifikirii kua katika Mji wa Madina kuna Mtu kama Rabiah.''**

Imam Rabiah Al Ray alifariki mnamo mwaka 136 Al Hijra ambapo alisema Mutarrif kua Imam Malik alisema kua: **'Utamu wa Ladha nzuri ya Fiqh ulitoweka baada ya kufariki Rabiah'** nami nikasema: '**Rabiah alikua ni Chombo cha Ilm na alikua ni mwenye kuaminika sana.'**

IMAM ABU ZUR BILAL BIN SA'D

Imam Abu Zur Abu Amr Bilal Ibn Sad Ibn Tamim Al Ashari Al Dimashaq alizaliwa katika mji wa Dimashq katika kipindi cha Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwani baba yake ni Sahaba Said Ibn Tamim *Radhi Allahu Anhu.*

Hivyo Imam Abu Amr Bilal Ibn Sad alisoma Ilm ya Dini ya Kiislam kutoka kwa Baba yake laikini pia alisoma kwa Masahaba wengineo wakiwemo kina Bilal Ibn Rabbah *Radhi Allahu Anhu*, Muawwiyah Ibn Abu Sufyan *Radhi Allahu Anhu,* Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*. Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu na wengineo.*

Ambapo kwa upande wa Wanafunzi wake basi ndani yake tunakutana na Imam Al Awzai, Imam At Ibn Abi Rabbah, Said Ibn Abd Al Aziz na wengineo kwani kwa upande maeneo ya ardhi ya Syria basi ilikua hakuna mwenye Ilm kama Imam Abu Zur na hivyo Wanazuoni wanasema kua: **'Bila Ibn Sad Kwa Dimashq ni sawa na Hasan Al Basr kwa Basra.'**

Imam Abu Zur ni mwenye kuifafanua ile aya isemayo:

﴿يٰعِبَادِىَ ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ إِنَّ أَرْضِى وَاسِعَةٌ فَإِيَّاىَ فَٱعْبُدُونِ﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ya AAibadiya alladheena amanoo inna ardhee wasiAAatun fa-iyyaya faoAAbudooni *(Surat Al Anqabut 29:56)*

Tafsir: ***Enyi Waja wangu ambao mlioamini hakika ardhi yangu ni pana sana hivyo niambuduni mie tu.***

Kua inamaanisha kua: '**Kama ukiona kua umejibana au umebanwa kwa mitihani katika sehemu uliyokuwepo basi nenda katika sehemu nyengine kwani kwa hakika Ardhi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni pana sana'**

Alisema Imam Abu Zur kua: '**Ni kua na kiburi kwa Muislam kukumbuka amali zake njema na kusahau kuhusiana na Dhambi zake, kwani ni muhimu kwa Muislam kukumbuka Dhambi zake hata ziwe na udogo gani, kutokana na kua dhambi hizo amezimefanya mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala'***
Na akausia tena kwa kusema: ***'Allah Subhanah wa Ta'ala*** **anatuamrisha kua na umakini katika kutoangukia kwenye yaliyo ya haramu na yenye kushabihiana na pia kuachana na mengi mbali ya kua ni yaliyohalalishwa, lakini sisi kwa upande wetu tumekua ni wenye kupenda zaidi Dunia na kuikumbatia, ambapo jambo hili limekua kama ni kosa lenye kututosheleza sisi.'**

Imam Abu Zur alikua ni mtu Mcha Mungu sana kiasi ya kua Dua zake zilikua zikijibiwa hapo hapo kwani mwaka mmoja ilikua kuna ukame mkubwa sana katika maeneo ya Ardhi ya Sham, hivyo akatoka na kuenda kusali Sala ya kuomba Mvua pamoja na watu wengine na alipofika basi akasema: **'Enyi watu hakika nyinyi nyote ni wenye dhambi nyingi sana, hivi jee mnakubali kua mna dhambi nyingi sana?'** watu wakaitikia na kusema: '**Naam, hakika sisi tunakubali kua ni wenye Dhambi nyingi sana na tunatubu kwa makosa yetu.'**

Kisha Imam Abu Zur akanyanyua mikono yae na kuomba Dua kwa kusema: **'Ya Allah, Hakika wewe umeahidi kwenye Qur'an kua: 'Hakika mimi nnakubali maombi ya wale wenye kutubu na kusema kweli' nasi tukubali kua tuna madhambi mengi sana na tunatubu hivyo tusamehe na tujaalie kupata neema ya Mvua'** ambapo haikuchukua mda baada ya hapo na mvua ikaanza kunyesha.

Siku moja Mtoto wake Imam Abu Zur alifariki Dunia kwa kuupata ushahidi katika mapigano ya Jihad, hivyo akaja mtu mmoja na kusema kua: '**Hakika mimi namdai Mtoto wako Dinari 20'** Imam Abu Zur akamuuliza Mtu huyo kwa kusema: '**Jee unae shahidi juu ya hili au mliandikiana?**' Mtu huyo akasema: '**La sina Shahidi wala hatujaandikiana'** Imam Abu Zur akauliza: **'Jee Unaweza kuapa juu ya hilo?'** Mtu huyo akasema: **'Naam, bila ya shaka.'**

Hivyo Imam Abu Zur akampa mtu huyo Dinari hizo 20 bila ya kumuapisha,na kisha kasema: '**Kama unasema kweli basi itakua nimelipa Deni la Mtoto wangu, na kama unasema uongo basi itakua nimetoa Sadaqa'**

Imam Abu Zur alikua akisema: **'Kama ikiwa Dhambi imefanywa kwa siri basi madhara hua ni kwa yule aliefanya Dhambi tu, lakini kama ikiwa imefanywa hadharani basi madhara yake hua ni kwa kila mtu alieona'**

'Ndugu anaekukumbusha kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kukuamrisha mema na kukushauri juu ya mema basi ni bora kuliko yule rafiki atakae kua anakupa Dhahabu, hivyo ukikutana na mtu kama huyu basi mwambie: 'Ewe ndugu yangu kama ukiona na kasoro yeyote basi usinifiche nijuulishe ili nipate kuirekebisha''

Akasema tena Imam Abu Zur kua: **'Ibada za Watu watatu hazikubaliwa, watu hawa ni Mshirikina, Kafiri na Rai.'** Imam Abu Zur akaulizwa: **'Jee Rai ndio ndani?' ambapo nae akasema: 'Rayi ni yule mtu ambae anaefuata rai za mtizamo wake na kuachana na mtizamo na hukmu za Dini ya Kiislam.'**

'Mtu akisifiwa Nafsi yake na kisha akahesabu kua sifa hizo sio nzuri kwake yeye, basi hua ni bora kuliko akisifiwa na kisha akafurahia sifa hizo kwani hua ni mwenye kula hasara.'

'Ukimuona mtu anabishana sana na kupingana, na kua ni mwenye kupenda kusisitiza mitizamo yake tu, basi fahamu kua ubishi wake umemkamilia.'

'*Allah Subhanah wa Ta'ala* hamuachii Mtu ambae ni Muumini bila ya kuangalia amali zake, kua anapofanya Amali hizo hua ni mwenye kuachana yenye shaka ama la, na kisha huangalia nia yake, kama nia yake ni safi basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* humrekebishia makosa yake Muumini huyo.'

Imam Abu Zur alimuuliza mmoja kati ya Wanafunzi wake kwa kusema **'Hivi Jee unataka kufariki sasa hivi ama la?'** ambapo Mwanafunzi huyo akajibu: **'La Nataka niendelee kuishi ili nipate kufanya Mema zaidi na kisha ndio nifariki'** Imam Abu Zur akasema: **'Kama hali ni hiyo basi fahamu kua wewe ni miongoni mwa wanaoiendekeza Dunia yao.'**

Imam Abu Zur alisema: **'Enyi watu, Mche *Allah Subhanah wa Ta'ala*, kwani hakuna wa kukunusurini isipokua yeye katika siku ya Malipo, ambapo hesabu ya kila mtu itakua wazi, ambapo mara baada ya watu wa Peponi kupelekwa Peponi na watu wa Motoni kuingizwa Motoni, basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataamrisha kua**

watolewe watu wawili ndani ya Moto ambao atawauliza: 'Jee ni ipi hali yenu kwenye Moto?'

Ambapo nao watu hao watasema: 'Ewe Mola wetu hakuna sehemu yenye hali ngumu na mbaya kama sehemu yetu' ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **atawaambia watu hao: 'Hii ni kutokana na kile mlicho kichuma, kwani kwa hakika mimi sijawahi kumdhulumu yeyote, haya rudini katika sehemu zenu.''**

Ambapo mmoja kati ya Watu hao atarudi kuwa kukimbia mbio, na mwenzake atarudia kwa hatua za kawaida na kisha atasimama na kuangalia nyuma. Kisha ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **ataamrisha kua watu hao warudishwe tena mbele yake. Na watakapofikishwa mbele yake basi atamuuliza yule aliekua akikimbia mbio: 'Hivi kwanini wewe ukawa ni mwenye kukimbilia mbio?'**

Ambapo yule aliekua kaikimbilia mbio Motoni atasema: 'Ya Allah hakika wewe ni mwenye kujua zaidi, kua mimi nastahiki kua Motoni kutokana na niliyokua nikiyafanya Duniani kwa kutotii maamrisho yako, hivyo hapa ulipoamrisha kua turudi kwenye sehemu zetu mimi nikaona nikimbilie kwenye sehemu yangu ili nisiwe ni miongoni mwa wenye kutotii amri zako hata hapa mbele yako.'

Na kisha ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **atamuuliza yule alieondoka taratibu na kisha akaangalia Nyuma : 'Na wewe kwanini uliondoka taratibu na kisha ukasimama na kuangalia nyuma?'**

Ambapo nae atasema: 'Ya Allah hakika wewe ni mwenye kujua kila kitu zaidi, kwani kwa hakika mimi niliondoka taratibu na kisha nikaangalia nyuma kwa sababu nilidhania kua ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **hatomrudisha yule mwenzangu kwenye Moto baada ya kumtoa ndani yake, hivyo nilikua naangalia nyuma kuangalia nipate kujua kua labda huenda ukawa ni mwenye kumwita.'**

Hivyo ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **atasema kuwaambia Malaika wake: 'Hakika mimi niko kama anavyonifikiria Mja wangu, hivyo wachukueni waja wangu wawili hawa na kisha waingizeni Peponi.' Na kisha watu wawili hao wataingizwa Peponi.**

Imam Abu Zur alikua ni mwenye kusali Tahajjud kwa Rakaa 1000 kila sikua Usiku na kwani alikua akisema kua: '**Ewe Ibn Adam fahamu kua kila siku usiku unapoenda kulala basi kifo hua kinakusubiri chini ya Mto wako, na unapoamka basi fahamu kua kifo kiko mbele yako na huenda ukafa ndani ya siku hio iliyo mbele yako'**

Imam Abu Zur alifariki mnamo mwaka 120 Al Hijra.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM MAYMUN IBN MIHRAN 40 AH

Imam Abu Ayub Maymun Ibn Mihran alizaliwa mnamo mwaka 40 Al Hijr katika ardhi ya Kufah nchini Iraq kutoka katika familia ya Watumwa waliotekwa katika maeneo ya Istakhar, na kununuliwa na watu wa kabila la Hawazin, ambapo baadae Imam Maymun Ibn Mihran akaachiwa huru.

Imam Mymun Ibn Mihran alipopata uhuru wake akawa ni mtu mwenye kujitafutia Ilm ya Dini ya Kiislam ambapo alifanikiwa kua ni mwenye kusoma kutoka kwa Masahaba wakiwemo Abu Hurayrah, Aisha, Abd Allah Ibn Abbas, Abd Allah Ibn Umar, Ummu Darda *Radhi Allahu Anhum*, na waliofuatia baada yao wakiwemo Imam Ad Dahhak, Umar Ibn Abd Ul Aziz, Nafii, Amr Ibn Uthman, Yazid Ibn Al Asam na wengineo.

Ambapo kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi yeye anasema kua: '**Maymun Ibn Mihran ni muaminifu kuliko Ikrimah**'

.

Na anasema Said Ib Abd Ul Azizi kua: '**Amesema Sulayman Ibn Musa kua: 'Kuna watu wanne ambao walikua ni Wanazuoni katika wakati wa Hisham Ibn Abd Ul Malik ambao ni Makhul, Hasan Al Basr, Al Zuhri na Maymun Ibn Mihran.**''

Na Abu Al Malih Al Raqqi amesema kuhusiana nae kua: **'Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu mwenye Ilm kama Maymun Ibn Mihran.**'

Imam Maymun Ibn Mihran alikua ni Mcha Mungu sana kiasi ya kua alipochaguliwa kufanya kazi kwa Umar Ibn Abd Al Aziz basi alisema: '**Hakika mimi nnatamani kua Vidole vyangu vingekatika na hivyo ikawa siwezi kufanya kazi kwa Umar Ibn Abd Ul Aziz.**'

Na pia alisema Habib Ibn Marzuk kua: '**Maymun alisema kua: 'Natamani kua moja kati ya Macho yangu halioni na hivyo kua si mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa Umar Ibn Abd Ul Aziz.**''

Harun Al Barbari anasema kua: '**Maymun Ibn Mihran alimuandikia barua Umar Ibn Abd Ul Aziz kwa kumwambia: 'Hakika mimi Mtu mzima halafu wewe umenipa jukumu la kutoa hukumu baina ya Watu, na kusimamia Zakkah na Mahkama kwa watu wa Jazira'**

Umar Ibn Abd Ul Azizi akajibu: **'Hakika mimi sikukuteua wewe juu ya kile usichokiweza, hivyo simamia Zakkah kutokana na kile kilichokua wazi kwako ama juu ya kile kisichokua wazi kwako basi niletee kwangu mie, kwani watu wakiwa wazee na kisha wakaachana na wanavyoviacha basi haitakua Madeni wala Dunia itakayobakia''**

Na amesema Imam Maymun Ibn Mihran kua: '**Ibn Adam hawezi kua Mcha Mungu hadi pale atakapokua ni mwenye kujihesabia Nafsi yake zaidi ya anavyojihesabia nafsi ya mwenzake na pale atakapojua uhalali wa chakula chake, kinywaji chake na mavazi yake.**'

Abu Al Malih anasema kua: '**Kuna Mtu alimwambia Maymun kua: 'Ewe Abu Ayyub, Watu hawana tatizo pale inapokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawaweka mbali nawe, Ambapo Maymun akasema: 'Nakubaliana nawe kua Watu hua hawana matatizo pale inapokua ni wenye Kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**''

Amesema Imam Maymun kua: '**Yeyote yule anaefanya dhambi kwa siri basi na aombe msamaha kwa Mola wake kwa siri, na yeyote anaefanya Dhambi hadharani basi na aombe msamaha hadharani, kwani watu hulaumu lakini hua hawasamehe wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* halaumu lakini ni mwenye kusamehe.'**

Na akasema tena Imam Maymun Ibn Mihran: '**Inakuaje Mtu anaenda kwenye Nyumba za wenye Mamlaka ambazo zimezibwa na Geti Kubwa la Mlango yao badala ya kuenda kwenye Nyumba ya Mwingi wa Rehma ambae Milango yake iko wazi, hivyo mwache asali Rakaa mbili na kumuomba kile akitakacho.'**

Abu Malih anasema kua: '**Mimi nimemsikia Maymun akisema kua: 'Kupewa jukumu la kusimamia Mali kwangu mie ni bora zaidi kuliko kuambiwa kua nimsimamie Mwanamke.**''

Imam Maymun Ibn Mihran aliusia kwa kusema kua: '**Hakuna Mtu ambae ni mwenye kupanda Darja ya kufanya mema isipokua ni mwenye kua na wingi wa Subra.**'

Imam Maymun Ibn Mihran anasema kuhusiana na *Takbirat Ihram:* '**Hakika mimi nakumbuka wakati watu walipokua wakifanya Takbira katika Masiku 10 ya *Dhul Hijjah* mpaka ilikua ni mwenye kuifananisha na Mawimbi ya Bahari.**'

Na akasema tena kua: '**Kuchangia kwangu mie Dirham moja wakati nikiwa hai ni bora kuliko kuchangishiwa Dirham 1000 baada ya kufariki kwangu.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Maymun Ibn Mihran alisema pia kua: '**Jihadhari na kubishana na Mwenye Ilm kuhusiana na Dini na pia kubishana na Mjinga kuhusiana na Dini, Kwani Mwenye Ilm ataizuia Ilm yake na hatojali utakayofanya kwa ujinga wako, ama kuhusiana na Mjinga basi atakusababishia magharibi ya Moyo wako na kisha pia hatoufuata mtizamo wako.**'

Alisema tena Imam Maymun Ibn Mihran kua: '**Hakika mimi nimekutana na watu ambao ni wenye kuona haya hata kuzungumza, na nimekutana na watu wasiosema kitu chochote isipokua ukweli tu badala yake au kukaa kimya, na pia nimekutana na watu ambao hata macho yao hayajawahi kuangalia vizuri juu Mbinguni kutokana na kua na Taqwa juu ya Mola wao.** '

Imam Maymun Ibn Mihran alisema kua: '**Mambo Matatu yanatakiwa yapewe kwa Waja wema na kwa waja waovu: 'Udugu Lazima uunganishwe, iwe kwa Mtu mwema au Muovu, Amana lazima irudishwe iwe kwa Mtu mwema au Muovu na Ahadi lazima Itimizwe iwe kwa Mtu Mwema au Muovu.**'

Kuna mtu alienda kuposa kwa Imam Maymun Ibn Mihran lakini Imam Maymun akamwambia: **'Hakufai Siwezi kukuozesha'** yule mtu akauliza: **'Kwanini?**' Imam Maymun Ibn Mihran akasema: **'Kwa sababu Binti yangu anapenda mapambo ya Dhahabu na Nguo nzuri'** yule Mposaji akasema: '**Hamna tatizo kwani mimi nnavyo vyote kwa kadiri ya atakavyohitaji'** Imam Maymun Ibn Mihran akasema: '**Sasa hivi wewe ndie humfai Binti wangu'**

Imam Maymun Ibn Mihran alisema pia kua: **'Hakika Mambo rahisi katika kufunga ni kujizuia Kula na Kunywa.'**

Imam Maymun Ibn Mihran anasema kua: **'Mimi nilikua nimekaa na Hasan Ibn Ali *Radhi Allahu Anhu*, ambapo mara akaja mtu ambae alimwambia kwa kusema: 'Ewe Mjukuu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kwa hakika fulani ananidai na anataka kunikamata'**

Hivyo Hasan Ibn Ali *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Wa Allahi hakika mimi sina uwezo wa kukulipia Deni lako.' Hivyo yule mtu akasema: 'Jaribu kuzungumza nae' hivyo nae akanyanyuka na kuchukua viatu vyake, nami nikamwambia Al Hasan: 'Ewe Mjukuu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, hivi jee umesahau kua wewe umenuia kukaa *Itikaf?*'

Ambapo Hasan Ibn Ali *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'La Sijasahu, lakini nimesikia Baba yangu akisema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua: 'Yeyote yule atakaemsaidia shida yake Muislam mwenzake basi Mtu huyo hua ni

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

sana na aliemuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa mda wa miaka 9000, kufunga katika wakati wa Mchana na kusimama *Qiyam Al Layl* wakati wa usiku.''

Siku moja Imam Maymun Ibn Mihran anasema kua : '**Siku moja kuna Mtu alikua akisoma Qur'an mbele ya Salman Al Farisi *Radhi Allahu Anhu* na hivyo kufikia katika aya isemayo**:

﴿وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمَوْعِدُهُمْ أَجْمَعِينَ﴾

Wa-inna jahannama lamawAAiduhum ajmaAAeena *(Surat Al Hijr 15:43)*

Tafsir: ***Na kwa Hakika Jahannam ni sehemu waliyoahidiwa wote kwa pamoja.***

Ambapo hapo hapo Salman Al Farisi *Radhi Allah Anhu* akaanza kulia na kukishika kichwachake, na kuondoka kutoka katika sehemu hio huku akiwa katika hali ya mtu aliechanganyikiwa bila ya kujua anaelekea wapi, kiasi ya kua Salam Al Farisi *Radhi Allahu Anhu* hakuweza kuoekana tena hadi katika siku ya tatu.

Siku moja Imam Maymun Ibn Mihran alikua ametoka nje na kutembea pamoja na *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Abd Ul Aziz, na wakafika kwenye Makaburi, baada ya kufika katika eneo hilo, basi *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Abd Ul Aziz akaanza kulia na kusema: **'Wa Allahi mimi sijui ni yupi kati ya Watu hawa waliopo ndani ya Makaburi haya kua ni mwenye bahati kubwa sana na yupi miongoni mwao si mwenye bahati kati yao.'**

Imam Maymun Ibn Mihran aliulizwa: **'Hivi kwa nini wewe na marafiki zako hua si watu wenye kugombana, inakuaje?'** ambapo nae akasema: **'Kwa sababu mimi sina madhara wala uadui kwa marafiki zangu, na hivyo si mtu wa kubishana nao wala kugombana nao'**

Anasema Imam Maymun Ibn Mihran kua: **'Siku moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitembea na akaona sehemu ya kumwagia Taka ambapo ndani yake kuna vitambaa vilivyooza na Mifupa na kadhalika, hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Njoo Duniani, Uiangalie Dunia, kwani hii ndio Dunia na hivyo ndivyo itakavyokua Mwisho wake.''**

Imam Maymun Ibn Mihran anasema kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Watu watakaoadhibiwa sana katika Siku ya Malipo ni wale wenye**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kuwalaani Mitume, na kisha wale wenye kuwalaani Masahaba zangu na kisha wale wenye kuwalaani Waislam.'

Imam Maymun Ibn Mihran anasema kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Hakuna Tiba ya mtu mwenye Ujinga wa kutoridhika na Majaaliwa ya Mola wake Juu yake.**

Imam Maymun Ibn Mihran anasema kua: **'Kuna aina mbili za watu wakiharbika basi watawaharibu watu wote na wakiokoka basi watawaokoa watu wote, watu hao ni Wanazuoni na Sultani.'**

Imam Maymun Ibn Mihran anasema kua: **'Kama kuna Mtu ambae ni mwenye wivu juu ya Mambo yako, nawe unakata kujilinda kutokana nae, basi fanya mambo yako kwa siri kutokana nae.'**

Imam Maymun Ibn Mihran anasema kua: **'Mtu anaewapa Chakula wageni wake, bila ya kuwapa kitafunio baada ya Kula kwao wakati uwezo huo anao basi hua ni sawa na Mtu aliesali Qiyam Al Layl bila ya Kusali Witr baada yake.'**

Imam Maymun Ibn Mihran anasema kua: **'Mtu anaweza akawa ni mwenye kusali na kisha akawa ni mwenye kujilaani yeye mwenyewe kwa Nafsi yake'** Hivyo akaulizwa: **'Inakuaje hali hio?'** ambapo nae akasoma aya ifuatayo:

﴿أَلَا لَعۡنَةُ ٱللَّهِ عَلَى ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

Ala laAAnatu Allahi AAala aldhdhalimeena *(Surat Hud 11:18)*

*Tafsir: **'Bila ya shaka, Laana ya Allah ipo juu ya wenye kujidhulumu.'***

Kisha akasema: **'Kuna baaadhi ya Watu hua ni wenye Kusali na kisha hujidhulumu kwa kufanya baadhi ya Dhambi, kwa kuchukua Mali za watu bila ridhaa za wenye Mali, au Ruhusa na kutosimamia haki zao, na hivyo hua n mwenye kuwadhulumu wengine, na hivyo hua ni mwenye kujidhulumu.'**

Imam Maymun Ibn Mihran Al Jazari alifariki mnamo mwaka 116 Al Hijra.

IMAM MALIK IBN DINAR 41 AH

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Malik Ibn Dinar basi tunamzungumzia Imam Ambae alizaliwa katika Mji wa Basra kwenye Familia ya Imam Abu Yahya.

Ambapo tunapomzungumzia Imam Abu Yahya basi hua tunamzungumzia Imam wa Hadith wa Mji wa Basra na ni Mtu mwenye Taqwa ambae alikua ameihifadhi Qur'an kwa Moyo wake kiasi ya kua moja kati ya kazi yake ilikua ni Kuandika Misahafu na Kuiuza katika Mji wa Basra.

Imam Abu Yahya alikua ni mwenye Kujipatia Riziki yake kwa njia bora na ya Halali kabisa ya Kuuza Misahafu hio Imam Abu Yahya ndie aliekua Baba ya Imam Malik Ibn Dinar Abu Yahya Al Basr.

Hivyo haishangazi kuona namna alivyokua na Ucha Mungu Imam huyu Malik Ibn Dinar kwani alikua ni kopi ya Baba yake ambapo yeye alikua amemzidi Baba yake kwa Ucha Mungu zaidi.

Ambapo alisema Imam Malik Ibn Dinar kua: ‘**Kama Wanafiq Wangekua na Mikia basi ingekua haiwezekani kutembea Barabani kwa wingi wa mikia hio’**
Kwani alisema Imam Malik Ibn Dinar kua: ‘**Hakika mimi nimechunguza Dhambi Nyingi sana na nimegundua kua chanzo chake ni Mali.’**

Na akasema tena: ‘**Tangu nianze kuwafahamu watu basi nimekua si mwenye kufurahishwa kutokana na kunisifu kwao na wala sichukii kutokana na Kunitoa kasoro kwao, kwani yule anaekusifu hua ni mwenye kuongeza chumvi kama afanyavyo yule anaekutoa kasoro.’**

Kwani katika wakati wa kipindi chake Imam Malik Ibn Dinar basi Mji wa Basra alikua ni kawaida kama ilivyo sasa kwetu kua Nyumba zinafungwa Milango na watu wakiondoka basi hutia Kufuli.

Lakini Nyumba ya Imam Malik Ibn Dinar kamwe haikuwahi kufungwa Mlango wake, kwani alitangazia kua: **‘Mtu yeyote yule atakaeingia kwenye Nyumba yake na Kuchukua kitu Chochote ndani yake basi kitu hicho hua ni Sadaka yake na ni halali yake mtu huyo aliechukua, hivyo yeye hahijati Kufuli wala Ufunguo wala kufunga Mlango wangu’**

Naam..siku Moja Imam Malik Ibn Dinar alikua amekaa Barazani mara akapita Gavana wa Basr akiwa na Walinzi wake huku akitembea kwa kujiona, basi Imam Malik Ibn Dinar akamnadia Gavana huyo kwa Kumwambia: ‘**Regeza Mdundo wa Mwendo wako ewe Kijana’**

Hapo hapo Walinzi wa Gavana huyo wakamkamata Imam Malik Ibn Dinar, na kisha Gavana akamuuliza Imam Malik Ibn Dinar: ‘**Hivi wewe Unanjijua Mimi ni nani?’**

Imam Malik Ibn Dinar akasema: ‘**Kwanini nisikujue wakati wewe mwanzo wako Ulikua ni Tone chafu la Manii na Mwisho wako ni Maiti inayonuka na kutoka Mafunza, kutokana na kua sasa hivi umebeba Uchafu ndani ya Tumbo lako’**

Gavana huyo akatafakar kisha akasema: ‘**Mwachieni Twende zetuni!’**

Imam Malik Ibn Dinar ambapo tumeona kua kutokana na Ucha Mungu wake basi hakua ni mwenye kumuogopa Mtu yeyote wala kitu chochote. Kwani yeye alikua ni mwenye Kumuogopa Mola wake tu basi.

Kwani Imam Malik Ibn Dinar kutokana na Ucha Mungu wake basi hata chakula chake alikua akijilinda sana, kiasi ya kua alikua anakimbia kufanya Israfu katika chakula, na hivyo alikua akifunga na katika siku asizofunga alikua anakula Vipande viwili tu vya Mkate, kimoja ni Asubuhi na cha Pili Jioni.

Imam Malik Ibn Dinar alikua ni Mtu ambae alikua hali Nyama Mwaka Mzima kwani alikua akisema: ‘**Hakika mimi sipendi kula Nyama na sili Nyama mwaka mzima isipokua katika siku ya *Idd Al Adhha,* na hii ni kwa sababu katika siku ya *Idd Al Adha* hua ni Sunna kula Nyama’**

Subhana Allah! Hivi Wangapi wanajua kua katika Siku ya *Idd Al Adhha* ni Sunnah kula Nyama?

Kwani Kutokana na kutokujua kwetu basi ndio maana akasema Imam Malik Ibn Dinar kua: **‘Watu wanao iendekeza Dunia hua ni wenye kuondoka Duniani bila ya kuonja ladha ya kitu bora zaidi ya vyote**’

Imam Malik Ibn Dinar alipoulizwa: **‘Ni kitu gani hicho?’**

Basi Imam Malik Ibn Dinar akasema: ‘**Kuhisi kuwepo kwa Muumba’**

Hivyo jee tunajua kua Ibn Adam unapohisi kuwepo kwa Muumba basi ndipo Unapojua Dhumuni la kuumbwa kwako na Maslahi yaliyokuwemo katika yale Maamrisho ya Mola wako juu yako? Na Madhara yaliyomo kwenye Makatazo aliyoyakataza Mola wako juu yako? Hivyo basi katika Kuchinja kwa ajili ya Mola wako hua kuna kupata Thawabu za kutekeleza Amrisho la *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na katika Kugawa Nyama kuna Thawabu za kutoa Sadaka na Katika Kula Nyama hua kuna Thawabu za kutekeleza Sunna ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Sunna ya Nabii Ibrahim *Alayhi Salam* na hivyo kua ni mwenye kudumisha Milat Ibrahim.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na Hio ndio Raha ya Uislam kwani katika kila kitu utakachofanya kwa kuanza na *Biismi Allah* yaani Kwa Ajili ya Jina la Allah ambae ni Mola wako hua tayari unadhihirisha kuwepo kwa Muumba na unalipwa Thawabu zako Imam Malik Ibn Dinar ambae alikua akiishi katika Mji wa Basra ambae alikua ni Mtu mwenye kupenda Kusali Sala ya Tahajjud na hivyo kabla ya hata kutia nia ya Sala yake hio basi kwanza alikua akipenda kuzikamata Ndevu zake huku akisema: '**Ya Allah, Nakuomba Umsitiri Na Moto huyu Mzee Malik Ibn Dinar katika siku ambayo utakayo wakusanya watu wa Mwanzo na wa Mwisho kuishi Ulimwenguni'**

Imam Malik Ibn Dinar alisema kua: '**Wakati Ibn Adam anapofanikiwa Kuyateka Nyara Matamanio ya Nafsi yake, basi hata Shaytan hua ni mwenye Kuogopa hadi Kivuli cha Ibn Adam huyo.'**

Na kutokana na Ucha Mungu wake basi Imam Malik Ibn Dinar alikua ni Mtu mwenye Subra kubwa sana kiasi ya siku Moja alinadiwa mbele za watu na Mwanamke mmoja wa Basra kwa kusema: '**Mnafik Mkubwa wewe!'**

Imam Malik Ibn Dinar akamtabasamlia Mwanamke huyo na kisha akasema: '***Ma-shaa Allah* hakika wewe Umenipatia Mimi Jina Ambalo Watu wote Wa Mji wa Basra Wameshindwa Kuliona!'**

Kwani katika kujihesabia Nafsi yake basi Imam Malik Ibn Dinar alikua hafanyi kitu bila ya kukaa na kufikiria kwanza kwanini anataka kufanya kitu hicho na kujiuliza Nafsi yake kwa kusema: '**Ewe Malik Kwanini unataka kufanya kila unachokitamani? Hivi jee kweli wewe unataka kupanda kila kipando cha hapa Duniani? Hii ni Tabia Mbaya ewe Malik Ibn Dinar'**

Ambapo ingawa tunapoyaangalia haya basi kwa leo hii wengi wetu wanayaona kua hayaingii akilini lakini hivi ndivyo walivyokua wenye Kumuogopa Mola wao, kwani hua wanajihesabu Nafsi zao kabla hazijahesabiwa Mbele ya Mola wao.

Safari moja Imam Malik Ibn Dinar alienda katika Ibada ya Hijja na akakutana na Mwanamke ambae alikua analia sana na hivyo akamwambia: '**Ewe Mwanamke usiwe ni mwenye kupenda kulia sana kwani utayaharibu macho yako'** ambapo Mwanamke huyo akasema: '**Ewe Malik Ibn Dinar, hakika kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* atanijaalia mimi kua Mtu wa Peponi basi atanijaalia Macho mengine mazuri zaidi kuliko haya, na kama nikiwa Mtu wa Motoni basi nitakua na Macho yaliyoharibika zaidd ya haya.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Malik Ibn Dinar alifariki mwaka 131 Al Hijra baada ya Kuumwa kwa Mda hadi kufikia kua akisema: ‘**Ya Allah Fahamu kua Mimi sivutiwi na chochote ndani ya Ulimwengu huu, si matamanio ya Wanawake wala si matamanio ya Tumbo langu’**

Ambapo baada ya kufariki kwake basi mmoja kati ya Wanafunzi wake alimuona Malik Ibn Dinar Ndotoni na hivyo akamuuliza: ‘**Ewe Imam Ibn Dinar hivi Jee amekupokeaje *Allah Subhanah wa Ta'ala* ulipowasili Mbele yake?’**

Nae akajibu: ‘**Wa Allahi Hakika mimi nimewasili Mbele ya Mola wangu nikiwa na Mizigo ya Dhambi Lakini hata hivyo alinisamehe Dhambi zangu kutokana na kua Mimi Daima nilikua Nikimkumbuka na Nikimfikiria Vizuri *Allah Subhanah wa Ta'ala*.’**

IMAM THABIT AL BUNANI 41 AH

Imam Thabit Al Bunani alizaliwa katika ardhi ya Mji wa Kufa mnamo mwaka 41 Al Hijra, hiki kilikua ni kipindi ambacho Mji wa Kufah umesheheni Wanazuoni wa Tabiina, mazingira ambayo yalimsaidia sana Imam Thabit Al Bunani katika maandalizi yake ya kukulia katika Ucha Mungu, kwani alisoma kwa Sahaba Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*, kwa mda wa miaka 40 na alikua akifika mbele yake basi humkimbilia kama mtoto mdogo na kuukamata mkono wake na kuuanza kuubusu bila ya kutaka kuuachia huku akisema: ‘**Hakika Mkono wako umegusana na Mkono wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam***’

Imam AdDarimi anasema kua: ‘Amesema Imam Thabit Ibn Bunani kua: **‘Anas Ibn Malik alikua akiwakusanya Watoto wake na familia yake baada kusoma kwake Qur’an na kuhitimisha na kuomba dua na kisha alikua akiomba dua kwa ajili yao’’**

Imam Thabit Ibn Bunani alisoma pia kwa Wanazuoni wengine wakubwa hivyo alipokua mkubwa alikua akijulikana kama ni miongoni mwa *Sawt Al Rahman* kwani alikua kila siku akimaliza kusoma Mas-haf nzima wakati akiwa Msikitini na alikua ni mwenye kuuhuisha usiku wake, na hivyo hata baada ya kufariki kwake basi watu walikua wakisikia sauti ya kisomo chake cha Qur’an kutoka kaburini mwake.

Kwani alikua akisema kua: ‘**Hakuna mtu anaeweza kujihesabu kua ni Mfanya Ibada wa kweli kwa Mola wake bila ya siku isiyokua na *Qiyam Al Layl* na Siyam ndani yake.**’

Akaendelea kusema kua: ‘**Hakika mimi nilipigana kwa miaka 20 kwa ajili ya Qiyam Al Layl na baada ya hapo katika miaka 20 iliyofuatia ndio nikawa nahisi utamu wake, kwani Hakuna kitu chenye utamu zaidi kwenye Moyo wangu mimi kuliko *Qiyam Al Layl’***

Na pia alikua akisema kua: ‘**Hakika mimi hua ni mwenye kusali rakaa 300 katika kila usiku**’ na hivyo linapochomoza jua basi miguu yake hua ni yenye kuvimba kwa kusimama, hivyo hua ni mwenye kujichua huku akisema: **‘Wenye kufanya Ibada hasa hawapo tena na mimi sina la kufanya.’**

Ambapo alisema Imam Malik Ibn Anas kua: ‘**Kuna Mifunguo michache ya Wema na Thabit Ibn Bunani ni miongoni mwao.**’

Imam Thabit Al Bunani alikua ni mtu mwenye Taqwa na ni mwenye kupenda kufanya Ibada na hivyo alikua ni Imam, Qadhi na Kiongozi wa Imani na Taqwa kwa watu wa Mji wa Kufah, kwani ilikua hakuna Msikiti katika mji wa Kufah isipokua ameshasali ndani yake tena katika sehemu tofauti ya Msikiti huo na wala si kwa rakaa mbili wala tatu bali kwa wingi zaidi na ni mwenye kulia zaidi katika kila sijda yake ndani ya msikiti husika, kwani alisema: ‘**Hakika mimi siipiti Nguzo yeyote ya Msikitini bila ya kusali chini yake na kusoma Qur’an Mas-haf nzima na Kulia.’**

Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* alikua kama hajamuona Thabit Ibn Bunani basi alikua akisema: **‘Yuko wapi Thabit Al Bunani? Hakika mimi nazipenda tabia zake.’**

Imam Thabit Al Bunani alikua akifunga takriban kila siku na hivyo alisema Bakr Ibn Abd Allah kua: ‘**Thabit Al Bunani ni mtu bora miongoni mwa watu wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* wa wakati wake kwani alikua ni mwenye kuyapokea maisha kwa kilio cha Khofu juu ya Mola wake na kufanya Istighfar kwa Mola wake huku akiendesha maisha yaliyojaa huzuni, alikua akilia kama Mama aliempoteza mtoto wake hadi mbavu zake zilikua zikigusana.**’

Kulia kwake huko kulimpelekea Imam Thabit Ibn Bunani kua ni mwenye kuumwa na Macho, na alipoambiwa na Daktari wake kua anatakiwa apunguze kulia basi Imam Thabit Ibn Bunani alisema: ‘**Jee kuna maana gani ya Kua na macho yasiyotoka machozi kwa kulia kwa ajili ya Mola wake**?’ na hivyo akakataa kutibiwa Macho yake. Amesema Imam Thabit Ibn Bunani kua: **‘Tumepokea sisi kua mara moja Ibilisi alijitokeza mbele ya Nabii Yahya, ambapo nae baada ya kumuangalia basi akamuona kua anakamba nyingi sana ambazo ameshika mkononi mwake, hivyo akamuuliza : ‘Ewe Ibilisi Jee hizo Kamba za nini?’**

Ibilsi akajibu: ‘Hizi kamba ni kwa ajili ya Matamanio tofauti ambayo hua nnawafungia nazo Ibn Adam’ Nabii Yahya akauliza: ‘Hivi Jee unayo kamba

ambayo hua unaweza kuitumia kwa ajili yangu?' Ibilis akasema: 'Naam, ni pale unapokua Umeshiba kwa chakula na hivyo kua ni mwenye kuhisi uzito ambapo kutokana na uzito huo basi hua unashindwa Kusimamia Ibada yako ya Sala, Dhikr na maombi yako' baada ya kusikia maneno hayo basi Nabii Yahya akasema: '*Wa Allahi* nnaapa mimi kua sitokula tena hadi nikashiba' Ibilis akasema: 'Wallahi na mimi nnaapa kua sitompa tena ushauri Ibn Adam.''

Imam Thabit Al Bunani alikua ni mwenye kupenda kutumia pia mda wake kwenye maeneo ya Makaburini, ambako katika baadhi ya siku hua ni mwenye kulala katika maeneo hayo. Ambapo anasema Imam Thabit Al Bunani kua: **'Siku moja nilikua nikitembea Makaburini na mara nikasikia sauti ikisema: 'Thabit, usiyaone Kimya na kuhadaika nayo haya Makaburi kwani ndani yake mna watu wengi sana wanaoadhibika' na nilipogeuka nyuma kuangalia anaeniambia hivyo basi sikuona Mtu.'**

Siku moja alipoalala Makaburini akaota kua Maiti wote wametoka kwenye Makaburi yao huku wakiwa wamevalia vizuri nakupendeza na nyuso zao zikiwa zinang'ara na kua ni wenye kupokea sinia zenye vyakula vizuri tofauti.

Lakini hata hivyo mmoja kati ya Maiti hao alikuwepo yule ambae alikua ni mwenye kua na nywele timtim huku uso wake uki uko katika hali ya kusawijika, na nguo zake zikiwa zimechanika chanika na pia alikua hajapewa sahani yeyote kama walivyopewa wengine. Baada ya mda watu hao wakarudi Makaburini mwao katika hali kama waliyokua nayo hapo kabla, yaani wenye kuvutia na kupendeza na hata yule kijana aliekua na hali ya nguo zilizochanika nae alirudi huku akiwa katika hali hio hio huku akiwa ameinamisha chini uso wake kwa huzuni.

Hivyo Imam Thabit Al Bunani akaamua kumfuata kijana huyo ili apate kumuuliza imekujae akawa na hali kama hio, ambapo alipokuatana nae akamsalimia na kumuuliza: '**Hivi wewe ni nani na imekuaje hadi ikawa wenzako wana furaha na wamependeza na kua na vyakula lakini wewe hukua katika hali hio? na pia unarudi mikono mitupu kama ulivyotoka?**'

Hivyo kijana huyo akasema: '**Ewe Imam Al Bunani, hakika mimi nimekua ni mgeni miongoni mwao, kwani hakuna anaenikumbuka hata kwa dua wala kwa ukarimu, ama kuhusiana nao basi wao wana Watoto wao, Familia zao na jamaa zao wanaosali ambao hua ni wenye kuwatumia wao amali njema na Sadaqa, hivyo kila siku ya Ijumaa hua wanapokea kile wanachotumiwa.**'

Ama kuhusiana na mimi basi sina familia, lakini nnae Mama yangu ambae baada ya kufariki kwangu aliolewa na mume mwengine baada ya baba yangu, na katika wakati wa Uhai wangu niliamua kufanya Ibada ya Hija na Mama yangu, na katika

safari hio tulipofika njiani basi mimi nikafariki Dunia, na hivyo Mama yamgu hakunikumbuka tena baada ya kuolewa kwake na kufariki kwangu.

Hivyo Imam Thabit Al Bunani akamuulizia kuhusiana na Mama yake huyo jina lake na anapoishi ili amuelezee kuhusiana na habari hio.

Yule kijana akasema: **'Mimi natoka katika Mji fulani na Nyumba fulani, na Mama yangu jina lake ni Fulani, hivyo muelezee mama yangu hali yangu. Na kama haamini basi mwambie kua katika sehemu fulani kuna mfuko nimeuficha ambao ndani yake Dinar 100 ambazo aliniwachia Baba yangu, na hivyo kua achukue yeye ni mali yake, na hivyo atakuamini.'**

Hivyo baada ya Imam Al Bunani kuamka basi akafuatilia kuhusiana na aliyoyaona kwenye ndoto yake, na akafanikiwa kuonana na Mama wa Mtoto huyo na kumtaarifu namna alivyomwambia na hali yake. Baada ya Mama huyo kusikia habari hio basi akautafuta mfuko, alipoambiwa kua umefichwa na akauona na ndani yake akakuta mna Dinar 100, basi hapo hapo Mama huyo akazimia, na alipozindukana akazichukua Dinari hizo na kumpa Imam Al Bunani kwa ajili ya kuzitoa sadaqa kwa ajili ya Mwanawe huyo.

Ambapo baada a tukio hilo, basi Imam Thabit Al Bunani akawa na hamu sana ya kumuona tena kijana yule na hivyo alipoalala katika siku ya kuamkia Ijumaa akaota tena ndoto kama ile aliyoiota siku ile isipokua mara hii watu wa Makaburini walipotoka basi nae akatoka huku akiwa katika hali ya kupendeza, na kufurahisha huku akiwa na Ruzuku katika Sinia yake, ambapo kijana huyo akamfuata Imam Thabit Al Bunani na kumwambia:

'Ewe Imam Al Bunani, namuomba Allah akuingize kwenye Rehma zake kwa mapenzi yako juu yake kama vile ulivyoonesha mapenzi yako juu yangu, kwani bila ya shaka walio hai wanao uwezo wa kuwadhuru walio Makaburini wanapofanya Madhambi, na hapo hapo wanao uwezo pia wa kuwanufaisha walio Makaburi kwa wema wao.'

Anasema Imam At Tirmidhii kua : **'Amesema Imam Thabit Al Bunani kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayh wa Salam* kua: 'Wacha Mtu awe ni mwenye kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kila kitu chake hadi katika kamba ya kufungia Kiatu chake.''**

Ambapo anasema Hamad Ibn Salamah kua: **'Thabit Al Bunani aliomba dua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema: 'Ya Allah kama utataka kumjaalia Mtu awe ni mwenye Kusali ndani ya Kaburi lake basi nijaalie mimi niwe mmoja wao.''**

Na bila ya shaka Dua hio ilikubaliwa kwani baada ya kufariki kwake mnamo mwaka 123 Al Hijra, basi Mwanafunzi wake alimuonaa akiwa anasali ndani ya Kaburi lake pale aliposema: **‘Wa Allahi nnaapa kwa Jina la Allah ambae ameniumba mimi kua nilimzika Thabit Al Bunani katika siku ya kufariki kwake na baada kumzika pamoja nami alikuwepo Humaid At Tawiil, ambapo baada ya kuwekea mawe juu ya Kaburi lake basi moja liliaangukia ndani yake na nilipoliangalia nikamuona Thabit Al Bunani akiwa anasali ndani ya Kaburi lake.’**

IMAM SAID IBN JUBAYR 45 AH

Mnamo mwaka 45 Al Hijra katika ardhi ya Kufa alizaliwa Mtoto ambae A*llah Subhanah wa Ta’ala* alimjaalia kua ni miongoni mwa waja wake aliowachagua kua ni Wanazuoni wa kuisimamia na kuiendeleza Dini yake, kwani mtoto huyu alikua na kua ni Tabiina Mwanazuoni na Mcha Mungu ambae aliishi katika kipindi kimoja na Mwanazuoni Mcha Mungu maarufu aitwae Hasan Al Basr lakini yeye alikua ni mwenye asili ya Uhabeshi

Yaani alikua ni Mwanazuoni Muafrika aliekua akimilikiwa na Ukoo wa Banu Walibah ambao ni watu wa kabila la Banu Saad lakini baada ya kubelegh kwake basi alijikomboa na akaachiwa Huru.

Kwani huyu si Mwanazuoni yeyote yule isipokua yule Mwanazuoni anaejulikana kwa jina la Imam Said Ibn Jubayr, Imam Said Ibn Jubayr As Saadi Al Kufi alikua ni Mwanazuoni Mcha Mungu mkubwa sana ambae alikua akijulikana pia kwa jina la Abd Allah.

Ambapo tunapomzunguzia Imam Said Ibn Jubayr basi wenye kumjua wanasema kua: ‘**Kama ilikua Hasan Al Basr ni mtu mwenye huzuni na asiecheka, basi kwa upande wa Said Ibn Jubayr alikua si mtu mwenye kuhuzunika tu bali alikua ni mtu mwenye kulia hasa.**’

Ambapo mji wa Basra pia ndio Mji Unaoongoza kwa kua na Wairaq Wenye asili ya Afrika wengi lakini kwa upande wa Imam Said Ibn Jubayr basi yeye alikua akiishi katika Mji wa Kufah uliopo katika ardhi ya Iraq na ndio Maana akawa anaitwa Said Ibn Jubayr Al Kufi.

Katika wakati wa Uhai wake basi Imam Said Ibn Jubayr alikua ni Mwanazuoni ambae alikua akisifika kwa Ilm yake, Ucha Mungu wake na Unyenyekevu wake mbele ya *Allah*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Subhanah wa Ta'ala. Na alikua anapenda sana kusoma Qur'ani kiasi ya kua anamaliza Mas-haf nzima kusoma ndani ya siku mbili.

Kiasi ya kua alikua haombi Dua isipokua Dua hio hua ni yenye kupokelewa na kujibiwa hapo hapo na *Allah Subhanah wa Ta'ala*, ama kwa upande wa Ilm basi, bila ya shaka haishangazi kuona kua Mara nyingi utasikia: '**Ama kuhusiana na Mtizamo wa Said Ibn Jubayr kuhusiana na jambo hili basi yeye anasema kadhaa w kadhaa**'

Na hii ni kwa sababu Imam Said Ibn Jubayr alikua ni Mwanazuoni anaeogelea kwenye Bahari ya kina kirefu ya Ilm za Hadith, Fiqh, Tafsir ya Qur'an,Tarikh na Usomaji wa Qur'an na Lugha ya Kiarabu.

Ambapo kwa Upande wa Walimu wake basi Imam Said Ibn Jubayr alikua ni mtu ambae alisoma kwa Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambae ndie aliekua Mwalimu wake mkuu.Na pia Imam Said Ibn Jubayr alikua ni Mwanafunzi wa Sahaba Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu*, Sahaba Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu*, na pia alisoma kwa Sahaba Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*.

Kwani hata Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alipokua akiulizwa masuali na watu wa Kufah basi alikua akiwaambia watu hao kua: '**Hivi Jee nyinyi Hamna Mtoto wa Mwanamke wa Kiafrika katika Mji wenu?'**

Yaani Bahr ul Ilm Abdalla Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alikua akiwauliza watu hao wanaotoka Mji wa Kufah: '**Hivi kwanini mnaniuliza mimi masuali haya wakati katika Mji wenu mnae Mwanazuoni mwenye Ilm ambae ni Muafrika aitwae Said Ibn Jubayr?'**

Naam...hio ndio darja ya Imam Said Ibn Jubayr ambae moja kati ya sifa yake kuu ni kua: **'Alikua haruhusu watu kusengenya wengine mbele yake, na wala haruhusu watu kusema uongo Mbele yake'**

Na ingawa Imam Said Ibn Jubayr alikua akiishi katuka Mji wa Kufah nchini Iraq lakini alikua kila mwaka anafunga safari mara mbili kuelekea katika Mji wa Makkah kwa ajili ya kuenda katika Ibada ya Hija na kisha pia hua ni mwenye kuenda kwenye Ibada ya Umra.

Na alikua akifika katika Mji wa Makka na anapoliona Al Kaabah mbele yake basi husali sala ya Rakaa mbili ambayo katika Rakaa ya Kwanza tu basi hua ni mwenye kusoma Msahafu Mzima wa Qur'an...yaani Juzuu 30.

Si hivyo tu kwani Imam Said Ibn Jubayr alikua na Macho yasiyokauka Machozi kutokana na kumuogopa Mola wake na Udhaifu wake mbele yake

Ambapo anasema Mwanafunzi wake aitwae Imam Al Araj kua: **'Said Ibn Jubayr alikua ni mwenye kulia sana katika kipindi cha wakati wa Usiku, kiasi ya macho yake yaliharibika na kua si mtu mwenye kuona vizuri, na kulia kwake kuliwapelekea wale waliokua karibu yake nao kuanza kulia baada ya kuambiwa sababu zinazomliza Imam Said Ibn Jubayr**'

Kwani hivyo ndivyo walivyokua Waliotangulia kabla yetu walikua wakiijua na kuifanyia kazi ile hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliyoipokea Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambae ndie Mwalimu wake Imam Said Ibn Jubayr ambayo inasema: '**Macho ya aina mbili hayatoguswa na Moto wa Jahannam, Jicho lililokua likitokwa na Machozi kwa sababu ya kumuogopa Mola wake na Jicho ambalo halikufungika usiku kutokana na kusimamia ulinzi kwa ajili ya *Jihad fi Sabili Allah*.**'*(Imam At Tirmidhii)*

Na pia ile kauli ya Mwalimu wa pili wa Said Ibn Jubayr ambae ni Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua akisema: '**Hakika yangu Mimi ni bora Kulia tone Moja la Chozi kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuliko Kutoa Sadaqa Dinari Moja ya Dhahabu'**

Kwani amesema Said Ibn Jubayr kua: '**Kwa Hakika *Al Khashiyah* maana yake hua ni Kua Mtu unaemuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kiasi ya kua, Khofu yako inakaa baina yako wewe na kumuasi Mola wako'**

'**Na *Dhikr Allah* hua ni Kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na yeyote yule anaemtii *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni Mwenye kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* hata Kama Mtu huyo atakua ni Mwenye Kufanya Tasbih nyingi sana na hata kama akiwa anasoma sana Qur'an.**'

Amesema Imam Said Ibn Jubayr kua: **'Kama ikiwa Kifo kitasahaulika ndani ya Moyo wa Mtu kwa muda wa saa moja tu, basi Moyo wa Mtu huyo utakua ni wenye kuoza.'**

Naam...huo ni Wasia wa Imam Said Ibn Jubayr Ambae ni Miongoni mwa Maimamu wakubwa wacha Mungu na wenye Taqwa katika Kizazi cha Tabiina ambae pia ni Imam Mwenye Asili ya Kiafrika. Ambapo alisema Imam Abu Qasim Al Tabari kua: '**Said Ibn Jubayr ni Imam anaeaminika wa Waislam na ni Uthibitisho wa Dini ya Kiislam**'

Na akasema Imam Muhammad Ibn Hibban Al Busti kuhusiana na Imam Said Ibn Jubayr kua: ‘**Said Ibn Jubayr ni Imam wa Fiqh, Ni Mwenye Kufanya Ibada, Ni Muadilifu na ni Mwenye Taqwa**’

Kwani Imam Said Ibn Jubayr ni Imam wa Hadith ambae amenukuu Hadith 147 ambazo Imam Muhammad Ismail Al Bukhari amezikusanya katika Kitabu chake cha Hadith cha Sahih Bukhari.

Na pia Imam Said Ibn Jubayr amenukuu Hadith 78 ambazo Imam Asakir Ad Din Muslim Al Hajjaj Ibn Muslim Ibn Ward Al Qushayr Al Nishapuri amezikusanaya katika kitabu chake cha Hadith cha Sahih Muslim.

Naam..alisema Imam Said Ibn Jubayr kua: ‘**Maisha ya Dunia ni sawa na Wiki Moja Katika Wiki Nyingi sana zisizokua na Mwisho wa Idadi za Akhera**’

Ambapo Tunapozungumzia Ucha Mungu wake na Kuihesabia Nafsi Yake kutokana na kua na Neema zisizohesabika kutoka kwa Mola wake, na Khofu yake ya Kuulizwa kuhusiana nazo Neema hizo, basi siku Moja alileteWa Kibuyu Cha Asali, na baada ya Kuionja Asali hio basi aliacha kwa kuogopa kua akiendelea kula basi itakua Israfu na akasema: ‘**Wallahi Hakika Mimi Nitaulizwa Kuhusiana na Asali hii pia**’

Katika kipindi cha miaka ya mwanzoni ya Uislam yaani katika kipindi cha kati ya Mwaka 20 Al Hijra hadi mwaka 95 Al Hijra, ndio kipindi alichoishi Imam wa Tabiina mwenye asili ya Afrika aitwae Said Ibn Jubayr ambae ndio tunaangalia historia ya Maisha yake aliyoishi kwa mda wa miaka 75.

Na tunapoiangalia Historia ya *Amir ul Muuminina* Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* na *Amir ul Muuminina Sayydina* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* basi tunaona pia Mifarakano iliyotokea baina ya Waislam baada ya Kuuliwa Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* na Madaraka kuchukua Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu.* Ambapo Mifarakano hii ilisababisha kutokea kwa Vita na hivyo Waislam kugawanyika Makundi tofauti.

Ambapo kulikua kuna Kundi la Wafuasi wa *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na kundi la wafuasi wanaounga mkono Ukoo wa Banu Ummayad ambao walikua wakingozwa na Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu.*

Na hii ni historia ndefu ambayo mara kadhaa tumeshaizungumzia hivyo katika Kipindi alichokua akiishi Imam Said Ibn Jubayr basi ilikua ni baina ya Mtafaruku huo hadi katika kipindi cha Uongozi wa Jemedari Katili sana wa Utawala wa Banu Ummayad aitwae Hajjaj Ibn Yusuf.

Na ingawa alikua akijulikana kwa ukatili lakini kwa upande mwengine basi Hajjaj Ibn Yusuf ingawa aliua Waislam wengi sana waliokua hawataki kumtii yeye na Utawala wa Banu Ummayad wa Syria lakini hata hivyo, Hajjaj Ibn Yusuf alifanya Jambo Kubwa Sana ambalo ni Jambo la kuyatia Irabu maandishi ya Kiarabu ya Qur'an.
Yaani hapa zamani ilikua Qur'an haiwezi kusomeka kiusahihi kwa wasiokua Waarabu kwa sababu ilikua haina Fat-ha, wala Kisra, wala Dhuma, wala Sakin. Lakini ni Jemedari Hajjaj Ibn Yusuf ndie ambae aliesimamia kazi ya kuzitia Irabu hizo, hivyo kwa upande mmoja basi Irabu zote, za Kisra, Dhamma, Fat-ha na Sakin zote ni Bidaa.

Lakini ni Bidaa Hasan yaani Bidaa Nzuri iliyopelekea mimi na wewe Waswahili na Watu wengine Duniani tusiojua Lugha ya Kiarabu kua ni wenye kuweza kuisoma Qur'an ipasavyo naam..Historia ya Hajjaj Ibn Yusuf ambae alikua ni Mwalimu wa Madrasa kabla hajawa Jemedari Katili ni historia nyengine, na sipendi kuizungumzia.

Ila itabidi tuzigusie kwa juu juu kutokana na kua Imam Said Ibn Jubayr aliuawa kutokana na Amri ya Hajjaj Ibn Yusuf baada ya Kumuwekea wazi kua yeye ni dhalim na kisha kabla ya kutoa shahada yake basi Imam Said Ibn Jubayr akaomba Dua kua Allah amjaalie Hajjaj Ibn Yusuf asiue watu wengine baada yake yeye Imam Said Ibn Jubayr.

Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Kiongozi bora Miongoni mwenu ni yule ambae Nyinyi mnampenda na nyinyi anakupendeni, nyinyi mnamuomeba Dua na nyinyi akuombeeni, na kiongozi Muovu miongoni mwenu hua ni yule ambae mnamchukia nanyi anakuchukieni, mnamlaani nanyi anakulaanini.**' *(Sahih Muslim)*

Ambapo tunapomuangalia Hajjaj Ibn Yusuf katika Historia yake basi tunaona kua alikua ni kiongozi Qatili sana kwani aliua Waislam zaid ya 100, ndani yake akiwema Sahaba Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu.*

Ambapo katika wakati wa Kipindi cha Utawala wake uliokua ni wa Kinguvu basi Waislam walimlalamikia Hasan Al Basr na kumuomba Ushauri wafanye nini kuhusiana na Hajjaj Ibn Yusuf.

Lakini Hasan Al Basr akawaambia Waislam kua: '**Hakika Mimi nna khofu juu ya kile kitakachotokea baada ya kushindwa katika kupigana nae. Na pia nna Khofu kitakachotokea kuhusiana na kile kitakachofuata baada ya Kumshinda, kwani Huenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* ikawa ametujaribu ili atuangalie Subra yetu, Hivyo kama Mkimuua basi Inawezekana kua tukaletewa Kiongozi Muovu zaidi ili atuadhibu hivyo Mnatakiwa kua na Subra.**'

Huo ndio uliokua Mtizamo wa Hasan Al Basr kuhusiana na Hajjaj Ibn Yusuf. Ambapo hata hivyo Waislam hao hawakusitia hapo, bali wakatafuta Mtizamo mwengine ambao ulikua unaamrisha kupigana Vita.

Kwani Ndani ya waliokua na Mtizamo huu basi alikuwemo pia Imam Said Ibn Jubayr ambae yeye aliungana na Kiongozi wa Jeshi aitwae Ibn Al Shaath.

Na hivyo Wakaandaa Jeshi lao na kupigana na Jeshi la Hajjaj Ibn Yusuf, na matokeo yake Wakashindwa vibaya sana kiasi ya kua Said Ibn Jubayr ilimbidi akimbie mapigano na atafute pa kijifichia.

Na Hivyo Imam Said Ibn Jubayr akakimbilia katika Mji wa Makkah na kwa bahati mbaya basi Hajjaj Ibn Yusuf akapata Habari kua Imam Said Ibn Jubayr kakimbilia katika Mji wa Makkah.

Hivyo nae akaelekea katika Mji wa Makkah na kisha Hajjaj Ibn Yusuf alipofika katika Mji huo basi akatoa Onyo kwa kusema kua:

‘**Mimi simtaki Mtu yeyote isipokua namtaka Said Ibn Jubayr, na najua kua amejificha katika moja ya Nyumba zenu hivyo kwa usalama wenu basi nataka Said Ibn Jubayr aletwe Mbele yangu, na kama hakuletwa nami nikamkuta ndani ya Nyumba amejificha basi Kichwa cha Mwenye Nyumba hio pamoja na cha Said Ibn Jubayr kitakua halali yangu, na kisha pia nitavunja Nyumba hio na Nyumba zote za Jirani ya nyumba hio**’

Baada ya kupatikana habari hio basi Imam Said Ibn Jubayr ikabidi ajisalimishe kwa ajili ya kukatwa kichwa chake peke yake na Hajjaj Ibn Yusuf, na Imam Said Ubn Jubayr alipofikishwa mbele ya Hajjaj Ibn Yusuf, mbele ya Waislam wenzake na akiwemo Mtoto wake basi hali ilikua kama ifuatavyo; Hajjaj Ibn Yusuf alimuuliza Imam Said Ibn Jubayr kwa kusema: ‘**Unaitwa Nani?**’

Imam Said Ibn Jubayr akajibu: **‘Said**’

Hajjaj akauliza: **‘Baba yako anaitwa nani?’**

Imam Said ibn Jubayr akasema: **‘Jubayr’**

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: ‘**La wewe Jina lako ni Shaqiy Ibn Kusayr’**

Hajjaj Ibn Yusuf alisema hivi kumkejeli Imam Said Ibn Jubayr kwa *Said* maana yake hua ni Jambo Zuri na *Jubayr* maana yake Kitu kilichotengenezwa sawia Hajjaj Ibn

Yusuf akageuza na kumuita *Shaqiy* yaani Alieharibika *Ibn Kusair* yaani Mtoto wa Alievunjika

Hapa Imam Said Ibn Jubayr akasema: **'Mama yangu anajua zaidi maana ya Jina langu kwani yeye ndie alienipa**'
Hajjaj Ibn Yusuf akasema: '**Mama yako na wewe Mwenyewe Nyote hamna aibu**'

Imam Said Ibn Jubayr akajibu: '**Wewe si Mwenye kujua juu ya yasiyojulikana, kwani ajuae juu ya Ghayb ni mwengine'**. Jibu hili lilimtia hasira Hajjaj Ibn Yusuf hivyo akasema: **'Nitakukata shingo yako sasa hivi'**

Imam Said Ibn Jubayr akatabasam kisha akasema: '**Hii inamaanisha kua Mama yangu Sahih kwa kunipa jina langu hili**'

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: '**Angalia Mdomo wako, nitakupeleka Jahannama sasa hivi!'**

Imam Said Ibn Jubayr akajibu: **'Kama ningejua kua wewe unao uwezo huo basi mimi ningekufanya wewe kua mungu wangu'**

Hajjaj Ibn Yusuf akamuuliza: '**Unaaamini nini kuhusiana na Mtume wake?'**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: **'Hakika yeye ni Mtume mwenye Rehma na ni *Nabiyu Allah* alietumwa kwa ajili ya kuonesha njia bora ya Uongofu'**

Hajjaj Ibn Yusuf akauliza: **'Unasemaje kuhusiana na Makhalifa wanne?'**

Said Ibn Jubayr akajibu: **'Hakika mimi si Msimamizi wao, na kila mtu ataulizwa juu ya matendo yake.'**

Kwani Hajjaj Ibn Yusuf alikua akiulizia kuhusiana na Allah, Mtume *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* na Makhalifa wake, kwa sababu yeye alikua ni mwenye kua na Mtizamo tofauti kuhusiana na Ukhalifa wa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na ndio maana Hajjaj Ibn Yusuf akauliza Suali lifuatalo: '**Jee ni yupi Miongoni Mwao ambae ndie mwenye Darja ya juu zaid?**'

Imam Said Ibn Jubayr akajibu: **'Mwenye Darja ya juu zaid mbele ya Allah miongoni mwao ni yule ambae aliefanikiwa kupata radhi zaid za Mola wake**'

Hajjaj Ibn Yusuf akauliza: **'Jee ni yupi aliefanikiwa kupata radhi zaid?**'

Imam Said Ibn Jubayr akasema: ‘**Hilo linajulikana na mwenyewe alieridhishwa kwani yeye ni mwenye kujua yaliyofichikana ndani ya Vifua na ndani ya Nyoyo’**

Hajjaj Ibn Yusuf akauliza: ‘**Jee Nani yuko Peponi na nani yuko Motoni?**’

Imam Said Ibn Jubayr akajibu: ‘**Siwezi kujua juu ya hilo hadi nitakapotembelea sehemu hizo na kuangalia Waliomo ndani yake’**

Hajjaj Ibn Yusuf akasema : ‘**Na mimi unaonaje nitakua wapi?’**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: ‘**Hakika mimi sijafikia darja ya kupokea habari za Ghayb**’

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: **‘Hakika wewe hukusudii kuniambia ukweli’**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: ‘**Na sijakuambia Uongo pia’**

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: **‘Kwanini wewe hua si mwenye kucheka’**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: **‘Sioni sababu ya kunichekesha. Inakuaje mtu awe ni mwenye kucheka wakati akiwa ameumbwa kutokana na udongo na itambidi asimame katika siku ya malipo huku akiwa amezongwa na mashakil mengi sana?**’
Hajjaj akasema: **‘Sasa mbona mimi hua nnacheka.**’
Imam Said Ibn Jubayr akasema: ‘**Allah ametuumba sisi kulingana na kua na Maumbile yenye tabia tofauti.’**

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: ‘**Ama sasa hivi itabidi nikuue.’**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: ‘**Ahadi juu ya kifo changu imeshakadiriwa katika sehemu yake na wakati wake na aina ya kifo chake’**

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: **‘Jee unajua kua Allah amenipandisha mie darja juu yako?’**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: ‘**Hakuna Ambae anaweza kujisifu kuhusiana na darja yake mbele ya Mola wake, isipokua yule mwenye kuijua darja hio, kwani ni Allah tu ndie mwenye kujua kuhusiana na yasiyojulikana.’**

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: **‘Sawa, Jee unataka nikuue kwa njia gani?’**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: ‘**Kama vile ambavyo ungependa wewe kuuliwa.’**
Hajjaj Ibn Yusuf akauliza: **‘Au unataka nikusamehe?’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Said Ibn Jubayr akasema: **‘Usamehevu wenye Thamani ni wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, hivyo usamehevu wako hauna maana yeyote.’**

Hajjaj Ibn Yusuf akaamrisha Watu wake kwa kusema: **‘Muueni!’**

Amri ambayo ilimfanya Imam Said Ibn Jubayr kucheka, hivyo Hajjaj Ibn Yusuf akauliza: **‘Wewe si mtu wa kucheka, jee ni kipo kilichokuchekesha?’**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: **‘Nnacheka kutokana na Uthubutu wako mbele ya Allah na Rehma zake juu yako.’**

Kwani Hajjaj Ibn Yusuf akasema kutokana na majibu hayo kua: ‘**Hakika mimi nnamuua Mtu ambae ni mwenye kusababisha Ufa miongoni mwa Waumini, hivyo Muueni sasa hivi.’**

Imam Said Ibn Jubayr akaomba kua apewe nafasi ya kusali Sala ya Rakaa 2, na akapewa nafasi hio ambapo baada ya kusali basi akasoma aya ifuatayo:

﴿إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلْأَرْضَ حَنِيفاً وَمَآ أَنَاْ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ﴾

Inni Wajjahtu Wajhiyya Lilladhii Fatara Al Samawati wa Al Ardha Haniifan wama Ana mina Al Mushirkiina *(Surat Al Anaam 6:79)*

Tafsir: ***Hakika Mimi nimeuelekeza Uso wangu Yule ambae Ndie alieumba Mbingu na Ardhi ikiwa ni mwenye kumuabudu Allah bila ya kumshirikisha na Mimi si Miongoni mwa Washirikina***

Hivyo Hajjaj Ibn Yusuf akawaambia watu wake: ‘**Msimuelekeze kwenye Kibla chetu Waislam, Muelekezeni kwenye Kibla cha Manasara kwani wao ndio pia ni wenye kuanzisha Ufa na Mvutano katika Dini yao**’

Hivyo hapo hapo Imam Said Ibn Jubayr akaelekezwa Uso wake upande tofauti na lilipo Al Kaabah.

Kwani Imam Said Ibn Jubayr nae alipogeuziwa upande mwengine ili akatwe kichwa basi akasema:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

﴿وَلِلَّهِ ٱلْمَشْرِقُ وَٱلْمَغْرِبُ فَأَيْنَمَا تُوَلُّوا۟ فَثَمَّ وَجْهُ ٱللَّهِ إِنَّ ٱللَّهَ وَاسِعٌ عَلِيمٌ﴾

Walillahi Al Mashriqu wa Al Maghribu Faayna ma Tawaluu fathama wajhu Allahi Inna Allah wasiAa'un aAlimun. *(Surat Al Baqara 2:115)*

Tafsir: ***Na Kwake Allah ndiko kwenye Umiliki wa Mashariki na Magharibi, Hivyo Kokote kule Mtakapogeukia basi Mnaangaliana na Uso wa Allah Hakika Allah ni Mwenye kutosheleza Mahitaji ya Viumbe wake, na ni Mwenye kujua kila kitu***

Hajjaj Ibn Yusuf kusikia aya hio basi akawaambia Watu wake: '**Muelekezeni Uso wake Ardhini**'

Ambapo Imam Said Ibn Jubayr akasema:

﴿مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ﴾

Minha Khalaqnakum wafiiha nuaAidukum wa minha nukhrijukum Taratan Ukhra *(Surat Ta-Ha 20:55)*

Tafsir: ***Kutokana Nayo (Ardhi) tumekuumbeni na Ndani yake Tutakurudisheni na Kutokana nayo Tutakutoeni (Tutakufufueni) Kwa Mara nyengine tena.***

Hajjaj Ibn Yusuf akasema: **'Mkateni Kichwa!'**

Imam Said Ibn Jubayr akasema: '**Nakutakeni kua muwe Mashahidi Wangu juu ya nnachokisema, ambacho ni Ya Allah usimpe Hajjaj Ibn Yusuf uwezo juu ya watu wengine zaidi yangu, hakika mimi nashuhudia kua hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokua Allah na** ***Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam*** **ni Nabii na Mtume wake.**'

Kisha baada ya Kutoa shahada hio basi Imam Said Ibn Jubayr akauliwa kwa kukatwa Kichwa.

Baada ya Imam Said Ibn Jubayr kukatwa Kichwa basi Hajjaj Ibn Yusuf akashangaa kuona kua Mwili wa Imam Said Ibn Jubayr ukiwa unatoka Damu Nyingi sana tena taratibu bila ya kufoka.

Alipouliza basi akaambiwa kua hio ni kwa sababu ya Utulivu wa Moyo wa Imam Said Ibn Jubayr ambao ulikua ni hali tofauti na Watu wenye Khofu ya Kifo, na baada ya kuuawa Imam Said Ibn Jubayr basi na Hajjaj Ibn Yusuf nae hakuchukua Mda akafariki.

Naam, huyo ndio Imam Said Ibn Jubayr ambae kabla ya kifo chake alimwambia Mtoto wake aliekua akilia kua:

Ewe Mtoto wangu Kwanini Unalia? Kwani mimi nimeshaishi kwa miaka 75, hivi jee haitoshi? Ulikua unataka niishi kwa Miaka mingapi?

Kwani amesema Amr Ibn Maymun kua: ‘**Amesema Baba yangu kua Said Ibn Jubayr alifariki Dunia lakini hata hivyo kila mtu ananufaika na Ilm yake**’

IMAM AL QARI IBN KATHIR AL MAKKI 45 AH

Imam Abd Allah Ibn kathir Ibn Amr Ibn Abd Allah Ibn Zadhan Ibn Hurmuz Al Makki Al Dari alikua ni mwenye asili ya Uajemi na alizaliwa katika Mji wa Makkah mnamo mwaka 45 Al Hijra.
Na alikua ni mwenye Ilm kubwa ya Qiraa cha Quran ambapo Amr Al Dani basi yeye anasema kua: ‘**Imam Ibn Kathir alisoma kwa Abd Allah Ibn Saib Al Makhzumi**’ kwani Imam Abd Allah Ibn Kathir ni mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa wa Ilm ya Qiraa ambao wanawakilisha aina saba za Qiraa au kisomo cha Qur’an kinachukubalika Ulimwenguni ambapo ndani yake

Lakini wengi miongoni mwa Wanazuoni wanasema kua Imam Ibn Qathir alisoma Ilm ya Qiraa cha Qur’an kwa Imam Mujahid Ibn Jabr na pia alisoma kwa *mawla* wa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, ambacho hiki Qiraa chake kilikua ni Qiraa cha Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kutokea kwa Zayd Ibn Thabit na Ubay Ibn Qaab *Radhi Allahu Anhum* na ndio pia aina ya Qiraa ambacho alikua akipenda kukitumia *Mujaddid Ad Din Mujtahid* Imam Muhammad Idris Al Shafii.

Imam Abd Allah Ibn Kathir alisoma Ilm ya Hadith kutoka kwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwemo Malik Ibn Anas na Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhum* na hivyo katika wakati wa uhai wake basi kutokana na Ilm yake alikua ni Qadhi wa Mji wa Makkah.

Imam Abd Allah Ibn Kathir alikua ni mtu mrefu mwenye muonekano wa ngozi nyeupe na alikua ni mtu ambae mwenye ilmu kubwa pia ya Lugha ya Kiarabu na hivyo Imam Ibn Kathir alikua ni Mwalimu mwenye Wanafunzi wengi sana waliokua wenye

kufuatilia Ilm ya Qiraa cha Qur'an wakiwemo Imam Ahmad Ibn Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Qasim Ibn Nafi Al Buza ambae alikua ni mwenye asili ya Uajemi pia. Ambae alisilimishwa na Imam Saib Ibn Abi Al Saib Al Makhzumi.

Na Mwanafunzi wake mwengine maarufu wa Imam Ibn Kathir ni Imam Muhammad Ibn Abd Rahman Ibn Khalid Ibn Muhammad Abu Amr Al Makhzumi ambae nae pia baadae alisoma kwa Imam Al Buza na hivyo akawa ni miongoni mwa viongozi wa Ilm ya Qiraa katika maeneo ya ardhi ya Hijaz.

Imam Ibn Kathir alifariki mnamo mwaka 120 Al Hijra katika Mji wa Makkah.

IMAM NAAFI MAWLA IBN UMAR

Kuna kutofautiana kuhusiana na asili ya Imam Naafi Mawla Ibn Umar, kwani kuna wanaosema kua alikua ni mwenye asili ya Kabul, kuna wanaosema kua ni mwenye asili ya Nishapur, na kuna wasemao kua ni mwenye asili ya Khurasan na kuna wasemao kua alikua ni mwenye asili ya Uajemi na alikua ni mateka wa Vita waliokamatwa kutoka katika maeneo hayo katika mwaka wa 44 Al Hijra na hivyo akawa ni Mtumwa wa Sahaba Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu.*

Ambapo anasema Imam Naafi kua: '**Wakati mimi na Bwana wangu tulipoenda kwenye makazi ya Abd Allah Ibn Jafar Ibn Abi Talib, basi Abd Allah Ibn Jafar Ibn Abi Talib alikua anataka kuninunua kwa bei kubwa sana ya Dinar 12000, ambapo Abd Allah Ibn Umar akatafakkari kisha tuliporudi Nyumbani basi akamuuliza mke wake Safiyah Bint Abi Ubayd ambae nae akajibu: 'Unasubiri nini, muuze tu kwa Abd Allah Ibn Jafar kwa Dirham 12000' lakini hata hivyo Abd Allah Ibn Umar akasema: 'Subiri nadhani kua kuna bahati nzuri zaidi, kwa bora kua ni mwenye kumuachia huru kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*''** na hivyo baada ya kumuachia huru basi Naafi akamuombea Dua Abd Allah Ibn Umar kwa kusema**: 'Ya Allah Muachie Huru Abd Allah Ibn Umar kutokana na Moto.'**

Hivyo Imam Abu Abd Allah Naafi Ibn Sarjis Ibn Abu Abd Allah Ad Daylami alikua maarufu kama Nafii *Mawla* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allah Anhu* kwa sababu alikua ni Mtumwa alieachiwa huru wa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* na hivyo alikua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith kupitia kwa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kiasi ya kua Sanad yake kupitia kwa Mwalimu wake huyu hua ni yenye kujulikana kama *Sanad* ya Dhahabu, na ndio zinazotumika sana na kuaminika kwenye Fiqh ya Madhhab Imam Malik, kwani Imam Naafi alikua pia ni Imam wa Fatwa na alisema

Imam Malik Ibn Anas kua: ‘**Kama Naafi akitoa Hoja kuhusiana na jambo fulani basi Hoja hio hua ni yenye uthibitisho tosha**’

Siku moja Imam Ibn Abi Hatim alimuuliza Baba yake kuhusiana na Nafi Ibn Umar ambaponae akasema**: ‘Naafi ni Thiqa’** na kisha akamuuliza tena: **‘Hivi Jee Uthibitisho wake unaweza kukubalika kua ni wenye kutosheleza kutoa Hukmu?’** ambapo nae akasema: **‘Naam’**

Na Khalili Ibn Abd Allah Al Khalili Al Qazwini alisema kua: ‘**Naafi ni Miongoni mwa Maimamu wa Tabiina wa Madina, alikua ni mtaalamu wa Ilm tofauti, alikua ni mwenye Hadith sahih na hivyo mitizamo yake ilikua baadhi ya wakati inaenda sambamba na ya Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar na baadhi ya wakati Mtizamo yake ilikua inapewa kipaumbele zaid**’

Anasema Imam Ibn Asakir kua: ‘**Amesema Khalaf Al Bazzaz kua : ‘Mimi nilimuuliza Ahmad Ibn Hanbal: ‘Hivi jee ni Sanad zipi ambazo zimethibitishwa?’ ambao nae akasema: ‘Ni Naafi kutokea kwa Ibn Umar, na kama ikiwa imetokea kutoka kwenye hadith ya Hammad Ibn Zayd basi ni yako wewe’**’’

Na pia akasema tena kua: ‘**Amesema Muhammad Ibn Sulayman Al Nishapuri kua: ‘Nimemsikia mimi Muhammad Ibn Ismail Al Bukhari kua: ‘Hadith bora zenye Sanad iliyokuasahihi ni za Malik kutokea kwa Naafi kutokea kwa Abd Allah Ibn Umar.**’’’

Na pia alisema Imam Sufyan At Thawry kua: ‘**Hadithi zinazoaminika zaidi ni za Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kupitia kwa Naafi.**’

Kwani Imam Malik Anas mwenyewe alikua ni Mwanafunzi mkubwa sana wa Imam Naafi Ibn Sarjis kama anavyoelezea mwenyewe Imam Malik Ibn Anas pale aliposema: **‘Hakika mimi nilianza kwenda kwa Naafi *Mawla* Ibn Umar wakati bado nikiwa mdogo, na alikua akishuka kutoka ngazini kwake huku Mfanyakazi wake akimshika mkono, na hutoka nyumbani kwake katika maeneo ya Baqi na huenda katika Masjid An Nabawi ambapo mimi hua ni mwenye kumuuliza Masuali na kusoma hadith kutoka kwake.**’

Imam Malik Ibn Anas anaendelea kusema kua: ‘**Nilipokua nikisikiliza Hadith kutoka kwa Nafii Ibn Sarjis kutokea kwa Ibn Umar basi nilikua simjali mtu mwengine yeyote isipokua yeye kwani alikua juu kuliko wengine wote.**’

Imam Naafi Ibn Sarjis alikaa na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kwa mda wa miaka 30, na hivyo alikua ni mwenye kunufaika sana na Ilm yake na muongozo wake kwani ilikua kila anapoenda Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* basi na Naafi yuko

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

nyuma yake kama anavyosema mwenyewe kua: '**Mimi nilienda kwenye Ibada ya Hija na Umra pamoja na Abd Allah Ibn Umar zaidi ya mara 30**'

Imam Naafi alisoma pia kwa Abu Hurayra *Radhi Allahu Anhu*, Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu*, *Ummu ul Muuminin* Aisha, Umm Salamah na Hafsa *Radhi Allahu Anhuma*, na pia alisoma kwa mke wa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu.*

Hivyo Imam Naafi Ibn Sarjis alikua ni mtu ambae anaeaminika sana tunapozungumzia Hadith za Abd Allah Umar *Radhi Allah Anhu* na Fatwa zake na alikua ni miongoni mwa watu wa mwanzo kua ni mwenye kuandika, hadith zake kutoka kwa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu.*

Imam Naafi Ibn Sarjis alikua ni mcha Mungu sana, alikua ni mwenye kupenda kukaa peke yake kila baada ya kusali Sala ya Alfajir kufanya *Dhikr Allah* bila ya kuzungumza na mtu yeyote hadi pale linapochomoza jua, kwani anasema kua: '**Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allah Anhu* alikua akisali Sala za Usiku hadi alfajiri, na kisha huniuliza: 'Hivi Jee asubuhi Tayari?' na humjibu kua tayari, na hivyo hunyayuka na kuanza kufanya Istighfar'**

Imam Naafi Ibn Sarjis anasema kua: '**Amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua amesema: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Mtu yeyote yule anaeneemeshwa zaidi neema za *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake, basi hua pia ni mwenye kuongezewa jukumu juu ya watu wengine juu yake.''**

Imam Naafi Ibn Sarjis anasema kua: '**Siku Moja Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* aliletewa Dirham 60,000 na Ibn Ma'mar, hivyo Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akazigawa zote kwa wale waliopo mbele yake. Mara akaja Masikini anaeomba hivyo Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akazichukua tena zile baadhi ya Dirham kutoka kwa baadhi ya wale aliowapa na kumpa yule Masikini.**

Na ingawa alikua ni mwenye ilm kubwa sana na Mcha Mungu lakini Imam Naafi pia alikua ni Mtu wenye tabia za ukali kwa Wanafunzi wake kiasi ya kua ilikua ni vigumu kwa Wanafunzi kusomeshwa nae isipokua wale wenye ustahamilivu mkubwa sana kama anavyosema Ismail Ibn Abi Uwais kua: '**Tulikua tukisoma kwa Naafi lakini tabia ya ukali wake ilinibidi niache kusoma kwake, lakini baadhi ya marafiki zangu wenye uvumilivu waliendelea kusoma kwake na walinufaika kutokana na Ilm yake kubwa sana aliyokua nayo Naafi.**'

Safari moja Imam Muhammad Ibn Shihab Al Zuhri ambae alikua ni Mwanafunzi wa Imam Naafi alisomeshwa hadith kutokana nae kupitia kwa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*, na kisha hadith hio hio akasomeshwa tena na Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar na kosa alilolifanya ilikua ni pale alipoinukuu hadithi hio hio hakua ni mwenye

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kuinukuu kupitia kwenye Sanad ya Imam Nafii bali alinukuu kupitia kwenye Sanad ya Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* hivyo ikawa kuna ugomvi baina yake Imam Muhammad Ibn Shihab Az Zuhri na Imam Naafi kwa kosa hilo kwanini hakumnukuu Imam Naafi.

Kwa upande wa Wanazuoni wa Hadith basi tunaona kua Imam Naafi ni Imam anaeaminika sana na amenukuliwa kwenye vitabu tisa vya Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Ambapo amesema Salih Al Misri kua: '**Naafi ni Hafidh, Thiqah na anaeheshimika katika Mji wa Madina na alikua akipendelewa zaidi ya Ikrimah Mawla Abd Allah Ibn Abbas**'

Ambapo anasema Hammad Ibn Zayd kua: '**Amesema Ubayd Allah Ibn Umar kua Umar Ibn Abd Al Aziz alimtuma Naafi katika ardhi ya nchini Misri kwa ajili ya kuwafundisha Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* watu wa nchi hio.**' na pia Khalifa Umr Ibn Abd ul Aziz alimwahi kumtuma Naafi kua ni msimamizi wa ugawaji wa Zakkah katika ardhi ya Yemen.

Miongoni mwa Wanafunzi wake wengine ni pamoja na Imam Qatadah, Imam Ubayd Allah, Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Shihab Al Zuhri n.k na alifariki mnamo mwaka 117 Al Hijra, ambapo kabla ya kufariki kwake alikua kitandani anaumwa na mara akawa analia, alipoulizwa kwanini analia basi alijibu: '**Nimekumbuka Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pale aliposema: 'Hakika ya Kaburini kuna Adhabu na kama kuna mtu ataepukana nayo basi ni Said Ibn Muadh.'**'

IMAM IBN ABI MULAIKAH

Imam Abu Muhammad Abd Allah Ibn Ubayd Allah Ibn Abi Mulaika At Taymi Al Qureshi Al Makki alizaliwa katika kipindi cha utawala wa *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* au baada yake na alifariki katika Mji Makkah mnamo mwaka 117 ambao ndio pia mji aliozaliwa ndani yake.

Imam Ibn Abi Mulaika alikua ni Mwanazuoni mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith, Qur'an na Qiraa chake na Fiqh kwani alisoma kutoka kwa Masahaba wengi wakiwemo *Amir ul Muuminin* Al Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Sad Ibn Abi Waqas *Radhi Allahu Anhu,* Aisha *Radhi Allahu Anha,* Asma Bint Abu Bakr *Radhi Allahu Anha,* Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Jafar *Radhi Allahu Anhu, Abu Hurayrah Radhi Allahu Anhu,* Miswar Ibn Mikhramah *Radhi Allahu Anhu,* Uqbah Ibn Harith *Radhi Allahu Anhu, n.k*

Kutokana na ukubwa wa Ilm yake basi Imam Ibn Abi Mulaika alikua ni Qadhi wa Mji wa Taif na Mji wa Makkah katika kipindi cha Mamlaka ya Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu* katika Mji huo, na alikua ndio Muadhini wa Miskiti Mtukufu wa Mji wa Makkah na pia Imam wa *Salat At Tarweh* katika Mwezi wa Ramadhan katika Msikiti wa Makkah.

Miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Amr Ibn Dinar, Imam Abd Rahman Ibn Abu Bekr, Imam Ata Abi Rabah, Imam İbn Jurayj, Imam Yazid Ibn İbrahim, Imam Jariri Ibn Hazim, Imam Nafii Ibn Amr na wengineo.

Ambapo amesema Imam Abu Zurah na Imam Abu Hatim kua: **'Ibn Abi Mulaika ni Thiqah na naeaminika ambae ni *Mukthirun* (Alienukuaa hadith nyingi sana)'**

Alisema Imam Ibn Abi Mulaikah kua: **'Ikrimah Ibn Abu Jahal *Radhi Allahu Anhu* alikua akichukua Qur'an na kisha akijiwekea usoni na kusema: 'Kitabu cha Mola wangu, Maneno ya Mola wangu.''**

Na akasema tena Imam Ibn Abi Mulaikah kua: **'Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha kua:* 'Hata maumivu ya mtafuno wa mdudu au mtihani mkubwa zaidi yake ukimkuta Muumini basi huani sehemu ya kufutiwa dhambi kwake.''**
Na akasema tena Imam Ibn Abi Mulaikah kua: **'Mimi nimekutana na Masahaba 30 ambao wote walikua wakiogopa kuangukia kwenye hali ya Unafiq, na ilikua hakuna hata Sahaba mmoja ambae alikua akijinadia kua ni mwenye Imani kubwa ya kufikia Malaika Jibril au Mikail'**

Imam Ibn Abi Mulaikah ni miongoni mwa Maimamu walionukuliwa Kauli zao katika kuthibitisha kua Masahaba wa walisali Taraweh rakaa 20 katika kipindi cha Utawala wa *Amir ul Muuminin*.

Amesema pia Imam Ibn Abi Mulaikah kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakachukuliwa na kuhesabiwa Amali zake basi atakua ni mwenye kuadhibiwa.''**

IMAM SAFWAN IBN SULAYMI

Imam Abu Harith Safwan Ibn Sulaymi alizaliwa katika Mji wa Madina mwanzoni mwa miaka 100 ya mwanzo ya Uislam, na hivyo alikua ni mwenye kusoma kwa Masahaba kama kina Abd Allah Ibn Umar, Anas Ibn Malik, Abu Umamah Ibn Sahl, Imam Abd

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Rahman Ibn Ghanim, *Radhi Allahu Anhum*, na pia alisoma kwa Imam Said Ibn Musaayib, Imam Abu Salamh Ibn Abd Rahman, Imam Ataa Ibn Yasir, nk.

Hivyo Imam Safwan Ibn SulaymIi alikua ni Thiqah na ni mweye kuaminika kutokana na kua na Ilm kubwa sana ya Hadith na Qur'an na Fiqh na hivyo aliwasomea Maimamu wakubwa wakiwemo Imam Ibn Jurayj, Imam Zayd Ibn Aslam, Imam Ibn Al Munkadir na wengineo.

Alisema Imam Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na Imam Safwan Ibn Harith kua: '**Abu Harith alikua ni aliechaguliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na kua na ucha Mungu mkubwa sana, na yeye ni Mwanazuoni ambae anaaminika katika fani ya Hadith.'**

Ambapo anasema Abu Damr kua: '**Mimi nilimuona Abu Harith, katika hali ambayo ilikua kama angeambiwa kua siku ya Kiama ni kesho basi angekua hana haja ya kuongezea katika amali zake kutokana kua ni mwenye kutumia jitihada zake zote katika kufanya Ibada.**'

Ambapo alisema Yaqub Ibn Shayba *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Safwan ni Mwanazuoni aliesoma na mwenye kujulikana kwa ucha Mungu wake, kwani hata miguu yake ilikua inavimba kutokana na kusali sana Usiku.**'
Abd Al Azizi Ibn Hazim nae akasema: **'Sisi tulifunga safari nae kuelekea Makkah na Ngamia na kamwe sikuwahi kumuona akiwa ni mwenye kulala'**

Amesema Safwan Ibn SulaymI kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ibn Adam hua ni mwenye kufuata Imani ya Dini ya rafiki yake, hivyo wacha Mtu achague rafiki mzuri''**

Amsema Safwan Ibn SulaymI kua: '**Amesema Sulayman Ibn Yasar kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kuna Nguzo ya Nuru mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo pale Mja anaposema *La Ilaha Illa Allah*, basi hua ni yenye kutikisika, ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* huiambia Nguzo hio: 'Tulia' na nguzo hio hua ni yenye kusema: 'Nitatuliaje mimi wakati kuna mja ambae amesema *La Ilaha Illa Allah* na hajasemehewa Dhambi zake?' hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* husema: 'Nimeshamsamehe, Nimeshamsamehe' hivyo Nguzo hio hua ni yenye Kutulia.**'

Amesema Safwan Ibn Sulaymi kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Katika wakati wa uhai wenu, jifunzeni mambo mema, simamieni neema za *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yenu na ziombeni zikufikieni, kwani neema hizo za *Allah Subhanah wa Ta'ala* huwafikia wale ambao ni mwenye kuwataka yeye, hivyo Muombeni ili akuhifadhieni sehemu zenu zihifadhike na kukuondoleeni khofu zenu.'**

Ambapo anasema Abu Damra Anas Ibn Iyadh kua: **‘Ilikua ni mwezi wa Ramadhani au katika siku ya Idd Al Hajj ambapo kwa Safwan Ibn Sulaym alienda nyumbani kwake akiwa na masikini ambae alimpa Sadaqah, na kisha baada ya hapo, masikini huyo akaondoka na kuja tena baadae, ambapo Imam Safwan hakumfukuza, wala hakumwambia kua ameshampa, bali aliingia ndani akachukua Dinari nyengine na kisha akampa’**

Abi Kathir Ibn Yahya anasema kua: ‘**Khalifa Sulayman Ibn Abd Al Malik alikuja kutembelea katika Mji wa Madina, wakati Umar Ibn Abd Al Aziz alipokua Gavana wa Madina, hivyo baada ya kusaliwa sala ya Adhuhuri basi Khalifa Sulayman Ibn Abd Al Malik, akakaa pembeni ya Nguzo na macho yake yakaangukia kwa mtu ambae ingawa hata hamjui lakini muonekano wake ni wa kidarja ya pekee, hivyo akamuuliza Umar Ibn Abd Al Aziz: ‘Huyu Mtu anaonekana kua ni mwenye Darja kubwa kutokana na muonekano wake.**’

Hivyo Umar Ibn Abd Al Aziz akasema: ‘***Ewe Amir ul Muuminin*, Huyo ndie Safwan Ibn Sulaym’ Hivyo Khalifa Sulayman Ibn Abd Al Malik akamwambia mfanyakazi wake: ‘Niletee mmoja kati ya ile mifuko yenye Dirham 500’ na kisha alipoletewa basi akamuamrisha mfanyakazi wake huyo kua mfuko huo apewe Safwan Ibn Sulaym akishamaliza kusali, kwani alikua akisali pembeni kwa upande mwengine.’ ‘Baada ya Safwan Ibn Sulaym kumaliza kusali basi Mfanyakazi huyo akampelekea mfuko huo ambapo nae Imam Safwan Ibn Sulaym akasema kwa kuuliza: ‘Naam ulikua unashida nami?’ ambapo mfanyakazi huyo akasema: ‘Amir ul Muuminin amenituma niupe huu mfuko wako wenye Dirham 500 ndani yake’ Safwan Ibn SulaymI akasema: ‘La itakua mmekosea, kwani sio mfuko wangu.’’**

Yule mfanyakazi akamuuliza: ‘Kwani wewe si ndie Safwan Ibn Sulaym?’ Sufyan Ibn Sulaym akasema: ‘Ndie’ Mfanyakazi akasema: ‘Basi hatujakosea ndie wewe uliekusudiwa na *Amir ul Muuminin.’* Hivyo Safwan Ibn Sulaym akasema: ‘Kama ni hivyo basi mimi siwezi kuzipokea’ yule Mfanyakazi akasema: ‘We kamata tu huu mfuko.’ Safwan Ibn Sulaym akasema: ‘La siwezi’ kisha Safwan Ibn Sulaym akanyanyuka na kuchukua Viatu vyake na hakurudi tena Msikitini hapo hadi aliposikia kua Khalifa Sulayman ameondoka kutoka katika Mji wa Madina.’

Kuna mtu alifunga safari kutoka katka Mji wa Dimashq na kuelekea katika Mja wa Madina, na alipofika basi akaulizia kwa kusema: ‘**Mimi nataka kuonana na Safwan Ibn Sulaym, wa sababu nimemuona kwenye Ndoto yangu akiwa ni mwenye kuingia Peponi.’**

Hivyo Mtu huyo akaulizwa: **‘Ilikuaje mpaka ukamuona Safwan Ibn Sulaym mkiwa Peponi kwenye Ndoto yako ulifanya nini?’** hivyo mtu huyo akasema: **‘Labda**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

inawezekana ikawa ni kwa sababu ya Shati' watu wakamuuliza: 'Shati limefanya nini?' ambapo mtu huyo akasema: 'Nilikuja katika Mji wa Madina katika usiku wa kipindi cha kipupwe, nikaingia katika Masjid An Nabawwi na kisha nilipotoka nikamuona Masikini akiwa amejikunyata hana nguo anaona baridi, nami nikavua Shati langu na kumvisha.'

Amesema Safwan Ibn Sulaym kua: '**Katika siku ya Vita vya Uhud, Ibilisi alimtokezea Abd Allah Ibn Hanzala *Radhi Allahu Anhu* na akamwambia: 'Ewe Abd Allah hakika kama utanisikiliza mimi basi mimi nitakufundisha jambo zuri sana' hivyo Abd Allah akasema: 'La hakika mimi sina haja ya kua na Mwalimu' Ibilisi akasema: 'Ewe Abd Allah Ibn Hanzala nitakuambia mimi ukitaka usitake kua, usimuombe yeyote yule zaidi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na angalia hali yako unapokua na hasira, na jilinde katika kila kitu chako au mimi nitakudhibiti wewe. ''**

IMAM TALHA IBN MUTARRIF

Imam Abu Muhammad Talha Ibn Mutarif alizaliwa pia mwanzoni mwa karne ya kwanza ya Kiislam katika ardhi ya Kufah nchni Iraq. Imam Talha Ibn Mutarrif alisoma kwa Masahaba wakiwemo Malika Ibn Anas, Abd Allah Ibn Ubay *Radhi Allahu Anhum* na pia alisoma kwa Wanazuoni wa Tabiina ambao ni pamoja na Imam Zayd Ibn Wahb, Imam Said Ibn Juabayr, Imam Said Ibn Abd Rahman, Imam Mujahid, Imam Abu Is-haq, Imam Al Amash na wengineo.

Imam Talha Ibn Mutarrif alikua na Ilm Kubwa ya Hadith na pia ya Qiraa cha Qur'an, kwani alikua kwa watu wa Mji wa Kufah basi akijulikana kama pia kama *Sayyid Al Qurra* yaani Bwana wa Wasomaji wa Qur'an, alikua ni Thiqah na mwenye Taqwa.

Ambapo amesema Imam Al Ijli kua: '**Hakika Ibn Mutarrif ni mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa sana ni ni miongoni mwa watu wa Kufaf Waliochaguliwa** ' na akasema Imam Abu Masir kua: '**Ibn Mutarrif ni Mwanazuoni mwenye uadimu wa aina yake'**

Katika wakati wa uhai wake basi watu walikua wakimisifu sana Imam Talha Ibn Mutarrif kua ni mwenye Ilm kubwa kuliko wote katika mji wa Kufah, hivyo kila habari hii ilipokua inamfikia basi nae alikua anaamua kuenda kwa Mwanazuoni yeyote yule amjuae Mjini humo ambae ni mwenye Wanafunzi wengi, na kisha hua ni mwenye kupiga magoti mbele yake Mwanazuoni huyo ili asomeshwe nae, safari moja Imam Talha Ibn Mutarrif aliamua awe ni mwenye kuenda kwa Imam Al Amash kwa ajili ya

Kusoma Qur’an na hivyo kua ni mwenye kuwaonesha watu kua, hivyo wafikiriavyo juu yake kua sivyo.

Miongoni mwa Hadith alizozinukuu Imam Talha Ibn Mutarrif ni ile isemayo kua: **‘Amesema Murra Ibn Shurahbil kua amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipewa Vitu vitatu katika safari yake ya Miraj, ambavyo ni Sala Tano, Aya 2 za Mwisho za *Surat Al Baqara* na Kusamehewa kwa Dhambi kubwa kwa Waumini wake wale wasiomshirikisha *Allah Subhanah wa Ta’ala.’’***

Imam Talha Ibn Musarrif alikua ni Mtu Mcha Mungu sana na mwenye kujiepusha na vya haramu kiasi ya kua, siku moja alikua amefunga, na nyumbani kwake ilikua hakuna chakula isipokua Nyama ambayo hata hivyo hakuna jiko la kuipikia, na mke wake alikua anataka kuipika Nyama hio kwa ajili ya iftar, hivyo akaja mfanyakazi wa Jirani ambae alikua amekuja na jiko kwa ajili kuomba moto wa kupikia, hivyo Mke wa Imam Talha Ibn Mutarrif akamuomba Mfanyakazi huyo jiko hilo apikie Nyama hio kwanza kisha atampa na moto wake, na mfanyakazi huyo akakubali na nyama ikapikwa, kisha mfanyakazi akapewa jiko lake na moto wake akarudi kwa ajili ya kupika kwao.

Imam Talha Ibn Mutarrif alipopata habari hii basi ingawa alikua amefunga na nyumbani hakuna Futari basi aligoma kula Nyama hio na alipoulizwa kwanini basi akasema: ‘**Siwezi kuila kwa sababu Jiko lililopikiwa limepikiwa bila ya kupatikana ruhusa ya mwenye jiko, na kisha ulimzuia mfayakazi kukusubiri bila ya kuomba ruhusa ya anaemlipa mfanyakazi huyo**, **hivyo siwezi kuila Nyama hii, bila ya Idhini ya Jirani yangu.’**

Imam Talha Ibn Mutarrif alikua mfanya biashara lakini baadae akaachana na Biashara kwa kusema kua: ‘Sijisikii kua na uadilifu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* ambae ni mwenye kuna na kujua kila kitu, jee itakuaje pale Waislam wenzangu watakaposema kua mimi nawauzia ghali bidhaa zangu?’

Imam Talha Ibn Mutarrif alikua si mtu anaeonekana akiwa ni mwenye kucheka kwani kila wakati alikua ni mwenye kujawa na huzuni kutokana na kutafakkari kwake juu ya Mola wake na kitakachofuata katika siku ya Malipo.

Kutokana na Ucha Mungu wake basi Imam Talha Ibn Mutarrif alikua anaona kua haifai kabisa kuzugvumza kuhusiana na jambo ambalo Wanazuoni wametofautiana juu yake, na alikua hataki kabisa kusema kua Wanazuoni wametofautiana, kwani alikua akisema kua: **‘Hakika sisi tumekutana watu wakubwa sana kiasi ya kua kama ungewaona na kisha kuanza kujifananisha nao basi ungeona na sisi si chochote si lolote mbele yao.’** Kisha akaendelea kusema: **‘Kumkosoa mtu husababisha Uadui kua ni wenye**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kutokea kwenye Moyo wa Mtu husika dhidi ya aliekosolewa, ambapo hilo sio jambo kubwa sana kama kua na kinyongo.'

Kua Mkarimu kwa Mtu Mjinga, kwani kufanya hivyo hukupelekea wewe kua ni mwenye kujilinda na Moto.

Kama mtu anakufuata na kukuomba Msamaha baada ya kukukosea basi mpokee kwa Tabasamu.

IMAM AL QARI NAAFI IBN NUAYM

Imam Abu Ruwaym Ibn ʿAbd ar-Rahman Ibn Abi Naʿim al-Laythi maarufu kama Naafi Ibn Abi Nuaym alikua ni Imam Naafi wa pili wa mji wa Madina ambae pia alikua ni Mwalimu wake Imam Malik Ibn Anas lakini yeye alikua ni mtaalamu mahiri zaidi wa Ilm ya Qiraa cha Qur'an, kwani yeye ni mmoja kati ya Wanazoni 7 wa Ilm ya Qiraa kinachotambulika Ulimwenguni.

Ingawa Imam Naafi alikua ni mwenye asili ya Isfahan nchini Iran lakini yeye alizaliwa a kukulia katika Mji wa Madina na alisoma Ilm ya Qiraa kwa Wanazuoni Tabiina wafikao 70 na pia alisoma Ilm ya hadith ambapo kwa upande wake nae basi wanasema Wanazuoni wa Hadith kua hakua na Hadithi isiyokua si sahih hata moja. Ambapo kuhusiana na Ilm ya Qiraa basi aliulizwa Imam Malik Ibn Anas na Abu Said Abd Ul Malik Ibn Qurayb Al Asmai kuhusiana na *Bismi Allah* basi alisema: '**Katika Kila Fani ya Ilm, basi waulize wenye kujua juu yake, ambapo kuhusiana na Naafi basi yeye ni Imam wa watu wenye Ilm ya Qiraa.**'

Imam Naafi alikua ni Imam wa wanazuoni wa Qiraa kwa mji wa Madina kwa muda wa miaka 70, na hivyo mamia ya watu kutoka katika sehemu mbali mbali walikua wakienda kwake kwa ajili ya kusomeshwa nae Qiraa cha Quran katika mji wa Madina, na hivyo hiki kua ndio kinachojulikana kua ni Qiraa cha Madhhab ya Imam Malik na watu wa Madina, ambacho leo hii ni Qiraa kinachopendwa na Wafasi wa Madhhab ya Imam Malik katika maeneo ya Qatar, Morocco, Tunia, Algeria na Magharibi mwa bara la Afrika.

Ambapo anasema tena Imam Malik Ibn Anas kua: '**Qiraa cha Nafii ni Sunnah na hakuna kitu cha ajabu juu yake**'

Na alisema Imam Al Layth kua: **'Mimi nilienda katika Ibada ya Hija ya mwaka 113 Al Hijra na Imamu wa Watu wa Madina alikua ni Naafi.'**

Ama kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi aliulizwa na Mtoto wake aitwae Abd Allah: **‘Hivi Jee ni Qiraa gani kinachokuvutia zaidi’** ambapo Imam Ahmad Ibn Hanbal akasema: **‘Qiraa cha Watu wa Madina.’**

Ambapo Abu Amr Ad Dani alisema kua: **‘Kuna mtu miongoni mwa waliosoma Qiraa cha Naafi alisema kua: ‘Wakati Naafi anaposoma Qura’n basi harufu ya Misk hua inahanikiza kutoka Mdomo mwake’ nami nikamuuliza Imam Naafi: ‘Ewe Abu Abd Allah hivi jee hua unatumia Manukato wakati unapokaa na kuwasomesha watu?’’**

Imam Naafi akasema: **‘La hata siyagusi manukato, isipokua mimi nilimuona kwenye ndoto zangu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa ni mwenye kunisomea Qur’an ndani ya Mdomo wangu na kuanzia hapo basi nikawa nahisi harufu ya Manukato kutoka mdomoni mwangu ninaposoma Qur’an’**

Anasema Imam Said Ibn Musayyib kua: **‘Imam Naafi aliambiwa. Mashaa Allah Uso wako una Nuru na mwili wako unaonekana mzuri kila siku’** ambapo Imam Naafi akajibu: **‘Na kwanini isiwe hivyo wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amenipulizia mimi mdomoni wakati nikisoma Qur’an ndani ya usingizi wangu?’**
Imam Naafi Ibn Nuaym alifariki mnamo mwaka 169 Al Hijra.

IMAM AMR IBN DINAR 46 AH

Imam Abu Muhammad Amr Ibn Dinar Al Jumahi alizaliwa katika waka 46 Al Hijra katika ardhi ya Mji wa Makkah, na alikua ni mwenye kutokana na familia ya Watumwa waliokua wanamilikiwa na ukoo wa Banu Jumah, na alisoma kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Amr Ibn Al Aas, Jabir Ibn Abd Allah, Abd Allah Ibn Umar, Abd Allah Ibn Jafar, Urwa Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhum* na wengineo na pia alisoma kwa Imam Ataa Ibn Abi Rabah na Imam Tawus Ibn Kaysan.

Ambapo baada ya kufariki Imam Ata Ibn Abi Rabah basi Imam Amr Ibn Dinar akachaguiwa kua Mufti wa Mji wa Makkah ambapo nae akakataa na hivyo akachaguliwa Mufti mwengine ambae alikua ni Imam Qays Ibn Sad lakini hata hivyo Qays Ibn Sad hakukaa kwa mda nae akafariki hivyo Imam Amr Ibn Dinar akachaguliwa tena kuushika wadhifa huo na hivyo ikambidi mara hii akubaliane na kubeba majukuu ya wadhifa huo.

Imam Amr Ibn Dinar alikua ni mwenye kutoa Fatwa katika Mji wa Makkah kwa mda wa miaka 30, kwani Imam Amr Ibn Dinar alikua ni Chombo kilichosheheni Ilm na miongoni mwa Wanafunzi wake wakuu Imam Amr Ibn Dinar alikua ni Imam Sufyan

Ibn Uyaynah ambae alikua pia akiziandika Hadith za Mwalimu wake huyo, ingawa Imam Amr Ibn Dinar mwenyewe alikua akisema: **‘Wakati mimi nilipokua nnasoma katika umri kama wako sikiwa ni mwenye kuandika Hadith, bali nilikua ni mwenye kuzihifadhi Moyoni tu.’**

Na anasema Suwayd Ibn Sad kua: **‘Sufyan Ibn Uyaynah alisema kua: ‘Mtu wa kwanza kunitia moyo moyo kusomesha Hadith alikua ni Abu Hanifa, pale nilipotembelea Mji wa Kufah ambapo yeye alinitangazia kwa kusema: ‘Huyu Bwana ana hadithi nyingi sana kutokea kwa Amr Ibn Dinar’ na hivyo watu wakaanza kunizunguka na mimi nikaanza kuwanukulia.’’**

Ambapo anasema Imam Shu’bah kua; **‘Hakika mimi sijawahi kuona Mtu ambae ni mwenye kuaminika kwenye Hadith zake kama Amr Ibn Dinar kutokea kwa Sufyan Ibn Unaynah. Kwani Amr Ibn Dinar alikua ni Mwanahadith na Mwanafiqh.’**

Abd Allah Ibn Abi Najih alisema kua: **‘Sijawahi mimi kuona mtu mwenye Ilm kubwa kama Amr Ibn Dinar, kwani alikua hafikiwi na Tawus, wala Mujahid wala Ataa.’**

Ambapo Abd Abd Allah Ibn Muhammad Al Zuhri anasema kua: **‘Ametuambia sisi Sufyan kua, amesema Ibn Abi Najih kua: ‘Hakuna mwenye Ilm kubwa zaidi katika ardhi yetu na maeneo mengine kama Amr Ibn Dinar.’’**

Na Imam Abd Allah Ahmad Ibn Hanbal anasema kua: **‘Amesema baba yangu kua, amesema Sufyan Ibn Uyaynah kua: ‘Amr Ibn Dinar alikua akiugawa Usiku wake katika sehemu tatu, ambapo ya kwanza alikua akilala, ya pili alikua akisoma Hadith ndani yake na ya tatu alikua akisali.’’**

Ambapo amesema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: **‘Mimi nilimuuliza Masa’r: ‘Hivi Jee umemuona nani mwenye ilm Kubwa ya Hadith zaidi ya niliemuona mimi?’ Ambapo nae akasema: ‘Mimi sijaona mwenye Ilm kubwa ya Hadith kama Al Qasim Ibn Abd Rahman na Amr Ibn Dinar.’’**

Imam An Nasai Amesema kua**: ‘Amr Ibn Dinar ni Mwenye kuaminika na ni Thiqah.’**

Anasema Ali Ibn Hasan An Nasai kua: **‘Amesema Sufyan Ibn Uyaynah kua: ‘Amr Ibn Dinar alikua anaumwa, hivyo Al Zuhri akamtembelea, na aliponyanyuka na kutaka kuondoka basi akasema: ‘Mimi sijaona Mtu Mzee anaesikiliza Hadith kutoka kwa huyu’’’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na kwa upande wa Imam Ibn Al Mahdi basi yeye anasema kua: **'Mimi sikuwahi kumuona mtu mwenye ilm kubwa kama Imam Abu Hanifa kwani kupitia kwake ndio tumemjua Amr Ibn Dinar'**

Imam Bukhari amesema kua: 'Amesema Ali Ibn Maldini kua: **'Amr ana takriban Hadithi 400' nami nikasema: 'Mimi nnajua kua Ibn Uyaynah amenukuu Hadith 950 kutoka kwake, hivyo labda yeye Ali alikusudia ni Musnad tu.'**

Anasema Al Waqidi kua: **'Imam Amr Ibn Dinar alifariki mnamo mwaka 125 Al Hijra akiwa na umri wa miaka 80'**

IMAM IYAS IBN MUAWWIYAH 46 AH

Imam Abu Wasil Iyas Ibn Muawwiyah alizaliwa mnamo mwaka 46 Al Hijra, hivyo Imam Iyas Muawwiyah alikua ni Mjuku wa Sahaba, na alisoma kwa Sahaba Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu,* Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu,* akasoma kwa Imam Said Ibn Musayyib Imam Said Ibn Jubayr n.k ambapo nae aliwasomesha Maimamu wengi wakiwemo kina Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Shu'bah, Imam Daud Ibn Hind na wengineo.

Imam Abu Wasil Iyas Ibn Muawwiyah alikua ni Mwanazuoni mwenye Ilm kubwa sana, ya Qur'an, Hadith, Fiqh, Firasat na kadhalika na alikua na ufahamu mpana, upeo mkubwa wenye kuona mbali, hikma na busara kiasi ya kua mfano wa mithili ya maumbile yake ilikua ni wenye kutumika kwenye Mashairi ya Lugha ya Kiarabu, na hivyo haishangazi kuona kua *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Abd Al Aziz alipoingia Madarakani basi alimteua Imam Iyas Ibn Muawwiyah kua ndie Qadhi wa Mji wa Basra.

Ambapo Amir Ul Muuminin Umar Ibn Abd Al Aziz alimuandika barua Gavana wake aitwae Adiy Ibn Aata kumwambia kua: '**Muite Iyas Ibn Muawwiyah na Qasim Ibn Rabia Al Hirasi halafu chagua miongoni mwao yeyote yule atakaekua na uwezo wa kua Qadhi'** hivyo wawili hao waitwa mbele ya Gavana huyo.

Ambapo katika kuzungumza kwao na kuambiwa walichoitiwa basi Imam Iyas Ibn Muawwiyah akasema: '**Kwanini juu ya hili usiwaulize Wanazuoni wakubwa wa Mji huu wa Basra ambao ni hasan Al Basr na Muhamamd Ibn Sirin?**'

Ingawa hata Imam Qasim Ibn Rabiah mwenyewe alikua anajua kua Imam Hasan Al Basr na Imam Muhamamd Ibn Sirrin wakiulizwa juaa ya suali hio basi watasema kua aliekua juu Kiilm ni Imam Iyas Ibn Muawwiyah. Hivyo Imam Qasim Ibn Rabiah

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

akasema: **‘Wa Allahi Iyas Ibn Muawwiyah ana I’lm kubwa zaidi yangu, na ni mwenye Hikma zaid na Busara zaid yangu mie, na hivyokama itakua mimi nasema uongo asi bila ya shaka sistahki kua Qadhi kwa sababu Qadhi hatakiwi kusema uongo, na kama maneno yangu ni ya kweli basi bila ya shaka, maneno yangu hayo itabidi yakubalike kua Iyas Ibn Muawwiyah ndio anastahiki kua awe Qadhi wa Basra kuliko mimi.**’

Hibyo Gavana huyo akamgeukia Imam Iyas IbnMuawwiyah na kumwambia: ‘**Umeona Hakika wewe ndie unaestahiki kua Qadhi Mkuu wa Basra, na ndio umeshakua’** na hivyo Imam Iyas Ibn Muawwiyah akawa Qadhi wa Basra.

Ambapo anasema Imam Iyas Ibn Muawwiyah kua: **‘Sisi tulikua pamoja na Umar Ibn Abd Al Aziz *Radhi Allahu Anhu* na watu wakawa wanazungumzia kuhusiana na maisha mbele yake.ambapo nae akasema: ‘Haya ni Sehemu ya Dini, na ukweli ni kua Haya ndio Dini yenyewe hasa’’ na kisha mimi nikafafanua kua: ‘Babu yangu alisema kumwambia Baba yangu kua: ‘Sisi tulikua mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na hivyo Masahaba wakasema: ‘*Ya Rasul Allah*, Jee Haya ni sehemu ya Dini? Si nido?’ ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Naam, na ukweli hasa Haya ni ndio Dini yenyewe hasa’’’**

Imam Iyas Ibn Muawwiyah anasema kua: **‘Yeyote yule asieijua Haya basi hua ni Mjinga’** na akasemapia kua: **‘Tende zilizopea hua ni zenye kuuburudisha Ufahamu’**

Alisema Imam Iyas Ibn Muawwiyah anasema : ‘**Mimi wakati ninapokua nnazungumza na watu basi hua natumia nusu ya Ufahamu wangu kuwasikiliza na nusu kutoa hukumu juu ya wanayoyazungumzia baina ya watu wasioelewana, hua ni mwenye kuskiliza na kua na umakini sana katika jambo husika. Hua ni mwenye kua na tahadhari sana ninapokua nazungumza na watu wasiokua na Imani, wenye Imani dhaifu na pia wenye mitizamo potofu.**’

Siku moja Muawwiyah aliulizwa kuhusiana na Mtoto wake, yaani Imam Iyas na hivyo nae akajibu: ‘**Mtoto wangu ni Kijan mzuri sana ni mwenye kusimamia mahitaji yangu, sina tatizo nae na pia ni mwenye kuniongoza kuhusiana na mambo ya Kiakhera, Alhamd Lillah nami ni mwenye kutekeleza majukumu yangu vizuri kwa kadiri niwezavyo’**

Safari moja Imam Muawwiyah alimsikia Yahudi mmoa akiwa anasema mbele yake kua: **‘Wajinga sana hawa Waislam, watu ambao ni wenye kujiita ua ni watu wa Peponi, kwani hua ni wenye kula na bila ya kua ni wenye kukatishi Udhu wao katika kula kwao’**

Hivyo Imam Iyas IbnMuawwiya akamuuliza Yahudi huyo: **‘Hivi Jee nyinyi hua mnaenda kutia Udhu kila baada ya kula chakula chenu?’ ambapo Yahudi huyo akasmea: ‘La’**

Hivyo Imam Iyas Ibn Muawwiyah akasema: **‘Naam, hivyo badhi ya vitu wanavyokula Waislam hua ni Vyakula, na *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni wenye uwezo juu ya kila kitu. Hivyo amejaalia kua kila kinacholiwa na Watu wa Peponi kua ni Chakula, hivyo hua hakitengui Udhu wao.’**

Na baada ya Jibu hilo basi Yahudi huyo akakaa kimya.

Imam Iyas Ibn Muawwiyah alitembelea katika Mji wa Wasit, na alipofika kwenye sehemu yenye uwanja mpana hivi, akaona kua kwenye Uwanja huo kuna mapande mawili ya vigae, hivyo akasema kua: ‘**Chini ya Mapande mawili haya kuna kiumbe’** hivyo watu waliokuwepo hapo wakayanyanyua mapande hayo na chini yake wakakuta Nyoka amejificha chini yake, hivyo watu wakashangaa na kumuuliza:

‘Ilikuaje hadi ukajua kua kuna kiumbe hapa chini yake?’ ambapo nae akasema**: ‘Katika eneo lote hili imi nilikua nnaona kua kuna ukavu isipokua pembeni ya magae haya mawili na hivyo nikajua kua hapa lazima itakua kuna kiumbe’**

Na siku Imam Iyas Ibn Muawwiyah. Alikua safarini naakafika kwenye sehemu ya maji ambao mara akasikia kuna mbwa wanabweka, Imam Iyas Ibn Muawwiyah akakaakimya kisha kasema: **‘Katika hili eneo kutakua kuna mbwa mgeni’ akaulizwa: ‘Kwanini?’ ambapo nae akasema: ‘Kwa sababu nasikia kuna mbwa wanabweka, ambapo mmoja wao anabweka kwa sauti ndogo lakini wengine wanabweka kwa sauti kubwa.’** Hivyo watu wakatoka kuendak uangalia kwenye milio ya mbwa hao nawaliporudi wakasema: **‘Kweli, kuna mbwa mpya amefungwa kwenye sehemu na kishakuna mbwa wa hapa wanambwekea.’**

Kuna siku nyengine pia alikua njiani na kisha akaona tundu Ardhini na hivyo akasema: **‘Hapa itakua kuna Mnyama’** alipoulizwa kwanini basi akasema: **‘kwa sababu wanyama wadogo hua ni wenye kuichimba Ardhi au wenye kuitoboa Miti’**

Na katika safari zake Imam Iyas Ibn Muawwiyah alisafiri na hivyo wakaishiwa na Maji, watu wake wakatafuta maji hadi wakachoka bila ya kuyaona katika sehemu hio. Lakini mara Imam Iyas Ibn Muawwiyah akasikia Mbwa anabweka, hivyo akasema: **‘Huyu Mbwa atakua yupo kwenye sehemu ambayo ina kisima mtafuteni’** hivyo watu wake wakamtafuta mbwa huyo hadi wakamuaona na kisha wakarusi na Maji, hivyo wakamuuliza Imam Iyas iBn Muawwiyah, jee alijuaje, ambapo nae akasema: **‘Kwa sababu mlio wa ubwekaji wake ulikua unaonesha kua kama anatoka Kisimani’**

IMAM IBRAHIM AN NAKHAI 46 AH

Imam Abu Ammar Ibrahim Ibn Yazid Ibn Al Aswad Ibn Amr Ibn Rabiah Ibn Harithah Ibn Saad Ibn Malik Ibn Nakhai alizaliwa mnamo mwaka 46 Al Hijra katika ardhi ya Iraq.

Imam Ibrahim An Nakhai alikua ni Mwanafunzi wa Masahaba wakiwemo Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* na pia alikutana na Umm ul Muuminina Aisha Radhi Allahu Anha, na pia alisoma kwa Wanazuoni wa Tabiina kama kina Imam Masruq Ibn Ajda, Imam Alqamah, Qadhi Shuraykh Ibn Harith Al Kindi, Imam Abd Rahman Ibn Yazid, Imam Abu Zurah na wengineo.

Na hivyo Imam Ibrahim An Nakhai alikua ni mwenye kua na Ilm kubwa sana miongoni mwa Wanazuoni kiasi ya kua katika wakati wa uhai wake alikua akijulikana kama Faqih wa Iraq. Na hii ni kutokana na Ilma yake ya Hadith na Fiqh na Qur'an kwani Hadith zake zimo nyingi sana katika vitabu 6 maarufu vya hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ambapo anasema Imam Amr Ash Shabi kua: '**Kwa hakika katika ardhi za Kufah, Sham, Hijaz hakuna aliekua na Ilm kubwa na ufaham wa Dini kama Ibrahim An Nakhai**'

Ukweli ni kua Imam Ibrahm An Nakhai alikua ni mtu mwenye uwezo mkubwa pia katoka kusomesha na hivyo amechangia sana katika fani ya ilm ya hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na pia alikua ni mtu mpole na mkarimu sana ambapo anasema Ismail Ibn Abi Khalid kua: '**Ilikua Amr Ash Shabi, Ibrahim An Nakhai na Abu Adh Dhuha wanapokaa pamoja Msikitini kusomesha Hadith, basi wengine wanapokwama kutokana na kutojua hua ni wenye kumgeuzia macho Ibrahim An Nakhai'**

Imam Ibrahim An Nakhai pia likua ni mwenye kupenda kufanya Ibada ikiwemo Kufunga ambapo alikua akifunga Funga ya Nabii Daud ambayo ni kufunga siku moja na kuacha siku moja. Na pia alikua ni mwenye kudumu na *Qiyam Al Layl* huku akiwa ni mwenye kuvaa mavazi mazuri na yenye kupendeza na kunukia manukato mazuri wakati anapokua katika Ibada zake za Usiku.

Miongoni mwa Wanafunzi wake Imam Ibrahim An Nakhai wamo pia Imam Hammad Ibn Sulayman. Imam Malik Ibn Anas, Imam Abu Hanifa, Imam Said Ibn Musayyib, Imam Amr Ash Shabi, Imam Al Hakam Ibn Utaibah na wengineo.

Imam Ibrahim An Nakhai alikua ni mnyenyekevu sana na asiependa Umaarufu wala kujumuika na watu wengi bali alikua ni mwenye kupenda kukaa kimyaa peke yake huku akiwa ni mwenye kudumisha ufahamu wake kwenye Dhikr Allah. Ambapo anasema Imam Al Amash kua: '**Siku moja mimi nilikua nimekaa na Ibrahim An Nakhai ambae alikua akisoma Qur'an, halafu mara akatokea mtu na hivyo Imam Ibrahim Ibn Adham akaufunga msahafu wake huku akisema kua: 'Usiniangalie kama hivyo kwani mimi ni kawaida yangu kusoma Qur'an kila saa**''

Kuna wakati Imam Ibrahim An Nakhai alikua akiulizwa masuali basi hua ni mwenye kujibu kwa kusema kua: '**Hivi jee hakuna mtu mwengine wa kuulizwa juu ya hili isipokua mie?**' na pia alikua ni mwenye kusema: '**Baadhi ya wakati mimi hua nna hamu ya kua si mwenye kuweza kuzungumza pale nnapoulizwa kwani hua sina nia ya kujibu ninayoulizwa.**'

Na akasema tena Imam Ibrahim An Nakhai kua: '**Yeyote yule mwenye kutafuta Ilm kwa nia ya kupata ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atampa Ilm itakayomtosheleza.'**

Imam Said Ibn Jubayr alifuatwa na kuulizwa Suali ambapo nae akasema: '**Inakuaje Mnataka Fatwa kutoka kwangu wakati miongoni mwenu mnae Ibrahim An Nakhai?'**

Katika kuonekana kwa Ucha Mungu wake basi Imam Ibrahim An Nakhai siku moja aliazima Punda kwa ajili ya kuelekea katrika safari yake, na alipofika njiani basi akaangusha Fimbo yake, hivyo Imam Ibrahim Ibn Adham akamsimamisha Punda huyo na kisha akashuka na kurudi kuiokota fimbo yake hio, na alipoulizwa kwanini hakurudi na Punda wake basi Imam Ibrahim Ibn Adham alisema: **'Hakika mimi Punda huyu nilimuazima kwa ajili ya kuenda nae tu na wala si kwa ajili ya kurudi nae.**'

Imam Ibrahim An Nakhai alikua ni mwenye kua na Kanzu maalum ambayo aliinunua kwa Dirham 200 ambayo alikua akiitumia kwa ajili ya Ibada za *Qiyam Al Layl* tu.

Imam Ibrahim An Nakhai alifariki mnamo mwaka 96 Al Hijra na kifo chake kiliwahuzunisha wengi sana kwani pia wakati kifo kilipokua kinamkaribia Imam Ibrahim Ibn Adham basi alianza kulia na alipoulizwa kwa nini analia basi alisema: **'Kwanini nisilie wakati namsubiri Mjumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambapo sijajua kama atanibashiria Pepo au Moto?'**

Na anasema Imam Shuayb Ibn Al Habbab kua: '**Hakika mimi nilikua ni miongoni mwa watu waliohudhuria maziko ya Ibrahim An Nakhai, na hivyo Amr Ash Shabi akaniuliza: 'Jee umekuja kumzika Rafiki yako?' Nami nikasema: 'Naam' kisha**

Amr Ash Shabi akasema: 'Wallahi, Ibrahim hakurithisha kitu chochote kwa yeyote yule isipokua Ilm yake, kwani hakuna aliekua na Ilm kubwa na Al Faqih kama yeye.''

IMAM ABD RAHMAN AL SUDDI 49 AH

Imam Ismail Abd Rahman Ibn Abd Al Karimah Al Suddi alizaliwa kabla ya mwaka 49 Al Hijra ambao huu ndio mwaka aliofariki Al Hasan Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* na alizaliwa katika Nyumba ya Zaynab Bint Qays *Radhi Allahu Anha* ambapo ndani yake ilikua ni yenye mazingira mazuri kwa ukuaji na ulelewaji wake katika maadili ya Din ya Kiislam.

Imam Abd Rahman Al Sudi alisoma Masahaba wakiwemo Saad Ibn Abi Waqqas, Abu Said Al-Khudri, Abd Allah Ibn Umar, Abu Huraira, and Abd Allah Ibn Abbas, *Radhi Allahu Anhum.*

Imam Abd Rahman Al Suddi alikua pia akijulikana kwa jina la umaarufu kama Abu Muhammad Al Hijazi na hii ni kwa sababu alizaliwa katika Ardhi ya Hijaz halafu akahama na kuhamia katika ardhi ya maeneno ya Kufah. Imam Abd Rahamn Al Sudi alikua pia akijulikana kwa Jina la Al Suddi kwa sababu alipohamia katika Mji wa Kufah basi alikua akipenda kukaa kwenye Kizingiti cha Msikiti mkuu wa Kufah, kwani kwa kwa Lugha ya Kiarabu hua kinaitwa kama *Sudda*, na pia kuna wasemao kua alikua akikaa katika eneo ambalo lilikua likijulikana kama *Al Sadd.*

Ama kuhusiana na Ilm ya Qur'an basi Imam Al Suddi alikua ni mtaalamu mkubwa wa Tafsir ambapo alisema Ismail Ibn Abi Khalid kua: '**Al Suddi alikua na Ilm kubwa sana ya Qur'an kuliko Ash Shabi**'

Na alisema Imam Yahya Ibn Main kua: '**Hakika mimi sijawahi kusikia mtu yeyote akimzungumzia Al Suddi isipokua kwa wema.**'

Ambapo Imam Salama Ibn Abd Rahman anasema kua: '**Ibrahim An Nakhai alipita katika sehemu ambayo Al Suddi alikua amekaa akitafsiri Qur'an ambapo nae akasema: 'Anatoa Tafsir inayoeleweka kwa Watu.'**'

Imam Al Suddi alikua na Ilm kubwa ya Tafsir kwa sababu ndio iliyokua ikimvutia zaidi na pia kwa sababu Mwalimu wake Mkuu alikua ni Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, ambapo Imam Al Suddi alikaa na kusoma kutokana nae kwa mda wa miaka 29.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na hivyo haishangazi kuona kua Imam Abd Rahman Al Suddi amenukuliwa mara nyingi sana mitizamo yake Kitafsir katika Tafsir ya Imam At Tabari.

Na ingawa alikua na Ilm Kubwa ya Tafsir lakini pia alikua na Ilm kubwa ya Tarikh - Historia na Maghazi yaani Mapigano ya Vita vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na tunapozungumzia kuhusiana na Ilm ya Hadith basi Wanazuoni wanasema kua Imam Al Suddi ni mwenye darja ya tatu katika fani hio, na hii kumaanisha hakua mzuri sana katika fani hio kulingana na vigezo vya Wanazuoni wa Hadith.

Ambapo anasema Imam Ath Thalabi kua: '**Ingawa Imam Al Suddi alikua ni Imam anaeaminika lakini alikua si mtu mwenye umakini katika Hadith'** na ndio maana hadithi zake hazikutikani kwenye Vitabu vya Hadith vya Imam Bukhari na Muslim, bali hua zinakutikana kwenye Vitabu vya Imam An Nasai, Imam At Tirmdhii na Imam Ibn Majah.

Miongoni mwa Wanafunzi wake Imam Abd RahmanAl Suddi ni pamoja na Hussein Ibn Waqid, Sammak Ibn Harb, Imam Ismael Ibn Abi Khallad, Asbat Ibn Nasr, n.k

Imam Al Suddi alifariki mnamo mwaka 102 Al Hijra.

IMAM ATAA AL KHURASAN 50 AH

Imam Abu Muhammah Ataa Ibn Abd Allah Ibn Maysara Al Khurasani alizaliwa katika mwaka wa 50 Al Hijra katika maeneo ya Mji wa Balkh na ingawa alikua ni mfanyakazi wa Muhallab Ibn Abi Sufra lakini alijitahidi kutafuta I'lm kwa kusafiri na kuishi katika Mji mbali mbali ikiwemo Madina, Dimashq, Jerusalem, nk.

Na hivyo Imam Ataa Al Khurasani alikua na Ilm kubwa ya Qur'an, Hadith na Fiqh kiasi ya kua baadae alikua ni Qadhi Mkuu na Mufti Mkuu wa Khurasan, na alikua mtaalamu mkubwa wa kutoa Fatwa na ni mwenye Ikhlasi katika kila jambo lake kuanzia katika Ibada hadi katika Mapigano dhidi ya Nafsi yake na mapigano dhidi ya maadui wa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani alisoma kwa Masahaba na Matabiina wakiwemo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*, Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu*, Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu*, Imam Hasan Al Basr, Imam Said Ibn Jubayr, Imam Ataa Ibn Abi Rabah, Imam Said Ibn Musayyib, Imam Zaid Ibn Aslam, Amr Ibn Shuayb, Nafii n.k.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo anasema Imam Abd Rahman Ibn Zaid Ibn Aslam kua: **'Baada ya Masahaba kufariki, kina Abd Allah Ibna Abbas. Abd Allah Ibn Amr Ibn Al As na Abd Allah Ibn Zubayr Radhi Allahu Anhum basi Watu wakawageukia Wanazuoni ambapo Ataa Ibn Abi Rabah alikua Qadhi wa Ardhi ya Makkah, Tawus alikua Qadhi wa Ardhi ya Yemen, Hasan Al Basr alikua Qadhi wa Basra, Yahya Ibn Abi Qathir alikua Qadhi wa Yamamah, Makhul alikua Qadhi wa Sham, Ibrahim An Nakhai alikua Qadhi wa ardhi ya Kufa na Ataa Al Khurasan alikua Qadhi wa Khurasan.'**

Ambapo anasema Yaqub Ibn Shaybah kua: **'Ataa Al Khurasan ni mwenye kujulikana sana kwa sifa zenye kuufaisha kwa Ilm, Fatwa na kujitolea kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ni muaminifu na Mcha Mungu wa Mji wa Khurasan.'**

Ambapo anasema Abd Al Rahman Ibn Yazid Ibn Jabir kua: '**Tulikua tukienda Vitani na Ataa Al Khurasani na alikua akiuhuisha usiku wake kuanzia mwanzo wake hadi mwisho wake na halali isipokua kidoogo tu.**'

'Katika wakati wa Usiku Imam Ataa Al Khurasan alikua akituambia kua: '**Kusali katika wakati wa Usiku na Kufunga wakati wa Mchana ni bora kuliko kunyeshwa Usaha, kuvishwa Minyororo ya Moto na kulishwa Zaqqum.**''

Imam Ataa Al Khurasan alikua akisema kua: **'*Qiyam Al Layl* hua ni kiburudisho cha Mwili, ni Nuru ya Nyoyo na Macho na ndio kinachoupa ukakamavu viungo vya Mwili.**'

Ambapo anasema Abu Khalifa kua: '**Ataa Al Khurasan alisali pamoja nasi Sala ya Magharibi, na kisha akauchukua mkono wangu na tukaondoka pamoja na kuniambia: 'Unaona Wakati huu wa baina ya kuzama Jua na Chakula cha usiku hua ni wakati wa mghafiliko na ni wakati ambao Dua hua zinakubaliwa, hivyo wanaosoma Qur'an katika wakati huu na kufanya Dhikr Allah hua ni waliokuwepo kwenye Bustani za Peponi.**''

Mnamo mwaka mwaka 152 Al Hijra Imam Ataa Al Khurasan alienda katika Ibada ya Hija na kisha akaelekea katika Mji wa Jerusalem na hivyo mwanzo mwa mwaka 153 Al Hijra Imam Ataa Al Khurasan alifariki katika maeneo ya Al Quds na akazikwa katika ardhi ya *Bayt Al Maqdis.*

Alisema Imam Ataa Al Khurasan kua: '**Mja hawezi kua huru hata kama atakua ni mwenye kuheshimika na mwenye Mali, hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapomuachia huru kutokana na Moto. Dunia imeitwa Dunia kutokana na Uduni wake ndani yake na Akhera imeitwa Akhera kwa sababu ya kuakhirishwa kwa malipo yake hadi hapo baadae katika wakati ambao hakuna cha kuchuma ndani yake.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ataa Al Khurasan aliwausia watu kwa kusema: '**Hakika mimi nakuoneni nyinyi kua ni wenye kuipenda Dunia, lakini mimi nakupendekezeeni Akhera yenu, hivyo kamwe msiisahau Akhera yenu wakati mkiwa mnashughulikia Dunia yenu. Kwa msione kua mtu ana Mamlaka na Mali hapa Duniani na Kauli yake inasikilizwa na kila Mtu lakini hata hivyo kila kitu chake hakiwezi kumzuia yeye kutokana na kuangukia motoni na kisha kuunguzwa na mto huo.**

Kwani Hukmu hua inatokana na *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hivyo humuadhibu yule amtakae na humuingiza Peponi yule amtakae kwa maana hio basi ni muhimu kwa Mtu kutafuta radhi za *Allah Subhanah wa Ta'ala* hapa Duniani, kwa kua ni miongoni mwa wenye kuamini, wenye kufanya mema na kukatazana maovu na kukabiliana na mitihani itokanayo na hayo kwani Dunia ni sehemu ya Mitihani.'

Na Unapofanya Dhambi basi fanya *Istighfar* baada yake kwa kufanya hivyo hua ni sehemu ya Unyenyekevu kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani yeyote yule mwenye kujidhulumu nafsi yake na kisha akaomba msamaha kwa Mola wake basi atamkuta Mola wake kua ni mwingi wa Huruma na usamehevu kwani iliposhushwa aya isemayo:

﴿وَمَن يَعْمَلْ سُوٓءاً أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ ٱللَّهَ يَجِدِ ٱللَّهَ غَفُوراً رَّحِيماً﴾

Waman yaAAmal soo-an aw yadhlim nafsahu thumma yastaghfiri Allaha yajidi Allaha ghafooran raheeman *(Surat An Nisaa 4:110)*

Tafsir: ***Na yeyote atakaejidhulumu nafsi yake (kwa kufanya dhambi) na kisha akaomba msamaha kwa Allah Subhanah wa Ta'ala basi atamkuta Allah Subhanah wa Ta'ala akiwa ni mwingi wa Usamehevu na Mwingi wa Rehma.***

Basi Ibilisi alilia kwa sauti kali sana ya Maumivu kiasi ya kua jeshi lake lote la ardhini lilimfuata na kumuuliza: 'Jee una hali gani? Kimetokea nini? Mbona umetoa ukelele wa maumivu makali sana' ambapo nae akasema: 'Kuna aya imeshushiwa Ummah wa Muhammad kuhusiana na usamehevu na usamehevu wa Dhambi ambazo mimi nimewasababishia watu wa Ummah huu kutokana na mbinu zangu zote.'

'Kwani katika aya hii *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawaahidi usamehevu kwa hayo na kwa wale wenye kuomba wasamehewe hivyo jee kuna njia gani nyengine ya kuwalaghai? Hivyo nendeni katafuteni njia ya kuwalaghai labda mtaipata huku na mimi ikiwa ni mwenye kuitafuta njia hio.' kisha baada ya Jeshi hilo kutoka basi

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ibilisi akalia kwa sauti kali zaidi, hivyo Jeshi hilo likarudi haraka sana na kuuliza kilichotokea ambapo nae akasema: 'Jee mmeshagundua njia hio?'

Nao wakasema: 'La bado' ambapo Ibilisi akasema 'Nimegundua njia ya kuwalaghai' na alipoulizwa ni njia gani basi akasema: 'Baada ya Mtume wa Ummah huu kuondoka na Makhalifa kwake na Masahaba zake basi tutawashughulisha na uzushi wa kila aina ambao watauona kua ni bora na hivyo watachanganya baina ya Sunna za Mtume wao na Bidaa na hivyo kua ni wenye kudumu zaidi na Uzushi huo na hawatoomba msamaha kwa Mola wao kwa mambo hayo na kisha wataingizwa Motoni kutokan anuzushi huo na hivyo nasi tutakua tumefanikiwa kupata kile tukitakacho'

Imam Ataa Al Khurasan amesema kua: **'Amesema Hasan Al Basr kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kuna Majirani wa aina 3, ambapo jirani wa kwanza ana haki 1, jirani wa pil ana haki 2 na jirani wa 3 ana haki 3''**

Ambapo Jirani wa kwanza ni yule ambae si Muislam na wala si Jamaa huyu hua ana haki moja ambayo ni ya Ujirani.

Jirani wa Pili ni yule ambae ni Muislam lakini si ndugu huyu hua ana haki mbili ambazo ni Haki ya Jirani kwa Jirani yake na Haki ya Muislam kwa ndugu ya kewa Kiislam.

Jirani wa Tatu ni yule ambae ni Muislam na pia ni Ndugu na huyu hua ana haki 3 ambapo haki ya kwanza ni ya Ujirani, haki ya pili ni ya Uislam ya Muislam kwa Muislam mwenzake na haki ya 3 ni ya Udugu ya Ndugu kwa ndugu.

Ambapo haki ya mwisho kabisa kwa Jirani ni ya kutomuadhibu Jirani yako kwa harufu ya Nyama na aina nyengine za chakula chako unachokipika, lakini kama na yeye utampelekea chakula hicho basi hua haihesabiwi kua umemuadhibi kwa harufu yake katika wakati wa kukipika.

Alisema Imam Ataa Al Khurasan kua : **'Mmoja kati ya Wacha Mungu alikua akiandika dhambi zake kwenye kiganja chake na mema yake kwenye kiganja hicho, na hivyo anapokua anapoangalia kiganja chake hicho basi mikono yake hua inatetemeka kutokana na kukumbuka dhambi zake hizo'**

Imam Ataa Al Khurasan anasema kua: **'Mambo matatu hua ni yenye kuhitajika katika kudumisha udugu wa kweli, kwanza kutembeleana mmoja anapokua anaumwa, kusaidiana wanapokua na matatizo na kukumbushana wanaposahau'**

'Mtembelee ndugu yako Mgonjwa hata kama ikiwa yupo umbali wa masafa ya kilomita moja, na nenda kwa ndugu yako kwa ajili ya kupatana nae hata kama ni masafa ya kilomita 2 na nenda kwa hata kwa kilomita 3 kwa ajili ya kumsalimia ndugu yako kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'*

Imam Ataa Al Khurasan alisema kua: **'Ibilisi ana sindano ambayo hua ni maalum kwa ajili ya kuwachoma machoni wapate usingizi pale wanapokua wanafanya *Dhikr Allah.'***

Imam Ataa Al Khurasan aliusia kwa kusema kua: '**Kila siku fanyeni mema kwani mema huyaangamiza maovu, jihesabie kua umeachana nayo maovu kwa sababu ya kua mwishoni utaachana nayo Dunia, jihisi kua kama kwamba umeshayaonja mauti kwani iko siku utayaonja kweli mauti, pale utakapohama kutoka Duniani na kuhamia Akhera, hivyo kuazia sasa hivi jihesabu kua wewe tayari umeshafika Akhera. Kwani hicho ni kituo ambacho kila mtu atafikia. Na kawaida ni kua kila mtu hua ni mwenye kujitayarisha na safari pale anapotaka kusafiri.**

Hua ni mwenye kuchukua kila anachokihitaji katika safari yake hio, hua anajitayarisha na kile kitakachompatia kivuli kutokana na joto la Jua, na Chakula na Kinywaji chake, Nguo zake na Blanketi kwa ajili ya Baridi ya Usiku na kisha huanza safari yake. Na daima hua ni mwenye kuonewa choyo yule ambae ni mwenye kujitayarisha kabla ya safari yake, na asiejitayarisha na safari hua ni mwenye kujuta baada yake. Kwani hua ni mwenye kua na kiu na ni mwenye kukosa maji kwa ajili ya kujikinaisha kiu yake, anapokua anahisi baridi usiku hua hana cha kujihifadhia na kutokana na baridi hio.

Tatizo la Dunia hii ni kua, ni sehemu ya mpito, hivyo siku moja mtu hua na matatizo na siku ya pili matatizo hayo hua ni yaliyokwisha, lakini jee atakua na hali gani atakapokumbana na mitihani ya Akhera? Atakapokutana na maumivu ya Akhera? Hivyo kutokana na hali hii basi yule mwenye Busara hua ni mwenye kujitayarisha vizuri kwa ajili ya Akhera yake kwani ndio kwenye makazi yake ya kudumu. Ambapo katika siku ya Malipo wakati Vitisho vyake vitakapo nguruma na joto la Jua kali halitomuathiri kutokana na kua chini ya Kivuli cha Arshi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kua si wenye matatizo yeyote'

Anasema Imam Ataa Al Khurasan: '**Alisema Imam Abu Al Juwayni kua: 'Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua : *'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akipenda sana mambo manne, ambapo mawili yalikua ni kwa ajili ya Mwili ambayo ni Sala na Funga. Na mawili yalikua kwa ajili ya Mali ambayo ni Jihad na Sadaqah''**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Al Khurasan alisema kua: **‘Dhambi inapofanywa basi inatakiwa ufiatiwe na Allahuma Ighfirlii, kwani kufanya hivyo hua ni kuonesha kujisalimisha na kurudi kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala*’**

Imam Ataa Al Khurasani alisema pia kua: **‘Moto una Milango 7, ambapo Mlango wenye harufu mbaya na moto mkali sana ni ule ambao anaingizwa yule ambae ni mwenye kujua kua Zina ni Haram na kisha akazini.’**

Na akasema tena kua: **‘Udugu hua ni kuwajibika kulingana na hali tatu. Kwanza ni kutembeleana mmoja wao anapokua naumwa, Pili ni kusaidiana pale mmoja wapo anapokua amekwama na Tatu ni kukumbushana pale mmoja wapo anaposahau.’**

Na pia akasema kua: ‘**Mtembelee ndugu yako anaeumwa hata kama yuko kwa umbali wa kilomita 1, Wapatanishe ndugu zako waliogombana hata kama watakua wapo kwa umbali wa kilomita 2 na Mtembelee ndugu yako unaempenda kwa ajili ya *Allah Subhaanah wa Ta’ala* hata kama yuko umbali wa kilomita 3.’**

Imam Ataa Al Khurasani alisema kua: **‘Hakika mimi nnaona kua Kua na Ilm na kisha kuelezea kuhusiana na Maamrisho na Makatazo ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa watu kua ni ninaloliamini zaidi.’**

Na akasema tena kua: **‘Mikusanyiko ya Dhikr hua ni sehemu ambazo *Allah Subhanah wa Ta’ala* amejaalia kua ni zenye kukumbushana kuhusiana juu ya halali na haramu.’**

Na pia akasema: **‘Waliotangulia kabla yetu walikua wakiandika Dhambi zao na Mema yao kwenye mikono yao, na kisha wanapoangalia mikono yao na kukumbuka Madhambi na Mema yao basi mikono yao hua ni yenye kutetetemeka.’**

IMAM DAUD AT TAI 50 AH

Imam Abu Sulayman Siraj Ad Din Daud At Tai alizaliwa katika Mji wa Kufah nchi Iraq na alitokana na Kabila la watu wa At Tayy ambao ni wenye asili ya maeneo ya Khurasan.

Imam Daud At Tai alianza kusoma tangu katika wakati akiwa mtoto mdogo kupitia kwa Wanazuoni mbali mbali wakiwemo kina Imam Abd Ul Malik Ibn Umayr, Imam

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Sulayman Ibn Amash, Imam Habib Ibn Abi Amri, Imam Abd Rahma Ibn Abi Layla, Imam JafarAs Sadiq, Imam Abu Hanifa na wengineo.

Na ingawa alikua ni mwenye kuipata Ilm hio wakati akiwa mdogo lakini hata hivyo alikua si tu mwenye kupenda kuachana na Dunia yake hadi pale siku moja alipokua anasikiliza nyimbo ambayo ilikua inasema: ‘**Una Uso wenye Sura Nzuri ambao haukuweza kua Udongo, na macho ya kupendeza ambayo hayjaanguka kwenye udongo**’ ambapo baada ya kusikia maneno hayo basi akamua kuachana na Dunia yake kwani ilikua ikimwamsha kua kila kitu mwisho wake kitaangukia kwenye udongo.

Hivyo Imam Daud At Tai akaelekea kwenye mji wa Baghdad ambapo alikutana na Imam Nuuman Ibn Thabit yaani Imam Abu Hanifa na akaanza kusoma kwake kwa mda wa mwaka mmoja, huku akiwa si mwenye kujichanganya na watu hadi pale Imam Abu Hanifa alipomwambia kua inabidi ajichanganye na Wanafunzi wake wengine na hivyo baada ya mwaka mmoja kumalizika basi Imam Daud At Tai alaamua kubakia kwa Imam Abu Hanifa na hivyo akaamua kubakia kwake ambapo alibakia na kusoma kwa mda wa miaka 20 an kufikia darja ya kua ni mwenye uwezo wa kufanya Ijtihad.

Imam Daud At Tai alisoma pia kwa Imam Ismail Ibn Aliyyah, Imam Abu Nuaym Al Fadhl Al Ibn Dukyan, na pia kwa Imam Jafar As Sadiq ambapo siku moja Imam Daud At Tai alimwambia Imam Jafar As Sadiq kwa kusema kua: ‘**Ewe Mjukuu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hivi kwanini mimi nnahisi kua Moyo wangu una kiza? Jee unanishauri nini?**’

Imam Jafar As Sadiq akasema: ‘**Wewe ni miongoni mwa wanaojitolea kuhusiana na wakati wao kwa ajili ya Mola wao hivyo inakuaje unaniuliza mimi hivyo?’**

Imam Daud At Tai akasema: ‘**Ewe Mjukuu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nakuuliza kwa sababu wewe una damu tukufu ndani ya mwili wako na hivyo una darja ya juu zaidi ya watu wengine, hivyo nataka kujua ushauri wako**’

Imam Jafar As Sadiq akasema: **‘Ewe Daud hakika katika siku ya Malipo sitoulizwa kuhusiana na babu yangu kua ni *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* bali nitaulizwa kwanini sikushikamana na Dini ya Uislam ipasavyo? Kwani Uislam haunasibishwi na kua ni mwenye kutokana na ukoo wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, bali ni kutokana na Kutekeleza Maamrisho ya *Allah Sabhanah wa Ta’ala* na kauchana na Makatazo yake, hivyo mimi nnakhofia juu ya hili zaidi.’**

Hivyo Imam Daud At Tai akaanza kulia na kusema: **‘Ya Allah kama ikiwa hali iko hivyo kwa huyu mtu ambae amebeba damu tukufu ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* jee hali yangu mie Daud At Tai itakuaje?’**

Kutokana na kua ni mwenye kuthamini muda wake basi Imam Daud At Tai alikua katika wakati wa Kula basi hachukui Mkate kisha akauchovya ndani ya Maji au Maziwa na kisha akala kwa kutafuna, bali alikua akiuchukua mkate kisha huutia ndani ya maziwa au chai na kisha huuwacha ulainike na kisha huunywa kama uji kwani alikua akisema kua: '**Baina ya mda wa kuchuua mkate na kuuchovya ndani ya Maji na kuuliza na kuuchovya tena basi mimi hua nnao uwezo wa kusoma aya 50 za Qur'an baina yake hivyo kwanini nipoteze mda wangu?**'

Imam al Ayyash Anasema kua: '**Mimi nilienda kumtembelea Daud At Tai na nikamkuta akiwa amekamata kipande cha Mkate huku akiwa analia. Nami nikamuuliza kwanini analia?' ambapo nae akasema: 'Nnataka kukila kipande hiki cha mkate lakini sijui kama kina shimo ama la.'**

Imam Daud At Tai alikua hana mke hivyo aliulizwa kwanini hakuoa, na akajibu: **'Kwa sababu sitaki kumlaghai Muumini wa Kike'** akaulizwa : **'Kwanini utakua umemhadaa'** nae akajibu: **'Kwa sababu nikimuoa Mwanamke basi itakua tayari nimeshaahidi kua nitamsimamia mambo yake yote ya Akhera na Dunia wakati mimi sina uwezo huo, hivyo kufanya hivyo itakua ni sawa na kumlaghai.'**

IMAM MAKHUL AL SHAMI 50 AH

Imam Abu Abd Allah Makhul Al Hudhali Ibn Abi Muslim Shahraab Ibn Shazil Ibn Sanad Ibn Sherwan Ibn Yazdak Ibn Yaghouth Ibn Kisra Al Shami alizaliwa katika Ardhi ya Mjini Kabul Afghanistan, ambapo alipokua mdogo alikamatwa na kuuzwa na hivyo kua Mtumwa aliekua akiuzwa na kununuliwa na Mwanamke wa Al Hudhaliyah aliekua akiishi katika ardhi ya Misri, ambapo baadae mwanamke huyo alimuachia huru Imam Makhul.

Ambapo anasema Imam Al Makhul kua: '**Nimetembea ardhini kwa ajili ya kutafuta Ilm baada ya kuachiwa huru katika ardhi ya Misri, nikaelekea katika ardhi ya Iraq na halafu nikaelekea katika Mji wa Madina na sikua ni mwenye kuchukua Ilm isipokua kama ilivyokua na kama nilivyoiona, na kisha nikawasili katika ardhi ya Sham na nikaanza kuichuja, na sikuwahi kuhifadhi kitu chochote ndani ya Kifua changu isipokua hua ni mwenye kukipata pale ninapokihitaji.'**

Imam Al Makhul alikua ni Mwanazuoni wa watu Sham, na alikua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Qura'n, Hadithi na Fiqh na alisoma kwa Masahaba wakiwemo Ubay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu*, Thawban *Radhi Allahu Anhu*, Ubaidah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu*, Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*, Abu Thalaba Al Khashmi *Radhi Allahu Anhu*,

Abu Jandal Ibn Suhayl *Radhi Allahu Anhu*, Umm Ayman *Radhi Allahu Anha*, *Umm ul Muuminin* Aisha *Radhi Allahu Anha*, Sulayman Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu, n.k*

Ambapo Imam Az Zuhri alisema: ‘**Wanazuoni wako wanne, Said Ibn Musayyib wa Madina, Amr Ash Shabi wa Kufah, Hasan Al Basr wa Basra na Makhul wa Sham ambapo ilikua hakuna mwenye kuruhusika kutoa Fatwa isipokua yeye. Na alikua hatoi Fatwa bila ya Kusema *La Hawla wal Quwwata Illa Bi Allah*, hivi ndivyo ninavyojua mimi, Fatwa hii inaweza ika si sahihi lakini ni ya ukweli.’**

Na Said Ibn Abd ul Azizi kua: ‘**Sulayman Ibn Musa alikua ni mwenye kusema: ‘Kama Ilm ikija kwetu kutoka Hijaz kutoka kwa Al Zuhri basi tunaikubali na kama ikiwa inatoka Sham kwa Makhul basi tunaikubali, na kama ikiwa inatoka Jazira kwa Maymun Ibn Mihran basi tunaikubali na kama ikiwa inatoka Iraq kwa Hasan Al Basr basi hua tunaikubali kwani hawa ndio Wanazuoni wa Utawala wa Khalifa Hisham Ibn Abd Ul Malik.**’’
Ambapo amesema Marwan Ibn Muhammad kua: ‘**Amesema Said Ibn Abd Ul Aziz kua: ‘Makhul alikua na Ilm kubwa sana kuliko Al Zuhri, na Makhul alikua na Ilm kubwa zaid kuliko watu wote wa Sham.**’’

Mbali ya kua na Ilm kubwa sana lakini Imam Makhul alikua si mwenye kujibu kila analoulizwa kwani anasema Taymi Ib Atiyya Al Ansi kua: ‘**Mimi nilimsikia mara kadhaa Makhul akiwa ni mwenye kujibu suali pale anapoulizwa kwa kusema kua: ‘Sijui’’**

Na Imam Al Makhul anasema kua: ‘**Amesema Abd Rahman, kua amesema Ghanim kua amesema Abd Rahman kua, watu 10 miongoni mwa marafiki zangu wameniambia mie kua Tulikua kwenye Masjid Quba, tukisoma Ilm na akatokea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kusema kua: ‘Tafuta Ilm utakavyoweza, lakini kama ikiwa huifanyii kazi kulingana na kile unachokijua basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* hatokulipa wewe juu yake.**’’

Imam Al Makhul alisema kua: ‘**Kamwe usiwe ni mwenye kuchunguza Maovu, wala Usiwe ni mwenye kupenda kusifu Watu, na wala usiwe ni mwenye kupakazia Maovu ya Watu na wala usikae bure bila kufanya jambo lolote.’**

Na Imam Al Makhul anasema kua: ‘**Amesema Anas Ibn Malik kua: ‘Yeyote yule atakaesema *Allahuma Inni Ashhaduka wa Ashhadu Hamalat Arshika Wa Malaikatak fi Jamii Khalkik, Innaka Anta Allaha La Ilaha Illa Anta Wahdak wala Sharika Laka, wa Ashhadu Anna Muhammad Abduka wa Rasulika’* Basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* atamuepusha Mtu huyo na Moto kutokana na robo ya Mwili wake, na akisema mara 4 basi sehemu 3 ya mwili wake na akisema mara 2 basi**

Nusu ya Mwili wake na akisema mara 4 basi Mwili wake wote utakua huru kutokana na Moto.’

Wakati Imam Makhul Al Shami alipokua akiona Maziko basi hua ni mwenye kusema: **‘Kama ikiwa umeondoka asubuhi basi sisi Tutakufuata Jioni, kwani Maziko ni wasia tosha na ni jambo lenye kutosheleza kujifunza kutokana nalo, lakini mghafiliko ni mkubwa sana, waliotangulia wamepita na kuondoka lakini wale waliopo hua hawajali’**

Imam Makhul Al Shami alisema: **‘Yeyote yule mwenye kuutumia usiku wake katika *Qiyam Al Layl* basi anapofika asubuhi yake hua ni sawa na asiekua na Dhambi kama aliezaliwa kutoka tumboni mwa Mama yake kwa siku hio.’**

Imam Makhul Al Shami alisema: **‘Ingawa Kuna faida nyingi kuishi katika jamii lakini kuna usalama zaid wa maovu unapokua ni mwenye kujitenga peke yako’**

Imam Makhul Al Shami alisema: ‘**Wale wenye kunukia vizuri hua ni wenye ufahamu zaidi na wenye Nguo safi hua ni wenye furaha zaidi kuliko huzuni.’**

Imam Makhul Al Shami alisema: **‘Kama ukiwa unasoma Qur’an na kisha haikuweki mbali na Madhambi basi wewe si miongoni mwa wenye kusoma Qur’an.’**

Imam Makhul Al Shami alisema: **‘Yule ambae Ilm yake haimnufaishi basi hua ni mwenye kudhurika na ujinga wake.’**

Imam Makhul Al Shami alisema: ‘**Wenye Nyoyo Laini miongoni mwa Watu ni wale wenye Dhambi kidogo.’**

Imam Makhul Al Shami alisema: **‘Adhabu ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* haiwashukii watu hadi pale Wanazuoni wa watu hao watakapokua ni waovu.’**

Imam Makhul Al Shami aliulizwa kuhusiana na ile aya isemayo:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوا۟ عَلَيْكُمْ أَنفُسَكُمْ لاَ يَضُرُّكُم مَّن ضَلَّ إِذَا ٱهْتَدَيْتُمْ إِلَى ٱللَّهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعاً فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ya ayyuha alladheena amanoo AAalaykum anfusakum la yadhurrukum man dhalla idha ihtadaytum ila Allahi marjiAAukum jameeAAan fayunabbi-okum bima kuntum taAAmaloona *(Surat Al Maidah 5:105)*

Tafsir: ***Enyi wale ambao Mlioamini hakika ni juu yenu Nafsi zenu, Kwani hawawezi kukudhuruni wale waliopotea kama ikiwa mko kwenye njia iliyonyooka, kwani marejeo yenu kwa pamoja ni kwa Allah na kisha mtabainishiwa juu ya yale mliyokua mkiyafanya.***

Ambapo Imam Makhul akasema: 'Wakati Yule mwenye kutakiwa kutoa ushari anapokua ni mwenye kuogopa na mwenye kutakiwa kupokewa ushauri huo hataki kuukubali,basi hapo ni wajibu wako kujilinda Nafsi yako, na hivyo hakuna aliepotoka atakaeweza kukusababishia Madhara'

Imam Makhul Al Shami alikua amekaa kwenye Darsa yake mara akaja Yazid Ibn Abd Ul Malik ambae ni Mjukuu wa Khalifa Marwan, na alipofika basi watu wakanyanyuka na kutaka kumpisha yeye ili akae, ambapo Imam Makhul Al Shami akawaambia watu hao: **'Kaeni katika sehemu zenu msimpishe, mwacheni mwenyewe atafute sehemu ya kukaa kwa ajili yake, kwani kutokana na kufanya hivyo basi ndio atakua ni mwenye kujifunza kua na Unyenyekevu.'**

Imam Makhul Ash Shami alipikua anakaribia kifo chake basi alisema: '**Kua Karibu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae usamehevu wake ni wenye kupatikana hua ni bora kuliko kua karibu na Ibn Adam ambae ubaya wake hautabiriki.**'

IMAM YAZID IBN ABI HABIB 53 AH

Imam Abu Raja Yazid Ibn Abi Habib alizaliwa nchini Sudan mnamo mwaka 53 Al Hijra na baadae familia yake ikahamia nchini Misri ambapo ndipo alipofariki mnamo mwaka 128 Al Hijra.

Imam Yazid Ibn Abi Habib alisoma kwa Masahaba wakwemi Abu Tufayl *Radhi Allahu Anhu* na Abd Allah Ibn Harith *Radhi Allahu Anhu* na Masahaba wengineo waliokua wakiishi nchini Misri, na hivyo alisoma Ilm ya Qur'an, Hadith na Fiqh na hivyo kua ni mwenye Ilm kubwa sana, kwani alikua ni Mwanafiqh wa mwanzo wa Misri kuanzisha mpangilio wa kuainisha vilivyo Halali na vilivyo Haramu.

Imam Yazid Ibn Abi Habib aliwasomesha Wanazuoni wengi sana wa Misri akiwemo Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Sulayman At Taymi, Imam Yahya Ib Ayub n.k na

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

baadhi ya Hadith zake alizozinukuu zinapatikana katika Sahih Bukhari. Ambapo anasema Imam Al Layth As Saad kua: ‘**Imam Yazid Ibn Abi Habib, ni Mwalimu wangu ni Sheikh wetu’**

Kutokana na Ilm yake na Ucha Mungu wake basi Imam Yazi Ibn Abi Habib basi alichaguliwa na Khalifah Umar Ibn Abd Al Aziz *Radhi Allahu Anhu* kua ndie Qadhi Mkuu wa Misri, na alikua ni miongoni mwa Wanazuoni waliokuwemo kwenye jopo la uchaguzi wa Gavana wa Misri na pia wa Khalifa wa Banu Ummayad, kwani Imam Yazid Ibn Abi Habib alikua si mtu mwenye kusema uwongo wala mwenye kuficha ukweli.

Katika wakati wa kipindi chake kulikua kuna na Gavana ambae alikua si muadilifu aliekua akiitwa Al Haythar Ibn Suhayl, alimtembelea Imam Yazid na kisha akamuuliza kuhusiana na Fatwa ya kua jee inakubalika kusali huku nguo ikiwa ina damu ya Nzi? Hivyo Imam Yazid akamwambia Gavana huyo kua: ‘**Inakuaje wewe unawadhulumu watu wasiokua na hatia na kumwaga Damu zao kila siku, na huulizii kuhusiana na Damu zao halafu unaulizia kuhusiana na juu ya uhalali wa kusali na nguo iliyokua na Damu ya Nzi?’**

Ambapo safari moja pia, Khalifa wa wa Banu Umayyad alitembelea Ardhi ya Misir na kisha akamtuma Mtoto wake aende nyumbani kwa Imam Yazid akamwite, ambapo Imam Yazid akamwambia kijana huyo akamwambie baba yake kua: **‘Mwanazuoni kutokana na Ilm na Heshima yake basi hatakiwi kumfuata Mtawala, kwani kufanya hivyo hua ni kujivunjia heshima yake na pia kivunja heshima ya Mtawala wake, na kwa Mtawala kumtembelea Mwanazuoni hua ni Pambo na ni Heshima juu yake.’**

Na akasema Imam Yazid Ibn Abi Habib kua: **‘Miongoni mwa Matamanio ya Mwanazuoni hua ni katika Kauli yake, kwani hua anaipenda sana kuliko kimya chake, kwani hua kuna ukimya na usalama katika kukaa kimya ambapo katika kusema hua kuna mapambo ya maneno iwe mengi au kidogo. Hivyo kama ikiwa kuzungumza kwake Mwanazuoni ni mwenye kumvutia zaidi kuliko kukaa kimya kwake basi huu tayari ushakua ni Mtihani mkubwa sana juu yake Mwanazuoni.**’

Imam Yazid Ibn Abi Habib alisema tena kua: ‘**Masahaba Allah awaridhie walikua hawali chakula kwa ajili ya starehe ya kushiba au kupata utamu wa Ladha ya chakula chake, na wala hawatokua ni wenye kuvaa nguo kwa ajili ya kupendeza, bali walikua wanakula kwa ajili ya kuondaa njaa, na kupata nguvu za kufanya Ibada na walikua wanavaa kwa ajili ya kujihifadhi sehemu zao za Siri na miili yao kutokana na hali ya hewa ya baridi na joto.** ’

Na akasema Imam Yazid Ibn Abi Habib kua: **‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Hatakiwi hata mmoja wenu miongoni mwenu anaetakiwa kuuvunja Udhu wake katika wakati akiwa ameelekea Kibla.’’**

IMAM YAHYA IBN YAMAR

Imam Yahya Ibn Yamar alizaliwa katika maeneo ya Ihwaz katika ardhi ya Khurasan kutokana na familia ya Wanazuoni na hivyo Mwalimu wake wa kwanza alikua ni baba yake mzazi, ambapo baadae Imam Yahya Ibn Yamar akahamia katika Mji wa Basra na kupata nafasi ya kusoma kwa Masahaba kadhaa wakiwemo *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*, kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allah Anhu*, Abu Al Aswad Al Duali *Radhi Allahu Anhu*, Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu*, Abu Dhar *Radhi Allahu Anhu*, Abd Rahman Ibn Is-haq *Radhi Allahu Anhu* na Masahaba wengineo.

Imam Yahya Ibn Yamar alisoma sana Ilm ya Lugha, Hadith na Qur’an na hivyo akawa pia na Ilm ya Fiqh, hadi akafikia kua Qadhi wa Mji wa Khurasan na pia aliwahi kua Qadhi wa Mji wa Basra. Imam Yahya alikua ni *Thiqah* kwa upande wa Ilm ya Hadith na alikua ni miongoni wa Wanazuoni waliopewa kazi na Hajjaj Ibn Yusuf katika kuitia Harqah Qur’an.

Na hivyo Msahafu wa Mwanzo kua na Harkah yaani *Kisra, Fat-ha, Dhumma, Shadda, Sakna* na alama nyenginezo ulikua ni wa Imam Yahya Ibn Ammar kama alivyosema Imam Abu Daud.

Kwani alikua ni Hajjaj Ibn Yusuf ndie aliemtoa Imam Yahya Ibn Yamar kutoka katika ardhi ya Khurasan alipokua Qadhi na kumleta katika Ardhi ya Basra na kumfanya kua ndie Qadhi wa Mji huo baada ya Imam Yahya Ibn Yamar kugombana na Qadhi Qutaybah Ibn Muslim wa Khurasan, ambapo kabla ya hapo Imam Yahya Ibn Amar alikua ni Qadhi wa Mji wa Nishapuri, Marwazi na Herat, hivyo alipohamia katika ardhi ya Basra basi alibakia kua Qadhi wa Mji huo hadi alipofariki mnamo mwaka 122 Al Hijra.

Ambapo katika vipindi hivi vyote alipokua Qadhi alikua pia akisomesha tangu katika ardhi ya Khurasan na hivyo alitoa Wanafunzi wengi sana akiwemo Imam Qatadah Ibn Diama, Imam Yahya Ibn Ukayl, Imam Ataa Al Khurasani, Imam Sulayman At Taymi. Imam Umar Ibn Ataa Ibn Abu Huwayr, Imam Ikrimah, Imam Abd Allah Ibn Barida, Imam Abd Allah Ibn Kulayb. Abd Allah Ibn Abu Is-haq n.k

Imam Yahya Ibn Yamar alikua ni mtu ambae asieogopa kusema Ukweli mbele ya Mtu yeyote yule, kwani alikua ni mtu mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee na hivyo alikutana na Mitihani mingi sana, na ndio maana akasema Imam Abd Malik Ibn Umayr kua: '**Miongoni mwa watu walioteswa sana katika nyakati zao ni Musa Ibn Talha, Qabisah Ibn Jabr na Yahya Ibn Yamar.'**

Ambapo wakati Hajjaj Ibn Yusuf Al Thaqafi alipoutembelea Mji wa Al Wasit basi aliwauliza watu wa Mji huo kua: '**Hivi Jee nyinyi watu wa Mji huu hamna aibu?'**

Hivyo watu wa Mji huo wakamwambia Hajjaj Ibn Yusuf: **'Hakika sisi si wenye kujua juu ya hilo, lakini wacha tumuulize mwenye kujua miongoni mwa wenye kujua katika Mji wetu, ambae anaitwa Yahya Ibn Yamar.'**

Hivyo Imam Yahya Ibn Yamar akatafutwa na kuletwa mbele ya Hajjaj Ibn Yusuf na kisha nae akaulizwa suali hilo hilo. Ambapo Imam Yahya Ibn Yamar akajibu suali hilo kwa kusema: '**Nyinyi mliujenga Mji huu kwa pesa za Dhulma, hivyo bila ya shaka watakaoishi ndani yake mji huu ni wengine na wala si watoto wenu**' Hajjaj Ibn Yusuf akamuuliza Imam Yahya Ibn Yamar kwa kusema: '**Imekuaje wewe unakua na uwezo wa kusema maneno hayo?**'

Imam Yahya Ibn Yamar akasema: '***Allah Subhanah wa Ta'ala* amechukua Ahadi kutoka kwa Wanazuoni kua hawatakiwi kuficha Ilm ya Hadith na Ukweli wanaoujua.'**

Ambapo safari nyengine Imam Yahya Ibn Yamar alikua amekaa katika Barza na Hajjaj Ibn Yusuf alikua nae pi amehudhuria pia, katika baraza mara likatajwa jina la Husayn Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*,ambapo kutokana na kua Hajjaj Ibn Yusuf ni mwenye kusimamia Manufaa ya Utawala wa Banu Umayyah basi akasema: '**Husein hakujumuishwa ndani ya kizazi cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*'**

Hivyo Imam Yahya Ibn Yamar akasema: **'Ewe Hajjaj, hakika huko sahih kwa kauli yako hio'** Hajjaj Ibn Yusuf akasema: '**Siko Sahih? Basi thibitisha juu ya mjumuisho wake huo kwa kutumia aya ya Qur'an ama sivyo basi Kichwa chako kitakua halali yangu sasa hivi.'**

Imam Yahya Ibn yamar akasoma aya ifuatayo:

﴿وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ كُلاًّ هَدَيْنَا وَنُوحاً هَدَيْنَا مِن قَبْلُ وَمِن ذُرِّيَّتِهِ
دَاوُودَ وَسُلَيْمَانَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ وَمُوسَىٰ وَهَارُونَ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Wawahabna lahu ishaqa wayaAAqooba kullan hadayna wanoohan hadayna min qablu wamin dhurriyyatihi dawooda wasulaymana waayyooba wayoosufa wamoosa waharoona wakadhalika najzee almuhsineena *(Surat Al Anaam 6:84)*

Tafsir: ***'Na tukampa kutokana na Is-haq na Yuaqub, na kila mmoja wao tukamuongoza, na kabla yake tulimuongoza Nuh na kutokana na Kizazi chake (tukamuongoza) Daud, Sulaiman, Ayub, Yusuf, musa na Harun' na hivyo ndivyo tunavyowalipa wenye kufanya Mema.***

Hivyo inakuaje ewe Hajjaj unakataa mjumuisho wa Husein kutokana na ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **kupitia kwa Fatima Bint Rasul?'**

Hapo Hajjaj Ibn Yusuf akakaa kimya, huku akiwa amejawa na hasira.

Mara nyengine tena Hajjaj Ibn yusuf alimuuliza Imam Yahya Ibn Yamar: **'Hivi Jee unauonaje usomaji wangu wa Qur'an?'**
Ambapo Imam Yahya Ibn Yamar akasema kumwambia Hajjaj Ibn Yusuf baada ya kumsikiliza kisomo chake hicho kua: ***'TarfaaAa Maa Yahfadh wa Tahfadh Maa YarfaAa*** **– Unasoma kwa sauti kile unachotakiwa usikihifadhi na unakihifadhi kwa sauti kile unachotakiwa kukinyanyulia sauti.' A**mbapo kwa lugha ya Kiarabu maneno haya pia hua yanamaanisha: **'Unamnyanyua yule anaetakiwa kumhifadhi Jela na Unamuingiza Jela yule unaetakiwa kumpandisha cheo.'**

IMAM AL ZUHRI 58 AH.

Muhammad Ibn Muslim Al Zuhri alizaliwa mnamo mwaka 58 Al Hijra katika Mji wa Madina na alikua akitokana na ukoo wa Banu Zuhra ambao ni wenye kutokana na Kabila la Quraysh kwani jina lake kamili lilikua ni Muhammad Ibn Muslim Ibn Ubaid Allah Ibn Abd Allah Ibn Shihab Ibn Abd Allah Ibn Al Harith Ibn Zuhrah Ibn Kilab Ibn Murrah Ibn Ka'b Ibn Luayy Ibn Ghalib.

Imam Sufyan Ibn Uyaynah alisema kua: '**Nilimuona Al Zuhri akiwa na Nywele nyekundu na Ndevu huku Nywele zake zikiwa zimeanza kufifia rangi yake inaonekana kama alikua amepaka hina**' na Yaqub Ibn Abd Rahman alisema kua: '**Mimi nilimuona Az Zuhri kua ni mtu mfupi mwenye ndevu kidogo na asiekua na nywele nyingi usoni.**'

Imam Al Zuhri alijaaliwa kua na ufahamu mzuri sana tangu katika kipindi cha utotoni wake, na alikua ni mwenye kupenda sana kutafuta Ilm ya Qur'an ambayo aliihifadhi

yote, Ilm ya Hadith na pia Maghazi Mapigano ya Vita vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kiasi ya kua alikua kila akisikia kua chakula fulani kinasaidia katika kuongeza Ufaham basi alikua akikitumia chakula hicho.

Imam Al Zuhri alisoma kwa baadhi ya Masahaba wakiwemo kina Anas Ibn Malik, Abu Hurayrah, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum* n.k na Tabiina Wanazuoni wakubwa wa Ilm wa Mji wa Madina kama vile Said Ibn Musayyib, Urwa Ibn Zubayr Ibn Awwam *Radhi Allahu Anhu*, Ubayd Allah Ibn Abd Allah, Abu Salama Ibn Abd Rahman Ibn Awf *Radhi Allahu Anhu n.k*

Imam Al Zuhri pia alikua ni mwenye kutafuta Ilm katika meneo mengine kwa ajili ya kutafuta Ilm ya hadith kwani anasema Shuayb Ibn Hamzah kua alisema Imam Az Zuhri kua: '**Nilikua nikisafiri baina ya Hijaz na Sham kwa mda wa miaka 40 na sikuwahi kupata Hadith yeyote yenye upekee na sikuwahi kukutana na yeyote mwenye hadith ya upekee**'

Ambapo anasema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua Imam Az Zuhri alisema kua: '**Hakika sisi tulikua tunaweza kupata hadith kutoka kwa Ibn Musayyib pale anapokua na hasira tu, kwani mimi nilikaa nae chini yake kwa miaka 6 huku goti langu likigusana na lake huku nikiwa sithubutu kumuuliza kuhusiana na hadith bila ya kuongezea kwa kusema fulani na fulani amesema hiki na hiki na fulani na fulani amesema hiki na kile**'

Na amesema Imam Abu Daud At Taylasi kua: '**Hakika sisi tumeona kua hadithi zinapatikana kwa watu wanne tu. Az Zuhri, Qatadah, abu Is-haq na Al Aamash, ambapo Az Zuhri alikua ndie m-bora wao kuhusiana na Sanad za Hadith**'

Ambapo amaesnema Imam Malik kua: '**Hakika mimi nimesoma hadithi 70 kwa Az Zuhri na nilifanya makosa ya kilugha kwenye Hadith moja ambapo nae akamtikisa Ngamia wake na kusema: 'Watu wameshakua hawafaham**''

Na anasema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Amesema Imam Malik kua: 'Anapoingia Az Zuhri katika Mji wa Madina basi hakuna Mwanazuoni anaesomesha Hadith hadi pale atakapoondoka yeye.**''

Na kwa upande wa Imam Al Layth Ibn Saad nae amesema kua: **'Simjui Mwanazuoni yeyote yule mwenye Ilm Kubwa kama Ibn Shihab, kwani ukimsikia anazungumzia kuhusiana na kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi utasema kua huyu Ilm yake hii ndio fani yake, na ukimsikia anazungumzia kuhusiana na historia basi utasema ndio somo alilolisomea, na ukimsikia anazungumzia kuhusiana na Sunnah na Hadith basi maneno yake katika upande huo hua ni mazito sana.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo kwa upande wa Marmar basi yeye anasema kua: ‘**Watu wanaomtaja Az Zuhri hawawezi kumfananisha nae na yeyote isipokua na Ash Shabi.**’

Na akasema tena Imam Al Madini kua: **‘Wanazuoni wenye kutoa Fatwa ni wanne, Hakam, Hammad, Qatadah na Az Zuhri. Lakini kwa mtizamo wangu basi Mwenye Ilm kubwa zaidi kati yao ni Az Zuhri.**’

Wakati Imam Amr Ibn Dinar alipokua akitajiwa jina la Imam Az Zuhri basi alikua akisema: ‘**Az Zuhri ana I’lm gani? Hakika mimi nimekutana na Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* nae hakuwahi kukutana nae, mimi nimekutana na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* nae hajawahi kukutana nae**’ hivyo Imam Az Zuhri alipowasili katika Mji wa Makkah basi Imam Amr Ibn Dinar alikua anaumwa, na hivyo alipopewa habari kua amekuja basi akaomba kua abebwe apelekwe kwa Imam Az Zuhri.

Wanafunzi wa Imam Amr Ibn Dinar wakambeba hadi kwa Imam Az Zuhri na alipofika huko hakuondoka tena usiku wake katika siku hio, siku ya pili alipoulizwa: **‘Vipi umemuonaje Az Zuhri’** basi Imam Amr Ibn Dinar akasema: ‘**Wa Allahi Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu yeyote kama mtu huyu wa Quraysh.’**

Imam Ibn Al Madini alisema: ‘**Ilm kuhusiana na Watu wanaoaminika kihadithi inazunguka kwa watu sita tu, ambao ni Az Zuhri na Amr Ibn Dinar kwa Hijaz, Qatadah na Yahya Ibn Abi Kathir kwa Basra na Abu Is-haq na Al Amash kwa Mji wa Kufah.**’

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Ilm ya Nukuu za Hadith baina ya Masahaba na Tabiina basi hakuna Sanad fupi na zenye uhakika kama za Imam Az Zuhri, na ndio maana Wanazitilia maanani sana na kuzipa kipaumbele nukuu zake kupitia kwa Wanafunzi wake ambapo miongoni mwao ni kina Imam Malik Ibn Anas, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Ubayd Allah Ibn Umar, Imam Al Awzai, Imam Al Layth Ibn Saad.

Ambapo amesema Imam Az Zuhri kua: ‘**Kuna Mambo matatu akiwa nayo Qadhi basi huyo hua si Qadhi: Kutopenda Kukosolewa, Kupenda Kusifiwa na Kukwepa kuvuliwa Madaraka yake.**’

Imam Az Zuhri alisema pia kua: **‘Kukwepana na Watu Wajinga hua ni Hikma na Busara, kwani kukwepana nao hua ni bora zaid kuliko kuzungumza nao.**’

Imam Az Zuhri alimuusia Umar Ibn Abd Ul Azizi kwa kumwambia: **‘Ewe *Amir ul Muuminin* muondoe Al Walid madarakani kwani hili hua ni jukumu lako katika kusimamia Amanah yako mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala***’ ambapo Umar Ibn

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Abd Ul Aziz akasema: '**Nataka kufanya hivyo lakini nnakhofu kua Jeshi linaweza kupingana nami juu ya hilo.**'

Hivyo Imam Al Zuhri akasema kumwambia *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Abd ul Aziz: '**Basi niruhusu mimi nizungumze nao hao wanajeshi kwani nitawathibitishia na watafahamu kua anatakiwa aondolewe Madarakani.'** Lakini hata hivyo Umar Ibn Abd Ul Aziz akakataa juu ya shauri hilo.

Baada ya tukio hilo basi Al Walid akawatuma watu kwenye Nyumba ya Imam Az Zuhri na kuivunja yote na baadae akalitekeza shamba lake lote la Mitende, na baada ya Imam Az Zuhri kujua juu ya hilo basi akamshtaki Al Walid kwenye Mahkama ya Umar Ibn Abd ul Aziz na kutoa hati za umiliki wa Shamba lake na Nyumba yake na kumwambia Umar Ibn Abd Ul Aziz kua atoe hukmu ya kesi yake.

Lakini Umar Ibn Abd ul Aziz akamwambia Imam Al Zuhri kua: '**Hakuna atakaeweza kutoa hukumu juu ya Jambo isipokua wewe mwenyewe.**'

Hivyo Imam Az Zuhri akasema: '**Ewe Amir ul Muuminin Muamrishe kua apande Mtende katika kila sehemu aliyoukata Mtende, na kisha ausimamie hadi uwe mkubwa kufikia katika hali ilivyokuwa wakati alipoikata mitende hio. na pia anilipe fidia kutokana na kazi yangu yote niliyoifanya kuisimamia Mitende hio**'

Hivyo Umar Ibn Abd Ul Aziz akakubaliana na Fatwa hio na hivyo Al Walid akaamrishwa kufanya kama ilivyosema Fatwa hio, na baada ya hapo Al Walid akamwambia Imam Az Zuhri kua: **'Kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* akinipa Mamlaka dhidi yako basi utanijua mie nani**' Ambapo Imam Az Zuhri akasema: **'*Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Muadilifu sana kiasi ya kua hawezi kumpa Mtu mjinga kama wewe kua na Mamlaka Dhidi yangu.'**

Imam Az Zuhri alikua n mtu mkarimu sana na ni mwenye kupenda kusaidia watu wenye shida kiasi ya kua alikua anafikia kua na madeni kutokana na kusaidia kwake ambapo kuna watu walimwambia Imam Az Zuhri kua: **'Watu hawajawahi kuona kosa lolote dhidi yako isipokua Una deni kubwa'**

Imam Az Zuhri akajibu: **'Deni langu mimi ni Dinar 20000, na mimi nna umiliki wa chemchem 5 ambapo kila chemchem moja ina thamani ya Dinar 40000, na hakuna wa kunirithi isipokua Mjukuu wangu na mimi pia sijali hata kama hakunirithi kwa sababu Mjukuu huyo ni *faasiq.'***

Zayad Ibn Asad alimuandikia barua Imam Az Zuhri kua: '**Uwezo wako wa kufafanua Hadith unanishangaza na kunivutia sana, ila tatizo ni kua mimi sina uwezo wa**

kukufuata na kuja kusoma kwako' Imam Az Zuhri akajibu: '**Njoo kwangu nami nitakusomesha Hadith na pia nitakuhudumia kwa mahitaji yako kimatumizi.**'

Amesema Imam Sufyan Ibn 'Uyaynah kua: '**Mimi nimekaa kwenye Darsa za Al Hasan Al Basr na wengineo lakini sijawahi kuona Mtu kama Az Zuhri.'**

Imam Malik Ibn Anas alisema: '**Kila Az Zuhri alipokua anawasili katika Mji wa Madina basi ilikua hakuna anaesomesha Hadithi hadi atakapoondoka yeye.'**

Alisema Imam Al Zuhri kua: **'Mimi nilimtembelea Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* katika mji wa Dimashq na nikamkuta analia, hivyo nikamuuliza: 'Jee unalia nini?' ambapo nae akasema: 'Sijawahi mimi kukuta kitu chochote kile kutoka katika wakati wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hadi sasa isipokua hii Ibada ya Sala ambapo hata hivyo nayo pia watu wanaachana nayo.''**

Imam Az Zuhri alifariki katika mwezi wa Ramadhani mnamo mwaka 124 Al Hijra miezi michache kabla ya kuingia Madarakani Khalifa Al Walid ambae aliahidi kua kama akipewa Mamlaka dhidi yake Imam Az Zuhri basi atamuonesha yeye ni nani.

IMAM ABU MUNDHIR HISHAM IBN URWA 61 AH

Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa Ibn Zubayr Ibn Al Awwam Al Asad Al Qureish alizaliwa katima mji wa Madina Al Munawaara katika siku ya Ijumaa ya mwezi Muharaam mnamo mwaka 61 Al Hijra na alikua ni Mjukuu wa mmoja kati ya Masahaba 10 waliobashiriwa Pepo na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Imam Abu Mundhir alihamia katika mji wa Kufah baada ya kuishi katika ardhi ya mji huo wa Madina aliozaliwa na kusoma kwa kujipatia Ilm kwa miaka kadhaa kutoka kwa Masahaba wakiwemo Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu,* Sahl Ibn Sad *Radhi Allahu Anhu*, Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu*, Abd Alla Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu,* n.k

Baada ya kumalizakusoma katika Mji wa Madina basi Imam Abu Mundhir akaamua kuhamia katika Mji wa Kufah kusoma Hadith na pia kuanza kusomesha, ambapo Miongoni mwa Wanafunzi wake aliowasomesha Imam Abu Mundhir ni Imam Ayub As Sakhtiyyani, Imam Ibn Jurayj, Imam Ibn Is-haq, Imam Shu'bah, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Hammad Ibn Salamah Imam Hammad Ibn Zayd, Imam Abd Allah Ibn Mubaraka, Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Shuyraikh Ibn Abd Allah, Imam Malik, Imam Abu Hanifa na wengineo.

Ambapo anasema Imam Ibn Saad kua: **‘Hisham Ibn Urwa ni thiqah, na ni mwanazuoni wa Ilm ya Hadith na ni Hujjat katika fani ya Ilm ya Hadith’**

Ambapo Imam Ibn Hibban anasema kua: **‘Hisham Ibn Urwa ni anaeaminika na ni mwenye kuachana na yenye kua na shaka na mtu mwenye uhifadhi mzuri sana katika ufahamu wake’** Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa alikua ni miongoni mwa Maimamu waliokua wakipendekeza kuaandikwa kwa Hadith**.**

Baada ya kukaa kwa mda katika Mji wa Kufah basi akahama na kisha akaelekea katika Mji wa Baghdad ambapo alimalizia uhai wake, na sala yake ya Maiti iliongozwa na Khalifa Al Mansur.

Ambapo kabla ya tukio hilo basi siku moja Khalifa Al Mansur alikutana nae Imam Hisham Ibn Urwa na hivyo akamwambia: **‘Ewe Abu Mundhir siku moja Mimi, Ndugu zangu na Baba yangu tuliingia na kukuta unakunywa Supu kwa kijiko, unakumbuka? Basi tulipoondoka Baba yetu akasema kutuambia sisi kua: ‘Huyu Mzee mliemuona Mtu mzuri sana, huyu ndio miongoni mwa Wanazuoni waliobakia leo hii’’ ambapo Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa akatabasam na kisha akasema: ‘Ewe *Amir Ul Muuminin* Wallahi mimi sikumbuki’**

Hivyo *Amir ul Muumin* Khalifa Mansur kuondoka basi watu wakamwambia Imam Hisma Ibn Urwa: **‘*Amir ul Muumin* Khalifa Mansur anakukumbuka vizuri sana, hii inamaanisha kua anataka kukusaidia lakini wewe umesema kua humkumbuki’**

Imam Hisham Ibn Urwa akasema: **‘Kwa hakika *Allah Subhanah wa Ta’ala* hatukumbushii sisi kitu chochote isipokua wema’**

Imam Hisham Ibn Urwa alikua ni mtu ambae si mwenye kuiweka mbele Dunia yake bali alikua ni mtu alieipa mgongo Dunia yake, kwani alikua ni mwenye kuiweka mbele Akhera yake n ahivyo kutopenda kujulikana na kutokua na ukariu na watu maarufu, alikua ni mwenye kupenda kuwasaidia watu wasiokua na uwezo na kuwausia watu kuhusiana na Akhera yao.

Kwani anasema Imam Hisham Ibn Urwa kua: **‘Wakati Abu Bakr alipoteuliwa kua Khalifa, na watu wakakubaliana kukubaliana nae, basi aliwakusanya Maansari kwa ajili ya kutatua mzozo uliopo baina yao kuhusiana kumtuma Usama *Radhi Allahu Anhu* Vitani na hivyo akasema: ‘Usama atakwenda Vitani’**

Hiki kilikua kipindi ambacho ni cha fitna kubwa sana kwani Waarabu walikua baadhi yao wameritadi, na hivyo Wakristo, Mayahudi na Mitme wengineo walioibuka walikua wanataka kuuangamiza Uislam. Na kwa sababu ya wingi wa

maaduai, na uchache wa Waislam miongoni mwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hivyo Masahaba waliposikia kuhusiana na mpango wa Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* basi nao wakamwambia kua: 'Masahaba wote wanakukosoa kutokana na mtizamo wako huo hivyo tahadhari usije ukawasababisha wakakupinga''

Ambapo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Wa Allahi, mimi nnapa kwa yule ambae ndie aliemjaalia Abu Bakr kuishi akiwa na uwezo na Mamlaka haya, kua hata kama watatokea Simba na kunirarua, basi mimi nitamtuma Usama vitani kama vile ambavyo alivyoamrisha R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* hata kama itakua nnajua kua hakutokua na mtu mwengine katika Mji wa Madina, basi nitamtuma tena Vitani, na hivyo Jeshi la Usama likaenda vitani, na hivyo Jeshi la Musallima lilipoona wingi wa jeshi la Waislam basi likaogopa kuvamia kutokana na kua na khofu ya kuona kua kama ikiwa hawa wamekuja kiasi hiki basi huenda ikawa wana jeshi kubwa zaidi lililobakia Madina. Na hivyo Masahaba wakaona kwa namna gani Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alivyokua amejitolea kwa ajili ya R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'*

Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa alisema kua: **'Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifunga kwa mfululizo siku moja baada ya nyengine kiasi ikawa tunadhania kua hatokula tena, na kisha akawa hafungi kwa masiku kadhaa kiasi tukawa tunadhani kua hatofunga tena, ambapo miongoni mwa Funga za Sunna alizokua akizipenda *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ilikua ni mwezi wa Shaban.'**

Nami nikasema: '*Ya Rasul Allah,* hakika mimi nakuona kua unafunga katika mwezi wa Shaaban hivi jee kuna hikma gani ndani yake?' ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nae akasema: 'Ewe Aisha, Shaaban ni Mwezi ambao ndani yake yanaandikwa majina ya watu watakaofariki kwenye mwaka huo na kisha hua anakabidhiwa *Malakat al Mawt,* hivyo hua nnafunga ili kifo changu kiandikwe nikiwa nimefunga'

Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa alisema kua: **'Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* Hunyeshea Rehma Katika Usiku Minne, Usiku hio ni Eid Al Adhha, Eid Al Fitr na Mwezi 15 Shaaban, ambao ndani yake hua mnaandikiwa Kifo, Mnaandikiwa Riziki na Watakaoenda Hijja ndani ya Mwaka huo. Na Usiku wa nne ni Usiku wa Arafa hadi Alfajir yake.''**

Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa alisema kua: **'Amesema Urwa *Radhi Allahu Anhu* kua amesema Sadi Ibn Zayd *Radhi Allahu Anhu,* kua amesema *Rasul Allah***

***Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaechukua hata inchi moja tu ya ardhi kwa dhulma, basi atazamishwa nayo Ardhi hio hadi Ardhi ya saba mara saba huku sehemu hio ya ardhi ikiwa amefungwa nayo shingoni mwake.''**

SHAYKHA FATIMA BINT AL MUNDHIRI

Fatima Bint Al Mundhir alizaliwa katika Mji wa Madina na alikua ni Mwanamke mwenye Ilm kubwa sana ya Fiqh, na alikua akijulikana pia kwa jina Al Faqiiha, na alikua ni Ibn Ami yake Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa na pia alikua ndie mke wake Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa Ibn Al Zubayr.

Ijapokua wawili awa walikua ni Binamu wenye kutoka kwenye familia moja lakini Fatima alikua ni mwenye kua na Hadithi nyingi zaidi hususan kutoka kwa Asma Bint Abu Bakr Radhi Allahu Anha kuliko Imam Abu Mundhir na hivyo Fatima alikua pia ni Mwalimu wa Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa, na pia aliwasomesha Maimamu wengine kama Imam Muhammad Ibn Is-haq.

Na hivyo baadhi ya wakati Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa alikua anapokwama kuhusiana na baadhi ya mas-sala ya Fiqh na Hadith basi hua ni mwenye kuenda kumuuliza Fatima, na kisha huwaambia Wanafunzi wake kua amefundishwa na Mke wake, na bila ya shaka kuna Hadith nyingi sana ambazo Imam Abu Mundhir Hisham Ibn Urwa amenukuu kutoka kwa mke wake ambazo zime katika vitabu vya Hadith kama Sahih Muslim, Sahih Muslim, Sunan An Nasai, Sunan Ibn Majah, n.k.

Ambapo miongoni mwa Hadith hizo ni kama, '**Amesema Imam Hisham Ibn Urwa kua: 'Amesema Mke wake kua amesema Bibi yake (yaani) Asma *Radhi Allahu Anha* kua: 'Kuna Mwanamke alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kusema kua: *'Ya Rasul Allah,* hakika mimi nna binti yangu ambae amechumbiwa, lakini ana hasbah-maradhi- na nywele zake zimekua dhaifu sana. Hivyo jee nnaruhusika kumunganishia Nywele juu yake?' ambapo *RasulAllah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Amelaaniwa yule anaeunganisha Nywele na yule anaeuliza juu ya hilo'''**

'**Amesema Imam Hisham Ibn Urwa kua: 'Fatima ameniambia mie kua amesema Bibi yake (yaani) Asma *Radhi Allahu Anha* kua: 'Sisi tulikua mmoja kati ya Farasi wetu katika kipindi cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam''***

‘**Amesema Imam Hisham Ibn Urwa kua: ‘Amesema Fatima kua amesema Bibi yake (yaani) Asma *Radhi Allahu Anha* kua: amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Saalm* kua: ‘Toeni sehemu ya Mali zenu, Tumieni na lipeni msizing’ang’anie, kwani venginevyo basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* atakuzuilieni, na wala msizihesabu ama vyenginevyo *Allah Subhanah wa Ta’ala* atakuhesabieni pia juu yenu.’**

IMAM SULAYMAN AL AMASH 62 AH

Imam Abu Muhammad Sulayman Ibn Mihran Al Kahili ni Imam ambae anajulikana kwa umaarufu kwa jina la Imam Al Amash alizaliwa mnamo mwaka 62 Al Hijra na alikua ni mwanazuoni wa Ilm ya Hadith na pia alikua ni Al Qari na alikua akiitwa Imam Al Amash kwa sababu ya kua alikua na matatizo ya macho yake kutoona vizuri.

Imam Al Amash alikua ni Mwanafunzi wa Sahaba Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* na alikua ni Imam Mwenye Ulimi mkali sana, ambao alikua anautumia kwa wale watu ambao ni wenye kustahiki kuonjeshwa ukali wa Ulimi wake huo. Na ingawa Imam Al Amash alikua ni mtu mwenye sifa hio lakini alikua pia ni mtu ambae mwenye kuheshimu sana Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo ulimi wake huo alikua akiutumia zaidi kwa wale watu wasioheshimu Hadith hizo.

Mbali ya kua na sifa hizo lakini Imam Al Amash pia alikua na sifa ya kua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith na Ucha Mungu, na alikua pia ni mwenye kupendwa sana na Wanafunzi wake kutokana na uzuri wa sauti yake hususan katika wakati anapokua anasoma Qur’an.

Mbali ya kua ni mwenye Ilm kubwa sana lakini Imam Al Amash alikua pia ni Mtu mwenye maneno ya Maskhara pia kwani siku moja aliingia kwenye Bafu la kijamii la Kukogea na ndani yake akakutana na Daud Al Awdy ambae alikua anakoga huku akiwa Uchi kabisa. Hivyo hapo hapo Imam Al Amash akafunga Macho yake ili asiendelee kumuona akiwa katika hali hio, ambapo Daud Al Awdy alipomuona Imam Al Amash amefunga Macho basi akamuuliza: ‘**Tangu lini umekua Kipofu ewe Abu Amr?**’

Ambapo Imam Al Amash akajibu: ‘**Tangu pale ilipoanguka chini suruali yako’**

Na mara moja aliulizwa Imam Al Amash: ‘**Hivi jee inaruhusika kwa Mwenye kufanya Ibada ya Hija kujikuna?**’ Imam Al Amash akajibu: ‘**Naam**’ alieuliza suali akauliza: ‘**Kwa kiasi gani?**’ Imam Al Amash akajibu: ‘**Mpaka pale itakapochomoza sehemu ya Mfupa wa hapo unapojikuna nje ya ngozi yako**’

Ambapo anasema Imam Ibn Asakir kua: ‘**Kuna Mtu alikuja kwa Al Amash na kumuuliza: ‘Hivi Jee Ibilisi anae Mke?**’’

Imam Al Amash akajibu: ‘**Hakika hii ni miongoni mwa Ndoa ambazo mimi sikuhudhuria**’ na kisha Imam Al Amash akaendelea kusema kua: ‘**Lakini nakumbuka kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* amesema andani ya Qur’an kua:**

﴿وَإِذَا قُلْنَا لِلْمَلآئِكَةِ ٱسْجُدُواْ لِآدَمَ فَسَجَدُوٓاْ إِلاَّ إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ ٱلْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَآءَ مِن دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلاً﴾

Wa-idh qulna lilmala-ikati osjudoo li-adama fasajadoo illa ibleesa kana mina aljinni fafasaqa AAan amri rabbihi afatattakhidhoonahu wadhurriyyatahu awliyaa min doonee wahum lakum AAaduwwun bi/sa lil*dhdha*limeena badalan *(Surat Al Kahf 18:50)*

Tafsir: ***Na kumbuka tuliposema kuwaambia Malaika: ‘Msujudieni Adam’ hivyo nao wakasujudu isipokua Ibilisi, alikua ni miongoni mwa Majini, aliasi Amri ya Mola wake. Hivyo Jee mtamchukua Ibilisi na Kizazi chake kua kua ni Walinzi na Wasaidizi wenu zaidi yangu wakati wao wakiwa ni Maadui zenu? Jee kuna ubaya zaidi badala yake kwa wenye kufanya Udhalimu?***

Imam Al Amash akamalizia wa kusema: ‘**Hii ndio imenikumbusha kua haiwezekani kua na Kizazi kwake Ibilis kama hana Mke.**’

Ingawa Imam Al Amash alikua ni masikini lakini alikua na muonekano mzuri na hivyo Mke wake alikua ni Mwanamake mzuri, ila alikua hana utulivu ndani ya Ndoa yake nyumbani kwake na hivyo alikua akipenda sana kutumia mda wake na Wanafunzi wake zaidi ya anavyoutumia nyumbani kwake, hivyo Wanafunzi wake siku moja wakamuuliza: **‘Kwanini wewe hupendi kukaa nyumbani?**’

Ambapo nae akajibu: ‘**Kwa sababu nyinyi mna rehma kubwa kwangu kuliko yule alie nyumbani kwangu.’**

Hivyo mmoja kati ya Wanafunzi hao wakasema: **‘Natumai kua sikukeri Ewe Imam!’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Al Amash akasema: **'Bora wacha nikuambie, hakika wewe unanikera mimi hata kama ukiwa uko nyumbani kwako, hivyo unafikiria mimi najihisi vipi wakati ukiwa nami hapa?'**

Gavana Isa Ibn Musa alimtuma mtu wake kwa Imam Al Amash na kumpa kitabu ambacho ndani yake aliweka Dirham 1000 na kutaka aandikiwe Hadith ndani yake na kisha akaandika ujumbe usemao: ***'Bismi Allahi AlRahmani AlRahim.'***

Imam Al Amash alipopokea Kitabu hicho na akakifungua kisha Ndani yake akaandika: '***Qul huwa Allahu ahadun'*** na kisha akakirudisha kitabu hicho kwa Gavana huyo, abapo baada ya Gavana huyo kupokea kitabu hicho na kukisoma basi akampa mfanyakazi wake akirudishe kwa Imam Al Amash huku kikiwa na ujumbe usemao: **'Unadhani kua mimi sijui hata kidogo Qur'an?'** Imam Al Amash alipokipokea Kitabu hicho na akakifungua kisha ndani yake akaandika: '***Unadhani kua mimi nnauza Hadithi?'*** na kisha akamrudishia mwenyewe.

Kutokana na ucha Mungu wake basi Imam Al Amash alikua hawezi kulala bila ya kua na udhu, kiasi ya kua siku moja alikua akikosa maji ya kutilia Udhu basi hua ni mwenye kufanya *Tayammam* kwa kutumia Udongo wa ukutani mwa Nyumbani kwake, na alipoulizwa kwanini anafanya hivyo basi alisema: '**Nna khofu kua nisije nikafariki huku nikiwa sina Udhu.**'

Safari moja Imam Al Amash alitoka mapema kueleka kwenye safari zake, na hivyo Alfajiri ikamkutia akiwa njiani na akkakimbilia kwenye Msikiti wa *Banu Asad*. Hivyo akaingia ndani na Kusali pamoja nao, ambao katika Rakaa ya kwanza Imam wa Msikiti huo akasoma *Surat Al Baqarah*, na Rakaa ya pili Imam akasoma *Surat Al Imran.*

Baada ya kumaliza kusali basi Imam Al Amash akamfuata Imam huyo na kumuuliza: **'Hivi wewe humuogopi Mola wako? Jee hujawahi kusikia kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua: 'Yeyote yule atakaesalisha watu katika Sala basi awafanyie urahisi watu hao, kwani nyuma yake kuna Wazee, waliodhaifu na wenye shughuli zao?''**

Imam Huyo akasema: ***'Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema katika *Surat Al Baqara* kua'**

﴿وَٱسْتَعِينُواْ بِٱلصَّبْرِ وَٱلصَّلاَةِ وَإِنَّهَا لَكَبِيرَةٌ إِلاَّ عَلَى ٱلْخَاشِعِينَ﴾

WaistaAAeenoo bialssabri waalssalati wa-innaha lakabeeratun illa AAala alkhashiAAeena *(Surat Al Baqara 2:45)*

Tafsir: ***Tegemeeni Msaada kwa kupitia katika Subra na katika Sala, na hakika katika hili kuna uzito isipokua kwa wenye kumuogopa Allah.***

Ambapo Imam Al Amash akasema: **‘Na mimi ni Mjumbe nilietumwa kutokana na wale wenye Kumuogopa Allah, kukuambia wewe kua unawafanyia watu ugumu katika Dini.’**

Safari moja Imam Al Amash alikua amesimama anataka kuvuka mto, hivyo akatokea askari akampandia Imam Al Amash mgongoni na kumwambia: **‘Twende mbele..Utukufu ni wake yeye alie tujaalia haya kwa ajili yetu.’**

Imam Al Amash akatii amri hio kimya kimya kwa kuanza kuvuka mto kwa haraka hadi alipofika katikati ya mto basi akasema:

﴿وَقُل رَّبِّ أَنزِلْنِى مُنزَلاً مُّبَارَكاً وَأَنتَ خَيْرُ ٱلْمُنزِلِينَ﴾

Waqul rabbi anzilnee munzalan mub<u>a</u>rakan waanta khayru almunzileena *(Surat Al Muuminun 23:29)*

Tafsir: ***‘Na sema Ewe Mola nishushe kwa mshusho wa baraka zako kwani wewe ni mbora miongoni mwa wenye kutuwezesha kushuka’***

Na kisha akamtupa Askari huyo kwenye maji ya mto huo na kukimbia.

Safari moja Imam Shabib Ibn Shaybah na wenzake kumtembelea Imam Al Amash nyumbani kwake, na walipofika Mlangoni wakagonga Mlango, ambapo Imam Al Amash akauliza: **‘Nani?’** hivyo Imam Shabib Ibn Shaybah akasoma sehemu ya aya ifuatayo:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِن وَرَآءِ ٱلْحُجُرَاتِ﴾

Inna alla<u>dh</u>eena yun<u>a</u>doonaka min war<u>a</u>-i al<u>h</u>ujur<u>a</u>ti *(Surat Al Hujrat 49:04)*

Tafsir: ***Kwa hakika wale ambao ni wenye kukuita kutoka ndani ya makazi yao.***

Ambapo hapo hapo Imam Al Amash akamalizia aya hio, ambayo mwisho wake ilikua inasema:

﴿أَكْثَرُهُمْ لاَ يَعْقِلُونَ﴾

Aktharuhum la yaAAqiloona *(Surat Al Hujrat 49:04)*

Tafsir: ***Wengi wao hawana Akili.***

Katika kutembea kwake Imam Al Amash alikutikana akiwa amevaa koti la sufi ndani nje yaani baada ya manyoya kua ndani basi yeye alilivaa huku manyoya yakiwa nje, hivyo akaulizwa: '**Ewe Abu Muhammad kwanini hujalivaa kwa kuifanya Sufi ikawa ndani?'** Imam Al Amash akajibu: '**Kwanini hukumpa ushauri huo Kondoo mwenyewe?'**

Alisema Imam Al Amash kua: **'Mimi nilimsikia Salim akisema kua: 'Nimemsikia Umm Darda akisema kua: 'Abu Darda alikuja kwangu mie huku akiwa amekasirika, hivyo nami nikamwambia: 'Mbona umekasirika, ni kitu gani kilicho kukasirisha?' ambapo nae akasema: 'Wa Allahi mimi sijui chochote katika Ummah huu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isipokua ni kuwaona wanasali Sala ya Jamaa.''''**

Alisema Imam Al Amash kua: '**Wanazuoni walikua kamwe hawaulizi kuhusiana na hali ya Dini ya mtu baada ya kujua mambo matatu juu ya mtu huyo ambayo ni: 'Anakutana na nani, anatembea na nani katika matembezi yake na marafiki zake ni nani.**'

Imam Al Amash alifariki mnamo mwaka 147 Al Hijra akiwa na Umri wa miaka 85.

IMAM QATADAH AL SADUSI 62 AH

Imam Abu Al Khattab Qatadah Ibn Diama Al Sadusi Al Basri alizaliwa huku akiwa kipofu katika Mji wa Basra mnamo mwaka 62 Al Hijra. Ingawa alikua na mtihani wa Ulemavu wa Macho lakini Imam Qatadah hakua ni mtu mwenye kuhisi vibaya na kulemaa kutokana na ulemavu huo, bali alikua ni mtu mwenye kujitolea katika kuendeleza Maisha yake katika njia sahih ya Imani ya Dini ya Kiislam.

Imam Qatadah aliitwa Al Sadusi kwa sababu kua katika sehemu aliyokua akitoka kulikua kuna Mwanazuoni aitwae Sadus Al Shaybani ambae alikua ni mwenye kusomesha Wanazuoni wengi sana wa Kabila lake.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Qatadah Al Sadusi alikua ni mtu mwenye Ufahamu makini sana kiasi ya kua alikua akikamata kila anachoasikia hapo hapo bila ya kuomba kurudiwa kwa jambo hilo kama anavyosema mwenyewe kua: '**Hakika mimi kamwe sijawahi kumwambia Mtu kua arudie kile alichoniambia. Kwani masikio yangu mawili hayasikii kitu isipokua hua ni yenye kukikamata hapo hapo na kukiweka kwenye Moyo wangu.'**

Tangu alipokua mtoto mdogo Imam Qatadah alikua ni mwenye hamu kubwa sana ya kujua kuhusiana na fani mbali mbali za Ilm ya Dini ya Kiislam, na hivyo alikua ni mwenye kujitolea kwa ajili ya kusafiri kutoka sehemu moja kuelekea sehemu nyengine kwa ajili ya kutafuta Ilm bila ya kujali kikwazo cha kutokua na uwezo wa kuona kwake.

Imam Qatadah Al Sadusi alisoma kwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwemo Anas Ibn Malik, Abd Allah Ibn Sarjis, Hanzala Al Khatib, Abu Razi *Radhi Allahu Anhum* na wengineo. Imam Qatadah alisoma pia kwa Wanafunzi wa Masahaba wakiwemo Imam Said Ibn Musayyib, Imam Abu Aliyah, Imam Ataa Ibn Abi Rabah, Imam Muhammad Ibn Sirrin, Imam Hasan Al Basr ambae alisoma chini yake kwa muda wa miaka 12, Imam Abu Mulih Ibn Usamah na wengineo.

Imam Qatadah Ibn Diama alikua hanukuu Hadith bila ya kua ni mwenye kua na Udhu, na alikua na kawaida ya kubadilika kwa muonekano wa Uso wake kutokana na kusikiliza Hadith kwa hisia kali sana ndani ya Moyo wake. Na alikua akijulikana pia kwa jina la *Faris ul Ilm* yaani Jeshi la Mtu mmoja la Ilm kutokana na ukubwa wa Ilm yake.

Kutokana na ufahamu wake, basi Imam Qatadah alikua ni mwenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi kile anachosomeshwa na Walimu wake, na hivyo alikua na Ilm kubwa ya Qur'an, Hadith na Fiqh ambapo Imam Ahmad Ibn Hanbal anasema kuhusiana nae kua: '**Ni nadra sana kumkuta mtu ambae ni mwenye uwezo wa kumzidi Imam Qatadah, lakini kama watu wakisema kua kuna kama yeye, basi hlo hua linawezekana**'

Imam Ahmad Ibn Hanbal anaendelea kusema kua: '**Qatadah ni mtu mwenye Ufahamu mkubwa sana wa kuhifadhi miongoni mwa watu wa Basra, kwani alikua hasikii kitu isipokua hua ni mwenye kukihifadhi hapo hapo.**'

Safari moja wakati Imam Qatadah alipokua akisoma kwa Imam Said Ibn Musayyib basi aliamua kua atakaa kwenye nyumba ya Said Ibn Musayyib kwa wiki moja tu, ambapo ilipofika siku ya tatu tu basi Imam Sayid Ibn Mussayib akamwambia Imam Qatadah: '**Nenda zako Ewe Kipofu kwani tayari umeshaniibia Ilm yangu yote**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na pia siku moja Imam Said Ibn Musayyib aliwaambia Wanafunzi wake: '**Hakika mimi sifikirii kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameumba mtu mwengine mwenye ufaham kama wake yeye huyu Qatadah**'

Na akasema tena Imam Said Ibn Musayyib kua: '**Hakuna Mtu aliekuja kwetu kutoka Iraq mwenye ufaham mkubwa wa kuhifadhi kama Qatadah**'

Imam Muhamamd Ibn Sirin amesema kuhusiana na Imam Qatadah kua: '**Qatadah ni Mtu mwenye uwezo mkubwa sana miongoni mwa watu wa Basra.**'

Imam Muammar nae alisema kua: **'Mimi nimemsikia Qatadah akisema kua: 'Hakuna Aya ya Qur'an ambayo mimi sikuwahi kusikia kitu chochote juu yake.''**

Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema pia kua: **'Qatadah ni mwenye kujua ufafanuzi wa Qura'na na tofauti juu ya mitzamo baina ya Wanazuoni juu yake'**

Imam Humaam amesema kua: **'Alisema Qatadah kua: 'Imepita miaka 20 na mimi sijawahi kutoa Fatwa kutokana na Mtizamo au Makisio yangu.'** Kwani alikua ananukuu kila kitu anachoulizwa juu yake, kutokana nakua na uhifadhi mkubwa sana wa kuhifadhi juu ya kila jambo.

Imam Sufyan Ath Thawry aliwahi kuuliza kuhusiana na Imam Qatadah kwa kusema: **'Hivi Jee kuna mtu kama Qatadah?'**

Imam Muamar aliwahi kusema kua: '**Sijawahi mimi kuona Mwanafiqh kama Az Zuhri, Hammad na Qatadah.'**

Imam Adh Dhahabi anasema kua: **'Mbali ya kua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith na mwenye uhifadhi mkubwa sana lakini Qatadah alikua ni pia ni mtaalamu mkubwa wa Lugha ya Kiarabu, Matukio ya Historia ya Kiarabu na Histori ya Makabila ya Kiarabu'**

Imam Qatadah Al Sadusi alikua ni mwenye kumaliza kisomo cha Qur'an kila baada ya siku Saba na ilipokua ikifikia mwezi wa Ramadhani basi alikua akisoma Mas-haf nzima ndani ya siku 3.

Akasema Abu Ubayd kua: '**Sisi tulikua tukikusanyika kwenye Nyumba ya Qatadah kila siku kwa ajili ya kumuuliza masuali ya fanimbali mbali ya I'm, kwani alikua yuko juu sana katika Fani tofauti kiasi ya kua ilikua ni nadra kukutana na mtu mwenye sifa zake, alikua na Ilm kubwa ya Tafsir, Hadith, Fiqh na kila somo kuanzia kwenye Historia hadi kwenye Mashairi**'

Na Imam Muhamamd Ibn Sirin kua: **‘Qatadah ni mmoja kati ya Watu ambao wenye Ufahamu madhubuti sana katika kuhifadhi.’**

Anasema Umar Ibn Abd Allah kua: **‘Qatadah Ibn Diamah alienda kwa Said Ibn Musayyib, na akamuulizia kuhusiana na masuali kadhaa ndani ya siku nne na akapata majibu yake, wakati anaendelea kuuliza, basi Said Ibn Musayyib akamuuliza: ‘Hivi wewe tangu umekaa kwangu, umekua ukiuliza masuali tu, hivyo Jee nanifahamu lakini?’ Qatadah akasema: ‘Naam, nilikuuliza kuhusiana na hili ukanijibu hivi, nikakuuliza na lile ukanijibu vile, nikakuuliza na hili ukanijibi vile’ na hivyo akayaelezea masuali yote aliyouliza na kisha akayaelezea majibu aliyopata kutoka kwa Said Ibn Musayyib, hivyo Said Ibn Musayyib akashangazwa na Ufahamu wake Qatadah Ibn Diama na hivyo akasema: ‘*Subhanah Allah,* wewe ni Mtu wa ajabu sana ambae ni vigumu kupatika mfano wake.’’**

Amesema Imam Qatadah Ibn Diamah kua: **‘Amesema Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Kama Nyinyi mngekua mnajua kile nnachokijua mimi basi mngecheka kidoogo na mngelia sana’’**

Na alisema Imam Qatadah kua : **‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Yeyote yule anaependa kukutana na *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* nae pia anapenda kukutana nae, na yeyote yule asiependa kukutana nae *Allah Subhanah wa Ta’ala basi* na *Allah Subhanah wa Ta’ala hapendi kukutana nae.’* Hivyo Aisha *Radhi Allahu Anha* akasema: ‘Ya Rasul Allah, hivi jee mtu huyo asiependa kukutana na *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni kwa sababu ya Kifo au? Kwani kama ni hivyo basi sisi sote hatupendi kifo’’**

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘La sio hivyo, bali ni kutokana na kua Muumini anapopewa habari njema kuhusiana na Rehma za *Allah Subhanah wa Ta’ala,* na Raha ya Peponi basi hua ni mwenye kupenda kukutana na *Allah Subhanah wa Ta’ala,* Lakini mtu asieamini hua si mwenye kupenda kukutana na *Allah Subhanah wa Ta’ala* kutokana na kubashiriwa Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta’ala* juu yake.’

Amesema Imam Qatadah Ibn Diamah kua: ‘***Allah Subhanah wa Ta’ala* hua ni mwenye kufurahia *Istighfar* ya Mja wake kuliko vile anavyofurahia Mtu anaesafiri Jangwani na kisha akampoteza Ngamia wake, lakini akamuona Ngamia huyo baada ya kulala na kuamka kwake.**’

Imam Qatadah Al Sadusi alisema pia kua: ‘**Dua hua haikubaliwi bila ya kufanya Mema, hivyo yeyote yule atakaefanya Mema basi Dua yake hua ni yenye**

kukubaliwa.’ Na **‘Dua ya Mtu mwenye kumkumbuka Mola wake anapokua faragha na anapokua hadharani hua ni yenye kukubaliwa.’**

Na akasema tena kua: ‘**Kamwe Usiwaheshimu watu kutokana na Mali zao au kutokana na Watoto wao, bali waheshimu watu kutokana na Imani yao na Amali njema zao.**’

Na pia akasema: **‘Kufanya Dhambi ndogo humpelekea Mtu kufanya Dhambi zaid na kwenye maangamizo, na kuzikimbia Dhambi ndogo humpelekea Mtu kua ni mwenye kuokoka kutokana na kufanya Dhambi kubwa zaidi.’**
Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi alisema: **‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* huinyanyua Darja ya Mtu mwenye Unyenyekevu.’**

Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi alisema: ‘**Enyi Ibn Adam hakika nyinyi mnataka kutoa Sadaqah bila ya ugumu wala matatizo yeyote?, wakati Nafsi ya Ibn Adam hua ni yenye kuadharau, yenye uvivu na kuona aibu, hivyo Muumini anatakiwa awe ni mwenye Subra, Ustahmilivu juu ya ugumu wa mambo hayo na kisha ndio ataweza kua na uwezo wa kufanya mema na kutoa Sadaqa.’**

Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi alisema kua: ‘**Kabla ya kuja Uislam basi Watu walikua wamelala katika usingizi wa upotovu, na Uislam ulipokuja, basi wale walioamini wakawa ni wenye kuamka kutokana na Usingizi huo, na kushikamana na njia zitakazo wapatia wao ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* usiku na mchana kwa kutumia Mali zao na Uhai wao, na wakafanikiwa kuipata ridhaa hio ya Mola wao.’**

Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi alisema kua: **‘Wale watakakua ni wenye kumtii *Allah Subhanah wa Ta’ala* katika Dunia hii basi ndio watakaokua ni miongoni mwa waliochaguliwa kupata Rehma za *Allah Subhanah wa Ta’ala* katika Siku ya Malipo.’**

Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi alisema tena kua: **‘Peponi kuna Dirisha linalooneshea upande wa Motoni, ambapo watu wa Peponi watawaona watu wa Motoni kupitia kwenye Dirisha hilo na kisha watawauliza watu hao wa Motoni: ‘Hivi Jee mna hali gani huko? Kwani sisi tumeingizwa Peponi kutokana na kuyafuata Maarisho ya Kiislam’ ambapo nao watasema: ‘Na Sisi tumeingizwa Motoni kutokana na kuasi kwetu kwa kukataa yale tuliyokua tukiamrishwa’’**

Imam Qatadah Al Sadusi alifariki mnamo mwaka 117 Al Hijra akiwa na umri wa miaka 85 katika maeneo yanayojulikana kama Al Wasith yaliyopo baina ya Baghdad na Basra.

UMAR IBN ABD AL ‘AZIZ 63 AH.

Khalifah Umar Ibn Abd al ‘Aziz ambaye pia alijulikana kama *Amir ul Mu’minin* wa tano wa Uislam, alizaliwa nchini Misri mwaka 63 *Al Hijr* wakati Baba yake Abd al ‘Aziz alikua ni mtoto wa *Khalifah* Marwan na Mama yake alikua anaitwa Layla Bint Asim Ibn Umar Al Khattab *Radhi Allahu A’nhu*.

Abu Usama Zaid Ibn Aslam, anasema kua Babu yake alihadithia kua ‘**Siku moja nilikua pamoja na Sayyidna Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A’nhu* katika matembezi ya usiku kufuatilia matatizo ya watu wake, walisimama katika nyumba moja na kuegemea ukuta wa nyumba hiyo ili kupumzika. Mara wakasikia sauti ya mama na bint yake zinazungumza ndani ya nyumba hiyo, ambapo yule mama alikua akimwambia binti yake maziwa yamepatikana kidogo hivyo wayatie maji kabla kuyauza asubuhi yake.**

Binti yule alimwambia Mama yake ‘**Hujui kua *Amir Al Mu’minin* amekataza kutia maji katika Maziwa?’** Mama akamjibu ‘**Hata kama amekataza lakini sasa hivi hayupo karibu yetu na wala hatuoni**’, yule Binti akagoma na kumwambia Mama yake, ‘**Hata kama *Amir ul Mu’minin* hayupo lakini *Allah Subhanahu wa Ta’ala* yupo na anatuona, hivyo siwezi kumtii Allah mbele za watu na kumuasi wakati wa faragha.**’

Amir Al Mu’minin aliposikia habari hizi alimtuma babu yake Zaid ibn Aslam, awafuatilie watu wale wanaokaa ndani ya nyumba ile asubuhi yake, ili kujua kama Bint yule ameolewa au la. Jawabu alilolipata lilikua kwamba yule bint bado hajaolewa. Kwa kua *Amir al Mu’minin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A’nhu* alikua na watoto watatu wa kiume na mdogo kati yao aliekua akiitwa Asim alikua bado hajaoa. Hivyo *Amir al Mu’minin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A’nhu* aliamua kumposea Bint yule kwa jili ya Asim Ibn Umar. Kwa bahati nzuri katika ndoa hiyo wakajaaliwa kupata mtoto wa kike alieitwa Layla, mtoto huyu ndio baadae akaolewa na Abd al ‘Aziz na wakapata mtoto wa kiume ambae walimwita Umar Ibn Abd al ‘Aziz.

Umar Ibn Abd al ‘Aziz alipokua mkubwa kidogo aliondolewa Misri ambako wazee wake walikua wakiishi na akapelekwa Madinah ili akakulie katika mazingira mazuri ya dini ya kiislam. Alipofika Madinah alisoma *Qur’an*, *Hadith* na *Fiqh* kwa Walimu na Wanazuoni mbalimbali. Alipofariki Baba yake, *Khalifah* Abdul Malik alimchukua Umar Ibn Abd al ‘Aziz katika makao makuu ya utawala huo nchini Syria katika mji wa Damascus na kumuozesha bint yake anaeitwa Fatimah bint Abdul Malik.

Mwaka 86 *Al Hijr* Umar Ibn Abd al 'Aziz alichaguliwa kua Gavana wa mji wa Madinah ambako alitawala hadi mwaka 93 *Al Hijr*. Umar Ibn Abd Al 'Aziz alikua akisifika kwa utawala wake wa haki na uadilifu. Zaid Ibn Aslam alisema '**Sikuwahi kusali nyuma ya Imam baada ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ambae anafana nae katika sala zake kama Umar Ibn Abd al 'Aziz** '.

Mwaka 88 *Al Hijr*, *Khalifah* Al Walid Ibn Abd Al Malik alimuamrisha Umar Ibn Abd Al 'Aziz, autanue na kuuzidisha *Masjid An Nabawi* wa Madinah, hivyo ikabidi chumba chenye kaburi la Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, Abu Barkr Saddiq na Umar Ibn Al Khatab kuingizwa ndani ya Msikiti huo. Wanazuoni saba wa Mji wa Madinah wa wakati huo miongoni mwao akiwemo Umar Ibn Abd Al 'Aziz, walikubaliana juu ya jambo hilo, isipokua Said Ibn Al Musayib ambaye alishauri kua chumba hicho kisiingizwe ndani ya Msikiti bali na kiwachwe kama kilivyo ili kiwe kama kumbukumbu kwa Waislam kuona na kujizoesha maisha halisi aliyokua akiishi Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* hivyo kuacha kuendekeza maisha ya Dunia.

Katika wakati wa kipindi hicho, Miskiti ilikua haina Mihrab (*Sehemu ya kibla ambayo Imam anakaa wakati wa kusalisha*), lakini ilikua na alama tu ya kuonesha kua upande fulani ni Kibla. Hivyo wakati matengenezo ya Masjid Nabawi yanaendela, Umar Ibn Abd Al 'Aziz akaamrisha ijengwe *Mihrab* ya nusu duara ili iwe ndio alama ya kuonesha upande wa Kibla. Huo ndio ukawa mwanzo wa Miskiti duniani kua na *Mihrab*.

Historia ya Dunia inaonesha kua Wislamu ni watu wa mwanzo kuanzisha Maktaba na Hospital, Hospitali ya mwanzo Duniani ilijengwa na *Khalifah* Al Walid Ibn Abdul Malik katika mwaka 88 *Al Hijr*, na ilikua ikijulikana kama *Bimaristan*, Bimaristan hii ilijengwa karibu na mji wa Damascus, na ilikua wodi za kulalia wagonjwa wa maradhi ya aina tofauti.

Baada ya kufariki *Khalifah* Al Walid, alitawala *Khalifah* Sulayman ambae hata hivyo hakutawala mda mrefu na baada ya miaka mitatu aliumwa sana hadi kukaribia kufa, hivyo aliamua kumchagua Umar Ibn Abd Al 'Aziz ambae alikua binamu yake, awe mrithi wake wa *ukhalifa*. Mwaka 99 *Al Hijr* baada ya kufariki *Khalifah* Sulayman, Umar Ibn Abd Al 'Aziz akawa *Khalifah* ambae katika Makhalifah wote wa Kiislam hamna aliewahi kuwekwa katika daraja moja na *Amir ul Mu'minin* wanne wa mwanzo wa Uislam isipokua Umar Ibn Abd Al 'Aziz.

Umar Ibn Abd Al 'Aziz baada ya kuchaguliwa aliletewa gari la Farasi la Kikhalifah apande, lakini akakataa na kusema kua yeye ni sawa na watu wengine hivyo haina haja ya kupanda gari la farasi na pia alikataa kukaa katika kasri la kifalme na badala yake aliamua kuishi katika nyumba yake ya kawaida tu. Umar Ibn Abd Al 'Aziz kwanza alijiweka sawa yeye, akaiweka sawa familia yake na kumwambia mkewe Fatimah, kua

mapambo yote aliyokua amepewa na Baba yake ayarejeshe *Bait ul Maal*, aidha watengane na mapambo hayo au watengane wao wenye kwa wenyewe. Hivyo Fatima ambae alikua mtoto wa *Khalifah* na pia dada wa *Khalifah*, aliamua kuyarejesha mapambo yale *Bayt ul Maal* na kukaa na Umar Ibn Abd Al ‘Aziz.

Baadae Umar Ibn Abd Al ‘Aziz alizitaifisha mali zote za Banu Umayyah zilizopatikana kwa kutumia mali ya Waislam na kuzirudisha katika *Bayt ul maal*. Halafu akabadilisha viongozi wote waliokua sio waadilifu na kuweka waadilifu. Na kuwataka wasikilize na kutatua matatizo ya wale walio chini yao kwa haki na uadilifu.

Umar Ibn Abd Al ‘Aziz aliamua kurudisha tena nguvu ya Mamlaka ya *Ijmaá* au *Shura* katika Utawala kama vile ilivyokua hapo kabla, katika kipindi cha *Amir ul Muúminun* wanne waliotangulia. Mamlaka hayo yalikua na wawakilishi Wanazuoni wakuu 70 wa Ummah wa Kiislam uliokua chini ya Mamlaka yake. Miongoni mwa Wanazuoni hao, 10 walikua ni wenye kutoka katika Mji wa Madina ambao walikua ni: **Urwa Ibn Al Zubayr, Ubaydu Allah Ibn Abd Allah Ibn Utbah, Abu Bakr Ibn Abd Rahman, Abu Bakr Ibn Sulayman Ibn Abi Khaythama, Sulaiman Ibn Yassar, Al Qasim Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr As Siddiq, Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab, Abd Allah Ibn Amir Ibn Rabbiah na Kharijah Ibn Zayd.**

Akawaambia Wawakilishi wa *Ijmaá* hiyo: **‘Kwa hakika nimekuiteni na kukuchagueni kwa ajili ya kazi ambayo malipo yake yapo kwa Allah *Subhanah wa Taála* na kua nyinyi mtakua ndio wasimamizi wa haki. Sitamani kuamua jambo lolote lile bila ya kuwepo kwa *Ijmaá* yenu nyote, au ya baadhi yenu miongoni mwa watakaokuwepo katika *Ijmaá* husika. Ikitokea kua miongoni mwenu atamuona mtu anamdhulumu mwenzake au itakapotokea mkajua kuhusiana na dhulma yeyote ya Magavana wangu basi Wallahi ni wajibu wenu kwangu kunijuulisha.’**

Siku moja Gavana wa Khurasan Jarrah Ibn A’bd Allah alimlalamikia kwa barua *Khalifah* Umar Ibn Abd Al ‘Aziz na kumwambia kua watu wake ni watukutu na hawakubali kumtii hadi atumie nguvu ya Mjeledi au Upanga. Umar Ibn Abd Al ‘Aziz akamjibu na kumwambia **‘Kauli yako ya kua watu wako hawasikii hadi utumie Upanga ama Mjeledi haingii akilini, inaonekana utawala wako hauna uadilifu na si wa haki hivyo eneza haki na uadilifu kwa watu wako na hapo watakutii**’.

Aliusia Umar Ibn Abd Ul Aziz kwa kusema kua: ‘**Yeyote yule asiekua na kitu cha kutoa Sadaka basi na afunge bada yake.’**

Umar Ibn Al Aziz alikua ni mtu mwenye kua na khofu sana juu ya jukumu la uadilifu kwa watu waliokua chini yake, kwani alikua akijua uzito wa jukumu lake mbele ya Allah *Subhanah wa Taála*. Anasema Fatima mke wa Umar Ibn Abd Al ‘Aziz anasema ‘**Usiku**

unapoingia, ninapokua pamoja na Umar kitandani, alikua akikumbuka kuhusu wajibu wake juu ya watu wake na uzito wa jukumu hilo mbele ya Allah, alikua anakua kama ndege alieanguka ndani ya maji na huanza kulia, hadi humfunua shuka alilojifunika na husema 'Ya Allah, ningependa sana hili jukumu langu nililokua nalo lingelikua mbali nami kama ulivyo umbali baina ya Mashariki na Magharibi''.

Anasema Ata'a '**Kila siku usiku Umar alikua akikaa na Wanazuoni na kukumbushana kuhusu kifo na siku ya Kiama na huanza kulia kama vile kuna mtu amefariki**'.

Amir ul Mu'minin Umar Ibn Abdul Aziz alikua mara kwa mara akiomba ushauri wa watu wenye *I'lm* kuhusiana na mambo mbali mbali juu ya utawala wake, mara moja alimuandikia barua Hasan Al Basr kumuomba ushauri kuhusiana na utawala wake, hivyo Hasan Al Basr akamjibu Umar Ibn Abdul Aziz katika barua kwa kumwambia.

'**Fahamu ewe *Amir ul Mu'minin*, kua Allah *Subhanah wa Ta'ala*, amemfanya Imam Muadilifu kua kigezo kwa kila anaejifunza, rekebisho kwa kila asiekaa sawa, muongozo kwa kila aliepotoka, nguvu kwa kila alie dhaifu, uadilifu kwa kila aliedhulumiwa, liwazo kwa kila aonewae huruma. Imam Muadilifu ewe *Amir ul Mu'minin*, ni kama mchungaji, akiwaangalia Ngamia awachungao, akiwatafutia Majani yaliyonawiri kwa ajili yao, akiwapeleka mbali na malisho hatari, akiwalinda kutokana na wanyama wakali, na pia akiwalinda kutokana na madhara ya joto na baridi.**

Na Imam Muadilifu, ewe *Amir ul Mu'minin*, ni mteteaji wa Mayatima, ni hazina ya masikini, mlezi wa watoto wadogo na mhudumiaji wa watu wazima. Imam Muadilifu ewe *Amir ul Mu'minin*, ni moyo kwa viungo vya mwili: vyote hua salama pale unapokua salama na vyote hupotoka pale unapopotoka. Imam Muadilifu ewe *Amir ul Mu'minin* hua ni muombezi baina ya Allah *Subhanahu wa Ta'ala* na viumbe wake, anasikia maneno ya Mola wake na kuwasikilizisha watu wake maneno ya hayo, humuangalia Mola wake na kuwaonesha watu Mola wao, humtii Mola wake na kuawafnya watu wake kumtii.

Hivyo ewe *Amir ul Mu'minin*, usifanye kwa kile alichukupa Allah *Subhanah wa Ta'ala*, kama vile mtumwa aliepewa kila kitu na bwana wake, utajiri wake, mali yake halafu akaitumia sivyo mali hiyo ya bwana wake na kuwafukuza watoto wa bwana wake, akajitia ufukara na kuiteketeza mali yake.

Ewe *Amir ul Mu'minin*, faham kua *Allah Subhanahu wa Ta'ala* ameteremsha amri zake kwa ajili ya kuhukumu ki sharia'h ili kuwalinda watu na uovu. Jee itakuaje,

ikiwa yule anaewasimamia anawastahiki? Na yeye akateremshia hukmu ya kulipiza kisasi kwa kuwapa maisha waja wake. Jee itakuaje ikiwa mtu anaesimamia kulipiza kisasi akatoa adhabu ya kifo badala yake?

Ewe *Amir ul Mu'minin*, kumbuka kifo na kile kinachofuata baada yake, na udogo wa wasaidizi uliokua nao kujilinda na kifo. Hivyo jitayarishe na kifo na yale mabaya zaid yatakayofuatia baada ya kifo.

Ewe *Amir ul Mu'minin*, faham kua kuna sehemu kwa ajili yako mbali na hiyo sehemu uliyokua nayo hivi sasa, na utakaa kwa mda mrefu sehemu hiyo, na utatengana na marafiki zako. Utakua peke yako na katika hali ya upekee. Hivyo fanya matayarisho ambayo utakwenda nayo huko kwani kumbuka:

﴿يَوْمَ يَفِرُّ ٱلْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ۞ وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ ۞ وَصَـٰحِبَتِهُ وَبَنِيهِ﴾

Yawma yafirru almar'u min akheehi; Waummihi waabeehi; Wasahibatihi wabaneehi (*Surat Abasa 80:34-36*).

Tafsir: ***'Katika siku ambayo, mtu atamkimbia ndugu yake, na mama yake na baba yake na mke wake na watoto wake'***

Na kumbuka ewe *Amir ul Mu'minin*:

﴿أَفَلاَ يَعْلَمُ إِذَا بُعْثِرَ مَا فِى ٱلْقُبُورِ ۞ وَحُصِّلَ مَا فِى ٱلصُّدُورِ﴾

Afala yaAAlamu idha buAAthira ma fee alquboori; Wahussila ma fee alssudoori (*Surat Al Adiyat 100:9-10),*

Tafsir:'**Hajui yeye kuhusiana na Wakati vilivyokuwemo ndani ya makaburi vitakapotolewa nje, Na vilivyokuwemo ndani ya vifua vikawekwa wazi.**

Na kumbuka ewe *Amir ul Mu'minin* siku watu watakaposema:

﴿مَا لِهَـٰذَا ٱلْكِتَابِ لاَ يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلاَ كَبِيرَةً إِلاَّ أَحْصَاهَا﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ma lihadha alkitabi la yughadiru sagheeratan wala kabeeratan illa ahsaha. (*Surat Al-Kahf 18:49*).

Tafsir: ***'Ni kitabu gani hiki ambacho hakikuacha kitu, makubwa wala madogo, yote yamerikodiwa kwa nambari.'***

Na sasa hivi ewe *Amir ul Mu'minin,* unao wasaa, mbele ya kifo na mwishoni mwa matumaini, Hivyo ewe *Amir ul Mu'minin,* usije ukatoa hukmu za zama za kijahiliya juu ya waja wa Allah *Subhanahu wa Ta'ala,* na usipite katika njia za wale waliovuka mipaka, usjie ukampa nguvu mwenye kibri, dhidi ya mpole, kwani huyo hatotekeleza haki ya Muumin, wala ya yale yanayotakiwa kutekelezewa, kiasi ya kua itakubidi ukubali makosa yako na makosa ya wengine, na kubeba mizigo yako na ya wengine pia.

Usihadaike na wale watakao endesha maisha ya anasa kutokana na kukuharibia wewe, na kufaidika na mazuri ya dunia kwa kusababisha mazuri yako ya akhera kutoweka. Na usihesabie nguvu na uwezo wako hapa duniani bali kufikiria ni kipi kitakachokua katika uwezo wako utakapokua katika fundo la mauti, na kulazimishwa kusimama mbele ya Allah *Subhanahu wa Ta'ala* pamoja na *Malaika*, Mitume, na nyuso zitakapo geukia kwa yule asiekufa na anayeishi milele.

Na mimi, ewe *Amir ul Mu'minin*, ijapokua sina *I'lm* sana kama wale waliotangulia na waliokua na *I'lm* zaid yangu, lakini kamwe sikusita kukuusia na kukupa ushauri, nnakutumia wewe barua yangu kama daktari anaemlazimisha rafiki yake mpendwa kunywa dawa chungu isiokubalika, kwa sababu tu ana hamu na matumaini ya kumpa afya na uzima.

***Asalaam Alaykum ya Amir ul Mu'minin*, Rehma na Baraka za Allah ziwe juu yako'**

Umar Ibn Abd Al Aziz alikua ni mtu mnyenyekevu sana hata pale anapokua ndani ya nyumba yake, kiasi ya kua siku moja alikuja mwanamke kuomba msaada nyumbani kwa Umar Ibn Abd al 'Aziz na baada ya kupiga hodi, Fatima alifungua mlango na kumkaribisha ndani Mwanamke yule, baada ya kuinga ndani yule Mwanamke alishangaa na kumuuliza Fatima '**Humuogopi Allah ewe mke wa *Khalifah* Umar? Unakaa katika hali ya kujistiri namna hivyo wakati ukiwa mbele ya mfanyakazi wako ndani wa kiume?**', Fatima akatabasamu na kujibu '**Huyo umfikirae kua ni mfanyakazi, ndio *Khalifah* Umar Ibn Abd al 'Aziz mwenyewe!**'

Umar Ibn Abd al 'Aziz alikua ni kiongozi wa mwanzo kujaribu kwa dhati kupatanisha tofauti za kisiasa zilizokuwepo baina ya Waislam. Kwani tangu wakati wa Muawiyah, ilikua ni jambo la kawaida kwa Makhatibu kulikashifu jina la Ali Ibn Abi Talib *Radhi*

Allahu Anhu, hivyo Umar Ibn Abd Al ‘Aziz aliifuta tabia hii na badala yake akaamrisha kuanzishwa kusomwa kwa aya ya 90 ya *Surat An Nahl* inayosomwa katika mwishoni mwa kila khutba ya sala za Ijumaa na Idd zote Duniani kote tangu wakati wa Utawala wake hadi hii leo. Aya hiyo inasema:-

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يَأْمُرُ بِٱلْعَدْلِ وَٱلْإِحْسَانِ وَإِيتَآءِ ذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنْكَرِ وَٱلْبَغْىِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ﴾

Inna Allaha ya’muru bialAAadli waal-ihsani wa-eeta-i dhi alqurba wayanha AAani alfahsha-i waalmunkari waalbaghyi yaAAi*dh*ukum laAAallakum tadhakkaroona (*Surat An-Nahl, 16:90*)

Tafsir: ***Hakika Allah anaamrisha uadilifu na ihsan, na kuwasaidia ndugu na jamaa, na amekataza al Fahshaa (Madhambi), uovu na udhalim wa aina zote, Anakuonyeni ili muwe wenye kukumbuka.***

Hivyo ingawa kusudio la A*mir ul Mu’minin* Umar Ibn Abd Al Aziz kuamrisha kuanza kutumika kwa aya hii katika kila Khutba ya Sala ya Ijumaa ni kwa ajili ya kuleta umoja miongoni mwa Waislamu Duniani, lakini inasikitisha kua baadhi ya wasiojua asili, kusudio wala maana ya aya hua ni wenye kusoma Khutba za Sala za Ijumaa zenye mifarakano baina yawafuasi wa Madhhab tofauti ya Kiiislam ndani yake na kisha kumalizia Khutba hizo kwa kuisoma aya hii.

Umar Ibn Abd al ‘Aziz aliwapa heshima na haki zao Bani Hashim na wanaopingana nao, na aliwakaribisha *Muhakkimah* pia kwa kumwandikia barua kiongozi *Muhakkimah* wa wakati huo ambae ni Abu Ubaydah Muslim Ibn Abi Karima na kumualika kuja kufanya majadiliano kuhusu *Khalifah* Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu A’nhu,* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu A’nhu,* na Muawwiyah Ibn Abu Sufyan na kumwambia kua kama wakiweza kumsadikisha kihoja juua yao basi Umar Ibn Abdul Aziz atakua pamoja nao. Jambo ambalo liliwafanya *Muhakkimah* kutuma wajumbe wao 6 sita wenye kujua zaidi ki I’lm miongoni mwao, ambao ni:-

Hatat Ibn Khatib, Salim Ibn Zaqwani Al Hilali, Jafar Ibn Samak Al Abdi, Abu Al Hur Abdi Ibn Al Husein, Hayyan Al Araj na Al Mutabar Ibn Umara, na baada ya mazungumz baina yao na Khalifa Umar Ibn Abdul Aziz walikubaliana juu ya mambo mengi na wakakosana katika mambo kidogo sana. Ambapo baada ya watu hao kurudi basi Abu Ubaydah Muslim Ibn Abi Karimah akasema: ‘Ya Laiti Kama watu wote wangemtii’. Yaani akimaanisha kua walikubaliana hata katika hayo

mambo waliyokua wamekhtilafiana. Na hadi hii leo vitabu vya Wafuasi wa Madhhab ya Ibadh iwe vya dini, hadith au mashairi basi vimejaa sifa bora na za uadilifu za Khalifa Umar Ibn Abdul Aziz.

Umar Ibn Abd Al ‘Aziz alikua ni Kiongozi wa kwanza wa Kiislam kuacha kushughulikia kuhodhi maeneo ya ardhi ya sehemu nyengine, na kuanza kushughulikia kuuimarisha Uislam ndani ya eneo lililo ndani ya utawala wake, kitu ambacho kilisababisha kua na utawala usio na upinzani wala uasi ndani ya Utawala yake.

Katika kipindi hiki cha Utawala wa umar Ibn Abd Al Aziz, Uislam ulinawiri kama ulivyonawiri wakati wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A’nhu* na hizi ndio miongoni mwa sababu zilizowafanya Wanazuoni kumuweka Umar Ibn Abd Al ‘Aziz katika cheo cha *Amir ul Mu’minin* wa tano baada ya Abu Bakr Siddiq *Radhi Allahu A’nhu*, Umr Ibn ul Khattab *Radhi Allahu A’nhu* Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu A’nhu* na Ali Ibn Abu Talib. Sufyan Ath Thawri na Imam Al Shafi’i walisema **‘Makhalifah wako watano, Abu Bakr, Umar, Uthman, Ali na Umar Ibn Abd al ‘Aziz ’**.

Imam Ibn Hajar anasema katika *Fat-hul Barri*, **‘Mtu wa mwanzo kuandika *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* ni Muhammad Ibn Muslim Ibn Ubayd Allah Ibn Shihab Al-Zuhri, mwishoni mwa karne ya kwanza baada ya kuamrishwa na Umar Ibn Abd Al ‘Aziz kufanya hivyo**’.

Imam Bukhari anasema kua: **‘Umar Ibn Abd Al ‘Aziz aliwaandikia Wana*fiqh* wote walio chini ya mamlaka yake na kuwaambia kua wazitafute na kisha wazikusanye *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam*.**’

Katika barua yake aliyomuandikia Abu Bakr Muhammad Ibn Amr Ibn Hazm Al Ansari alielezea sababu ya kuamrisha ukusanywaji na uandikwaji wa *Sunnah* za Nabii *Salallahu A’layhi wa Salam* kwa kusema: **‘Tafuteni *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam*, au *Sunnah*, au vitendo vyake, halafu mniandikie, kwani nnaogopa kua *I’lm* hii itapotea pamoja na Wanazuoni wake.’**

Umar Ibn Abd al ‘Aziz ni *Khalifah* wa kwanza kuruhusu kutafsir *Qur’an* kutoka katika tafsir ya kiarabu kwenda lugha nyengine. Utawala wa *Khalifah* Umar Ibn Abd Al ‘Aziz ulidumu kwa miaka miwili na miezi mitano na kumalizika baada ya kufariki kwake katika mwezi wa Rajab, mwaka 101 *Al Hijr* Nyumbani kwake katika mji wa Homs ulioko nchini Syria akiwa na umri wa miaka 39.

Kipindi hiki pia kilikua ni kipindi cha mwishoni cha maisha ya Masahaba wa Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* kwani Sahaba wa mwisho kufariki alikua ni

Sahaba Amr Ibn Wathilah Ibn A'bd Allah *Radhi Allahu Anhu* ambae alifariki mwaka wa 100 *Al Hijr*.

IMAM ABU ZINAD 65 AH

Imam Abu Zinad Abd Allah Ibn Dakwan alikua ni mwanazuoni wa Mji wa Madina ambae alizaliwa kabla ya kufariki Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*. Ambapo Imam Abu Zinad alizaliwa mnamo mwaka 65 Al Hijra na alikua ni mwenye asili ya Uajemi katika familia ya Watumwa waliokua wakimilikiwa na Ramla Bint Shaybah Ibn Abd Shams Ibn Abd Ul Manaf.

Imam Abu ZinAd alikua ni mwenye kukutana na Anas Ibn Malik, Zaid Ibn Thabit na Abd Allah Ibn *Umar Radhi Allahu Anhum.* Na pia alisoma kwa Wanazuoni wakubwa wa kizazi cha waliofuatia baada ya Masahaba kama vile Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar, Imam Kharijah Ibn Zaid Ibn Thabit, Imam Sulaiman Ibn Yasar, Imam Qasim Ibn Muhammad Ibn Abi Bakr, Imam Urwah Ibn Zubayr, Imam Abd Allah Ibn Abd Allah Ibn Mas'ud, Imam Said Ibn Musayyab, Imam Ubaid Allah Ibn Abd Allah na Imam Al Qasim Ibn Muhammad na hivyo Imam Abu Zinad alikua ni mwenye Ilm kubwa ya Qur'an Hadith na Fiqh.

Imam Abu Zinad alikua ni kama Mfalme katika enzi zake kutokana na wingi wa Wanafunzi aliokua nao na alikua akijulikana kama *Amir Ul Muuminin* wa Hadith ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake alikuwemo pia Imam Malik, Imam Al Layth Ibn Saad na Imam Sufyan Ath Thawry.

Kwani anasema Imam Al Layth Ibn Saad kua: '**Abu Zinad aliingia kwenye Msikiti wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama Sultan kwani alikua akifuatwa na Wanafunzi 300 ambao walikua wakiuliza Masuali juu ya Hadith, Fiqh, na Lugha na hukaa nae kwa mda mrefu kabla ya kumfuata Rabiah**'

Ambapo alisema Imam Sufyan ATh Thawry kua: '**Abu Zinad alikua ni *Amir ul Muuminin* wa fani ya Ilm ya Hadith.**'

Imam Yahya Ibn Main akasema kua: '**Abu Zinad ni Thiqah na mwenye hadith sahih**'

Na akasema Imam Ali Ibn Madini kua: '**Hakuna katika Mji wa Madina Mtu ambae baada Tabiina alikua ni Mcha Mungu kama Ibn Shihab, Yahya Ibn Said, Abu Zinad na Bukayr Ibn Ashaji.**'

Ambapo anasema Abu Zara Al Dimashq kua: **'Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema kua Abu Zinad alikua na Ilm kubwa zaidi kuliko Rabiah.'**

Na Imam Abu Abu Hatim akasema: **'Imam Abu Zinad ni Mwanafiqh anaeaminika, Mwenye kufuata Sunnah na mwenye hoja ambazo hua zinasimamia kwenye watu wanaoaminika katika kunukuu kwake.'**

Anasema Imam Abu Yusuf kua amesema Imam Abu Hanifa kua: '**Mimi nilienda katika Mji wa Madina na nikaenda kwa Abu Zinad na niakmuona Rabiah na watuwalikua wamemzonga Rabia huku Imam Abu Zinad akiwa na Ilm kubwa zaidi miongoni mwao watu wawili hao.'**'

Imam Ahmad Ibn Abi Khaytham alisema kua: '**Imam Abu Zinad ni Mwanafiqh wa Watu wa Madinah na alikua ni muweka Mahesabu wa Khalid Ibn Abd Ul Malik Ibn Al Harith Al Hakam katika Mji wa Madina.**'

Imam Abu Zinad aliulizwa siku moja: '**Kwanini unazipenda Dirham wakati hua ni zenye kuweza kukuangusha Duniani?**' ambapo nae akasema: '**Kama zitaweza kunivuta karibu na Dunia basi zitaweza pia kunisukuma kutokana nayo.'**

Na anasema Imam Muhamamd Ibn Saad kua: '**Abu Zinad alikua ni Muaminifu mwenye Hadith nyingi, Ufasaha wa Lugha na mwenye Hikma.**'

Imam Abu Zinad alifariki katika usiku wa mwezi 17 wa Ramadhani ndani ya siku ya Ijumaa wakati akiwa katika hali ya kutia udhu mnamo mwaka 130 Al Hijra.

IMAM AL QARI ABU AMR AL BASR 68 AH

Imam Al Qari Abu Amr Zuban Ibn Al Ala Ibn Ammar Al Mazini Al Basr alizaliwa mnamo mwaka 68 Al Hijra na ni mwenye asili ya maeneo ya Uajemi na kuzaliwa katika Mji wa Makkah na baadae wazee wake walihamia katika Mji wa Basra, na kisha yeye baadae akahamia katika maeneno ya Mji wa Kufah, Makkah na Madina kwa ajili ya kutafuta Ilm.

Imam Al Qari Abu Amr alikua ni Imam wa Qiraa cha Qur'an ambae amesoma kwa wanazuoni wengi zaidi kuliko Maimamu wote wa Qira'a, na alikua akifuatwa kwa aina ya Qiraa chake na watu wengi zaid ikiwemo watu wa Syria, Sudan, Misri na Yemen pia ingawa yeye mwenyewe alikua ni Mtu wa Basra. Ambapo Imam Al Asmai anasema

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kuhusiana nae kua: **‘Nimemsikia Abu Amr akisema kua: ‘Sijui mimi mtu yeyote yule kabla yangu ambae amesoma zaidi yangu.’’**

Ambapo ingawa Imam Abu Amr alikua ni mwenye Ilm kubwa ya Qur’an kiasi ya kua watu wengi walikua wakifuata aina ya kisomo chake cha Qur’an lakini Imam Abu Amr alikua si mwenye Ilm kubwa ya Hadith za *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* na ndio maana akaawa anasema Imam Abu Khaytham kua: **‘Hakuna pingamizi dhidi ya Abu Amr isipokua, hakua ni mwenye kuhifadhi Hadith’**

Imam Abu Muawwiyah Al Azhari nae anasema kua: **‘Abu Amr alikua ni mwenye Ilm kubwa zaidi miongoni mwa watu wenye Ilm ya Qiraa vya aina tofauti, na lugha ya Kiarabu na utofauti wa Kauli na lafdhi zake na mashairi pia’**

Imam Abu Amr alifariki katika ardhi ya Kufah mnamo mwaka 154 Al Hijra na kuacha Mwanafunzi wake mkuu ambae ni Yahya Ibn Mubarak Al Yazidi ambapo Imam Al Jazari anamzungumia kwa kusema kua: **‘Alikua ni mtaalamu wa Ilm ya Nahw, Mwalimu wa Kisomo cha Qur’an na alikua ni mtu mwenye kuaminika na mwenye Ilm kubwa sana’**

IMAM HASAN IBN SINAN 68 AH

Imam Abu Abd Allah Hasan Ibn Sinan alizaliwa mwaka 68 A Hijra katika maeneo ya Basra na hivyo alikua ni Mwanafunzi wa Imam hasan Al Basr, Imam Malik Ibn Dinar na Imam Thabit Al Bunani na alikua mtaalamu mkubwa wa Lugha tofauti ikiwemo Lughaya Kiarabu, Kiajeni na Kiyahudi pia.

Imam Hasan Ibn Sinan alikua ni mwenye Ilm kubwa sana na ni mcha Mungu sana kiasi ya kua aliamua kuifanyia kazi Ilm hio moja kwa moja, na hivyo kuachana na kusomesha Ilm ya Hadith, na moja alifunga Mwaka mzima kutokana na kua ni mwenye kujiuliza kuhusiana na ukuta uliojengwa na jirani yake, kua ukuta huo ulijengwa lini? Jambo ambalo yeye lilikua halimhusu.

Imam Hasan Ibn Sinan alikua ni mwenye Taqwa sana na kwake yeye ilikua rahisi kufanya hivyo kuliko kufanya kitu chengine chohote kile, kwani alikua anasema kua: ‘**Hakika kwangu mimi hakuna kitu rahisi kuliko kua na Taqwa kwani hua ni kuachana na kitu ambacho unashaka nacho na kufanya kile ambacho hua shaka nacho**.’

Ambapo safari moja Ima Hasan Ibn Sinan alirudi Nyumbani baada ya kutoka kuenda kusali Sala ya Idd, na alipoingia ndani basi mke wake akasema: **‘Hakika mimi nimeona Wanawake wengie sana wazuri’** na Imam Hasan Ibn Sinan akasema: ‘**Na mimi nilitoka lakini sikuona kitu chengine chochote zaidi ya dole gumba langu la mguu wangu.**’

Imam Hasan Ibn Bunani alikua ni mtu mkarimu sana na alikua akisema: ‘**Kama ingekua hakuna Masikini basi mimi nisingekua mfanya biashara**’ na alikua ni mwenye kufanya biashara pamoja na rafiki yake ambae ndie aliekua msimamizi wa Biashara hio, ambapo alikua akitumia pesa zake zote kwa ajili ya kuwasaidia Masikini.

Imam Hasan Ibn Sinan alikua ni mwenye kuenda kusimama katika wakati wa Usiku kufanya Ibada zake, kwani anasema Mke wake kua : ‘**Hasan alikua kila unapofika usiku mapema basi alikua anazima taa na kupanda na kitandani na kisha hua ananikumbatia ili nilale kama Mama anavyombembeleza Mtoto wake alale, na anapohakikisha kua nimelala basi huondoka Kitandani na kuenda zake kusali’.**

‘Hivyo siku moja nikamwambia: ‘Ewe Abu Abd Allah kwanini unajitesa hivyo hebu kua ni mtu mwenye msimamo wa kati na kati kwa nafsi yako’ hivyo nae akasema huku macho yake yakiwa yamejawa na machozi: ‘Usiseme zaidi kwani karibuni tu mimi nitakua ni mwenye kulala na sitoamka tena’’

Imam Hasan Ibn Sinan alikua si mtu mwenye kupenda kula sana hivyo katika Iftar yake na Daku Yake ilikua anakula kipande kimoja tu cha mkate. Na hivyo alikua ni mwenye mwili uliokonda sana, na mwishowe akawa taabani kutokana na kuumwa, hivyo Marafiki zake walimtembelea wakati alipokua anaumwa na wakamuuliza kuhusiana na afya yake ambapo nae akasema: **‘Hakika mimi nitakua mzima sana pale nitakapookolewa kutokana na Adhabu ya Moto.’**

Na alipoulizwa kama kuna kitu ambacho anakitamani basi alisema: **‘Natamani kua katika uhai wa siku ambao kumalizika kwa Mchana wake na usiku wake hua ni sawa na kipindi nilichoishi Duniani.’** Imam Hasan Ibn Sinan alifariki mnamo mwaka 151 Al Hijra.

IMAM ABD ALLAH IBN AWN 68 AH

Imam Abd Allah Ibn Awn Ibn Artaban Al Muzani Al Hafidh alizaliwa katika mji wa Basra ambapo alaisoma kwa Imam Hasan Al Basr, Imam Muhamamd Ibn Sirrin, Imam Makhul Al Shami na Wanazuoni wengineo wa kipindi cha wakati wake.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abd Allah Ibn Awn alisoma pia kwa Wanazuoni wa miji tofauti ikiwemo Sham, Hijaz na katika mji wa Kufah pia na alikua mwenye kuifadhi Hadith 7000 na muungaji mkono mkubwa wa Utawala wa Banu Ummayah na hivyo alihamia katika ardhi ya Sham kwa ajili ya kupigana vita vya Jihadi tu dhidi ya Maadui wa Uislam.

Imam Abd Allah Ibn Awn alikua ni Mtu ambae Mcha Mungu na asietumia ulimi wake kwa maneno yasiyokua na maana hivyo alikua si mtu wa kufanya Maskhara, na hakuwahi kumtukana si mtu tu bali hata mnyama kwani alikua ni mtu mwenye unyenyekevu wa hali ya juu, kiasi ya kua Watu walimfananisha na Imam Abd Allah Ibn Mubarrak.

Imam Abd Allah Ibn Awn alikua akisema: **'Kama ingekua hakuna kinachoandikwa basi mimi ningezungumzia sana kuhusiana na neema za *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu ya Waislam.'**

Kutokana Ucha Mungu wake basi safari moja Imam Abd Allah Ibn Awn ilimbidi awaachie huru watumwa wake wawili kwa ajili ya kujisafisha baada ya kuzungumza na Mama yake mzazi huku akiwa ameinyanyua sauti yake juu zaidi ya sauti ya Mama yake.

Ambapo anasema Qurrah Ibn Khalid kua: '**Sisi tulikua tukishangazwa na Ucha Mungu wa Muhammad Ibn Sirrin, lakini tulipouona Ucha Mungu wa Abd Allah Ibn Awn basi ulitufanya tuusahau Ucha Mungu wa Muhammad Ibn Sirrin**'

Imam Abd Allah Ibn Awn alikua ni Shaykh wa Hadith katika kipidi chake katika mji wa Basra, na alikua ni mtu ambae hajichanganyi na watu na alikua ni wenye kuaminika katika kila kitu na kila jambo. Na alikua ni mwenye kubakia kwenye Msala wake baada ya *Salat Al Fajr* haondoki hadi baada ya wakati wa *Salat Dhuha*.

Ambapo anasema Muadh Ibn Muadh kua: '**Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu Mcha Mungu kama Abd Allah Ibn Awn.**' Kwani Imam Abd Allah Ibn Awn alikua kila anapofikwa na mitihani na kua na hasira basi alikua akijiangalia Nafsi yake na hivyo hua ni mwenye kuiambia Nafsi yake: '**Ewe Nafsi yangu Allah akuingize kwenye Rehma zake.'**

Na ilipokua zinatajwa kasoro za wengine mbele yake basi alikua akisema: **'Hakika Allah ni mwingi wa Rehma.'**

Ambapo Imam Kharijah Ibn Musab anasema kua: '**Hakika mimi nilikua pamoja na Abd Allah Ibn Awn kwa mda miaka 24 na sikuwahi kufikiria hata mara moja kua Malaika watakua wamemuandika dhambi yeyote ile dhidi yake.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abd Allah Ibn Awn alikua ni mfanya biashara anaemiliki milango ya Maduka kadhaa ambayo alikua akiikodisha katika maeneo ya Soko la Basra, lakin alikua hakodishi mtu yeyote ambae ni Muislam bali alikua akiwakodisha wale wasiokua Waislam tu, na alipoulizwa kwanini hua anafanya hivyo basi alisema: '**Kila unapofika mwishoni mwa mwezi basi Kodi hua hua inawatia khofu wapangaji na mimi sitaki kua chanzo cha sababu ya kuwatia khofu na kuwakosesha utulivu Waislam wenzangu.'**

Imam Abu Awana amesema kua: '**Hakika mimi nimewaona watu lakini kamwe sikuwahi kuona watu kama wafuatao, Ayub Sakhtiyani, Yunus na Abd Allah Ibn Awn**'

Anasema Bikar kua: '**Hakika mimi sijawahi kumuona Abd Allah Ibn Awn akimfuatilia mtu yeyote kwa sababu yeye mwenyewe alikua ni mwenye kuishughulikia Nafsi yake tu.'**

Siku moja Imam Abd Allah Ibn Awn aliitwa na Mama yake, na hivyo katika kuitikia kwake basi akaitikia kwa sauti ya chini sana kiasi ya kua Mama yake huyo hakua ni wenye kumsikia na hivyo ikambidi amwite tena, na kutokana na kumsababishia Mama yake kua amwite mara mbili basi Imam Abd Allah Ibn Awn akaamua kuwaachia huru Watumwa wawili kua kama Fidya kutokana na kosa lake hilo.

Imam Abd Allah Ibn Awn alikua si mwenye kukasirika, kwani alikua ni wenye kumuombea Dua ya kusamehewa na Mola wake kila mtu anaetaka kumkasirisha yeye.

Ambapo alisema Imam Abd Ibn Mubarak kua: '**Hakika mimi sijawahi kumuona mtu akisali kama anavyosali Abd Allah Ibn Awn'**

Na akasema Muhamamd Ibn Fudayl kua: '**Mimi nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika ndoto usingizini huku akisema Mtembeleeni Abd Allah Ibn Awn kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* wanampenda Abd Allah Ibn Awn'**

Alisema Imam Abd Allah Ibn Awn: '**Enyi Ndugu zangu hakika mimi nakuusieni nyie pendeni mambo matatu: Kusoma Qur'an Asubuhi na Usiku, Kushikamana na Jamaa na Kukatazana Maovu.'**

Aliulizwa Imam Abd Allah Ibn Mubarak: 'Hivi ilikuaje mpaka Abd Allah Ibn Awn akafikia Darja aliyoifikia?' ambapo nae akajibu: '**Kwa Haki na Ukweli.'**

Alisema Imam Abd Allah Ibn Awn: '***Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam* Kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* Hua Ni Mwenye Kupenda Kumsaidia Yule**

Ibn Adam Mwenye Kupenda Kuwasaidia Ibn Adam Wenzake Wanapofikwa Na Matatizo'

Alisema Imam Abd Allah Ibn Awn: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam* Kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* Ana Malaika Ambao Katika Kila Wakati Wa Sala Hua Wenye Kunadia Kwa Kusema: 'Enyi Ibn Adam Simameni Dhidi Ya Moto Mliojiingiza Wenyewe Ndani Yake, Kisha Muuzime Kwa Sala.''**

Imam Abd Allah Ibn Awn Alifariki mnamo mwaka 151 Al Hijra.

IMAM AYUB AL SAKHTIYANI 68 AH

Imam Ayub Ibn Tamim Al Sakhtiyani alizaliwa katika Mji wa Basra nchini Iraq katika mwaka 68 Al Hijra ambao ulikua ndio mwaka aliofariki *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na alisoma kwa Imam Hasan Al Basr, Imam Muhamamd Ibn Sirrin, Imam Mujahd Ibn Jabr, Imam Said Ibn Jubayr, Ikrimah Mawla Ibn Abbas, Shaykhat Hafsah Bint Sirin, Imam Qatadah Al Sadusi, Imam Jabir Ibn Zayd, Imam Amr Ibn Shuayb, Imam Ibn Abi Malik, Imam Al Qasim Ibn Muhammad n.k

Ambapo kutokana na Ilm yake basi Imam Hasan Al Basr alimpa Imam Ayub Al Sakhtiyani jina la *Sayyid Al Fityan* yaani Bwana wa Vijana wadogo, kwani alikua na Ilm kubwa sana kiasi ya kua baadhi ya watu walikua pia wakimuita kwa jina Imam Hasan Al Basir *Al Saghir* yaani Imam Hasan Al Basr Mdogo na wengine walimwita kwa jina la *Imam Muhammad Ibn Sirrin Al Saghir*.

Anasema Maymun Al Ghazali alisema kua: **'Alikuja Ayub kwa Hasan Al Basr na akamuuliza masuali, na kisha akanyanyuka na kuondoka na alipoondoka basi Hasan Al Basr akasema: 'Huyu ni *Sayyid Al Fityan wa Mji wa Basra*''**

Ambapo kwa upande wa Imam Muhamamd Ibn Sirrin basi ilikua hakuna Mtu anaemheshimu na kumpenda kama Al Sakhtiyani kwani anasema Hammad Ibn Zayd kua: **'Hakuna Mtu aliekua akiheshimwa na Ibn Sirrin kama Ayub'**

Kwani Imam Muhammad Ibn Sirin alikua kama akinukuu Hadith kutoka kwa Imam Ayub Al Sakhtiyani basi alikua akisema: ***'Al Saduq* ameniambia mimi, kua..'**

Kwani ilikua kama utamuona Imam Al Sakhtiyani katika wakati akiwa anafanya Ibada ya Sala basi katika kusujudu kwake alikua na utulivu mkubwa kama Malaika, na anapozungumza basi hua ni mwenye kutiririkwa na Hikma na Busara tupu kutoka ndani ya Moyo wake na alikua ni mwenye kuachana na Dunia yake.

Ambapo anasema Imam Al Humaidi kua: '**Sufyan Ibn Uyaynah amekutana na Tabiina 86, na hapo hapo alikua ni mwenye kusema kua: 'Hakika mimi sijawahi kukutana na Mtu kama Al Sakhtiyan.'**'

Ambapo anasema Malik kua : **'Sisi tulikua tukienda kwa Ayub Al Sakhtiyani, na tunapomtajia Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi alikua akilia hadi ikawa tunamuonea Huruma.'**

Na amesema Hisham Ibn Urwa kua: '**Hakika mimi sijawahi kuona mtu katika Mji wa Basra kama Ayub Al Sakhtiyani na wala sijawahi kuona Mtu kama Masar katika Mji wa Kufah.**'
Ambapo Imam Shu'bah alikua akimwita Imam Ayub Sakhtiyani kua ni : '**Imam wa Wanazuoni.'**

Ambapo amesema Imam Hamamd Ibn Zaid kua: '**Ayub alikua akisoma Qur'an basi hasimami katika aya yeyote isipokua hua ni mwenye kusema *Inna Allaha wa Malaikatahu Yussaluna Aaala Nabbi* na kisha hukaa kimya**'

Ambapo anasema Imam Shu'bah kua: '**Sikuwahi mimi kuweka ahadi na Ayub isipokua hua ni mwenye kuniambia kua : 'Hakuna Ahadi baina yetu' na kisha hua namkuta ameshanitangulia katika kukutana kwetu.**'

Anasema Yunus Ibn Ubayd kua: '**Hakuna mtu aliekua akiwausia sana watu kama Sakhtiyani na Hasan Al Basr.'**

Imam Ash Shath anasema kua: **'Ayub ni Mwanazuoni bora.'**
Salam Ibn Abi Muti alisema kua: **'Mwenye kujua zaidi kuhusiana na Dini miongoni mwa wenye kujua basi ni Ayub.'**

Ambapo Wahib akasema pia: '**Mimi nimemsikia Ayub akisema: 'Wacha Mungu wakitajwa basi mimi nitatengenishwa kutokana nao''**

Imam Hammad Ibn Zaid alisema pia kua: **'Ayub alikua ni rafiki wa Yazid Ibn Al Walid, hivyo Yazi alipopata Madaraka ya Ukhalifa basi Ayub aliomba Dua kwa kusema: 'Ya Allah! Mjaalie Yazid kua ni mwenye kunisahau mie.''**

Ambapo alisema Imam Ayub Sakhtiyani kua: **'Wacha mtu awe ni mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na kama ni Mwenye kuachana na Dunia basi asikufanye kuachana kwake huko na Dunia kua ni kwenye kuwakera wengine**.'

Tunapoangalia ukubwa wa Ilm yake Imam Ayub Al Sakhtiyani basi tunaona kua hadi wa mji wa Makkah walikua wakivutiwa kutokana na Ilm yake kwani anasema Ayub Ibn Sulaiman kua: **'Mimi nilimwambia Ubaid Allah Ibn Umar kua: 'Nnaona kua mnajitayarisha kutokana na kujawa na hamu ya kukutana watu wa Iraqi katika wakati huu wa Hija' ambapo nae akasema: 'Naam Wa Allahi, hakika mimi hua sifurahii Mwaka wangu isipokua katika kipindi cha wakati wa Hija'** ambapo Imam Al Sakhtiyani katika uhai wake basi aliendа katika Ibada ya Hija mara 40.

Imam Al Sakhtiyani alikua ni mwenye kutopenda kuonekana wakati akifanya Ibada zake kiasi ya kua hata Imam Ibrahim Ibn Adham anapoingia nyumbani kwa Imam Al Sakhtiyani kusalimiana nae basi Imam Al Sakhtiyani alikua akiufunika Msahafu wake ili asionekane kua alikua akisoma Qur'an. Na katika wakati wa Usiku alikua ni mwenye kukesha kwenye Msala, lakini inapofika wakati wa Alfajir hua ni mwenye kujifanya kama kwamba ndio kwanza ameamka.

Na alipokua akiulizwa suali kuhusiana na Dini basi alikua akisema kua: **'Waulize wenye kujua juu ya hilo',** kama vile yeye si miongoni mwa wenye kujua.

Ambapo Shu'bah anasema kua**: 'Mimi nilikua nikitoka na Ayub basi alikua haniruhusu kutoka pamoja nae, na hivyo alikua akiniwacha hapa na pale ili watu wasimuone'**

Tunapozungumzia Ucha Mungu wa Imam Ayub Sakhtiyani basi tunauzugumzia Ucha Mungu ambao ulikua ukiwaathiri hadi watu wengine wengi kwani ilikua kila akiingia Sokoni na kisha watu wakimuona basi walikua wakifurahia, wakimtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kufanya Takbir, kwani walikua wakiona Uso uliojaa nuru ya Ucha Mungu.

Hamamd Ibn Zayd anasema kua: **'Sikuwahi mimi kumuona Ayub akitoka sokoni isipokua hua ni mwenye kua ni mwenye kununua kitu kwa ajili ya familia yake, na nilimuona akiwa na chupa ya Manukato, hivyo nikamuulizia kuhusiana nayo nae akasema: 'Mimi nimemsikia Hasan Al Basr akisema kua Muumini hua ni mwenye kupata Ukarimu kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hivyo akipata hutumia kwa ajili ya kuwakirimu na wengine na akizuia basi hua amejizuilia.''**

Anasema pia Hammad Ibn Zayd kua: **'Hakika mimi sijawahi kumuona mtu ambae alikua akitabasam sana anapokua mbele za watu kama Al Sakhtiyani'**

Anasema Bishr Ibn Mansur kua: **'Sisi tulikua na Ayub nae akatuusia na kuzungumza nasi na kisha akasema: 'Basi inatosha, kwani kama ningekua nataka kukuambieni kila kitu ambacho nnataka kukuambieni leo hii basi ningekua nimeshafanya hivyo''**

Imam Ayyūb Al Sakhtiyānī aliulizwa**: ‘Hivi Jee Ilm ya leo ni kubwa zaidi au ni ndogo zaidi?’ ambapo ane akajibu: ‘Leo kuna maneno zaidi kuliko Ilm, lakini zamani kulikua na Ilm zaidi.’**

Imam Malik alisema kuhusiana na Ayub Al Sakhtiyani kua: **‘Ayub Sakhatiyani alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni ambao waliokua wakiifanyia kazi Ilm yake na kumuogopa Mola wake’**

Imam Hamad Ibn Zayd amesema kua: **‘Ayub Sakhtiyani alikua ni Mtu mcha Mungu sana miongoni mwa watu niliowahi kuwaona na ni mwenye kufuata kikamilifu Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na alikua juu sana kwenye Ilm ya Fiqh miongoni mwa Wanazuoni wetu’**

Imam Ayub Al Sakhtiyani alikua ni mwenye kusema kua: **‘Mtu aliejuu hua ni yule mwenye sifa mbili ambazo ni kua Hatarajii chochote kutoka kwa Yeyote na hua ni mwenye kua na Subra pale anapofikwa na mitihani inayotokana na watu.’**

Na akasema tena: **‘Tawwakul hua ni kuuelekeza mwili kwa ajili ya kuutumikia Moyo kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kua ni mwenye kuridhika na unachokipata’**

Imam Al Sakhtiyani alisema tena kua: **‘Hakika mimi namuonea sana huruma yule mja ambae ni mwenye kughafilika kutokana na fadhila za Mola wake, na kutotimiza jukumu lake mbele ya Mola wake na kunyimwa hali ya kufanya Ibada.’**

Imam Al Sakhtiyani aliusia Wanazuoni kwa kusema**: ‘Enyi Ndugu zangu, msijipandishe Darja kutokana na kuhifadhi maneno ya wale waliosema kuhusiana na Ilm ya Dini, kwani huo hua ni unafiq na kujionesha, kwa sababu maneno hayo sio yenu na nyinyi sio mnaoyatamka’**

Imam Al Sakhitiyani alisema kua **: ‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* huwashusha Darja wale wanaopenda kua juu na huwapandisha darja wale wenye kujishusha kwa kuonesha Unyenyekevu’**

Imam Ayub Al Sakhtiyani alifariki mnamo mwaka 131 Al Hijra katika ardhi ya Basra.

IMAM AL QARI ABU AMR IBN A'ALA A L BASR 70 AH

Imam Abu Amr Zibban Ibn Amar Ibn Abd Allah Ibn Huasyn, Ibn Harith Ibn Julhum Ibn Huzaa Ibn Al Mazin Ibn Malik Ibn Amr Ibn Al Tamim Al Basr alizaliwa katika Mji wa Makkah mnamo mwaka 70 Al Hijra.

Imam Abu Amr alikua akiitwa Al Mazini kwa sababu alikua ni mwenye kutoka kwenye Ukoo wa Al Mazini na Al Tamimi kwa sababu Tamim ni ndani yake uko wa Al Tamim ndio mlimotoka ukoo wa Al Mazin na pia akaitwa Al Basr kwa sababu baadae alihamia Nchini Iraq na kawa anaishi kwenye Mji wa Basra, baada ya kusoma kutoka kwa Masahaba na Tabiina wa Mji wa Makkah na Madina wakiwemo kina Imam Yahya Ibn Yamar, Imam Hasan Al Basr, Imam Said Ibn Jubayr, Imam Ikrimah, Imam Mujahid Ib Jabr, n.k.

Imam Abu Amr alikua ni mtu mwenye Ilm kubwa sana na ni mwenye utaalamu mkubwa wa Lugha ya Kiarabu kwani Ukoo wa Banu Tamim ndio ukoo wenye kujulikana sana kwa Ufasaha wa Lugha ya Kiarabu katika wakati wake na pia Imam Abu Amr alikua ni mwenye kuaminika kwani alikua ni mtu ambae ameachana kabisa na Dunia yake, na hivyo alikua ndie Muanzilishi wa Skuli ya mwanzo ya Kisomo cha Qur'an na llm ya Nahw mjini Basra.

Imam Abu Amr aliadnika vitabu vingi sana kuhusiana na Ilm ya Nahaw na kisha akavigawa Vitbu vyake vyote, kwa Wanafunzi wake wakiwemo kina Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Al Asmai, Imam Yahyha Ibn Yazid, Imam Abu Amr Hafs Ibn Umar, Imam Abu Suayb Salih Ibn Ziyad, Imam Sibawayh, n.k

Ambapo Qiraa cha Imam Abu Amr hadi hi leo kinasomwa katika maeneo ya Afrika hususan katika nchi ya Sudan, na alisema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Qiraa cha Abu Amr ni chenye kunivutia sana mimi, kwani Qiraa chake ni ni cha Qurasysh na wanafasihi wao.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Sufyan Ibn Uyaynah amesema kua: '**Mimi nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwenye Ndoto na hivyo nikmauuliza: 'Ya Rasul Allah, hivi nimfuate nani mimi kwenye Qiraa?' ambapo nae akaniambia kwa kusema: 'Mimi nakupendekezea wewe usome Qiraa cha Abu Amr Ibn Ala''**

Ambapo Imam Adh Dhahabi anasema kua: **'Hadith zake Imam Abu Amr ni kidogo, lakini ni sahih na yeye ni Uthibitisho kwenye Qir'aa.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo amesema Imam Yahya Ibn Muadh kua: **'Imam Abu Amr ni Thiqah katika Ilm ya Hadith.'**

Ambapo anasema Imam Abu Al Warith kua: **'Sisi tulikua tunaenda Kwenye Ibada ya Hija pamoja na Abu Amr, na tukapiga kambi katika sehemu ambayo haina Maji, na tulikua tumebanwa na kiu sana, na hivvyo Abu Amr akaondoka na kutuacha sisi kambini, hivyo baada ya mda nami nikatoka na kumtafuta, ambapo baada ya mda nikamuona Abu Amr akiwa anatia udhu kwenye sehemu ambayo ina chemchem, katikati ya Jangwa, na liponiona basi akasema: 'Ewe Abu Warith usimwambie mtu yeyot kuhusiana na hili lililotokea hapa.' Hivyo nami sikumwambia mtu yeyote hadi alipofariki'**

Imam Al Asmai anasema kua: **'Mimi nilimuliza Abu Amr masuali 1000 ambapo nae akanijibu kwa kunipa hoja na vithibisho 1000'** Imam Al Asmai anaendelea kutuambia kua: **'Abu Amr alikua ni mwenye kuchuma asilimia moja ya Dinar katika kila siku moja ya uhai wake, ambayo alikua akiitumia kwa ajili kununua Maji na Nanaa, na kisha hutumia maji hayo kwa ajili ya kunywa na kutoa sadaqa wakati wa jioni wa wenye haja, na alikua akinukia kama nanaa'**

Alisema Imam Abu Amr kua: '**Kuna haliya uzuri ulioje kwa mtu mwenye kukaa kimya mbele ya mtu mwenye kua na Ilm, na kisha akauliza masuali, na kisha akaelezewa, na kisha akasambaza yale aliyolezewa.'**

Aliulizwa Imam Abu Amr: **'Hivi Jee si aibu kwa Mtu mzima kua nim wenye kutafuta Ilm kutoka kwa kijana mdogo?' ambapo nae akajibu: 'Kama Ujinga wa Mtuzima hua ni aibu kwanini kutafuta Ilm kwake iwe aibu?'**

Alisema tena Imam Abu Amr: '**Wakati tunapoona Maiti, basi hua ni wenye kua na khofu, lakini baada yakuizika basi hua tunarudi kwenye michezo na mambo ya starehe tena, imekua kama vile ambavyo Mbwa mwitu anapolitia khofu Kundi la Kondoo anapolivamia, na hivyo baada ya kuchukua Kondoo atakae basi Kondoo waliobakia huendelea kula kama kwamba hakuna kilichotokea.'**

Na akasema tena kua: **'Kama Dunia ikwa inaonekana kubwa mbele ya macho ya Mtu basi Nafsi ya mtu huyo hua ni yenye kuzungukwa na Kiburi'**

Imam Abu Amr Ibn Al Aala alifariki mnamo mwaka 154 Al Hijra mjini Kufa wakati alipokua safarini akitokea Basra kueleeka Dimashq.

IMAM ABU ABD RAHMAN IBN LAILA 76 AH

Imam Abu Abd Rahman Muhammad Ibn Abd Rahman Ibn Abi Laila Ibn Abi Laila Yasar Ibn Bilal Ibn Bulayl Ibn Ahiha Ibn Al-Jalah Ibn Al-Harith Ibn Jahba Ibn Kalfa Ibn Awf Ibn Amr Al Awsi Al Ansari alizaliwa katika Mji wa Kufah nchini Iraq mnamo mwaka 76 A l Hijra.

Baba yake Imam Abu Abd Rahman Ibn Abi Layla ambae ni Imam Abu Isa Ibn Abi Laila alifariki wakati Imam Abd Rahamn Ibn Abi Layla akiwa mdogo mwenye umri wa miaka minane. Hivyo Imam Abu Abd Rahman Ibn Abi Layla pamoja na kaka yake aitwae Isa Ibn Abi Laila wakawa ni wenye kuishi pamoja kwa kutegemeana, huku wakiwa ni wenye kutafuta Ilm ya Dini ya Kiislam katika ardhi hio ya Mji wa Kufah.

Ambapo Imam Abd Rahman Ibn Isa akasoma kwa kaka yake huyo Isa Ibn Abu Isa Abd Rahman Abi Layla na akasoma pia kwa Imam Ataa Ibn Abi Rabah, Imam Na'fi Mawla Ibn Umar, Imam Amr Ibn Murra, Imam Minhal Ibn Abd Allah Ibn Masud, Imam Hakam Ibn Utba, Imam Abu Zubayr Al Makki, Imam Amr Ash Shabi na wengineo.

Ambapo nae akawasomesha Wanazuoni wengineo kama Sufyan Ath Thawyr, Imam Qais Ibn Rabii, Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Amr Ibn Qais, Imam Ukbah Ibn Khalid, Imam Mukhtar Ibn Abd Allah Ibn Isa Ibn Abi Laila, Imam Jurayj Ibn Imran Ibn Abd Rahman Ibn Abi Laila, na wengineo.

Ingawa Imam Abu Abd Rahman alisoma sana kwa Wanazuoni wengi sana wakubwa wakubwa wa fani tofauti lakini kwa upande wake yeye alikua si mtu mwenye Ilm kubwa ya Hadith na badala yake alikua ni mtu mwenye Ilm kubwa sana ya Qur'an na Fiqh kiasi ya kua alifikia Darja ya kua Qadhi Mkuu wa Mji wa Kufa kwa mda wa miaka 33 ndani ya mamlaka ya Gavana aitwae Isa Ibn Musa.

Ambapo Imam Abu Abd Rahman Muhamamd Ibn Abd Rahman Ibn Abi Layla anasema kua alimwambia Gavana Isa Ibn Musa kua: **'Takriban Wanazuoni wote walikua hawana asili ya Uarabu' hivyo Isa Ibn Musa (Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Abd Allah Ibn Al Abbas *Radhi Allahu Anhu)* akaniuliza: 'Hivi Jee ni Nani Mufti wa Basra?' Nami nikasema: 'Al Hasan Ibn Hasan Al Basr na Muhamamd Ibn Sirrin' nae akauliza: 'Jee ni nani watu wawili hawa?' nami nikasema: 'Wote hawa walikua ni Watumwa walioachiwa huru' nae akasema: 'Na ni nani Qadhi wa Makkah?' nami nikasema: 'Ataa Ibn Rabah, Mujahid na Said Ibn Jubayr' nae akauliza: 'Na ni nani watu hao?' nami nikasema: 'Watumwa walioachiwa Huru.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Nae akauliza: 'Jee ni Nani Qadhi wa Mji wa Madina?' nami nikasema: 'Ni Zayd Ibn Aslam, Muhammad Ibn Al Munkadir na Nafi'i Ibn Abi Junayh' nae akauliza: 'Ni nani hao?' nami nikasema: 'Ni Watumwa walioachiwa huru' hivyo hapa muonekano wa Uso wake ukabadilika, na kisha akasema: 'Jee ni nani Qadhi wa Quba?' nami nikasema: 'Ni Rabia Ar Rai na Ibn Abi Zinad' nae akauliza: 'Ni Nani hao?' nami nikasema: 'Ni miongoni mwa Watumwa walioachiwa huru.'

Hapa muonekano wa uso wa Isa Ibn Musa ukawa ni wenye kuingia kiza, na kisha akasema: 'Jee ni nani Qadhi wa Yaman?' nami nikasema: 'Tawus, Watoto wake na Wahb Ibn Munabih' Isa Ibn Musa akasimamakutoka kwenye kiti chake huku akiwa ametokwa na mishipa ya uso na kuuliza: 'Na ni Nani Qadhi wa Khurasan?' nami nikasema: 'Ataa Ibn Abd Allah Al Khurasan' nae akaniuliza : 'Na ni nani huyo?' nami nikajibu: 'Ni Mtumwa alieachiwa Huru'

Uso wa Isa Ibn Musa ukawa mwekundu lakini akaamua kua mtulivu na hivyo akauliza: 'Jee ni nani Qadhi wa Syria?' Nami nikasema: 'Ni Makhul' nae akauliza: 'Jee Ndio nani huyo?' nami nikasema: 'Ni Mtumwa alieachiwa huru' hivyo akauliza: 'Ni Nani Qadhi wa Kufah?' nami nikataka kujibu kua ni Al Hakim Ibn Utbah na Amar Ibn Abi Salman, lakini nikawa na khofu juu ya kitakaochotokea nikisema hivyo, hivyo nikajibu: 'Ibrahim An Nakhai na Ash Shabi' nae akasema: 'Ndio nani hao?' nami nikasema: 'Ni Waarabu' nae akasema: 'Allahu Akbar' kisha akakaa kitako chini.

Hivyo ingawa alikua Qadhi wa Mji wa Kufa kutokana na kua na Ilm kubwa sana ya Fiqh inayotegema Ijtihad ndani ya Qur'an, Hadith Sahih na Rai kama anavyosema Imam Sufyan Ath Thawry kua: **'Wanafiqh wetu sisi ni Abi Laila na Ibn Shabrama'** ambapo kwa upande wa Qadhi Abu Yusu basi yeye anasema kua: **'Hakuna mwenye Mamlaka ya Kutoa Hukumu anaeijua zaid Dini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama Ibn Abi Laila.'**

Lakini alikua na udhaifu wa Ilm ya Hadith kama wanavyosema Wanazuoni, kwani Imam Zaida Ibn Qudamah na Yahya Ibn Al Qattani waalikua hawataki kabisa hata kuzinukuu Hadith zake, na alisema Imam Shuba Ibn Al Hajjaj kua: '**Sijawahi mimi kuona mtu mwenye hifadhi mbovu kama Ibn Abi Laila**'

Na akasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Abu Abd Rahman Ibn Abi Laila alikua ni mbaya katika kuhifadhi, lakini Fiqh yake ni yenye kupendwa zaidi kwetu kuliko Hadith zake**' na akasema Imam Abu Zaraa Al Razi kua : '**Abu Abd Rahman Ibn Abi Laila alikua ni mcha Mungu lakini Hadith zake hazikua zikiaminika sana**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na ingawa hadith zake hazikua zikaaminika sana na Wanazuoni lakini kwa upande wa Imam Ibn Majah, Imam Abu Daud na Imam Al Tirmidhi basi wamezinukuu hadith zake katika vitabu vyao kwani anasema Al Ajli kua: '**Abu Abd Rahman Ibn Abi Liaila ni Mwanazuoni mwenye kudumu na Sunah, Mkweli Muaminifu na Hadithi zake zinakubalika, na alikua ni Msomaji wa Qur'a mwenye kujiua hasa.'**

Hivyo kwa upande wa Qur'an basi Imam Abu Abd Rahman Ibn Abu Laila alikua ni mwenye Ilm kubwa sana nayo na alikua ni bingwa miongoni mwa wenye kuijua na wenye kuihifadhi Moyoni mwao, na alikua na Qiraa kizuri sana kwani akimsomesha pia kaka yake ambae ni Isa Ibn Abu Isa Ibn Abi Laila, Imam Amr Ash Shabi, Imam Hamza Al Zayyati, Imam Al Minhal na wengineo.

Na anasema Imam Hafs Ibn Ghiyadh kua: '**Kutokana na Ufalme wa Qiraa chake Ibn Abi Laila basi aliwasomesha Quran Mashaykh 10 wa Qiraa**.'

Ambapo miongoni mwao ni Imam Hamza Al Zayyat ambae yeye anasema kua: '**Tumejifunza sisi uzuri wa kusoma Qur'an kuilingana na Ibn Abi Laila ambae yeye alikua ni Mtu Makini zaidi kuhusiana na Qiraa cha Qur'an na alikua akiiandika kwa mkono wake, alikua ni Mtu mzuri sana na mwenye Darja.'**

Kwani Imam Abu Abd Rahman Ibn Abi Laila alikua ni mwenye mfumo unaokaribiana kifiqh na Imam Abu Hanifa na hivyo wakawa ni wenye kuvutana kwa ukubwa wa Ilm ya Fiqh na Imam Abu Hanifa kiasi ya kua Wanazuoni walikua wakiwafuatilia na kuandika vitabu kuhusiana na ufafanuzi wa Fatwa zao na tofauti baina yao, ambapo miongoni mwao Imam Abu Yusuf ambae ni Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa lipoandika kitabu kiitwacho *Ikhtilaf Ibn Hanifa Wa Ibn Abi Laila* Tofauti baina ya Abu Hanifa na Ibn Abi Laila ambacho ndani yake mna sehemu 35 zinazozungumzia kuhusiana na mambo tofauti waliyotofautiana, na hata Imam Al Shafii nae aliielezea mitizamo ya Fatwa zao katika kitabu chake cha Al Umm huku akianisha Mitizamo yake pia juu ya jambo husika.

Ambapo safari moja katika wakati wake Imam Ibn Abi Laila aliwasilishiwa Mashtaka kutoka wa Wanawake wawili ambao walikua wamevaa Niqab, ambapo Imam Ibn Abi Laila akataka waoneshe Sura zao kabla ya kuwasilisha mashtaka yao mbele yake, ili awaona wakati wakiwa wanasungumza nae, hivyo Wanawake hao wakafungua Nyuso zao,kisha Imam Ibn Abi Laila akauliza: '**Jee ni nani kati yenu atakaeanza kuzungumza?**'

Hivyo Mwanamke mmoja akamwambia mwenzake '**Anza wewe.'** na hivyo Mwanamke huyo aliepewa ruhusa akaanza kwa kusema: '**Ewe Qadhi, Hakika Baba yangu mimi amefariki na huyu ni Shangazi yangu, ambapo Mume wangu amemuoa Binti yake, baada ya Shangazi yangu kuona namna Mume wangu anavyonijali na**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kunishughulikia, na baada ya kumuoa basi Shangazi yangu na Mume wangu wakanifuta na kuniambia kua: 'Mume wako amemuoa Binti yangu hivyo sasa wewe pia uko chini ya himaya yetu na hivyo umeachika.''

'Ambapo baada ya kupita mda si zamani sana Mume wa Shangazi yangu akarudi kutoka safarini ambako alikua amekaa kwa mda mrefu sana na aliponiona akataka kunioa, hivyo nami nikakubaliana nae kwa sharti la kua anikabidhi mamlaka ya Shangazi yangu juu yangu, ambapo nae akakubali, hivyo baada ya kuoana basi nikamfuata Shangazi yangu na kumwambia: 'Ulikua umeolewa na fulani Ibn fulani na sasa umeshaachika.''

Baada ya kusikia kisa hiki basi Imam Abu Abd Rahman Ibn Ali Laila akanyanyuka kutokana na mshtuko wa kisa hiki kinachochanganya na kutoingia akilini, Ambapo Mwanamke huyo akaendelea kusema: '**Baada ya mda Mume wa Shangazi yangu ambae ndie wangu akafariki, hivyo mimi nikakaa Eda na baada ya kumalizika Eda ikawa kuna mvutano wa Mirathi baina yangu na Shangazi yangu.'**

Na baada ya Eda kumalizika Mume wangu wa zamani akaniona na kuvutiwa nami tena, na akakumbuka mapenzi yetu ya zamani hivyo akataka kurudia kunioa, nami nikamwambia kua: '**Nitakubaliana nawe kama ukinipa mamlaka juu ya Binti wa Shangazi yangu, ambapo nae akakubaliana nami, na kisha tukaoana, nami nikamwambia Binti ya Shangazi yangu kua: 'Hakika wewe uliolewa na Fulani Ibn Fulani na sasa hivi umeshaachika.''**

Hivyo Imam Ibn Abi Laila akakamata kichwa na kuuliza: '**Hivyo jee Suali liko wapi?**' yule Shangazi akauliza kwa kusema: **'Suali ni kua hivi jee kweli inaruhusika kwangu mimi na Binti yangu kua ni tulioachika? na jee hatuwezi kua ni wenye kupata mirathi?'** ambapo Imam Ibn Abi Layla akasema: '**Wa Allahi mimi sioni Kisichokubalika, na kuna haramu gani kwa huyu Bwana alieoa mara mbili na kisha akaacha mara mbili na kuutoa uwezo wa Mamlaka yake juu yake na kumpa mke wake mara mbili?**'

Baada ya hapo Imam Abu Abd Rahman akaelekea kwa Al Mansur na kumuelezea kisa hicho, ambapo nae akacheka sana baada ya kukisikia hadi akaishiwa na nguvu na kuanguka chini, na kisha akasema: '**Amemkatili Allah huyu Mama mzee aliejichimbia shimo na kisha akatumbukia ndani yake mwenyewe.'**

Imam Abu Abd Rahman Ibn Abi Laila alifariki mnamo mwaka 148 Al Hijra, miaka miwili kabla ya kufariki Imam Abu Hanifa na miaka miwili kabla ya kuzaliwa Imam Al Shafii.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM MANSUR AL MU'TAMIR

Imam Abu Atab Mansur Ibn Al Mutamir Ibn Abd Allah Ibn Rabia Al Bahta Ibn Sulaym alizaliwa katika mji wa Kufah nchini Iraq katika miaka 60 ya mwanzoni ya Uislam na pia alijipatia Ilm yake ya Dini ya Kiislam katika mji huo wa Kufah na miji myengineyo na alisoma kwa Imam Mansur An Nakhai, Mujahid Ibn Sulyaman, Imam Jafar As Sadiq, Imam Al Baqir.

Imam Mansur Al Mutamir alikua ni Mtu mwenye Ilm kubwa sana na Mcha Mungu sana, na Hadith zake zimenukuliwa kwenye Vitabu 6 vya Hadith huku zikiwa na sifa ya kua ni Hadith Sahih, na pia mwenye Ufahamu mkubwa sana kiasi ya kua anasema Imam Shu'bah kua: 'Aliniambia mimi Mansur kua: '**Haikuwahi kutokea hata mara moja kwangu mimi kua ni mwenye kuandika Hadith nnazosomeshwa''**

Anasema Imam Ibn Saad akamalizia kwa kusema kua: **'Imam Al Mutamir ni mtu mwenye kuaminika na mwenye kua na sifa nzuri na Hadith zake ni Sahih'** Na kisha akasema Imam Ibn Sad kua: **'Imam Mansur Al Mutamir alipoteza Macho yake kutokana na kulia kwake sana kunakotokana na Taqwa na alikua kila wakati anatembea na kitambaa chake cha kufutia Machozi.'**
Kwani Mama yake alimlalamikia kwa kumwabia: **'Ewe Mtoto wangu, Macho yako yana haki juu yako na mwili wako pia na haki juu yako.'** Ambae nae alikua akimjibu Mama yake kwa kusema kua: **'Ewe Mama yangu mwachie Mansur kama alivyo kwani kuna kulala kwa mda mrefu sana baina ya pumzi mbili.'**

Anasema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: **'Mansur Al Mutamir alikua ni mwenye kufunga kwa miaka 40 mfululizo na alikua ni mwenye kusimama kwenye Qiyam Al Layl na kulia kila siku usiku.'**

Ambapo katika kipindi cha utawala wa Gavana Yazid Ibn Umar Ibn Hubaira alipokua Gavana wa Kufah basi Imam Mansur Ibn Mutamir alichaguliwa kua Qadhi Mkuu wa mji huo lakini hata hivyo nae alikataa wadhifa huo. Imam Mansur Ibn Mutamir alisomesha Wanazuoni wengi sana akiwemo Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Abd Rahman Ibn Mahdi, Imam Al Amash, Imam Al Taymih, Imam Shu'bah na wengineo.

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi anasema kua: **'Hakuna mtu yeyote yule katika Mji wa Kufa mwenye kuhifadhi Hadith kama Mansur Al Mutamir'**

Imam Mansur Al Mutamir alikua ni mwenye hisia kali sana kiasi ya kua hata alipokua akisomesha Wanafunzi wake basi alikua akitokwa na Machozi na muonekano wa

Macho yake ulikua ni wa mtu mwenye huzuni na kuvimba macho kwa kutokwa kwake na machozi sana. Kwani anasema Imam Yahya Al Qattan kua: **'Amesema Sufyan Ath Thawry kua: 'Kama ukimuona Mansur Ibn Mutamir basi unaweza kua ni mwenye kusema Wakati wa Kiama umewadia.'**

Ambapo anasema Imam Al Dhahabi kua: **'Aliniambia mimi Al Abbas Ibn Muhammad kua amaeambiwa na Abu Bakr Ibn Al Aswad kua alimsikia Imam Abd Rahman Ibn Mahdi akisema kua: 'Hakuna Thiqah katika mji wa Kufah isipokua watu wanne ambao ni Mansur, Abi Hasiin, Salamah Ibn Kahil na Amr Ibn Murra, lakini Mansur amewazidi wote.''**

Miongoni mwa sifa kuu za Imam Mansur Al Mutamir iliakua ni kua anaposomesha Hadith basi hua ni mwenye kusomesha Hadith kidogo kwa muda mrefu kwa sababu alikua akizama katika kufafanua Hadithi anazozisomesha ili Wanafunzi wake wafaham zaid, kiasi ya kua Imam Sufyan Ath Thawry anatuambia kwa kusema kua: '**Mimi nilikua nikienda kwa Mansur Mutamir makusudi ili asiniongezee Hadith zaidi ya zile alizozisomesha'** na kisha akasema tena kua: **'Mimi nilikua naenda kwa Al Amash na Mansur, na nilikua nasikiliza Hadith 4-5, halafu hua ni mwenye kuondoka na kuomba kua bora ningepata Hadith zaidi'**

Anasema Imam Ali Ibn Madani kua: **'Mimi nilimsikia Yayha Ibn Qatani akisema kua: 'Kama mtu ukipata kunukuu hadith kutoka kwa Mansur basi mikono yako hua ni yenye kuhisi ukarimu mkubwa bila ya kuwahitajia wengine, na mimi sijawahi kumuona mtu mwenye kuaminika katika kunukuu Hadithi za Ibrahim An Nakhai na Mujahid kama Mansuri Al Mutamir''**

Imam Ahmad Ibn Sinan Al Qatani anasema kua: **'Mimi nimemsikia Abd Rahman Ibn Mahdi kua: 'Watu wanne kutoka katika Mji wa Kufah hawafai kupingwa kwa nukuu za hadithi zao kwani yeyote yule atakaepingana nao basi atakua amefanya makosa makubwa, ambapo mmoja miongoni mwao watu hao ni Mansur Ibn Mutamir''**

Kutokana na Ucha Mungu wake na Khushuu yake Imam Mansur Al Mutammar basi alikua akisali husimama kama tulii kama nguzo au kisiki kilichoota mizizi cha Mti, kiasi ya kua kuna mtoto wa Jirani yake ambaea alikua kila sikua anakaa Dirishani baada ya Sala ya Isha na kuangalia mandhari ya Usiku kupitia Dirishani kwao, na kila siku usiku alikua akiona kuna kisiki kimesimama juu ya Varanda ya Nyumba ya Imam Mansur Al Mutamir, kisiki ambacho hata hivyo hua hakioni katika wakati wa mchana. Hivyo kisiki hiki kilikua kikimshangaza sana.

Siku moja mtoto huyo alikua amekaa dirishani na alipoangalia upande wa Nyumba ya Imam Al Mutamir hakua ni mwenye kuweza kukina kisiko hicho, hivyo akajiuliza

imekuaje leo kisiki hicho hakipo? Kwa hivyo akaamua kumkimbilia mama yake kumuuliza kuhusiana na kisiki hicho kama aliwahi kukiona ama la, na kama aliwahi kwanini kinakuweo usiku tu, na leo hakipo?

Mama wa mtoo huyo akshangazwa na suali hilo, kwa shabu haiwezekani kua kisiki kikae juu ya nyumba,lakini baada ya kutafakkari basi akagundua kua mtoto wake huyo anazugumzia kuhusiana na Imam Mansur Al Mutamir ambae alikua na kawaida ya kusali usiku kuchan juu ya nyumba yake, hivyo akamwambia mtoto wake huyo kua: **‘Ewe mtoto wangu, kile hakikau ni kisiki bali alikua ni Imam Mansur Al Mutamir ambae ndie yule aliefariki na kuzikwa leo’**

Ambapo anasema Imam **‘Abd Allah Ibn Imam Ahmad Ibn Hanbal kua : ‘Mara nyingi mimi nilikua nikimsikia Baba yangu akiisoma Dua ifuatayo katika Sijda**

اللَّهُمَّ كَمَا صُنْتَ وَجْهِي عَنِ السُّجُودِ لِغَيْرِكَ فَصُنْ وَجْهِي عَنِ الْمَسْأَلَةِ لِغَيْرِكَ

Allahumma kama sunta wajhi ‘anis sujudi li ghayrika fasun wajhi ‘anil mas-alati li ghayrika.

Tafsir: ***Ya Allah kama vile ambavyo umenihifadhi mimi kutokana na kutomsujudia yeyote yule isipokua wewe basi nakuomba unihifadhi kutokana na kutomuomba yeyote yule isipokua wewe.***

Hivyo nami nikamuuliza Baba yangu: ‘Mbona mimi nimekusikia wewe ukiwa ni mwenye kuomba Dua hii kwenye Sijda? Hivi jee unao uthibitisho wowote kutoka kwenye nukuu?’

Ambapo nae akaniambia: **‘Naam, hakika mimi nimekua nikimsikia Waki Ibn Jarrah akiyarudia maneno haya kwenye Sijda, hivyo nami nikamuuliza kama wewe ulivyoniuliza mimi, ambapo nae akathibitisha kua amemsikia Sufyan Ath Thawry, ambae nae alisema kua nae amemsikia Mansur Ibn Al Mutamir akiwa ni mwenye kupenda kuisoma Dua hii.’**

IMAM HAYWA IBN SHURAIH

Imam Abu Zaraa Haywa Ibn Shuraykh Ibn Safwan Malika Al Tajibi Al Kindi Al Masri, alikua ni Mwanazuoni wa Fiqh na Hadith wa Misri na alikua ni Mcha Mungu na mwenye Taqwa, na hivyo alikua akijulikana kwa Jina la Shaykh Ad Diyar Al Misri.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na alisoma kwa Imam Rabi'a Ibn Yazid, Imam Uqba Ibn Muslim, Imam Yazid Ibn Abi Hubayb, Imam Abu Yunus Salim Ibn Jubayr, nk.

Alisema Imam Abu Zaraa kuwaambia Watawala wa Misri kua: **‘Hamtakiwi muiwache Nchi bila ya Kua na Silaha, kwani sisi tunaishi pamoka na watu wa Qubt na hivyo hatujui lini watavunja makubaliano yao, tuko karibu na Warumi na hatujui lini watatuvamia, na tumepakana na Mabedui wa Jangwani hatujui lini watasababisha Uasi, na tumepakana na watu wa Abyssinia na hutujui lini watatudanganya.’**

Miongoni mwa Wanafunzi aliowasomesha Imam Haywa Ibn Shuraikh ni pamoja na Imam Ibn Mubaraka, Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Abd Allah Ibn Wahb, Hani Al Mutawakil na wengineo.

Ambapo alisema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: **‘Abu Zaraa ni mwenye Ilm kubwa sana ya Fiqh na Hadith, na ni Thiqah’**

Ambapo kwa upande wa Imam Yahya Ibn Main basi yeye amesema kua: **‘Imam Al Zaraa ni Thiqah’**

Na akasema Imam Ibn Abi Htaim kua: **‘Wakati Baba yangu alipoulizwa kuhusiana na Haywa, Yahya Ibn Ayub na Said Ibn Abi Ayub kuhusiana na Hadith za Haywa wa Misri basi alisema kua: Haywa aliku ni Mwanazuoni bora wa Misri, na ndie Mwanazuoni mwenye kuaminika zaidi, na kua ni mwenye kujipenda zaidi kuliko Mufaddal Ibn Fidal.’**

Mbali ya kua ni mwenye kuaminika na ucha Mungu, lakinipia Imam Abu Zaraa alikua pia ni mwenye kua na ukarimu mkubwa sana na unyenyekevu mkubwa sana kwani alikua ni mwenye kutoa kila alichokua kikipata kwa kuwapa Masikini kua kama sadaka na Zakkah.

Ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Wahb kua; **‘Mimi sijawahi kumuona Mtu yeyote yule aliekua akiyaficha mema yake kama Haywa, na kila mtu alikua ni mwenye kujua Dua zake ni zenye Kujibiwa, sisi tulikua tukienda kwake kwa ajili yakujifunza kutoka kwake Ilm, alikua kila siku ni mwenye kuwepo Msikitini na ni mwenye kusali Nyuma ya Nguzo.’**

Ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: ‘Hakika mimi nilikua nikimuona kila mtu anae elezewa kwangu kua ni mwenye kua chini ya Sifa anazoelezewa juu yake, isipokua Haywa Ibn Shuraykh, kwani yeye alikua yuko juu zaidi ya namna anavyoelezewa kwa kila sifa.’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ibn Wahda anasema kua: 'Siku moja kuna Mtu alikua anatufu kwenye Al Kaabah, mtu huyo alikua ana Madeni mengi sana kwani alikua akiomba kwa kusema kua: 'Ewe Mola wangu hakika mimi nina madeni mengi sana hivyo niwezeshe kua ni mwenye kuweza kuyalipa Madeni hayo' ambapo mtu huyo alipolala katika siku hio basi akaoteshwa na kuambiwa kua:

'Kama unataka kua na uwezo wa kulipa Madeni yako basi nenda kwa Haywa Ibn Shuraikh mwambie akuombee utafanikiwa' hivyo Mtu huyo akafunga safari hadi katika ardhi ya Alexandria nchini Misri na akawasilia katika ardhi hio katika siku ya Ijumaa mchana, na akaenda moja kwa moja hadi kwa Haywa Ibn Shuraykh, na alipofika tu na kukaa basi akaona sehemu hio imejaa Dhahabu, hivyo akaanza kutaka kucukua lakini Haywa Ibn Shuraykh akamwambia: 'Muogope Mola wako chukua kiasi kile tu ambacho unachodaiwa' ambapo Hayw Ibn Shuraykh akachukua Dhahabu yenye thamani ya Dina 300.'

Imam Ibn Hibban anasema kua: **'Haywa Ibn Shuraykh ni Mtu ambae Dua zake zinakubaliwa haraka sana na hapo hapo, kwani anapoomba Dua basi hata Changarawe mkononi mwake huweza kugeuka kua dhahabu.'**

Anasema Ahmad Ibn Sahl kua: **'Haywa alikua ni mtu mwenye kulia sana, na wala hakua ni mwenye kulalamika kuhusiana na Umasikini wala matatizo yeyote, siku moja wakati alipokua anaomba Dua, basi mimi nilikuja na kukaa pembeni yake na kumwambia kua: 'Natamani kua bora ungemuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akakuzidishia kutoka katika Rizki yako na kukutoa katika matatizo yako.'**

Hivyo Haywa akaangalia kulia na kushoto na alipoona hakua mtu basi akainama na kuokota kijiwe kisha akanirembea nacho, na nilipokidaka nikaona kua kimegeuka kua ni kipande cha Dhahabu, ambacho mimi kamwe sijawahi kuona uzuri wake Dhahabu kama hio.'

Kisha Haywa akasema: 'Hakuna Faida wala Maana kwa Mambo ya Kidunia ambayo hayatokunufaisha na Akhera yako, kwa Hakika *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kujua ni lipi lililobora kwa Mja wake' hivyonami nikamuonesha kile kipande cha Dhhabu na kumuuliza: 'Hivyo Jee ikifanye nini hiki?' ambapoane akasema: 'Tumia kwa mahitajio yako' hivyo nami nikaogopa kuuliza masuali zaidi.'

Amesema Imam Abd Allah Ibn Wahb kua: **'Wakati Haywa Ibn Shuraih alipopokea mshara wake wa Dinar 60 alikua akizigawa zote kama sadaqa na kisha akienda nyumbani kwake hua ni mwenye kuzikuta Dinari zake hizo zikiwa chini ya Godoro lake. Ambapo Haywa alikua na Ibn Ami wake ambae alipojua kuhusiana na tukio hilo basi nae akafanya kama alivyofanya Haywa yaani alipopata mshahara wake**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

basi nae akazitoa sadaqa zote na kisha alipoenda nyumbani kwake na kuangalia chini ya Godoro lake akakuta hakuna kitu.

Hivyo Ibn Ami huyo akamlalamikia Haywa kuhusiana na tukio lake hilo kua na yeye alifanya kama alivyofanya Haywa lakini hakukuta Dinar zake chini ya Godoro lake, ambapo Haywa akasema: 'Tatizo ni kua mimi nilitoa kwa Ikhlasi kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini wewe ulitoa kwa ajili ya kumjaribu *Allah Subhanah wa Ta'ala.* ''

Amesema Imam Haywa Ibn Shuraikh kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Watu 70,000 kutoka kwenye Ummah wangu wataingia Peponi bila kuhesabiwa na miongoni mwao watakua na muonekano wa Mwezi.'''**

Amesema Imam Haywa Ibn Shuraikh kua: **'Siku moja Abd Rahman Ibn Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alienda kwa Aisha *Radhi Allahu Anha* na kutia Udhu, hivyo akasema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: 'Ewe Abd Rahman tia Udhu ipasavyo kwa mimi nimemesikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua: 'Ole wake kila kisigino cha Jahannam (cha Mtu anaetia udhu kisha asikitie maji kisigino chake)''**
Imam Abu Jafar alifariki mnamo mwaka 158 Al Hijra.

IMAM ABU BASR AL BASR

Imam Abd Al Wahid Ibn Zayd Abu Basr Al Basr alizaliwa katika kipindi cha ndani ya miaka 100 ya Mwanzoni mwa Uislam katika ardhi ya Basra nchini Iraq.

Imam Abu Basr Al Basr alisoma kwa Wanazuoni kadhaa Imam Hasan Al Basr, Imam Abu Is-haq, Imam Al Amash, Imam Amr Ibn Maymun, Imam Asim Al Ahwal na wengineo, na hivyo alikua ni Mwanazuoni mkubwa sana wa Qur'an, Hadith na Fiqh ambae ni mwenye kudumu katika Qiyam Al layl na hivyo alikua ni mwenye kawaida ya kua ni mwenye kusali Sala ya Alfajir kwa Udhu wa Salat Al Isha.

Ambapo anasema Imam Yahya Ibn Said kua: **'Imam Abu Basra Al Basr ni Thiqah na ni mwenye kuaminika sana katika Ilm ya Hadith.**'

Imam Abu Basr Ibn Al Basr aliku ai mwenye kuwasomesha Wanazuoni wengi pia wa hadith kwani Hadith zake pia zimo kwenye vitabu Vikuu Sita vya Hadith, kwani ailikua ni kawaida yake kila siku ya Ijumaa baada *Salat Al Jumaa* basi nyumbani kwake hua ni kwenye kujaa Wanafunzi wenye kutafuta Ilm, na alikua ni mwenye kusomesha bila ya

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kuchoka wala kuona uvivu, na hua ni mwenye kupumzika katika wakati wa Sala ya Al Asr tu na kisha huendelea tena hadi Magharibi.

Na alikua hasomeshi Hadith tu, bali alikua anasomesha Qur'an na Fiqh pia ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Abd Rahman Ibn Mahdi, Imam Kays Ibn Hawas, Imam Yahya Ibn Yahya Al Nishapuri n.k.

Imam Abu Basr Al Basr alikua ni mtu alieachana na Dunia yake kwani yeye alikua ni mwenye kuijali Akhera yake tu, na alikua ni mwenye Hikma na ukarimu mkubwa sana na ni mwenye kupendwa sana na watu wake kwani alikua ni mfano wa kuigwa katika jamii yake.

Ambapo anasema Imam Abu Basr Al Basra kua: **'Safari moja mimi nilienda katika Ibada ya Hija, nikakutana na kijana ambae alikua anamsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa mfululizo bila ya kusita, jambo ambalo lilinivutia na hivyo nikamuuliza: 'Kwanini unapenda sana kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* bila ya kufanya Dhikr nyenginezo?' ambapo nae akasema: 'Safari moja Mimi nilikua ni mwenye kuenda katika Ibada ya Hija pamoja na Baba yangu. Tulipofika njiani tukapiga kambi na kisha tukalala.'**
'Na mara nikajiona kua imefika asubuhi huku nikiamshwa kwa kuambiwa kua niamke kwani Baba yangu ameshafariki na nilipoamka basi nikamuona Baba yangu akiwa amefariki, huku so wake ukiwa mweusii.'

'Tukio hili lilinihuzunisha sana kwani mbali ya kua Baba yangu amefariki lakini pia amefariki huku akiwa na uso ambao ni mweusi. Lakini mara usingizi ukanijia tena na nikalala, na nikaona tena kua kuna watu wengine Wanne wenye Nyuso Nyeusi pia ambao wamekuja na Mijeledi wanataka kumpiga Baba yangu.'

'Na walipokua wanataka kumpiga basi mara akatokea Mtu ambae alikua na uso wenye kung'ara sana ambae aliwaambia watu hao wenye Mijeledi kua wasimpige Baba yangu, ambapo nae akamsogelea Baba yangu na kuanza kumpapasa uso wake ambao nao mara ukawa unag'ara pia, na kisha akaniambia mie: 'Amka kwani Baba yako tayari uso wake ni mweupe' na nilioamka nikauona uso wa Baba yangu ukiwa mweupe, hivyo nikamuuliza yule Mtu: 'Kwani wewe ndie nani?' ambapo nae akasema kua: 'Mimi ndie *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nimemumbea Baba yako kutokana na kunisalia kwake' hivyo ndio maana mimi nikawa ni mwenye kudumu na Salat An Nabii.'

Imam Abu Basr Al Basr anasema kua: **'Safari moja mimi na Ayyub Sakhtiyani tulikua safarini kuelekea mjini Dimashq, ambapo njiani tukakutana na Mtumwa Mweusi, ambae alikua amebebea chakula cha kutosha pamoja nae. Hivyo tukamuuliza: 'Jee ni nani mmiliki wako?' ambapo akajibu: 'Ni Mtumwa kama**

mimi' yaani akimaanisha kua mmiliki wake halisi ni A*llah Subhanah wa Ta'ala*, kisha akanyanyua mikono yake juu na kusema: 'Ya Allah ijaalie ile miti pale mbele yetu iwe ni ya Dhahabu' ambapo nasi tukaona Miti iliyokua mbele yetu imegeuka na kua Dhahabu.'

Na kisha akasema kutuuliza sisi : 'Hivi Jee mmeona?' ambao nasi tukasema: 'Naam tumeona' kisha akanyanyua tena mikono juu na kusema: 'Ya Allah irudishe ile Miti iwe ya mbao kama kawaida yake.' Miti hio ikarudi katika hali yake kama kawaida, kishaakasema kutuambia sisi kua: 'Waulizeni wenye kujua kwani kwa hakika hali zao za Kimiujiza kamwe haziwezi kubadilika''

Ayyub As Sakhtiyani akasema: **'Hakika mimi nimeshangazwa na hali ya Mja huyu na kauli yake na pia nimeadhirika na nnaona haya mbele yake' kisha akamuuliza mtu huyo: 'Hivi Jee unacho chakula cha kutosha?' ambapo nae Mtu huyo akanyoosha Mkono wake na hapo hapo ikatokea Asali ndani ya Chupa yake, ambapo rangi ya Asali hio ilikua nyeupe zaidi ya Theluji na harufu yake ni zuri zaidi ya Miski.**

Kisha akatuambia sisi: 'Karibuni kuleni, pamoja nami, Wa Allahi mimi nnaapa kua Asali hii sio kama Asali ya Nyuki hawa wa Duniani' hivyo nasi tukala pamoja nae, ambapo Asali hio ilikua ni tamu kuliko kitu chochote kile tulichowahi sisi kukionja hapo kabla, jambo ambalo lilitushangaza sana sisi. Ambapo Mtu huyo akatuambia: 'Kwa hakika wale wanaoshangazwa na Miujiza ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua si wenye Hikma, na yeyote yule asieamini kua haya hua yatokanayo kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi yukoa mbali sana nae, na yeyote yule atakaeona Miujiza hii ni kisha ndio akaanza kua ni mwenye kufanya Ibada basi mtu huyo ni mwenye hali ya Ujinga.'

Imam Abu Basr Al Basr anasema kua: **'Safari moja mimi nilikua nikielekea katika Ardhi ya Sham, ambapo kabla sijafika mwisho wa Safari yangu basi njiani nikapotea kabisa, kiasi ya kua nikawa sijui hata nielekee wapi, na mara nikamuona Mwanamke Mtu mzima ambae alinifuata na kuniuliza: 'Ewe Mtu mgeni Jee umepotea Njia?**' na kisha akasema: **'Lakini inawezekanaje mtu mcha Mungu awe ni mwenye kupotea njia?' na kisha akachukua fimbo yake na kuniambia huku akinishikisha: 'Kamata hii fimbo na tembe mbele yangu'**

Na hivyo nami nikashika ncha ya fimbo hio na kuanza kutembea mbele yake, ambapo nilitembea kwa hatua 7 na kisha nikauona Masjid Al Aqsa ukiwa mbele yangu, hivyo nami nikafikicha macho yangu kutokana na kutoamini macho yangu huku nikisema: 'Inaonekana sioni vizuri au nnaona vitu vyengine sivyo?' ambapo mwanamke huyo akasema: 'Ewe Mja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwendo wako ni mwendo wa Mcha Mungu wakati mwendo wangu mimi ni wa mwenye Hikma,

ambapo mcha Mungu hua ni mwenye kutembea kwa miguu lakini mwenye hikma hua ni mwenye kutembea kwa kuruka, hivyo jee itakuaje yule anaetembea kwa miguu kua ni mwenye kumfikia yule anaeruka?' na kisha Mtu akatoweka.'

Imam Abu Basr Al Basr anasema kua: **'Mimi nilimnunua Mtumwa kwa ajii ya kunisaidia katika kazi zangu, na nilikua ni mwenye kutaka kua awe ni mwenye kulala pia ndani ya nyumba yangu, lakini ikawa kila siku usiku nagundua kua alikua halali ndani mbali ya kua nilikua ni mwenye kufunga Milango yangu yote, ambapo siku ya pili yake asubuhi alikua akija mbele yangu na kunipa Dirham moja ya Dhahabu, hivyo nikamuuliza mimi: 'Hivi Unazipata wapi hizi Dirham wewe?'**

Ambapo nae akaniambia kwa kusema kua: **'Usiwe na wasi wasi kwani mimi kila siku nitakua nnakupa Dirham moja ya Dhahabu kwa sharti la kua uniruhusu nitoke katika wakati wa usiku.'**

Hivyo akawa ni mwenye kufanya hivyo kila siku, hadi pale siku moja alipokuja Jirani yangu na kuniambia kua Mtumwa wako hua anatoka usiku na kuenda kuchimba Makaburi na kuiba ndani yake, ambapo hili ni jambo ambalo lilinihuzunisha sana mimi, hivyo nikasema kua sasa hivi nitamfungia ndani asitoke tena, hivyo usiku wa siku hio nikamfungia ndani, lakini baada ya sala ya Isha nikamuna yue mtuwa ameshatoka, huku ikiwa sijui ametokaje, lakini nilipomuona nje basi nikaamua kumfuata kimya kimya.

Mtumwa huyo alitoka na kuenda hadi katika sehemu ambayo haina watu na kisha akabadilisha nguo zake na kuvaa nguo nyengine zilizochakaa na kuanza kusali hadi Alfajiri. Kisha akanyanyua mikono juu na kusema: 'Ewe Mola wangu nitumie ada yangu ili nipate kumlipa anaenimiliki' na mara hapo hapo ikaanguka Dirham moja kutoka juu, hivyo nae akaichukua na kuitia mfukoni mwake na kaondoka, ambapo nami ikanibidi nisali rakaa 2 kwa ajii ya kumuomba Msahama *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na kumfikiria sivyo mtu huyo.

Na kisha nikaamua kua bora nimuachie huru Mtumwa huyo, lakini hata hivyo nilipomtafuta Mtumwa huyo basi sikumuona na alikua ametoweka, na mimi ikawa siioni hata njia ya kurudi nyumbani, hivyo nikawa ni mtu mwenye majuto makubwa na huzuni kubwa sana, katika kuhuzunika kwangu huko mara akatokea mtu mbele yangu, ambae aliniuliza kwa kusema: 'Ewe Abu Basr Al Basr, hivi unafanya nini hapa katika wakati kama huu?'

'Nami nikamuelezea kua niliku anamtafuta Mtumwa wangu ili nimuwache huru lakini pia nimepotea kwani hata njia yakurudi nyumba siioni, hivyo Mtu huyo akasema: 'Hivi Jee unajua umbali wa masafa uliyokuwepo hapa na nyumbani

kwako katika Mji wa Basra?’ ambapo nami nikasema: ‘La Sijui’ hivyo mtu huyo akasema: ‘Kwa safari ya mpanda Farasi anaeenda kwa kasi basi ni safari ya masaa 60, hivyo usiondoke bora bakia hapo hapo kwani Mtumwa wako hana mda atakuja.’’

‘Hivyo nami nikakaa kitako hapo hapo, na mara nikajikuta nimekaa pembeni ya Mtumwa wangu huku mbele yetu kukiwa kuna Meza ambayo imejaa vyakula vya kila aina, ambapo Mtumwa wangu huyo akasema: ‘Karibu Kula Bwana wangu’ hivyo kimya kimya nami nikala, na kisha ukaingia wakati wa Sala ya Alfajir nasi tukasali sala ya Al Fajir na kisha akanikamata mkono wangu na tukatembea hatua 2-3 na mara tukajikuta tuko mbele ya Nyumba yangu.’

Kisha mfanyakazi huyo akasema: ‘Si ulisema kua unataka kuniachia huru?’ nami nikasema Naam, nae akainama na kuokota Jiwe lilipo chini pembeni yetu ardhini ambao alipoliokota na kuinuka nacho basi kikawa pande la Dhahabu, na akanipa huku akisema: ‘Haya hapo ndio malipo ya kujiachia huru kwangu kutokana nawe’ na kisa nilipopokea Dhahabu hio basi Mtumwa huyo akatoweka.

Asubuhi yake nikamfuata Jirani yangu alieniambia kua Mtumwa wangu ni mwenye kufukua Makaburi, na kumwambia yaliyotokea ambapo nae akawa ni mwenye kusema kua: ‘Kweli yule Mtumwa alikua ni wa Miujiza’ huku akiwa na Majuto na kulia kutokana na kufikiria kinyume chake, na hivyo akawa ni mwenye kuomba msamaha kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala.*

Imam Abu Basr Al Basr anasema tena kua: **‘Mimi nilikua najitayarisha kwa ajili ya *Jihad Fi Sabil Allah* pamoja na Wanafunzi wangu, ambapo mmoja kati yao akasoma aya ya *Surat At Tawb*a isemayo:**

﴿إِنَّ ٱللَّهَ ٱشْتَرَىٰ مِنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ ٱلْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِى
سَبِيلِ ٱللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعْداً عَلَيْهِ حَقّاً فِى ٱلتَّوْرَاةِ وَٱلإِنْجِيلِ وَٱلْقُرْآنِ وَمَنْ
أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ مِنَ ٱللَّهِ فَٱسْتَبْشِرُواْ بِبَيْعِكُمُ ٱلَّذِى بَايَعْتُمْ بِهِ وَذٰلِكَ هُوَ ٱلْفَوْزُ
ٱلْعَظِيمُ﴾

Inna All<u>a</u>ha ishtar<u>a</u> mina almu/mineena anfusahum waamw<u>a</u>lahum bi-anna lahumu aljannata yuq<u>a</u>tiloona fee sabeeli All<u>a</u>hi fayaqtuloona wayuqtaloona waAAdan AAalayhi <u>h</u>aqqan fee alttawr<u>a</u>ti waal-injeeli waalqur-<u>a</u>ni waman awf<u>a</u>

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

biAAahdihi mina All<u>a</u>hi faistabshiroo bibayAAikumu alla<u>dh</u>ee b<u>a</u>yaAAtum bihi wa<u>dha</u>lika huwa alfawzu alAAa<u>dh</u>eemu *(Surat At Tawba 9:111)*

Tafsir: ***Na kwa hakika Allah amenunua kutoka kwa Waumini Maisha yao na Mali zao, kwa Bei ambayo kwao wao itakua ni Pepo. Kwani wanaigana kwa ajili ya Allah, Wanaua na Kuuliwa. Na ahadi ya Allah ni ya Kweli katika Tawrat, katika Injil na katika Qur'an, na jee ni yupi yule ambae ni mkweli kwa ahadi zake zaidi ya Allah? Hivyo furahieni bei ambayo mmeshapatana nae, kwani huko ndiko Kufuzu kukubwa zaidi.***

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wangu alikuwepo kijana mwenye umri wa miaka 15, ambae alikua amefiliwa na Baba yake karibuni na alikua amemuachia mali nyingi sana, kijana huyo akasimama na kusema: 'Hivi kweli atapewa Pepo yule atakaetoa Mali zake na Uhai wake kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*?'

Ambapo aliesoma aya hio akasema: 'Naam hio ni ahadi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Ahadi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni yenye kutimizika.'

Hivyo kijana huyo mwenye umri wa miaka 15 akasema: 'Kuweni Mashahidi wangu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua mimi nimemuuzia *Allah Subhnah wa Ta'ala* Roho yangu na Mali yangu.'

Ambapo hata hivyo aliesoma aya hio basi akasema: '*Subhanah Allah!* Wewe ni Mtoto mdogo na unataka kufanya Jambo kubwa sana, hivyo nnaogopa mimi kua huenda wewe ukashindwa baadae kustahamili'

Kijana huyo akasema: '*Subhanah Allah!* Ewe Sheikh hivi itakuaje mtu awekeane ahadi na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha awe ni mwenye kushindwa kustahmili bila ya kua na msaada? Mimi najua kua hakuna kitu kama hicho, hivyo kuweni mashahidi kua mimi nimefanya Biashara na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wala sitojuta'

Kisha akatoa mali zake kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na tukaenda ane pamoja katika vita vya Jihad, ambapo akawa ni mwenye kutusaidia sisi na kuwahudumia Wanyama wetu, akawa ni mlinzi wetu wakati sisi tunapolala usiku, kiasi ya kua tulivutiwa sana na ari ya kijana huyu na tukawa nae hadi tulipofika kwenye Ardhi ya Warumi, ambapo kijana huyu akawa ni Mtu kama aliechanganyikiwa kwani alikua kila wakati akisema kua: 'Nahitaji *Aynah Al Maradhiyyah* ili nikutane nae.'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Hivyo mimi nikamuuliza kwa kusema: 'Mbona mimi sikufahamu hivi unaposema kuhusiana na *Aynah Al Maradhiyyah*? Hua unakusudia nini?' ambapo nae akasema: 'Jana nilipolala niliota nikiambiwa kua niende kwa *Aynah Al Maradhiyyah*, na mara nikajikuta nipo kwenye Bustani nzuri sana, ambayo ndani yake kulikua kuna Mito yenye maji safi na meupee na pembeni yake kuna Hur Al Ayn wengi sana na wazuri sana kiasi ya kua uzuri wao hauelezeki, ambapo waliponiona mimi basi wakawa wanasema: 'Hizi hapa ni Habari njema kwani amekuja Mume wa *Ayna Al Maradhiyyah*''

Hivyo nilipowakaribia basi nikawasalimia kisha nikawauliza: 'Hivi jee *Ayna Al Maradhiyyah* yuko wapi miongoni mwenu?' nao wakasema: 'Hayuko miongoni mwetu kwani sisi ni Watumishi wake tu, endelea mbele zaidi utakutana nae' hivyo nami nikaendelea mbele zaid na nikaingia kwenye Bustani ambayo ni nzuri zaidi ya ile ya mwanzo kwani ina Mito yenye kutiririka Maziwa na mna *Hur Al Ayn* wazuri zaidi ya wale niliowaona kabla yake, nikawasalimia na kuwauliza yuko wapi A*yna Al Maradhiyyah* ambapo nao wakaambiana kua: 'Huyu ndio Mume wa *Ayn Al Marddhiyah*' kisha wakasema : 'Sisi ni Wafanyakazi wake, tu endelea mbele zaidi utakutana nae.'

Hivyo nikaendelea mbele zaidi na nikajikuta niko kwenye Bustani nyengine ambayo ni nzuri zaid, ambayo ndani yake kulikua kuna Mito yenye kutiririka Asali nyeupee na pembeni yake kuna *Hur Al Ayn* wengi sana na wazuri sana zaidi ya wale waliotangulia hapo kabla kiasi ya kua uzuri wao hauelezeki, nikawasalimia na kuwauliza yuko wapi A*yna Al Maradhiyyah* ambapo nao wakaambiana kua: 'Huyu ndio Mume wa *Ayn Al Maradhiyah*' kisha wakasema : 'Sisi ni Wafanyakazi wake tu, endelea mbele zaidi utakutana nae.'

Hivyo nikaendeela mbele zaidi na nikakutana na Hema ambalo lilikua limejengwa kwa Lulu na nguzo za Nuru, ambapo nje yake kulikua kuna Hur Al Layn wawili wamesimama wakiwa wamependeza vizuri sana na waliponiona basi wakasema: '*Ayn Al Maradhiyah* huyu ndie yule ambae amejaaliwa kua Mume wako' hivyo nikakaribishwa ndani na nilipoingia nikakutana na *Ayn Al Maradhiyyah,* alikua amekaa juu ya Kiti cha Dhahabu, kilichopambwa kwa Lulu na Rubi na nilipomuona tu uzuri wake Mwanamke huyo basi, nilichanganyikiwa kwani alikua ni Mzuri kuliko *Hur Al Ayn* wote.

***Ayn Al Maradhiyah*' aliponiona katabasamu kwa tabasamu lenye uzuri ambao sijawahi kuuona na kisha akaniambia kwa sauti nzuri na inayovutia kwa kusema: 'Karibu ewe Mja mpendwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kua na subira kwani sasa hivi bado uko Duniani, hivyo bado mda unao, kwani utakua pamoja nasi kesho**

usiku'' na kisha baada ya hapo nikazindukana, huku nikiwa siwezi kusubiri hadi hio kesho kutokana na Uzuri wa *Ayn Al Maradhiyah.*

Ambapo wakati ananielezea hivyo basi mara mashambulizi ya vita yakaanza, na hivyo kijana huyo akawa ni mwenye kupigana kwa ari kubwa sana na ushujaa mkubwa sana, na akajeruhiwa vibaya sana, na akaanguka chini huku akiwa ni mwenye kutabasamu kwa tabasamu kubwa sana, na baada ya vita alionekana akiwa amekufa na kuupata ushahidi huku akiwa na hali ya furaha kubwa sana.

Anasema Imam Fudayl Ibn Ayadh alisema kua: '**Abu Basr aliniambia mimi kua: Mimi nilisali kwa siku tatu mfululizo usiku nikiomba dua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema kua: 'Ya Allah nakuomba hebu nioneshe rafiki yangu nitakaekua nae Peponi' ambapo katika siku ya tatu nikaoteshwa kuambiwa kua: 'Ewe Abd Wahid Ibn Zayd mwenzako wa Peponi ni Maymun Ibn Siwda' nami nikauliza: 'Jee anapatikana wapi Mtu huyu?' nikaambiwa kua anapatikana katika Mji wa Kufah katika Kabila fulani, liliopo sehemu fulani.'**

Hivyo nami nikafunga safari hadi katika Mji wa Kufah na kuelekea katika sehemu niliyoelekezwa ndani ya Ndoto yangu, na nilipofika nikamuulizia Maymun Ibn Siwda, nikaambiwa kua ni Mwendawazimu aliepo katika eneo fulani akichunga Kondoo. Hivyo nikaelekea kwenye eneo hilo na nilipofika katika eneo husika nikamkuta mtu ambae alikua amevaa nguo za zamani akiwa anasali huku pembeni yake kukiwa kuna Kondoo ambao nao pia wamechanganyika na Mbwa mwitu pamoja, amapo baada ya kumaliza kusali basi akanigeukia na kuniambia: 'Karibu ewe Ibn Zayd, ila hapa haiwezekani kwako wewe kukaa hivyo wacha tuoana baadae'

Nami nikasema: 'Allah akuingize kwenye rehema zako, Jee ulijuaje kua mimi ndie Ibn Zayd?' nae akasema: 'Mimi nakujua wewe kabla tangu hujazaliwa' nami nikasema: 'Jee unaweza kuniusia?' nae akasema: 'Inakuaje hadi unamshukuru Kiumbe aliekupa kitu? Ila unatakiwa umshukuru *Allah Subhana wa Ta'ala* kwa kuumba na kisha kukujaalia kila neema aliyokujaalia, hivyo bila ya shaka shukrani zote anastahiki yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala'*

Nami nikauliza: 'Inakuaje hadi Kondoo wako unaowachunga wakawa wanachanganyika na Mbwa Mwitu pamoja bila ya kudhuriana?' nae akasema: 'Hakika mimi nnamuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika hali ambayo hua hakuna Ukuta wala pazia baina yangu na yake, kutokana na hali hii basi haiwezekani ikawa kuna uadui baina ya Kodoo hawa na Mbwa mwitu na hivyo hua kuna urafiki tu baina yao.'

Hivyo amesema Imam Abu Basr Al Basr kua: **‘Hata kama tutasali Sala za Viumbe wote Duniani basi kamwe hatutoweza kuonesha shukran stahiki mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kutokana na Neema zake juu yetu Duniani.’**

Na akasema tena kua: **‘Kama ukijihisi kua una uvivu katika kufanya Ibada zako kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi achana na kula vyakula vizuri na vitamu kwa mda na badala yake kula vyakula vyenye chumvi.’**

Imam Abu Basr Al Basr alisema: **‘Njia ya Mkato kuelekea Peponi ni kupitia katika Vita vya Jihad’**

Na akasema: ‘**Yeyote yule atakaeweza kulilinda Tumbo lake kutokana na vitu vya Haram, basi hua ni mwenye kuweza kuilinda Dini yake na Tabia zake, na yeyote yyule asieweza kulilinda na vitu vya Haramu basi mtu huyo hatoweza kuilinda Dini yake wala Tabia zake.’**

Imam Abu Basr Al Basr anasema: ‘**Kuna siku tulikua tunasafiri Baharini, na mara Jahazi letu likakubwa na Kimbunga, na hivyo likavutwa hadi kwenye Kisiwa Kimoja, nasi tukashuka na kuanza kutembea kwenye Kisiwa hicho, na nikakutana na mtu ambae alikua anaabudu Sanam kwenye Kisiwa hicho. Hivyo nikamuuliza: ‘Mbona Unaabudu kile ambacho hakitokufaa kitu wala kutokukudhuru?’**

Nae akaniuliza: ‘Kwani nyinyi mnaabudu Nini?’ nami nikasema: ‘Sisi Tunamuabudu *Allah Subhanah wa Ta’ala* alieumba kila kitu’

Mtu huyo akauliza: ‘Jee ni nani aliekuambieni kuhusiana na huyo Allah?’

Nami nikasema: ‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* alituma Mtume *Salallahu Alayhi wa Salam* ambae emetutaarifu sisi juu ya hilo’

Mtu huyo akauliza: ‘Yuko wapi huyo Mtume?’

Nami nikajibu: ‘Amefariki baada ya kufikifsha ujumbe wake alietumwa na *Allah Subhanah wa Ta’ala* juu ya watu’

Ambapo mtu huyo akauliza; ‘Jee amewacha uthibitisho wowote ule?’

Nami nikamwambia: ‘Naam amewacha kitabu kinachoitwa Qur’an’

Nae akasema: ´Hebu nioneshe hicho Kitabu’ nami nikamuonesha, ambapo nae akasema kua: ‘Kwa nbahati mbaya mimi sijui kukisoma hiki kitabu.’’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na hivyo mimi nikamsomea baadhi ya Sura, nae akaanza kulia baada ya kumaliza kumsomea na kisha kasema: ‘Maneno yake ni sahih haifai kua ni muasi dhidi ya yule alieiumba Dunia na kila kitu chake’ na kisha akasilimu na kua Muislam. Na tukamsomesha Ilm ya Dini na baadhi ya Sura za Qur’an.

Usiku huo tukasali Sala ya Isha nakisha ulipofika wakati wa kulala tukaenda kulala, lakini yeye hakuenda Kulala bali alikaa akiomba na Kusali Hadi Alfajiri, hivyo nikawaambia Wanafunzi wangu: ‘Huyu ni Muislam mwenzetu mpya hivyo inabidi tumchangie japo kidogo sadaqa ili asipate shida’ hivyo tukachanga na kisha tukampa, ambapo nae akauliza: ‘Za nini hizi?’ tukamwambia chukua zitakusaidia.

Ambapo nae akasema: ‘La Ilaha Illa Allah, wakati nilipokua peke yangu kwenye Kisiwa hiki na ilikua nikabudu Masanamu kwa miaka bila ya kumjua *Allah Subhanah wa Ta’ala*, ambapo nae hakunitupa, na alinilinda jee atanitupa na kunisababishia madhara leo hii baada ya kujuana nae?’

Ambapo tulikaa nae kwa siku tatu kisha akaumwa na akawa taabani anakaribia kufariki nikamuuliza: ‘Jee unahitaji kitu chochote?’ nae akanijibu: ‘Usiwe na khofu kwani *Allah Subhanah wa Ta’ala* ameshanitekelezea haja zangu.’ Halafu akafariki.

Hivyo tukamkosha, tukamsalia na kumzika, ambapo katika siku tuliyomzika nilipolala usiku wake nikamuona kwenye Ndoto kua kua yupo Peponi, huku akiwa kwenye Kasri kubwa sana na *Hur Al Layn* huku akiwa anasema:

﴿جَنَّاتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَالمَلاَئِكَةُ
يَدْخُلُونَ عَلَيْهِم مِّن كُلِّ بَابٍ۞سَلاَمٌ عَلَيْكُم بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَىٰ ٱلدَّارِ﴾

Jannatu AAadnin yadkhuloonaha waman salaha min aba-ihim waazwajihim wathurriyyatihim waalmala-ikatu yadkhuloona AAalayhim min kulli babin; Salamun AAalaykum bima sabartum faniAAma AAuqba alddari *(Surat Ar Rad 13: 23-24)*

Tafsir: ***Aden Peponi wataingia wale ambao ni waliofanya Mema kutoka katika Mabab zao, Wake zao na Watoto wao. Na Malaika watawakaribisha katika kila Mlango huku wakiwaambia: ‘Salaam Alaykum kutokana na Subra yenu, hii ni Neema kubwa sana iliyoje.’***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abu Basr Al Basr aliulizwa: **'Hivi Jee Muumini anatakiwa awe vipi?'** ambapo nae akajibu kwa kusema kua: **'Awe ni mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* awe ni mwenye kusawijika uso wake anapotajwa Mola wake, awe ni mwenye kuachana na mambo maovu, na kushikamana na maamrisho ya Mola Wake, awe ni mwenye kufikiria siku ya Malipo, na awe ni mwenye kutetemeka kuokana na kutajiwa Moto wa Jahannam, kutokana na Madhambi ambayo ameyafanya, awe ni mwenye kuona haya mbele ya Mola wake, awe ni mwenye kujihesabia Nafsi yake, kabla ya hata kusema neno lolote awe ni mwenye uyapima maneno yake hayo, kiasi ya kua kama ni ovu basi awe si mwenye kulitamka neno hilo, kwa kuogopa kusababisha madhara kwa mwenzake, kwani madhambi yake ni yenye kuumiza sana, hua si mwenye kuona makosa na kasoro za Ibn Adam wenzake, na kumsalimisha mwenzake kutoka na mkono wake. '**

Alisema Imam Abu Basr Al Basr kua: **'Hata kama ingekua sisi ni wenye kusjudu kwa siku nzima kila siku basi bado haitoshelezi kwetu sisi kua ni wenye kuonesha Shukran kwa Mola wetu kutokana na Sijda hizo. Hivyo kua na shukrani kwa Mola wako mara kwa kadri uwezavyo.'**

Anasema Imam Abu Basr Al Basr alifariki mwaka 177 Al Hijr.

IMAM YUNUS IBN UBAYD

Imam Abu Abd Allah Yunus Ibn Ubayd alizaliwa katika miaka 100 ya mwanzoni ya Uislam katika Mji wa Basra. Na alisoma kutoka kwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwemo Anas Ibn Malik *Radhi Allahi Anhu* na hivyo kua ni Mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith, na hivyo kua ni mwenye kuaminika katika uhifadhi wa Hadith na alikua ni mwenye kuhifadhi Hadith 100,000 pamoja na Sanad zake.

Imam Yunus Ibn Ubayd ni mwenye Ilm kubwa na Ucha Mungu pia kwani ni mwenye kuenda sambamba na Imam Thabit Ibn Bunani, Imam Ibrahim At Taymi, Imam Hasan Al Basr, Imam Muhamamd Ibn Sirrin, Imam Said Ibn Jubayr, Imam Ataa Ibn Abi Rabiah, n.k.

Ambapo nae amewasomesha kina Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Shub'ah Ibn Hajjaj, Imam Hammad Ibn Salim, Imam Hammad Ibn Zayd, Imam Bishr Ibn Mufazal, n.k

Imam Yunus Ibn Ubayd alikua pia ni mfanyabiashara wa Mapazia, na kutokana na Ucha Mungu wake basi alikua ni mwenye kutopenda kujihusisha na Vitu vya vyenye shubha kwani alikua akiogopa hua huenda vikampelekea kua ni mwenye kula vya Haram, kiasi ya kua alikua si mtu mwenye kufungua Duka lake katika siku za Mvua au zenye Mawingu kwani alikua akiona kua hali ya hewa inapokua sio nzuri basi Wanunuzi hua si wenye kuona vizuri ubora wa Bidhaa zake.

Ambapo na kua na Ucha Mungu sana basi siku moja alimuona mmoja kati ya watu waliokua Sokoni hapo akiwa na Pazia ambalo alikua ni mwenye kua na uhakika kua amelinunua kwenye Duka lake, hivyo akamsalimia na kisha akamuuliza Mtu huyo, kwa kusema: '**Hili Pazia umenunua wapi na bei gani?'**

Yule Mnunuzi akasema kua amelinunua kwa Dirham 400 na kisha akamuelekeza aliponunua na hivyo Imam Unus Ibn Ubayd akawa na uhakika kua ni katika Duka lake, ila sasa mbona kauziwa ghali? Hivyo akamwambia yule Mnunuzi kua: '**Hili Pazia umeuziwa si kwa bei yake, kwani hilo ulilonunua ni Duka langu hivyo rudi nenda kachukue Diram 200 zako'**

Hivyo Mnunuzi akasema: '**La, Hili Pazia kutokana na Uzuri wake basi thamani yake ni Dirham 500, hivyo hain ahaja ya mimi kurudi kuchukua Dirham 200. '**

Imam Yunus Ibn Ubayd akasema: '**Vyovyote itakavyokua basi wewe twende ukachukue pesa zako zilizobakia'** hivyo baada ya kulazimishwa basi mnunuzi huyo akarudi na Imam Yunus Ibn Ubayd hadi Dukani kwake na kisha akapewa Dirham 200 zake, kisha baada ya hapo Imam Yunus Ibn Ubayd akasema kumwambia Muuzaji wa Duka lake ambae ni Mtoto wa Dada yake kua: '**Kwanini ukamuuzia kwa bei kubwa lile Pazia?**' ambapo kijana huyo Muuzaji akajibu kwa kusema: **'Wa Allahi amelipa kwa ridhaa yake, kwani mimi wala sikumlazimisha**' Imam Yunus Ibn Ubayd akasema: '**Hata kama kwa ridhaa yake basi hua haifai.'**

Siku moja Imam Yunus Ibn Ubayd alimuona mfanyakazi wake wa Dukani kwake akimuonesha Mnunuzi moja kati ya Mapazia hayo, ambapo nae akasema kutokana na uzuri wa Pazia hilo kwa kusema: '**Ya Allah! Nijaalie Mimi pia kua na Pazia kama hili la Peponi'** na hivyo baada ya hapo hakua ni mwenye kutaka kuliuza Pazi hilo, kutokana na kuhisi kua tayari ameshakisifia na kukiona kizuri kile anachokiuza, na hivyo kua ni mwenye kujiona kutokana na tukio hilo.

Kwani Imam Yunus Ibn Ubayd alikua ni mtu mwenye kuitolea mhaga Dunia yake kwa ajili aya Akhera yake, mtizamo ni kua Biashara ya Kidunia si chochote mbele ya faida inayopatikana kutokana na Biashara ya Kiakhera, na hivyo alikua akisema: '**Kuna umuhimu wa kula chakula cha halali vyovyote vile itakavyokua, hivyo kama nikipata Sentimoja itakayonipatia Chakula cha Halali, basi hua ni mwenye**

kuitumia haraka sana kwa ajili ya kununulia unga na kupika chakula kutokana nayo, na kisha hua ni mwenye kumpa mgonjwa yeyote yule ale kwani Chakula hihiki hua ni Dawa kutokana na Uhaali wake kwa Idhini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Anasema Imam Yunus Ibn Ubayd kua: '**Hakika mimi nnaweza kujua kuhusiana na mtu anaeweza kujiokoa na venye shubah kutokana na namna anavyozungumza, kwani kuna kitu ambacho hua ni chenye kuingilia kati baina ya amali njema zake, lakini kama akiweza kuudhibiti ulimi wake basi hali hua ni vyenginevyo, kwa sababu hua hakuna kinachoweza kuingilia baina ya amali njema zake.**

Ambapo hata kama mtu huyo atakua anasali sana, anafunga sana lakini hapo hapo hua ni mwenye kufungua Funga yake kwa vyakula vya Haramu, hivyo kamwe hatokua ni mwenye uwezo wa kunufaika na Funga yake, na hata kama akiwa ni mwenye kusimama usiku kwa ajili ya *Qiyam Al Layl*, basi Moyo wake hua katika hali ya Unafiq, kujionesha na kuridhika na Ibada zake, kwani katika wakati wa Mchana hua ni mwenye kusema Uongo, Kutotekeleza ahadi zake na kusema maneno yasiyokua na maana, mambo haya yanapotokea basi hua hakuna jema moja wanalolifanya kua ni lenye kuweza kuwanufaisha. Lakini kama wakiwa ni wenye kuweza kudhibiti ndimi zao, basi na amali zao pia hua ni zenye kuwanufaisha, na huo ndio mtizamo wangu'

Imam Yunus Ibn Ubayd anaendelea kusema kua: **'Hakika mimi nnajiona kua ni kama Mtu ambae ni mwenye kuona ndani ya Ndoto zake kile akipendacho na kile akichukiacho, ambapo ingawa watu wengine ni wenye kuona hayo pia katika Ndoto zao, na hivyo pale watakapofariki ndipo watakapo zindukana na kujiona kua kumbe walikua wamelala na hakuna kilichobakia kutoka katika usingizi wao na hivyo hawana cha zaidi isipokua majuto makubwa badala yake kutokana na kupoteza vile vitu vyote ambavyo walikua wakivipenda na kuvithamini Duniani'**

Ingwa Imam Yunus Ibn Ubayd alikua ni mwenye kujichunga sana na ni Mcha Mungu sana lakini hata hivyo alikua ni mwenye kusema kua: **'Najua mimi kua Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Kubwa sana na sina shaka juu ya hilo, lakini sasa sina uhakika kua kama kweli mimi nitakua ni miongoni mwa watakaoingizwa kwenye Rehma hizo, na nna khofu pia kua huenda watu wengine wanaweza kutoingizwa kwenye rehma kutokana nami.**'

Imam Yunus Ibn Ubayd anaendelea kusema kua: **'Kama ukitaka kumjua mtu aliekua tofauti nje yake na ndani yake basi niangalie mimi' alipoulizwa kwa nini akasema hivyo basi nae akajibu: 'Kwa sababu mimi nnaweza kuhesabu tabia na akhlaki njema zaidi ya 100, lakini hata hivyo mimi siioni hata moja kati yao ndani yangu,**

na nnapoyahesabu mambo maovu basi yote nnayaona kua nayo ndani ya Nafsi yangu.'

Imam Yunus Ibn Ubayd amesema pia kua: **'Kuachana na kauli sizo hua ni vigumu kwa Nafsi kuliko kufunga kwa siku Moja, sifananishi kutogombana au kusema maneno siyo kuhusiana na watu katika siku ya Kiangazi, huku ukiwa umefunga, kwani mimi hua nnaiona siku hio kufunga hua ni ngumu sana inapokua kuna joto kuliko kuuzuia ulimi'**

'Kuna mambo mawili ambayo yakikamilia ndani ya mtu, basi hali zake zote hua ni zenye kukamilika kutokana na mambo mawili hayo, ambapo kwanza ni Kusali Sala za Fardhi katika wakati wake, na pili hua ni kuulinda Ulimi kutokana na mambo yasiyokua na maana, kwani kama mtu akiweza kuulinda Ulimi wake kutokana na mambo sio, basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamnyooshea mambo yake'

'Kwani hakuna yeyote yule anaejihesabia maneno yake kutokana na kua na uangalifu juu ya kile anachokisema isipokua utauona tu uzuri wa matendo yake.'

'Yeyote yule anaeidharau Ibada za Sunnah basi hua ni mwenye kuzishusha thamani Ibada za Fardhi'

Ghassan Ibn Mufadhal amesema kua: **'Kuna mtu alikuja kwa Yunus Ibn Ubayd na kisha akaanza kulalamikia ugumu wa hali yake ya Maisha na wasiwasi wake juu ya ugumu wake huo, ambapo Yunus Ibn Ubayd akamuuliza Mtu huyo: 'Hivi Jee uko tayari kuyatoa Macho yako kwa ajili ya kulipwa dirham 1000?' ambapo Mtu huyo akasema : 'La' Yunus Ibn Ubayd akauliza: 'Na vipi kuhusiana na Masikio yako?' mtu huyo akasema: 'La' Yunus Ibn Ubayd akasema: 'Vipi kuhusiana na Ulimi wako?' Mtu huyo akasema: 'La' Yunus Ibn Ubayd akauliza: 'Vipi kuhusiana na Ufahamu wako?''**

Mtu huyo akasema : 'La, kamwe siwezi hata unipe kitu chochote kile Ulimwenguni' Yunus Ibn Ubayd akasema: 'Hizo zote ni baadhi tu ya neema za *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yako ambapo ukizijumlisha Neema zote alizokujaalia *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yako basi unaweza kupata zaidi ya Milioni ya Dirham, halafu unalalamikia kuhusiana na Ugumu wa Maisha yako.''

Imam Yunus Ibn Ubayd alisema: **'Sijui kitu chengine chochote mimi ambacho ni adim zaidi ya Dirham ya halali, kisha ikatumiwa katika njia ya halali, au Ndugu wa Kiislam ambae unapokua nae basi unapata utulivu wa Moyo wako, kwani vitu viwili hivi vinakua ni adimu sana kila siku zinavyoenda.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Siku moja Imam Yunus Ibn Ubayd alimuona Mtoto wake akiwa anatoka kwenye Nyumba yenye kua na matamanio ya Kidunia Ndani yake, hivyo akamwambia Mtoto wake huyo kwa kusema kua: **'Ewe Mtoto wangu, umetokea wapi' ambapo Mtoto huyo nae akajibu: 'Nimetoka kwenye Nyumba ya Amr Ibn Ubayd'**

Imam Yunus Ibn Ubayd akasema: 'Ewe Mtoto wangu hakika mimi kukuona wewe ukiwa unatoka kwenye Nyumba ya Mtu mwenye kuiendekeza Dunia yake ni bora zaidi kuliko kukuona ukiwa unatoka kwenye nyumba ya Fulani ibn Fulani, Ewe Mtoto Wangu kwangu mimi kukuona wewe ukiwa umekutana na Mola wako wakati ukiwa katika nyumba ya Mzinifu, Mwizi, Mfanya madhambi ni bora kwangu kuliko kua umekutana na Mola wako huku ukiwa katika Nyumba ya Mtu Mpotovu ambae atakupelekea wewe kua ni mwenye kutoka kwenye Dini yako.'

Alisema Imam Yunus Ibn Ubayd kua: **'Hakuna kitu kigeni kama Sunna na kilichokua kigeni zaidi kama mwenye kuijua Sunna na kuifanyia Kazi'**

Imam Yunus Ibn Ubayd alifariki mnamo mwaka 756 (H.139).

IMAM YAHYA IBN ABI KATHIR

Imam Abu Nadhr Yahya Ibn Abi Kathir Salih Ibn Al Mutawwakil alikua n Mtumwa alieachiwa huru na Abu Nasr Al Yamani alizaliwa mjini Basra nchini Iraq na kisha akahamia katika Mji wa Madina ambapo aliishi kwa miaka 10 na kisha akaelekea katika Ardhi ys Al Yamamah nchini Syria, na alifariki nchini Syria mnamo mwaka 129 Al Hijra.

Kutokana na kuishi kwake huko katika maeneo hayo tofauti kutokana na kutafuta Ilm basi Imam Yahya Ibn Abi Kathir alikua na Ilm kubwa sana ya Qur'an Hadith na Fiqh, kwani alisoma kwa Masahaba wakiwemo kina Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*, Abu Salamah Ibn Abd Rahman Ibn Awf *Radhi Allahu Anhu*,na pia alisoma kwa Wanazuoni wa Tabiina wakiwemo kina Imam Hilal Ibn Abi Maymun, Imam Muhammad Ibn Ibrahim At Taymi, Imam Yaala Ibn Hakim, Imam Abd Rahman Ibn Qatadah n.k.

Ambapo anaema Imam Shu'bah kua: '**Yahya Ibn Abi Kathir yuko juu zaidi kwa Ilm kuliko Al Zuhri.'**

Na Imam Ahmad Ibn Hanbal akasema kua: '**Yahyha Ibn Abi Kathir na Al Zuhri ni watu wenye Ilm kubwa sana miongoni mwa watu.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ayub Ibn Sakhtiyani akasema kua: '**Hakuna aliebakia katika ardhi hii kama Yahya Ibn Kathir'**

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Hatim basi yeye anasema kua: **'Yahya Ibn Abi Kathir ni Thiqah'**

Na Imam Al Madini akasema: **'Watu sita ndio waliohifadhi Ilm iliyofikishwa kwenye Ummah huu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, ambao ni Amr Ibn Dinar wa Makkah, Az Zuhri wa Madina, Abu Is-haq Ash Shabi na Al Amash wa Kufah, Qatadah na Yahya Ibn Abi Kathir wa Basra.'**

Imam Amr Ibn Yasir amesema kuhusiana na Yahya Ibn Abi Kathir kua: **'Yahya alikua ni mwenye kuvaa nguo nzuri sana na ni mwenye kupenda kuonekana kua amependeza'**

Imam Ibn Hibban akasema: **'Yahya ni miongoni mwa Wacha Mungu, ambae anapohudhuria Maziko basi hua si mwenye kulala kwa mda wa siku tatu kutokana na Khofu, na haiwezekani kabisa kuzungumza nae ndani ya siku hizo tatu'**

Miongoni mwa Hadith alizozinukuu Imam Yahyha Ibn Abi Kathir ni: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaeshindwa kutekeleza Nadhiri juu ya kitu ambacho hana, Kumlaani Muumini hua ni sawa na Kumuua, na kama mtu akijiua hapa Duniani, basi ataadhibiwa kutokana na kile alichojiulia katika siku ya Malipo. Yeyote yule anaeapa kiapo cha Dini nyengine basi ni mwenye kusema Uongo na ni mwenye kuingia kwenye Dini aliyoiapia. Na yeyote yule atakaemsingizia Muislam kuhusiana na kufuru basi hua ni sawa na mtu aliemuua Mtu huyo.''**

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule anaezungumza sana basi hua ni mwenye kufanya makosa mengi sana na yeyote mwenye kufanya makosa mengi sana hua ni mwenye ua na Dhambi nyinyi sana. Hivyo yeyote yule mwenye kuamini juu ya Siku ya Malipo basi na asema Mambo mema au akae kimya.'

'Kama watu waliofunga watafungua funga yao kwenye meza yako, na watu wema wakawa ni wenye kula chakula chako basi Malaika pia huhudhuria'

'Uislam hua unasimamia kwenye mambo matatu ambayo ni:

La Ilaha Illa Allah,* hivyo usimwabie mtu aliesema maneno hayo kua ni Kafiri, kwa sababu yakufanya Dhambi, na wala usiwe shahidi juu ya jambo hilo. Kujua na kuamini kua wema na maovu yote ni yenye kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala

na Jihad inaendelea hadi siku ya Malipo, na hivyo hakuna Dhulma ya anaefanya dhulma inayoweza kuiondoa na hakuna Uadilifu wa Muadilifu unaoweza kuiondoa'

Alisema Imam Yahya Ibn Abi Kathir kua: **'Kile ambacho hakiwezekani kuharibiwa na Mchawi kwa mwezi mzima hua kinawezekana kuharibiwa na mwenye kufanya Namima (mfitinishaji) kwa saa moja tu.'**

'Kama ni ya Mtu iko sahih, basi matendo yake yatakua sahih, lakini kama nia yake si sahih basi na matendo yake pia hayatokua sahih.'

'Amali kubwa sana ni kua na Unyenyekevu.'

'Kama mtu akiwa na sifa 6 basi Imani yake itakamilia, kupigana jihadi na adui wa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Kupenda kufunga katika siku za Kiangazi, kuchanua vidole vya miguu kwa vidole vya mkono katika wakati wa kutia udhu katika kipindi cha Kipupwe. Kusali sala ya Alfajir katika siku za kipupwe, kuachana na kubishana japo kua unauhakika kua wewe uko sahih, na kua na Subra katika wakati wa mitihani.'

'Katika siku ya Malipo Mtu ataulizwa kwanza kuhusiana na Sala yake, hivyo kama Sala yake imekamilika basi na amali zake zote zitakua zimekamilika.'

'Kusoma Qur'an na kusoma Fiqh ni sehemu ya Ibada.'

Imam Yahya Ibn Abi Kathir alimuusia mtoto wake kwa kumwambia kua: **' Ewe Mtoto wangu, jihadhari na Muadhiriko, kwa sababu ni mkali zaidi ya Upanga, jihadhari na kua na Hasira kwani Hasira ni yenye kumilikiwa na wenye kufanya Dhulma, na hua ni sawa na mali ya kifo, Kamwe usibishane na watu kwani hua hakuna maana na huani kwenye kusababisha uadui baina ya ndugu.**

'Ewe Mtoto wangu shikamana na kitabu cha *Allah Subhanaha wa Ta'ala,* ewe Mtoto wangu Jihadhari na hasira kwani hua ni yenye kuuangamiza Moyo, Ewe Mtoto wangu usijali kuhusiana na hali ya walioangamia, bali jali kuhusiana na hali ya waliokoka na kuupata uongofu wa Milele, ewe Mtoto wangu fahamu kua Afya ya mwili wako ni bora kuliko Mali.'

Mbali ya kua Imam Yahya Ibn Abi Kathir alikua ni mwenye kujipenda alipofariki alikua hajawacha kitu chochote isipokua sarafu 30 za fedha ambazo zilitumika kwa ajili ya kununulia Sanda yake.

Imam Yahya Ibn Abi Kathir anasema kua: **‘Mwenye kupenda kumtii *Allah Subhanah wa Ta’ala*, Hua ni mwenye kupenda kuiheshimu Nafsi yake na mwenye kupenda kumuasi *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua ni mwenye kupenda kuiadhirisha Nafsi yake.’**

Anasema Imam Al Awzai kua: **‘Imam Yahya Ibn Abi Kathir ilikua kila unapowadia Mwezi wa Ramadhani basi alikua ni mwenye kuomba Dua ifuatayo:**

اللَّهُمَّ سَلِّمْنِي لِرَمَضَانَ وَسَلِّمْ لِي رَمَضَانَ وَتَسَلَّمْهُ مِنِّي مُتَقَبَّلً

Allahuma Salimni Li Ramadhana wa Salim Li Ramadhana, wa Tasalamhu Minni Mutakkabala.

Tafsir: ***Ya Allah nisalimishe mimi kwa ajili ya Ramadhani, na Isalimishe Ramadhani kwangu mie na zipokee Amali zangu ndani yake kwa kuzikubali.***

IMAM IBRAHIM IBN ABI ABLA

Imam Abu Said Ibrahim Ibn Abi Abla alikua ni Mwanazuoni wa Tabiina ambae alizaliwa katika Ardhi ya Palestina katika kipindi cha baada ya Mwaka wa 60 Al Hijra, na alisoma kwa Masahaba na Wanazuoni mbali mbali akiwemo Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*, Ummu Dardaa Al Sughra, Abu Ubay Ibn Umm Hiram, Bilal Ibn Abi Darda, Abd Allah Ibn Ad Daylami n.k

Ambapo ane aliwasomesha Maimamu wengine wakiwemo kina Imam Malik Ibn Anas, Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Abd Allah Ibn Mubarakah, Imam Muhamamd Ibn Ishaq, Imam Damra Ibn Rabia, Imam Muhammad Ibn Humayr na Wanazuoni wengineo.

Ambapo anasema Abd Allah Ibn Hani anasema kua: ‘**Amesema Baba yangu kua amesema Ibrahim Ibn Abi Abla kua: ‘Khalifa Hisham aliniita mimi na kuniambia kua: Hakika mimi nnakujua wewe sana kua ni mwenye Uadilifu na ni mtu mwenye kuaminika. Hivyo nimeamua kukufanya kua ni mwenzangu wa karibu sana katika Mamlaka yangu, na hivyo nimekuteua kusimamia Malipo ya kodi ya Ardhi ya Misri’**

Hivyo nami nikasema: ‘Ama kuhusiana na maamuzi yako, ewe Amir ul Muuminin basi nami namuomba *Allah Subhanah wa Ta’ala* akulipe kwa malipo yaliyo bora,

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

na bila ya shaka yeye ni mbora na ni mwenye kutosheleza juu yetu katika wanaolipa malipo bora, ama kuhusiana na mimi basi bila ya shaka sina sifa stahiki za kusimamia kazi hio na wala uwezo juu yake’

Hivyo Khalifa Hisham akakasirika kiasi ya kua macho yake yalimtoka na uso wake akaukunja na kisha akawa ni mwenye kusema: ‘Utalainika tu kwa mamrisho yangu ukitaka usitake’ hivyo mimi nikakaa kimya, kisha nikasema: ‘Jee unaniruhusu kusema?’ nae akasema : ‘Naam’ Nami nikasema: ‘Amesema *Allah Subhanah wa Ta’ala* katika kitabu chake kua:

﴿إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ وَٱلْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَن يَحْمِلْنَهَا وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا وَحَمَلَهَا ٱلإِنْسَانُ إِنَّهُ كَانَ ظَلُوماً جَهُولاً﴾

Inna AAaradhna al-amanata AAala alssamawati waal-ardhi waaljibali faabayna an yahmilnaha waashfaqna minha wahamalaha al-insanu innahu kana *dh*aluuman jahuulan *(Al Ahzab 33:72)*

Tafsir: ***Kwa hakika tuliipa Amana, Mbingu na Ardhi na Milima lakini vikaikataa kuichukua; kwa sababu ya kuogopa: lakini Mtu akaichukua: Hakika alikua ni mwenye kujidhulumu na ni mjinga.***

‘Wa Allahi ewe *Amir ul Muuminin,* si unaona *Allah Subhanah wa Ta’al*a hakua na hasira na viumbe vyake hivyo pale vilipokataa kubeba majukumu hayo na wala hakuvilazimisha’

Na baada ya maneno hayo basi hapo hapo nikamuona Khalifa Hisham akianza kucheka kwa sauti sana, hadi jino lake la gego likawa linaonekana na kisha akasema: ‘Uko mbali sana kwa Ilm na bado unasisitizia nayo, nenda zako kwani tumekusamehe’ na akaniruhusu niondoke.

Duhaym Ibn Fadhl anasema kua: **‘Hakika mimi nimemsikia Damra akisema kua: ‘Mimi sikuwahi kuuonja utamu wa Maisha isipokua pale nilipokua nikiishi kwa kula Ndizi na Asali chini ya kivuli cha Al Quds na kumsikiliza Ibn Abi Abla akitoa Darsa lake, na sikuwahi kuona mtu mwenye lugha nzuri kama yeye.’’**

Na kwa upande wa Muhammad Ibn Himyar basi yeye alisema kua: **‘Amesema Ibrahim Ibn Abla kua anaesoma yale yasiyofaa kwenye Ilm basi hua ni mwenye kujifunza mabaya mengi’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Muhammad Ibn Zayd Al Maqdisi nae alisema kua: **‘Mimi nilimsikia Ibn Abi Abla akisema kuwaambia wale wanaorudi Vitani katika vita vya Jihadi kua: ‘Mmerudi kutoka katika Jihadi ndogo lakini jee mmefanikisha nini katika Jihadi kubwa ya Nyoyo zenu?’’**

Ambapo anasema Imam Ibrahim Ibn Abi Abla kua : **‘Walid Ibn Abd Al Malik alitutembelea sisi, na kisha akaniomba nitoe Mawaidha, nami nikatoa Mawaidha na kisha Umar Ibn Abd Al Aziz akaniambia mimi kua: ‘Ya Ibrahim, hakika wewe unatoa Mawaidha yanayogusa Nyoyo hasa.’’**

Imam Ibrahim Ibn Abi Abla anaendelea kutuambia kua : **‘Walid Ibn Abd Al Malik alikua akinipa mimi Bakuli la Dhahabu ambalo nami nilikua nalitumia kwa kuligawa kwenye Masjid Al Aqsa.’**

Miongoni mwa Hadithi alizozinukuu Imam Ibrahim Ibn Abi Abla ni ile isemayo kua: **‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Inatosheleza kumuoneshea Mtu kidole kua ni Dhambi’ ambapo Masahaba wakauliza: ‘*Ya Rasul Allah*, hata kama kwa jambo jema?’ ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Hata kama ikiwa ni Jema, kwani kufanya hivyo hua ni uovu juu yake mtu huyo isipokua *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni mwingi wa Rehma, na kama ikiwa ni juu ya uovu basi ndio ushakua uovu.’’**

Imam Ibrahim Ibn Abi Abla amesema pia kua: **‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Kitu cha Mwanzo atakachokihisi harufu yake Mtu atakapoingia Kaburini, ni Tumbo lake, Hivyo Ruhusuni vile vilivyo vya halali tu ndani ya Matumbo yenu.’**

IMAM ZAYD IBN ZAYN AL AABIDIIN 79 AH

Imam Abu Al Husayn Zayd Ibn Ali Ibn Zayn Al Abidiin Hussein Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alizaliwa katika ardhi takatifu ya Mji wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, Madina mnamo mwaka 79 Al Hijra.

Na bila ya shaka Imam Zayd Ibn Zayn Al Abidiin alizaliwa katika familia tukufu na ukoo mtukufu wa Banu Hashim ambao ni ukoo wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na alisoma kwa baba yake ambae ni Imam Zayn Al Abidiin, na akasoma kwakaka yake ambae ni Imam Muhammad Al Bakir, Imam Urwa Ibn Zubayr, Imam Abd Allah Ibn Hasan, Imam Abd Allah Ibn Rafii na Wanazuoni wengineo.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Zayd Ibn Zayn Al Abidiin hakua ni mwenye kusoma kwenye mji wa Madina tu bali pia laikua ni mwenye kutembea katika maeneo tofauti kwa ajili ya kujitafutia Ilm na alikutana na Masahaba kadhaa wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Saalam* ambao alisoma chini yao, na mbali ya kua na Ilm kubwa lakini pia *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimjaalia kua ni mwenye kua na kipaji cha kuwavutia watu wake wanaomsikiliza pale anapozungumza, kwani alikua na Lugha nzuri na maneno yenye kuvutia sana.

Na hivyo alikua ni mwenye kukubalika na kua na wafuasi wengi sana kiasi ya kua sifa na kipaji chake hicho kilimpelekea kumuingiza kwenye Mitihani kwani maadui zake wasiopenda mafanikio yake walikua ni wenye kumsingizia kwa Khalifa wa Banu Umayyad kua safari zake zilikua ni za Kisiasa na wala hazikua ni za kutafuta na kueneza Ilm ya Dini ya Kiislam, jambo ambalo lilipelekea Imam Zayd Ibn Zayn Al Abidiin kua ni mwenye kupigwa marufuku kutoka nje ya Mji wa Madina.

Ambapo anasema Imam Abu Hanifa kua: **'Katika wakati wa Zayd Ibn Zayn Al Abidin ilikua hakuna Mwanazuoni mkubwa wa Fiqh kama yeye mwenye kua na majibu ya haraka kwa haraka na mwenye Lugha fasaha na yenye kuvutia kama yake.'**

Imam Zayd Ibn Al Zayn Al Abidin alikua ndie Imam wa Kwanza kuandika kitabu cha Ilm ya Fiqh kiitwacho *Majmu al Kabir Al Fiqh* ambacho alikiandika kwa ajili ya kuwasomesha Wanazuoni wengine wakiwemo watoto wake a watoto wa kaka yake akiwemo Ima Jafar Al Sadiq.

Imam Zayd Ibn Zayn Al Abidiin baadae alihama kutoka katika Mji wa Madina na kuelekea katika mji wa Kufah na kua ni mwenye kuishi katika mji huo, ambapo baadae alifariki mnamo mwaka 122 Al Hijra baada ya mapigano ya vita dhidi ya majeshi ya Khalifa Hisham Ibn Abd Malik na alizikwa katika Mji wa Kufah huku kichwa chake kikiwa ni chenye kuzikwa kwenye ardhi ya Misri.

IMAM SHAQIQ AL BALKHI

Imam Shaqiq Al Balkhi alikua ni mfanyabiashara Tajiri sana wa Mji wa Balkhi nchini Afghanistan ambae alisoma kwa Imam Jafar As Sadiq, Imam Ibrahim Ibn Adham, Imam Abu Hanifa, Imam Abu Yusuf, Imam Al Zufah, Imam Malik Ibn Dinar, Rabiyah Al Adawwiyah na Wanazuoni wengine wa Hadith na hivyo Imam Shaqiq Al Balkh alikua ni Mtaalamu mkubwa sana wa Ilm ya Fiqh, Qur'an, Hadith na Tasawwuf.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Siku moja Imam Shaqiq Al Balkhi alimuuliza Imam Ibrahim Ibn Adham kuhusiana na namna anavyomtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kujitafutia Riziki zake ambapo Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: **'Mimi hua ni mwenye kumshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale nnapopata riziki yangu na nisipopata hua nnakua na Subra'**.

Ambapo Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: '**Hivyo ndivyo wanavyofanya Mbwa wa Balkhi**' na hivyo Imam Ibrahim Ibn Adham akamuuliza Imam Shaqiq Al Balkhi jee yeye anafikiriaje kuhusiana na *Tawakkul* ambapo nae akasema: '**Sisi hua ni wenye kuigawa tunapoipata riziki yetu na hua ni wenye kushukuru pale tunapokosa**'

Imam Shaqiq Al Balkhi alikua ni mwenye aliusia kwa kusema kua: **'Achana na hali ya Matamanio ya kupata, na kushikamana na sababu za kujipatia riziki na kujitayarisha na Akhera yako halafu mtegemee Mola wako.**'

Na akasema tena kua: '**Mahitajio ya Ibn Adam yote hua ni yenye kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie mmiliki wa kila kitu hivyo *Tawakkul* hua ni kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* kikamilifu'**

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema tena kua: **'Kama vile ambavyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* hawezi kukuhesabia kuhusiana na Sala za kesho ambazo hujazifanya basi na wewe hutakiwi kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na riziki ya kesho, kwani huenda ukawa si mwenye kufika kesho katika kuishi kwako.'**

Imam Shaqiq Al Balkhi alipoulizwa kuhusiana na Az Zuhd yaani kuachana na Ulimwengu alikua akisema kua: '**Al Zuhd ni kutoenda kinyume na mamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, kutotaka kua na Umaarufu, kukaa kimya, kula kidogo, na kujitenga na watu kua na umasikini.'**

Imam Shaqiq Al Balkhi alisema kuhusiana na kufanya Ibada kua: '**Kufanya Ibada hua kunajumuisha sehemu 10 ambapo 9 kati yao hupatikana na kujitenga na watu na 1 kati yao hupatikana na hali ya kukaa kimya'** na hivyo alikua akisema kua: **'Kua na Urafiki na watu kama vile unavyokua na urafiki na Moto utumie ule utakao kufaa na kisha ukimbie ule unaotaka kukudhuru.'**

Imam Shaqiq Al Balkhi alisema kua: **'Ilmu hua ina manufaa pale inapokua ni yenye kukupelekea kuupata ukaribu na Mola wako, hivyo wingi wa Ilm huweza kupatikana kutokana na namna mtu unavyousafisha Moyo wako kutokana na matamanio ya Kidunia'**

Na hivyo akasema kua: **‘Ibn Adam hawezi kua na fukara hadi pale atakapokua na khofu ya kuupoteza Utajri wake na pale atakapokua na khofu ya kuupoteza umasikini wake**.’

‘Hikma na Busara hua ni pale mtu anapokua anajua kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni mwenye juu ya kila kitu na hivyo hua ni mwenye uwezo kuchukua mali yake hio aliyokua nayo na kumpa mtu mwengine kabisa, hivyo mtu mwenye kujua juu ya hili hua ni mwenye kujua kua yeye si mwenye kua na kitu chochote, kwani ni *Allah Subhanah wa Ta’ala* ndie mmiliki wa kila kitu na ndie mwenye uwezo wa kutoa na kuhifadhi kila kitu.’

IMAM IBN SHABRAMA

Imam Abu Shabrama Abd Allah Ibn Shabrama Ibn Tufail Ibn Hassan Al-Dhabi alizaliwa na kuishi katika Mji wa Kufa ndani ya kipindi cha miaka 100 ya Al Hijra ambapo alisoma kwa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu,* Imam Abu Al Tufail Amir Ibn Wathila, Imam Abu Wael Shaqiq, Imam Amr Al-Sha’bi, Imam Abu Salamah Ibn Abdul Rahman, Imam Ubaid Allah Ibn Abd Allah Ibn Utbah, Imam Ibrahim Al Taimi, Imam Ibrahim Al Nakha’i, Imam Muhammad Ibn Sirrin, Imam Hasan Al Basr, Imam Salim Ibn Abd Allah, Imam Nafi’, Imam Salem Ibn Abi Al-Jaad, Imam Abd Allah Ibn Shaddad Ibn Al-Had, Imam Abu Zara’a, na wengineo.

Hivyo Imam Shabrama alikua ni *Al Allamah*, Mufti na ni Qadhi wa Mji wa Kufah, ambapo nae akasomesha kina Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Sufan Ibn Uyaynah, Imam Al-Hassan Ibn Saleh, Imam Abd Allah Ibn Al Mubarak, Imam Abd Al Wahed Ibn Ziyad, Imam Abd Al Warith Ibn Said, Imam Ahmed Ibn Bashir, Imam Wahib Ibn Khalid, Imam Shuaib Ibn Safwan, na Wanazuoni wengineo.

Ambapo Imam Ahamd Ibn Hanbal na Imam Abu Hatim Al Razi wanasema kua: ‘**Ibn Shabrama ni Thiqah, na ni Imam wa Usul na kuhusiana na Hadith basi hakua nazo nyingi alikua nazo kama 60 au 70.’**

Na anasema Imam Ahmad Ibn Abd Allah Al Ijli kua**: ‘Ibn Shabrama alikua ni Mcha Mungu, alieachana na Dunia, Mkarimu, Mwanamashairi mzuri na mwenye Hadith takriban 50 ’**

Ambapo anasema Al Harith Alku kua: **‘Amesema Hashim kua amesema Fudayl Ibn Ghazwan kua: ‘Sisi Ibn Shabrama, Al Harith Ibn Yazid Al Akli, Al Mughira na Al**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Al Qaqa Ibn Yazid tulikua tukikaa katika wakati wa Usiku tukisoma Fiqh na hatukua wenye kulala hadi tunaposikia Adhana ya Alfajir.''

Mbali ya kua ni mcha Mungu na ni mwenye kuachana na Dunia lakini Imam Abd Allah Ibn Shabramah alikua ni mtu mwenye Misimamo thabit kwani kwa upande wa Ibn Fudayl basi nae amesema kua: '**Amesema Ibn Shabrama kua: 'Kama Al Harith Al Akil akikaa pamoja nami na kisha tukaamua jambo basi hua hatujali kuhusiana na wale ambao hawatokubaliani nasi''**

Na Abd Al Warith akasema kua: **'Hakika mimi sijawahi kuona Mtu mwenye uwezo wa Kutoa Fatwa kwa haraka sana kama Ibn Shabrama'**

Imam Abd Allah Ibn Shabrama alikua ni Imam mnynyekevu kiasi ya kua anasema Muamamr kua: **'Nilimuona mimi Ibn Shabrama ambae alikua kama mtu akimwambia: 'Niko tayari kutolewa Kafara kwa ajili yako' basi hua ni mwenye kukasirika na kusema: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* akusamehe Dhambi zako''**

Anasema Imam Ibn Sammak kua: '**Amesema Ibn Shabrama kua: 'Yeyote yule atakaezama zaidi kwenye migogoro basi hua ni mwenye kufanya Dhambi, na yeyote yule asieingilia kutatua basi hua ni mpinzani, kwani ukweli hua hauwezi kutokukubaliana na yule ambae ni mwenye kujali juu ya jambo husika.''**

Kwa upande wa Imam Abd Allah Ibn Mubarak basi amesema kua: '**Amesema Ibn Shabarama kua: 'Hakika mimi nashangazwa na wale watu ambao hua ni wenye kuachana na aina Fulani ya vyakula kwa kuogopa aina fulani ya Maradhi, lakini hapo hapo hawaachani na kufanya dhambi kutokana na kuogopa Moto.''**

Anasema Yazid Ibn Harun kua: '**Mimi nilimuona Abd Allah Ibn Shabrama, alikua akiitwa Abu Shabrama, alikua ni Muarabu mwenye tabia nzuri, na alikua akivaa nguo nzuri, alikua ni mtungaji Mashairi ambapo yeye pamoja na Abd Rahman Ibn Abi Laila walikua wakimtembelea Isa Ibn Musa kila siku usiku, na walikua wakizungumza nae, walikua wakija basi hua wanabakia kwenye vipando vyao na hawaingii ndani hadi watakapoitwa.'**

Anasema Imam Abd Razzaq kua: '**Amesema Muammar kua: 'Ibn Shabrama alikuja kwetu kwa Gavana wa Yemen, ambapo baada ya Wanazuoni wa Shia kuondoka na watu wengine pia kuondoka na kubakia mimi nae basi akaniambia: 'Ewe Abu Urwa, Alhamd Lillah, hakika mimi sijabadilisha Kanzu yangu hii tangu niivae' kisha akakaa kimya kama kwa saa moja na kisha akasema: 'Mimi nakwambia lile ambalo ni ruhusa kulizungumza ama kuhusiana na lile la haram basi hakuna njia**

ya kulizingumzia wala kulifanya' Na Ibn Shabrama alikua ni Mwanafiqh mwenye kuaminika japo kua ni mwenye Hadithi kidogo sana'

Imam Abd Allah Ibn Shabrama alifariki mnamo mwaka 144 Al Hijra katika ardhi ya Kufah.

IMAM AL QARI HAMZA AL KUFI 80 AH

Imam Al Qari Hamza Ibn Habib Ibn Ammar Ibn Ismail Abu Ammara Al Kufi Al Tamimi alizaliwa mnamo mwaka 80 Al Hijra katika maeneo ya Kufah nchini Iraq ambae alisoma kwa Imam Sulayman Ibn Amash, Imam Humran Ibn Ayan, kwa Imam Abd Rahman Ibn Abi Layla na Imam Talha Al Masraf na hivyo bila ya shaka Imam Al Qari Hamza Al Kufi alikua ni Mtaalamu mahiri sana wa Ilm ya Qiraa.

Ambapo Imam Abu Hanifa alimwambia Imam Hamza Al Kufi: '**Katika mambo mawili wewe umefikia uwezo wa hali ya juu kabisa dhidi yetu ambayo sisi hatuna uwezo mkubwa nayo zaidi yako ambayo ni Qur'an na katika utekelezaji wa Majukumu yako ya Kidini**'

Ambapo Imam Sufyan Ath Thawry alisema kua: '**Hamza amefikia uwezo wa hali ya juu kabisa dhidi ya watu wengine katika Ilm ya Qiraa cha Qur'an na kutekeleza Majukumu ya kidini.**'

Ambapo Imam Al Amash alikua akimuona Imam Hamza Al Kufi basi alikua akisema kua: '**Huyu ni Mwenye Mamlaka kulingana na Qur'an**'

Tunapomzungumzia Imam Al Qari Hamza Al Kufi basi hua tunamzungumzia Imam ambae Imam Ibn Muin anasema kua ni : **'Imam anaetegemewa kwenye Ilm ya Hadith'** na pia Imam Imam An Nasai anamkubali pia, ambapo kwa upande wa Imam Al Ijli basi alikua anasema kua Imam Hamza alikua ni mwenye kuaminika na mtu ambae ni Mcha Mungu. Na Imam Ibn Saad basi yeye anasema kua: '**Imam Hamza alikua ni Mcha Mungu mwenye kuzijua Hadith, mwenye kuaminika na alikua ni mwenye kukusanya Hadith pia.'**

IMAM MUHAMAMD IBN IS-HAQ 80 AH

Imam Muhamamd Ibn Is-haq Ibn Yasar alizaliwa mnamo mwaka 80 Al Hijra katika mji wa Madinah. Babu yake Imam Muhamamd Ibn Is-haq alikua ni Mtumwa alieachiwa

huru na Qays Ibn Makhramah Ibn Abd Ul Muttalib na hivyo ni mwenye kujulikana kwa jina la Abu Baqr, na kuna wasemao kua alikua akijulikana kwa jina la Abu Abd Allah.

Imam Muhammad Ibn Ishaq alikua ni mwenye kusoma kwa Wanazuoni wakubwa wa Mji wa Madina ambao miongoni mwao ni Masahaba wakiwemo kina Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*, Imam Said Ibn Musayyib, Imam Said Ibn Maqbiri, Imam Abd Rahman Ibn Hurmuz, Imam Amr Ibn Shuayb, Imam At Taymi, Imam Jafar Al Baqir, Imam Az Zuhri, Imam Muhammad Ibn Al Munkadir n.k.

Mbali ya kua ni mwenye kusoma kwa Wanazuoni hao wa Mji wa Madina lakini pia Imam Muhamamd Ibn Is-haq alisafiri kwa ajili ya kutafuta Ilm katika maeneo ya Iraq, Kufa, Iran, Rayy, Baghdad na Misri na hivyo mbali ya kua ni mwenye kutafuta Ilm katika maeneo hayo lakini pia alikua ni mwenye kuacha Wanafunzi wengi pia katika maeneo hayo kutokana na Ilm aliyokua nayo hapo kabla.

Imam Muhammad Ibn Is-haq alikua ni Mwenye Ilm kubwa sana na alikua ni mwenye kuiandika Ilm hio, kwani anasema Imam Adh Dhahabi kua: '**Imam Muhammad Ibn Is-haq alikua ni mtu wa mwanzo kuiandika Ilm aliyokua nayo kwenye mji wa Madina na hii ilikua kabla ya Malik na Dhawayh, kwani Muhamamd Ibn Is-haq alikua ni mwenye Bahari ya Ilm ingawa alikua hana umakini sana.**'

Imam Az Zuhri anasema kua: **'Wakati Imam Muhamamd Ibn Is-haq yuko ndani ya Mji wa Madina basi ndani yake hua kuna Ilm kubwa sana.'**

Imam Muhammad Ibn Is-haq ni Imam ambae alikua ni Imam mwenye Ilm kubwa ya Maghazi pia yaani Mapigano ya Vita vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na alikua ni Imam wa Mwanzo kuandika kitabu cha Maghazi, ambapo alisema Imam Al Shafii kua: '**Yeyote yule anataka kujua kwa kina kuhusiana na Ilm ya Maghazi basi hana la kufanya isipokua kua ni mwenye kumtegemea sana Muhamamd Ibn Is-haq**'

Na Imam Ibn Addiy alisema kua: '**Kama Ibn Is-haq atakua hana jema zaidi ya ukweli wa kua aliwafanya Watawala kuelekeza mtizamo wao kwenye vitabu ambavyo hamna lolote la kujifunza ndani yake isipokua Mapigano ya Vita ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* namna alivyoanza matayarisho yake, na mwanzo wa kuumbwa kwa Ulimwengu basi hili litakua Jema tosha kwake kumfanya yeye kua mbele zaidi ya wengine.** '

Na Imam Adh Dhahabi alisema kua: **'Imam Muhammad Ibn Is-haq ni Mwanazuoni mkubwa sana wa Maghazi.'**

Ambapo Imam Shubah Ibn Al Hajjaj alisema kuhusiana nae kua: **‘Imam Muhammad Ibn Is-haq alikua ni Amir ul Muuminin wa Hadith.’**

Imam Abu Muawwiyah Ad Darir nae akasema kua: **‘Muhammad Ibn Is-haq alikua ni mwenye ufahamu bora zaidi, kiasi ya kua ilikua kama mtu anaeweka hadith kama 50 au zaidi, kwa Muhammad Ibn Is-haq na kumwambia kua: ‘Nihifadhie na kama nikizisahau basi utakua umezihifadhi kwa ajili yangu.’’**

Imam Sufyan Ath Thawry alisema : **‘Mimi nilikaa na Ibn Is-haq miaka 7 iliyopita na hakuna hata mtu mmoja wa Madina aliekua akimtuhmu kuhusiana na ovu lolote juu yake’**

Ali Ibn Abd Allah anasema kua: **‘Nimeangalia mimi katika vitabu vya Ibn Is-haq na sikuwahi kuona kitu chochote kile ambacho mimi nilikua nacho katika hifadhi yangu isipokua Hadith mbili tu, ambazo zinaweza kua ni sahih.’**

Imam Muhamamd Ibn Is-haq alifariki mnamo mwaka 151 Al Hijra.

IMAM SHU’BAH IBN HAJJAJ 80 AH

Imam Abu Bistami Shu’bah Ibn Hajjaj Ibn Al Ward Al Azdi Al Wasity Al Basr alikua ni mwanazuoni wa Hadith aliezaliwa mnamo mwaka 80 Al Hijra katika maeneo ya ardhi ya Irak katika mji wa Al Wasith ambao upo baina ya Mji wa Baghdad na Basra.

Imam Shu’bah alisoma Ilm ya Hadith kwa wengi sana akiwemo Imam Hasan Al Basr, Imam Muhamamd Ibn Srin, Imam Qatadah Ibn Diamah, Imam Ayyub As Sikhtiyani, Imam Abu Is-haq na wengineo wafikao 400, ambapo Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Malik, Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Muhamamd Ibn Jafar ambae alimsomesha kwa mda wa miaka 20 na Imam Abd Rahman Ibn Mahdi, na pia ndani yake wamo Walimu wake waliomfundisha basi nae pia amewasomesha baadae kama Imam Al Amash, Imam Ayub Al Sakhtiyani, Imam Said Ibn Ibrahim, nk.

Ingawa Imam Shu’bah alikua ni masikini lakini umasikini wake haukumzuia kutafuta Ilm ya Hadith kwani ilifikia wakati ilimbidi kuuza Mirathi yake aliyorithi kwa mama yake kwa ajili ya kupata matumizi ya kujitafutia Ilm ya Dini yake na alifikia kua tayari kuuza Nguzo za Nyumba yake kwa ajili ya Ilm ya Dini.

Ambapo anasema Imam Abu Qathan kua: ‘**Hakika mimi sijawahi kumuona mtu ambae mwenye kufanya Ibada sana kama Shu’bah. Kwani alikua akirukuu kiasi**

ya kua nilikua nikidhania kua amejisahau na alikua hakai baina ya Sijda mbili isipokua nilikua nikidhani kua amejisahau pia.'

Imam Shu'bah alikua ni mtu mwenye kupenda sana kufanya Ibada na hivyo alikua akifunga kila baada ya siku, na kua ni mwenye kukesha katika *Qiyam Al Layl* na hivyo mwili wake ulikua mwembemba na uliokauka kama anavyosema Imam Abu Baqr Al Bakrawiy kua: **'Sijawahi kumuona Mtu akimuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama vile alivyokua akiabudu Shu'bah kwani alikua akimuabudu hadi kufikia kukauka kwa ngozi inayozunguka mifupa yake, hadi inakua hakuna nyama kwenye mifupa yake.'**

Imam Shu'bah alikua ni Mcha Mungu na mwenye kupenda kusaidia wenye matatizo yao kwani anasema Imam At Tayalisy amesema kua: '**Sisi tulikua tukikaa pembeni ya Shu'bah, mara akaja Sulayman Ibn Mughirah aliekua akilia, na hivyo Shu'bah akamuuliza: 'Unalia nini?' Sulayman akajibu: 'Ewe Abu Said Punda wangu amefariki Ijumaa hii na hivyo sina la kufanya'**

Ambapo Imam Shu'bah akauliza: 'Jee ulimnunua kwa bei gani?' Sulayman Ibn Mughirah akasema: 'Kwa Dinar 3 Imam Shu'bah akasema: 'Mimi nnazo Dinar 3 chukua kwa ajili ya Allah' kisha Imam Shu'bah akamwambia Mtoto wake: 'Hebu lete huo mfuko hapo' na ulipoletwa mfuko huo, ndani yake mkawa mna Dinar 3 akazitoa na kumpa Sulayman Ibn Mughirah huku akimwambia: 'Basi usilie tena chukua hizi Dinar 3 kanunue Punda mwengine.''

Imam Shu'bah alikua ni mwenye kusema: '**Kama mimi ningekua na Unga na Utumbo, basi sijali kuhusiana na amambo mengine yatakayonipita ya Kidunia.**'

Amesema Imam Abu Abdillahi Al Hakim kua: '**Shu'bah alikua ni Imam wa Maimamu katika Mji wa Basra katika fani ya Ilm ya Hadith, alikutana na Anas Ibn Malik na Amr Ibn Salamah *Radhi Allahu Anhum* na Ilm yake inatokana na Wanazuoni 400 wa Tabiina ambao alisoma kwao**.'

Na kwa upande wa Imam Muhammad Idris Al Shafii basi yeye amesema kua: **'Kama sio Shu'bah basi Ilm ya Hadith isingejulikana nchini Iraq.**'

Imam Abu Daud At Tayalisi anasema kua: **'Mimi nimesoma Hadithi 7000 na Kauli za Wanazuoni kutoka kwa Shu'bah**'

Imam Sufyan Ath Thawry anasema kua: '**Shu'bah ni *Amir ul Muuminina wa Hadith***'

Imam Shu'bah Al Hajjaj alikua ni mtu ambae alikua ni mwenye kufuatilia ipasavyo kuhusiana na Wanazuoni wa Ilm ya Hadith na ni mwenye umakini mkubwa sana, kwani

alikua akiwafuatalia mtu mmoja mmoja aliekuwemo kwenye Sanad ya Hadith aliyoisikia, safari moja alisikia kua kuna Hadith ambayo imepitia kwa Abd Allah Ibn Athain ambae yuko katika Mji wa Makkah. Hivyo Imam Shu'bah akafunga safari kutoka Iraq na akaelekea katika Mji wa Makkah na alipofika katika Mji wa Makkah kwa Abd Allah basi akaambiwa kua yeye ameipata kwa Saad Ibn Ibrahim ambae yuko katika Mji wa Madina.

Hivyo Imam Shu'bah akafunga safari hadi katika Mji wa Madina kwa Saad Ibn Ibrahim na alipofika kwake basi akaambiwa kua hadithi hiuo imepatikana kwa Ziyad Ibn Mikhraaq ambae anaishi katika mji wa Basra tena katika maeneo anayoishi yeye mwenyewe Imam Shu'bah. Na hivyo Imam Shu'bah akafunga safari na kurudi Iraq katika Mji wa Basra kwa Ziyad Ibn Mikhrak na alipofika akaambiwa kua Hadithi hio imepatikana kwa Shahr Ibn Hawsayb ambae hata hivyo Hadith zake ni dhaifu.

Hivyo Imam Shu'bah akasema: **'Kama hadithi hii ingekua ni Sahih basi mimi ningekua naipenda zaidi kuliko hata familia yangu, na mali zangu na watu wote.'**

Katika kuthibitisha jitihada zake Imam Shu'bah basi alisema Imam Wakii Ibn Jarah kua: '**Mimi nna matumaini ya kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* atainyanyua Darja ya Shu'bah juu Mbinguni kwa sababu ya jitihada zake za kumpigania kwa kumlinda *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*'**

Na anasema Qurad Abu Nuh kua: '**Siku moja Shu'bah aliniona mimi nikiwa nimevaa Shati ambalo aliniuliza: 'Umenunua bei gani Shati hili?' nami nikajibu : 'Dirham 8' Shu'bah akasema: 'Ole wako, hivi wewe humuogopi *Allah Subhanah wa Ta'ala*? Kwanini hununui nguo za Dirham 4? Na kisha Dirham 4 ukazitolea sadaqa? Kufanya hivyo ingekua ni bora zaidi kwako.'**

Safari moja Shu'bah aliambiwa kua: '**Sufyan anapingana na wewe kuhusiana mtizamo wako juu ya hili'** ambapo nae akasema: **'Shukran umenisaidia kutoutilia maanani mtizamo wangu.'**

Siku moja Imam Shu'bah alikua amekaa anawasomesha Wanafunzi wake Hadith mara akatokea Masikini aliekua anaomba, hivyo Imam Shu'bah akawaambia Wanafunzi wake kua: **'Mpeni Sadaqa Masikini kwani mimi nimesikia kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Jitengeni na Moto kwa Sadaqa hata kama kwa kutoa nusu ya kokwa ya Tende''**

Lakini hata hivyo Wanafunzi wake wakakaa kimya hakuna hata mmoja alietoa Sadaka, hivyo Imam Shu'bah akairudia kauli yae hio mara 3, lakini hata hivyo Wanafunzi hao hawakutoa kitu chochote hivyo Imam Shu'bah akawaambia: '**Ondokeni Wallahi mimi sitokufundisheni Hadith kwa muda wa miezi mitatu.'** Kisha Imam Shu'bah

akaondoka na kuenda Nyumbani kwake na kuchukua Unga uliokua umeshakandwa na kumpa Masikini huyo.

Imam Shu'bah alikua nimiongoni mwa Maimamu ambao waliokua wakiandika vitabu lakini alipokaribia kufariki basi alimuamrisha Mfanyakazi wake kua avitie Maji Vitabu hivyo ili wino wake uyayuke.

Imam Shu'bah alifariki katika mwezi wa Rajab mnamo mwaka 160 Al Hijra.

IMAM JAFAR AS SIDDIQ 80 AH

Imam Jafar As Sadiq ambae jina lake halisi ni Jafar Ibn Muhammad Ibn Ali Zain ul Abidin Ibn Al Husein Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu A'nhu*. Alizaliwa Madinah kati ya mwaka 80 na 83 *Al Hijr*. Alikua ametokea moja kwa moja katika ukoo wa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* kupitia kwa Fatma bint *Rasul Allahi Salallahu A'layhi wa Salam* na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu A'nhu*, na mama yake alikua ni Farwah bint Al Qassim Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr *Radhi Allahu A'nhu*.

Hivyo Imam Jafar alikua na sifa za kipekee unapozungumzia Maimamu wenye *I'lm*, kwani baba yake alikua ni Mwanazuoni mkubwa katika mji wa Madinah, na mababu zake wote wawili wa upande wa baba na mama pia walikua ni Wanazuoni wakubwa. Kama Al Qasim alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni saba wanaotajika Madinah katika kizazi cha *Tabi'in*.

Wakati huo Madinah ilikua ndio kitovu cha *I'lm*, ndio sehemu ambayo Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* alipoishi na Masahaba wengi pia walikua wakiishi kuliko sehemu nyengine. Jafar As Sadiq alikua na wingi wa *I'lm* ambao unaonekana pale unapoangalia majina ya Wanafunzi wake aliowasomesha ambao wote ni Wanazuoni wakubwa wakubwa, ingawa wengine walikua na umri kama wake, wengine wadogo yake lakini pia walikuwapo ambao walimzidi umri, kati ya Wanafunzi aliowasomesha ni pamoja na Imam Abu Hanifa, Imam Malik, Sufyan Ath Thawri, Yahya Ibn Said, Abdul Malik Ibn Jurayj, Sufyan Ibn Uyaynah, Muhammad Ibn Ishaq, Shubah Ibn Al Hajjaj na wengineo wengi.

Hivyo Maimamu wa *Madhhab* yote ya kiislam wanakubali kua Imam Jafar As Sadiq ni mmoja kati ya Maimamu wakubwa wa Kiislamu na pia ni Mwalimu wa Maimamu wakubwa na alikua hayuko katika upande wowote ule isipokua wa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* na Masahaba zake.

Imam Jafar aliitwa As Sadiq kwa sababu alikua muaminifu katika kila kitu katika maisha yake ikiwemo kutafuta na kutoa *I'lm* ya dini na katika kukaa mbali na matamanio ya dunia. Imam Jafar Sadiq alikua akisomesha katika Msikiti wa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* uliopo Madinah kama vile alivyokua akisomesha baba yake pia.

Anasema Imam Malik '**Nilikua nikihudhuria darsa la Jafar Ibn Muhammad aliekua kila wakati anatabasamu, lakini pale anapotajwa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* hua ni mtu asie na maskhara, kuna kipindi nilikua nikimtembelea sana na sikuwahi kumkuta akiwa hasali, au kama hasali basi hua anasoma *Qur'an*, na karibu mara zote hua yupo katika saumu, alikua hasomi wala hasomeshi *Hadith* yeyote ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ila kwanza hutia udhu'**.

Imam Jafar As Sadiq alikua ni mcha mungu mkubwa, alikua hamna anaemuogopa isipokua Allah, hamuogopi mtu yeyote hata kiongozi awe mkatili kiasi gani. Alikua na ujasiri ambao ulitokana katika damu ya *Sayyidna* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu A'nhu* lakini pia alikua mkarimu sana kwa watu kiasi kwamba hata kama mtu akimkosea basi humsamehe na kumuombea dua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* amsamehe.

Siku moja Sufyan Ath Thawry alimuomba Imam Jafar As Sadiq amfundishe moja katika vitu vyenye manufaa. Imam Jafar As Sadiq akamwambia **'Sufyan ukiwa una neema ambayo unaipenda na ungelipenda kufaidika nayo kwa mda mrefu, basi mshukuru na umtukuze Allah kwa neema hiyo, kwani Allah *Subhanahu wa Ta'ala* anasema:**

﴿لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ﴾

La-in shakartum laazeedannakum. (*Surat Ibrahim 14:7*)

Tafsir: '***Mtakaponishukuru nitakuongezeeni zaid'***

Na ukiona rizki zako zinakuja kidogo kidogo basi fanya kuongeza *Istighfar* kila mara kwani Allah *Subhanahu wa Ta'ala* anasema:

﴿ٱسْتَغْفِرُوا۟ رَبَّكُمْ إِنَّهُۥ كَانَ غَفَّاراً ۝ يُرْسِلِ ٱلسَّمَآءَ عَلَيْكُم مِّدْرَاراً ۝ وَيُمْدِدْكُم بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ وَيَجْعَل لَّكُمْ جَنَّاتٍ وَيَجْعَل لَّكُمْ أَنْهَاراً﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Istaghfiroo rabbakum innahu kana ghaffaran; Yursili alssamaa AAalaykum midraran; Wayumdidkum bi-amwalin wabaneena wayajAAal lakum jannatin wayajAAal lakum anharan (*Surat Nuh 71:10-12)*

Tafsir: ***Muombe Mola wako akusamehe dhambi zako, Hakika yeye ni mwingi wa kusamehe, Atakuleteeni mvua kutoka mawinguni, na atakuzidishieni katika mali na watoto, na atakupeni bustani na mito.***

'Sufyan ukiwa na tatizo linalokuzidi uwezo wako basi sema:

لا حَوْلَ وَلا قُوَّةَ إِلا بِاللهِ

La hawla wala quwwata ila billah **(Hakuna nguvu wala uwezo isipokua kwa Allah) huo ndio ufunguo wa kuondoa matatizo yako na kufungua mali za mbinguni'.**

Sufyan akajibu **'Hakika leo umenifundisha** ***I'lm*** **kubwa sana',** Jafar As Sadiq akasema**, 'Sufyan ameyafahamu na** ***Allah Inshaa Allah*** **atamnufaisha na atamsaidia'.**

Imam Jafar As Sadiq alisema **'Ikiwa kuna mtu yeyote miongoni mwa wana** ***Fiqh*** **ambae anaweza kuilinda** ***Nafsi*** **yake, kuilinda dini yake, kuyazuia matamanio yake na kua mtiifu kwa Mola wake, basi watu wanatakiwa wamfuate (Wafanye** ***Taqlid*** **kwa mtu huyo).**'

Siku moja Imam Abu Hanifa aliulizwa '**Jee ni Mwanafiqh gani mwenye** ***I'lm*** **zaid kati ya uliowahi kukutana nao?**' Imam Abu Hanifa akasema '**Sikuwahi kuona Mwanafiqh mkubwa kuliko Jafar Ibn Muhammad (***Al Sadiq***)**'

Anasema Imam Abu Hanifa: '**Siku moja** ***Khalifah*** **Mansour, alimwita Jafar bin Muhammad, na kisha akaniambia kua watu wanavutiwa nae sana. Akaniomba nitayarishe maswali magumu kabisa ya Ki*fiqh*. Nikachagua maswali 40 magumu kabisa nnayoyajua. Nilipoingia kwenye ukumbi, nikamuona Jafar amekaaa upande wa kulia. Heshima na ukubwa wake ulinivaa na hapo sikuona ukubwa wa cheo wa** ***Khalifah*** **alie mbele yangu. Nikasalimiana nao kisha nikaa mbele yao.**

Khalifah **Mansour akamtambulisha Jafar Ibn Muhammad kisha akamuuliza: 'Jee unamjua?' Jafar Ibn Muhammad akajibu 'Naam'.** ***Khalifah*** **Mansour akanigeukia mie na kuniambia: Haya uliza maswali yako. Nikaanza kuuliza maswali. Katika kila swali nililouliza, Imam Sadiq alizungumzia mtazamo wa watu wa Madinah**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

na mtizamo wa watu wetu wa Iraq, kisha akatoa mtazamo wake yeye. Baadhi ya wakati mtizamo wake unafanana na wetu, na wakati mwengine unafanana na watu wa Madinah na pia wakati mwengine hakubaliani na mitazamo yote. Nikamaliza maswali yangu na kusema yule anaejua yote kuhusu tofauti za Wanazuoni katika mambo ya *Fiqh* ndio mwenye *I'lm* zaid baina yetu.'

Imam Jafar Sadiq amenukuliwa katika vitabu vingi vya Historia vya Maimamu wakiwemo Imam Al Tabari, Al Yaqubi, Al Masudi, Al Dhahabi na Al Numan. Imam Al Shafi'i, An Nasai, Ibn Hiban wanasema kua Imam Jafar Sadiq ni *Thiqa* (*Hadith* zake ni Sahih).

Ibn Shiham akasema '**Watu watukufu wawili wamedhuriwa kwa sababu ya watu wabaya: Jafar Ibn Muhammad na Ahmad Ibn Hanbal**'. Vile vile Ibn Salah alisema '**Maimamu wawili wamedhuriwa kwa sababu ya wafuasi wao ingawa wao hawana makosa, Maimamu hao ni: Ahmad Ibn Hanbal na Jafar al Sadiq**'.

Salim bin Abi Hafsa alisema: '**Nilimuuliza Abu Jafar na mtoto wake Jafar kuhusu Abu Bakr na Umar, nae akajibu: Ya Salim, kua marafiki wao na jitenge na maadui zao kwani wao ni Maimamu waongofu.**

Kisha Jafar akasema**: Ya Salim! Jee ni nani anaemtukana babu yake? Abubakr ni babu yangu. Nisipate Shifaa ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* siku ya Kiama ikiwa siwapendi na sijitengi na maadui zao.**'

Imam Jafar As Sadiq alifariki tarehe 25 Shawal 148 *Al Hijr*, miaka miwili kabla kufariki Imam Abu Hanifa na pia miaka miwili kabla kuzaliwa Imam Al Shafi'i. Imam Jafar As Sadiq alinukuu takriban *Hadith* 2000 ambazo zote hizo hupatikana katika vitabu tisa vya *Hadith* vya Sunni, na *Hadith* 110 miongoni mwao zinapatikana katika *Sihah al Sita* (Vitabu sita vikubwa vya *Hadith*), kwani kwa wafuasi wa Ahlu *Sunnah* wal Jamaah, Imam Jafar As Sadiq alikua akijulikana kama *Shaykh al Ulama* na pia ni *Imam Al Fuqaha.*

Imam Jafar As Sadiq hakuwahi kuwacha kumbukumbu yeyote ya maandishi. Lakini Mwanafunzi wa Imam Jafar Sadiq anaeitwa Hishan bin al-Hakam, aliandika kitabu kinachoitwa *Kitab-ul-Alfaz Wa Mabahithiha* ingawa haijulikani katika kitabu hiki alizungumzia nini. Vitabu vya *Fiqh* ya Imam Jafar Sadiq viliandikwa katika miaka ya baadae na Ja'far Ibn Husain Al Qummi, Yunis Ibn Abdur Rahman, Ahmad Ibn Muhammad Ibn Khalid al-Barqi, Muhammad Ibn Muhammad Ibn An Nu'man (*Al-Mufid*), Muhammad Ibn Abdur Rahman Ibn Qibbah Ar Razi, Muhammad Ibn Yaqub Al Kulayni, Ibn Babawayh, Nasir Din Al Tusi n.k.

IMAM ABU HANIFA 80 AH

Thabit Ibn Zuta alikua ni kijana mwenye Imani kubwa sana ya dini ya Kiislam. Siku moja alipokua akitembea karibu na mto, mara mda wa Sala ukaingia na hivyo ikambidi ayasogelee maji ya mto huo ili atie udhu kwa ajili ya kumuabudu Mola wake, wakati alipoanza kutia udhu, akaliona Tufaa (*Tufaha au Apple*) linaelea juu ya maji ya mto huo yenye mwendo wa taratibu kuelekea kusiko julikana, Tufaa lile lilielea hadi karibu yake hivyo akalichukua na kulisogeza mdomoni mwake.

Ghafla mara tu baada ya meno yake kuzama ndani ya nyama ya Tufaa hilo, zikamjia hisia za kua na makosa katika ufahamu wake, na kuanza kujiuliza inakuaje nnataka kutia ndani ya tumbo langu kile ambacho kisicho halali yangu? Hivyo, bila ya kulitupa Tufaa lile akageuka na kuanza kufuata yanakotokea maji ya mto ule, kwa kua na mtizamo wa kua huenda akaona lilikotokea Tufaa lile na hivyo kuweza kumjua mmiliki wa Tufaa hilo ili kuomba msamaha na pia kupata ridhaa yake.

Baada ya muda si mrefu akakutana na Mtufaa ambao sehemu ya matawi yake yananing'inia kwa juu ya sehemu ya mto ule, akaona inawezekana ikawa lile Tufaa limetokana na Mtufaa huo, hivyo akajaribu kuangaza huku na kule kuona kama atakuwepo mtu ambae anamjua mmilikia wa Mtufaa huo, kwa bahati nzuri akamuona mkulima anapalilia sehemu ya ardhi ya shamba lililoota Mtufaa huo ndani yake. Akamkaribia na kumsalimia na kisha akamuuliza kama anamjua mmiliki wa Mtufaa ule, na kumpa sababu ya yeye kumtafuta kwake.

Mkulima yule akajitambulisha kua yeye ndie mmilikia wa Shamba hilo, baada ya kuvutiwa kutokana na uaminifu wa Thabit akajitambulisha kua jina lake ni Salih, na kisha akamjaribu Thabit kama kweli alikua na nia ya kuomba msamaha kwa sababu ya kumuogopa Mola wake, baada ya Salih kuhakikisha kua kweli Thabit alikua ni miongoni mwa vijana wanaomcha Allah *Subhanahu wa Ta'ala*, akamshawishi Thabit na kumtaka awe msaidizi wa kumsaidia kazi katika shamba lake, na baada ya kukubali Thabit akafanya kazi kwa Salih kwa muda.

Baada ya muda kupita Salih akapendekeza kua itakua vyema kama Thabit atakubali kumuoa mtoto wake wa kike aliekua akiitwa Abidat ul Azhar, hivyo wakakubaliana na kutayarihsa harusi hiyo, baada ya kuoana Thabit na Abidat ul Azhar wakajaaliwa kupata watoto wanne ambapo mmoja miongoni mwao alikua akiitwa Nu'man.

Nu'man Ibn Thabit ambae pia alikua akijulikana kwa jina la Abu Hanifa alizaliwa katika mwaka 80 *Al Hijr* wakati ambao Thabit Ibn Zuta akiwa na umri wa miaka 40. Abu Hanifa alikulia katika mazingira yaliyojaa Iman kubwa sana ya dini sana hivyo

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

alihifadhi *Qur'an* akiwa na umri mdogo na aliamua kujifunza *Hadith*i za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ili aweze kuendesha biashara zake katika njia sahih na halali kama isemavyo dini ya kiislamu, biashara ambazo zilitokana na asili ya kazi ya wazee wake.

Abu Hanifa alijaaliwa kua na kumbukumbu na ufahamu mzuri sana, alikua akipenda sana kuingia katika midahalo kitu ambacho kilimpa msingi mzuri katika kutafuta kwake *I'lm* ya dini. Siku moja Amir Al Shaabi alimwambia Abu Hanifa **'Bora ungejishughulisha na *I'lm* ya dini kwa kusoma kutoka kwa Wanazuoni waliokuwepo, kwani unaonekana una akili na ufahamu mzuri'.**

Abu Hanifa aliamua kuyafanyia kazi maneno hayo kwa kuanza kusoma kwa undani njia za *Fiqh* za Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A'nhu* inayoangalia manufaa ya jamii zaid, *Fiqh* ya Ali Ibn Abu Talib *Radhi Allahu A'nhu* yenye msingi wa kuchuja na ufahamu zaid wa *Sharia'h* za kiislam, *Fiqh* ya A'bd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu A'nhu* yenye msingi wa mantiki na *Fiqh* ya Abd Allah Ibn 'Abbas *Radhi Allahu A'nhu* kupitia katika *Qur'an*. Abu Hanifa alisoma kwa Walimu tofauti wa wakati huo miongoni mwao akiwemo Hammad Ibn Abu Sulaiman Mwanafunzi mkubwa wa Amir Al Shaabi na Ibrahim An Nakhai'i.

Abu Hanifa alikua mrefu, mpana, mwenye macho makubwa na ndevu nyingi hadi kifuani lakini sharubu ndogo, Imam Abu Hanifa alikua akiongeza *I'lm* yake kila alipokua akienda kuhiji Makkah na Madinah, kwani huko alikua akipata *I'lm* kutoka kwa Walimu wa sehemu tofauti wakiwemo Imam Jafar As Sadiq ambae alikua nae sawa kiumri na pia Imam Malik ambae alikua mdogo kuliko Imam Abu Hanifa kwa miaka kumi na tatu.

Mwalimu wake Hammad Ibn Abu Sulaiman alifariki mwaka 120 *Al Hijr*, hivyo Abu Hanifa akarithi nafasi yake ya kutoa *I'lm* badala yake. Hapo ndipo alipoanza kupata umaarufu wa *I'lm* yake akiwa na uwezo mkubwa wa kupambanua mambo ya dini huku akiendelea na biashara zake za nguo katika misingi ya kiislamu pia na kuendelea kutafuta *I'lm* ya *Fiqh* na *Hadith* kwani alikua akisema **'Yeyote yule anaejifunza *Hadith* bila kujifunza *Fiqh* hua ni sawa na mfamasia anaejua dawa aina zote lakini hajui jinsi ya kuzitumia hadi pale atakapokuja daktari na kumfahamisha, hivyo hivyo Mwanafunzi wa *Hadith* humbidi kumsubiri Mwalimu wa *Fiqh*.'**

Abu Hanifa alikua akiwapenda sana Wanafunzi wake kama vile ambavyo baba awapendavyo watoto wake, alikua akiwasaidia katika kutafuta *I'lm* na pia katika kuendeleza maisha yao, kama ikitokea Mwanafunzi wake anataka kuoa na hana uwezo wa kifedha kusimamia harusi yake basi Abu Hanifa husimamia kila kitu, hivyo Wanafunzi wake walikua wakimpenda pia. Moja katika njia zake za kusomesha ilikua ni kuwatengenezea tatizo na njia zinazotakiwa kufuatwa ili kutatua tatizo hilo, halafu

kukaa nao kulijadili tatizo hilo ambapo kila mmoja baina yao huchangia jinsi ya kulipatia ufumbuzi tatizo hilo kwa jinsi anavyojua hadi pale watakapopata ufumbuzi wote kwa pamoja.

Imam Abu Hanifa alikua ni mtu mwenye mawazo huru, alikua hakubaliani na kitu, hatoi Fatwa au kutatua tatizo bila kulifikiria kwa umakini kupitia njia na kanuni zote zinazohitajika katika kitu hicho. Abu Yusuf alisema: '**Imam Abu Hanifa alikua na umbo zuri na muonekano mzuri, alikua na kauli nzuri na sauti ya kuvutia na alikua muwazi katika kuelezea hisia zake**'.

Na mtoto wa Imam Abu Hanifa aitwae Hamad Ibn Abi Hanifa alisema: '**Baba yangu alikua ana sura ya kuvutia, ananukia mafuta mazuri kila wakati, mrefu, hasemi isipokua kujibu kile alichoulizwa na alikua haingilii kile kisichomhusu**'

Imam Abu Hanifa alikua ni mwenye subira na ustahamilivu, alikua hapokei pesa wala zawadi kutoka kwa viongozi au watawala, katika jambo hili alikua sawasawa na Imam Ahmad Ibn Hanbal ambae alikua akiishi kwa kujitegemea mwenyewe japo kwa umasikini, tofauti na Imam Malik ambae alikua akichukua malipo kutoka kwa watawala kama mshahara wake ambayo alikua akiyatumia kuwasaidia Wanafunzi wake na Imam Al Shafi'i ambae alikua akipata malipo aliyokua akilipwa na *Khalifah* wa wakati huo kwa sababu ya kutoka katika kizazi cha ukoo wa *Quraysh* na kua na ujamaa na Mtume Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*.

Katika biashara zake Imam Abu Hanifa alikua ni mfano wa kuigwa kwa uaminifu, kwa huruma na kufanya bishara kiuadilifu. Wanaomjua wanasema alikua kama Sayyidna Abu Bakr katika kuendesha biashara zake. Siku moja mwanamke mmoja alikua anauza kitambaa cha sufi kwa dirham 100, lakini Abu Hanifa alikataa kukichukua kwa sababu bei yake ilikua chini sana, na kumwambia yule mwanamke kua kitambaa hicho thamani yake ni kubwa zaid, hivyo bora aongeze bei, yule mwanamke akapandisha, Abu Hanifa akamwambia bado, akapandisha hadi ikafikia dirham 400, Abu Hanifa akamwambia bado si bei yake, yule mwanamke akakasirika, Abu Hanifa akamwambia amwite mtu mwengine anaeuza vitambaa amuulize bei yake, alipoitwa yule muuzaji mwengine akasema kitambaa kile kina thamani ya dirham 500, na hapo Abu Hanifa akakinunua kwa bei hiyo.

Imam Abu Hanifa aliishi wakati wa utawala wa Ummayad, lakini alijua kua utawala huo hauna haki ya kutawala. Gavana wa utawala wa Umayyad aliekua akitawala Kufah wakati huo alikua akiitwa Ibn Hubairah, alikua akitaka Abu Hanifa awe pamoja nae, hivyo akataka kumpa muhuri wa Gavana ili ikitokea kesi Abu Hanifa atie muhuri na hukmu ya kesi hiyo ipitishwe, lakini Abu Hanifa alikataa na kusema **'Hata kama akiniambia nimuhisabie milango ya msikiti mkuu tu basi sitomhisabia, itakuaje**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ikitokea nipige muhuri wa kesi ya mtu anaehukumiwa kukatwa kichwa? Sitofanya kazi yake hata siku moja'.

Ibn Hubairah alijaribu kuwatumia watu wengine wazungumze na Abu Hanifa lakini Abu Hanifa aligoma, hivyo ikabidi awekwe ndani kwa kukataa kutii amri ya Gavana. Abu Hanifa aliwekwa ndani lakini baadae Ibn Hubairah akaona jambo hilo litaleta sura mbaya zaid kwa utawala wake, hivyo akamtoa jela na kumuachia huru. Baada ya kuachiwa huru Abu Hanifa alihama Kufah na kuhamia Makkah pamoja na familia yake yote mwaka 130 *Al Hijr*.

Ulipotawala utawala wa Al Abbas, Abu Hanifa alikua na uhusiano mzuri na watawala wake, lakini ghafla watu wa Mosul wakamuasi *Khalifah* Al Mansour. Na waasi kukamatwa na kuwekwa ndani, hapo Al Mansour akawaita Wanazuoni kuwauliza awafanye nini wale waasi na kutaka kujua Jee inaweza kutumika Adhabu kifo kama alivyosema Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*?

Kila mmoja akatoa rai yake ilipofika zamu ya Abu Hanifa akasema **'Wameomba kile kisichokua chao, na we wewe pia umewafikisha katika hali ambayo hukutakiwa kuwafikisha. Adhabu ya kifo haiwezi kutekelezwa juu ya Waislam isipokua kwa kesi za aina tatu tu, ambazo ni: Damu kwa damu (alieua auliwe), mzinifu alieoa au kuolewa na alieiacha dini yake na kujitenga na Ummah. Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ameruhusu adhabu hiyo kwa mambo hayo, hali ambayo wewe unatakiwa uiheshimu, ukifanya unavyotaka wewe, utakua unawaua watu hawa bila ya kuwafanyia haki'.**

Baada ya kusikia haya, Al Mansour aliwatoa Wanazuoni wote na kumbakisha Abu Hanifa na kumwambia **'Abu Hanifa umesema kweli nenda zako nyumbani lakini mara nyengine usitoe mbele ya watu Fatwa ambazo zitamtenga *Khalifah* wako kwani unaweza ukawapa nguvu waasi'**

Siku moja *Khalifah* Mansour na mkewe anaeitwa Hurran Khatun waligombana pale *Khalifah* Mansour alipotaka kuongeza mke mwengine, hivyo Hurra Khatun akataka ugomvi huo uje kutatuliwa na Imam Abu Hanifa, *Khalifah* Mansour akamwita Imam Abu Hanifa na kuanza kujadiliana nae huku Hurran Khatun akiwa amekaa baina ya pazia lililozuia kuonekana kwake huku akiwasikiliza, *Khalifah* Mansour akamuuliza Imam Abu Hanifa '**Jee Mwanamme wa Kiislam anaruhusiwa kuoa wake wangapi kwa wakati mmoja**?'.

Imam Abu Hanifa akajibu '**Wanne**'.

Khalifah Mansour akamwambia Hurra Khatun '**Jee umesikia alivyosema Imam?**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Hapo Imam Abu Hanifa akaingilia kati na kusema '**Lakini ruhusa hii hutokana na sharti la kua, mwanamme huyo anao uwezo wa kutekeleza haki zote kwa usawa miongoni mwa wake zake hao**, jibu ambalo lilikuwa limepingana na hoja ya *Khalifah* Mansour alipokua akibishana na Hurran Khatun.

Imam Abu Hanifa akaondoka na kurudi kwake, alipofika nyumbani akakutana na mfanyakazi wa Hurran Khatun akiwa na zawadi na barua ya kumshukuru Imam Abu Hanifa, hapo Imam Abu Hanifa akamrudisha yule mfanyakazi na umwambia akamwambie Hurran Khatun kua ni wajib wa Imam Abu Hanifa kusema ukweli bila ya woga wala kupendelea.

Imam Abu Hanifa alikua Mwanazuoni mkubwa katika historia ya *Fiqh* na katika historia ya maisha ya Uislam. Anasema Imam Al Shafi'i **'Katika *Fiqh* watu wote wanamtegemea Imam Abu Hanifa'**, na Ibn Mubarak anasema **'Imam Abu Hanifa ni shina la *I'lm*'** nae Imam Malik anasema **'Abu Hanifa ni Mwanazuoni wa kweli wa *Fiqh*'.**

Katika kuweka wazi njia alizokua akitumia katika masuala ya *Fiqh*, Imam Abu Hanifa alikua akisema '**Hua nnategemea kitabu cha Allah, na nisipopata jawabu ndani yake hua nnangalia *Hadith* za Mtume wake, na ninapokosa humo hua nnachukua walivyosema Masahaba wa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, siwachi kile walichokisema au walichokifanya kwa kuchukua kutoka kwa watu wengine kama Al-Ashabi au Hasan Al Basr, kwani wao ni kama mimi hivyo ni bora kufanya *Ijtihad* yangu mwenyewe**'.

Imam Sufyan Ibn Uyayna anasema, Imam Abu Hanifa na Imam Awzai walikutana katika Mji wa Makkah, Imam Awzai akamwambia Imam Abu Hanifa '**Ya Abu Hanifa kwa nini katika Sala hamnyanyui mikono mnapotaka kurukuu [*raf al yadain*] na pia mnaponyanyuka kutoka katika rukuu?**' Imam Abu Hanifa akajibu '**Hatunyanyui mikono kwa sababu Mtume Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* hakufanya hivyo**' Imam Awzai akaanukuu *Hadith* na kusema: '**Al Zuhri amesema kutoka kwa Salim na yeye amesikia kutoka kwa Ibn Umar kua Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* alikua akinyanyua mikono kabla ya kurukuu na baada ya kuruu**'.

Imam Abu Hanifa akajibu '**Hamad amenukuu kutoka kwa Ibrahim Al Nakhai na yeye amenukuu kutoka kwa Alqama na Al Aswad ambao wamemsikia A'bd Allah Ibn Masud kua Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, hanyanyui mikono katika Sala isipokua mwanzoni wa Sala kwenye takbir ya kwanza [*tahrima*]**'.

Hapo Imam Awzai akasema '**Katika *Hadith* yangu kuna maunganisho matatu ya walionukuu baina yangu na Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, lakini**

kuna maunganisho manne katika *Hadith* yako’. Hapa akiwa na maana ya kua *Hadith* yake inaweza kua Sahih zaid kuliko ya Abu Hanifa.

Hivyo Imam Abu Hanifa akajibu: ‘**Hammad yuko juu zaid katika *Fiqh* kuliko Al Zuhri, Ibrahim Nakhai yuko juu pia kuliko Salim, na Alqama hayuko chini ki*fiqh* kuliko Ibn Umar, Ikiwa Ibn Umar ana sifa za kuwa Sahaba, basi Alqama ana sifa zenye uhakika zaid, na kwa kiunganisho cha mwisho cha wanukuaji wangu, basi haina hata haja ya kutaja sifa za Abd Allah Ibn Masud**’. Hapo Imam Awzai ikambidi anyamaze kimya.

Imam Abu bakr Ibn Al Arabi ameandika katika maelezo ya kisa hiki cha Imam Abu Hanifa na Imam Awzai katika *Sunan Al Tirmidh*i kua ‘**Ikiwa kuna migongano katika maoni ya A’bd Allah Ibn Umar na A’bd Allah Ibn Masud basi wa kufuatwa ni A’bd Allah Ibn Masoud**’.

Safari moja wakati Imam Abu Hanifa anasomesha Darsa, alikuja mtu na kusema kua hajui kama jirani yake ni Muislam ama la, hivyo alikua anataka kujua Jee kama jirani huyo akifariki anayo haki ya kumkosha na kumzika Kiislam ama la?

Imam Abu Hanifa akamuuliza mtu huyo : ‘**Jee ni kitu gani kilichokufanya wewe ufikirie kua si Muislam?’**.
Yule Bwana akajibu: ‘**Jirani yangu ana mambo saba ambayo yamenifanya niwe na wasi wasi juu ya Uislam wake. Kwanza anasema hana Imani na dalili za Allah anazoziona, Pili anasema kua hamuogopi Allah. Tatu anasema kua Hana matumaini na Pepo. Nne anasema kua Hauogopi Moto. Tano ni kua nimemuona kila anapokua akisali alikua akisali bila ya Kurukuu au Kusjudu. Sita anasema kua anakula nyama ambayo tayari imeshakufa. Saba ni kua anasema haipendi Haki na anaifurahia Fitna!**’.

Imam Abu Hanifa akatabasamu kisha akawatazama Wanafunzi wake akiwemo Qadhi Abu Yusuf na Ash Shaybani na kuuliza : ‘**Jee mnasemaje kuhusiana na Jirani huyu baada ya kuelezewa mambo yake?’.** Wanafunzi wote wakaona kua kila kitu kiko wazi kua Jirani huyo hana dalili za kua na Uislam. Hivyo Imam Abu Hanifa akawauliza tena Wanafunzi wake kuhusiana na mtizamo wao huo. Wanafunzi wakajibu hivyo hivyo.

Hapo Imam Abu Hanifa akakaa kimya na kutafakkari kisha akatabasamu na kusema: ‘**Jee hamkuwahi kuisikia *Hadith* ya Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* isemayo - *Dhunnu bi’l-mu’minīna khayran* – Wadhanieni Waumini wenzeni katika hali ya kheri? ’**, kisha akaendelea : ‘**Hivyo**, **kama ikiwa Imani ya mtu inaweza kugaiwa katika makundi 100, na ikiwa sehemu 99 ya Imani mtu huyo ni ziro, na sehemu 1 tu ya Imani yake ni Sahih, basi hua tunachana na ile asilimia 99 yote, na tunaichukua ile asilimia 1, na hivyo tunamhesabu mtu huyo kua ni Muumini.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abu Hanifa akaendelea kwa kusema**: ‘Hata hivyo, hali hua kaiko rahisi kama hivyo, lakini baada ya kusikia muonekano wa mtu huyu ambae ni jirani yake huyu bwana, basi mimi nimefurahia habari hiyo na ningependa kua kila mtu miongoni mwetu awe na *Aqida* kama ya jirani wa huyu bwana’**

Watu wote waliokuwepo hapo wakashangaa na kuanza kutizamana, huku kila mmoja akijiuliza moyoni mwake inakuaje leo hii mtu mwenye mambo kama haya awe ni mfano wa kuigwa?.

Imam Abu Hanifa akaendelea**: ‘Nitakuambieni ni kwa sababu gani mimi nikafurahia Aqida ya huyo bwana na kwa nini nikataka awe ni mfano wa kuigwa miongoni mwetu .’**

‘Ama kuhusiana jambo la Kwanza juu ya kauli ya kusema kua : ‘Hana Imani na Dalili za Allah’ basi jee hamkusoma nyie katika *Qur’an* pale Nabii Musa *A’layhi Salaam* alipomuomba Allah *Subhanahu wa Ta’ala* kujionesha mbele yake kama inavyoelezewa ndani ya *Qur’an*:

﴿وَلَمَّا جَآءَ مُوسَىٰ لِمِيقَاتِنَا وَكَلَّمَهُ رَبُّهُ قَالَ رَبِّ أَرِنِيٓ أَنظُرْ إِلَيْكَ قَالَ لَن تَرَانِى وَلَٰكِنِ انْظُرْ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ تَرَانِى فَلَمَّا تَجَلَّىٰ رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكّاً وَخَرَّ موسَىٰ صَعِقاً فَلَمَّآ أَفَاقَ قَالَ سُبْحَانَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَأَنَاْ أَوَّلُ ٱلْمُؤْمِنِينَ﴾

Walamma jaa moosa limeeqatina wakallamahu rabbuhu qala rabbi arinee andhur ilayka qala lan taranee walakini ondhur ila aljabali fa-ini istaqarra makanahu fasawfa taranee falamma tajalla rabbuhu liljabali jaAAalahu dakkan wakharra moosa saAAiqan falamma afaqa qala subhanaka tubtu ilayka waana awwalu almu/mineena *(Surat Al A’raf 7:143)*

Tafsir: ***Na ulipomfikia Musa wakati tuliomuwekea na Mola wake akazungumza nae, nae akasema ‘Ya Rabbi! Nioneshe ili nipate kukuona.’ Nae (Allah) akasema: ‘Huwezi kustahmili kuniona mimi, lakini uangalie Mlima kama ikiwa utabakia katika sehemu yake, basi utaweza kuniona. Lakini Mola wake alipouonesha Utukufu wake kwa Mlima huo, basi uliufanya Mlima huo kuporomoka na Musa akaanguka***

***kwa kuzimia. Na alipopata ufahamu akasema : Utukufu ni wako pekee, nakuelekea na kua ni miongoni mwa Waumini wa mwanzo*.**

Hivyo Musa hakuziona dalili za Allah alizoziomba kuoneshwa, lakini aliamini. Tofauti na Firáwn, ambae wakati wa kuzama kwake aliziona dalili za Allah na akasema kua ameamini.

﴿حَتَّىٰٓ إِذَآ أَدْرَكَهُ ٱلْغَرَقُ قَالَ آمَنتُ أَنَّهُ لآ إِلَٰهَ إِلاَّ ٱلَّذِى آمَنَتْ بِهِ بَنوٓاْ إِسْرَائِيلَ وَأَنَاْ مِنَ ٱلْمُسْلِمِينَ﴾

Hatta idha adrakahu algharaqu qala amantu annahu la ilaha illa alladhee amanat bihi banoo isra-eela waana mina almuslimeena *(Surat Yunus 10:90)*

Tafsir ***: Hadi pale alipokua akizama, akasema : Nnaamini kua hakuna Mola isipokua yule ambae Bani Israel wanamuamini na mimi ni miongoni mwa walioamini.***

Na Allah *Subhanahu wa Ta'ala* akamwambia:

﴿ءَالَنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنتَ مِنَ ٱلْمُفْسِدِينَ﴾

Al-ana waqad AAasayta qablu wakunta mina almufsideena *(Surat Yunus 10:91)*

Tafsir : ***Sasa hivi tena! Wakati uliniasi hapo kabla na ulikua ni miongoni mwa wenye kufanya ufisadi.***

Hivyo hapa Fir'awn aliziona alama za Allah, lakini alikua tayari ameshachelewa kwani iliikubali Iman pale tu alipoiona. Hivyo inawezekana kua huyu Jirani anasema kua hana Imani na zile aina za alama za Allah, ambazo hazitomfaa baada ya kuziona kwake. '

'Ama kuhusiana jambo la Pili juu ya kauli ya kusema kua : 'Hamuogopi Allah, basi kila mtu hua anajua kua katika Siku ya Malipo. Allah atakua na amri juu ya kila kitu na hakuna mtu akaeweza kumhoji kutokana na hukmu na maamuzi yake. Anayo haki ya kuhukumu atakavyo kwa Haki na Uadilifu au kuhukumu bila mambo hayo. Lakini, anasema kua atahukumu kwa Haki na Uadilifu:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

﴿وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِٱلْحَقِّ وَهُمْ لاَ يُظْلَمُونَ﴾

Waqudhiya baynahum bialhaqqi wahum la yudhlamoona *(Surat Az Zumar 39:69)*

Tafsir: ***Na watahukumiwa baina yao kwa Haki na wala hawata dhulumiwa.***

Na pale aliposema katika sehemu nyengine:

﴿وَقُضِيَ بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ وَهُمْ لاَ يُظْلَمُونَ﴾

Waqudhiya baynahum bialqisti wahum la yudhlamoona *(Surat Yunus 10:54)*

Tafsir ***: Na watahukumiwa baina yao kwa uadilifu na wala hawata dhulumiwa.***

Hivyo inawezekana kua huyu bwana anasema kua haogopi kua Allah atahukumu bila ya Haki na Uadilifu, kwani ana uhakika kua Allah atahukumu kwa Haki na Uadilifu.'

'Ama kuhusiana jambo la Tatu na la Nne juu ya kauli ya kusema kua Hana Matumaini ya Pepo na Haogopi Moto wa Jahanam. Basi sote tunajua kua mambo yote haya ni miongoni mwa Viumbe vya Allah, na hivyo havina mamlaka ya kuamua ni nani atakaeingia ndani yake na ni nani ambae hatoingia ndani yake. Ni yule alieviumba tu ndie mwenye Mamlaka ya kujaalia ni nani ataingia Peponi na ni nani ataingia Motoni. Hivyo inawezekana ikawa huyu bwana anasema hakhofii kuingia Motoni wala hana matumaini ya kuingia Peponi, kwa sababu anajua kua ni Allah ndie atakaeamua anakostahiki kuelekea.'

'Ama kuhusiana na jambo la Tano juu ya kauli ya kusema kua kila unapomuona anasali, alikua akisali bila ya kurukuu wala kusjudu. Basi fahamu kua Nabii *Salallahu A'layhi wa Salam* amesema kua: Muumini ana haki sita juu ya Muumini mwenzake, Anapokutana nae basi Aamkiane nae, Anapoumwa basi amtembelee, Anapomualika basi akubali mualiko, Anapoenda chafya basi amuombee Rehma, Atakapokuwepo au atakapokua hayupo basi anatakiwa amfikire mema, na Atakapokufa basi amsalie Sala ya maiti juu yake. Hivyo inawezekana kua wakati ulipomuona mtu huyu alipokua akisali bila ya kurukuu au kusjudu basi labda alikua akisali sala ya Maiti ambae alikua hayupo na hivyo inawezekana kua katika wakati huo kuna maziko katika sehemu yeyote za ardhi za Kiislam.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Sote tunajua kua sio lazima kwa Maiti kuwepo mbele yako ili kusali Sala ya Maiti, kwani *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* alisali ya Maiti kwa ajili ya Najash aliefariki Uhabeshi wakati *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* alikua yuko Madina. Hivyo inawezekana kua kila wakati unapomuona anasali hua anasalia Sala ya Maiti kwa ajili ya Muumini yeyote aliefariki Ulimwenguni na hivyo hua anatekeleza Jukumu lake juu ya Muumini mwenzake.'

'Ama kuhusiana jambo la Sita juu ya kauli ya kusema kua anakula Nyama ambayo tayari imeshakufa (al-maytah).' Basi fahamu kua *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* amesema kua - *Uhillat lana al-damān wa'l-maytatān* - Tumehalalishiwa damu aina mbili na Maiti aina mbili [yaani aina mbili za Damu tulizohalalishiwa ni zilizomo ndani ya figo na Maini ya Mnyama aliekua Halali na Maiti wawili ni Samaki na Nzige. Muislam yuko huru kula vitu hivi kama ikiwa anaweza.]'.

Hivyo faham kua inawezekana akawa anazungumzia Samaki waliokufa na Nzige waliokufa ambao hua anapenda kula. Hivyo basi kauli yake hii inakua ni Sahihi na isiyokua na shaka.'
'Ama kuhusiana jambo la Saba juu ya kauli ya kusema kua anapenda Fitnah na anachukia Haki. Basi hua hana tofauti na mtu yeyote yule miongoni mwenu, kwani anaposema kua anachukia Haki, basi jee hamkumbuki kua katika *Qurán Allah Subhana wa Ta'ala* anasema kua:

﴿وَجَاءَتْ سَكْرَةُ الْمَوْتِ بِالْحَقِّ ذَٰلِكَ مَا كُنتَ مِنْهُ تَحِيدُ﴾

Wajaat sakratu almawti bialhaqqi dhalika ma kunta minhu taheedu *(Surat Qaf 50:19)*

Tafsir: ***Na yatakuja Sakarat al Mauti (Hali ya hisia za Mauti) kwa Haki. Hicho ni kile mlichokua mkikimbia.***

Naam..hakuna mtu yeyote yule miongoni mwetu anaependa *Sakarat ul Maut* na pia hakuna ambae hayachukii. Kwa sababu Hakuna mtu mwenye akili zake timamu kua ni mwenye kupenda *Sakarat ul Maut.* Hivyo inawezekana kua wakati anasema kua anaichukia Haki basi hua anamaanisha jambo hili.

Kwa upande mwengine vile vile Qurán inasema kua:

﴿إِنَّمَآ أَمۡوَٰلُكُمۡ وَأَوۡلَٰدُكُمۡ فِتۡنَةٞ﴾

Innama amwalukum waawladukum fitnatun *(Surat At Taghabun 64:15)*

Tafsir: ***Hakika ya Mali zenu na Watoto wenu ni Fitnah***

Hivyo hakuna mtu miongoni mwetu asiependa Mali na Watoto wake, sasa jee kuna tofauti gani baina yetu sisi na jirani yake huyu bwana? Inawezekana kua anaposema kua anapenda *Fitnah* basi hua anakusudia Mali na Watoto.

Kamwe hamjawahi kukutana na jirani wa huyu bwana wala hamjawahi kuzungumza nae, lakini hata hivyo nyote mmekubaliana kua huyo bwana si Muislam. Na hii ni kwa sababu hamkufikiria wema bwana huyo baada ya kuyasikia mambo saba aliyokua nayo. Hivyo baada ya kusikia mtizamo wangu juu yake basi labda mtafahamu kwa nini A*qida* yake ni Sahih. Na mtajua kwa nini kila Muislam anatakiwa awe na *Aqida* hiyo.'

Wale wote waliokuwepo katika Darsa hiyo wakashangazwa na Mtizamo wa kina, *I'lm*, Hikma na Busara alizokua nazo Imam Abu Hanifa.

IMAM MUQATIL IBN SULAYMAN 80 AH

Imam Abu Al Hasan Muqatil Ibn Sulayman Al Balkhy alizaliwa mnamo mwaka 80 AH katika maeneo ya Balkh, ambapo baadae akahamia katika maeneo ya Marw ambapo alioa na kisha akakaa kwa mda kabla ya kuamua kuhama katika maeneo hayo na kuelekea katika Ardhi ya Iraq na kua ni mwenye kuishi katika mji wa Basra.

Imam Muqatil Ibn Sulayman alianza kusoma kwa Wanazuoni wakubwa wakubwa akiwemo Imam Ad Dahhaq Ibn Muzahim, Mujahid Ibn Jabr na Imam Ataa Ibn Abi Rabah ambao wote walikua ni Wanafunzi wa *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na pia alisoma kwa Imam Said Ibn Musayyib hivyo Imam Muqatil kua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Sira na Tafsir ya Qur'an.

Ambapo anasema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Watu ni wenye kumtegemea Muqatil katika fani ya Ilm ya Tafsir:**' na akasema tena kua: '**Yeyote yule anaetaka**

Tafsir basi na achukue ya Muqatil Ibn Sulayman’ na kwa upande wa Imam Ibrahim Al Harbi basi yeye amesema kua: **‘Tafsir ya Ibrahim Al Qalbi ni sawa na Tafsir ya Muqatil’**

Kwani tunapoangalia maneno hayo ya Imam Muhammad Idris Al Shafii basi tunaona kua hii ni kutokana na upekee wa Ilm ya Wanazuoni wa Mji wa Basra ambao ndio waliomsomesha Imam Muqatil Ilm ya Tafsir ya Qur’an ambao ulikua unaathari kubwa sana za njia za Tafsir zinazotumiwa na Wanazuoni wa Mji wa Madina ambao wao walikua ni wenye kutotilia maanani sana Ilm ya Sanad ya Hadith kwani wao walikua wakitilita maanani zaidi maana na ujumbe uliomo kwenye hadith husika.

Na hii ni kwa sababu Wanazuoni wa Basra walikua wakijali zaidi kuhusiana na Ilm ya Kuisafisha Nafsi kupitia katika Maonyo juu ya kuachana na Mtamanio ya Kidunia, na kuikimbilia Akhera kwa kufanya mema zaidi na kuachana na Maovu na ndio hivyo walikua wanavutiwa sana kuhusiana na mafunzo yaliyomo kwenye visa vilivyotajwa kwenye Qur’an na maonyo yake, malipo yake na adhabu zake.

Wanazuoni wa Miji hii walikua ni wenye kutumia njia za kufikisha ujumbe wao kwa kutumia utaalamu mkubwa wa Lugha ya Kiarabu na hivyo kua ni wenye kufikisha ujumbe wa Qur’an kihisia kwa wale wanaolengwa na ujumbe wa Qur’an na kuwaboresha kimani, kinafsi na kijamii.

Hivyo Ingawa Imam Muqatil Ibn Sulayman alikua ni mwenye kusoma Ilm ya Tafsir kutoka kwa Wanafunzi wa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* lakini kwa upande mwengine basi alisoma pia kwa Wanazuoni wa Basra ambao walikua wakitegemea kwa asilimia kubwa sana mitizamo ya Masahaba wawili Wanazuoni ambao ni Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* na Ubay Ibn Qaab *Radhi Allahu Anhu* ambao Ilm yao ilikua pia ni katika kutafsiri maneno ya aya kulingana na aina tofauti za utamkwaji wa baadhi ya wa maneno ya Qur’an, na hivyo Imam Muqatil Ibn Sulayman kua ni mwenye kuchanganya sifa zote hizo za Walimu wake katika Ilm ya Tafsiri yake na kua ndie Baba wa Wanazuoni wa Ilm ya Tafsir.

Ambapo Imam Al Athram anasema kua: ‘**Mimi nilimuuliza Ahmad kuhusiana na Muqatil ambapo nae akasema: ‘Sijawahi mimi kuona yeyote yule mwenye Ilm kubwa ya Tafsir kama Muqatil Ibn Sulayman’**

Imam Muqatil Ibn Hayyan aliulizwa: **‘Ewe Abu Bastami hivi ni nani mwenye kujua zaidi baina yenu? Wewe au Muqatil Ibn Sulayman, ambapo nae akajibu: ‘Mimi sijawahi kuona Mtu mwenye Ilm ya Muqatil isipokua ilikua kama Bahari ya Kijani katika Maji ya Bahari.’**

Na ingawa Imam Muqatil alisoma pia kwa Imam Az Zuhri, Imam Nafi Mawla Ibn Umar, Imam Amr Ibn Shuayb, Imam Ibn Buraidah lakini alikua si Mtaalamu mkubwa wa Ilm ya Hadith, ambapo anasema Imam Yahya Ibn Main kua: ‘**Hamna kitu katika Hadith**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

zake' na Imam Abd Rahman Ibn Al Hakam anasema kua: '**Kila Mtu hua ni mwenye kuachana na Hadith zake.**'

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake Imam Muqatil Ibn Sulayman ni pamoja na Hamza Ibn Ziyad Al Tusi, Hammad Ibn Muhammad, Abu Al Junaid Al Ghurair, Abdul Razzaq Ibn Hammam, Sufyan Ibn Uyaynah, Abd Allah Ibn Al Mubarak, n.k.

Siku moja katika wakati wa Utawala Khalifah Abu Jafar Al Mansur alipoteuliwa kua Khalifah wa Dola la Al Abbas basi Imam Muqatil alimtembelea na alipofika mbele yake, Khalifah Al Mansur akamwambia Imam Muqatil: **'Naomba uniusie ewe Muqatil.'**

Imam Muqatil akauliza: **'Nikupe wasia kulingana na nilichokiona kwa macho yangu au kulingana na nilichokisikia kwa masikio yangu?'**

Khalifa Mansur akajibu: **'Kutokana na kile ulichokiona.'**

Imam Muqatil akasema: **'Ewe *Amir Ul Muuminin*, Khalifa Umar Ibn Abd ul Aziz alikua na watoto 11, nae akawawachia Urithi wa Dinar 18, Dinari 5 zikawa kwa ajili ya Sanda yake, na Dinari 4 zikawa kwa ajili ya Kuzikwa kwake, Dinari 9 zilizobakia zikagaiwa kwa watoto wake 11.**

Baadae Khalifa Hisham Ibn Abd Ul Malik alipofariki aliwacha wake wanne na kila Mke akabakia na Dinar 80000 na hivyo Dinari za wake wote hao zilikua 320 ambazo ni sehemu moja kati ya nane ya Mirathi yake yote.'

Imam Muqatil akaendelea kusema: '**Wa Allahi mimi nimeona kwa macho yangu pale mmoja kati ya watoto wa Khalifa Umar Ibn Abd ul Aziz alipotoa Sadaqa Farasi 100 kwa ajili ya *Jihad fii Sabili Allah*, na hapo hapo nikashuhudia kwa macho yangu mmoja kati ya Watoto wa Khalifa Hisham Ibn Abd ul Malik alipokua akiomba barabarani hadharani.**'
Hivyo mali zote zilizopo Ulimwenguni hua hazina maana na ni za mpito kwani ni muhimu zaidi kuacha Watoto wenye Ucha Mungu na weye Taqwa. Imam Muqatil Ibn Sulayman alifariki mnamo mwama 150 Al Hijra.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM ABD UL MALIK IBN UMAR 82 AH

Imam Abd Al Malik Ibn Umar Ibn Abd ul Aziz ambae ni Mtoto wa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Abd Aziz alizaliwa mnamo mwaka 82 Al Hijra, na hivyo kukulia katika mazingira bora ya Kiimani, Ucha Mungu na Kiilm, kwani wazee wake wote wawili walikua ni wacha Mungu sana na Baba yake ni mwenye Ilm kubwa sana, kiasi ya kua Imam Abd Ul Malik Ibn Umar alikua ni mwenye Hikma zaidi ya watu wengine waliomzidi kiumri.

Kwani Abd Ul Malik Ibn Umar ingawa alikua ni Mdogo kiumri lakini alipofikia umri wa miaka 16 basi tu alikua tayari ni kijana mwenye kujua majukumu yake kamilifu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ni mwenye kubeba Majukumu ya Kumsaidia Baba yake katika kumshauri kuhusiana na Mamlaka yake juu ya Watu wake na mbele ya Mola wake na hivyo alikua ni mwenye kupendwa sana na Baba yake.

Ambapo anasema Sayyar Ibn Al Hakkam ambae alikua ni mfanyakazi wa Umar Ibn Abd ul Aziz kua: **'Abd ul Malik Ibn Umar alikua akimuusia Baba yake kwa kumwambia kua: 'Ewe Baba yangu Jaribu kusimamia Uadilifu japo kwa saa moja ndani ya kila siku moja**''

Anasema Imam Maymun Ibn Mihran kua: '**Mimi nilimtembelea Abd ul Malik Ibn Umar, naniakamkuta na chakula chake mkononi ambacho kilikua ni vipande vitatu vya mikate na kibakuli cha siki na samli.**'

Mara nyingi vijana hua ni wenye kuendekeza Ujana wao, hivyo hua si wenye kua na utiifu kwa Mola wao kuliko wazee katika wakati wa uzeeni mwao, lakini kwa upande wa Abd Ul Malik Ibn Umar basi yeye alikua ni kina aliekua katika malezi ya kua ni mwenye kua na utiifu kwa Mola wake.

Ambapo anasema Abd Asim Ibn Bakr Abd Ul Aziz kua: '**Mimi nilienda kwa Sulayman Ibn Malik pamoja nasi akiwemo Umar Ibn Abd ul Aziz nami nikaenda kwa mtoto wake Abd ul Malik ambae alikua hajaoa bado. Na nilikaa kwenye nyumba yake akazima taa na kisha akaanza kusali hadi pale mimi nilipopata usingizi, na nilipoamka nikamsikia akiwa analia huku akisoma aya isemayo:**

﴿أَفَرَأَيْتَ إِن مَّتَّعْنَاهُمْ سِنِينَ۝ثُمَّ جَآءَهُم مَّا كَانُواْ يُوعَدُونَ۝ مَآ أَغْنَىٰ عَنْهُم مَّا كَانُواْ يُمَتَّعُونَ۝﴾

Afaraayta in mattaAAnahum sineena; Thumma jaahum ma kanoo yooAAadoona; Ma aghna AAanhum ma kanoo yumattaAAoona *(Surat Ash Shuara 26:205-207)*

Tafsir: ***Niambie, Hata kama tukiwaacha wastarehe kwa miaka, Kisha kikawajia walichoahidiwa (Adhabu); Basi hayatawafaa kitu yote waliyokua wakiyastarehea.***

Na kisha hua ni mwenye kuirudia na kuirudia aya hio hio huku akilia mpaka mimi nikadhania kua naweza kufikwa na mauti kutokana na kilio hicho, hivyo nami nikasema: 'Allah akuingize kwenye Rehma zake', hivyo nae akakaa kimya.

Umar Ibn Abd Ul Aziz kumwambia Abd Ul Malik kua: '**Kama wewe usingekua mtoto wangu basi ningesema kua: 'Wewe ni mwenye Ilm kubwa zaidi miongoni mwa watu' Shukrani zote anastahiki *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kukujaalia wewe kua msaidizi wangu, ewe mtoto wangu Abd Ul Malik.'**

Anasema Ismail Ibn Abi Hakam kua: **'Siku moja Umar Ib Abd ul Aziz alikasirika sana, wakati akiwa mbele ya Abd ul Malik na kisha baada ya mda hasira zake zikapoa, ambapo Abd ul Malik akasema: 'Ewe Amir ul Muuminin, faham kua umo ndani kipimo cha Rehma za *Allah Subahanh wa Ta'ala,* na katika cheo ambacho yeye ndie aliekupa, ambacho ni kua juu ya usimamizi wa waja wake walio chini yako, na hivyo hasira zako zinaweza zikakuathiri.'**

Umar Ibn Abd Azizi akasema: 'Unasemaje sijakufaham.' Hivyo Abd ul Malik akarudia kauli yake hio, na hivyo Umar Ibn Abd ul Aziz akauliza: 'Hivi jee wewe huwi na Hasira ewe Abd Ul Malik?' Abd Ul Malik akajibu: 'Uwezo wangu wa ndani ya kiroho hauniwezeshi mimi kukasirika mbele ya yule ambae hana cha kunichukiza kutoka kwake.'

Anasema Ibrahim Abi Abi Abla kua: '**Siku moja Umar Ibn Abd ul Aziz alikaa na kusimamia majukumu yake kwa watu wake hadi ilipofika mchana, na hivyo akawa amechoka sana, hivyo akawaambia watu wake hao: 'Enyi watu endeleeni na shughuli zenu hadi nitakaporudi, kisha akaingia ndani na kumpumzika kwa mda wa saa na mara akaja Abd ul Malik ambae akamuuliza baba yake kwa kusema: 'Ewe *Amir ul Muuminin* mbona uko ndani' Umar Ibn Abdul Aziz akajibu: 'Napumzika kidogo kama kwa saa moja hivi' hivyo Abdul Malik akasema: 'Hivi jee unafikiriaje pale kifo kitakapokuja na kukuta wewe ukiwa umekaa ndani huku wachungwaji wako, wako nje wanakusubiri?' hivyo Umar Ibn Abd Al Aziz akanyanyuka na kutoka nje kwa watu wake.'**

IMAM HAMMAD IBN SALAMAH 82 A.H

Imam Abu Salma Hammad Ibn Salamah Ibn Dinar Al Basr alizaliwa mnamo mwaka 82 Al Hijra katika maeneo ya ardhi ya Basra nchini Iraq.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Hammad Ibn Salamah alikua ni Mtumwa alieachiwa huru wa Banu Tamim na alikua na Ilm kubwa sana ya Historia, Lugha, Hadith na Qur'an kwani alisoma kutoka kwa Wanazuoni wengi sana wakiwemo Imam Thabit Ibn Aslam Al Bunani, Imam Qatada Al Sadusi, Imam Hamid Ibn Abi Hamid, Imam Ishaq Ibn 'Abd Allah Ibn Abi Talha, Imam Anas Ibn Sirin, Imam Thamam Ibn 'Abd Allah, Imam Muhammad Ibn Ziyad, Imam Muhammad Ibn Muslim Ibn Tadras, Imam 'Abdul Malik Ibn 'Umayr al-Qabti, Imam 'Abdul 'Aziz Ibn Suhaib, Imam Abu 'Imran Al Jauni, 'Amr Ibn Dinar, Imam Hisham Ibn Zayd Ibn Anas, Hisham Ibn 'Urwa, Yahya Ibn Sa'id Al-Ansari, Ayoub Al Sakhtiyani, Imam Khalid Ibn Mihran Al-Hadha', Imam Da'ud Ibn Abi Hind, Imam Sulaiman Ibn Tarkhan al-Taymi, Imam Smak Ibn Harb Ibn Aws na wengineo.

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Ibn Jurayj, Imam Sufyan Ibn Sa'id Ath-Thawri, Imam Shu'bah Ibn Al-Hajjaj, Imam 'Abd Allah Ibn Mubarak, Imam 'Abdur Rahman Ibn Mahdi, Imam Yahya Ibn Sa'id Ibn Farroukh al-Qatan, Imam Sulaiman Ibn Da'ud Ibn Al-Jarud, Imam Hisham Ibn 'Abdul Malik Al-Tayalasi, Imam Musa Ibn Isma'il Al Munqari Al Tabudhaki, Imam Aadm Ibn Abi Iyas, Imam Al-Hasan Ibn Musa Al 'Ashayb, Imam Al 'Aswad Ibn 'Amir Shadhan, Imam Bashr Ibn Al Sari Al Afwah, Imam Bahz Ibn Asad Al 'Ami, Imam Sulaiman Ibn Harb, Abu Nasr Al Tamar, Imam Hadba Ibn Khalid Ibn Al Aswad, Imam Shayban Ibn Farroukh, Imam 'Ubaidullah Ibn Muhammad Al 'Aishi, Imam Sulayman Ibn Da'ud Ibn Al-Jarud n.k
Miongoni mwa Wanafunzi wa wakubwa na maarufu sana wa Imam Hamad Ibn Salamah kutokana na utaalamu wake wenye upekee katika Historia ya Kiislam ni Imam Abu Bishr Amr Ibn Uthmān Ibn Qanbar Al Sibawayh maarufu kama Imam Al Sibawayh ambae ni bingwa wa Lugha ya Kiarabu na ndie Uthibitisho wa Lugha ya Kiarabu.

Imam Hammad Ibn Salamah ni Imam ambae ni mwenye kuaminika sana katika fani ya Tarikh, Hadith na Tafsir, kwani alikua pia ni Mcha Mungu sana na amenukuliwa sana katika vitabu vya hadith vya Imam Bukhari na Imam Muslim, ambapo anasema Imam Abd Rahman Ibn Mahdi kua: **'Kama ingekua Hamamd Ibn Salamah anaambiwa kua: 'Kesho ndio siku yako ya kufariki' basi kamwe asingekua ni mwenye kuhitaji kuongeza jambo jema jengine lolote katika mambo yake kwani yeye alikua ni mtu ambae wakati wake wote anautumia katika Ibada na kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala*.'**

Ambapo anasema Affan Ibn Muslim kua: **'Hakika mimi nimewaona watu wengi sana wenye kufanya Ibada zaidi ya Hammad Ibn Salamah, lakini miongoni mwao hakuna hata mmoja nnaemjua ambae amemzidi Hammad katika kufanya mema, kusoma Qur'an na kutoa Sadaqah kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Ambapo anasema Imam Musa Ibn Ismail kua: **'Kama nikikuambieni kua mimi sikuawahi kumuona Hamamd Ibn Salamah akiwa ni mwenye kucheka basi mtaniamini na hii ni kwa sababu Hammad alikua anautumia mda wake wote**

kusomesha Hadith, kusoma Qur'an, Kufanya *Dhikr Allah* na kusali. Kwani alikua ni mwenye kuigawa siku yake katika kufanya mambo haya tu.'

Ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: **'Wakati nilipoingia kwenye Mji wa Basr basi sikua ni mwenye kumjua mtu yeyote yule ambae alikua akiishi kama walivyoishi Masahaba isipokua Hammad Ibn Salamah.'**

Alisema Hammad Ibn Salamah kua: **'Yeyote yule ambae ni mwenye kunukuu Hadith kwa ajili ya wengine yeyote isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Mtu huyo amedanganyika kutokana na hadith hio.'**

Na Imam Ibn Hajar Al Asqallani amesema kua: **'Hammad Ibn Salamah ni mnukuaji wa Hadith anaeaminika na ni mcha Mungu, alikua ni mtu ambae yuko makini sana na Hadith na alinukuu pia kutoka kwa Thabit Al Bunani, na mwishowe alipokua mzee alikua na udhaifu wa kumbukumbu.'**

Imam Hammad Ibn Salamah alifariki mnamo mwaka 167 Al Hijra. Ambapo anasema Imam Yunus Ibn Muhammad Al Muaddab kua: **'Hammad Ibn Salamah alifariki wakati alipokua akisali Msikitini.'**

IMAM KHALAF IBN HAWSHAB

Imam Abu Abd Rahman Khalaf Ibn Hawshab Al Kufi alikua ni Mwanazuoni aliezaliwa katika Mji wa Kufah alikua ni Mwanazuoni aliesoma kwa Tabiina wakiwemo Imam Al Shabi, Imam Iyas Ibn Salamah, Ataa Ibn Abi Rabah Imam Amr Ibn Mura na wengi wengineo.

Imam Khalaf Ibn Hawshab aliwasomesha pia Wanazuoni wengei kama vile Imam Shubah Ibn Hajjaj, Imam Marwa Ibn Muawwiya, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Shujaa Ibn Walid, Imam Shuraykh An Nakhai na wengineo.

Ambapo Imam Al Ijli anasema kua: **'Khalaf Ibn Hawshab alikua ni Thiqah'**

Na kwa upande wa Abu Rashid basi yeye anasema kua: **'Baba yangu alikua akimpenda sana Khalaf Ibn Hushab, hivyo nami nikamuuliza: 'Ewe Baba yangu hivi kwanini wewe unampenda sana mtu huyu kiasi hicho?' ambapo nae akasema: 'Ewe Mtoto wangu hakika huyu alikua ni mwenye kuishi katika njia bora ya maisha na hakua ni mwenye kuachana nayo njia hio''**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Aliusia Imam Khalaf Ibn Hawshab kwa kusema kua**: 'Yule anaekikumbuka Kifo basi hua ni mwenye kufaham kua hakuna Uzuri katika Maisha ya Dunia'**

Na akasema tena Imam Khalaf Ibn Hawshab kua: **'Waachieni Watawala Dunia yao'.**

IMAM MISAR IBN KIDAM

Imam Mus-haf Abu Salama Misar Ibn Kidam alikuani Imam mwenye Ilm kubwa sana ya Hadiha ambae alisoma kutoka kwa Masahaba wakiwemo kina Hakam Ibn Utayba *Radhi Allahu Anhu,* Amr Ibn Murrah *Radhi Allahu Anhu Imam* Ady Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu* na wengineo na hivyo alikua ni Imam mwenye kuaminika sana katika Fani ya ilm Ya Hadith kaisai ya kua alikua akiitwa Msahafu kutokana na kuaminika kwake.

Imam Abu Salama Misar Ibn Kidam aliwasomesha pia Maimamu wengi wakiwemo kina Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Yahyha Ibn Al Kattan, Imam Muhamamd Ibn Bishir, Imam Yahya Ibn Adem na wengineo na hadith zake zinapatikana kwa wingi kwenye Vitabu sita vya Hadith.

Ambapo amesema Imam Yahya Ibn Kattan kua: **'Mimi sijawahi kuona mtu anaeaminika katika Ilm ya Hadith kama Misar'**

Na Imam Ahmad Ibn Hanbal amesema kuhusiana nae kua : **'Thiqah hau ni sifa ya watu kama Misar na Shu'bah'**

Imam Waki Ibn Jarrah akasema pia kua: **'Shaka ya Misar hua ni sawa na Hakika ya Mwanazuoni mwengine'**

Imam Misar alikua ni mtu mcha Mungu sana kiasi ya kua ilikua kila siaku halali hadi awe nimwenye kusoma Qur'an japo nusu Msahafu. Na hili linathibitishwa na mtoto wake pale aliposema kua: '**Baba yangu alikua hawezi kulala kama hajasoma Quran Nusu Msahafu'**

Imam Yala alisema: **'Misar alikusanya Ilm na kisha akawa ni mwenye kujitenga na yenye kushabihiana'**

Imam Sufyan Ath Thawry nae akasema**: 'Misar ni asili ya Haki na ukweli'**

Imam Misar Ibn Kidam alikua pia ni Mtu mwenye kusimamia kiadilifu haki za wazee wake, kwani usiku mmoja alitumwa maji na mama yake, hivyo alipotoka nje kuenda

kuchukua na kurudi ndani basi alimkuta Mama yake akiwa tayari ameshalala, hivyo Imam Misar Ibn Kidam akabakia hapo hapo na Jagi lake la Maji hadi alfajiri akimsubiri Mama yake aamke ili ampe maji hayo.

Imam Misar Ibn Kidam alikua ni Mtu ambae ni mwenye Khofu kubwa sana ya siku ya Malipo na hivyo alikua kila anapokumbuka juu yake bas hua ni mwenye kulia na hivyo alikua akisema kua: **'Hakika kama sio Mama yangu basi mimi ningeutumia mda wangu wote nikiwa msikitini tu'**

Kutokana na Ilm na ucha Mungu wake basi Khalifa Mansur alipoingia Madarakani alimteua Imam Misar Ibn Kidam awe Qadhi lakini hata hivyo Imam Misar akakataa wadhifa huo kwa kusema: '***Ewe Amir Ul Muuminin,* hakika ya familia yangu mimi ni yenye kuhitaji Mahitajio yao, na hivyo hua ni mwenye kuwaambia kua nitawatufatia, lakini hata hivyo hua si wenye kuridhika na ninavyowahudumia, halafu wee unataka kunipa mimi majukumu wakati watoto wangu bado hawajaridhika na usimamizi wangu juu yao'** na hivyo Khalifa Mansur akaamua kumsamehe kutokana na kumpa wadhifa huo.

Miongoni mwa Hadith alizopokea Imam Misar Ibn Kidam ni pamoja na kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakae Sali sala za Jamaa ndani ya Mwezi mzima wa Ramadhan absi atakua nimwenye kujaaliwa sehemu yake katika Usiku wa Laylat Ul Al Qadr''**

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Jee unafikiri kua yule anaenyanyua kichwa kabla ya Imam hua ni mwenye kua na khofukua huenda kua Allah Subhanah wa Ta'ala atakigeuza kichwa chake kua ni cha Mbwa?'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ''Unaposjudu fanya kama afanyavyo Ndege anaekula Nyama, usilaze mikono yako yote ardhini bali weka viganja vyako tu na utanue kwapa zako, kwaniukifanya hivyo basin a Mwili wako wote utakua ni wenye Kusjudu'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kinapokuja Kiwingu na Kikatokea kivuli chake na Upepo ukavuma basi Omba dua *kwa Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani huo hua ni wakati wa kufanya Toba'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Wanapotokea Mawalii wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kukumbukwa.'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kila kinacholevya hua ni Haramu'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule anaeenda katika Ibada ya Hija kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, *Basi Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kumsamehe Dhambi zake zilizotangulia na hua ni mwenye kumkubalia Maombi ya anaowaombea'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Mtu yeyote yule atakaekuja katika siku ya Malipo akiwa na kosa la Kuwakashifu Masahaba zangu basi Mtu huyo hatopata uombezi wangu juu yake'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Aidha kua Mwanazuoni au Mwanafunzi au mwenye kupenda Ilm au miongoni mwa wenye Ilm lakini usiwe wa tano yaani mtu asiependa Ilm na asiewapenda watu wenye Ilm.'

'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua ni mwenye kuomba Dua kwa kusema kua: 'Ya Allah nakuomba unilinde kutokana na kua na tabia mbaya, matamanio ya Nafsi yangu na Maradhi, Ya Allah usiniwache peke yangu hata mara moja, na wala usininyang'anye vile vizuri ulivyonijaalia'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ukubwa wa Darja ya Sala ya ndani ya Qiyam Al Layl na Sala ya Mchana hua ni sawa na Darja ya Sadaqa iliyotolewa kwa kificho na Sadaka iliyotolewa kwa dhahiri'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaempa Maji ya kunywa Baba yake wakati yeye akiwa mtoto mdogo, basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atampa Mtu huyo Vikombe 7 kutoka katika mto wa Al Kawthar'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaeniona mimi kwenye ndoto yake basi hua amenionakweli kwani Iblisi hawezi kuimngia kwenye muonekano wa maumbile yangu.'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Baina ya Kaburi langu na na Mimbar yangu basi kuna Bustani miongoni mwa Bustani za Peponi'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Wakati Mwili wa Muislam unapokua unaumwa basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* humuamrisha Malaika anaemlinda amuandikie amali za mambo mema aliyokua kaiyafanya wakati alipokua na afya yake Muislam huyo kila siaku usikau na mchana'

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'ndoa zanguzote na Wake zangu na ndoa za Mabinti wanu wote na waume zao zimefungwa kulingana na ruhusa ya Malaika Jibril kutokea kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* hatouchoma Moto mwili wa yule mja ambae ndani ya Moyo wake mna mapenzi yake juu yangu’

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Mtu yeyote yule atakaeona ovu basi mwache alirekebishe kwa Mkono wake, na kama hatoweza kwa mkono wake basi alirekebishe kwa Ulimi wake na kama atashindwa kwa ulimu wake basi na alichukie kwa Moyo wake na hivyo ndio darja ya Mwisho ya Udhaifu wa Imani’

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Kila Mtume alikua na Dua yake kwa Ummah wake na Dua yangu mie kwa Ummah wangu ni Maombezi katika siku ya Malipo’

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Nyoosheni Safu zenu kwani Kunyooka kwa safundio ukamilifu wa Sala’

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Dua inayoombwa baada ya kusomwa kwa Qur’an hua ni yenye kukubaliwa.’
‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Hata kama Ibn Adam atakua Mtu mzima na atapotea lakini Matamanio na Tamaa yatabakia kama yalivyokua hapo kabla ndani yake.’

Baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumaliza kusoma nakuhifadhi Quran basi alikua akiwakusanya watu wake na kusali nakuomba dua’

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* hua ni mwenye kuyasamehe makosa yaliyomo ndani ya Nyoyo za Waja wa Ummah wangu pale inapokua makosa hayo hayajafanywa bado na hayajatamkwa kwa ulimi’

‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua amelala kwenye Jamvi huku akiwa amefanya alama kwenye mwili wake kutokana nalo, hivyo *Aisha Radhi Allahu Anha* akasema: ‘Ya Rasul Allah, Mfalme Kisra wa Uajemi na Mfalme Kaisar wa Bizentium wana Mamlaka makubwa, lakini wewe kwa upande wako ni Mtume wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* huna kitu, unalala kwenye Jamvi na unavaa nguo zisizokau na maana’

Ambapo akasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Ewe Aisha, kama mimi ningetaka basi Mlima wa Dhahabu ungekua ni wenye kutembea nami, kwani Jibril amenilete mimi funguo za Hazina zote za Ardhi, lakini sitaki’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

'Amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Mimi nilimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam: 'Jee ni ipi amali njema zaidi?' ambapo akasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ni Sala inayosaliwa kwenye wakati wake, Ukarimu kwa Wazee na Jihad fii Sabili Allah.''

'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: 'Kama Mja wangu akinikaribia mimi kwa inchi moja basi mimi namkaribia kwa dhiraa moja, na kama mja wangu akinikaribia mimi kwa dhiraa moja basi mimi namkaribia yeye kwa pima moja, na kama mja wangu akija kwangu kwa kutembea basi mimi nitamuelekea kwa kumkimbilia, hata kama mja wangu akija kwangu na makosa yanayojaza Ardhi nzima basi mimi nitamsamehe yeye pale itakapokua hakunishirikisha mimi na chochote.''

Miongoni mwa wasia wa Imam Misar Ibn Kidam ni kua: **'Wenye Ilm zaidi ni yule Mtu ambae ni mwenye Taqwa zaidi miongoni mwa watu'**

'Ewe Mtoto wangu kamwe usiwe mtu mwenye kufanya Matani au kujionesha kwani mimi nimejaribu kuyafanya yote hayo lakini kamwe sikuwahi kuona jambo la kujionesha wala la kulifanyia Matani, kwani kufanya hivyo hua ni ujinga na ujinga hua ni wenye kumshushia mtu thamani yake kwenye jamii.'

Imam Misar Ibn Kidam alikua ni mwenye kuziita Sura zenye kuanzia na Harfu Muqataat kua ni kua: **'Mabwana Harusi wa Sura za Qur'an.'**

Imam Misar Ibn Kidam alifariki mnamo mwaka 155 Al Hijra katika Mji wa Makkah ambapo anasema Musab Ibn Mikdam kua: '**Mimi nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* usingizini huku Sufyan Ath Thawry akiwa ameshika mkono wake huku akiwa ni mwenye kusema: 'Ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, Jee unajua kua Misar Ibn Kidam amefariki Dunia?' ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam* akasema: ''Naam najua kua amefariki Dunia hivyo tangazia juu ya hili kwa watu wa Peponi'**

Ambapo kwa upande wa Imam Sufyan Ibn Uyaynah basi yeye anasema kua: **'Wakati Misar Ibn Kidam aliofariki basi mimi nilihisi kama kua Taa zimezimika.'**

Wakati Imam Misar Ibn Kidam anakairibia kufariki basi alietembelewa nyumbani kwake na Imam Sufyan Ath Thawry na hivyo akamkuta Imam Misar akiwa analia na hivyo Imam Sufyan Ath Thawry akasema: '**Unalia nini ewe Misar, Wa Allahi kama mimi ningekua wewe basi nigependa nife sasa hivi.'**

Ambapo Imam Misar akazidi kulia huku akisema: '**Subhanah Allah! Ewe Ath Thawry ama kwa hakika wewe unajiamini sana na Amali zako, wakati mimi mwenzako**

najihisi kama mtu aliepo juu ya Mlima mrefu sana na nnataka kuanguka na sijui nitaangukia wapi.’

Na hivyo Imam Sufyan Ath Thawry akaanza nae kulia na kusema: **‘Hakika wewe Misar ni Mcha Mungu sana zaidi yangu.’**

IMAM ABD AL AZIZ IBN ABI RAWWAD

Imam Abd Al Aziz Abi Rawwad Ibn Maymun alizaliwa katika ardhi ya Khurasan na kisha baadae akahamia katika maeneno ya Makah Mukarammah baada ya kua Mtumwa wa Mughira Ibn Muhallaib Ibn Abi Sufra na kisha baada akachiwa huru, na alifariki mnamo mwaka 159 Al Hijra.

Imam Ibn Abi Rawwad alisoma kwa Wanafunzi wa Masahaba ambao ni Maimamu kama kina Imam Ikrimah Mawla Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Imam Muhammad Ibn Ziyad, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Husain Al Jafi, Imam Abu Asim An Nabil n.k.

Hivyo Imam Ibn Abi Rawwad alikua na Ilm kubwa sana ya Hadith ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Mubaraka kua: **‘Abd Al Aziz Ibn Abi Rawwad alikua ni mwenye kufanya Ibada sana na ni mwenye kuaminika katika Ilm ya Hadith’**

Hadithi za Imam Ibn Abi Rawwad zimenukuliwa kwenye vitabu vya Imam Bukhari na Muslim ambapo miongoni mwao ni zile zisemazo kua: **‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Ndoto ya Mcha Mungu hua ni moja kati ya sehemu 99 za Utume’**

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kuweni Wanyenyekevu, kaeni kitako na Masikini na mtakua ni wenye Darja kubwa mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala*, na mtakua ni wenye kuachana na Dharau na Kibr’

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kuficha Mitihani, Maradhi na Sadaqa hua ni sehemu ya Hazina ya Waja wema.’

‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kama vile ambavyo Kutu inavyokua inatolewa kutoka kwenye chuma basi ndivyo pia inavyotolewa Kutu ya Nyoyo.’ Na hivyo Masahaba wakauliza: ‘Jee ni nini kinachong’arisha Nyoyo?’ ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Kusoma Qur’an.’

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Anapotaka mmoja wenu kuelekea kwenye Sala ya Ijumaa basi na akoge Janaba.'

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Wanapokua wamekaaa watu wawili wakizungumza faragha basi hairuhusiki kwa mtu mwengine kuenda kukaa nao bila ya ridhaa yao.'

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaezungumza bila ya kutoa Salam basi msimjibu.'

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakae achana na watu wa Bidaa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamjazia Moyo wake Mtu huyo kwa Salama na Imani.'

Imam Ibn Abi Rawwad amesema kua: **'Amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaemchukia Mtu mwenye Bidaa basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamnyanyua Mtu huyo kwa Darja moja ya juu Peponi.'**

Imam Ibn Abi Rawwad amaesema kua: **'Amesema Baba yangu kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaeshikamana na Sunnah katika wakati wa upotovu wa Ummah wangu basi atakua ni mwenye kupata Malipo ya Shahid''**

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaefuatana na Muislam mwenzake kwa ajilia ya kumnasihi na kumuusia kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamchimbia Mahandaki 70 baina yake na Moto wa Jahannam katika siku ya Malipo, ambapo kila Handaki hua ni sawa na ukubwa Mbingu na Ardhi.'

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Muabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama kwamba ni mwenye kumuona kwani kama wewe humuoni basi yeye ni mwenye kukuona wewe.'

Imam Sufyan Ibn Uyaynah anasema kua: **'Kuna siku ilinyesha Mvua kubwa sana katika Mji wa Makkah, na hivyo Nyumba nyingi sana zikaangamia, isipokua Nyumba ya Abd Al Aziz Ibn Abi Rawwad ambayo ilikua iko salama kabisa, na kutokana na tukio hilo basi akamuachia huru Mtumwa wake kwa ajili ya Kumshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Rehma zake juu yake.'**

Mwishoni mwa uhai wake Imam Ibn Abi Rawwad alikua ni Kipofu ambapo anasema Imam Shaqiq Al Balkhi kua: **'Macho yake yalikua si yenye kuona kwa mda wa miaka**

20, na hivyo alikua si mwenye kuwaona watoto wake, hivyo siku moja mtoto wake siku moja alimwambia Baba yake: ‘Baba nakuonea huruma sana kua macho yako hayaoni’ ambapo Imam Ibn Abi Rawwad akajibu kwakusema kua: ‘Ewe Mtoto wangu hakika mimi ni mwenye kuridhika na kile nilichojaaliwa na Mola wangu’’

Akasema Imam Ibn Abi Rawwad kua: **‘Yeyote yule asiepata Wasia kutokana na Uislam, Na Quran na Kua na Mvi basi mtu huyo kamwe hatoweza kukubaliana na ushauri wa aina yeyote’**

Imam Ibn Abi Rawwad aliulizwa: **‘Vipi unajisikiaje asubuhi hi ya leo?’ ambapo nae akajibu huku akilia kwa kusema: ‘Hivi jee atakua na hali gani yule mtu ambae ni mwenye kukisahau Kifo wakati akiwa ana dhambi nyingi sana? Kwani kifo kinakaribia na uhai unapungua kwa kila siku kwa kadri siku zinavyoenda zake, jee itakuaje mwisho wake mtu huyo? Ataishia Peponi au Motoni? Itakuaje kama akiangukia Motoni?’**

IMAM YAHYA IBN MUADH AL RAZI

Imam Abu Zakkariyah Yahya Ibn Muadh Ibn Jafar Al Razi alizaliwa katika maeneo ya ardhi ya Ray nchini Iran, katika familia ya watu wenye Ucha Mungu na iliyokua na watoto watatu ambao ni Yahya, Ibrahim na Ismail ambao wote walijipatia Ilm ya Dini yake katika maeneo hayo kabla ya kuelekea katika maeneo mengine kwa ajili kutafuta Ilm zaidi ambapo kwa upande wa Imam Yahya basi yeye aliekea katika maeneo ya Balkh na Baghdad kwa ajili ya kutafuta Ilm zaid.

Imam Yahya Ibn Muadh alisoma kwa Walimu wengi sana katika kusafiri kwake kutafuta Ilm wakiwemo pia Imam Is-haq Ibn Sulayman Al Razi na Imam Maki Ibrahim Al Balkhi, Imam Yahya Ibn Muadh alikua ni mtu mwenye sifa ya Ucha Mungu sana na ni mwenye kuweza kupigana vita na kuidhibiti Nafsi yake.

Safari moja Imam Yahya Ibn Muadh alipata barua kutoka kwa kaka yake ambae alikua yuko katika maeneo ya Makkah, ambapo sehemu ya ujumbe wa barua hio ilikua inasema: ‘**Hakika mimi nna hamu na mambo matatu, kwanza ni kuumalizia Uhai wangu katika sehemu tukufu kuliko zote Duniani, kisha kua na Mtumwa wa kumtuma na kisha kukutana tena na wewe kabla ya kufariki kwangu, na *Alhamd lillah* nimeshafanikiwa kuyapata mawili kati ya hayo kwani sasa hivi niko katika mji mtukufu wa Makkah na namiliki Mtumwa, hivyo nakuomba uniombee kua nipate jambo langu la tatu ambalo ni la kuonana nawe kabla ya kufariki kwangu.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo Imam Yahya Ibn Muadh akamjibu kaka yake huyo kwa kusema: '**Ingawa wewe ni mmoja kati ya watu bora nnaowajua, na Alhamd lillah unaishi katika sehemu uliyotaka uishi lakini unatakiwa ujue kua, sehemu hua ni yenye thamani kutokana na watu wenyewe na wala si watu kutokana na sehemu yenyewe. Na kutokana na kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua katika sehemu mbili hizo Tukufu basi sehemu hizo zimekua tukufu kutokana nae.**

Ama mimi kwa upande wangu sitamani kua na umiliki wa Mtumwa kwani Ukubwa wa kumiliki hua ni sifa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na sifa ya kumilikiwa hua ni sifa ya Mja ambae ni kiumbe, hivyo haifai kwa Mja kumfanya mwenzake kua Mtumwa wake na hivyo kua ni mwenye kumzuia kutokana na kua ni Mtumwa wa Mola wake.

Ama kuhusiana na kuonana nami basi unachotakiwa kufanya ni kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* kila wakati katika kila jambo lako na hivyo hutokua na haja ya kunikumbuka mimi, kwani wewe sasa hivi uko katika sehemu ambayo kama inakubidi basi unatakiwa umtoe kafara hata mtoto wako kwa ajili yake, kwani ukimpata *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hutokua na haja nami, lakini kama ukimkosa yeye basi jee mimi nitakusaidia nini?'

Alisema Imam Yahya Ibn Muadh kua: '**Dunia ni sehemu ya Usingizi na Akhera ni sehemu ya kua macho. Hivyo yeyote yule atakaelia usingizini basi atacheka wakati akiwa macho, hivyo jitahidi ulie kwa ajili ya Mola wako kwenye uhai wako hapa Duniani'**

Amesema Yusuf Ibn Husayn Al Razi kua: '**Mimi nimetembelea Miji 120 kwa ajili ya kutafuta Wanazuoni wa kunisomesha na kuniongoza, lakini sijawahi kuonana na yeyote yule anaezungumza kwa umakini na kwa vizuri zaidi kama Yahya Ibn Muadh.**'

Ambapo baadhi ya wasiawa Imam Yahya Ibn Muadh ni pamoja na:

'Wanazuoni wenye Ilm hua ni wenye huruma na rehema kwa Waislam kuliko Mama zao na Baba zao Waislam hao kwa sababu Wanazuoni hao ndio wanaowaokoa Waislam hao na kuhakiskisha kua hawaingii Motoni kesho akhera, kwanikwa upande wa Wazee wao hua ni wenye kuwaokoa watu kutokana na Moto na madhara ya Kidunia tu.'

'Kama ikiwa Mwanafunzi hawezi kunufaika na vitendo na tabia za Mwalimu wake basi Mwanafunzi huyo kamwe hatoweza kunufaika na maneno ya Mwalimu wake.'

‘Funga ni Nuru, Shibe hua ni Moto na Matamanio hua ni Kuni, hivyo inapokutana Shibe na Matamanio basi Moto huanza kuwaka na kumuangamiza mwenye kua nayo mambo hayo.’

‘Kaa mbali na watu walioghafilika, wajinga na wenye kukusifu.’

‘Jihadhari na Dunia hii, kwani hii ni sehemu ya mpito kama nyumba ya kusimamia wasafiri, leo tuko hapa na huenda kesho tukahamia sehemu nyengine au kabla yake, hivyo wacha tufanye kile kidogo kinachostahiki hapa ulipo kwa haraka iwezekanavyo kiasi ya kua haina haja hata ya kutumia mda kwa ajili ya kuzungumza, kwani mazungumzo yanatakiwa yawe Akhera.’

‘Awliya ni watu ambao wanawaokoa watu kutoka kwenye mikono ya Shaytan.’

‘Ukikichukua kifo na kukiweka kwenye Sahani na kukiuza Sokoni basi watu wa Akhera hawatotafuta kitu chengine chochote isipokua Kifo kwa ajili ya kukinunua.’

‘Ni Ujinga kufanya mambo ya Motoni halafu kua ni mwenye kujiombea Pepo.’

‘Dhambi moja baada ya Toba hua mbaya zaidi kuliko dhmabi 70 kabla ya toba, hivyo jambo jema zaidi la kufanya ni kuachana na Dhambi.’

‘Ikhlasi hua ni Kusafisha amali zako kutokana na kasoro.’

‘Kukosa kutekeleza wajibu wa Kidini hua kuna ugumu zaidi kuliko kifo.’

‘Kila mmoja hua ni mwenye kukuenda wewe zaidi kulingana na unavyompenda *Allah Subhanah wa Ta’ala,* na kila mtu hua ni mwenye kukuogopa kulingana na namna unavyomuogopa *Allah Subhanah wa Ta’ala* hivyo wakati unapokua ni mwenye kumtumikia *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi kila mtu atajaribu kukusaidia.’

‘Ni vigumua kuachana na mapenzi ya Kidunia, lakini ili kuifikia Pepo basi ni wajibu kuachana na Dunia.’

‘Dunia ni kama shamba, na watu ni kama mazao, kifo hua ni kisu cha kuvunia mazao hayo, Izrail ndie mmiliki wa sehemu ya kutenganisha baina ya mazao na majani, Kaburi ndio sehemu ya kutenganishia mazao na majani. Pepo na Moto ndio ghala ambalo hutenganishwa mazao husika, ambapo baadhi yake yataenda Motoni na baadhi Peponi.’

‘Hakika ya Kitu nnachokifurahia zaidi na kukipenda zaidi ni neema ya Imani ambayo *Allah Subhanah wa Ta’ala* amenijaalia, na kitu nnachokiogopa zaidi ni kua asije akaachana nami.’

‘Pesa ni Nge hivyo usipokua na Dawa ya kujitibu sumu yake basi usimchezee kwa sababu inaweza ikakuangamiza, ambapo dawa yake hua ni kuichuma kihalali na kuitumia kihalali.’

‘Kumtii *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua ni kama sanduku la hazina ambapo ufunguo wake hua ni Sala na meno yake ufunguo huo hua ni kitafunio cha halali.’

‘Katika Kila moyo wa Mtu ha kuna upendo wa mwenye ukarimu juu yake na chuki kwa mwenye ubakhili juu yake.’

‘Mtu mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta’ala* zaidi hapa Duniani basi ndie atakae kua ni mwenye kujiamini zaidi katika siku ya Malipo.’

‘Kuna uadhirisho kwa wale watu ambao ni wenye kutafuta vitu ambavyo viawapeleka kua mbali na *Allah Subhanah wa Ta’ala,* na kuna heshima kwa wale ambao ni wenye kuikimbilia Akhera yao. Kinacho shangaza zaidi ni uadhirisho unaotokana na kutafuta vitu visivyodumu na kuachana na vinavyodumu na vitakavyompelekea mtu kua ni mwenye kufuzu.’

‘Yule anaezungumza bila kutafakkari hua ni mwenye kujuta baada yake na mwenye kuzungumza baada ya kutafakkari hua ni mwenye kuupata utulivu.’

‘Jambo gumu zaidi kwa yule mwenye kufuata njia ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni kujikuta kua uko katikati ya watu waliokua na ugeni kwako.’

‘Heshima ni nzuri kwa yeyote mwenye nayo na hua ni nzuri zaidi kama ikiwa ni sehemu ya mtu mwenye Mali, na Kiburi ni kibaya kwa yeyote aliekua nacho lakini kama kikikutikana kwa Mtu masikini basi hua ni kibaya zaid.’

‘Umasikini wa kweli ni kuogopa kua Masikini na Utajiri wa kweli ni kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta’ala.’*

‘Katika siku ya Malipo hautopimwa Utajiri wala umasikini bali kitakachopimwa ni Shukrani kutokana na kujaaliwa Utajiri na Subra kutokana na kujaaliwa Umasikini, hivyo jambo la muhimu si kua na Utajiri mkubwa au kua na wala si kua na Umasikini mkubwa bali kua na Shukrani na pia kua na Subra.’

'Ewe Mola wangu, Kitu kitamu zaidi kwenye ufahamu wangu mie ni kua na matumaini ya Rehma zako, kitu kitamu zaidi kwenye Ulimi wangu ni katika kukutukuza kwangu na mda mtamu zaidi kwangu mie ni pale nitakapokuona dhahiri.'

Imam Yahya Ibn Muadh alisema pia kua: **'Kuna bashirio jema kwa yule ambae ni Mwenye kuifanya Ibada kua ndio Kazi yake, Akhera yake ndio shughulisho lake, Kujitenga na watu ndio Matamanio yake, Kifo ndio Tafakkur yake, Toba ndio Maombi yake, Mola wake ndio kimbilio lake, Kuachana na Dunia ndio Nia yake. Kuyaangamiza matamanio ya Nafsi yake ndio Mtizamo wake, Majuto ni Juu ya Dhambi zake, Kilio cha Usiku wake ni kwa ajili ya Mola wake.**'

Na akasema tena kua: '**Mambo matatu yafuatayo yafanye kwa ajili ya Muislam mwenzako: Kama huwezi kumnufaisha basi Usimdhuru, Kama huwezi kumfurahisha basi Usimkasirishe na kama ukimzungumzia basi usimseme kwa mabaya.**'

Imam Yahya Ibn Muadh alifariki mnamo mwaka 258 Al Hijra katika ardhi ya Nishapur.

IMAM AL-AWZAI 88 AH

Imam Abd Rahman Ibn Amr Ibn Yuhmad Abu Amr Al Awzai alizaliwa mnamo mwaka 88 Al Hijra katika familia ya kimasikini iliyotoka katika kabila la Al Awzai katika maeneo ya Baalbek nchini Syria ambapo alifiwa na Baba yake na hivyo baadae familia yake ikahamia katika maeneo ya Lebnan.

Imam Al Awzai alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa miongoni mwa Tabiina ambapo miongoni mwa wenye darja kama yake kiilm wanaingia kina Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Daud Az Zahiri Imam Ibn Jurayj, Imam Abu Hanifa n.k

Imam Al Awzai alikua ni Uthibitisho wa Hadith zake, na ndio maana akawa anasema Imam Muhamamd Idris Al Shafii kua: '**Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu ambae Ilm yake ya Fiqh inafanana na Hadith zake kama Al Awzai.'**

Imam Al Awzai alisoma kwa Wanazuoni wa *Tabiina* wakiwemo kina Imam Ata' Ibn Abi Rabah, Imam Abu Ja`far Al Baqir, Imam Amr Ibn Shu`ayb, Imam Makhul, n.k Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Qatadah, Imam Rabi`a Ibn Yazid al-Qasir, Bilal Ibn Sa`d, Imam al-Zuhri, Imam Yahya Ibn Abi Kathir.

Ambapo anasema Abass Ibn Al Walid kua: **'Hakika mimi sikuwahi kuona mtu ambae alikua akimhusudu kwa kumpenda mtu kama vile ambavyo Baba yangu alivyokua alivyokua akimpenda Al Awzai na alikua akisema: 'Utukufu ni wako, fanya ufanyavyo, ewe mtoto wangu Wafalme hawana uwezo kujisimamia nafsi zao na kusimamia nafsi za watoto wao kama vile ambavyo Al Awzai anavyoweza kuisimamia Nafsi yake.**

Kwani sijawahi kumsikia akisema maneno bora kwa msikilizaji anaeambiwa isipokua yule anaesikia hua ni mwenye kujua kua yeye ndie mlengwa, na wala sijawahi kumuona akicheka bila ya kujidhibiti, na kila alipokua akizungumzia kuhusiana na kurudi kwa Mola wetu, basi mimi hua ni mwenye kujiuliza : 'Jee kuna Moyo hata mmoja ambao haulii humu ndani?'''

Al Hiql alisema: '**Al Awzai alitoa fatwa juu ya mambo 70,000' ambapo Abd Rahman Al Mahdi nae akasema: 'Watu waliokuwepo katika nyakati zao ni wanne, Hamad Ibn Zayd wa Basra, Sufyan Ath Thawry wa Kufah, Malik wa Hijaz na Al Awzai wa Sham**'

Imam Ismail Al Ayash alisema: **'Mimi nimesikia watu wakisema kua katika mwaka 140 kua Mwanazuoni bora katika wa Ummah wetu ni Al Awzai**' na Imam Al Awzai alipokuja katika Mji wa Makkah basi Sufyan Ath Thawry alitembea mbele yake na kuwaambia watu kwa kusema: '**Tanueni njia kwa ajili ya Shaykh'**

Imam Malik aliwalinganisha Imam Sufyan Ath Thawry na Imam Al Awzai kwa kusema kua: **'Mmoja wao (Sufyan Ath Thawry) ni mwenye kujua zaidi ya mwengine lakini haifai mmoja kua Imam wakati mwengine tayari ni Imam.'**

Imam Al Awzai alikua ni mtu asiekua na khofu na mtu yeyote katika kusema ukweli kwa wenye Mamlaka, kiasi ya kua, mara baada ya Mapinduzi ya Banu Umayyah basi basi aliitwa mbele ya Abd Allah Ibn Ali Al Safwah ambae ni Ami yake Khalifah alieshika Mmalaka ya Utawala wa Banu Al Abbas na kuulizwa: '**Hivi jee ni upi mtizamo wako kuhusiana na tuliyoyafanya**'

Imam Al Awzai anaelezea hali ilivyokua kwa kusema: '**Hakika mimi nilifikiria sana na hivyo nikaamua kusema ukweli, hivyo nikamwambia: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Hakika ya Amali hua integemeana na Nia'**

Nae Al Safwah akasema: **'Hivi jee ni upi mtizamo wako kuhusiana na hawa watu tuliowaua waliokua kwenye Mamlaka'** nami nikasema: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kumuua Muislam kumeharamishwa isipokua**

kwa Mzinifu alieoa, Mtu alieuhama Uislam na kuingia katika Dini Nyengine na Mtu alieua Mtu mwengine bila kuruhusika Kisharia.''

Al Safwah akasema: **'Niambie kuhusiana na Ukhalifa, Jee huu sio Urithi wetu kama ilivyoelezewa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*?' Nami nikasema: 'Kama hali ingekua ni hivyo, basi Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* asingempisha mtu yeyote kua Khalifa wakati yeye yupo'**

Al Safwah akauliza: **'Hivi jee unasemaje kuhusiana na Mali za Banu Umayyah?' nami nikasema: 'Kama zilikua ni halali kwao wao basi pia ni haramu kwenu nyie, na kama zilikua ni haramu kwao wao basi kwenu nyie ni haramu zaidi.'**

Ambapo amesema Al Walid Ibn Mazyad kua: '**Hakuna aliekua akimzidi Al Awzai katika ufanyaji wa Ibada zake**' kwani Imam Al Awzai alikua kila baada ya kusali sala ya Alfajir basi alikua haondoki katika Msala wake hadi pale litakapochomoza Jua na kuingia katika wakati wa *Dhuha* na husimama na kusali.

Na alipoulizwa kuhusiana na Khushuu basi Imam Al Awzaii alisema: '**Khushuu katika Sala ni kuangalia chini huku ukiinamisha Bawa la Unyenyekevu na Ulaini wa Moyo ambao ndani yake mmejaa huzuni na khofu'**

Ambapo Al Walid Ibn Mazyad alisema kua: **'Mimi nilimuona Awzai alipokua akitembea, na alikua kama mtu kipofu kutokana na unyenyekevu wake.'**

Ama kuhusiana na *Al A'ablah* yaani mtu asiekua na uzoefu wa kitu basi alisema kua ni : **'Ni yule ambae ni kipofu kwa ujinga na hivyo asiejali juu ya kufanya mema.**' Na pia akasema: '**Yeyote yule anaekumbuka sana kifo, basi humtosheleza Riziki yake hata kama ikiwa kidogo, na yule mwanye kufaham juu ya hilo basi hata maneno yake hua ni amali njema na kauli yake huhifadhika.'**

Ambapo alisema Imam Al Awzai wenyewe kua: '**Yeyote yule atakaesimama Usiku katika Qiyam Al Layl kwa mda mrefu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamrahisishia kisimamo cha Siku ya Malipo kwa ajili yake.**'

Amesema Imad Abd Allah Ibn Mubarak kua amesema Imam Al Awzaii kua: '**Ilm hii ilikua ni yenye kuheshimika sana, na hivyo watu walikua ni wenye kuhadithiana miongoni mwao, lakini pale ilipoanza kuwasilishwa kwenye maandishi ya vitabu, basi wale wasiokua wasimamizi sahihi wakaanza kushughulikiana nayo.**'

Na akasema tena Imam Al Awzai kua: '**Wale wenye kuchukua Darja ya juu isiyokua ya kawaida miongoni mwa Wanazuoni wametangulia mbele ya haki na kuachana na Uislam.'**

Alisema Imam Al Awzai kua pia: **'Mimi nilijiona nikiwa nimebebwa na Malaika wawili, ambao wamenikumbatia mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae aliuliza kwa kusema kua: 'Jee wewe ndie Mja wangu Abd Rahman ambae ndie mwenye kuamrisha Mema?' nami nikasema: 'Kwa utukufu wako na uwezo wako basi wewe ni mwenye kujua zaidi' kisha Malaika hao wakanichukua na kushuka na kunirudisha katika sehemu niliyokuwepo hapo awali'**

Ambapo miongoni mwa Fatwa zake Imam Al Awzai basi ni kua Paja la Mwanamme hua ni sehemu ya Awra anapokua Msikitini lakini anapokua kwenye Hammam basi hua si Awra.

Imam Muhammad Ibn Abd al-Rahman Al Sulami anasema kua: **'Mimi nilimuona Al Awzai na alikua ni mtu mwenye urefu wa kawaida, mwembamba na si mweupe sana bali mwenye weupe wa kiza na alikua akitumia hina' na alikua akivaa kilemba kisichokua na mkia mkubwa.**

Anasema Imam Adh Dhahabi kua: **'Mbali ya kua Al Awzai alikua ni mwenye Ilm kubwa sana lakini pia alikua ni mahiri sana wa kuandika barua.'**

Ambapo baada ya kufariki kwake Mjini Jerusalem basi Jeneza lake lilibebwa na Waislam, Mayahudi, Wakristo na pia Watu wa Qubt.

Na anasema Yazid ibn Madh`ur kua: **'Mimi nilimuona Usingizini Al Awzai na hivyo nikamwambia: 'Ewe Al Awzai hebu nioneshe njia ya Kumkaribia *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambapo nae akajibu: 'Hakika mimi sioni Darja ya kumkaribia *Allah Subhanah wa Ta'ala* zaidi ya ile ya Mwanzuoni mwenye Busara na baada yake basi ni mtu mwenye kua na huzuni.**''

Imam Abdur Rahman Al Awza'i alisema kua: '**Pale A*llah Subhanah wa Ta'ala* anapotaka kuwasababishia watu Madhara basi huwajaalia kua ni wenye kua na ubishano usiokua na mwisho ambao utawazuia wao kutofanya amali njema.'**

Na akasema pia kua: **'Hapo mwanzoni Ilm hii ilikua iko wazi na ni yenye darja kubwa sana, kwani watu walikua *yatalaqawhanu baynahum* – Wakiusiana baina yao juu yake, lakini ilipoingia kwenye vitabu - *Dhahaba nuruhu wa sara ila ghayr ahlihi* - basi Nuru yake ikatoweka na ikawafikia watu wasiokua na vigezo.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Al Awzai alifariki mnamo mwaka 155 Al Hijra.

IMAM AL QARI ASIM AL QUFI 90 AH

Imam Asim Ibn Abd Al Nujud Abu Bakr Al Asad Al Qufi alizaliwa mnamo mwaka 90 Al Hijra alikua ni mmoja kati ya Wasomaji wa Qur'an wa Mji wa Kufah ambae alisoma kwa Imam Abu Abd Rahmani Al Sulami.

Kwani yeye mwenyewe alikua ni mwenye kusema kua: **'Hakuna alienisomesha mimi hata herufi moja ya Qur'an isipokua Abd Rahman Al Sulami, kwani nilikua nikiondoka kwake na kumsomea Qur'an**'

Ambapo anasema Mwanafunzi wake Imam Asim aitwae Hafs kua: '**Aliniambia mimi Asim kua: 'Qiraa nilichokusomesha wewe ndio nilichokisoma kutoka kwa Abu Abd Rahman Al Sulami ambae yeye alisoma kutoka kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*, na Qiraa niichomsomesha Abu Bakr Al Ayyash ndio nilichomsomea Zarr Ibn Hubaysh, kutoka kwa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*''**

Imam Ibn Sad anasema kua: **'Asim ni Mtu anaeaminika katika Hadith ingawa hua ni mwenye kufanya makosa madogo madogo' ambapo Imam Al Ijli alisema kua: 'Asim alikua ni mwenye kukusaya hadithi na ni miongoni mwa Wanazuoni wa Qiraa, ambapo alikua ni miongoni mwa Viogozi wa Qiraa na alikua ni mwenye kumuunga mkono Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu*'**

Ambapo Imam An Nasai basi yeye anasema kua: '**Asim ni mtu mwenye kukubalika Hadith zake.**'

Na kwa Ya'qub Ibn Sufyan basi yeye amesema kua: '**Baadhi ya Hadith zake ni zenye kuchanganya lakini ni mwenye kuaminika.**'

Imam Asim alifariki mnamo mwaka 128 Al Hijra na kuwacha Wanafunzi wake wakuu wawili ambao ni Imam Hafs Ibn Sulayman Al Asadi na Imam Shu'bah Ibn 'Ayyash Ibn Salim Al Hannat Al Asadi Al Kufi.

Ambapo kwa upande wa Imam Shu'bah basi tumeshaiangalia historia yake na kwa upande wa Imam Hafs basi yeye alikua ni kijana alielelewa na Imam Asim mwenyewe kwani alikua ni mtoto wake wa kambo na alikua pia ni mtaalamu mzuri wa Qiraa lakini hakua ni mzuri katika Ilm ya Hadith pia.

Ambapo Imam Adh Dhahabi anasema kuhusiana nae kua : '**Hafs alikua ni mwenye kuaminika kwenye Qiraa chake na umakini wake, lakini hakua mzuri kwenye Hadith**' na Hafs hakua ni mtu mwenye kuachana aina ya kisomo cha Mwalimu wake

Asim isipokua kwa herufi moja tu katika *Surat Rum* aya ya 54 ambapo Hafs hua anasoma *Dhu**AAfin*** wakati ambapo Asim hua anasoma *DhaAAfin* katika aya ifuatayo:

﴿ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَكُم مِّن ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِن بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةٍ ثُمَّ جَعَلَ مِن بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفاً وَشَيْبَةً يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ وَهُوَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْقَدِيرُ﴾

Allahu alladhee khalaqakum min dhaAAfin thumma jaAAala min baAAdhi dhaAAfin quwwatan thumma jaAAala min baAAdi quwwatin dhaAAfan washaybatan yakhluqu ma yashao wahuwa alAAaleemu alqadeeru *(Surat Rumi 30:54)*

Tafsir: ***Allah ndie ambae aliekuumbeni nyinyi katika hali ya udhaifu na kisha akakupeni nguvu baada ya kua dhaifu, na kisha baada ya kukupeni nguvu akakupeni udhaifu na nywele zenye mvi. Yeye ni mwenye kuumba akitakacho na yeye ndie mwenye kujua juu ya kila kitu na ni mwenye uwezo juu ya kila kitu.***

Imam Hafs alifariki mnamo mwaka 180 Al Hijra.

IMAM MALIK 93 AH

Malik Ibn Anas Ibn Malik Ibn Amr Al Asbahi alizaliwa katika mji wa Madinah mwaka 93 *Al Hijr*. Wazee wake ni watu wa Yemen wanaotoka katika kabila la Asbah. Babu yake Malik Ibn Anas ambae ni mzee Malik Ibn Amr, alienda Madinah kuwasilisha malamiko yake kwa *Khalifah* wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A'nhu* kuhusu gavana wa Yemen, lakini alipofika Madinah alivutiwa na mazingira ya *I'lm* ya dini aliyaona huko, kwani alikutana na Masahaba wengi wakiwemo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A'nhu*, Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu A'nhu*, Sayyida Aishah *Umm ul Mu'minina Radhi Allahu A'nha*, Talha na wengineo. Hivyo alitafuta *I'lm* na alipoipata akaanza pia kusomesha, kitu ambacho kiliirahisishia familia yake kujua mambo mengi kuhusiana na Dini ya Kiislam.

Baba yake Malik ambae alikua akiitwa Anas alikua na watoto wawili, An Nadhir Ibn Anas na Malik Ibn Anas. An Nadhr alikua ni mwingi wa *I'lm* kiasi ya kua wakati Malik anatafuta *I'lm*, basi watu walikua wakimwita Malik kwa jina la '*Ndugu yake An Nadhr*' jina ambalo lilibadilika baada ya Malik kujulikana zaid kutokana na uwezo wake wa *I'lm*, na hivyo watu wakaanza kumwita An Nadhr mwenyewe kwa jina la, '*Ndugu yake Malik*'.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Malik alihifadhi *Qur'an* akiwa bado na umri mdogo baada ya hapo akawa anatafuta *I'lm* ya *Hadith* na *Fiqh*. Mama yake Malik alimsimamia mtoto wake katika kutafuta *I'lm* kwa kumchagulia aende kwa nani na nani ndio anatakiwa akasome. Kwani alimpeleka akasome kwa Rabiah Ibn Abd Al Rahman na kumwambia kua **'Jifunze tabia zake kwanza kabla ya kujifunza lolote lile kutoka kwake'**.

Halafu akampeleka kwa Sayyib Ibn Al Musayib, kisha kwa Al Zuhri, kwa Imam Jafar As Sadiq, kwa Abu Az Zinad, kwa Yahya Ibn Said Al Ansari na Abdurahman Ibn Hurmuz. Wakati *Amir ul Mu'minin* Umar Ibn Abd al 'Aziz anatawala Imam Malik alikua na umri wa miaka kumi. Imam Malik hakusoma *Qur'an* na *Hadith* tu bali pia alisomea hukmu zilizowahi kutolewa na Masahaba na *Tabi'ina* na waliofuatia baada yao.

Imam Malik alipokua tayari ameshafikia kiwango cha kusomesha, aliwauliza Wanazuoni wa Madinah wapatao 70 kama kiwango cha kusomesha ameshakifikia au la, kama anavyosema mwenyewe, '**Sikuanza kusomesha hadi pale nilipopata ridhaa ya Wanazuoni wafikao 70 kua sasa hivi ninao uwezo wa kusomesha.**'

Alipoanza kusomesha alikua akipenda kukaa alipokua akikaa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A'nhu* katika Masjid Nabai na pia aliishi katika nyumba aliyokua akiishi A'bd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu A'nhu*, hivyo alikua amezungukwa na mazingira ya Masahaba katika kuishi kwake, kusomesha kwake na hata makazi pia. Imam Malik alikua hatoi Fatwa wala hatoi jibu kwa kitu ambacho hakijui au hana uhakina nacho, na alikua akisema '**Hamna kitu rahisi katika kua Mwanazuoni, kila kitu ni kigumu hususan ukiangalia kua kuna maswali ya kujibu mbele ya Mola wako kesho Akhera**'

Kiasi ya kua safari moja kulitokea mtu wa Morroco ambae alikuja Madinah kwa Imam Malik na kumwambia '**Nimetumwa na watu wangu nije nikuulize suali, mimi natoka Morroco na imenichukua miezi sita hadi kufika kwako**'. Imam Malik alimsikiliza yule mtu na swali lake kisha akamwambia '**Mwambie aliekutuma kua sina ujuzi na *I'lm* ya kutosha ya kukujibu swali hili**'.

Yule mtu akamuuliza **'Sasa jee ni nani atakaeweza kulijibu? Kwani huko nilikotoka watu wanasema hamna mwenye *I'lm* zaid yako**' Imam Malik akajibu '**Yule aliepewa *I'lm* ya kulijibu, mimi sina uwezo wa kulijibu swali hili**'.

Imam Malik alikua na kumbukumbu nzuri sana, kama alivyo msifu Mwalimu wake Al Zuhri kwa kusema:'**Malik ni chombo kikubwa cha *I'lm***' na Mwanafunzi wake Imam Al Shafi'i pia alisema '**Unapozungumzia masuali ya *Hadith* Imam Malik hua ni nyota kali inayong'ara sana.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Malik aliandika na kuchapisha kitabu cha *Fiqh* na *Hadith* kinachoitwa *Al Muwwata*. Kabla kuandikwa kitabu hiki, Wanazuoni walikua hawaandiki vitabu bali walikua wanategemea akili zao, na hujiandikia wakati mwengine ili wasiyasahahu waliyoyahifadhi hivyo hawaandiki kwa ajili ya watu wengine. Hivyo Imam Malik aliandika na kuchapisha *Al Muwwata* ndani yake mkiwa na mpangilio wa masuali tofauti ya *Fiqh,* zikiwemo *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, kauli za Masahaba na pia makubaliano ya Wanazuoni na mawazo yake yeye katika masuala ya *Fiqh* ili watu mbalimbali wanaojua na wasiojua waweze kukitumia katika masuali ya *Fiqh*.

Ama kuhusiana na muonekano wake, basi Isa bin 'Umar alisema: '**Sikuwahi kuona kitu chochote cheupe au chekundu ambacho ni kizuri zaid kuliko uso wa Malik, na sikuwahi kuona nguo nyeupe kuliko zake.**'

Watu wengine pia walisema Malik alikua mrefu, mkakamavu, mwenye nywele, sharubu na ndevu nyeupe. Muhammad Ibn Dahhak Al Hizami alisema: '**Nguo za Malik zilikua safi na laini**'. Ashhab akasema: '**Malik alikua akivaa kilemba alichokua akikipitisha chini ya kidevu chake na upande mmoja huuachia mgongoni kwake, hua ananukia harufu ya kuvutia ya mafuta mazuri**'

Imam Malik alikua akiitwa *Dar Al Hijr* kwa sababu hajawahi kuhama Madinah, alizaliwa Madinah, alikulia Madinah na alifariki katika mji wa Madinah, hajawahi kutoka nje ya mji wa Madinah ila kwa kuenda Makkah wakati wa Hija, mwenyewe alikua akisema kua anaupenda sana mji wa Madinah. Imam Malik aliishi kimasikini, alikua akifanya biashara yenye mtaji mdogo na alipoanza kujulikana kwa *I'lm* yake alianza kupata malipo yake kutoka kwa *Khalifah*, alikua akitumia chote kile anachokipata sio kwa familia yake tu bali kwa Wanafunzi wake pia.

Imam Malik alikua na msimamo kua *Khalifah* lazima achaguliwe kupitia kwa *Ijma'a*, na hata kama hakuchaguliwa kisheria inabidi atiiwe ikiwa atatawala kwa haki na *Sharia'h*, na akiwa ni dhalim basi haikubaliki kuanzisha uasi dhidi yake kwani uasi huo utasababisha maafa na dhulma kubwa zaidi kwa watu wake. Hivyo mtizamo wake ni kua dhalim anatakiwa ashauriwe kwa dhati pale itakapopatikana nafasi.

Baadhi ya watu walikua wakimuuliza Imam Malik, kuhusu mambo ambayo hayajawahi kutokea, na alikua hapendi kuulizwa maswali hayo na kusema kua haina haja ya kuuliza mambo ambayo hayajatokea bado. Imam Malik na Imam Abu Hanifa, walikua wakikutana wakati wa Hija. Kabla ya kukutana Imam Malik alikua akisema '**Kaa mbali na watu wa Rai**'.

Skuli ya Imam Abu Hanifa ilikua inaitwa Skuli ya Rai kwa sababu ya kutumia Rai sana katika *Fiqh* yao. Mwaka mmoja katika Hija wakakutana Imam Malik, Imam Abu Hanifa

na Imam Al Layth, hivyo wakaamua kuzungumzia masuala matatu waliyotofautiana kati ya *Fiqh* za Madinah na Iraq. Jambo la kwanza ilikua ni kuhusu mambo ya kesi ambazo hazijawahi kutokea. Jambo ambalo ingawa katika *Fiqh* ya Imam Malik hawafuatilii masuala hayo lakini kwa Abu Hanifa walikua wakifuatilia na kuyafanyia uchunguzi.

Imam Malik alikua akisema hatuwezi kukaa tukafikiria kesi ambazo hazijawahi kutokea, kwanza hazina maana na pia kufanya hivyo kutawaondoa watu katika kufikiria jinsi ya kutatua mambo waliyokua nayo hivyo kutatokea mifarakano. Imam Malik alitoa ushahidi wake kutoka katika *Qur'an 2:189* isemayo:

﴿يَسْأَلُونَكَ عَنِ ٱلأَهِلَّةِ قُلْ هِىَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ﴾

Yas-aloonaka AAani al-ahillati qul hiya mawaqeetu lilnnasi *(Surat Al Baqara 2:189)*

*Tafsir: '**Wanakuuliza kuhusu miezi mpya Sema, hiyo alama ni alama kwa ajili ya kuweka nyakati kwa Bani Adam**.*

Akatoa ushahidi kutoka kwa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A'nhu* aliwaambia wale waliokua wakiuliza maswali hayo kwa kuwaambia '**Msiulize mambo ambayo hayajatokea, na badala yake fanyeni yale mambo yaliyopo**'

Imam Abu Hanifa alikua akibuni masuala ambayo hayajawahi kutokea. Alibuni kesi karibu 60,000. Hivyo alipokutana na Imam Malik, Imam Abu Hanifa akamwambia Imam Malik kua maisha na mazingira ya Iraq ni tofauti na yale ya Madinah. Iraq ni makao makuu ya *Ukhalifa* hivyo kila siku hutokea kesi za aina mpya ambazo hazijawahi kutokea kabla yake, hivyo inabidi kila wakati wawe tayari kujua nini wafanye inapotokea kesi aina fulani. Lakini Madinah hamna matatizo kama hayo.

Abu Hanifa akatoa mfano alipokaa na kujadiliana na Wanafunzi wake kuhusu mwanamke ambaye mumewe amesafiri na akachelewa kurudi kwa mda mrefu na hamna mawasiliano yeyote baina yao, kiasi ya kua mwanamke akafikiria mumewe amefariki, hivyo akaamua kuolewa na mtu mwengine. Halafu ghafla mume aliesafiri akarudi. Jee itakuaje? Imam Abu Hanifa akasema Madinah kesi hizi zinaweza zisitokee lakini Iraq zinaweza kutokea kwa sababu askari hua wanaenda vitani na mambo kama hayo huweza kutokea. Hivyo inabidi wajitayarishe kuyatatua. Hapo Imam Malik akakaa kimya.

Imam Abu Hanifa akamkumbusha alivyosema Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* wakati alipokuja mtu kwake na na kumuuliza '**Fikiria ikiwa atakuja mtu na akataka kunipokonya pesa zangu, jee nifanyeje?**' Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* akamwambia usimpe.

Yule mtu akauliza ‘**Fikiria, na ikiwa atapigana nami?**’ Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* akamwambia pigana nae, yule mtu akauliza tena ‘**Fikiria kama akiniuwa?**’, Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* akamwambia utakua umekufa Shahidi, yule mtu akauliza tena ‘**Na nikimuua mimi?**’ Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* akamwambia mtu huyo : ‘**Atakua ni mwenye kuingia Motoni**’. Abu Hanifa akasema Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* ameulizwa maswali ambayo hayajatokea mara nne!.

Imam Malik akajibu lakini ilikua ni kwa sababu maalum, Imam Abu Hanifa akajibu nasi tunafanya hivyo kwa sababu maalum. Hapo Imam Al Layth akasema ‘***Subhana Allah*! Mnastawisha Uislam**’. Hivyo Maimam wote wakakubaliana kua kila mmoja afanye anavyofanya kuhusu hilo lakini kwa manufaa ya Uislam.

Jambo la pili walilozungumzia lilikua kuhusu *Ijma’a* au makubaliano. Kiislam ili kupata ufumbuzi wa kitu chochote kile, unaangalia kwenye *Qur’an*, kama hamna unaangalia katika *Hadith* na kama hamna unaumia *Sharia’h* waliokubaliana *Ijma’a* ya Wanazuoni. Imam Malik anaamini kua *Ijma’a* iwe ya watu wa Madinah tu kwa sababu Madinah, ndio mji wa wa Masahaba na wake wa Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* waliishi na kufia hapo pia, wao ndio ambao waliona mambo mengi ya Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam*. Madinah kulikua na takriban Masahaba 10000.

Kuna mtu alikuja kumuuliza Imam Malik kuhusu mambo fulani fulani, Imam Malik akamwambia ‘**Angalia walivyofanya watu wa Madinah. Na ukiikuta jua kua huo ndio uhakika**’ kisha akamwambia mwengine ‘**Unaweza kupata *I’lm* Madinah kwani *Qur’an* haijashushwa katika mto wa Euphrates (Iraq)**’.

Ingawa Imam Abu Hanifa alikua mkubwa kuliko Imam Malik, lakini alikua akimheshimu sana Imam Malik. Hivyo akamjibu Imam Malik, ‘**Malik, wakati wa utawala wa Umar Ibn Al-Khattab *Radhi Allahu A’nhu* aliwatawanya Masahaba kila sehemu. Unasema kua Madinah kulikua na Masahaba 10000. Katika vita vya mwisho alivyopigana Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* kulikua na Masahaba karibu 120,000 jee hao wengine waliobakia wameenda wapi? Huwezi kukataa kua Umar Ibn Al-Khattab *Radhi Allahu A’nhu* aliwatawanya Masahaba ili kuwapa *I’lm* watu wengine**.’

Imam Abu Hanifa akaanza kuwatathmini Masahaba akiwemo Mua’dh Ibn Jabal ambae Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* alisema kua ni mwenye *I’lm* zaid na akampeleka Yemen. A’bd Allah Ibn Masud ambae usomaji wake wa *Qur’an* ulipendekezwa kwa watu, akamtaja Abu Dhar, Zubair Ibn Al Awam, na Saad Ibn Al Waqas waliokwenda Misri. Hudhayfah Ibn Yaman, A’bd Allah Ibn Masoud, Ali Ibn Abu Talib waliokwenda Iraq. Abu Ubaydah Ibn Jarah, Bilal na Abu Darda waliokwenda Syria n.k.

Kisha akasimulia *Hadith* ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* pale aliposema Masahaba wake ni kama nyota ambazo huwaongoza watu. Akasema ustadi wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu A'nhu* ndio uliowatawanya Masahaba wengine sehemu tofauti duniani, na akawaacha wengine Madinah ili kuweka usawa. Hivyo kutawanywa huko kwa Masahaba ilikua ni kwa ajili ya manufaa ya kuushikamanisha Ummah wa kiislam. Al Layth akasema, '**Ya Allah, Hii pia ni kwa ajili ya Kuushikamanisha Ummah**.'

Jambo la tatu walilolizungumzia likua ni kuhusu mawazo juu ya tafsir ya *Hadith*. Imam Abu Hanifa hutanua tafsir ya maana ya *Hadith* hadi kufikia kutoa mafunzo 100 katika *Hadith* moja. Imam Malik alikua akiona jambo hili ni la kutoa maana 100 katika hadith ni kukuzisha mno kitu ambacho hakifai. Imam Abu Hanifa Akajibu kua katika maeneo ya Iraq, Ugiriki, Rumi na Uajemi, I'lm za Falsafa na Sayansi zinawavamia na kuwashambulia watu kiakili hivyo inabidi atafute njia ya kuwaweka watu katika njia iliyonyooka ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*.

Lakini Madinah hamna watu wengine isipokua Masahaba na wafuasi wao. Hivyo kwa Madinah haina haja ya kuitanua tafsir na maana ya *Hadith*. Al-Layth akasema, '**Hii pia ni kwa ajili ya Mshikamano wa Kiislam**'. Hivyo Maimamu wote wakapongezana.

Baada ya Maimam wote kuagana Imam Al Layth akamfuata Imam Malik ambae alisema '**Ya Allah! Abu Hanifa kanitoa jasho, Hakika yeye ni Mwanafiqh wa kweli, sikuwahi kumuona mtu ambaye anajadiliana kama vile, kwani akikuambia chuma hiki kimetengenezwa kwa dhahabu basi atakuthibitishia**', na Imam Abu Hanifa alimwambia Imam Al Layth walipokutana baadae kua, '**Nimefanya mjadala na watu zaid ya mia, lakini sikuwahi kukutana na mtu anaekubali ukweli haraka kama Malik**'

Kilichotokea baada ya hapo Imam Abu Hanifa alimpeleka mtoto wake Hammad, Madinah ili akajifunze *Fiqh* ya Imam Malik na kitabu chake cha Al Muwwata na Imam Malik akataka apelekewe vitabu vya *Fiqh* ya Imam Abu Hanifa ili anufaike navyo.

Siku moja Imam Malik aliulizwa '**Jee Allah ataonekana katika siku ya Kiama?**' Imam Malik akajibu **'Naam kwani Allah anasema:**

﴿وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ﴾

Wujoohun yawma-idhin nadhiratun *(Surat Al Qiyama 75:22)''*

*Tafsir:'**Na baadhi ya uso zitang'ara katika siku hiyo (kwa kumuona Mola wao) .***

Ibn Naafi na Ash-hab wakauliza '**Watamuangalia Mola wao?**' Imam Malik akajibu '**Naam, kwa macho yao mawili**', hapo mmoja wao akasema '**Kuna watu wanasema kua Allah hawezi kuangaliwa, na kua maana ya kumuangalia ni kutegemea malipo**', Imam Malik akasema '**Wamesema uongo, kwani Allah ataonekana!**'

Imam Malik alikua na kawaida ya kua kila siku lazima atumie saa moja ya muda wake kwa ajili ya kua pamoja na Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Na ingawa Masahaba hao walikua wameshafariki miaka kabla kuzaliwa kweke, lakini yeye alikua akiwatafuta kwa kujitengenea nafasi kwa ajili ya kua nao pamoja kwa kusoma habari zao kupitia katika vitabu vyao na pia vitabu vya Wanafunzi wao, kwani hii ilikua inamzidishia ari yakufanya mema zaid.

Imam Malik alisomesha Wanafunzi wengi wakiwemo Imam Al Shafi'i, Muhammad Ibn Hasan Ash Shaibani ambae pia alikua Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa, Abdu Rahman Ibn Qasim Al Misri. Imam Malik alifariki mwaka 179 *Al Hijr* akiwa na miaka 86. Akiwacha watoto watatu wa kiume ambao ni Yayha, Muhammad na Hammad.

IMAM AL LAYTH IBN SAAD 94 AH

Imam Al Layth Ibn Saad Ibn Abdul Rahman Al Fahmi alizaliwa katika mwaka 94 *Al Hijr* katika maeneo ya Qarqashanda, eneo ambalo liko umbali wa kilomita 22 kutoka katika mji wa Fustat nchini Misri. Imam Al Layth alisoma kwa Mwanafunzi wa Sahaba A'bd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* ambae ni Muhammad Ibn Muslim Ibn Ubayd Allah, Ibn Shihab Al Zuhri, Ibn Ajlan, Ata Ibn Rabah, Ibn Abi Malika, Naafi', Ad Daylami na wengineo wengi.

Imam Al Layth Ibn Saad alikua ni mwenye kupenda sana kutafuta Ilm kiasi ya kua hadi alipokua na umri 65 alielekea katika Mji wa Baghdad na alipofika akaulizia ilipo nyumba ya Imam Hisham Ibn Bashir ambae alikua na Ilm kubwa ya Hadith miongoni mwa Wanazuoni wa Baghdad, na kisha akamuomba vitabu vyake alivyokua navyo ili apate kusoma, na bila ya shaka alipopewa alivisoma vyote na kisha akawa ni mwenye kutoa Darsa katika Mji wa Baghdad na akapata umaarufu mkubwa sana kwenye Mji huo.

Alisema Imam Al Shafi'i, '**Al Layth alikua na *I'lm* kubwa ya *Hadith* kuliko Imam Malik, lakini Wanafunzi wake waliitupa *I'lm* yake**'. Imam Al Layth alikua anaitwa Imam Mkuu wa Misri. Watu wa Misri walikua wakiacha kutii amri za *Khalifah* Mansour, lakini wakawa wanatii amri za Imam Al Layth, kiasi ya kwamba *Khalifah* Mansour alitaka kumteua awe Gavana wa Misri lakini Al Layth akakataa.

Imaam Al Layth alisifika kutokana na Wanazuoni wenzake kua alikua mjuzi wa *Hadith* na anaeaminika katika *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*. Na aliporudi katika Mji wa Misri basi alianza darsa yake kwa kuwasomesha watu msikitini. Na mara akawa maarufu sana na Wanafunzi wake walikuja kutoka sehemu tofauti za Dunia kuja kwake kusoma. Alikua akiigawa siku yake katika sehemu nne:-

- Kipindi cha kuzungumzia mambo na vitendo vya Viongozi wa Misri. Imam Al Layth alikua akiheshimika na kuaminika kwa *Khalifah* kiasi ya kua kama Sultan au Hakim wa Misri atafanya kosa kisha Imam Al Layth akamtaarifu *Khalifah* kuhusu kosa hilo basi kiongozi huyo husimamishwa kazi.
- Darsa ya kusomesha *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam.*
- Darsa ya kujibu maswali ya Dini.
- Kipindi cha kuwahudumia matatizo ya maskini na wenye shida. Imam Al Layth alikua hakatai kutoa msaada.

Imam Al Layth Ibn Saad alikua pia ni miongoni mwa Walimu wa Imam Al Shafi'i kupitia kwa Wanafunzi wake. '***I'lm* ipo chini ya misingi mitatu. Imam Malik, Imam Al Layth na Imam Sufyan Ibn Uyaynah**' alisema Imam Al Shafi'i. '**Al Layth ana kiasi kikubwa cha *I'lm* (*Kathir Al I'lm*) na *Hadith* zake ni Sahihi**', alisema Imam Ahmad Ibn Hanbal, na Al 'Alaa Ibn Kathir alisema; '**Al-Layth Ibn Sa'd ni kiongozi wetu, Imam wetu na Mwanazuoni wetu.**'

Hivyo Imam Al Layth Ibn Saad alikua ni Imam Mkuu wa Fiqh na Hadith wa ardhi ya nchi ya Misri ambapo anasema Imam As Sudfi kua: '**Mimi nilishuhudia Jeneza la Imam Al Layth Ibn Sad nikiwa pamoja na Baba yangu. Na sijawahi kuona Jeneza la maiti kama huyo kwani niliona watu wote wakiwa ni wenye huzuni na walikua wakipeana pole huku wakilia, nami nikamwambia Baba yangu: 'Ewe Baba yangu mbona inaonekana kua kama hili Jeneza ni la Maiti wa kila Mtu?' Baba yangu akaniambia kwa kusema kua: 'Ewe Mtoto wangu, hakika hutowahi kuona Jeneza kama hili tena'**'

Miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Shuayb, Imam Muhammad Ibn Ajlan, Imam Hashim Ibn Bashir, Imam Qasi Ibn Rabii, Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Marwan Ibn Muhammad, Imam Abu Walid Ibn Muslim, Imam Amr Ibn Khalid Al Haraani, nk.

Muhammad Ibn Muawwiyah anasema kua: '**Nilimuona mimi Imam Al Layth siku moja alipokua ametoka nje na kusimama huku akiwa amevaa ngu, na Kipando chake na Pete ambapo vyote vilikua na thamani ya takriban dirham 18000**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Mbali ya kua ni mwenye kupendeza kimavazi lakini pia Imam Al Layth Ibn Sad alikua ni mkarimu sana kwani siku moja alikuja kwake Mama mmoja ambae alilalamika kwa kusema: ‘**Ewe Abu Harith mimi nna mtoto ambae anaumwa na anahitaji Asali.**’ Imam Al Layth Ibn Saad akaamrisha mfanyakazi wake kwa kumwambia: ‘**Mpe Lita 50 za asali**’

Na anasema Imam Asad Ibn Musa kua: ‘**Mimi niliingia kwenye mji wa Al Qahira ambao ulikua chini ya Mmalaka mapya na nikaenda kujitafutia Ilm yangu kwa Imam Al Layth, na baada ya kumaliza na kutaka kuondoka, basi mfanyakazi wake akanifuata na kuniambia: ‘Subiri hapahapo usiondoke mpaka nije’ hivyo nikakaa na kusubiri, hadi ikawa nimebakia peke yangu na kisha mfanyakazi huyo akaja akanipa bahasha ambayo ndani yake mlikua na Dirham 1000’**

‘Mfanyakazi huyo akasema: ‘Imam Al Layth amesema kua tumia hizi pesa kwa ajili ya mahitajio yako.’ Nami nikasema: ‘Mimi ni mwenye uwezo na hivyo siwezi kupokea pesa hizi, hivyo naomba kuonana nae tena Imam Al Layth’ nikaruhusiwa na kuonana nae na Kujitambulisha ukoo wangu na kisha nikamwambia: ‘Samahani kwani mimi siwezi kuchukua hizi pesa ni nyingi sana, hivyo inabidi nikurudishe ili nipate niondoke’ Imam Al Layth akaniambia: ‘Hii ni zawadi sio Sadaka kwako.’

Nami nikasema : ‘Kutokana na hali yangu basi mimi ni mtu nnachukia kurudi Nyumbani ikiwa na kiasi hiki cha pesa’ Imam Al Layth Ibn Saad akasema: ‘Chukua halafu igawe kwa wale ambao utaona kua wanastahiki kupata kutokana nazo miongoni mwao’ na nilipokataa basi Imam Al Layth akanisisitizia hadi ikabidi nizichukue na kuenda kuzigawa kwa wanaostahiki.’

Na anasema Harmalah Ibn Yahya kua: ‘**Mimi nilimsikia Wahb akisema: ‘Malik alimuandikia Al Layth huku akisema: ‘Nataka kumuozesha Binti yangu hivyo nilikua nahitaji Mauwa’’ hivyo Imam Layth Ibn Saad akamtumia Malik Maua 300 ambayo alitumia na mengine yakabakia na kuyauza kwa Dinari 500.**’

Imam Adh Dhahabi anasema kua: ‘**Imam Al Layth alikua ni Mufti wa Misri, Mwanahadithi na kiongozi mwenye upekee, miji mingi ya Misri ilikua ikijivunia juu yake, kwani alikua akiaminika, alikua ni Qadhi na kiongozi wa juu ambapo viongozi wengine wote walikua chini yake wakitegemea maamuzi yake na mitizamo yake, Al Masur alitaka kumpa Mamlaka ya Ardhi ya Misri lakini Imam Al Layth akakataa’**

Ambapo anasema Abu Walid kua: ‘**Mimi nilimsikia Baba yangu akisema kua: ‘Hakika mimi sijawahi kuona Mtu alietimia kisifa kama Imam Al Layth kwani**

alikua ni *Al Faqih* mwenye Ilm kubwa sana kiasi ya kua mpaka damu yake ikimwagika basi ndani yake itaonekana Ilm yake, alikua ni mtaalamu mkubwa wa Lugha, Mtaalamu mkubwa wa Qur'an na Balagha na Hadith, na Mashairi na Ilm ya mengineyo.''

Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema kua: '**Imam Al Layth alikua na Ilm kubwa sana na Hadith zake ni Sahih'**

Imam Al-Layth alifariki siku ya Ijumaa katikati ya mwezi wa Shaaban mnamo mwaka 175 Al Hijr na alizikiwa Mjini Al Qahira, Misri.

IMAM AL AYYASH 95 AH

Imam Abu Bakr Ibn Ayyash Ibn Salim Al Asadi Al Kufi alizaliwa katika Mji wa Kufah mnamo mwaka 95 Al Hijra. Imam Al Ayyash alisoma kwa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*, Imam Asim, Imam Abu Is-haq Al Subai, Imam Al Amash, Imam Al Muradi Ibn Mutamir, Imam Hisham Ibn Urwa n.k

Na hivyo Imam Al Ayyash alikua ni mwenye Ilm kubwa ya Qur'an, Hadith na Fiqh, na alikua Mcha Mungu mkubwa sana, ambapo anasema Imam Abu Bakr Ibn Ayyash kua: **'Mimi nimesoma Qur'an mara tano kutoka kwa Asim, na sikusoma kwa mtu wengine yeyote yule'**

Abu Bakr Ibn Ayyash akasema tena: '**Kuna mtu aliniambia mimi nilipokua Mdogo: 'Ewe Kijana iokoe shingo yako kwa kadiri utakavyoweza kutokana na Dunia hii dhidi ya utumwa wa Kesho Akhera, kwani Mtumwa wa kesho Akhera hua hana wa kumuombea na hivyo hatoachiwa huru' hivyo nami kamwe sikuwa ni mwenye kuyasahau maneno hayo.**'

Na akasema Al Hafidh Yaqub Ibn Shaybah kua: '**Abu Bakr alikua akijulikana kutokana na Ucha Mungu wake, Ustadi wa kusoma Qur'an na Fiqh**'

Ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Ahmad Ibn Hanbal kua: **'Baba yangu aliniambia mimi kua: 'Nilimuona mimi Abu Bakr Ibn Ayyash katika mji wa Kufah katika siku ya Ijumaa, ambapo alikuja Msikitini akiwa amepanda Punda. Akashuka kisha akaelekea kwenye moja kati ya Nguzo za Msikitini hapo, na akasimama tuli na kusali, kisha baada ya kumaliza akaukunja mkono wa shati lake nami nikauona mkono wake ambao ulikua hauna kitu isipikua Mfupa, hivyo**

nikashangazwa na subra yake katika kusimama kwake katika sala kutokana na udhaifu wa mwili wake’’

Na alisema Imam Al Ayyash kua: ‘**Manufaa ya chini kabisa ya Kukaa kimya hua ni kukupa Usalama, na hua kunatosheleza kukupa na Afya, na na madhara ya chini kabisa ya usemaji hua ni Umaarufu na hutosheleza kutokanna na maamngamizo yake.’**

Anasema Imam Imam Sufyan Ibn Uyaynha kua: ‘**Aliniambia mie Al Ayyash kua: ‘Nimeiona mimi Dunia kwenye usingizi wangu kua ni Mwanamke mzee sana aliekua na sura mbaya sana.**’’

Ambapo Imam Abd Allah Ibn Mubarak amesema kua: ‘**Sijawahi mimi kuona mtu anaekimbilia haraka sana katika kufanya mambo ya Sunnah kama Abu Bakr Al Ayyash**’

Ambapo anasema Yahya Ibn Said kua: **‘Mimi nilienda kwenye Mji wa Makkah pamoja na Abu Bakr Al Ayyash na yeye ilikua hakuna mcha Mungu kama yeye na ni mwenye uaminifu mkubwa.’**

Imam Al Ayash alikua si mtu mwenye kudumu na *Qiyam Al Layl* kiasi ya kua hakuwahi kuuweka ubavu wake kwenye Kitanda katika wakati wa usiku hata mara moja ndani ya miaka 40 kwani alikua akisema kua: **‘Yeyote yule anaeuhuisha Usiku wake hua ni mtu asiefanya maovu, hivi kwani jee hamjasikia nyinyi maneno ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* yasemayo:**

﴿ٱتْلُ مَا أُوحِىَ إِلَيْكَ مِنَ ٱلْكِتَابِ وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ
ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ وَلَذِكْرُ ٱللَّهِ أَكْبَرُ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ﴾

Otlu ma oohiya ilayka mina alkitabi waaqimi alssalata inna alssalata tanha AAani alfahsha-i waalmunkari waladhikru Allahi akbaru waAllahu yaAAlamu ma tasnaAAoona *(Surat Al Anqabut 29:45)’*

Tafsir: ***Wasomee kile ambacho umeshushiwa (Ewe Muhammad) katika Kitabu na simamisha Sala, kwani kwa hakika Sala ni yenye Kuzuia Maovu na Dhikr Allah ni bora zaidi, na Allah ni mwenye kujua juu ya kila mnachokifanya.’***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Al Ayyash alisema: **‘Kama mtu akinidanganya Mara moja basi mimi sitomsikiliza tena Mtu huyo.**’

Wenye kumjua walikua wakisema kua : ‘**Abu Bakr Al Ayyash hajakuzidini nyinyi chochote katika Kusali kwake wala kufunga kwake bali amekuzidini nyinyi katika kile alichohifadhi ndani ya Kifua chake**’

Imam Al Ayyash alifariki mnamo mwaka 193 Al Hijra akiwa na umri wa miaka 98 ambapo anasema mtoto wake aitwae Ibrahim Ibn Abi Bakr Ibn Ayyash kua: **‘Mimi nililia wakati kifo kilipokua kinamkaribia baba yangu ambapo nae akasema: ‘Kwanini unalia? Huoni kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* amenipa miaka 40 baada yako kwa ajili ya kuimaliza kuisoma katika Qur’an kila usiku?’**

Ambapo kwa upande mwengine basi Dada yake Imam Al Ayyash pia alikua analia na hivyo Imam Al Ayyash akamwambia Dada yake huyo kua: **‘Usilie kwani Kaka yako alikua akimaliza Kisomo cha Qur’an kwenye Pembe ile pale ya Nyumba hii mara 18000’**

Miongoni mwa Wanafunzi wake Imam Ayyash ni pamoja na Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Yahya Ibn Muin,Imam Is-haq Ibn Rahwayh, Imam Abu Dawud, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Abu Bakr Ibn Abi Shaybah, Hannad n.k.

Amesema Haytham Ibn Harith kua: ‘**Mimi nilimuona Abu Bakr Ibn Ayyash katika ndoto yangu, huku mbele yake kukukiwa kuna sahani ya Tende’** ambapo nami nikasema: **‘Ya Abu Bakr Unajua kua mimi nnapenda Tende, hivyo kwanini hunialiki?’** ambapo nae akasema: ‘**Ewe Haytham hizi ni Tende za Watu wa Peponi, hivyo wewe ulie Duniani huwezi kula’**

Nami nikamuuliza: **‘Uliifikiaje Darja hio?’** ambapo nae akajibu: **‘Ni kwa sababu mimi sikuwahi hata siku moja katika maisha yangu kuupitisha Usiku wangu bila kusoma Qur’an.’**

Anasema Bishr Ibn Harith kua**: ‘Mimi nilimsikia Abu Bakr Al Ayyash akisema: ‘Enyi Malaika Kiraman Katibin wa kulia na kushoto kwangu, nakuombeni mniombee kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* anisamehe, kwa sababu kwa hakika nyinyi ni wenye Kumtii yeye zaidi yangu na bora zaidi yangu na ni wenye kutekeleza maamrisho yake’’**

Alisema Imam Al Ayyash kua: **'Viumbe wako wa aina 4, aina ya kwanza ni ya Wanyama, ambao kutokana na kua hawana Ufahamu, basi hawakupewa Majukumu ya Makatazo na Maamrisho na *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yao.**

Aina ya Pili ni Wale walioingizwa kwenye kupewa Mitihani ambao ni Ibn Adam, ambao wao wataulizwa juu ya kila kitu chao walichokifanya hapa Duniani na watalipwa malipo yao kutokana na yale waliyofanya.

Aina ya Tatu ni Malaika ambao wao ni wenye Jukumu la Kumuabudu *Allah Subhanah wa Taa'ala* tu, wao hawaasi na hivyo hawana Dhambi.

Aina ya Nne ni Ibilisi ambae ndie alielaaniwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ameangamia.'

Alisema Imam Al Ayyash kua: **'Manufaa madogo kabisa ya kukaa kimya hua ni kujiepusha na matatizo, na kwa kua kukaa kimya hua ni jambo jema basi humtosheleza mtu kutokana na wema wake, na Madhara madogo kabis aya kusema sana hua ni kupata umaarufu, na kutokana na adhabu yake basi umaarufu unamtosheleza mtu kiadhabu.'**

Alisema Imam Al Ayyash kua: **'Mimi nilipokua Mdogo basi kuna mzee aliniambia kua: 'Ewe Kijana jiokoe kutokana na kua Mtumwa wa Dunia hii. Ielekee Akhera yako, kwani Sad Ibn Abi Waqqas *Radhi Allahu Anhu* alikua ni kijana na mtu wa mwanzo kuachia Upinde wake kwa ajili ya kumpigani *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Alisema Imam Al Ayyash kua: **'Hakika mimi Umri wangu ni zaidi ya miaka 80. Hivi jee nitatamani nini? Kwani miaka imekuja na kuondoka na kuniacha mimi, huku ikiwa ni yenye kunimomonyoa mimi, imeikondesha Mifupa yangu na kuyafanya kua madogo zaidi macho yangu, nimekua kama kanzu ya zamani kutokana na udhaifu wangu'**

IMAM WAHB IBN WAHB

Imam Al Qadhi Abu Bakhtari Wahb bin Wahb bin Kathir Ibn Abd Allah Ibn Zama'a Ibn Al Aswad Ibn Al-Muttalib Ibn Asad Al-Qurashi Al-Asadi Al-Madani alizaliwa katika Mji wa Madina katika kipindi cha Tabii Tabiina na alisoma kwa Wanazuoni wakubwa wa Mji wa Madina akiwemo Imam Jafar Al Sadiq ambae alianza kusoma kwake baada ya kufariki baba yake na hivyo mama yake aliekua akiitwa Abdat Bint Ali Ibn Yazid Ibn Rukanah Al Muttalibiya ambae alikua ni mwenye kutokana na familia

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ya Aqil Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* ambae ni kaka yake *Amir Ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*.

Hivyo Abdat Bint Ali Ibn Yazid akaolewa na Imam Jafar Al Sadiq na hivyo Imam Wahb Ibn Wahd akapata nafasi ya kua na ukaribu sana na Imam Jafar As Sadiq na kua mtoto wake na pia Mwanafunzi wake. Imam Wahb Ibn Wahb alisoma pia kwa Imam Said Ibn Musayyib, Imam Ubayd Allah Ibn Umar,n.k na kisha baada ya hapo akaelekea katika ardhi ya Syria na miongoni mwa aliowasomesha yeye ni pamoja Imam Hisham Ibn Urwa Imam Rajaa Ibn Sahl.

Imam Wahb Ibn Wahb alikua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Qur'an, Hadith, Fiqh, Historia na Lugha ya Kiarabu. Ambapokatika kipindi cha utawala wa Khalifa Harun Rashid basi Imam Wahb Ibn Wahb alihamia katika ardhi ya Baghdad na hivyo badae akawa ni *Qadhi* mkuu wa maeneo ya Magharibi mwa Iraq na hivyo baadae akawa ni mwenye kuchukua nafasi ya *Qadhi* Abu Yusuf baada ya kufariki kwake na hivyo Imam Wahb IbnWahd akawa na cheo cha *Qadhi Al Qudhat* kuanzia mwaka 182 Al Hijra ambae aliutumikia hadi kufariki kwake mnamo mwaka mwaka 200 Al Hijra.

Ambapo anasema Imam Wahb Ibn Wahb kua: **'Hakika mimi kila siku hua ni mwenye kupenda kuapamoja na watu wenye kujua zaidi yangu katika Jamii yangu, kuliko kua pamoja na watu wasiojua zaidi yangu, kwa sababu ingawa wale wenye ndogo hua ni wenye kuweza kunufaika wanapokua pamoja nami, lakini mimi hua siwezi kunufaika nnapokua pamoja nao.'**

Ambapo amesema Imam Wahb Ibn Wahb kua: **'Amesema Imam Jafar As Sadiq kua:** '**Mambo matatu hua ni yenye kuyazidisha macho nguvu yake ambayo ni Kuangalia Mimea ya Kijani, Kuangalia Maji (ya Mito, Maziwa na Bahari) na kuangalia Nyuso zilizokua nzuri.'**

Imam Wahb Ibn Wahb anasema kua: **'Yeyote yule atakae hifadhi Hadith 40 na kuzifanyia kazi basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamjaalia kua ni mmoja kati ya Wanazuoni wa Fiqh.'**

IMAM SUFYAN ATH THAWRY 97 AH

Imam Abu Abd Allah Sufyan Ibn Said Ibn Masruq Ibn Habib Ibn Rafii Ibn Abda Allah Ibn Mauhabah Ibn Ubai Ibn Abd Allah Ibn Munqidh Ibn Nasr Ibn Al Harith Ibn Ath Thalaba Ibn Amir Ibn Mikaan Ibn Ath Thawry hivyo Imam Sufyan Ath Thawry alikua ni mtu mwenye kutokana na kabila la Ath Thawry.

Imam Sufyan Ath Thawry alizaliwa kutoka katika familia ya Wanazuoni kwani baba yake ambae ni mzee Said Ibn Masruq Ath Thawry alikua ni mwanazuoni mwenye Ilm kubwa sana, na hivyo yeye alikua ndie nguzo ya msingi wa Ilm ya Imam Sufyan Ath Thawry ambayo ilimpelekea kujulikana kama Kiongozi wa Wanazuoni wa wakati wake, na pia akawa anajulikana kama *Amir Ul Muuminin* wa Hadith.

Mbali ya kua Imam Sufyan Ath Thawry alisoma kwa Baba yake lakini pia alisoma kwa Wanazuoni wengine wakubwa wakiwemo Imam Amr Ash Shabi, Imam Sulayman Al Amash, Imam Khaitham Ibn Abd Rahman, Imam Amr Ibn Dinar, Imam Sulayman At Taymi, Imam Muhammad Ibn Al Munkadir, Imam Hisham Ibn Urwa, Imam Rabia Al Ray, na wengineo wakati akiwa bado katika umri mdogo.

Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimjaalia pia Imam Sufyan Ath Thawry ufahamu mzuri sana wa kuhifadhi kwani yeye mwenye Imam Sufyan Ath Thawry alikua akisema: '**Hakuna kitu ambacho mimi niliwahi kukitia ndani ya Moyo wangu nikakisahau, Moyo wangu kamwe haujawahi kunisaliti'**

Ambapo anasema Imam Wakii Ibn Jarrah kua: '**Siku moja Mama yake Sufyan Ath Thawry alimwambia Kijana Sufyan Ath Thawry kua: 'Ewe mtoto wangu tafuta Ilm nami nitakusimamia wewe kimaisha kwa kufuma kwangu, Ewe Mtoto wnagu utaapoandika Hadith kumi, basi jiangalie kama itakua kuna mabadiliko katika mwendo wako wa kutembea kwako, katika subira yako na katika heshima yako. Kwani kama ikiwa huoni mabadiliko basi fahamu kua Ilm yako haikunufaishi bali inakudhru badala yake**''

Hivyo Imam Sufyan Ath Thawry alikua ni mwenye wasimamizi wenye kusimamia maisha yake na kumuongoza katika njia sahih tena ipasavyo kiasi ya kua athari ya nzuri ya malezi ya kiislam kutoka kwa wazazi wake hao ilionekana mwanzoni mwa ujana wake na kumboreshea Imani yake na Ilm yake na hivyo kua ni mwenye kukubalika wakati akiwa na umri mdogo bado, kwani anasema Imam Abu Muthanah kua: **'Nilipokua katika maeneo ya Marw nilisikia watu wakinadia kwa shangwe kwa kusema: 'Ath Thawry amekuja' hivyo nami nikatoka kuenda kumuangalia na nikakutana na Kijana ambae ndio kwanza anaanza kuota Ndevu'**

Imam Sufyan Ath Thawry alikua ni Mwanazuoni mwenye kupenda kusafiri, kwani kwake yeye ilikua kila anaposikia kua kuna mwanazuoni ambae hamjui basi alikua akifunga safar kwa ajili ya kumfuata Mwanazuoni huyo ili anufake na Ilm yake. Ambapo anasema Humaid Ibn Aswad kua: '**Siku moja Sufyan aliniambia mimi: 'Tufunge safari twende zetu kwa Yunus Ibn yazidi Al Ailee' nami nikamwambia: 'Wewe huna majukumu ya kidunia hivyo nenda tu kwani mimi nna watu wanaonitegemea kwa ajili ya kuwahudumia**''

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na jitihada zake zilimpelekea Imam Sufyan At Thawry kua ni Imam ambae ni wenye Ilm kubwa sana kiasi ya kua aliwasomesha na Walimu wake pia wakiwemo Imam Al Amash, Imam Ibn Ajlan, Imam Ibn Jurayj, Imam Jafar As Sadiq, Imam Abu Hanifa, Imam Shubah, Imam Ibn Abu Dhib, Imam Al Awzaii n.k

Ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Mubarrak kua: ‘**Mimi nimenukuu Hadith kutoka kwa Wanazuoni zaidi 1100 na sijawahi kumuona mbora kati yao Wanazuoni hao kama Sufyan Ath Thawry’**

Katika kipindi cha mwezi wa Ramadham Imam Sufyan Ath Thawry alikua hafanyi amali yeyote zaid ya kusoma Qur’an.

Ambapo safari moja Imam Sufyan Ath Thawry alifuatwa na mmoja kati ya jamaa zake na kuambiwa: **‘Ewe Abu Abd Allah, kwa hakika wewe mtu unaeshangaza sana’** ambapo nae akauliza: ‘**Jee ni kitu gani kinachokushangaza ewe Jamaa yangu?’** jamaa yake huyo akajibu: ‘**Kinachonishangaza ni kua wewe hua unasafiri sana kutoka sehemu moja kuelekea sehemu nyengine, wakati Ibd Ada hua ni wenye kua Makaazi ya kufikia kujipumzisha unapoingia usiku, na hata wanyama pia lakini wewe huna’**
Ambapo Imam Sufyan A Thawry akauliza: **‘Jee alikua ni mtu gani Mughira Ibn Muqsim?’** na akajibiwa: **‘Alikua ni cha Mungu’ Imam Sufyan Ath Thaywr akauliza: ‘Jee alikua ni mtu gani Ibrahim An Nakhai?’** nae akajibiwa: ‘**Alikua ni Mcha Mungu’** Imam Sufyan Ath Thawry akauliza: **‘Jee alikua ni mtu gani Alqamah?’ Imam Sufyan At Thawry akajibiwa: ‘Usiulize kuhusiana nae kwani uthibitisho tosha’** Imam Sufyan Ath Thawry akauliza: **‘Jee alikua ni mtu gani Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*?’** yule mtu akajibu: **‘Alikua ni kigezo cha Ukweli na uamainifu.’**

Hivyo Imam Sufyan Ath Thawry akasema: **‘Naam ndivyo inavyokua kwani amesema Al Mughira, kua amesema Ibrahim kua amesema Alqamah kua amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Nuru ilimurika juu ya watu wanaoishi Peponi ambapo bado kidogo tu iwapofue macho yao watu hao, Nuru hio ilikua ni yenye kutokana na mng’aro wa Jino la Hur wa Peponi ambae alicheka wakati akiwa mbele ya Bwana wake’ hivyo huwezi wewe kunisababisha mimi na maneno yako kua ni mwenye kuachana na kutafuta Ilm kutakako nipelekea mimi kuingia Peponi.’**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak alisema pia kuhusiana na Imam Sufyan At Thawry kua: **‘Kila wakati mtu anapoelezewa kwangu mie na kisha nikamuona mtu huyo basi hua namuona kua ni mwenye muonekano tofauti kidogo kuliko na nilivyoelezewa juu yake, isipokua Sufyan Ath Thawry kwani alikua kama anavyoelezewa**.’

Imam Ayub Sakhtiyani alisema kua: '**Sijawahi mimi kuona Mwanazuoni kutoka katika Mji wa Kufah ambae nnamuona kua ni bora zaidi ya Ath Thawry.**'

Ambapo Imam Yunus Ibn Ubayd alisema kua: **'Sijawahi kuona Mtu bora zaid ya Ath Thawry' ambapo nae akaambiwa : 'Inakuaje unasema hivyo wakati wewe hukuwahi kumuona Said Ibn Jubayr, Ata, Ibrahim An Nakhai na Mujahid?' Yunus Ibn Ubad akasema: 'Bado nnaendelea kusema kua hakika mimi sijawahi kumuona mtu kama Ath Thawry**''

Imam Sufyan Atha Thawry alikua ni Imam Mwenye Taqwa sana kiasi ya kua Siku moja alienda kwa Sonara na hivyo wakati anakaa kitako akaangusha Dinari moja ya Dhahabu na hivyo akainama kwa ajili ya kuiokota lakini alipotupa macho chini basi akaona kua kuna Dinari mbili za Dhahabu, hivyo hapo hapo akanyanyuka na kuondoka bila ya kuokota hata Dinari moja kwa sababu ya kua na Khofu ya kua huenda akaokota Dinari ambayo sio yake na hivyo akawa ni mwenye kudhulumu.

Safari moja Imam Sufyan Ath Thawry alikua akitembea na mwenzake katika wakati wa Usiku na mara wakaona taa mbele yao, hivyo Imam Sufyan Atht Thawry akamwambia rafiki yake huyo: **'Ule mwangaza wa taa ni wanani?' ambapo mwenzake huyo akajibu kua ni wa Askari, basi Imam Sufyan Ath Thawry akasema: 'Tugeuze njia kwani mimi sitaki kunufaika hata na mwangaza wao.'**

Alisema Imam Sufyan Ath Thawry kua: **'Mtu yeyote yule mwenye kuipenda Dunia na kuifurahia basi hua si mwenye kua na khofu ya Akhera yake'** na alikua pia hapendi kujionesha au watu kuoneshana juu yake kwa kukhofia kua huenda akajiona ndani ya Moyo wake kiasi ya kua kama akipita njia na mbele yake akaona kua kuna watu wanamjua na kisha wataoneshana kua yule ndie Imam Sufyan Atha Thawry basi alikua akigeuza njia badala yake.

Amesema Al Hasan Ibn Utayba kua: **'Sufyan Ath Thawry alimwambia Sufyan Ibn Uyaynah: 'Mbona huzungumzi?' Sufyan Ibn Uyaynah akajibu: 'Wakati wewe uko hai, la siwezi kuzungumza''**

Imam Sufyan Ath Thawry alikua ni mwenye kuomba Dua kwa kusema: **'Ya Allah iweke hii Dunia ndani ya mikono yetu na wala usiiweke ndani ya Nyoyo zetu.'**

Kutokana na unyenyekevu wake na Ucha Mungu wake basi ilikua ukimuona Imam Sufyan Ath Thawry amekaa basi huwezi kumjua kua ndio yeye, hadi atakaposema, ndio utamjua kua ndiop yeye kutokana na maneno yake, kwani Ali Ibn Thabit alisema kua: **'Mimi nilikutana na Sufyan Ath Thawry na ilikua vigumu kumjua kua ndio yeye kutokana na muonekano wake kwani kila kitu chake kilikua hakina thamani, kiasi**

ya kua kama mtu ungeua na pesa kidogo ungempa kutokana na kudhania kua ni omba omba.'

Imam Sufyan Ath Thawry aliiahidi Nafsi yake mambo matatu ambayo ni kua: '**Hakuna mtu atakaemhudumia yeye, Hakuna Mtu atakae mkunjia Nguo zake na Kamwe hatoweka Tofali juu ya tofali jenzake juu ya ardhi**'

Imam Sufyan Ath Thawyr alikua akasema kua: '**Shughulikia Dunia yako kulingana na Mda utakaokaa ndani yake, na shughulikia Akhera yako kulingana na mda utakaokaa ndani yake'**

Ambapo amesema Imam Yahyha Al Hamaani kua: **'Kama Sufyan Ath Thawry angekua ametokana na kizazi cha Tabiina basi angekua ni miongoni mwa wenye Darja pamoja nao'**

Na anasema Ababs Ad Duri kua: **'Mimi nimemuona Yahya Ibn Muiin, ambapo alikua hakubaliani na mtizamo wa mtu yeyote dhidi ya mtizamo wa Sufyan Ath Thawry, si katika Fiqh, si katika Hadith wa si katika Zuhd na wala si kwa jambo jengine lolote lile'**

Imam Sufyan Ibn Uyaynah amesema kua: '**Mimi sijawahi kumuona mtu mwenye kujua kuhusiana na Halali na Haramu kama Sufan Ath Thawry**' na siku moja pia Imam Sufyan Ibn Uyaynah alimwambia Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Mpaka utakufa hutowahi kuona Mtu ambae ni sawa na Sufyan Ath Thawry**'

Ingawa Imam Sufyan Ath Thawry alikua anapenda kusali Sala za usiku kwani amesema ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **kua:** '**Jibril aliniambia mie kua Ewe Muhammad Fahamu kua Utukufu wa Mtu hupatikana kutokana na Qiyam Al Layl na heshima yake hutokana na kua huru kwake kutokana na kuwategemea Watu.**'

Lakini kuna kipindi Imam Sufyan Ath Thawry alikua anashindwa kuuhuisha Usiku wake kama anavyosema mwenyewe kua: '**Wallahi mimi niliharamishiwa kusali Sala za usiku kwa mda wa miezi 6 kwa sababu ya Dhambi niliyokua nimeifanya**' alipoulizwa dhambi gani basi Imam Sufyan Ath Thawry akasema: '**Nilimuona mtu akilia siku moja hivyo nami nikasema kua huyu mtu halii kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akaniadhibu.**'

Imam Abu Bakr Ibn Abu Shaibah alisema kua: '**Mimi nimemsikia Yahya Al Qattan akisema kua:** '**Sijawahi kuona mtu aliehifadhi mengi kama Sufyan Ath Thawry, na baada yake basi anaefuatia ni Shu'bah**''

Na Imam Abu Ubaidah Al Aujrii akasema kua: ‘**Kila wakati walipokua wakibishana kuhusiana na jambo baina ya Ath Thawry na Shu’bah basi mwisho wake huishia katika hali ya kua Ath Thawry alikua sahih kimtizamo. Na waliwahi kubishana katika hadith zaidi ya 50, ambapo mtizamo sahih ulikua ni ule mtizamo wa Ath Thawry**’

Anasema Imam Abu Bakr Ibn Ayaysh kua: ‘**Hakika mimi nikimuona mtu amefuatana na Sufyan Ath Thawry basi hua nnamheshimu sana mtu huyo kutokana na kua na uhusiano nae Sufyan Ath Thawry**’

Imam Ibn Muin alisema kua: ‘**Hakuna mwenye Ilm zaidi ya Hadith kama Al Amash, Mansur, Abu Is-haq na Ath Thawry**’

Imam Sufyan Ibn Uyaynah akasema pia kua: **‘Wanazuoni wa Hadith ni watatu ambao ni Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* katika wakati wake, Amr Ashabi katika wakati wake na Ath Thawry katika wakati wake’**

‘Kuwahi mapema katika Sala ya Jamaa hua ni kuiheshimu Sala ya jamaa.’

‘Jishughulishe na kukumbuka dhambi zako na hivyo hutokua na mda wa kukumbuka dhambi za wenzako’

‘Hakuna jambo gumu kwangu mie kuliko kurekebisha Nia yangu, kwani kila wakati hua ni yenye kujaribu kujibadilisha’

‘Anaewaombea wazazi wake Dua hua ni mwenye kuhesabiwa katika siku ya Malipo kua alikua ni mtoto mwema’

‘Mtu hawezi kua na ufahamu wa Dini hadi pale atakapofahamu kua wepesi hua ni Mtihani na ugumu hua ni Neema.’

Kuna mtu alimwambia Imam Sufyan Ath Thawry kua: **‘Hakika sisi hua tunawapiga watoto wetu wanaokua hawasali**’ ambapo nae akasema: ‘**La, bali unatakiwa umuhimize na kumuusia habari njema mtoto wako kutokana na Sala.’**

‘Mtu yeyote yule mwenye Mali kwenye mikono yake, basi na aitumie vizuri kwani tuko katika wakati ambao, kama mtu atapata shida basi jambo la kwanza atakalolifanya kutokana nazo ni kuitolea kafara dini yake.’

Imam Sufyan Ath Thawry alisema: **‘Enyi wenye Ilm, nyanyueni Nyuso zenu kwani njia iko wazi, fanyeni kazi na msiwabebeshe watu mizigo, kwani Mwanazuoni**

akiwa hana njia ya kujipatia riziki yake basi na atumie njia za halali katika kujipatia mahitajio yake na wala asizidishe zaidi ya anachohitaji'

Anasema Imam Waki Ibn Jarrah kua: 'Sisi tulienda kwa Sufyan Ath Thawry, katika siku ya Idd, ambapo nae akasema kua: 'Jambo la Kwanza leo hii ni kua tunainamisha macho yetu chini''

Imam Sufyan Ath Thawry alisema kua: 'Yeyote yule mwenye Ilm kisha ikamfanya kua ni mwenye kulia basi huyo ni Mwanazuoni wa kweli'

'Kua ni mwenye kua na Subra katika nyakati zote na sehemu zote, kwani Subra hua ni yenye kumpelekea mtu kua ni Mcha Mungu na Ucha Mungu humpelekea Mtu kuingia Peponi. Hivyo usiwe na Hasira wala Hamaki kwani hisia mbili hizo humpelekea mtu kua ni mwenye uovu na uovu humpelekea mtu kuingia Motoni.'

'Eneza Ilm yako, lakini hapo hapo kua makini na umaarufu'

'Zifuatazo ni sifa za kua na Subra: Kutolalamikia Mitihani yako, Kutolalamikia maumivu yako na Kutoisifia Nafsi yako'

'Hakuna mtu anaempotosha mwenzake au kumuongoza zaidi ya rafiki yake'

'Kama Ibilis alinishinda Jana, basi hakika mimi nitamshinda leo hii kwa Istighfar na Amali njema'

'Hajajitayarisha na kifo yule ambae anadhani kua kesho atakua hai'

'Kama unajijua Nafsi yako basi hutoathirika nakile kinachozungumzwa juu yako'

'Yeyote yule anaempenda yule anaempenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni mwenye kumpenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* Yeyote yule anaemheshimu yule anaemheshimu *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni mwenye kumheshimu *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

'Kaa pamoja na wale ambao ni wenye kukuusia kutamani kidogo katika matamanio ya Dunia na kukutia ari kua na matumani makubwa ya Akhera, hivyo usikae na wale wenye kuzungumiza kuhusiana na Dunia yao kila mara kwani wataiangamzia Dini yako na kuutosha kutu Moyo wako. Kikumbuke Kifo kila mara na Muombe Maghfira Allah kila wakati kutoka na makosa yako yaliyopita na muombe *Allah Subhanah wa Ta'ala* akuweke Salama katika maisha yako yajayo, boresha tabia zako na usiende kinyume na Jamaa, kwani Usalama hupatikana pale unaposhikamana na Jamaa'

المستكشف أبو منال دانة
AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

‘Kama unampenda kweli Ndugu yako kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi kua mkarimu sana kwake Kinafsi na Kimali’

‘Mtu anaepigania Nfai yake kwa ajili ya Dunia hii hua ni sawa na yule anaejenga Nyumba moja ya mpito na kuivunja nyengine ambayo ni ya Kudumu’

‘Kua na Subra na Ustahmilivu katika kila wakati na katika kila sehemu kwani Subra na Ustahmilivu hukupelekea kwenye Ucha Mungu na Ucha Mungu hukepelekea kuingia Peponi, Usiwe ni mwenye hasira na ghadhabu kwani hisia hizo mbili hukupelekea kuingia Motoni ’

‘Jitahid ukaa mbali na matamanio ya kidunia na hivyo *Allah Subhanah wa Ta’ala* ataweza kukuonesha kasoro na Madhara ya Dunia’

‘Achana na mambo yenye shaka ndani yake na kisha fanya yale ambayo ni yenye uhakika kwako ndani yake na utakua salama kwa upande wa Dini yako’

‘Mkumbuke *Allah Subhanah wa Ta’ala* kila wakati na hivyo nae atakuweka mbali na Matamanio ya Dunia yako na kukurahisishia maisha ya Dunia yako’
‘Itamani Pepo na *Allah Subhanah wa Ta’ala* atakusaidiakatika kumtii kwako, na Uogope sana Moto na hivyo *Allah Subhanah wa Ta’ala* atakurahisishia Mitihani ya Kidunia’

‘Kua Mkarimu katika kutoa kwako na hivyo *Allah Subhanah wa Ta’ala* atakuhifadhia kasoro zako na katikamsiku ya malipo kukurahisishia hesabu yako’

Imam Sufyan Al Thawry basi alikua akijisuta Nafsi yake pale tunapozungumzia hali ya Nafsi ya mja katika kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi kila wakati alipokua akisali na kusoma *Surat Al Fatiha* basi alikua akilia sana pale anapofikia katika aya isemayo:

﴿إِيَّاكَ نَعْبُدُ وإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ﴾

Iyy<u>a</u>ka naAAbudu wa-iyy<u>a</u>ka nastaAAeenu *(Surat Al Fatiha 1:5)*

Tafsir: ***Ni wewe pekee ndie tunaekuabudu na ni wewe tu ndie tuneokuomba msaada.***

Sufyan Ath Thawry alipoulizwa ni kwa nini alikua akilia sana na kuikariri ayah hii wakati anapoisoma basi alijibu kwa kusema: ‘**Kwa hakika mimi hua naalia kwa sababu sisi hua tunamwambia *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua Ni wewe tu tunae kutegemea na ni wewe tu ndie tunakuomba msaada lakini ukweli ni kua sisi**

tunasema tu, lakini hatuoneshi kua tunamtegemea yeye kwani tunategemea zaidi *Dinar* na *Dirham* kuliko tunavyometegemea Mola wetu.'

Imam Ataa Al Khafaf anasema kua: '**Nilikua kila nikimkuta Sufyan Ath Thawry alikua analia na nilipomuuliza kwanini unalia basi alikua ni mwenye kusema kua: 'Hakika Mimi nna khofu kua huenda maneno ya Aya ya Qur'an yatanipa sifa ya kua mimi ni miongoni mwa Waasi. ''**

Imam Qabisah anasema kua: '**Hakika mimi sijawahi kukaa pamoja na Sufyan Ath Thawry isipokua nilikua nikikikumbuka kifo, kwani hakuna anaekikumbua kifo zaidi kama yeye.**'

Imam Sufyan Ath Thawry alisema kua: '**Wanazuoni ni Matabibu wa Dini, na Utajiri ni Maradhi ya Dini hivyo kama Watabibu wataambukizwa Maradhi jee ni nani atakaewatibu Watu?**'

Aliulizwa Imam Sufyan Ath Thawry: **'Hivi hadi lini wewe utasita kufuatilia kusoma Hadith?'** ambapo nae akajibu **'Hivi Jee kuna Ilm bora zaidi hapa Duniani kuliko Hadith?'**

Imam Sufyan Ath Thawry alisema: **'Haijawahi kunifika mimi Hadithi ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isipokua hua ni mwenye kuifanyia kazi kwa vitendo Hadith hio.'**

Imam Hammad Ibn Salamah anasema kua: '**Wakati Sufyan At Thawry alipokuja katika mji wa Basra alikua akisema: 'Huenda mimi nigekufa basi nigekua ni mwenye kupata utulivu, natamani mimi ningekua sasa hivi nimo kwenye Kaburi langu.**''

Ambapo Imam Hammad akamuuliza: '**Hivi kwanini wewe hua unaomba kufa wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekujaalia Ufahamu wa kua ni mwenye kuijua na kuifaham Qur'an na Ilm nyengine?**'

Imam Sufyan Ath Thawry akasema: '**Ewe Abu Salamah, Hivi nitajuaje mie kua wakati gani nnaweza nikapotoka? Huenda ikawa ni mwenye kufanya kile ambacho ni haramu kwangu, au nitapatiwa mtihani wa Dini yangu na kisha nikafariki?**'

Imam Sufyan Ath Thawry alisema: '**Mtizamo wa Macho umekususidiwa kua ni Mtizamo wa Kidunia, na Mtizamo wa Moyo umekususdiwa kua ni Mtizamo wa Kiakhera, Hivyo Mtu anapotizama kwa Mtizamo wa Macho hua si mwenye kunufaika, bali hunufaika pale anapotizama kwa Mtizamo wa Moyo.'**

Imam Mahdi ambae alikua akimsimamia Imam Sufyan Al Thawry wakati alipokua akiumwa alimuuliza Imam Sufyan Ath Thawry kuhusiana na kutosali sala ya Jamaa, ambapo Imam Sufyan Ath Thawry akasema: **'Kumshughulikia Muislam mwenzako ambae ni mwenye Shida hua ni bora kuliko Kusali sala ya Jamaa'** Imam Ibn Mahdi akauliza: **'Hivi jee umeyasikia wapi haya wewe?'**

Imam Sufyan Ath Thawry akasema: **'Asim Ibn Ubayd Allah ameniambia mimi kutokea kwa Abd Allah Ibn Amir Ibn Rabia kutoka kwa baba yake (Amir Ibn Rabia Al Anzi *Radhi Allahu Anhu*) amesema kua: 'Kwangu mimi ni bora Kumsaidia Muislam mmoja mwenye Shida katika siku moja kuliko kusali Sala ya Jamaa katika Safu ya Mwanzo kwa Mda wa miaka 60.''**

Imam Sufyan Ath Thawry aliandika baadhi ya vitabu ambavyo kabla ya kufariki kwake basi alivikabidhi kwa Ammar Ibn Sayf na kumwambia kua atakapofariki basi anatakiwa achimbe shimo kisha navyo avizike.

Mnamo mwaka 160 Al Hijra Imam Sufyan Ath Thawry aliingia matatani baada ya kua ni Mwanazuoni aliekua akiwakosoa sana Khalfa Al Mansur na Al Mahdi na hivyo wakawa wanamtafuta ili wamuadhibu, hivyo nae akakimbilia katika Mji wa Basra ambapo alikaa mafichoni kwa mda wa miaka miwili hadi mnamo mwezi wa Shaabani waa mwaka 161 Al Hijra alipofariki Dunia.

Ambapo anasema Abd Rahman Ibn Ishaaq Al-Kilaanee kua: '**Sufyan Ath Thawry alipokua amejificha katika Mji wa Basra alinitumia ujumbe nami nikaenda kumtembelea, na nilipofika basi alikua taabani kifo kinamkaribia hivyo akauingiza mkono wake nyuma ya kichwa chake na kunirushia mfuko uliokua unapesa, katika wakati huo kulikua kuna Mwanamke aliekua akizungumza nyuma ya pazia, hivyo Sufyan At Thawry akaniambia: 'Huyu ni mwanamke ambae nilimuoa na ananidai Dirham 30 kutoka kwenye Mahari yake hivyo mlipe''**

Ambapo kwa upande mwengine basi anasema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: **'Sisi tulienda kwenye nyumba ya Umm Hasan Al Kuffiya, nasi tukaiona kua ni nyumba ambayo ndani yake ahakukua na kitu chochote isipokua sehemu ya Jamvi moja la zamani, hivyo At Thawry akasema kumwambia Umm Hassan Al Kuffiya kua: 'Bora ungemuandika mmoja kati ya Binamu zako kukubadilishia hali yako'**

Ambapo Umm Hassan Al Kuffiyah akasema: 'Sufyan hakika wewe ni mtu mkubwa sana kwa kwenye macho yangu, na kwenye Moyo wangu pia kabla ya kuniambia Jambo hili, kwani mimi kamwe sitoulizia kuhusiana na Dunia kutoka kwa yule ambae ni mmiliki wake, na mwenye uwezo juu ya kila kitu chake, na kuisimiamia, hivyo itakuaje niwe ni mwenye kuomba kitu chake Dunia kutoka kwa yule ambae si mmiliki wake na wala hana uwezo wowote juu yake?

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Wa Allahi Sufyan mimi kamwe sitamani kua utokee wakati ambao nitakua ni mwenye kushughulikia kitu chochote zaidi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika wakati wa kushughulika na *Allah Subhanah wa Ta'ala'* haya ni maneno ambayo yalimfanya Sufyan alie, na baadae nilisikia kua Sufyan alimuoa Umm Hasan Al Kuffiyah '

Imam Sufyan Ath Thawry alifariki kutokana na ugonjwa wa kuharisha ambapo katika aliyofariki basi alitia udhu mara 60 kutokana na kutoka kwake udhu huo kila wakati anapoutia, ambapo Imam Ibn Mahd anasema kua: '**Wakati Sufyan Ath Thawry alipokua anataka kufa basi alisema: 'Ewe Abd Rahman Ni kugumu sana Kufa, hebu nisomee Surat Yasin kwani mimi nimeambiwa kua hua inamrahisishia Mgonjwa na kifo chake**' Imam Ibn Mahdi anamalizia kusema kua: '**Hivyo mimi nikamsomea ambapo sikuwahi kuimaliza nae akafariki Dunia.**''

Imam Ibrahim Ibn Ayan basi yeye anasema kua: '**Mimi nililala na nikamuota Sufyan Ath Thawry na nikamuuliza: 'Vipi imekuaje?' nae akasema: 'Niko pamoja na Kiramin Bararatin.**'

﴿كِرَامٍ بَرَرَةٍ﴾

Kiramin bararatin *(Surat Abbasa 80:16)*

Tafsir: ***Wenye kua na Heshima na Utiifu.***

Imam Musab Ibn Miqdatin anasema kua: **'Mimi nililala na kumuota *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa amemshika mkono Sufyan Ath Thawry na kumshukuru.**'

Imam Sufyan Ath Thawry alisema kua: **'Kama mtu akiniamini mimi kuniachia Nyumba ambayo imejaa Hazina ya mali basi nitajiaminisha bila ya Wasi wasi, lakini kamwe asiniaminishe kwa kuniachia Mtumwa Mwanamke mweusi.'**

IMAM HAMMAD IBN ZAYD 98 AH

Imam Abu Ismail Hamad Ibn Zaid Ibn Dirham Al Azraq alizaliwa mnamo mwaka 98 Al Hijra katika Mji wa Basra nchni Iraq kutoka katika familia yenye asili ya Sijisitan iliyokua ikimilikiwa na Jarir Ibn Hazm Al Jahdami. Kwa maana hio basi Imam Hamad

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ibn Zaid alikua akitokea kwenye familia ya Watumwa ambao baadae walioachiwa huru na watoto wa Jarir Ibn Hazm ambao ni Yazid na Jarir baada ya kufariki Baba yao.

Baba yake Imam Hamad Ibn Zaid alikua ni Mwenye Ilm kubwa sana kwani alisoma kwa Masahaba, na hivyo alikua ni miongoni mwa Walimu wa mwanzo waliomsomesha Mtoto wake ambae baadae akakulia na kua na darja ya Uimamu kutokana na Ilm yake, kwani mbali ya kusoma kwa Baba yake lakini Imam Hamad Ibn Zaid alisoma kwa Maimamu wengi sana akiwemo Imam Thabit Al Bunani, Imam Asim Ibn Abi Najd, Imam Amr Ibn Dinar, Imam Abd Allah Ibn Tawus n.k

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Al Shaath Ibn Is-haq As Sijistan ambae ni baba yake Imam Daud, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Ali Al Madini, Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Abd Rahman Ibn Mahdi.

Ambapo ingawa Imam Hamad Ibn Zaid aliishi katika kipindi kimoja na Imam Ayyub As Sakhtiyani lakini anasema Imam Hamad Ibn Zaid kua: '**Hamad Ibn Abi Sulayman alitembelea Mji wa Basra lakini hakua ni mwenye kumtembelea Ayyub As Sakhtiyyani, hivyo nasi hatukua ni wenye kumtembelea, kwa sababu kama Ayyub hakumtembelea Mtu fulani basi na sisi hua hatumtembelei pia.'**

Na anasema Imam Yahya Ibn Main pia kua: '**Hamad Ibn Zaid alikua akimjua vizuri sana Ayyub As Sakhtiyyani'**

Imam Ibn Saad nae anasema kua: '**Hammad Ibn Zayd alikua alikua ni *Thiqah* – anaeaminika na *Thabit* mwenye misimamo na *Hujjah* mwenye Mamlaka ya Ilm na ni Mwanazuoni wa Hadith'**

Ambapo Imam Ahmad Ibn Hanbal akasema kua: '**Hammad Ibn Zayd ni Imam miongoni mwa Waislam.**'

Imam Abu Ya'ala anasema kua: **'Hamad Ibn Zaid alikua ni Thiqah na kuna makubaliano ya Wanazuoni kuhusiana na kukubalika kwake na kunufaisha kwake, na amenukuliwa katika vitabu viwili vya Hadith Sahih vya Bukhari na Muslim, na Maimamu wanakubaliana kua kulikua kuna mawasiliano bania yake na Imam Malik Ibn Anas na alikua akivutiwa sana mitizamo yake, ambapoWajukuu wake ni Wanazuoni wa Fiqh na ni wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik.'**

Ambapo amesema Imam Abd Rahman Ibn Mahdi kua: '**Sijaona mimi mtu mwenye Ilm kubwa kama Hammad Ibn Zayd'** na akasema tena kua : '**Maimamu ni wanne katika wakati wa kipindi chao ambao ni Hammad Ibn Zayd Al Basra, Sufyan Ath**

Thawry Al Kufi, Malik Ibn Anas Al Hijaz na Al Awzai al Shami ' na pia alisema kua: '**Sijaona mimi mwenye Ilm kubwa zaidi ya Imani na Hadith kuhusiana nayo zaidi ya Hammad Ibn Zayd Al Basr**'

Imam Yazid Ibn Zuraj aliulizwa: **'Jee ni upi mtizamo wako kuhusiana na Hammad Ibn Zayd na Hammad Ibn Salamah.' Ambapo nae akajibu: 'Hammad Ibn Zayd ni Mcha Mungu sana.'**

Imam Sulayman Ibn Harb alisema kua: **'Mimi nimemsikia Hammad Ibn Zayd akinuua hadith na kisha akasema: 'Nimeisikia Hadith hii miaka 50 iliyopita na sijainukuu tena hadi sasa''**

Ambapo alisema Imam Ubayd Allah Ibn Al Hasan kua: **'Ni kupitia katika Hamamd wawili tu, hivyo kama unatafuta Ilm basi itafutae kupitia kwa Hammad wawili hawa.'** Yaani Imam Hammad Ibn Salamah na Imam Hammad Ibn Zayd.

Imam Ibn Hibban anasema kua: '**Hamamd Ibn Zayd alikua ni ustadi wa kuhifadhi na ucha Mungu, na alikua kinukuu hadith kutoka kwenye ufahamu wake na alikua ni kipofu'**

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi yeye anasema kua: '**Hammad Ibn Zaid alikua ni mwenye kuaminika na Mwanafiqh mwenye Mamlaka, na alikua ni Kipofu, ambapo upofu huo ulimjia baadae katika maisha yake, kwani imenukuliwa kua alikua akiandika.**'

Na akasema Imam Abd Rahman Ibn Mahdi kua: '**Kama ukimuona mtu katika mji wa Basra anampenda Hamamd Ibn Zayd basi fahamu kua mtu huyo ni mwenye kufuata Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam***'

Na Imam Adh Dhahabi akasema kua: '**Hakika mimi sijui kuhusiana na kutokukubaliana kwa Wanazuoni kuhusiana na Hamamd Ibn Zayd kua alikua ni mmoja kati ya Maimamu wa Salaf na mwenye uwezo na ucha Mungu na kutokua na kasoro katika hadith zake, mbali ya kua amenukuu hadithi nyingi. Allah amuingize kwenye Rehma zake.'**

Anasema Bishr Ibn Al Sari kua: **'Nilimuuliza Hamamd Ibn Salamah: 'Ewe Abu Ismail, hivo jee unasema kuhusiana na Hadith isemayo kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* anashuka kwenye Mbingu ya mwisho ya chini kabisa?' ambapo nae akasema: 'Naam ni kweli na hua anashuka kwa namna anavyotaka yeye mwenyewe.'''**

Imam Hamad Ibn Zayd alfariki katika siku ya Ijumaa ya mwezi 10 Ramadhani ya mwaka 179 Al Hijra akiwa na umri wa miaka 81.

SHAYKHA RABIA AL ADAWWIYAH 98 AH

Usiku mmoja katika mji wa Basra katika familia moja ya kimasikini, yenye watoto wanne wa kike alizaliwa mtoto wa kike ambae hata hivyo kutokana na umasikini wa familia hio basi ilikosekana hadi nguo ya kumfunika mtoto huyo, na ndani ya nyumba hio kulikua kiza kutokana na kukosekana mafuta ya kuwashia taa pia. Hivyo mama wa binti huyo akamuomba mume wake aende kwenye nyumba ya jirani angalau akaombe mafuta ya taa, lakini mume huyo akasema kua, yeye ni wenye kumtegemea Mola wake tu katika kila kitu hivyo haijuzu kwake kuenda kuomba mafuta kutoka kwa jirani yake.

Baada ya tukio hilo familia hio ikapitiwa na usingizi na kulala, ambapo baada ya mda mzee huyo akaona ndoto usingizini ambayo ndani yake alimjia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliekua akimwambia: **'Usiwe na Khofu kwani Binti aliezaliwa atakua ni Mcha Mungu mkubwa sana, na watu wengi watamkubali na kumpenda na kumtukuza, hivyo andika barua na kisha mwambie Amir Isa Zadhan wa Basra kua, ingawa yeye ni mwenye kunisalia mimi mara 100 kwa siku kila siku na mara 400 katika usiku wa kuamkia Ijumaa, lakini kutokana na kukosa kunisalia mimi katika usiku wa kuamkia Ijumaa hii basi itambidi akupe Dinar 400'**

Hivyo asubuhi yake Baba wa mtoto huyo akaadika barua hio na kuituma kwa Amir Isa Zadhan ambapo nae alipoipokea na kuisoma barua hiyo basi akaamrisha kua Baba wa Mtoto huyo apewe Dinar 2000, ambapo mtoto huyo aliezaliwa ndie aliekua akijulikana kwa jina la Rabia Al Adawwiyah.

Rabia Al Adawiyah alikua ni mtoto aliezaliwa mnamo mwaka 98 Al Hijra mjini Basra nchini Iraq katika familia yenye watoto wanne, na hivyo alipewa jina la Rabia kutokana na yeye kua ndio mtoto wa nne, watoto hawa hawakuishi sana na wazee wao kwani walikua ni mayatima baada ya Baba yao kufariki wakati Rabia alipokua na umri wa miaka 10, na muda mfupi baada akafarikia mama yao pia.

Hivyo watoto hawa wakawa hawana wa kuwasimamia na wala hawana kitu isipokua Mashua waliyoachiwa na Baba yao ambayo ilikua inatumika kuwavusha watu kwenye Mito ya Basra na hivyo kua ndio njia pekee ya kuwapatia riziki yao ambayo nayo hata hivyo ilikua haiwatoshi. Mwaka mmoja baadae kulitokea Ukame katika mji wa Basra familia hii ikatawanyika kwa kila mtu kuelekea upande wake kwa ajili ya kujitafutia

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

riziki yake, hivyo kwa bahati mbaya au nzuri Rabia akakamatwa na kuuza kama Mtumwa.

Rabia Al Adawwiyah alinunuliwa na mtu ambae alikua si mwenye kumjali bali alikua ni mwenye kumuadhibu sana hadiikafikia hali ya kua Rabia akaamua kukimbia, hivyo katika sikua aliyoamua kukimbia basi katka kukimbia kwake akateleza na akaanguka kwenye dimbwi lililojaa tope nyingi sana, huku akiwa ameteguka mguu na alipojikuta katika hali hio basi akamuomba *Allah Subhanah wa Taa'ala* kua amuepushe kutokana na hali ya Utumwa wake huo, kwa kusema: '**Ya Allah, ingawa mimi mja wako ni Yatima nilieingizwa kwenye Utumwa, lakini haja yangu ilikua ni kutaka kujua kama umeridhika nami ama la**' na hapo akasikia sauti inayomwambia kua: **'Usiwe na khofu kwani utapanda Darja na kua ni mwenye cheo kama utakua ni mwenye subra'**

Hivyo Rabia akaamua kurudi nyumbani kwa mmiliki wake, na kua ni mwenye kufanya kazi za mmiliki wake katika wakati wa asubuhi, mchana hadi jioni na kisha kua ni mwenye kufanya Ibada usiku kucha. Ambapo anasema Imam Farid Al Attar kua: '**Siku moja katika wakati wa usiku, Rabia alipokua akifanya Ibada zake, mara mmiliki wake akaja chumbani kwake na alipochungulia akamuona Rabia akiwa anaomba Dua kwa kusema:** '**Ewe Mola wangu, Hakika kama isingekua kutokana na ukali wa huyu mmiliki wangu, basi mimi ningeutumia mda wangu wote kwa ajili ya kukuabudu wewe tu.'**

Baada ya Dua hio, basi mmiliki wake akaona kua kuna mwangaza mubwa sana umetoka kwenye taa aliyokua akiitumia Rabia kujimurikia katika wakati wa Ibada hio, Mwangaza ambao ulijaa kwenye nyuma nzima na kisha ukatoweka, hivyo Mmiliki huyo akastaajabishwa sana na tukio hilo na hivyo siku ya pili yake asubuhi akaamua kumuachia huru Rabia al Adawwiyah.

Baada ya kuachiwa huru basi Rabia Al Adawwiyah aliulizwa: **'Hivi Jee unampenda *Allah Subhanah wa Taa'ala*?'** ambapo nae akajibu : **'Naam' akaulizwa: 'Na jee unamchukia Ibilisi?'** ambapo nae akasema: **'La, Kwani mapenzi yangu hayaniwezeshi mimi kua ni mwenye kua na chuki''**

Rabia Al Adawwiyah akaanza kumtumikia Mola wake tu, kwani kwake yeye ilikua ni mwenye hali ya maumbile ya Mapenzi ya kumpenda kweli Muumba wake bila ya kujali wala kutegemea Pepo yake kwani alikua akisema katika Dua zake kua: **'Ya Allah hakika kama mimi nakuabudu wewe kutokana na kuuogopa Moto wako, basi nichome mimi ndani yake, na kama nakuabudu kwa kutegemea Pepo basi usiniingize mimi ndani yake, lakini kama ikiwa nnakuabudu wewe kwa ajili yako basi usinizuie mimi kukuona katika hali ya uzuri wako.'**

Siku moja Imam Sufyan Ath Thawry alimuuliza Rabia Al Adawwiyah kuwa kusema: **‘Hivi jee, ni kitu gani ambacho Mja anatakiwa akifanye ili aupate ukaribu na Mola wake?**’ ambapo Rabia Al Adawwiyaha akasema: **‘Kitu kitakchomkarbisha Mja karibu ya Mola wake ni kwa mja kua na hali ambayo ya kutopenda kitu chochote hapa Duniani na Akhera pia isipokua Mola wake.’**

Kutokana na ukubwa wa Mapenzi yake kwa Mola wake basi Rabia Al Adawwiyah hakua ni mwenye kua na hamu wala kutaka kuolewa na mtu yeyote kwani alikua akisema kua: **‘Ndani ya Moyo wake hamna sehemu yeyote iliyobakia kwa ajili ya kupenda kitu chengine zaidi ya Mola wake’**

Safari moja ulipokaribia msimu wa Ibada ya Hija Rabiya Al Adawwiyah alifunga safari kuelekea katika mji wa Makkah, na alipofika njiani basi katika kati ya safari akaliona Al Kaabah likiwa linakuja na kumfuata yeye badala yake, na hivyo akasema: **‘Hakika mimi ni mwenye haja ya kukutana na Mola wangu na wala si mwenye haja ya kukutana na Nyumba yake, kwani yeye ndie aliesema kua Mja akinikaribia mimi kwa hatua moja basi mimi nitamkaribia kwa nyanda moja, Hivyo Al Kaabah halina uwezo dhidi yangu, kwani siwezi kufurahika na uzuri wa Al Kaabah ndani ya Moyo wangu’**

Ambapo katika wakati huo huo Imam Ibrahim Ibn Adham alikua ni mwenye kuelekea kwenye Ibada ya Hija, na ingawa aliwasili kwenye Mji wa Makkah katika Mda ambao Ibada ya Hijja ilikua bado haijaanza, lakini alishanganzwa kwa kutoliona Al Kaabah katika sehemu yake pale alipofika mbele yake. Hivyo ikawa si mwenye kuamini macho yake, kwani imemchukua miaka 14 tangu aanze safari yake ya kuenda katika Ibada ya Hija kwani katika kila sehemu anayopitia basi Imam Ibrahim Ibn Adham alikua ni mwenye kutaka kuisujudia sehemu hio kwa kusali rakaa 2 juu yake.

Hivyo Imam Ibrahim Ibn Adham akafumba na kumbua macho yake huku akajiuliza: ‘**Macho yangu hayaoni Al Kaabah imekuaje?’**

Imam Ibrahim Ibn Adham akasikia sauti ikisema: ‘**La tatizo sio Macho yako Ewe Ibrahim kwani macho yako ni Mazima, bali ni Al Kaabah lenye ndio lililohama na kumfuata Mwanamke anaelikaribia eneo hili la Al Kaabah’** Imam Ibrahim Ibn Adham akauliza: **‘Hivi jee ni mwanamke gani huyo?’** na mara alipogeuka na kuangalia alikotoka basi akamuona Rabia Al Adawiyah akiwa anakuja na kisha alipogeuka kwenye Al Kaabah akaliona kua Al Kaabah liko kwenye sehemu yake.

Hivyo Imam Ibrahim Ibn Adham akasema kumwambia Rabiah Al Adawwiyah: ‘**Ewe Rabia, hivi jee unaona ni usumbufu gani huo unaosababisha?’** Rabial Al Adawwiyah akasema: **‘La hakika mimi sijasababisha usumbufu wowote, bali ni**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

wewe uliechelewa kufanya Ibada ya Hija kwa mda wa miaka 14’ ambapo Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: **‘Mimi nimetumia mda wote huo kutokana na kua ni mwenye kusali ndani yake.’** Rabiah Al Adawwiyah akasema: **‘Hukuutumia mda huo kwa ajili ya Mola wako bali kwa ajili ya maombi yako binafsi’**

Alisema Rabi Al Adawwiyah kumwambia Mola wake kua: ‘**Hakika mimi nnakupenda wewe mara mbili, kwanza kama mpenzi ampendavyo yule ampendae na hivyo hua si mwenye kuzungumza na yeyote zaidi yako, na pili ni kama mja anavyostahiki kumpenda aliemuuba, kutokana na kunijaalie mimi kukujua wewe.’**

Alisema Imam Sufyan Ath Thawry kua alisema Rabiah Al Adawwiyah kua: **‘Ewe Ibn Adam, hakika umri wako ni siku chache tu, hivyo siku moja yako inapotoweka basi na sehemu ya uhai wako hua imetoweka, na hivyo baada ya kila sehemu ya uhai wako yako kutoweka, basi nawe utakua umeshatoweka.’**

Rabia Al Adawwiyah alikua ni mwenye kupenda kuomba kwa kusema: **‘Ya Allah hakika mimi nafanya Istighfar kwako kutokana na kukosekana na Ikhlasi pale nnaposema Astaghfir Allah’**

Na anasema Abdah Bint Abi Shawwal ambae alikua ni mfanyakazi wa Rabiah Al Adawwiyah kua: ‘**Rabiah Al Adawwiyah alikua ni mwenye kusali Usiku kucha, na kabla ya kuingia Alfajir alikua ni mweye kulala kidogo na kisha hua ni mwenye kunadia kwa sauti kubwa akisema: ‘Ewe Roho yangu, hivi kwa mda gani wewe unataka kua ni mwenye kuendelea kulala? Wakati karibuni tu utakua ni mwenye kulala kwa mda mrefu bila ya kuamka hadi katika siku ya Malipo itakapowadia?’’**

Rabiah Al Adawwiyah alikua nmtu mwenye kua na shukuran kwa Mola wake bila ya kujali hali aliyokua nayo, iwe furaha au huzuni kwani alikua akimshukru kwa kusema kua: ‘**Utukufu ni wako ewe Mola wangu kwani kwa hakika wewe ndie mwenye kunipa Uhai na pia kunipa riziki yangu’**

Rabiah Al Adawwiyah alisema kua: ‘**Siku moja nilifanya *Dhikr Allah* kuanzia Usiku hadi kukaribia Alfajir na kisha nikalala na kuona ndani ya Ndoto Mti mkubwa uliokua usioelezeka uzuri wake huku ukiwa umenawiri na kua na Nuru kubwa sana, na ukiwa na Matunda ya aina tatu, ambayo kamwe sikuwahi kuyaona hapo kabla hapa Duniani yakiwa na maumbile kama ya Maziwa ya Binti aliekua mwari yenye rangi ya Manjano, Nyeupe na Nyekundu yaking’ara kama kama Jua katika eneo la anga la Mti huo, nami nikavutiwa nayo sana na kuuliza: ‘Huu Mti na haya matunda ni kwa ajili ya Nani?’ nami nikasikia sauti ikisema: ‘Haya nikwa ajili yako kktokana na *Dhikr Allah* zako.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Hivyo nikaanza kuuzunguka huku nikiuangalia vizuri mti huo kwa kushangazwa na uzuri wake, na mara chini yake nikaona, matunda ambayo idadi yake ni 18 yakiwa yameanguka juu ya Ardhi yenye rangi ya Dhahabu hivyo nikasema. 'Natamani kama Matunda haya yangekua pamoja na Matunda mengine yaliyo juu ya mti huu.'

Ambapo mara nikasikia sauti ikinijibu: 'Bila ya shaka yangekua juu kama usingekua unafikiria kitu chengine pale wakati ulipokua ukifanya *Dhikr Allah* zako, kwani ulikua ukifanya *Dhikr Allah* huku ukiwa ni mwenye kufikiria kama jee unga ulioukanda na kuuwacha uumke umeshaumuka ama la? hivyo Matunda haya yakaanguka.'

Siku moja kuna watu walimtembelea Rabia Al Adawwiyah nyumbani kwake, na kutokana na hali yake ya maisha basi mmoja kati ya watu ao akamwambia Rabia Al Adawwiyah kua: **'Ewe Rabia Mimi nnao watu wanao uwezo mkubwa ambao wanaweza kukusaidia wewe kimaisha.'**
Ambapo Rabia Al Adawwiyah akahoji kwa kusema: '**Hivi jee wewe unadhani kua anaenipa mimi riziki na anaewapa wao ni tofauti au?'**

Mtu huyo akasema: **'La'** Rabia Al Adawwiyah akasema: **'Basi umefanya kosa kubwa sana kuniambia hivyo, hivi jee unadhania kua mwenye kutoa riziki amewasahau Masikini kutokana na Umasikini wao na anawakumbuka Matajiri tu kutokana na Utajiri wao?'** Mtu huyo akasema: **'La'** Rabia Al Adawwiyah akasema: **'Hivyo jee kama yeye ni mwenye kuijua Hali yangu, itakuaje mimi kua ni mkumbushe kuhusiana na kile akipendeleacho kunipa juu yangu?'**

Siku moja Rabia Al Adawwiyah aliwasikia watu wakisema: **'Ya Allah hakika sisi tunaomba Radhi zako, kua uturidhie'** hivyo Rabia Al Adawwiyah akasema kuwaambia watu hao kua: **'Hivi nyinyi hamuoni haya? Inakuaje muwe ni wenye kuomba Ridhaa za Mola wenu wakati nyinyi wenyewe bado hamjaridhika na Mola wenu.'**

Aliulizwa Rabia Al Adawwiyah aliulizwa: **'Hivi** Mapenzi ni nini?' Rabia Al Adawwiyaha akasema: **'Mapenzi hua ni yenye kutokana kwenye Umilele na kumalzikia kwenye umilele, na hakuna alieonekana kwenye Dunia 70, 000 alieonja hata tone moja la Mapenzi isipokua yule aliezama kwenye mapenzi na *Allah Subhanah wa Ta'ala*, ambapo ndani yake ndio tunakutana na maneno yasemayo:**

﴿يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Yuhibbuhum wayuhibboonahu *(Surat Al Maidah 5:54)*

Tafsir: ***Yeye Anawapenda na wao wanampenda.***

Rabia Al Adawwiyah aliomba Dua kwa kusema: **'Ya Allah, Nakuomba kua kama kuna chochote kile ambacho umenichagulia mimi cha Kidunia basi usinipe mimi bali wape maadui zako, na chochote kile ulinichagulia mimi cha Kiakhera basi wape Marafiki zako, kwani mimi ni mwenye kutoshelezeka nawe.'**

Rabia Al Adawwiyah alisema kua: **'Kuna watu wa aina tatu, ambapo aina ya Kwanza ni wenye kuamini kua mikono yake na watoto wake ndio vinavyomsaidia yeye kupata mafanikio ya Kidunia, aina ya pili ni ile ya wale ambao ni wenye Kuomba kwa Mola wao ili mikono yao ichume kile kilichokua cha Akhera, wa tatu ni wale ambao ni wale ambao mikono yao imefungwa kwenye viganja vyao na mapenzi ya kumtumikia *Allah Subhanah wa Ta'ala* bila ya kuhitajia malipo yeyote'**

Rabia Al Adawwiyah alisema kua: **'Kua kama Mshumaa uitie Nuru Dunia huku ukiwa si mwenye kudumu bali mwenye kuangamia, kua kama Sindano na unufaishe bila ya kutegemea Kitu'**

Rabiah Al Adawwiyah alifariki mnamo mwaka 180 Al Hijra.

IMAM YUSUF AL ASBATI 100 AH

Imam Abu Muhammad Yusuf Ibn Asbati Ibn Wasil Ibn Al Shaybani alizaliwa katika Mji wa Aleppo na aliishi katika maeneo ya Antakiya hii kilikua ni katika kipindi cha miaka 200 ya mwanzo ya Al Hijra kwani alifariki mnamo mwaka 190 Al Hijr.

Tunapomzungumzia Imam Yusuf Al Asbati basi hua tunamzungumzia Imam ambae ni Mwanafunzi wa Imam Sufyan Ath Thawry ambae alikua akitegemewa na Watawala katika wakati wa Uhai wake, lakini hapo hapo alikua sio mtu mwenye kupokea Zawadi kutoka kwa Watawala. Na alikua hatoi Fatwa kwa Mtawala ambae amekuja kwake huku akiwa amevalia kifahari.

Imam Yusuf Al Asbati alikua ni Mtu ambae yuko Makini sana katika Riziki yake kiasi ya kua kwake yeye ilikua bora akae na njaa kuliko kula chakula ambacho ana shaka nacho juu ya uhalali wake katika kupatikana kwake Na hii ni kwa sababu Imam Yusuf Al Asbati alikua akisema kua:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

‘Ucha Mungu ni kujitenga na vilivyo haramu na kujua kua Utaadhibiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* utakakikimbilia kisicho halali yako’

Kwani Aliulizwa Imam Yusuf Al Asbati: **‘Hebu tuelezee kuhusiana na Unyenyekevu wa Kiiman!’**

Ambapo Imam Yusuf Al Asbati akasema: ‘**Unyenyekevu wa Kiimani hua ni pale Mtu unapotoka Nyumbani kwako na kisha kwako wewe ikawa kila mtu unaemuona basi hua namuona na kumfikiria kua ni Bora zaid yako.**’

Naam..Huyo ndio Imam Yusuf Al Asbati ambae alikua akipenda kufunga sana funga za Suna na kusema kua: ‘**Njaa inalainisha Nyoyo na ndio Msingi wa Ucha Mungu hapa Duniani**’

Kwani Imam Yusuf Al Asbati kamwe hakua ni mwenye Kuficha Neno Lolote lile ambalo kutamkwa kwake hua ni kwa ajili ya kupata Ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*

Na alikua akisema kua: ‘**Taqwa ni kuridhika na ulichopata na kutosikitikia ulichokipoteza’**

Na kutokana na ucha Mungu wake basi alikua ni mwenye kujua namna ya kuidhibiti Nafsi yake kwa kila wakati alikua ni mwenye kudumu na Dhikr Allah na akujiepusha na mambo ya haramu na yenye kushabihiana nayo na alikua ni mwenye kuyakimbilia yale yaliyo halali kwake tu kwani alikua akisema kua: ‘**Sehemeu 9 kati ya 10 zinazojumuisha kupatikana kwa Radhi za *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua ni katika kupata Riziki yako ya halali.**’

Ingawa Imam Al Asbati alikua ni mfumaji kwa ajili ya kujitfutia riziki yake lakini yeye mwenyewe alikua si mtu wa kuvaa sana kwani alikua ni mwenye kuvaa kanzu mbili tu ndani ya miaka 40, leo hii kesho ile, na hiii ni kutokana na kutoitilia maanani Dunia yake kwani mtizamo wake ulikua ni kama mtizamo wa *Amir ul Muumini*n Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* ambae alisema kua: ‘**Dunia hii ni kama sehemu ya kumwagia taka, hivyo yeyote anaevutiwa nayo basi ajitayarsihe na matatizo yake’**

Kuna kipindi Imam Al Asbati alikua anaumwa, hivyo Wanafunzi wake wakamtafutia Daktari ambae alikua ni mwenye kuwtaibu Matajiri tu, hivyo alipopata habari hio basi Imam Al Asbati akawauliza Wanafunzi wake: ‘**Hivi Jee huyo Daktari hua anatibu kwa kiasi gani hao Matajiri?**’ Ambapo nao wakasema: **‘Dinari moja ya Dhahabu’**

Hivyo Imam Al Asbati akatoa mfuko wake wa pesa na kuwapa Wanafunzi wake hao kua ni malipo ya Daktari huyo na Wanafunzi walipoangalia wakaona kua mna Dinari 15 za Dhahabu, hivyo wakamuuliza: '**Mbona nyingi sana?'** Imam Al Asbati akasema: **'Mlipeni tu kwani kusudio langu mie ni kumuonesha kua kuwatibu Masikini kuna Thamani kubwa zaidi kuliko kuwatibu Matajiri.'**

Imam Yusuf Al Asbati alimuandikia barua Imam Hudhayfah Ibn Marashi kwa kumwambia: '**Kua ni mwenye Taqwa, achana na vya haramu, Ifanyie kazi Ilm uliyokua nayo, Ishughuliie Nafsi yako na mkumbuke A*llah Subhanah wa Ta'ala* katika kila wakati, ambapo hakuna anaetakiwa kuijua hali yako isipokua Mola wako, kwani baada ya Kifo hua hakuna kinachofuata isipokua Majuto na majuto'**

Imam Al Asbati alikua ni mwenye kupenda sana kulia kutokana na khofu juu ya udhaifu wake wa kimuambile wa Kiibn Adam kutokana na kutoweza kutimiza wajibu wake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ipasavyo kwani alikua akisema: **'Hakika mimi nnakhofia kua siwezi kufungamana na maamrisho ya Qur'an ipasavyo, na hivyo nikiona aya inayozungumzia kuhusiana na Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi khofu yangu huongezeka na hivyo hua nashindwa kuendelea kwa kulia, kutokana na hali hio basi ndio maana mimi hua ni mwenye kufanya Istighfar mara 70 kwa kila siku**'

Na mbali ya Ucha Mungu wake lakini Imam Al Asbati alikua kila siku akijiona kua ni mwenye dhambi nyingi sana kwani akiyahesabu mema yake basi anayoana kua ni kidogo sana, hivyo alipoulizwa kama anataka kufariki mapema ama la basi alisema: **'La nnahitaji kuishi zaidi kwani labda iko siku mimi nitajuta zaidi kuhusiana na dhambi zangu na hivyo kua ni mwenye kufanya mema zaid na hivyo kujumuishwa na wenye kufanya mema'**

Mke wake Imam Al Asbati alikua ni mcha Mungu sana pia na alikua akijulikana kwa jina la Nassiyah Bint Salman kiasi ya kua alipojaaliwa kupata Mtoto wake wa kwanza basi Nasiyyat basi alihisi kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amempa Mtihani kwani mda wake mkubwa itabidi awe ni mwenye kuutumia kwa ajili ya kumsimamia mtoto wake kuliko kwenye kumuabudia Mola wake hivyo aksema kumwambia *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: **'Ya Allah, hivi jee umeniona mimi kua sistahiki kua ni mwenye kuabudu ipasavyo kwa hivyo ndio umeamua kunipa Mtoto atakaeuchukua mda wangu wote kwa ajili yake dhidi yako?'**

Imam Yusuf Al Asbati aliusia kwa kusema: **'Kufanya mema huku ukiwa na unyenyekevu kidogo hua ni bora zaidi kuliko kufanya mema mengi ambayo hayako Moyoni mwako'**

'Kuachana na Dunia hua ni kua na subra katika wakati wa mitihani, kuachana na matamanio na kua na umakini juu ya uhalali wa chakula unachokula.'

'Dalili ya tabia njema ni Kutojali nini alichosema Rafiki yako na kukikubali, kua na huruma kwa Nafsi yako na kwa Nafsi za wenzako na pia kwa kila kiumbe na kutochunguza kasoro za wengine, kwani kuona kosa la mwenzako hua ni sawa na kufikia kua kasoro hio imefanywa kwa makusudi, Kuwasamehe wanaokuomba msamaha. Nakua na tabasamu kwa kila mtu mkubwa na mdogo.'

'Dalili za Kua na Haya hua ni: Kufikiria ukubwa wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hali itakavyokua katika siku ya Malipo. Kutozungumza bila ya kufikiria kabla juu ya kile unachotaka kukizungumza, Kutokufanya yale mambo ambayo yatakupelekea kua ni mwenye kujuta baadae, Kukaa mbali na mambo yasiyohusiana na Uislam. Kutopenda kujionesha. Kukikumbuka kifo na kujitayarisha nacho katika siku yeyote.'

Imam Al Asbati alisema kua: **'Kila mtu unavyomhitaji Mola wako basi ndivyo unavyozidi Kumuabudu na kumtii, na kila unayoujua uwezo wake basi ndio unavyozidi mtetemeko na khofu yako juu yake.**'

Alisema Imam Al Asbati kua: **'Kama mtu akiniamini mimi kuniachia Nyumba ambayo imejaa Hazina ya kila mali basi nitajiaminisha bila ya Wasi wasi, lakini kamwe asiniaminishe mtu kwa kuniachia Mtumwa mweusi Mwanamke, kwa sababu sifikirii kua mimi mwenyewe nitaweza kujiaminisha Nafsi yangu.'**

IMAM KHALIL IBN AHMAD 100 AH

Imam Khalil Ibn Ahmad alizaliwa mnamo mwaka 100 Al Hijra katika ardhi ya Basra nchini Iraq, ambapo inasemekana kua baba yake Imam Khalil Ibn Ahmad ndio mtu wa mwanzo kuanza kupewa na kutumia jina la Ahmad baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Imam Khalil Ibn Ahmad alikua ni mtaalamu mkubwa sana wa Ilm ya *Lugha na Nahau* miongoni mwa Tabiina, ingawa alikua na utaalamu wa Ilm ya Hadith na Fiqh pia.

Kwani Imam Khalil Ibn Ahamd alisoma kwa Imam Ayub Al Sakhtiyani, ambapo anasema Imam Hammad Ibn Zayd kua: **'Kila Khalil Ibn Ahmad alikua ni mfuasi wa Imani ya Ibadhi hapo kabla, lakini *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimpandisha Darja pale alipompa nafasi ya kuzungumza na Ayub Sakhtiyani na hivyo akahamia katika Imani ya *Ahl Al Sunnah wa Al Jamaah*'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Khalil Ibn Ahmad alisoma pia kwa Imam Asim Ibn Ahwal, Imam Awwab Ibn Khawsab, na Maimamu wengineo, na hivyo yeye akawasomesha kina Imam Harun Ibn Musa An Nahwi, Imam Hammad Ibn Zayd, Imam Nadr Ibn Hawsab, Imam Asim Ibn Al Ahwal, Imam Wahb Ibn Jarir n.k.

Safari moja Imam Khalil Ibn Ahamd alienda katika Ibada ya Hija na alipofika kwenye Al Kaabah basi akaomba Dua kua ajaaliwe Ilm ambayo hakuna aliepewa, na hivyowatu wanufaike na Ilm hio kutoka kwake, na aliporudi katika Ibada ya Hija basi akawa na Ilm kubwa ya Al Arudh.

Imam Khalid Ibn Ahmad alikua ndie muanzilishi wa uboreshaji wa mfumo wa *Ilm Al Arudh* ambayo ni Ilm ya Lugha ya mashairi kuhusiana Bahri, Vina, Mizani n.k na matumizi yake kiusahihi katika Lugha.

Na anasema Imam Hamza Ibn Hasan Al Isfahan kua: **‘Wanazuoni kama Khalil Ibn Ahmad ni wachache sana kwani yeye ndie alievumbua Ilm mpya kabisa ya Al Arudh ambayo ilikua haina kanuni lakini alipokuja yeye basi akaibainisha Kanuni yake na kuifanya kua na mfumo kamili.’**

Imam Khalil Ibn Ahmad alikua ni mtu mcha Mungu sana, mwenye ufahamu mkubwa, mnyenyekevu na mwenye kukubalika sana, ambapo miongoni mwa vitabu vyake maarufu ni pamoja na Kitab Al Ayn ambacho ni Kamusi la Lugha ya Kiarabu, Kitab Al Arudh, nk.

Imam Nadr Ibn Shumayl anasema kua: **‘Khalil Ibn Ahmad alikua ni mtu mnyenyekevu sana.’**

Ambapo kwa upande wa Al Sirafi basi yeye anasema kua: **‘Khalil Ibn Ahmad alikua ni mtu aliekua juu sana katika Ilm ya Nahaw, alikua amekalikia, na Amir wa Basra alimwita Nyumbani kwake na kumtaka amsomeshee watoto wake, lakini Khalil akatoa mkate wake na kusema kua: ‘Wakati nnao huu pamoja nami basi sina haja na jambo hilo.’**

Gavana wa Ehwaz aitwae Sulayman Ibn Habib Al Azdi aliahidi kumlipa mshahara Imam Khalil Ibn Ahmad tangu alipoanza kujuana nae hadi atakapofariki, na hivyo safari moja Sulayman Ibn Habib Al Azdi alimualika Imam Khalil Ibn Ahmad, lakini Imam Khalil Ibn Ahmad hakutaka kumfuata Gavana huyo na hivyo akamwandikia barua na kumwambia kua:

‘Kutokana na msaada wako basi mimi niko salama na sina shida yeyote, na ingawa mimi si mtu Tajiri lakini sijawahi kumuona Mtu akifa kwa udhaifu, na hakua Ibn

Adam anaebakia katika hali hio hio milele, na riziki ni kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na kutokana na ukweli wa kua mtu anaeonekana kua ni dhaifu hua ni dhaifu lakini hata hivyo kuonekana kwake Dhaifu hakumpelekei yeye kua ni mwenye kuthaminika. Na muonekano wa mtu mwenye nguvu haumpelekei mtu huyo kua ni mwenye thamani zaidi juu yake.

Utajiri na Umasikini ni vitu ambavyo haviangaliwi kutokana na kua na Mali bali huangaliwa kutokana kile kilichomo ndani ya Moyo'

Hivyo baada ya Sulayman Ibn Habib kuisoma barua hio ya Imam Khalil Ibn Ahmad basi akaamua kukatisha kumlipa Mshahara Imam Khalil Ibn Ahmad, na hivyo baada ya hapo Imam Khalil Ibn Ahmad akaandika Barua nyengine na kumpelekea Sulayman Ibn Habib ambayo ilikua ikisema kua: **'Hakika uliahidi kua utanilipa hadi kufa kwangu, lakini hukua ni mwenye kutimiza ahadi hio, hivyo fahamu kua hukunipunguzia kitu isipokua kidogo tu, na inabidi ujue kua hutoweza kujiongezea Mali yako kutokana na kuukata Mshahara wangu.'**

Baada ya kusoma Barua hio basi Gavana Sulayman Ibn Habib akaandika Barua na kuomba Msamaha kwa Imam Khalil Ibn Ahmad na kisha akamtumia Mshahara wake na akaamua kumuongezea ziada juu yake.

Alihoji Imam Khalil Ibn Ahmad kwa kusema kua: **'Hivi jee kuna umuhimu gani wa kua na Marafiki wa Karibu na ukaribu wa Nyumbani pale inapokua hakuna ukaribu wa Moyoni?**

Imam Khalil Ibn Ahmad alisema kua: **'Pale unapotaka kuficha Kitu, kuhifadhi au kukiandaa basi huwezi kukipata kitu hicho kama amali njema, na muonekano mzuri wa kitabia hua ni miongoni ma Amali njema'**

Imam Khalil Ibn Ahmad alijielezea hali anayokua nayo wakati anapokua nyumbani kwake kwa kusema kua: **'Nnapokua ndani ya Mlango wa Nyumba yangu hua sifikirii kuhusiana na nje ya mlango wangu.'**

Imam Khalil Ibn Ahmad alisema kua: **'Wakati ambao Ufahamu wa Ibn Adam unakua uko safi na kua na afya zaidi ni wakati wa Alfajir'**

IMAM HASAN IBN SALIH 100 AH

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abu Abd Abd Allah Hasan Ibn Salih alizaliwa mnamo mwaka wa 100 Al Hijra katika maeneo ya Hamadan nchini Iran na alikua ni mwenye kujipataia Ilm yake ya mwanzo kutoka kwa Baba yake ambae ndie alikua Mwalimu wake wa mwanzo na baadae alihamia katika maeneo ya ardhi ya Iraq kwa ajili ya kujitafutia Ilm zaidi ya Dini ya Kiislam.

Imam Hasan Ibn Salih alikua na I’lm kubwa sana na alikua akiaminika, kwani alikua ni mwenye kusoma kutoka kwa Wanazuoni wakubwa wa Hadith akiwemo Imam Abu Is-haq, Imam Abd Allah Muhamamd Ibn Akil, Imam Amr Ibn Dinar, Imam Muhamamd Ibn Amr Al Alqamah, Imam Said Ibn Urwa na wengineo.

Ambapo anasema Imam Yahya Ibn Main kua: **‘Hasan Ibn Salih alikua ni Thiqah na ni mwenye kujiamini.’** Ambapo hadith zake Imam Hasan Ibn Salih ni zenye kupatika kwenye Sahih Muslim, Sunan At Tirmidhi, Sunan Abi Daud, Sunan An Nasai, na Sunan Ibn Majah.
Ambapo anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: ‘**Hadith za Hasan Ibn Salih ni Sahih kwani Al Faqih ni mtu ambae ni Makini sana kuhusiana na Hadith’** Hadith za Imam Hasan Ibn Salih zimenukuliwa pia na Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Waqi Ibn Jarrah, Imam Humayd Abd Rahman Al Rawasi na wengineo.

Ambapo anasema Imam Waqi Ibn Jarrah kua: **‘Hasan na ndugu yake aitwae Ali na Mama yao waliugawa Usiku wa siku zao mara 3 kiibada, ambapo kila mmoja miongoni mwao alikua akitumia sehem moja kati ya 3 za Usiku kiibada, na alipofariki Mama yao, basi wakawa ni wenye kuugawa Usiku katika sehemu 2 ambapo sehemu ya Kwanza ikasa inatumiwa na Ali na ya pil ikawa inatumiwa na Hasan, na alipofariki Ali basi Hasa akawa anaukhuisha Usiku wake wote Kiibada’**

Ambapo anasema Imam Abu Sulayman Ad Darani kua: **‘Khofu ya A*llah Subhanah wa Ta’ala* ilikua ni yenye kuonekana wazi kwenye uso wa Hasan Ibn Salih’**

Na Imam Ibn Saad basi yeye amesema kua: **‘Hasan Ibn Salih alikua ni Mcha Mungu sana mwenye kudumu kwenye Ibada kwa mda mrefu na mwenye Hadithi zilizokua sahih’**

Imam Hasan Ibn Salih anasema kua: ‘**Baada ya kutia Udhu wa kukoga Janaba basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua hatii udhu wa Sala.’**

Imam Hasan Ibn Salih anasema kua: ‘**Hali yangu baadhi ya wakati hua ni kama Dunia yote imo mikononi mwangu kwa utajiri wangu na kuna siku ambapo hua ni mwenye kuamka huku nikiwa sina kitu mifukoni mwangu.**’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Hasan Ibn Salih anasema kua: '**Kufanya Mema hua kuna unufaisha Mwili, kuna unawirisha Moyo na kuyatia Macho Nuru, ambapo kufanya Maovu hua kunauregeza Mwili, kunautia kiza Moyo na kunayapofua Macho.**

Imam Hasan Ibn Salih anasema kua: '**Ibilisi hua ni mwenye kufungua Milango 99 ya wema kwa ajili ya mtu ili kumfanya mtu huyo afanye Dhambi kubwa mara moja'**

Anasema Yahya Ibn Yunus kua: **'Kila ninapoenda Masjid kwa ajili ya kusali basi nilikua nikumuona Hasan Ibn Salih akiingizwa ndani huku akiwa hana fahamu, kwani alikua akitembelea Makaburi tu basi hua ni mwenye kukumbuka hali ya Kaburini na mitihani anayokutana mtu ndani yake, na hapo hua ni mwenye hisia nzito sana na kuanguka na kuzimia.'**

Imam Hasan Ibn Salih anasema kua: '**Kwa Usiku na Mchana hua ni vyenye kuvifaya vitu viya kua ni vya zamani, vya mbali kua ni vyenye kukaribia, kila ahadi kua kweli, na kila kilichozungumziwa kuangamia: 'Kwani Siku hua ni yenye kunadia kwa kusema: 'Enyi Ibn Adam labda hamtokua na siku nyengine zaidi badala yangu, kwani mnaweza mkafariki, bila ya kujua hivyo nitumieni mimi kua ni kama bahati, kwa kujishughulisha kufanya mema, ambapo na Usiku pia ha ni wenye kuusia hivyo hivyo.''**

IMAM AL YAMAN AL ASWAD

Imam Abu Muawwiyah Al Yaman Al Aswad aliishi katika mji wa Tartus nchini Syria katika kipindi alichoishi Imam Sufyan Ath Thawry na alikua na ukaribu sana na Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Ibrahim Ibn Adham na Imam Fufayl Ibn Iyadh.

Imam Al Yaman Al Aswad alikua akiwajali sana marafiki zake kiasi ya kua alikua yuko tayari vyovyote vile itakavyokua kua pamoja nao na kuwasadia wanapofikwa na mitihani kwani anasema Abu Muhammad Ibn Hayyan kua alikua akisema kua: **'Amesema Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Hasan kua amesema Muhamamd Ibn Is-haq kua: 'Ndugu zangu wote ni wema sana zaidi yangu mie'**' na alipoulizwa kwanini basi akasema: **'Hua ni wenye kunipendelea mimi zaid ya Nafsi zao, na yeyote yule anaenipendelea mimi zaidi ya Nafsi yake basi huyo ni mtu bora zaidi yangu mie'**

Na anasema Umar Ibn Ahmad kua: **'Mimi nimemsikia Abd Allah Ibn Daud akisema kua: 'Wakati Ali Ibn Fudayl alipofariki, basi Abu Muawwiyah alifunga safari kutoka Tartus hadi Makkah kwa ajili ya kumpa pole Fudayl Ibn Iyadh pale**

alipofiliwa na mtoto wake Ali ibn Fudayl, na akakaa huko bila ya kurudi hadi pale alipofanya Ibada ya Hija na kurudi''

Imam Al Yaman Al Aswad alikua ni Mcha Mungu mkubwa sana na ni mwenye Taqwa, kiasi ya kua ingawa mwishoni mwa Uhai wake alikua ni kipofu lakini alikua na Miujiza mikubwa sana kwani anasema Abu Zahirriyah kua: **'Nilienda mimi katika maeneo ya Tartus kukutana na Abu Muawwiyah Al Aswad katika nyumba yake baada ya kua ni kipofu, ambapo ndani ya Nyumba yake nikauona Msahafu ukiwa umewekwa Ukutani hivyo ni kamwambia : 'Allah akuingize kwenye Rehma zake ewe Abu Aswad, Una Msahaafu wakati hata kuona huoni'**

Ambapo nae akajibu: 'Ewe ndugu yangu, Jee unaweza kunitunzia Siri yangu? Hadi nitakapofariki?' nami nikasema: 'Naam' nae akasema: 'Kwa hakika pale nnapotaka kusoma Qur'ani kutoka kwenye Msahafu basi macho yangu hua ni yenye kuona kama kawaida''

Ambapo alisema pia Abu Hamza Nasir Ibn Faraj Al Islami ambae alikua ni mfanyakazi wa Imam Al Aswad kua: **'Ingawa Abu Muawwiya alipoteza macho yake, lakini pale alipokua akitaka kusoma Qur'an basi hua ni mwenye kuutafuta msahafu Nyumbani hadi akaupata, na mara tu baada ya kuupata na kuufungua basi hua ni mwenye kuona, na pale anapoufunga tu basi macho yake hupotea'**

Aanasema Abu Muhammad Ibn Hayyan Ibn Fadhl Al Aki kua: **'Abu Muawwiyah pamoja Na Jeshi la Waislam waliizingira Ngome ya Maadui katika vita, na ikawa mmoja kati ya Walinzi waliopo juu akawa anawapiga Mawe na Mishale Waislam, na hua hawakosi, hivyo Waislam wakamwambia Abu Muawwiyah Al Aswad, hivyo nae akasoma aya isemayo:**

﴿وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَٰكِنَّ ٱللَّهَ رَمَىٰ﴾

Wama ramayta idh ramayta walakinna Allaha rama *(Surat Al Anfal 8:17)*

Tafsir: ***Na hukurembea uliporembea lakini Allah ndie alierembea.***

Kisha akachukua Upinde akasema: Ya Rabb, hakika umewasikia walivyosema hivyo wape, kisha akasema Bismi Allahi na akauachia upinde huo ambao uliruka hadi kwenye sehemu aliyoka amekaa Mlinzi huyo na kumuua.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Alisema Imam Al Yaman Al Aswad kua : **‘Yule ambae anaekua na wasi wasi mkubwa kuhusiana na Dunia yake, basi kesho yake itakua na matatizo makubwa sana ndani ya Kaburi lake’**

Alisema Imam Al Yaman Al Aswad kua **: ‘Ewe Mja kama unajitakia kheri kwa ajili yako basi usilale usiku isipokua kwa mda mchache tu.’**

‘Fanya mema wakati mda unao, kimbilia kufanya Mema kabla ya kuangukia kwenye maumivu ya Kifo, pale utakapotishiwa kua pamoja na familia yako, utakapowaona wamekuzunguka lakini huna wa kumtegemea isipokua amali zako.’

Ewe Ibn Adam kua na subra kwani subra ndio kiongozi wa kila kitu na kutokana nayo hua kuna malipo bora zaidi, hivyo mkumbuke Mola wako kwa ajili ya hali yako ya hapo baadae itakavyokua na udhibiti ulimi wako kwa kuuchunga kutokana na kila unachotaka kukifanya.

Imam Abu Aswad Al Yaman alisema: **‘Ibn Adamu wote ni Wacha Mungu, na wale Waovu miongoni mwao hua ni wenye kukimbia katika sehemu ambayo ukubwa wake haufikii ukubwa wa bawa la Nzi’** na alipoulizwa ndio sehemu gani hio ambayo ukubwa wake haufikii hata bawa la Nzi basi akasema: **‘Dunia.’**

IMAM IBRAHIM IBN ADHAM 101 AH

Imam Ibrahim Ibn Adham Ibn Mansur At Taymi Al Balkhi alizaliwa mnamo mwaka 101 Al Hijra katika Mji wa Balkh. Imam Ibrahim Ibn Adham alitokana na familia ya kitajiri ya miongoni mwa watu wa Balkh ambapo yeye alijitolea na kuachana na kuachana na kufuatilia utajiri wenye manufaa ya Kidunia na kuanza kufuatilia utajiri wa Ilm ya Dini kwa ajili ya manufaa ya kiakhera.

Imam Ibrahim Ibn Adaham alikua ni mtu mwenye Ilm ya Fiqh, Taqwa na Imani ya kweli juu ya Mola wa Ulimwengu wote ambae ni *Allah Subhanah wa Ta’ala*, kiasi ya kua alikua akijulikana pia kama Chifu wa watu walioachana na Dunia kwani kwake yeye Dunia ilikua haina thamani hata chembe ni sawasawa na vumbi chini ya viatu vyake.

Ambapo kuna mtu alimfuata na kumuuliza Imam Ibrahim Ibn Adham kwa kusema: ‘**Ewe Abuu Is-haq hivi kwanini Moyo wangu mimi hauwezi kumfikiria *Allah Subhanah wa Ta’ala* kila wakati?**’ Imam Ibrahim Ibn Adham akajibu: ‘**Kwa sababu Moyo wa Ibn Adam hua unapenda vile ambavyo vimekatazwa na Mola wake, kwa kuipenda Dunia na kuzama kwenye mambo ya kijinga.**’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ibrahim Ibn Adham alikua ni mkulima na ni mwenye kuachana kwa mbali sana na makatazo ya Mola wake na hivyo alikua ni mwenye kujibiwa Dua zake na hivyo alikua akiwausia watu kwa kusema: '**Kuleni kilicho halali yenu na kisha Muombeni Allah kwa chochote mkitakacho katika maombi yenu.**'

Ambapo anasema Imam Sufyan Ath Thawri kua: '**Ibrahim Ibn Adham alikua anafanana na Nabii Ibrahim kwa sifa zake, kiasi ya kua kama angekua anaishi pamoja na Masahaba basi angekua ana sifa za upekee miongoni mwao.**'

Kwani alikua akisema Imam Ibrahim Ibn Adham kua: '**Kuachana na Dunia ni Wajibu, kwani ni kwa ajili ya usalama na manufaa yake Ibn Adam, ambae hua na Wajibu katika kuachana na yaliyoharamishwa, hua na Usalam katika yenye kua na shaka ndani yake na hua na manufaa katika kujipatia vilivyo halali yake.**

Safari moja Imam Ibrahim Ibn Adham alikua akisafiri Baharini kwenye Jahazi pamoja na watu wengine ndani yake, mara ghafla usiku wakati Imam Ibrahim Ibn Adham akiwa amelala basi hali ya hewa ikabadilika upepo ukawa mkali na mawimbi yakawa makubwa zaid, hivyo hali ya Jahazi na Abiria wake ikawa iko hatarini watu wakaanza kuomba dua na wengine wakilia, vilio ambavyo vilimuamsha Imam Ibrahim Ibn Adham ambae nae akaamka na kutaka kujua ni nini kinachoendelea.

Baada ya kuuliza akaambiwa kuhusiana na hali ya Bahari ilivyokua, hivyo Imam Ibrahim Ibn Adham akasimama kisha akanyanyua mikono yake juu na kuomba dua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema: '**Ya Allah hakika wewe umetuonesha Sifa ya Ukubwa wake na Uwezo awako, hivyo nakuomba kua sasa hivi Utuoneshe sifa ya Wingi wa Rehma na Usamehevu wako**' na kisha baada ya hapo haikuchukua hata dakika isipokua hali ya Maji ya Bahari ilitulia tulii na kua kama vile hali ya Mafuta yaliyotiwa ndani ya Bakuli na kuwekwa juu ya Meza.

Siku moja Imam Ibrahim Ibn Adham alifuatwa na mmoja kati ya Wanafunzi wake ambae alimwambia Imam Ibrahim Ibn Adham kwa kusema: '**Ya Imam, hakika mimi hua nnajitahidi kujidhibiti ili nisifanye Dhambi lakini nashindwa, hivyo nakuomba unisaidie kwa kunipa ushauri nifanyeje?'**

Ibrahim Ibn Adham akasema: '**Nnakupa Masharti Matano ambayo kama utayaweza na kuyafanyia kazi basi bila ya shaka utakua ni mwenye kuweza kujidhibiti Nafsi yako**'

Manafunzi akasema: '**Naam, nakusikiliza masharti gani hayo?**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: ‘**Kwanza Unapotaka kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Inabidi usile kitu chochote kile alichokuruzuku yeye’**

Mwanafunzi akashangaa na kusema: ‘**Sasa itakuaje nisile chochote alichokiruzuku yeye wakati kila kitu kinatoka kwake?**’

Imam Ibrahim Ibn Adham akasema; ‘**Kwa Hivyo Jee ni Haki Kula Riziki yake anayokupa na hapo hapo Kumuasi?**’

Mwanafunzi akasema: ‘**La si Haki, haya sema la pili.’**

Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: ‘**Pili ni kua Unapotaka kumuasi basi Nenda katika Sehemu ya Ulimwengu ambayo sio yake, Mwanafunzi akauliza tena: Hio ndio haiwezekani zaid, sasa mimi nitaishi wapi? Kwa sababu Yeye ndie alieumba Ulimwengu.**’

Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: ‘**Hivyo Jee kweli ni Haki kumuasi wakati ukiwa katika Ardhi yake?’**

Mwanafunzi akajibu: ‘**La, hivyo bora niambie la tatu.’**

Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: ‘**Tatu ni kua mbali ya kua unapotaka Kumuasi basi Usile riziki yake, Usifanye dhambi kwenye ardhi yake lakini pia Inabidi utafute sehemu ambayo hatokuona.**’

Mwanafunzi akajibu: ‘**Huu unakua wazimu sasa kwa sababu Allah Anaona na anajua kula kitu kinachotokea hata kwa kificho.**’

Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: ‘**Hivyo Jee ni Haki kuamisi wakati Unaula Riziki yake, Kuishi kwenye Ardhi yake na pia unajua kua kokote pale ulipo anakiona?’**

Mwanfunzi akajibu: ‘**La Bila ya shaka si Haki..na la nne?’**

Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: ‘**Nne ni kua Anapokuja *Malakat ul Maw*t kuchukua Roho yako, basi Mwambie kabla ya Kuchukua Roho yako kua akupe mda ili utubu kabisa na kufanya mema kwanza.**’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Mwanafunzi akasema: '**Hata kama ingekua nitamuona basi asingeweza kunisikiliza na kunikubalia, hivyo unajua kua hio haiwezekani, haya niambie hilo la tano.'**

Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: '**Tano ni kua Ukishafariki watakapokuja Malaika wa kukupeleka Motoni basi usikubali kuenda nao.**'

Mwanafunzi akacheka na kusema: '**Kama huwajui Malaika vile, Watanipeleka nikitaka nisitake..Naam Ya Imam, itanibidi kurudi kwa Mola wangu na kufanya Istighfar.**'

Naam..huo ndio Ushauri wa Imam Ibrahim Ibn Adham kwangu na kwako pia na kila mwenye Kutafakkari, hivyo kufanya Istighfar ni lazima ambapoanasema Imam Al Hujwiri kua: '**Imam Ibrahim Ibn Adham alikua ni Mwanafunzi wa Al Khidr.**'

Na aliulizwa Imam Ibrahim Ibn Adham: '**Hivi kwanini sisi tunaomba Dua lakini hazijibiwi?**' **Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: 'Kwa sababu nyinyi mnamjua *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini hamumtii maamrisho yake, Mnamjua Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* lakini hamumfuati Suna zake, Mnaijua Qur'an lakini hamshikamani nayo, Mnakula Neema za *Allah Subhana wa Ta'ala* lakini hamumshukuru, Mnaijua Pepo lakini hamuikimbilii, Mnaujua Moto lakini hamuukimbii, Mnamjua Shaytani lakini hampigani nae, bali mnashirikiana nae, Mnakijua Kifo lakini lakini hamjitayarishi nacho, Mnazika Maiti wenu lakini lakini hamjifunzi kutokana na vifo vyao, Na mnadharau makosa yenu na badala yake mnaangalia makosa ya wengine.**'

Kwani Imam Ibrahim Ibn Adham aliulizwa siku moja: '**Hivi kwanini wewe hutaki kukaa pamoja nasi ukazungumza nasi kuhusiana na Mambo ya Dini, kwani tutanufaika sana na Ilm yako.**'

Ambapo Imam Ibrahim Ibn Adham akasema: '**Kuna mambo manne ambayo mimi hua yananitia wazimu sana na hivyo sina mda wa kukaa na watu kutokana na kuyafikiria mambo hayo.'**

Imam Ibrahim Ibn Adham alipoulizwa: **'Jee ni Mambo gani hayo?'**
Basi akajibu: **'Ni mambo yafuatayo:**

1-Ni kuhusiana na Ile siku ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* alichukua Ahadi kutoka kwa Watu wake: *Allah Subhanah wa Ta'ala* alisema kua kuna baadhi

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ya Watu watakua ni wenye kuenda Peponi na huku wengine Watakua ni wenye kuenda Motoni, Hivyo Mimi sina utulivu kwa sababu sijui ni Mtu nitakae elekea wapi, kwani sijui nipo katika kundi gani.

2-Ni kuhusiana na Wakati ambao Mtoto anapokua ndani ta Tumbo la Mama yake, Wakati Malaika wanapomuuliza Allah Subhanah wa Ta'ala kuhusiana na Majaaliwa ya Mtoto huyo ni ya wapi? Hivyo mimi sijui Majaaliwa yangu ni yepi.

3-Ni kuhusiana na Malaika wa Kifo anapochukua Roho za Watu, hua ni Mwenye kumuuliza *Allah Subhanah wa Ta'ala* roho hio inaelekea wapi kwa Walioamini ama Waliokufuru? Hivyo Mimi sijui Jibu atakalojibiwa Malaika wa Mauti atakapouliza Juu ya Roho yangu.

4-Ni kuhusiana na Siku ya malipo ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakaposema 'Tenganeni Enye Nyote Wenye Hatia' Hakika Mimi Sijui katika Siku hii nitakua katika Upande gani.

Kwani inabidi tujue kua Mtu mwenye kutafakkar na kujua hali yake mbele ya Mola wake basi hua ni mwenye hali nne zifuatazo:

1-Hua ni Mtu aliekinai na hivyo hua si mwenye kuyakimbilia Matamanio ya Kidunia.

2-Hua ni mtu mwenye kukosa Utulivu kama ilivyokua kwa Imam Ibrahim Ibn Adham kuhusiana na Akhera yake na hivyo hua ni mwenye kukimbilia kufanya mema zaidi kwa ajili ya Akhera yake.

3-Hua ni Mwenye kujitahid kuisoma na kuijua Dini yake ili awe na uhakika kuhusiana na namna anavyotakiwa kuzifanya Ibada zake na kusimamia Majukumu yake mbele ya Mola wake na Viumbe wenzake.

4-Hua ni Mwenye Kujijali Nafsi yake na Kuwajali Viumbe wenzake na kuwatakia Mema juu yao.

Safari moja Imam Sufyan Ath Thawry aliekea katika sehemu ambayo alikua anaishia Imam Ibrahim Ibn Adham, na hivyo Imam Ibrahim Ibn Adham akawatuma watu wakamwite Imam Sufyan Ath Thawry aje katika eneo lake azungumze, hivyo watu hao wakauliza: '**Inakuaje unamwita Mtu kama Sufyan Ath Thawry aje kuzungumza badaa ya sisi kumfuata yeye alikofikia**?'

Imam Ibrahim Ibn Adham akawaambia watu hao kua: ‘**Nataka kukuonesheni Unyenyekevu wake Sufyan Ath Thawry’** na hivyo Imam Sufyan Ath Thawry alipopata wito huo wa Imam Ibrahim Ibn Adham basi akaenda katika eneo hio na kusomesha Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.

Katika safari zake Imam Ibrahim Ibn Adham njiani aliona kisma hivyo akaenda kwenye kisima hicho na kushusha ndoo ya ya Maji na alipoileta juu basi akaiona kua imejaa Madini ya Fedha, hivyo akaimimina kwenye kisima kisha akaishusha tena ndoo hio na ilipokuja juu ikaja ikiwa imejaa madini ya Dhahabu, na hivyo akaimimina tena kisimani na kuiingiza tena ndoo na alipoivuta ilipokuja juu akakuta imejaa hazina, hivyo akairudisha tena ndani na kisha akasema: ‘**Ya Allah Hakika mimi sitaki Mali bali nataka maji ya kutia Udhu, hivyo nipe Maji’ na kisha akaivuta juu ndoo hio na safari hii ilipokuja juu ikawa imejaa maji safi na meupe.**

Imam Ibrahim Ibn Adham aliombwa atoe wasi ambapo nae akasema: **‘Fungeni kile kilichokua wazi na fungueni kile kilichofungwa miongoni mwa vitu vyenu’** watu wakasema **‘Hatujafaham**’ hivyo akasema: **‘Fungueni Vifuko vyenu vya Pesa kwa ukarimu na Fungeni Midomo yenu msiwe ni wenye kusema ovyo.’**

Imam Ibrahim Ibn Adham alikua na rafiki yake ambae siku moja alimuuliza: **‘Mimi nawe tumekua marafiki kwa mda mrefu, hivyo kama ukiniona nna kasoro yeyote ile basi nijuulishe’** ambapo Imam Ibrahmi Ibn Adham akasema: ‘**Ewe ndugu yangu hakika mimi sijawahi kuona kasoro yako, kwani mimi hapa nakuangalia kwa mtizamo wa jicho lililojaa upendo, hivyo hua nakuona kua wewe ni Mtu mzuri kwangu, kwa hivyo kama unataka kutafuta kasoro zako na aibu zako basi waulize wengine’**

Alisema Imam Ibrahi Ibn Adham kua: ‘**Katika siku ya Malipo basi mtu ataulizwa kuhusiana na hesabu zake mbele ya watu ambao ni wenye kumjua ili awe ni mwenye kuona aibu zaidi juu ya yale aliyokua akiyafanya’**

Na aksema tena: ‘**Tafuteni Ilm kwa ajili ya kufanya Amali njema, kwani wengi wenye kukosea juu ya hili. Kwa sababu utakuta watu wana Ilm kama mlima lakini amali zao njema ni kidogo sana kama chembe ya mchanga.’**

Imam Ibrahim Ibn Adham alikua ana shamba lake ambalo alikua akilivuna katika siku za mwezi wa Ramadhani na kisha kutolea sadaka mavuno yake yote katika mwezi huo wa Ramadhani, na hua niwenye kufanya Ibada Usiku kucha bila ya kulala ndani ya mwezi mzima, na alipolizwa inakuaje hadi ikawa anaweza kukaa bila ya kulala mwezi

mzima basi alisema: '**Nitalala vipi wakati ziwezi kujizuia kulia hata kwa sekunde moja, jee utalalaje katika hali kama hio?'**

Na alikua kila baada ya kumaliza kusali lazima ajizibe uso wake kwani alikua akisema kua: '**Hakika mimi nna khofu kua huenda Ibada yangu hii ikawa haikukubaliwa na hivyo nitapigwa nayo usoni kama tambara bovu'**

Alisema Imam Ibrahim Ibn Adham kua: **'Safari moja nilienda katika Masjid Al Aqsa na kulala kwa usiku mmoja baada ya kujificha kwenye mazulia ili wasimamizi wasinione wanapotaka kuufunga Msikiti wakati wa Usiku. Ulipowadia wakati wa usiku wa manane mara mlango ukafunguliwa na wakaingia watu 40 ambao wote walikua wamevaa kidaruwesh, kisha mzee kuliko wote miongoni mwao akakaa kwenye Mihrab na wakasali rakaa 2, kisha mmoja wao akawageukia wenzake na kusema'**

'Humu ndani leo hii kuna mtu ambae si miongoni mwetu, hivyo yule Mzee wao akasema: 'Naam, kuna mtu mpya yule pale ndie Ibrahim Ibn Adham, ambae hajawahi kusali kwa utulivu ndani ya moyo wake kwa miaka sasa' Imam Ibrahim Ibn Adham anasema kutuambia kua : 'Hivyo nami nikaona kua nimeshaonekana hivyo ikabidi nijitokeze na kuuliza: 'Naam ni kweli ila ni kwanini ikawa hivyo?' yule Mzee akaniambia: 'Kuna siku Ulinunua Tende katika Mji wa Basra, na hivyo kuna tende ambayo ilikua imeanguka chini na wewe ukaiona Tende chini na ukaiokota kwa kudhani kua ni yako, na hiyo kutokana na kuokota kwako huko Tende hio na kuichanganya na Tende zako basi ndio maana ukawa ni mwenye kukosa utulivu ndani ya Sala zako.''

Hivyo mii niliporudi nyumbani nikamfuata yule alieniuzia Tende na kumuomba msamaha wa kumuambia yaliyotokea ambapo nae akasema: 'Hii ni jambo ambalo limenigusa sana mimi kutokana na Imani yako, hivyo itabidi nami niwe kama wewe' na akafunga Duka lake na hivyo kua ni mwenye kumtumikia Mola wake tu.

Imam Ibrahim Ibn Adham alifariki mnamo mwaka 161 Al Hijra.

IMAM ABU MUAWWIYAH HUSHAYM IBN BISHR 104 AH

Imam Abu Muawwiyah Al Wasiti Hushaym Ibn Bishr Ibn Kasim Ibn Dinar Al Sulami alizaliwa mnamo mwaka 104 Al Hijra katika mji wa Baghdad, na alikua ni Mwanazuoni wa Ilm ya Hadith, Tafsir, Qiraa na Fiqh.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Al Wasiti alikua ni mwenye kuhifadhi hadith 20000 kwa Moyo, ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: '**Wakati hua ni wenye kuweza kubadilisha kila kitu lakini haukufanikiwa kuubadilisha Ufahamu Hushaym Ibn Bishr.'**

Hivyo Iman Abu Muawwiyah Hushaym Ibn Bishr alikua na ufahamu mzuri sana na pia ni Mcha Mungu sana kwani anasema Imam Ibn Abi Dunya kua: '**Husaym Ibn Bishr alikua akisali sala ya Al Fajir kwa Udhu wa Sala ya Isha kwa mda wa miaka 10 Mfululizo kabla ya kufariki kwake.'**

Imam Hushaym Ibn Bishr alisoma kutoka kwa Imam Al Zuhri, Imam Amd Ibn Dinar, Imam Mansur Ibn Zazan, Imam Husayn Ibn Abd Rahman Imam Abu Bishr, Imam Ayub Al Sakhtiyani, Imam Sulayman At Taymi, Imam Amr Ibn Abi Salama na wengineo.

Imam Hushaym Ibn Bishr alikua na Wanafunzi wengi pia Wanazuoni ambapo miongoni mwao ni Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Shu'bah Ibn Hajjaj, Imam Yahya Al Qattani, Imam Ziyad Ibn Ayub, Imam Malik Ibn Anas, Imam Wakii Ibn Jarrah, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Said Ibn Hushaym Bishr, Imam Ahmad Ibn Hanbal, n.k

Imam Hushaym Ibn Bishr alikua ni mwenye Darja kubwa sana ya Ilm na hivyo kua ni mwenye kufananishwa na Imam Al Zuhri ambapo anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua : **'Mimi nilikua na Hushaym kwa mda wa miaka minne, na sikuweza kumuuliza kitu chochote kile isipokua mambo mawili tu kutokana na ukubwa wake wa Ilm'**

Imam Hushaym Ibn Bishr alikua ni mwenye kudumu na *Dhikr Allah*, kwani kila baada ya kunukuu hadith alikua ni mwenye kusema *Subhanah Allah, au La Ilaha Illa Allah* kwani anasema Imam Ibn Nasr Ad Din kua: '**Hushaym Ibn Bishr alikua ni Thiqah anaeishi Baghdad na ni mwenye Ilm kubwa na ufahamu mkubwa sana, ambapo Wanazuoni wote wa Hadith wanamuamini na wamekubaliana na Ucha Mungu wake na Uadilifu wake**'

Ambapo Wahb Ibn Jarir anasema kua: **'Sisi tulimuuliza Shu'bah : 'Hivi jee tuaandike Hadith kutoka kwa Hushaym?' ambapo nae akasema: 'Naam, kwani uaminifu wake na ufahamu wake haupingiki''**

Anasema Imam Is-haq Ibn Izayyad kua: **'Mimi nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwenye Ndoto ambae alikua akiniambia: 'Sikiliza Hadith kutoka kwa Hushaym, kwani yeye ni mtu mzuri sana''**

Imam Wakii Ibn Jarrah nae anasema kua: **'Chukueni kila kitu mnachotaka kutoka kwenye maneno ya Hushaym, kama vile ambavyo nilivyofanya mimi.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Alisema Ammar kua: 'Kama Abu Awn na Hushaym wakihitilafiana basi maneno ya Hushaym hua ni yenye kukubalika zaidi kwa sababu yeye hua si mwenye kufanya makosa kwenye Hadith zake'

Imam Maruf Al Kharki nae akasema kua: **'Mimi nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam usingizini ambae alikua akisema kua: 'Ewe Hishaym, namuomba Allah akupe Ridhaa zake kutokana na kazi uifanyayo, kwa sababu kazi unayoifanya ni nzuri sana kwa Ummah wangu''**

Ambapo amesema Imam Abu Muawwiyah Hushaym Ibn Bishr kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kukoga Janaba katika siku ya Ijumaa bila ya shaka ni Haki ya Muislam na wacha kila mmoja wenu awe ni mwenye kunukia Manukato kuanzia Majumbani mwenu katika siku hio, na kama hatoweza kufanya hivyo basi Maji humtosheleza kufidia manukato badala yake''**

Ambapo amesema Imam Abu Muawwiyah Hushaym Ibn Bishr kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* amenipa mimi mambo matano ambayo hakumpa Mtume mwengine yeyote ambayo ni:**
1-Khofu imejazwa ndani ya Nyoyo za Maadui zangu.

2-Ardhi imejaaliwa kua ni tohara na Msikiti kwa ajili yangu, hivyo mtu yeyote katika Ummah wangu atakapofikwa na wakati wa Sala basi na Asali sehemu yeyote itakapomkuta.

3-Ngawira imejaaliwa kua Halali juu yangu, kwani haikua halali kwa Mitume wengine wote.

4-Nimejaaliwa kuwaombea watu wote.

5-Kila Mtume ametumwa kwa Watu wake ila mimi nimetumwa kwa watu wote.

IMAM SUFYAN IBN UYAYNAH 107 AH

Imam Sufyan Ibn Uyaynah Ibn Abu Imran alizaliwa mnamo mwaka 107 Al Hijra katika ardhi ya Mji wa Kufah katika nchi ya Iraq ambapo baba yake alikua ni Gavana wa Khalid Ibn Abdillah Al Qasr na yalipoangushwa Mamlaka yake basi Mzee Uyaynah Ibn Abu Imran akahamisha familia yake na kuhamia katika Mji wa Makkah ambayo ilikua na watoto wa kiume watano ambao ni Sufyan mwenyewe, na Muḥammad, Ibrahim, Adam na Imran.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ingawa Imam Sufyan Ibn Uyaynah alikua ni Mfanyakazi wa Muhammad Ibn Muzahim lakini alikua ni mwenye kujitahid kutafuta Ilm wakati bado akiwa mtoto mdogo, kwani alihifadhi Quran wakati kabla ya kutimia umri wa miaka 7 kwani alianza kusoma hadithi alipokua na umri wa miaka saba na alipokua na umri wa miaka 12 alikua tayari ni mwenye kuhudhuria Darsa za Imam Amr Ibn Dinar, Imam Zayd Ibn Asalam, Imam Al Aswad Ibn Qays, Imam Ziyad Ibn Allaqah, Imam Abu Is-haq, Imam Al Zuhri, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Al Qari Abd Allah Ibn Kathir Ad Dari n.k

Imam Sufyan Ibn Uyaynah aliusiwa na Baba yake pale alipotimia umri wa miaka 15 kwa kuambiwa kua: **'Ewe Mtoto wangu umri wa utoto tayari umeshakuacha Mkono, hivyo achana namambo yasiyokua siyo na jishikamanishe na watu wenye kufanya mema, na fahamu kua hakuna mtu atakaetosheka na Wanazuoni isipokua atakaewatii Wanazuoni hivyo kua ni mwenye utiifu juu yao na kua mwenye kutosheka kutokana nao, wahudumie na ikumbatie sehemu ya Ilm yao.**'

Hakika huu ulikua ni ushauri mzito na wenye maana sana kwa wenye kuufanyia kazi akiwemo Imam Sufyan Ibn Uyaynah mwenyewe kwani siku ya kwanza alipoenda katika Mji wa Makkah na kukutana na Imam Amr Ibn Dinar ambae alikua ndie Imam mkuu wa Hadith wa Mji wa Makkah basi anatuelezea hali ilivyokua kwa kusema:

'Tulipoenda katika Sala ya Dhuhr, basi nilimuona Mwanazuoni mzee akiwa amepanda Punda ambae alisema kwa kuniambia: 'Ewe Kijana nikamatie huyu Punda wangu mpaka nimalize Kusali Msikitini' nami niksema kumwambia Mwanazuoni huyo: 'La siwezi kukukubalia hadi pale utakaponiahidi kua utanifundisha baadhi ya Hadith unazozijua'

Mwanazuoni huyo akaniangalia na kuniona kua ni mdogo sana kiumri na hivyo akaniuliza: 'Halafu hizo Hadithi utazifanya nini?' nami nikamwambia: 'Mimi sitakia Hadithi Nyingi nataka hadithi nane tu' na hivyo akanihadithia hadithi 8 nami nikamkamatia Punda wake nae akaenda kusali, huku mimi nikijaribu kuhifadhi Hadithi hizo 8 na alipomaliza kusali akatoka na kuniambia: 'Jee umezifanya nini zile hadith 8 nilizokupa kabla ya kuenda kusali? Kwani umenifanya nirudi haraka kutoka katika Sala yangu.' hivyo nami nikamnukulia hadhithi hizo 8. Nae akaniambia: '*Baraka Allahu Fiik, Mashaa Allah* njoo kesho kwenye Darsa langu' huyo alikua ni Imam Malik Ibn Dinar'

Hivyo Imam Sufyan Ibn Uyaynah akaanza kua na ukaribu na Imam Malim Ibn Dinar kwa muda wa miaka minne alikaa nae huku akisoma Hadith kutoka kwake, ambapo pia akawa ni mwenye kusoma kwa Imam Az Zuhri, ambapo hawa ndio Wanazuoni wawili waliomuachia athari kubwa sana ya Ilm Imam Sufyan Ibn Uyaynah Kiilm.

Ambapo Imam Sufyan Ibn Uyaynah alipotimia umri wa miaka 20 basi alielekea katika ardhi ya Iraq katika Mji wa Baghdad na akawa ni mwenye kufuatwa na Wanafunzi mbali mbali wa Hadith ambapo Imam Abu Hanifa alipomuona akitoa Darsa basi alisema kuwaambia watu: **'Sasa hivi mtapata Ilm ya Amr Ibn Dinar'**

Anasema Imam Abd Rahman Al Mahdi kua: **'Hakika mimi sijawahi kumuona mtu mwenye Ilm miongoni mwa wenye Ilm ya hadith katika maeneo ya ardhi ya Tihama kama alivyokua Imam Sufyan Ibn Uyaynah**'

Ambapo Imam Abd Rahman Al Mahdi anaendelea kusema kua: **'Imam Sufyan Ibn Uyaynah ni mwenye kua na Ilm zaidi katika fani za Ilm za Quran na Hadith kuliko Imam Sufyan Ath Thawry'**

Imam Muhammad Idris Al Shafii nae anasema kuhusiana na Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: **'Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu ambae ni mwenye uwezo wa kufafanua maana ya Hadith kama alivyokua Imam Sufyan Ibn Uyaynah'** na akasema tena kua: **'Sufyan Ibn Uyaynah alikua hapendi kutoa Fatwa.'**

Imam Sufyan Ibn Uyaynah alisema kua: **'Mwenye kuongezeka kwa Ilm ya Dini katika ufahamu wake basi hua ni mwenye kuonekana katika kupungukiwa kwa mali zake Kidunia.'**

Ambapo amesema Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: **'Imam Sufyan Ibn Uyaynah ni Babu wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii katika fani ya Ilm ya Fiqh.'**

'**Hatua ya kwanza katika Ilm ni kusikiliza, halafu kua kimya halafu kua na umakini nayo, halafu kuihifadhi halafu kuifanyia kazi na kisha kuisambaza.**'

Ambapo alisema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: '**Wanapotajwa Wanazuoni basi Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua zinateremka.**'
Na akasema tena kua: **'Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hua zinapotosha isipokua kwa Wanazuoni wa Fiqh.**'

Imam Sufyan Ibn Uyaynah siku moja alipolala alimuona Imam Sufyan Al Thawry ambae katika wakati huo alikua ameshafariki na hivyo akamuuliza: '**Ya Ath Thawry hivi jee ni Amali gani ambayo imemfanya *Allah Subhanah wa Ta'ala* akupende?**'

Imam Sufyan Ath Thawry akasema: '**Kutokujua kitu juu ya Watu**' Imam Sufyan Ibn Uyaynah akasema kumwambia Imam Sufyan Ath Thawry: '**Naomba uniusie ewe Ath Thawry!**'

Imam Sufyan Ath Thawry akasema: '**Kifanyie kazi hicho nilichokuambia**' Imam Sufyan Ibn Uyaynah akasema: '***Allah Subhanah wa Ta'ala* akuingize kwenye Rehma zake ewe Ath Thawry, kwani huku kuna ndugu wengi wazuri na kila mmoja mongoni mwao anaweza akamuombea mwenzake katika siku ya Malipo.'**

Imam Sufyan Ath Thawry akasema: '**Ya Ibn Uyaynah, hakika mimi sitaki kujuana nawe tena kuanza leo. Hivi wewe umeshawahi kuona madhara yanayotokana na mtu mwengine yeyote yule zaidi ya unaejuana nae?** ' Imam Sufyan Ibn Uyaynah anaendelea kusema: '**Hapo hapo mimi nikaamka kutoka usingizini huku nikiwa nnalia kwa sauti**.'

Miongoni mwa Wanafunzi wa Imam Sufyan Ibn Uyaynah ni pamoja na Imam Al Amash, Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Zayd Ibn Aslam, Imam Abd Allah Ibn Dinar, Imam Yahya Ibn Main, Imam Abd Rahman Ibn Mahadi, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Ibn Jurayj, Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal, n,k.

Imam Sufyan Ibn Uyaynah alianza kusomesha Ilm ya Hadith alipokua na umri wa miaka 35, na bila ya shaka kwa Mwalimu wa Ilm ya Hadith basi huu ni umri mdogo sana kua ni mwenye kufundisha, lakini kutokana na Ufahamu wake basi Imam Sufyan Ibn Uyaynah ingawa alikua ni mdogo lakini alikua ni mwenye Ilm kubwa sana, na alianza kusomesha baada ya kulazimishwa na Imam Misar Ibn Khidam pale alipomwambia baada ya kukataa kwake kua: '**Hakika wewe umesoma Ilm ya Hadith kwa Imam Az Zuhri na Imam Amr Ibn Dinar**'

Imam Yahya Ibn Yahya Al Nishapuri anasema kua: **'Safari moja mimi nilikua na Sufyan Ibn Uyaynah na mara akaja mtu ambae alisema kwa kumwambia kua: 'Ewe Abu Muhammad mimi nakulalamikia wewe kuhusiana na fulani Bint fulani**' yaani akaimaanisha Mke wake mtu huyo. Ambapo Sufyan Ibn Uyaynah akatafakkari kidogo kisha akasema: '**Labda wewe ulimuoa kwa sababu ya kunyayua Darja yako**' Mtu huyo akasema: '**Bila ya Shaka Ewe Abu Muhammad.**'

Imam Sufyan Ibn Uyaynah akasema: '**Mtu yeyote yule anaeoa kwa sababu ya kujipandisha Darja basi atapewa mtihani wa kushuka kwa Darja yake, na aneoa kwa ajili ya Mali basi atapata Mtihani wa kufikwa na Umasikini, lakini yeyote yule atakaeoa kwa ajili ya Dini yake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamjaalia mtu huyo kupanda Darja na pia kua na Mali.'**

Kisha Imam Sufyan Ibn Uyaynah akaanza kumhadithia mtu huyo kisa kifuatacho kwa kusema kua: 'Sisi tulikua tuko ndugu wanne ambao ni Muhamamd, Ibrahim, Umran na mimi. Umran ndio mdogo mimi niko baina yao. Hivyo wakati

Muhamamd alipotaka kuoa basi akachagua Darja na hivyo akamuoa Mwanamke mwenye Darja ya juu kabisa na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akampa Mtihani wa kuadhirika. Umran nae akaoa Mwanamke kutokana na Mali yake na *Allah Subhanah wa Ta'ala* akampa Mtihani wa Umasikini kwani familia yake mwanamke huyo ilichukua kila kitu chake.

Hivyo mimi nikatafakkari hai yao, ambapo siku moja alikuja kwetu Muammar Ibn Rashid nami nikamwambia kuhusiana na tukio hilo la ndugu zangu hao nae akaniambia kuhusiana na Hadith ya Yahya Ibn Jaddah na Hadith ya Aisha ambapo Hadith ya Yahya Ibn Jaddah inasema kua: 'Mwanamke huolewa kwa mambo manne: Dini yake, Darja yake, Mali yake na Uzuri wake, hivyo mchagueni mwenye Dini na ndio mtanufaika'

Ambapo hadithi ya Aisha *Radhi Allahu Anha* inasema kua: 'Mwanamke bora ni yule ambae ni rahisi kumhudumia.' Hivyo mimi nikachagua mwanamke mwenye Dini na asiekua na mahari makubwa kulingana na Sunnah ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akanipa mimi Darja na Mali pamoja na Dini.'

Amesema Imam Muhamamd Idris Al Shafii kua: **'Aliambiwa Sufyan Ibn Uyaynah kua: 'Kuna watu wanatokna katika kila pembe ya Dunia na baadhi ya wakati hua unawakasirikia, hivyo wanaweza kuondoka na kuachana na wewe' Imam Sufyan Ibn Uyaynah akasema: 'Kwa hali hio basi watakua wajinga kama wewe kwa kuachana na chenye manufaa nao kutokana na ubaya wa tabia zangu''**

Alisema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: **'Kamwe usiwache kuomba Dua na wala usiruhusu mambo maovu uliyoyafanya kukuzuia kuomba Dua, kwani kwa hakika *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimkubalia Dua yake Iblisi mbali ya kua yeye ni muasi kuliko wote tunapozungumzia viumbe wa Allah.**'

Amesema Imam Ibn Wahb kua: **'Mimi sijawahi kuona Mtu mwenye Ilm kubwa sana ya Tafsir ya Qur'an kama Sufyan Ibn Uyaynah**' na Imam Ahmad Ibn Hanbal amesema kua: '**Hakika mimi sijawahi kuona mtu ambae ni mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith zaid ya Sufyan Ibn Uyaynah.**'

Imam Sufyan Ibn Uyaynah alihifadhi hadith 7000, lakini hakuwahi kuandika kitabu chochote, na alifariki mnamo mwaka 198 Al Hijra katika mwezi wa Jamad Al Akhira huku akiwa na umri wa miaka 91, ambapo anasema Al Hasan Ibn Umran Ibn Uyaynah kua: **'Baada ya Arafah na tulipofika Muzdalifah na Ami yangu Sufyan Ibn Uyaynah kumaliza maombi yake basi alikaa chini na kulala huku akiniambia: 'Hakika mimi nimewahi kutembelea sehemu hii mara 70 na katika kila mara hua nnaomba kwa kusema: 'Ewe Mola wangu Usiifanye mara hii kua ndio mara yangu**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ya mwisho kutembelea hapa, na mara hii naona haya kuomba tena' na hivyo akafariki katika mwaka huo '

IMAM ZUFAYR IBN HUZAYL

Imam Zufayr Ibn Huzayl alizaliwa mnamo mwaka 110 Al Hijra katika ardhi ya Isfahan alikua ni Mwanazuoni wa Ilm ya Hadith na ni mfuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kwani alikua ni Mwanafunzi mkubwa wa Imam Abu Hanifa kwani alisema Imam Abu Hanifa mwenyewe kuhusiana nae kua: **'Zufayr ni Mwanafunzi wangu mkalimifu kuliko wote.'** Na hivyo Imam Zufayr alikua na darja ya *Mujtahid* katika Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Tangu utotoni Imam Zufayr Ibn Huzayl alikua ni mwenye kuelelewa katika hali ya mazingira ya watu wenye I'lm kwani Baba yake ambae alikua ni Gavana wa Mji wa Basra na hivyo alimpeleka mtoto wake huyo kwa Wanazuoni wa Mji wa Basra kwa ajili ya kujipatia Ilm ya Qur'an na Hadith.

Na kisha baada ya hapo Imam Zufayr Abi Huzayl akahamia katika Mji wa Kufah na kuanza kusoma kwa Imam Abu Hanifa Ilm ya Fiqh na fani nyenginezo za Ilm ya Dini ya Kiislam na hivyo kua ni Mwanazuoni mwenye darja ya pili katika Wanazuoni wa Fiqh Madhab ya Imam Abu Hanifa, na pia Imam Zufayr alikua na urafiki wa karibu sana na Imam Daud At Tayi ambae alikua ni Mwalimu wake pia.

Imam Zufayr alikua ni Mtu mcha Mungu na aliechana kabisa na Dunia yake na hivyo Imam Zufayr alipooa katika Mji wa Kufah na Khutba ya Ndoa yake ilitolewa na Imam Abu Hanifa ambae alisema ndani yake Khutba hio kua: **'Zufayr ni mmoja kati ya Maiamamu wa Waislam, na ni mtu mwenye kujulikana sana kwa sifa za Heshima, Kujihesabia Nafsi yake na Kiukoo pia'**

Kuna wakati Imam Zufayr alitembelea Mji wa Basra na alipofika akakumbana na mvutano kuhusiana na kesi ya Mirathi kutoka katika miongoni mwa watu wa Mji huo, hivyo alipokabidhiwa kesi hio basi akaitatua kwa urahisi sana, ambapo hili ilikua ni jambo liliowavutia sana watu hao wa Mji wa Basra, na wakamuomba abakie nao ili awanufaishe

Hivyo Imam Zufayr akababakia katika Mji huo na akawa anasomesha na alikua na Wanafunzi wengi wakiwemo kina Imam Abd Allah Al Ansari, Khalfef Ibn Ayub, Hilal Al Ray na kadhalika.

Na hivyo Imam Zuyfar na hapo hapo akapewa Mamlaka ya kua Qadhi wa Mji wa Basra. Imam Zufayr alikua ni mtu ambae asiependa kukaa pamoja na watu wanaozungumzia

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

mambo ya Kidunia, yaani kama akikaa kwenye sehemu na kisha watu wakaanza kuzungumzia mambo ya kidunia basi yeye hau ni mwenye kuondoka kabisa.

Siku moja Imam Zufayr aliulizwa kuhusiana na Imam Abu Hanifa ambapo nae akasema: **'Sisi kwa Abu Hanifa ni kama Ndege Kijumba mshale mbele ya Mwewe.'**

Na aliulizwa Imam Al Muzani kuhusiana na Wanazuoni wa Fiqh wa Iraq ambapo nae akasema: **'Imam Abu Hanifa ni Imam na Mkubwa miongoni mwa Wanazuoni wakubwa wa Fiqh'** na alipoulizwa kuhusiana na Imam Abu Yusuf basi alisema: **'Abu Yusuf ni Imam anaefuatia kwa Kina Ilm ya Hadith na Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*'** na alipoulizwa kuhusiana na Imam Muhammad Ibn Hasan basi akasema: **'Muhammad Ibn Hasan ni Imam anaeelezea kwa kina Ilm Al Furuu'** na alipoulizwa kuhusiana na Imam Zufayr basi alisema: **'Zufayr ni Imam mwenye Uwezo wa hali ya juu sana katika makisio ya kiasi kwa kufananisha na kutofautisha'**

Kwani alikua akisema mwenye Imam Zufayr kua: **'Wakati tunatafuta ufumbuzi juu ya kitu basi, tunaangalia kama kuna Hadith juu ya jambo husika na kama ipo basi hua tunatatua kulingana na Hadith husika, na kuachana na Qiyas na kama hakuna basi hua ni wenye kutumia makisio.'**

Mnamo mwaka 150 Imam Abu Hanifa alipofariki basi Imam Zufayr alikua ni miongoni mwa Wanazuoni wanaotegemewa kwenye Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa, ambapo hata hivyo hakuishi mda mrefu sana bali kwa mda wa miaka minane tu ambapo alinufaisha sana kwenye Ilm ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa na ingawa alikua ni mwenye kua na mitizamo yake kwenye Fiqh ya Madhhab hayo lakini hata hivyo hakua ni mwenye kupingana na Mitizamo ya Mwalimu wake, yaani Imam Abu Hanifa. Ambapo alisema Imam Ibn Abd Al Barr kua: **'Zufayr Ibn Huzayl alikua n mtu mwenye Ufahamu mkubwa sana na akili nyingi, alikua ni Imam mwenye Misimamo na mwenye kuachana na Haramu mwenye kupenda kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ni mwenye kuaminika kwenye Ilm ya Hadith'**

Wakati Imam Zufayr alipokua anakaribia kufariki Dunia, basi Imam Abu Yusuf alimuusia kwa kumwambia: **'Zufayr andika Wasia'** ambapo Imam Zufayr akasema kua: **'Zufayr Mali hii itakua inamilikiwa na Mke wangu, ma hizi zitakua zinamilikua na Mtoto wa Kaka yangu'.**

Ambapo Imam Abu Yusuf na Maimamu wengineo waliokuwepo hapo wakashangaa kwanini Imam Zufayr akasema hivyo, kwa sababu wakati yeye anae kaka aliekua hai basi mtoto wa kaka yake hatopata kitu katika Mirathi lakini Maimamu hao wakakaa kimya. Na hivyo hawakuweza kujua alichomaanisha Imam Zufayr hadi pale alipofariki, kwani baada ya kufariki basi Mke wake Imam Zufayr akaolewa na Kaka yake Imam

Zufayr ambae alikua na Mtoto wa kiume na hivyo hii ikawa inamaanisha kua Mtoto huyo atamrithi Kaka yake Imam Zufayr .

IMAM AL FUDAYL IBN IYADH 110 AH

Ingawa mwanzoni alikua ni Muasi lakini ulipowadia mda wa kuachana na Ulimwengu na kurudi kwa Mola wake, basi siku moja *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimuonesha njia hivyo nae akaamua kuifuata.

Kwani siku hi Fudayl Ibn Iyadh alikua amepanda Juu ya Nyumba yake, na mara akasikia kutoka katika Nyumba ya pili inasomwa *Surat Al Hadid* ambapo Msomaji huyo alikua amefikia katika aya ya 16 ambayo inahoji kwa maneno yasemayo:

﴿أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوٓاْ أَن تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ ٱللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ ٱلْحَقِّ وَلاَ يَكُونُواْ كَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْكِتَابَ مِن قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ ٱلأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ﴾

Alam ya/ni lilladheena amanoo an takhshaAAa quloobuhum lidhikri Allahi wama nazala mina alhaqqi wala yakoonoo kaalladheena ootoo alkitaba min qablu fatala AAalayhimu al-amadu faqasat quloobuhum wakatheerun minhum fasiqoona *(Surat Al Hadid 57:16)*

Tafsir: ***Hivi Jee haujawadia wakati kwa wale walioamini, kua Nyoyo zao ziwe nyenyekevu kujisalimisha kutokana na kukumbushwa juu ya Allah na kile kilichoshushwa kwa haki? Na wala wasiwe kama wale ambao waliopewa vitabu hapo kabla na kisha wakaongezewa mda kwa ajili yao na Nyoyo zao zikawa Ngumu? Na wengi miongoni mwao walikua ni wenye kufanya dhambi***

Naam..Haya ndio maneno ambayo yalimzindua Fudayl Ibn Iyadh na kumgusa sana kiasi ya kua hapo hapo alianza kulia kama mtoto mdogo na kuanza kujuta kuhusiana na Makosa yake yote aliyokua akiyafanya hapo kabla na kusikitika huku akisema: '**Hivi kwa nini haujafika Wakati wangu mimi wa kua na khofu nawe Ewe Mola wangu?**'

Kisha baada ya hapo akaamua kufanya Hijra kutoka katika Maisha yake aliyokua akiyaishi hapo kabla ya kuyasikia maneno ya Aya hii, na kuamua kuhamia kwenye Maisha mapya baada ya Kuzinduliwa na maneno haya.

Hivyo Fudayl Ibn Iyadh akahama katika Mji wake wa Samarqand na moja kwa moja akaanza kutafuta Ilm katika Miji myengine ya Kiislam kuanzia Kufah, Basra hadi katika Mji wa Makkah ambapo katika safari yake hio basi aliwahi kua Mwanafunzi wa Imam Nuuman Ibn Thabit yaani Imam Abu Hanifa. Na alipowasili katika Mji wa Makkah basi alikua tayari ameshaujaza Ufaham wake na Ilm ya kutosha juu ya Mola wake.

Imam Fudayl Ibn Iyadh akawa ni mwenye kuishi kwenye Ardhi ya Mji wa Makkah na kua ni Mhudumu na Msimamizi wa Jengo la Al Kaabah na ni katika kipindi hiki Fudayl Ibn Iyadh alikua ni Mtu ambae asiecheka ovyo kwani kila wakati alikua ni mwenye kutafakkar yale yote aliyoyafanya hapo kabla, na kua ni mwenye kuona haya juu ya Mola wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na Makosa yake mbele yake.

Kiasi ya kua Ilikua Fudayl Ibn Iyadh kila akisikia Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi alikua analia kwa Majuto na hisia za khofu ya Adhabu za Mola wake.

Ambapo anasema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: '**Hakika mimi sijawahi Kukutana na Mtu anaemuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama Fudayl Ibn Iyadh.'**

Na anasema Imam Abu Ali Al Razi kua: '**Hakika mimi niliishi kwa mda wa Miaka 30 na Fudayl Ibn Iyadh lakini sikuwahi kumuona akiwa ni mwenye Kucheka au kutabasam, isipokua katika Siku ambayo alifiwa na Mtoto wake wa Kiume. Alipoulizwa kwanini akawa anacheka basi akasema: Allah amepanga Mipango yake nami nimeridhika na kujisalimisha katika Mipango yake aliyopanga.'**

Imam Fudayl Ibn Iyadh alikua ni mtu mwenye kupenda kukaa peke yake na kivyake vyake, kwani alikua ni mtu ambae anaogopa kua atakapokaa pamoja na Watu basi watu watamtukuza na kumpandisha Darja kutokana na Ilm yake na hivyo hali hii huenda ikampeleka kua ni mwenye kujiona ndani ya Nafsi yake. Hivyo ilikua kila anapokua peke yake basi anajikumbusha Madhambi aliyoyafnya hapo kabla na kuendelea kujuta na kufanya toba kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ili amsamehe Madhambi Yake.

Kwani anasema Imam Ashath kua: '**Siku Moja mimi niliingia Msikitini nikamuona Fudayl Ibn Iyadh akiwa anairudia na kuirudia ile aya isemayo:**

﴿وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ ٱلْمُجَاهِدِينَ مِنكُمْ وَٱلصَّابِرِينَ وَنَبْلُوَ أَخْبَارَكُمْ﴾

Walanabluwannakum hatta naAAlama almujahideena minkum waalssabireena wanabluwa akhbarakum *(Surat Muhammad 47:31)*

Tafsir: ***Na Tutakujaribuni hadi Tutakapowajua Wenye Kufanya Jitihada Miongoni mwenu na Wenye Subra Na Tutakujaribuni Ukweli wa Habari zenu Kama wakweli au Waongo***

Kwa wanaofaham basi haya maneno ya Aya hii ni Mtihani Mkubwa Sana! Na ndio maana Imam Fudayl Ibn Iyadh alikua akiyarudia na kuyarudia na kisha akaanza kulia huku machozi yakimtiririka na akisema: '**Ya Allah! Hakika Kama utatujaribu basi sisi tutaishiwa na Matumaini ya kuokoka na kisha wewe utatudhihirishia kasoro zetu na kisha Utatuadhibu.'**

Kwani alisema Imam Fudayl Ibn Iyadh kua: '**Dunia hii si sehemu ya Kudumu bali ni sehemu ambayo Baba yetu Adam aliletwa kwa ajili ya Kuadhibiwa.**'

Na akasema tena Imam Fudayl Ibn Iyadh kua: '**Kwa Hakika Ladha ya Imani ya Dini ya Kiislam imeharamishwa kwa Nyoyo za watu hadi pale watakapokua ni wenye kuachana na Dunia yao.**'

Ambapo anasema Khalifa Harun Rashid kua: '**Hakika Mimi sikuwahi Kumuona mtu kama Fudayl Ibn Iyadh, kwani aliniusia mimi kwa kusema kua: Niufanye Moyo wangu kua ndio Nyumba yangu iliyojaa Khofu na Huzuni kuhusiana na Siku ya Malipo. Kwani Vitu hivyo ndivyo vitakavyo ufanya Moyo wangu kua ni wenye Kuzikimbia Dhambi na Kuuepuka Moto wa Jahannam.**'

Na anasema Fadhl Ibn Rabi kua: '**Nilifuatana mimi na Khalifah Harun Rashid kwenye Ibada ya Hija, ambapo baada ya kumaliza Ibada hio basi akaniuliza mimi: Hivi Jee Kuna Mja wa** *Allah Subhanah wa Ta'ala* **ambae tunaweza kumtembelea?'**

Nami Nikajibu: **'Naam Yuko ambae anaitwa Imam Abd Al Razzaq Al Sanaani.'**

Hivyo tukatoka hadi kwa Imam Abd Al Razaq Al Sanaani na tukazungumza nae kwa mda, na tulipotaka kuondoka basi Khalifa Harun Rashid akaniomba mimi nimuulize Imam Abd Razak kama anadaiwa na Mtu yeyote yule, ambapo Imam Abd Razak Al Sanaani akasema: **'Naam'**, hivyo Khalifa Harun Rashid akaamrisha watu wake kua wanaomdai Imam Al Sanaan walipwe kutokana na pesa zake Khalifa Harun Rashid.

Tulipotoka Khalifa Harun Rashid akaniambia kwa kusema: **'Ewe Al Fadhl Hakika mimi Moyo wangu unataka kuonana na Mtu mwenye Ilm zaid ya huyu.'**

Nami nikamwambia: '**Twende kwa Imam Sufyan Ibn Uyaynah, na tulipoenda basi ziara yetu ilimalizika kama ilivyomalizika kwa Imam Al Sanaani, yaani Khalifah Harun Rashid akaamrisha kua alipiwe madeni yake kutokana na Pesa zake.**

Kwani hivyi ndivyo walivyokua Viongozi wa Kiislam wenye kujua Majukumu yao, walikua hawajali kuhusiana na maslahi yao tu, bali walikua wakijali na ya Watu wao, Wanazuoni wao na pia kuhusiana na Akhera yao.

Naam..Imam Fadhl Ibn Rabu anaendelea kutuambia kua: **‘Khalifa Harun Rashid akasema: ‘Hakika mimi nakumbuka kua Imam Fudayl Ibn Iyadh yupo katika Mji huu hivyo wacha twende tukamtembelee.’**

Hivyo tukatoka na Khalifa Harun Rashid hadi kwa Imam Fudayl Ibn Iyadh, tulipofika tukamsikia anasoma Qur'an nasi tukamgongea Mlango, Imam Fudayl Ibn Iyadh akasoma kisha akanyamaza na kuuliza: **‘Nani?’** Nami nikajibu: ‘**Ni *Amir Ul Muuminin* Harun Rashid’**

Imam Fudayl Ibn Iyadh akasema: **‘Nimehusiana nini mimi na *Amir Ul Muuminina*?’**

Nami nikasema: ‘**Hivi Jee Hakuna Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua hakuna Mtu asietakiwa Kujinyenyekesha kwa ajili ya Kumtumikia *Allah Subhanah wa Ta'ala*?’**

Imam Fudayl Ibn Iyadh akajibu: ‘**Ndio lakini ni katika kuitafuta ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia kwenye hali ya Ukimya na Utulivu. Hakika nyinyi mnaona Unyenyekevu wangu lakini mimi nnaona upandaji wa Darja yangu’**

Kisha Imam Fudayl Ibn Iyadh akashuka kutoka alipokua amekaa akafungua Mlango na kisha akazima taa, na akakaa pembeni kabisa kiasi ya kua Khalifa Harun Rashid alipoingia ndani ilimbidi amtafute kwa kupapasa pasa kutokana na kiza.

Na mara mikono ya Khalifa Harun Rashid ikakutana na mikono ya Imam Fudayl Ibn Iyadh na hapo Imam Fudayl Ibn Iyadh akasema: ‘***Subhanah Allah*, hakika mimi sijawahi kuhisi mikono milaini kama yako, Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* aiharamishie mikono hii kutokana na Moto wake**.

Hapo hapo Khalifa Harun Rashid akazidiwa na Hisia akashindwa kujizuia na akaanza kulia kisha akasema: **‘Ewe Fudayl nakuomba uniusie!’**

Imam Fudayl Ibn Iyadh akasema: ‘**Ewe *Amir Ul Muuminin* Hakika wewe unatokana na kizazi cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo Mzee wako Al Abbas ni Ami yake. *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo Al Abbas alimuomba *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ampe Mamlaka juu ya Watu.**

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamjibu kwa kumwambia: ‘**Ewe Ami yangu hakika mimi nitakupa nafasi moja tu ya kua na Mamlaka juu ya nafsi yako, kwani kua na nafasi ya kuidhibiti nafsi yako kwa ajili ya kumtii, Mola wako ni bora kuliko kua na udhibiti wa miaka 1000 juu ya jamii ya watu kwani udhibiti wa nafsi hukuwezesha kupata usamehevu katika siku ya malipo.**’

Ambapo alicholenga Imam Al Fudayl Ibn Iyadh hapa ni kua Bora Mtu uwe na Jukumu la Kuisimamia na Kuidhibiti Nafsi yako kutokana na Kutomuasi Mola wako, kuliko kupewa Jukumu la kuwasimamia watu kwa miaka 1000 kwani katika kuwasimamia kwako basi utakua na masuali ya kujibu juu ya nafsi yako na nafsi za waliopo chini yako. Ambapo hii ni hali ambayo inakua vigumu kujitatua kwani unakua na mzigo mzito juu yako utaulizwa namna ulivyowasimamia watu wako.

Nao watakukimbilia na kukudai haki zao..hapo ndipo kwenye Mtihani kwani utahukumiwa Dhidi ya haki za Mola wako, dhidi ya Nafsi yako na Dhidi ya Nafsi za Waliochini ya Mamlaka yako. Lakini unapokua na jukumu la kusimamia nafsi yako tu basi utahukumiwa na kujibu Masuali baina yako na Mola wako tu ambae huenda akakusamehe.

Hivyo Khalifa Harun Rashid akamwambia Imam Al Fudayl Ibn Iyadh kua: ‘**Endelea Kunipa Mawaidha zaidi ewe Al Fudayl’**

Imam Al Fudayl akasema: ‘**Ewe *Amir ul Muuminin*, Faham kua wakati *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Abd Al Aziz alipoewa cheo cha Ukhalifa basi alimchagua Imam Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab na Imam Rajaa Ibn Hayat na pia Imam Muhammad Ibn Kaab Al Qurazi na akawaambia kwa kuwahoji: ‘Hivi Jee mimi nnatakiwa kufanya Nini kuhusiana na Huu Mtihani wa Ukhalifa niliopewa?, kwa sababu mimi nauhesabu kua ni Mtihani, Lakini watu wanaona kua ni Neema!***’*

‘**Hivyo Imam Salim Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamwambia Khalifa Umar Ibn Abd Ul Aziz kua:**

Kwa hakika Kama unataka kua ni mwenye Kuokoka kesho Akhera kutokana na Adhabu z*a Allah Subhanah wa Ta'ala*, basi Wachukulie Watu Wazima walio chini ya Mamlaka yako kua kama ni Mababa na Mamama zako, Na Wachukulie Vijana kua kama Ndugu na Kaka zako, Na Wachukulie Watoto Kama Watoto wako.

Na Yachukulie Mamlaka ya Utawala wako Kama Mamlaka ya Ndani ya Nyumbani mwako na hivyo Watu wako kua ndio Familia yako, Hivyo Watembelee Wazee wako, Waheshimu Ndugu na Kaka zako na Waonee Huruma Watoto wako’

Imam Al Fudayl Ibn Iyadh akaendelea kwa kusema: ‘**Ewe *Amir ul Muumiin,* Harun Rashid Hakika mimi Nnakhofia Uzuri wa Uso wako Usije Ukaangamia Ndani ya Moto wa Mola wako, Hivyo Mche Mola wako, Muogope Mola wako Mtekelezee Majukumu yako juu yake kwa vizuri zaid kuliko hivi ufanyavyo.**’

Maneno haya yalimfanya Khalifa Harun Rashid kujawa na Machozi kutokana na kufahamishwa juu ya uzito wa Mamlaka yake na Majukumu yake kwa Nafsi yake, kwa watu wake na kwa Mola wake. Hivyo akasema: ‘***Subhanah Allah!* Naam bila ya shaka Neema aliyonineemsha *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni kubwa hivyo nami sina sababu kulalamikia juu yake.’**

Kisha Khalifa Harun Rashid akachukua Dinar 1000 za Dhahabu akamkabidhi Imam Al Fudayl Ibn Iyadh lakini hata hivyo Imam Fudayl Ibn Iyadh akakataa kupokea na akamwambia Khalifa Harun Rashid kua: ‘**Hizi Pesa Bora zitumie kwa njia Nyengine iliyo bora zaid kwani Ewe *Amir ul Muuminin* Hakika mimi nnaona kua Mawaidha yangu hayajakusaidia Kitu**.’

Khalifa Harun Rashid akauliza: **‘Kwanini Unasema hivyo?’**

Imam Al Fudayl Ibn Iyad akasema: ‘**Kwa sababu ingawa umenisikiliza lakini huna Uadilifu, kwani mimi nnataka kukuokoa wewe kutokana na Moto, lakini wewe unataka kuniangamiza mimi kwa kutumia hizi Dinar unazotaka kunipa, jee huo ndio uadilifu?**’

Kwani kuona hivyo basi Khalifa Harun Rashid akasema: ‘**Hivi Jee kwani Imam Fudayl Ibn Iyadh hudaiwi wewe?**’

Imam Fudayl Ibn Iyadh akajibu: ‘**Bila Ya Shaka Nadaiwa, Lakini Na Mola wangu kwani ananidai Utiifu wangu kwake, na Ole wangu kama ikiwa sikutekeleza Wajibu huo kwake**!’

Khalif Harun Rashid akaona bado Imam Al Fudayl Ibn Iyadh hajafaham kuhusiana na kwanini akataka kumpa Dirham 1000, kwani kusudio lake ni kua kama anadaiwa basi alipe madeni anayodaiwa kutokana na Dinari hizo na hivyo kua ni zenye kumpunguzia Mzigo. Hivyo akamuuliza tena Imam Fudayl Ibn Iyadh kwa kumwambia kua: **‘Ewe Imam Al Fudayl Hakika mimi nnazungumzia kuhusiana na Madeni ya Watu na wala si ya Muumba**’

Ambapo Imam Al Fudayl akajibu: ‘***Alhamd Lillah* Neema za Mola wangu Juu yangu ni Nyingi sana kiasi ya kua mimi sina Haja ya Kumlalamikia yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wala sina haja ya Kuwalalamikia Viumbe wake**’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na baada ya kupata Jibu hilo kutoka kwa Imam Fudayl Ibn Iyadh basi Khalifa Harun Rashid akamwambia mwenyeji wake ambae ni Imam Fadhl Ibn Raba kua: ‘**Bila ya Shaka Imam Al Fudayl Ibn Iyadh ni Mfalme juu ya Ardhi hii.**’ Na kisha wakaaga na Kuondoka.

Kwani alisema Imam Al Fudayl Ibn Iyadh kua: ‘**Dunia ni Nyumba ya Wenda Wazimu, Na kila aliemo Ndani yake ni Mwenda Wazimu ambae amevaa Pingu na Minyororo ambapo Matamanio ya Nafsi Ndio Pingu na Madhambi ndio Minyororo!’**

Na akasema tena: ‘**Yeyote yule anaemjua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ipasavyo basi hua ni mwenye Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ipasavyo.**’

Naam..hio ndio kauli tunayomalizia kisa cha Imam Al Fudayl Ibn Iyadh, ambapo Kauli hii inatupelekea sisi wenyewe Mimi na Wewe kuulizana: **‘Hivi jee mimi nawe tunamjua *Allah Subhanah wa Ta’ala* ipasavyo? Na Je tunamuabudu ipasavyo?**

Imam Fudayl Ibn Iyadh siku moja alimtembelea Mwanamke mmoja Mcha Mungu aitwae Ghufayra Al Abida, na kisha akamuomba amuombee Dua ambapo Al Ghufayra Al Abida akasema: **‘Hivi jee unafikiria kua kuna kitu baina yako na *Allah Subhanah wa Ta’ala* kitakachopelekea akujibie Dua yako?’** na hivyo hapo hapo Imam Fudayl Ibn Iyadh aanguka na akazimia.

Shaykha Ghufayrah Al Abida alikua ni mwanamke Mcha Mungu alieishi katika Mji wa Basra nchini Baghdad, katika kipindi cha Imam Fudayl Ibn Iyadh na alifariki mnamo mwaka 101 Al Hijra.

Kutokana na Ucha Mungu, Mapenzi yake na khofu yake juu ya Mola wake basi wake Shaykha Ghufayrah alikua ni mwenye kulia sana hadi kufikia kua akawa kipofu kutokana na kulia sana huko.

Ambapo anasema Imam Muhammad Ibn Husayn Al Burjulaini kua: **‘Yahya Al Bistami anasema kua siku moja kuna mtu alimwambia Ghufayrah kwa kusema: ‘Ni ugumu ulioje kua ni mtu asieona’ ambapo Ghufayrah akasema: ‘Kuwekewa pazia la kutomjua Mungu hua ni Kugumu zaid, na Upofu wa Moyo kutokana na kutofahamu makusudio ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua ni Kugumu zaidi.’**

IMAM ABD ALLAH IBN ABDI LAILA

Imam Abu Humam Abd Allah Ibn Abdi Laila Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Al Basr alikua akijulikana pia kwa jina la Al Sharahi Al Qurayshi alikua ni Mtu aliezaliwa katika Mji wa Makkah lakini baadae familia yake ikahamia katika mji wa Basra ambao ndio sehemualyoishi hadi kufariki kwake mnamo mwaka 189 Al Hijra.

Imam Abu Humma alisoma kwa Imam Yahya Ibn Abi Is-haq, Imam Yunus Ibn Ubayd, Imam Mamar Ibn Rashid, Imam Daud Ibn Abi Hind, Imam Said Ibn Urba, ambapo Hadith zake zimenukuiwa katika vitabu 6 vya Hadith na miongoni mwa aliowasomesha yeye ni pamoja na Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Abu Bakr Ibn Abi Shayba, Imam Amr Ibn Ali Al Falas, n.k

Ambapo anasema Imam An Nasai kua: **'Imam Ibn Abdi Laila ni Thiqah'** na huo pia ndio mtizamo wa Imam Ibn Hiban.

Ambapo alisema Imam Abdi Laila kua: **'Yeyote yule aliepewa Ilm Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha Ilm hio ikawa si yenye kumfanya kua ni mwenye kulia kwa ajili ya Mola wake basi Ilmyake hio si yenye kumufaisha mtu huyo.'**

Anasema Mis Arbin Kida Radhi Kua: **'Abd Allah Ibn Abdi Laila alikua ni mwenye kuuogopa Moto wa Jahannam sana kiasi yakua alikua akisjudu basi hutokwa na machozi huku akisema: 'Ewe Mola wangu niongezee khofu juu yako kama vile amabvyo unavyoiongezea chuki juu ya maadui zako, nakuomba usizifunike na Moto Nyuso zenu zinazokusujudia''**

Kutokana na Ucha Mungu wake basi anasema Imam Ibn Abd Laila kua: **'Kuna mambo mawili ambayo yananifanya mimi nisiendekeze Dunia ambayo ni: Kujua kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ananiona kila wakati na kila sehemu, na kujua kuhusiana na Uhakika wa Kifo.'**

Imam Ibn Abd Laila alikua ni mwenye kusema kua: **'Pepo na Jahannam ni zenye kumsogelea karibu Muislam na hivyo ikiwa mtu ni mwenye kuikaribia Pepo kwa matendo yake basi Pepo hio hua ni yenye husema 'Ewe Mola wangu Mjaalie aingie Ndani yangu' na kama Mtu huyo akiwa ni mwenye kuukaribia Moto kwa matendo yake basi Moto huo husema: 'Ewe Mola wangu Muepushe na kua ni miongoni mwa wenye kuingia Ndani yangu''**

SHAYKHA SHA’WANA

Sha’wana alikua ni mwanamke Mcha Mungu ambae anapolisikia jina la *Allah Subhanah wa Ta’ala* tu basi machozi hua ni yenye kummwagika kama mvua kutokana na mapenzi yake juu ya Mola wake kwani alikua akisema: **‘Macho yanayozuiliwa kutokana na kumuona Mola wake na bado yakawa ni yenye kua na hamu kumuona Mola wake huyo, basi hua hayatoshelezi kuupata muoekano huo bila ya kua ni yenye kulia**’

Sha’wana alikua ni mwenye kulia kutokana na kua ni mwenye kujawa Mapenzi na Mola wake na pia mwenye kujawa hisia za kutubu na kuomba msamaha mbele ya Mola wake ambapo anasema Muadh Ibn Fazi kua: **‘Sha’wana alikua akilia sana kiasi ya kua sisi tulikua tukifikiria kua atakua kipofu, na nilimgusia juu ya hili basi alikua ni mwenye kusema: ‘Wa Allahi ni bora kwangu mie kua kipofu kwa sababu ya Machozi hapa Duniani kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kuliko kua kipofu katika siku ya Malipo kwa ajili Moto. ’’**

Ambapo Imam Malik Ibn Daigham anasema kua: **‘Kuna Mtu ambae alimtembelea baba yangu, na akawa anamuelezea Baba yangu kuhusiana na Sha’wana na hali yake, hivyo Baba yangu akataka aelezewe vizuri zaidi anavyolia ambapo mtu huyo akasema: ‘Jee unataa nikuelezee anavyolia usiku na mchan bila ya mapumziko?’**

Malik akasema: ‘La sio hivyo, bali sema namna anavyaonza kulia’

Ambapo mtu huyo akasema: **‘Anapolisikia jina la *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi machozi huanza kummwagika kama mvua’**

Malik akasema: **‘Hivi jee machozi hayo huanzia kutiririka kutoka pembeni mwanzoni mwa macho karibu na mgongo wa pua au huanzia pembeni mwishoni mwa macho’**

Mtu huyo akasema: **‘Ah, Machozi yake ni mengi sana inakua ni vigumu kusema kua yanaanzia wapi mie naona yanamwagika tu, linapotajwa jina la *Allah Subhanah wa Ta’ala* hivyo macho yake hua kama nyota 4 zenye kung’ara sehemu moja.’**

Hivyo Abu Kathir akaanza kulia na kusema: ‘Kumuogopa kwake Mola wake, kunaonesha kua Moyo wake wote hua ni wenye kuripuka Moto, kwani wanasema kua kulia kwa mtu hua kunategemeana na wingi wa Moto ndani ya Moyo wake.’

Imam Malik Ibn Daigham anaendelea kusema kua: **‘Siku moja Baba yangu alienda kwa Sha’wana pamoja na Manbudh na Abu Humam kumtembelea, hivyo**

Manbudh akamsalimia na kumwambia kua yeye ni mtoto wa kaka yake, ambapo Sha'wana akasema: 'Salaam kwa Mtoto wa Kaka yangu ambae kamwe sijawhi kumuona hapo kabla, lakini nimpendae sana wa Allahi, mimi nilikua nna hamu ya kumtembelea Baba yako, lakini siwezi, kwani nna khofu kua kufanya kwnagu hivyokutampelekea yeye kua ni mwenye kukosa kufanya Ibada, wakati kutekeleza Majukumu yake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Muhimu zaidi kwake kuliko kuzungumza kwake na Sha'wana, kwani ni nani Sha'wana isipokua ni kiumbe asiekua na ukamilivu na muovu' na kisha akaanza kulia na kulia hadi tulipoondoka alikua anaendele akulia'

Al Qurashi nae anasema kua: **'Mimi nilienda na rafiki yangu kwa Uballah, na tukamuomba Sha'wana ruhusa ya kumtembelea, ambapo baada ya kuturuhusu kumtembelea katika kibanda kidogo ambacho kilikua hakina hali nzuri, basi rafiki yangu akasema kumwambia Sha'wana kua: 'Sha'wana Ya Laiti kama ungejihurumia japo kidogo kwa kujipunguzia kulia, kwani hio pia ingesaidia katika kuyafikia malengo yako'**

Ambapo Sha'wana akanza kulia tena na kusema: 'Wa Allahi miminingependa kuendelea kulia hadi machozi yangu yote yakamalizika, na yakaanza kutiririka machozi ya damu na kuendelea kulia hadi damu yote pia ikamalizika ndani ya mwili wangu'

Rafiki yangu akaendelea kumuusia Sha'wana, lakini Sha'wana nae hakusikia kitu bali aliendelea kulia hadi akazimia, hivyo nasi tukanyanyuka na kuondoka huku tukimuacha kama alivyo.'

Ambapo kwa upande wa Muhib basi yeye anasema kua: '**Hakika mimi sijawahi kumuona mtu yeyote anaelia sana kama Sha'wana na wala sijawahi kusikia sauti kama yake ikiongoza sauti za wale wenye kulia kwa kumuogopa A*llah Subhanah wa Ta'ala*'**

Na akasema Muhammad kua: **'Mimi nilimuuliza Abu Umar Dharir kua: 'Jee umeshawahi wewe kumuona Sha'wana?' nae akajibu : 'Naam, Mimi mara kadhaa nilikua nikimtembelea Sha'wana katika mkusanyiko wake lakini alikua akizama kwenye machozi yake, kiasi ya kwamba nilikua sifahamu mawaidha yake.' Nami nikamuuliza : 'Hivi jee unakumbuka chochote kile kwenye mawaidha yake?' ambapo nae akasema: 'Sikumbuki kitu isipokua maneno yasemayo kua:**

'Yeyote yule anaeweza kulia wakati yupo hapa basi na alie, na kama hawezi basi ayahurumie machozi ya wanaolia. Kwani yeyote anaelia, kwani anaelia sasa hivi hapa hua ni mwenye kulia kutokana na kuhisi na kujua namna Nafsi yake

ilivyozama kwenye madhambi na kua ni kutokaa na matamanio ya nafsi yake basi ndio maana akawa ni mwenye kuvuka mipaka.''

Alisema Sha'wana kua: **'Kutaka kubakia milele katika Dunia unayoipenda hua ni sawa na kua na malengo usiyoweza kuyafikia, Kumbuka hali ya Mtende unaosima baada ya Mwenye shamba kutangulia.'**

Safari moja Sha'wana aliend a katika Ibada ya Hija pamoja na Mume wake, na wakati wlaiokua wanamalizia Tawaff ya 7, basi mume wake akamwambia Sha'wana: '**Mimi nna kiu sana ya Mapenzi juu ya Allah kiasi ya kua na hisi Ulimi wangu umeachana nami'**

Ambapo Sha'wana akasema: **'Maumivu yaliyotawanyika hua yana matibabu yenye kutawanyika pia, kwani matibabu ya wanaompenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni katika Rehma zake.'**

Sha'wana alikua na mtoto wa kiume ambae alilelewa katika mazingira maalum ya kiucha Mungu, na alipofikia umri wa kubalegh basi akamuomba Sha'wana amruhusu ajitolee kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini hata hivyo Sha'wana akamwambia mtoto wake huyo kua: **'Haujafikia bado mda wako wewe wa kukuelekeza kwa Wafalme na wenye Hikma, hivyo ni bora kwako kua pamoja na watu wa kawaida wenye tabia njema, halafu pia ewe mtoto wangu wewe bado hujaupita ujana wako, hivyo huna vigezo juu ya yale unayotakiwa kuyapitia na kukuzidishia ustahmilivu'**

Hivyo mtoto huyo wa Sha'wana akakaa kimya, na haukupita mda mrefu isipokua mtoto huyo aliend a mlimani kukusanya kuni pamoja na Farasi wake na alipofika milimani basi akamfunga Farasi wake na kisha akakusanya kuni zake, na kisha aliporudi kwa Farasi wake akakuta Farasi wake yuko chini amesharar uliwa na kuanza kuliwa na Simba wa milimani. Hivyo kijana huyo akasimama na kisha taratibu akanyoosha mkono wake na kisha akamfuata Simba huyo taratibu huku akisema: **'Ewe Mnyama wewe ama vile ulivyomsababishia madhara Farasi wangu basi kwa uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* mimi nitakubebesha huu mzigo wangu.'**

Na kisha akamsogelea na kumpapasa shingo Simba huyo Simba huyo akatulia, na kisha kijana huyo akambebesha Simba huyo mzigo wake wa kuni, na kumuongoza na kurudi nae hadi kwa Mama yake, na alipofika kwa Sha'wana akagonga mlango, Sha'awana akauliza: **'Nani anaegonga Mlangoni?' kijana huyo akasema: 'Ni mimi mtoto wako, anaeomba Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie mwenye kuwapa riziki waja wake wote'**

Hivyo Sha’wana akafungua Mlango na alipofungua na kuona hali ya Simba aliebebeshwa kuni na mtoto wake basi akashangaa na kuulizia kilichotokea, na alipoelezewa basi akasema: **‘Naam ama sasa hivi ewe mtoto wangu umefikia wakati wa kujitolea kwa ajili ya Mola wako.’**

Anasema Kurdiyyat Bint Amr ambae alikua ni Mfanyakazi wa Sha’wana kua: **‘Hakika mimi kamwe sikua ni mwenye kuipenda Dunia tangu nianze kufanya kazi kwa Sha’wana, na kamwe sikuwa ni mwenye kuhangaika juu ya Riziki yangu, na wala sijawahi kua ni mwenye kutamanai yale makubwa waliyokua nayo watu ya Kidunia.’**

IMAM DAIGHAM IBN MALIK

Imam Daigham Ibn Malik Abu Bakr Al Rasbi Al Basri alikua ni mcha Mungu ambae ni mwenye asili ya maeneo ya Al Rasibi ambalo ni eneo baina ya Mji wa Makkah na Madina lakini alikua akiishi katika maeneo Basra katika kipindi cha Imam Fudayl Ibn Iyadh, Sha’wana, Imam Abd Rahman Ibn Mahdi na alifariki katika mwaka 180 Al Hijra. Ambapo anasema Imam Abd Rahman Ibn Mahdi kua: **‘Hakika mimi sijawahi kuona mtu kama Daigham Ibn Malik katika Ucha Mungu na kufanya mema.**’

Mbali ya ucha Mungu wake wote huo lakini alikua akijiona kua ni mwenye kua na Dhambi nyingi sana na hivyo kua ni mwenye kulia sana kutokana na kumuogopa Mola wake, na kutokana na kulia sana kwake basi siku moja aliulizwa na Mama yake: **‘Daigham hivi jee unakitamani kifo?’** ambapo nae akasema: **‘La’ akaulizwa: ‘Kwanini?’** ambapo nae ajibu: **‘Kwa sababu ya Madhami niliyokua nayo na kasoro zangu.’** Na kisha akaanza kulia huku na familia yake ikiendelea kulia pamoja nae.

Na Imam Ibn Arabi alisema: **‘Daigham Ibn Malik alikua ni mwenye kusali rakaa 400 kwa kila siku usiku na mchana hadi mgongo wake ulikua umepinda kwa kusali, na alikua ni mwenye kua na khofu na kulia sana kwa kumuogopa Mola wake’**

Safari moja Imam Daigham Ibn Malik alikua amekaa na Abu Ayyub na kumsikiliza kile akisemacho, na mara ghafla Imam Daigham akasema: **‘Hakika kama mimi ningekua najua kua Radhi za *Allah Subhanah wa Ta’ala* zinaweza kupatika kwa njiaya kujikata kata nyamo yako mtu basi mimi ningejikata nyama ya mwili wangu mkasi’**

Siku moja Hakam Ibn Nuh alimuelezea Malik Ibn Daigham Ibn Malik kuhusiana na baba yake Imam Daigham Ibn Malik kwa kumwambia kua: **‘Safari moja sisi tulikua**

safarini Baharini, na Digha alilia Usiku kucha, lakini hakusali wala hakusujudu na siku ya pili asubuhi yake nikamkumbusha kua jana usiku kucha Hakusali bali alikua akilia tu, baada ya kumkumbusha hivyo basi Daigham akaanza kulia tena hadi akazimia, na kisha alipopata fahamu zake basi akasema:

'Ya Laiti kama viumbe wangejua kile kitakachotokea kesho basi wasingecheka wala kufurahia maisha bali wangelia tu, usiku wa Jana kutokana na kiza kikubwa mimi niikumbuka siku ya Malipo ambapo kila mtu atakua ni mwenye kuifikiria nafsi yake na hivyo Baba na Mtoto wake hawatokua ni wenye kuthaminiana.' Na kisha hapo hapo Daigham akatetemeka na kupiga kelele, kwa huzuni.

Siku moja Imam Daigham Ibn Malik aliitwa na Mama yake, ambapo nae akaitikia kwa sauti ya upole,na kusema: **'Naam Mama, unasemaje?'** Mama yake akasema: **'Uko tayari kuelekea kwa Mola wako?'** ambapo hao hapo Imam Daigham Ibn Malik akazimia, na hivyo Mama akamsogelea karibu na kusema**: 'Inakua haiwezekani kumtaja Mola wako mbele yako'**

Anasema Imam Ali Al Madini kua: **'Daigham alivizika vitabu vyake vyote , na alikua akilala robo moja ya usiku na wakati uliobakia alikua akifanya Ibada ndain yake.'**

Alisema Imam Daigham Ibn Malik kua: **'Jitahidini kuutafuta Utamu wa Ladha ya Ibada inayoingia ndani ya Nyoyo.'**

IMAM ABU YUSUF 113 AH

Imam Abu Yusuf Yaqub Ibn Ibrahim alikua ni mwenye kutokana na ukoo wa Sad Ibn Hatim Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* ambae ni miongoni mwa Masahaba waliotaka kupigana katika Vita vya Badr lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua ni mdogo Kiumri, kwa hivyo hakuweza kushiriki katika vita hivyo kutokana na umri wake ambapo baadae Sad Ibn Hatim Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* alihamia katika Mji wa Kufah na kutokana na kizazi chake basi ndio alizaliwa Imam Abu Yusuf mnamo mwaka 113 Al Hijra katika ardhi ya Kufah nchini Iraq.

Imam Abu Yusuf alianza kusoma tangu utotoni kwa Wanazuoni wengie wakubwa kama kina Imam Abu Is-haq Ash Shaybani, Imam Sulyaman At Tamimi, Imam Yahya Ibn Said Al Ansari, Imam Sulayman Al Amash, Imam Hisham Ibn Urwa, Imam Muhammad Ibn Abd Rahman Ibn Abi Layla na pia kwa Imam Abu Hanifa ambae ndie aliekua Mwalimu wake Mkuu na ndie aliemsimamia Imam Abu Yusuf kimaisha baada ya Imam Abu Yusuf kua Yatima.

Kama anavyoelezea mwenye Imam Abu Yusuf pale aliposema: ‘**Mimi nilikua napenda kuendelea kusoma Ilm ya Hadith na Fiqh lakini nilikua mtu masikini sana na sikiwa na uwezo, na Baba yangu pia alifariki wakati nikiwa mdogo, hivyo siku moja wakati nikiwa na Imam Abu Hanifa, basi Mama yangu aliniambia: ‘Ewe Mtoto wangu hakika sasa hivi umebadilika baada ya kukutana na Abu Hanifa, kwani huko kama ulivyokua hapo kabla hivi jee hujui kua yeye mwenzako kila kitu chake ameshatayarishiwa mkate wake uko tayari, na chakula chake kiko tayari? Lakini wewe inakubidi ujitafutie chakula kwanza?’’**

‘**Hivyo mimi baada ya maneno haya kutoka kwa mama yangu basi nikaona kua bora nifanye kazi kwa ajili ya kujitafutia riziki yangu na ya Mama yangu, hivyo nikawa siendi Darsa, baada ya kutoniona mara kadhaa basi Imam Abu Hanifa akaamua kuniulizia, akawaambia Wanafunzi wenzangu waniite niende kwake, na nilipofika akaniuliza: ‘Hivi Kwanini mimi na wewe tumekua ni wenye kutengana?’ hivyo nami nikamwambia: ‘Njia za kutafutia Riziki yangu’**

Baada ya jibu hilo basi akaniambia nimsubiri, na baada ya kumsubiri na Darsa kumalizika basi akanisaidia vitu mbali mbali na baadhi ya Sarafu za fedha. Na kisha akasema: ‘Tumia hizi kwa ajili ya riziki yako na zikisha malizika basi nijuulishe, lakini kamwe usiondoke kwenye Darsa zangu, nataka kila siku uhudhurie’

Hivyo nami nikabakia na kuendelea kusoma kwake, na pesa zilipokua zikimalizika basi alikua akinipa bila ya mimi kumwambia, kiasi ya kua ikawa najiuliza hivi Jee anajuaje au *Allah Subhanah wa Ta’ala* anamtaarifu kwa njia zake? Nahivyo Imam Abu Hanifa alikua akijua kutokana na Miujiza yake? hivyo kutokana na Neema hii kutoka kwa Mola wangu, basi nami nikafikia malengo yangu katika Il’m chini ya mikono yake, namuomba *Allah Subhananh wa Ta’ala* amjaalie kila la kheri masamehe makosa yake na amlipe kila la kheri’

Na anasema Imam Shujaa Ibn Muhammad kua: **‘Amesema Imam Abu Yusuf kua: ‘Wakati Baba yangu alipofariki mimi sikuweza kuhudhuria kwenye Maziko yake, ila nilihakikisha kua jamaa zangu na majirani wanashughulikia shughuli zote za maziko hayo, na hii ni kwa sababu ya kutokua na uwezo wa kukosa Darsa za Imam Abu Hanifa, kwani nikikosa basi hisia zangu Moyoni mwangu kuhusiana na maumivu hayo ya kukosa darsa yake yangekua ni yenye kudumu na mie kwa mda mrefu hadi kufariki kwangu’**

‘Na nimejifunza Ilm ya Faraidh, Haydh kutoka kwenye Darsa ya Imam Abu Hanifa na Ilm ya Nahau vyote hivi pamoja chini yake’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Siku moja Imam Abu Yusuf alikua anaumwa sana, hadi watu wadhania kua ameshafariki, na hivyo watu wakamfuata Imam Abu Hanifa na kumwambia kua Imam Abu Yusuf ameshafariki, ambapo Imam Abu Hanifa akasema: **'Haiwezekani kua amefariki katika kipindi hiki'** alipoulizwa kwanini?

Basi Imam Abu Hanifa akajibu: **'Kwa sababu Abu Yusuf ana Ilm kubwa sana hivyo hawezi kua ni mwenye kufariki kabla hajaona Matunda yanayotokana na Ilm yake hio'**

Na bila ya shaka Imam Abu Hanifa alikua yuko sahih, kwani alisema tena pia Imam Abu Hanifa: **'Hakuna upinzani kwa kijana huyu wakati yuko hai kutokana na Ilm yake',** hivyo Imam Abu Yusuf hakufariki katika siku hio, kwani alikua amezimia tu, na alifariki baadae baada ya kufikia Darja ya *Mujtahid* wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, na hivyo Wanafunzi wake kuenea katika maeneo mbali mbali ya Dunia.

Imam Abu Yusuf alikua na ufahamu mzuri sana kwani alikua na uwezo wa kuhifadhi hadithi 60 katika kila siku, na kwa kua alisoma kwa Imam Abu Hanifa kwa miaka 16 basi bila ya shaka alipomaliza alikua tayari ameshakomaa Kiilm.

Imam Talha Ibn Muhammad anasema kua: **'Imam Abu Yusuf alikua ni mwenye Ilm kubwa sana miongoni mwa Wanafunzi wa Imam Abu Hanifa, kwani ni yeye ndie alieieneza Ilm ya Imam Abu Hanifa Duniani kote'**

Kwani Imam Abu Yusuf alikua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Qur'an, Tafsir, Fiqh na Hadith ambapo alikua ni mwenye kuhifadhi Hadith 300,000 ndani ya ufahamu wake. Na hivyo baada ya kufarki Imam Abu Hanifa basi Imam Abu Yusuf akawa ni mrithi stahiki wa Imam Abu Hanifa, hivyo akawa ni mwenye kusomesha baada yake na pia akawa ni mwenye kuandika vitabu kadhaa pia.

Kutokana a ukubwa wake Kiilm basi Imam Abu Yusuf alichaguliwa kua Qadhi Mkuu wa Utawala wa Al Abbas chini ya Mamlaka ya Khalifa Harun Rashid, na hivyo Imam Abu Yusuf kua ni mtu wa mwanzo kupewa Darja ya cheo cha *Qadhi Al Qudhat* kutokana na Ilm yake ya kua na uwezo wa kutoa Fatwa kulingana na mtizamo ya Fiqh ya Madhhab Tofauti, wadhifa ambao aliutumikia kwa mda wa miaka 16.

Ambapo siku moja kuna Mtu ambae ni tajiri sana aliweka Nadhiri kua, kama akipata Mtoto wa Kiume basi atachinja Kondoo mwenye Pembe nne. Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamjaalia Mtu huyo kua ni mwenye kupata mtoto wa kiume, na hivyo ulipofika wakati wa kutekeleza nadhiri hio basi akatafuta Kondoo wa aina hiyo katika kila sehemu lakini akakosa Kondoo mwenye Pembe nne. Hivyo akaambiwa kua ili kutatua tatizo lake hilo basi anatakiwa aonane na Qadhi Abu Yusuf.

Hivyo Mtu huyo akamfuata Imam Abu Yusuf na kumuelezea kadhia yake, na ingawa Mtu huyu ni Tajiri lakini alikua ni bakhili na hivyo aliweka Nadhiri hio makusudi ili asipate kuitekeleza kwa sababu aliku akaijua kua hakuna Kondoo mwenye pembe nne. Hivyo alipofika kwa Imam Abu Yusuf basi Imam Abu Yusuf akamwambia Tajiri huyo kua: '**Hili tatizo lako linatatulika lakini kwa sharti la kua inakubidi uujengee Ummah wa Kiislam Madrasa Ili Watoto Masikini wa Kiislam wapate kusoma**'

Na hivyo Mtu huyo akakubaliana na sharti hilo kwa kusema: '**Lakini sasa tatizo ni kua ujenzi hua si jambo la hapo hapo bali ni jambo linalochukua mda, nami nitaishiwa na subira juu ya jambo hili kwani nataka kutekeleza Nadhiri yangu haraka ili nimalizane nalo jambo hili.**'

Hivyo Imam Abu Yusuf akamwambia Mtu huyo kua: '**Kama ni hivyo basi, wacha tufanye hesabu kuhusiana na Pesa zinazohitajika katika ujenzi wa Madrasa hio, na kisha utalipa pesa hizo ambazo tutaziingiza kwenye *Bayt Al Maal* na kisha mimi ndio nitatoa Fatwa juu ya Jambo hili**' na hivyo Mtu huyo akakubaliana na sharti hilo na zikafanywa hesabu stahiki na kisha pesa hizo zikaingizwa kwenye *Bayt ul Maal*.

Imam Abu Yusuf alipopata habari ya kuingizwa kwa Pesa hizo kwenye *Bayt ul Maal* basi akamwambia Mwaafunzi wake kua: **'Nenda kanitafutie Kondoo mwenye Pembe kubwa kuliko wote, kisha niletee**' hivyo Mwanafunzi huyo akaenda kutafuta Kondoo huyo na alipompata akamleta kwa Imam Abu Yusuf, ambapo Imam AbuYusuf akamchukua Mtoto mdogo wa miaka mitano na kisha akamwambia azipime Pembe hizo kwa nyanda zake, ambapo kulingana na nyanda za Mtoto huyo mdogo mwenye urefu wa nyanda wa inchi 4 basi zikatoka Nyanda 4 kwa kila pembe.

Kisha Imam Abu Yusufu akamwambia Tajiri kua: '**Huyu hapa Kondoo wako nenda kamchinje utekeleze Nadhiri yako, kwani kwa hakika wewe hukuainisha ukubwa wa Pembe za Kondoo uliemtaja, ila ulisema tu kua ni Kondoo mwenye Pembe nne, na kulingana na ukubwa wa Pembe za Kondoo huyu mmoja basi Pembe zake ni sawa na urefu wa Pembe za Kondo wanne wa kawaida. Hivyo nami nimetoa Fatwa hii juu yake kulingana na jambo lako.'**

Imam Abu Yusuf siku moja alikua amekaa na Khalifa Harun Rashid wakiwa wanakula, ambapo Khalifa Harun Rashid akamwambia Imam Abu Yusuf: '**Karibu kula Mkate na Samli kwa Nyama, ambavyo ni chakula Adhimu na Adhimu sana**' hivyo Imam Abu Yusuf akashukuru na wakakaa na kuanza kula Chakula hicho kilichopo mbele yake, na mara Imam Abu Yusuf akatabasamu peke yake, hivyo Khalifa Harun Rashid akamuuliza Imam Abu Yusuf: '**Vipi mbona unatabasamu peke yako?'** Imam Abu Yusuf akasema: '**Nimekumbuka jambo fulani**' Khalif Harun Rashid akauliza : '**Jee ni Jambo gani?'**

Imam Abu Yusuf akasema: **‘Kuna siku mimi nilikua nimekaa nnasomeshwa Darsa na Imam Abu Hanifa, mara akaja Mama yangu akamwambia Imam Abu Hanifa: ‘Ewe Abu Hanifa hakika wewe una maisha mazuri yasiyokua na shida, lakini sasa sisi kwa upande wetu ni Masikini, na hivyo kwetu sisi ni vigumu kujipatia riziki yetu bila ya kusaidiana mimi na mtoto wangu huyu.’**

Hivyo Imam Abu Hanifa akasema: ‘Huyu Mtoto wako unaemuona hapa basi yupo katika kujifunza njia za kujitafutia Mkate wake na Samli kwa kwa Nyama kwa njia ya halali’ na kisha akampa Mama yangu pesa, na hivyo nami nikabakia kwake Imam Abu Hanifa na kuendelea kusoma hadi nikafikia kua Mwanazuoni na kua Qadhi ambae leo hii nipo mbele yako nikiwa nakula Mkate kwa Samli na Nyama, chakula ambacho kwa mtu wa kawaida hua ni vigumu kula kila siku.’ Ambapo baada ya kuelezea kisa hicho basi Imam Abu Yusuf na Khalifa Harun Rashid wakamuombea Dua Imam Abu Hanifa.

Miongoni mwa mifano yenye kudhihirisha ukubwa wa ufahamu wa Imam Abu Yusuf na Ilm yake ni pale ilipotokea kua: ‘**Khalifa alipogombana na mke wake na hivyo akamwambia kua: ‘Leo hii kama utalala kwenye sehemu ya Ardhi ninayoitawala basi utakua umeachika.’** Na tatizo ni kua Khalifa alikua anatawala eneo kubwa la Ardhi na usafiri ni wa Farasi au Ngamia tu, hivyo kamwe haiwezekani kutolala nje ya Mamlaka ya utawala wakati ukiwa umetoka kwe Maakao makuu ya Mamlaka na katika siku hizo ilikua hakuna usafiri wa haraka kama wa Ndege.

Hivyo baada ya Khalifa kupata utulivu kutokana na hasira zake basi akagundua kua katika siku hio kuna uwezekano mkubwa sana wa kua ni mwenye kumuacha mke wake kwa talaka inayokamilika kutokana na kutimizwa kwa masharti, hivyo ikabidi amtafute Qadhi Abu Yusuf, na alipoitwa basi akasema: ‘**Wacha Mke wako akalale kwenye Msikiti kwa sababu Msikiti ni eneo lisilomilikiwa na Mtu Yeyote bali ni eneo linalomilikiwa na *Allah Subhanah wa Ta’ala* tu’**

Kwa upande mwengine basi safari moja pia kuna mtu alimfuata Imam AbuYusu na kumuuliza suali ambapo nae akajibukua hajui jibula suali hilo. Hivyo Mtu huyo akasema: **‘Inakuaje kua unasema hujui wakati wewe nimtu mwenye kulipwa pesa nyingi kutoka katika *Bayt ul Maal* kwa ajili ya kutuhudumia sisi?’**

Hivyo Imam Abu Yusuf akasema: **‘Ewe Ndugu yangu hakika sisi tunalipwa malipo hayo kulingana na kile tulichokua na Ilm nacho juu yake, na wala si kwa kile tusihcokijua, kwani kama ingekua tunalipwa kulingana na kile tusichokujua basi Bayt ul Maal isingetosheleza kutulipa kutokana na wingi wa hayo tusiyoyajua.’**

Imam Abu Yusuf aliusia kwa kusema kua: **‘Mwanzo wa Neema hua ni katika neema tatu zifuatazo: Kwanza Neema ya Imani ya Dini ya Kiislam ambayo ndani yake**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

inajumuuisha Manufaa ya kulipwa kwa Kila Jema, Neema ya Pili ni Afya ambayo inajumuisha ndani yake kua na Uhai na kua na Uwezo wa Kufanya Mema, na ya Tatu ni Mali ambayo inajumuisha ndani yake Manufaa ya kutumia wa ajili ya Kuwanufaisha pia Ibn Adam Wenzako.'

Na akasema tena: **'Urafiki kwa wale wasiokua na Ilm na wale wasiokua na Haya basi hua ni wenye kumuadhirisha Mtu katika siku ya Malipo.'**

'Ilm kamwe haiwezi kukupa wewe kitu chochote kile hadi pale wewe utakapoanza kujitolea kwa ajili yake'

Imam Abu Yusuf alimuusia Khalifa Harun Rashid kwa kumwambia kua: '**Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akupe umri mrefu wenye neema na baraka ndani yake, akupandishe darja na akupe heshima ya kua ni mwenye kukukutanisha na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kesho Peponi.**

Ewe *Amir ul Muuminin*, fahamu kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekupa wewe zawadi kubwa sana miongoni mwa zawadi lakini pia amekupa adhabu kubwa sana miongoni mwa adhabu, kwa kukubebesha jukumu la kuusimamia Ummah huu, hivyo baada ya kulibeba jukumu hilo, basi umeingizwa mtihanini kutokana na watu unaowasimamia na kuaminiwa juu yao.

Umeaminiwa Mamlaka ya usimamizi wa Jengo ambalo kama hukulisimamia kwa kulijenga kwa msingi wa Uadilifu Taqwa basi litaporomoka kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataliangamiza na kisha atalikosha Jengo hilo juu ya wale walioliporomosha. Hivyo usighafilike na majukumu yako uliyopewa na Mola wako na hivyo kusababisha kupotea kwa haki yako, kwa sababu ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie anaetoa Uwezo wa kusimamia jambo husika.'

Na hivyo usiwache jambo la kulifanya leo kua ni lenye kutakiwa kulifanya kesho, au utakua ni mwenye kupoteza jukumu lako na haki zake kabla ya kufikia wakati wako, kama vile alivyokua Mchungaji ambae ni mwenye kua na jukumu la kuwasimamia Wanyama wake, hivyo wenye kusimamia pia watatakiwa kujibu kuhusiana na waliowasimamia, hivyo hata kama utakua ni mwenye kudumu kwa saa moja kwenye Mamlaka yako basi hakikisha kua unasimamia majukumu yako, kwani katika siku ya Malipo watakaokua na na furaha mbele ya *Allah Subhana wa Ta'ala* basi ni wale ambao walioridhiwa na wanaowasimamia.

Kamwe usiteleze na kuangukia kwenye sehemu yenye umbali na ukweli, kwani vyenginevyo basi wale unaowatawala nao pia watakua ni wenye kupotea, tahadhari na kua ni mwenye kutoa maamrisho kulingana matamanio ya Nafsi yako na kutoa mamuzi unapokua na hasira, hivyo unapokabiliana kuhusiana na

mambo mawili yenye utofauti wa Akhera na Duniani, basi fanya lile la Kiakhera, kwani Ulimwengu wa Kiakhera ni wenye kudumu, na hivyo kua ni mwenye khofu dihi ya Mola wako, na wala usikhofie lawama zozote utakazopata kutokana na kua ni mwenye kusimamia Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Daima kua na umakini ambapo umakini unaotakiwa si wenye kuuangalia Ulimi wako bali uwe ni wenye kuungalia Moyo wako, na kimbilia kwa Mola wako, Ogopa Adhabu zake na tumainia Rehema zake, kwani ulizi wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* hutokana na kua na Khofu nae na hapo hapo kua ni mwenye kumtegemea yeye tu. Kwani yeyote yule mwenye kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi daima hua ni mwenye kuwepo kwenye ulinzi wake *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Daima simamia kwenye njia iliyonyooka, ambayo ndio yenye kuelekea kwenye mwisho mwema, jitahidi katika yale mambo yenye kudumu kwa ajili ya Akhera yako, kwa sababu huko ndiko ambako Nyoyo hua zinashtuka kutokana na kutokuwepo kwa visingizio, hii ni katika siku ambayo Viumbe wote watainamisha vichwa vyao mbele ya Muumba wao, huku wakiwa wanasubiri hukumu zao, kutokana na kuogopa Adhabu zake, hapa hua ndio mwisho wa kila kitu.

Kwani kwa hakika yule mwenye kuijua siku ya Malipo, na kisha akawa si mwenye kuitilia maanani basi atakua ni mwenye kua na majuto makubwa sana katika siku ya hio, hioni siku ambayo miguu itateleza, nyuso zitabadilika rangi kisimamo kitakua kirefu na mahesabu yatakua magumu sana.

Hakika utakua mbaya sana mtelezo wa miguu katika siku hio, na yatakua makubwa sana Majuto katika siku hio, kwani kutokana na kua siku zetu zinahesabika kwa kupishana baina ya usiku na mchana, basi kila siku mpya huifanya iliyopita kua tayari ni kuukuu, na hivyo bila ya shaka itakileta na kukifanya kila kilichokua mbali kua ni chenye kukaribia, na hivyo kuikaribisha karibu ahadi iliyoahidiwa.

Bila ya shaka kwa kimahesabu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwepesi sana, hivyo Muogope *Allah Subhanah wa Ta'ala,* usimuasi kwani maisha ni mafupi sana na kila kilichomo ndani yake ni cha mpito, na yale ya Akhera ndio yenye kudumu. Hivyo jitahidi kua katika siku ya Malipo usiwe ni mwenye kusimama na wenye kufanya Maovu, kwani katika siku hio watu hawatosimama kulingana na Vyeo vyao bali kulingana na Amali zao, na hivyo ndivyo atakavyohukumu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie mfalme wa siku hio ambayo kila mtu ataulizwa juu ya aliyoyatenda na kulipwa kutokana nayo, hivyo fikiria namna utakavyojibu wakati utakapokuja kuulizwa masuali hayo.

Kumbuka kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Katika Siku ya Malipo hautanyanyuka mguu wa mtu hadi awe ni mwenye kujibu masuali manne yafuatayo; Aliutumiaje Uhai wake hapa Duniani, Aliitumiaje Ilm yake hapa Duniani, aliitumiaje Mali yake hapa Duniani, na aliutumiaje Ujana wake hapa Duniani' na Kila atakaenisalia mie mara moja basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamlipa Thawabu 10 na atamfutia Madhambi 10.'**

Na bvila ya shaka yeye *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yuko Peponi na kila kitu chake, na fahamu kua Pepo imezungukwa na yale yasiyopendezwa na Nafsi na Jahannam imezungukwa na yale yanayovutiwa na Nafsi. Hivyo kama ikiwa litafunguka Pazia moja la maovu yanayopendwa na Nafsi yake mtu na hivyo Mtu huyo akawa ni mwenye kua na Subra na kuidhibiti Nafsi yake basi mtu huyo atakua ni mwenye kuikaribia Pepo yake, lakini kama kama ikiwa litafunguka Pazia moja la maovu yanayopendwa na Nafsi yake mtu na hivyo Mtu huyo akawa ni mwenye kushindwa na kutokua na Subra ya kuidhibiti Nafsi yake basi mtu huyo atakua ni mwenye kuukaribia Moto wake. Hivyo kua na Hikma na Busara ili uwe ni mwenye kutua kwenye sehemu iliyokua sahih kwa ajili yako.

Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* awe ni mwenye kuutia Nuru Uso wa yule mwenye kuyasikia maneno yangu na kisha akayafikisha japo wakati akiwa si Mwanazuoni, na pia kuna Wanazuoni wengi ambao ni wenye kufikisha yale wanayoyasikia kwa wale ambao ni wenye Ilm kubwa zaidi yao, kuna mambo matatu ambayo kila Moyo wa Muislam hua haudanganyiki kutokana nayo ambayo ni: 'Kutoelekea kwenye upotovu, kutofanya kile wakifanyacho kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuwausia Viongozi wa Kiislam kwa ajili ya Manufaa ya Ummah wa Kiislam, kwani Jamaa hua ni yenye kumlinda Mtu kutokana na Uovu.' Ewe *Amir U Muuminin* Jitayarishe kwa ajili ya kujibu Masuali juu ya Majukumu yako, kwani kila kitu hua ni chenye kuandikwa kwenye kitabu cha Amali zako, juu ya yale uliyoyafanya hapa Duniani, kumbuka kua mambo yote uliyoyafanya yatasomwa katika siku ya Malipo, na utauliziwa juu yake, hii ni siku ambayo kila kitu kitadhihirishwa mbele ya Vithibitisho.

Ewe *Amir Ul Muuminin* simamia kwa uadilifu kile ulichopewa Madaraka ya kukisimamia na kihifadhi kile unachotakiwa kukihifadhi, nami nakuhimiza kuyasimaia majukuu yako kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani usiposimamia basi njia yako itakua ni ngumu sana na yenye vikwazo, na macho yako yatakua ni yenye kupofuka, na alama na dalili zote zitatoweka na ukweli pia utatoweka. Njia itakua nyembamba kwa ajili yako, hivyo idhibi Nafsi yako. Usisababishe Madhara juu ya wale waliokua chini ya usimamizi wako, kwani vyenginevyo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakupokonya haki zao juu yako

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

nakisha nawe utapoteza haki yako juu yako na malipo yako kutoka kwa Mola wako.

Hivyo usipoghafilika kutokana na majukumu yako uliyopewa na Mola wako basi nawe pia hutokua ni mwenye kughafiliwa na Mola wako, kama utakua mwenye uongofu juu ya haki zao basi nawe hutosahauliwa abadan hapa Duniani, nami namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* auongoze Ulimi wakona kua ni wenyekudumu na *Dhikr Allah* na kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ewe *Amir ul Muuminin,* zihifadhi neema ulizojaaliwa juu yako na kuonesha shukrani kutokana nazo, kwani ukiwa na shukrani kutokana nazo basi nawe utaongezewa na Mola wako, kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ وَلَئِن كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِى لَشَدِيدٌ﴾

Wa-idh taadhdhana rabbukum la-in shakartum laazeedannakum wala-in kafartum inna AAadhabee lashadeedun *(Surat Ibrahim 14:7)*

Tafsir: ***Nakumbuka Mola wako aliponadia kwa kusema: 'Kama ikiwa utanishukuru basi nami nitakuzidishia, lakini kama ukinikufuru basi Adhabu yangu nikali sana.'***

Hivyo Mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakuna kitu kizuri kuliko kujiboresha kitabia na hakuna kitu kibaya na kinachokirihisha kama kubakia kua ni mwenye kufanya maasi, kwani kufanya Maasi hua ni kutoonesha Shukrani mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Na ndio maana watu wa Mataifa yaliyotangulia waliadhibiwa na kuangamizwa kutokana na kukosa shukrani kutokana na Neema za Mola wao juu yao na hivyo wakavulia vyeo vyao na heshima zao na kuangamizwa.

Ewe *Amir ul Muuminin* namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akulinde kutokana na kua ni mwenye kuifuata Nafsi yako juu ya neema alizokuneemsha, na namuomba akunuemeshe neema alizomneemsha kipenzi chake *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Imam Abu Yusuf alifariki mnamo mwaka 182 Al Hijra.

IMAM ABD ALLAH IBN MUBARAK 117 AH

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Baba yake Imam Ibn Mubarrak alikua ni mtu ambae aliajiriwa kufanya kazi kwenye shamba la Mikomamanga, liliopo kwenye ardhi ya Marwazi na siku moja mwenye shamba akamwambia kijana Mubarak kua anahitaji Komamanga kutoka kwenye mkomamanga mtamu zaidi kuliko yote.

Hivyo kijana Mubarrak akamwambia tajiri wake kua yeye hawezi kutofautisha baina ya Mikomamanga yenye Makomamanga Matamu na Makali kwa sababu hajawahi hata mara moja kuonja Makomamanga hayo. Na alipoulizwa kwanini ikawa hakuwahi kuonja Makomamanga hayo basi nae akajibu kua: '**Sijaruhusiwa kufanya hivyo na ndio maana ikawa najizuia nisionje.**'

Hivyo Tajiri huyo akavutiwa sana na uaminifu wa kijana huyo na hivyo akamwambia Mubarrak kuhusiana na nani anaestahiki kumuoa Binti yake, ambapo kijana huyo akasema: '**Watu wa Ujahiliya walikua wakioa kulingana na Ukoo, Mayahudi walikua wakioana kwa kulingana na Mali, Wakristo wanaoana kwa kulingana na Uzuri na Waislam hua wanaoa kwa kulingana na Imani ya dini.**' Na baada ya kusikia majibu hayo basi Tajiri huyo akaamua kumuozesha Bint yake kwa Kijana Mubarak, ndoa ambayo ilitoa mtoto aitwae Abd Allah Ibn Mubarrak.

Ambapo Imam Abu Abd Rahman Abd Allah Ibn Mubarak Ibn Tamim Ibn Hanifa alizaliwa mnamo mwaka 22 Al Hijra katika ardhi ya Marwazi. Ambapo anasema Imam Ibn Asakir kua : **'Imam Ibn Mubarak anasema kua: 'Wakati nilipokua mdogo, nilikua nimekaa shambani kwenye Mikomamanga pamoja na marafiki zangu, hiki kilikua ni kipindi ambacho Makomamanga yalikua yamepea hivyo tulikua na kuyanywa pia, na mimi nilikua nikipenda kupiga Ala ya Muziki ya Aina ya Udi.**

Hivyo nikaamka ndani ya usiku wa manane, na nikaona tawi lililokua likichezaja juu yangu, na kuchukau Udi wangu na kutaka kuaza kupiga na hapo Udi ukaniambia'

﴿أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوٓاْ أَن تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ ٱللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ ٱلْحَقِّ وَلاَ يَكُونُواْ كَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْكِتَابَ مِن قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ ٱلأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ﴾

Alam ya/ni lilladheena amanoo an takhshaAAa quloobuhum lidhikri Allahi wama nazala mina alhaqqi wala yakoonoo kaalladheena ootoo alkitaba min qablu fatala

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

AAalayhimu al-amadu faqasat quloobuhum wakatheerun minhum fasiqoona *(Surat Al Hadid 57:16)*

Tafsir: ***Hivi Jee haujawadia wakati kwa wale walioamini, kua Nyoyo zao ziwe nyenyekevu kujisalimisha kutokana na kukumbushwa juu ya Allah na kile kilichoshushwa kwa haki? Na wala wasiwe kama wale ambao waliopewa vitabu hapo kabla na kisha wakaongezewa mda kwa ajili yao na Nyoyo zao zikawa Ngumu? Na wengi miongoni mwao walikua ni wenye kufanya dhambi***

Hivyo na mie hapo hapo nikauchukua Udi huo na kuupiga piga nao chini hadi ukavunjika, na nikaachana na kila kitu ambacho kilikua kinanifanya mimi kua ni mwenye kua mbali na *Tawfiq ya Allah Subhanah wa Ta'ala*, kwani kila jema hua ni lenye kutokana kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

Anasema Imam Ahmad Ibn hanbal kua: '**Hakukua na msukumo wala hamu ya kutaka kutafuta Ilm iliyotokana na mtu yeyote yule katika kipindi chake Abd Allah Ibn Mubarak isipokua ni kutokana na yeye Mwenyewe, na hivyo alisafiri kuifuata Ilm katika maeneo mbali mbali ya ardhi ikiwemo Yemen. Misri, Kufah, Basra na Sham na alikua mtu mwenye kuitafuta na kuitoa Ilm yake ni mwenye Darja juu ya jambo hilo, kwani alinukuu hadithi kutoka kwa Wazee na Vijana, alinikuu kutoka kwa Abd Rahman Al Mahdi na pia aliandika kutoka kwa Al Fazari na alikua ana Ilm kubwa sana.'**

Ambapo Imam Ibn Abi Ḥatim anasema kua: '**Amesema Baba yangu kua Ibn Al Mubarak alitembea nusu ya Ardhi kwa ajili ya kutafuta Ilm ya Hadith kwani hakuwacha sehemu katika Ardhi ya Yemen, Sham, Hijaz, Basra na Kufah**'

Na ndio haishangazi kuona kua Imam Adh Dhahabi alikua akimwita Imam Abd Allah Ibn Mubarak kwa jina la *Al Saffar*, yaani mwenye kupenda kufunga Safari. Kutokana na kupenda kwake kusafiri kwa ajili ya kutafuta Ilm basi siku moja Imam Abd Allah Ibn Mubarrak aliulizwa: '**Hivi jee hadi lini wewe utakua ni mwenye kusafiri kwa ajili ya kutafuta Ilm?'** Ambapo Imam Ibn Mubarrak akasema: '**Hadi pale nitakapopata neno ambalo halitoninufaisha kitu kutokana nalo.**'

Hivyo katika kusafiri kwake basi Imam Abd Allah Ibn Mubarrak alisoma kwa Imam Ibn Abi Layla, Imam Hisham Ibn 'Urwa, Imam Al A'mash, Imam Sulayman At Tamimi, Imam Humayd At Tawil, Imam Yahya Ibn Sa'id, Imam Abd Allah Ibn 'Awn, Imam Musa Ibn 'Uqba, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam al Awza'i, Imam Ibn Abu Dhib, Imam Malik, Imam Shu'ba, Imam Haywa Ibn Shuraykh , nk

Ambapo anasema Ibn Wahb kua: **'Abd Allah Ibn Mubarak alisoma kwa Mashaykh wetu wote isipokua Amr Ibn Harith'**

Imam Ash Shirazi alisema kua: **'Abd Allah Ibn Mubarak alisoma Fiqh kutoka kwa Malik na Ath Thawry, na alikua ni miongoni mwa wafuasi wa Imam Abu Hanifa lakini baadae akaachana na Madhhab yake.'**

Kwa upande wa Ibn Wahda basi anasema kua: **'Imam Abd Allah Ibn Mubarak mwishoni aliamua kuachana na kumnukuu Imam Abu Hanifa katika vitabu vyake na akawa si mwenye kuwasomea watu mitizamo ya Imam Abu Hanifa.'**

Imam Abu Is-haq Al Fazzari nae anasema kua: **'Imam Abd Allah Ibn Mubarak alikua ni Imam wa Waislam.'**

Ingawa Imam Abd Allah Ibn Mubarak alikua na Walimu wengi lakini miongoni mwa Walimu wake basi aliokua na ukaribu nao zaidi ni Imam Sufyan Ath Tahwry na Imam Fudayl Ibn Iyadh ambao hata hivyo walikua ni wakubwa zaidi yake kiumri lakini Wawili hawa alikua na ukaribu nao sana.

Ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Mubarak mwenyewe kua: **'Mimi nimesoma kutoka kwa Wanazuoni 1001 lakini hakuna hata mmoja anaemkuta Sufyan Ath Thawry kwa Ilm'** na akasema tena kua: **'Nilikaa mimi na Sufyan Ath Thawry, na baada ya kumsikiliza basi nikasema kua kwa hakika mimi nimeshaichukua Ilm yake yote, na kisha nikakaa nae mara nyengine ambapo baada ya kuzungumza wake basi nikasema mimi sijawahi kusikia kuhusiana na Ilm yake hii. '**

Ambao kwa upande wa Imam Sufyan Ath Thawry mwenyewe basi anasema Abd Rahman Ibn Abu Jumay kua: **'Sisi tulikua karibu na Ibn Mubarak katika Mji wa Makkah na hivyo tukamwambia Ibn Mubarak: 'Ewe Mwanazuoni wa Mashariki hebu zungumza nasi basi' ambapo Imam Suyfan Ath Thawry alikua yuko karibu pia na aliposikia maneno hayo basi nae akasema: *'Wayhakum!* Kuweni Makini kwani yeye ni Mwanazuoni wa Mashariki, Magharibi na kila kilichomo baina yake pia**'

Imam Ibn Mahdi anasema kua: '**Mimi nimekutana na Wanafiqh wanne ambao ni Malik Ibn Anas, Shub'ah, Sufyan Ath Thawry na Ibn Mubarak, ambapo sijawahi kuona mtu mwenye Ilm juu ya watu tofauti kama Ibn Mubarak, hivyo kama Ibn Mubarak hakuikubali hadith basi na sisi pia ilikua hatuikubali hadith hio.'**

Imam Ahmad Ibn Hanbal anasema kua: **'Ibn Mubarak alikua akinukuu kutoka kwenye Vitabu na yeyote yule anaenukuu kutoka vitabuni basi hua si mwenye**

kufanya makosa, ambapo Waki alikua akinukuu kutoka kwenye ufaham wake na matokeo yake alikua akifanya makosa, na jee ni kwa kiasi gani mtu anaweza kuhifadhi kwenye uhifadhi wake?'

Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema tena kua: '**Katika wakati wa Ibn Mubarak ilikua hakuna mtu aliekua akitafuta Ilm kama yeye, kwani alienda Yemen, Misri, Sham, Hijaz, Basra na Kufa, na kwa yeyote yule mwenye Ilm na kukubalika, kwani aliandika kutoka kwa Wazee na Vijana, na alikua akinukuu Hadith kutoka kwenye Vitabu'**

Na Imam Abd Allah Ibn Mubarak hakua tu ni mwenye kusoma lakini pia alikua ni mwenye umahiri wa kuandika kiasi ya kua alikua akiulizwa: 'Jee utaandika hadi lini?' Ambapo nae akasema: **'Inawezekana ikawa kuna kitu ambacho sijakiandika hapo kabla.'**

Ambapo katika kuandika kwake basi Imam Abd Allah Ibn Mubarak alikua hachagu ni nukuu kutoka kwa nani kwani kwake yeye muhimu ilikua ni Hikma iliyomo ndani ya maneno husika, kama anavyoelezea Imam Al Munawi kwa kusema kua: **'Abd Alla Ibn Mubaraka alifiliwa na Mtoto wake, hivyo miongoni mwa watu waliokuja kumpa pole alikuwemo mmoja ambae alikua ni Majusi anaeabudu Moto, hivyo Majusi huyo alimwambia Ibn Mubarak kua: 'Mwenye Akili na Ufaham hua ni wenye kukifanyia kazi Leo kile ambacho Mjinga na asiekua na Ufahamu hupanga kukifanyia Wiki moja baadae'** Yaani akimaanisha kua awe mstahamilivu katika wakati huo wa Msiba na baada ya kusikia maneno hayo basi Imam Abd Allah Ibn Mubarak akasema: **'Hebu niandikie maneno hayo'**

Anasema Ali Ibn Fudayl Ibn Iyadh ambae ni mtoto wa Imam Fudayl Ibn Iyadh kua: **'Mimi nilimsikia baba yangu akimwambia Ibn Mubarak: 'Hakika wewe unatuusia sisi tuwe ni wenye kuachana na Dunia, Kuridhika na kidogo tulichokua nacho, lakini tunaona kua wewe unakuja na Mali, hivyo jee inakuaje hali hii?'**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak akasema: **'Ewe Abu Ali, hakika mimi nnafanya hivyo kwa sababu ya kuuhifadhi uso wangu, na heshima yangu na hua naitumia mali kwa ajili ya kunisaidia kumtii Mola wangu'**

Hivyo Imam Fudayl Ibn Aayadh akasema: 'Ya Ibn Mubarak, bila ya shaka hakuna kitu bora kama hicho kama inawezekana kutekelezwa.'

Imam Ibn Mahdi aliulizwa: **'Hivi baina ya wewe na Sufyan Ath Thawry yupi ni mwenye Ilm zaid?'** Imam Ibn Mahdi akajibu: **'Abd Allah Ibn Mubarak'** hivyo akaulizwa tena: **'Jee kama watu hawatakubaliana nawe juu ya hilo?'** nae akasema:

‘Watu hao watakua hawakuchunguza, kwani mimi sijawahi kumuona Mtu mwenye Ilm zaidi ya Ibn Mubarak, kwani Ibn Mubarak ana upekee wa peke yake’

Imam An Nasai anasema kua: ‘**Hakuna mtu anaejulikana katika wakati wa Ibn Mubarak mwenye sifa bora na Ilm kubwa kama yeye na hakuna mwenye kufanya mema kama yeye**’

Imam Ibn Waddah anasema kua: ‘**Mimi niliwasikiliza watu wenye Ilm walipokua wakitoa Ilm yao, Hadith zao, Taqwa yao, Muonekano wa kukubalika kwani, Lugha yao, Ukarimu wao, Ibada zao na umakini wao na nimekuta kua yote hayo yamejumuishika kwa Ibn Mubarak’**

Anasema Qadhi Abu Al Fadhl kua amesema As Safadi kua Ibn Mubarak alipotimia umri wa kubalegh basi baba yake alimpa Dirham 50,000 ili afanyie biashara, hivyo Ibn Mubaraka akaitumia pesa hio hadi ikamalizika na ilipomalizika basi akakutana na Baba yake ambae alimuuliza: **‘Ile pesa umeifanyia biashara gani?’**

Hivyo Abd Allah Ibn Mubarak akaingia ndani na kisha akatoka na vitabu na kumwambia Baba yake: **‘Hii hapa andio biashara yangu niliyoifanya’** ambapo baba yake huyo nae akaingia ndani na kutoka na Dirham 30, 0000 na kusema: ‘**Chukua na hizi endeleza Biashara yako.’**

Imam Ibn Al Mubarak alisema kua: ‘**Mimi nilisoma Adabu kwa miaka 30 na kisha baadae ndio nikasoma Ilm kwa miaka 20’**

Anasema Imam Yahya Ibn Yahya Al Laythi kua: ‘**Siku moja alikuja mtu mmoja mwenye Tabia na Adabu nzuri wa Imam Malik, na ilikua nikimuona Malik akisema: ‘Njoo ukae karibu yangu hapa’ na kisha akasogea na kumtayarishia nafasi ya kukaa kwenye Barza yake, ambapo mimi sijawahi kumuona Malik akifanya hivyo hata siku moja hapo kabla.**

Alimuweka Mtu huyo chini yake, na baadhi ya wakati Malik alikua akiulizwa masuali na kujibu basi baada yake alikua akimuinamia Mtu huyo na kumuuliza: ‘Jee wanasema watu wako juu ya hili?’ ambapo Mtu huyo alikua akijibu kwa sauti ya chini kiasi ya kua hatukuweza kusikia wala kufaham, mtu huyo alikua akifanya hivyo kwa siku kadhaa, na hivyo nami nikapenda Tabia na Adabu zake.’

‘Lakini sikuuliza chochote kile hadi pale mtu yule alipoondoka, huku akiwa ametosheka na yale aliyokua akiyasema Malik na hivyo Malik akatuambia sisi kua: ‘Huyu alikua ni Ibn Mubarak Mwanafiq wa Khurasan’’

Alisema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: **‘Mwenye kuachana na Dunia hua ni yule ambae hua si mwenye kufurahika anapoipata na si mwenye kuhuzunika anapokosana nayo’**

Imam Ibn Shahin anasema kua: ‘**Ibn Mubarak alikuja pamoja na Hamamd Ibn Zayd na tukamsalimia. Watu wa Hadith wakaenda kwa Hammad na kumtaka Ibn mubaraka awanukulie Hadith, ambapo Ibn Mubarak akasema: ‘Nitanukuu vipi mimi Hadithi wakati niko pamoja nawe’ yaani pamoja na Hammad, ambapo Hammad akasema: ‘Nukuu, minfadhlik’ Hivyo Ibn Mubarak akasema: ‘Amesema Abu Ismail Hammad Ibn Zayd kua..na hivyo Ibn Mubarak akanukuu hadithi nyingi sana ambaoz zote ni kutoka kwa Hammad Ibn Zayd’’**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak alisema kua: ‘**Mwanzo wa Ilm ni kua na nia, kisha kusikiliza, kisha kuifaham, kisha kuifanyia kazi, kisha kuihifadhi na kisha kuitawanya.**’

Imam Abd Allah Ibn Mubarak alikua akienda kwenye vita vya Jihad mwaka mmoja na mwaka unaofuatia alikua akienda kwenye Ibada ya Hija, na ilikua kila akienda kwenye Mji wa Madina alikua akiwaambia Maimamu wa Madina na kila mtu anaetaka kuenda katika Ibada ya Hija kua atawasimamia kimatumizi kama vile anasema wakati akienda kwenye *Jihadi fii Sabili Allah*

Ambapo anasema Al Fasawi kua: **‘Mimi nilikua na Ibn Mubarak katika Jihadi katika usiku wa baridi kali sana na Mvua ilikua ikinyesha, Ibn Mubarak alikua akilia hivyo nami nikamuuliza: ‘Jee unalia kutokana na hali kama hii?’ nae akasema: ‘Nalia kwa sababu katika usiku wa Jana hatukua na hali ngumu kama hii hivyo tumekosa malipo makubwa zaidi.’’**

Anasema Ibn Said Ibn Mussayyib kua: **‘Ibn Mubarak alimtumia Abu Bakr Al Ayyash Dirham 70,000 na kumwambia: ‘Tumia hizo kwa ajili ya kujilinda na kujidhibiti Nafsi yako.’’**

Nuaym Ibn Hammad anasema kua: ‘**Ibn Mubarak alikua anapenda kukaa ndani peke yake, hivyo akaulizwa: ‘Mbona unapenda kukaa ndani peke yako’ hivyo nae akasema: ‘Inakuaje kua niwe peke yangu wakati mimi hua niko na *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam na Masahaba zake?’’**

Siku moja Imam Ibn Mubarak alikua akitia udhu, hivyo akaambiwa na mmoja kati waliokua pembeni yake kua: **‘Hukutia maji’** Imam Abd Allah Ibn Mubarak akasema: **‘Nimetia Maji’** akaambiwa tena: ‘**Hukutia maji bwana’** nae akajibu: **‘Sawa wewe ndie mwenye madai hivyo toa uthibitisho vyako.’**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak aliusia kwa kusema: **‘Usiisahau siku ambayo *Allah Subhanah wa Ta’ala* ameitaja kwenye kitabu chake mara 63’**

Kuna Mtu alimwambia Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: **‘Jana mimi nilisimama nikasali na kusoma Qur’an nzima katika rakaa ya kwanza tu.’** Imam Abd Allah Ibn Mubarak akajibu: **‘Kuna mtu ambae nnamjua ambae yeye alikua kwenye *Surat At Takathur* tu usiku kucha hadi Alfajir bila ya kuimaliza.’**

Katika safari moja ya msimu wa Hija Imam Abd Allah Ibn Mubarak alifunga safari kuelekea katika Ibada ya Hija na alipowasili kwenye Mji wa Kufah, basi akakutana na Mwanamke ambae alikua amekaa juu ya chungu ya taka taka huku akiwa anamnyonyoa Bata manyoya, na alipomuangalia vizuri zaidi Bata huyo basi akamuona kua ni Bata aliekufa na ana kichwa chake yaani hakuchinjwa. Hivyo Imam Ibn Mubaraka akamsalimia bibi huyo na kumuuliza: ‘**Hivi huyo Bata ni Mzima aliechinjwa au ni aliekufa?**’

Yule mwanamke akasema: ‘**Ni aliekufa zamani’** Imam Abd Allah Ibn Mubaraka akamuuliza Mwanamke huyo: ‘**Kama amekufa zamani kabla ya kuchinjwa basi kwanini unamnyonyoa Manyoya?**’ Mwanamke akasema: ‘**Ili familia yangu ipate chakula cha kula kama riziki yake’**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak akasema: **‘Ewe Mwanamke hivi hujui wewe kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* amekataza kula Nyama ya Mnyama aliekufa wakati wewe ukiwa kwenye Ardhi ya Waislam kama hii?’** hapa sasa ukaanza kutokea mzozo baina ya Mwanamke huyo na Imam Ibn Mubarak, kwani Mwanamke alikua anasema kua kulingana na hali ya njaa aliyokua nayo yeye Mjane na watoto wake Mayatima wasiokua na mtu wa kuwasimamia basi Nyama hio ni halali kwao na ni haram kwa Imam Ibn Mubarak kutokana na utofauti wa hali yake.

Lakin hata hivyo Imam Ibn Mubarak akamuuliza yule Mwanamke anakaa katika maeneo gani katika Mji huo, na Mwanamke akasema sehemu anayokaa. Hivyo Imam Abd Allah ibn Mubarak akaelekea kwenye nyumba ya wageni kisha akakodi chumba kwenye nyumba hio. kisha akachukua Farasi wake na kila kitu chake akikisheheni juu ya farasi huyo, na kisha akaelekea kwenye Nyumba aliyoelekezwa na yule Mwanamke aliekutana nae akiwa anamnyonyoa Bata.

Alipofika kwenye nyumba hio, akagonga mlango wa Nyumba hio na alipofunguliwa basi akamuingiza ndani Farasi wake na kumwambia yule Mwanamke mwenye Nyumba hio kua: ‘**Farasi huyu na kila kitu kilichopo juu yake ni chako kwa ajili yako na familia yako na hivyo utakua ni mwenye kupata kila cha halili kutokana nae hapa Duniani na Akhera.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kisha Imam Abd Allah Ibn Mubarak akarudi kwenye Nyumba ya kulala wageni na akajificha Chumbani kwake hadi baada ya kumalizika Ibada ya Hija. Na kisha akaanza Safari ya kurudi nyumbani kwake, ambapo alipofika basi Watu walikuja kwake kwa ajili ya kumpongeza na kuomba dua zake baada ya Ibada ya Hija, lakini nae aliwaambia watu hao kua, safari hio hakuenda kwenye Ibada ya Hija kwani alipapatwa na matatizo njiani yaliyompelekea kuaghirisha Ibada yake hio, lakini hata hivyo baadhi ya Mahujaji walippinga kuhusiana na jambo hilo kwani walisema kua Walimuona Imam Abd Allah Ibn Mubarak akiwa pamoja nao katika Ibada hio.

Imam Abd Allah Ibn Mubarak akasema: **'Hakika mimi sifahamu nyinyi mnazungumzia kuhusiana na jambo hani na mtu gani kwa sababu mimi sikuwa ni mwenye kuenda kwenye Ibada ya Hija mwaka huu.**' Ambapo usiku huo alipolala basi Imam Abd Allah Ibn Mubarak akaota kua anaambiwa usingizi kua: '**Hongera Ewe Ibn Mubarak kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekukubalia Sadaqah yako na hivyo amemtuma Malaika kukufanyia Ibada ya Hija kwa ajili yako.**'

Safari moja baada ya Ibada ya Hija, Imam Abd Allah Ibn Mubarak alilala karibu ya Al Kaabah, ambapo akaona ndoto ndani yake kua kuna Malaika wawili wanashuka kutoka Mbinguni huku wakiwa wanazungumza, kwa kuulizana: '**Hivi jee unajua watu wangapi waliokuja katika Ibada ya Haji ya Mwaka huu'** ambapo mwenzake akajibu: **'Ni watu 600,000'**

Kisha mmoja akamuuliza mwenzake: '**Na jee unafkiria ni Hija za Watu wangapi zimekubaliwa?'** Mwenzake akajibu: **'Sidhani kama yuko aliekubaliwa Hija yake mwaka huu.'**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak akajiuliza: **'Hivi kweli watu wote hao wamefunga safari kutoka sehemu mbali mbali za ardhini halafu iwe hakuna hata mtu mmoja aliekubaliwa Hija yake ikiwemo mie? Kwani bila ya Shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* hawezi kuwafanyia watu wote hawa Hija zao kua ni za bure'**

Ambapo wakati anajiuliza suali hilo basi mmoja kati ya wale Malaika akamwambia mwenzake: 'Kuna Mshona Viatu mmoja wa Syria anaeitwa Ali Ibn Mufiq ambae hakuweza kuja kwenye Ibada ya Hija ingawa alitia nia ya kuja, lakini hata hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemkubalia nia yake hio na hatopata malipo ya Hija tu basi pia kutokana nae basi Hija za mwaka huu za *Mahujaj* wote zitakua ni zenye kukubaliwa.'

Hivyo baada ya maneno hayo basi Imam Abd Allah Ibn Mubarak akazindukana huku akiwa na suali moja tu kwenye ufahamu wake ambalo ni : **'Huyu Ali Ibn Mufiq ndio nani, na kwanini hakuenda Hija lakini hata hivyo nia yake imekua ndio sababu ya**

kukubaliwa Hija za wengine wote akiwemo yeye Abd Allah Ibn Mubarak mwenyewe?'

Na hivyo akaamua kufunga safar kuelekea katika Ardhi ya Sham kwa ajili ya Kumtafuta Ali Ibn Mufuqi tu, ambapo alipofika katika ardhi ya Sham basi akamuulizia mtu huuyo na akafahamishwa katika nyumba anayoishi, hivyo Imam Ibn Mubarak akaenda kwenye Nyumba hio na kisha akagonga Mlango wa Nyumba hio na kisha Imam Abd Allah Ibn Mubarak akajitambulisha na kisha akamuuliza mwenye nyumba hio kama yeye anaitwa Ali Ibn Mufiq.

Ambapo suali hilo lilimshangaza mwenye nyumba hio kwani katika Ardhi za Kiislam katika wakati huo basi kila alikua ni mwenye kulijua jina la Imam Abd Allah Ibn Mubarak, ila mshangao wake mkubwa ni kua imekuaje Imam Abd Allah ibn Mubaraka amefunga safari alikotoka hadi katika Ardhi ya Sham na kisha kua ni mwenye haja ya kuonana nae? Hivyo nae akasema: '**Naam, mimi ndie Ali Ibn Mufiq, lakini suali langu imekuaje kuna nini?'**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak akasema: **'Nilikua nataka kujua wewe unafanya kazi gani?'** ambapo Ali akajibu : **'Mimi sina kazi nyengine isipokua hii niifanyayo ya kushona viatu'** Imam Abd Allah Ibn Mubaraka akamuuliza Ali : **'Hivi jee ulikua una mipango yeyote ile ya kufanya ibada ya Hija?'**

Ali Ibn Mufiq akasema: **'Kwa takriban miaka 30 sasa nimekua nikiishi huku nikiwa na matumaini ya kufanya Ibada ya Hija, na nimedunduliza pesa zangu kwa mda mrefu kwa ajili ya Ibada hio hadi mwaka huu zilipotimia, lakini hata hivyo *Allah Subhanah Wa Ta'ala* hakunijaalia mimi kufanya Ibada hio mwaka huu. Na nimeshindwa kuitekeleza Nia yangu wa vitendo'**

Imam Abd Allah Ibn mubarak akamuuliza Ali: '**Ilikuaje mpaka ikawa haikuwezekana kwako wewe kuenda Hija mwaka huu?'** Ali akasema: **'Ni kutokana na majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*'. Hivyo Imam Ibn Mubarak akasisitizia tena suali lake hilo. Hivyo Ali akasema: 'Kwa sababu mimi nilimtembelea Jirani yangu, ambae yeye na familia yake walikua ndio kwanza wanajitayarisha kwa ajili ya chakula cha usiku, hivyo nikadhani kua atanialika chakula hicho lakini hata hivyo Rafiki yangu huyo alikua ni mwenye kusita na nilihisi hili kuotkna na kukosa kwake utulivu rafiki yangu huyo'**

Hivyo baada ya mda rafiki yangu huyo akasema: 'Samahani lakini mimi siwezi kukualika kwenye chakula changu cha usiku wa leo kwa sababu sisi tumekaa na njaa kwa mda wa siku tatu mfululizo, hadi mimi nikashindwa kustahamili kuangalia namna watoto wangu walivyokua na maumivu ya njaa, hivyo nilipotoka

nje nikakutana na Punda aliefariki, kwa hivyo nami nikamkata sehemu ya Paja lake na kulileta Nyumbani ili angalau watoto wangu wapate kula, nikampa mke wangu na ameshalipika Paja hilo na kwetu sisi ni halali kulla ila kwako wewe ni haramu hivyo siwezi kukualika.'

Ali Ibn Mufiq anasema kua: '**Baada ya Mimi kusikia aneno hayo basi Moyo Wangu ukatokwa na machozi, hivyo nikatoka nyumbani kwa rafiki yangu huyo na moja kwa moja nikaelekea nyubani kwangu na kisha nikachukua Dinar 3000 nilizozidunduliza kwa ajili ya Ibada ya Hija ya Mwaka huu na kisha nikampelekea Jirani yangu huyo ili zimsaidie, kwani ingawa mimi katika kuzikusanya kwangu ilikua inanibidi nikae na njaa baadhi ya wakati lakini baada ya kusikia hali ya Jirani yangu basi nikaona kua bora nimpe akiba yangu hio, kuliko kuzitumia pesa hizo kwa ajili ya kufunga safari ya kuelekea katika Ibada ya Hija ingawa bado nnayo nia ya kuenda kwenye Ibada ya Hija kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* akinijaalia.'**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak alifurahishwa na kutiwa ari sana kutokana na kisa hicho, na hivyo akaamua kumhadititthia kile kilichompelekea yeye kufunga safari kwa ajili ya kumtafuta hadi akampata na kumtaarifu kua nia yake imewapelekea kuwanufaisha Mahujaji wengine wote.

Imam Abd Allah Ibn Mubarak aliulizwa: 'Jee ni nani mwenye Darja ya juu baina ya Muawwiyah Ibn Abi Sufyan na Umar Ibn Abd Al Aziz?' nae akajibu: 'Wallahi! Vumbi lililoingia kwenye Pua ya Muawwiyah wakati alipokua pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* liko juu zaidi Ibn Umar kwa mara 1000 zaidi. Kwani Muawwiyah alisali nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alipokua akisema: '*Sami Allahu liman Hamida*' basi Muawwiyah alikua akaitikia kwa kusema: '*Rabbana wa Laka Al Hamd*' hivi jee kuna kitu chengine bora zaidi ya hicho?'

Safari moja Imam Abd Allah Ibn Mubarak aliulizwa suali wakati akiwa mbele ya Imam Sufyan Ibn Uyaynah ambapo nae akajibu: **'Hakika sisi tumekatazwa kuzungumza tunapokua mbele ya Wakubwa zetu.**'

Alisema Imam Abd Allah Ibn Mubarak aliusia kwa kusema kua: '**Kimbilia kusali rakaa mbili za kuupata ukaribu kwa Mola wako pale unapokua na wakati wa kupumzika'**

'Unapotaka kusema Uongo basi Mtukuze Mola wako badala yake.'

‘Kukaa Kimya ni Bora kuliko kuzungumza hata kama wewe ni mwenye uzuri wa maneno’

Imam Ibn Al Mubarak alifariki katika mwezi wa Ramadhani mnamo mwaka 181 Al Hijra.

Alisema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: ‘**Kufunga Funga ya Sita katika mwezi wa Shawwal kuna malipo makubwa kwa sababu Mwezi wa Shawwal umeshikamana na mwezi wa Ramadhan kitukufu, hivyo kufunga Ndani yake hua ni kwenye kumpatia mtu malipo yanayofanana**.’

Wakati Imam Sufyan Ibn 'Uyayna alipotaarifiwa kuhusiana na kifo cha Abd Allah Ibn Mubarak basi alisema: ‘**Allah amuingize kwenye Rehma zake, kwani Ibn Mubarak alikua ni Mwanafiqh, Mwana Ilm, Mwenye kufanya Ibada alieachana na Dunia, Mkarimu sana, Shujaa na ni mwandishi pia.’**

Ambapo anasema Zakarriyah Ibn Adi kua: ‘**Mimi nilimuona Ibn Mubarak katika ndoto na nikamuuliza: ‘Hivi *Allah Subhanah wa Ta’ala* amekupokea vipi?’ Ibn Mubarak akasema: ‘Amenisamehe kutokana na safari zangu za Kutafuta Ilm ya Hadith.’**’

IMAM AL QARI YAQUB IBN IS-HAQ 117 AH

Imam Al Qari Yaqub Ibn Is-haq Ibn Yazid Ibn Abd Allah Abu Muhammad Al Hadhrami alizaliwa katika mji wa Basra, alikua ni miongoni mwa Maimamu 10 wa Qiraa cha Qur’an.

Ambapo anasema mwenye Imam Yaqub kua: **‘Mimi nilisoma kwa Salam kwa mda wa mwaka mmoja na nusu halafu nikahamia kwa Shihab Ibn Shanfara nikasoma kwake kwa siku tano, ambapo Shihab alisoma kwa Masalama Ibn Muharib ambae nae amesoma kutoka kwa Abu Al Aswad Al Duali ambae nae alisoma kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu.***’

Ingawa Imam Yaqub alikua na Ilm ya Hadith pia lakini wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Hadith wanasema kua si mwenye kuaminika katika hadithi zake, ambapo kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Abu Hatim wanasema kua Imam Yaqub ni mtu mwenye kuaminika Hadith zake na huo ndi pia mtizamo wa Imam Ibn Hayyan.

Imam Yaqub alifariki mnamo mwaka 205 A Hijra akiwa na umri wa miaka 88.

Imam Yaqub aliwacha Wanafunzi wake wakuu wawili ambao ni Muhamamd Ibn Al Mutawakkil Abu Abd Allah Al Lului Al Basri ambae alikua ni Mwanafunzi mzuri sana na Mwalimu wenye Ilm kubwa sana pia na hivyo akajizolea umaarufu mkubwa.

Na Mwanafunzi mwengine ni yule ambae alikua akiitwa Abu Hasan Ibn Abd Al Muumin Al Hudhali ambae alikua pia mtaalamu wa Lugha ya Kiarabu na Nahw wa Mji wa Basra, alikua ni Mwalimu mzuri sana na ni mwenye umakini mkubwa sana katika Ilm ya Qiraa.

IMAM AL QARI AL KISAI AL KUFI 119 AH

Imam Al Qari Ali Ibn Hamza Ibn Abd Allah Ibn Rahman Ibn Firiuz Al Asadi Al Kisai alizaliwa mnamo mwaka 119 Al Hijra katika ardhi ya Uajemi na alikua akiitwa Al Kisai kwa sababu alikua akipenda kuvaa aina ya koti kubwa au joho linalojulikana kwa jina la Kisai.

Imam Al Kisai alisoma kwa Imam Muhammad Ibn 'Abd Al-Rahman Ibn Abi Layla, 'Isa Ibn 'Amr al A'mash, Imam Abu Bakr Ibn 'Ayyash Imam Sulayman Ibn Arqam, Imam Ja'far al Sadiq, Imam Hamad Ibn Salamah, Imam Al Abu Hanifa, Imam Sufyan Ibn 'Uyaynah.

Baada ya kumaliza kujipatia Ilm ya Hadith na Fiqh basi Imam Al Kisai akahamia katika Ilm ya Qiraa kwa kuanza kusoma kwa Imam Hamza Al Zayyat, ambae andie aliekua na Ilm kubwa ya Qiraa katika Mji wa Kufah, ambapo alisoma Qiraa chake na kurudia kwake kwa mara nne, na akapewa Ijaza, na hivyo baadae Imam Al Kisai akawa ni Al Qarii mkuua wa Mji wa Kufah.

Na ndio maana akasema Imam Al Jazari kua: '**Ali Ibn Hamza alikua ni Kiongozi wa Ilm ya Qiraa baada ya kufariki Hamza na Al Zayyat waliokua viongozi wa Qiraa wa Mji wa Kufa**'

Imam Al Kisai alisoma kwa Al Qari Imam Hamza ambapo anasema Imam Abu Ubayd kua: '**Al Kisai alikua ni Mtu mwenye uchaguzi sana katika kisomo chake, kwani alikua ni mwenye kufuata baadhi tu ya aina ya kisomo cha Hamza na kuachana na baadhi ambazo hakubaliani nazo katika kusoma kwake**'

Imam Al Kisai alisoma pia Ilm ya Lugha kutoka kwa Imam Muaz Ibn Hira, Imam Abu Jafar Ruasi, na akasoma kwa Imam Abu Amr, Imam Amr Ibn Yala, Imam Yunus Ibn Habib, Imam Sulayman Ibn Mihran, na kisha akaelekea katika Mji wa Basra ambapo alijiongezea Ilm zaid ya Lugha kwa Mabedui, na kisha akaelekea Hijaz na Tihama, ambako alikaa kwa mda wa miaka 15 na kisha akarudi katika Mji wa Kufah.

Ambapo alisema Imam Muhammad Idris Al Shafii kuhusiana nae kua: **‘Yeyote yule anaetaka kuzama kwenye Ilm ya Nahw basi atakua kama mtoto mbele ya Al Kisai’** na akasema Imam Al Anbari kua: ‘**Wanasema kua yeye Al Kisai alikua ni Mtaalamu mkubwa sana wa *Nahw* na ni mwenye kuongoza katika *Ilm al Gharib fi Lugha* na ni mwenye kuongoza katika Ilm ya Qiraa.**’

Imam Al Kisai alipowasili katika mji wa Kufah basi akapokea mwaliko wa Khalifa Harun Rashid wa kumtaka aende katika Mji wa Baghdad ili awe Mwalimu wa Qur’an wa watoto wawili wa Khalifa Harun Rashid ambao ni *Al Maamun* na Al Amin na alikua akipendwa sana na Khalifa Harun Rashid.

Imam Al Kisai siku moja alimuota *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambaae alimuomba amsomee Qur’an, na hivyo Imam Al Kisai akamsomea *Surat As Saffat* ambapo baada ya kuisoma basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamkosoa kidogo na kisha akampiga piga nyuma ya bega huku akimwambia: **‘Najivunia juu yako kwa Waandishi wa *Qur’an al Karim* na kwa Malaika.’**

Imam Al Kisai aliwasomesha Ilm ya Qiraa kwa Wanazuoni wengi akiwemo Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Yahya Ibn Main, Imam Yahya Ibn Ziad, Imam Ali Ibn Mubaraka, Imam Abu Harith Al Layth Ibn Khalid, Imam Abu Tayb, Imam Maymun Ibn Nafis n.k

Ambapo anasema Imam Abu Hatim Sahl bin Muhammed As Sijistani ambae ni mwenye kusifika kwa Ilm yake ya Qiraa kua: **‘Safari moja Gavana wa mji wa Kufah alikuja katika Mji wa Basra, alikua ni Mwanazuoni mkubwa na Mtu mcha Mungu, nami nikaenda kumtembelea, ambapo nae akaniuliza jee ni nani wenye Ilm miongoni mwa watu wa Basar, na hivyo mimi nikamwambia Zayyadi katika Qiraa, Maazin katika Nahaw, Hilal Ibn Yahya Al Ray katika Fiqh na Shaziquni katika Hadith ndio Wanazuoni bora, na mie pia, kwani kuna wanaosema kua nna Ilm ya Qiraa cha Quran.’**

‘Hivyo Gavana huyo akataka watu hao wote waitwe mbele yake, na walipofika basi akawa ni mwenye kuwauliza masuali yaliyo nje ya fani zao ambapo nao wakasema kua masuali hayo waulizwe wenye kujua zaidi. Hivyo Gavana huyo akasema: ‘Hata kama mtu akiwa anajishughulisha kwa umri wa mia 50, hivyo ni aibu kubwa ilioje juu ya yule mtu anaeitwa Mwanazuoni kisha akawa ni Mtu ambae ni mwenye Ilm ya Fani moja tu, na hivyvo kutoweza kujibu yaliyo nje ya fani moja yake hio, kwani Mwanazuoni wetu wa Kufa Al Kisai kama angekuwepo hapa basi angeyajibu Masuali yote haya.’’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo anasema Abu Bakr Al Anbari kua: '**Imam Al Kisai alikua anasifa ambazo wengineo walikua hawana, ambapo moja wapo ni hiiya kua na Ilm ya Qiraa cha Qur'an, kwani kila mtu alikua anataka kusoma Qur'an kwa kutumia aina ya Qiraa chake, na hivyo watu walikua wanakuja kwake na Misahafu, na alikua ni mwenye Ilm kubwa ya Nahau, na mwenye uhifadhi wa maneno mengi sana ya Kiarabu na hukmu za kilugha.'**

Na akasema Is-haq Ibn Ibrahim Al Musili kua: **'Mimi niliwaona watu wanne wenye umahiri mkubwa sana katika fani zao, ambapo moja wao ni Al Kisai, kwani ilikua hakuna Mtu aliekua bora zaidi yake katika *Nahaw*'**

Ambapo safari moja Khalifa Harun Rashid alikua amekaa kwenye Baraza yake na kisha akauliza: **'Jee ni Nani mwenye kustahiki heshima kubwa zaidi kutokana na Ilm yake miongoni mwa walio hai leo hii?'** ambapo kila mmoja kati ya walikuwepo kwenye mkusanyiko huo akataja mtu wake, na Khalifa Harun Rashid akawakataa watu wote hao, na kisha akasema: **'Ni Mwalimu wa watoto wangu, Al Kisai.'**

Na akasema Imam Ibn Arabi kua: **'Al Kisai alikua ni Mwenye Ilm kubwa sana ya kukosoa Maneno na Matamshi ya Lugha ya Kiarabu.'**

Imam Al Kisai alifariki mnamo mwaka 197 Al Hijra. Na kuwacha Wanafunzi wakuu wawili pia ambao ni Imam Al Layth Ibn Khalid na Imam Hafs Ibn Umar.

Ambapo anasema Abu Mishil Abd Allah Ibn Hurjaysh kua: '**Baada ya kufarki kwake Imam Al Kisai basi mimi nilimuona kwenye Ndoto yangu, akiwa na uso wenye kung'ara kama Mwezi mweupe wa Mwezi 15, na nikamuuliza hali yake ambapo alisema kua amesamehewa kutokana kisomo chake cha Qur'an.'**

Imam Al Kisai alikua ni mtu mcha Mungu sana ambae ni mwenye kuvaa mavazi yakawaida anapokua nyumbani kwake na Darsani kwake lakini hua ni mwenye kuvaa vizuri sana na kupendeza anapokua mbele ya Khalifah na alikua ni mwenye kuzngumza na Khalifa kulingana na Lugha ya utaalamu wa hali ya juu na anapokua na wasiojua basi alikua akizungumza kwa kutumia Lugha inayofaa kwa ufahamu wao.

IMAM AL MUAFI IBN IMRAN 120 AH

Imam Abu Masud Muafi Ibn Imran Ibn nafail Ibn Jabir Ibn Jabla Al Mawsul alizaliwa mnamo mwaka 120 na kitu Al Hijra katika maeneo ya ardhi ya Mosul nchini Iraq. Na

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

alikua ni Imam mwenye Ilm kubwa sana miongoni mwa watu wa Mji wa Mosul kwani alisoma kwa Imam Ibn Jurayj, Imam Al Awzai, Imam Abu Dhib, Imam Saif Ibn Sulaiman Al Makki, Imam Musa Ibn Ubaydah, Imam Yunus Ibn Ishaq, Imam Sufyan Ath Thawry, n.k

Ambapo anasema Imam Sufyan Ath Thawry kua: '**Al Muafi alikua ni Lulu ya Ilm**' na akasema pia: **'Ukitaka kuwajua watu Mosul basi mtizamo Al Muafi.'** Kwani Imam Al Muafi alikua ndie Mwanazuoni wa Mkuu wa mwezi wa Mji wa Mosul.

Na anasema Imam Bishr Ibn Harith kua: '**Ameniambia mimi Sufyan Ath Thawry kua: 'Kama Mja akiwa hana haja na Maj wake basi humtupia kwa Watawala.**''

Imam Al Muafi alisomesha pia Wanafunzi wengi waliokua Maimamu ambapo miongoni mwao ni pamoja na, Imam Musa Ibn Ayyan, Imam Abd Allah Ibn Mubaraka, Imam Baqiah Ibn Al Walid, Imam Bishr Ibn Al Harih, Imam Ibrahim Ibn Abd Allah Al Harawi, Imam Muhammad Ibn Jafar Al Warkani, Imam Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Amar Al Mawsil n.k.

Imam Abd Allah Ibn Mubarrak alikua akimwita Imam Muafi kwa jina la: **'Mcha Mungu, Muafi Ibn Imran.'**

Ambapo Imam Bishr Ibn Al Harith alisema: **'Nakumbuka mimi Al Muafi leo hii, hivyo nanufaika kutokana na kumkumbuka kwake na nakumbuka kumuona kwake.'**

Imam Al Awzai aksema; '**Hakika mimi siwezi kumkubali tu yeyote yule kwa Ilm zaidi ya Al Muafi.'**

Na Imam Muhammad Ibn Saad akasema: **'Al Muafi ni Thiqah, Mcha Mungu, ni mwenye upekee katika Ilm ya Hadith na ni Mtu mwenye kushikamana na Sunnah.'**

Anasema Imam Bishr Al Hafi kua: '**Al Muafi alikua ni mtu mchangamfu hata katika wakati wa Mitihani kwani Khawarij waliwaua watoto wake wawili wa kiume, ambapo nae akawaalika wakafanya kisomo na kisha wakala na kuwaambia: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* akulipeni nyie kwa ajili ya Fulani na fulani''** na akasema tena kua: **'Al Muafi alikua ni mwenye kuhifadhi Ilm ya Hadith na Ilm nyenginezo na alikua si mwenye kubadilika muonekano wake katika wati wa furaha au katika wakati wa mitihani, kwani aliku ana muonekano wa hali hio hio kwa nyati zote'**

Alisema tena Imam Sufyan Ath Thawry kumwambia Imam Al Muafi kua: **‘Jina lako ni kama lilivyomaana yake, kwani unapokua na wau basi hua unawafanya wawe ni wenye kupata Utulivu na kujisikia kua na hali nzuri’**

Ambapo anasema Muhamamd Ibn Abd Allah Ibn Ammar kua: **‘Mimi nilikua na Isa Ibn Yunus ambapo yeye alisema kua: ‘Mimi sidhani kua mtu yeyote yule ambae amewahi kusikia Ilm ya Al Muafi na kisha mtu huyo akawa ni mwenye kutaka kujifunza kutoka kwa mtu mwengine zaidi yake’’**

Anasema Ali Ibn Harb kua: ‘**Mimi nilimuona Al Muafi akiwa amevaa Shati jeupe la mikono mirefu hadi vidoleni mwake, akiwa a Ndevu nyeupe na Nywele yeupe**’

Imam Yahya Ibn Main alisema kua: **‘Al Muafi ni Thiqah’**

Imam Al Muafi alikua ni Mcha Mungu sana aliechana na Dunia na kila kitu chake na alikua ni mwenye kupenda kukaa kimya na ilikua hasemi isipokua kitu chenye maana ndani yake, kwani anasema Imam Bishr Al Hafi kua: **‘Kuna mtu alisema: ‘Leo ni siku ya Baridi sana’ ambapo Imam Al Muafi alikuwepo pembeni yake na hivyo akamwambia Mtu huyo: ‘Hivi jee umefanya Dhikr leo hii? Kwani kama ingekua umekaa kimya basi ingekua bora zaidi kwako.’’**

Imam Al Muafi alifarki mnamo mwama 185 Al Hijra.

Anasema Imam Ibrahim Ibn Abd Allah Al Harawi kua: **‘Muafi Ibn Imran ni Mcha Mungu, Mkarimu, mwenye Hikma na Busara na ufaham mkubwa ambae alikua hajali kuhusiana na mambo ya Dunia’**

Anasema Imam Al Junayd Al Baghdad kua: **‘Mimi nilimsikia Sarri As Sakati akisema kua: ‘Kuna Mtu aliekua akiitwa Bishri Al Harith ambae alikuja na kisha akaingia Msikitini katika siku ya Ijumaa, ambapo mlinzi wa Msikitini hapo hakuweza kumjua kutokana na muonekano wake kwani alifikiria kua ni omba omba na hivyo akakataa kumruhusu kuingia ndani ya Msikiti huo.**

Hivyo Bishr Ibn Harith akabakia nje na kukaa pembeni ya Msikiti huo huko akiwa analia, na mara akatokea Imam Muafi Ibn Imran akamsogelea Bishr Ibn Harith na kumuuliza: ‘Vipi?. Kumetokea nini mbona unalia?’

Bishr Ibn Harith akasema: ‘Nilikua nataka kuingia ndani Msikitini lakini Mlinzi hakuniruhusu kuingia ndani yake’ Imam Muafi akamuuliza: ‘Yaani unali kwa sababu hio, unajisikia vibaya si ndio?’ Bishr Ibn Harith akasema: ‘Naam’ Hivyo

Imam Al Muafi akasema: 'Basi Nyamazi Na kisha nyanyuka, ili tuingie pamoja Msikitini' Bishr Ibn Harith akasema: 'La sitaki tena kuingia ndani ya Msikiti huu'

Ambapo Imam Al Muafi akasema kumwambia Bishr Ibn Harith: 'Twende bwana, unajua mimi nimemsikia Sufyan Ath Thawry akisema kua: 'Muumini hawezi kuonja ladha ya Ukweli wa Imani yake hadi pale atakapofikwa na Mitihani kutoka katika pande zote'' Hivyo Bishr Ibn Harith akanyanyuka na kuelekea Msikitini na Imam Al Muafi Ibn Imran''

Amesema Imam Al Muafi kua: **'Amesema Ibn Al Haytham, kua Bilal Radhi Allahu Anhu alimsogelea *Rasul Allah Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumwambia kua: 'Fulani bint Fulani amefariki Dunia na Alhamd Lillah atakua ameshapumzika' Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akapandwa na hasira na kusema: 'Mtu anaepata mapumziko hua ni yule tu ambae alieupata usamehevu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ''**

Amesema Imam Al Muafi kua: **'Amesema Imam Sufyan Ath Thawry kua: 'Kama Subira ingekua ni Ibn Adam basi ingekua mtu mwenye Hikma sana''**

Amesema Imam Al Muafi kua: '**Amesema Ibn Umara kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Msaada wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua unapatikana kutokana na Dua, Ikhlasi juu ya udhaifu wenu miongoni mwenu'''**

IMAM ABD ALLAH IBN HUBEYK

Imam Abu Muhamamd Abd Allah Ibn Hubeyk Al Kufi Al Antaki alizaliwa katika ardhi ya Mji wa Kufah nchini Iraq na alietmbelea katika sehemu mbali mbali kwa ajili ya kujitafutia Ilm ya Dini ya Kiislam na mwishowe alihamia katika ardhi ya Antakiya na alikua ni Mwanafunzi mkuu wa wa Imam Yusuf Al Asbati.

Imam Abd Allah Ibn Hubeyk alisoma pia kwa Imam Sufyan Ath Thawry na hivyo alikua ni mwenye kufuata pia nyayo za Imam Sufyan Ath Thawry na hivyo kua ni miongoni mwa Wacha Mungu wakubwa sana wenye kuachana na Dunia yao, kiasi ya ya kua alikua ni mwenye kupatiwa jina la : '**Mtu mwenye sifa za Nabii Yahya *Alayhi Salam* katika Ummah huu'**

Imam Abd Allah Ibn Hubeyk aliombwa Wasia na mmoja kati ya Wanafunzi wake alikua anatoka katika maeneo ya Khurasan, hivyo nae akamwambia Mwanafunzi huyo kua: **'Ewe Mwenye Kutoka Khurasani Usiseme uongo kwa Ulimi wako, Usiangalie ya**

haram kwa kutumia macho yako, Usimuonee wivu Muislam mwenzako kwa kutumia Moyo wako na wala usimuwekee kinyongo na wala usitamani mambo mazuri ya kiduni kwani ukifanya hivyo basi utakua ni mwenye kuangamia.'

Alisema Imam Abd Allah Ibn Hubeyk kua: **'Mtu Bakhili hua ni kama Mtu aliekufa na kufungwa na minyororo, kwani Muumini wa kweli hua hawi mbakhili na wala hajiwachii kwenye Matamanio ya Nafsi yake.'**

'Aina bora ya Khofu ni ile inayomlinda Mtu kutokana na kufanya Dhambi, kwani hukufanya ufikirie yale uliyoyafanya na kufikiria yanayokuja, ambapo Tamaa bora hua ni ile inayompelekea Mtu kua na urahisi katika kufanya Amali njema.'

Kwani Tamaa imegawika katika hali tatu zifuatazo: **'Tamaa ya kufanya Mema huku ukiwa na matumaini ya kukubaliwa Amali hizo, Tamaa ya kutegemea kusamehewa baada ya kufanya maovu na kuomba msamaha, na Tamaa ya aina ya tatu isiyokubalika ambayo ni Tamaa ya kuendelea kufanya Maovu huku ukitegemea kusamehewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*.'**

'Ikhlasi hua ni ngumu zaidi kupatikana kuliko kufanya Mema kwani Mja anapokua na Ikhlasi katika mambo ambayo ni baina yake yeye na Mola wake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* humdhihirishia hazina ya Ulimwengu wa Ghayb.'

'Ingawa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameumba Nyoyo kwa ajili ya kumkumbuka yeye, laki iwatu hua ni wenye kuzijaza Nyoyo hizo matamanio, kwani ni kutokana na kua na khofu juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndiko kunakoupelekea Moyo kua ni wenye kuachana na Matamanio'

'Utaangamia pale usipokua na khofu ya kua utaadhibiwa, kwa kutegemea Amali zako njema.'

'**Pale watu waliohifadhi Qur'an wanapofanya Dhambi basi Qur'an iliyomo kifuani mwake hua ni yenye kusema: 'Hakika mimi naapa kua wewe hukunihifadhi mimi kwa ajili ya jambo hili.' Na hivyo kama mtu huyo angekua ni mwenye kuisikia sauti ya manenno hayo basi angelikua ni mwenye kuanguka chini na kufariki kutokana nayo**'

'Kua na khofu juu ya yale yatakayo kuangamizia furaha yako kesho Akhera, na wala usifurahie kile ambacho hakitokunufaisha kesho Akhera'

'Yeyote yule mwenye kuona haya mbele ya Mola wake basi na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamuonea haya na kumuepusha na Adhabu zake'

‘Kusikiliza maneno maovu sana hukuondolea utiifu na hali ya kufanya Ibada ndani ya Moyo.’

‘Moja kati ya Tabia Njema ni kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa Moyo na kwa Ulimi usiku na Mchana, ambapo kumkumbuka kwa Moyo ndio bora zaidi.’

‘Moyo wako Unapomkumbuka *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi hua ni wenye kujaa hofu, na hivyo kua ni weye hamu ya kukutaa nae, na hivyo mapenzi yako juu yako hua ni yenye kuongezeka kidogo kidogo, na Moyo hua ni wenye kurekebisha malengo na nia yako na hivyo hua ni wenye kuyaangamiza matamanio na kukusafishia amali zako’

‘Kuna mambo matano ambayo huulainisha Moyo unapokua mgumu. Kwanza Kukutana na Waja wema na kua pamoja nao katika Mikusanyiko yao. Pili Kusoma Qur’an huku ukiwa ni mwenye kutafakari maana yake, Tatu ni kutokula chakula kisichokua cha Haram, kwani Chakula cha Halali huung’arisha Moyo. Nne ni kufikira kuhusiana na ukali wa Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa yule atakaemuasi. Tano ni kujihesabu kua huna uwezo wa kutekeleza kikamilifu Majukumu yako mbele ya Mola wako kutokana na kufikiria na kuona neema zake juu yako.’

IMAM ABD ALLAH IBN WAHB 125 A.H

Imam Abu Muhammad Abd Allah Ibn Wahb Ibn Muslim Al Fihr alizaliwa mnamo mwaka 125 Al Hijra katika ardhi ya Al Qhira nchini Misri alikua ni Mwanazuoni mkubwa sana wa Ilm ya Fiqh na Hadith ambayo aliipata kutoka kwa Wanazuoni wengi wakubwa akiwemo Imam Malik Ibn Anas, Imam Layth Ibn Saad, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Ibn Jurayj, Imam Sulayman Ibn Bilal na wengineo.

Ambapo Mwalimu Mkuu wa Imam Abd Allah Ibn Wahb alikua ni Imam Malik ambae alisoma kwake kwa mda wa miaka 10 na walikua na ukaribu sana kiasi ya kua Imam Malik alikua akimwita Imam Abd Allah Ibn Wahb kwa jina la Faqih Abu Muhamamd wa Misri, kwani Imam Malik hakuwahi kumuita Mtu yeyote yule kua ni Faqih isipokua Imam Abd Allah Ibn Wahb.

Anasema Imam Ahmad Ibn Salih ambae pia ni Mwanafunzi wa Imam Malik kuhusiana na Imam Abd Allah Ibn Wahb kua: **‘Sikuwahi mimi kuona Mtu mwenye kunukuu hadithi nyingi sana kuliko Ibn Wahb.’** Imam Abd Allah Ibn Wahab alikua akijulikana pia kwa jina la Diwan ul Ilm, na pia kwa jina la Mtu aliekusanya Ilm ya Hadith na Fiqh.

Imam Malik aliulizwa kuhusiana na ni nani mwenye Ilm baina ya Imam Ibn Abi Qasim na Imam Ibn Wahb ambapo nae akajibu: **‘Ibn Wahb ni Mwanazuoni wa Fani zote za Ilm wakati Ibn Qasim ni Mwnye Ilm ya Fiqh’**

Kutokana na ukubwa wake wa Ilm na uwezo wake basi hata watu wa Madina walipokua wakitofautiana kuhusiana na jambo fulani basi walikua wakimsubiri Imam Ibn Wahb aje ili awatatulie jambo hilo.

Ambapo Imam Abd Allah Ibn Wahab alikua akisema kua: **‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* ameniongoza mimi kupitia kwa Imam Malik na Al Layth Ibn Sad’** na alipoulizwa ni kwanini akawa ni mwenye ni kusema hivyo basi alisema**: ‘Wakati nilipokua nnakusanya Hadith nilishangazwa na nukuu tofauti ambazo zilizokua zimenifikia mimi, hivyo nilipokutana na Imam Malik na Imam Layth Ibn Saad wakanifahamisha kwa kuniambia chukua hii hio achana nayo, maana ya hadith hii ni kama ifuatavyo n.k hivyo waliniongoza nami nikawa si miongoni mwa waliopotea’**

Katika wakati wa Uhai wake Imam Abd Allah Ibn Wahb aliombwa kua awe Qadhi na Khalifa wake lakini nae akakataa na hivyo akaulizwa: ‘**Kwanini hutaki kukubali jukumu hilo? Wakati utakua unatoa hukmu kulingana na Sharia za Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta’ala* na Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*?’**

Ambapo Imam Abd Allah Ibn Wabh nae akajibu kwa kusema kua: **‘Hivi Jee nyinyi hamjui kua katika Siku ya Malipo basi Wanazuoni watafufuliwa pamoja na Mitume na Mahakimu watafufuliwa pamoja na Wafalme?’**

Ambapo anasema Yahya Ibn Bakr kua: ‘**Sehemu moja ya uhai wa Imam Abd Allah Ibn Wahb alikua akiitumia kwa ajili ya Kusoma Ilm ya Dini ya Kiislam na kujihesabia Nafsi yake, sehemu ya pili lilikua ni katika kusomesha Ilm ya Dini ya Kiislam na sehemu ya tatu ilikua ni kwa ajili ya Kufanya Ibada ya Hija**’ kwani Imam Ibn Wahb alienda katika Ibada ya Hija mara 36 katika uhai wake.

Imam Abd Allah Ibn Wahb siku moja alikua anapita sehemu na kisha akamsikia mtu anasoma Qur’an na kufikia katika aya isemayo:

﴿وَبَرَزُواْ لِلَّهِ جَمِيعاً فَقَالَ ٱلضُّعَفَاءُ لِلَّذِينَ ٱسْتَكْبَرُوۤاْ إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنتُمْ مُّغْنُونَ عَنَّا مِنْ عَذَابِ ٱللَّهِ مِن شَيْءٍ قَالُواْ لَوْ هَدَانَا ٱللَّهُ لَهَدَيْنَاكُمْ سَوَآءٌ عَلَيْنَآ أَجَزِعْنَآ أَمْ صَبَرْنَا مَا لَنَا مِن مَّحِيصٍ﴾

Wabarazoo lillahi jameeAAan faqala aldhdhuAAafao lilladheena istakbaroo inna kunna lakum tabaAAan fahal antum mughnoona AAanna min AAadhabi Allahi min shay-in qaloo law hadana Allahu lahadaynakum sawaon AAalayna ajaziAAna am sabarna ma lana min maheesin *(Surat Ibrahim 14:21)*

Tafsir: ***Na wao wote watakusanywa pamoja mbele ya Allah Subhanah wa Ta'ala (Katika siku ya Malipo), na kisha wale waliokua dhaifu watasema kuwaambia wale viongozi wao: 'Sisi tulikufuateni nyinyi hivyo sasa jee mnaweza kutupunguzia baadhi ya Adhabu ya Allah Subhanah wa Ta'ala?' ambapo nao (Viongozi hao watasema): 'Kama Allah angetuongoza sisi basi nasi tungekuongozeni nyie, sasa hivi hakuna tofauti baina yetu kama tukikasirika au tukistahmili adhabu hii kwani hakuna kwa kukimbilia.'***

Hivyo hapo hapo Imam Abd Allah Ibn Wahb akaanza kutetemeka kwa khofu na akabakia katika hali hio ya khofu kwa mda wa masaa kadhaa.

Imam Abd Allah Ibn Wahb aliulizwa na Wanafunzi wake: **'Hivi jee tufanye nini ili nasi tuwe ni wenye kua salama?'**

Ambapo Imam Abd Allah Ibn Wahb akasema kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Wakati mmoja wenu anapotoka nje ya nyumba yake basi na aseme: '*Audhu bi kalimati Allahi tammati min sharri ma khalaka*' na hivyo hakuna kitakachomdhuru hadi atakaporudi.''**

Imam Abd Allah Ibn Wahb aliusia kwa kusema: **'Ingekua ni vizuri sana kama mtu angemfanyia mwenzake kile ambacho anapenda kufanyiwa yeye, kwani yeyote yule asiejinufaisha basi hatoweza kumnufaisha yeyote.'**

Amesema Imam Abd Allah Ibn Wahb kua: **'Wakati Haywa Ibn Shuraih alipopokea mshara wake wa Dinar 60 alikua akizigawa zote kama sadaqa na kisha akienda nyumbani kwake hua ni mwenye kuzikuta Dinari zake hizo zikiwa chini ya Godoro lake. Ambapo Haywa alikua na Ibn Ami wake ambae alipojua kuhusiana na tukio hilo basi nae akafanya kama alivyofanya Haywa yaani alipopata mshahara wake**

المستكشف ابو منال دانا
AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

basi nae akazitoa sadaqa zote na kisha alipoenda nyumbani kwake na kuangalia chini ya Godoro lake akakuta hakuna kitu.

Hivyo Ibn Ami huyo akamlalamikia Haywa kuhusiana na tukio lake hilo kua na yeye alifanya kama alivyofanya Haywa lakini hakukuta Dinar zake chini ya Godoro lake, ambapo Haywa akasema: 'Tatizo ni kua mimi nilitoa kwa Ikhlasi kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini wewe ulitoa kwa ajili ya kumjaribu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ''

Imam Abd Allah Ibn Wahb alifariki mnamo mwaka 197 Al Hijra wakati alipokua akisomewa Kitabu chake cha Hadithi alizokua akaimfundisha Mwanafunzi wake katika Mlango uliyokua ukizungumzia kuhusiana na Siku ya Malipo ambapo akazimia kwa Khofu na hakuzindukana tena.

IMAM IBN ABD RAZZAQ AL SANAANI 126 AH

Imam Abd Razzaq Ibn Hamam Ibn Nafii Al Himyari Al Sanaani alizaliwa katika familia ya ukoo wa Banu Himyari ambao ni wenye asili ya Watumwa waliokua wakiishi katika Mji wa Sanaa nchini Yemen mnamo mwaka 126 Al Hijra. Baba yake Imam Abd Razzaq alikua ni Mwanazuoni wa Ilm ya Hadith ambapo nae akamsomesha mwanawe huyo na baadae akamhamishia kwa Imam Ma'mar Ibn Rashid ambapo alikaa na kusoma chini yake kwa mda wa miaka minane.

Baada ya hapo Imam Abd Razzaq akafunga safari katika maeneno mbali mbali yakiwemo Hijaz, Syria na Iraq kwa ajili ya kujitafutia Ilm ambapo alifanikiwa kusoma kwa Imam Ibn Jurayj, Imam Sufyan Ibn Uyaynah na Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Malik, Imam Al Awzai, pia na mbali ya kua alikua ni mwenye kuziandika hadith anazozisoma na kufanikiwa kutayarisha Kitabu chake cha Hadith kiitwacho Mussanaf Ibn Abd Razzaq ambacho ndani yake mna hadithi alizozipangilia kulingana na mitizamo ya Ilm ya Kifiqh, hiki ni kitabu chenye matoleo 11, lakini pia Imam Abd Razzaq alikua ni Al Hafidh ambae alihifadhi Hadithi 17,000.

Miongoni mwa Wanafunzi wake walikuwemo Maimamu maarufu kama Imam Yahya Ibn main, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahaweyh na Imam Ali Ibn Al Madini. Imam Abd Razzaq alikua ni mwenye kukubalika Kilim zaid ya Mwalimu wake ambae ni Imam Ma'amar Ibn Rashid kwani anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: **'Kama ikiwa kuna utofauti wa Hadith za Maamar basi zinakubalika hadithi alizonukuu Abd Razzaq**'

Ambapo kwa upande wa Imam Ali Al Madini basi yeye anasema kua: '**Abd Razzaq ni mmoja kati ya waliobora miongoni mwetu katika Ilm hii na katika kuhifadhi.**'

Na kwa upande wa Imam Bukhari basi yeye anasema kua: **'Pale inapokua Abd Razzaq anaponukuu hadithi kutoka kwenye kitabu chake basi Hadithi hio hua ni Sahih zaidi'**

Na hii ni kwa sababu ingawa Imam Abd Razzaq alikua ni mzuri sana kwa hadithi lakini hata hivyo alipokua mzee wa miaka 70 basi macho yake na ufaham wake ulidhoofika pia kama anavyoelezea Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Sisi tulikua tukimtembelea Abd Razzaq kabla ya mwaka 200 Al Hijra, wakati alipokua na nguvu ya macho yake, lakini yeyote yule aliemtembelea Abd Razzaq miongoni mwetu baada ya kupungua nguvu macho yake basi hua ni mwenye kupewa sifa ya kutoaminika kwa usahihi wa hadith zake alizonukuu kutoka kwake.'**

Imam Abd Razzaq alikua si mtu wa kufatilia Ilm ya Hadith tu, lakin ipiaalikua akipenda kufuatilia Ilm ya Tarikh, na katika kufuatilia kwake akawa ni mwenye kufuatilia historia ya Madhhab ya Shia pia, jambo ambalo liliwapelekea baadhi ya watu kusema kua alikua ni mfuasi wa Madhhab ya Shia. Lakini hata hivyo juu ya hili basi anasema Imam Abd Allah Ibn Hanbal kua: '**Ama mimi binafsi sikuwahi kusikia kuhusiana na hilo ila majua kua alikua ni mtu mwenye kuvutiwa sana na habari za kihistoria**'

Imam Abd Allah Ibn Ahmad Ibn Hanbal anasema pia kua: '**Alisema Imam Abd Razzaq kua: 'Wa Allahi, kwa hakika mimi siwezi kutoelemea katika kumpendelea Ali dhidi ya Abu Baqr na Umar, namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* awaingize kwenye rehma zake Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali kwani mtu asiewapenda wao hua si Muislam**''

Imam Abd Razzaq Al Sanaani hakua ni mwenye kuandika vitabu vya Hadith tu lakini pia aliandika vitabu vya Historia ya Maisha ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na pia Tafsir ya Qur'an.

Imam Abd Razzaq Al Sanaani alifariki mnamo mwaka 211 Al Hijra.

IMAM WAKI IBN JARRAH 127 AH

Imam Abu Sufyan Waki Ibn Jarrah Al Rawasi Al Kufi alizaliwa katika ardhi ya Kufa nchini Iraq mnamo mwaka 127 Al Hijra ambapo baba yake alikua ni msimamizi wa *Bayt Ul Maal.*

Imam Waki Ibn Jarrah alisafiri sana katika mji mbali mbali wa ajili ya kutafuta Ilm na hivyo alisoma kwa wanazuoni wengi ikiwemo Imam Abu Hanifa, Imam Hisham Ibn Urwa, Imam Sulayman Al Ayyash, Imam Ibn Jurayj, Imam Al Awzaii na wengineo.

Imam Waki Ibn Jarrah alikua ni mwanazuoni mkubwa sana wa Ilm ya Fiqh na Hadith kwani alikua ni Mwanafunzi mkuu wa Imam Abu Hanifa na hapo hapo akawa ni Mwalimu wa Imam Abd Allabh Ibn Mubarak, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Muhammad Idris Al Shafii na pia Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Abd Rahman Ibn Mahdi na wengineo kwani alitafuta Ilm wakati alipokua mdogo kiasi ya kua alipotimia umri wa miaka 30 alikua tayari ni Mwanazuoni wa Hadith, na baada ya hapo akawa ni mwenye kusomesha kwa zaidi ya miaka 40.

Ambapo anasema Imam Adh Dhahabi kuhusiana nae kua : '**Waki Ibn Jarrah ni Muhadith ambae anaaminika na kukubalika sana.**' Kwani Imam Waki Ibn Jarrah alikua akijulikana kama Mwanahadith wa Iraq kutokana na Ilm yake na Ufahamu wake namna ulivyokua na uwezo mkubwa wa kuhifadhi.

Ambapo anasema Imam Is-haq Ibn Rahawayh kua: '**Ufahamu wa Imam Waki ni wa Kimaumbile wakati ufahamu wetu sisi ni wenye kuhitaji kupandikizwa kwa nguvu kubwa sana.**'

Na pia akasema Imam Rahawayh kua: '**Ufahamu wangu na Ufahamu wa Ibn Mubarak ni mgumu, lakini kwa upande wa Ufahamu wa Waki basi ni msafi sana, kwani siku moja alisimama na kuweza kunukuu Hadith 700 kutoka kwenye ufahamu wake.**'

Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema kua: **'Mimi sijawahi kumuona mtu ambae ni mwenye Ilm kubwa sana kama Waki, kwani ilikua hakuna mwenye Ufahamu mkubwa sana wa kuhifadhi Hadith kama yeye**'

Mbali ya kua Imam Waki Ibn Jarrah alikua ni mwenye Ilm kubwa ya Dini lakini pia alikua pia ni mtu mwenye busara na hikma katika kutatua mambo mbali mbali ya Kidini na kijamii kiasi ya kua Khalifa Harun Rashid alimteua kua awe Gavana wake wa Mji wa Kufah lakini hata hivyo Imam Waki alikataa kubeba jukumu la uteuzi huo.

Anasema Imam Yahya Ibn Main kua: '**Waki katika kipindi cha uhai wake alikua kama Imam Al Awzai katika kipindi cha Uhai wake. Kwani mimi sijawahi kukuta**

Mtu muhimu kama yeye na alikua ni mwenye Kufunga kila baada ya siku na kusali *Qiyam Layl* kila siku usiku na alikua akitoa Fatwa kulingana na Fiqh ya Imam Abu Hanifa.'

Ambapo kwa upande wa Imam Abd Allah Ibn Mubarrak basi yeye anasema kua: '**Waki ni mtu mkubwa wa Miji miwili ya Kufa na Basra'**

Na Salim Ibn Junadah kua: 'Mimi nilikua nikihudhuria Darsa ya Waki kwa mda wa miaka 7, na sijawahi kumuona akitema mate wala kuokota vijiwe au kukaa huku akiwa ni mwenye kuutikisa mwili wake, na kila siku nilikua nikimuona kua anapokaa chini basi hua ni mwenye kuelekea Kibla, na wala sijawahi kumsikia akiwa ni mwenye kuapa kwa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

Anasema Said Ibn Mansur kua: '**Safari moja Imam Waki aliingia kwenye Mji wa Makkah huku akiwa amenenepa, hivyo Imam Fudayl Ibn Iyadh akamuuliza: 'Imekuaje hadi ukawa na mwili mrefu na ulionenepa kama huo? Wakati wewe ni Mwanazuoni mkubwa wa Iraq?'**

Imam Waki Ibn Jarrah akasema: 'Kunenepa kwangu kunatokana na furaha ya kuridhika kwangu kua mimi ni Muumini wa Dini ya Kiislam' hivyo Fudayl Ibn Iyadh akakaa kimyaa'

Safari moja Imam Waki Ibn Jarrah aliomba wino kwa ajili ya kuandikia na hivyo baada kuandikia, basi Imam Waki Ibn Jarrah akampa mtu huyo malipo ya pesa kutokana na kua ndie aliempa Wino huo alioandikia na kumwambia Mtu huyo: '**Samahani lakini sina zaidi ya kukupa isipokua pesa hizi'**

Imam Ahmad Ibn Hanbal anasema kuhusiana na Imam Waki kua: **'Hakika mimi sijawahi kumuona Waki akisoma Hadithi kutoka kwenye vitabu wakati anaposomesha'** na akasema tena kua: **'Sijawahi mimi kuona mtu wenye ufahamu mkubwa zaidi ya Waki na hakuna mfano wake kuhusiana na ufanyaji wa Ibada zake'**

Imam Ali Ibn Hasyram anasema kua: **'Sikuwahi mimi kumuona Waki akiwa na Kitabu kwani alikua daima ni mwenye kuutegemea ufahamu wake.'**

Imam Adh Dhahabi anasema kua: **'Imam Waki Ibn Jarrah alikua ni Al Hafidh, Mnukuaji, Mwanahadith mkubwa sana kutoka Iraq na alikua ni mfano wa Kuigwa miongoni mwa Wanazuoni.'**

Kutokana na ukubwa wake huo wa ufahamu basi wau wengi walikua wakishangazwa nae na hivyo safari moja watu wakamuuliza: **'Hivi kwa nini wewe Ufahamu wako ni**

mkubwa kiasi hicho? Kuna siri gani' ambapo nae akasema: 'Jee nikikuambieni siri yangu mtaitekeleza?' watu wakasema 'Naam'. Imam Waki Ibn Jarrah akasema: 'Acheni kufanya Dhambi tu hakuna siri wala dawa yeyote'

Amesema Imam Muhamamd Idris Al Shafii kua: **'Mimi safari moja nililalamika kwa Waki kuhusiana na ugumu wa ufahamu wangu, ambapo nae akaniambia kua niwache kufanya Dhambi, kwani Ilm ni Nuru ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo Nuru hio haiwezekani kua ni yenye kupewa wenye kufanya maasi'**

Ambapo tunapomzungumzia Imam Al Shafii basi hua tunamzungumzia Imam ambae ni mwenye uwezo mkubwa wa kiufahamu kama tutakavyoona kwenye historia ya maisha yake katika kurasa za mbele, lakini alipomlalamikia Imam Waki kuhusiana na tatizo lake hilo, basi Imam Waki akamwambia kua kuna Dhambi itakua ulifanya hebu kumbuka, na Imam Al Shafii alipofikia kwa makini basi akagundua kua kuna siku moja alimuona mwanamke anapanda kwenye Farasi na katika kupanda kwake basi sehemu ya chini ya mguu wake mmoja ikawa ni yenye kuonekana na macho ya Imam Al Shafi ambae hata hivyo nae hapo hapo aligeuza mtizamo wa macho yake.

Imam Waki Ibn Jarrah alikua ni mwenye kusali sala zake za Fardhi zote Msikitini kwani alikua ni mwenye kusema kua: '**Yeyote yule asieonja utamu wa Takbir ya Kwanza pamoja na Imam Msikitini basi hua si mwenye kutakiwa kua na matumaini sana juu ya wema wake**'

Mbali ya kua ni mwenye kupenda sana kufanya Ibada lakini hata hivyo Imam Waki Ibn Jarrah alikua anapenda sana kusomesha Hadithi za *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* zaidi kwani alikua anasema kua: **'Kama ingekua Sala za Sunnah ni Muhimu zaidi kuliko kusomesha Hadith basi mimi nisingesomesha Hadith.'**

Na akasema tena kua: **'Kama ingekua katika Ilm Ya Hadith hakuna Dhikr na kupatikana kwa Baraka za kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi mimi nisingesomesha Hadith.'**

Kutokana na Ucha Mungu wake na Taqwa basi Imam Waki Ibn Jarrah alikua ni mtu ambae hazungumzii kuhusiana na watu wengine kwani anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal anasema kua: '**Imam Waki Ibn Jarrah alikua hazungumzii kuhusiana na watu wengine' na pia alikua ni Imam asiependa umaarufu wala kupenda kua watu wajue kuhusiana na Ibada anazofanya.'**

Imam Waki Ibn Jarrah alisema kua: **'Kama kuachana na Dunia hii bila ya kufikia darja ya Masahaba kama Salman Al Farsy, Abu Dhar Al Ghifari *Radhi Allahu Anhum* basi mimi siwezi kusema kua mtu huyo ni mwenye kuachana na Dunia yake, kwani kwangu mie ndani ya Dunia hii mna vya Halali, Vya Haramu na *Shubhat* ambapo vya Halali vitauliziwa juu yake na Vyenye *Shubhat* vitalaaniwa**

basi hali ya Dunia hii hua ni kama Mzoga, yaani chukua kutoka katika Dunia hii kile tu ambacho kitakuwezesha wewe kua hai'

Imam Waki Ibn Jarrah alifariki mnamo mwaka 197 Al Hijra baada ya Ibada ya Hija, na alikua na mtoto wake ambae alimwambia: **'Ewe Mtoto wangu angalia mkono wangu na kisha shushudia kua mimi sijawahi kumpiga mtu yeyote kwa kutumia mkono wangu huu.'**

IMAM MUSA AL KADHIM 128 A.H

Imam Abu Hasan Musa Al Kadhim Ibn Jafar As Sadiq Ibn Muhammed Bakir Ibn Ali Zayn Al Abidin Ibn Huseyn Ibn Ali Ibn Ebi Talib *Radhi Allahu Anhu* alizaliwa mnamo siku ya mwezi 7 wa Safar ya mwaka 128 Al Hijra katika meneo ya Abwa ambayo yapo baina ya Mji wa Makkah na Madina. Mama yake alikua akiitwa Humayda Barbariyah.

Imam Abu Hasan alipewa jina la Al Kadhim kwa sababu alikua ni mtu mwenye uwezo mkubwa sana wa kujidhibiti hasira zake na hivyo alikua ni mtu ambae ni mwenye kuwaonea huruma na kuwapenda hata maadui zake.

Imam Al Kadhim alikua na Ilm kubwa sana na Ucha Mungu mkubwa sana kwani alikua ni mwenye kusoma kwa baba yake ambae ni Imam Jafar Al Sadiq kwani anasema Imam AbuHanifa kua: '**Safari moja baada ya kufanya Ibada yangu ya Hija basi nilienda katika Mji wa Madina kumtembelea Imam Jafar As Sadiq na nailipofika Nyumbani kwake basi nikagonga na kusubiri niruhusiwe kuingia ndani na mara akatoka mtoto mdogo, na akanisalimia na baada ya kumjibu basi nikamuuliza: 'Hivi hapa katika Mji wenu ni sehemu Mtu mgeni anaweza kujisaidia?'**

Ambapo Mtoto huyo akasema: **'Inabidi we mbali kutokana na ukingo wa Mto, mbali na sehemu inayoangua matunda, mbali na uwa wa Miskiti na sehemu za barabarani za wapita njia, na unatakiwa ujifiche nyuma ya kitu kitakachokuficha huku ukiwa hujakipa mgongo wala hujakielekea Kibla, ukipata sehemu kama hio basi inatosheleza kujisaidia ''**

Imam Abu Hanifa anaendelea kusema kua: **'Hakika mimi nilifurahishwa sana na majibu ya mtoto huyo hivyo nikamuuliza: 'Jee jina lako ni nani?' ambapo ane akasema: 'Jina langu ni Musa Ibn Jafar Ibn Muhamad Ibn Ali Ibn Husain Ibn Ali Ibn Abi Talib' hivyo nami nikamuuliza: 'Hivi Jee unajuaje kuhusiana na asili ya Matendo maovu kwa Muumba.'**

Ambapo nae akajibu: 'Asili ya Maovu bila ya shaka hua ni kutokana na moja kati ya vyanzo vitatu; ambavyo ni Muumba, au Muumba na Kiumbe au Kiumbe;

ambapo kama ikiwa chanzo ni Muumba (ambalo si jambo sahih) basi hua si uadilifu kwake Muuumda kumuadhibu Kiumbe kutokana na kitendo ambacho yeye sio chanzo chake'

Na kama asili yake ni Muumba na Kiumbe (ambalo si jambo sahih) basi hua si sahih kwa sababu kutokana nao mtizamo huu basi hua inamaanisha yu;e mwenye nguvu amefanya yule aliedhaifu kufanya ovu husika'
Na kama asili yake ni Kiumbe (ambalo ni jambo sahih) basi bila ya shaka Muumba atamsamehe Kiumbe wake kutokana na Ukarimu wake na uhuru wa maamuzi yake au atamuadhibu kutokana na ufanywaji wa Ovu husika.'

Imam Abu Hanifa anaendelea kusema kua: 'Baada ya kupata Mjibu hayo basi nami nikaondoka bila ya kuonana na Jafar As Sadiq kwa sababu maneno hayo yalikua ni yenye kunitosheleza.'

Hivyo Imam Al Kadhim alikua alikua ni mwenye kuifikia Darja ya Mwanazuoni mwenye kua na uwezo wa kufanya Ijtihad kutokana na kua ni mwenye kusomeshwa na baba yake ambae ni Imam Jafar Al Sadiq kwa mda wa miaka 20, na pia alisoma kwa Maimamu wengineo, na alikua ni Imam mwenye kuaminika kwenye Ilm ya Hadith na miongoni mwa Hadith zake zenye *Sanad* kupitia kwa baba yake hadi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi ni pamoja na ile isemayo kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kukosha Mikono Kabla ya Kula hua ni kwenye kuondoa Umasikini na Kuikosha baada ya Kula hua ni kwenye kuondoa Huzuni''**

Mbali ya kua alikua ni Mwenye sifa ya kua na Ilm kubwa, Ucha Mungu, Usamehevu na ukarimu na kua ni mwenye kujiweka mbali na mambo ya siasa kwani ni mwenye kuachana na Dunia yake, Lakini Imam Al Kadhim alipatwa na Mitihani ya Kidunia pale alipokamatwa na Khalifa Muhammad Ibn Mahdi na kuwekwa ndani katika mji wa Baghdad kutokana na ukubwa wa athari za Umarufu wake, ambapo baada ya kufungwa kwake basi Khalifa Muhammad Ibn Mahdi akamuona usingizini *Amir Al Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akimuamrisha kua amuachie huru Mjukuu wake huyo.

Na hivyo asubuhi yake Khalifa Muhamamd Ibn Mahdi akamuachia Huru Imam Al Kadhim na kumtaka aahidi kua asije akasababisha Uasi katika Mamlaka yake, na alipokubaliana na kuthibitisha ahadi hio basi Imam Al Kadhim akarudishwa katika Mji wa Madina lakini hata hivyo baadae akakamatwa tena na Khalifa Harun Rashid na kukaa ndani kwa mda wa miaka 7 hadikufariki kwake mnamo mwaka 186 Al Hijra na alizikwa katika Ardhi ya Baghdad katika maeneo ya Kadhmiye, katika eneo ambalo ulijengwa Msikiti mkubwa sana pembeni yake kama kumbukumbu yake.

Ambapo wakati alipokua ndani kifungoni basi Imam Al Kadhim alimuandikia barua Khalifa Harun Rashid na kumwambia: **'Mitihani na Mtatizo kwa upande wangu**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

haitomalizika, na wewe kwa upande wako utakua na utulivu na na mwenye starehe, lakini usisahau kua mimi nawe tutakutana katika kesho yenye Kudumu.' Imam Musa Al Kadhim alikua ni mtu amabe anapoingia Msikitini basi hua ni mwenye kukaa mde mrefu sana katika Ibada zake, ambapo siku moja aliingia katika Masjid An Nabawi na kusali Sala ya baada ya Sala ya Isha na ndani ya Sijda ya mwisho ya Sala hio basi alikua akisikika akiomba Dua kwa kusema: **'Ya Rabbi Hakika ya Dhambi zangu ni Nyingi sana, lakini na Usamehevu wako ni mkubwa sana'** ambapo alidumu na Dua hio ndaniya Sijda hio hadi katika wakati wa Sala ya Alfajir akiwa katika hali hio hio ya Sijda na kuendelea kumba Dua hii hio.

Aliusia Imam Al Kadhim kwa kusema kua: '**Kama ikwia kuna mtu ambae ni Rafiki yako aliekuvutia kutokana na Ufahamu wake, lakini akawa na matatizo ndani ya Myo wake, basi usiachane nae hata kama ukiwa ni mwenye kujua rafiki yako huyo amepotoka, bali bakia nae huku ukiwa ni mwenye kusubiri Nusura ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake.'**

Na akasema tena: 'Inapokua kuna Uadui ndaniya familia baina ya Ndugu wa familia basi ili kuuondoa Uadui huo inabidi kupeana mikono kila mnakutana, kwani kusalimiana kwa kupeana mikono huondoa Uadui baina ya Watu.'

Ambapo anasema Imam Al Shibli kua: **'Imam Al Kadhim alikua ni Mtu mcha Mungu sana na Walii wa wakati wake, alikua ni mwenye Hikma na busara Mkarimu na mwenye huruma kwa wote, alikua ni mwenye kuwatembelea Wagonjwa na kuwasaidia wenye mitihani wote huku akiwa ni mwenye kufanya Ibada zake za Siri kwa ajili ya Mola wake, na alikua akipenda kuomba Dua kwa kusema kua: 'Ya Allah kifanye Kifo kiwe rahisi kwangu na uwe ni mwenye kunisamehe katika kuhesabiwa Madhambi yangu katika siku ya Malipo''**

Muumini wa kweli hua ni sawa na Mezani yenye sahani mbili za kupimia uzito, kwani kila kila akiwa na Imani zaid basi ndio huzidi kukabiliana na mitihani zaid.

Yeyote yule mwenye kumuaminia *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hatakiwi kumlaumu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na kuchelewa kupatikana kwa riziki yake.

Muogope *Allah Subhanah wa Ta'ala* na sema ukweli hata kama utakuepeleka kupoteza maisha yako kwani uokovu wako uko kwenye kusema ukweli wako na kuangamia kwako kuko katika kusema uwongo kwako.

Mwenye kuutafuta Uungu, Basi ataangamia, Mwenye Kutafuta Mamlaka ataangamia na mwenye kutafuta kujionesha kwa Nafsi yake basi ataangamia.

Machumo ya Kidunia na Kidini ni magumu sana, kwani kila ukinyoosha mkono wako kwa ajili ya Machumo ya Kidunia basi utakuta kua wenye Dhambi hua tayari wameshakutangulia juu ya hilo na kila ukinyoosha mkono kwa ajili ya Machumo ya Kidini basi hutakutana na yeyote wa kukusaidia.

Ujirani mwema hua si katika kujizuia kutokana na madhara ya Majirani bali hua ni kutokana na ustahmilivu wa Madhara ya Majirani.

Inapokua Dhulma imetawala basi Kiislam hua haikubalikia kupokea kitu chochote kutoka kwa yeyeote bila ya kukifanyia uchunguzi kwanza juu ya uhalali wake.

Jaribu kuugaw amda wako katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni iwe ni kwa ajili ya kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa siri; Sehemu ya pili iwe ni kwa ajili ya kujitafutia riziki yako,; Sehemu ya Tatu ni kwa ajili ya kua na jamaa na marafiki zako na Sehemu ya nne ni kwa ajili ya Uadilifu juu ya Haki za matamanio yako ambako kutokana na hii sehemu ya nne basi ndio utaweza kuyataekeleza haya matatu yaliyobakia.

Kamwe usifikirie kuhusiana na Umasikini wala Umri mrefu, kwani ukiufikiria umasikini basi Utakua ni Bakhili na Ukiufikiria Umri mrefu basi utakua na Tamaa.

Jifunze Ilm ya Dini kwani Ilm ya Fiqh hua ni dio Ufunguo wa Ufahamu na ukamilisho wa Ibada zako na ndio chanzo cha kuifikia Darja inayoheshimika hapa Duniani na Akhera pia, ukubwa wa Darja ya Mwenye Ilm kulingana na mwenye kufanya Ibada hua ni sawa na ukubwa wa Darja ya Jua kulingana na Nyota, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* si mwenye kupokea Amali za wale wenye kufanya Ibada bila ya kua na Ilm juu ya Ibada husika.

Katika wakati wa Mtawala Muadilifu basi Onyesha shukurai kwa Mola wako nawe utapanda Darja na katika wakati wa Mtawala Dhalimu basi kua na Subra nae atakubebea Mzigo wako wa Dhambi.

Tahadhari na Kufanya Maskhara kwani hukuzimia Nuru ya Imani yako na kukuadhirisha na tahadhari na Uvivu kwani hukukosesha sehemu ya manufaa yako ya Kidunia na ya Akhera pia.

IMAM MIMSAD AD DINAWARI 130 AH

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abu Ali Ahmad Mimsad Ad Dinawari (Ad Dinuri) alizaliwa katika ardhi ya Nishapuri nchini Iran katika maeneo ya Dinawari ambapo wengine hua wanasema Dinuri, na alisoma katika Mji huo huo wa Dinawari pia ambapo baadae akafunga safari kutafuta Ilm katika maeneo mengine ya Ardhi za Kiislam.

Imam Al Dinawari alikua akiitwa Mim Sad ambalo jina lenye kutokana na herufi mbili yaani herufi *Mim* na Herufi *Sad* na hivyo jina hio kua ni lenye kumaanisha : ‘*Mwenye furaha ya Kuridhika*’ na Ilm kubwa sana na alikua akijulikana kwa sifa ya Diwwan Al Sahih, Imam Zukhruf Al Maani, Shaykh Ad Din, Miftah Al Madhhab, na pia Shaykh Al Hudda.

Imam Mimsad Ad Dinawari laikua ni mtu mwenye Mali nyingi sana, ambazo alikua ni mwenye kuzitumia kwa jili ya kuwasaidia Masikini wa eneo la Mji wake wa Dinawar aliokua akiishi, ambapo mwaka mmoja aliamua kufunga safari ya kuelekea katika Mji wa Makkah kwa ajili ya Ibada ya Hija, na hivyo akatoa Sadaqa mali zake zote, na kisha akaiwacha familia yake na kuelekea katika Ibada hiyo huku akiomba Dua kwa kusema: **‘Ya Allah Hakika mimi nnakukabidhi wewe familia yangu kua chini ya usimamizi wako’**

Na kisha baada ya hapo akafunga safari yake hio kuelekea katika Mji wa Makkah, ambapo njiani alipofika Jangwani akakutana na mtu ambae hata hivyo alikua hamjui na wala hajawahi kumuona hapo kabla, ambapo mtu huyo alikua na sahani iliyojaa vyakula na alipofika mbele yake akamsalimia Imam Ad Dinawari, na kisha akakaa kitako na kumkaribisha Imam Ad Dinawari katika kula chakula hicho, hivyo Imam Ad Dinawari akamuuliza: **‘Jee wewe ni Nani?’**

Ambapo mtu huyo akasema: **‘Mimi ni mtu kutoka katika Ulimwengu usioonekana na nimekuja mbele yako kukuletea chakula kwa ajili yako kama vile ambavyo ninavyowapelekea watu wa familia yako chakula chao kutoka kwenye sahani hii kila siku kama nilivyokua nimeamrishwa na *Allah Subhanah wa Ta’ala.’***

Imam Ad Dinawari aliishi kipindi kimoja na Imam Al Junad, na aliwahi kukutana na Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Sarri Al Sakati, Maaruf Al Kharki, Imam Yahya Al Jila na akasoma kwa Imam Hubayrat Al Basr ambae ndie aliekua Mwalimu wake Mkuu na akawa ni mwenye kuendeleza darsa lake baada ya kufariki kwake Imam Hubayrat.

Ambapo mwanzoni katika wakati wa uanafunzi wake Imam Ad Dinawari alikua ni mtu mwenye kupingana na Ilm ya Tasawwuf, na alikua hataki kabisa kusikia kuhusiana nao hususan na Imam Al Junayd, ambapo nae alipopata habari hio basi Imam Al Junaid akaamua kumuandikia barua Imam Al Dinawari, kama anavyosema Imam Abu Nasr Sarraj Al Tusi kua: **‘Mimi nimemsikia Ahmad Ibn Ali Al Kharki akisema kua: Al**

Junayd alimwandikia Barua Mimsad Al Dinawari ujumbe ambao ulipomfikia Al Dinawari na kuisoma basi akaamua kuijibu barua hio kwa kusema: 'Kilichoandikwa na ujumbe wako ni kitu cha ukweli ambacho mimi sikuwahi kukijua, kwani huu ni ukweli usioshikamana na Uongo ndani yake.''

Katika safari zake za kujitafutia Ilm Imam Ad Dinawari alipofika katika Mji wa Basra basi akawa ni mwenye kusoma kutoka kwa Imam Hubayrat Al Basr kwa mda mrefu na na siku moja basi Imam Hubayrat akamwambia Imam Ad Dinawari kwa kusema kua: **'Nenda Katie Udhu kisha njoo.'** Hivyo Imam Ad Dinawari akaenda kutia Udhu kisha akasogea karibu ya Mwalim wake Imam Hubayrat na alipofika mbele yake basi Imam Hubayrat akauchukua mkono wa Imam Ad Dinawari na kisha akanyanyua mikono kwa kusema: **'Ya Allah Mjaalie Mimsad Ad Dinawari awe ni mwenye kufikia Darja ya Darwesh**'

Na kisha hapo hapo Imam Ad Dinawari akaanguka na kuzimia na kisha kupata fahamu na kuzimia tena na hivyo hali hii kua ni yenye kujirejea mara kadhaa, na mwishoni Imam Ad Dinawari akatulia, na kisha kasimama na kuuchukua mkono wa Mwalimu wake na kuubusu, na hapo Imam Ubayrah akauliza: **'Jee umepata kile ulichokua unakitaka?'** na Imam Ad Dinawari akasema: **'Naam Alhamd Lillah, hakika mimi nimekua nikijitahidi kupigania hali hii kwa mda wa miaka 30 sasa, chini ya usimamizi wako na leo nimefanikiwa kupata kile nilichokua nikikitamani.'**

Hivyo Imam Hubayrat akampa Ijaza Imam Ad Dinawari na Imam Ad Dinawari akawa ni mwenye kusomesha Wanafunzi waliobakia kwa kumsaidia Imam Hubayrat, ambae nae alikua akimpenda sana Imam Ad Dinawari.

Ambapo anasema Imam Muhamamd Ibn Abd Allah Al Yafi kua: **'Anasema Imam Mimsad Ad Dinawari kua: 'Mimi nililala nikamuota *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na kumuuliza *Ya Rasul Allah!* Hivi jee unakumbuka kitu chochote kuhusiana na sauti za kuimba?' ambapo nae akasema: 'Sizikatai, lakini waambie kua wakianza basi na waanze na kusoma Qur'an' na hivyo nami nikasema: '*Ya Rasul Allah* lakini wenzangu hawa hua wananikera na pia kunifurahisha' ambapo nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Ewe Abu Ali Wastahamilie, kwani hao ni wenzako' Mimsad anasema kua: 'Hakika baada ya kusikia hayo basi nilifurahi sana kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameniita kwa jina langu.''**

'Safari moja kuna kundi la watu wa Tassawuf walihudhuria kwenye nyumba ya Hasan al Qazaz na hivyo wakawa wanafanya Dhikr na Kuimba huku wakiwa katika hali ya kunanesa nesa kutokana na raha wanayoihisi kutokana nayo, na mara akaingia Mimsad na hivyo watu hao hapo hapo wakasimama na kusitisha kila kitu walichokua wakikifanya, ambapo Mimsa akawaambia Watu hao:

'Mbona mmesita na kukaa kimya? Endeleeni na mliyokua mkiyafanya, kwani kama nikiendelea kusikia kuhusiana na starehe za Dunia ndani ya masikio yangu, basi sitoweza kujishughulisha juu ya kile nnachotaka kujishughulisha na wala sitoweza kujitibu maradhi ya Nafsi yangu.''

Anasema Imam Ad Dinawari kua: **'Siku moja nilipokua safarini nilikutana na mtu mmoja ambae alikua ni mzee sana, bada ya kusalimiana nae nikamwambia kwa kumuuliza: 'Jee unaweza kuniusia chochote kile?' ambapo nae akasema: 'Kua na Huruma, Kua na Ikhlasi katika Nia juu ya kila kitu chako, kwani Vitendo vyote vya mtu mwenye Ikhlasi hua ni vyenye kupokelewa kwa mtizamo mwema, na hivyo Matendo hayo hua ni kua ubora zaidi katika hali yake na upokewaji wake.''**

'Mara moja mimi nilikua nnadaiwa deni ambalo lilikua limenikaa kwenye Moyo wangu, hadi pale usiku mmoja nilipoona kwenye Ndoto usingizini mwangu kua naambiwa kua: 'Ewe Mwenye Ubakhili wa kupindukia, hivi kwanini hutuamiani sisi kutokana na Deni lako? Kwani Deni lako umetukabidhi sisi na sisi ndio wenye dhamana ya kukulipia Deni lako, hivyo usiwe na wasi wasi na Deni lako.' Na hivyo baada ya kuota ndoto hio basi mimi kamwe sikua ni mtu mwenye kujali kuhusiana na Madeni nnayodaiwa, kwani ilikua kila siku inapatikana njia ya kuyalipa.'

Kuna mtu alimfuata Imam Ad Dinawari na kumuomba kua amuombee Dua ili aweze kupata kazi, kwani alikua hana kazi, hivyo Imam Ad Dinawari akamwambia mtu huyo huyo kua: **'Nenda kaishi katika sehemu ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameiridhia juu yake na hivyo hutokua ni mwenye kuhitaji Dua za Mimsad'** na hivyo mtu huyo akauliza: **'Jee sehemu hio inapatikana wapi?'** Imam Mimsad akasema: '**Katika sehemu ambayo hawaishi watu**'

Hivyo Mtu huyo akahama mji na kuhamia nje ya mji na akawa anaishi peke yake, na akawa nimwenye kufanya Ibada katika maeneo hayo hadi akafikia katika hali ya juu ya Ucha Mungu. Safari moja katika mji wa Dinawari yakatokea Mafuriko, na hivyo watu wakakimbilia kujitafutia hifadhi kwenye jengo analoishi Imam Mimsad ambalo lilikua halijafikiwa na Maji.

Ambapo miongoni mwao watu hao alikuwemo na yule mtu aliehama Mji pia, ambae alikuja hukua akiwa anaelea juu ya Maji baada ya kutandika msala wake, na hivyo Imam Ad Dinawari akamuuliza Mtu huyo: **'Hii unayofanya ndio nini?**' Mtu huyo akasema: **'Unaniuliza hii ndio nini wakati wewe ndie ulie nisababishia mimi kua na hali hii? Kwani ni kutokana na Dua za Mimsad basi mimi ndio nimekua ni mwenye kufikia hali hii kutokana na Idhini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Alisema Imam Ad Dinawari kua: **'Njia ya kuifikia Haki ndefu sana na ni ngumu, hivyo inabidi kua na subira unapokua katika njia hiyo'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

‘Mwenye kutafuta Ilm anatakiwa amheshimu Mwalimu wake, Awasaidie Ndugu zake, Aachane na Dunia yake, ajilinde kwa ajili kuihifadhi Imani ya Dini yake’

‘Vile vitu anavyoviabudu Mtu hua viko tofauti, kwani kuna yale anayopenda sana kuyafanya kwa ajili ya Matamanio ya Nafsi yake, ambapo kuna baadhi hua wanawapenda wake zao, kuna baadhi wanawapenda watoto wao, kuna baadhi wanazipenda Darja na vyeo vyao, n.k na kila mtu hua ni mwenye kuviweka vitu hivyo ndani ya Moyo wake, na hivyo hua ni vigumu sana kuachana na kushikamana na vitu hivyo, ambapo wale wenye kujijua Nafsi zao na kutojiamini juu yao Nafsi zao, Mali zao, Madaraka yao, n,k hua ni wenye kua kutokana na kua na mapenzi na vitu hivyo basi hua kamwe hawawezi kumuabudu ipasavyo *Allah Subhanah wa Ta’ala* ambae ndie Mola wao, na hivyo hu ani wenye kuona na kujua kua daima wyale wanayoyafanya kua ni yenye kasoro ndani yake, na hivyo hua ni wenye kujilaumu Nafsi zao, na kutokana na kujilaumu Nafsi zao basi ndio hua ni wenye kuupata uokovu kutoka kwa Mola wao.’

‘Tawakkul hua ni kuachana na Kila kitu ambacho Moyo wako na Nafsi yako inavutiwa nacho.’

‘Kama Ibn Adam akiwa ni mwenye kumfikiria *Allah Subhana wa Ta’ala* tu peke yake, basi hakna kitu kitakachoweza kumdhuru Ibn Adam huyo.’

Ambao anasema Imam Abd Rauf Al Manawi kua: ‘**Mimsad Ad Dinawari ni mmoja kati ya Mashaykh wakubwa, wenye Ilm, Ucha Mungu, Unyenyekevu. Kiongozi wetu na Tabira nzuri sana mwenye kufuata nyayo za Maimamu waliotangulia katika Ilm ya Tasawwuf, alikua ni mwenye kushikamana na Dini kuachana na Dunia, Mwenye kudumu na Adhkari maalum katika kila wakati wake, n.k’**

Na Imam Abd Rahman Al Jamii alisema kuhusiana nae kua: **‘Ad Dinawari alikua ni Mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa ambao ni Vijana wa Iraq, mwenye upekee katika Ilm na kuheshimika sana na mwenye Tabia njema, alikua na ukaribu na Yahya Al Jalaa.’**

Imam Abu Nasr Sarraj Al Tusi kua: ‘**Masikini walikua wakienda kwa *Mimsad Ad Dinawari*, ambapo nae alikua akienda Sokoni kwa ajili ya kuwanunulia mahitaji yao na kuwagaia kama Sadaka yao kutoka kwake, kutokana na unyenyekevu na ukarimu wake.’**

Imam Mimsad Ad Dinawari alikua ni mtu mwenye kua katika Ibada ya kufunga katika Maisha yake yote, kwani alikua kila sikua nafunga isipokua katika siku ya wanza ya Eid Al Fitr na katika siku nne za Idd Al Adha.

Miongoni mwa kauli zake za Wasia Imam Mimsad Ad Dinawari basi ni kua: '**Njia ya Haki ni ndefu sana, Na wenye Subra na juu ya Haki hua ni wenye kua na wakati mgumu sana, Ilm ya kweli hua ni katika kujisalimisha kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Uongofu hua ni Kumtii yule ambae asieghafilika na Utiifu wako, Mghafiliko hua ni kudharau kumkumbuka yule ambae asiesahau kumkumbuka kwako ndani ya Moyo wako.'**

'Wenye kushikamana na Wacha Mungu hua ni wenye kurithishwa Ucha Mungu ndani ya Nyoyo zao, na wanaoshikamana na Wapotovu hua ni wenye kurithishwa Upotovu ndani ya Nyoyo zao.'

Imam Ad Dinawari alisema kua: **'Adabu ya mwenye kutafuta Ilm hujumuisha mambo manne ambayo ni Kushikamana na mipaka ya Shaykh wako, Kuwahudumia Waislam wenzako, Kuachana na Visingizio na kusimamia Sharia kwenye Tabia zako.'**

Siku moja Imam Ad Dinawari alitoka nyumbani kwake asubuhi na mara akatokea mbwa na kuanza kumbwekea, ambapo Imam Ad Dinawari akageuka na kumtizama Mbwa huyo na kusema: '***La Ilah Illa Allah***' na hivyo mbwa huyo akaanguka chini na kufariki hapo hapo.

Kabla ya kufariki kwake mnamo mwaka 299 Al Hijra, basi Imam Ad Dinawari alikua akiumwa na hivyo alipoulizwa hali yake basi alisema kua: '**Imepitia zaidi ya miaka 30 sasa mimi nimekua ni mwenye katika kupigana kutokana na kuupoteza Moyo wangu, lakini sikufanikiwa kuuteka tena upya Moyo wangu, na hivyo haiwezekani sasa hivi mimi kua ni mwenye kuutena tena Moyo wangu kwani nnaishi miongoni mwa watu ambao ni wenye kuzipoteza nyoyo zao'.**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM ABU YA'LA

Imam Abu Ya'la Muallah Ibn Mansur aliishi nchini Iraq katika Mji wa Iraq katika kipindi cha mwanzoni mwa miaka 100 na miaka 200 ya mwanzoni ya Uislam na alifariki mnamo mwaka 211 Al Hijra.

Imam Abu Ya'ala alisoma kutoka kwa Imam Anas Ibn Malik, Imam Saad Al Layth, Imam Ali Ibn Madini, Imam Abu Bakr Ibn Abi Shaybah, Imam Abu Haytham, Imam Abu Yahya, Imam Abu Yusuf, Imam Muhammad Ash Shaybani na Maimamu wengineo.

Ambapo Imam Abu Ya'ala alikua ni kiongozi miongoni mwa Wanafunzi wa Al Qadhi Imam Abu Yusuf Al Hanafi na alikua ni Thiqah mwenye Ilm kubwa sana ya Hadith. Imam Abu Ya'ala alimwambia Imam Abu Zurah kua: **'Hakika mimi napenda sana kutafuta Ilm na nimesafiri sana kwa ajili ya kutafuta Ilm'**

Ambapo anasema Imam Ahmad Al Ijli kua: **'Abu Ya'ala alikua ni mtu mwenye kuaminika, ni Thiqah, ni mtu ambae mbali ya kua ni mwenye kujua lakini mara nyingi sana alikua ni mwenye kutopendelea kua ni miongoni mwa wenye kuchaguliwa katika utoaji wa Fatwa'**

Ambapo anasema Imam Yahya Ibn Main kua: '**Siku Moja Mualla Ibn Mansur alikua anasali na mara kuna kitu kikamuangukia kutoka juu kwenye dari, lakini hata hivyo yeye mwenyewe hakua hata ni mwenye kushtuka kutokana na kuangukiwa na kitu hicho wala kukiangalia ni kitu gani kilimuangukia bali aliendelea na Sala yake kwa utulivu hadi akamliza'**

IMAM AL WAQIDH 130 AH

Imam Abu Abd Allah Muhamamd Ibn Umar Al Waqidh Al Aslami alizaliwa katika Mji wa Madina mnamo mwaka 130 Al Hijra, na alikua ni Mtumwa aliechiwa huru wa Abd Allah Ibn Burayda Bani Aslam. Ambapo anasema Imam Abu Faraj Al Isfahan kua Mama yake Al Waqidhi alikua ni Binti wa Isa Ibn Jafar Ibn Saib Ibn Kathir ambae ni mwenye asili ya Uajemi na Baba yake alikua ni Mtu wa Marwazi.

Imam Al Waqidhi alikua ni mtoto mwenye kujaaliwa kua na ufaham mkubwa sana ambae alikua katika Mji wa Madina ambao aliishi ndani yake kwa mda wa miaka 50, ambapo alisoma Ilm za Fani tofauti za Dini ya Kiislam, ikiwemo Hadith, Qur'an, Fiqh, Siyar, Maghazi n,k kwani Imam Al Waqidh alisoma kwa Imam Abi Thahab Ma'mar Ibn Rashid, Imam Malik Ibn Anas, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Thawr Ibn Yazid, Imam Ibn Jurayj, Imam Na'afi, Imam Sulayman Ibn Muslim, Imam Muhamamd Ibn Abd Allah Ibn Muhammad, Imam Usama Ibn Zayd Al Layth, nk

Kwani katika kutafuta kwake Ilm Imam Al Waqidhi hakua ni mwenye kubakia katika Mji wa Madina tu bali alitembelea sehemu mbali mbali za Ardhi za Waislam kwa ajili ya kuwafuata Wanazuoni wakiwemo wa mji wa Kufah, Basra, Damascus, Homs na Al Raqqa.

Baadae Imam Al Waqidhi akawa ni Mfanyabiashara wa Ngano katika Mji wa Madina, na kisha akahamia katika Mji wa Baghdad mnamo mwaka 180 Al Hijra katika kipindi cha Utawala wa Mamlaka ya Khalifa Harun Rashid, ambapo alichaguliwa kua Qadhi maeneo ya Mashariki ya mji wa Baghdad na baadae pale ulipoingia Madarakani utawala wa Khalifa Al Mamun basi akachaguliwa kua Qadhi wa Kambi ya Jeshi ya Risafa.

Imam Al Waqidhi alikua ni Mwanazuoni mkubwa sana wa Fani ya Maghazi na Tarikh kuliko fani nyengine zozote zile ambazo alizokua nazo zinazojumuisha Ilm ya Qiraa, Fiqh, Hadith, Tafsir, ambapo anasema Imam Muhammad Ibn Is-haq kua: **'Hakika kama mimi sikua ni mwenye kujua kua ni *Thiqah*, basi nisingenukuu hadithi hata moja kutoka kwake**'

Imam Al Waqidhi alikua utaalamu mkubwa wa Uandishi kwani alikusanya maelezo na habari za vita kutoka kwa Wajane wa Vita, Watoto wa Mashahidi, Wapiganaji wenye na watu wa karibu wa wapiganaji hao wa Kiislam, alikua ni mwenye kua na Ilm ya kuyaelezea maisha ya Masahaba na waliofuatia baada yake tangu kuanzia katika wakati walipozaliwa hadi kufariki kwao, na alikua pia ni mwenye kuyatembelea maeneo husika ya matukio ya Vita hivyo na Matukio mengine muhimu katika Historia ya Kiislam, kifupi alikua ni Muandishi Mpelelezi.

Imam Muhammad Ibn Umar Al Waqidhi alisema kua: **'Mtu wa mwisho kufariki katika Mji wa Kufah miongoni mwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua ni Abd Allah Ibn Abi Awf *Radhi Allahu Anhu,* Sahaba wa mwisho kufariki katika mji wa Dimashq ni Abd Allah Ibn Yassar *Radhi Allahu Anhu,* Sahaba wa mwisho kufariki katika Mji wa Madina alikua ni Sahl Ibn Saad *Radhi Allahu Anhu* ambae alifariki akiwa na umri wa miaka 94. Sahaba wa mwisho kufariki katika ardhi ya Basra alikua ni Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* na Abu Tufayl *Radhi Allahu Anhu* alikua ni Sahaba wa mwisho kufariki katika Mji wa Makkah na huyu ndie aliekua amefariki katika mwaka wa 100 Al Hijra.**'

Ambapo Imam Ibn Saad ambae ni Mwanafunzi wa Imam Al Waqidhi na muandishi wake pia anasema kua: **'Wanazuoni wa walikua wakija kwa Al Waqidhi na kuuliza juu ya yale wasiyoyajua na kisha kuchukua majibu wanayopewa bila ya kupinga wala kubishana.'**

Imam Muhammad Ibn Salam Al Jumahi anasema kua: **'Al Waqidhi alikua ni Mwanazuoni wa wakati wake'**

Imam Muhamamd Ibn Umar Al Waqidhi alikua na sifa ya na kipaji cha upekee pia ya kuelezea matukio yaliyotokea katika historia ya Uislam kiasi ya kua ilikua kama yanaonekana katika wakati huo anayoyaelezea, na hivyo kua ni mwenye kudhihirisha ujasiri wa Wapiganaji wa Kiislam kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na namna

walivyokua wakijitolea kwa ajili ya Dini yao, na pia mabadiliko ya maendeleo yaliyosababishwa na Mapigano hayo katika ardhi husika baada kutekwa na Waislam kutokana na uadilifu wa Viongozi wa Kiislam.

Imam Abd Allah Ibn Ubayd Allah anasema kua: **'Amesema Muhamamd Ibn Umar Al Waqidhi kua: 'Khalifa Harun Rashid alikuja katika Mji wa Madina, baada ya Ibada ya Hija, na kisha akamuuliza Waziri wake Yahya Ibn Khalid Ibn Barmaki kwa kumwambia: 'Kama tutaweza kupata Mtu ambae atatuhadithia matukio yaliyotokea kwenye Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake na kutuonesha sehemu yaliyotokea matukio hayo basi itakua vizuri zaid.' Ambapo watu wakanitaja mimi na kuelezewa kua nnapatika katika Masjid An Nabawi katika Sala ya Isha**'

Hivyo baada ya Sala ya Isha Al Barmaki akaniita na kunitambulisha mbele ya Khalifa Harun Rashid, **na kisha baada ya hapo, mimi na Barmaki na Harun Rashid tukapanda Punda huku nikiwatembeza Usiku kucha, huku nikawaonesha sehemu ambazo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akipokelea Wahy kutoka kwa Malaika Jibril, Makaburi ya Masahaba, na yaliyowatokea katika maeneo mbalimbali waliyoishi katika maisha yao, na ilikua katika kila sehemu tukifika baada ya kuelezea basi walikua wakishuka kwenye Punda wao na kisha husali Rakaa mbili na kisha huomba Dua huku wakiwa ni wenye kulia usiku kucha**'

'Hali hii iliendelea hadi pale ilipoadhiniwa Adhana ya Sala ya Alfajir, nasi tukarudi Msikitini na Kusali sala ya Alfajir, na kisha baada ya hapo Al Barmaki akasema kua: 'Khalifa Harun Rashid amevutiwa sana na kurufahia sana ziara yetu na hivyo ananitaka nipokee zawadi ya Dirham 10000, na kusema kama nikitaka zaidi basi niwaambie watanipa', hivyo nami nikachukua Dirham hizo na kusem akua zinanitosha kwanza hizi kulipa madeni yote iliyokua nikidaiwa, na hivyo nikalipa na kua si mwenye Madeni ndani ya mwaka huo mzima.'

Imam Al Waqidh alikua ni mtu mkarimi anaendelea kusema kua: **'Baada ya Mda ulipokaribi Mwezi wa Ramadhani ambapo ilikua imebakia siku 10 tu kabla ya Ramadhani, mim inilikua sina hata akiba nyumbani kwangu na sijafanya matayarisho yeyote kwa ajili ya Ramadhani, hivyo ikawa nnafikiria kua kusema kua: 'Kama sikua na akiba wala pesa safari hii itanibidi niende nikakope kwa Marafiki zangu.**

Hivyo siku mbili kabla ya kuandama mwezi, nikatoka hadi kwa rafiki yangu mmoja na kugonga mlango wake, na kumuelezea hali yangu ilivyokua, ambapo rafiki yangu huyo akafikiria kidogo kisha akaingia ndani na kutoka na kimfuko ambacho akanipa, nami nikachukua na kumshukuru na kisha nikarudi nyumbani,

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

na nilipofika nikamwita Mfanyakazi wangu na kuanza kuchukua kartasi na kuorodhesha vitu nnavyovihitaji, wakati nnaorodhesha vitu hivyo vyote mara mlango wa nyumba yangu ukagongwa, na nilipoufungua nikaona kua anaegonga alikua ni mtu mtukufu kwani alikua ni mmoja kati ya Wajukuu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*’

Na nilipomuuliza haja yake basi akaniambia kua: ‘Nna shida ya pesa kwani Ramadhani inakuja na sina kitu chochote nyumbani kwangu.’, hivyo nami nikashindwa kujizuia kwani sikutaka kutomsaidia Mjukuu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuachia aondoke akiwa mikono mitupu kutoka kwangu. Hivyo nikakichukua kile kifuko nilichopewa na rafiki yangu kisha nikamkabidhi yeye, na kisha akashukuru na kuondoka.’

Nikamwambia mke wangu yaliyotokea ambapo nae pia akanipongeza na kufurahia kutokana na kufanya wema huo wa kumsaidia Mjukuu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam, na kisha tukamshukuru Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa kumjaalia Mjukuu huyo wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutufuata sisi kwa ajili ya kumsaidia shida yake.

Na kisha baada ya hapo akanijia akilini rafiki yangu mwengine ambae anaweza kunisaidia, hivyo nikatoka na kuelekea nyumbani kwake, ambapo baada ya kufika na kumuelezea shida yangu basi akaingia ndani na kutoka na kifuko na kusema: ‘Chukua Nusu kutoka katika Mfuko huu na kisha nusu nibakishie mimi.’ Nami nikafanya kama alivyonielekeza, ambapo wakati nakifungua kifuko hicho basi nikagundua kua kifuko hicho ndio kile kile ambacho mimi nilimpa Mjukuu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.

Hivyo nikachukua nusu kilichokuwemo na nusu nikabakisha na kisha nikamkabidhi rafiki yangu huyo nami nikarudi nyumbani, na kisha nikakaa kitako na kuanza kuandaa listi nyengine mpya ya mahitaji ninayoyahitajia kwa ajili ya mwezi wa Ramadhan, ambapo wakati naandika mara mlango ukagongwa tena, na ulipofunguliwa akaingia ndani mfanyakazi wa Waziri Yahya Ibn Khalid Al Barmaki ambae alinimbia kua : ‘Waziri Yahya Khalid Al Barmaki anataka nikaonane nae nyumbani kwake alikofikia’

Hivyo nami nikajitayarisha na kuelekea kwenye nyumba aliyofikia Al Barmaki na nilipofika tukasalimiana na kisha akasema: ‘Ramadhani inakaribia, hivyo jee kuna hitajio lolote lile ambalo unalihitajia kwa ajili ya matayarisho yake.’
Nami nikamwambia kua: ‘Mkasa wangu ni mrefu sana’ ambapo nae akaniambia nimuelezee. Nami nikamuelezea kila kitu kilichonitokea katika siku hio, ambapo baada ya hapo akamuita mmoja kati ya watu wake na kumwambia anipatie kifuko kwa ajili yangu, kwa ajili ya rafiki yangu, kwa ajili ya Mjukuu wa *Rasul Allah*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

***Salallahu Alayhi wa Salam* na yule rafiki yangu mwengine pia, ambapo kila mmoja wetu akawa ni mwenye kufurahia jambo hilo na kua ni mwenye kumuombea Dua Al Barmaki.**

'Lakini hata hivyo mwaka uliofuatia Madeni yakarudi tena kwangu upya kwa wingi zaidi, na kutokana na kutiwa Moyo na Mke wangu basi nikafunga Safari kuelekea Baghdad kwa Wazir Al Barmaki, ambae alinipokea kwa heshima na taadhima na kunikaribisha Iftar katika kila siku kwani ilikua ni mwezi wa Ramadhan, na yeye alikua ni Imam na hivyo alikua ni mwenye kusalisha na kunifanya nikae pembeni yake katika kila Sala na katika baraza ya Ilm iliyokua ikikusanyika kila baada ya Iftar, ambapo alikua haulizi masuali yeyote kwa yeyote yule isipokua mimi, ambapo kila siku baada ya Barza hio alikua akinizawadia kifuko chenye Dirham 5000.'

Hivyo nami nikanunuanYumba katika Mji wa Baghdad, na kununua Farasi na kua na mfanyakazi pia, na kisha nikatuma Pesa nyumbani pia kupitia kwa Qadhi Zubayr ambae alifunga safari kuelekea katika Mji wa Madina. Ilipowadia mwishoni mwa mwezi wa Ramadhani katika siku ya sikukuu ya Idd a Fitr nasi Wazir Yahya Al Barmaki akaniambia nivalie vizuri kwani anataka kunipeleka kwa Khalifa Harun Rashid.

Ambapo baada ya Khalifa Harun Rashid kugundua kua ndio mimi niliekuea nae katika ziara ya Mji wa Madina alipotembelea baada ya Ibada ya Hija basi nae akanizwadia Dirham 30, 000, ambapo baada ya sherehe za Iddi Al Fitr basi nikaombaruhusa ya kurudi katika Mji wa Madina, na hivyo Yahya Al Barmaki akatafuta mtu wa kunisaidia kununua zawadi na kusafiri pamoja nami katika safari hio ya kurudi katika Mji wa Madina, hivyo nikafunga safari na kurudi katika Mji wa Madina huku nikiwa na msindikizaji huyo ambae sikutakiwa kumlipa hata dirham moja kwani kila kitu kilikua kimesimamiwa na Waziri Yahya Ibn Khalid Al Barmaki, hakika mimi sijawahi kuona mtu mzuri kwangu na mkarimu kama Al Barmaki.

Alisema Ibrahim Al Harb kua: **'Al Waqidhi alikua ni Mtu mwenye kuwapa Usalama Waislam wenzake.'**

Tunapoangalia Vitabu vya Imam Al Waqidhi basi tunaona kua alikua ni mwenye kuelezea kila kitu anachokielezea kwa kina, alikua akiielezea kuhusiana na Vita basi huelezea mandhari ya sehemu vilipopiganwa, mipango ya Vita ya Waislam na matayarisho yao yalikuaje na kwa upande wa Makafiri pia, idadi yao na matayarisho yao na kila kitu kama vile anavyoelezea hali ilivyokua katika kipindi cha Utawala wa *Amir ul Muuminin* Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* : **'Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alikua akitayarisha Jeshi kwa ajili kuiteka aradhi ya Dimashq, na hivyo akawa ni mwenye kutuma Barua kwa ajili ya Jambo hilo. Na hivyo akawa ni mwenye kutuma barua katika ardhi ya Yemen pamoja na Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua akijulikana pia kama Hadim *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alikua akaisubiri habari kutoka katika maeneo hayo ya Yemen.**

Siku zikapita, na mwishowe Anas *Radhi Allahu Anhu* akawasili katika Mji wa Madina, na akampa habari njema Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kwa kumwambia: 'Watu wa Yemen wamekubaliana na wito wako hivyo jee ewe Khalifa wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nimpe nani akusomee Barua yako hii kwani wamekubaliana nawe na wanajitayarisha kwa ajili ya Vita hivyo. Ewe Khalifa wa *Rasul Allah Salallahu Alayahi wa Salam* kwani wamekuja kwa idadi ya wingi sana, watu hawa ambao ni Majasiri wa Yemeni wakiwa na kila chao na vizazi vyao, wanakuja kama kwamba vile wewe ukiwa pamoja nao, wamekukaribia sana kiukaribu na wanakaribia kuwasili, hivyo jitayarishe kuwapokea.'''

Ambapo Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* anasema kua: 'Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alikua ni mwenye kufurahia sana habari hizo nzuri nilizompa na kisha siku ya pili watu hao wa Yemen waliokua wakitegemewa wakawasili. Na walikua ni waliojaa vumbi kutokana na safari yao hio, na hivyo Watu wa Madina na watu wa kutoka sehemu nyengine wakafungua Bendera za utambusho wao na kuanza kupitisha gwaride lao mbele ya Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu*, na kisha Makabila tofauti yakapita mbele ya Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu*, Koo tofauti zikawa zinapita kwa kufuatana moja baada ya nyengine, ambapo mwanzoni mwa Gwaride hilo ulikua ukiongozwa na watu wa Himyari wa Yemen ambao walikua wamevaa nguo za kivita kuanzia kichwani hadi miguuni.'

Ambapo kiongozi wao alipomkaribia Abu Bakr basi akawa ni mwenye kusoma ubeti ufuatao:

Watu wa Himyar wamekuja kwako wakiwa na Watoto wao.
Wakiwa katika kila Darja kila mmoja ni mwenye kuvijua vita miongoni mwao.
Simba vijana wakiwa ni wenye kusubiri maamrisho kutoka kwako kiongozi wao.

Ambapo Abu Bakr alikua ni mwenye kujawa na tabasamu kutokana na maneno hayo, na kisha kamwambia Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu:* '***Ewe Abu Hasan*, Hivi hujawahi kusikia wewe alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Nakubashirieni habari njema za msaada kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* dhidi ya Washirikina pale watu wa Kabila la Himyar watakapokuja pamoja na Wanawake wao wakiwa wamebeba na Watoto.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* **akajibu: 'Naam, uko sahihi kwani mimi pia nimemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua: 'Watu wa Kabila la Himyar wanaenda Vitani na Jeshi lao lote na kila kitu chao, wakiwa na kiongozi wao Kays Ibn Hubayra mbele yao.''**

Qays Ibn Hubayra alipofika mbele ya Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* basi akasema: 'Msalieni *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam*' na kisha akasema; 'Wapiganaji Mahiri wakiwa na mataji yao, wamekuja kwako, tuko mbele yako ili upate kuona Mashujaa wenye Mapanga marefu.'

Na kisha akafuatia aliekua chini yake kicheo na kisha likafuata Jeshi la Kabila la Tai ambao walikua wanaongozwa na Chifu wao aitwae Harith Ibn Masud Al Tai, na alipofika mbele ya Abu Bakr basi akataka kushuka kutoka juu ya Farasi wake, lakini wakati alipoanza kunyanyua Mguu tu basi AbuBakr akamwambia haina haja ya kushuka kwenye Farasi wake huyo, na hivyo wakamkaribia Abu Bakr na kutoa heshima zao, na hivyo Jeshi la watu wa Yemen linaendela kutoa heshima zao kwa wingi kulingana na makabila tofauti.

Ambapo hali yao hii na uhalisia wa kua wote wamekuja katika Mji wa Madina kwa ajili ya kutafuta radhi za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ilimfurahisha sana Abu Bakr, na hivyo akamshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Kisha jeshi hilo likatembea kutoka nje ya Mji wa Madina, huku Abu Bakr, akiwafuata pamoja na Masahaba wengine wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwemo Umar, Uthman na Ali *Radhi Allahu Anhum.*

Jeshi hilo lilitembea kwa Hashima na uwezo mkubwa sana, na lilipofika nje ya Mji wa Madina likanadia *Takbir: 'Allahu Akbar'* maneno ambayo yaliitikiwa na kurudishwa kwa kusikika tena baada ya sauti yake kugonga Milima iliyozunguka Mji wa Madina, na hivyo Ardhi na Mbingu zikawa ni zenye kuitikia Takbir hio pamoja na Wanyama na Ndege, kuutukuza ukubwa wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* aliliangalia hilo Jeshi na kuona namna lilivyokua limejaa Vumbi huku likiwa limejaa ari basi akasema: **'Ya Rabb, Wajaalie kua na Subra, Wasaidie wasijisalimishe kwa Maadui zao, hakika wewe ni mwenye uwezo juu ya kila kitu.'**

Abu Bakr akawaita watu tofauti na kisha akawapa Bendera, ambapo mmoja kati ya mwanzoni kupewa alikua ni Yazid Ibn Abu Sufyan ambae alikabidhiwa Jeshi la watu 1000, na pia akampa Bendera Rabia Ibn Amir ambae ni shujaa wa Hijaz ambae nae akapewa usimamizi wa watu 1000, na kisha Abu Bakr akamgeukia Yazid Ibn Abi Sufyan na kumwambia: '**Rabia Ibn Amir ni shujaa maarufu wa Hijaz, namkabidhi**

chini yako hivyo mtangulize mbele, na shauriana nae katika kila kitu na wala usipingane nae'

Baada ya hapo kila mmoja ndani ya Jeshi hilo akachukua Silaha yake na wakakusanyika kwa kupanda juu ya Farasi wao, ambapo kwa upande wa Abu Bakr akawa ni mwenye kutembea kwa miguu, ambapo baada ya kuona tukio basi Yazi Ibn Abu Sufyan akasema: **'Ewe Khalifa wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, yeyoyote yule atakaekufurahisha wewe basi atakua ni mwenye kupata Ridhaa ya *Allah*, hivyo wakati wewe unatembea kwa miguu basi Nyoyo zetu sisi haziwezi kuridhika tukiwa kwenye Farasi wetu, hivyo aidha nawe upande Farasi au sisi tushuke na tutembee kwa miguu kama wewe'** lakini Abu Bakr akasema: **'Sitopanda Farasi mimi na wala nyinyi hamtoshuka kwenye Farasi wenu.'** Ambapo alitembea nao hadi alipofika katika meneo ya Saniyat Al Wada.

Na kisha akasimama na Yazid Ibn Abu Sufyan akamkaribia Abu Bakr na kusema; **'Ewe Khalifa wa Rasul Allah, nakuomba uniusie'** ambapo Abu Bakr akasema: **'Ushauri wangu ni kua usijichoshe wewe Nafsi yako na wala usiwachoshe waliokua chini yako, shauriana nao katika kila kitu, na wala usiwakasirikie watu wako au na marafiki zako, kua ni mwenye kufanya Uadilifu, kwa sababu Jamii ya watu wenye kudhulumiana hua kamwe hawawezi kuupata uokovu, kamwe haitoweza kwao kupata ushindi dhidi ya maadui zao, Na utakapokabiliana na Maadui zako basi usiwageuke wenzako na kurudi nyuma na wala usikimbie.**

Kwani yeyote yule atakaegeuka na kuingia kwenye kundi la maadui zake bila ya kua na sababu ya kutaka kuwaghilibu na kupigana nao ndani kwa ndani au kwa kujifanya kua anawakimbia ili kuwavuta maadui weke kuelekea kwa Waislam wenzake na kisha akawageukia katika siku hio ya mapigano basi atakua ni mwenye kuzipata Ghadhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na sehemu yake itakua ni Motoni, na hakuna sehemu mbaya kama hio'

Kamwe usisahau aya ya *Surat Al Anfal* isemayo:

﴿يَاأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ إِذَا لَقِيتُمُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ زَحْفاً فَلاَ تُوَلُّوهُمُ ٱلأَدْبَارَ۞وَمَن يُوَلِّهِمْ يَوْمَئِذٍ دُبُرَهُ إِلاَّ مُتَحَرِّفاً لِّقِتَالٍ أَوْ مُتَحَيِّزاً إِلَىٰ فِئَةٍ فَقَدْ بَآءَ بِغَضَبٍ مِّنَ ٱللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ ٱلْمَصِيرُ﴾

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ya ayyuha alladheena amanoo idha laqeetumu alladheena kafaroo zahfan fala tuwalloohumu al-adbara; Waman yuwallihim yawma-idhin duburahu illa mutaharrifan liqitalin aw mutahayyizan ila fi-atin faqad baa bighadhabin mina Allahi wama/wahu jahannamu wabi/sa almaseeru(*Surat Al Anfal 8:15-16*)

Tafsir: **Enyi wale ambao mliomini kama mkikutana na wale waliokufuru kwenye uwanja wa Vita basi msiwape mgongo; Na yeyote yule atakaewapa mgongo katika siku kama hio – isipokua kwa ajili ya kutumia mbinu ya Vita au kuwakimbilia wenzake – basi kwa hakika atakua amejiingiza kwenye Ghadhabu za Allah na makazi yake ni Jahannam, na hayo ni makazi mabaya sana.**

Na kama mkiwa mmepata ushindi dhidi ya Maadui zenu basi msiwaue Watoto na Wazee, na wala msikate Miti yenye Matunda yanayoliwa, Wala msiwaue Wanyama wao, na mkiweka ahadi basi zitekelezeni, msivunje ahadi zenu, na mkikubaliana mapatano ya usulihishi basi msivunje makubaliano ya mapatano hayo ya usuluhishi, mkikutana na Mapandri Makanisani mwao basi msiwaguse wala msiyavunje Makanisa yao, na mkikutana na watu wanaoabudu Masanamu, ambao hawatoukubali Uislam na wasipokubali kutoa Jizya basi wakutanisheni na Upanga, nami na kukabidhini kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na kisha Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akamkumbatia Yazid Ibn Abi Sufyan na kumuaga na kumwambia Rabia: 'Ewe Rabia onyesha Ujasiri wako leo hii, nami namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akusameheni nyinyi na sisi kwa makosa yetu.' Na kisha Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akarudi katika Mji wa Madina na Masahaba wenzake.

Ambapo Rabia Ibn Amir akasema kumwmabia Yazid Ibn Abu Sufyan: **'Ewe Yazid, tunaelekea wapi? Na kwanini Abu Bakr akukutaka uwe Mpole?'** hivyo Yazid Ibn Abu Sufyan akasema: **'Ewe Amir, hakika Abu Bakr anatuma Jeshi kubwa sana katika Ardhi ya Dimashq, hivyo mimi nataka kuwasili katika ardhi hio kabla ya Mtu yeyote yule, kwani huenda tukauteka Mji huo kabla ya kuwasili Jeshi hilo.'**

Hivyo jeshi hilo likaelekea katika ardhi ya Dimashq na kuwasilia katika maeneno ya baina ya Tabuk na Jabiyah na habari za safari yao hio ikamfikia Hirkalius ambae anae akajiandaa na Jeshi lake la Warumi kwa ajili ya kukabiliana na Jeshi hilo. Na Yazid na Rabia Ibn Amir na jeshi la Waislam wengineo pamoja nao wakawasili katika ardhi ya Tabuk kabla ya kuwasili Jeshi la Warumi, na kisha siku ya nne yake wakaelekea kwenye ardhi ya Dimashq. Ambapo Yazid Ibn Abi Sufyan akatoa Khutba ifuatayo kuliambia Jeshi lake ambao lilikua lina Idadi ndogo ya Wapiganaji kuliko Idadi ya Warumi kwa kuwaambia kua:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

‘Enyi Waislam fahamuni kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* amekuahidini Ushindi, kwani amekuungeni mkono kwa Malaika kwa uwezo wake:

﴿قَالَ ٱلَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلاَقُواْ ٱللَّهِ كَم مِّن فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ ٱللَّهِ وَٱللَّهُ مَعَ ٱلصَّابِرِينَ﴾

Qala alladheena yadhunnoona annahum mulaqoo Allahi kam min fi-atin qaleelatin ghalabat fi-atan katheeratan bi-idhni Allahi waAllahu maAAa alssabireena *(Surat Al Baqara 2:249)’*

Tafsir: ***‘Wakasema wale ambao ni wenye uhakika kua watakutana na Allah Subhanah wa Ta’ala : ‘Jee ni mara ngapi wale waliokua Kidogo wamewashinda waliokua wengi kwa Idhini ya Allah, na Allah ni mwenye kua pamoja na wenye Subra’’***

Hivyo nyinyi ni watu wa Mwanzo kuingia katika Mji wa Dimashq na kupigana na watu wako.

Na mara wakatokea Warumi mbele yao, ambao waliopouona udogo wa kiidadi wa Waislam bais wakaambiana kwa kusema: ‘Wacha tupigane na hawa Waislam wanaotaka kuchukua Ardhi yetu’ na hivyo wakawavamia Waislam hao, lakini Warumi hao wakakutana na upinzani mkubwa sana wa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.

Kwani Waislam waliokua wakiongozwa na Rabia Ibn Amir walivamia kwa *Takbir, Tahlil, Salat* Nabii kutoka ndani ya Nyoyo zao, na hivyo Warumi wakashangazwa na Ujasiri wa Waislam hao, *Allah Subhanah wa Ta’ala* akaingiza khofu ndani ya nyoyo za Warumi na wakaanza kuzidiwa huku Rabi Ibn Amr akizidi kuwatia ari Waislam kwa maneno na kwa kupigana na maadui zake kwa nguvu zaidi, baada ya kuona hali hii basi Warumi wakaanza kukimbia ovyo kutoka katika uwanja wa Vita na hivyo kwa siku hio Waislam wakaibuka na ushindi.’

Imam Al Waqidh anaendelea kusema kua: **‘Saad Ibn Aws pia analielezea tukio hili la makabiliano baina ya Waislam na Warumi katika ardhi ya Tabuk kwa kusema kua: ‘Jeshi lililokua chini ya usimamizi wa Yazid Ibn Abu Sufyan na Rabia Ibn Amr lilipokutana na Warumi katika maeneo ya Tabuk, basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* aliwapa ushindi Waislam, ambapo Waislam 120 walipata Ushahidi na Warumi 1200 waliuliwa, na baada ya Warumi kushindwa basi Kiongozi wao**

akasema: ‘Ole wenu, Jee nyinyi mtauweka wapi uso wenu mbele ya Hiraklius? Waislam wametudhalilisha sana, kwani kila sehemu imejaa miili ya maiti wetu.’

Baada ya kusema hayo basi Warumi wakakusanyika nje na kisha wakamtuma mmoja kati ya Waarabu kua muwakilishi wao kwa kumwambia: ‘Nenda kawaambie Waislam kua watutumie mmoja kati ya Kiongozi wao, ili tuzungumze nao kuhusiana na nini wanachokitaka kutoka kwetu.’ Hivyo Muarabu huyo akapanda Farasi wake na kuelekea kwa Waislam’ ambapo nao wakamuuliza anachokitaka nae akajibu: ‘Kiongozi wetu anataka kuzungumza nanyi kwa ajli ya usuluhishi.’’

Hivyo Waislam wakamwambia Yazid kuhusiana na maombi hayo, na Rabi akasema: ‘Wacha Mimi niende nikazungumze’ lakini Yazi akasema: ‘Ewe Yazid hakika mimi nna khofu kua huenda wakakudhuru kwa sababu Jana uliwaulia Kiongozi wao.’ Hivyo Rabi akasema: ‘Usiwe na Khofu kwani hakuna kitakachtufika isipokua kile ambacho *Allah Subhanah wa Ta’ala* ametuandikia kitufike, kwani yeye ndie msimamizi wetu, hivyo Waumini wanatakiwa wawe ni wenye kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta’ala* kama alivyosema katika Qur’an kua’

﴿قُل لَّن يُصِيبَنَآ إِلاَّ مَا كَتَبَ ٱللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلاَنَا وَعَلَى ٱللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ ٱلْمُؤْمِنُونَ﴾

Qul lan yuseebana illa ma kataba Allahu lana huwa mawlana waAAala Allahi falyatawakkali almu/minoona *(Surat At Tawba 9:51)*

Tafsir: ***Sema Hakitotufika kitu isipokua kile alichokiandika Allah Juu yetu, kwani yeye ni ndie Msimamizi wetu na kwake yeye Allah ndio wanakokutegemea Waliamini.***

Rabia akaendelea kusema kua: ‘Hivyo nifuatilieni kwa umakini ili muweze kinisaidia kama mkiwaona wanaenda kinyume na maneno yao basi mtawashambulia.’ Na kisha akapanda Farasi wake na kuelekea kwa Warumi.
Na alipofika mbele ya la Jeshi Warumi basi Warumi wakasema kumwambia kua: ‘Shuka kutoka juu ya Farasi wako, kuonesha heshima kwa Jeshi la Mfalme’ ambapo Rabia akasema: ‘Haiwezekani kwangu kushuka kutoka katika hali ya kua ni mwenye kuheshimika na kuingia katika hali ya kua ni mwenye kudharaulika, na wala sitompa Farasi wangu mtu yeyote miongoni mwenu na sitosogea zaidi za kwenye Mlango wa Hema la kiongozi wenu, vyenginevyo basi mimi nitarudi kwani ni nyinyi ndio mliotuita sisi.’

Hivyo Mjumbe wa Warumi akafikisha ujumbe huo, na hivyo Warumi wakakubaliana na msimamo wake huo, na hivyo Rabia akasogea na Farasi wake hadi kwenye Hema la kiongozi wa Warumi na kisha akashuka kwenye Farasi wake, huku akiwa na silaha zake na mara akaja kiongozi wa Warumi aitwae Jurjis huku akiwa ameongozana na Kasisi wao, basi Jurjis akasema kumwambia Kasisi huyo: 'Muulize kuhusiana na Dini yao'

Hivyo Kasisi huyo akasema: **'Ewe ndugu yangu wa Kiarabu, kualingana na tunavyojua sisi basi ni kua Allah atamtuma Mtume katika Ukoo wa Banu Hashim katika Kabila la Quraysh katika Ardhi ya Hijaz, na kuja na dalili ya Miujiza ya kupandishwa Mbinguni katika wakati wa Usiku, hivyo jee tukio hilo limetokea ama la?'**

Ambapo Rabia akasema: 'Naam, hili limeshatokea kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amelithibitisha hilo kwenye Qur'an Karim pale aliposema:

﴿سُبْحَانَ ٱلَّذِى أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِ لَيْلاً مِّنَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ إِلَىٰ ٱلْمَسْجِدِ ٱلأَقْصَى
ٱلَّذِى بَارَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَآ إِنَّهُ هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلبَصِيرُ﴾

Subhana alladhee asra biAAabdihi laylan mina almasjidi alharami ila almasjidi al-aqsa alladhee barakna hawlahu linuriyahu min ayatina innahu huwa alssameeAAu albaseeru*(Surat Al Israa 17:1)*

Tafsir: ***Utukufu ni wake yule ambae amemsafirisha Usiku Mja wake katika Usiku kutoka katika Masjid Al Haram kueleka katika Masjid Al Aqsa ambao ameyabariki maeneo yake kwa ajili ya kumuonesha Dalili zetu, kwani kwa hakika yeye ni mwingi wa kusikia na ni mwenye kuona juu ya kila kitu.***

Hivyo Kasisi huyo akasema: 'Katika Maandiko yetu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemfardhisha Mtume wenu na Umma wake kua wafunge Mwezi wa Ramadhani' Rabia akasema: 'Naam, kama ilivyoelezewa kwenye aya ifuatayo ya Qur'an pale aliposema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:'

﴿شَهْرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيَ أُنْزِلَ فِيهِ ٱلْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ ٱلْهُدَىٰ
وَٱلْفُرْقَانِ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ وَمَن كَانَ مَرِيضاً أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلْيُسْرَ وَلاَ يُرِيدُ بِكُمُ ٱلْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُواْ ٱلْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُواْ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَاكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

Shahru ramadana alladhee onzila feehi alqur-anu hudan lilnnasi wabayyinatin mina alhuda waalfurqani faman shahida minkumu alshshahra falyasumhu waman kana mareedhan aw AAala safarin faAAiddatun min ayyamin okhara yureedu Allahu bikumu alyusra wala yureedu bikumu alAAusra walitukmiloo alAAiddata walitukabbiroo Allaha AAala ma hadakum walaAAallakum tashkuroona *(Surat Al Baqara 2:185)*

Tafsir: ***mwezi wa Ramadhani ndio mwezi ambao imeshushwa ndani yake Qur'an, kua ni muongozo kwa ajili ya Watu na kuwabainishia njia ya uongofu na kigezo cha kubainisha baina ya Baya na Ovu, hivyo yeyote yule atakaeushuhudia Mwezi wa Ramadhani basi na afunge Mwezi huo, na kama atakua ni mwenye kuumwa au ni mwenye kua safarini basi na alipe idadi ya siku hizo katika siku nyengine, kwani Allah ni mwenye kuwatakia Wepesi na wala hakutakieni ugumu. Na mumtukuze Allah kwa kukuongozeni ili mpate kua ni wenye shukurani.***

Kasisi huyo akasema: 'Katika maandiko yetu inaonesha kua: 'Yeyote yule atakaefanya Jema moja basi ataandikiwa mara 10 zaidi yake kimalipo' Rabia akasema; 'Naam, yamesemwa hayo katika Qur'an tukufu pia kua:

﴿مَن جَآءَ بِٱلْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا وَمَن جَآءَ بِٱلسَّيِّئَةِ فَلاَ يُجْزَىَ إِلاَّ مِثْلَهَا وَهُمْ لاَ يُظْلَمُونَ﴾

Man jaa bialhasanati falahu AAashru amthaliha waman jaa bialssayyi-ati fala yujza illa mithlaha wahum la yudhlamoona *(Surat Al Anaam 6:160)*

Tafsir: ***Yeyote yule atakaekuja na Jema moja basi kwa ajili yake ni kumi mithili yake, na atakaekuja na Ovu Moja basi atalipwa mithili yake na wala hatodhulumiwa.***

Kasisi huyo akasema: **'Katika maandiko yetu basi ni kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawaamrisha watu wamsalie *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, jee hilo ni kweli?'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Rabi akasema: ‘Naam hio pia imeamrishwa kwenye Qur’an Karim pale ilipoamrisha kwa kusema:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلاَئِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِيِّ يٰأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ صَلُّواْ عَلَيْهِ وَسَلِّمُواْ تَسْلِيماً﴾

Inna Allaha wamala-ikatahu yusalloona AAala alnnabiyyi ya ayyuha alladheena amanoo salloo AAalayhi wasallimoo tasleeman *(Surat Al Ahzab 33:56)*

Tafsir: ***Hakika Allah na Malaika wake wanamsalia Nabii (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) hivyo enyi mlioamini nanyie pia Muombeeni na Msalimieni kwa Kiislam.***

Ambapo majibu haya yalimshangaza sana Kasisi huyo na hivyo akasema kuwaambia wenzake: ‘Hawa watu wako kwenye Upande uliokua Sahih’ ambapo mmoja kati ya waliokuwepo hapo akasema kumwambia Kasisi huyo kua: ‘Huyu ndio yule aliemuua Kaka yako’ na hivyo Warumi hao wakamvamia Rabia.

Wakati Warumi hao wanamvamia Rabia basi Yazid Ibn Abi Sufyan akaona tukio hilo na hivyo nae akawavamia Warumi hao na Jeshi lake, na hapo mapigano makubwa sana yakaendelea, hadi mwishoni Waislam wakaibuka na tena ushindi na kuteka Mateka na kupata Ngawira ambazo walizituma katika Mji wa Madina pamoja na Jeshi la watu 500. Ambapo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alipoiona hali hio basi alisjudu kwa ajili ya kumshukuru *Allah Subhanah wa Taa’ala.*

Katika kuangalia mfano wa tukio jengine ambalo Imam Al Waqidh analielezea kama alivyoelezea mengine yote kwa kina basi na tuangalie ule mfano wa Barua iliyoandikwa na Abu Bakr kwa ajili ya Watu wa Makkah kwa kusema:
Abu Bakr aliwaandikia watu wa Makkah wajikusanye kwa ajili ya kujiunga na Jeshi la kupigania Dini ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kama ifuatavyo:

Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahim.

Kutoka kwa Abu Bakr.

Kuelekea kwa Watu wa Makkah na Waislam wengine.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Namtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae hana mshirika, na kumtumia Sala na Salamu kwa Mtume wake Muhammad *Rasul Allah Salallahu A'alayhi wa Salam.*

Ama baada ya hayo basi nawaita Waislam kwa ajili ya *Jihad Fi Sabili Allah* kwa ajili ya kuiteka ardhi ya Dimashq, nakualikeni nyinyi na Waislam wengine juu ya kile ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekiamrisha pale aliposema katika Surat At Tawba kua:

﴿ٱنْفِرُواْ خِفَافاً وَثِقَالاً وَجَاهِدُواْ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ﴾

Infiroo khifafan wadhiqalan wajahidoo bi-amwalikum waanfusikum fee sabeeli Allahi dhalikum khayrun lakum in kuntum taAAlamoona *(Surat At Tawba 9:41)*

Tafsir: **Kimbilieni iwe mna uhafifu au uzito, na piganeni Jihadi kwa Mali zenu na Nafsi zenu kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwani kufanya hivyo ni kheri kwenu kama mngekua mnajua.**

Ambapo nyinyi ndio watu wa kwanza kushikamana na aya hii na maamrisho yake, na nyinyi ndio mnaostahiki kutii maamrisho ya aya hii kutokana na mshikamano huo, na yeyote yule atakaemsaidia *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Dini yake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamsaidia Mtu huyo, na yeyote yule atakaekua mbakhili katika hili basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hahitaji chochote kutoka kwake Mtu huyo. Hivyo enyi watu wa Makkah kimbilieni Pepo ambayo ni:

﴿قُطُوفُهَا دَانِيَةٌ﴾

Qutoofuha daniyatun *(Surat Al Haqaat 69:23)*

Tafsir: ***Matunda yake yako Chini sana katika kuchumwa kwake.***

Allah Subhanah wa Ta'ala amewatayarisha kwa ajili yake Muhajirina na Ansari, hivyo yeyote yule atakaefuata Njia zao basi atakua ni miongoni mwa waliochaguliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*, kwani yeye ni mwenye kusema:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

﴿وَلاَ تُؤْمِنُوٓاْ إِلاَّ لِمَنْ تَبِعَ دِينَكُمْ قُلْ إِنَّ ٱلْهُدَىٰ هُدَى ٱللَّهِ أَنْ يُؤْتَىَ أَحَدٌ مِّثْلَ مَآ أُوتِيتُمْ أَوْ يُحَآجُّوكُمْ عِندَ رَبِّكُمْ قُلْ إِنَّ ٱلْفَضْلَ بِيَدِ ٱللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَآءُ وَٱللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ﴾

Wala tu/minoo illa liman tabiAAa deenakum qul inna alhuda huda Allahi an yu/ta ahadun mithla ma ooteetum aw yuhajjookum AAinda rabbikum qul inna alfadhla biyadi Allahi yu/teehi man yashao waAllahu wasiAAun AAaleemun *(Surat Al Imran 3:73)*

Tafsir: ***Na Msimuamini yeyote isipokua yule ambae ni mwenye kuifuata Dini yenu. Sema: 'Hakika ya uongofu ni uongofu wa Allah' ambao aliepewa amepewa kama uliopewa wewe au watabishana na wewe mbele ya Mola wao? Sema: 'Fadhila zote ziko ndani ya Umiliki wa Allah, humpa amtakae na Allah ni mwenye kuwatosheleza Waja wake na ni mwenye kujua juu ya kila kitu.'***

Kisha Abubakr *Radhi Allahu Anhu* akaifunga barua hio na kumpa Abd Allah Ibn Hudhayfah *Radhi Allahu Anhu*, na Abd Allah Ibn Hudhayfah *Radhi Allahu Anhu* alipoipata akaipokea na kuondoka kuelekea kwenye Mji wa Makkah kwa ajili ya kuikabidhi, ambapo alipofika basi akawaita watu wa Makkah mbele yake, na walipokusanyika akawakabidhi Barua yao kutoka kwa Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu.*

Barua hio ikasomwa na kisha baada ya kusomwa basi Sahl Ibn Amr, Harith Ibn Hisham, Ikrimah Ibn Abi Jahal *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Sisi tumekubaliana na wito huo, na tunathibitisha juu ya tuliyoambiwa' ambapo Ikrimah akasema: 'Bila ya shaka kwani tutakaa hadi lini huku tukiwa ni wenye kuachana na kujitolea mhanga na nafsi zetu? Kila mtu hua ana mwisho wake na walioshinda ndio wameshinda na hivyo hata kama tukiwa tuko nyuma yao, basi tutakutana nao waliotutangulia na kuupata Ushahidi kutokana na Jihad, na hivyo sisi pia tutakua miongoni mwao.' na kisha baada ya hapo Sahl Ibn Amr, Harith Ibn Hisham, Ikrimah Ibn Abi Jahal wakaondoka pamoja na watu wa Banu Mahzum *Radhi Allahu Anhum.*

Na walipofika katika mji wa Madina basi Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akawa anafikiria ni nani miongoni mwao ampe Bendera na kumtanguliza mbele katika Jeshi lake ambapo Sahl Ibn Amr, Harith Ibn Hisham, Ikrimah Ibn Abi Jahal *Radhi*

Allahu Anhum wakasema: 'Shuhudia kua sisi tumejitolea kwa ajili ya _Allah Subhanah wa Ta'ala,_ kwa maana hio basi hatutorudi nyuma kutoka katika mapigano haya'

Na baada ya kuskia maneno yao hayo basi Abu Bakr _Radhi Allahu Anhu_ akaomba Dua kwa kusema: 'Ya Allah, wajaalie wawe bora zaidi ya wanavyotegemea kua' na kisha akamwita Amr Ibn Al Aas _Radhi Allahu Anhu_ na kumwambia: 'Nakupa wewe Mamlaka ya Jeshi la watu wa Makkah, Taif, Banu Kilab na Hawzin kua chini ya uongozi wako, nenda nao hadi katika ardhi ya Sham ukishafika zungumza na Abu Ubaydah Ibn Jarrah ili umsaidie katika mapigano yake na usichukue maamuzi bila ya kushauriana nae, namuomba _Allah Subhanah wa Ta'ala_ akuingizeni katika Rehma zake wewe na Abu Jarrah.' Na kisha akamuusia kuhusiana na Masharti ya Vita na hukmu zake na kisha akamruhusu kuondoka na jeshi lake.

Kisha Abu Bakr _Radhi Allahu Anhu,_ akawakusanya Wapiganaji Mahiri zaidi waliopigana katika vita mbali mbali pamoja na _Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam_ na kisha akamwita Khalid Ibn Walid _Radhi Allahu Anhu_ na kumwambia: 'Nakukabidhi Mamlaka ya uongozi juu ya Jeshi lililo na wapiganaji mahiri zaid, hivyo Ewe Abu Sulayman nenda nalo jeshi hili katika ardhi ya Iraq na Iran, na namuomba _Allah Subhanah wa Ta'ala_ akusaidieni na akupeni ushindi' na kisha akaagana nalo Jeshi hilo la _Khalid Ibn Walid Radhi Allahu Anhu._

Jeshi la Amr Ibn Al Aas _Radhi Allahu Anhu_ lilipowasili katika ardhi ya Sham basi akawakusanya Muhajir na Ansar na kukaa na kushauriana nao kuhusiana na mapigano hayo. Ambapo akatokea Adi Ibn Amir _Radhi Allahu Anhu_ ambae alikua ni Shujaa miongoni mwa Waislam, na alikua ni mwenye kutembelea sana maeneo ya Dimashq na hivyo ni mwenye kuujua mji huo ndani nje na ni mwenye kuwajua watu wa Dimashq ndani nje.

Na hivyo alipofika mbele yao basi Waislam wakamuweka pembeni ya Amr Al As _Radhi Allahu Anhu_ ambapo nae akamuuliza: 'Jee ni nini kinachoendelea katika Mji wa Dimashq?' ambapo Adiy _Radhi Allahu Anhu_ akasema: 'Wakristo wanakuja na Jeshi lao kubwa sana, wako kama sisimizi wingi wao lakini hawana mpangilio wala mshikamano.'

Amr Ibn Al Aas _Radhi Allahu Anhu_ akasema: 'Hakika sisi tunamuamini _Allah Subhanah wa Ta'ala_ nja tunamumba msaada wake, _La hawla wala Quwwata Illa bi Allah._ Hakika sisi hatuna tofauti baina yetu kwani sisi sote ni sawia, tunamuomba _Allah Subahanh wa Ta'ala_ kwa msaada wake, kwani tunapigana kwa ajili ya Kauli yake na utukufu wake, ambapo yeyote yule anaepigana katika hali kama yetu basi hua ni mwenye kupigania Ushahidi kama akifariki na hua ni mwenye furaha

kubwa sana pale anaposhinda, hivyo sasa hivi nataka kila mtu miongoni mwetu atoe ushauri wake, kuhusiana na nini cha kufanya ili kuwashinda maadui zetu hawa.'

Hivyo kila mmoja akatoa ushauri wake na mmoja kati ya Muhajirina akasema: 'Sisi tulikua tukiyashinda Majeshi yenye idadi kubwa sana wakati sisi tukiwa ni wenye kua na idadi ndogo pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametuahidi kua atatusaidia, kwa kuahidi ushindi na wema kwa wale wenye kua na subra kama alivyosema kwenye Qur'an:

﴿يأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ قَاتِلُواْ ٱلَّذِينَ يَلُونَكُمْ مِّنَ ٱلْكُفَّارِ وَلِيَجِدُواْ فِيكُمْ غِلْظَةً
وَٱعْلَمُوۤاْ أَنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلْمُتَّقِينَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo qatiloo alladheena yaloonakum mina alkuffari walyajidoo feekum ghil*dh*atan waiAAlamoo anna Allaha maAAa almuttaqeen*(Surat At Tawba 9:123)*

Tafsir: ***Enyi mlioamini, Piganeni na wale ambao wako karibu nanyi miongoni mwa Makafiri, na wakutane na Ukali wa Nguvu kutoka kwenu, fahamuni kua Allah Subahanh wa Ta'ala yuko pamoja na wenye Taqwa.***

Hivyo mwishoni Waislam wakaamua kupigana na adui yao kwa nguvu na uwezo wao wote, ambapo Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* akaikabidhi Bendera kwa Abd Allah Ibn Umar Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na kumkabidhi pia Jeshi la watu 1000 kua chini yake ambao miongoni mwao walikuemo wapiganaji shupavu kutoka katika mji wa Taif na kabila la Banu Thaqif, Jeshi hili lilitembea usiku kucha na asubuhi yake wakakutana na alama za miguu za watu wengi sana. Ambazo zilikua zinaelekea upande mmoja ambapo Abd Allah Ibn Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Hizi ni nyayo za Majeshi, na nnafikiria kua zimeachwa na Wapiganaji waliojitolea kwa hiari yao kwa ajii ya kuwaunga mkono Warumi.' Na kisha akasimamisha Jeshi lake ambalo miongoni mwao kuna waliokua wakisema: 'Wach atuwafuate'

Lakini Abd Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akapinga kwa kusema: 'La hakuna hata mmoja anaetakiwa kuwafuata hadi tujue wanaongozwa na nani na wako wangapi.'

Na baada ya kufuatilia na kupatikana majibu ya uchunguzi kua watu hao walikua na idadi ya watu 10,000, basi Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kuwaambia wapiganaji wake kua: 'Kamwe tusiikose nafasi hii ya kupigana nao watu hawa kwani hapa Pepo ipo chini ya vivuli vya Mapanga yetu' na hivyo Waislam hao wakanadia kwa kuitikia '*La Ilaha Illa Allah! Muhammadun Rasul Allah!'* wito ambao uliitikiwa na Milima, Miti, Wanyama na Mawe pia. Na kisha wakaelekea lilikoelekea Jeshi hilo na walipolikaribia wakalivamia.

Ambapo mtu wa kwanza kushambulia alikua ni Ikrimah Ibn Abi Jahal akifuatiwa na Shal Ibn Amr na Dahkak *Radhi Allahu Anhum*. Majeshi mawili hayo yakavamiana ambapo Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* anaielezea hali ilivyokua kwa kusema: 'Katika wakati huo, niliona mmoja kati ya viongozi mashujaa wa Warumi, ambae ni mtu mwenye mwili mkubwa sana ambae alikua akipiga kwa kushambulia kulia na kushoto kwa mapigo ya haraka sana, na alikua ndie kiongozi wao na ndie mboni ya jicho la Warumi na hivyo kua ni mwenye kuwatia sana mori na ari watu wake.'

Hivyo nami nikamshambulia kwa kumrushia Mkuki wangu lakini hata hivyo aliukwepa mkuki huo, hivyo nikamkaribia nikiwa na hamu ya kutaka kumuua na nikaitumia nafasi hio kwa kumjeruhi kwa kumpiga na Upanga wangu, lakini ilikua mashambulizi yangu yalikua si sawa nakupiga Upanga kwenye Jiwe kwani wakati nikimpiga ilikua nikisikia sauti kua kama nnapiga jiwe hadi nikadhania kua Upanga wangu umekatika, lakini mwisho wake Kiongozi woa huyo akaanguka chini ardhini.

Baada ya kuona tukio hili basi Wagiriki wakawa wamejawa na khofu, na Waislam wakaitumia nafasi hio kwa kupigana kwa ari na nguvu zaidi, na kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambapo Dahhak na Harith Ibn Hisham walionesha ujasiri mkubwa sana na Warumi wakatekeza Wapiganaji wengi sana na kushindwa, ambapo baadhi yao wakakimbia na hivyo mapigano hayo yakamalizikia kwa kuwapatia Ushindi Waislam.'

Baada ya Vita basi Waislam waliokua wametawanyika kila sehemu katika Uwanja wa vita, wakarudi katika sehemu moja na kujikusanya huku wakiwa ni wenye kukusanya Ngawira za Vita hivyo, zilizoachwa na Warumi, lakini Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anah*u alikua haonekani. Hivyo Waislam wakaanza kuulizana yuko wapi Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu?*

Hivyo baadhi wakasema kua Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* Yuko kwenye Ibada zake kwani ni Mtu mwenye kupenda kufanya Ibada sana. Na kuna wengine wakasema kua la, kwani kuna mtu alieonekana kwenye Uwanja wa vita akiwa kama Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akipigana kwa ustadi mkubwa sana, na hivyo wakawa wanamsifu sana na mara wakasikia sauti ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* ikisikika miongoni mwao ikinadia kwa kusema

***‘Allahu Akbar wa Alhamd Lillah! Allahuma Ssali aAla Muhamamd wa Alihi Muhamamd!’* Huku Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akiwa amenanyayua Juu bendera na walipomuuliza alikua wapi basi nae akasema kua: ‘Akili yangu yote ilikua kwa yule Kiongozi wa Warumi niliemuua.’**

Hivyo hizo ni baadhi tu ya sehemu ya kurasa ya baadhi ya vitabu vyake Imam Al Waqidhi, ambazo zinadhihirisha kua alikua ni Muandishi Mahiri sana na aliandika vitabu vingi sana na maarufu sana katika Ulimwengu wa Kiislam, ambapo kuna wanaosema kua baada ya kufariki kwawe Imam Al Waqidhi aliwacha Masanduku 600 ya vitabu, ambavyo ndani yake vinajumuisha Vitabu vya Maghazi, Sirra, Hadith, Fiqh na makubaliano na kutokukbaliana kwa Wanazuoni wa Hadith katika Hadith.

Ambapo Khalifa Al Mamum alikua akivipenda sana Vitabu vyake Imam Al Waqidhi na kusema kua: **‘Haijawahi kutokea katika Mji wa Baghdad kua na Vitabu vya Mtu mwengine yeyote yule kama ilivyokua wingi wa vitabu vya Al Waqidhi.’** Imam Al Waqidhi alifariki mnamo mwezi 11 wa Dhulhijja ya Mwaka wa 207 Al Hijra (April 27, 823) na Sala yake ya Jeneza ilisalishwa na Ibn Simaa At Tamimi na alizikwa kwenye Makaburi ya Hayzuran yaliyopo katika maeneo ya Magharibi ya Mji wa Baghdad.

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani kua: ‘**Al Waqidhi ni mwenye kukubalika katika Hadith zake za Mapigano, na hii ni kulingana na mitizamo ya Wenzetu na *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni mwenye kujua zaidi.**’

IMAM MA`RUF AL-KARKHI 132 AH

Imam Asad Al Din Abu Mahfuz Shaykh Ma'ruf Ibn Feruz Al Karkhi ni Imamu wa 9 na Shaykh wa *Silsila Aaliyah Qadiriyah Barakatiyah Razaviyah Nooriyah.* Imam Ma’ruf Al Karkhi alizaliwa mnamo mwaka 132 Al Hijra kwenye Mji wa Karkhi nchini Iraq.

Imam Ma’ruf Al Karkhi alizaliwa katika familia ambayo haikua ni ya wafuasi wa Dini ya Kiislam lakini kutokana na kua ni mwenye kucheza na Watoto wa Kiislam basi alikua akivutiwa sana na Dini ya Kiislam na kuwaambia Wazee wake kua anataka awe Muislam lakini hata hivyo nao wakaamua kumpeleka kwa Kasisi wa Ukristo ili asomee Dini hio, ambapo alipofika tu basi Kasisi huyo akamuuliza Ma’ruf Al Karkhi: ‘**Hivi katika familia yako kuna watu wangapi?**’ Ma’ruf Al Karkhi Akasema: ‘**Kuna Baba yangu Mama yangu na mimi Mwenyewe.**’

Ambapo Kasisi huyo akasema: ‘**Vizuri sana, sasa sema Isa ni Mungu wa Tatu.**’

Hivyo Imam Mar'uf Al Karkhi anasema kua: '**Tangu wakati huo nilipokua si Muislam basi Moyo wangu haukukubali kusema maneno hayo aliyokua akiniamrisha kuyatamka, na nilipogoma kuyatamka basi alinipiga sana, na kila aliyokua akinipiga basi na mimi ndivyo nilivyozidi kutokukubaliana na mafunzo yake, hadi mwisho wake akachoka na kumwambia Baba yangu kua anifungie ndani bora.**

'Hivyo nikafungiwa ndani kwa siku 3, ambapo kila siku nilikua naletewa mkate ambao hata hivyo akuna hata siku moja ambayo ndani yake niliugusa mkate huo, na katika siku ya tatu nilipofungulia basi nikakimbia kutoka nyumbani, na kwa kua nilikua ndio mtoto pekee katika familia yangu basi wazee wangu walikua na huzuni kubwa sana kutokana kukimbia kwangu. Na hivyo wakatuma mjumbe kuniambia kua nirudi nyumbani na nitakua huru kufuata Dini niitakayo na kisha wao pia watafuata Dini ninayoifuata mie'

Na hivyo nikaenda kwa Ali Ibn Musa Al Rida na kusilimu na kua Muislam na baada ya hapo nikaenda Nyumbani na kuwasilimisha wazee wangu.' Hivyo Imam Ma'ruf Al Karkhi akawa anasoma chini ya Ima Ali Ibn Musa Rida na kisha baadae akasoma kwa Imam Daud At Tai na Imam Abu Hanifa.

Imam Mar'uf Al Karkhi alikua ni mtu ambae mwenye kupenda sana kuhuisha usiku wake kwa *Qiyam Layl* mbele ya ukumbi wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Sala, Istghfar, kisomo cha Qur'an na kilio cha machozi, ambapo alisema Imam Abd ul Wahhab kua; '**Hakika mimi sijawahi kumuona mtu alieachana na Dunia yake kama Mar'uf Al Karkhi, kwani Darja yake ni ya juu kiasi ya kua hata Kaburi lake lenye baraka hua ni sehemu ya kujipatia Baraka**'

Imam Sari Saqati alisema kua: **'Kila kitu nilichokifikia mimi ni kutokana na Sadaqa za Mar'uf Al Karkhi**' Imam Sari Saqati anaendelea kusema kua: '**Siku moja mimi nilimuona Mar'uf Al Karkhi akikusanya Tende katika siku ya sikukuu ya Idd, hivyo nikasimama na kumuuliza kwanini anafanya hivyo?**' **ambapo nae akasema kua**: '**Kuna mtoto ambae analia kwa sababu watoto wengine wote wamevaa nguo mpya isipokua yeye hana nguo mpya, hivyo akusanya Tende hizi nikaziuze ili nipate kumnunulia mtoto huyo nguo mpya za sikukuu ili asijisikie mnyonge katika siku ya Idd apate kucheza na wenzake**'

Nami nikasema: 'Haina haja kwako wewe kufanya hivyo wacha mimi nitamnunulia nguo mpya mtoto huyo kwa ajili ya Idd' na kisha nikamchukua mtoto huyo na kuenda nae kumnunulia nguo mpya za Idd na baada ya hapo nikahisi kua kuna Nuru fulani imeingia ndani ya Moyo wangu.

Alisema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: ‘**Watu wa Mji huu watakua wako salama wakati Abu Mahfuz Ma’rfu Al Karkhi anaishi ndani yake pamoja nao.**’

Safari moja ilikua kuna uhaba wa mvua kwa mda mrefu katika ardhi ya Mji Wake, hivyo Imam Ma’ruf Al Karkhi akanyanyua mikono yake juu kumuomba *Allah Subhanah wa Ta’ala* ambapo kabla ya hata hajarudisha chini mikono yake basi Dua hio ikajibiwa na Mvua ikaanza kunyesha.

Imam Mar’uf Al Karkhi alikua ni mtu asiependa kuikumbatia Dunia yake kwani alikua akisema kua: **‘Dunia hii ni sawa na Chungu cha Moto kinachotokota Jikoni, na Uani ambapo hua kunaelekeza njia ya Jikoni huko.’**

Aliulizwa Imam Ma’ruf Al Karkhi: **‘Jee ni nini dawa ya matatizo ya Kidunia?’** nae akajibu**: ‘Kukaa mbali na Viumbe wake na kukaa karibu na Muumbaji wake’**

Na akasema tena kua: **‘Kutafuta Pepo bila ya kuifanyia kazi kwa kufanya Mema hua ni sawa na kufanya Dhambi na kusubiri kufadhiliwa na *Allah Subhanah wa Ta’ala* bila ya kutumia ufahamu wako hua ni sawa na kufanya ulaghai’**

Ingawa Imam Ma’ruf Al Karkhi alikua ni mwenye kupenda sana Ibada ya kufunga lakini safari moja alipokua amefunga basi alipita sokoni na kusikia mtu anaegawa maji huku akisema: ‘**Allah amuingize kwenye Rehma zake anaekunywa Maji haya**’ hivyo baada ya usikia Dua hio, basi Imam Ma’ruf Al Karkhi akamfuata mtu huyo na kumuomba ampe maji hayo anywe, na hivyo akafungua funga yake kwa sababu ya Dua hio.

Siku moja Imam Ma’ruf Al Karkhi aliingia Msikitini na ulipowadia wakati wa Sala basi Imam Ma’ruf Al Karkhi akakimu Sala hio, na kisha akawambia Imam wa Msikiti huo kua asalishe, ambapo nae akasema: ‘**Mimi nikikusalisha wewe kwenye Sala hii basi huenda ikawa sitoweza kusalisha tena**’ ambapo Imam Mar’uf Al Karkhi akajibu: ‘**Yaani wewe unategemea kua utafikia mda wa kusali katika Sala nyengine, hakika sisi hua ni wenye kuomba hifadhi kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* kutokana na kua na mategemeo marefu kama hayo yako wewe, kwa sababu hua yanatuzuia sisi kufanya mema.**’

Imam Mar’uf Al Karkhi alikua kila wakati anapenda awe na udhu wake, kiasi ya kua safari moja alikua anakaribia Mto Tigris kwa hatua kadhaa na udhu ukamtoka, hivyo hapo hapo akatayammam na waliomuona akifanya hivyo basi wakashanagaa na kumuuliza: ‘**Mbona una *Tayamam* wakati Mto Tigris ule pale?’** ambapo nae akasema: **‘Inawezekana ikawa mimi nikafariki kabla ya kuufikia Mto Tigris’**

Imam Mar’uf Al Karkhi aliulizwa: ‘**Jee ni kitu gani kilichokufanya wewe uachane na Dunia na Viumbe wake *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kua ni mwenye kujitenga huku ukimkumbuka *Allah Subhanah Wa Ta’ala* tu, au ni kwa sababu ya khofu ya Kifo na Kaburi? Au ni kwa sababu ya khofu ya Moto? Au ni kwa ajili ya kutaka kuipata Pepo?**’

Imam Mar’uf Al Karkhi akasema: ‘**Enyi Rafiki zangu mnazungumzia kuhusiana na mambo madogo sana yasiyokua na uzito, kwani kama vyote hivyo vingekua na thamani mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala,* basi visingemnyenyekea *Allah Subhanah wa Ta’ala*, kwani mkifikiria kuhusiana na kuupata ukaribu wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi kamwe hutokua ni mwenye kuvifikiria vitu hivyo mlivyo vitaja**.’

Imam Ma’ruf Al Karkhi alikua ni Walii wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* na alikua na Miujiza mingi sana kutokana na Ucha Mungu wake. Safari moja katika ardhi anayoishi kulikua kuna mtu ambae alikamatwa na hivyo akaadhibiwa Adhabu ya Kifo na kunyongwa na Gavana wa Mji huo, na kisha mwili wake ukaachwa hapo hapo kwenye sehemu ya kunyongea ukiwa unaning’inia.

Mara akapita Imam Ma’aruf Al Karkhi na kuona kilichotokea, jamb ambalo lilimhuzuisha sana hivyo akasema: ‘***Ya Arhama Rahimin,* hakika mtu huyu amepata Adhabu yake hapa Duniani kutokana na aliyoyafanya, hivyo ewe Allah kama utamsamehe kulingana na Imani yake basi usamehevu huo hautapunguza kitu kwenye hazina ya Usamehevu wako.**’ Na mara hapo hapo ikasikika sauti ikitangazia kusamehewa kwa Mtu huyo.

Na watu waliposikia sauti hio wakakusanyika na kisha wakauondoa mwili wa maiti huyo wakamkosha na kisha wakamvisha Sanda, wakamsalia na kumzika. Katika usiku huo mmoja kati ya watu wa Mji huo akaota kua umewadia wakati wa siku ya Malipo na watu wakawa wanafufuliwa huku yule alienyingwa na kuzika siku iliyopita akiwa na muonekano wa hali ya kupendeza sana, hivyo akamuuliza mtu huyo imekuaje akawa na hali kama hio ya kupendeza?

Ambapo mtu huyo akajibu: ‘***Allah Subhanah wa Ta’ala* ameikubali Dua ya Ma’ruf Al Karkhi na kunisamehe madhambi yangu**’

Safari nyengine Imam Mar’uf Al Karkhi alionekana amekaa kitako chini akiwa anakula Mkate na pembeni yake kukiwa kuna Mbwa ambae amelala huku akiwa anakula kipande cha Mkate ambacho Imam Ma’ruf Al Karkhi alimrushia, hivyo watu wakamuuliza Imam Ma’ruf Al Karkhi akaulizwa: ‘**Mbona umekaa na kula karibu ya Mbwa?**’

Ambapo Imam Ma’ruf Al Karkhi akaangalia juu na kumuona ndege anaruka angani, hivyo akamuamrisha Ndege huyo ashuke chini kwenye Mkono wake kwa Idhini ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* na ndege huyo akashuka na kutua kwenye mkono wake huku akiwa amejifunika uso wake kwa mbawa zake kutokana kuona haya mbele ya Imam Ma’ruf Al Karkhi, Hivyo Imam Ma’ruf al Karkhi akasema: ‘**Mnaona? Kila kitu hua ni chenye kuona haya kwa yule ambaye ni mwenye kuona haya mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala.*’**

Safari moja pia Imam Ma’ruf Al Karkhi alikua na Wanafunzi wake wakiwa wanapita katika mwambao wa Mto Tigris, mara wakawaona vijana wakiwa wanapiga mziki huku wakiwa wanaimba na kucheza na kuywa Pombe pia, hivyo Wanafunzi wa Imam Mar’uf Al Karkhi wakamuomba Imam Mar’uf Al Karhki awaombee watu hao, ambapo nae akanyanyua mikono juu na kusema:

‘***Ya Allah, Ya Arhama Rahimin* nakuomba kama vile ambavyo ulivyo wajaalia vijana hawa kua ni wenye uhuru na uwezo wa kufanya anasa hapa Duniani basi wajaalie pia Uhuru na uwezo huo pia wa kufanya anasa kesho Akhera**..**Amin’**

Na kila mmoja kati ya Wanafunzi wake wakashangaa sana juu ya uzuri wa maneno ya Dua hio, kisha baada ya hapo Wanafunzi wakataka kuendeleea na safari yao, lakini Imam Ma’ruf Al Karkhi akasema: **‘Subirini muangalie Matokeo yake’** na mara wakawaona vijana hao wakiwa wanapiga chini vinanda vyao, na kumwaga vinjwaji vyao na kumkimbilia Imam Ma’ruf Al Karkhi na kuanza kulia huku wakimuomba Imam Ma’ruf Al Karkhi kua awaombee kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* wasamehewe makosa yao, hivyo nae akawaombea na kisha akawaambia Wanafunzi wake: **‘Jee mmeona matokeo ya niliyoyaomba?’**

Miongoni mwa Wasi wasia wa Imam Ma’ruf Al Karkhi ni:

‘Ulinde Ulimi wako kutokana na kujisifu kama vile ambavyo unaulinda kutokana na kufanya Dhambi.’

‘Yule asiekua Faqir basi hua si mtu wa *Tasawwuf*.’

‘Fumba Macho yako kwa pande zote kama ikiwa kuna kitu mbele yako.’

‘Mapenzi hua hayapatikana kutokana na kusoma na kufanya mazoezi bali kutokana na majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta’ala.*’

‘Utatuzi wa Matatizo na Mitihani hua ni katika kuificha Mitihani yako.’

‘Ingawa mwenye kujua hua hawezi kuidhibiti mipaka yake, bali hua ni mwenye kuzungukwa na miaka hio.’

‘Bila ya kufanya Mema hua ni Dhambi kutegemea Pepo, Bila kusimamia Sunah na kisha kutegemea Uombezi wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hua ni Usaliti na kujisifu bila ya kua na unyenyekevu hua ni kutegemea Rehma za *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua ni Ujinga.’

‘Wale wenye njaa ya kua na utajiri hawatoweza kua na hali ya kukinai.’

‘Pale A*llah Subhanah wa Ta’ala* anapomtakia mema Mja wake basi humfungulia Milango ya kufanya mema.’

‘Funga Macho yako kwa kila kitu na Kamwe usimwangalie mwenzako kwa mtizamo wa nia mbaya.’
‘Unapoachana na Dunia hii, basi achana na kila kitu chake, kwani ukiwa na sehemu ndogo tu ya kitu chake ndani ya Moyo wako, basi hata ndani ya sijda yako hutoweza kukisahau kitu hicho.’

‘Mtu mwenye busara hua ni yule ambae ni mwenye kufanya kitu stahiki katika siku ya mwanzo ambacho hua ni chenye kufanywa na mjinga katika siku ya tatu baada ya mitihani.’

‘Chochote kile kitakachokukuta katika Mithani hua ni bahati yenye mafanikio ya siri ndani yake.’

‘Shirki ya dhahir ni kujidhihirisha kwa maneno na shirk ya siri ni kuwategemea viumbe katika mambo yako.’

‘Unyenyekevu hua ni katika kuwaona wengine kua ni bora zaidi yako, iwe mkubwa au mdogo, iwe Mwanazuoni au Mjinga, iwe Muislam au Kafiri.’

‘Mwenye kufanya Mema kwa nia ya kupata Malipo ya Kiakhera hua ni mfanya biashara, Mwenye kufanya mema kwa Khofu ya Moto hua ni Mtumwa, kama vile Mtumwa anavyokua anakhofia Mijeledi mgongoni mwake na hivyo hua ni mwenye kuendelea kufanya kazi. Na mwenye kufanya mema kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* tu basi hua ni mwenye Hikma na Busara na hua ni mtu huru.’

Ibada yeyote hua haina maana bila ya kua na Imani Thabiti.

Imam Mar’uf Al Karkhi alifariki mnamo mwaka 200 Al Hijra katika siku ya Ijumaa ya mwezi 2 Muharram.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM IBN QASIM

Imam Abu Abd Allah Abd Rahman Ibn Qasim alizaliwa nchini Misri mnamo mwaka 132 Al Hijra na alikua ni Mwanazuoni mwenye Ilm ya Quran, Hadith na Fiqh ya Imam Malik, na alikua akijulikana kwa jina la Imam Ibn Qasim.

Imam Ibn Qasim alikua ni mwenye kufanya Jitihada sana katika kujitafutia Ilm kwani alijaaliwa kua na Mali nyingi ambazo alizitumia zote kwa jili ya kujitafutia Ilm ambayo aliitafuta kwa mda wa miaka 20 na alisoma kwa Wanazuoni wengie sana akiwemo Imam Yazid Ibn Abd Al Malik, Imam Nafi Ibn Abi Nuaym, Imam Bakir Ibn Mudar na wengieno.

Imam Ibn Qasim alikua ni mwenye Ilm kubwa sana kiasi ya kua alikua ni Imam wa Darja ya Pili ya Madhhab ya Imam Malik na hivyo kua Mujtahid wa Madhhab ya Imam Malik na alikua ni mwenye kua Taqwa na Ucha Mungu mkubwa sana, na ni yeye ndie alieyaenezea zaidi Madhhab ya Imam Malik katika maeneo ya ardhi za Magharibi ya nchi ya Misri baada ya kuandika *Kitab Al Mudawwana* ambacho ni chenye kukubalika na kutumika zaidi katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Malik.

Kitab Al Mudawwana ni kitabu ambacho kimetolewa mara kadhaa na kupitiwa na kufafanualiwa mara kadhaa pia na Wanazuoni wakubwa na maarufu akiwemo Imam Ibn Sahnun, Imam Asad Ibn Furut, Imam Abu Fadhl Iyadh Al Yahsabi, Imam Al Ahmad Al Sharani n.k

IMAM ABD RAHMAN IBN MAHDI 135 AH

Imam Abu Said Abd Rahman Ibn Mahdi Ibn Hasan Al Anbari Al Azdi Al Hafidh Al Kabir Imam ul Ilmi alizaliwa mnamo mwaka 135 Al Hijra katika ardhi ya Basra nchini Iraq.

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alikua ni mtu ambae mwenye kuvutiwa na kutafuta Ilm tangu alipokua mtoto mdogo kwani alianza kutafuta Ilm wakati akiwa na umri wa miaka 10, kwani alisema Imam Abd Rahman Ibn Mahdi kua: '**Ibn Adam ni mwenye kuihitaji Ilm Takatifu kuliko vile anavyohitaji Maji na Chakula chake'** na hivyo Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alikimbilia kusoma kutoka kwa Imam Sufyan Ibn Ath Thawry, Imam Sufyan Ibn Uyaynah,Imam Hamamd Ibn Salamah, Imam Hammad Ibn Zayd,

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Shu'bah, Imam Ayman Ibn Nabil, Imam Umar Ibn Abi Zaida, Imam Yunus Ibn Is-haq, Imam Muhammad Idris Al Shafii, na wengineo.

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alikua ni mwenye kupendwa na Walimu wake kutokana na na Ufahamu wake na umakini wake kiasi ya kua anapohudhuria darsa ya Mwalimu husika basi Mwalimu huyo hua ni mwenye kuburudika na kufurahika Moyoni mwake na hivyo furaha hio hua ni yenye kuonekana wazi kwenye uso wa Mwalimu huyo, kwani anasema Imam Ahmad Ibn Sinan kua: '**Abd Rahman Ibn Mahdi alikua n imwenye kua na sifa ya kua na umakini na ukamilifu wa kujua kuhusiana na Ilm ya Hadith na wanukuaji wake, hivyo Hamamd Ibn Zayd alikua kila akimuangalia Abd Rahman Ibn Mahdi akiwa miongoni mwa Wanafunzi waliokaa kwenye Darsa yake basi Uso wake hua ni wenye kuzidi kujawa na Nuru inayovutia'**

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alisoma pia kwa Imam Malik Ibn Anas ambae alikua na ukaribu sana nae, na alimsomesha mambo mengi sana ikiwemo Fiqh, Hadith, Ilm Rijal n.k ambapo anasema Imam Ali Al Madini kua: '**Abd Rahman Ibn Mahdi alikua ni mwenye kuchukua Ilm kutoka kwa Imam Malik ambae nae amechukua kutoka kwa Sulayman Ibn Yasar ambae nae amechukua kautoka kwa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.'***

Na bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimjaalia Abd Rahman Ibn Mahdi kua na ufahamu mzuri sana kwani alikua ni mtu asieandika kwenye kitabu kile anachosomeshwa bali hua ni mwenye kuhifadhi moja kwa moja kama anavyosema Muhamamd Ibn Yahya kua: '**Sijawahi kuona hata siku moja kitabu kwenye mikono ya Abd Rahman Ibn Mahdi.'**

Ambapo anasema Ayyub Ibn Al Mutawakkil kua: **'Kama mtu anataka kutofautisha baina ya Dunia na Dini yake basi na aende kwenye nyumba ya Abd Rahman Ibn Al Mahdi.'**

Kwani kutokana na kua ni mwenye Ilm na ni mwenye kuaminika basi Imam Abd Rahman Ibn Al Mahdi akawa ni mwenye kuwasomesha Maimamu wengineo akiwemo Imam Abd Allah Ibn Al Mubarak, Imam Ibn Rahawayh, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Ali Ibn Al Madini, Imam Ibn Wahab, Ibn Abi Shaibah, Imam Ahmad Ibn Sinan, Imam Harun Ibn Sulaiman na wengineo.

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alikua ni Mcha Mungu sana na ni mwenye kupenda kuhuisha Usiku wake kama anavyosema Imam Ali Al Madini kua: '**Kama ni kawaida ya Uradi wake Abd Rahman Ibn Mahdi aikua akisoma nusu Msahafu katika kila sehemu ya Usiku.**'

Kutokana na ucha Mungu wake basi Imam Abd Rahman alikua ni mtu ambae anapokutana na mtu basi hua ni mwenye kua na hali zifuatazo: **‘Kama mtu huyo akiwa ni alie juu zaidi yake Kiilm basi alikua ni mwenye kujikusanyia Ilm kutoka kwa mtu huyo, na anapokua anakutana na mtu ambae yuko sawa nae kiilm basi alikua ni mwenye kumueleimisha mtu huyo na yeye ni mwenye kutaka kuelimishwa nae mtu huyo, na anapokutana na mtu ambae yuko chini zaidi yake kiilm basi alikua ni mwenye kumnyenyekea ili aweze kumsomesha mtu huyo.’**

Kwani anasema Imam Abu Is-haq Ash Shirazi kua: ‘**Imam Muhamamd Idris Al Shafii aliiandika Al Risala kwa ajili ya Imam Abd Rahman Ibn Mahdi, kwani Abd Rahman Ibn Mahdi pamoja na Ahmad Ibn Hanbal walikua wakisoma kwa Imam Muhamamd Idris Al Shafii ambapo Imam Al Shafii alikua baadae akiwaambia wote wawili hao kua: ‘Niambieni mimi pia kuhusiana na hadith nilizonazo zipi ziko Sahih ili nizifuate kwa sababu nyinyi mnajua zaidi kuhusiana na Ilm ya Hadith kuliko mimi’ kwani Imam Malik alimpa Imam Muhamamd Idris Al Shafii hadith** ***Mursal*** **kutoka kwa Abd Allah Ibn Masud** ***Radhi Allahu Anhu*** **hivyo Imam Al Shafii akazipitia tena Hadith hizo kutoka kwa Abd Rahman Ibn Mahdi.’**

Ambapo amesema Imam Ahmad Ibn Sinan kua: **‘Ilikua katika Darsa yake Abd Rahman Ibn Mahdi hakuna anaezungumza, anaechonga penseli yake, wala hakuna aliekua akitabasam, na wala ilikua hakuna anaesimama, hali ilikua kama vila Wanafunzi wake wapo katika Sala au kama wamewekewa ndege juu ya vichwa vyao huku wakitakiwa kua ndege hao wasiruke na akiona mmoja kati ya Wanafunzi wake anazungumza au anatabasamu basi hua ni mwenye kukatisha Darsa kwa siku hio na kutoka nje.’**

Ambapo alisema Ubaid Allah Ibn Said kua: **‘Mimi nimemsikia Abd Rahman Ibn Mahdi akisema kua: ‘Mtu hawezi kua Mwanahadith hadi pale atakapoweza kutofautisha kile kilicho sahih na kila kisicho sahih.’ Na akasema tena kua: ‘Hakika mimi siwachi kunukuu Hadith kutoka kwa Mtu hadi pale ninapokua nimemuombea Dua na kumtaja jina lake.’’**

Imam Nu'aim Ibn Hammad alisema kua: ‘**Mimi nilimuuliza Abd Rahman Ibn Mahdi kwa kusema: ‘Hivi Jee wewe hua unajuaje kuhusiana na waongo katika Hadith?’ ambapo nae akasema: ‘Hua nnajua kama vile Daktari anavyojua kua mgonjwa wake ni Mwendawazimu.’’**

Ambapo amaesema Imam Muhamamd Idris Al Shafii kuhusiana nae kua: ‘**Hakika mimi sijawahi kukutana na mtu yeyote anaefanana na Abd Rahman Ibn Mahdi katika fani hii ya Ilm ya Hadith**’

Imam Ahmad Ibn Hanbal akasema: ‘**Imekua kama kwamba Ibn Mahdi ameumbwa kwa ajili ya Hadith.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ali Al Madini amesema kua: '**Ilm ya Abd Rahman Ibn Al Mahdi kwenye Hadithi ilikua ni kama Uchawi'** na akasema tena Imam Ali Al Madini kua: **'Hakuna mtu Mcha Mungu nnaemjua miongoni mwa Wanazuoni wa Hadith kama Abd Rahman Ibn Mahdi.'**

Ibn Al Lubbad alisema kua: **'Abd Rahman Ibn Mahdi alikua akiuza Mapambo ya Dhahabu.'**

Na alisema pia Imam Ali Al Madini kua: **'Kama ingekua natakiwa nile kiapo baina ya Pembe ya Yemen ya Al Kaabah na Maqam Ibrahim, basi ningekula kiapo na kuthibitisha kua hakuna mtu zaidi nnaemjua ambae ana ilm kubwa sana kama Abd Rahman Ibn Mahdi.'**

Imam Ahamd Ibn Hanbal amesema kua: '**Abd Rahman Ibn Mahdi alikuja kwetu sisi Mjini Baghdad wakati akiwa na umri wa miaka 46 au 45 na alikua ni mwenye kupaka hina Nywele zake.'**

Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema: '**Kama ingekua kuna tofauti baina ya Waqii na Abd Rahman Ibn Mahdi basi Abd Rahman angekua yuko juu zaidi kiwakati kutokana na kua yuko karibu zaidi na Qur'an, ambapo wawili hawa wametofautiana kuhusiana na Hadith takriban 50 ambazo ni za kutoka kwa Sufyan Ath Thawry nasi tulipozipitia tukagundua kua Abd Rahman Ibn Mahdi alikua yuko Sahih.'**

Imam Muhammad Muhammad Ibn Al Muqaddami alisema kua: '**Sijawahi kuona mtu ambae ni mwenye ufahamu mkubwa wa kuhifadhi kuhusiana na kile kilichonukuliwa na kisichokua kimenukuliwa katika Hadith kama Abd Rahman Ibn Mahdi'**

Ambapo Ibrahim Ibn Ziyad Sabalan alisema kua: **'Siku moja mimi nilimuuliza Abd Rahman Ibn Mahdi, : 'Hivi jee wewe unaonaje kuhusiana na mtizamo wa kua Qur'an kua imeumbwa?' nae akasema: 'Kama ningekua nnao uwezo, ningesimama kwenye Daraja na kisha nikawa ni mwenye kumzuia kila anaepita na kumuuliza, na kama akijibu kua Qur'an ni Kiumbe na sio *Kalamu Allah* basi ningemkata Shingo yake na kisha kumrembea kwenye Maji mtoni''**

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alisema: '**Yeyote yule atakaesoma Lugha ya Kiarabu basi mwisho wake atakua ni Muandishi, atakaetafuta Ilm ya Mashairi basi atakua ni mwenye kusifia na kutoa kasoro kulikojaa uongo, atakaefuatilia *Ilm Al Kallam* basi atapotoka na atakaefuatilia Ilm ya Hadith na kuifanyia kazi basi mwisho wake atakua ni Imam.**'

Na anasema Imam Abu Hatim kua: '**Abd Rahman Ibn Mahdi ni mtu mwenye kuaminika na ni Mcha mungu wa maneno na vitendo, wakati Sufyan Ath Thawry alipokua anataka kufariki basi alimwambia Hamid ambae ni mfanyakazi wake kua: 'Nenda kwa Abd Rahman Ibn Mahdi mwambie kua nataka aje hapa kwangu kwa ajili ya kunifunga Macho yangu baada ya kufariki kwangu, na Vitabu vyangu viko katika mji wa Kufah kwa Mzee fulani hivyo nataka ukivipata basi vichukue kisha mpe Abd Rahman Ibn Mahdi.**''

Anasema Imam Ali Ibn Madini kua: '**Nilienda mimi kwenye mji wa Kufah kwa ajili kukusanya Hadith za Al Amash na nikazikusanya, kisha nikaelekea Basra na nikakutana na Abd Rahman Ibn Mahdi na kusalimiana nae ambapo nae akaniambia: 'Nipe kile ulichokua nacho' nami nikasema: 'Hakuna mtu yeyote yule alieniambia mimi Hadith yeyote kutoka kwa Al Amash.''**

Ambapo ane akakasirika na kusema: 'Jee, haya ndio maneno ya watu wenye Umakini kwenye Ilm? Na wenye kuifaham kama wewe wanasema hivi? Jee unayo sehemu yeyote ya kuandikia?' nami nikasema: 'Naam' ambapo nae akasema: 'Andika' nami nikasema: 'Niambie labda itakua nnazohadith ambazo unazo'

Abd Rahman Ibn Mahdi akasema: 'Nitakunukulia zile hadithi ambazo wewe huna hata moja' kisha akaninukulia Hadith 30 ambazo mimi sikua nazo hata moja. Kisha kaniuliza: 'Jee nirudie?' nami nikasema : 'La'

Malik anasema kua: **'Mwaka mmoja Sulayman alikuja kwetu na kutuambia: 'Hebu tupeleke kwa Ibn Mahdi ili tupate kumng'arishia kuhusia na Fiqh ya Ibada ya Hija' kwani Sulayman alikua ni miongoni mwa Watu wanaoijua vizuri sana Fiqh ya Ibada ya Hija'**

Hivyo nasi tukatoka na kuelekea kwa Abd Rahman Ibn Mahdi na tulipofika tukasalimiana nae nakisha tukakaa kitako chini yake nae akasema: 'Mmekuja kufanya nini? inaonekana kua kama kuna kitu mmekifuata, nadhani wewe Sulayman itakua kuna kitu unaka kusema, hivyo hebu sema.'

Sulayman akasema: 'Naam, hebu tuambie kuhusiana na Fiqh ya Ibada ya Hija kwani hakuna alietuambia ju yake'

Abd Rahman Ibn Mahdi akasema: 'Hivi kwani wewe Sulayman unasemaje kuhusiana na mtu ambae ameshafanya Ibada zote za Hija isipokua Tawwaf na kisha akamuingilia mke wake?'
Sulayman akajibu: 'Wataachana walipokutaniana na watakutana walipoachana'
Abd Rahman Ibn Mahdi akasema: ' Jee Wataachana wakati gani na watakutana wakati gani?' Sulayman akakaa kimya, hivyo Abd Rahman Ibn Mahdi akasema:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

'Andikeni' kisha akatunukulia masuali 30 na katika kila suali akatunukulia Hadithi moja au mbili kujibu masuali hayo kisha akasema: 'Nilimuuliza Malik na nilimuuliza Sufyan na Abd Allah Ibn Hasan.'

Kuna mtu alienda kwa Imam Abd Rahman Ibn Mahdi na kusema: '**Ewe Abu Said, unasemaje kuhusiana na Hadith ambayo Al Hasan amesema kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kila atakae cheka kwenye Sala basi anatakiwa akatie Udhu tena na kisha asali tena''**

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi akasema: **'Hadith hii imenukuliwa na Hafsa Bint Sirrin, kutoka kwa Abu Al Aliyya kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam'***

Hivyo mtu huyo akasema: **'Hivi jee wewe unasema juu ya jambo hili'**

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi akasema: **'Hivi jee unapoenda kwa mbadilishaji wa pesa na Dinari zako na kisha nae akakuambia: 'Unanichanganya' si hua unaweza kumwambia: 'Nakuchanganya vipi hebu nifahamishe, sasa hadithi hii imenukuliwa na Hafsa Bint Sirrin tu, ambapo Hisham Ibn Hasan ameisikia kutoka kwake kwani alikua kwenye nyumba yake wakati Al Hasan alipoinukuu, ambapo Al Hasan alisema: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema hivyo'''**

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi akaulizwa: **'Hivi jee Az Zuhri yeye ameisikia kutoka wapi?' ambapo Imam Abd Rahman Ibn Mahdi akasema: 'Sulayman Ibn Arqam alikua akipenda kuwatembelea sana Al Hasan na Al Zuhri, hivyo yeye akaisikia kutoka kwa Al Hasan na kisha akainukuu kwa Al Zuhri'**

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alikua akinukuu hadith kutoka kwa wale watu anaowaamini tu, hivyo Yahya Ibn Saidi anasema kua: **'Hakika mimi bora nimsikilize Abd Rahman Ibn Mahdi akiwa anasinzia kuliko kumsikiliza yule anaemnukuu mwengine.'**

Ambapo anasema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: '**Abd Rahman Ibn Mahdi ni mtu mwenye kukuongezea mema katika kila siku utakayokutana nae'**

Imam Abu Dawud alikua ni mwenye kupenda kusema kua: '**Mtu mwenye kuaminika Abd Rahman Ibn Mahdi amesema kua..'**

Al-Qasim Ibn Salam anasema kua : **'Niliingia katika Mji wa Basra mimi kwa ajili ya kusoma kwa Hammad Ibn Zaid lakini nikasikia kua ameshafariki, hivyo nikamlalamikia Abd Rahman Ibn Mahdi ambae aliniambia kua: 'Chochote kile**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ulichonyimwa ni bora kwako kuliko kunyimwa kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

Al Qawariri anasema kua: **'Nilimuona Abd Rahman Ibn Mahdi akiwa juu ya Minbar akitoa khutba huku Baba yake akiwa amekaa sehemu ya Juu zaidi yake na Babu yake amekaa sehemu ya juu zaidi ya baba yake'**

Alisema Abd Rahman Ibn Mahdi kua: **'Kua na wale wenye kubeba Vitabu, kwani wao hua ni sawa na Migodi ambapo wanaoshuka ndani yake basi hutoka na Madini haya au yale ya Dhahabu n.k'**

Alisema Abd Rahman Ibn Mahdi kua: **'Kama ingekua sichukii pale watu wanapomuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi ningependa mimi kubakia ndani ya Mji huu huku nikiwa ni mtu pekee ambae kila mtu anamsengenya ndani yake na kumzulia, kwani hakuna jambo zuri kuliko kufika katika siku ya Malipo huku ukiwa na mambo mema usiyoyajua kufanyiwa lini wala wapi yakiwa yameandikwa ndani ya kitabu chako'**

Aliambiwa Imam Abd Rahman Ibn Mahdi kuhusiana na Ahl Al Bidaa ambapo nae akasema: '***Allah Subhanah wa Ta'ala* anakubali yale aliyaamrisha yafanywe na yale yaliyokuwemo ndani ya Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwani amesema ndani ya Qur'an kua:**

﴿ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلَىٰ آثَارِهِم بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ٱبْنِ مَرْيَمَ وَآتَيْنَاهُ ٱلْإِنجِيلَ وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ ٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُ رَأْفَةً وَرَحْمَةً وَرَهْبَانِيَّةً ٱبتَدَعُوهَا مَا كَتَبْنَاهَا عَلَيْهِمْ إِلاَّ ٱبْتِغَآءَ رِضْوَانِ ٱللَّهِ فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا فَآتَيْنَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ مِنْهُمْ أَجْرَهُمْ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ﴾

Thumma qaffayna AAala atharihim birusulina waqaffayna biAAeesa ibni maryama waataynahu al-injeela wajaAAalna fee quloobi alladheena ittabaAAoohu ra/fatan warahmatan warahbaniyyatan ibtadaAAooha ma katabnaha AAalayhim illa ibtighaa ridwani Allahi fama raAAawha haqqa riAAayatiha faataynа alladheena amanoo minhum ajrahum wakatheerun minhum fasiqoona *(Surat A Hadid 57:27)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: ***Kisha tukawatumia baada yao Mitume wetu, na tukamtuma Isa Ibn Maryam na tukampa Injili, na tukajaalia ndani ya Nyoyo za wale wanaomfuata kua na Rehma na Huruma, lakini Utawa waliouvumbuwa hatukuwaamrisha waufanye, ila wao walifanya kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah na hawakuufanya ulivyokua unatakiwa kufanywa, hivyo tukawapa wale ambao walioamini miongoni mwao malipo yao kamili ila wengi wao ni Wenye kufanya Maovu.***

Hivyo kama unavyoona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakuwakubalia Utawa wao bali amewakemea, hivyo kinachotakiwa ni kushkama na Sunnah.'

Amesema Imam Abd Rahman Ibn Mahdi kuhusiana na hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo : '**Amali hua zinategemeana na Nia, kwani kila mtu atalipwa kutokana na kile alichokitilia nia. Hivyo yeyote yule atakaehama kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake basi amehama kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake, na yeyote yule aliehama kwa ajili ya mafanikio ya kiduni au kwa ajili ya kuoa Mwanamke basi atalipwa kulingana na alichokikusudia katika nia yake'** kua: **'Mtu yeyote yule anaetaka kuandika Kitabu basi anatakiwa aanze kuandika kwa kutumia Hadith hii, kwani mimi kama ningekua nimeandika Kitabu chenye Sura tofauti basi ningeanza na Hadithi hii katika kila Sura.'**

Ambapo Imam Al Shafii amesema kuhusiana na Hadith hii kua: **'Hadithi hii inajumuisha robo tatu ya Ilm na inahusiana na asilimia 70 ya masuala ya Fiqh'**

Na kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal amesema kuhusiana na Hadith hii kua: '**Msingi wa Uislam unasimamia kwenye Hadithi 3 za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*:**

Ya kwanza ni hii ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua: Amali hua zinategemeana na Nia.

Ya pili ni ya Aisha *Radhi Allahu Anha* isemayo kua: Yeyote yule atakaefanya Jambo ambalo halimo katika Maamrisho yetu basi jambo lake hilo liwe ni lenye kukataliwa.

Ya Tatu ni ni ya Numan Ibn Bishr ambayo ni yenye kusema: Halali na Haramu ziko wazi.'

Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alifariki mjini Basra ikatika mwezi wa Jumada al-Akhira wa mwaka 198 akiwa na umri wa miaka 63.

Amesema Imam Ali Ibn Al Madini kua: **'Nilikutana na mke wa Abd Rahman Ibn Mahdi baada ya kufariki kwake nyumbani kwake, na nikaona kua kuna alama nyeusi kwenye upande wa kibla ya Nyumba yake, hivyo nikamuuliza: 'Hii alama**

nyeusi hapa ni ya nini' mke wake akasema: 'Hii ndio sehemu ambaayo aliakua akipumzika Abd Rahman Ibn Mahdi na ndio sehemu ambayo aliyokua akiitumia kwa Qiyam Al Layl na ndio sehemu ambayo huweka paji lake la uso pale anapohisi kusinzia wakati wa usiku'' '

IMAM BISHR AL-HAFI

Imam Bishr Ibn Harithi Ibn Ali Marwazi Abu Nasr Al Hafi alizaliwa katika maeneo ya Marwazi na baadae familia yake ikahamia katika ardhi ya Baghdad, ambapo baadae Imam Bishr Al Hafi akaanza kusoma Ilm ya Hadith kutoka kwa Wanazuoni wa Iraq ingawa pia alikua ni Mwanafunzi wa Mjomba wake ambae alikua ni Mwanazuoni anaejulikana kwa jina la Ali Ibn Khashran, kwani Ali Ibn Khashran alikua ni kaka wa mama yake Imam Bishr Al Hafi.

Ingawa Imam Bishr Al Hafi alikua ni Mwanazuoni mwenye Taqwa sana lakini hata hivyo mwanzoni mwa maisha yake katika kipindi cha Ujana wake alikua ni mtu mwenye kuipenda Dunia yake na siku moja alipokua amelewa alikuta kipande cha Kartasi ardhini ambacho kilikua kimeandikwa *Bismi Allahi AlRahmani AlRahim* na hivyo akainama na kukiokota kipande hicho cha kartasi akakikosha kisha akakitia manukato na kisha kukihifadhi katika sehemu nzuri ili watu wasikikanyage, kama anavyoelezea mwenyewe kwa kusema pale alipoulizwa: '**Safari yako ya Ucha Mungu ilianza anzaje? Kwa sabbu hali imekua kama kwamba Jina lako limekua kama la Mitume miongoni mwa watu**'

Ambapo nae akajibu: '**Ilikua ni kutokana na majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, sijui niseme nini kwani mwanzoni mimi nilikua ni *Ayyar* (Mhuni) na nilikua Kiongozi wa genge langu, ambapo siku moja nilipokua navuka barabara niliona kipande cha kartasi ardhini na hivyo nikakiokota, na kuona kua kimeandikwa *Bismi Allahi AlRahmani AlRahim* hivyo nikakitia mfukoni mwa Suruali yangu, ambapo ndani yake mlikua na Dirham 2, hivyo nikaenda kwenye Duka la manukato na kuzitumia Dirham 2 hizo kwa ajili ya manukato ambayo niliikoshea kartasi hio, na usiku huo nilipolala basi nikaota nnaambiwa kua 'Ewe Bishr, nimekuona kua umelipendezesha Jina langu na hivyo nami nitalipendezesha Jina lako hapa Duniani na kesho Akhera na kama ulivyolitoharisha Jina langu basi nami nitakutoharisha.'**

Imam Bishr Al Hafi alipoamka kutoka usingizini humo na kutafakkar ndoto yake hio basi akaomba msamaha kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuamua kuhamia kwenye

njia iliyonyooka kwa kua ni mwenye kutafuta Ilm, kua na Taqwa na mwenye kulia sana kwa ajili ya makosa yake. Na hivyo alikua kisema kua: ‘**Wenye kumfikiria Allah hua kamwe hawawezi kumuasi**’

Imam Bishr Al Hafi alikua ni Imam mwenye kuachana kabisa na Dunia yake na alikua ni mwenye ucha Mungu mkubwa sana kwani alikua ni mwenye kusema kua: ‘**Az Zuhd ni Mfalme anaeishi ndani ya Moyo ambao hautaki kitu chochote kutokana na Dunia**’ na aliwahi kusema kua: ‘**Yeyote yule anaeipenda Dunia, basi hua si mwenye kukipenda Kifo, na yule asieipenda Dunia hua ni mwenye kukipenda kifo.**’

Imam Bishr Al Hafi alikua si mtu mwenye kupenda umaarufu kiasi ya kua siku moja baada ya sala ya Ijumaa wakati anarudi nyumbani aliamua kukimbia watu na hivyo kupita kwenye bonde la Abu Layth ambapo akakutana na Watoto waliokua wakicheza katika bone hilo, hivyo watoto hao walipomuona Imam Bishr Al Hafi basi wakaanza kunadia: **‘Bishr! Bishr! Bishr! hivyo Imam Bishr Al Hafi akasimama na kujiuliza : ‘Itakuaje hali ya Moyo wangu ukisikia hali ya kushangiliwa kama hivi? Hivyo kwa hakika sitopita tena mimi kwenye bonde hili hadi nitakapokutana na Mola wangu’** na kisha akabadilisha njia moja kwa moja.

Imam Bishr Al Hafi alisema kua: ‘**Njaa huupendezesha Moyo na kudhibiti matamanio na huunda maarifa maalum**’ na akasema kua: ‘**Kamwe hutoweza kuonja Utamu wa Ibada hadi pale utakapojenga ukuta baina ya Nafsi yako na matamanio yako.**’

Kutokana na Ucha Mungu wake basi Imam Bishr Al Hafi alikua ni mwenye kuyasimamia Matamanio yake kisawasawa kwani kila kinachotamaniwa na Moyo wake basi ilikua anakihesabu kuna mtihani kwake kiasi ya kua alikua hasomeshi hata Hadith kutokana na kua a khofu ya Matamanio hayo kama pale alipoulizwa: **‘Kwanini wewe husomeshi Hadithi?**’ ambapo nae akasema: ‘**Natamani kusomesha Hadithi lakini kila kitu kinachotamaniwa na Moyo wangu basi mimi hua ni mwenye kuachana nacho.**’

Imam Bishr Al Hafi anasema kua: ‘**Kwa miaka 50 nimekua nikitamani Nyama ya kuchoma na Mkate laini, lakini sikua ni mwenye uwezo wa kupata hata Dirham moja kwa ajili yake, nami siachani na kitu kutokana na kuvutiwa nacho bali hua nachukia hali ya kua na matamanio nacho**’

Mnamo mwezi wa Ramadhani Imam Bishr Al Hafi aliambiwa: ‘**Mashaa Allah katika mwezi huu wa Ramadhan Alhamd lillah watu wenge wamejipinda kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*'** ambapo ane akajibu: ‘**Hivi ni watu waovu gani hao ambao ni wenye kuzijua haki za *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika mwezi wa**

Ramadhani tu? Mja wa kweli anaezijua haki za Mola wake hua ni yule ambae ni mwenye kujipinda mwaka mzima na wala si katika mwezi wa Ramadhani tu.'

Siku moja Imam Bishr Al Hafi alikua amekaa nyumbani kwao huku akiwa na muonekano wa mtu mgonjwa kwenye uso wake, hivyo dada yake akamuuliza anaumwa ama imekuaje? Imam Bishr Al Hafi akasema: **'Tumbo langu linaniuma'** hivyo Mama yake akasikia kuhusiana na lalamiko hilo na hivyo akamwambia Imam Bishr Al Hafi: **'Nikufanyie Uji, nnao Unga utakusaidia.'** Na hivyo Imam Bishr Al Hafi akasema: '**Hakika mimi nnakhofia kua nitakuja kuulizwa ulipatika wapi unga huo?**' na kisha yeye akaanza kulia na mama yake pia akawa ni mwenye kulia.

Kuna mtu alimuuliza Imam Bishr Al Hafi kwa kumwambia: '**Naomba wasia wako**' ambapo nae akajibu: '**Angalia unakotoka Mkate wako.**'

Imam Bishr Al Hafi aliulizwa: **'Jee ni kitu gani kinalainisha Nyoyo?'** ambapo nae akasoma aya ifuatayo:

﴿ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُم بِذِكْرِ ٱللَّهِ أَلَا بِذِكْرِ ٱللَّهِ تَطْمَئِنُّ ٱلْقُلُوبُ﴾

Alladheena amanoo watatma-innu quloobuhum bidhikri Allahi ala bidhikri Allahi tatma-innu alquloobu *(Surat Ar Rad 13:28)*

Tafsir: ***Wale wenye kuamini (Allah Subhanah wa Ta'ala) na wakapata utulivu wa Nyoyo zao kutokana na Dhikr Allah, kwani kutokana na Dhikr Allah Nyoyo hupata Utulivu.***

Imam Bishr Al Hafi alikua si Mtu mwenye kupenda kuvaa viatu kutokana na unyenyekevu wake na hivyo ilipokua akiulizwa kwanini hapendi kuvaa viatu basi hua ni mwenye kusema: '**Ardhi ni Zulia nami hua naona kua si sahihi kutembea juu ya Zulia hili huku kukiwa kuna kizuizi baina ya nyanyo zangu na Ardhi hii**'.

Alisema Imam Bishr Al Hafi kuhusiana na Zakah ya Hadith kua: **'Kwa kila hadith 200 unazosomesha basi chagua 5 kwa ajili ya kuzifanyia kazi.'**

Na akasema tena kuhusiana na Ilm kua: **'Bila ya kuifanyia kazi Ilm basi hua haina maana na hivyo bora kuachana nayo, kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwafikishia Masahaba zake ambao walishikamana nayo na kuifanyia kazi, na kisha wao wakaifikisha kwa waliofuata baada yao, ambapo sasa hivi Ilm imefika kwa wale ambao ni wenye kuitumia kwa ajili ya kujitafutia riziki yao.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Bishr Al Hafi anaendelea kusema kua: **'Haitakiwi kwa mtu yeyote yule kutumia Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kujipatia mahitaji yake ya kidunia.'**

Na ingawa alikua ni mwenye Ilm kubwa zaidi na ucha Mungu zaidi kuliko Imam Ahmad Ibn Hanbal lakini alikua akiulizwa kuhusiana na suali hilo basi hua ni mwenye kusema: **'Ni nani mimi kulinganisha na Ahmad Ibn Hanbal? hakika yeye ni mwenye Ilm kubwa zaidi.'**

Kwani Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua na ukaribu sana Imam Bishr Al Hafi kiasi ya kua alikua takirban kila siku lazima akutane nae, hivyo Wanafunzi wa Imam Ahmad wakamuuliza siku moja: **'Hakika wewe ni Mwanazuoni ambae uko juu kifiqh, hadith Ijtihad na Ilm nyenginezo, hivyo inakuaje hadi kufikia kua lazima takriban kila siku lazima uende kwa Bishr Al Hafi?' Ambapo Imam Ahmad Ibn Hanbal akasema: 'Inawezekana ikawa mimi nna Ilm ya yote hayo mnayoyasema zaidi yake lakini yeye ni mwenye kujua zaidi kuhusiana na Ilm ya Moyo zaidi yangu.'**

Imam Bishr Al Hafi aliulizwa: **'Imekuaje hadi ukawa na hali ya kuifikia hio Ilm uliyokua nayo?' ambapo nae akasema: 'Kwa kutumia chakula kichache, kwani yule anaekula na kucheka hua si sawa na yule anaekula na kulia.'**

Kutokana na Taqwa yake basi Imam Bishr Al Hafi aliiathiri vizuri sana familia yake kutokana na Ucha Mungu wake, kwani Imam Bishr Al Hafi alikua na Dada zake wawili ambao walikua wakiitwa Zubda na Mudgha.

Ambapo alisema Zubda kua: '**Kitu kizito zaidi kwa Mja mbele ya Mola wake hua ni Dhambi, na kitu chepesi zaidi hua ni Istighfar, hivyo kwanini mtu haachani na kile kilicho kizito kwa ajili ya kilicho chepesi?'**

Siku moja wakati walipokua wako nyumbani basi walitembelewa na Mtumwa wao ambao walikua ni wenye kumuachia huru, lakini alikua anawasikitisha kwa sababu alikua ni mwenye kuiendekeza Dunia yake mbali ya kua ni mwenye kuachiwa huru, hivyo akahoji kwa kusema kua: '**Hivi inakuaje hadi inafikia hali kua wewe huongozeki kumuelekea *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wala wewe Mwenyewe hutafuti njia kumuelekea yeye?'**

Imam Bishr Al Hafi alifariki mnamo mwaka 227 Al Hijra.

Siku moja Mudgha alienda kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal na kumuuliza: '**Sisi ni wenye kufanya kazi ya kusuka na kufuma katika wakati wa usiku, na hivyo baadhi ya wakati hua wanapita wawasha taa wa Banu Tahir (Khalifa wa Baghdad) na hivyo**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

sisi hua tunanufaika nayo Nuru ya mwangaza wa taa za Moto wao hivyo nilikua nataka kujua kuhusiana na kipato chetu ni cha halali ama la?'

Imam Ahmad Ibn Hanbal akashangazwa na suali hilo, linalotokana na Ucha Mungu wa Mwanamke huyo, hivyo akamuuliza: **'Ewe Mja wa Allah unatoka katika nyumba ya familia gani?'** Mukha nae akasema: **'Katika Nyumba ya Bishr Al Hafi mimi ni Mudgha dada yake Bishr Al Hafi**' Imam Ahmad Ibn Hanbal akalia na kusema: '**Nenda zako kwani bila ya shaka kiasi hicho cha Taqwa hua hakipatikani isipokua kwenye Nyumba Bishr Al Hafi.**'

Ambapo anasema Bilal Al Khawwas kua: **'Mimi nililala na nikaota kua nimekutana na Al Khidr na nikamuuliza kuhusiana na Darja baina ya Bishr Al Hafi na Ahmad Ibn Hanbal ambapo nae akasema: 'Alipofariki Bishir Al Hafi basi hakuacha mtu kama yeye badala yake.''**

IMAM ABU SULYAMAN AD DARANI AL ANSI

Imam Abu Sulayman Ad Darani Abd Rahman Ibn Ahmad Al Ansi alifariki na kuzikwa katika mwaka 205 Al Hijra katika ardhi ya Damascus, na ailijipatia Ilm yake kutoka kwa Wanazuoni wengie akiwemo Imam Sufyan Ath Thawry.

Imam Al Darani alikua akijulikana kwa jina la umaarafu la Rayhan al Qulub yaani Mrehani wa Moyo kutokana na kua ni mwenye uwezo mkubwa wa Kiilm wa kuuburudisha Moyo kwa kuusia namna ya kuupa utulivu kwa kuusia kuhusiana na umuhimu wa kua na hali ya matumaini zaid ndani yake juu ya Rehma za Mola wake kuliko kua na Khofu zaidi, na kwa kutumia njia ya ufafanuzi wa umuhimu wa wakati.

Imam Al Darani aliulizwa: **'Ilikuaje hadi wewe ukawa na hali uliyoua nayo?'** ambapo nae akasema: **'Mimi nilikau nikithudhuria Darsa ya mmoja kati ya Maimamu Msikitini, hivyo siku moja Darsa yake ikanigusa sana, lakini hata hivyo nilipotoka nje athari hio ikafutika Moyoni mwangu, hivyo nikarudi tena na kusikiliza tena kwa mara ya pili ambapo nikabakia na athari hio ambayo ilikaa kidogo na kisha ikanitoka tena.**

Hivyonikaenda tena mara nyengine ya tatu na athari ya Mawaidha hayo ikabakia nami hadi Nyumbani kwangu pale nilipoondoka Msikitini na nilipofika Nyumbani nikavunja ala zangu za muziki zote, na kisha nikaanza kufuata njia itakayo nipelekea kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na hivyo Yayha Ibn Muadh aliposikia

kua nimetubu basi akasema kua: 'Ndege mdogo aina ya Kijumba Mshare amemkamata Flamigo.''

Ambapo ndani ya wasia wake hua mna hoja zifuatazo: **'Hakika sisi tupo hapa Duniani kwa ajili ya kutakiwa kumridhisha *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**

'Mtizamo wa Maisha yetu leo hapa Duniani hua unategemeana na matokeo yanayotarajiwa Kesho Akhera.'

'Kile tukifanyacho Hapa Duniani ni kwa ajili ya matayarisho ya Utulivu na starehe ya Milele ya Peponi.'
'Tunasoma Qur'an kwa sababu ya kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kutegemea Rehma zake.'

'Tunasoma Hadith kwa sababu ya kujikumbusha kuhusiana na Roho, Nafsi, kitakachofuatia Kaburini, n,k.'

Imam Abu Sulayman ad Darani alikua ni mwenye ukarimu sana, busara sana na mwenye utaalamu mkubwa wa kuidhibiti Nafsi yake kutokana na matamanio ya Nafsi na kidunia kwa ujumla na alikua si mtu ambae ameoa kwani kutokana na kuhisi uzito wa majukumu yake juu ya nafsi yake basi alikua anahisi uzito kujibebesha kusimamia majukumu ya nafsi nyengine zaidi yake na hivyo alikua akisema kua: **'Yeyote yule mwenye kutamani Watoto hua ni Mjinga, Kwa sababu haiwezekani kuchanganya Dunia na Akhera, kwani kama mtu akitaka kula, kulala au kuingiliana kimwili na Mke wake basi hii huweza kuingilia kati starehe ya Ibada na hivyo huweza kumkosesha umakini juu ya Akhera yake'**

Ambapo anasema Imam Ahmad Al Hawari kua: **'Mimi nilikua naenda kwenye Ibada ya Hija pamoja na Mwalimu wangu Sulayman Ad Darani, nami nikaangusha na kupoteza kibuyu changu cha Maji na hivyo tukawa hatuna maji, nami nikamwambia Mwalimu wangu kua: 'Hatuna Maji hata kidogo'**

Ambapo nae akanyanyua mikono na kusema: 'Ewe Mola wangu hakika wewe ni mwenye kujua yanayoonekana na yasiyoonekana, na niwenye kuyarudisha kwa mwenyewe yaliyopotea na ni mwenye kuwaongoza njia waliopotea, hivyo turudishie tulivyopoteza.' Ambapo mara tu baada ya kumaliza kuomba Dua hio basi akatokea mtu na kuuliza: 'Jee ni nani aliepoteza kibuyu hiki cha Maji?' hivyo tukachukua kibuyu chetu a kuendelea na safari yetu.''

Anasema Imam Abu Sulayman Ad Darani kua: **'Siku moja mimi niliua naomba Dua katika wakati wa usiku, ilikua ni moja kati ya siku zenye Baridi kali sana, hivyo nikatumia mkono wangu mmoja kuuweka kwenye kifua changu huku mwengine**

nikiuelekea juu kwa ajii ya kuomba dua, ambapo mara nikasikia sauti ikisema: 'Ewe Abu Sulayman, hivi jee tumekupa nini kutokana na kuomba Dua kwa kuyanyua mkono mmoja? Kwani kama ungenyanyua na huo Mkono mwengine basi tungeupa nao sehemu yake pia.' Hivyo tangu siku hio basi nikaahidi nafsi yangukua vyovyote vile itakavyokua hata iwe baridi vipi basi kamwe sitoomba Dua wa kunyoosha mkono mmoja tu, bali nitanyanyua mikono yote juu Mbiguni.'

Imam Abu Sulayman Ad Darini anasema pia kua: 'Siku moja nililala na nikaota, nikamuona Hur Al Ayn mmoja mzuri sana, nikamuuliza imekuaje hadi ukawa na Uzuri wa kupita kiasi kama huo?' ambapo nae akanijibu: 'Siku moja wewe Ulikua unalia usiku na hivyo machozi yako yakaangukia kwenye uso wako, kwa uwezo wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* machozi hayo yakawa kiumbe mwenye uzuri wangu kwani kutokana nayo machozi ya Wacha Mungu kama wewe basi yakaunga'risha uso wangu, na kila yakiwa mengi zaidi basi hua ni bora kwangu kwani huunga'risha zaidi uso wangu.'

Aanasema mmoja kati ya Wanafunzi wa Imam Abu Sulayman Ad Darani aitwae Ahmed kua: **'Mimi siku moja nilisali Usiku, na ndani yake Sala hio nikajisikia kua ni mwenye kuonja utamu mkubwa sana wa Ladha ya *Qiyam Layl* hivyo siku ya pili nikamwambia Mwalimu wangu ambapo anae akaniambia kua: 'Ongeza Jitihada ili uweze kua ni mwenye kuipata Ladha hio unapokua pamojana miongoni mwa baadhi ya Watu''**

Aliulizwa Imam Sulayman Ad Darani: **'Hivi jee kuna siri gani ambayo ilikupelekea wewe kua ni mwenye kupendwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala?'*** ambapo nae akasema: **'Ni kutokana na ukweli wa kujua kua Ibn Adam hua huna Malengo yeyote ndani ya Dunia hii na Akhera yake isipokua kupata Ridhaa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Imam Sulayman Ad Darani alisema: '**Hakika mimi nnapenda kula kidogo kutokana na chakula cha halali kuliko Kusali kuanzia asubuhi hadi jioni, kwa sababu Mtu akilia sana basi Moyo wake hua ni wenye kughafilika na Mtu huyo hua ni mwenye kumsahau Mola wake. Hivyo kama ikiwa hali hii humkuta yule mtu ambae amekula chakula kingi cha halali, jee itakuaje kwa yule atakaekula chakula kingi cha Haramu?'**

Usiku mmoja mmoja kati ya Wanafunzi wake Imam Sulayman Ad Darani alilala na kisha akaota kua amemuona Imam Sulayman Ad Darani akiwa ana Mbawa na anaruka huku akisema: **'Alhamd lillah, Ama Sasa hivi mimi niko huru'** hivyo Mwanafunzi huyo baada ya kuamka asubuhi ya siku hio basi moja kwa moja akaenda kwa Imam Sulayman Ad Darani na alipofika na kugonga Malngo basi alipofunguliwa akaambiwa kua Imam Sulayman Ad Darani ameshafariki Dunia.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Katika siku pili baada ya kuzikwa kwake basi Imam Sulayman Ad Darani akamjia tena kwenye Ndoto Mwanafunzi huyo na hivyo Mwanafunzi akamuuliza Imam Ad Darani: **'Vipi Hali yako? *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekupokeaje?' ambapo Imam Sulayman Ad Darani akasema: 'Alhamd lillahi nimeingizwa kwenye Rehma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala*, ila kuonyeshewa vidole kumeniumiza sana.'**

Imam Sulayman Ad Darani alisema: '**Kuudhibiti Ulimi wako Mtu hua ni Ngome Imara sana, Kauli ya Ibada ni Njaa na Kuyapenda yanayokukimbiza katika kumuelekea *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ndio Chanzo cha Maasi yote.**

Imam Sulayman Ad Darani alisema: '**Mja asieijua Nafsi yake hua kamwe hawezi kua Mnyenyekevu. Asiejua kua Dunia haidumu basi kamwe hawezi kua Mcha Mungu.'**

'Kuifikiria Dunia hua ni Uovu, Kuifikiria Akhera hua ni kua na Hikma na Busara na Kuukhuisha Moyo, Ilm hua ni yenye kuongezeka kutokana na Kujifunza na Kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* huzidi kutokana na Kutafakkari'

'Mawazo ya Kidunia yanapohamia ndani ya Moyo basi mawazo ya Akhera hua ni yenye kuhama ndani ya Moyo husika.'

'Jambo jema zaidi hua ni kuenda kinyume na Matamanio ya Nafsi.'

'Wakati Mja anapofanya jambo jema na kisha akajua kua, haiwezekani kwake kua na uwezo wa kufanya jema hilo bila ya Rehma na Neema za *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake, basi hua haiwezekani kwa mja huyo kua ni mwenye kukosa kupenda kumuabudu Mola wake.

'Subra ni moja kati ya Vitu vigumu sana na pia ni moja kati ya Vitu Muhimu na vinavyokubalika sana, ambapo Subira imegawika katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza hua ni Kuachana na aliyotukataza *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ndio yanayopendwa na Nafsi zetu, na sehemu ya pili hua ni kushikamana na Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala ambayo ndio* yanayochukiwa na Nafsi zetu.'

'Pale Mja atakapokua ni mwenye kuona Haya mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi ndio *Allah Subhanah wa Ta'ala* anapokua anamfichia aibu zake na kumsamehe Dhambi zake, na katika siku ya Malipo humrahisishia uzito wa hesabu yake.'
'Kila linaponijia wazo ndani ya Ufahamu wangu basi kwanza hua ni mwenye kulichunguza hivi jee linaendana na Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na

Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama ndio basi nakubaliana nalo kama la basi naachana nalo.'

'Usiwe na ukaribu na mtu ambae hatokunufaisha na Akhera yako'

'Hata kama watu wote watataka kuninyanyasa mimi na kuniweka kwenye hali ya mwisho kabisa ya unyanyaso basi hawatoweza kuninyanyasa kwa sababu mimi ni mwenye kujijua Nafsi yangu kua siwezi kua juu zaidi ya Mtu yeyote kwani niko chini zaidi ya manyanyaso ya watu wote'

'Kuridhika na Rehma na Majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu ya Waja wake ni miongoni mwa sifa za Mitume'

'Kama mtu atakua ni mwenye kuitumikia Dini yake na kuchukua sehemu ya malipo yake kutoka ndani yake basi mtu huyo kamwe hatoweza kuonja Ladha na Manufaa ya Huduma anayoitoa kwa Dini yake'

'Katika Kila jambo kama litakua na Nia na lengo la Mja kumridhisha Mola wake basi hua na Kheri jambo hilo mwisho wake.'

'Kama Mja akimshusha hadi Muumini mwenzake kwenye Macho yake na kujiona kua ana thamani kuliko Muumini huyo mwenzake, basi hata afanye Ibada vipi Mtu huyo Kamwe hatoweza kuonja Ladha ya Utamu wa Ibada zake.'

'Kuna Madhara 6 kwa kila Mtu mwenye kula sana kwa kujaza tumbo lake: Hua haonji Ladha ya Ibada zake; Hua hawezi kuhifadhi kitu ndani ya Ufahamu wake; Hua Hawezi kua na Huruma na Ukarimu kwa viumbe wenzake; Hua ni Mzito katika Kufanya Ibada zake; Hua ni mwenye Matamanio mengi zaidi ya wenzake, Hua kila wakati hukimbilia chooni wanapoenda Msikitini Waislam wenzake.'

'Unapoona kasoro kutoka kwa Muislam Mwenzako basi usimkosoe hapo hapo kwani huenda akawa na tatizo zito na kubwa zaidi analojaribu kulitatua kwa kupitia katika kasoro hizo.'

IMAM AHMAD IBN ASIM AL-ANTAKI

Imam Abu Abd Allah Ahmad Ibn Ismail Ibn Asim Al Antaki alizaliwa katika ardhi ya Mji wa Antakiya na alitokana katika familia ya watu wenye Ilm kubwa sana ya Dini ya Kiislam na hivyo kutokana na jitihada zake basi pia za kutafuta Ilm alikua ni mtu ambae ni mwenye kujipatia Ilm kubwa sana kutoka kwa Wanazuoni tofauti, akiwemo Imam Fudayl Ibn Iyadh, Imam Bishr Al Hafi, Imam Sari As Saqati ambapo Mwalimu wake mkuu alikua ni Imam Abu Sulayman Ad Darani.

Ambapo Imam Abu Sulayman Ad Darani alimpa Imam Ahmad Ibn Asim Al Antaki jina la **'Muwindaji wa Nyoyo'** kwani alikua ni mtu ambae ni mwenye kuzipatia Nyoyo dawa zake kwa kila mwenye maradhi ya Nafsi na Nyoyo. Imam Ahmad Ibn Asim aliwausia wale wenye matatizo ya Nafsi kwa kusema:

'**Enyi Ndugu zangu, fahamuni kua Khofu yenye manufaa zaidi miongoni mwa Khofu ni ile inayowapelekea watu kua mbali na Dhambi, kutokana na vitu visivyopendwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuwafanya kua na huzuni juu ya Akhera yao, kwani ni khofu ambayo inayomfanya mtu kufikira kuhusiana na yatakayofuatia baada ya kuvuta pumzi ya mwisho.**

Ambapo Tamaa yenye manufaa zaidi ni ile tamaa ambayo inayompelekea mtu kua ni mwenye kufanya mema zaidi. Na Jambo la usahihi zaidi ni la kua ni mwenye kua na Uadilifu kwa watu, kwa kutowatakia wengine kile ambacho hakitakiwi na Nafsi yako, na kukubali kauli ya kweli kutoka kwa yule alie chini yako. Kwani Kauli ya ukweli ni kukubaliana na uhalisi wa kua na kasoro ya Nafsi kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'

Haya yenye manufaa zaidi ni ile ambayo ya kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa ajili ya kitu ambacho kinamfurahisha na hivyo kutofanya kile asichokiridhia. Shukran ya bora zaidi ni kumjua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatufichia makosa yetu bila ya kuyadhihirisha kwa yeyote yule katika waja wake.

Mali yenye manufaa zaidi ni ile ambayo ni yenye kuondoa khofu ya Umasikini na kua na umasikini. Aina bora ya Umasikini ni kua na ustahmilivu, kushikamana na malengo na kujitahidi kwa kadri utakavyoweza bila ya kulalamikia hali yako na kuonesha kuridhika na kukinai juu ya kila kitu kinachotoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.'*

Darja ya juu ya ustahmilivu na msimamo hua ni kuachana na uvivu wa kusema nitafanya hiki au kile baadae, pale unapopata bahati ya kufanya jambo husika wakati watu wengine wote wakiwa wameghafilika na Dunia yao na kusahau Akhera yao. Aina bora ya Subra hua ni ya kua na ustahmilivu katika kupigana na Matamanio ya Nafsi yako na kutoonesha aina yeyote ya Kibri au kujiona.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Amali njema zaidi ni ile ambayo inapofanywa hua haisababishi madhara na hua ni yenye kukubaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Heshima bora zaidi na maombi hua ni kufikiria na kuzama kwenye msimamo kwa kina hadi mwisho wa jambo husika. Kwani hii hua inahakikishia kubainisha kwa kina gani jambo husika limefanywa na kwa manufaa gani na kama kunamadhara yeyote, hivyo mtu yeyote atakaefanya hivyo basi hatakua ni mwenye kujilinda Nafsi yake na Dhambi lakini pia atakua ni miongoni mwa wenye kuonewa wivu katika siku ya Malipo.

Tabia bora zaidi ni ile inayoondoa kibri na hasira. Maneno bora za ni yale yanayoendana na ukweli. Maneno yanayodhuru zaidi ni bora yasipozungmzwa. Jambo muhimu zaidi ni kusimamia haki ya fardhi za *Allah Subhanah wa Ta'ala,* haki za Wazee na Watoto na kuwahakikishia maisha yao, kuwasomesha maamrisho ya *Allah Subhanan wa Ta'ala* na kutimiza majukumu ya kuwasimamia. Ilm yenye manufaa ni ile yenye kusaidia kuondoa Ujinga na Uovu, kufahamu ukubwa na uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na hivyo hua ni yenye kufunza kua ni wajibu kumtumikia na kujitayarisha kwa ajili ya Akhera. Jihadi kubwa zaidi ni kupigana dhidi ya Nafsi ili kuzoea kukubaliana na ukweli.

Adui mkubwa zaidi ni yule ulienae karibu nae na ndie wa siri zaidi lakini ni mwenye uadui mkubwa zaid. Adui huyu hua ni mwenye kuamsha ari zaidi kuliko maadui wengine wote dhidi yako. Adui huyu ni Shaytani anaekushughulisha Moyo wako na kukupotosha. Ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee ndie anaemlinda mja kutokana na maovu yake: 'Kuogopa dhambi zako ni jambo ambalo *Allah Subhanah wa Ta'ala* analipenda, na wala si kutoogopa dhambi zako.'

Imam Ahmad Ibn Asim aliulizwa: **'Hivi ni vipi sisi tunaweza kuzipata sifa bora zaid?'** ambapo nae akajibu: **'Kwa anaetaka kua na sifa bora zaidi basi na amuombe *Allah Subhanah wa Ta'ala* ampe ulinzi wa Nafsi yake kutokana na Maovu. Kwani Dhambi kubwa zaidi ni kufanya yale yaliyokatazwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo kusema nitafanya kama ninavyoona Sahih na si kama alivyoamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam na Allah Subhanah wa Ta'ala* ataridhika nami.**

Katika hali kama hii basi ni wajibu kufanya Ibada kama alivyoamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na hili hua ni lenye kuwezekana pale Mtu utakaposoma Uislam, kwani Mtu asiesoma Dini yake kama inavyostahiki basi hua si mwenye kuweza kuepuka kuishi katika dini yake kulingana na Matamanio ya Nafsi yake katika wakati wa kutekeleza majukumu ya Dini yake. Na hivyo mtu hua ni mwenye kubeba mzigo mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'*

Na hivyo Mtu hua anatakiwa aombe msaada kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa ajili ya kujilinda kutokana na matamanio ya Nafsi yake, dhidi ya kutekeleza matamanio yake, na kupigana vita kutokana nayo na kuogopa adhabu zake huku akiwa ni mwenye kumhitaji na kutegemea malipo yake katka kumkumbuka kwake.

IMAM AL SIBAWAYH AL NAHWI 143 A.H

Imam Al Sibawayh Abu Bishr Amr Ibn Uthman Ibn Qanbar alizaliwa mjini Al Baydha ambao upo karibu na Mji wa Shiraz nchini Iran katika mwaka 143 Al Hijra. Ambapo Jina Sibawayh linatokana na neno Sib ambalo hua linamaanisha Tufaha kwa Lugha ya Kiajemi kutokana na kua alipokua mdogo Imam Al Sibawayh alikua na Mashavu Mazuri ambayo yaliyowivia kwa mbali wekundu wa Damu, hivyo Mama yake akawa anamuita Sibawayh kutokana na Mashavu yake kua kama Tufaa Jekundu lililopea na kua na harufu nzuri ya kuvutia.

Imam Al Sibawayh alikua ndio mtu wa kwanza kuitwa kwa jina hilo katika Historia, na bila ya shaka uzuri wake na upekee wake huo ulionekana zaidi alipokua na kua ni mtu wa kwanza katika Historia kua ni Mtaalamu mkubwa sana wa Lugha ya Kiarabu mbali ya kua ni mwenye asili ya Iran kiasi ya kua ikawa anajulikana kwa cheo cha *Hujjat Al Arabi*, na pia kama *Imam Al Nuhaa* na pia *Al Nasr Al Nahwi* yaani Ndege aina ya Tai kwa Nahau, kutokana na kua juu zaidi kwa upande wa Ilm ya Lugha ya Kiarabu, kwani kama ilivyokua Tai Ndie Mfalme wa Anga basi ndivyo alivyokua Imam Al Sibawayh ni Mfalme wa Lugha ya Kiarabu.

Kwani Imam Al Sibawayh aliandika kitabu cha *Al Kitab* - *Qur'an Al Nahwu* ambacho ndani yake kimekusanya mpangilio kamilifu wa Hukmu na Kanuni zote za Lugha ya Kiarabu na hivyo Imam Al Sibawayh kua ni Imam mwenye sifa ya kuilinda na kuihifadhi Lugha ya Kiarabu na kua tegemezi kubwa sana katika kila mtu mwenye kutafuta Ilm ya Lugha ya Kiarabu na pia katika kutafsir Qur'an. Kwani Wanazuoni mabingwa wa Nahw wanasema kua hiki ni kitabu ambacho hakina mpinzani kabla yake wala baada yake.
Ambapo amesema Al-Jahiz kua : '**Watu hawakuandika Kitabu cha Nahw kama alivyoandika yeye, kwani watu wote wanaoandika kuhusiana na Nahau basi ni wenye kumtegemea Sibawayh katika kitabu chake.**'

Na akasema Imam Uthman Ibn Al Mazini kua: '**Yeyote yule anaetaka kuandika Kitabu cha Nahaw kikubwa na bora zaidi ya kitabu cha Al Sibawayh basi anatakiwa ajionee haya Nafsi yake.**'

Ambapo kwa upande wa Abu Al Abbas Al Mubarid amesema kuhusiana na Al Kitab kua: ‘**Yeyote yule atakaekuambia kua anataka kusoma *Kitab Al Sibawayh* basi muulize:** ‘**Hivi Jee wewe umeshawahi kusafiri kwenye Bahari ya kina kirefu?’** kwani *Kitab Al Sibawayh* si kwa ajili ya Mtu mwenye Ufahamu na Moyo mwepesi kwani kama mtu hana umakini basi anaweza kuzama na kupotea ndani yake.

Kabla ya Imam Al Sibawayh kua na Ilm kubwa sana ya Lugha ya Kiarabu, basi alikua ni Ilm ya Qur’an na Hadith, kwani mwanzoni mwa uhai wake alikua na hamu kubwa ya kutaka kua na Utaalamu wa Ilm ya Tarikh na Hadith na hivyo akaamua kuhamia nchini Iraq kwa ajili ya kujiendeleza zaidi na akaanza kwa kusoma kwa Imam Hamamd Ibn Salamah.

Siku moja wakati akiwa anasomeshwa na Imam Hamamd Ibn Salamah basi alikosolewa kutokana na kukosea matamshi ya Kiarabu yaliyomo ndani ya Hadith aliyokua akisomeshwa ambapo ilikua inasema kua ‘**Alishuka *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Ardhi ya Al Safa’** ambapo Imam Al Sibawayh akasema: ‘**Alishuka *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Ardhi ya Al Safa’a**’ hivyo Imam Hamamd Ibn Salammah akasema: ‘**Ewe Sibawayh usiweke hamza mbele ya neno Safa kwani neno hilo halina hamza mwishoni mwake’**

Ambapo kwa upande mwengine basi anasema Al Quffi kua: ‘**Sibawayh alikua ni mtu mwenye ari kubwa na jitihada sana katika kutafuta kwake Ilm, hivyo siku moja wakati anasomeshwa Hadith isemayo: Amesema *Rasul Allah Salallauh Alayhi wa Salam* kua:**

م من أصحابي أحد ألا ولو شئت لأخذت عليه ليس أبا الدرداء

‘Hakuna hata mmoja miongoni mwa Masahaba zangu ambae nisingempendelea kama nigetaka, ila si Abu Ad Darda’

Basi Sibawayh aliporudia maneno hayo kutokana na kujua kanuni ya matumizi ya neno *Laysa* baada ya kusema Abu Ad Darda basi akasema Aba Al Darda. Hivyo Hammad akasema: ‘Nimekwambia ewe Sibawayh kua ni Abu Ad Darda na sio Aba Al Darda. Kwani hii haiwi kama unavyofikiria wewe bali hua ni kutokana na upekee wa mfumo wa kilugha’ Hivyo Sibawayh akasema: ‘Hamna tatizo, basi mimi nitatafuta Ilm ambayo kamwe hakuna atakaeweza kunikosoa.’

Hivyo Imam Al Sibawayh akaanza kutafuta Mwanazuoni wa Ilm ya Lugha ya Kiarabu kwa ajili ya kuisoma kwanza na kuifahama vizuri zaid kabla ya kuendelea na masomo yake, kwani Imam Al Sibawayh alikua ni mwenye kujua kua: ‘**Mtu hawezi kujua**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kuhusiana na kasoro ya Mwalimu wake hadi pale atakapokaa na kusomeshwa na Mwalimu mwengine'

Hivyo Imam Al Sibawayh akakutana na Imam Al Khalil Ibn Ahmad Al Farahidi ambae alikua ni Mwanafunzi wa Imam Abu Al Alaa na akaanza kusoma kwa Imam Al Khalil Lugha ya Kiarabu, Imam Al Khalil ndie alieandika *Kamus Al Ayn* ambayo ni Kamusi ya kwanza ya Lugha ya Kiarabu.

Ambapo Imam Al Khalil ambae ni Mwenye Ilm kubwa ya Tassawuf alikua akimpenda sana Imam Al Sibawayh kutokana na ufahamu wake kwani ilikua akimpa kipaumbele sana Imam Al Sibawayh kila wakati anapokua anasomesha au kila wakati wanapokutana, kiasi ya kua anapotokea imam Al Sibawayh basi Imam Al Khalili hukosa umakini wa mambo mengine na hivyo huacha kila anachofanya kwa ajili ya kumhudumia Imam Al Sibawayh. Ambapo hili ni jambo lililokua pia baadhi ya wakati halifumrahishi Imam Al Sibawayah kwani alikua anajihisi kua anapewa kipaumbele sana na Mwalimu wake ambae pia ni rafiki yake mkubwa kuliko anavyostahiki, kwani yeye ni Mwanafunzi wa Mwalimu wake.

Kwani anasema Imam Marzubani kua: '**Wanafunzi wengi sana walisoma kwa Al Khalil lakini hakuna hata mmoja aliefikia Darja ya Al Sibawayh ambae alikua ni mwenye I'lm kubwa sana baada ya Al Khalili, Sibawayh aliandika kitabu chake ambacho watu walikiita Qur'an ya Nahaw.'**

Imam Al Sibawayh alisoma pia kwa Imam Abū Al Khaṭṭāb ʿAbd Al Ḥamīd Ibn ʿAbd Al Majīd Al Akhashaf ambae nae alikua ni mtaalamu mkubwa wa Lugha pia na mcha Mungu sana, ambapo katika wakati huu ndio Imam Al Sibawayh akaanza kuandika kitabu chake cha Kwanza ambacho kinaitwa Al Kitab ambacho hata hivyo hakukitoa kwa watu.

Kisha baada ya kuhitimu basi Imam Al Sibawayh akaendelea kufanya uchunguzi wake katika Lugha ya Kiarabu kwa mda wa miaka kumi na kitu kwa kutembelea vijijini na majangwani kwa Mabedui na kufanya uchunguzi katika Mashairi yao, Hikaya zao, Historia zao ili kupata vithibitisho vya kila hoja yake ya ufafanuzi wa Nahaw na matumizi yake na kanuni zake katika vitabu vyake baada ya Imam Al Sibawayh kutumia miaka 20 kwa ajili ya kusoma Lugha ya Kiarabu tu.

Na ingawa Historia ya Lugha ya Kiarabu basi inaonesha kua mtu wa mwanzo kutayarisha mpangilio wa Nahaw katika Kiarabu alikua ni *Amir Ul Muumiin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* pale alipomwamrisha mwandishi wake aitwae Abu Al Aswad Al Duali kuandaa utaratibu maalum wa mpangilio huo, lakini tunapomuamngalia Imam Al Sibawayh basi bila ya shaka kutokana na kitabu chake basi yeye anadhihirisha kua ndie Baba wa Nahaw.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo tunapokiangalia Kitabu cha *Al Kitab* basi ndani yake Imam Al Sibawayah katika kuelezea kwake ametumia mifano ya takriban Aya 400 za Qur'an, Hadith za *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam*, Methali na Misemo ya Lugha ya Kiarabu, Lugha ya Mashairi ya Kiarabu, Lugha ya Kiarabu cha Asili cha Kibedui na baadhi ya maneno na sentensi za Lugha ya Kiarabu.

Ambapo anasema Imam Abu Tayyib kua: '**Siku moja Ibn Kaysan alilala akaota kua kuna Majini ambao wamekusanyika huku wakiwa wanazungumzia kuhusiana na mambo mbali mbali za Ilm ya Kiislam, hivyo Ibn Kaysan akawauliza: 'Hivi Jee nyinyi hua mnatumia kitabu gani cha Nahau?' ambapo nao wakajibu: 'Bila ya Shaka Kitabu cha Sibawayh.'**

Na Imam Al Baghdadi anaendelea kusema kuhusiana na kisa hiki cha Ibn Kaysan kua: '**Habari hii ya Ibn Kaysan ikamfikia Abu Musa ambae nae aksema: 'Haishangazi kwani Sibawayh mwenyewe alikua ni Jini pia.**''

Imam Al Sibawayh alisoma pia kwa Imam Yaʿqub Ibn ʾIsḥāq Ibn Zayd Ibn ʿAbd Allāh Al Haḍrami, ambae alikua ni Mtaalamu wa Lugha na Ilm ya Qiraa pia, na kisha yeye Imam Al Sibawayh akasomesha Wanazuoni wengineo akiwemo Imam Abū Al Ḥasan Saʿid Ibn Masada, maarufu kama Al Akhfash Al Awṣat. Na akamsomesha Imam Abu Ali Quṭrub Ibn Aḥmad Al Mustanir Al Baṣrī ambae alikua haganduki kutoka kwenye Mlango wa Nyumba ya Imam Al Sibawayh.

Ambapo anasema Muawwiyah Ibn Bakr kua: '**Mimi nilimuona Al Sibawayh akiwa kijana na kusikia kua ni Mwanafunzi wa Al Khalil Ibn Ahmad, lakini sasa nilipomsikia akizungumza basi nikagundua kua alikua na kasoro katika Lugha yake, ambapo kwa upande mwengine unapoangalia Vitabu vyake basi unaona kua Ilmu iliyomo ndani ya Vitabu vyake ni kubwa sana kuliko iliyomo ndani ya Ulimi wake.'**

Imam Al Sibawayh baada ya kumaliza utafiti wake juu ya Lugha ya Kiarabu basi alirudi katika ardhi ya Barsa na kuendelea kuishi katika mji wa Basra huku akiwa ni mwenye sifa ya kua na umri mdogo na kusomesha Wanafunzi wake na umaarufu wake kuzidi kukua, ambapo bila ya shaka unapokua na neema ya uzuri na wingi wa kitu fulani basi ni lazima kua na Wapinzani, na mmoja kati ya wapinzani wa Imam Al Sibawayh alikua pia ni Mwanazuoni wa Ilm ya Lugha na Qiraa cha Qur'an ambae ni Mwanazuoni wa Mji wa Kufah ambae ni Imam Al Kisai.

Hivyo Imam Al Sibawayh akaamua kumalizana na upinzani huo kwa kutaka kuitishwe mahojiano ya hoja baina yao lakini rafiki yake Al Sibawayh aitwae Yahya Ibn Khalid

Al Barmaki akapinga juu ya shauri hilo, lakini hata hivyo Imam Al Sibawayh akatilia mkazo juu ya mahojiano hayo. Hivyo Yahya Ibn Khalid akaanda mahojiano hayo na kisha wakachagua eneo la Mahojiano hayo, ambapo kabla ya mahojiano hayo basi Wanafunzi wa Imam Al Kisai wakiwemo wawili waitwao Al Ahmar na Al Farrah walikua wakienda kwa Imam Al Sibawayh na kujaribu kumchuma akili kutokana na kile anachokijua katika fani yake, kwa ajili ya matayarisho ya tukio muhimu kuliko yote la mahojiano baina ya Imam Al Sibawayh na Imam Al Kisai.

Ambapo anasema Al Farrah kua: ‘**Sibawayh alikua ametilia mkazo kuhusiana na mahojiano baina yake, na Al Kisai, hivyo Yahya akaandaa mahojiano hayo, na mimi na Al Ahmar tukahudhuria, kulikua kumewekwa viti katikati ya uwanja ambavyo juu yake alikua amekaa Yahya na Wanazuoni wengine wa Lugha, ambapo Al Ahmar akaanza kwa kumuuliza suali Sibawayh, ambapo katika kila suali analolijibu Sibawayh basi Al Ahmar alikua akisema Umekosea, nami pia nikamuuliza masuali ambapo nae akakosea, hivyo Sibawayh akasema: ‘Nitasita kuzungumza nanyi, au la sivyo mleteni rafiki yenu Al Kisai ili nihojiane nae.’**

‘Hivyo Al Kisai akaitwa na kuingia na alipokaa akauliza: ‘Naam..nianze mimi kuuliza au utaanza wewe?’ Al Sibawayh akasema: ‘Anza wewe.’ Hivyo Al Kisai akasema: ‘Hivi jee unasemaje kwa Lugha ya Kiarabu kuhusiana na maneno yasemayo:

قد كُنْتُ أَظُنُّ أنَّ الْعَقْرَبَ أَشَدُّ لَسْعَةً من الزُّنْبُوْرِ فَإِذَا هُوَ هِيَ أو فَإِذَا هُوَ إِيَاهَا

Hakika mimi nilikua nadhania kua kutafunwa na Nge kunauma zaid kuliko na Dunduvule lakini kumbe yeye (Nge) ni kama yeye (Dunduvule). Jee utatumia hali ya *Faidha Huwa hiya* au *Faidha Huwa Iyaha? Au hali zote mbili?*

Ambapo Imam Al Sibawayh akasema: ‘**Ni hali ya kwanza tu ndio sahih yaani *Faidha Huwa Hiya’*** na kisha akatoa vithibitisho vyake, ikiwemo kua maneno *Huwa hiya* yako katika hali ya Nomino na maneno *Huwa Iyaha* yako katika hali ya Kivumishi cha Kushutumu.

Ambapo Imam Al Kisai akakubaliana nae Imam Al Sibawayh kuhusiana na usahih wa kutumiwa kwa *Huwa Hiya* lakini akapingana na Imam Al Sibawayh kuhusiana na *Huwa Iyaha* inaweza kua katika hali ya nomino na pia kivumishi. Hivyo wakaanza kubishana bila ya kufikia muafaka.

Hadi pale Yahya Ibn Khalid alipomaua kusema: **‘Inaonekana kua kama kamwe hamtoweza kukubaliana, wakati nyinyi nyote wawili ni viongozi wa Vyuo vyenu ya Lugha hivyo itabidi tutafute mtu atakaetoa Hukmu juu ya hili’**

Ambapo mara Al Kisai akaoneshea upande wa Mlangoni ambapo kulikua kuna Mabedui wanne, kua ndio pekee waliokua wanaweza kutatua mabishano hayo, na walipoulizwa Mabedui hao wakasema kua Imam Al Kisai yuko sahih na hivyo Imam Al Sibawayh akawa ni mwenye kushindwa ijapokua alikua ni mwenye kua sahih, jambo ambalo lilimvunja Moyo sana Imam Al Sibawayh.

Imam Sibawayh akalipwa Dirham 10,000 kama fidia kwa kushindwa kwake, na hivyo akaamua kuihama ardhi ya nchi ya Iraq na kurudi katika Ardhi ya Uajemi ambapo hakukaa kwa mda mrefu sana akafariki huku akiwa na umri wa miaka 43 mnamo mwaka 180 Al Hijra.

Ambapo baadae Imam Al Kisai alikipitia kitabu cha Al Kitab cha Imam Al Sibawayh ambacho kina kurasa 2511 na kisha kuanza kukitumia kua ni miongoni mwa vitabu anavyotumia katika mitaala yake kama walivyofanya Wanazuoni wa wakati huo na waliofuati baada yake.

Na akasema Al Farra baata ya kukisoma kitabu cha Imam Sibawayh kiitwacho Al Kitab kua: ‘**Sibawayh alikua ni *Udla Mim al Udal’*** yaani Imam Al Sibawayh ni Mtu ambae mwenye ufahamu ambao wenye kubeba kitendawili ndani ya Vitendawili, siri ndani ya siri au asiekua wa kawaida kutokana na Ufahamu wake na Upekee katika uandishi wake.

SAYYIDA NAFISA 145 AH

Sayyida Nafisa Bint Hasan Al Anwar Ibn Zaid Al Ablaj Ibn Hasan Ibn Ali Ibn Abi Talib alizaliwa katika mji wa Makkah mwezi 11 *Rabi al Awwal* mwaka 145 *Al Hijr*, hivyo alimzidi kiumri kwa miaka mitano Imam Al Shafi’i, lakini kama Imam Al Shafi’i, nae alitoka katika familia ya Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam*. Baada ya kuzaliwa Sayyida Nafisa aliishi katika mji wa Makkah kwa mda wa miaka mitano ambapo baadae wazee wake walihama na kuhamia katika mji wa Madinah, ambako aliishi na kujipatia *I’lm* yake kutoka kwa Wanazuoni mbali mbali na baadae kuolewa na mtoto wa Imam Jafar As Saddiq aitwae Is-haq Ibn Ja‘far Ibn Muhammad As-Sadiq, katika ndoa ambayo ilitoa watoto wawili ambao ni Al Qasim na Umm Kulthoum.

Kutokana na kua ni miongoni mwa wanawake wenye *I’lm* kubwa sana ya *Tafsir*, *Fiqh* na *Hadith* katika historia ya dini ya Kiislam basi alikua akijulikana pia kama *Nafisat Al*

I’lm. Sayyida Nafisa na familia yake walihamia nchini Misri miaka mitano kabla ya Imam Al Shafi’i nae kuhamia Misri, kwani Sayyida Nafisa aliwasili *Al Arish* ambao ni mji ulioko kaskazini mashariki mwa Misri katika siku ya Jumamosi mwezi 26 wa Ramadhan ya mwaka 193 *Al Hijr* na akakaribishwa na kukaa kwa muda katika nyumba ya mfanyabiashara mkuu wa mji huo ajulikanae kwa jina la Jamal Ad Din Abd Allah Al Jassas, na kisha baadae wakahamia mjini *Al Qakhira* (Cairo).

Katika mji wa *Al Qakhira* walifikia nyumbani kwa Umm Han ambae alikua ni mwenye nyumba kubwa sana hivyo aliitoa sehemu ya nyumba hiyo kwa ajili ya watu wenye kutafuta *I’lm*, lakini hata hivyo baada ya Sayyida Nafisa kuhamia katika nyumba hiyo, ikawa ndogo haraka sana kwani watu walijazana katika nyumba hiyo kiasi ya kua kwa sababu Sayyida Nafisa alikua hana sehemu nyengine ya kufanyia Ibada kama ilivyo kawaida yake anapokua peke yake, akaamua kutaka kuhama katika mji huo na kurudi tena katika mji wa Madinah, lakini hata hivyo umati aliokua akiusomesha uligoma na hivyo kuzuka mgogoro mkubwa sana, ambao uliingiliwa kati na kutatuliwa na As-Siry Ibn Al Hakam aliekua ni Gavana wa *Al Qakhira* kwa wakati huo, ambae alimnasihi na kumtaka Sayyida Nafisa kubakia *Al Qakhira* na kumuahidi kumpatia nyumba kubwa zaidi ili aendeleze kutoa *I’lm* ya dini ya Kiislam, na hivyo wakakubaliana kua atasomesha kwa siku mbili kwa kila wiki na siku zilizobakia atakua akifanya Ibada zake mwenyewe za kawaida.

Waandishi wa Al Qaramayn ambao ni wandishi wa vitabu sahih vya historia vya *Al Gharar* na *Al Mustatraf* wanasema kua: '**Wakati wa Utawala wa Ibn Tulun watu walikua wakilalamika kutokana na kutokua na uadilifu katika uongozi wake, hivyo siku moja, Sayyida Nafisa alipata habari kua kiongozi huyo atapita karibu na nyumba yake, hivyo Sayyida Nafisa akaandika barua, na Ibn Tulun alipopita na kumuona Sayyida Nafisa, akashuka kwenye farasi wake na kumsalimia Sayyida Nafisa ambapo nae akampa barua yake iliyokua ikisema: 'Unatawala bila ya uadilifu na kuyatumia sivyo madaraka yako kwa kuwadhalilisha walio chini yako, unawadhulumu na kuwabania mapato yao, Jee unajua kua dua za waliodhulumiwa hua zinakubaliwa wakati wa Usiku?. Kila mtu atafikia mwisho wake. Hivyo wewe fanya unavyotaka kufanya, sisi tunamlalamikia Allah, na karibuni tu wale wasiofanya uadilifu watayaona matokeo yatakavyokua**'. **Tangu kuazia siku hiyo udhalimu uliomo katika utawala huo wote ulitoweka**. *(Tarikh Al Qaramani)*

Imam Al Shafi`i alipohamia Misri alikua akimtembelea Sayyida Nafisa na kusomeshwa *Hadith* wakati alipokua akienda akirudi kusomesha katika Masjid Amr Ibn Al`Aas na mwezi wa Ramadhan Imam Shafi`i alikua akisalisha *Salat Taraweeh* katika Masjid Sayyida Nafisa na Sayyida Nafisa alikua ni miongoni mwa *Ma’amuma* wake, katika mwezi mzima wa Ramadhan.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kila mara Imam Al Shafi`i alipokua akiumwa alikua akimtuma Mwanafunzi wake aende akasome kwa Sayyida Nafisa, ambae humwambia Sayyida Nafisa, '**Binam yako Al Shafi'i anaumwa na anaomba dua zako**'. Kisha Sayyida Nafisa humuombea dua Al Imam Al Shafi'i. Mwishoni mwa uhai wake Imam Al Shafi`i alikua akiumwa sana na akaandika wasia wa kuomba atakapofariki basi Sayyida Nafisa amsalie sala yake ya maiti (*Salat al Janaza*).

Alisema Sayyidah Nafisa kua: '**Namuomba Allah amuingize kwenye Rehma zake Al Shafii kwa sababu ya namna ya uzuri katika kutia udhu kwake'** ambapo Sayyida Nafisa alisema hivi kwa sababu ya kujua kua Ukamilifu wa Ibada kiubora hua unategemea na kwanza ana Ukamilifu wa Udhu.

Ambapo aliulizwa Zaynab ambae ni mtoto wa kaka yake Sayyidah Nafisah aliekua akikaa pamoja nae nyumbani kwake kuhusiana na namn alivyokua akiishi ndani yake ambapo nae akasema kua: **'Sayyidah Nafisa, alikua ni mwenye kula mara moja tu katika kila usiu wa siku 3, na alikua akining'iniza mfuko mbele yake katika sehemu anayosalia na hivyo ilikua kila akitakacho hua kimo ndani yake. Kiasi ya kua mlikua mna vitu ambavyo kamwe huwezi kufikiria, vimetokea wapi, jambo ambalo mimi lililkua likinishangaza sana, hivyo siku moja nikamuuliza ambapo nae akasema: 'Ewe Zaynab yeyote yule atakaeweza kurekebisha uhusiano wake na Mola wake, basi kila kitu Ulimwengu huweza kua ni chake.''**

Miongoni mwa majirani waliokua wakikaa karibu na Sayyidah Nafisa kulikua kuna Mwanamke mzee mjane aliekua na watoto wanne mayatima, ambae alikua na kazi ya ufumaji nguo, hivyo siku moja wakati anaelekea sokoni na kikapu cha cha vitu alivyovifuma, mara ghafla alitokea ndege ambae alikikwapua kikapu hicho kutoka kichwani mwake mwanamke huyo, na kuruka nacho. Mjane huyo akababakiwa na mshangao, huzuni na vilio kutokana na yaliyotokea kwani alikua akitegemea kua auze vitu alivyovishona ili apate riziki yake kwa ajili ya Mayatima wake.

Hivyo kutokana na kulia kwake na huzuni yake basi watu wakamchukua na kumpeleka Sayyidah Nafisa, ambapo baada ya kufika na kusikiliza yaliyotokea basi akamsomea Dua Mjane huyo. Na kisha akamwambia akae apumzike kwanza kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye uwezo juu ya kila kitu. Hivyo mwanamke huyo akapumzika huku akifikiria nini cha kufanya kwa ajili ya kuwapatia riziki watoto wake.

Baada ya kupita masaa kadhaa, mara kuna watu wakaja kugonga mlango wa Sayyidah Nafisa na baada ya kusalimia basi nao wakaelezea kisa chao, kua wao walikua ni wafairi wa Baharini ambao Jahazi lao lilikwaruza mwamba na hivyo likawa linaingiza maji na likawa halizibiki kila wakijaribu kuliziba, katika jitihada zao hizo mara akatokea ndege na kuwaangushia kikapu chennye nguo zilizofumwa ndani yae ambazo walizitumia kwa

ajili ya kuzibia Jahazi lao, na kuweza kuendelea na safari yao hadi bandarini kwa uwezo wa Mola wao, hivyo wamesikia habari ya Mjane aliekuwepo kwake katika wakati huo na wamekuja kulipa Dinari 500 kama shukuran kwa msaada walioupata kutokana na kikapu hicho.

Baada ya Sayyidah Nafisah kusikia habari hio, basi akasema: **'Ewe Mola wangu Ya Rabb hakika wewe ni mwingi was Rehma na Huurma kwa waja wako'** na kisha akamwita Mjane yule na akampa zile Dinar 500 na kumuelezea yaliyotokea na majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake, kwani ingawa akikapu kilikua na vitu vyenye thamani ya Dinar 25, lakini badala yake *Allah Subhanah wa Ta'ala* amejaalia kua ni mwenye kupata Dinar 500 kutokana nacho.

Sayyida Nafisah alifariki miaka minne baada ya kufariki Imam Al Shafii ambapo nae pia alifariki kwenye mwezi wa Ramadhan wa mwaka 208 Al Hijra.

Ambapo anasema Imam Al Munawi kua: **'Wakati Sayyidah Nafisah alipokua anakaribia kufariki, basi waliokua karibu nae walijaribu kumshauri kua sifunge kutokana na udhaifu wa hali ya afya yake, lakini nae akakataa na kusema kua: 'Itakuaje nisifunge wakati mimi nimekua ni mwenye kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa muda wa miaka 30 anijaalie nikutwe na mauti wakati nikiwa katika hali ya kufunga, halafu leo hii mimi niwe si mwenye kufunga ndani ya Ramadhani hii?'**

Ambapo katika siku aliyofariki Dunia basi alikua anasoma Qur'an na alipofikia kwenye aya isemayo:

﴿لَهُمْ دَارُ ٱلسَّلَامِ عِندَ رَبِّهِمْ وَهُوَ وَلِيُّهُم بِمَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ﴾

Lahum daru alssalami AAinda rabbihim wahuwa waliyyuhum bima kanoo yaAAmaloona *(Al Anaam 6:127)*

Tafsir: ***Na kwa ajili yao kuna makazi ya Salama mbele ya Mola wao ambae ni Rafiki yao kutokana na yale waliyoua wakiyafanya.***

Na baada ya kumaliza aya hii basi Sayyidah Nafisah akafariki Dunia, na alizikwa ndani ya Nyumba yake.

IMAM AHMAD IBN ABI AL-HAWARI

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ahmad Ibn Abi Al Hawari alizaliwa katika ardhi ya Dimashq nchini Syria na alitoka katika familia yenye watu ambao ni wacha Mungu sana, na hivyo haya yalikua ni mazingira ambayo yalimtayarishia yeye mwenyewe pia kua ni mwenye ucha Mungu na kushikamana na Suna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwani alikua akisema kua: ‘**Yule ambae ni mwenye kufanya mambo yake bila ya kushikamana na Sunnah basi kila kitu chake hua ni mchezo’**

Imam Ahmad Al Hawari alisoma kwa Imam Abu Sulayman Ad Darani ambapo alisema Imam Al Junayd kuhusiana nae kua: ‘**Ahmad Al Hawari ni Ua sana zuri la Sham’** na ingawa alikua ni mtu wa Sham lakini Imam Al Hawari alikua ni mtu ambae anapenda kutembea kwa ajili ya kutafuta Ilm, ambapo katika kutembea kwake kwa ajili ya kutafuta Ilm basi akakutana na Imam Sufyan Ibn Uyaynah na hivyo akawa na ukaribu nae sana.

Ingawa alikua ni mwenye kupenda kutembea sana Ardhini lakini Imam Al Hawari hakua ni mtu mwenye kuipenda Dunia kwani alikua ni mwenye kusema: ‘**Hii Dunia ni kama chungu ya Uchafu unaokirihisha, na ni sehemu ambayo Mbwa hua wanakusanyika kwa ajili yake hivyo yeyote yule mwenye kupenda kubakia ndani yake hua ni zaidi ya Mbwa, kwani Mbwa hua ni mwenye kuchukua kile akitakacho na kisha huondoka, lakini mwenye kuipenda Dunia hua si mwenye kuondoka na kuachana nayo kwa wakati wa karibuni.**’

Baada ya Imam Al Hawari kusoma kwa Imam Sufyan Ibn Uyaynah na kuwiva katika Ilm ya Hadith basi alivichukua vitabu vyake vyote na kisha akavizamisha kwenye Mto na kusema: **‘Baada ya kuyafikia Malengo basi haina haja ya kutafuta muongozo.’**

Imam Al Hawari alirudi na kuendelea kusoma kwa Imam Sulayman Ad Darani ambapo siku moja walikaa wakakubaliana kua isitokee hata mara moja ikawa hawakukubaliana juu jambo fulani, hivyo baada ya hapo Imam Sulayman alimwambia Imam Al Hawari huku akimuoneshea kwenye Jiko la kupikia Mikate lililokua pembeni yake kua aende akaingie kwenye Jiko hilo.

Hivyo Imam Al Hawari akaenda na kuingia kwenye jiko hilo ambalo lilikua lina moto wake, baada ya mda Imam Sulayman akawa anamtafuta Imam Al Hawari ikawa hamuoni lakini akakumbuka kua alimtania aingie kwenye Tanuri hilo hivyo huenda ikawa ameingia kweli, na hivyo akamfuata ndani ya Tanuri hilo na akamkuta Imam Al Hawari akiwa kweli amekaa ndani yake pembeni yake hivyo akamwambia atoke kwenye jiko hilo na hivyo Imam Al Hawari akatoka huku akiwa hajaathirika hata kidogo kutokana na Moto huo kwani hayo yalikua ni matayarisho ya kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta’ala* na hivyo kutotegemea wala kutoogopa kitu chengine chochote, hivyo Imam Sulayman hivyo akasema:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

‘Kama mtu itakua hajafanya toba na kujuta kwa kutumia Moyo, na badala yake akawa ametumia Ulimi tu basi kazi yake yote hua bure, na hali kadhalika hua hakuna jitihada katika Ibada kama ikiwa hujaepukana na Dhambi.’

Kwani mtu mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta’ala* pekee hua ni mwenye kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta’ala* peke yake. Kwani yule anaempenda *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi hua ni mwenye kupenda kufanya Ibada na hivyo hua ni mwenye kupata ridhaa yake, kutokana na kupendwa kwake na Mola wake.

IMAM AHMAD IBN HADRAWAYHH 145 AH

Imam Abu Hamid Ahmad Ibn Hadrawayh Ibn Muhammad Ibn Abi Amr Al Balkhi alizaliwa katika ardhi ya Balkhi nchini Afghanistan na alikua ni Mwanafunzi wa Imam Hatim Al Asim na alikua ni mwenye ukutana na Imam Ibrahim Ibn Adham, Imam Abu Hafs Al Haddad na pia na Imam Abu Turab An Nahasubi.

Imam Ahmad Ibn Hadrawayh alikua ni mtu mwenye I’lm kubwa sana, Mcha Mungu na alieachana na Dunia na kila kitu kilichomo ndani yake. Na alikua ni mwenye kusema kua: ‘**Yeyote yule anaetaka kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* ashikamane nae kila wakati na katika kila jambo basi wacha ashikamane na Ukweli.’**

Na akasema tena kua: **‘Njia iko wazi na ukweli uko dhahir na mtangaziaji ameshasikika, hivyo baada ya yote hayo kushangazwa hua kunatokea kutokana na upofu’**

Aliulizwa Imam Abu Hafs: **‘Hivi jee ni nani mtu mwenye darja kubwa katika kipindi chetu’** ambapo nae akajibu: **‘Sijaona mtu yeyote ambae ni mcha Mungu zaidi na mwenye Darja zaidi ya Ahmad Ibn Hadrawayh’** na akasema pia kua: **‘Kama Ahmad Ibn Hadrawayh angekua hayupo hai basi ingekua hakuna *Futuuwa* wala *Muruuwa*’**

Katika Mji wa Balk kulikua na Mwanamke wa Sultan wa Balkh ambae alikua ni Mcha Mungu pia na alikua aitwae Fatima na alikua hajaolewa, hivyo Fatma akaamua kumtuma mtu kwa Imam Ahmad Ibn Hadrawayh kwa ajili ya kuomba kutaka kuolewa nae, ambapo hata hivyo Imam Hadrawayhh akakataa maombi hayo.

Hivyo Fatma akatuma Mtu mwengine, kwa Imam Ahmad Ibn Hadrawayh na kumpa ujumbe usemao: **‘Hakika mimi nilidhani kua wewe ni miongoni mwa wale wanaoongoza watu, na wala si mwenye kuwawekea vizingiti wale ambao ni wenye**

kuutafuta muongozo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*.' Na baada ya kuupokea ujube huo, basi Imam Ahmad Ibn Hadrawayhah akaona bora akampose Mwanamke huo, na hivyo akamposa na kumuoa.

Mbali ya kua Fatma alikua ni mwanamke wa kitajiri lakini ndani mwake alikua si mwenye kuweka kitu chochote cha thamani, kwani kila akipatacho hua si mwenye kukitoa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na hivyo ilikua hakuna kitu chenye thamani ndani ya nyumba yake, hivyo siku moja katika nyumba yake akaingia Mwizi ndani ya Nyumba yake, lakini hakukuta kitu cha kuiba, na hivyo akaamua kutoka nje, lakini kabla ya kutoka akakamatwa na Imam Ahmad Ibn Hadrawayhh, ambae alimuamrisha kwa kumuambia: **'Adhabu yako ni kua nenda kachukue ndoo ile pale kisha ijaze maji, na kisha natakata utie udhu, kisha usali kiasi ya kua kama itakua kuna kitu ndani ya Nyumba yangu nikupe uondoke nacho ili usiwe ni mwenye kuondoka mikono mitupu. '**

Hivyo mwizi huyo akajaa maji ndoo akatia udhu na kisha akasali na kisha hakaruhusiwa kuondoka, kwani alikua anatakiwa abakie humo humo ndani ambamo alikaa hadi asubuhi yake na mara Imam Ahmad Ibn Hadrawayh akapokea ugeni wenye kumzawadia vipande 50 vya Dhahabu. Hivyo Imam Ahmad Ibn Hadrawayh akampa Kijana huyo aliekua anataka kuiba vipande vyote hivyo vya Dhahabu na kumwambia: **'Haya ndio malipo ya ile sala uliyosali jana usiku chukua.'**

Na hivyo kijana huyo hapo hapo akasema: **'Hakika mimi ni mwenye kujidhulumu nafsi yangu na nimefanya jema moja tu jana usiku na *Allah Subhanah wa wa Ta'ala* amenilipa malipo makubwa kiasi hiki, hivyo nnatubu kwa Mola wangu na naomba niwe ni mwenye kusomeshwa nawe.'** Hivyo kijana huyo akawa ni Mwanafunzi wa Imam Ahmad Ibn Hadrawayhh.

Kutokana na kua ni mwenye kutoa sana basi Imam Ahmad Hadrawayh alikua na baadhi ya madeni na hivyo wakati anakaribia kufariki basi aliwaita wale wote waliokua wakimdai na kisha akaomba Dua mbele yao kwa kusema: **'Ya Rabbi, Unataka kuchukua Roho yangu wakati bado mimi sijawa huru kutokana nao, na Utumwa wao ni madeni yao juu yangu nao wanamtafuta mtu wa kulipa madeni hayo, hivyo nakuomba mjaalie fulani ibn fulani awe ni mwenye uwezo wa kuwalipa madeni yangu, halafu baada ya hapo ndio uichukue Roho yangu.'**

Baada ya kumaliza Dua hio basi mara watu hao wakasikia kutoka nje sauti isemayo kua: **'Wenye kumdai Abu Hamid watoke nje kuja kuchukua malipo ya madeni yao'** na hivyo baada ya watu hao kua ni wenye kulipwa madeni yao basi Imam Ahmad Ibn Hadrawayh akafariki Dunia mnamo mwaka 240 Al Hijra wakati akiwa na umri wa miaka 95.

Ambapo anasema Muhammad Ibn Hamid ambae alikua karibu na Imam Ahmad Ibn Hadrawayh kua: '**Ahmad Ibn Hadrawayh alikua na umri wa miaka 95 wakatio alipokua kwenyekitanda chake cha muati ambapo alisema huku akiwa anatokwa na machozi machoni kua: 'Ewe Mtoto wangu kuna mlango ambao nilikua nikiugonga kwa mda wa miaka 95, hivyo sasa hivi ndio mlango huo umefunguka kwa ajili yangu, ila sijajua kama unafungua kwa ajili ya kheri yangu au kwa ajili ya mitihani juu yangu, hivyo nitajibu vipi masuali yatakayo ulizwa juu yangu.'**'

Ambapo alisema Imam Ahmad Ibn Hadrawayh kua: **'Marifah ya kweli hua ni kumpenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Moyo wako na kumkumbuka kwa Ulimi wako na kuachana na kila kitu kisichohusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**

'Hakuna usingizi mzito kuliko usingizi wa mghafiliko, hakuna Utumwa wenye nguvu kama utumwa wa matamanio, na kama si kuwepo kwa uzito wa kudharau basi Matamanio yasingekua ni yenye kusinda.'

'Yeyote yule mwenye kuwahududmia Masikini basi hua ni mwenye kujaaliwa kua na sifa tatu zifuatazo: Hua ni Mwenye Unyeneyekevu, Hua ni Mwenye uzuri wa Adabu na hua ni mwenye ukarimu.'

'Yeyote yule aliekua na ukaribu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni mwenye Kua na Tabia bora zaidi.'

'Ichunge heshima yako katika kua na umasikini wako, yaani usiwaambie watu kua wewe ni masikini kwani Umasikini ni Zawadi kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

'Subira hua ni neema ya Masikini na Kinaya hua ni Darja ya wenye Hikma na Busara'

'Moyo ni chombo ambacho kinapokua kimejaa mapenzi juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni kilichojaa nuru inayoving'arisha viungo vyengine, na unapokua umejaa Kufuru hua ni wenye kujaa kiza ambacho ni chenye kuvijaza kiza Viungo vyengine'

Aliulizwa Imam Ahmad Ibn Hardawayh: **'Jee niAmali gani ndio bora zaid?'** ambapo nae akajibu: '**Ni kujilinda na kujizuia kutokana na kutomsifu yeyote isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Amesema Imam Ahmad Ibn Hardawayh kuhusiana na aya isemayo:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

﴿فَفِرُّوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ إِنِّي لَكُم مِّنۡهُ نَذِيرٞ مُّبِينٞ﴾

Fafirroo ila Allahi innee lakum minhu nadheerun mubeenun *(Surat Dhariat 50:51)*

Tafsir: ***Kimbilieni kwa Allah kwani kwa hakika mimi kutoka kwake ni uthibitisho ulio wazi.***

Kua aya hii inamaanisha kutufahamisha sisi kua hakuna kimbilio bora dhidi ya kila kitu isipokua kukimbilia kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Imam Ahmad Ibn Hadrawayhh alikua ni Mtu ambae asiependa umaarufu kwani alikua ni mwenye kuogopa madhara yake na hivyo alikua akisema kua: '**Muumba hakua ni mwenye kujipa Umbo wala hakutaka kuwepo katika sehemu maalum, hivyo na Walii hua anatakiwa asiwe na sifa wala jina'**

SHAYKHA RABIA BINT ISMAIL AL DIMASHQ

Rabia Bint Ismail Al Dimashq alikua ni mmoja kati Wanawake wakubwa wenye Ilm na Mali katika Mji Dimashq nchini Syria, ambae alitumia Mali yake aliyoachiwa na Mume wake aliefariki hapo kabla kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani baada ya kutoka eda basi Rabia akamfuata Imam Ahmad Ibn Abi Al Hawari na kumwambia kua: **'Hakika mimi sina matamanio nawe bali ni mwenye kutaka kuzitumia Mali zangu kwa ajili ya A*llah Subhanah wa Ta'ala* baada ya kuolewa nawe na hivyo utumie Mali hizi kwa ajili ya Uislam, kwani mimi sikupendi wewe kwa mapenzi ya Mwanamke kwa Mwanamme bali nakupenda kwa Mapenzi ya Muislam kwa Muislam mwenzake, na hivyo nataka niwe msaidizi wako katika maisha yako'.**

Hivyo Imam Ahmad Ibn Abi Hawar akazungumzia juu ya jambo hilo kwa Mwalimu wake ambae ni Imam Abu Sulayman Ad Darani ambae nae akamwambia akubaliane na ndoa hio na hivyo Rabia akaolewa na Imam Ahmad Ibn Abi Hawar.

Kwani Rabiah Bint Ismail alitumia Mali yake hio katika kumuunga mkono Mume wake katika kuendeleza Dini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala, a*mbapo na yeye mwenyewe pia alikua ni Mwalimu mwenye Ilm kubwa sana na alikua akiwasomesha Wanafunzi mbali mbali wa Kike na wa Kiume na alikua na Ilm kubwa sana ya Tasawwuf na ni mwenye kudumua katika Dhikr Allah.

Ambapo anasema Imam Ahmad Al Hawari kua: ‘**Siku moja mimi nilimwata Rabia ambae ingawa alikua yupo mbele yangu lakini sikuhisia hisia zozote kua alikua ni mwenye kunisikia, ambapo baada ya saa moja nikamwita tena na akaniitikia na nilipomuuliza kwanini mara ya kwanza hakuniitikia basi akasema: ‘Moyo wangu ulikua umejaa Furaha juu ya Mola wangu, na hivyo sikuwa na uwezo wa kuhisi chochote hata kuusikika wito wako.’’**

Imam Al Hawari anaendelea kusema tena kua: **‘Usiku mmoja mimi nilikua nimezama kwenye *Qiyam Al Layl*, na mara nikamuona Rabia katika hali ambayo sikuwahi kumuona hapo kabla, kwani alikua yuko macho huku akiwa yuko katika hali ya umakini na utulivu mkubwa sana’** ambapo Rabia akasema: **‘*Subhanah Allah*, usiseme hivyo kwani nilikua niko katika hali ya kawaida tu.’**

Rabia Bint Ismail alifariki na kuzikwa kwenye mji wa Jerusalem mwenye Mlima wa Tini.

SHAYKHA HALIMA AL DIMASHQ

Halima Al Dimashq alikua ni mwenye kutokana na ukoo wa kisharifu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na alikua ni Mwanamke mwenye Ilm kubwa sana pia na ndie Mwalimu wa Rabia Bint Ismail ambae ni mke wa Imam Ahmad Al Hawari.

Ambapo siku moja Rabia Bint Ismail alimtembelea Halima, na alipoingia akamkuta anasoma Qur’an, hivyo baada ya kusalimiana basi Halima akamwambia Rabia kua: ‘**Rabiah, hakika mimi nimesikia kua Mumeo anataka kuoa mke mwengine zaidi yako, hivi jee ni kweli?’**

Rabia Bint Ismail akaitikia kwa kusema:‘**Naam ni kweli’.**

Na kisha Halima akaendelea kusema: **‘Hivi inakuaje? Mbali ya ufahamu wote aliokua nao kisha anaamua kutafuta mke mwengine na hivyo kutaka kua na wake wawili watakaoufanya Moyo wake uwe ni wenye kukosa umakini na Mola wake? Hivi jee hujasikia wewe kuhusiana na zile aya zisemazo kua’**

﴿يَوْمَ لاَ يَنفَعُ مَالٌ وَلاَ بَنُونَ ۝ إِلاَّ مَنْ أَتَى ٱللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ﴾

Yawma la yanfaAAu malun wala banoona; Illa man ata Allaha biqalbin saleemin
(Surat Ash Shuara 26:88-89)

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: ***Siku ambayo haitomfaa mtu Mali wala Watoto wake; ila yule ambae atakafika mbele ya Allah Subhanah wa Ta'ala akiwa na Moyo ulio salama.***

Jee unajua maana yake?'

Ambapo Rabia akasema : **'La'**

Hivyo Halima akasema: **'Inavyotakiwa kwa Ibn Adam ni kumshughulikia *Allah Subhanah wa Ta'ala* peke yake ndani ya Moyo wako, usiwe na kitu chochote ndani yake zaidi yake.'**

Ambapo anasema Rabia kua: **'Baada ya maneno hayo mimi nikaondoka huku, nikiwa nimejawa na hisia zilizonigusa sana ndani ya Moyo wangu, kiasi ya kua nilikua natembea huku nikiwa napepesuka na hivyo kua na khofu kua huenda wapita njia wakadhania kua mimi ni mlevi kutokana na mwendo wangu.'**

SHAYKHA AL LUBABA AL MUTA AL A'ABBIDA

Al Lubaba Al Muta Al Abida alikua ni Mwanamke Mcha Mungu ambae anaishia Dimashq nchini Syria, alikua ni Mcha Mungu mwenye Ilm ya Tasawwuf na Mujahadat yaani mwenye kupigana Jihadi na Nafsi yake ipasavyo.

Anasema Imam Ahmad Ibn Abi Hawari kua: **'Alisema Muhammad Ibn Rawah alisema kua: 'Lubaba alikua ni Mcha Mungu ambae alikua akisema kua: 'Hakika mimi nnaona aibu mbele ya Mola wangu kuniona mie Ndani ya Moyo wangu nikiwa nna mwengine yeyote zaidi yake'''**

Ambapo anasema Lubaba kua: **'Kila ninavyopigana na Nafsi yangu basi ndivyo nnavyozidi kujihisi Raha ndani ya Nafsi yangu na hivyo nikichoka kua pamoja na kukutana Ibn Adam wengine basi hua ni mwenye kua na ukaribu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kufanya Dhikr Allah na kumtumikia yeye'**

Siku moja aliambiwa Lubaba na mtu mmoja aliekua anataka kuenda katika Ibada ya Hija kwa kusema: **'Mimi nataka kwenda kwenye Ibada ya Hija hivyo jee niwe nafnya Dhikr Allah gani zaidi?**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo Al Lubabah akasema: **‘Muombe *Allah Subhanah wa Ta’ala* Awe ni mwenye kuridhika nawe ili uwe ni mwenye kuifikia Daraja ya wale aliowaridhia na kisha atakupadisha Darja ya kua ni miongoni mwa Awliyyah wake’**

Na anasema Abad Allah Ibn Muhammad Al Antakiyah kua: **‘Amesema Ahmad Ibn Abi Hawari kua: ‘Ahmad Ibn Muhammad amesema kua: ‘Al Lubaba alisema: ‘Hakika nnaona haya mbele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* ili asinione nikiwa nna kitu chengine chochote ndani ya Moyo wangu zaidi yake, baada ya kumjua yeye’’’**

Na akasema pia kua: **‘Ilm ya kumjua *Allah Subhanah wa Ta’ala* humpelekea mtu kua ni mwenye kumpenda yeye, na kumpenda yeye *Allah Subhanah wa Ta’ala* humpelekea mtu kua ni mwenye kumtamani Mola wake, na kwa mja kumtamani Mola wake hua ni kwenye kumpelekea kua na ukaribu na Mola wake, na kua na ukaribu na Mola wake humpelekea Mja kua ni mwenye Kumtumikia na kumtii Mola wake’**

IMAM MANSUR IBN `AMMAR

Imam Mansur Ibn Ammar alizaliwa katika mji wa Khurasan lakini baadae akahamia katika mji wa Baghdad nchini Iraq na hivyo kua ni mtu mwenye kukubalika sana katika maeneo yote mawili ya Khurasan na Iraq kutokana na ukubwa wa Ilm yake, kwani alikua ni mtaalamu mkubwa sana na Al Hafidh wa Qur’an, Hadithi, Tasawwuf, Fiqh n.k

Ambapo amesema Imam Mansur Ibn Ammar kua: **‘Utukufu ni wake tu *Allah Subhanah wa Ta’ala* ambae ameufanya Moyo wa Mawalii kua ni chombo chenye uwezo wa kubeba *Dhikr Allah,* Moyo wa aliechana na Dunia kua ni chombo chenye uwezo wa kubeba *Tawakkul* na Nyoyo za wenye kuamini kua ni chombo chenye uwezo wa kubeba Ridhaa, na Moyo wa Darwesh kua ni chombo chenye kuweza kubeba Kinaya, na Moyo wa Wenye kuendekeza matamanio kua ni chombo chenye uwezo wa kubeba Matamanio.’**

Kwani ni muhimu kujua kua mbali ya kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* amejaalia kila kiungo kua ni chenye kazi yake, kwama miguu kwa ajili ya kutembelea, mikono kwa ajili ya kukamatia, na macho ni kwa ajili ya kuona na masikio ni kwa ajili ya kusikia.

Lakini hata hivyo ameweka Moyo kwa kila Ibn Adam kulingana na upekee wa sifa zake na matamanio yake, na hivyo Moyo huo kua ni sehemu ya uongofu au kua ni sehemu ya upotovu, au kua ni sehemu ya kukinai, au sehemu matamanio na kadhalika, ambapo amesema mwenye *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua: **‘Ibn Adam wote wanaweza kua**

katika hali mbili: 'Yaani yule Mtu ambae ni mwenye kujijua Nafsi yake na hivyo hua ni mwenye kujichunga na kujirekebisha. Na yule Mtu ambae ni mwenye kumjua Mola wake na kazi yake hua na kumuabudu Mola wake na hivyo kazi yake hua ni kumuabudu *Allah Subahanah wa Ta'ala* na kumridhisha.''

Ambapo ibada ya mtu wa mwanzo yaani mwenye kuijua Nafsi yake hua ni katika hali ya kufanywa kutokana na kua inastahiki, lakini ibada ya mtu anaemjua Mola wake hua inafanywa kutokana na kua ni mwenye kujua ukubwa wa Mola wake. Na Ibada ya mtu wa kwanza hua ni katika hali ya kujitolea ili mhusika apate darja ya juu lakini Ibada ya mtu wa pili hua inafanywa huku mtu huyo akiwa tayari ameshapata Darja ya juu, hivyo jee kua tofauti gani baina ya hali mbili hizi?

Tofauti ya kwanza ni hali ya Mtu mwenye kujitahidi na hali ya pili ni hali ya Mtu Mwenye kutafakkar kutoka na kua tayari ni mwenye kushuhudia, kwani kuna aina mbili za watu ambapo aina ya kwanza ni Wale wanaomhitaji *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na mahitajio yao ambao hua ni wenye darja ya juu kulinga na Sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na aina ya pili ni ya wale ambao ni wasiojali kuhusiana na mahitajio yao kutoka kwa Mola wao kwani wanajua kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* tayari ameshajaalia kwa ajili ya viumbe wake kila kitu chao riziki zao, kifo na uhai, furaha na huzuni hivyo wao hua wanamhitaji *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee, na hivyo kua nae huwa kunawapa uhuru wa juu ya kila kitu.

Hivyo watu wa aina ya kwanza basi wao wamezibwa mtizamo wa kuona kwao kutokana na kuyaona mahitajio yao kwanza na hivyo hua hawaoni kuwepo kwa riziki kutoka kwa Mola wao, wakati wale ambao ni wa aina ya pili hua hawaoni yale mahitajio yao na hivyo hua waliofunuliwa pazia la mtizamo wa macho yao na kua huru na huona kila kitu.

Ama kuhusiana na wale wa kwanza basi wao hua ni wenye kupata raha ya furaha, wakati wale wa hali ya pili hua ni wenye kupata raha kutokana na yule ambae ni chanzo cha furaha hio.

IMAM ABU DHIB

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Shaykh Ul Islam Imam Muhammad Ibn Abd Rahman Ibn Mughira Ibn Harith Ibn Abu Dhib.

Huyu ni Imam ambae aliishi katika kipindi kimoja na Imam Jafar As Saddiq, Imam Abu Hanifa Nuuman Ibn Thabit, Imam Malik Ibn Anas na mwanzoni mwa uhai wa Imam Muhammad Idris Al Shafii.

Kwani Imam Ibn Abu Dhib alikua ni mtu ambae Mcha Mungu, asiesengenya Watu, mwenye kujilinda na Mazungumzo yasiyokua na maana, na alikua si mwenye kumdharau mtu hata mmoja, alikua akimthamini kila mtu na ni mwenye kutoomuogopa Mtu yeyote kuhusiana na kumwambia ukweli Mtu yeyote.

Alikua anawapenda Masikini na alikua na *Qawlan Sadidah*, yaani Kauli zisizopinda na zenye kugonga moja kwa moja kwenye moyo wa mtu husika kama inavyotakiwa kufikisha Ujumbe uliokusudiwa.

Alikua ni mwenye kudumu katika Funga kwani alikua siku moja anafunga na siku moja anawacha na alikua ni mtu wa kukimbilia kila lenye kuonesha Utiifu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* tena kwa ridhaa na furaha.

Kwani Siku moja Imam Ibn Abu Dhib alienda katika Ibada ya Hija na akakutana na Khalifa Jafar Abu Mansur wa Dola la Kiislam la Al Abbas ambapo sambamba wakakutana na Imam Malik Ibn Anas mwanzilishi wa Madhhab ya Imam Malik.

Baada ya Ibada ya Hija Khalifa Abu Jafar Mansur akamualika Imam Ibn Abu Dhib Ambapo Khalifah Abu Jafar Al Mansur akamuuliza Imam Ibn Abu Dhib kuhusiana na Gavana wa Mji wa Madina aitwae Hasan Ibn Zayd.

Ambapo Imam Ibn Abu Dhib akajibu: ‘**Hakika Ibn Zayd ni Mtu Mzuri anajaribu kusimamia haki na Uadilifu.’**

Khalifa Abu Jafar Al Mansur akamuuliza Imam Ibn Abu Dhib: ‘**Jee nini mtizamo wako kuhusiana na mimi?’** Imam Ibn Abu Dhib akajibua: ‘**Wa Allahi Hakika Mimi nnaapa Wakati nikiwa Mbele ya Al Kaabah kua Wewe Ni Kiongozi Dhalimu alietimia’**

Na baada ya kusema maneno hayo basi Walinzi wa Khalifa Abu Jafar Al Mansur wakamvamia Imam Ibn Abu Dhib.
Lakini Khalifa Abu Jafar Al Mansur akawazuia Walinzi hao na kisha akampa Imam Ibn Abu Dhib zawadi ya Dirham 300. Ambazo hata hivyo Imam Ibn Abu Dhib alikataa kuchukua.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kwani siku moja Imam Ibn Abu Dhib alikua amekaa ndani ya Masjid An Nabawi katika Mji wa Madina.

Khalifa Mahdi Abu Jafar Al Mansur ambae ni Khalifa alierithi Ukhalifa wake baada ya kufariki baba yake ambae ni Khalifa Abu Jafar Al Mansur.

Hivyo Khalifa Mahdi alipoingia katika Masjid An Nabawi basi kila Mtu akasimama kwa ajili ya Kuonesha Heshima yake mbele ya Khalifa huyo.

Lakini kwa Upande wa Imam Ibn Abu Dhib basi yeye ndie peke yake aliebakia huku akiwa amekaa kitako chini kama kawaida yake na wala hana habari kabisa kuhusiana na ujio huo wa Khalifa Mahdi.

Hivyo mmoja kati ya Watu waliokuwemo Msikitini humo alikaribu na Imam Ibn Abu Dhib akamwambia Imam Ibn Abu Dhib: '**Hebu Simama kwani alieingia ni *Amir ul Muuminin'***

Ambapo Imam Ibn Abu Dhib akabakia hapo hapo chini huku akisema kwa sauti kubwa: **'Ibn Adam Wanatakiwa Wasimame kwa ajili ya Mola wao tu.'**

Kiasi ya kua Khalifa Mahdi aliposikia sauti hio basi Yeye mwenyewe kijasho chembamba kilianza kumtoka kwenye paji lake la uso, hivyo akasema: **'Mwacheni akae kama alivyo kwani hata nywele zangu zimesimama kwa msisimko wa maneno yake.'**

Kwani alisema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Hakika mimi nilisikitikia Kifo cha Imam Ibn Abu Dhib kuliko kifo cha Mtu yeyote yule mwengine**' Na akasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Hakuna anaemfikie kwa Mfano wake kwa ucha Mungu wake miongoni mwa walioishi karibu nae Imam Ibn Abu Dhib.**'

Kwani Hata Imam Malik Ibn Anas alikua hamfikii Imam Ibn Abu Dhib kwa Ucha Mungu na Uadilifu.

IMAM AL SHAFI'I 150 AH

Katika mwaka 163 *Al Hijr*, mjini Makkah, kijana mdogo wa kabila la *Quraysh* mwenye umri wa miaka kumi na tatu aliondoka na furaha baada ya kupata barua kutoka kwa

Gavana wa Makkah iliyotakiwa kupelekwa kwa Gavana wa Madinah, kwani barua hiyo ilikua ni zana yake ya pili anayoitegemea katika kutekeleza ndoto ya maisha yake ya kupata *I'lm* ya dini baada ya zana muhimu aliyokua nayo ambayo ni kipaji alichojaaliwa na Allah *Subhanahu wa Ta'ala*.

Kabla ya kuondoka nyumbani kwao, Mama wa kijana huyo alimuombea dua mtoto wake kwa Allah *Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema '**Ya Allah, Mola wa Ulimwengu wote, mtoto wangu huyu anafunga safari ndefu, kutafuta rehma zako, nami nimemuachia ili aweze kutafuta *I'lm* zaid, ambayo ndivyo alivyoamrisha Mtume wako. Hivyo nnaomba msaada wako, ya Allah, umlinde na kumuongoza, na umpe umri mrefu ili niweze kushuhudia moyo wake ukiwa umejaa *I'lm* yenye manufaa..Aamin**'

Na kisha akamkumbatia mtoto wake huku machozi yakimtoka na kumwambia '***Allah Ma'ak!* (Allah yuko pamoja nawe) *In shaa Allah*, utakua ni mwenye *I'lm* kubwa na kunga'risha maisha yako, Nenda kwa sababu nimeamua kukuachia, na kumbuka kua hakuna sehemu bora ya kuomba msaada na kujilinda na chochote isipokua kwa Allah**', akambusu mtoto wake na wakaagana.

Baadae kijana huyu alielezea hali aliyokua nayo baada ya kuagana na mama yake kwa kusema: '**Kila mara nilikua nikigeuka nyuma kumpungia mama yangu mkono, alikua amesimama tuli, nje ya nyumba yetu, bila ya macho yake kuacha kuniangalia, hatimae muonekano wake kwangu mie ukawa unafifia na kufifia katika hewa iliyojaa ukungu wa alfajiri, Niliondoka katika mji mtakatifu wa Makkah, bila ya kuwa na hata pesa za matumizi mfukoni mwangu, matumizi pekee niliyokua nayo ilikua ni Imani thabit, Moyo uliojaa uaminifu kwa Allah *Subhanahu wa Ta'ala*, na Dua aliyoniombea mama yangu, nilijitolea na kumtegemea Allah pekee, Mola wa Ulimwengu**'.

Baada ya kufika Madinah, Gavana wa Madinah alisita kufanya kama vile inavyoamrisha ile barua kwani ilimtaka amchukue kijana yule mdogo na ampeleke kwa Imam Malik ambae alikua ni mtu wa dini anaeheshimiwa na kuogopewa na watu wa chini hadi viongozi wakubwa kwa *I'lm* yake. Lakini kutokana na kipaji na akili za kijana alieileta barua ile, ilimbidi Gavana wa Madinah kwanza kutafakkar kwani anajua kua Imam Malik hapendi watu kujipendekeza kwa wenye Mamlaka ili kupata wanachokitaka, hivyo basi Gavana huyo bila ya kutaka, akamchukua kijana yule na kuenda nae moja kwa kwa moja hadi nyumbani kwa Imam Malik.

Baada ya Gavana wa Madinah na yule kijana kufika kwa Imam Malik, wakakutana na mfanyakazi wake ambae nae akaipokea barua ile na kisha akampelekea Imam Malik, ambae nae akaisoma barua hio, baada ya kuisoma akawakaribia walioleta barua hio huku akiwa Imam Malik amekunja uso, kuonesha kua hajafurahikia ujumbe uliomo ndani ya

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

barua hio akuitupa chini na kisha akahoji: ‘**Inakuaje! Tunashuka chini kiasi hiki? hadi kufikia kua watu kutafuta *I’lm* ya *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* basi huwabidi wapitie kwa wenye Mamlaka na vyeo vikubwa, vikubwa!**’

Hapo Gavana wa Madinah akanywea na kukaa kimya bila kujua aseme nini. Hivyo yule kijana mdogo aliekuja nae ikabidi atumie silaha yake ya pili kwa kujitambulisha na kusema ‘**Allah akuingize kwenye rehma zake, mimi ninatoka katika ukoo wa Ibn Al Muttalib katika kabila la *Quraysh* na hadi sasa hapa nilipofikia nimeshafanya kadha w kadha w kadha**’.

Imam Malik akamsikiliza kijana huyo huku akiwa ni mwenye kupigwa na butwaa, kwani yalikua ni maelezo ambayo yana mambo ambayo hakuyatarajia kua yanaweza kufanywa na kijana mdogo kama huyo, maelezo ambayo yalimtuliza na yakamvaa na kumuingia akilini, yakamuonesha ukubwa wa ufahamu wa kijana aliekuwepo mbele yake, ufahamu ambao ulibadilisha monekano wa uso wake kutoka katika kua ni wenye kukunjana na kua wenye kung’ara kwa kujaa katabasam.

Hivyo akamuuliza kijana jina huyo lake, ambapo kijana nae akajibu: ‘**Mimi naitwa Muhammad Idris Al Shafii**’.

Imam Malik akasema ‘**Muhammad, kua mcha Mungu na uzikimbie dhambi kwani una sifa za kipekee zinazokupeleka kupanda kwenye ngazi za juu. Allah ametia mwangaza ndani ya Moyo wako. Hivyo usisababishe kuzimika kwa mwangaza huo kwa sababu ya kufanya dhambi…Njoo kesho usome**’.

Huo ulikua ndio mwanzo wa kukutana na kujuana baina ya Mwanazuoni mkubwa Imam wa *Madhhab* ya Malik ambae alikua anakaribia miaka 70 na Imam Muhammad Idris Al Shafi’i aliekua kwenye miaka 13 akielekea kwenye maisha ambayo Allah *Subhanahu wa Ta’ala* alimjaalia awe Mwanazuoni mkubwa katika historia ya Kiislam na muanzilishi wa Madhhab ya Al Imam Al Shafi’i

Amesema Abdur Rahman Ibn Mahdi Ibn Hasan Al Ambari ambae alikua pia Mwanafunzi wa Imam Malik kua nimemsikia Imam Malik akisema: ‘**Hamna *Quraysh* ambae amekuja na ufahamu mkubwa kuliko kijana huyu**’, akimaanisha Imam Shafi'i.

Muhammad Ibn Idris Al ‘Abbas Ibn Uthman Ibn Al Shafi’i Ibn Al Saib Ibn Ubayd Ibn Abd Yazid Ibn Hashim Al Muttalib Ibn Abd Manaf Ibn Qusay bin Kilaab bin Murrah, au alijulika kama Imam Al Shafi’i, Abu A’bd Allah Al Shafi’i Al Hijazi Al Makki Al Azdi Al *Quraysh* Al Hashimi Al Muttalib Ibn Abd Manaf Ibn Qusay Ibn Kilaab Ibn Murrah alizaliwa mwaka 150 *Al Hijr* katika maeneo ya *Asqalan* katika mji wa Gaza

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

uliopo nchini Palestina. Mwaka ambao Imam Abu Hanifa anafariki dunia ndio mwaka huo huo ambao alizaliwa Imam Idris Al Shafi'i.

Imam Al Shafi'i ametoka katika kabila la Quraish, hivyo familia ya Imam Al Shafi'i imeungana na familia ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* kupitia kwa babu yake Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* Al Mutalib Ibn Abd Manaf ambae ni babu wa tisa wa Imam Al Shafi'i. Mama yake Imam Al Shafi'i anaitwa Fatimah bint A'bd Allah Ibn Al Hasan Ibn al Husein Ibn Ali Ibn Abi Talib hivyo ameungana na Ali Ibn Abi Talib kwa Upande wa Mama.

Kuna habari ambayo inanasabishwa na Ibn Abd Al Hakam kua Fatimah, mama yake Imam Al Shafi'i alipokua ana mimba ya Muhammad Idris Shafi'i, siku moja alilala akaota kua kuna nyota inayong'ara imetoka ndani ya fuko lake la uzazi na kupaa angani na kutua katika maeneo ya Misri, lakini mishare ya mwangaza wa nyota hiyo ilitapakaa dunia nzima. Alipoamka asubuhi na kuulizia maana ya ndoto hiyo aliambiwa kua atapata mtoto ambae *I'lm* yake ya Dini itaenea Misri na katika sehemu nyengine watu watanufaika na *I'lm* hiyo.

Baba yake Imam Al Shafi'i alifariki wakati yeye akiwa bado mdogo, alipotimia umri wa miaka 2 mama yake alimchukua na kumhamishia katika Mji wa Makkah ambako aliishi na kujifunza mambo mbalimbali, ikiwemo kujifunza ufasaha wa lugha na mashairi ya kiarabu katika kabila la Al Huzail, pia alijifunza kutumia silaha ya upinde na kua mtaalamu wa hali ya juu wa silaha hiyo, kiasi ya kua ilikua kama akitunga shabaha mara kumi hakosi hata mara moja.

Imam Al Shafi'i alikua na uwezo mkubwa wa kiakili, kumbukumbu, ufahamu na utaalamu wa hali ya juu wa lugha ya kiarabu na historia, alihifadhi *Qur'an* yote na hukmu zake akiwa na miaka minane tu na kuhifadhi kitabu cha *Hadith* Malik Muwata cha Imam Malik wakati akiwa na umri wa miaka 10.

Anasema Al Shafi'i '**Baada ya kusoma *Qur'an* nilikua nikienda msikitini, huko hukaa na Wanazuoni wa *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* na *I'lm* ya dini. Nilikua nikiishi na watu wanaoishi katika mahema nikiwa katika hali duni na ya umasikini sikua na uwezo hata wa kununua karatasi kwa ajili ya kuandikia nilikua nikiandikia kwenye mifupa**'.

Al Shafi'i alisomeshwa na Imam Muslim Ibn Khalid Az Zanj ambae alikua Shaykh na Mufti wa Makkah kwa wakati huo ambae alisomeshwa na Ibn Jurayj aliesoma kutoka kwa A'ta Ibn Rabah ambae alisomeshwa na Abd Allah Ibn 'Abbas *Radhi Allahu A'nhu* na A'bd Allah Ibn Zubayr. Al Shafi'i pia alisomeshwa na Imam Muslim Ibn Khalid Al Zanj na baada ya kuona uwezo wa Al Shafi'i katika yale aliyomsomesha Imam Muslim

Ibn Khalid Al Zanj alimuambia Al Shafi'i, '**Ya Abu A'bd Allah toa Fatwa kwani tayari umeshafikia wakati wa kutoa Fatwa!**'.

Imam Al Shafi'i pia alisoma kwa Imam Sufyan Ibn Uyaynah Al Hilal ambaye alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni watatu wakubwa wa *I'lm* ya *Hadith* katika mji wa Makkah, Sufyan Ibn Uyaynah alisomeshwa na Amr Ibn Dinar ambae amesomeshwa na Abd Allah Ibn 'Abbas *Radhi Allahu A'nhu* na A'bd Allah Ibn Umar.

Anasema Ahmad Ibn Muhammad Ibn Bintush Shafi'i kua **'Hakika nimemsikia baba yangu na mjomba wangu wakisema 'Kila anapokuja mtu kwa Sufyan Ibn Uyaynah, kutaka kujua kuhusu *Tafsir* au Fatwa, Sufyan alikua akimuachia Al Shafi'i kutafsir au kutoa Fatwa hiyo.''**

Imam Ahmad Ibn Hanbal anaelezea umuhimu wa Imam Al Shafi'i pale aliposema kua, '**Imam Al Shafi'i alikua kama Jua kwa Dunia, na Afya njema kwa *Bani Adam*, Jee vitu viwili hivi vinavyo mbadala wake?**'

Imam Nawawi aliandika sifa tatu alizokua nazo Imam Al Shafi'i kua: **Ametokana na ukoo wa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* wa Abd Manaf; Amezaliwa katika ardhi takatifu ya Palestina na amekulia katika ardhi takatifu ya Makkah.**

Imam Ibn Hajar nae akasema, '**Alisema Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* 'Ya Allah, waongoe Ma*quraish* kwani sayansi ya *I'lm* ya wanazuoni itakayokuja kutoka kwao, itaifunika Dunia, Ya Allah! Umewaonjesha uchungu waliotangulia, hivyo wajaalie watakao wafuatia waonje utamu wake**'

Na pia akasema Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* '**Hakika Allah atatuma kwa Ummah wangu, kila baada ya miaka mia, mtu ambae atakuja kuiweka sawa dini ya Uislam kwa ajili yao**'.

Wanazuoni wanakubaliana miongoni mwao akiwemo Abu Qilaba na Imam Ahmad Ibn Hanbal kua *Hadith* ya mwanzo ilikua inambashiria Imam Al Shafi'i na *Hadith* ya pili inabashiri mtu wa miaka mia ya mwanzo ambae ni Umar Ibn Abd Al 'Aziz na wa miaka mia ya pili kua ni Imam Al Shafi'i.
Hakika Al Shafi'i alikua na sifa za mtu aliejaaliwa kipaji cha pekee na aliekua akijua jinsi ya kikutumia, sifa ambao zilimvutia Gavana wa Makkah baada ya kumuona Al Shafi'i na akapendekeza apelekwe kusoma katika mji wa Madinah kwa Imam Malik. Hivyo Al Shafi'i akaanza kusoma Madinah kwa Imam Malik.

Siku moja wakati Al Shafi'i alikua amekaa chini ya miguu ya Imam Malik akisomeshwa, alikuja mtu na kumwambia Imam Malik: '**Hakika mimi nimeshamuacha mke wangu jee nifanye nini?**'.

المستكشف أبو منال دانا
AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Malik akamuuliza: **'Kwanini unasema hivyo jee imekuaje?'**

Yule mtu akajibu: **'Mimi kazi yangu ni kuuza ndege, hivyo dukani kwangu alikuja mnunuzi akataka kumnunua ndege aina ya Kasuku, alipofika akaniuliza kama yule Kasuku analia ama la, nikamuapia kua kama halii basi mke wangu awe ameachika, kwani yule Kasuku alikua akilia, yule mnunuzi akamnunua yule Kasuku lakini baada ya siku kadhaa alimrudisha na kusema kua yule Kasuku halii.'**

Imam Malik akajibu, '**Hakika umeshamuacha mke wako, hivyo usimkaribie**'. Al Shafi'i akaingilia kati na kusema: '**Subiri kwanza nikuulize.** '**Jee, baina ya kulia na kunyamaza kwa Kasuku wako kupi ni kukubwa zaidi?**''

Yule muuzaji akajibu**,** '**Kulia kwake ni kukubwa zaidi kuliko kunyamaza kwake**'.

Al Shafi'i akajibu '**Basi mkeo hajaachika**'.

Hapo Imam Malik akaingilia kwa kusema '**Ya Al Shafi'i unajuaje?**'.

Al Shafi'i akajibu '**Kwa sababu ulinidadithia kua kutoka kwa Al Zuhri, kutoka kwa Abu Salam Ibn Abd al Rahman, kutoka kwa Umm Salama ambae amesema kua Fatima bint Qayis alisema 'Ya Rasul Allah! Abu Jahm na Muawiyah wote wawili wameniposa'** ***Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salaam*** **akajibu 'Muawiyah hana pesa, na Abu Jahm hatui mzigo chini kutoka kwenye bega lake (kwa Safari), akiwa na maana: Hali ya kila mara; Kwa Waarabu hutumia hali ya kila mara kutokana na utokeaji wa mara kwa mara kwa kitu au jambo. Hivyo kwa kua Kasuku wake alikua akilia kwa mda mrefu zaidi na kunyamaza kwa mda mfupi, basi hii inamaanisha kua Kasuku ni mwenye kulia**'.

Imam Malik akaridhika na kumwambia Al Shafi'i '**Naam uko Sahih!**'.

Tukiangalia tutaona kua hapa Al Shafi'i alitumia hali ya kulia na kunyamaza kwa ndege kutokana na kufananisha ukubwa wa muda ambao yule Kasuku alikaa dukani akilia kabla ya kuuzwa na udogo wa muda ambao yule Kasuku hakulia kwa yule mtu aliemnunua.

Wakati Al Shafi'i anasoma Madinah kwa Imam Malik, Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa aitwae Muhammad Ibn Hasan alikua akitembelea mji Madinah na alikua akienda kwa Imam Malik kusoma, hivyo alikua akisomeshwa pamoja na Al Shafi'i na kwa upande wa Imam Al Shafi'i basi alikua akiutumia mda wake wote kwa ajili ya kusoma

na alikua akienda Makkah mara moja moja kumtembelea Mama yake na wakati mwengine hutoka nje ya mji wa Madinah na kukaa na Mabedui.

Safari moja Al Shafi'i alirudi Makkah na kumkuta mama yake anaumwa na anakaribia kufariki. Fatima aliuchukua mkono wa mtoto wake na kusema '**Mtoto wangu mpenzi, Allah amekujaalia kipaji na nuru ya *I'lm*, hivyo sitaki nuru hii itoweke kutokana na raha za kidunia, Unakumbuka wakati unaondoka kuelekea Madinah nilipokuaga, nilimuomba *Allah Subhanahu wa Ta'ala* akufanye uwe nuru kama jua linavyoangaza mbingu ya *I'lm*, ewe mtoto wangu sitaki Mawingu ya raha na utajiri wa dunia upunguze nuru ya jua hilo. Namuomba Allah aiangaze njia ya uongofu kwa Ummah kupitia katika *I'lm* yako, na aijaalie nuru hii iwanufaishe pia Waumini siku ya malipo, Aamiin**'.

Wakati Fatimah anataka kufariki, Al Shafi'i alijawa na huzuni na kusema '**Mama yangu mpendwa, unaondoka wakati mimi sikuwahi kupata nafasi ya kukutumikia**', na hapo Fatima akajibu '**Mtoto wangu, kamwe sikukulea ili unitumikie mimi**'.

Baada ya kufariki mama yake, Idris Al Shafi'i alirudi tena Madinah na akakaa huko hadi mwaka 179 *Al Hijr* alipofariki Imam Malik, kisha akaondoka Madinah na kurejea katika mji wa Makkah, alipokua katika mji wa Makkah alikutana na Gavana wa Yemen aliekua akitembelea Makkah, baada ya Gavana huyo kumuona kutokana na *I'lm* yake akuamua kumchukua na kumpatia kazi ya Qadhi katika mji wa Najran ambako alikaa kwa muda wa miaka mitano, huku akitoa hukmu, akielimisha watu na pia akisoma kwa undani *Fiqh* ya Wanazuoni wa Yemen akiwemo Mutraf Ibn Mazzin, Hisham Ibn Yusuf aliekua Qadhi wa Sana'a, Amr Ibn Abi Salama na Yahya Ibn Hasan.

Imam Al Shafi'i alikaa Yemen kwa miaka mitano na baada ya kuingia mwaka 184 *Al Hijr* haikuchukua mda mji wa Najran ukapata Gavana mpya ambae alikua si mtu muadilifu, na Imam Al Shafi'i alikua mara kwa mara akimkosoa kwa kutofanya uadilifu, kwa bahati mbaya au nzuri ikatokea migogoro ya kisiasa baina ya Yahya Ibn Abd Allah ambae alikua Mwanazuoni wa Shia na Gavana huyo mpya wa Najran.

Hivyo Gavana wa Najran akatumia nafasi hiyo ili kumuondoa Imam Al Shafi'i karibu yake na hapo akamtuhumu Imam Al Shafi'i kushirikiana na Yahya Ibn Abd Allah, hivyo Gavana huyo akaandika barua kwa *Khalifah* Harun Rashid na kumuelezea kua '**Sina nguvu juu ya mtu huyu kwani ni mwenye uwezo wa kushinda kwa ukali wa ulimi wake kuliko mpiganaji anavyoweza kushinda kutokana na kutumia upanga wake**'. Barua ambayo ilisababisha Imam Al Shafi'i akamatwe, pamoja na watuhumuiwa wengine na kupelekwa Iraq chini ya ulinzi kwa ajili ya kuhukumiwa.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Baada ya Imam Al Shafi'i kufikishwa katika mji wa Al Raqqa, Iraq. *Khalifah* Harun Rashid aliitisha jopo la washauri ili kuhukumu kesi hiyo, na mmoja kati ya washauri hao alikuwemo Muhammad Ibn Hasan Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa ambae pia alisoma kwa Imam Malik. Wakati huo Muhammad Ibn Hasan alikua Mwanafiqh Mkuu wa *Khalifah*, hivyo akamtetea na kusema kua Imam Al Shafi'i ni mtu mwenye *I'lm* ya hali ya juu na muadilifu kwani walisoma pamoja kwa Imam Malik na haiwezekani kua ni miongoni mwa waasi, hivyo jopo hilo likajadiliana na baadae Imam Al Shafi'i akaitwa na akajitetea hadi Harun Al Rashid akaridhika na kumwachia huru na pia akampa pesa kama fidia kutokana na kutuhumiwa bila ya kufanya makosa, na watuhumiwa wengine walionekana na makosa na wakapewa adhabu ya kifo. Baada ya kuachiwa huru Imam Al Shafi'i alizichukua zile pesa zote akazigawa na kuzitolea sadaqa kwa maskini bila kubakisha hata dinar moja mfukoni mwake.

Imam Al Shafi'i akabakia Baghdad na akawa anaishi kwa Muhammad Ibn Hasan jambo ambalo lilimsaidia sana Imam Al Shafi'i kwani kwa wakati huu alipata nafasi ya kuisoma kwa undani zaid *Fiqh* ya Imam Abu Hanifa kupitia kwa vitabu na *I'lm* ya Muhammad Ibn Hasan na Muhammad Ibn Shayban ambao walikua ni Mujtahid wa *Madhhab* ya Hanafi na pia akasoma kwa Waki Ibn Jarrah, Hammad Ibn Usama na Abd Al Wahab Ibn Abd al Majid. Alikua akifanya nao mijadala mbalimbali ya kidini na kuhojiana katika kuelimishana na kutatua maswali mbalimbali ya ki*fiqh* yatokanayo na utofauti baina ya *Fiqh* ya Imam Malik na Imam Abu Hanifa. Al-Shafi`i aliukubali ubora wa misingi ya *Fiqh* ya Imam Abu Hanifa kwa kauli yake maarufu isemayo: '**Watu wote ni watoto wa Abu Hanifa katika *Fiqh***.'

Imam Al Shafi'i alisema '**Sikuwahi kufanya mahojiano na mtu yeyote bila ya kuomba Dua: Ya Allah! uoneshe ukweli moyo wake na ulimi wake, ili ikiwa mimi ni mkweli anifuate na ikiwa yeye ni mkweli basi nimfuate**'. Maisha aliyoishi katika maeneo mengi yenye wataalamu tofauti wa *I'lm* yalimfanya, Imam Al Shafi'i kua mtaalamu wa *Hadith* ambazo hazijulikani Makkah, Madinah wala Yemen na pia kua mtaalamu wa Ilm ya *Fiqh, Mantiq, Firasa* na Tofauti za Wanazuoni wa Madinah kwa Imam Malik, Wanazuoni wa Iraq kwa Imam Abu Hanifa na pia *Fiqh* ya Wanazuoni wa Yemen na hivyo kua ni mwenye kuifikia Darja ya *Mujtahid* yaani Mtu mwenye uwezo wa kufanya *Ijtihad.*

Ambapo anasema Imam Abu Hamid Muhamamd Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafi'i kua; **Kitafsiri nguvu ya *Al Ijtihad* hutegemea mambo matatu:**

1. ***Al Ijtihad* -** Kutumia uwezo wa *Ijtihad* yenyewe.
2. ***Al Mujtahid* -** Mtu atakaefanya *Ijtihad.*
3. ***Al Mujtahid fihi* -** Kitu kinachotakiwa kufanyiwa *Ijtihad.*

Anasema Imam Al Ghazal kua, ***Ijtihad* haitumiki hadi pale inapotumika nguvu na uwezo wote. Ndio maana watu husema *Ijtihada fi haml hajar al raha* (Alifanya juhudi zote kulibeba jiwe la kusagia). Lakini hawasemi *Ijtihad fi haml khardala* (Alifanya Juhudi zote kubeba punje ya ufuta). Lakini neno hili hutumika maalum kwa jitihada zinazofanywa na *Mujtahid* katika kupata ufahamu wa hukmu za ki sharia'h. *Ijtihad* kamilifu ni kufanya bidii ya hali ya juu katika kufikia kusudio lililolengwa ambapo hua haiwezekani kufanyika jitihada zaid**. (*Al-Mustasfa min usul al-Fiqh*).

Hivyo '***Ijtihad* maana yake ni kujitahid (kwa upande wa *Mujtahid*) kwa bidii zote katika kutafuta hukmu ya jambo ambalo halina vithibitisho vya kutosheleza katika maandiko na hivyo kutowahi kutolewa hukmu yake kabla yake.**'

Na Imam Al Shafi'i anasema kuhusu *Ijtihad*: '**Haruhusiwi mtu yeyote kutoa Fatwa katika Uislam isipokua kwa yule mwenye *I'lm* katika *Qur'an*: Kuhusu kilichobatilishwa, na kilichobatilisha, kipi ni *Muhkam* (Kilichowazi, chenye uhakika, kilichokua hakijafichika) na kipi ni *Mutashabihat* (Hakiko wazi, kilichofichika, chenye maana nyingi), Tafsir yake, Kushuka kwake, ni ipi aya ya Makkah na ipi ya Madinah, nini kimekusudiwa katika aya hiyo na kwa sababu gani aya hiyo ikashuka, halafu awe ni mtaalamu wa *Hadith*: ajue pia kilichobatilisha na kilichobatilishwa katika *Hadith* na ajue kuhusu *Hadith* kama vile anavyotakiwa ajue kuhusu *Qur'an*. Awe mtaalamu wa (*Fus-ha*) lugha ya Kiarabu na lugha ya Mashairi ya kiarabu, atumie Uadilifu, asiwe msemaji sana na ajue mazingira yanayomzunguka au mahala anapoishi, ikiwa anajua hayo hapo ataruhusika kuzungumzia Halali na Haram, na ikiwa hana yote hayo basi anaruhusika kuzungumza kuhusu sayansi ya Kiislamu lakini si kutoa Fatwa.'** (*Kitab Ul Umm*).

Hivyo mtu afanyae *Ijtihad* (*Mujtahid*) hutakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

1. Kuijua na kuifahamu lugha ya kiarabu na kanuni zake (Katika *Fus-ha, Sarf, Nahw, I'lm Balagha, I'lm ul Huruf*).
2. Kuijua na kuifahamu *Qur'an* (Katika *Ulum ul Qur'an, Ahkam, Tafsir, Asbab An Nuzul, Al Nasikh wal Mansukh*).
3. Kuijua na kuzifaham *Hadith*i na *Sunnah* (Katika *Ulum ul Hadith*).
4. Kuzijua na kuzifahamu hukmu za sheria, kanuni zake na makusudio yake (*Usul ul Fiqh na Maqasid ash Sharia'h*).
5. Kujua historia ya Uislam, makubaliano na kutofautiana kwa *I'jmaa* na pia miongoni mwa Wanazuoni.
6. Kua na Busara na *Mantiq*.
7. Kua na *Taqwa*.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazal anaielezea maana ya *Mantiq* kwa kusema kua: ‘**Ni Kanuni inayotofautisha baina ya ukweli halisi wa hoja na makisio yake kutokana na udhaifu wa hoja, kanuni ambayo hutoa uwezo wa kufahamika usahihi wa kitu kiakili na kiufahamu kwa uwazi zaidi’**

Vitabu vya *Fiqh* vimetaja aina tofauti za Mujtahid, na miongoni mwao ni wafuatao:

- ***Mujtahid Mutlaq au Mujtahid Mustaqil*** – Mujtahid Kamili au Mujtahid anejitegemea: Mfano maimamu wa *Madhhab* kama vile Imam Jabir Ibn Zayd, Imam Jaffar Sadiq, Imam Abu Hanifa, Imam Malik, Imam Al Shafi’i na Imam Hanbal.
- ***Mujtahid Madhhab*** – Mujtahid wa *Madhhab* huyu hua ni mtu ambae hawezi kutoa hukmu moja kwa moja kutoka katika vyanzo wa *Sharia’h*, lakini ana *I’lm* kubwa inayohusiana na ufahamu wa msimamo wa Imam wa *Madhhab* yake, kiasi ya kua anaweza akatoa ushahidi vile ambavyo Imam wake angelisema kuhusiana na jambo ambalo hajaliwekwa wazi. Mfano katika *Madhhab* ya Imam Al Shafi’i, Mujtahid al *Madhhab* wake ni Imam Al Haramayn Al Juwayni na Imam Al Ghazal. Katika *Madhhab* ya Al Shafi’i, Mujtahid huyu pia hujulikana kama *As-haab al Wujuuh*.
- ***Mujtahid fil Tarjeeh*** – Mujtahid wa vipimo. Huyu hua Mujtahid ambae hawezi kutoa hukmu moja kwa moja katika vyanzo wa *Sharia’h*. Kazi yake ni kupima msimamo baina ya mambo fulani ndani ya *Madhhab* na kuamua lipi lina uzito na lipi dhaifu na pia kujua sababu za uzito na udhaifu wa jambo hilo. Mfano katika *Madhhab* ya Imam Al Shafi’i, *Mujtahid Tarjeeh* ni Imam Nawawi na Imam Rafi‘i. Katika *Madhhab* ya Al Shafi’i, Mujtahid huyu hujulikana pia kama *Mujtahid Fatwa. (Shafi’iFiqh.com)*

Hivyo baada ya kua na Darja ya *Mujtahid* basi Imam Al Shafi’i alikaa Iraq hadi mwaka 186 *Al Hijr*, kisha akaamua kuondoka na kuelekea Harran, Syria na kisha Makkah ambako alikaa hadi mwaka 195 *Al Hijr*, katika kipindi hiki Imam Al Shafi’i alikua akitoa *I’lm* katika msikiti wa Makkah, lakini safari hii akiwa na msimamo tofauti ki*fiqh* na ule aliokua nao mwanzo baada ya kutoka Madinah kwa Imam Malik. Kwani alikua amepata muangaza ambao ulimuonesha baadhi ya kasoro zilikowepo katika *Fiqh* ya Imam Malik na pia katika *Fiqh* ya Imam Abu Hanifa, kitu ambacho kiliwavutiwa wafuasi wengi akiwemo Ahmad Ibn Hanbal ambae wakati huo alitembelea mji wa Makkah katika moja ya harakati za kuhiji na kutafuta *I’lm* akiwa na rafiki yake aitwae Is-haq Ibn Rahawayh ambaye baada ya kumsikiliza Imam Al Shafi’i bila ya kumjua aliuliza ‘**Jee tuache kumsikiliza Sufyan Ibn Uyaynah na badala yake tumsikilize kijana huyu?**’ ambapo Ahmad Ibn Hanbal akajibu ‘**Ukiukosa uwezo wa kufikiri wa kijana huyu wa *Quraysh*, basi huwezi kuupata sehemu nyengine yeyote ile, lakini ukiikosa *Hadith***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kutoka kwa Mwanazuoni wa hali ya juu unaweza ukaipata *Hadith* hiyo hiyo kwa Mwanazuoni wa chini.' Huo ulikua ndio mwanzo wa kijana Ahmad Ibn Hanbal kuona na kuvutiwa na uwezo mkubwa wa *I'lm* aliokua nao kijana ambae Allah *Subhanahu wa Ta'ala* alikwisha muandikia kua baadae atakua ni rafiki yake mkubwa na pia ni Mwalimu wake mkuu.

Imam Ahmad Ibn Hanbal anasema, '**Al Shafi'i ni *Hujjat* (uthibitisho) wa lugha ya kiarabu**' na akasema Mwanazuoni mkubwa Al Karabisi aliewahi kuishi wakati wa Imam Al Shafi'i kua '**Sikuwahi kuona darsa nzuri na yenye busara kama ya Al Shafi'i, katika darsa yake walikua wakihudhuria watu wenye *I'lm* ya *Hadith*, *Fiqh* na Mashairi pia, na walikua wakimtembelea na wakisikiliza darsa zake katika fani zote**'.

Abu Ubayd Al Qasim Ibn Salam alisema '**Ikiwa ufaham wa Taifa zima uwekwe pamoja, basi ufaham wa Imam Al Shafi'i ungeliufunika ufaham huo**'. Anasema Imam Bayhaqi, kutoka kwa Ibn Hisham kua: **'Nilikua nimekaa na Imam Al Shafi'i mda mrefu na kamwe sikuwahi kumsikia akizungumza bila kutumia maneno ambayo yana umakini na ufasaha wa lugha ya kiarabu'.**

Anasema Imam Bayhaqi kua amesema Al Hasan Ibn Muhammad Al Zafarani kua: '**Kuna kundi la Mabedui ambalo lilikua likija hujitenga na kukaa pembeni kusikiliza darsa za Imam Al Shafi'i. Siku moja nilimwambia kiongozi wao 'Ah! Nyinyi hamvutiwi na mambo ya *I'lm* ya dini lakini inashangaza kuona kua mnakuja na kukaa pamoja nasi, Jee hua mnafuata nini?**'', Bedui huyo Akanijibu '**Tunafuata utamu wa lugha anayoitumia Al Imam Al Shafi'i**'.

Imam Al Shafi'i alikua ni mtu ambae anaeshikamana na *Qur'an* na *Hadith* katika maisha yake. Anasema Ahmad Ibn Hanbal kua '**Sikuwahi kumuona yeyote yule ambae anashikamana na *Hadith* kama Imam Al Shafi'i, hamna aliempita katika kuandika *Hadith* katika kitabu**'. Hii inamaanisha kua Al-Shafi`i alikua ana ufahamu mkubwa wa *Hadith* ambao pia Ahmad Ibn Hanbal alikua akiutafuta. Ahmad Ibn Hanbal anasema '***Fiqh* ni chache sana miongoni mwa Wanazuoni wa *Hadith***'. Yaani inawezekana mtu akawa na ufahamu wa *Fiqh* bila ya kua na mwana *Fiqh* kwani Sufyan Ibn Uyayna mwenyewe alikuwa akiwaelekeza watu kwa Al Shafi`i katika mambo ya Tafsir na Fatwa.

Abu Na'im Al Haafidh anasema '**Nimemsikia Suleiman Ibn Ahmad akisema: 'Nimemsikia Ahmad Ibn Muhammad bint Shafi'i akisema: 'Ilikuwa vikao vya *Fatwa* kwenye Msikiti wa Makka, kwanza vilifanyika chini ya Abd Allah Ibn 'Abbas, kisha vikawa chini ya Ataa Ibn Rabaah, kisha Abd Allah Ibn Jarah, kisha vikawa chini ya Muslim Ibn Khalid, kisha Said Ibn Salim, na baada yake vikao hivyo vikawa chini ya kijana Muhammad Ibn Idris Al Shafi'i.'**

Siku moja mtu mmoja alimuuliza Imam Al Shafi'i swali, na Imam Al Shafi'i akaanza kulijibu kutokana na *Hadith* ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* inayotoa hukmu na jawabu la swali hilo, yule mtu akamwambia Imam Al Shafi'i '**Mimi nataka nijue mtazamo wako wewe unaonaje kuhusu jambo hili**'. Pale pale Imam Al Shafi'i alibadilika rangi ya uso wake na kusema '**Jee ni sehemu gani ya Ardhi au Mbigu itakayokubali kunisitiri mimi ikiwa nitashauri kitu ambacho Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* alishauri na mimi nikashauri vyenginevyo?**'.

Mmoja katika Wanafunzi wa Imam Al Shafi'i anasema '**Kila Mwanazuoni hukupa *I'lm* zaid pale unaposoma vitabu vyake kuliko anapokusomesha uso kwa uso, isipokua Al Shafi'i ambae ukikaa nae uso kwa uso unapata zaid kuliko unaposoma vitabu vyake**'.

Unapoangalia na kusoma vitabu vya Imam Al Shafi'i ambae ndie mtu wa mwanzo kuanza kutumia neno *Madhhab* kumaanisha Kundi La watu wanaofuata Mtizamo mmoja basi utauona ukubwa wa *I'lm* na uwezo aliokua nao katika kufafanua kwa kina na kuweka wazi mambo mbalimbali na hapo utajiuliza ikiwa kwa maandishi tu anakupa ufahamu wa kina kiasi hiki jee hiyo uso kwa uso ambayo Wanafunzi wake hufaham zaid kusoma vitabu vyake itakuaje?

Imam Al Shafi aliona utofauti uliokuwepo baina ya Maimamu waliomtangulia. Kama inavyoonekana katika utambulisho wa kitabu chake Al Umm kua:

1. Skuli za *Madhhab* ya Imam Malik na Imam Abu Hanifa wanazikubali na kuzitumia baadhi ya *Hadith* Mursal na *Hadith* Munkati ambazo japo hua hazina misingi na zinagongana na *Sunnah*. Kwa hivyo Imam Al Shafi'i alikataa kuzikubali Mursal *Hadith*.
2. Aligundua kua Wanazuoni waliopita, hawakuweka kanuni yeyote yenye msimamo katika kutafuta uthibitisho wa ushahidi pale inapotokea upingano wa ushahidi wa aina mbili ambao huenda ukailinda *Ijtihad* kutoka katika kukosea. Hivyo Imam Al Shafi'i akalipa kipaumbele jambo hili katika kazi yake.
3. Aligundua kua baadhi ya *Hadith* Sahih zilikua hazijulikani na wana*fiqh* wa Tabi'ina, hivyo mara nyingi *Ijtihad*, ilikua ikipingana na *Hadith* Sahih, hata hivyo pale ambapo Wanazuoni waliopita walipojua kuhusu *Hadith* Sahih ambayo ilikua inapingana na Fatwa za Wanazuoni wa mwanzo, basi walikua hawaziachi Fatwa za wale waliopita. Wakisema kua *Hadith* hizo zilikua zikienda kinyume na *Madhhab* yao, hivyo lazima kutakua kuna makosa kwani zilikataliwa na waliotangulia, kutokana na hili Imam Al Shafi'i alitoa hoja ya kua, tufuate kanuni za walioptia, lakini sio kwa kuwaiga wao tu, Kwani kanuni zao zilikua, inapotokea tatizo jipya linalotaka ufumbuzi, walikua huangalia *Hadith* kuhusu jambo hilo, na kama

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

hawakulikuta basi watatumia mantiki na njia nyengine. Lakini hawakufunga milango ya *Ijtihad* yao ya kukubali *Hadith*, bali wakipata *Hadith* inayopinga *Ijtihad* yao ya rai, huiacha *Ijtihad* yao na kufuata *Hadith*. Hivyo, Imam Al Shafi'i anatoa hoja ya kua kama ikiwa wao walikua wakielezea wazi kasoro ya *Hadith*, haitokua haki kuchukulia kua hawakulikubali hilo kutokana na kosa la *Hadith* hiyo.

4. Wakati wa Imam Al Shafi'i kauli zote za Masahaba (*Athari*) zilikua zimekusanywa. Akaona nyingi kati ya kauli hizo zinapingana zenyewe kwa zenyewe, akafanya utafiti na kuona kua kauli nyingi pia zilikua zikipingana na *Hadith* Sahih. Sababu kubwa ni kua walikua hawazijui *Hadith* hizo Sahih, Akagundua kua katika hali kama hiyo Wanazuoni waliopita waliamua kuziacha *Athari* na kufuata *Hadith* Sahih. Hivyo Imam Al Shafi'i akaamua kufuata njia hiyo hiyo akisema kua Masahaba ni *Bani Adam* kama sisi.
5. Aligundua kua baadhi ya Wanaf*iqh* walikua wakichanganya *Rai* na *Qiyas*, ambapo *Sharia'h* inapinga Rai na imeruhusu *Qiyas*, Akimaanisha kua, kwa Rai huzingatia uchunguzi potovu au mantiki au dhana kama ni msingi wa kanuni ya *Sharia'h*, na kwake yeye *Qiyas* ni kutumia akili katika hukmu ya kitu ambacho kimo katika vitabu na katika msingi wa kutoa hukmu ya kitu chengine. Aliipinga Rai kabisa na akasema kuhusu *Istihsan* kua yule anaefanya *Istihsan* anataka kua ni muweka *Sharia'h*.

Imam Al Shafi'i aliandika kitabu kinachoitwa ***Khilaf Al Malik***, kinachozungumzia khitilafu za ki *Fiqh* zilizomo katika *Madhhab* ya Imam Malik na kisha akaandika chengine kiitwacho ***Khilaf Al Iraqiyin,*** kinachozungumzia khitilafu za ki *Fiqh* zilizomo katika *Madhhab* ya Imam Abu Hanifa. Jambo ambalo lilimfanya awe mwanzilishi wa Skuli ya tatu katika *Madhhab* ya *Ahlu Sunnah wal Jamaa* na kuweka wazi *Sharia'h* na misingi ya kufuata katika kutafuta ufumbuzi wa maswali ya *Fiqhi* unaoitwa *Usul ul Fiqh*. Imam Al Shafi'i alikaa kwa mda mrefu katika mji wa Makkah na baadae akaamua kurudi tena Iraq.

Wanafunzi wakubwa wa Imam Al Shafii aliowaacha Makkah.

1. Abu Bakr Al-Hamidi, Ibn A'bd Allah Al Zubair Al-Makki.
2. Abu Wahid Musa Ibn 'Ali al-Jarud Al-Makki.
3. Abu Is-hak Ibrahim Ibn Muhammad Ibn al 'Abbas Ibn' Uthman Ibn Shafi 'Al-Muttalibi
4. Abu Bakr Muhammad Ibn Idris.

Alipofika Iraq ilikua mwaka 195 *Al Hijr*, safari hii akiwa na upeo mkubwa zaid katika *I'lm* ambapo Wanazuoni wote walimkubali na kuwa chini ya mwamvuli wa *I'lm* yake. Katika kipindi hiki ndio Ahmad Ibn Hanbal na Is-haq Ibn Rawaeh ambae ndie Mwalimu wake Imam Bukhari wakajiunga nae ili kupata *I'lm* zaid kutoka kwake. Siku moja Yahya Ibn Ma'in alishangaa baada ya kumuona Ahmad Ibn Hanbal amesimama chini

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ya Imam Al Shafi'i akiwa amezuia vikanyagio vya farasi wakati Imam Al Shafi'i akiwa amekaa juu ya farasi, hapo Ahmad Ibn Hanbal akamwambia Yahya '**Ukiwa unataka kusoma *Fiqh*, njoo umzuilie kikanyagio chengine**' (Ibn Abdul Barr katika *Al-Intiqa*')

Siku moja pia Ahmad Ibn Hanbal alimkataza Yahya Ibn Mai'n ambae alikua akimkosoa Imam Al Shafi'i na kumwambia '**Macho yako hayajawahi kuona mtu kama Al Shafi'i, na hujui wala hufaham, Ewe Abu Zakaria maana ya maneno ya Al Shafi'i, na yule asiekifaham kitu, hukipinga!**'(*Ibn Abdul Barr katika Al-Intiqa*).

Imam Al Za`farani anasema, Imam Al Shafi'i alipokua Baghdad mwaka 195 *Al Hijr* alikua akipaka hina ndevu zake. Kila baada ya *Salat Al Fajr* Imam Shafi`i alikua akisomesha Wanafunzi wake *Qur'an* na *Tafsir* na Wanazuoni wengine walikua wakikaa na kusoma kutoka kwake. Mara tu baada kuchomoza jua Wanafunzi wa *Hadith* huingia na wa *Tafsir* huondoka baada ya hapo huingia Wanafunzi wa *Tafsir* na ufanunuzi wa *Hadith*, ambao hufuatiwa na utafiti wa kifalsafa (kalam) na halafu hufuatia Wanafunzi wa *Fiqh* kabla ya adhuhuri. Hivyo Imam Al Shafi'i hukaa zaid ya masaa sita akisomesha na kutoa *I'lm* tofauti alizokua nazo kwa Wanafunzi mbalimbali.

Imam Al Shafi'i na Ahmad Ibn Hanbal walikua Mwalimu na Mwanafunzi wake na pia walikua ni marafiki wakubwa sana. Ahmad Ibn Hanbal alikua akimpenda na kumsifu sana Imam Al Shafi'i kutokana na utukufu wake na *I'lm* ya hali ya juu na *Taqwa* aliyokua nayo. Siku moja Ahmad Ibn Hanbal alimualika Imam Al Shafi'i nyumbani kwake, wakala chakula cha usiku na Imam Al Shafi'i akala hadi akashiba halafu akaenda kupumzika katika chumba cha wageni.

Siku ya pili asubuhi mke wa Ahmad Ibn Hanbal akauliza '**Ya Ahmad! Kweli huyu ndie yule Al Shafi'i ambae kila siku unanisifia?**' Ahmad Ibn Hanbal akajibu '**Naam, ndie mwenyewe!**' Mke wa Ahmad Ibn Hanbal akajibu ***'Nimeona mambo matatu ambayo yanatia madoa katika sifa zake unazompa!*** **Kwanza, tulipomkaribisha chakula alikula sana! Pili alipoenda kulala chumba cha wageni alilala bila kusali *Tahajud!* Tatu aliposali pamoja nasi sala ya alfajiri, alisali bila ya kutia udhu! Sasa jee kweli huyu ndio yule umsifiae? Mbona anaonekana ana kasoro kasoro**'. Hivyo Ahmad Ibn Hanbal ikambidi amfuate Imam Al Shafi'i amuulize kuhusu hayo mambo matatu imekuaje?

Imam Al Shafi'i akamuelezea Ahmad Ibn Hanbal kama vile baba anavyomfahamisha mtoto wake na kumwambia '**Ya Ahmad! Nimekula hadi nikashiba kwa sababu nilijua kua chakula chako ni cha halali, na wewe ni mtu mwema na mkarimu, chakula cha mtu alie karimu ni Dawa na chakula cha mtu bakhili hudhuru kwani kina maradhi, hivyo nilikula sana si kwa sababu nishibe bali nilikula sana ili niondoe maradhi mwilini mwangu.**

Na sikusali sala ya *Tahajud* kwa sababu nilipoingia chumbani nilikuta *Qur'an* na vitabu vya *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* vimejaa tele mbele yangu, hivyo sikupata wakati wa kusali wala kulala kwani nilisoma na kupata majibu ya Fatwa 72 ambazo zitawanufaisha Waislam.

Na kuhusu *Salat Alfajir,* sikutia udhu kwa sababu sikuwahi kulala hivyo haikuwa na haja ya kutia udhu, nilisali na udhu wangu niliosalia jana *Salat al Isha.'* Majibu haya yalimridhisha na kumtosheleza Ahmad Ibn Hanbal..

Anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal, '**Sikuweza kufaham *Al Nasikh wal Mansukh* hadi pale niliposomeshwa na Imam Al Shafi'i**'.

Al Nasikh wa Mansukh maana yake kitu kimoja kukibatilisha chengine kama vile aya moja ya *Qur'an* kuibatilisha aya au *Hadith* moja kuibatilisha *Hadith* nyengine. Ibn Dunya anasema '**Nimemsikia, Abu Bakr Al Khallad akisema** '**Nimemsikia Ibn Mahdi akisema ninaomba katika kila mwishoni mwa sala yangu kumuombea Al Shafi'i** *''*.

Katika kipindi fulani mji wa Iraq kulitokezea na majadiliano na malumbano makubwa baina ya wafuasi wa *Madhhab* Abu Hanifa na wafuasi wa Imam Malik, hivyo Imam Al Shafi'i akajikuta yuko katikati ya mabishano hayo baada ya kuombwa na Imam Abd Rahman Ibn Mahdi Ibn Hasan Al Ambari aandike kitabu kinachoelezea kuhusu *Sharia'h* ya Kiislam au *Fiqh*, hivyo Imam Al Shafi'i akamuandikia ktabu kiitwacho *Al Risala* na kumpelekea.

Neno *Ar Risalah* maana yake ni 'Barua au Ujumbe' kitabu hiki kinaelezea masuala mbalimbali ya ki *Fiqh*. Ar Risala kilikua kitabu cha kwanza cha *Usul ul Fiqh* – Asili au Chanzo cha *Fiqh* kuandikwa na Mwanafiqh wakati wa uhai wake, kwani ilikua hamna kitabu kilichokua kikizungumzia kuhusu *Usul ul Fiqh,* kitabu hiki kilimpatia Imam Al Shafi'i jina la '**Baba wa Usul ul *Fiqh***'.

Imam Al Shafi'i alikiandika kitabu hiki katika njia ya kuelimisha, njia ya mahojiano na kwa maswali na majibu kikielezea Asili ya *Fiqh*; Ni nini *Sharia'h*? *Sharia'h* inatokana na vyanzo gani vya msingi? Vipi unaweza kuipata *Sharia'h*? vipi inawezekana kusuluhisha tofauti zilizomo ndani ya vyanzo vya msingi wa *Sharia'h*? Inawezekana vipi kuweka Shar'iah mpya? Vipi inawezekana kuibatilisha *Sharia'h* ya zamani? *Ar Risala* ya Imam Al Shafi'i inayajibu maswali hayo na mengineyo na kuelezea kwa mifano, na kwa *Sharia'h* za lugha ya kiarabu, kwa kupata faida zaidi tuangalie kwa juu juu jinsi Imam Al Shafi'i alivyoipanga *Al Risala*.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kwani Al Imam al Shafi'i alikianza kitabu chake cha Al Risalah kwa kuelezea hali waliyokua nayo *Bani Adam* kabla ya kuja Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, kua walikua wamegawika katika makundi mawili:

1. *Ahl al Kitab* 'Watu wa Kitabu'; au wafuasi walioteremshiwa vitabu na Allah *Subhanahu wa Ta'ala* na wakayabadilisha maandiko yake. Watu hawa wametumbukia kwenye kufuru na pia wakajaribu kuchanganya upotovu wao na ukweli walioshushiwa na Allah *Subhanahu wa Ta'ala*.
2. *Mushrikun na Kafirun*, wale ambao wanaabudu masanamu badala ya kumuabudu Allah *Subhanahu wa Ta'ala*.

Kisha Imam al Shafi'i akaendelea kwa kusema kua Allah amewaokoa *Bani Adam* kwa kuwatumia Mtume wa mwisho, na kumshushia kitabu chake, ili kiwaokoe kutoka katika upofu uliojaa kufru na kuingia katika nuru ya uongofu:

﴿وَإِنَّهُۥ لَكِتَٰبٌ عَزِيزٌ ۝ لَّا يَأۡتِيهِ ٱلۡبَٰطِلُ مِنۢ بَيۡنِ يَدَيۡهِ وَلَا مِنۡ خَلۡفِهِۦ تَنزِيلٌ مِّنۡ حَكِيمٍ حَمِيدٍ﴾

Wa-innahu lakitabun AAazeezun; La ya/teehi albatilu min bayni yadayhi wala min khalfihi tanzeelun min hakeemin hameedin (*Surat Fusilat 41:41-42*).

Tafsir: ***Na kwa kwa hakika, (hiki) ni kitabu kitakatifu, hakuna uongo unaoweza kuingia iwe kwa uwazi au kwa kificho. (kwani) kimeshushwa na kutoka kwa mwenye wingi wa hikma na mwenye kustahiki sifa zote njema.***

Kisha, Imam al Shafi'i akaelezea cheo cha *Qur'an* katika Uislam na uzito wa kauli zake kuhusu nini Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ameamrisha na nini amekataza, ni vipi *Bani Adam* anatakiwa amuabudu Mola wake, Malipo ya wale watakaomtii, Adhabu za wale watakaomuasi na jinsi alivyowaonya kwa kuwatolea mifano ya *Hadith* za watu waliotangulia.

Kisha, Imam al Shafi'i akawaelezea wale wanaotafuta *I'lm* ya Kiislam, kua wasome lugha ya kiarabu hususan sayansi ya utaalamu wa lugha iliotumika katika *Qur'an* na *Sunnah*, kwani ili kufahamu *Qur'an* na *Sunnah* unatakiwa ujue zaid ya kuzungumza kwa kiarabu, katika sehemu hii Imam al Shafi'i anazungumzia vyanzo vya tofauti katika mitazamo tofauti ambayo inatokana na lugha. Na akagusia maumbile ya lugha ya kiarabu ya *Qur'an* na *Sunnah* ambayo ni maumbile ya kiarabu ya dini ya Kiislam.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Allah *Subhanahu wa Ta'ala* anaelezea maumbile ya *Qur'an* kama '***Qur'an* ya kiarabu**' kama alivyosema:

﴿وَكَذَٰلِكَ أَنزَلْنَاهُ حُكْماً عَرَبِيّاً﴾

Wakadhalika anzalnahu hukman AAarabiyyan (*Surat Ar Rad 13: 37*)

Tafsir ***Na kadhalika tukaishusha Qur'an iwe Hukmu (yenye mamlaka kwa Kiarabu)***.

Hivyo, ufahamu wa *Qur'an* na dini yote ya Kiislam unahitaji ufahamu wa lugha ya kiarabu. Imam Al Imam Shafi'i anatilia mkazo hili pale aliposema: '**Kila Muislam anawajibu wa kujifunza lugha ya kiarabu kwa juhudi zake zote, ili aweze kutamka shahada kwa lugha hiyo' Hamna Mola anaestahiki kuabudiwa isipokua Allah, na Muhammad ni mtume wake', na pia kutamka yale yalio wajibu juu yake kama *takbir*, yale aliyoamrishwa, *tasbih, tashahhud* na mengineyo**'(*Ar Risala ukurasa wa 93*).

Hebu tujiulize kwa nini Imam Al Shafi'i akatilia mkazo kujifunza lugha ya kiarabu? Jawabu liko wazi pale tunapoangalia maneno ya *Qur'an* kua maumbile ya lugha ya kiarabu hayawezi kutenganishwa na dini, lugha ya kiarabu inatumika katika kila kitendo cha Ibada na sehemu zote zinazoweza kufikirika za Dini ya kiislamu. Hivyo Muislam anatakiwa ajifunze kiarabu sio tu kwa ajili ya kufanya Ibada bali pia kuifahamu dini yake kwa undani zaidi, kwani haiwezekani kuufahamu Uislam vizuri zaid bila ya kufahamu lugha ya kiarabu. Hivyo Waislam tunatakiwa tutilie mkazo kujifunza lugha ya kiarabu.

Mwishoni wa utangulizi wa *Al Risalah* Imam Al Shafi'i akasema: '**Hamna tatizo ambalo litakalomtokezea mfuasi yeyote yule wa Dini ya Allah *Subhanah wa Ta'ala,* isipokua kutakua na muongozo ndani ya kitabu cha Allah *Subhanahu wa Ta'ala* kumuelekeza katika njia iliyo sahih, kwani Allah *Subhanahu wa Ta'ala* amaesema**:

﴿الٓر كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ ٱلنَّاسَ مِنَ ٱلظُّلُمَاتِ إِلَى ٱلنُّورِ بِإِذْنِ رَبِّهِمْ إِلَىٰ صِرَاطِ ٱلْعَزِيزِ ٱلْحَمِيدِ﴾

Alif-lam-ra kitabun anzalnahu ilayka litukhrija alnnasa mina al*dhdh*ulumati ila alnnoori bi-idhni rabbihim ila sirati alAAazeezi alhameedi (*Surat Ibrahim 14:1*).

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir ***Alif-lam-ra (Hiki ni) Kitabu tumekuteremshia wewe, ili uwaongoze Bani Adam kutoka katika dhulma (kiza) kuwaingiza katika nuru, kwa ruhusa ya Mola wao, katika njia ya mwenye wingi wa utukufu, na mstahiki wa sifa zote njema***.

Na kisha akasema:

﴿وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ ٱلذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ﴾

Waanzalna ilayka aldhdhikra litubayyina lilnnasi ma nuzzila ilayhim walaAAallahum yatafakkaroona (*Surat An Nahl 16:44*).

Tafsir: ***Na tumekushuhia ukumbusho, ili uwaelezee wazi Bani Adam kile tulicho washushia, ili wawe ni wenye kutafakkar***.

Na pia:

﴿وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ ٱلْكِتَابَ تِبْيَاناً لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ﴾

Wanazzalna AAalayka alkitaba tibyanan likulli shay-in wahudan warahmatan wabushra lilmuslimeena. (*Surat An Nahl 16:89*).

Tafsir **:** ***Na tumekuteremshia kitabu kama ufafanuo wa kila kitu, na kama muongozo, na rehma na kuwabashiria wema Waislamu***.

Na pia:

﴿وَكَذٰلِكَ أَوْحَيْنَآ إِلَيْكَ رُوحاً مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنتَ تَدْرِى مَا ٱلْكِتَابُ وَلاَ ٱلإِيمَانُ وَلَـٰكِن جَعَلْنَاهُ نُوراً نَّهْدِى بِهِ مَن نَّشَآءُ مِنْ عِبَادِنَا وَإِنَّكَ لَتَهْدِيۤ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ﴾

Wakadhalika awhayna ilayka roohan min amrina ma kunta tadree ma alkitabu wala al-eemanu walakin jaAAalnahu nooran nahdee bihi man nashao min AAibadina wa-innaka latahdee ila siratin mustaqeemin. (*Surat Ash Shuraa 42:52*).

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: ***Na kadhalika, tumekushushia (wewe Muhammad) muongozo wa amri yetu. Hukujua wewe ni nini kitabu wala ni nini Iman, Lakini tumeijaalia (Qur'an) iwe nuru ambayo humuongoza tumtakae katika waja wetu, na Hakika utaongozwa katika njia iliyonyooka***.

Baada ya Utangulizi ikafuatia Sura inayoelezea *Al Bayan* au Ubainisho wa *Sharia'h*, kisha ukagaiwa katika Sura zinazoelezea dhumuni la *Qur'an* kuonesha mambo yenye umuhimu kisharia. Sura hizo zimegawika mara tano:

1. Zile ambazo Allah *Subhanahu wa Ta'ala* amezielezea kua ni hukmu maalum zilizotolewa ambazo hazihitaji ufafanuzi zaid ya maana iliokusudiwa. Aina hii ya *Al Bayan* haihitaji kuwekwa wazi na chochote isipokua na *Qur'an* yenyewe.
2. Zile ambazo *Qur'an* imetaja katika maandishi ambayo yanaweza kutafsiriwa kwa njia tofauti; na ambazo *Sunnah* inatoa ufafanuzi uliokusudiwa.
3. Zile ambazo zimeelezwa wazi kua ni wajib, na ambazo Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* kaelezea vipi, kwanini,wapi,kwa nani na wakati gani zitumike na wakati gani zisitumike.
4. Zile ambazo zimelezewa na Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, lakini hazikutajwa katika *Qur'an*. Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ameamrisha katika *Qur'an* kua Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi Wasalam* atiiwe na hukmu zake zikubaliwe. Hivyo yale ambayo ameyasema Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ameyasema kutokana na amri ya Allah *Subhanah wa Ta'ala*.
5. Zile ambazo Allah *Subhanahu wa Ta'ala* anataka viumbe wake wajaribu kufanya *Ijtihad*. Kutokana na ufahamu wa Imam Al Shafi'i hii ni *Qiyas*, ambayo ni njia ya kupata hukmu kisheria kutokana na msingi wenye ushahidi ambao ufahamu na ufanisi unaotakiwa hutumika.

Kisha Imam al Shafi'i akaendelea kufafanua aina tano hizo kila moja katika Sura yake, akatoa mifano na ushahidi katika kila aina anayoizungumzia. *Al Risalah* inazungumzia Sura zifuatazo pia:

- Sura ya dhumuni kuu linalobainishwa ndani ya *Qur'an* limekusudiwa kuwa ni la Ujumla (*'Amm-kwa watu wote)*, lakini lina Upekee Maalum (*Khass-kwa watu Maalum).*
- Sura ya dhumuni kuu la dhahir la *Qur'an* ambalo ndani yake ni la Ujumla na la Kipekee.
- Sura ya dhumuni kuu la dhahir la *Qur'an* ambalo linaonekana kua ni la Ujumla lakini limekusudiwa maalum liwe la Kipekee.
- Sura ya *Al Bayan* katika *Qur'an*, kwa njia ambayo imefafanuliwa kwa upana.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

- Sura ya *Al Bayan* katika *Qur'an* kwa maneno ambayo yanaoneshea maana iliyojificha *al Batin* kuliko iliokua dhahir *al Dhahir*.
- Sura ya *Qur'an*, kua imeshushwa kama kwa Ujumla lakini *Sunnah* inaonesha imekusudiwa maalum kwa Upekee.

Katika Sura zilizotajwa juu Imam al Shafi'i anafafanua kukubalika kwa *Sunnah* kama ushahidi na mamlaka yake katika dini. Kwa sababu hiyo akazungumzia Sura zifuatazo pia:

- Wajibu uliowekwa na Allah *Subhanahu wa Ta'ala* kufuata *Sunnah* za Mtume wake Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*.
- Amri za Allah *Subhanahu wa Ta'ala* zinazotuamrisha kumtii Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* zinajumlisha na utiifu kwa Allah *Subhanahu wa Ta'ala* na zimeamrishwa kwa kujitegemea.
- Mambo ambayo Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ametuamrisha kuyatii kwa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam.*
- Vipi Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ameweka wazi kua Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* aliwajibika kufuata kile alichoshushiwa na kutii amri alizoamrishwa. Na kua Allah *Subhanahu wa Ta'ala* atamuongoza yeyote yule atakaemfuata.

Katika Sura hii, Imam Al Shafi'i anathibitisha kua sehemu ya *Sunnah* ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* inasimamia na inahusiana na *Qur'an*, lakini sehemu nyengine zimeelezea mambo ambayo hayana uhusiano wa maandiko katika *Qur'an*.

Imam Al Shafi'i alionesha pia kua *Sunnah* inajitegemea na haitegemei *Qur'an*, na akanukuu ushahidi kuwadhihirishia wale wasiokubaliana nae katika jambo hilo kwa kusema: '**Nitaelezea kuhusu kile ambacho nimeshasema kuhusu *Sunnah*, kama ikiwa inaihusisha *Qur'an* au inatupa maelekezo zaidi katika kutoa hukmu za mambo ambayo hayakutajwa ndani yake; na hili litaelezea kile nilichokwisha zungumzia hapo juu, In-shaa Allah, kwanza nitazungumzia kuhusu *Sunnah* kwa kutegemeana na kitabu cha Allah, kwa kuangalia njia za kupunguza hoja, katika mada inayohusiana na *Sunnah* na ubatilishwaji *Al Nasikh* na kilichobatilishwa *Al Mansukh* katika aya za *Qur'an*.**

Baada ya hapo, nitataja; Mambo ya *Fardh* yaliyoainishwa ndani ya *Qur'an* na *Sunnah*, kuhusu mambo hayo; Mambo yaliyofardhishwa kwa Ujumla ambayo Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ameyafanya ya kipekee kutokana na uainisho wa maelezo yake, kuhusu kipekee kivipi na wakati gani; Maandiko ya Ujumla ambayo yamekusudiwa kua ya Ujumla, na maandiko ya Ujumla ambayo

yamekusudiwa kua ya Upekee; na mwisho, *Sunnah* za Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam* ambazo hazina mamlaka ya kimaandiko kutoka katika kitabu cha Allah *Subhanahu wa Ta’ala.*’

Baadae inafuata Sura inayozungumzia Asili ya *Al Nasikh wal Mansukh* ambayo inaelezea kua Allah *Subhanahu wa Ta’ala* ametumia ubatilisho ili kurahisisha *Sharia’h* iwe nyepesi. Ukiangalia sura hii, itaingia akilini kwako tofauti baina ya vitabu vya dini vilivyotangulia na *Qur’an*. Ndani ya *Qur’an* na *Sunnah* kuna sehemu ambazo maneno ya zamani yamebatilishwa na maneno mapya. *Qur’an* iliteremshwa kwa kipindi cha miaka 23, hivyo baadhi ya amri zilishuka mwanzo kuliko nyengine, na hivyo zilibatilishwa na amri zilizoshuka baadae katika kushukua kwa *Qur’an*. Mmoja kati ya mifano aliyoigusia Imam Al Shafi’i ni kuhusu *Qiblah*. Allah *Subhanahu wa Ta’ala* anasema:

﴿سَيَقُولُ ٱلسُّفَهَآءُ مِنَ ٱلنَّاسِ مَا وَلَّىٰهُمْ عَن قِبْلَتِهِمُ ٱلَّتِى كَانُوا۟ عَلَيْهَا قُل لِّلَّهِ
ٱلْمَشْرِقُ وَٱلْمَغْرِبُ يَهْدِى مَن يَشَآءُ إِلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ﴾

Sayaqoolu alssufahao mina alnnasi ma wallahum AAan Qiblahtihimu allatee kanoo AAalayha qul lillahi almashriqu waalmaghribu yahdee man yashao ila siratin mustaqeemin. (*Surat Al Baqara 2:142*)

Tafsir :‘***Watasema wajinga (Makafir, Wanafiq, Mayahudi) miongoni mwa watu ‘Ni kipi kilichowageuza kutoka katika Qiblah chao walichokua wakikielekea walipokua wakisali’ Sema ewe Muhammad! ‘Allah ndie mmiliki wa Mashariki na Magharibi. Humuongoza amtakae katika njia iliyonyooka’’***

Ayah hii inamaanisha kua Waislam wakati wa kusali walikua wanaelekea *Qiblah* chengine na baadae muelekeo ukabadilishwa kuelekea *Qiblah* chengine ambacho kimetajwa katika aya inayofuatia:

﴿قَدْ نَرَىٰ تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِى ٱلسَّمَآءِ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا فَوَلِّ وَجْهَكَ
شَطْرَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنتُمْ فَوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُۥ وَإِنَّ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟
ٱلْكِتَٰبَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ ٱلْحَقُّ مِن رَّبِّهِمْ وَمَا ٱللَّهُ بِغَٰفِلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ﴾

Qad nara taqalluba wajhika fee alssama-i falanuwalliyannaka qiblatan tardhaha fawalli wajhaka shatra almasjidi alharami wahaythu ma kuntum fawalloo wujoohakum shatrahu wa-inna alladheena ootoo alkitaba layaAAlamoona annahu alhaqqu min rabbihim wama Allahu bighafilin AAamma yaAAmaloona (*Al-Baqarah 2:144*)

Tafsir ***: 'Kwa hakika! Tumeona (Ewe Muhammd) muelekeo wa uso wako kuelekea Mbinguni, Hakika tutakuelekeza katika Qiblah ambacho kitakuridhisha. Hivyo geuzia uso wako kuelekea Al Masjid Al Haram. Na kokote kule mliko basi geuzeni Nyuso zenu katika muelekeo huo. Kwa hakik wale waliopewa Kitabu wanajua kua (kugeuzia kwenu muelekeo kuelekea Al Kaabah) Haki kutoka kwa Mola wao na Allah hakughafilika na wanayoyafanya.'***

Ayah hii imewafardhishia Waislam kusali na kuielekea *Al Kabah*, hivyo imeibatilisha amri iliyopita.

Imam Al Shafi'i ameonesha umuhimu wa kuwa na ushahidi unaonesha hukmu iliopita kubatilishwa na hukmu iliyofuata, na kwa kuangalia aya tu basi haitoshelezi kukuwekea wazi na kumfanya mtu aamue kua kuna batilisho.

Imam Al Shafi'i akaonesha katika *Ar Risala* kua ni aya ya *Qur'an* pekee ndio yenye uwezo wa kuibatilisha aya nyengine ya *Qur'an*, akitoa mifano mingi ikiwemo:

﴿وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالَ ٱلَّذِينَ لاَ يَرْجُونَ لِقَآءَنَا ٱئْتِ بِقُرْآنٍ غَيْرِ هَـٰذَآ أَوْ بَدِّلْهُ قُلْ مَا يَكُونُ لِيۤ أَنْ أُبَدِّلَهُ مِن تِلْقَآءِ نَفْسِيۤ إِنْ أَتَّبِعُ إِلاَّ مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ إِنِّيۤ أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ﴾

Wa-idha tutla AAalayhim ayatuna bayyinatin qala alladhina la yarjoona liqaana i/ti biqur-anin ghayri hadha aw baddilhu qul ma yakoonu lee an obaddilahu min tilqa-i nafsee in attabiAAu illa ma yooha ilayya innee akhafu in AAasaytu rabbee AAadhaba yawmin AAadhimin. (*Surat Yunus 10:15*)

Tafsir: '***Na wanaposomewa aya zetu zilizowazi, wale ambao wasiotarajia kukutana nasi husema 'Tuleteeni Qur'an nyengine badala ya hii au ibadilisheni'. Ewe Muhammad, sema: 'Sio juu yangu kuibadilisha jinsi nitakavyo; mimi nnafuata kile nilichoteremshiwa, Hakika mimi nnakhofia ikiwa nitamuasi Mola wangu, adhabu ya siku ya kufufuliwa''***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Allah *Subhanahu wa Ta'ala* hakumpa uwezo Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* kuibadilisha *Qur'an* kama anavyotaka yeye, bali amemuamrisha kufuata kile alichoteremshiwa, katika aya hiyo hapo juu, maneno yasemayo '**Sio juu yangu kuibadilisha jinsi nitakavyo**', yanathibitisha kua ni *Qur'an* pekee ndio iwezayo kuibatilisha *Qur'an*. Hamna katika viumbe wa Allah *Subhanahu wa Ta'ala* awezae kukibatilisha kitabu chake.

Uthibitisho wa hayo ni katika aya zifuatazo:

﴿مَا نَنسَخْ مِنْ آيَةٍ أَوْ نُنسِهَا نَأْتِ بِخَيْرٍ مِّنْهَا أَوْ مِثْلِهَا أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾

M<u>a</u> nansakh min <u>a</u>yatin aw nunsih<u>a</u> na/ti bikhayrin minh<u>a</u> aw mithlih<u>a</u> alam taAAlam anna All<u>a</u>ha AAal<u>a</u> kulli shay-in qadeerun (*Surat A Baqara 2:106*)

Tafsir :'***Kwa kila aya tuliyoibatilisha ama kuisababisha isahaulike, basi tunaleta aya bora zaid yake au mithili yake. Jee hamjui kua Allah ni mwenye uwezo wa kila kitu?***'.

Na vile vile akasema:

﴿يَمْحُو ٱللَّهُ مَا يَشَآءُ وَيُثْبِتُ وَعِندَهُ أُمُّ ٱلْكِتَابِ﴾

Yam<u>h</u>oo All<u>a</u>hu m<u>a</u> yash<u>a</u>o wayuthbitu waAAindahu ommu alkit<u>a</u>bi (*Surat Ar Rad 13:39*)

Tafsir: ***Allah hubadilisha kile akitakacho, na huthibitisha; Yeye ndie mmiliki wa Ummu ul Kitab'***

Hata *Hadith Mutawatir* (*Hadith* ambayo imenukuliwa na idadi kubwa ya watu kiasi ya kua kutokana na idadi hiyo ya walionukuu haiwezekani kua wamekubaliana wadanganye wote kwa pamoja) haiwezi kuibatilisha aya ya *Qur'an*, na hii ni moja kati ya mahitimisho mengi yanayojifafanua ya Imam Al Shafi'i.

Imam Al Shafi'i pia akatoa hukmu nyengine kua ni *Sunnah* tu ndio inaweza kuibatilisha *Sunnah* nyengine. *Sunnah* ni tofauti na vitu vyengine vinavyotokana na *Bani Adam* kwani yule anaefuata *Sunnah*, hufuata kutokana na kuamrishwa na *Qur'an*.

Hivyo hakuna kitu chengine kinachotokana na *Bani Adam* kinachoweza kuibatilisha *Sunnah*. Ikiwa aya fulani ya *Qur'an* imeibatilisha *Sunnah* fulani, basi ni lazima iwepo *Sunnah* nyengine ambayo inathibitisha kubatilishwa kwa hiyo *Sunnah* nyengine.

Anasema Imam Al Shafi'i kua kuhusu kubatilishwa kuko wazi: '**Ikiwa Allah *Subhanah wa Ta'ala*, alimshushia Mtume wake *Salallahu A'layhi wa Salam*, hukmu ambayo Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ameitoa katika *Sunnah* tofauti na vile ilivyosema *Qur'an*, basi Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* bila ya kukawia angelitoa *Sunnah* nyengine ili kuthibitisha hukmu yeyote ile aliyotumiwa na Allah *Subhanahu wa Ta'ala*** '. (*Al-Risala*)

Imam Al Shafi'i kisha akaelezea inawezekana mtu akauliza swali; **Jee kuna *Sunnah* ambayo imebatilishwa na *Sunnah* nyengine ambayo haijatufikia sisi?, ambapo akafafanua kua jambo hilo haliwezekani kutokea kwa sababu, ikiwa mtu atakua na mtizamo huo basi mtu huyo anaweza kuikataa *Sunnah* yote, kwa kudai kua imebatilishwa na pia hiyo iliyobatilisha bado haijatufikia sisi. Na kua pia si sahihi kudai kua *Sunnah* iliyobatilishwa imeshatufikia wakati iliyobatilisha haipo**.

Baada ya hapo akaelezea Fardhi za Sala na ufafanuzi katika *Qur'an* na *Sunnah* kuhusu wale ambao wameruhusiwa kutosali, na wale ambao Sala zao hazikubaliwi kutokana na baadhi ya maasi ambayo huenda waliyafanya.

Kisha Imam Al Shafi'i akaandika yale yaliyobatilisha na yaliyobatilishwa ambayo yameoneshwa na *Sunnah* na *Ijma'a*;

- Ya Wajib ambayo Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ameyaweka katika maandishi ya *Qur'an*,
- Ya Wajib yaliyowekwa ndani ya maandishi ya *Qur'an* ambayo pia Nabii Muhammad Salallahu A'layhi wa Salam ameyazungumzia ndani ya *Sunnah*.
- Ya Wajib yaliyowekwa ndani ya maandishi ya *Qur'an* ambayo *Sunnah* imeyaonesha kua yamekususidwa kwa kitu maalum.
- Ya Wajib kwa ujumla ambayo yako wazi kua ni wajib na ambayo Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ameelezea yafanywe vipi kama Sala, Hija, Zakah, idadi ya wake, wanawake ambao mwanamme haruhusiwi kuwaoa na vyakula vilivyoharamishwa.

Katika Sura iliyofuata Imam Al Shafi'i akazungumzia kasoro za *Hadith* na kuelezea kua kupingana kwa *Hadith* kunatokana na sababu mbali mbali. Akazielezea baadhi ya sababu hizo, kwa mfano kupingana kunaweza kutokea kwa sababu *Hadith* moja ilibatilishwa na *Hadith* nyengine au kwa sababu yalitokea makosa katika kunukuu *Hadith*. Akaelezea makosa ambayo yaliweza kusababisha kupingana kwa *Hadith*, na

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

sababu nyengine zaid za kusababisha kupingana huko. Kisha akazungumzia mambo tofauti yaliyokatazwa na akaelezea kua baadhi ya *Hadith* zinazifafanua *Hadith* nyengine Imam Al Shafi'i pia aliingiza Sura inayozungumzia *I'lm*, na kuelezea kua kuna aina mbili za *I'lm*.

Ya kwanza ni ile *I'lm* ambayo ya kawaida ambayo kila mtu mzima mwenye akili anakua nayo. Aina yote ya *I'lm* hii inaweza kuonekena imetajwa katika maandishi ya *Qur'an*, na kila Muislam anajua kila kitu kuhusu *I'lm* hiyo kwa sababu imeshapitishwa kwa Mitume kwa kila kizazi kilichofuatia. Hamna kupingana kuhusu uhalisi wa *I'lm* hii, na kila mtu anakubaliana nayo. Hakika, maumbile ya *I'lm* hii ni kua haiwezi kua na makosa katika kuisambaza au kutafsir.

Aina ya pili ya *I'lm* ni ile ambayo ina maelezo ya shina la majukumu, na sheria maalum zinazohusiana nayo. Hizi hazijatajwa katika maandishi ya *Qur'an*, na nyingi zao hazikutajwa katika maandishi ya *Sunnah*, mbali na *Hadith* ambazo zimehadithiwa na mtu mmoja mmoja, *Ahad*.

Hivyo Imam Al Shafi'i akatambulisha somo jipya, *Hadith* ya mtu mmoja, *Khabar al Wahid*. Imam al Shafi'i akaelezea nini maana ya neno hili, na masharti ambayo huonesha kua kama kweli *Hadith* au si kweli *Hadith* ni ya mhadithiaji mmoja. Tofauti baina ya ushahidi na ku*Hadith*ia (*Shahadah na Riwaya), akayaelezea yale mambo ambayo yanaweza kukubalika kupitia kwa Hadith ya mtu mmoja na yale mambo ambayo hayakubaliki kwa Hadith ya mtu mmoja.*

Kisha Imam Al Shafi'i akazungumzia mamlaka ya *Khabr al Wahid*, na kama *Hadith* hizo zinaweza kuchukuliwa kama ushahidi. Hitimisho lake, likiungwa mkono na kila hoja madhubuti, ni kua zinaweza kuchukuliwa. Miongoni mwa mifano hiyo ni pamoja na mfano wa Abd Allah Ibn Umar aliposema '**Tulikua tukifanya *mukhabara* (kukodisha ardhi ya kilimo kutokana na makubaliano maalum an kugawana mavuno), tukiona hamna madhara ndani yake hadi pale [Rafii Ibn Khadij] aliposema kua Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* amekataza. Hivyo tukawacha kufanya hivyo kutokana na alivyosema [Rafii]**'. Ingawa Ibn Umar alikua akipata faida kutokana na *mukhabara*, lakini hakuendelea tena kufanya hivyo baada ya kupata habari ya mtu anaeaminika kuhusiana na kukatazwa kwake na Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*.

Mfano mwengine muhimu ni kuhusiana na amri ya kubadilisha muelekeo wa *Qiblah* kutoka Jerusalem kuelekea Makkah. Amri iliwafikia watu wa *Quba* (Waislam wa mwanzo walioko katika mji wa *Quba* karibu na Madinah) na kutokana na *Khabr al Wahid*, habari ya mtu mmoja tu, basi bila kusita wakabadilisha muelekeo wa *Qiblah* na

kuilekea *Al Kaabah*. Hivyo Imam Al Shafi'i akafanikiwa katika kushinda hoja zote za waliokua wakimpinga kuhusu jambo hili.

Kisha zikafuatia Sura Zifuatazo:-

- Kuhusu *al Ijma'a*: Maana yake na Mamlaka yake Kisharia.
- Kuhusu *al Qiyas*: Maana yake na Maumbile yake, kuhitajika kwake, aina zake, na nani anaweza na asieweza kutumia *Qiyas*.
- Kuhusu *Ijtihad* : Kwa nini kwanza ikategemea katika *Qur'an,* kisha katika *Sunnah*; na nini kinachangia *Ijtihad* kuwa sahih na kutokua sahih.
- Kuhusu *al Istihsan*, Mapendekezo ya Mwana *Sharia'h ya kuwacha ushahidi dhaifu ulio wazi, na kuchukua ushahidi wenye nguvu uliofichika*: Imam al Shafi'i alikua muangalifu katika kuelezea kua Muislam yeyote haruhusiwi kutumia *al Istihsan* ili kuenda kinyume na *Hadith*, au kutoa Fatwa ambayo haijategemea katika *Qur'an, Sunnah, al Ijma'a* au *al Qiyas*. Na pia akaelezea tofauti ya *al Qiyas* na *al Istihsan*.
- Kuhusu kutofautiana baina ya Wanazuoni: Imam Al Shafi'i akaelezea kua tofauti hizi ziko aina mbili; Aina ya tofauti ambayo imekatazwa na aina ya tofauti ambayo imeruhusiwa. Aina ya tofauti ambayo zimekatazwa ni zile zinazohusu mambo ambayo Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ameyaweka wazi katika ushahidi wa *Qur'an* na *Sunnah*. Na tofauti ambayo inaruhusiwa ni kuhusu mambo ambayo yanaweza kutafsiriwa katika njia tofauti na ambayo kila Mwanazuoni akatafsir kutokana na ufahamu wake. Al Imam al Shafi'i akatoa mifano ambayo Masahaba walitofautiana, kama vile kuhusu '*Iddah*, kiapo na urithi. Katika Sura hii, Imam Al Shafi'i akaelezea njia zake anazotumia katika kupendelea maoni ya Sahaba pale walipo khitilafiana.

Al Risalah ikahitimisha kwa kuelezea maoni ya Imam Al Shafi'i juu ya '**Makundi ya ushahidi au vithibitisho**' aliyoyataja hapo juu:

'**Tunasimamisha Hukmu zetu, kwanza kwenye Qur'an na *Sunnah* inayokubalika na wote ambayo hakuna khitilafu kuhusu hilo na tunasema: 'Hii ndiyo hukmu yetu baada ya kuyaangalia yaliyowazi na yaliyojificha katika maana ya maandiko haya.' Halafu. Ikibidi kuangalia *Hadith* ambayo imehadithiwa na baadhi ya watu na hamna makubaliano, tunasema, tunaikubali *Hadith* kama ilivyo, lakini tunajua kua inaweza ikawa ina makosa yaliyojificha katika walioihadithia'. Baadae tutaangalia katika '*Ijma'a,* halafu utaangalia Al *Qiyas. Al Qiyas* ni dhaifu kuliko *Ijma'a* na hutumika tu pale itakapobidi kwa sababu si halali kutumia *al Qiyas* wakati kuna *Hadith* inavyozungumzia jambo husika**.'

Imam al Zarkashi anasema katika *Al Bahr al Muhit* kua, Imam Al Shafi'i ni mtu wa mwanzo kuandika kuhusu *Usul ul Fiqh*. Aliandika *Risalah*, *Ahkam al Qur'an* (Hukmu za kutafsir *Qur'an*), *Ikhtilaf al Hadith* (*Hadith*i zinazopingana), *Ibtal al*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Istihsan (Mapendekezo yasiyokubalika kisheria), *Jima' al 'Ilm*, na *al Qiyas* (Kiyasi) - Na kitabu alichozungumzia kuhusu kundi la Mu'tazilah, na kubadilisha mawazo yake kuhusu kukubali ushahidi wao. Baada ya hapo na wengine wakamfuatia kuandika vitabu vya Usul. Imam Al Shafi'i pia alikua ni mwanamashairi mkubwa. Mashairi yake mengi yamekusanywa na kuchapishwa katika kitabu kinachoitwa '***Al Diwan Imam Al Shafi'i***'.

Imam Al Muzani alisema '**Nimeiangalia *Ar Risala* ya Imam Al Shafi'i kwa miaka khamsini, lakini sikumbuki hata mara moja ambapo niliiangalia nikakosa kupata manufaa mapya zaid.**' Ibn Rahuyah anaelezea alivyomuona Imam Al Shafi'i Makkah kua alikua amevaa nguo nyeupee akiwa na ndevu nyeusii. Ibrahim Ibn Buranah alisema: '**Ash-Shafi'i alikua si mtu wa maskhara, mrefu na mwenye busara**'.

Yunus Ibn Abi Ya`la anasema: '**Kila wakati ambao al-Shafi`i akitoa tafsir ya *Qur'an*, alikua kama mtu aliekuwepo na kushuhudia iliposhushwa aya hiyo anayoitafsiri.**' Ahmad Ibn Hanbal pia alisema: '**Hamna Mwanazuoni wa *Hadith* ambae anagusa wino au kalamu isipokua anadaiwa deni kubwa na Al Shafi`i.**'

Anasema Imam Bayhaqi kua amesoma kutoka kwa Muhammad Ibn Al-Husayn As-Sulami aliemsikia Muhammad Ibn A'bd Allah Ibn Shaadhaan ambae amesema alimsikia Abil Qaasim Ibn Mani' akisema kua Ahmad Ibn Hanbal amesema, '***Fiqh* ilikua nzito, ngumu (*Thaqeela*) juu ya watu hadi pale Allah alipoifungua kupitia kwa Al Shafi'i**.' Alisema tena Ahmad Ibn Hanbal '**Kama si Al Shafi'i, tusingeliijua *Fiqh* ya *Hadith***'.

Alipoondoka Baghdad Imam Al Shafi'i alisema '**Nimeondoka Baghdad na sikiwacha mtu mwenye utukufu (*Afdal*), aliesoma (*Alim*) na mwenye *I'lm* ya *Fiqh* (*Afqah*) kuliko Ahmad Ibn Hanbal**'.

Wanafunzi wakubwa wa Imam Al Shafii aliowawacha Iraq - Nguzo za Al Qawl Al Qadim.

1. Abu A'bd Allah Ahmad Ibn Hanbal.

2. Abu Ali al-Hasan Ibn Muhammad Al Zafarani ambae alikua ni mfuasi wa *Madhhab* ya Abu Hanifa lakini baada ya kukutana na Imam Al Shafi'i akawa ni mfuasi wa Al Shafii. Huyu ndio nguzo ya *Qawl Al Qadim* katika *Madhhab* ya Al Imam Al Shafii.

Siku moja Imam Al Shafii wakati akiwa amekaa yeye na Ahmad Ibn Hanbal, Abu Thawr na Al Zafarani. Imam Al Shafi'i alimpa Al Zafarani kitabu cha Al Risala akisome, na baada ya kukisoma, Imam Al Shafii akamuuliza Al Zafarani '**Jee**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

wewe unatokana na kabila la Waarabu gani?'. Al Zafarani akajibu : '**Mimi si Muarabu. Mimi natoka katika kijiji cha Zafaraniyyah**'. Imam Al Shafi'i '**Basi wewe ndie Kiongozi wa Kijiji hicho.**'

3. Abu Thawr Ibrahim Ibn Khalid Al Kalbi ambae alikua ni mfuasi wa *Madhhab* ya Abu Hanifa lakini baada ya kukutana na Imam Al Shafi'i akawa ni mfuasi wa Imam Al Shafi'i.

4. Al-Harith Ibn Al Naqqal Suraij.

5. Abu Ali Al Husayn Ibn Ali Al Karabisi ambae alikua ni mfuasi wa *Madhhab* ya Abu Hanifa lakini baada ya kukutana na Imam Al Shafi'i akawa ni mfuasi wa Imam Al Shafi'i

6. Abu Abd RahmanAhmad Ibn Yahya Al Mutakallim.

7. Abu Zayd Abd Al Hamid Ibn Al Walid Al Misri.

8. Al Husayn Al Qallas.

9. Abd al 'Aziz Ibn Yahya Al Kannani.

10. Ali Ibn A'bd Allah Al Mudaiyini.

Maisha ya Imam Al Shafii Nchini Misri: Alisema Al Imam Al Shafi'i. '**Kamwe sikuwahi kuuogopa umasikini, Kutafuta zaidi ya kile unachokihitaji katika Dunia ni adhabu ambayo Allah *Subhanahu wa Ta'ala* anayowaadhibia *Ahlu Tawhid* (Watu wanomuamini Mungu mmoja)**'

Mwaka 199 *Al Hijr* Imam Al Shafi'i alipewa wadhifa wa Qadhi wa Baghdad na *Khalifah* Al Ma'mun lakini akaukataa na kuamua kuhama Baghdad, na kurudi Makkah na kisha kuelekea Misri. Katika maisha yake yote Imam Al Shafi'i alikua mtu wa kutafuta na kutoa *I'lm*. Hivyo kuhama kwake Iraq na kuhamia kwake Misri ilikua ni kwa ajili ya *I'lm*, kwani Misri kulikua na baadhi ya Wanafunzi wa Imam Malik na pia walikuwepo Wanafunzi wa Imam Al Layth Ibn Saad ambae Imam Al Shafi'i alikua hajapata *I'lm* iliyotoka kwake, Imam ambae alikua yuko juu katika *I'lm* ya *Hadith* kuliko Imam Malik.

Imam Al Layth Ibn Saad Ibn Abdul Rahman Al Fahmi alizaliwa katika mwaka 94 *Al Hijr* katika maeneo ya Qarqashanda, eneo ambalo liko umbali wa kilomita 22 kutoka katika mji wa Fustat nchini Misri. Imam Al Layth alisoma kwa Mwanafunzi wa Sahaba

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

A'bd Allah Ibn Umar, ambae ni Muhammad Ibn Muslim Ibn Ubaydullah, Ibn Shihab Al-Zuhri, Ibn Ajlan, Ata Ibn Rabah, Ibn Abi Malika, Naafi', Ad Daylami na wengineo wengi.

Alisema Imam Al Shafi'i, '**Al Layth alikua na *I'lm* kubwa ya *Hadith* kuliko Imam Malik, lakini Wanafunzi wake waliitupa *I'lm* yake**'. Imam Al Layth alikua anaitwa Imam Mkuu wa Misri. Watu wa Misri walikua wakiacha kutii amri za *Khalifah* Mansour, lakini wakawa wanatii amri za Imam Al Layth, kiasi ya kwamba *Khalifah* Mansour alitaka kumteua awe Gavana wa Misri lakini Imam Al Layth akakataa.

Imaam Al Layth alisifika kutokana na Wanazuoni wenzake kua alikua mjuzi wa *Hadith* na anaeaminika katika *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*. Alianza darsa yake kwa kuwasomesha watu msikitini. Na mara akawa maarufu sana na Wanafunzi wake walikuja kutoka sehemu tofauti za dunia kuja kwake kusoma. Alikua akiigawa siku yake katika sehemu nne:

- Kipindi cha kuzungumzia mambo na vitendo vya Viongozi wa Misri. Imam Al Layth alikua akiheshimika na kuaminika kwa *Khalifah* kiasi ya kua kama Sultan au Hakim wa Misri atafanya kosa kisha Imam Al Layth akamtaarifu *Khalifah* kuhusu kosa hilo basi kiongozi huyo husimamishwa kazi.
- Darsa ya kusomesha *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*.
- Darsa ya kujibu maswali ya Dini.
- Kipindi cha kuwahudumia matatizo ya maskini na wenye shida. Imam Al Layth alikua hakatai kutoa msaada.

Imam Al Layth Ibn Saad alikua pia ni miongoni mwa Walimu wa Imam Al Shafi'i kupitia kwa Wanafunzi wake. '***I'lm* ipo chini ya misingi mitatu. Imam Malik, Imam Al Layth na Imam Sufyan Ibn Uyaynah**' alisema Imam Al Shafi'i. '**Al Layth ana kiasi kikubwa cha *I'lm* (*Kathir Al I'lm*) na *Hadith* zake ni Sahihi**', alisema Imam Ahmad Ibn Hanbal, na Al 'Alaa Ibn Kathir alisema; '**Al-Layth Ibn Sa'd ni kiongozi wetu, Imaam wetu na Mwanazuoni wetu.**' Imam Al-Layth alifariki siku ya Ijumaa katikati ya mwezi wa Shaban mnamo mwaka 175 *Al Hijr* na alizikiwa Cairo.

Baada ya kuhamia Misri, Imam Shafi'i alikua amechanganya sifa za kipekee za *Mujtahid* mkubwa katika historia ya Ahlu *Sunnah Wal Jamaah* kwa sababu ya kupata *I'lm* ya skuli mbali mbali za *Fiqh* na kujua tofauti na pia uimara na udhaifu wa skuli hizo. Akawa anasomesha katika Masjid Amr Ibn Al Aas, ambapo alitoa Wanazuoni wakubwa na wenye kutajika. Alipokua Misri akapata changamoto ambazo zilimfanya abadilishe mitazamo katika baadhi ya Fatwa ambazo alizitoa kabla kuhamia Misri.

Fatwa hizi mpya zinajulikana kama *Al Qawl al Jadid* (Kauli au Mitizamo mipya), miongoni mwa Wanafunzi wa Imam Al Shafi'i waliopokea *Al Qawl Al Jadid* ni Al-Buwayti, Al-Muzani, Al Rabi` Al Maradi, na Al Bulqini katika kitabu cha *Kitab al-Umm* (Kitabu Mama). Na miongoni mwa Wanafunzi wake waliopokea Fatwa za zamani ni Ahmad Ibn Hanbal, Al Karabisi, Al Za`farani na Abu Thawr, katika kinachoitwa *Kitab al-Hujja* ('Kitabu cha Uthibitisho').

Imam Al-Shafi`i alikua ni mwenye kupita katika njia za Salaf, hivyo alikua akikataa kutafsiri aya yeyote au *Hadith* ambayo ilikua inagusia *Sifat wal Asma ul Husna* au sifa na Majina ya Allah *Subhanahu wa Ta'ala* alikua akifanya *Tafwîd al-mi`na* (kuacha kuelezea maana ya kitu) kama inavyojieleza katika kauli yake pale aliposema kua: '**Ninawacha *Tafsir* ya maana za aya zenye Sifa za Allah *Subhanahu wa Ta'ala* kwa Allah mwenyewe, na ninawacha *tafsir* ya maana za *Hadith* zenye Sifa za Allah kwa Mtume wak**e'. Hata hivyo, mara chache sana unaweza kupata tafsir za ina hiyo kutoka kwake, kama vile anavyosema Imam Al-Bayhaqi, amesema Imam Al-Muzani kua Imam Al Shafi`i amesema kuhusu aya ya *Surat al Baqara* (2:115) kua:

﴿وَلِلَّهِ ٱلْمَشْرِقُ وَٱلْمَغْرِبُ فَأَيْنَمَا تُوَلُّوا۟ فَثَمَّ وَجْهُ ٱللَّهِ إِنَّ ٱللَّهَ وَاسِعٌ عَلِيمٌ﴾

Walillahi almashriqu waalmaghribu faaynama tuwalloo fathamma wajhu Allahi inna Allaha wasiAAun Aaaleemun *(Surat al Baqara 2:115)*

Tafsir: ***Na Hakika Allah ni mmiliki wa Mashariki na Magharibi na upande wowote ule mtakaoelekea, kuna Wajh (muonekano) wa Allah*. *Hakika Allah ni mwenye kujitosheleza kutokana na mwenye kujua kila kitu***'

'**Maana yake ni kua *Allahu Aa'alam* (Allah anajua zaid) – Huu, ndio upande ambao Allah amekuelekezeni.'**, *Al Hakkari* anasema katika kitabu chake cha *Aqida al Shafi'i* kua amesema Imam Al Shafi'i kua '**Tunazikubali Sifa hizo, na tunazikanusha kutokana na kufananishwa baina yake na viumbe wake (*al tashbih*), kama alivyozikanusha mwenyewe kwa kusema katika *Surat Ash Shuara* :**

﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَىْءٌ﴾

Laysa kamithlihi shay-un *(Surat As Shuara 42:11)*

Tafsir: ***Hakuna chochote chenye mithli naye***.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Rabi’ Ibn Sulayman ambae ni Mwanafunzi wa Imam Al Shafi’i wakati akiwa Misri, anasema: ‘**Siku moja tulikua tumekaa na Imam Al Shafi’i, akatokea mzee mmoja aliekua anatembelea mkongojo akiwa amevaa nguo za Sufi akaja hadi mbele yetu. Imam Al Shafi’i akanyanyuka akaweka nguo yake vizuri halafu akamsalimia yule mzee huku akimuangalia kwa jicho la kuvutiwa naye**.

Yule mzee akasema: Jee Nikuulize?

Al-Shafi’i akajibu: Naam! uliza.

Mzee akauliza: Jee ni nini *Hujjah* (Uthibitisho) katika dini ya Allah?

Al-Shafi’i: Kitabu cha Allah.

Mzee akauliza: Na nini?

Al-Shafi’i: Na *Sunnah* za Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam*.

Mzee akauliza: Na nini?

Al-Shafi’i: *Ijma’a*.

Mzee akauliza: Jee umeitoa wapi ‘*Ijma’a*?

Al Shafi’i akatafakkar kwa mda ambapo yule mzee akasema: **Nakuachia siku tatu. Ukipata jibu katika kitabu cha Allah, sawa kama hujapata basi fanya *istighfar* kwa Allah *Subhanahu wa Ta’ala,*** na kuondoka kuelekea alikotokea.

Uso wa Imam Al Shafi’i ulibadilika rangi halafu na yeye hakukaa tena akaondoka. Imam Al Shafi’i alikaa ndani na hakutoka hadi siku ya tatu baina ya *adh Dhuhr* na *al Asr*. Uso wake, mikono yake na miguu yake ilikua imevimba, ilikua wazi kua yuko taabani na anaumwa. Akakaa kitako lakini hakukaa sana mara yule mzee akatokezea. Imam Al Shafi’i akasimama na kumsalimia na kisha yule mzee akakaa kitako na Imam Al Shafi’i nae akakaa kitako.

Mzee akauliza: Jee umepata nilicho kuuliza?

Al-Shafi’i: Naam..*Au’dhubillahi minna shaitani rajiim,* Allah, *Subhanah wa Taala* amesema:

﴿وَمَن يُشَاقِقِ ٱلرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ ٱلْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ ٱلْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصْلِهِ جَهَنَّمَ وَسَآءَتْ مَصِيراً﴾

Waman yushaqiqi alrrasoola min baAAdi ma tabayyana lahu alhuda *wayattabiAA ghayra sabeeli almu/mineena* nuwallihi ma tawalla wanuslihi jahannama wasaat maseeran (*Surat An-Nisa 4:115*)

Tafsir : ***Na yeyote yule akayebisha na kumpinga Mtume, baada ya kua ameoneshwa wazi njia iliyonyooka, na akafuata njia nyengine isiyokua ya walioamini, Tutamuelekeza katika njia aliyochagua, na tutamchoma motoni - na huo hua ni mwisho mbaya sana'***

Al-Shafi'i akamalizia kwa kufafanua **:Na yeye (Allah *Subhanahu wa Ta'ala*) hatomchoma mtu motoni kwa kuwapinga walioamini katika kitu, isipokua kwa sababu ya kua kitu hicho ni cha Wajib.**

Yule Mzee akasema: Umesema ukweli.

Kisha akanyanyuka na kuondoka.

Imam Al-Shafi'i akawaambia wale waliokuwepo pamoja nae: **Niliisoma *Qur'an* yote mara tatu kila siku kwa siku tatu, hadi nilipoipata ayah hii.** (*Siyar A'lam al-Nubala)*

Yunus Ibn Abi Ya`la anasema kua al Shafi'i amezielezea '**Kanuni**' Kua: '***Qur'an, Sunna, Al-Qiyas na Al Ijma'a***'; na akaielezea *Ijma'a* kua : '**Ni kushikamana na jamaa ya Waislam katika kupata hitimisho la kisharia katika kile kilichoamrishwa na kilichokatazwa baada ya kufariki kwa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*.**'

Siku Moja Imam Al Shafi'i alisema '**Katika *Qur'an* kuna aya ambayo inauma kama mkuki ndani ya moyo wa mtu anaedhulumu lakini hapo hapo ni kama faraja ndani ya moyo wa yule aliedhulumiwa**'. Watu waliokua wakimsikiliza wakauliza '**Jee ni aya gani hiyo? Ya Al Shafi'i**', Imam Al Shafi'i akajibu:

﴿وَمَا كَانَ رَبُّكَ نَسِيّاً﴾

Wama kana rabbuka nasiyyan (*Surat Maryam 19:64*)'.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: ***Na kamwe hakuwa Mola wako ni mwenye kusahau***.

Anasema Ibrahim Al Muzani kua, nilimsikia Imam Al Shafi'i akiielezea kuhusu aya ya *Surat Al Mutaffifin* isemayo:

﴿كَلاَّ إِنَّهُمْ عَن رَّبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّمَحْجُوبُونَ﴾

'**Kalla innahum AAan rabbihim yawma-idhin lamahjooboona** *(Surat Al Mutaffifin 83:15)*

Tafsir: ***Na hakika wao (waliokufuru) watakua katika siku hiyo, wamezibiwa pazia (ili wasimuone Mola wao)****'*

Imam Al Shafi'i anasema kua, '**Katika aya hii kuna ushahidi kua *Awliyah Allah* (Vipenzi vyake wanaomtiii na wanaomuabudu) watamuona Mola wao katika siku ya Kiama**'. Ar Rabii Ibn Sulayman anasema '**Nilikua nipo na Imam Al Shafi'i, na mara ukaja ujumbe kutoka Kaskazini mwa Misri ambao ulikua ukiuliza, Jee unasemaje kuhusu kauli ya Allah *Subhanahu wa Ta'ala* isemayo**: **Na hakika wao watakua katika siku hiyo, wamezibiwa pazia wasimuone Mola wao**' Imam Al Shafi'i anasema kua '**Kwa vile baadhi ya watu watakua hawamuoni, huu ni uthibitisho kua wengine watamuona**'.' Hapo Al Rabii akauliza '**Ya Al Shafi'i. Jee huu ndio msimamo wako?**' Imam Al Shafi'i akajibu '**Naam, hivi ndivyo nnavyoichukulia dini yangu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala***'.

Adh Dhahabi anamuelezea Al Muzani kua alisema: Ikiwa kuna mtu ambae anaweza kuituliza akili yangu kuhusu Tawhid, basi atakua Imam Al Shafi'i. Hivyo nikasubiri wakati alipoingia Msikitini Misri alipokaa nikampigia magoti mbele yake na kumwambia, '**Kuna jambo linalohusu Tawhid, halinipi utulivu. Na nnajua hamna anejua kama wewe, Jee unasemaje?'**

Imam Al Shafi'i alikasirika na kuniuliza **'Jee unajua uko wapi?'**

Nikamjibu '**Naam**'.

Imaml Shafi'i akasema '**Hii ni sehemu ambayo Allah alimuangamiza Firauni, Jee umewahi kisikia kua Rasul Allah, aliamrishwa kuuliza kuhusu jambo hilo?**'.

Nikajibu '**La**'

Imam Al Shafi’i akasema ‘**Jee umeshawahi kusikia Masahaba wakizungumza kuhusu jambo hilo?**’

Nikajibu ‘**La**’

Imam Al Shafi’i akasema ’**Jee unajua katika mbingu kuna nyota ngapi?**’

Nikajibu ‘**La**’

Imam Al Shafi’i akasema ‘**Hivyo, hujui kuhusu hata sayari moja iko vipi, wakati gani inaonekana na wakati gani haionekani**’,

Nikajibu ‘**La**’

Imam Al Shafi’i akasema ‘**Hivyo kuna kitu fulani katika vilivyoumbwa ambacho unakiona kwa macho yako, lakini hujui chochote kuhusu kitu hicho, Halafu unazungumzia kuhusu *I’lm* ya Alieumba?**’.

Halafu akaniuliza kuhusu kutia udhu, na nikakosea katika kujibu kwangu, hapo akanielezea kuhusu udhu katika mitazamo minne tofauti na akaniuliza maswali ndani ya mitazamo hiyo na mara zote nikakosea kujibu. Imam Al Shafi’i akasema ‘**Hivyo unaacha *I’lm* ambayo unaihitaji mara tano kwa siku, na badala yake unaibebesha akili yako mzigo wa kutafuta *I’lm* ya Muumbaji? kila swali hilo litakapokujia akilini basi kumbuka kauli ya Allah *Subhanahu wa Ta’ala* isemayo:**

﴿وَإِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ لَّآ إِلَٰهَ إِلاَّ هُوَ ٱلرَّحْمَٰنُ ٱلرَّحِيمُ۞إِنَّ فِي خَلْقِ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ وَٱخْتِلاَفِ ٱللَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ وَٱلْفُلْكِ ٱلَّتِي تَجْرِي فِي ٱلْبَحْرِ بِمَا يَنفَعُ ٱلنَّاسَ وَمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مِن مَّآءٍ فَأَحْيَا بِهِ ٱلأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِن كُلِّ دَآبَّةٍ وَتَصْرِيفِ ٱلرِّيَاحِ وَٱلسَّحَابِ ٱلْمُسَخَّرِ بَيْنَ ٱلسَّمَآءِ وَٱلأَرْضِ لآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ﴾

Wa-ilahukum ilahun wahidun la ilaha illa huwa alrrahmanu alrraheemu; Inna fee khalqi alssamawati waal-ardhi waikhtilafi allayli waalnnahari waalfulki allatee tajree fee albahri bima yanfaAAu alnnasa wama anzala Allahu mina alssama-i min

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ma-in faahya bihi al-ardha baAAda mawtiha wabaththa feeha min kulli dabbatin watasreefi alrriyahi waalssahabi almusakhkhari bayna alssama-i waal-ardhi laayatin liqawmin yaAAqiloona *(Al Baqarah 2:163-164).*

Tafsir: ***Na Mola wako ni mmoja; Hamna Mola isipokua yeye, Yeye ni mwingi wa Rehma kubwa kubwa na ndogondogo. Hakika katika kuumba mbingu na ardhi, na kutofautiana baina ya Usiku na Mchana, na kuzifanya Meli kuelea juu ya bahari kwa ajili ya manufaa ya watu, na kuteremsha kwake Allah maji kutoka katika mbingu kuihusiha ardhi baada ya kufa kwake, na viumbe aina tofauti vilivyotawanyika kwenye ardhi, na kubadilika mwendo wa upepo na mawingu ambavyo vimewekwa baina ya mbingu na ardhi. Hakika ni ishara kwa wenye akili.***

Hivyo tumia viumbe kama ushahidi kwako wa ukubwa wa alieviumba, na wala usijibebeshe mzigo wa kile kilicho kikubwa kuliko ufaham wako' (*Siyar A'laamin-Nubala(10/31))*

Imam Bayhaqi anasema katika *Isnad* hadi kwa Muhammad Ibn Awf ambae aliemsikia Ahmad Ibn Hanbal aliesema, '**Al Shafi'i ni mtaalamu mkubwa katika mambo manne: *Lugha*, *Al-Khilaf* (Tofauti baina ya Wanazuoni), *Al-Ma'aani* (Maana) na *Al-Fiqh***'.

Ibn Abi Haatim anasimulia Al Hasan Ibn Muhammad As-Sabbaah amesema kua Yahya Ibn Sa'id Al-Qattan amesema: '**Nnamuombea dua Ash-Shafi'i katika kila Salah!**' Na alisema pia, '**Sijawahi kumuona mtu mwenye akili ('*Aql)* na ufahamu mkubwa wa Dini na *Fiqh* kuliko Imam Al Shafi'i**'.

Al Muzani anasema: '**Sijawahi kuona mwanamme mwenye sura ya kuvutia kama Imam Al Shafi'i, na alikua akizikamata ndevu zake zilikua hazitoki nje zaidi ya mkono wake.** Ibn Abd al-Salam alisema kua '**Hamna hata *Hadith* moja ambayo iliyokua haikumfikia Al-Shafi'i kwa njia moja ama nyengine, iwe *Musnad*, *Mursal*, au *Munqati***'. (*Ibn Kathir katika Bidayah 10:276*).

Imam Al-Bayhaqi anasema katika '*Manaqib Al-Shafi*' (2:154) kua Imam Ahmad: **Hamad Ibn Ahmad Al Basri alisema**: '**Nilikua na Ahmad Ibn Hanbal na tulikua tukizungumzia hukmu fulani, hivyo kuna mtu miongoni mwetu akasema kumwambia Ahmad Ibn Hanbal : 'Ya Abu Abd Allah, lakini hakuna ushahidi wa *Hadith* kuhusiana na hukmu hiyo'.**

Hivyo Ahmad Ibn Hanbal akasema **: 'Hata kama ikiwa hakuna ushahidi wa *Hadith* sahih kuhusiana na jambo hili lakini fahamu kua kuna ushahidi wa mtizamo wa Al Shafi'i na uthibitisho wake unatosheleza kuhusiana na Hukmu ya jambo hili**.'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Anasema Ibrahim Ibn Muhammad Al Shafií kua: '**Sijawahi kumuona mtu yeyote anaesali vizuri kama Al Shafii, nah ii ni kwa sababu yeye amechukua namna alivyosali Mulim Ibn Khalid Al Zanj, na Muslim amechukua namna alivyosali Ibn Jurayj, na Ibn Jurayj amechukua kutoka kwa Ata'a na Ataá amechkukua kutoka kwa Ibn Az Zubayr, na Ibn Az Zubayr amechukua kutoka kwa Abu Baqr As Siddiq, ambae nae amechukua kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam***'

Imam Al Shafi na Sayyidah Nafisa: Sayyida Nafisa Bint Hasan Al Anwar Ibn Zaid Al Ablaj Ibn Hasan Ibn Ali Ibn Abi Talib alizaliwa katika mji wa Makkah mwezi 11 *Rabi al Awwal* mwaka 145 *Al Hijr*, hivyo alimzidi kiumri kwa miaka mitano Imam Al Shafi'i, lakini kama Imam Al Shafi'i, nae alitoka katika familia ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*. Baada ya kuzaliwa Sayyida Nafisa aliishi katika mji wa Makkah kwa mda wa miaka mitano ambapo baadae wazee wake walihama na kuhamia katika mji wa Madinah, ambako aliishi na kujipatia *I'lm* yake kutoka kwa Wanazuoni mbali mbali na baadae kuolewa na mtoto wa Imam Jafar As Saddiq aitwae Is-haq Ibn Ja'far Ibn Muhammad As-Sadiq, katika ndoa ambayo ilitoa watoto wawili ambao ni Al Qasim na Umm Kulthoum.

Kutokana na kua ni miongoni mwa wanawake wenye *I'lm* kubwa sana ya *Tafsir*, *Fiqh* na *Hadith* katika historia ya dini ya Kiislam basi alikua akijulikana pia kama *Nafisat Al I'lm.* Sayyida Nafisa na familia yake walihamia nchini Misri miaka mitano kabla ya Imam Al Shafi'i nae kuhamia Misri, kwani Sayyida Nafisa aliwasili *Al Arish* ambao ni mji ulioko kaskazini mashariki mwa Misri katika siku ya Jumamosi mwezi 26 wa Ramadhan ya mwaka 193 *Al Hijr* na akakaribishwa na kukaa kwa muda katika nyumba ya mfanyabiashara mkuu wa mji huo ajulikanae kwa jina la Jamal Ad Din Abd Allah Al Jassas, na kisha baadae wakahamia mjini *Al Qakhira* (Cairo).

Katika mji wa *Al Qakhira* walifikia nyumbani kwa Umm Han ambae alikua ni mwenye nyumba kubwa sana hivyo aliitoa sehemu ya nyumba hiyo kwa ajili ya watu wenye kutafuta *I'lm*, lakini hata hivyo baada ya Sayyida Nafisa kuhamia katika nyumba hiyo, ikawa ndogo haraka sana kwani watu walijazana katika nyumba hiyo kiasi ya kua kwa sababu Sayyida Nafisa alikua hana sehemu nyengine ya kufanyia Ibada kama ilivyokawaida yake anapokua peke yake, akaamua kutaka kuhama katika mji huo na kurudi tena katika mji wa Madinah, lakini hata hivyo umati aliokua akiusomesha uligoma na hivyo kuzuka mgogoro mkubwa sana, ambao uliingiliwa kati na kutatuliwa na As-Siry Ibn Al Hakam aliekua ni Gavana wa *Al Qakhira* kwa wakati huo, ambae alimnasihi na kumtaka Sayyida Nafisa kubakia *Al Qakhira* na kumuahidi kumpatia nyumba kubwa zaidi ili aendeleze kutoa *I'lm* ya dini ya Kiislam, na hivyo wakakubaliana kua atasomesha kwa siku mbili kwa kila wiki na siku zilizobakia atakua akifanya Ibada zake mwenyewe za kawaida.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Waandishi wa Al Qaramani ambao ni wandishi wa vitabu sahih vya historia vya *Al Gharar* na *Al Mustatraf* wanasema kua: '**Wakati wa Utawala wa Ibn Tulun watu walikua wakilalamika kutokana na kutokua na uadilifu katika uongozi wake, hivyo siku moja, Sayyida Nafisa alipata habari kua kiongozi huyo atapita karibu na nyumba yake, hivyo Sayyida Nafisa akaandika barua, na Ibn Tulun alipopita na kumuona Sayyida Nafisa, akashuka kwenye farasi wake na kumsalimia Sayyida Nafisa ambapo nae akampa barua yake iliyokua ikisema: 'Unatawala bila ya uadilifu na kuyatumia sivyo madaraka yako kwa kuwadhalilisha walio chini yako, unawadhulumu na kuwabania mapato yao, Jee unajua kua dua za waliodhulumiwa hua zinakubaliwa wakati wa Usiku?. Kila mtu atafikia mwisho wake. Hivyo wewe fanya unavyotaka kufanya, sisi tunamlalamikia Allah, na karibuni tu wale wasiofanya uadilifu watayaona matokeo yatakavyokua**'. **Tangu kuazia siku hiyo udhalimu uliomo katika utawala huo wote ulitoweka**. *(Tarikh Al Qaramani)*

Imam Al Shafi`i alipohamia Misri alikua akimtembelea Sayyida Nafisa na kusomeshwa *Hadith* wakati alipokua akienda akirudi kusomesha katika Masjid Amr Ibn al`Aas, na mwezi wa Ramadhan Imam Shafi`i alikua akisalisha *Salat Taraweeh* katika Masjid Sayyida Nafisa na Sayyida Nafisa alikuani miongoni mwa *Ma'amuma* wake, katika mwezi mzima wa Ramadhan.

Kila mara Imam Al Shafi`i alipokua akiumwa alikua akimtuma Mwanafunzi wake aende akasome kwa Sayyida Nafisa, ambae humwambia Sayyida Nafisa, '**Binam yako Al Shafi'i anaumwa na anaomba dua zako**'. Kisha Sayyida Nafisa humuombea dua Al Imam Al Shafi'i. Mwishoni mwa uhai wake Imam Al Shafi`i alikua akiumwa sana na akaandika wasia wa kuomba atakapofariki basi Sayyida Nafisa amsalie sala yake ya maiti (*Salat al Janaza*).

Anasema Imam Al-Muzani kua: '**Nilimtembelea Imam Al Shafi'i alipokua akiumwa kabla ya kifo chake, na nikamuuliza: 'Vipi Hali yako?'**

Imam Al Shafi'i akajibu: '**Nnasafiri kutoka dunia hii, na nnaondoka kutoka kwa ndugu zangu, nikinywa kutoka katika kikombe cha mauti, na juu ya Allah - Zimetukuka kumbukumbu zake - zinawasili – Na, la! Ya Allah, Sijui kama roho yangu inasafiri kuelekea Peponi au Motoni!**'

Akaanza kulia na kusema: '**Juu yako ewe Muumba, nnanyanyua maombi yangu, hata kama nikiwa mwenye dhambi na muasi, Ewe mwingi wa upole na Huruma. Wakati moyo wangu umebanwa na njia imekua nyembamba, Nnatumainia msamaha wako kama upenyo na uokozi.**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Dhambi zangu ni kubwa kwangu, lakini nikizilinganisha na msamaha wako, Nnaona msamaha wako ni mkubwa zaid, Kwani wewe ni pekee uwezae kusamehe madhambi, Unatoa msamaha na kusamehe madhambi kutokana na ukarimu wako.

Labda yule ambae ni chanzo cha kila jema atanisamehe na hatoyaangalia makosa yangu, Na atayaficha madhambi na mizigo ambayo nimeikusanya, Dhambi zangu ni kubwa sana kwangu, hivyo nnakugeukia wewe kwa unyenyekevu, Kama si, kutosheka kwangu kwako, basi *Ya Rabb* nisingeridhika, Kwani ukinisamehe, itakua umemsamehe mwenye madhambi, alieasi, aliedhulumu na bado akiwa na madhambi.

Kwani makosa yangu ni makubwa sana, yaliyopita na ya sasa, lakini msamaha wako ambao unamkumbatia mja wako ni wa hali ya juu na mkubwa sana. Kwani yeyote yule alieshikamana na Allah katika *Bani Adam* basi kwa hakika ameokoka, na yeyote yule mwenye kumtegemea Allah, ataondokewa na majuto yote.'

Mwezi 30 Rajab mwaka 204 *Al Hijr*, Imam Al Shafi'i alifariki Dunia akiwa na miaka 54 baada ya kuishi Misri kwa miaka mitano. Baada ya kufariki, mwili wake ukatolewa katika nyumba yake na kupelekwa katika Masjid Sayyida Nafisa na hapo Sayyida Nafisa akamsalia Salat al Janaza katika upande wa wanawake wa msikiti akimfuata Imam Al Buwayti aliekua akisalisha sala hiyo na akazikwa katika Mtaa wa Imam Al Shafi'i, uwanja wa Al Shafi'i katika Al Qarafa Al Sughra, mjini *Al Qakhira*, Misri. Ambapo miaka minne baadae Sayyida Nafisa nae akafariki ukiwa ni mwaka 208 *Al Hijr*.

Imam Al Shafi'i ni Imam pekee ambae ameacha kumbukumbu ya maandishi ya Kitabu cha Ilm ya Usul ul *Fiqh* ambayo alikua akiitumia katika *Fiqh* yake wakati wa uhai wake. Usul ul *Fiqh* ambao umetumika kwa karne na karne na bado unaendelea kutumika hadi leo.

Imam Al Shafi'i aliacha watoto watatu: Abu Uthman, Muhammad *(Ambae alikulia Syria na baadae akawa Qadhi wa Madinah)*; Fatimah na Zainab.

Hivyo Imam Shafi'i amenukuu kutoka kwa: Imam Malik, ambae amenukuu kutoka kwa Safwan ibn Sulaym, ambae amenukuu kutoka kwa Sa'id bin Salamah ambae amenukuu kutoka kwa familia ya Al Azraq, ambao wamenukuu kutoka kwa Al Mughirah Ibn Abi Burdah Ibn 'Abd Al Dar, ambae amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah Radhi Allahu A'nhu.

Imam Shafi'i amenukuu kutoka kwa: Ibrahim Ibn Muhammad, ambae amenukuu kutoka kwa 'Abd Al'Aziz Ibn 'Umar, ambae amenukuu kutoka kwa Sa'id Ibn Thauban, ambae

amenukuu kutoka kwa Abu Hind al-Fisarasi, ambae amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah Radhi Allahu A’nhu.

Imam Shafi’i pia amenukuu kutoka kwa: Ibrahim Ibn Muhammad, ambae amenukuu kutoka kwa Zayd bin Aslam, ambae amenukuu kutoka kwa baba yake, ambae amenukuu kutoka kwa ‘Umar Ibn Al-Khattab Radhi Allahu A’nhu.

Imam Shafi’i pia amenukuu kutoka kwa: Ibrahim Ibn Muhammad, ambae amenukuu kutoka kwa Sadaqah Ibn ‘Abd Allah, ambae amenukuu kutoka kwa Abi Al Zubayr, ambae amenukuu kutoka kwa Jabir Ibn ‘Abd Allah Radhi Allahu A’nhu.

Imam Shafi’i pia amenukuu kutoka kwa: Sufyan Ibn ‘Uyaynah, ambae amenukuu kutoka kwa ‘Asim, ambae amenukuu kutoka kwa Mu’adhah al-‘Adawiyya, ambae amenukuu kutoka kwa ‘A’ishah Radhi Allahu A’nha

Imam Shafi’i pia amenukuu kutoka kwa: Imam Malik, ambae amenukuu kutoka kwa Ibn Shihab, ambae amenukuu kutoka kwa ‘Ubaydullah bin ‘Abd Allah, ambae amenukuu kutoka kwa Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu A’nhu.

Wanafunzi wa Imam Al Shafii aliowawacha Misri – Nguzo za Al Qawl Al Jadid

1. Al-Muzani – Abu Ibrahim Isma'il Ibn Yahya Al-Muzani alikua ni Mwanafunzi na rafiki yake wa karibu Imam Al Shafi'i kwa miaka yote minne aliyokaa Misri. Al-Muzani alijulikana kwa kuandika vitabu vya *Fiqh* ya Imam Al Shafi'i kwa kina. Akaziandika katika *Mukhtasar al-Muzani*, kitabu ambacho kinasomwa sana katika *Madhhab* ya Imam Al Shafi’i.

2. Abu Muhammad Ar Rabii' Ibn Sulaiman Al-Maraadi – Ar Rabii alikua msimulizi mkuu wa vitabu vya Imam Al Shafi’i - *'Al-Umm'*, *Al Risalah* na vyenginevyo aliviandika katika uhai wa Imam Al Shafi’i. Anasema Imam Ibn Al Athir katika *Musnad Imam Al Shafii* kua: ‘**Al Shafi'i alikaa Misri kwa miaka minne, katika kipindi hiki Ar Rabií aliandika zaidi ya kurasa 1500. Kurasa 1000 zikiwa ni kutoka katika kitabu cha *Al Umm* na zilizobakia zilikua kutoka katika *Al Sunan* n.k. Kurasa zote hizo ziliandikwa katika kipindi cha miaka minne**’

3. Abu Yusuf Yaqub Ibn Yahyaa Al Misri Al Buwayti – Mrithi wa Imam Al Shafi'i alikua Mwalimu mkuu wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi’i.

4. Harmalah Najib Abu Yahya Ibn Al Tajibi.
5. Abu Musa Yunus Ibn Abdul A'la Al Sadaghi.

6. Abu A'bd Allah Muhammad Ibn A'bd Allah Ibn Abdul Hakam Al-Misri.
7. Al Rabi Ibn Sulaiman Al-Jiziri.

Al Qawl Al Qadim na Al Qawl Al Jadidi Katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii.

Al Qawl Al Qadim au Kauli ya Zamani ni zile kauli alizoziandika zenye mitazamo ya *Fiqh* aliyoitoa wakati akiwa Iraq hususan katika kitabu cha *Al Risala* kabla kuhamia kwake Misri na Al *Qawl Al Jadid* au Kauli Mpya ni zile kauli alizoziandika zenye mitazamo aliyoitoa baada ya kuhamia Misri ikiwemo ile ambayo aliitoa Iraq lakini akawa hakuiandika hadi alipohamia Misri. Kauli hizi zinapatikana katika kitabu chake cha *Al Umm*.

Kuna mitazamo tofauti kuhusiana na kauli mbili hizi za za Imam Al Shafi'i, yaani kauli ya zamani na kauli mpya, kuna mtazamo wa wale ambao wanasema kua sababu zilizompelekea Imam Al Shafi'i kubadilisha kauli, ni pamoja na:-

Iraq - Utamaduni wa Iraq ulikua uko wazi kwa mitihani, maadili na *Madhhab* mbalimbali.

Misri - Utamaduni wao ulikua una athari za umagharibi hivyo akaamua kuandika *Fiqh* mpya kwa jamii ya watu wa aina hiyo katika cha *Al Umm* au kitabu Mama ambacho ndio kitabu ambacho cha mwisho kuandikwa kwa mikono yake.

Na mtizamo mwengine ni kua Imam Al Shafi'i hakubadilisha kauli zake kutokana na sababu zilizotajwa na wale wenye mtizamo nilioutaja hapo juu, kwa sababu kubadilika kwa njia za *Fiqh* hakuhusiani na mambo hayo, bali huhusiana na kubadilika kwa mtizamo mwengine kifikra, na hii ndio iliokua sababu kuu kwa Imam Al Shafi'i kubadilisha mtizamo.

Kwani Imam Al Shafi'i kwanza aliandika *Usul ul Fiqh*, asili ya *Fiqh* katika *Ar Risala*, wakati akiwa Iraq kabla ya kuhamia Misri, na wakati huo alikua bado ni kijana mdogo, mwenye *I'lm* kubwa sana, lakini hata hivyo alikua hajafikia kileleni mwa *I'lm* yake na hajawiva vizuri, hivyo alikua akiipitia na kuirekebisha *Ar Risala* hapa na pale, na alipohamia Misri na kuongeza *I'lm* zaid, na hivyo kupevuka zaid ki *I'lm* na kifikra, na hapo akaandika pitio la pili la *Ar Risala*.

Anasema Dr. Muhammad Baltaaji katika kitabu chake *Manahij ul Tashri al Islaami fil Qarn al Thani Al Hijri* (Njia za *Sharia'h* za Kiislam katika Karne ya pili ya Hijra), kua '**Al Shafi'i alikua akilaumiwa kutokana na kubadilika badilika. Lakini, alikua**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

akijibu lawama hizo. Ibn Abi Hatim anasema kua Imam Al Shafi'i alimuuliza Amr Ibn Sawad Al Serhi: ‘Kwa nini hukopii vitabu vyangu?’.

Amr Ibn Sawad hakujibu na badala yake akakaa kimya. Lakini Mwanafunzi mwengine akamwambia Imam Al Shafi'i: ‘Anasema kua unaandika, halafu unabadilisha, halafu unaandika tena, halafu unabadilisha tena’.

Hapo Imam Al Shafi’i akajibu : ‘Sasa hivi tayari vimeshawiva’’

Vile vile, Imam Ahmad Ibn Hanbal aliulizwa siku moja na Muhammad Ibn Muslim Al Razi ‘**Nichague vitabu vipi vya Al Shafi'i?**’. Imam Ahmad Ibn Hanbal akajibu: ‘**Chagua vile alivyoviandika Misri. Vitabu alivyoviandika Iraq aliviandika kwa utaalamu, lakini alipohamia Misri aliviandika kwa utaalamu wa kina zaid**’.

Utamaduni mpya katika sehemu mpya, unaweza kumfanya *Mujtahid*, atoe Fatwa tofauti katika jambo fulani, hata hivyo, hukmu ya kitu inayowakabili watu wa Baghdad na hukmu wanayohukumiwa watu wa Baghdad inatakiwa iwe sawia na hukmu ya watu wa Misri au Hijaz au Indonesia kwani mabadiliko ya mazingira au wakati hayafanyi Zinaa kua haramu katika sehemu moja na halali katika sehemu nyengine.

Kwa wakati huo Baghdad na Misri zilikua ni taifa moja, na ilikua hamna tofauti iliyokua wazi baina ya miji hiyo kwa wakati huo, bali tofauti iliyokuwepo ni kuwepo kwa Skuli ya Imam Al Layth katika maeneo ya Misri, na Imam Al Shafi’i alikua hajapitia bado *I’lm* ya skuli hiyo, hivyo alipofika Misri alipata nafasi ya kuisoma na kuijua kwa undani zaid, jambo ambalo lilimfanya Imam Al Shafi’i awive na kua na upeo mkubwa zaid katika *I’lm.*

Tuchukulie mfano wa mwanamke aliesilimu lakini mumewe akakataa kusilimu, hili si jambo jipya, kwani jambo hili lilitokea katika wakati wa Nabii Muhammad *Salallahu A’layhi wa Salam*, wakati binti yake Zaynab *Radhi A’llahu Anha* alipoingia katika Uislam na mumewe akakataa kusilimu, hivyo ili kutatua kesi kama hii katika wakati tuliokua nao, inatubidi turudi katika maandiko, kuyasoma na kuyachunguza ili kupata hukmu yake Kiislamu. Na njia hii hii inabidi itumike kutatua mambo mengine vile vile.

Dr Muhammad Al Zuhayly *ambae ni Mkuu wa Kitengo cha Idara ya Sharia’h, katika Chuo Kikuu cha Sharjah anaelezea mambo ambayo hukmu zake hazibadiliki kutokana na wakati, sehemu au jamii fulani, nazo ni:*

1. Hukmu za msingi ambazo zimetajwa ndani ya *Qur’an* na *Sunnah* ambazo pia zimethibitishwa na maandiko ya *Sharia’h*: Maamrisho na Makatazo, kama makatazo ya Kudhulumu, Zina, Ribba, Ulevi na Wizi. Mfano mwengine wa

Hukmu za msingi ni pamoja na wajibu wa makubaliano katika kufunga mkataba na wajibu wa kupiga vita uhalifu na kugombania haki. Hukmu hizo haziwezi kubadilishwa kutokana na wakati kwa sababu zimewekwa ki *Sharia'h* zinazofaa kwa wakati wa vizazi vyote lakini njia zake huweza kubadilika.

2. Nguzo za Uislam na ule ukweli uliothibitishwa na *Sharia'h* hua haviwezi kubadilishwa wala kupanguliwa. Zitabakia vile vile kama zilivyokua katika kizazi cha mwanzo kwa sababu haziwezi kubadilishwa.

3. Hukmu zote zinazohusiana na Ibada hazitegemeani na mtizamo wala *Ijtihad* ya mtu. Hivyo hazibadiliki kutokana na wakati, eneo, sehemu au jamii.

4. Mambo yanayohusiana na Aqidah pia yamekamilika na msimamo wake ni Imara, hivyo hayahitaji kufanyiwa mabadiliko au *Ijtihad*. Yamekamilika tangu yalipoteremshwa tangu katika nyakati za Mitume waliotangulia hadi kitakapokuja kiama. Hayawezi kubadilika kutokana na wakati. (*Al Qawa`id Al Fiqhiyyah `Ala Al Madhhab Al Hanafy wa Al Shafi`y*).

Kuna kutofahamu katika maumbile ya Uislam, na mienendo ya *Fiqh*, kwani kuna mambo ambayo hukmu yake haibadiliki, kweli kuna mambo mapya ambayo yanatokea na kutaka kufanyiwa *Ijtihad* kutoka katika vyanzo vya *Sharia'h* lakini hayategemeani na sababu ya kua mambo haya yametokea Mashariki au Magharibi. Hivyo kubadilisha hukmu za Kiislam kutegemeana na utofauti wa sehemu moja ama nyengine au kutegemeana na wakati mmoja ama mwengine kwa kuchukulia mfano wa Al Imam Idris Al Shafi'i, Hua haikubaliki.

Ili kufahamu zaidi kuhusiana na *Al Qawl Al Qadim na Al Qawl Al Jadid* basi bora tuangalie mambo yafuatayo:

1. Ikiwa tunazungumzia kutoa Fatwa zinazoendana na mazingira tofauti, basi Imam Al Shafi'i asingeliwaamrisha Wanafunzi wake kutoendelea kukopia kutoka katika vitabu vyake alivyoviandika Iraq, kwani Imam Az Zarkashi anasema katika kitabu chake *Al Bahri al Muhit* kua Imam Al Shafi'i alikua akisema '**Hakusamehewa yule anaeninukuu mimi kutokana na Skuli ya *Madhhab* ya zamani',** na badala yake angelizitenga Fatwa zinazoendana na mazingira ya Iraq peke yake na zinazo endana na mazingira ya Misri peke yake.

2. Ikiwa Fatwa zinabadilika kulingana na mazingira, basi Wanafunzi wake wa Iraq wangelitumia vitabu vya *Al Qawl Al Qadim* vya Iraq, wakati hiyo ni kinyume chake kama tulivyoona mfano wa Imam Hanbal alimwambia Muhammad Ibn Muslim Ar Razi kua achague vitabu alivyoviandika Misri.

3. Hakuna hata Mwanafunzi au Mwanazuoni mmoja wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i, ambao wamefanya *Ijtihad* na wanajua na kufahamu njia alizokua akizitumia Imam Al Shafi'i katika kufanya *Ijtihad* aliesema kua Imam Al Shafi'i alibadilisha mitizamo yake kwa sababu ya kubadilika kwa mazingira au wakati. Hata wale walio walioona kua *Al Qawl Al Qadim* ina nguvu katika baadhi ya mambo machache, wamesema kua wanafuata mitizamo hiyo kwa sababu ya kua ina ushahidi wenye nguvu zaid kutokana na mitizamo yao.

4. Wanazuoni wakubwa wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i wameweka wazi kua hairuhusiwi kufuata *Al Qawl Al Qadim* ya Imam Al Shafi'i, hata kama ikiwa mfuasi huyo ni mtu wa Iraq.

5. Ikiwa ni kweli Imam Al Shafi'i alibadilisha mtizamo wa *Madhhab* yake kutokana na kubadilika kwa mazingira au kwa wakati, basi wafuasi wake waliokua nje ya Misri wangelikataa kumfuata, ni jambo lililo wazi kua Wanazuoni wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i iwe wa Iraq, Malaysia, Afrika Mashariki n.k wanafuata *Al Qawl Al Jadid, yenye* hukmu mpya za Misri, anasema Imam Al Nawawi katika *Al Majmu'a* kua '**Kila swali la dini ambalo lenye mitizamo miwili ya Imam Al Shafi'i, mtizamo mpya na mtizamo wa zamani, basi mtizamo mpya ndio mtizamo Sahih na ndio unaotakiwa kufuatwa',** na pia akasema '**Si juu ya Mufti au kwa mfuasi wa kawaida anaefuata *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i, panapokua na swali ambalo lenye mitizamo miwili, kufuata analolipenda yeye, bali anatakiwa afuate mtizamo mpya kati ya mitizamo hiyo**'. Angalia, Imam Al Nawawi hakutofautisha baina ya Mufti wa Iraq au Misri au Mufti wa popote pale.

Wale wanaosema kua Imam Al Shafi'i, alibadilisha mitazamo ya *Fatwa* zake kutokana na kubadilika kwa mazingira, wakati na utamaduni, wanamaanisha kua Imam Al Shafi'i alitoa *Fatwa* hizo ili kuwarahisishia watu wa Misri, hivyo inaruhusika kutoa *Fatwa* ili kurahisisha mambo hata kama ikiwa Fatwa hizo zinaenda kinyume na ushahidi uliomo katika vyanzo vikuu vya *Fiqh*. Hawajui kua mitizamo ya *Fatwa* za *Al Qawl Al Jadid* za Imam Al Shafi'i alizozitoa Misri ni **mkali zaid** kuliko za kuliko mitizamo ya Fatwa za *Al Qawl Al Qadim* alizozitoa Iraq.

Kwani katika *Fatwa* za Misri aliacha kutumia kanuni za *Masail Mursala* (Kupendelea mapendekezo ya watu wanapotokezewa na jambo jipya, ambalo vyanzo havikusema kitu kuhusu jambo hilo), hakutilia maanani utamaduni wala desturi, na akatilia maanani maandiko zaid na kufuata maana ya kina zaid ya maandiko. Na ukiangalia kwa undani utaona kua hakuna hata jambo moja la *Fiqh* ambalo amelibadilisha kutokana na utofauti wa mazingira baina ya Iraq na Misri.

Baadhi ya Fatwa za Imam Al Shafi'i alizozitoa zenye mtizamo *Al Qawl Al Qadim* za Iraq na mtizamo *Qawl Al Al Jadid* za Misri ni pamoja na:-

1. Kutumia vyombo vya dhahabu au fedha wakati wa kula, katika mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim* ni *makruh* (haipendekezwi) lakini katika mtazamo *Al Qawl Al Jadid* hairuhusiwi na ni *haram*.

2. Kugusana ngozi baina ya mwanamke na mwanami ambao ni Mahram baina yao (hawawezi kuoana) katika mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim*: Hakubatilishi udhu lakini katika mtizamo wa *Al Qawl Al Jadid*: Udhu unabatilika.

3. Kupangusa *khuff* (Soksi za ngozi) zilizo toboka. Inakubalika kwa mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim:* ikiwa tobo hilo sio kubwa kuzuia mvaaji kutembea, lakini kwa mtizamo wa *Al Qawl Al Jadid* haikubaliki hata kwa kitundu kidogo kitachoonesha sehemu ya mguu.

4. Kusahau kusoma *Surat Al Fatiha* katika sala, kutokana na mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim* si wajib ikiwa umesahahu, lakini kwa mtizamo wa *Al Qawl Al Jadid* ni wajib hata kama umesahau.

5. Kukosha chombo kilichorambwa na mbwa, kutokana na mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim*, si wajib kukikosha, lakini kwa mtizamo wa *Al Qawl Al Jadid* ni lazima kikoshwe mara sita.

6. Kusahau na kusababisha kupanguka kwa mpangilio wa sehemu ya kiungo kinachotakiwa kukoshwa wakati wa kutia udhu, Kutokana na mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim*, udhu unakua haujatenguka lakini mtizamo wa *Al Qawl Al Jadid* udhu huo haufai.

7. Kulala wakati wa kusali. Katika mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim* udhu hautenguki lakini katika mtizamo wa *Al Qawl Al Jadid*, udhu huo unatenguka.

8. Mke wa mume aliepotea. Katika mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim*, inambidi mke asubiri kwa miaka minne kuanzia siku aliyopotea mumewe, na kisha ndio aingie katika kipindi cha eda ambacho ni kipindi cha miezi minne na siku kumi, ambao huu ni mtizamo wa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu A'nhu*, lakini mtizamo wa *Al Qawl Al Jadid* ni kua hakai eda wala haolewi tena hadi pale atakapokua na uhakika kua mumewe amefariki ambao ni mtizamo wa Sayyidna Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu A'nhu*.

Al Qawl Al Jadid ndio inayofuatwa na wafuasi wa Imam Al Shafi’i isipokua katika baadhi ya masuala kama ishirni na kitu hivi, kama anavyosema Imam Al Nawawi ‘**Kila jambo ambalo lina mitizamo miwili katika *Fiqh* ya Imam Al Shafi’i, *Al Qawl Al Jadid na Al Qawl Al Qadim,* basi *Al Qawl Al Jadid* ndio msimamo wake na ndio la kulitegemea, kwa sababu ameuondoa msimamo wa *Al Qawl Al Qadim* katika jambo hilo. *As hab (Mujtahid)* wa *Madhhab* yetu wameyachagua mambo kama ishirini na kitu, ambayo wamesema kuhusiana na mambo hayo kua, Fatwa zake zifuatwe kutokana na upande wa *Al Qawl Al Qadim*’**. (*Sharh al-Muhadhdhab*).

As-hab al Madhhab au *As-hab al Wujuh* anaowazungumzia Imam Al Nawawi hapa, ni wale *Mujtahid* ambao waliiendeleza na kuisambaza *Fiqh* ya *Madhhab* ya Imam Al Shafi’i kuanzia kwa Wanafunzi wa Al Imam Al Shafi’i katika mwaka 200 *Al Hijr* kwa miaka mia tatu kupitia kwa Maimamu mbalimbali wakiwemo Al-Buwayti, Abu Thawr, Al Rabbi, Al Muzani, Al Zafarani, Al Darimi, Al Mundhir, Al Qaffal, Al Marwazi, Imam Abu Hamid Al Isfarayini, At Tabari, Imam Al Haramayn Al Juwayni, Imam Ibn Al Sabbagh, Imam Al Ruyani hadi kufikia kwa Mlinzi wa Uislam Imam Abu Hamid Al Ghazali katika mwaka 500 *Al Hijr*.

Katika kipindi hiki *Madhhab* ya Imam Al Shafi’i yalienea kuanzia Misri, Makkah hadi Iraq na Khurasan yote kwa kasi kubwa sana, ambapo baada ya hapo ikawa kuna haja kubwa ya kusimamisha kuiendeleza na hivyo kuiboresha na kuikusanya katika mfumo mmoja, kazi ambayo ilifanywa na Imam Abu Qasim Muhammad Al Rafi’i, ambae alifanya *Ijtihad* kubwa kupitia katika vitabu vya Imam Al Ghazali na Maimamu waliomtangulia kabla yake.

Hivyo Imam Abu Qasim Muhammad Al Rafi’i alizikusanya *Fatwa* zao na kuchunguza vyanzo vyao walivyopitia vidogo na vikubwa, ushahidi wao na vithibitisho vyao inavyotakiwa kwa pamoja.

Baadae akafuatia Imam Abu Zakariya Yahya Al Nawawi, ambae nae pia alivipitia vitabu vya Imam Al Rafi’i na Maimamu waliomtangulia kabla yake, akavifanyia *Ijtihad* na kuvichunguza kwa kina zaid ili kupata msimamo mmoja katika kila jambo unaokubalika baina ya Mujtahid wote wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi’i, na kisha akaandika mukhtasar wake *Al-Sharh Al-Kabeer* katika *Al-Rawdah* na akaelezea zaid katika *Al-Muhadhdhab* na katika *Al-Majmu'*.

Imam Al Kurdi anasema ‘**Ikiwa Shaykhan (Al Nawawi na Al Rafi’i) hawakuzungumzia kuhusu kitu fulani, na Mufti ni miongoni mwa *Ahl Al Tarjih* (Mwenye kujua mapendekezo ya *Madhhab*), basi anaweza kujibu kutokana na mtizamo ambao Maimamu wa *Madhhab* wanautegemea. Hairuhusiwi kwa Mufti kutoa Fatwa kutokana na mtizamo ambao ni dhaifu kutokana Maimamu wa**

***Madhhab*, hata kama ikiwa huo ni msimamo ambao yeye anauona kua ni bora. Kwa sababu yeye anaulizwa kutokana na msimamo wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i na hauliziwi kuhusu msimamo wake, isipokua pale atakapoweka wazi kua huo ni mtizamo dhaifu. Inaruhusiwa kufuata msimamo dhaifu pale ambapo inapokua tayari ameshaweka wazi kua huo ni msimamo dhaifu, ikiwa si miongoni mwa *Ahl Al Tarjih*, na hawa ni miongoni mwa waliokuwepo katika wakati wetu, basi hiyo hua ni kesi nyengine.**'

Miongoni mwa Maimamu wakubwa baada ya Shaykhan Al *Madhhab* Al Shafi'i ni pamoja Shaykh Al Islam Zakariyya Al Ansari, Imam Al Shihab Al Ramli, Imam Al Khatib Al Shirbini, Imam Ibn Hajar na Imam Al Shams Al Ramli.

***Al Qawl Mashhur na Al Qawl Mutammad* katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii.**

Katika *Madhhab* ya Imam kuna kauli aina mbili, ambazo ni *Qawl al Mashhur* na *Qawl Ala Al Mutamad*.

Al Qawl Al Mashhur (Kauli Mashhur) ni kauli ambayo inajulikana sana katika *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i, inaweza kua inatokana na tofauti baina ya *Al Qawl Al Qadim* na *Al Qawl Al Jadid* za Imam Al Shafi'i mwenyewe au ikatoka katika mtizamo wa *Mujtahid* wengine aliefuatia baada yake, lakini baada ya kufanyiwa *Ijtihad* zaid baadae na *Mujtahid* waliofuatia ikaonekana kua ni *dhaif* kulinganishwa na ushahidi uliokuwemo katika kauli nyengine, wakati mwengine *Al Qawl Al Mashhur* inaweza kua *Al Qawl Ala Al Mutamad* pia.

Al Qawl Ala Al Mutamad (Kauli ya mwisho inayokubalika) ni kauli ambayo inakubalika, kauli ya mwisho na ndio msimamo wa *Madhhab*, *Al Qawl Al Mutamad* ndio kauli ambayo inayofuatwa na wafuasi wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i.

Qawl Ala Al Mutamad inahusishwa maalum na Imam Ibn Hajar Al Haytami, kwa sababu Imam Ibn Hajar alikua akilitumia neno hilo wakati akizungumzia mapendekezo ya mitizamo ya Wanazuoni wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i kuhusu jambo analolizungumzia katika kitabu chake kinachoitwa *Tuhfah al Muhtaj bi Sharh Al Minhaj*. Imam Ibn Hajar alianza kuandika *Tuhfah* mwezi 12 Muharram mwaka 958 *Al Hijr* na kukimaliza mwezi 27 Dhul Qaadah, na Imam Ramli alianza kuandika *Nihayat Al Muhtaj ila Sharh Al Minhaj* katika mwaka 963 *Al Hijr* na kukimaliza tarehe 19 *Jamada Al Akhir* mwaka 973 *Al Hijr*.

Mufti yeyote wa *Madhhab* ya Imam Al Shafi'i hutegemea na kufuata *Manhaj* (Njia) zinazotokana na vitabu viwili, kitabu cha *Tuhfah al Muhtaj bi Sharh Al Minhaj* cha

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ibn Hajar Al Haytam au kitabu cha *Nihayat Al Muhtaj ila Sharh Al Minhaj* cha Imam Shams Din Al Ramli.

Vitabu viwili hivi vya *Tuhfah* na *Nihayat* ni ufafanuzi wa kitabu cha Imam Al Nawawi kinachoitwa *Minhaj Al Talibin*, ambacho ni mukhtasar wa kitabu cha Imam Rafi'i kinachoitwa *Muharrar*, ambacho ni mukhtasar wa kitabu cha Imam Al Ghazali kinachoitwa *Wajiz*, ambacho pia ni mukhtasar wa kitabu chengine cha Imam Al Ghazali kinachoitwa *Basit*, ambacho ni mukhtasar wa kitabu cha Imam Al Haramayn kinachoitwa *Nihayat Al Matlab* ambacho pia ni ufafanuzi wa kitabu cha Imam Al Muzani ambae ni Mwanafunzi wa Imam Al Shafi'i, kinachoitwa *Mukhtasar Al Muzani*.

Ingawa Imam Al Shafi'i ni Mujtahid mkuu wa *Madhhab* ya Al Imam Al Shafi'i na mitizamo yake ina kauli katika *Madhhab* na pia aliondoa baadhi ya mitazamo yake katika *Al Qawl Al Qadim* wakati alipokua akitayarisha *Al Qawl Al Jadid*, Lakini kwa kua mtizamo wa *Madhhab* hutokana na *Ijtihad* za *Mujtahid* wengi, hivyo *Mujtahid* wengine waliomfuatia wakiwemo *Mujtahid Al Tarijih* wa *Madhhab*, waliirejesha baadhi ya mitizamo hiyo, baada ya kuifanyia *Ijtihad* zaid ya kina na kuona kua baadhi ya mitizamo ya *Qawl Qadim* ina ushahidi wenye nguvu zaid kuliko ushahidi wa mitizamo ya *Qawl Jadid.*

Mabadiliko haya yalifanyika kutokana na kuwepo kwa ugumu sana au mashaka (*Mashaqqa*) katika utekelezaji wake [*ta'assur al-'amal*]. Na miongoni mmifano ya wa hukmu hizo ni pamoja na kua *walii* (msimamizi wa mwanammke anaetaka kuolewa) anatakiwa asiwe na sifa ya *fasiq* (mtu asiemtii Allah *Subhanah wa Ta'ala*) hukmu hii ilibadilishwa na Wanazuoni waliofuata baadae na wakawa wanaruhusu (unaweza kuiona habari inayohusiana na jambo hili katika Bughya ya Ba'Alawi), na vile vile mfano mwengine ni kutosheleza kwa *niyyah* (nia) ya mwanzoni mwa Sala kulingana na *Takbirat al Ihram* (Takbir ya mwanzo ya Sala) kama ikiwa inawezekana kulingana na kujua [*muqarana 'urfiyyah*] badala ya kulingana na uhakika [*muqarana haqiqiyah*], ambapo inatakiwa kuwepo kuanzia mwanzoni mwa neno la mwanzo la *Allahu Akbar* hadi mwishoni mwake.

Miongoni mwa baadhi ya *Al Qawl Al Qadim* ambazo *Mujtahid* waliofuatia wa *Madhhab* ya Al Imam Al Shafi'i walikubaliana nayo na kuzifanya kua *Al Qawl Ala Al Mutamad* za Skuli ya *Madhhab* ya Al Imam Al Shafi'i ni pamoja na:-

1. Kufanya *Tathwib* [Kusema, 'Sala ni bora kuliko usingizi'] iwe katika adhana ya kwanza au ya pili ya Sala ya Asubuhi; *Al Qawl Al Qadim*: *Mandub* (inapendekezwa); *Al Qawl Al Jadid*: *Makruh* (Inachukiza).

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

2. Kujitenga na uchafu katika maji yanayozidi qullatayn [lita 216]; *Al Qawl Al Qadim*: Haina haja; Al *Qawl Al Jadid*: Inayo Haja.

3. Kusoma Sura katika rakaa mbili za mwisho za Sala; *Al Qawl Al Qadim*: *Makruh* (inachukiza); *Al Qawl Al Jadid*: *Mandub* (Inapendekezwa).

4. Kugusana baina ya ngozi ya mwanamme na mwanamke ambao ni *mahram (hawawezi kuoana)* baina yao; *Al Qawl Al Qadim*: Hakubatilishi udhu; *Al Qawl Al Jadid*: Udhu unabatilika.

5. Maji yanayotembea yakigusana na uchafu; *Al Qawl Al Qadim*: Hayawi machafu, ila maji hayo yatakapo badilika; *Al Qawl Al Jadid*: Yanakua machafu ikiwa maji hayo yatabadilika ama la.

6. Kusali 'Isha' mapema; *Al Qawl Al Qadim*: *Mandub* (Inapendekezwa); *Al Qawl Al Jadid*: *Mandub* kuchelewa kusali 'Isha'.

7. Wakati wa Sala ya Maghrib; *Al Qawl Al Qadim*: humalizika hadi wakati wa 'Isha'; *Al Qawl Al Jadid*: Humalizika hadi pale mtu atakapomaliza kutia udhu,kuhifadhi *awra* (uchi) yake, kuadhini, na kusalia ukubwa wa rakaa tano zisizo za haraka (yaani kusali sala ya Maghrib na sunna yake).

8. Kutia nia ya kufuata Sala ya jamaa katikati ya sala baada ya Takbirat Al Ihram ya Ma'mum; *Al Qawl Al Qadim*: Inaruhusiwa; *Al Qawl Al Jadid*; Hairuhusiwi.

9. Kula ngozi ya mnyama aliechinjwa kiislam iliokwa moto (kama vile ngozi ya kondoo); *Al Qawl Al Qadim*: Haram; *Al Qawl Al Jadid*: Halal.

10. Kumkata kucha maiti; *Al Qawl Al Qadim: Makruh* (Inachukiza); *Al Qawl Al Jadid*: *Mandub* (Inapendekezwa), isipokua kwa wale walifariki wakiwa katika hali ya Ihram wakati wa Hija.

11. *Muhrim* (Alie katika hali ya Ihram katika Hija) ana hiari ya *Tahallul* [kutoka katika hali ya Ihram] anapokua anaumwa; *Al Qawl Al Qadim*: Anaruhusika (lakini lazima achinje kafara [dam]); *Al Qawl Al Jadid*: Haruhusiki.

12. Kuhesabia *Nisab* [Kiwango cha chini] kwa *Zakat Rikaz* [Zakat ya kugundua mali iliyofichwa kabla ya wakati wa kuja Uislam; *Al Qawl Al Qadim*: Haina kiwango cha chini; *Al Qawl Al Jadid*: Inayo kiwango cha chini.

13. ***Ma'muma*** **kuitikia 'Amiin' kwa sauti, wakati Imam anapofanya hivyo katika sala ya kusoma kwa sauti;** ***Al Qawl Al Qadim: Mandub*** **(Inapendekezwa);** ***Al Qawl Al Jadid: Makruh*** **(Inachukiza).**

14. Ikiwa mtu atafariki bila kumalizia kufunga saum; mtu anaehusika (Walii) katika familia yake anaweza kumfungia badala yake: ***Al Qaul Al Qadim*****: Inaruhusika;** ***Al Qawl Al Jadid*****: Hairuhusiki.**

15. Kuchora mstari mbele yake kwa mtu anaetaka kusali, ikiwa hakuna ***Sajjada*** **[msala] au** ***Sutra*** **[kizuizi];** ***Al Qawl Al Qadim: Mandub*** **(Inapendekezwa);** ***Al Qawl Al Jadid*****: Haipendekezwi.**

16. Washirika wawili wanapokua katika ***'Aqd Sharika*** **[Mkataba wa kushirikiana] mmoja akakataa kutumia pesa zake kwa ajili ya mradi wao, ikiwa hawakuweka wazi majukumu yao katika mkataba wa makubaliano yao;** ***Al Qawl Al Qadim*****: mwenzake anaweza kumpuuza na kutoa mtaji;** ***Al Qawl Al Jadid*****: mwenzake hatakiwi kumpuuza yule aliekataa, lakini hutosheleza kulipa fidia kwa kutoa katika faida itakayopatikana.**

17. Fidia ya Mahari ya kulipwa bwana harusi; ***Al Qawl Al Qadim: Daman Yad*** **[kulipwa fidia kamili];** ***Al Qawl Jadid: Daman 'Aqd*** **[kulipwa fidia kwa makubaliano].**

Imam Al Shafi'i alisema: '**Ni bora kwangu mie kuzungumzia kitu kisha nikaambiwa 'umekosea' kuliko nikazungumzia kitu kisha nikaambiwa 'umekufuru'**'.

Amesema Imam Abd Al Hakam Kua: **'Mimi Nilimuota Imam Al Shafii na Nikamuuliza: 'Allah Amekupekeaje?' Nae akasema: 'Amenimwagia Rehma Zake Na Amenisamhe,Na Kunipambia Pepo Kama Bi Harusi Anavyopambwa Kwa Ajili Ya Mumewe, Nami Nikarushiwa Mapambao Na Malaika Kama Arushiwavyo Bwana Harusi Anapooa Duniani.' Nami Nikamuuliza: 'Umefikiaje Darja Hio?' Nae akasema: Kuna Mtu Aliniambia Nisome Salat Nami Nikaisoma - Salat Al Shafi''** Ambayo ni hii ifuatayo:

اللَّهُمَّ صَلَّى عَلَى مُحَمَّدٍ عَدَدَ مَا ذَكَرَهُ الذَّاكِرُونَ وَغَفَلَ عَنْ ذِكْرِهِ الْغَافِلونَ

Allahuma Ssali aAala Muhammad a'adada ma dhakarahu AlDhakiruna wa ghafala aAAn Dhikrihi Al Ghafilina

Ukidumu Nayo Unaingia Peponi Bila Ya Kuulizwa Masuali.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo tunapoangalia upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua ni Madhhab ambayo yamesimamia katika kusimamia Maslahi ya Jamii na umoja wa Waislam kiujumla, na ingawa hili ni lengo kuu la kila Madhhab lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii wao ndio wanaoongoza katika fanikisho la lengo hili.

IMAM ABU AL HASAN ALI RIDHA 153 AH

Imam Abu Al Hasan Ali Ridha Ibn Musa Al Kazim Ibn Jafar As Sadiq Ibn Muhammad Al Bakir Ibn Ali Zayn Al Abidin Ibn Husein Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alizaliwa katika siku ya Al Khamis ya Mwezi wa *Rabi al Akhir* wa mwaka 153 Al Hijra ambayo ni sawa na tarehe 1 -1-765 katika mji wa Madina.

Baba yake Imam Ali Ridha ambae ni Imam Musa Al Kazim alikua ni mtu mwenye Ilm kubwa sana na Mcha Mungu na hii ni kwa sababu alikua ni Mtoto wa Imam Jafar As Saddiq ambapo anasema mmoja kati ya Wanafunzi wake Imam Musa Al Kazim kua: **'Siku moja tulipanda Farasi wetu na kuelekea katika maeneo wanauzwa Suriyah' na tulipofika tukaoneshwa Wanawake takriban kama 7 hivi, ambapo Imam Musa Al Kazim alipowatizama basi akawa hakuridhika nao hata mmoja miongoni mwao.'**

Ambapo baadae tukasikia kua kuna Mwanamke mwengine ambae hayupo pamoja nao lkwa sababu alikua anaumwa, na hivyo Imam akaiambia mie kua: 'Njoo kesho, In-shaa Allah na kisha mnunue huyo Mwanamke ambae leo hakuwepo na mlipie kwa kiasi chochote kitakachotakiwa kua malipo ya bei yake. Na hivyo mimi siku ya pili yake nikarudi tena katika maeneo hayo na kuonana na yule Muuzaji wa Jana yake aliesema kua kuna mmoja kati ya Wanawake hao hayupo'

Na nilipofika, basi nikamuulizia yule Mwanamke wa Jana na nikaoneshwa na kutajiwa bei yake, na nikaambiwa kua anauanzwa kwa bei ya ghali sana, na wala haipungui, hivyo nami nikasema kua nitamnunua kwa bei yeyote itakayokua, nilipotajiwa bei basi nikakubaliana nayo ambapo nae muuzaji akaniuliza: 'Jee unamnunua kwa ajili ya nani?'

Nami nikajibu kua: 'Namnunua kwa ajili ya yule Mtu niliekuja nae Jana' nami nikaniuliza: 'Anatoka wapi huyu Mwanamke?' ambapo Muuzaji akasema: 'Anatoka Marakkesh Maghrib, na nilipomnunua, basi muuzaji alikua ni mwanamke ambae aliniuliza pia ninamnunua kw ajili ya nani? Na nilipojibu kua ni kwa ajili yangu basi Muuzaji akaniambia kua: 'Haiwezekani Mwanamke huyo

awe kwa ajili yako, kwani huyu Mwanamke ni Mwanamke Adhimu sana ana darja kubwa sana, hivyo atakaemnunua na kumuoa basi ni Mtu ambae lazima awe na Darja kubwa sana pia'

'Na akisha alipomuoa basi watapata mtoto ambae atakua na Ilm kubwa sana na Darja kubwa sana hapa Duniani' na hivyo nikamuelezea Darja ya Imam Musa Al Kazim na kuniuzia Mwanamke huyo nami nikamnunua kwa ajili yake, nae akamuoa na kutokana nae ndio akazaliwa Imam Ali *Ridha Radhi Allahu Anhu.'*

Mwanamke huyu alienunuliwa na kuolewa na Imam Musa Al Kazim alikua ni mwanamke mcha Mungu na ni mwenye kujulikana kwa jina la Najma na asili yake ilikua ni katika maeneo ya ardhi ya Morocco katika mji wa Marakesh, na alikamatwa na kuuzwa kama Mtumwa.

Ambapo anasema Hamida Hatun ambae ni Mama yake Imam Musa Al Kazim kua: **'Siku moja mimi nilikua nimelala usiku na usingizini nikamuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alikua akiniambia: 'Karibuni utapata Mjukuu ambae atakua na Darja kubwa sana mbele ya watu''**

Imam Al Ridha alikua kweli ni Mtoto mwenye Ilm kubwa sana na Mtoto ambae alikua akipendwa sana na Khalifa Al Maamun kiasi ya kua alipendekeza kua awe Mrithi wa Mamlaka yake baada ya Kufariki kwake, na kumuozesha Binti yake na kumuahidi kua akiarithi Mamlaka yake basi atakua ni mwenye kuwekwa picha yake kwenye Dinar na Dirham za Utawala wake, ambapo hata hivyo hali hio haikuwezekana kufikika kwani Imam Al Ridha akafariki mwanzo kabla ya kufariki Khalifa Al Maamun.

Na kutokana na mapenzi hayo basi Imam Musa Al Kazim ambae ni baba yake Imam Al Ridha alilizwa: **'Hivi unamwita Abu Al Hasan kwa sababu Khalifa Al Maamun ameridhika nae ama?'** ambapo Imam Musa Al Kazim akasema: **'La, nimemwita hivyo kwasababu ya kua *Allah Subhaanh wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* wameridhika nae'** na bila ya shaka maneno haya yalikua sahih kwani Imam Ridha alikua ni mwenye kupendwa pia na kila mtu marafiki zake na maadui zake pia.

Ambapo tunapouangalia utawala wa Khalifa Abu Al Abbas Abd Allah Al Maamun Ibn Harun Rashid wa Baghdad amabe alikua na Ilm Kubwa ya Dini ya Kiislam na ni mwenye kupenda Kusoma pia basi tunaona kua ulikua ni Utawala ambao ulikua Ukipenda kuwasimamia, kuwahudumia na kuwaunga Mkono Wanazuoni na ndio maana akawa ni mwenye kumpenda Imam Al Ridha kutokana na utukufu wake Kiukoo ambao ni sawa na ukoo wake kwani ukoo wake yeye umetokana na Ame yake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Al Abbas Ibn Abd Al Mutallib *Radhi Allahu Anhu* na Ukoo wa Al Ridha unatokana na Ali Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*.

Khalifa Al Maamun alikua pia ni Mtu ambae ni mwenye kupenda kuendeleza Ilm na hivyo alikua ni kuanzisha Maktaba mbali mbali katika ardhi yake anayoitawala ambazo zilikua aina vitabu vya fani za Ilm za aina tofauti bila ya kujali vitabu hivyo ni vya Wanazuoni wa Ilm ya Dini ya Kiislam au ni vya Wanazuoni wa Dini nyengine, na hivyo alikua ni mwenye kuanzisha *Bayt Ul Hikma* ambayo ilikua ni Maktaba maalum yenye vitabu vya Lugha mbali mbali ambayo ndani yae pia mlikua na watu Maalum ambao kazi yao ilikua ni Kufasiri Vitabu vya Lugha nyengine na kuviingiza kwenye Lugha ya Kiarabu ili Waislam wanufaike na Ilm za Wanazuoni wa Mataifa mengine kama India, China, Ugiriki n.k.

Khalifa Al Maamun katika kuwahudumia kwake Wanazuoni na kuwaunga mkono basi alikua pia ni Mtawala asiejali jinsia ya Wanazuoni yaani kama Wanazuoni hao ni Wanaume ama Wanawake na hivyo alikua akitilia mkazo kusomeshwa zaidi kwa Watoto wa Kike kwa kujenga Maskuli katika maeneo mbali mbali ya Utawala wake.

Katika safari zake mara moja Imam Abu Hasan Ali Ridha alitembelea maeneo ya Nishapuri na akakutana na Wanazuni wengi sana nao wakata awasomee Hadith ambapo nae akasema: ‘**Amesema Baba yangu Musa Al Kadhim, kua amesema Baba yake Muhamamd Al Bakir kua amesema Baba yake Ali Zayn Al Abidin kua amesema Baba yake Husein Ibn Ali kua amesema Baba yake Ali Ibn Abi Talib kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Jibril *Alayhi Salam* kua Amesema *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua: ‘La Ilaha Illa Allah Kalam’ yeyote yule atakaesema haya atakua ameingia kwenye Kalama, na atakaeingia kwenye Kalama basi atakua ni mwenye kuokoka kutokana na Adhabu zangu**’

Anasema mmoja kati ya Wanafunzi wa Imam Abu Hasan Ali Al Ridha kua: **‘Mke wangu mimi alikua ni mja mzito, hivyo nikamfuata Imam Al Ridha na kumwmabia : ‘Muombee Dua Mke wangu ili ajifungue Mtoto wa Kiume’ ambapo nae akasema; ‘Mke wako ni Mja mzito mwenye kubeba watoto wawili mapacha ndani yake’’**

Hivyo nami nikaondoka huku nikiwa na furaha kwani mmoja kati yao nimeamua kua nitamuita Muhammad na mwengine Ali lakini nilipofika Mlangoni basi Imam Al Ridha akaniita na kuniambia: ‘Muite mtoto mmoja kwa jina la Ali na mwengine muite kwa jina la Umm Amr’

Hivyo baada ya mda Mke wangu akajifungua watoto wawili mapacha mmoja Mwanamme na mwengine Mwanamke, Mwanamme nikamuita Ali na Mwanammke nikamuita Umm Amr, ambapo nilipomuuliza Mama yangu kuhusiana na jina la Umm Amr basi akasema kua: ‘Mama yangu alikua akiitwa kwa jina hilo.’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na akasema mmoja katia ya Wanafunzi wake kua: **‘Mimi nililala na kumuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwenye Ndoto akiwa amekaa pamoja na Mahujaj katika Msikiti wake, hivyo nami nikawasogelea na kuwasalimia, na kisha baada ya kuwasalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanipa gao moja la Tende za Sayhan zilizokua zipo kwenye sahani mbele yake, na nikazipokea na nilipozihesabu nikaona kua idadi yake ni 17, nami nikajiambia nafsini wangu kua nimebakisha miaka 17 ya kuishi.’**

Zikapita siku kadhaa baadae nikaenda Msikitini nikamkuta Imam Al Ridha akiwa amekaa ndani yake katika sehemu ile ile niliyomuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua amekaa kwenye ndoto nami nikamsogelea na kumsalimia ambapo nae alikua na sahani ya Tende pia mbele yake, hivyo akanipa gao la Tende nami nikazihesabu Tende hizo nikaziona kua ni 17, na hivyo nikamuomba zaidi lakini akaniambia kua: ‘Jee unataka zaidi ya alivyokua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam?’*

Ibrahim Ibn Abbas anasema kua: **‘Imam Ali Ridhaa alikua ni Mwanazuni mkubwa sana mwenye uwezo wa kujibu masuali mengi sana ya fani za Ilm tofauti, alikua hashindiw kujibu masuali, Khalifa Al maamun alikua akimpenda sana kutokana na namna anayvojibu masuali yake, Imam Al Ridha alikua simtu mwenye kulala sana bali alikua ni mwenye kufanya ibada zaidi na kuwasaidia wasiokua na kitu zaidi, wakati anapokaa alikua hakai juu ya kiti bali alikua anakaa juu ya jamvi na hata kulala kwake pia alikua akilala juu ya jamvi, alikua ni mnyenyekevu kwa Mola wake na ni mwenye kumtegemea juuya kila kitu na alikua anavaa pete ambayo ilikua imeandikwa *Hasbiya Allah* (Allah ni mwenye kunitosheleza) kwenye kito chake’**

Imam Abu Hasan Al Ridha alifariki mnamo mwaka 203 Al Hijra katika siku ya Alkhamis ya mwezi 21 Ramadhan

IMAM YAHYA IBN MAIN 158 AH

Imam Abu Zakarriya Yahya Ibn Main Ibn Aun Ibn Ziyad Ibn Bistami Al Ghatfan Al Baghdadi alizaliwa mnamo mwaka 158 Al Hijra kutoka katika familia ya Kitajiri sana katika ardhi ya Iraq kiasi ya kua baada ya baba yake kufariki basi Imam Yahya Ibn Main alirithi Dirham Milioni moja ambazo zote aliitumia kwa ajili ya kujitafutia Ilm ya Dini

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

yake, na hivyo alikua na Ilm kubwa sana ya Ilm ya Hadith kutokana na jitihada zake hizo.

Kwani Imam Yahya Ibn Main alitembea katika ardhi za nchi nyingi tofauti kwa ajili ya kutafuta Ilm ya Hadith ikiwemo Iraq, Misri, Hijaz, Sham na Al Jazira ambapo alisoma kwa Wanazuoni mbali mbali akiwemo Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Yahya Ibn Qattan, Imam Marwan Ibn Muawwiyah, Imam Waqi Ibn Jarrah, Imam Hisham Ibn Yusuf, Imam Isa Ibn Yunus, Imam Abd Rahman Ibn Mahdi na wengineo.

Imam Yahya Ibn Main anasema kua: **'Nimeandika kwa mikono yangu Hadithi Milioni moja.**'

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake walikuwemo Maimamu wakubwa kama Imam Ahmad Ibn Hambal, Imam Muhammad Ibn Sa`d, Imam Abu Khaitham, Imam Bukhari, Imam Muslim, Imam Abu Daud, Imam Abbas Ad-Duri, Imam Abu Bakar Ash-Shaghani, Imam Abdul Khalik Ibn Mansur, Imam Uthman Ibn Sa`id Ad-Darimi, Imam Abu Zur`ah, Imam Abu Hatim Ar-Razi, Imam Ibrahim Ibn Abd Allah Al-Junaid, Imam Ahmad Ibn Ali Al-Marwazi, Imam Muhammad Ibn Wadhhah, Imam Ja`far Al-Firyabi, Imam Musa Ibn Harun, Imam Abu Ya`la Al-Mushili, na wengineo.
Imam Yahya Ibn Main alikua na Ilm kubwa sana ya Hadith kama anavyobainisha Imam An Nasai ambae anaema kua: '**Abu Zakarriyah ni mtu mwenye kuaminika na ni Mtaalamu wa Hadith'**

Ambapo anasema Imam Ali Al Madini kua: '**Hakika mimi sijawahi kuona tangu kuanzia katika wakati wa kipindi cha Adam mtu mwenye kuandika Hadith vizuri sana kama anavyoandika Yahya Ibn Main, kwani Yahya Ibn Main ni Kilele cha Ibn Adam cha Ilm.**'

Ambapo anasema Imam Yahya Al Qathan kua: **'Hakuna Mtu aliekuja kwetu sisi kama watu hawa wawili Ahmad Ibn Hanbal na Yahya Ibn Main.'**

Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: **'Yahya Ibn Main ni Mtu anaefahamu sana kuhusiana na Ilm ya wanaonukuu hadith'**

Na Imam Adh Dhhabi akasema kua: **'Yahya Ibn Main ni Bwana wa Wanaohifadhi Hadith, kwani anajulikana sana kiasi ya kua haifai kwangu mimi kuelezea Ubora wake.'**

Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani alisema kua: **'Yahya Ibn Main ni Imam wa Ilm ya Mapendekezo ya uzuri na ubaya hadith Hadith'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema tena kuhusiana nae pale alipokua akimuelezea Imam Yahya Ibn Main kua: '**Huyu hapa ni Mtu ambae *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemuumba kwa ajili ya kuhifadhi Hadith na kuwadhihirisha wazushi wa Hadith.**'

Imam Yahya Ibn Main alifariki mnamo mwaa 233 Al Hijra mnamo mwezi wa *Dhul Hijja*h katika Ibada ya Hija.

Ambapo Imam Adh Dhahabi anasema kua: '**Hubaish Ibn Mubashir ambae ni mmoja kati ya Wanazuoni wanaoaminika sana amesema kua: 'Mimi nililala na nikamuona Yahya ibn Main usingizini na nikamuuliza: 'Hivi Jee *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekupokeaje?' nae akasema kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* amenipa starehe kwa kuniozesha Hur Layni 300 wa Peponi na kunifungulia Milango miwili'**''

IMAM AL ZAHID AL ISFAHANI 158 AH

Imam Abu Abd Allah Al Zahid Al Abid Muhammad Ibn Yusuf alikua ni miongoni mwa Wanazuoni wa Tabii Tabiina na alipewa jina la Al Zahid na pia Al Abid kutokana na Ucha Mungu wake na kuachana kikamilifu na na Dunia yake kwa ajili ya *Allah Subhanah Ta'ala.*

Imam Al Zahid alizaliwa katika maeneo ya ardhi ya Isfahan na baadae akahamia katika ardhi ya Makkah kwa ajili ya kujitafutia Ilm ya Dini ya Kiislam na kisha akahamia katika mji wa Basra na hivyo Imam Al Zahid Al Isfahani alikua ni Mwanafunzi aliesoma kwa Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Yunus Ibn Ubayd, Imam Hamad Ibn Salamah, Imam Sulayman Ibn Al Mihran, Imam Al Amash, nae akawasomesha kina Imam Al Awzai, Amir Ibn Hamad Al Isfahani, Imam Zubayr Ibn Abbad, Imam Yahya Al Kattani n.k

Anasema Imam Yahya Ibn Said Al Kattani kua: '**Hakika mimi nimewahi kuzungumza na Wanazuoni wengi sana, lakini hata hivyo sijawahi kuona Mtu Mcha Mungu kama Muhamad Ibn yusuf Al isfahani, na kwa mtizamo wangu ni kua yeye ni alie juu zaidi kuliko Sufyan Ath Thawry.**' Ambapo Imam Ahmad Ibn Hanbal akauliza: **'Hivi unamaanisha kuhusiana na kua juu ilm na kitabia?**' ambapo Imam Yahya Al Katani akasema: **'Naam, Kiilm na Kitabia'**

Imam Al Zahid Al Isfahani alikua ni mtu ambae si mwenye kupenda kujulikana na alikua ni mwenye kusali Usiku kucha na wala si mwenye kujichanganya na Watu kwani kwake yeye ilikua ni mwenye kujitosheleza kutokana na kile anachokipata kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Imam Ataa Ibn Muslim anasema kua: **'Muhamamd Ibn Yusuf Al Isfahani alikua akija mlangoni kila siku huku akiwa na muonekano unaoshangaza, huuliza analotaka kujifunza kwa njia za kushangaza, na kisha anapopata Jibu lake kutoka kwangu basi, hua ni mwenye kuondoka nyumbani kwangu kwa kustaajabisha, ambapo hali hii iliendela kwa mda wa miaka 20, huku nami sikuwa ni mwenye kumuuliza wewe ni nani, lakini nikasikia kuhusiana na mtu aitwae Muhammad Ibn Yusuf Al Isfahani hivyo nami nikavutiwa nae, ambapo siku moja tulipokua tumekaa Msikitini, akaja mtu anaemjua na kusalimia kisha akaniambia kua: 'Huyu ndie Muhamamd Ibn Yusuf Al Isfahani' hapo ndio nikajua kua huyu ndie Mtu ambae alikua akija Nyumbani kwangu na kuniuliza kwa mda wa miaka 20 bila ya kumjua ni nani na bila ya mimi kumuuliza wewe ni nani. '**

Imam Abd Allah Ibn Mubarak anasema kua: **'Mimi nilimuuliza Ibn Idris, hivi jee katika Mji wa Basra na nani anaeweza kuninufaisha zaidi, ambapo nae akasema kua hakuna zaidi ya Muhamamd Ibn Yusuf Al Isfahani, nenda kwake kwani atakunufaisha sana utamkuta katika sehemu yenye utulivu, kwani anaishi kwenye sehemu iitwayo Mesis katika Mji wa Basra', hivyo nami nilipotembelea katika Mji wa Basra nikaenda katika maeneo ya Mesis na nikamuulizia lakini ikawa hakuna hata mmoja anaemjua Muhamamd Yusuf Al Isfahan, na hii ni kutokana na Taqwa yake, hivyo nikaenda katika mmoja kati ya Miskiti ya eneo hilo na kumkuta Muhamamd Yusuf Al Isfahan akiwa amekaa kwenye sehemu tulivu na nikamuona kua kweli huyu mcha Mungu na mwenye Taqwa.'** Kwani kipindi hiki Imam Abd Allah Ibn Mubarrak alikua anakaribia miaka 60 na Imam Al Zahid Al Isfahani alikua ni kijana mdogo mno kwenye umri wa miaka 20.

Na akasema Imam Zuhayr Al Banani kua: '**Mtu aliekua akifanya Ibada kama Muhamamd Ibn Yusuf na asiejulikana kama yeye hatotokea tena Duniani.'**

Ambapo anasema Imam Abd Rahman Al Mahdi kua: **'Hakika mimi sijawahi kukutana na mtu kama Muhammad Ibn Yusuf.'**

Ambapo anasema Imam Darhim kua: '**Mimi nilikua nikihudhuria Darsa zake kwa mda mrefu na sijawahi kumuona akizungumzia kitu chochote ambacho hakihusiani na *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Ambapo anasema Ibn Zakarriyah kua: '**Safari moja Tulikua tuko kwenye msafara wa Safari pamoja na Muhamamd Yusuf Al Isfahani na tukawasili kwenye Nyumba**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ya kufikia wageni, tukapumzika halafu siku ya pili asubuhi tukatoka na kwa ajili ya kuendelea na Safari, ikabidi nikamwite kiongozi wa msafara, na nilipoenda kumuita nikamkuta akiwa taabani anaumwa kwani alikua ametafunwa na Nge hivyo hata kunyanyuka alikua hawezi.

Hivyo nikamwambia Muhamamd Yusuf Al Isfahan, ambae nikaenda nae kwa kiongozi huyo wa Msafara. Na alipofika akainamisha kichwa chake kwenye sehemu aliyotafunwa kiongozi huyo na kisha akampulizia huku akisoma maneno kimya kimya. Na baada ya kumaliza basi Kiongozi huyo akanyanyuka kama kwamba hakua yeye aliekua akiumwa. Hivyo nikamuuliza Muhammad Yusuf Al Isfahani: 'Hivi Jee Ulikua ukimsomea nini?' ambapo ane akasema: '*Umm ul Kitab*'

Nami nikamuuliza: 'Umm ul Kitab ndio nini?' nae akasema: '*Surat Al Fatiha*. Nimemsomea *Surat Al Faitha* tu.' Hivyo baada ya hapo na mimi pia kwa kila Mtu akiumwa basi namsomea *Surat Al Fatiha* lakini hakuna hata mmoja alieweza kupona kutokana na Kisomo changu hicho cha *Surat Al Fatiha.*'

Anasema Muhamamd Ibn Hilal kua: **'Imam Muhammad Ibn Yusuf Al Isfahan na Imam Fudayl Ibn Iyadh walikua hawajawahi kuonana ingawa walikua wanatafutana, hivyo siku moja wakakutana kwenye eneo la Sokoni, na hivyo walipokutana basi kila mmoja alimuuliza mwenzake kwa wakati mmoja kwani Imam Al Isfahan aliuliza 'Wewe ndie Fudayl Ibn Iyadh?' na Imam Fudayl akauliza 'Wewe ndie Muhammad Yusuf Al Isfahani?' kisha wote kwa pamoja wakasema: 'Naam.' Na kisha wote wakaanza kulia kwa pamoja na kuzimia, ambapo Imam Fudayl Ibn Iyadh akachukuliwa na kupelekwa nyumbani kwake huku Imam Al Isfahan alibakia hapo hapo sokoni kwani hakuna aliekua akimjua ni nani na anakaa wapi.**

Ambapo anasema Salih Ibn Mahdi kua: **'Sisi tulikua tunaenda katika mji wa Yahudiyah pamoja na Muhammad Ibn Yusuf, ambapo njiani tukakutana na Mkristo, ambae Imam Muhammad Ibn Yusuf akamsalimia kwa heshima kubwa sana hivyo nikajiuliza: 'Hivi Jee inakuaje Imam wa Waislam anaonesha heshima kubwa kwa mtu asieamini' hivyo nikamuuliza ambapo nae akasema: 'Huyu Mtu unaemuona kua ni Mkristo ni Muislam aliesilimu kwa Siri, na Kaka yangu alienda kwenye kijiji chake akiwa na Wanafunzi tisa. Hivyo bwana huyu alienda yeye mwenyewe kwa kaka yangu na na kumonesha heshima kubwa na pia akampa Dirham 1000 za Dhahabu lakini nae akakataa kuzipokea.''**

Safari moja kuna wezi waliiba Wanyama wote waliopo katika eneo analoishi Imam Al Isfahan wakiwemo wanyama wa Imam Al Isfahani pia. Hivyo watu wakawafuata wezi hao na kuwaambia: '**Wachukueni wanyama wetu wote, lakini tuachieni hawa wanyama wa Al Isfahan kwani huyu mtu ni Walii wa *Allah Subhanah wa Ta'ala***

na sisi tunaogopa Dua zake.’ Lakini hata hivyo wezi hao hawakurudisha hata mnyama hata mmojana hivyo Wanyama wote hao wakafariki isipokua Wanyama wa Imam Al Isfahan.

Imam Muhammad Al Isfahan alisema kumwambia Said Ibn Ghaffar kua: **‘Ewe Said uthamini Mda wako ambao ni wenye Thamani kubwa zaidi kwa kuutumia kwa mambo yenye Thamani kubwa zaidi.’**

Imam Muhamamd Al Isfahan alimwambia ndugu yake kwa kusema: **‘Ewe Ndugu yangu Muogope *Allah Subhanah wa Ta’ala* na Mtii, na kamwe usisahau juu ya Adhabu zake kwani hakuna anakaeweza kuzistahamilia Adhabu zake, na utakapopata pesa za Halali basi nenda katika Ibada ya Hija kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Yeyote yule atakaeenda Hija kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kutokana na mali ya halali na kufanya Ibada ya Hija basi akirudi hua hana dhambi hata moja kama vile alivyokua katika siku aliyotoka kwenye tumbo la Mama yake.’’**

Na akasema pia akasema: **‘Hakika mimi sitokua na furaha haa Duniani hata kama nikiuziwa Ardhi yote hii unayoiona kwa Dinar 2, kwani kila kitu kwenye Dunia hii ni cha mpito na chenye kuangamia baada ya mda nasi pia tutaangamia huku Mali zetu na vitu vyetu vitabakia baada yetu.’**

Na akamwambia Abd Rahman Ibn Umar wakati walipokua wakielekea kwenye Ibada ya Hija kwa kusema: **‘Ewe Abd Rahman, unapopita kwenye Milango ya Majumba makubwa makubwa ya watu wanaoendekeza matamanio ya Nafsi zao basi sema: ‘Jee wako wapi wale ambao walijenga Mjumba makubwa makubwa na kusema kua Dunia yote ni yetu? Bila ya shaka wote wamekufa’ na ukipita katika sehemu ambayo ina wale ambao ni wenye kufanya Ibada basi sema: ‘Enyi wenye kufanya Ibada utakapowadia wakati wa vifo vyenu nanyi mkaelekea Akhera basi jueni kua kitakachofuatia baada yake ni bora kwenu’’**

Imam Al Zahid Al Isfahani anasema kua: **‘Mimi nimemsikia Sulayman Ibn Mihran kua amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Kamwe Usiwache kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Siku ya Ijumaa kwa mara 1000’’**

Anasema Yusuf Ibn Zakariyyah kua: **‘Muhammad Ibn Yusuf alikuja kwetu na hivyo Wanazuoni wote wa Hadith wakawa ni wenye kumzunguka yeye. Hivyo hakuchukua mda isipokua akaamua kuondoka na kisha akelekea katika Mji wa Harran na kukaa katika maeneo ya Rasulen. Kisha baada ya mwezi mmoja akarudi, hivyo nikamuuliza kwanini akakaa mda mrefu hivyo ambapo nae**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

akasema kua: ‘Nimekaa sana kwa sababu hakuna Mtu anaenijua mimi na wala mimi sikua ni mwenye kujuana na Mtu yeyote.’’

Yusuf Ibn Zakarriyah anaendelea kusema kua: **‘Hakika mimi nilimuona Muhammad Ibn Yusuf akiwa ni mwenye kunua mkate katika Duka tofauti kila siku katika maisha yake, na nilipomuuliza kwanini basi akasema: ‘Kama nikiwa kila siku naenda kwenye Duka hilo hilo moja basi mwenye Duka la mikate atakua ananijua na hivyo kuanza kuniheshimu, na hivyo mimi nitakua najihisi kua natumia Dini yangu kwa ajili ya Dunia yangu, hivyo nikinunua katika maduka tofauti basi hakuna atakaenijua.’’**

Imam Al Zahid Muhammad Ibn Yusuf Al Isfahani alifariki Mjini Basra mnamo mwaka 188 Al Hijra akiwa na umri wa miaka 30.

IMAM SARI AL-SAQATI 160 AH

Imam Abu Hasan Sari Ibn Mughallis Al Saqati alizaliwa mnamo mwaka 160 Al Hijra katika mji wa Baghdad na alikua Mtoto ambae ni Mjomba wake Imam Al Junayd, kwani Mama yake Imam Imam Al Junayd alikua ni Dada yake Imam Sari al Saqati.

Imam Sari Al Saqati alisoma kwa Imam Habib Al Rai na pia alikua ni mwenye kusoma kwa Imam Maruf Al Karhi. Imam Sari Al Saqati alikua ni mwenye kufanya biashara katika soko kuu la Baghdad, na alikua si mwenye kupenda faida kubwa katika biashara zake kwani alikua akiweka asilimia 5 tu ya faida, kiasi ya kua siku moja alikua mtu ambae alikua akitaka kununua Lozi kutoka dukani kwake kwa bei kubwa zaidi kwa sababu Lozi zilikua zimeadimika, lakini hata hivyo Imam Sari Al Saqati akakataa kuuza kwa kusema: ‘**Si kanuni yangu kuuza kwa faida ya zaidi ya asilimia 5, hivyo siwezi kukiuka kanuni yangu**’

Ambapo baada ya mda soko la Baghdad likaungua Moto basi Imam Sari Al Saqati akasema kua: **‘Alhamd lillah Hakika sasa hivi mimi nitakua huru kutokana na Duka langu.’** Lakini hata hivyo baadae akagundua kua ingawa Maduka yote yameungua kwenye Soko hilo, lakini Duka lake halikuathirika hata kidogo kutokana na Moto huo basi akaamua kuvitoa na kuvigawa vitu vyote vilivyomo kwenye Duka hilo kua kama Sadaqah na kisha akaamua kumtumikia *Allah Subhanah wa Ta’ala* tu peke yake.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo kuna wanaosema kua: '**Imam Sari Al Saqati aliposikia kua Duka lake halikuungua basi akasema: 'Alhamd lillah' lakini baada akagundua kua kusema hivyo alikua akifurahia kutoungua kwa Duka lake wakati Maduka ya wenzake yakiwa yameungua, hivyo kutokana na kua na mtizamo huo basi Imam Sari Al Saqati akawa ni mwenye kufanya istighfar kwa miaka 30 baada yake tangu baada tukio hio.'**

Imam Sari Al Saqati aliulizwa: **'Hivi ilikuaje hadi ukawa ni mwenye kuelekea katika njia uliyoelekea baada ya kuachana na biashara?**' Imam Sari Al Saqati akajibu: '**Siku Mja Habib Al Rai alipita kwenye Duka langu, nami nikampa kipande cha Mkate na kumwambia kua awagaie Masikini, ambapo nae alipokichukua kipande hicho basi akasema: 'Namuomba Allah Akulipe kutokana na hili' na hivyo tangu siku hio nilipoombewa Dua hio basi Maisha yangu hayakunawiri tena**'

Hivyo akasema Imam Sari Al Saqati kua: '**Ya Rabb hakika kama umeamua kuniadhibu mimi basi usiniadhibu kwa muadhirisho wa kuwekewa pazia kutokana nawe, kwa sababu kama sikua ni mwenye kuwekewa pazia kutokana nawe basi adhabu zangu na mitihani yangu itapungua uzito wake kwa kukutafakkari na kukukumbuka wewe. Lakini kama ikiwa nitawekewa pazia dhidi yako basi bila ya shaka neema zako zitakua ni mbaya sana kwangu, kwani hakuna adhabu nzito na isiyostahmilika kwa watu wa Motoni kuliko kuwekewa pazia dhidi ya Mola wao.**

Kwani kama watu wa Moto wataondelewa pazia dhidi ya Mola wao, basi wao hawatoifikiria Pepo bali watakua ni wenye kuridhika na kupata afuweni, raha na furaha kutokana na kua hawatohisi Maumivu kwenye miili yao, na Peponi hakuna raha zaidi ya kutokua na Pazia dhidi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na hivyo hata kama watu hao watanufaaishwa na kila aina ya starehe na anasa, lakini bia ya kuodolewa pazia dhidi ya Mola wao basi watu hao watakua wamevunjika Moyo sana.

Hivyo ni kawaida ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuwaruhusu wale wenye Nyoyo zenye kumpenda kua ni wenye kuondolewa pazia dhidi yake, ili raha itokanayo na muonekano wake kuwazidishia ustahmilivu wa kustahmili kila aina ya Mitihani. Na hivyo hua ni wenye kusema kwa umoja kua: 'Hakika sisi tunatamani adhabu na mitihani yote isipokua kuwekewa pazia dhidi yako, kwani uzuri wako utakapodhihirishwa ndani ya Nyoyo zetu basi hua hatuhisi wala hatufikirii kuhusiana na Mitihani.''

Imam Sari Al Saqati alikua ni mtu ambae ni mwenye kujitenga na watu wengine alikua ni mtu mwenye kuachana na Dunia yake, na alikua akipenda kukaa ndani mwake tu huku akisema kua: **'Kwangu mimi ni bora kukaa ndani na ndio maana siwezi**

kuuwacha Mlango wangu wazi isipokua kwa ajili ya Sala ya Ijumaa na Sala ya Jamaa.'

Na alikua ni Mwenye kupenda sana kufanya Ibada kiasi ya kua anasema Imam Al Junayd kua: **'Hakika mimi sijawahi kumuona Mtu mcha Mungu kama Sari Al Saqati, kwani kwa mda wa miaka 78, hakuna mtu aliewahi kumuona akiwa amelala kitandani isipokua katika kipindi cha mwishoni alipokua anaumwa kabla ya kufariki kwake'**

Anasema Hasan Al Bazar kua: **'Hakika sisi katika kipindi ambacho Imam Ahmad Ibn Hanbal na Bishr Al Hafi wako hai basi tulikua tukimuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atulinde kutokana na kua wao wako pamoja nasi katika Mji wa Baghdad lakini baada ya kufariki wao basi tukawa tunamuomba atuhifadhi kwa sababu ya Sari Al Saqati'**

Alisema Imam Sari Al Saqati kua: **'Hakika mimi nnaona utiifu kwa Mola wangu kua ni biashara nzuri kwa utulivu wa Nafsi yangu na Uovu hua ni biashara mbaya na yenye uchovu mkubwa sana ndani yake kwa Nafsi na Mwili wangu.'**

'Hakuna Mtu yeyote yule atakaekua hawezi kuiheshimu Nafsi yake kisha akawa ni mwenye kuiheshimu Nafsi ya Mwenzake.'

'Dunia nzima haina thamani yeyote isipokua vitu vitano tu ndani yake: 'Chakula chake kwa ajii ya kuishi ndani yake, Maji kwa ajili ya kuondoa kiu ndani yake, Mavazi kwa ajili ya kujistiri ndani yake, Nyumba kwa ajili ya kujihifadhi ndani yake na Ilm kwa ajili ya kuifanyia kazi ndani yake.''

Kutokana na kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Imam Sari Al Saqati alikua kila siku anaiangalia pua yake, na hivyo akaulizwa kwanini mara kwa mara anaiangalia Pua yake basi akasema: **'Hakika mimi nna khofu kua Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* dhidi yangu sizije zikaugeuza rangi uso wangu.'**

Na alikua akisema kua: **'Mimi sipendi kufa katika sehemu ambayo ni mwenye kujulikana'** alipoulizwa kwanini basi akasema: **'Kwa sababu naogopa Ardhi isije ikanikataa na kisha nikaadhirika mbele ya watu wanaonijua.'**

Kuna mtu alimuuliza Imam Sari Al Saqati: **'Hivi jee nnawezaje mimi kuachana na Dunia yangu?'** Imam Sari Al Saqati akamuuliza: **'Jee unayo chumvi ya Unga Nyumbani kwako?'** Mtu huyo akajibu : **'Naam'** Imam Sari Al Saqati akasema: **'Basi hutoweza kuachana na Dunia yako.'**

Siku moja kua mtoto alipewa mzigo wa zawadi na baba yake ili akampelekee Imam Sari Al Saqati ambapo Imam Sari Al Saqati akamuuliza mtoto huyo: **'Jee hii zawadi ina Thamani gani?'** Mtoto akajibu: **'Sijui'** Imam Sari Al Saqati akasema: **'Kamwambie Baba yako kua sisi kwa miaka 50 sisi tumekua tukiwausia watu kua wasichukue malipo kutokana na Dini yao, hivyo jee leo itakuaje niwe ni mwenye kuchukua malipo kutokana na Dini yangu?'**

Kuna siku kuna mtu alikuja kwa Imam Sari Al Saqati na kumpa salam zake kutoka kwa rafiki yake anaeishi Milimani peke yake, hivyo Imam Sari Al Saqati akasema: **'Jitihada zake hazina maana kwani Mtu unatakiwa uwe ni mwenye kuishi katikati ya Soko huku ukiwa umeshughulika na Mola wako, kiasi ya kua usiwe ni mwenye kughafilika hata kidogo juu ya Mola wako.'**

Amesema Imam Sari Al Saqati kua: '**Amesema Yahya kua kuna mtu kutoka katika kabila la Al Tai ambae amesema kua: 'Mimi niliendelea kumummba Allah *Subhanah wa Ta'ala* anioneshe Jina lake tukufu zaidi ambalo akiombewa kutokana nalo basi dua hua ni yenye kujibiwa ambapo nae akanikubalia kwa kuiambia niangalie juu Mbinguni, na nilipoangalia basi nikaona kumeandikwa *'Ya Badi' al-Sammawat and wal-Ardh' ya Za-al-Jalal-i wal-Ikram''***

IMAM IBN SAHNUN 160 AH

Imam Ibn Sahnun Abd Salam Ibn Said Ibn Habib Al Tanukhi Al Arabi alizaliwa katika mwaka 160 Al Hijra katika Ardhi ya Sham katika mji wa Homs, katika familia ya baba ambae alikua ni askari mpiganaji, ambapo baadae familia hio ikahama katika Ardhi hio na kuelekea kwenye maeneo ya Al Maghrib yaani maeneo ya Afrika Kaskazini katika katika nchi ya Morroco na Tunisia.

Imam Ibn Sahnun alianzia kusoma Ilm ya Dini ya Kiislam tangu wakati akiwa mdogo katika Mji wa Homs na alikua anaitwa Ibn Sahnun kwa sababu ya ufahamu wake ulivyokua mzuri sana kwa kuhifadhi mambo tofauti, kwani ulikua unafanana na kama wa ndege aitwae Sahnun.

Hivyo baada ya familia yake kuhamia katika ardhi ya Maghrib basi Imam Ibn Sahnun alisoma Fiqh ya Imam Maliki kwa Imam Al Buhlul Ibn Rashid na Imam Ali Ibn Ziyad na alikua ni mwenye kua na hamu kubwa sana yakusoma cihni ya Imam Malik mwenyewe lakini kutokana na matatizo ya kiuchumi basi hakufanikiwa kuelekea katika ardhi ya Madina kwa ajili ya kusoma kwa Imam Malik, kwani Imam Malik alifariki

kabla ya Imam Ibn Sahnun kupata pesa za kumtosheleza kwa ajili ya safai ya kuelekea katika mji wa Madina.

Hivyo mnamo mwaka 178 Al Hijra wakati Imam Ibn Sahnun alipokua na umri wa miaka 18 akafunga safari kuelekea nchini Misri na kusoma kwa Imam Abd Rahman Ibn Al Qasim ambae alisoma kwa Imam Malik kwa miaka 20, na hivyo kua ni Mwanazuoni anaeaminika na kukubalika sana katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Malik, Imam Ibn Wahb na Ashab na Imam Abd Allah Ibn Al Hakam ambao wote walikua ni Wanafunzi wa Imam Malik Ibn Anas na akasoma pia kwa Imam Al Layth Ibn Saad.

Baada ya kumaliza kusoma nchini Misri basi Imam Ibn Sahnun akarudi katika ardhi ya Maghrib huku akiwa ni mtu mwenye kuwiva na kua na Ilm kubwa sana ya Fiqh na ni mwenye umaarufu na kukubalika, ambapo katika kipindi hiki akaandika kitabu cha *Al Mudawwanah* cha Fiqh ya Imam Malik chenye upekee ambacho hata Wanafunzi wakubwa wa Imam Malik walikua hawakuwahi kuandika, kwani hikini kitabu kinachotokana na Kitabu cha Malik kiitwacho *Al Muwaatha*. Kitabu cha *Al Mudawwanah* cha Imam Ibn Sahnun ndio kitabu kinachotegmewa sana katika Fiqh ya Madhhab Imam Malik na ndicho kilichoyaeneza Madhhab ya Imam Malik katika maeneo mengi zaidi kutokana na kusomwa kwake na kufahamika.

Aliulizwa safari moja Ashshab: **'Hivi Jee ni nani aliekuja kwenu kutoka Maghrib?'** nae akasema: **'Sahnun'** mtu huyo akauliza: **'Jee si Asad Ibn Furat lakini?'** Ashshab akasema: '**Wa Allahi Ibn Sahnun ni bora kwa mara 99 kwa Fiqh kuliko Ibn Furat'**

Asad Ibn Furat alikua ni Mwanafunzi wa Imam Malik ambae alikua *Ma-shaa Allah* amejaaliwa na kwa Ilm na umahiri wa kupigana vita, na alikua ni kiongozi wa Jeshi Waislam katika mapigano ya kuiteka Sicily na ndie alieisambaza zaidi Fiqh ya Madhhab ya Imam Malik katika maeneo ya Afrika Kaskazini na kusini mwa bara la Ulaya.

Ambapo anasema Imam Adh Dhahabi kua: '**Asili ya Kitab Al Mudawwnah cha Imam Ibn Sahnun ni kutokana na Masuali ambayo Asad Ibn Furat alimuuliza Ibn Qasim, hivyo Ibn Sahnun alipoenda kusoma kwa Ibn Qasim akakutana na kitabu hicho ambacho kina Masuali hayo ambayo hata hivyo hayajajibiwa, kwani Ibn Qasima aliwachana nayo, hivyo Ibn Sahnun akayajibu masuali hayo na kuyapangilia kwenye mpangilio maalum kwenye kitabu chake hicho, na kuongezea masuali yake na majibu ndani yake kitabu hicho.**'

Imam Ibn Sahnun ni mtu ambae ni mwenye kuaminika sana, Mcha Mungu, Mkweli na alikua ni mtu mwenye kuachana na Dunia, ambapo anasema Imam Abu Bakr Al Maliki kua: '**Ibn Sahnun alikua ni mtu mkarimu, mwenye Khushuu, mwenye kulia kirahisi na mkali sana kwa wapotovu na wazushi**'

Imam Ibn Sahnun alipokua katika Ardhi ya Maghrib ambapo alichaguliwa kua Qadhi Mkuu lakini hata hivyo alikataa kuichukua nafasi hio, kutokana na Ucha Mungu wake, ingawa baadae alipopewa tena nafasi hio akaichukua lakini kwa masharti ya kua hataki kulipwa mshahara wowote, wala hataki kua na ukaribu wowote na Watawala, ambapo wadhifa huo wa Qadhi mkuu aliutumikia kwa mda wa miaka sita na kisha akafariki Dunia katika siku ya Jumatatu ya mwaka 240 Al Hijra huku akiwa na umri wa miaka 80.

IMAM IS-HAQ IBN RAHAWAYH 161 AH

Imam Abu Yaqub Is-haq Ibn Rahawayh Ibrahim Ibn Makhlad Ibn Ibrahim Ibn Mathar Abu Yaqub Al Handhali Al Marwazy alizaliwa katika mwaka 161 Al Hijra, katika maeneo ya Ardhi ya Nishapur na alikua akiitwa Ibn Rahawayh kwa sababu Baba yake alizaliwa kwenye Mitaa ya Mji wa Makkah na hivo watu wa Mji wa Marwa wakawa wanamwita *'Rahawayh'* neno ambalo linalomaanisha *'Mtu aliezaliwa Mitaani'* na mtoto wake ndio akawa anaitwa Ibn Rahawayh yaani Mtoto wa Baba aliezaliwa Mitaani.

Anasema Imam Ibn Khallikan kua: '**Imam Ibn Rahawayh alilizwa na Abd Allah Ibn Tahir ambae ni Gavana wa Khurasan kwa kusema kua: 'Jee unasemaje kuhusiana na jina la Ibn Rahawayh? Hivi ni nini maana yake hii Rahawayh? Na jee hulichukii jina hili wewe?' Ambapo Ibn Rahawayh akasema: 'La, Hakika mimi nnajua kua Baba yangu alizaliwa Mitaani katika Mji wa Makkah, hivyo yeye analichukia Jina hili lakini kwa upande mimi silichukii Jina hili.**''

Ambapo anasema Ali Ibn Is-haq ambae ni mtoto wa Imam Is-haq Ibn Rahawayh kua: **'Baba yangu alipozaliwa kutoka tumboni mwa Mama yake basi alikua ametobolewa masikio yake, hivyo Babu yangu akaenda kwa Fadhl Ibn Musa Al Sinani na kumuuliza juu ya hali hio ambapo nae akasema: 'Mtoto wako atakua ni Kiongozi wa Mema au ni Kiongozi wa Maovu.''**

Imam Ibn Rahawayh alisoma kwa baba yake katika ardhi ya Nishapur hadi pale alipofariki baba yake basi akaamua kuondoka katika Mji wa Nishapuri kwa ajili ya kujiendeleza zaidi Ki Ilm katika maeneo mengine ikiwemo Iraq, Sham na Hija.

Katika kutafuta kwake Ilm basi Imam Is-haq Ibn Rahawayh alisoma kwa Wanazuoni wengi, wakiwemo Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Muhamamd Idris Al Shafii, Imam Yahyah Ibn Adam Ibn Waqiyah bin Walid, Imam

Ahmad bin Hanbal, Imam Jabir Ibn Abdul Hamid Al Razy, Imam Ismail Ibn Umaiyah, Imam Waqiyah Ibn Al Walid n.k

Na ingawa alisoma kwa Wanazuoni wakubwa sana tofauti lakini alikua hakuna Mwalimu anaempenda na kumkubali kama Imam Muhamamd Idris Al Shafii, na hivyo Imam Is-haq Ibn Rahawayh alikua ni Mwanazuoni mkubwa sana katika Ulimwengu wa Kiislam ambae alikua ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, na katika kipindi cha mwishoni mwa Uhai wake alihamia katika maeneo ya Nishapuri na kua Mwanafiqh maarufu asiekua na mfano wake katika fani ya Ilm ya Hadith na Fiqh katika Madhhab ya Imam Al Shafii katika wakati wa kipindi cha uhai wake na hii ni kutokana na uwezo mkubwa wa ufahamu wake aliojaaliwa na Mola wake hivyo Imam Ibn Rahawayh alikua ni Imam anaekubalika na watu wengi sana wa maeneo hayo ya Nishapuri.

Kwani nasema Imam Abu Hatim Al Razi kua: '**Ni Miujiza ulivyokua uwezo wa Ibn Rahawayh katika kuhifadhi, kwani Uhifadhi wake ulikua hauna kasoro ya kukosea.**'

Na akasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Hakuna Mtu kama Ibn Rahawayh aliewahi kufuka Daraja la kuelekea Khurasan.**' Na akasema tena kua: '**Hakika mimi siwezi kuona mtu wa kumfananisha na Ibn Rahawayh katika Ardhi ya Iraq.'**

Imam Is-haq Ibn Muhammad Al Rahawayh alikua pia ni rafiki mkubwa sana wa Imam Ahmad Ibn Hanbal na pia alimsomesha Imam Ahmad Ibn Hnabla na kuwasomesha Wanazuoni wengi sana wakiwemo Imam Abu Ibrahim Ismail bin Yahya Al Muzani, Imam Abu Daud, Imam Al Hafidh Ad Darimi, Imam Ibn Abi Dunya, Imam Abu Abdillah Al Marwazi, Imam An Nasa'i, Imam Al Junaid Al Baghdadi,Imam Al Bukhari, Imam Muslim, Imam At Tirmidhi, Imam Muhammad Ibn Nashr Al Mawarzi, Imam Ahmad Ibn Sayyar, Imam Al Rabbi Ibn Sulaiman, nk.

Ambapo anasema Imam Abu Daud kua: '**Ibn Ruhawayh alitusomea sisi hadith 11,000 kutoka kwenye Ufahamu wake na kisha akazirudia moja baada ya moja kama alivyozinukuu hapo awali bila ya kupunguza wala kuongeza hata neno moja.'**

Imam Ahmad Ibn Hanbal aliulizwa kuhusiana na Imam Ibn Rahawayh hivyo akasema: '**Mnamuulizia Is-haq kuhusiana na nini? Kwani kwetu sisi Is-haq Ibn Rahawayh ni Imam wa Waislam.**' Kisha akaendelea kusema: **'Kwetu sisi Al Shafii ni Imam, Al Humaydi ni Imam na Ibn Rahawayh ni Imam.**'

Imam Ahmad Ibn Hanbal amesema tena kuwaambia Wanafunzi wake kua: **'Wakati Abu Yaqub, Chifu wa Waumini atakapokunulieni Kitu basi shikamaneni nacho ipasavyo**'

Ambao kuna watu walimtaja Imam Ibn Rahawayh mbele ya Qutaibah Ibn Said ambapo nae akasema: **‘Is-haq ni Imam’**

Imam Abu Hatim Al Razi nae akasema: **‘Is-haq Ibn Rahawayh ni Imam miongoni mwa Maimamu wa Waislam’**

Imam An Nasai akasema tena pia kua: ‘**Abu Yaqub Ibn Is-haq Ibn Mukhlid ni Thiqah na anaeaminika sana.**’

Ambapo kwa upande wa Wahb Ibn Jarir alisema: ‘**Namuomba Allah amlipe Is-haq Ibn Rahawayh, Sadiq na Yamur kwani wao ndio walioipa uhai Sunna katika ardhi za Mashariki’**

Nu’aym bin Hammad akasema kua: ‘**Kama ukimuona Mtu anasema vibaya kuhusiana na Ahmad Ibn Hanbal katika ardhi ya Iraq basi kua na shaka na Uislam wake, na ukimuona mtu katika ardhi ya Khurasan anamsema vibaya Is-haq Ibn Rahawayh basi kua na shaka na Uislam wake, na ukimuona mtu wa Basra anamsema Vibaya Wahb Ibn Jariri basi kua na shaka na Uislam wake.’**

Ambapo Imam Sid Ibn Dhuib alisema: ‘**Hakika mimi sijawahi kuona juu ya uso wa Ardhi mtu kama Is-haq Ibn Rahawayh**’

Imam Ibn Khuzaimah nae amesema kua: ‘**Wa Allahi kama Is-haq Ibn Rahawayh Ibn Ibrahim Al Handhali angekuwepo katika wakati wa Tabiina basi Tabiina wangeukubali ufahamu wake, Ilm yake na Fiqh yake.’**

Imam Ibn Hibban alisema: ‘**Is-haq Ibn Rahawayh ni miongoni mwa Mabwana wa Fiqh, Ilm, Ufaham, Kuhifadhi na Upana wa Mitizamo kwenye Vitabu vilivyoandikwa na Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* zimegawiwa, kwani alikua ni Mlinzi wa Sunna na kumsukuma yeyote yule alietofautiana nayo Sunnah’**

Imam Abu Hatim Al Razi amesema kua: **‘Mimi nilimtaja Is-haq Ibn Rahawayh kwa Abu Zurah kuhusiana na uwezo wake wa kuhifadhi Hadith, Matn na Sanad zake ambapo nae akasema: ‘Hakuna Mwenye kunukuu Hadith aliekua bora kwa kuhifadhi kama Ibn Rahawayh.’**

Imam Abu Hatim anaendelea kusema kua: **‘Miujiza yake ni katika Ukubwa wa uwezo wake na kutokukosea kuhusiana na kile alichojaaliwa katika ufahamu wake’**

Ahmad Ibn Salamah alisema kua: **‘Mimi nilimwambia Abu Hatim kua Ibn Rahawayh alikua pia anatufafanulia Qur’an kutoka Moyoni mwake’ ambapo Ibn**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Abi Hatim akasema: 'Na hii ndio Miujiza mikubwa zaidi, kwani kua na uhakika wa Sanad katika Hadith ni rahisi zaidi kuliko kua na uhakika wa Ufafanuzi wa Aya za Qur'an a maneno yake'

Qutaibah Ibn Said amesema: **'Ma Hafidh wa Khurasan ni Is-haq Ibn Rahawayh, kisha Abd Allah Ibn Abd Rahman Al Samarqandi na kisha Muhammad Ibn Ismail.'**

Muhammad Ibn Yahya Adh Dhuhali alisema kua: '**Mimi nilikutana na rafiki yetu Is-haq Ibn Rahawayh mnamo mwaka 199 Al Hijra katika Mji wa Baghdad, na wenye Ilm kubwa zaid miongooni mwa wenye Ilm ya Hadith waliokusanyika katika maeneo ya Rasafah miongoni mwao alikuwemo Ahmad Ibn Hanbal, Yahya Ibn Main na wengineo, na moyo wa kikao hicho alikua ni Is-haq Ibn Rahawayh na ndie aliekua msemaji.'**

Imam Abu Nuaym Al Asbahani anasema kua: **'Na miongoni mwa ni mwenye Ufalme wa kuheshimika, Imam Maarufu katika Hifdh na Fiqh Is-haq Ibn Ibrahim Al Handhai, ambae ni rafiki wa karibu wa Mwenye kutukuzwa na kuheshimika Ahmad Ibn Hanbal na rafiki wa anaepenedelewa zaidi ambae ni Imam Muhammad Idris Al Shafii. Ibn Rahawayh alikua ni mwenye kuzipa nguvu athari za Hadith, ambapo kwa wazushi na watu wenye maradhi ya nyoyo alikua ni muangamizaji'**

Na akasema Imam Al Khatib Al Baghdadi kua: **'Imam Is-haq Ibn Rahawayh alikua ni Imam wa Waislam, mweny Ilm kubwa sana ya Dini kwani ndani ya Ufahamu wake mna mkusanyiko wa Ilmya Hadith na Fiqh, mwenye Ufaham wenye kuhifadhi vizuri sana mkweli na mwenye Taqwa na mwenye kujitenga na Dunia'**

Imam Ibn Hajar Al Asqalani amesema kuhusiana na Imam Ibn Rahawayh kua: **'Ibn Rahawayh alikua ni mwenye kuaminika, al Hafidh wa Hadithm Mujtahid Mutlaq na rafiki wa karibu wa Ahmad Ibn Hanbal**'

Ahmad Ibn Said Al Ribati alisema kuhusiana na Imam Ibn Rahawayh kua :'**Ukaribu wangu kwa Allah, Umenifanya nimpende AbuYaqub Is-haq. Hakuifanya Qur'an kua ni yenye kuumbwa, Kama wasemavyo Wahalifu. Sunna Kamili ndio Tabia yake, Kuwalinda waliodhoofu kutoka kwa wenye nguvu**. **Ni Uthibitisho wa Allah kwa Viumbe wake, Wale waliopita kwenye maeneo ya Baqi**. **Baba yako Ibrahim alikua ni mwenye Taqwa, Mwenye Kukimbilia Ushindi na Mtoto wa mwenye kuongoza nkatika katika kukimbilia.'**

Ali Ibn Hajar akasema kuhusiana na Imam Ibn Rahawayh:

'Hakuna aliempita Is-haq kwa Ilm na Ufahamu, Tangu siku aliyondoka Khurasan Yuko wapi kama yeye.

Namuomba Allah amtilie Nuru uso wake na amhifadhi, kutokana na khofu katika siku ngumu aliyo chini ya mamlaka yake.

Na amlipe Firdaws yule atakaeitikia Amina na kumjaalia kumpa akitakacho katika siku ya Malipo.'

Abu Bakr Ibn Muhamamd Ibn Al Nadr Al Jarudi alisema kua: '**Mashaykh wetu na wakubwa zetu na kila tunaesoma kwake hua ni mwenye kumsifia Abu Yaqub Is-haq Ibn Ibrahim.'**

Imam Al Hakim nae amesema kua: **'Ibn Rahawayh ni Imam wa wakati wake katika Hifdh na Fatwa'**

Imam Abu Is-haq Al Shirazi amesema kua: **'Ibn Rahawayh amechanganya Hadith, Fiqh na Ucha Mungu.'**

Amesema Abd Allah Ibn Muhammad Al Farwa kua: '**Mimi niliingia kwa Yahya Ibn Yahya na nikamuuliza kuhusiana na Is-haq ambapo nae akasema: 'Kwa siku moja ya Is-haq basi hua ni yenye kupendwa na mimi kuliko maisha yangu.**''

Ahmad Ibn Said Al Murbati akasema kua: '**Kama Ath Thawry na Hamdani wangekua wako hai basi wangehitaji mengi sana kutokna kwa Ibn Rahawayh'**

Imam Abu Muhamamd Al Darani akasema kua: '**Ibn Rahawayh amewazidi watu wote wa Mashariki na Magharibi kwa Ukweli**'

Abu Nuaim Al Hafidh alisema kua: **'Ibn Rahawayh ni rafiki wa Ahmad Ibn Hanbal, na alikua muamsho wa hazina ya zamani ya Ilm na kwa wazushi alikua ni mwenye nguvu sana.'**

Imam Muhamamd Idris Al Shafii amesema kua: **'Ibn Rahawayh ni miongoni mwa Maimamu, anaeaminika na aliesalimika, kwani mimi nimemsikia Said Ibn Dhuayb akisema kua: 'Simjui Mtu yeyote yule kwenye uso wa Dunia kama Is-haq.''**

Muhammad Ibn Abd Al Wahhab anasema kua: **'Mimi nilikua na Yahya Ibn Yahya, na Is-haq Ibn Rahawayh akawa anakuja na alipokaribia mlangoni, ikawa amechelewa hivyo akamwambia Yahya: 'Tangulia kuingia ndani' ambapo na Yayha nae akasema: 'La Tangulia kuingia wewe' Ibn Rahawayh akasema: 'Ewe Abu Zakkariyah, hakika wewe ni mkubwa kiumri zaidi yangu hivyo tangulia' Yahya akasema: 'Naam, mimi ni mkubwa zaidi yako kiumri lakini wewe umenizidi mimi ki Ilm, Hivyo Tangulia kuingia ewe Ibn Rahawayh' Hivyo Ibn Rahawayh akatangulia kuingia ndani.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Muhammad Ibn Daud Al Dhubi anasema kua: '**Mimi nilimsikia Muhamamd Ibn Al Tusi akisema wakati Is-haq Al Handhali alipofariki kua: 'Simjui mtu yeyote yule mwengine aliekua akimuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama Ibn Rahawayh, na kama Sufyan Ath Thawry angekua hai basi ankua ni mwenye kumhitaji Ibn Rahawayh'''**

Muhammad Ibn Abd Salam amesema: 'Nilimwambia mimi Ahmad Ibn Said Al Riyati kuhusiana na Ibn Rahawayh ambapo nae akasema: 'Wa Allahi kama Ath Thawry na Ibn Uyaynah na Hamamd wangekua hai basi wangekua wanamhitaji Ibn Rahawayh' ambapo Muhammad Ibn Yahya Al Saffar alisema: 'Wa Allahi kama Hasan Al Basr angekua hai basi angemhitajia Ibn Rahawayh kwa mambo mengi sana''

Imam Ibn Rahawayh ndie aliemtia ari Imam Bukhari kuandika kitabu chake cha Hadith cha Sahih Bukhari kwani anasema Imam Bukhari kua: **'Sisi tulikua na Mwalimu wetu Is-haq Ibn Rahawayh ambapo alisema: 'Ingekua vizuri kama angetokea Mtu ambae angeandika kitabu kilichokusanya Hadith Sahih za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam'* haya yalikua ni maneno ambayo yaliamsha ari ndani ya Moyo wangu na hivyo nikaandika *Jamii As Sahih.'***

Mara ya kwanza Imam Is-haq Ibn Rahawayh wakati alipokua pamoja na Imam Ahmad Ibn Hanbal katika kuanza kusoma kwa Imam Muhamamd Idris Al Shafii katika Masjid Khayf uliopo Minna basi yalitokea mahojiano baina ya mtu na Mwalimu wake bila ya kujuana kuhusiana na kuuzwa, kukodishwa na kurithiwa kwa nyumba za Mji wa Makkah, kwani Imam Is-haq Ibn Rahawayh yeye anajua kua hairuhusiki kukodi wala kununua lakini Imam Muhammad Idris Al Shafii alisema kua inaruhusika kufanya hivyo kulingana na hadithi isemayo: '**Usama Ibn Zayd *Radhi Allahu Anhu* alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema kua: 'Ya *Rasul Allah* Jee Tufikie kwenye Nyumba yako Makka kesho?' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: 'Hivi Jee Aqeel ametuachia Nyumba Makka?'***(Sahihayn)* ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliuliza hivyo kwa sababu Aqeel aliiuza Nyumba ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati alipokua hayupo.

Na pia katika kipindi cha utawala wa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* basi *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* aliinunua nyumba ya Safwan Ibn Umayyah katika Mji wa Makka kwa Dirham 4000 na kuifanya kua Gereza.

Imam Al Shafii akasema na pia amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala kua:*

﴿لِلْفُقَرَآءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُواْ مِن دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلاً مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَاناً وَيَنصُرُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُ أُوْلَئِكَ هُمُ ٱلصَّادِقُونَ﴾

Lilfuqara-i almuhajireena alladheena okhrijoo min diyarihim waamwalihim yabtaghoona fadhlan mina Allahi waridhwanan wayansuroona Allaha warasoolahu ola-ika humu alssadiqoona.*(Surat Al Hashr 59:8)*

Tafsir: ***(Na pia kuna sehemu ya Ngawira) Kwa ajili ya Muhajirina na Mafukara waliofukuzwa kwenye Majumba yao na Mali zao wakitafuta fadhila za Mola wao kwa ajili ya kumridhisha. Na katika kumsaidia Allah na Mtume wake (Salallahu Alayhi wa Salam), hao ndio waliosadiki.***

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alizigawa nyumba hizo kwa watu wake waliokua wakizimiliki hapo kabla, au alizigawa kwa watu wengine?

Imam Ibn Rahawayh akasema: '**Alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule atakaefunga Mlango wake basi atakua salama na yeyote yule atakaeingia ndani ya Nyumba ya Abu Sufyan atakua Salama.'** na pia **'*Rasul Allahu Salallahu Alayhi wa Salam,* Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum* walifariki bila ya kutokea mtu kudai Mali zao za Makkah isipokua Ngo'mbe waliokua wakitembea bila ya uangalizi. Hivyo yeyote yule aliekua akitaka, na asietaka waliwaruhusu wengine kufanya hivyo, na huo pia ndio mtizamo wa Tabiina.**'*(Sunan Ibn Majah)*

Imam Al Shafi akarudia suali kwa kusema: '**Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alizigawa nyumba hizo kwa watu wake waliokua wakizimiliki hapo kabla, au alizigawa kwa watu wengine?**'

Imam Ibn Rahawayh akasema: **'Ushahidi unathibitisha usahih wa kauli yangu kutokana na kua baadhi ya Tabiina walivyosema juu ya hilo'**

Imam Al Shafii akawageukia watu wengine waliokuwepo kwenye darsa yake hio, na kisha akauliza: '**Huyu Ndio Nani?**' watu wakasema: **'Is-haq Ibn Ibrahim Ibn Rahawayh**' Imam Al Shafii akasema: '**Hivyo kumbe wewe ndie yule ambae watu wa Khurasani wanadai kua ndie Mwanafiqh wao? Mimi nnazungumzia kile ambacho *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* amesema, halafu wewe unasema kua: 'Ataa, Tawus, Al Hasan Al Basr na Ibrahim Ibn Adham wamesema, hivi jee kuna mtu**

yeyote yule ambae anaweza kuhoji kauli za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam?''*

Imam Ibn Rahawayh akasema: **'Soma aya isemayo:**

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ٱلَّذِى جَعَلْنَاهُ لِلنَّاسِ سَوَآءً ٱلْعَاكِفُ فِيهِ وَٱلْبَادِ وَمَن يُرِدْ فِيهِ بِإِلْحَادٍ بِظُلْمٍ نُّذِقْهُ مِنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ﴾

Inna alladheena kafaroo wayasuddoona AAan sabeeli Allahi waalmasjidi alharami alladhee jaAAalnahu lilnnasi sawaan alAAakifu feehi waalbadi waman yurid feehi bi-ilhadin bi*dh*ulmin nudhiqhu min AAadhabin aleemin *(Surat Al Hajj 22:25)*

Tafsir: ***'Kwa hakika wale waliokufuru na kuwazuia watu kutokana na njia ya Allah, na Masjid Al Haram ambao tumeujaalia kua uliofunguliwa kwa watu wote sawia, wanaoishi ndani yake na wanaotembelea kutoka sehemu nyengine wako sawa ndani yake. Na yeyote yule atakaelekea kutaka kufanya dhulma ndani yake basi tutamuadhibu kwa adhabu kali sana'***

Imam Al Shafii akasema: **'Hii ni kuhusiana na ndani ya Masjidi Al Haram tu'** Imam Ibn Rahawayh anasema: **'Baada ya kuona kua nimeshindwa basi nikanyanyuka na kuondoka.'**

Ambapo kuhusiana na aya hii basi anasema *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Hii inamaanisha kua Kila Muislam anatakiwa kua ni mwenye kuruhusiwa kuingia kwenye Masjid Haram iwe Mwenyeji au Mgeni na anayo haki ya kuishi kwenye Mji wa Makkah**' ambapo huu pia ndio mtizamo wa Imam Mujahid, Imam Abu Salih, Imam Zayd Ibn Aslam na wengineo. Ingawa kua makubaliano ya Ijmaa kua Eneo zima la Masjid Al Haram ni eneo ambalo ni la Waqf kwa ajili ya Waislam wa Duniani kote.

Ambapo hapo zamani Nyumba za Makkah zilikua hazina Milango, hivyo katika wakati wa Utawala wa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kuna mtu mmoja akaanza kuweka Mlango kutokana na wezi, na *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akapinga juu ya jambo hilo, lakini Mtu huyo akajitetea kua anataka kuhakikisha usalama wa vitu vyake, hivyo *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akakaa kimya juu ya jambo hilo na hivyo watu wengine nao wakaanza kutia milango kwenye nyumba zao.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo hata hivyo *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akaamrisha kua milango inayoeleekea Msikitini isifungwe iwachwe wazi katika kipindi cha Ibada ya Hija, ilikuwaruhusu Mahujaji kuingia na kumpumzika wanapotaka, ambapo Imam Malik anasema kua hukmu hii ni kwa ajili Msikiti wa Makkah tu, lakini kwa watu wengine wanaruhusika kufunga milango ya nyumba zao, na huo ndio mtizamo unaokubalia hadi hii leo na Wanazuoni wengine pia.

Ambapo kwa upade wa Abd Allah Ibn Amr Radhi Allahu anh basi yeye alisema kua: **'Yeyote yule atakaekodisha Nyumba katika Mji wa Makkah basi hua ni mwenye kula Moto'** na huo pia ni mtizamo wa Imam Ataa Ibn Abi Rabah, Imam Mujahid na wengineo ambapo kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi yeye amesema kua: **'Nyumba za Mji wa Makkah zinaweza Kumilikiwa na kurithiwa lakini hairuhusiki kuzikodisha.'**

Ambapo anasema Imam Zakarriyah Al Saji kua: '**Kuna baadhi ya marafiki zangu waliniambia mimi kua Ibn Rahawayh alibishana na Al Shafii wakati pia Ahmad Ibn Hanbal akiwepo miongoni mwao, kuhusiana na Ngozi ya Mnyama aliekufa kama ikikaushwa inaweza kutumika ama la.**'

Ambapo Imam Al Shafii kua inaweza kutumiwa na hii ni kutokana na uthibitisho wa Hadith isemayo: **'Amesema Abd Allah Ibn Abbas kua amesema Maimuna kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipita kwenye sehemu ambayo kulikua kuna Kondoo aliefariki, hivyo akasema: 'Jee hamtaki kunufaika na Ngozi yake?'''**

Ambapo Imam Ibn Rahawayh akasema kua: **'Amesema Ibn Akiim kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitandikia sisi barua mwezi mmoja kabla ya kufariki kwake kutuambia kua: 'Msijinufaishe na kitu chochote kutokana na Mnyama aliekufa, hata kuche zake walamishipa yake''** Hivyo Imam Al Shafii akasema: **'Unayoyazungumzia wewe ni Maandishi ya kwenye Barua wakati mimi nnazungumzia maneno yake yaliyo sikikana'**

Imam Ibn Rahawayh akasema: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuandikia pia Kaisar na naKhasrow, na ulikua ni ushahidi dhidi yao kuhusiana na A*llah Subhanah wa Ta'ala*'** Ambapo Imam Al Shafii akakaa kimya, na Imam Ahmad Ibn Hanbal aliposikia kuhusiana na hayo, basi yeye akawa ni mwenye kutumia Hadith ya Aqim ya uthibitisho wa Imam Ibn Rahawayh katika kutoa fatwa zake juu ya jambo hilo, huku Imam Ibn Rahawayh nae akaachana na Hadith yake hio na kufuata Mtizamo wa Imam Al Shafii kwa kutumia uthibitisho wa Hadith ya Maimuna.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Harb al-Kirmani anasema: **‘Nilimwambia mimi Is-haq Ibn Rahawayh hivi unasema kuhusiana na aya isemayo:**

﴿أَلَمْ تَرَ أَنَّ ٱللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِى ٱلسَّمَاوَاتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ مَا يَكُونُ مِن نَّجْوَىٰ ثَلاَثَةٍ إِلاَّ هُوَ رَابِعُهُمْ وَلاَ خَمْسَةٍ إِلاَّ هُوَ سَادِسُهُمْ وَلاَ أَدْنَىٰ مِن ذَٰلِكَ وَلاَ أَكْثَرَ إِلاَّ هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُواْ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُواْ يَوْمَ ٱلْقِيَامَةِ إِنَّ ٱللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ﴾

Alam tara anna Allaha yaAAlamu ma fee alssamawati wama fee al-ardhi ma yakoonu min najwa thalathatin illa huwa rabiAAuhum wala khamsatin illa huwa sadisuhum wala adna min dhalika wala akthara illa huwa maAAahum ayna ma kanoo thumma yunabbi-ohum bima AAamiloo yawma alqiyamati inna Allaha bikulli shay-in AAaleemun*(Surat Al Mujadila 58:7)*

Tafsir: ***Hivi Jee hukuona wewe kua Allah Subhanah wa Ta’ala*** **ni mwenye kujua kila kilichomo Mbinguni na Ardhini? Hakuna Najwa(Makutano ya Siri) baina watatu isipokua yeye ni wa nne, wala Watano isipokua yeye hua ni wa sita na haiwi zaidi ya hivyo au chini ya ya hivyo, bali hua nao popote pale watakapo kuwepo na baada ya siku ya Malipo atawajuulisha juu ya kile walichokua wakikifanya, kwani kwa hakika yeye ni mwenye kujua Juu ya kila kitu.**

Ambapo Imam Ibn Rahawayh akasema:

﴿ٱلرَّحْمَٰنُ عَلَى ٱلْعَرْشِ ٱسْتَوَىٰ﴾

Alrrahmanu AAala alAAarshi istawa*(Surat Tah-Ha 20:5)*

Tafsir: ***Mwingi wa Rehma yuko juu ya Arshi amekaa.***

Kuna makubaliano ya Wanazuoni kua Hii inamaanisha kua yeye ***Allah Subhanah wa Ta’ala*** **amekaa kwenye Arshi na anajua kuhusiana na kila kitu hadi chini kwenye Ardhi ya Saba.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kuna siku aliambiwa Imam Ibn Rahawayh na mmoja kati ya watu kua: **'Hakika mimi siamini kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kushuka kutoka katika Mbingu moja kuelekea kwenye mbingu nyengine' hivyo Imam Al Rahawayh akasema: 'Hakika Mimi nnaamini juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua ni mwenye uwezo wa kufanya anavyotaka.**'

Alisema Imam Is-haq Ibn Rahawayh kua: '**Tashbih (kumshabihisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Viumbe wake) hua ni kusema Mkono kama mkono au Mithili ya mkono. Au kusema Kusikia ni kama kusikia au mithili ya kusikia, hivyo Mtu akisema kua: 'Kusikia kwake ni kama kusikia au mithili yake' basi hii hua ni Tashbih tayari, lakini kama mtu akisema kua: *'Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema: 'Yad (Mkono), Sam (Kusikia) na Basar (Kuona) bila ya kusema kwa namna gani au vipi basi hii hua si Tashbih.'**'

Imam Abu Yaqub Is-haq Ibn Rahawayh Ibrahim Ibn Makhlad Ibn Ibrahim Ibn Mathar Abu Yaqub Al Handhali Al Marwazy alifariki katika mwaka 238 Al Hijra, akiwa na umri wa miaka 77 na aliwacha Wanafunzi wengi sana wakubwa wakubwa akiwemo mtoto wake aitwae Imam Abu Hasan Al Marwazi Muhammad Ibn Is-haq Ibn Rahawayh, ambae alikua Qadhi wa Madhhab ya Imam Al Shafii wa maeneo ya ardhi ya Marwazi.

Ambapo Mjukuu wa Imam Ibn Rahawayh alikua pia n Imam aitwae Imam Abu Tayyib Muhamamd Ibn Muhammad Ibn Is-haq Al Rahawayh ambae yeye alikua ni mfuasi wa Madhhab tofauti ya baba yake na babu yake ambao walikua ni wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, kwani yeye alikua ni Mfuasi wa Imam Malik.

IMAM ALI IBN AL MADINI 161 AH

Imam Abu Hasan Ali Abd Allah Ibn Jafar Ibn Najih Al Madini alizaliwa mnamo mwaka 161 Al Hijra katika Mji wa Basra nchini Iraq kutokana na famili ayenye Asili ya Mji wa Madina na nadio maana akawa anajulikana kwa umaarufu wa Imam Ali Ibn Al Madini.

Imam Ali Ibn Al Madini alikulia katika mazingira ya kielimu kwani alianza kusomeshwa na baba yake ambae ni Imam Abd Allah Ibn Jafar alikua ni Mwanazuoni mwenye Ilm kubwa ya Hadith kwani babu yake na Baba yake walisoma kutoka kwa Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu* na kwa Imam Abd Rahman Ibn Qasim Ibn Muhammad Ibn Abi Bakar Al Siddiq *Radhi Allahu Anhu*.

Hivyo mbali ya kua Imam Ali Ibn Al Madini alisoma kwa wazee wake lakini pia Imam Ali Ibn Al Madini alisoma kwa Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Hamad Ibn Yazid,

Imam Abu Damra, Imam Bishr Ibn Mufaddal, Imam Hatim Ibn Wardan,Imam Khalid Ibn Al-Harith, Imam Bishr Ibn Al-Sari, Imam Azhar Ibn Saad Al-Samman, Imam Harami Ibn Umarah,Imam Hassan Ibn Ibrahim,Imam Yahya Ibn Said Al-Qattan, Imam Yazid Ibn Zura, Imam Muad Ibn Muadh, Imam Abd Allah Ibn Wahb na wengineo. Hivyo Imam Ali Ibn Al Madini alikua ni Mwazuoni ambae yuko juu sana miongoni mwa Wanazuoni wa Hadith wa Mji wa Basra na Iraq kwa ujumla.

Ambapo kwa upande wake Imam Ali Ibn Al Madini alikua ni mwenye kubobea zaidi kwenye fani ya Hadithi na historia ya maisha ya Wanazuoni wa Hadithi na uhakikishaji wa usahih wa Sanad na Matn kiasi ya kua aliku ani mwenye kutegemewa sana kwenye fani hio, ambapo Imam Abd Rahman Ibn Mahdi alisema kuhusiana nae kua: '**Ali Ibn Al Madini ni mtu ambae ana Ilm kubwa sana ya Hadith.**'

Ambapo kwa upande wa Imam Bukhari ambae alisoma pia kwa Imam Ali Ibn Al Madini kua: '**Hakika mimi sijioni kua niko chini ya Mtu yeyote Kiilm isipokua kwa Ibn Madini.**'
Na anasema Imam Abu Ubaid Al Ajri kua: **'Aliulizwa Imam Abu Daud: 'Hivi Jee nani ni mwenye Ilm zaidi? Ahmad Ibn Hanbal au Ali Ibn Al Madini?' ambapo nae akajibu: 'Ali Ibn Al Madini ni mwenye Ilm zaidi kwani yeye ni mwenye kujua kuhusiana na tofati ya Hadith zaid ya Ahmad Ibn Hanbal.'**'

Ambapo anasema tena Imam Bukhari kua: '**Nimemsikia mimi Ali Ibn Al Madini akisema kua: 'Kua na ufahamu wa maana ya Hadithi hua ni kua na nusu ya Ilm na kua na ufahamu wa Ilm ya wanaonukuu Hadith in nusu ya Ilm''**

Hivyo kutokana na ukubwa wa Ilm yake basi Imam Ali Ibn Al Madini alikua akijulikana pia kwa jina *la Imam Al Hujjah, Amir ul Muuminin fi Al Hadith* na hili linaonekana wazi pale tunapowaangalia Wanafunzi wake ambao ndani yake tunakutana na kina Imam Muḥammad Ibn Yaḥyā Al Dhuhalī, Muḥammad Ibn Ismāil Al Bukhārī, Imam Abū Dāwūd, Imam Al Zafarani, Imam Al Baghawi, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Sufyan Ibn Uyaynah pia na wengineo.

Kwani anasema Ahmed Ibn Yusuf Al-Bujairi: **'Amesema Al Ayni kua: 'Nimemuona Ali Ibn Madini akiwa amekaa huku Ahmad Ibn Hanbal akiwa kulia kwake na Yahya Ibn Main akiwa kushoto kwake huku yeye akiwa anawanukulia Hadith.'**

Ambapo anasema Imam Abu Hatim kua: '**Imam Ali Ibn Al Madini ni Mwanazuoni wa watu wenye Ilm ya Hadith na Sanad**'

Ambapo amesema Khalaf Ibn Walid Al Jawhari kua: '**Siku moja Sufyan Ibn Uyaynah alitoka na kuja kwetu huku Ali Ibn Al Madini akiwa pamoja nasi ambapo Ibn**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Uyaynah akasema: 'Kama si Ali Ibn Al Madini basi mimi nisingetoka na kukufuateni''

Kwani Imam Sufyan Ibn Uyaynah alikua pia na urafiki wa karibu sana na Imam Ali Ibn Al Madini kwani mbali ya kua yeye Imam Sufyan Ibn Uyaynah alikua ni Mwalimu wa Imam Al Madini lakini Imam Al Madini pia alikua akimsomesha Imam Ibn Uyaynah na iliku ahakuna anaezijua Hadith nyingi za Imam Sufyan Ibn Uyaynah kama Imam Al Ibn Al Madini.

Na akasema Imam Sufyan Ibn Uyaynah: '**Watu wananilaumu mimi kwa kua ni mwenye kumpenda Ali Ibn Al Madini, lakini Wa Allahi hakika mimi nnajifunza engi sana kutoka kwake kuliko anayojifunza yeye kutoka kwangu.**'

Na Imam Yahya Ibn Said Al Qattani akasema kua: **'Sisi tulikua tukinufaika nae sana Ali Ibn AlMadini kuliko yeye alivyokua akinufaika nasi.'**

Imam Yahya Ibn Main anasema kua: '**Ali ndie aliekua akiwanukulia watu kutoka kwa Yahya Al Qattan, mimi nilionana nae zaidi ya mara 10,000 na alikua na Ilm kubwa sana**'

Ambapo anasema Yaqub Al Fasawi anasema kua: '**Mimi nilimsikia Abd Rahamn Ibn Abi Abbad Al Qalzami ambae alikua ni rafiki yake Ali Ibn Al Madini akisema kua: 'Ali Ibn Al Madini alikuja kwetu siku moja na akasema: 'Nimeona mimi usingizini katika usiku huu kua nimenyoosha mikono yangu na kisha nikachomoa Nyota mbili na kisha nikazila, hivyo tukaenda nae kuulizia kwa wanaojua ambapo nao wakasema kua: 'Hii inamaanisha kua wewe utakua na Ilm kubwa sana'''**

Ambapo anasema Walid Ibn Al Qasim kua: **'Alisema Abd Rahman Al Nasai kua: 'Hali ilikua kama vile *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimuumba Ali Ibn Al Madini kwa ajili ya Ilm tu''**

Ambapo Muhamamd Ibn Yunus anasema kua: **'Nimemsikia mimi Ali Ibn Al Madini akisema kua: 'Nimeachana naHadithi 100,000 kutoka katika Hadith zangu ambapo 30000 kati yake hadith hizo ni kutoka kwa Abbad Ibn Suhayb''**

Abd Allah Ibn Abi Ziyad Al Qatwani anasema kua: '**Nimemsikia mimi Abu Ubayd akisema kua: 'Ilm imebakia kwa watu wanne ambao ni Abu Bakr Ibn Shaybah, Yahya Ibn Main, Ahamd Ibn Hanbal ambae ndie mwenye Ilm kubwa zaidi ya Ilm hio, Ali Ibn Al Madini ambae ndie mwenye kubwa zaidi ya Wote.**''

Na Abbas Al Anbari anasema kua: '**Nimeambiwa mimi kua kama ingekua kuna uchaguzi wa kuchaguliwa basi Ali Ibn Madini angempita Hasan Al Basr kwa Ilm,**

kwani watu walikua wanaandika kuhusiana na namna anavyokaa, anavyosimama, anavyovyaa na kila kitu anachofanya'

Imam Ali Ibn Al Madini aliandika pia vitabu vingi vya hadith ambapo kitabu chake kiitwachao Musnad Al Madini lakiin hata hivyo kitabu hicho kilitoweka baada ya kuliwa na mchwa kama anavyosema mwenyewe kumwambia Al Abbas Ibn Abd Azim kua: '**Niliandika mimi Musnad katika kufanya uchunguzi wangu, na kisha nikaiweka kwenye sanduku langu na nikasafiri lakini niliporudi nikakuta kitabu changu hicho kimeliwa na mchwa chote.'**

Muhammad Ibn Talib Ibn Ali Al Nasafi anasema kua : '**Nimemsikia mimi Salih Ibn Muhamamd akisema kua: 'Mwenye Ilm zaidi ya wale walionisomesha mimi Hadithi na Kasoro zake ni Al Ibn Al Madini, na mwenye Ilm kubwa ya Hadithi ni Ahmad na mwenye utaalamu zaidi ni Sulayman Al Shadhkuni**''

Imam Ali Ibn Al Madini alikua ni Mwanafunzi wa Imam Al Shafii pia ndie alieandika kitabu cha Imam Al Shafii cha Al Risala na kukichukua na kukipelekea kwa Khalifa Abd Rahma Ibn Mahdi

Hadith za Imam Ali Ibn Al Madini zinapatikana ndani ya Kitabu cha Imam Bukhari ambazo ni 303, na pia katika Al Tahdhib Al Tahdhib cha Al Hafidh Imam Ibn Hajar Al Asqallani, Imam Abu Daud, Imam Ibn Majah, Imam An Nasai, Imam At Tirmidhi n.k

Kwani amesema Imam An Nawawi kua: '**Ama kuhusiana na Ali Ibn Al Madini basi kuna makubaliano ya Wanazuoni kuhusiana na Ufalme wake, Uongozi wake na Umahiri wake katika Ilm hii ya Hadith**' na kwa upande wa Imam Adh Dhahabi basi yeye anasema kua: '**Ama kuhusiana na Ali Ibn Al Madini basi kwake yeye ndio mwisho wa Ilm ya kina ya Matokeo ya hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, ndio kwenye ukamilifu wa ukosajia wa wanaonukuu nauwezo wao wa kuhifadhi. Kwani Ali Ibn Al Madini ni mfano wa pekee katika kizazi chake ani bingwa pekee wa Ilm ya Hadithi**'

Na akasema Imam Abu Ya'la kua: '**Imam Ali Ibn Al Madini ni Al Hafidh mwenye upekee wa kipekee**'

Imam Abu Daud anasema kua: 'Al Farhayani aliulizwa kuhusiana na Yahya Ibn Main, Ali Ibn Al Madini, Ahmad Ibn Hanbal na Abu Khaitham ambapo nae akasema: '**Ama kuhusiana na Ali basi ndie mwenye Ilm kubwa zaidi ya Haidthi na Sanad zake miongoni mwao, ama Yahya basi ni mwenye Ilm ya Rijali walionukuu, ama Ahmad yeye basi ni mwenye Ilm kubwa ya Fiqh na Abu Khaitham ni mwingin wa Hikma.'**

Kwa kua Imam Ali Ibn Al Madini aliishi katika kipindi cha mitihani ya Mutazila basi nae pia alikumbwa na mitihani hio kutoka kwao ambapo anasema Imam Taqi Ad Din Al Subki kua: '**Ali Ibn Al Madini alikua ni miongoni mwa walioulizwa kuhusiana na uumbwaji wa Qur'an, na akajibu kwa kukubali, ambapo sisi ni wenye kusema kua kutokana na mtizamo wetu basi ni kua Ali Ibn Al Madini alijibu hivyo kwa sababu ya kuogopa Upanga.'**

Imam Al Hafiz Ibn Hajar Al Asqallani anasema katika Al Taqrib kua: '**Watu wanamlaumu Ali Ibn Al Madini kuhusiana na jibu lake kuhusiana na kuumbwa kwa Qur'an, lakini alikua ni mwenye kutubu baadae kwani alijibu kutokana na khofu.**'

Na anasema Ibn Uday kua: '**Mimi nimemsikia Musaddah Ibn Abi Yusuf Al Falusi akisema kua: 'Mimi nilimwambia Ibn Al Madini: 'Hivi kutokana na Ilm yako inakuaje ukajibu nilivyojibu mimi?' ambapo nae akasema: 'Ewe Abu Yusuf Upanga sio kitu rahisi kwako wewe, na kwa upande wangu mimi ningeuliwa, na hata kama ningepigwa mjeledi tu basi ningekufa.'**''

Imam Ali Ibn Al Madini alifariki katika siku ya Jumatatu ya mwaka 234 Al Hijra. Ambapo Imam Al Bukhari alisema kua: '**Ali Ibn Al Madini alifariki siku mbili kabla ya kumalizika mwezi wa Dhul Qaadah katika mwaka wa 234 Al Hijra'**

IMAM AHMAD IBN HANBAL 164 AH

Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hanbal Al Shaibani alizaliwa mwaka 164 *Al Hijr*, miaka 14 baada ya kufariki Imam Abu Hanifa, miaka kumi na nne baada ya kuzaliwa Imam Al Shafi'i na pia miaka kumi na tano kabla ya kufariki Imam Malik. Babu yake Ahmad ambaye ni mzee Hanbal alikuwa ni Gavana wa Khurasan, ambayo leo inajulikana kama Asia ya kati, eneo la Kaskazini ya Afghanistan, India na Pakistan ingawa alikua si mtu wa Khurasan bali alikua ni mwarabu wa Iraq. Ahmad Ibn Hanbal hakuwahi kumuona baba yake kwani alifariki wakati Ahmad akiwa mdogo sana.

Baada ya mda familia yao ikarudi Baghdad mji ambao kwa wakati huo ulikua umenawiri na kuwiva katika a *I'lm* ya dini. Ahmad na mama yake wakawa wanaishi kwa mjomba wake Ahmad ambae alishughulikia upatikanaji wa *I'lm* ya Ahmad, lakini aliemsaidia zaid alikua ni mama yake ambae alikua ni mtu mwenye Imani kubwa ya dini. Imam Ahmad Ibn Hanbal alihifadhi *Qur'an* akiwa bado na umri mdogo, baada ya kumaliza kuhifadhi *Qur'an* alienda moja kwa moja kwa Abu Yusuf, Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa na akawa anajifunza somo la *Fiqh*. Lakini baada ya kufikia miaka kumi na

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

mitano akawacha baada ya kuona bora kwanza aende katika bahari ya *I'lm* ya *Hadith* ambayo aliiogelea ndani yake kwa miaka saba.

Katika kipindi hiki cha miaka saba Ahmad Ibn Hanbal alihifadhi *Hadith* milioni moja, ingawa sio zote zilizokua tofauti, bali zilikua zinatofautiana wapokeaji. Alikua akihudhuria darsa za *Hadith* kwa Mwanahadith mkubwa katika mji wa Baghdad alieitwa Imam Hasheem Ibn Bashir As-Sulamy, vile vile alikua kila akisikia kuna Mwanazuoni amekuja Baghdad, alikua lazima afanye kila njia hadi aonane nae ili kupata kusoma darsa zake. Kwa njia hii pia alisoma kwa Nuaim Ibn Hammad, Abdul-Rahman Ibn Mahdi na `Umayr Ibn A'bd Allah Ibn Khalid.

Ahmad Ibn Hanbal alitembea kila sehemu ambayo husikia kuna *Hadith* za Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* kama vile Iran, Khurasan, Hijaz, Yemen, Syria, Iraq. Ambako alisoma *Hadith* kwa Wanazuoni wakubwa wakubwa miongoni mwao Yahya Ibn Sa`id Al-Qattan, Abu Daud At Tayalisi, Waki` Ibn Al-Jarraah, Abu Mu`awiyah Ad-Darir, Sufyan Ibn `Uyainah, na Imam Al Shafi'i.

Inasemakana kua kuna kipindi Ahmad Ibn Hanbal alisikia kua Yemen kuna mwanahadith anaeitwa Abdul Razaq Al Sanaani, hivyo akaamua kusafiri kutoka Iraq hadi Yemen kuenda kupata *Hadith* ambazo yeye Ahmad alikua hana, lakini alipofika Makkah akasikia kua Abdul Razaq Al Sanaani ameshafariki dunia. Hivyo ikambidi aakhirishe safari safari yake hiyo.

Abu Zurah anasema '**Imam Ahmad alihifadhi *Hadith* milioni, kati yao zikiwemo *Hadith Musnad* 30000**. Ukiangalia *Hadith* milioni moja ni nyingi lakini hazikua *Hadith* zote ni tofauti, bali ilikua nyingi kati ya hizo zinafana, kwa kua *Hadith* moja ika*Hadith*iwa na wapokeaji tofauti, hivyo ugumu wake unakuja pale inapobidi kuwatofautisha wapokeaji wa *Hadith* hizo. Miongoni mwa *Hadith* hizo pia kulikua na *Hadith* sahih na *Hadith* dhaif.

Imam Ahmad Ibn Hanbal alikusanya *Hadith Musnad* kutoka kwa Walimu 280, alikulia na kuishi ndani ya sunna kwani alisema '**Sikuwahi kuandika *Hadith* ambayo sikuwahi kuifanyia kazi**', hata watoto wake pia aliwalea katika maisha aliyokua akiishi, anasema mtoto wake anaeitwa A'bd Allah Ibn Ahmad Ibn Hanbal kua Imam Hanbal alikua akicheza nae kwa kumwambia '**Fungua sehemu yeyote ya *Musanaf* ya Waki, halafu niulize *Hadith* yeyote, nami nitakuambia msururu wa walioipokea, au nitajie msururu wa wapokeaji nami nitakutajia *Hadith* yenyewe**.'

Alipokutana na Imam Al Shafi'i, Ahmad Ibn Hanbal alijitolea kila kitu ili aweze kusoma kwa Mwanazuoni huyo mkubwa kwa wakati huo**,** ambapo alisoma *Fiqh* na Kanuni zake. Ahmad Ibn Hanbal pia hakuanza kusomesha wala kutoa Fatwa hadi mwaka 204 *Al Hijr* baada ya kufariki Imam Al Shafi'i. Hivyo Ahmad Ibn Hanbal akawa mrithi mkubwa wa

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam mkubwa alietangulia. Imam Ahmad Ibn Habal alikua akisomesha mara mbili, ya kwanza ilikua nyumbani kwake kwa Wanafunzi wake wenye hamu kubwa ya *I'lm* na ya pili ilikua baada ya Salat al Asr msikitini kwa watu wa kawaida wenye kutafuta *I'lm*.

Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua na Wanafunzi wengi na waliokua juu katika *I'lm* ambao baadae waliieneza *Fiqh* yake sehemu mbalimbali, Mwanafunzi wake mkubwa na ambae alikua nae karibu sana alikua akiitwa Abu Bakr Al-Maruzy, Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema kuhusu Al Maruzy kua '**Chochote kile Al-Maruzy akisema nimesema mimi basi mjue kua ni kweli nimesema mimi**.', Wanafunzi wake wengine ni pamoja na Abu Bakr Al-Athram, Ishaq Ibn Mansur At-Tamimi, Ibrahim Ibn Ishaq Al-Harbi, Al-Bukhari, Muslim, Abu Daud na Baqi Ibn Makhlad.

Imam Adh Dhahabi anamuelezea Imam Ahmad Ibn Hanbal kua ni '**Ni Shaykh wa kweli na ni kiongozi wa Waislam katika wakati wa Uhai wake,** mwanahadith **mkubwa na ni Uthibitisho wa Dini**'.

Imam Ahmad Ibn Hanbal aliandika kitabu cha *Hadith* kinachoitwa *Al Musnad* na *Az-Zuhd, As-Sunnah, Al-Wara` wa Al-Iman, na Fada'il As-Sahabah,* lakini hakuwahi kuandika Fatwa zake, kitabu cha *Fiqh* yake, wala hakumpa Mwanafunzi wake kazi ya kufanya hivyo, na alikua akisema '**Usifuate ushauri wangu, wala ushauri wa Malik wala ushauri wa Al Shafi'i, wala wa Awzai wala wa Ath Thauri, lakini chukua tulipochukua sisi**'.

Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua ni mtu ambae hapendi Fatwa zake ziandikwe, na ilikua hivyo hadi alipofariki na Abu Bakr Al-Khallal ambae ni Mwanafunzi wa Al-Maruzy alipokusanya na kuiandika *Fiqh* ya *Madhhab* ya Hanbal. Al Khallal alisafiri sehemu tofauti kutafuta na Fatwa ambazo ziliandikwa na Imam Hanbal na kuzikusanya katika kitabu chenye matoleo 20 kinachoitwa *Al-Jami` Al-Kabir*.

Abu Al-Qasim Al-Khiraqi ambae alikua Mwanafunzi wa Al Khallal aliandika mukhtasari wa kitabu kilichoandikwa na Al Khallal ambacho kiliitwa *Mukhtasar Al-Khiraqi*. Kitabu ambacho kilipendwa sana na wana *Fiqh* wa *Madhhab* ya Hanbal ambao nao baadae waliandika vitabu zaidi ya 300 wakiielezea *Mukhtasar Al Khiraqi*, na miongoni kati ya vitabu hivyo ni pamoja na *Al Mughni* kilichoandikwa na Ibn Qudamah Al-Maqdisi. Baadae, Imam Abd Salam Ibn Abd Allah, babu yake Imam Ibn Taymiyah, aliziharir upya Fatwa za Imam Ahmad na kuandika kitabu cha *Fiqh* kinachoitwa *Al-Muharir* .

Kabla ya kufariki *Khalifah* Harun Rashid ambae alikua ni mfuasi wa Ahlu Sunah wa Jamaah, aliwachagua watoto wake ambao walikua Wanazuoni wakubwa Al-Amin na Al-Mamun waongoze, Al Amin alikua Mutazilah lakini hakulazimisha al Itizal, lakini

ndugu yake Al Maamun ndie alieufanya Mutazilah kua ni jambo la kimataifa. Mutazilah ni kundi la mwanzo katika historia ya Kiislam ambalo hutumia fikra na ufahamu wa *Bani Adam* kutafsir mambo ya dini.

Wakati wa utawala wa Kikhalifah wa Al Maamun akida za Mutazilah zilichipukia na kuongezeka. Mutazilah waliingiza Falsafa za Mashariki katika dini na uhuru wa kifikra. *Khalifah* Ma'mun akaanzisha *'Halaqat Tarjuma' au* huduma za kutafsiri, katika kipindi hiki kila kitabu kilitafsiriwa vikiwemo vya mambo ya uchawi na uganga wa kienyeji pia, jambo ambalo lilileta sura mbaya kwa watawaliwa.

Mwaka 218 *Al Hijr*, alipokua akitawala *Khalifah* Al Ma'amun, Imam Ahmad Ibn Hanbal alikamatwa kufungwa jela kwa kosa la kukataa kukubali kua *Qur'an* imeumbwa. Wanazuoni wengi waliadhibiwa kwa kutokubaliana na hilo, na Imam Ahmad Ibn Hanbal alikuwa miongoni mwao, alifungwa jela kwa zaid ya miaka miwili. Alipotawala *Khalifah* Al Wathiq alimwachia Imam Hanbal lakini akamfunga kifungo cha nyumbani, hana ruhusa ya kuenda msikitini kusali wa kusomesha. Hali ilibadilika baada ya kutawala Al Mutawakil ambae alifuta muonekano wa kuwa *Qur'an* imeumbwa na akamruhusu Imam Hanbal kuendelea kusalisha na kusomesha msikitini.

Baada ya Imam Hanbal kua huru na kifungo cha nyumbani, Khalifah Al Mutawakil alimpelekea zawadi nyingi kumliwaza. Baada ya kuona zawadi hizo Imam Hanbal, alilia sana na kusema

'***Inni akhafu min fitnatil ni'ma akthar min fitnatil Mihna,***'

Tafsir, '**Hakika nnaikhofia fitna ya neema hii zaidi kuliko fitna ya kukaa jela**'. Na akaamua kuzigawa zawadi hizo kwa watu wengine.

Imam Ahmad Ibn Hanbal aliulizwa Jee Allah ataonekana siku ya kiama. Akajibu '**Hii imethibitishwa na *Hadith* Sahih, tunazoziamini na kuzikubali, nasi tunakubali kila kitu alichokisema Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* kikiwa na usahihi wa waliokipokea. Tunaamini na kuthibitisha**'.

Ibn Dharih al-'Ukbari alisema: '**Nilitaka kumuona Ahmad bin Hanbal. Hivyo nilionana nae, alikua mtu mzima aliepaka hina nywele zake, alikua mrefu na si mweupe sana**.'

Muhammad Ibn Abbas An Nahwi alisema: '**Nilimuona Ahmad bin Hanbal akiwa na uso mzuri na wa kuvutia, alipaka hina nywele zake ambazo zilikua si nyueusi sana. Alikua na ndevu nyeusi na nguo nyeupe. Alivaa kilemba na *izar*.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Abd al-Malik al-Maymuni amesema: ‘**Sijui kama nimewahi kumuona mtu alievaa nguo safi na nyeupe, anayejishughulikia na kupunguza sharubu zake na kuchana nywele zake vizuri na ndevu zake vizuri kama Ahmad Ibn Hanbal**.’

Al-Fadl Ibn Ziyad alisema: ‘**Nilimuona Abi Abdillah wakati wa kipupwe alivaa shati mbili na fulana ya rangi, na pia huvaa sweta nzito. Na pia nilimuona akivaa kilemba na nguo nzito, nikamsikia Abu 'Imran al-Warkani akimwambia: ‘Ya Aba Abdillah Nguo zote hizo?’** Abi Abd Allah alicheka na kusema: **‘Baridi mimi siiwezi.**’

Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua ni mtu mwenye kuwapenda sana watoto wake na alikua akiwausia kuhusiana na mambo ya Akhera na vile vile juu ya mambo ya kidunia, miongoni mwa wasia alimuusia mtoto wake alipokua akijitayarisha kuoa kumwambia kua: **Ewe mtoto wangu hutokua na furaha ndani ya nyumba yako hadi pale utakapokua na sifa 10 ambazo unatakiwa kumuonesha mke wako, hivyo zikumbuke, zisimamie na uzitekeleze kwa dhati.**

Ama kwa sifa mbili za mwanzo ni kua: Wanawake huhitaji uangalifu na kuwajali na hupenda kutamkiwa wazi kua wanapendwa. Hivyo usiwe mchoyo katika kuweka wazi mapenzi yako kwa mkeo. Ukiweka mpaka katika kuelezea mapenzi yako, utajenga ukuta baina yako na yake yeye, na hivyo kupunguza hisia za mapenzi baina yenu.

Wanawake hua wanachukia wanaume wakali, lakini huwatafuta wale wenye ulaini, hivyo zitumie sifa mbili hizi itakiwavyo. Jambo hili litaleta mapenzi zaidi na kukuletea utulivu akilini mwako.

Wanawake hupenda kutoka kwa waume zao kile ambacho wanaume hupenda kupata kutoka kwa wake zao, kama vile manenolaini, kupendeza,usafi na harufu nzuri. Hivyo daima dumu katika hali kama hiyo.

Kwa hakika, nyumba hua iko chini ya mamlaka ya mwanamke, hivyo anapoka ndani yake hua anajihisi amekalia taji lake la kimalkia, na kua yeye ndio kiongozi wa nyumba. Hivyo kaa mbali na kutaka kuyaangamiza Mamlaka hayo na kamwe usijaribu kufanya hivyo. Kwani mfalme hua na hasira sana kwa yule anaetaka kumvua madaraka yake, hata kama ikiwa alikua anajaribu kuonesha kitu chengine kilicho bora zaid.

Mwanamke hua anampenda mumewe, lakini wakati huo huo hua hataki kuwapoteza watu wa familia yake, hivyo usijaribu kujiweka katika darja moja na wazee wake, kwa sababu utamuweka katika kukuchagua wewe au familia yake.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na hata kama akikuchagua wewe na kuiwacha familia yake basi atakua katika hali ya wasi wasi, jambo ambalo alitapelekea kujenga chuki katika maisha yenu.

Kwa hakika mwanamke ameumbwa kutokana na mfupa wa mbavu iliopinda, na hii ndio siri ya kuvutia kwake. Na wala sio kasoro yake, kwa sababu 'Nyusi hua zinavutia kutokana na kua zimepinda'. Hivyo akikosea, usimkaripie katika hali ambayo itakua haina upole ndani yake, kwa kutaka kumnyoosha, vyenginevyo utakua ni mwenye kumvunja, na kumvunja kwake ndio Talaka yake. Vile vile usimuachie bila ya kumkosoa makosa yake, kwani vyenginevyo ubaya wake utazidi na atakua na kibri na Nafsi yake. Baada ya hapo hatolainika tena wala hatokusikiliza tena hivyo kua ni mtu wa kati na kati.

Ni maumbile ya mwanammke kutokua na shukrani na mume wake na kukataa neema zake. Hivyo ukiwa mkarimu kwa kwa miaka yote na ukawa mgumu kwa mara moja tu basi atasema, 'Sijawahi kuona wema wowote kutoka kwako'. Hivyo usiiruhusu tabia yake hii ikakufanya kua humpendi au kujitenga nae. Kwani ikiwa huipendi tabia yake hii basi utakuta tabia nyengine zinazokupendezea, hivyo tengeneneza uwiano katika hayo.

Kwa hakika kuna wakati ambao mwanamke hua anapitia kipindi cha mabadiliko ya udhaifu na uchovu wa kiakili. Kiasi ya kua Allah amemruhusu na kumuachia kutofanya mambo ya fardhi ya Ibada katika wakati huo;

Allah amemsamehe katika kusali, na akamuaghairishia siku za kufunga katika kipindi hiki hadi kipite na awe katika hali ya kawaida. Hivyo katika kipindi hiki kua nae pia katika hali kama ile alivyofanyiwa na Mola wake, kama vile Allah alivyomsamehe na kumrahisishia baadhi ya mambo basi nawe pia mpunguzie majukumu yake kwako katika siku kama hizo.

Mwishoni, fahamu kua mwanamke ni mtumwa wako hivyo kua ni mwenye ukarimu na rehma juu yake.

Imam Hanbal aliwasomesha watoto wake *I'lm* ya dini hadi nao wakawa pia ni miongoni mwa wenye *I'lm* kubwa kwani watoto wake A'bd Allah na Salih walikua walikua ni wana*fiqh* pia. Imam Ahmad Ibn Hanbal alifariki katika mwezi wa Rabi` Thani 12, AH 241 akiwa na umri wa miaka 77. Inasemakana maziko yake yalihudhuriwa na mji mzima wa Baghdad, kwani walihudhuria wanaume 100,000 na wanawake 60,000.

Ambapo anasema Imam Abi Yala kuhusiana na Imam Ahmad Ibn Hanbal na mke wake : **'Mke wa Imam Ahmad Ibn Hanbal aliefariki katika wakati wa uhai wake Hanbal ambae ni mama wa mtoto wake Salih, alikua akisifiwa na Imam Hanbal ambae**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

alikua kisema: 'Ummu Salih aliishi na mimi kwa mda wa miaka 20 na hatujawahi kupingana hata kwa neno moja''

Moja kati ya sifa waliyokua nayo baadhi ya wafuasi wa *Madhhab* ya Imam Hanbal ni kutokua na ustahmilivu dhidi ya mitizamo ya wafuasi wa *Madhhab* mengine ya Kiislam, jambo ambalo mara nyingi huwapelekea kuonekana kua ni wakaidi sana, baadhi ya sifa hizi bado pia bado ziko hadi leo miongoni mwa wafuasi wa *Madhhab* hayo, jambo ambalo limepelekea upunguaji wa kupendwa kwao, na kukirihisha kwa baadhi ya mitizamo ya Mashaykh wao kama vile mitizamo ya Shaykh Ahmad Ibn Taymiyyah na Shaykh Abdul Wahab.

IMAM MANSUR IBN AMMAR

Imam Abu Sirr Sulaymi Mansur Ibn Ammar Ibn Kathir alizaliwa Mjini Marwazi na aliishi katika maeneo ya Basra na alikua ni Mwanazuoni wa hali ya juu alisoma kwa Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Abd Allah Ibn Luheya, Imam Munkadir Ibn Muhammad, Imam Bishr Ibn Talha na kadhalika.
Safari moja Imam Mansur Ibn Amar alikua safarini ambapo njiani akaona kartasi ambayo imeandikwa *Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahim* na hivyo akaiokota lakini akashindwa kupata sehemu ya kuihifadhi na hivyo akaamua kuitia mdomoni na kuila badala yake, na alipolala katika usiku wa siku hio basi aliota akiambiwa kua: **'Kwa hakika tumekufungulia Mlango wa Hikma na Busara kutokana na Kartasi uliyoihifadhi kwa kuimeza.'**

Anasema Imam Mansur Ibn Ammar kua: 'Siku moja mimi nilienda nchini Misri, ambapo kulikua kuna ukame mkubwa sana, hivyo baada ya Sala ya Ijumaa, watau walilia na kuomba Dua, ambapo mimi nakumbuka kua mimi nilienda kati kati ya Msikiti nakuwausia watu wa nchini humo na kuwaambia: 'Enyi watu Mkaribieni *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kutoa Sadaqah kwani hio ndio njia pekee rahisi ya kumkaribia zaidi.'

Na kisha nikasema: 'Ewe Mola wangu, hakika mimi sina kitu isipokua Joho langu, lakini hata hivyo nalitoa kwa ajili yako, na hivyo nikalivua na kulirusha kwa watu, ambapo watu waliokuwepo hapo mbele yangu nao wakalipokea na kutoa kutia vitu vyao walivyokua wakivitoa na kisha tukavigawa vitu hivyo kwa masikini, na haukuchukua mda isipokua Mvua ikaanza kunyesha mpaka kila sehemu ikajaa Maji ya Mvua hio.''

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Siku moja Khalifa Harun Rashid aliwambia Imam Mansur Ibn Ammar kua: **'Ewe Abu Sirr nakuuliza suali ambao sitaki uwe na haraka katika kulijibu, bali nakupa mda wa siku 3. Suali hio ni: 'Hivi Jee ni nani mwenye Ilm zaidi miongoni mwa Watu na ni nai Mjinga zaidi miongoni mwa Watu''**

Ambapo Imam Mansur akatoka akaenda kutembea kwa mda na kisha akarudi kwa Khalifa Harun Rashid na Kumwambia: **'Ewe *Amir ul Muuminin* nimepata jibu lako, ambalo ni Mtu mwenye Ilm zaidi miongoni mwa watu ni yule mwenye kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* mbali ya kua ni mwenye kumuabudu na kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na mwenye ujinga zaidi miongoni mwa watu ni yule ambae ni mwenye kujiamini sana mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* mbali ya kua ni mwenye kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Imam Mansur Ibn Amar alikua ni Mtu mwenye kuaminika na kukubalika sana na watu wa Iraq na Khurasan kwa ujumla, na alikua ni mtu alieachana na Dunia yake na hivyo ingawa alikua ni mtu wa kawaida asiekua na Mali wala Utajiri lakini alikua ni mwenye utajiri wa kutoka Moyoni mwake.

Imam Mansur Ibn Ammar anasema kua: '**Kuna mtu aliomba dua usiku mmoja katika mji wa Kufah kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema: 'Ya Rabbi, kutokana na Utukufu wako na Heshima yako, kwa hakika mimi hua si mwenye kukusudia kukuasi wewe wakati nnapofanya dhambi, ila ni kutokana na kughilibiwa na nafsi yangu na matamanio yangu, na kuficha kwako makosa yangu kunanidanganya, na kutokana na ujinga wangu basi ndio nimekua ni mwenye kukuasi na kupingana na matendo yangu.'**

'Hivyo jee ni nani atakaeniokoa mimi kutokana na Adhabu zako, kama sikua ni mwenye kupata Rehma zako katika siku ya Malipo? Pale itakaponadiwa kwa wale wasiokua na Dhambi kua wavuke na wenye dhambi wasivue? Jee nitakua na uso gani mimi mbele yako? Jee mimi nitakuka katika kundi gani kati ya makundi hayo mawili? Ole wangu mimi kwani kila ninavyoishi zaidi basi ndio zinavyozidi dhambi zangu zaidi, naomba Msamaha wako ewe Mola wangu!''

Imam Mansur Ibn Ammar aliusia kwa kusema kua: '**Mtu asieona kasoro zake hua kamwe si mwenye kuweza kushughulikia kasoro za wenzake.**

Hakuna kitu kitakachoweza kumstiri Duniani yeyote yule ambae ni mwenye kuivua nguo yake inayomhifadhi na vya haram na hivyo hua ni mwenye kutokua na Taqwa.

Yeyote yule mwenye kuridhika na alichojaaliwa na Mola wake basi kamwe hua hawezi kukisikitikia kile alichokikosa badala yake.

Yeyote yule anaeipenda Mitizamo yake peke yake basi hua ni mwenye kupotoka.

Yeyote yule mwenye Kibri mbele za watu basi matokeo yake hua ni mwenye kuadhirika.

Yeyote yule atakaekula kitu kisichokua chake basi hua ni mwenye kudumu na umasikini.

Yeyote yule mwenye kuomba msamaha kwa Mola wake hua ni mwenye kua na Subra.

Yeyote yule mwenye kutaka kupingana na Mola wake hua ni mwenye kuangamia. Yeyote yule mwenye kukiona kifo chake hua si mwenye malengo ya Kidunia.

Unyenyekevu hua ni kua na Subra katika wakati wa Mitihani kua na ukweli na haya katika Dini, kutotamani vya wengine na kutojipandisha Darja.

'Kama ukitaka kutokua ni mwenye kuomba samahani basi udhibiti Ulimi wako.'

'Kama Ibn Adam atakua ni mwenye kulalamikia Mitihani yake basi mitihani hio huahamia kwenye Imani yake.'

Imam Mansur Ibn Ammar alifariki mnamo mwaka 225 Al Hijra.

Ambapo anasema Imam Abu Hasan Sharani kua: **'Mimi nilimuona Mansur Ibn Ammar kwenye Ndoto nilipokua usingizini, na hivyo nikamuuliza : 'Ewe Mansur! Hivi Jee *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekupokeaje?' ambapo nae akasema kua: 'Nilipofika nikasikia sauti ikiuliza: 'Hivi Jee wwe ndie Mansur Ibn Ammar?' nami nikasema : 'Naam, *Ya Rabb.'***

Nikalizwa: 'Hivi jee wewe ndie uliekua mwenye kuwausia watu waachane na Dunia na kuwataka wawe wacha Mungu huku ukiwa na umaarufu Duniani?' nami nikasema: 'Naam, *Ya Rabb!* Lakini sikua nikisema hivyo isipokua kwa kuanza na kumalizia bila ya kua ni mwenye kuonesha shukurani juu ya Rehma na Neema zako, na kisha kumsalia Mtume wako *Salallahu Alayhi wa Salam*, na pia nilikua ni mwenye kuwausia watu kwa Ikhlasi.'

Baada ya hapo, *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kuwaambia Malaika wake kua: 'Hakika Mansur Ibn Ammar amesema Kweli, hivyo mtayarishieni Jukwaa

kwa ajili yake na kisha akae juu yake na kisha awe ni mwenye kuutangazia Ufalme wangu Miongoni mwa Malaika wangu kama vile alivyokua akifanya Duniani kwa Waja wangu.' ''

IMAM IBN KULLAB

Imam Abu Muhamamd Abd Allah Ibn Said Ibn Kullab Ibn Muhamamd Ibn Kullab Al Qatani Al Tamim Al Basr aliishi katika kipindi cha Imam Harith Al Muhasibi, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Sari As Saqati, Imam Is-haq Al Rahawayh na wengineo na alikua akiishi katika maeneo ya Baghdad na kisha baadae akahamia kwenye maeneo ya Khurasan.

Miongoni mwa Wanafunzi wa Imam Ibn Kullab ni Maimamu wa Ahl ul Sunnah wa Al Jamaah wakiwemo kina Imam Al Junayd, Imam Abd Al Aziz Al Makki Al Kattani, Imam Al Husayn Al Bajali n.k.

Imam Ibn Kullab alikua ni mtaalamu wa Ilm Hadith, Quran. Fiqh na ni Mtaalamu mkubwa wa Ilm al Kalam na hivyo kua ndio miongoni mwa waanzilishi wa misingi ya asili ya Mitizamo ya Aqida ya Asharia ya Imam Abu Hasan Al Ashari.

Ambapo anasema Imam Ibn Abd Al Barr kua: '**Imam Ibn Kullab alikua na ukaribu sana na Imam Ahmad Ibn Hanbal ambae alikua ni rafiki yake mkubwa, na pia yeye na Imam Al Karabisi, lakini pale Imam Ibn Kullab alipoanza kusoma *Ilm al Kalam* na kuanza kupingana na Imam Ahmad Ibn Hanbali basi Urafiki wao ukafutika na hivyo ikawa kuna Uadui baina yao badala yake, na hii ni kwa sababu Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua ni mwenye kusema kua: 'Yeyote yule anaesema kua Qur'an imeumbwa basi ni Jahmi, na yeyote yule anaesema kua Qur'an ni kauli ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* bila ya kusema kua imeumbwa ama la basi hua ni *Wafiqi.'*** *Wafiqi hua ni mtu mwenye kusita kwenye misimamo yake wa Aqidah.*

Na yeyote yule mwenye kusema: 'Matamshi ya Qur'an yameumbwa basi hua ni Mzushi.' Hivyo Imam Al Karabisi, Imam Al Kullab, Imam Abu Tahwr, Imam Daud Ibn Ali na wengineo walikua ni wenye kusema kua: 'Qur'an ni Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni sifa miongoni mwa sifa zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo haiwezekani kua ni kiumbe. Na kisomo cha msomaji na kusema kwake kwa kutumia Qur'an hua ni hali yake mwenyewe na vitendo vyake, yaani vimeumbwa na ni nukuu ya kauli ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*…hivyo Wafuasi wa Ahmad Ibn Hanbal wakaachana na Al Karabisi na kusema kua yeye ni Mzushi na hivyo kuawsema vibaya kila anaefuata mtizamo wake'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo anasema Ibn Qadi Shuhbah kua: '**Imam Ibn Qullab alikua ni Miongoni mwa Wanazuoni wakubwa wa Ilm Al Kallamu kutoka miongoni mwa *Ahl Sunnah wa Al Jamah*, kwani njia yake ndio iliyokua ikifuatwa na Harith Al Muhasibi na Imam Al Ashari pia**'

Miongoni mwa Vitabu vyake ni pamoja na *Kitab Al Sifat*, *Khalq Al Af Aal* ambavyo vimenukuliwa na Imam Abu Hasan Al Ashari katika vitabu vyake ikiwemo kitabu cha *Al Maqalat,* na pi amenukuliwa na Imam Ibn Furaq.

Ambapo anasema Imam Taj Adin Al Subki kuhusiana nae kua: '**Ibn Kullab ni miongoni mwa Wanazuoni wa *Ahl al Sunnah wa Al Jammah* na baba yake Imam Al Razi Diya Al Din Al Khattib amemtaja Ibn Kullab Mwishoni katika kitabu chake cha *Ghayat al-Maram fi 'Ilm al-Kalam* kua miongoni mwa Wanazuoni wa *Ahl Sunaa wa Al Jamaa* katika kipindi cha Al Ma'amun aliewaangamiza Mutazila mbele ya Khalifa Ma'mun.'**

Ambapo Al Allamah Ibn Khaldun anasema kua: **'Hali iliendelea hivyo hadi pale Shaykh Abu Hasan Al Ashari alipoingia kwenye mazingira hayo..na yeye alikua ni mwenye kufuata nyayo za Abd Allah Ibn Said Ibn Kullab, Abi Abbas Al Qalanisi na Al Harith Al Muhasibi kupitia kwenye njia za Salafi na njia za Sunnah.'**

Na *Allamah* Bayadi anasema kua: **'Na Imam Abu Muhammad Abd Allah Ibn Said Al Qattani Al Kullabi alimtangulia Imam Al Ashari ni Walinzi wa Madhhab ya Ahl Sunnah.'**

Imam Abu Mansur Abd Al Qadir Al Baghdadi anasema kua: '**Miongoni mwa Wanazuoni wa wakati wa Al Ma'amun ni Abd Allah Ibn Said Al Tamim aliwaangamiza mbele ya Al Ma'amun na kuwachafua sana kwa ufasihi wake na ukosoaji wa makosa yao**.'

Imam Al Bukhari amesema kua: '**Ama kuhusiana na makundi haya mawili basi wafuasi wa Ahmad wamedai kua wana uthibitisho kwa kila mmoja akiwa na mtizamo wake. Ambapo yote wanayoyanukuu hayana uthibitisho kua ni Sahih. Hivyo bila ya shaka hawakua na uhakika wa mitizamo yao. Ila kile kinachojulikana kutokana kwa watu wafuasi wa Ahmad na Wanazuoni ni kua Kauli ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* haijaumbwa na vyengine vyote isipokua yeye basi vimeumbwa. Lakini sasa wao wanachukia kuzama kwenye mada husika ambalo ndani yake kuna mambo yasiyokua wazi, na hivyo kuachana kuhojiana na Wanazuoni wa Kallam na badala yake hugombana nao isipokua katika yale mambo ambayo yamedhihirishwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kuwekwa wazi.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na akasema Imam Al Kawthari kua: '**Ama kuhusiana na Maneno ya Ahmad Ibn Hanbal dhidi ya Ibn Kullab na Al Muhasibi basi ni kutokana na chuki yake ya kutopenda kuzungumzia juu ya Ufafanuzi wa kina wa Tafsiri na kutochunguza kwake, kwani ukweli ni kua kuna wajibu wa kuzungumzia haya pale inapokua inahitajika kufanya hivyo, tofauti na anavyofiiria Ahmad Ibn Hanbal'**

Na akasema Imam Al Shahrastani Kua: '**Hadi katika wakati wa kipindi cha Abd Allah Ibn Said Al Kullabi, basi Abu Abbas Al Qalanisi na Al Harith Al Muhasibi waliuka ni miongoni mwa vizazi vya Salaf, lakini walikua wakitumia *Ilm al Kalam* (Ilm ya Kuhoji na kuchunguza kwa kuzamia kwa kina zaidi) na walikua wakitumia Imani ya Salafi kulingana na vithibitisho vya Tawhid na ufahamu. Ambapo baadhi yao waliandika vitabu na baadhi yao wakawa wanasomesha hadi pale yalipotokea mabishano baina ya Abu Hasan Al Ashari na Walimu wake wenye Imani ya *Mutazila* kuhusiana na jambo ambalo linajulikana kama *Al salah wa al aslah* (yaani kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawajibika ama la kufanya jambo au kitu bora kwa ajili ya mja wake) hivyo wakabishana na Imam Al Ashari akajiunga na kambi hii na hivyo akawa ni mwenye kuwaunga mkono kwa kutumia njia ya kuhoji kwa kuchunguza kwa kina na hivyo ile iliyokua asili ya Madhhab ya *Al Sunnah wa Al Jammah* na kisha ikatwa *Sifatiyyah* (wenye kuthibitisha Sifa za *Allah Subhanah wa Ta'ala)* ikawa Ashariyah'** *(Al-Milal wa al-Nihal)*

Imam Ibn Kullab alifariki mnamo mwaka 240 Al Hijra.

Ambapo kuhusiana na kutofahamiana kwa abadhi baina ya Wanazuoni basi ameusia *Shaykh Ul Islami* Imam Taj Ad Din Abd Al Wahab Ibn Ali Al Subki: '**Hivyo fahamu ewe mwenye kutafuta uongofu kua hutakiwi kua ni mwenye kutaka kuwakosoa Maiamamu waliotangulia, na hivyo usizichukulie kauli zao miongoni mwao dhidi ya wenzao hadi pale utakapokua na uthibitisho unaokubalika kiushahidi. Hivyo kama utakua na uwezo wa kuyatafsiri maneno yao au kua na mtizamo mzuri juu yao basi ni bora, na kama ni vyenginevyo basi yafumbie macho yaliyotokea baina yao kwani wewe hukuumbwa kwa ajili hio.**

Hivyo ni bora kwako kujishughulisha na yale yanayokuhusu na kuachana na yasiyokuhusu, kwani Mwanafunzi wa Ilm hua ni mwenye hikma na busara mbele yangu hadi pale anapokua ni mwenye kuingilia kuhusiana na yaliyotokea baina ya Wanazuoni waliotangulia na kisha kuanza kutoa hukumu baina yao kwa kupendelea upande mmoja.

Hivyo usijaribu kuingilia yaliyotokea baina ya Imam Abu Hanifa na Sufyan Ath Thawry, au Malik na Abu Dhib, au Hanbal Ibn Salih na An Nasai au Harith Al Muhasibi na Ahmad Ibn Hanbal. Kwani ukijishughulisha nayo hayo basi mimi

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

nnakukhofia kua wewe huenda ukawa ni mwenye kuelekea kwenye kujiangamiza Nafsi yako.

Kwani hawa unaowahukumu ni Wanazuoni Wakubwa sana na hivyo Kauli zao hua ni zenye kuweza kutafsirika zaidi ya mara moja, na hivyo huenda miongoni mwao wakawa hawakufahamika ipasavyo maneno yao kwa watu, na hivyo mimi na wewe hatutakiwi kusema chochote juu ya yaliyotokea baina yao bali tunatakiwa kua ni wenye kuwaridhia, na hivyo kua ni wenye kuyachukulia hayo yaliyotokea baina yao kama yale yaliyotokea baina ya Masahaba *Radhi Allahu Anhum* *(Qaid fi Jarh wa al Taadil)'*

IMAM AL MUHASIBI 165 AH

Mnamo mwaka 165 Al Hijra ambao ni sawa na mwaka 782 C.E katika Mji wa Basra nchini Iraq alizaliwa Mtoto wa Kiume ambae aliepewa jina la Abu Abd Allah Al Harith Ibn Asad Al Anazi Al Muhasibi, ambaponeno Anazi linamaanisha kua anatokana na Ukoo wa Kibedui wa Anaza.

Imam Al Muhasibi aliitwa Al Muhasibi kwa sababu kutokana na Ilm yale alikua ni mtu Mcha Mungu sana kiasi ya kua alikua kila wakati ni mwenye hali ya *Kathirati li Muhasibatihi li Nafsihi fi Jamii Al Ahwal* yaani ni Mwenye Kujihesabia Nafsi yake katika kila kitu afanyacho na katika kila hali ili asimuasi Mola wake..na ndio maana akaitwa Al Muhasibi

Kwani anasema Ibn Zadr Al Saqli kua: '**Wakati Harith Ibn Asad Al Muhasibi alipokua mdogo, alipota katika sehemu ambayo aliwakuta Watoto wakiwa wanacheza mbele ya Nyumba ambayo inauzwa Tende, hivyo akasimama na kuwaangalia watoto hao wenzake waliokua wakicheza'**

Wakati amesimama, basi Mwenye Duka la Tende hizo akatoka nje huku akiwa na Tende na kumpa Al Muhasibi kama sadaka ale, ambapo mtoto Al Muhasibi akamuuliza Muuzaji huyo kwa kusema:"Jee unajua hizi Tende zimetoka wapi?"

Muuzaji akasema: 'Usiwe na wasi wasi kwani mimi nauza Tende na alikuja mtu kwangu kununua wakati nampimia basi hizi zilianguka kutoka kwenye Mfuko wake.'

Mtoto Al Muhasibi akampuuza Muuzaji Tende na kisha akawauliza watoto wenzake wanaocheza mbele yake kwa kusema: Jee Mnamjua huyu Mzee?

Watoto wakajibu: ‘Naam Mtoto Al Muhasibi akauliza :Jee huyu ni Muislam?’ Na watoto wakajibu: ‘Naam..Muislam.’

‘Baada ya kujibiwa hivyo basi mtoto Al Muhasibi akaondoka, huku akimuacha Muuzaji Tende akiwa na Masuali chungunzima ya kujiuliza, na aliposhindwa kupata Jibu akaamua kumfuata Al Muhasibi.’

Hivyo akamkimbilia Al Muhasibi na alippmfikia basi akamkamata na kumwambia: ‘Hivi kwanini wewe ukauliza yale masuali? Kwani unafikiria kua mimi ni nani?’

Al Muhasibi akajibu: ‘**Ya Shaykh kama wewe ni Muislam wa Kweli basi mtafute uliemuuzia Tende zikaanguka na kisha umpe mwenye Tende zake ili ujiwachie huru kutokana mzigo wake kama vile ambavyo utakavyotafuta Maji kwa ajili ya Kujiokoa kutokana na Kiu kali sana.’**

‘Hivi inakuaje ewe Shaykh unawalisha Watoto wa Kiislam *Al Suht* (Kisicho halali) wakati wewe unasema kua ni Muislam?’

Wanazuoni wa historia wanatuelezea kisa chengine cha Imam Al Muhasibi pale alipokua katika wakati wa utoto wake, ambapo siku moja wakati yupo Madrasa alikuja Mwanamke ambae alikua hajui kusoma wala kuandika, ambapo Mwanamke huyo akamuomba Mtoto Al Muhasibi amuandikie Barua, na hivyo Al Muhasibi akamuandikia Barua yake hio Mwanamke huyo kama alivyotaka na kisha akampa.

Baada ya kupewa Barua hio basi Mwanamke huyo akachukua Dirham Moja na akampa Al Muhasibi ambae na akakataa kuipokea Dirham hio.

Hivyo yule Mwanamke akashukuru na kuondoka, baada ya Mwanamke huyo kuondoka basi Mwalimu wa Al Muhasib akamuuliza: **‘Mbona alipokulipa Malipo ya Kumuandikia Barua hukuchukua ile Dirham?’**

Al Muhasibi akasema: **‘Kwa Sababu amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an kua:**

﴿وَلاَ يَأْبَ كَاتِبٌ أَنْ يَكْتُبَ كَمَا عَلَّمَهُ ٱللَّهُ﴾

Wal<u>a</u> ya/ba k<u>a</u>tibun an yaktuba kam<u>a</u> AAallamahu All<u>a</u>hu *(Surat Al Baqara 2:282)*

Tafsir: **Na Wala Asikatae Muandishi kuandika kama Alivyofundishwa na Allah.**

'Hivyo mimi nimemuandikia Barua yake kutokana na Kutii amrisho la Allah Subhanah wa Ta'ala, hivyo Jee itakuaje mimi nichukue Malipo kutokana na Kutii Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*?.'

Mwalimu akatabasamu kisha akauliza: '**Sasa kwanini hukuchukua kisha ukanipa Mie badala yake Wakati wewe ulikua unajua kua huwezi kuichukua? Si ungechukua kisha ukanipa mie.'**

Kwani Al Muhasibi akasema: '**Hakika mimi nilizuiliwa kufanya hivyo na ile Kauli ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni yenye kusema:**

﴿وَلَيَحْمِلُنَّ أَثْقَالَهُمْ وَأَثْقَالاً مَّعَ أَثْقَالِهِمْ وَلَيُسْأَلُنَّ يَوْمَ ٱلْقِيَامَةِ عَمَّا كَانُواْ يَفْتَرُونَ﴾

Walayahmilunna athqalahum waathqalan maAAa athqalihim walayus-alunna yawma alqiyamati AAamma kanoo yaftaroona *(Surat Al Ankbut 29:13)*

Tafsir: ***Na Kwa Hakika Watabeba mizigo yao wao na mizigo zaidi ya mizigo yao na wataulizwa katika siku ya Kiama kuhusiana na kile walichokua wakikizusha.***

Kwani ingawa aya kadhaa zinasema kua:

﴿وَلاَ تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ﴾

Wala taziru waziratun wizra okhra *(Surat Al Isra 17:15)*

Tafsir: ***Na hakuna mbebaji atakaebeba mzigo wa mwenzake.***

La kini Aya hii aliyoitumia Imam Al Muhasibi inasema kua: '**Kuna Watu katika Siku ya Malipo watabeba Mizigo Mizito yao wao wenyewe na kisha pia watabeba Mizigo Mizito ya wengine na kisha wataulizwa kihusiana na Mizigo yote hio kwani tayari mizigo hio imeshakua yao kutokana na kuwapotosha watu wengine.'**

Hivyo kisa kinatuonesha alivyokua Imam Al Muhasibi Tangu utotoni kua ni mwenye Kujihesabia kuhusiana na Uhalali wa kila kitu chake yeye Binafsi na pia uhalali juu ya Waislam wenzake, ambapo anasema Imam Abu Nuaym Al Isfahani katika *Hilyat Awliya* kua: '**Amesema Jafar kua Amesema Abu Hasan kua alisema Al Junayd kua:**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Katika Siku aliyofariki Baba yake Al Muhasibi basi Al Muhasibi alikua na shida kubwa sana ya Fedha ya Daniq (ambayo ina thamani ya robo ya Dinari).’

Na baba yake Al Muhasibi alipofariki aliwacha Dinari 30,0000, lakini Al Muhasibi hakuchukua chochote kutoka kwenye Pesa hizo za Baba yake. Kwani Imam Al Muhasibi alipoulizwa Kwanini huchukui hizi Dinar alizowacha Baba yako wakati wewe una shida?’

Basi akasema: **‘La kwani Watu waliotofautiana katika Dini tofauti hua hawarithiani.’**

Hivyo mbali ya kua Imam Al Muhasibi alikua ni Mtu mcha Mungu lakini pia alikua ni Mtu mwenye Misimamo Mikali kuhusiana na Imani ya Dini yake, kwani Baba yake Imam Al Muhasibi alikua ni mtu ambae ni Muislam lakini alikua ni mwenye Mitizamo tofauti ya Aqida kwani alikuu ni *Wafiqi* na Misimamo ya Imam Al Muhasibi ambae yeye alikua ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, hivyo alizichukua pesa hizo alizowacha Baba yake a kuzikabidhi katika *Bayt ul Mal.*

Hivyo basi mbali ya kua Imam Al Muhasibi aliishi kimasikini lakini Baba yake alikua Tajiri, lakini kwa kua wana Mitizamo tofauti ya Aqida basi kwake yeye Imam Al Muhasibi ilikua tayari Baba yake si Baba yake na wala hawezi kubakia na Mama yake, hivyo ndoa ya Baba yake na Mama yake Ivunjike na yeye hawezi kumrithi Baba yake.

Kwani hii inakua kama vile ambavyo leo hii mtu ambae ni Muislam aseme kua yeye Si Muislam, basi Mtu kama Mtu huyo hakutubu basi Kisharia tayari hua Hamrithi Baba yake wala Mama yake wala ndugu zake ambao ni Waislam na wala yeye harithiwi na pia ndoa yake kama kaoana na Muislam basi nayo hua inabatilika. Allah atustiri na Mitihani hii.

Na ndio maana siku moja mda kabla ya Kufariki kwa baba yake basi Imam Al Muhasibi alikutana na Baba yake njiani, na hapo hapo akamkata shingo na kumwambia: Achana Kukaa na Mama yangu kwani Wewe una Dini yako na yeye Ana Dini yake, Dini zenu tofuati.

Tukio hili analiezea Imam Abu Nuaym Al Isfahani kwa kusema: ‘**Amesema Abu Abu Hasan Ibn muqsim, kua amesema Abu Ali Khayran Al Faqih kua, Mimi nilimuona Abu Abd Allah Al Harith Ibn Asad katika maeneo ya Bab At Taq, katikati ya Barabara akiwa amemkaba Baba yake huku watu wakiwa wamewazunguka nae alikua akisema: ‘Achana na Mama yangu kwani Wewe una Dini yako na yeye ana Dini yake.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Hivyo kwa yeye Imam Al Muhasibi ilikua Ndgu yake ni Muislam mwenzake na yule alietofautiana nae Kidini na Kiaqida basi hataki hata kujuana nae hata kama akiwa ni Mzazi wake au ni Ndugu yake.

Imam Al Muhasibi alikua ni mwenye kusoma kutoka kwa Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Abbad Ibn Awwam, Imam Marwan Ibn Shujaa, Imam Hushaym Ibn Bashir. Na ingawa Imam Al Muhasibi alikua ni mwenye kusoma kwa Wanazuoni wenye Ilm kubwa sana, lakini alimteua Mwanazuoni mmoja kua ndie Mwalimu wa kufuata Nyayo zake na huyu hakua Imam mwengine yeyite yule isipokua Imam Abu Abd Allah Muhammad Idris A Shafii.

Kwani anasema Imam Ibn Salah Al Shahrazuri kua: **'Abu Mansur Al Tamimi anamhesabu kua Al Muhasibi kua ni Miongoni mwa Sahiba zake Al Shafii, na alisema kua: 'Al Muhasibi Ni Imam wa Fiqh, Al Usul, Tasawwuf, Hadith na Ilm al Kallam, Vitabu vyake kwenye Fani hizi hua ni Msingi wa Kila Mwanafunzi anaetaka kujua kuhusiana na Fani hizi.'**

Na bila ya kuwepo Harith Ibn Asad Al Muhasibi miongoni mwa Marafiki wa Al Shafii katika Ilm ya Fiqh, Ilm Al Kallam, Usul, Al Qiyas, Al Zuhd, Al Warai na Al Maarifah, basi ingekua ni Vumbi tu kwenye nyuso za Wapinzani wake, na Shukrani zote anastahiki *Allah Subhanah wa Ta'ala.'*

Ambapo amesema pia *Shaykh Ul Islami* Imam Taj Ad Din Abd Al Wahab Ibn Ali Al Subki kua: **'Abu Asim Al Abbadi amesema kua Al Muhasibi alikua ni Miongoni mwa walioishi katika wakati wa Al Shafii na akachagua kufuata Madhhab ya Al Shafii'**

Ambapo alisema Imam Abd Allah Ibn Hafif kuwaambia Wanafunzi wake kua: **'Wafuateni watu watano Miongoni mwa Mashaykh wetu ambao ni Imam Al Muhasibi, Imam Al Junayd, Imam Muhammad Al Rawaym, Imam Abu Abbas Ibn Ataa na Imam Amr Ibn Uthman Al Makki, kwani hawa wamekusanya Ilm za Kiroho ndani ya Mwili na Kimwili kwa muonekano wa nje wa Miili.'**

Na Kutokana na Ucha Mungu wake basi ilikua kama Imam Al Muhasibi akikaribishwa chakula na kuwekewa Mbele yake, kama Chakula hicho si cha Halali basi mishipa ya Vidole vyake hua ni yenye kucheza, bila ya kutaka na hivyo kama atashindwa kuvizuia Vidole hivyo kutokana na Mtikisiko huo basi hua anajua kua Chakula hicho hakina Uhalali hivyo hatakiwi kula.

Kwani anasema Imam Al Junayd ambae ni Mwanafunzi wa Imam Al Muhasibi kua: **'Siku Moja mimi na Harith Al Muhasibi tulikua tumekaa na nikauona Uso wake**

umesawijika kutokana na kua na njaa, hivyo nikamwambia: 'Ewe Ami Yangu nifuate ukapate kile ambacho tunaweza kupata.'

Nae akasema: 'Bila ya Shaka kama ni hivyo basi utakua umenifurahisha mimi na pia kunipa heshima zaid.'

Hivyo tukaongozana hadi kwa Mjomba wangu, ilikua ni nyumba Kubwa isiyopungua Chakula cha ziada kwa kila siku, ambacho nyumbani kwetu sisi hua hakuna hivyo nikaingia nae ndani kisha nikamkaribisha. Nikamletea Sahani yenye vyakula tofauti na kumuwekea mbele yake, ambapo nae Imam Al Muhasibi akanyoosha Mkono kisha akachukua Punje Moja tu ya Chakula hicho, akaitia Mdomoni, nami nikamuona wakati alipokua akiitafuna lakini sikumuona kua akiimeza.

Kisha Imam Al Muhasibi akanyanyuka na kuondoka bila ya kuniambia kitu chochote, nami nikashangaa, hivyo siku ya pili nilipokutana nae nikamwambia: **'Samahani Sana kama jana nilivunja Moyo, kwani naona kwanza Ulinifurahisha halafu baadae ukaniacha na mawazo mengi sana.'**

Kwani Imam Al Muhasibi akamwambia Imam Al Junayd: '**Ewe Mtoto wangu, shukran sana kwa kujaribu kunifurahisha, nami nilijaribu kwa kila njia kula chakula ulichoniwekea mbele yangu lakini kulikua na Dalili baina yangu na *Allah Subhanah wa Ta'ala,* zenye kunionesha kua kama chakula sio halali kwangu basi na hakikubaliki kwake basi hua kuna harufu ambayo siwezi kuistahmilia, hivyo samahani lakini ilinibidi niitupe ile Punje nje ya Nyumba pale nilipotoka nje na kuondoka.'**

Ambapo kwa upande mwengine basi siku moja pia Imam Al Muhasibi alialikwa Nyumbani kwa rafiki yake na akapewa mkate ambao alifanikiwa kuula bila ya matatizo yeyote na hivyo akamwambia Rafiki yake huyo kua: **'Kama utataka kutoa Sadaqa chakula kwa Masikini basi mpe Mkate kama huu.'**

Na anasema tena Imam Al Junayd kua: '**Al Harith Al Muhasibi alikua anakuja Nyumbani kwetu na kisha huniambia: 'Twende tukatembee'**

Nami nikamwambia: **'Unataka kunitoa Nyumbani ambapo niko salama na kutaka kunipeleka Majiani kwenye Mitihani ya Njiani na ya Matamanio ya Nafsi?'**

Nae akasema: **'Wewe Twende usiwe na khofu yeyote'**

'Hivyo nikatoka nae na kuelekea Jangwani, ambapo kila tunapopita njiani basi ilikua kama hakuna watu na wala hakuna kitu ambacho ni chenye kuchukiza wala

kukirihisha. Kisha tukafika kwenye sehemu aliyoichagua na kisha tukakaa kitako chini na akaniambia: 'Niulize Suali unalotaaka kuniuliza.'

Nami nikasema: '**Sina Suali Lolote nae akasema: Niulize kile kilichomo ndani ya Nafsi yako. Ambapo baada ya kuniambia hivyo basi mara ghafla yakaibuka masuali mengi sana ya mambo ambayo nilikua siyajui, hivyo nikaanza kumuuliza ambapo na yeye Al Muhasibi akaanza kunijibu hapo kwa hapo kwa haraka sana, kisha nilipomaliza kumuuliza basi tukarudi Nyumbani nami nikaanza kuyaandika Masuali na Majibu hayo kwenye Kitabu.'**

Imam Harith Al Muhasibi kwa kusema kua: **'Ni hasara kwetu kama ikiwa tutapoteza vitu vitatu ambavyo ni Muonekano Mzuri wa Sura zetu unaojumuisha kua na heshima, Kauli nzuri zinazojumuisha na Uaminifu na Umoja wa Kindugu wenye Nguvu Unaojumuisha Kutosalitiana'**
Imam Al Muhasibi aliulizwa: **'Hivi Jee Kuachana na Dunia hua kuna Faida gani na kwa nini huifanya Dunia kuonekana kua haina Thamani?'**

Ambapo Imam Al Muhasibi akasema: **'Kuna Sababu Tano zinazoweza kutupa Majibu ya Suali hili ambazo ni:**

1-Kwanza Dunia Hua ni yenye kuwahangaisha sana Ibn Adam kwa matatizo yake na Mitihani yake na hivyo Dunia huufanya Moyo wa Ibn Adam kua ni mwenye kumsahau *Allah Subhanah wa Ta'ala na* humzuia Ibn Adam kutokana na Kuifikiria Akhera yake.

2-Mbili ni kua Darja ya wale ambao ni wenye kuipenda Dunia hua iko chini zaid ya Darja ya wale wasioijali Dunia.

3-Tatu ni kua, Kutoipenda Dunia humpelekea yule alieidharau Dunia kua ni mwenye Ukaribu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Hivyo hua ni mwenye kunyanyuliwa Darja za juu za Peponi.

4-Nne ni ni kua wale wenye Kuipenda Dunia basi ndio watakaokua ni wenye kuchukua Mda mrefu zaidi katika kuhesabiwa hesabu zao katika Siku ya Malipo.
5-Tano ni Kua Thamni ya Dunia hua ni sawa na Thamani ya Bawa la Nzi mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*'.

Imam Al Muhasibi akaulizwa : **'Jee Subra ni nini?'**

Ambapo nae akasema: **Subira hua ni kukikaribisha na kukipokea kila kitu kitokachotoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa njia na hali nzuri, na wala si**

kwa njia ya Kuingiwa na Jazba kubwa wala kua ni mwenye kuvunjika Moyo, yaani kua na Ustahmlivu katika wakati wa Mitihani.

Imam Al Muhasibi aliusia kwa kusema pia kua: **Yeyote tule anaetaka kua ni miongoni mwa watu wa Peponi basi na akae na watu wacha Mungu.**

Na Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ipasavyo basi huanzia pale Mtu anapojijua na kufaham kua yeye hana chochote mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kila wakati hua ni mwenye kuhitaji msaada kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Imam Al Muhasibi anaendelea kutuambia kua: '**Pale inapokua Ibn Adam hana Khofu juu ya Mola wake ndani ya Moyo wake na kusahau kua atahesabiwa na kuadhibiwa katika siku ya Malipo, basi Dhambi zake Ibn Adam huyo hua ni zenye kuzidi na huanza kuangamia kwani hua hayaoni Mema ya Kufanya, na pia hua hayaoni maovu ya kuyaepuka. Hivyo Ibn Adam huyo hua ni Mfungwa wa Matamanio ya Nafsi yake, na hivyo Nafsi na Roho yake hua ni yenye kushuka thamani yake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha Moyo wake huanza kujaa Kutu na Imani yake hua ni yenye kudhoofika.'**

Alisema Imam Harith Al Muhasibi kua: '**Hakika Sisi Ibn Adam Hua Tunaishi na Tunakufa katika Kila Siku na katika Kila Usiku, Na hivyo bila ya Shaka Itafika Siku ambayo tutakufa na hatutokua ni wenye Kuishi.**
Kwani kwa hakika katika Hili Sisi tuko kama Baharia Katika Meli ieleayo Baharini, tukidhani kua Tumesimama lakini kumbe Wakati Unatukimbia nakutuacha mbali nasi.'

Naam..kila mmoja wetu ni mwenye kuijua ile hadithi isemayo kua: '**'Hakika ya Amali ni kutegemeana na Nia' ambapo anasema *Shaykh ul Islami* Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua:** '**Amesema Imam Al Muhasibi kuhusiana na Hadithi hii kua: Pale Amali inapofanywa kwa Ajili ya manufaa ya Kiakhera na Kidunia, basi Amali hio hua haikubaliki.'**

Na hii ni kwa sababu amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: **'Hakika mimi ndie Mwenye kutosheleza kwa Wanaotegemewa, hivyo yeyote yule atakaefanya Jambo lake ambalo ndani yake amemshirikisha yeyote ndani yake zaidi yangu Mimi basi mimi sina haja nae Mtu huyo.**'

Kwani Imam Al Muhasibi amesem kua: '***Ikhlasi* ni kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala* bila ya kua na mwengine zaid yake kwani amesema pia Imam At Tirmidhii katika kuifafanua Hadith hii kua:** '**Mwanazuoni bora na mkubwa zaidi kuzungumzia**

kuusiana na yaliyoharamishwa na yaliyohalali basi ni Mwanazuoni wetu na Chifu wetu Al Harith Al Muhasibi.'

Naam..na kwani Imam Al Muhasibi anatuwekea wazi haya na hivyo kutubainishia Uovu wa wengie miongoni mwetu wasemao kua: **'Jicho Halina Pazia au wale wasemao kua Jicho halibandui kitu kinachotizamwa.'**

Kwani Imam Al Muhasibi anatubainishia kwa kusema kua: **'Hakuna Ikhlasi katika kitu Kilichokatazwa au kile ambacho kimebainishwa kua ni makruh, kama vile kwa mtu ambae hua ni mwenye kuangalia kile alichokatazwa kuangalia huku akiwa anadai kua eti anaangalia kwa ajili ya kutathmini apate kusifu uwezo wa uumbaji wa *Allah Subhanah wa Ta'ala***'

Kwani Imam Al Muhasibi anaendelea kusema kua: '**Kusadiki hua ni sifa ya Mja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na hivyo kua kunamaanisha kua Mja huyo aliesadiki hua na hali sawia pale anapokua hadharani na anapokua faragha yaani peke yake haonekani na anapokua mbele za watu akiwa anaonekana.**

Hivyo hali ya kusadiki ya Mtu huonekana katika hali zote na Nyakati zote, hivyo Ikhlasi hua inahitajika kwa nia ya kila kitendo na katika kusadikisha kikweli kila kitu chako'

Kwani Ikhlasi hua inahitaji katika Kusadikisha, wakati Kusadikisha hua hakuhitaji kitu, kwani ijapokua Ikhlasi ya kweli hua inahitajika katika kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala,* lakini hapo hapo Mtu hua anaweza kumtafuta *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusali lakini Moyo wake ukawa umeghafilika ndani ya Sala yake.

Hivyo Kusadiki hua ni Kumtafuta *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kumuabudu kikamilifu na kuuhudhurisha Moyo mbele yake, hivyo kila aliekua ni mwenye kusadiki hua ni mwenye Ikhlasi lakini si kila mwenye Ikhlasi hua ni mwenye kusadiki.

Na hio ndio Maana ya Kua ni mwenye kushikamana na kutoshikamana, kwani Aliesadiki hua hakujishikamanisha na chochote kile isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwa kujihudhurisha mbele yake *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na hivyo hua ni mwenye kuachana na kila kitu kilicho zaid yake *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hujipamba kwa hisia za kua yupo kwenye hadhara ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na tunapoyaangalia maneno haya ya Imam Al Muhasibi basi tunaona kua ametumia maneno Mawili makuu ambayo ni Kusadiki na *Ikhlas.*

Ambapo neno Kusadiki linatokana na neno Sadaqa ambalo kwa Kiswahili hua linamaanisha Kua Mkweli, Ukweli, Kua na Moyo Msafi juu ya Jambo au Kitu Fulani, Kutimiza ahadi, Kusimamia Amanah, Kuthibitisha na pia huamanisha Kusadidi.

Na Neno *Ikhlas* ambalo limetokana na neno Khalasa ambalo kwa Kiswahili hua linamaanisha Kua na Usafi, Kua na Upekee, Kua na Uhuru, Kua ni maalum kwa ajili ya jambo au kitu fulani husika pekee. Ambapo neno *Khalasa* ndio lililotoa neno *Mukhlas* ambalo hua linmaanisha wale ambao ni wenye Imani thbait au Imani ya Kweli kweli.

Ambapo tunapoyaangalia maneno haya basi tunaona kua upande mmoja yamekua ni yenye kufanana kimaana mbali ya kua pia ni maneno yenye maana tofauti na kulingana na hali ya matumizi na ingawa yana Utofauti wa kiutamkwaji.

Hivyo pale Imam Al Muhasibi aliposema kua: '**Hivyo kila aliekua ni mwenye Kusadiki hua ni mwenye Ikhlasi lakini si kila mwenye Ihklasi hua ni mwenye kusadiki'** basi alikua akimaanisha kua: **'kila mwenye usafi wa Moyo kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua pia ni mwenye kua na uwezo wa kufanya mambo yake kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee tu. Lakini si kila mwenye uwezo wa kua na uwezo w kufanya mambo yake kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni mwenye usafi wa Moyo katika kufanya Ibada husika kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu.'**

Na Ndio Maana Imam Al Muhasibi akatutolea Mfano wa Ibada ya Sala kwa kusema kua: '**Mtu anaweza kua ni Mwenye Kusali lakini Moyo wake ukawa umeghafilika kutokana na Sala'**

Ambapo huu ni mfano hai ni mzuri sana kwa sababu mara kadhaa Mtu anapokua anasali bila ya Khushuu basi hua ni mwenye kuingiwa na Mawazo mengine ndani ya Sala. Hivyo Mtu husika hua ni Mwenye Kufanya Ibada hio Maalum ambayo ni ya Kusali kwa ajili ya Kumuabudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu kwa saba u ndio Mola wake. Hivyo Mtu huyu hua ni mwenye kua na Ikhlasi lakini kutokana na kukosa kua na Sadiki yaani Usafi wa Moyo wake katika Ibada ya Sala yenyewe basi hua ni mwenye kukosa Khushuu na hivyo hua si mwenye kuuhudhurisha Kikamilifu Moyo wake kwenye Sala na hua ni mwenye kughafilika ndani ya Sala yake.

Hivyo Ikhlasi hua inahitajika katika Kusadikisha Kitendo cha Ibada husika na hio ndio maana ya Hadith isemayo *Innama al aAmali bi niyat* - Hakika ya Amali hua inategemeana na Nia, kulingana na ufafanuzi wa Imam Al Muhasibi.

Imam Al Harith Al Muhasibi anausia kwa kusema kua: '**Muislam anaweza akatumai Kumtumikia *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kikamilifu katika Maisha yake yote lakini**

kama hatokua na Kutu ya Kuendekeza Matamanio ya Nafsi yake katika Amali zake na Mtizamo wa Mawazo yake.’

Kisha akaendelea kutuambia kua : ‘**Waislam tunatakiwa kujikumbusha kua kwa Kiislam basi Manufaa ya Kitu na Gharama ya kitu hua hayahesabiwi ndani ya Mipaka ya Kidunia na Mapambo ya Kidunia tu bali hua yanahesabiwa kulingana na Manufaa na Gharama ya Kiakhera zaidi, kwani kama Manufaa ya Kiakhera yatadharauliwa basi Uzito wa Manufaa utakua Mdogo sana na Gharama yake itakua Kubwa na hivyo kumtia hasara kubwa Muislam husika.’**

Na hapa ndio tunapokosea wengi miongoni mwa Waislam wa leo, kwani hua tunatafuta Manufaa ya Duniani zaid tena kwa Gharama yeyote, na hivyo kudharau juu ya Mafanikio ya Akhera. Kwani leo Watu wanajali kusomesha zaidi watoto wao kwa kuwalipia na kuwekeza zaid katika Elimu ya Kisekula bila ya Kujali kuhusiana na Elimu ya Dini yao.

Huu ni Mtihani Mkubwa sana hivyo kila Mmoja wetu atajitayarishe na la Kujibu kuhusiana na hili mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika siku ya Malipo, kwani mbali ya kua Mtu husika atakua amekula hasara yeye mwenyewe kuhusiana na Akhera yake lakini pia atakua ameilisha Hasara Familia yake pia tena kwa Gharama kubwa ambayo ni Moto.

Kwani ingawa Imam Al Muhasibi aliishi miaka 1200 iliyopita lakini anatuwekea wazi hali tuliyokua nayo sisi leo hii kua inatokana na kutokinai kwa kile tulichojaaliwa Kidunia na hivyo kutuambia kua: ‘**Fahamuni kua kamwe haikubaliki kua kutafuta Mali kua ndio Lengo kuu la Mtu, kwani Kiislam hua inakirihisha Kukusanya Mali, kwani Muislam anatakiwa awe ni mwenye Kukinai na alichojaaliwa, kwani Hata kama Muislam akiwa na Kisingizio cha kua Kukusanya kwake huko Mali hua ni kwa ajili ya Kufanya Mema, lakini hata hivyo hua inakirihisha na hii ni kwa sababu Mali hio huweza Kumletea Mtihani Mhusika kiasi ya kua Moyo wake ukawa ni wenye Kumsahau Mola wake Kidhikr, Kiibada na kimaamrisho, na hivyo kumpelekea Mhusika kua ni mwenye kufanya Dhambi ikiwemo Kujiona na kua na Kibri inayoota ndani ya Moyo kutokana na kua na Mali.’**

Hivyo Basi Waislam tunatakiwa kua ni wenye Kukinai na kutokua na Pupa katika Kutumia Gharama kubwa zaid kwa ajili ya Manufaa ya Kidunia kuliko kwa ajili ya Manufaa ya kiakhera kwani kutokinai kwetu kunatupelekea kutokua si wenye kuamini hali ya *Tawwakul*, yaani ya kumtegemea *Allah Subhana wa Ta'ala* pekee katika Riziki zetu mbali ya kua ni wenye kujua kua yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye Kuwaruzuku Viumbe wake wote.

Imam Al Harith Al Muhasibi anausia kwa kusema kua: **Amesema Abd Allah Ibn *Masud Radhi Allahu Anhu* kua: Kua ni mwenye Kuridhika na hali ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekujaalia kua nayo na hivyo utakua ni Tajiri zaidi ya Matajiri wote.'**

'Kaa mbali na vitu alivyoviharamisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na usivifanye na hivyo utakua Mtu mwenye Kuepuka Dhambi kuliko wote'

'Tekeleza Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* nawe utapendwa zaid na watu Wakilisha hali yako kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na usisite muombe msaada wake peke yake na wala usilalamike kwa Mtu yeyote.'

Kwani Imam Al Muhasibi kwa kusema kua: **Tahadhari na kua na Tabia za Kijahiliya, zionekanazo kwa Wafanyao Dhambi kwa kijiona Nafsi zao, kua na Kiburi, na kutokua na Matumaini ya Kusamehewa Na *Allah Subhanah wa Ta'ala,* fanya Mema, kisha Muamini kwa kumkabidhi *Allah Subhanah wa Ta'ala* kila Jambo lako.**
Kwani faham kua kuna aina tatu za Mapenzi ni Muhimu zaidi:

1-Kwanza ni kumpenda *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwa kupenda Kufanya Ibada zaid na kuachana na kufanya Dhambi.

2-Kumpenda *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa Imani iliyokua Thabiti na kushikamana na Sunnah zake.

3-Kumpenda Muumini mwenzako kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kumnufaisha na kutomsababishia Madhara.

Na akasema tena: **Ewe Ibn Adam fahamu kua: Kila kutu chako kina Fardhi yake, Ambapo Fardhi ya Ulimi na Lugha yako ni Kua na Utulivu katika wakati wa Hasira na Furaha, na wala usitumike kwa kuwadhuru Watu iwe kwa siri au kwa dhahiri, Fardhi ya Jicho ni Kujilinda kutokana na kutoangalia ya Haram, Fardhi ya Sikio ni Kutosikiliza mambo yasiyokua ya Halali, ambapo baada ya Ulimi basi kitu kinachofuatia kwa uhatari ni Masikio, Kwani Masikio ndio Balozi Mkuu wa Moyo, na ni kutokana na Sikio ndio watu hua wanatumbukia kwenye Dimbwi la Mitihani mikubwa sana, Fardhi ya Pua ni Kutonusa Harufu ya kitu kisichoruhusiwa, Fardhi ya Mikono na Miguu ni kutokaribia kitu kilichoharamishwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kukimbia visivyokua vyako na haki za wenzako'**

Kisha Imam Al Muhasibi anamalizia kwa kusema kua: '**Ewe Muislam Fahamu kua Dhambi hukuletea Mghafiliko, Mghafiliko hukusababishia Ugumu wa Moyo,**

ambapo ugumu wa Moyo humuondoa Mtu na kumuweka mbali na *Allah Subhanah wa Ta'ala*, Na kua na mbali na *Allah Subhanah wa Ta'ala* humpelekea Mtu kua ni mwenye kumbukia kwenye Moto wa Jahannam.'

Imam Al Muhasibi anatuusia kwa kusema kua: '**Enyi Ndugu zangu, Wanazuoni wa kidunia ni Watu wa Hatari sana kwa Waislam, kwani ni wenye kuipenda sana Dunia, na hivyo hua ni wenye kuipendelea Dunia zaid ya Akhera. Ambapo wale wanaoipenda Dunia zaid kuliko Akhera hua hawana uhuru na wala hawana wepesi katika maisha yao, Kwani raha na furaha yao hua imejawa na Huzuni na Mashakil, kwa sababu mwisho wao ni Maangamizo, kwani Dunia na Akhera ya watu hawa hua ni Maangamizo.**

Hivyo ewe ndugu yangu, Zindukana, Mche Mola wako *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na wala usimruhusu Shaytan akakulaghai, kwani bila ya shaka Shaytan na Wasaidizi wake Watakua ni wenye kuadhirika na kushindwa katika Siku ya Malipo Mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'

Imam Al Muhasibi anaendelea kutuambia kua : '**Kwa Ibn Adam hakuna kitu Kizuri kwa Mja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama Kukumbuka, Kutafakkar na Kuzingatia. Kwani mwenye kufanya hivyo basi hua ni wenye Kujiongezea Ilm katika Ufaham wao na hivyo hua ni wenye kujipandisha Darja mbele ya Mola wao. Kwani yule anaejipunguzia kutafakkari basi hua si mwenye kuzingatia ipasavyo, na asiezingatia basi hua ni mwenye kupungukiwa na Ilm, na anaepungukiwa na Ilm hua ni mwenye kujizidishia Ujinga badala yake.'**

Kwani yule anae Tafakkar na Kuzingatia hua ni mwenye kua na uwezo wa kutofautisha baina ya kipi ni chenye manufaa nae na kipi hua hakina manufaa nae, Na hivyo hujua ni kipi chenye madhara nae, na mtu huyu hua ndie mwenye uwezo wa kuyadhibiti maumbile ya Nafsi yake yenye kuvutia kwenye madhara ya kutaka kumpotosha kwa Matamanio yake.

Na hivyo hua ni mwenye kujua matokeo ya vitendo vyake baada yake, na hivyo hua ni mwenye Kumuogopa Mola wake, na hua ni mwenye kupendelea Raha na Starehe ya Ufahamu wake kuliko raha na Starehe ya Matamanio yake kwani Ladha ya Raha na Starehe ya Mwanazuoni mwenye Ilm hua ni yenye kuhisika kupitia kwenye Hisia za Ufahamu wake, Wakati ladha ya Raha na Starehe ya Mtu mjinga asiekua na Ilm hua ni yenye kuhisika kwenye Hisia za Matamanio ya nafsi yake.

Na hakuna Raha na Furaha nzuri zaid kuliko Raha ya Kua na Ilm kunakohisikana na Ufahamu wa Mtu mwenye Ilm kwani kupitia kwake Ilm hukuonjesha Raha ya kumjua zaid Muumba na hivyo Mja hua ni mwenye kujitafutia Ukaribu nae na

kujapandisha Darja kwa ajili ya Mafanikio ya kweli na ya kudumu ya Ulimwengu wa Milele mbele yake *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

***Allah Subhaanah wa Ta'ala* ambae ni mwenye kupatikana kwa kila mwenye kumtafuta. Mwenye kumsadia na kumtosheleza kila anaemuomba, kila anaemuogopa basi huipata hifadhi yake, kwa kila anaemkimbilia basi yeye humkimbilia kwa kasi zaid.**

Kwani *Allahu Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kumuita kila anaempa Mgongo, na Humkubalia na kumpokea Kila anaerudia kwake, Hukusifu na kukulipa kutokana na kile chake mwenyewe alichokupa wewe *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kukutia Moyo umkumbuke yeye kwa ajili yako, yeye ndie anaekupa Maradhi ili akuponeshe - Yalaiti kama ungekua Unajua.

***Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie anaekupa Umasikini ili baadae akutajirishe, Anaekuzuilia kile cha mpito ili baadae akuneemeshe kwa kile chenye kudumu, ndie anaekufisha ili baadae Akufufue.**
Imam Al Harith Al Muhasibi anaendelea kwa kusema kua: ‘***Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie yeye ambae anaekurushia Matatizo ili Moyo wako Ulainike juu yake kwa Manufaa yako. Ndie anaekupa Riziki hata bila ya kumuomba na kutosita kukupa hata kama hukumuonesha Shukrani, na hukuneemesha hata kama wewe ukimdhrau. Hivyo jee ewe Ndugu yangu, utakua na uwezo gani wa kuona na kujua kasoro na makosa yako, na utawezaje kuona Ukarimu na Ihsani yake juu yako, Bila ya kua ni mwenye kukumbuka, kutafakkar na kuzingatia?**’

Hivyo kumbuka, tafakkari na zingatia ili uweze kupigana vita na Nafsi yako na kuweza kujua kipi ni chenye kumridhisha Mola wako ukifanye na kipi ni chenye kumkasirisha uachane nacho.

Imam Al Harith Al Muhasibi anatubainishia kuhusiana na nini cha kufanya kwa kusema:

Watu wenye kujihesabia Nafsi zao hua ni wenye Sifa Maalum, ambazo wanapozifanyia kazi sifa hizo basi hua na Darja ya Juu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani kwa Ibn Adam basi bila ya shaka malengo ya kila kitu huweza kufikiwa kutokana na kua na Msimamo Thabiti wa Maamuzi ya kuamua kuachana moja kwa Moja na Matamanio ya Nafsi.

Kwani hua ni rahisi sana kwa Mtu mwenye Msimamo Thabiti katika Maamuzi yake kupingana dhidi ya Matamanio ya Nafsi yake.

Kwani ndani ya Maamuzi hayo Thabiti basi mtu anatakiwa awe na Msimamo wa Kujidhibiti katika mambo yafuatayo:

Kutokula Kiapo, Iwe cha kweli au cha Uongo.

Kujitenga na Kusema Uongo.

Kutomlaani Mtu yeyoye hata kama itakua Mtu huyo amekudhulumu.

Kutovunja Ahadi zako, pale unapokua unao uwezo wa kutekeleza ahadi hizo.

Usimdhuru Mtu iwe kwa Maneno au kwa vitendo.

Usitegemee Malipo kutokana na Mema uyafanyao, kwani ni wajibu wako.

Kua na Subra kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Usitoe Ushahidi dhidi ya yeyote, iwe Kafiri, Mshirikina au Mnafiq.

Kua ni Mwenye Huruma kwa kila mtu kwa ujumla - Kwani hili ni jambo bora zaid katika kujiokoa na Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*
Usifanye Dhambi unapokua Hadharani wala unapokua Faragha.

Vitenge Viungo vyako Vyote dhidi ya Dhambi.

Usimbebeshe Mtu yeyoye Mzigo wa Dhambi, iwe mkubwa au mdogo iwe kwa kukusudia au kwa kutokusudia.

Usitegemee chochote kutoka kwa mtu yeyote na wala usione wivu wala usitamani chochote alichokua nacho Mtu yeyote.

Naam..kwani Darja na Ukubwa wa Heshima ndani ya Dunia hii na Kesho Akhera hua haitegemeani na mtu yeyoye isipokua hua inategemeana na Majaaliwa na Makadirio ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kutoa kwake, na hivyo basi usijione kua labda uko juu mtu yeyote yule unaekutana nae.

Imam Al Harith Al Muhasibi alifariki 243 Al Hijra na alizikwa kwenye Mji wa Basra baada ya kuishi kwa umri wa miaka 73.

Na tumalizie na baadhi ya Wasia wake zaid ambapo anasema kwa kutuambia ndani yake kua: **'Kamwe usiwache chochote kile katika mema yanayotakiwa kufanywa kwa ajili ya Mola wako, na wala usiridhike na kuvutiwa na kile kilichofanywa nawe**

kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Unaposimama na Kusali mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi simama kikamilifu hukunukiwakilisha kila kiungo cha Mwili wako ndani ya Sala yako.

Mtu yeyote yule anaeachana na Dunia yake, hua ni mwenye kuachana nayo kulingana na Ilm yake, na Ilm yake hio hua ni yenye kulingana na Ufaham wake, ambapo ufahamu wake nao hua ni wenye kutegemeana na Wingi na Ukubwa wa Imani yake.

Na akasema tena Imam Al Muhasibi kua: **Kua na Tabia Nzuri hujumuisha Kua na Subra na Ustahmilivu, Kutokua na Hasira, Kua na Uso wenye kutabasamu kwa kila Mtu na kua na Kauli nzuri.**

Kwani yeyote yule anaejirekebisha Kitabia Ndani ya Nafsi yake kwa kua ni mwenye kujua Uangalifu wa kila wakati wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake, basi hua ni mwenye kupambwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa matendo mema na Kushikamana na Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*
Na aliusia pia Imam Al Muhasibi kua: **Ewe Ndugu yangu, kamwe usichukulie Dhambi yeyote kua ni Ndogo, na wala usiifanye kwa Siri, na wala Usifichue kile ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameamua kifichike.**

Jitahidi kutofikiria kuhusiana na kufanya Dhambi na wala usidumu katika kufanya Dhambi.

Mwenye Hikma hua ni yule Mtu ambae hairuhusu Akhera yake kua ni yenye kuchanganyika na Dunia yake, na wala haruhusu Akhera yake kua ni yenye kuchanganyika na Dunia yake Kwani Mtihani mkubwa kwa Ibn Adam ni Mghafiliko wa Moyo wake dhidi ya Akhera yake.

Kwani Ingawa ni Marafiki lakini Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua akitofautiana na Imam Al Muhasibi kuhusiana na Ilm Al Kalam na Tassawuf, hivyo siku moja akaambiwa na Wanafunzi wa Al Muhasibi kama anataka kumsikiliza Imam Al Muhasibi na kuthibitisha kama yuko sahih kimtizamo ama la?

Ambapo Imam Ahmad Ibn Hanbal akakubaliana na Rai hio, na hivyo akaalikwa kwenye Nyumba ambayo Imam Al Muhasibi hua anakutana na Wanafunzi wake, na kisha alipofika akawekwa katika Chumba cha pekee ili asionekana na Al Muhasibi lakini akiwa na uwezo wa kukisia kila kinachoendelea ndani yake. Hivyo Siku ya pili Imam Ahmad Ibn Hanbal akaeleze kile alichokiona kwa kusema kua:

Nilikaa na Wakati ilipoadhiniwa Adhana ya Isha Al Muhasibi akakimu Sala na kisha akasalisha, na baada ya Kusali kikaletwa Chakula, Al Muhasibi akakaa na

Wanafunzi wake kisha wakala, huku wakizungumza ambapo Inaruhusika kula huku ukiwa unazungumzia mambo mema, baada ya kula na kunawa na kila mmoja kutulia katika sehemu yake basi Al Muhasibi akawaluiza Wanafunzi wake kama kuna aliekua na Masuali ya kuuliza kuhusiana na Ikhalsi, Riya, na mengineyo basi na aulize

Wanafunzi waksuliza Masuali nae akawa anajibu kwa kutoa vithibitisho na alipomaliza ilikua ishakua usiku mkubwa tayari, Al Muhasibi akamuomba mmoja kati ya Mwanafunzi wake asome Qur'an, ambapo ndani yake kisomo hicho Al Muhasibi na Wanafunzi wake wakawa wanalia kutokana na kisomo hicho

Kisha baada ya kisomo Al Muhasibi akaomba Dua ndogo na kisha wakasali na Kulala, hadi Alfajir wakaamka. Hivyo hakika mimi sikuona kitu ambacho sicho kilichokua kikifanywa na Al Muhasibi na Wanafunzi wake.’

IMAM AL HARMALA AL SHAFII 166 AH

Imam Abu Abd Allah Harmala Ibn Yahya Ibn Abd Allah Ibn Harmala Ibn Imran Ibn Qaradh Abu Hafs Al Tajibi Mawla Abu Zumala Al Masri alizaliwa mnamo mwaka 166 Al Hijra nchini Misri.

Imam Al Harmala Ibn Yahya alikua ni mwenye Ilm ubwa sana ya Qur’an, Hadith na Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii, kwani alikua pia ni miongoni mwa Wanafunzi wakubwa wa Imam Muhamamd Idris Al Shafii walioshikamana nae kwa ajili ya kusoma kwake nchini Misri.

Imam Al Harmala alikua ni mwenye kuhifadhi hadith nyingi sana ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake wakubwani pamoja na Imam Muslim Ibn Hajjaj alieandika Sahih Muslim, ambapo ndani yake amemnukuu mara nyingi sana Imam Al Harmala.

Ambao anasema Imam Ahmad Ibn Salih Al Misri kua: **‘Imam Ibn Wahb alikusanya Hadith hadith 120,000 ambapo baadhi ya watu wanasema kua nusu yake ni kutoka kwake na nusu yake ni kutoka kwa Harmala.’**

Imam Al Harmala alikua ni Nguzo kati ya nguzo za Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kwa upande wa Al Qawl Al Jadid ya Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii, ingawa katika baadhi ya fatwa alikua ni mwenye kua na mitizamo yake kulingana na Ijtihadi yake mwenyewe kutokana na kua na uwezo mkubwa sana wa Ilm.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ingawa Imam Al Harmala alikua na uwezo mkubwa sana wa Ilm lakini hata hivyo hakuwa ni mwenye kumfikia Imam Al Muzani au Imam Al Rabii kwa Ilm kama anavyobainisha Imam Taj Ad Din Al Subki pale aliposema kua: '**Imam Al Harmala mbali ya kua juu na maarufu sana kwa Ilm ya Hadith na Fiqh, lkini hata hivyo hakuweza kuifikia Darja ya Al Muzani na Al Rabii Al Muradi katika Nukuu kutoka kwa Imam Al Shafii.'**

Ambapo Imam An Nawawi anasema kua: '**Sisi tumemnukuu Abu Sulayman Al Khattabi katika sehemu za mwanzoni mwakitabu chake cha Maalim Al Sunan, ambamo amesema kua Wanafunzi waliotangulia wa Imam Al Shafii walikua wanategemea sana I'lm yao kutoka kwa Al Muzan na Al Rabi Al Muradi kutokea kwa Al Shafii na walikua ahawamtegemea sana Al Harmala na Al Rabi Al Jauzy Allah awaingize wote kwenye Rehma zake.'**

Ambapo kwa upande mwengine basi mbali ya kua Imam Al Harmala hakua ni mwenye kutegemewa sana kwenye Fiqh lakini pia amenukuliwa mara kadhaa kwenye vitabu vikubwa vya Fiqh vya Madhhab ya Imam Al Shafii kama *Al Muhadhdhab, Al Wasit, Sharh Al Kabir na Al Rawdah.*

Imam Al Harmala alikua pia ni muandishi wa Vitabu na miogoni mwa Vitabu alivyoandika ni *Mukhtasar Al Harmalah* ambacho ndani yake kuna Mitizamo ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii, ikiwemo ya Imam Al Shafii Mwenyewe na mitizamo yake Imam Al Harmala.

Amesema Harun Ibn Said kua: 'Mimi nimemsikia Ashhab akisema huku akimuangalia Harmala kua: **'Huyu ndio Mtu bora zaidi miongoni mwa Watu wa Msikitini hapa''**

Anasema Imam Al Harmala kua: **'Nimemsikia Al Shafii akisema kua: 'Sijawahi mimi kuapa kwa jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* iwe kwa ukweli au kwa uongo'**

Imam Al Harmala anasema kua: **'Amesema Al Shafii kua: *'Al-bid`atu bid`atan: bid`a mahmuda wa bid`a madhmuma, fa ma wafaqa al-sunna fa huwa mahmud, wa ma khalafa al-sunna fa huwa madhmum.' Bidaa* kuna *Bidaa* za aina mbili, kuna Bidaa inayokubalika kwa uzuri wake na *Bidaa* inayokataliwa kutokana na ubaya wake, kila kile kinachoshikamana na *Sunnah* hua ni *Bidaa* inayokubalika, na kila kinachopingana na *Sunnah* hua ni *Bidaa* isiyokubalika.' Na ametumia Mfano wa Bidaa ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allau Anhu* alipoanzisha Sala ya Taraweh kusaliwa kwa Jamaa na kusema : 'Hii ni Bidaa nzuri sana'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Miongoni mwa Hadith zilizomo kwenye Sahih Muslim kutoka kwa Imam Al Harmala ni ile isemayo: **'Amesema Abu Tahir, kua amesema Harmala Ibn Yahya kua amesema Wahab kua amesema Yunus kua amesema Ibn Shihab kua amesema Hasan kua amesema Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Ali kua amesema Baba yao kua amemsikia Ali *Radhi Allahu Anhu* akimwambia Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza Ndoa za Mda mfupi na kula nyama ya Punda katika siku ya Khaibar''***(Imam Muslim)*

Imam Al Harmala anasema kua: **'Nimemsikia Al Shafii akisema kua: 'Hakuna jambo bora kuliko kutafuta Ilm baada ya majukumu ya Fardhi''**

Imam Al Harmala amesema kua: **'Amesema Al Shafii kua: 'Yeyote yule atakaesema kua anawaona viumbe Majini basi , sisi ha ni wenye kuukataa ushhdi wake ka sababu amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

﴿يَابَنِيٓ آدَمَ لاَ يَفْتِنَنَّكُمُ ٱلشَّيْطَانُ كَمَآ أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ مِّنَ ٱلْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْءَاتِهِمَآ إِنَّهُ يَرَاكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لاَ تَرَوْنَهُمْ إِنَّا جَعَلْنَا ٱلشَّيَاطِينَ أَوْلِيَآءَ لِلَّذِينَ لاَ يُؤْمِنُونَ﴾

Ya banee adama la yaftinannakumu alshshaytanu kama akhraja abawaykum mina aljannati yanziAAu AAanhuma libasahuma liyuriyahuma saw-atihima innahu yarakum huwa waqabeeluhu min haythu la tarawnahum inna jaAAalna alshshayateena awliyaa lilladheena la yu/minoona*(Surat Al Araf 7:27)''*

Tafsir: ***Enyi Ibn Adam, Msimwachie Shaytan akakudanganyeni kama vile ambavcyo alivyofitinisha Wazee wenu (Adam Na Hawa) akawatoa nje ya Pepo na kuwavua nguo zao kuwaonesha sehemu zao za siri. Kwani kwa hakika yeye na Kabila lake wanakuoneni kutoka katika sehemu ambayo wao hawakuoneni, kwani hakika tumewafanya Shaytani kua ni wasaidizi wa wale wasioamini.***

Imam Al Shafii akamalizia kwa kusema isipokua labda kama Mtu huyo atakua ni Mtume wa Allah.'

Imam Al Harmala amesema kua: **'Mimi nimemsikia Sufyan Ibn Uyaynah amesema kuhusiana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: 'Si Miongoni mwetu yule ambae si mwenye kuisoma Quran kwa sauti nzuri'' kua: 'Mwenye kutosheka nayo katika kuisoma kwake' ambapo Al Shafii amesema**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kua: ‘La, sio kama hivyo kwani kama ingekua kama hivyo basi angesema kua yule mwenye kuiimba kama nyimbo, hivyo hapa imekusudiwa ni yule ambae ni mwenye kuisoma huku akiwa katika hali ya kuhuzunika sana.’

Imam Abbas Al Duri anasema kua: **‘Amesema Yahya kua: ‘Kuna Shaykh nchini Misri anaitwa Harmala ambae ni mwenye Ilm kubwa sana ya Watu wa Ibn Wahb’’** Ibn Uday nae akasema kua: ‘**Nilimuuliza mimi Abd Allah Ibn Muhamamd Al Farhadani kua anielezea kuhusiana na Harmala ambapo nae akaniambia kua:’ ‘Harmala ni Dhaifu na kisha akaninukulia Hadith 3 juu yake’’**

Kisha Ibn Uday akasema kua: **‘Mimi nilizifuatilia Hadith zote za Harmala na sikukuta hadithi hata moja ambayo inaweekana ikawa ni dhaifu kutokana nae’**

Ambapo kwa upande wa Abu Umar Al Kindi basi yeye anasema kua: **‘Harmala alikua ni Mwanafiqh, na ilikua hakuna katika Mji wa Misri mwenye kuweza kuandika juu ya Ibn Wahb kutoka kwake kwa sababu Ibn Wahb alikaa ndani ya Nyumba yao kwa mwaka mzima na miezi kadhaa akijificha kutoka kwa Askari pale alipotakiwa awe Qadhi wa Misri.’**

Miongoni mwa Mitizamo ya Imam Al Harmala alifariki mnamo mwaka 243 Al Hijra.

IMAM IBN SAD 168 AH

Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Sad Ibn Mani Al Basri Al Hashimi Al Baghdadi alizaliwa mnamo mwaka 168 Al Hijra katika Mji wa Basra lakini baadae akahamia katika Mji wa Baghdad na alikua ni Mwanafunzi na mwandishi wa Imam Al Waqidhi na hivyo Imam Ibn Sad ni mmoja kati ya Maimamu wanaoheshimika sana kwa upande wa Ilm ya Maghazi na Historia ya Uislam katika karne za Mwanzoni mwa Uislam kwa Ujumla kwani ni mwenye kuenda sambamba ki Ilm na Wanazuoni maarufu na wakubwa sana wa Ilm hio kama kina Imam Muhamamd Ibn Is-haq, Imam Al Waqidhi na Imam Musa Ibn Uqba.

Imam Ibn Sad kama anavyojulikana kwa umaarufu wake alisoma pia kwa Maimamu wengi sana wa Hadith akiwemo Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Abu Al Walid Al Tayalisi, Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Sulayman Ibn Harb, Imam Al Walid Ibn Muslim n.k na hii ni kutokana na kutembea kwake katika kutafuta Ilm katika Miji ya Baghdad, Kufah, Makkah, Madina n.k na hivyo kumfanya kua na Ilm kubwa ya Hadith na Tafsir pia, na hivyo haishangazi kuona namna anavyokubalika na wengi miongoni mwa Wanazuoni wakubwa sana wa rika lake ambao nao pia ni Wanafunzi wake na pia

waliofuatia baada yake akiwemo Al Harith Ibn Abi Usama, Imam Ibn Abi Ad Duniya, Imam Al Baladhuri, Imam Al Husein Ibn Fahm na wengineo.

Ambapo anasema Imam Al Khatib Al Baghdad kua: '**Amesema Ibrahim Al Harbi kua: 'Katika kila siku ya Ijumaa Ahmad Ibn Hanbal alikua akinukuu Hadithi kutoka kwa Ibn Is-haq kupitia kwa Ibn Sad kupitia kwa Al Waqidhi kisha huzizungumzia'**

Imam Al Khatib Al Baghdad anaendelea kusema kua: **'Ibn Sad alikua ni Mwanazuoni mwenye Ilm kubwa na Manufaa makubwa sana. Na amesema Imam Muhammad Ibn Musa Al Barbari, akasema kua: 'Vitabu vya Al Waqidhi vimebebwa na Roho nne ambapo ya kwanza ni ya Muhammad Ibn Sad.''**

Hivyo Imam Ibn Saad alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni Mahiri waliokua wanaojulikana katika ardhi ya Baghdad wenye kua na Ilm kubwa ya Tafsir, Tarikh, Fiqh, Hadith, Qur'an, Lugha na Nahw, ambapo anasema Imam Al Husein Ibn Fahm kua: '**Ibn Sad alikua na Ilm kubwa sana, amehifadhi Hadith nyingi sana na nukuu nyingi sana, vitabu tofauti vya hadith, Ilm rijal na Fiqh.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Nadim basi anasema kua: **'Ibn Saad alikua na Ilm kubwa sana juu ya Masahaba na Tabiina'**

Na Imam Ibn Bardi akasema kua: **'Ibn Sad alikua ni Mcha Mungu, Imam, Mwanazuoni na mwenye sifa nzuri hivyo tumemnukuaa mara nyingi sana**.'

Imam Adh Dhahabi amesema kuhusiana na Imam Ibn Sad kua: **'Ibn Sad ni Al Allamah Al Hafidh, Al Hujjah nani Muaninifu.'**

Imam Ibn Hajjar Al Asqallani akasema kuhusiana na Imam Ibn Sad kua: **'Ibn Sad ni Al Hafidh mkubwa sana na ni Mchunguzi anaeaminika.'**

Miongoni mwa vitabu vya Imam Ibn Sad ni pamoja na *Tabaqat Al Kubra* ambacho kina sehemu 8 na sehemu ya 1na ya 2 ni yenye kumzungumzia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* peke yake kimaisha, halafu sehemu ya 3 na 4 ni zenye kuyazungumzia maisha ya Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na sehemu ya 5, 6 na 7 ni yenye kuwazungumzia Wanazuoni waliofuatia baada ya Masahaba na sehemu ya 8 ni yenye kuwazungumzia Wanazuoni wa kike.

Imam Ibn Saad aliandika pia vitabu vyengine kama Al Zukhruf Al Qasri, Iftikhar Al Qahtani Aala Ananiyah, Tarikh, n.k. ambapo anasema Imam Al Husein Ibn Fahm kua: **'Ndani ya Tabaqat ya Ibn Sad mna Hadithi nyingi sana na nukuu nyingi sana pia.'**

Na ingawa Imam As Safadi anasema kuhusiana na kifo cha Imam Ibn Saad kua: **‘Ibi Saad alifariki mjini Baghdad katika siku ya Jumapili ya mwezi nne ya Jummada Al Akhira mnamo mwaka 222 Al Hijra’**

Lakini Imam Al Husein Ibn Fahm basi yeye ansema kua : **‘Ibi Saad alifariki mjini Baghdad katika siku ya Jumapili ya mwezi nne ya Jummada Al Akhira mnamo mwaka 230 Al Hijra na alizikwa kwenye Makaburi ya Bab Sham wakati akiwa na umri wa miaka 62.’**

IMAM ABU AL HASAN AL TUSI

Imam Abu Al Hasan Muhammad Ibn Islam Ibn Salim Ibn Yazid Al Tusi aliishi ndani ya Karne ya 3 ya mwanzoni ya Uislam, na alikua ni mwenye kuishi katika Ardhi ya Tus katika maeneo ya Khurasan ndani ya nchi ya Iran.

Imam Abu Hasan Al Tusi alikua ni Mwanazuoni mwenye Ucha Mngu mkubwa sana na Ilm kubwa sana ya Hadith na n mwenye kuaminika, kwani alisoma kutoka kwa Imam Ya’ala Ibn Ubayd, Imam Jafar Ibn Awn, Imam Yazid Ibn Harun, Imam Ubayd Allah Ibn Musa Imam Al Mukri na wengineo.

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Ibn Khuzaymah, Imam Ibn Abi Daud, Imam Muhammad Ibn Waki Al Tusi, Imam Husayn Ibn Muhamamd Al Kubani, Imam Ibrahim Ibn Abi Talib, n.k

Imam Abu Hasan Al Tusi alikua ni Imam mwenye umakini sana katika kujichunga kutokana na kutumia visivyokua halali yake, na alikua ni mwenye kuikimbia sana Riya kiasi ya kua alikua akisali Sala zake kisirisi nyumbani kwake, kwani siku moja alipokua akisomesha Hadith basi aliokota Kokoto na kisha akawauliza Wanafunzi wake: **‘Hivi jee hili si Jiwe?’** Wanafunzi wake wakasema: **‘Naam.’** Na kisha akaoneshea kwenye Jabali kubwa liliopo mbele yao na kisha akauliza tena: **‘Jee na lile sio jiwe?’** Wanafunzi wake wakasema: **‘Naam.’**

Hivyo Imam Abu Hasan Al Tusi akasema: **‘Kama lilivyokua Jabali lililokua kubwa na Kokoto hii kua ndoto kua yote ni mawe basi ndio pia hali ilivyokua kwa upande wa Riya kubwa na ndogo zote ni hatari.’**

Kisha Imam Abu Hasan Al Tusi akaendelea kusema kua **‘Hivyo mimi niko tayari kuzificha Ibada za Sala zangu ili zisioneana na hata Malaika wangu wa kulia na kushoto kama ingekua inawezekana.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Alisema Imam Abu Hasan Al Tusi kua: **'Hakika hakuna kitu nnachokiogopa zaidi mimi kama kuja kujikuta nimeteleza na kutumbukia kwenye Shirk, kwani Shirk Ndogo hua ni sawa na Unafiq'**

Imam Abu Hasan Al Tusi alikua ni mwenye kulia kila siku usiku kwa ajili ya Khofu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, kiasi ya kua hadi majirani zake walikua wakimsikia kwa namna alivyokua akilia usiku hadi wakiwa ni wenye kumuonea huruma. Na alikua si mtu mwenye kucheka kwa sauti.

Katika kipindi cha wakati wa Mutazila basi Imam Abu Hasan Al Tusi alipatwa na mitihani ya kulazimishwa kukubaliana na mtizamo wa kua Qur'an imeumbwa, lakini hata hivyo akakataa kukubalina na mtizamo huo na hivyo ikabidi afungwe Jela kwenye chumba cha chini ardhini kwa mda wa miaka 2, ambapo katika kipindi hiki ambacho yuko ndani basi alikua kila siku ya Ijumaa ni mwenye kukoga halafu kuvaa nguo zake za Ijumaa na kuelekea kwenye Mlango wa sehemu aliyofungiwa na kuomba ruhusa ya kuenda Msikitini kwa ajili ya kusali sala ya Ijumaa, lakini alikua ni mwenye kuzuiliwa, na hivyo akawa ni mwenye kusema:

'Ewe Mola wangu hakika mimi nilidhamiria kuenda kusali sala ya Ijumaa katika Jamaa Msikitini lakini hata hivyvo sikuruhusiwa kama ulivyoona, hivyo mimi sina la kufanya, kwani hali yangu iko wazi kwako wewe.'

Safari moja Mji wa Tusi ulitembelewa na Gavana wa Khurasan aitwae AbAllah Ibn Tahir, ambapo watu wa mji huo wakakusanyika kwa ajili ya kumpokea Gavana huyo, na sherehe za kuwasili kwake huko zilidumu kwa mda wa siku 3. Na ilipomlizika siku ya 3 basi Gavana Abd Allah Ibn Tahir akauliza: **'Hivi Jee kuna mtu yeyote yule maarufu ambae hajaja kwenye tafrija hii**?'

Miongoni mwa waliokuwepo karibu yake akasema: **'Naam, kuna Ahmad Ibn Harb na Muhamamd Ibn Aslam Al Tusi ambao ni Mawalii wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'** Ambapo nae akauliza : **'Kwanini wakawa hawajaja?'** na hivyo akajibiwa kwa kuambiwa kua: '**Hawa ni watu wawili wakubwa sana ambao hua wanapenda kukaa na kuishi kivyao vyao peke yao, kwani hua ni wenye kudumu na Dhikri Allah na kufanya Ibada peke yao, na ni wenye kujitenga kutokana na mambo ya kidunia na pia kutokana na watu wengine'**

Hivyo Abd Allah Ibn Tahir akasema: **'Kama ni hivyo basi itabidi sisi ndio tuwafuate wao.'**

Na hivyo akaamua inabidi apelekwe anapoishi Imam Ahmad Ibn Harb kwanza, na Abd Allah Ibn Tahir alipomuona Ahmad Ibn Harb basi akasema: '**Hakika nilisikia mimi**

kua Muonekano wa Sura yako ni wenye kuvutia sana kwa uzuri wako, lakini nilipokutana nawe sasa hivi nimegundua kua muonekano wako ni mzuri zaidi kuliko unavyoelezewa. Hivyo nilikua nakuomba kua jitahidi kua uulinde uso wako huu usiharibike kutokana na Madhambi na kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* na usifanye dhambi.'

Na kisha baada ya hapo Abd Allah Ibn Tahir akaelekea kwa Imam Abu Hasan Al Tusi lakini walipofika na kugoga Mlango basi mlango huo haukufunguka na hivyo akawa ni mwenye kusema: **'Ya Allah huenda labda ikawa ananichukia mimi huyu mtu kwa sababu ya Madhambi yangu, hivyo kutokana na kua yeye ni mmoja kati ya Mawalii wako basi nakuomba unisamehe Madhambi yangu kwani ingawa mimi si mja wako mwema lakini ukweli ni kua nampenda sana huyu mja wako kwa ajili yako'**

Na kwa kua siku hio ilikua ni siku ya Ijumaa, basi Abd Allah Ibn Tahir akaamua kua asiondoke mlangoni hapo hadi pale utakapowadia wakati wa Sala ya Ijumaa kwani alikua anajua kua Mtu huyo anaemsubiri atatoka tu, hivyo akamsubiri na ulipofika wakati wa sala tu basi Mlango huo ukafunguliwa na akatoka Imam Abu Al Hasan Al Tusi.
Hivyo Abd Allah Ibn Tahir akamsalima na kujitambulisha na kisha akamuomba Imam Al Tusi amuombee Dua, ambapo nae akamuombea.

Kutokana na ucha Mungu wake basi Imam Abu Hasan al Tusi alikua akiombea Dua watu na zikijibiwa hapo hapo, na wenye kuumwa walikua wakipoa kutokana na dua zake na Idhini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Anasema mmoja kati ya wanaomjua Imam Abu Hasan Al Tusi kua: '**Siku moja miminilimuona Ibilisi ameanguka kutoka juu angani hadi ardhini na nilipomuuliza: 'We Maluun ndio unafanya nini?'** ambapo nae akasema: **'Sasa hivi nimemuona Muhamamd Ibn Aslam akiwa natia Udhu hivyo kutokana na khofu yangu nilikimbia na matokeao yake nikaanguka hapa badi kidogo nivunje mguu wangu.''**

Imam Abu Hasan Al Tusi alikua ni mwenye kuwatekelezea na kuwatatulia watu matatizo yao na alikua akiwalipia madeni yao wanaodaiwa pia na kuwaambia wanaodai kua wasiwaambie hao wanaodaiwa kua wamelipiwa na nani. Hivyo siku moja kuna Myhaudi alikuja kwa Imam Abu Hasan Al Tusi na kuomba msaada lakini Imam Abu Hasan alikua hana kitu, isipokua Penseli ambayo alikua akiichonga kwa kisu chake, hivyo Imam Abu hasan Al Tusi akamwambia yule Myahudi kua: **'Okoto hivyo vipande vya mbao ya penseli vilivyoanguka hapo chini.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Yule Myahudi akashangaa lakini akainama na kuokotoa vipande hivyo ambavyo navyo mara tu baada ya kuingia mikononi mwake basi vikageuka kua ni vipande vya Dhahabu, hivyo yule Myahudi akashangaa zaidi na ksuema: **'Kutokana na kuwepo Mtu kama wewe, na vipande vya mbao vinakua Dhahabu kutokana nawe basi sina la kufanya mimi isisokua kukubali kua Dini yako wewe unayoifuata ni Dini ya Haki, hivyo nami nimekubaliana nayo kuifuata.'**

Anasema Abu Abd Allah kua: **'Mimi nilienda kwa Muhamamd Ibn Aslam siku nne kabla ya kufariki kwake, ambapo aliniambia kua: 'Ewe Abu Abd Allah, Jee nikupe bashirio jema juu ya mema aliyonifanyia *Allah Subhanah wa Ta'ala*?' kwani sasa hivi wakati nakikaribia Kifo changu, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kujua kuhusiana na udhaifu wa mwili wangu kutokana na kustahmilia hesabu, basi hakuichia kitu cha kuhesabiwa juu yangu, hivyo baada ya ufariki kwangu na kukoshwa na kuvishwa Sanda, basi chukueni hili busatii nililolilalia juu yake, na nifunike na Msala wangu, na nguo zangu na bakulia nililokua nikilitumia kwa ajili ya kutilia Udhu, kisha mpeni mtu yeyote yule ambae nimasikini mwenye kusali.**

Ndani ya Kipochi changu mna Dirham 30, ambazo nimempa Mtoto wangu, hizo ni pesa za Halali, baada ya hivyo basi sina chengine cha kutoa. hivyo toka na kisha funga Mlango kwani nataka niwe peke yangu hadi wakati wa Kufariki kwangu, kwa sababu nilikua peke yangu hapo awali nilipokua kwenye sehemu za siri za Baba yangu, na nikawa peke yangu ndani ya Fuko la uzazi la Mama yangu. Nilikuja peke yangu nilipotoinga Ulimwenguni, hivyo pia nataka niwe peke yangu wakati naondoka Ulimwenguni, nitaua peke yangu nitakapofukiwa Kaburini, na nitakua peke yangu nitakapoulizwa masuali na Munkar na Nakir, kitakachofuatia baada yake iwe kizuri au kibaya basi nitakabiliana nacho peke yangu, hivyo kuna faida gani kwa watu kua pamoja nami ambao hata hivyo baadae wataniacha peke yangu?'

Imam Abu Hasan Al Tusi alifariki katika siku ya nne baada ya tukio hilo, ambapo wakati anaenda kuzikwa basi watu walikua wakiambiana: 'Enyi watu huyu ni Mwanazuoni ambae alikuja Ulimwenguni akiwa na malengo yake, kwanikwa hakika huyu hakua kama Watu wengine ambao walikua ni Watumwa kwa Matumbo yao. Muhammad Ibn Aslam alikua ni Mtu ambae yuko juu kiasi ya kua alikua si mwenye kuhadaika na Ulimwengu na wala Ulimwengu haukuweza kumhadaa yeye.'

Siku moja kabla ya kufariki kwake katika mwezi wa Muharram wa Mwaka 242 Al Hijra basi Mmoja kati ya Majirani yake, alilala akamuona Imam Abu Hasan Al Tusi akimwambia kwa kusema: **'Alhamd lillah, nimefanikiwa kuepukana na matatizo'** hivyo asubuhi yake akaamua kua aende akamwambie kuhusiana na ndoto yake hio lakini

alipofika akaambiwa kua Imam Abu Hasan Al Tusi ameshafariki. Maziko ya Imam Abu Hasan Al Tusi yalihudhuriwa na Maelfu ya watu.

Baada ya kufariki kwake Imam Abu Hasan Al Tusi, basi siku moja Imam Abu Ali Al Farmadi alikua akitoa Mawaidha Msikitini na kisha akaulizwa: **'Kulingana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi tunaona kua Wanazuoni ni Warithi wa Mitume, hivyo jee ni Wanazuoni gani waliotajwa kwenye Hadithi hii?'** ambapo Imam Abu Ali akasema huku akioneshea kwenye Kaburi la Imam Abu Hasan Al Tusi kua: **'Wanazuoni ni wachache sana, lakini mmoja miongoni mwao ni yule alielala Pembeni yetu Msikitini hapa.'**

Amesema Imam Abu Al Hasan Al Tusi kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alichora mstari ulionyooka ardhini na kisha akasema kua: 'Hii ndio njia ya *Allah Subhanah wa Ta'ala'* na kisha akachora vistari vyengine pembeni yake kushoto na kulia kwake na kisha akasema: 'Kuna njia za Ibilis katika kila sehemu ya njia hii ambazo hua anawaitia watu katika njia yake. Hivyo hii ndio njia sahihi, ifuateni njia hii na wala msiwe ni wenye kugawanyika kwenye makundi.''**

Kisha Imam Abu Hasan Al Tusi akasoma aya ifuatayo:

﴿وَأَنَّ هَٰذَا صِرَاطِى مُسْتَقِيماً فَٱتَّبِعُوهُ وَلاَ تَتَّبِعُواْ ٱلسُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ﴾

Waanna hadha siratee mustaqeeman faittabiAAoohu wala tattabiAAoo alssubula fatafarraqa bikum AAan sabeelihi dhalikum wassakum bihi laAAallakum tattaqoona *(Al Anaam 6:153)*

Tafsir: ***Na kwa hakika, hii ndio njia iliyonyooka, hivyo ifuateni na wala msifuate njia nyengine, kwani zitakutenganisheni kutokana na njia yake. Juu ya hili amekuamrisheni ili mpate kua wenye Taqwa****.*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema: 'Bani Israil waligawika katika makundi 71 ambapo 70 kati yao yamelekea Motoni, na Kundi moja limeokoka, Manasara waligawika katika makundi 72 na makundi 71 yameenda Motoni na kundimoja limeokoka, na baadae pia Ummah wangu utagawika katika makundi 73 ambapo makundi 72 yataenda Motoni na kundi moja litaokoka'**

Msahaba wakauliza: 'Ya Rasul Allah! Jee ni kundi lipi hilo litakalookoka?'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akajibu kwa kusema: 'Kundi litakalookoka ni la wale watakaofuata njia ninayoifuata mimi pamoja na Masahaba wangu'**

Imam Abu Al Hasan Al Tusi anaendelea kutuambia kua: '**Hivyo mimi nimeichukua Hadithi hii kua ndio kigezo cha kila kitu changu, kama kinaendana na hadithi hii basi hushikamana nacho na kama hakiendani na Hadithi hi basi nacho, hivyo kama Wanazuoni watafanya hivyo pia basi watakua ni wenye kushikamana na njia ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, lakini hata hivyo kuna ambao wamehadaiwa na Mapambo ya Dunia, kwani kama Hadithi ingesema kua: 'Wote wataenda Peponi isipokua Kundi moja tu' basi ingekua tunakhofu ya kuwepo kwenye kundi hilo, lakini sasa Hadith imesema wataenda Motoni wote isipokua Kundi Moja.**
Alisema Imam Abu Hasan Al Tusi kua: **'Imani hua ni kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala*, Malaika wake, Vitabu vyake, Mitume wake, Siku ya Mwisho na Makadirio yake iwe mazuri au mabaya'**

Ambapo mwanzo wa Iman hua ni Rehma na fadhila zake kwa yule amtakae miongoni mwa Waja wake, kwa kumfadhili Mja wake Imani ndani ya Moyo wake kwa kummurikia Nuru, ambayo kutokana nayo hua ni yenye kuunawirisha Moyo wa Mja wake na hivyo hua ni wenye kufunguka na kumtanulia kifua chake na kumzidishia Imani na hivyo kumfanya Mja kua ni mwenye kuzidi kumpenda Mola wake.

Hii hua ni hali ambayo Moyo huo hua ni wenye kuamini kuhusiana na hisia za kuamini kuhusiana na kufufuliwa baada ya kufa, kuhesabiwa juu ya kila alilolifanya, malipo ya Pepo au Moto ambayo yote haya hua ni kutokana na Nuru ya Imani inayomurika ndani ya Moyo wa mja husika kutokana na mmuriko huo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Mja wake.

Wakati Moyo wa Mja unapoamini basi hata Ulimi wake hua ni wenye kutamka na kuthibitisha ipasavyo na viungo vya mwili hua ni vyenye kutekeleza maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuachana na makatazo yake. Na linapotokea hili basi Mja husika hua ni Muislam aliekamilika na kupea na hapo hutokea ile hali iliyoelezewa katika aya ifuatayo:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

﴿وَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّ فِيكُمْ رَسُولَ ٱللَّهِ لَوْ يُطِيعُكُمْ فِى كَثِيرٍ مِّنَ ٱلْأَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلَـٰكِنَّ ٱللَّهَ
حَبَّبَ إِلَيْكُمُ ٱلْإِيمَـٰنَ وَزَيَّنَهُۥ فِى قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ ٱلْكُفْرَ وَٱلْفُسُوقَ وَٱلْعِصْيَانَ
أُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلرَّٰشِدُونَ﴾

WaiAAlamoo anna feekum rasoola Allahi law yuteeAAukum fee katheerin mina al-amri laAAanittum walakinna Allaha habbaba ilaykumu al-eemana wazayyanahu fee quloobikum wakarraha ilaykumu alkufra waalfusooqa waalAAisyana ola-ika humu alrrashidoona *(Surat Al Hujurat 49:7)*

Tafsir: ***Na fahamu kua yuko pamoja nanyi Rasul Allah(Salallahu Alayhi wa Salam), ambae lau kama angekutiini nyinyi basi katika mambo mengi yenu basi mngekua mmelaanika, lakini Allah ameipendea juu yenu Imani a akaipendezesha ndani ya Nyoyo zenu na akaikirihisha juu yenu Kufuru na uovu na uasi. Hao (wenye Imani) ndio walioongozwa.***

Na pia katika aya ifuatayo pale aliposema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿أَفَمَن شَرَحَ ٱللَّهُ صَدْرَهُۥ لِلْإِسْلَـٰمِ فَهُوَ عَلَىٰ نُورٍ مِّن رَّبِّهِۦ فَوَيْلٌ لِّلْقَـٰسِيَةِ قُلُوبُهُم
مِّن ذِكْرِ ٱللَّهِ أُو۟لَـٰٓئِكَ فِى ضَلَـٰلٍ مُّبِينٍ﴾

Afaman sharaha Allahu sadrahu lil-islami fahuwa AAala noorin min rabbihi fawaylun lilqasiyati quloobuhum min dhikri Allahi ola-ika fee dhalalin mubeenin *(Surat Az Zumar 39:22:)*

Tafsir: ***Jee yule ambae Allah amemfungulia Moyo wake kwa Uislam na hivyo kua ndani ya Nuru ya Mola wake(ni sawa na asiekua Muislam?) hivyo Ole wao wale ambao Nyoyo zao zimegukua ngumu kumkumbuka Mola wao, kwani wako katika Udhalili mkubwa sana.***

Imam Abu Al Hasan Al Tusi anaendelea kutuambia kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kua: 'Yule ambae ni mwenye Imani Iliyokamilia basi hua ni Mwenye Tabia bora zaidi''**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abu Al Hasan Al Tusi anaendelea kutuambia kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kua: 'Sala ya Fardhi hua kwa ajli ya kafara za kasoro za kuanzia Sala moja hadi nyengine, na Sala ya Ijumaa hua ni Kafara ya Makosa ya Ijumaa moja hadi nyengine''**

Imam Abu Al Hasan Al Tusi anaendelea kutuambia kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kua: 'Kikumbukeni Kifo, ambacho hua ni chenye kusitisha Matamanio ya Kustarehe''**

Imam Abu Al Hasan Al Tusi anaendelea kutuambia kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kua: 'Yeyote yule atakaesema *La Ilaha Illa Allah* ataingia Peponi' Mashab wakauliza: 'Jee hua kuna ishara gani juu ya hilo?' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kwani kauli hii hukukataza wewe kutokana na yale aliyoyaharamisha Allah.''**

Imam Abu Al Hasan Al Tusi anaendelea kutuambia kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kua: 'Haikua Dini ya Kiislam isipokua Kupenda kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'al*a na Kukasirika kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

﴿قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

Qul in kuntum tuhibboona Allaha faittabiAAoonee yuhbibkumu Allahu wayaghfir lakum thunoobakum waAllahu ghafoorun raheemun *(Surat Al Imran 3:31)*

Tafsir: **Sema Ewe (*Muhamamd Salallahu Alayhi wa Salam*) kua: 'Kama kweli mnampenda Allah basi nifuateni mimi na Allah atakupendeni na kukusameheni Dhambi zenu, kwani Allah ni mwingi wa Kusamehe na mwingi wa Rehma'**

Amesema Imam Muhamamd Ibn Rahawayh kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kua: 'Kwa hakika *Allah Subhaanh wa Ta'ala* haujaalii Ummah wa Muhammad kukubalia juu ya upotovu' ambapo Is-haq Ibn Rahawayh amesema kua: 'Pale Wajinga wanaposema haya hua wanamaanisha Watu wa Ummat Muhammmad, lakini Watu wa Ummat Muhammad hua ni Ummah wa Wanazuoni wanaofuata Nyayo zake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambao ni wenye kumfuata yeye na waliokua pamoja nae, na wale wanaopingana nao hua**

ni wenye kuachana na Ummah, ambapo Mmmoja wao Wanazuoni hao ni Muhamamd Ibn Aslam'

IMAM ABU UBAYD AL BUSRI

Imam Abu Ubayd Muhamamd Ibn Hasan Al Busri alizaliwa katika Kijiji cha Busri kilichomo katika Mji wa Dimashq nchini Syria. Imam Al Busri alikua ni mwenye kujipatia Ilm yake kutoka kwa Imam Abu Turab Hasabi, Imam Ahmad Ibn Yahya, Imam Abu Said Al Haraz na wengineo.

Imam Abu Ubayd alikua ni miongoni mwa Wacha Mungu na Mawalii wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, kwani anasema Imam Abu Zurah kua: '**Safari moja Abu Ubayd alipokua katika Ibada ya Hija pamoja na Mtoto wake walipokua katika mmaeneo ya Arafa, basi alimpongeza mtoto wake kwa kumwambia kua: 'Hongera kwa kupata Mpiganaji' ambapo Mtoto huyo huyo akauliza: 'Mpiganaji gani?' Abu Ubayd akasema: 'Leo hii sasa hivi umepata Mtoto wa Kiume' hivyo walipomaliza Ibada ya Hija na kurudi katika Syria basi mtoto wake akapata habari kua mke wake alijifungua Mtoto wa Kiume katika siku ya Arafah**'

Ambapo anasema mmoja kati ya Wanafunzi wa Imam Abu Ubayd kua: **'Safari moja Siku tatu kabla ya Ibada ya Hija walikuja Mawalii wawili kwa Abu Ubayd, na kisha wakamuuliza kama ataenda kwenye Ibada ya Hija, lakini nae akasema kua hawezi kwenda na kisha akanigeukia mimi usoni na kuniambia: 'Shaykh wako amepewa bahati ya kuwasili katika Mji wa Makkah kwa mda mfupi zaidi ya inavyotarajiwa tofauti na itakavyokuwa katika kuwasili kwa Mahujaji wengine, kwani yeye amejaaliwa *Tayy-al Ardh* (Kuikunja Ardhi)''**

Mbali ya kua Imam Al Busri alikua ni Mwanazuoni lakini alikua pia ni Mpiganaji Mahiri na mpandaji farasi mahiri sana. Ambapo safari moja wakati alipokua anaelekea kwenye Mapigano ya Jihadi basi Farasi wake alifariki Njiani, hivyo Imam Al Busri akamuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua amfufue Farasi wake huyo ili awe pamoja nae hadi atakaporudi kwenye Vita hivyo vya Jihad, ambapo kwa Idhini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Farasi huyo akayanyuka, na hivyo Imam Al Busri akaendelea na Safari yake hiyo kapigana Vita na kisha akarudi Nyumbani na Farasi wake.

Na aliporudi nyumbani basi akamwambia Mtoto wake kua amvue farasi wake huyo tandiko lake, hivyo Mtoto huyo akaelekea kwenye Farasi huyo na alipofika basi akamkuta Farasi huyo anatoka jasho jingi sana. Hivyo akaamua kuachana nalo tandiko hilo, lakini alipoachana nalo basi akasikia sauti inasema: '**Chukua Tandiko lenu kwani**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

limeazimwa tu nasi’ na hivyo akalichukua Tandiko hilo na baada ya kulichukua basi hapo hapo Farasi huyo akaanguka chini na kufariki.

Kwa upande mwengine basi Imam Al Busri alipokua katika Mji wa Dimashq alikua ni mwenye kuwasomesha watu kuhusiana na Ilm ya Dini ya Kiislam na kuwausia kufanya mema na kauchana na maovu, na unaowadia mwezi wa Ramadhani basi huhama chumbani kwake na huhamia katika chumba chengine ambacho hua anakua peke yake kwa ajili ya kufanya ibada peke yake yeye na Mola wake tu.

Ambapo anasema Imam Ahmad Ibn Yahya kua: ‘**Hakika mimi nimesoma kwa Wanazuoni 600 ambao wana Ilm kubwa sana lakini sijawahi kuona kama wanne hawa ambao ni Dhu Nun Al Misri, Abu Turab Al Nahsabi, Abu Ubayd Al Busri na Abu Al Abbas Ibn Ataa.**’

Siku moja Mtoto wa Imam Abu Ubayd ambae alikua anafanya biashara ya kuuza Mafuta, alikuja kwa Imam Abu Ubayd Al Busri na kulalamika kwa kusema; ‘**Baba jee unajua kua mimi nilikua na ule mtaji wangu wa mafuta lakini jana wakati natoka basi likanianguka lile Jagi la Mafuta na kuvujika na hivyo sasa hivyo sina mtaji wowote.**’
Hivyo Imam Al Busri akamwambia mtoto wake huyo kua asiwe na khofu wala wasi wasi kwani Mwenye kutoa riziki ni *Allah Subhanah wa Ta’ala*, hivyo atamjaalia njia nyengine na bahati nyengine kwajili ya kujipatia riziki yake, na haina haja ya kua ni mwenye kupendelea umiliki wa mambo ya kidunia, kisha akasema: ‘**Ewe Mtoto wangu, unaweza pia kuwekeza kwenye mtaji wa Baba yako, kwani Wa Allahi Baba yako hana Mtaji mwengine wowote ule isipokua *Allah Subhanah wa Ta’ala* hapa Duniani na Akhera.**’

Akausia Imam Abu Ubayd Al Busri kwa kusema kua: **‘Dhikr inatakiwa iwe ni yenye kuanza ndani ya Nyoyo, kwani ikifanywa kwa Ulimi tu na hivyo kua si yenye kuingia ndani ya Moyo basi hua ni Riya.**’

Ambapo anasema pia mmoja kati ya Wanafunzi wake Imam Al Busri kua: ‘**Mimi nilienda kumuaga Mwalimu wangu Imam Al Busri kwa ajili ya kupata Dua zake kabla ya Safari yangu ya Hija. Ambae nae baada ya Dua basi akaniuliza: ‘Jee una mzigo wowote ule pamoja nawe?’**

Nami nikasema: ‘La sina chochote isipokua kibuyu cha Maji’ ambapo nae akaniambia: ‘Sawa, hivyo utakapokua na shida yeyote ile njiani basi basi Sali Rakaa mbili huku ukiwa umekiweka hicho kibuyu chako cha Maji katika upande wa kulia, na kisha omba ukitakacho na baada ya sala yako angalia kwenye upande wa kulia kwako, kwani kila ulichokiomba utakiona kimetokea kwenye upande wa kulia kwako.’’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Hivyo nikamshukuru na kuagana ane na nilipokua kwanye Msafara wa Hija njiani basi ikawa hatukuweza kua ni wenye kupata Maji njiani, watu wakawa wanahaha kwa kiu, hivyo nami nikakumbuka ushauri wa Mwalimu wangu. Hivyo nikakitoa kibuyu changu nikakiweka kwenye upande wa Kulia kwangu kisha nikasali Rakaa mbili, na kuomba maombi yangu na nilipomaliza kusali na kuangalia upande wa kulia kwangu, mara ukatokea Upepo wenye kuvuma na kikatokea kiwingu na mvua ikaanza kunyesha, hivyo tukanywa Maji na kujaza vibuyu vytetu na kumshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Miujiza ya Mwalimu wangu.'

Imam Abu Ubayd Al Busri alifariki mnamo mwaka 245 Al Hijra.

IMAM AL BUWAYTI

Imam Abu Ya'qub Yusuf Ibn Yahya Al Buwayti Al Misri alikua ni mrithi na pia ni Mwanafunzi Mkubwa wa Muhammad Idris Al Shafii alizaliwa katika kijiji cha Buwaith kilichopo nchini Misri.

Imam Al Buwayti alianza kusoma tangu akiwa mdogo kwa kuanzia kwenye Qur'an, kisha Hadith na baadae akaingia kwenye fani ya Tafsri, Kalam, Lugha na Fiqh ambapo mwanzoni alikua ni mfuasi wa Fiqh ya Imam Malik kupitia kwa Imam Al Layth Ibn Sad, hadi pale Imam Al Shafii alipohamia katika ardhi ya Misri na kuanza kusomesha ambapo nae Imam Al Buwayti akaanza kusoma kwake na mfuasi wa Fiqh ya Imam Al Shafii, na hivyo kua miongoni mwa waendelezaji wakuu wa Fiqh hio.

Mara kadhaa Imam Muhamamd Idris Al Shafii alikua akiulizwa suali mbele ya Imam Al Buwayti basi alikua akisema kua: '**Muulizeni huyu hapa kwani yeye ndie mwenye Ulimi wangu.'** Na hivyo Imam Al Buwayti alikua ni mwenye kutoa Ftawa mbele ya Imam Al Shafii kulingana na Mitizamo ya Fiqh ya Imam Al Shafii kwa idhini ya Imam Al Shafii.

Siku moja Imam Muhamamd Idris Al Shafii alikua akiwasomesha Wanafunzi wake wawili ambao ni Imam Al Buwayti na Imam Al Muzani na hivyo akasema kumwambia Imam Al Buwayti kua: '**Wewe Utafariki wakati ukiwa Kifungoni**' na kisha akamtizama Imam Al Muzani kua: '**Na wewe Utafariki kutokana na Kubishana.**'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Mnamo mwaka 204 Al Hijra wakati Imam Al Shafiii akiwa taabani anaumwa kabla ya kufariki kwake, basi Imam Al Humaidi ambae ni Mwanafunzi ambae ni mkubwa kiumri miongoni mwa Wanafunzi wa Imam Al Shafii alimtembelea Imam Al Shafii na kumtaka achague kiongozi miongoni mwa Wanafunzi wake kwa ajili ya kuwaongoza baada ya kufariki kwake ili kuepusha mivutano baada kufariki kwake, ambapo Imam Al Shafii akasema; '**Hakuna anaestahiki kua kiongozi wenu miongoni mwenu zaidi ya Al Buwayti**'

Hivyo kabla ya kufariki kwake Imam Al Shafii basi Imam Al Buwayti alikua akiendesha Darsa ya Imam Al Shafii kama alivyoku akifanya Imam Al Shafii mwenyewe, na baada ya kufariki Imam Al Shafii basi Imam Al Buwayti akawa ndio kiongozi mkuu wa Madhhab ya Imam Al Shafii na hivyo kua ni mwenye kuota Wanafunzi wengi waliozidi kuisambaza Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii katika maeneo mengine Duniani.

Bila ya shaka kila kizuri hakikosi kua na Uadui na upinzani, kwani kutokana na kua na Ilm ubwa sana kwa Imam Al Buwayti hivyo huku umaarufu wa Imam Al Buwayti ukizidi kuogezeaka kutokana na ukubwa wa Ilm yake na wengi wa wafuasi wake basi wakatokea wale ambao walikua na nia ya kumuangusha kutoka katika Darja yake, ambapo miongoni mwao alikuwepo Imam Abu Layth Al Hanafi ambae pia alikua hafurahii kuongezeka kwa wafasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii na hivyo akaamua kumchongea Imam Al Buwayti kwa Khalifa Al Wathiq wa Utawaala wa Al Abbas wa Baghdad.

Ambapo katika kipindi hiki katika Ulimwengu wa Kiislam kulikua kuna fitna mitizamo ya Aqida kutoka kwa Mutazila, hii ni Fitna ambayo ndio iliyomuingiza pia Imam Ahmad Ibn Hanbal matatani na kufungwa jela pia amapo baadae akatolewa. Katika kipindi hiki cha Imam Al Buwayti utawala wa Khalifa Al Wathiq ulikua bado una nguvu hadi nchini Misri.

Hivyo Imam Abu Layth akatuma habari mjini Baghdad kua Imam Al Buwayti ana msimamo wa Kua Qur'an si kiumbe, ambao msimamo huo hua ni kuenda kinyume Aqida ya Mutazila ambao wao walikua wakisema kua Qur'an imeumbwa. Hivyo Khalifa Al Wathiq akatuma jeshi kutoka Baghdad kuelekea katika ardhi ya Misri kwa ajili ya kumkamata Imam Al Buwayti, ambapo jeshi hilo lilipofika nchini Misri na kumuuliza kuhusiana na Suali hilo basi akasema: '**Hakika mimi nna Wafuasi wengi ambao watapotoka kama nikijidai kutaka kujiepusha na kifungo.'** Hivyo Imam Al Buwayti akafungwa pingu na minyororo na kupelekwa mjini Baghdad.

Imam Al Rabbi Ibn Sulayman Al Shafii ambae ni Mwanafunzi pia wa Imam Al Shafii anasema kuhusiana na tukio hili kua: '**Mimi nilimuona Imam Al Buwayti akiwa amefungwa pingu ya mbao ya shingo na mnyororo ambao uzito wake ni takriban**

kilo 20, mikono yake na miguu ikiwa imefungwa pingu na minyororo ambayo nayo pia ina uzito wa takriban kilo 20. Ambapo katika wakati huo Imam Al Buwayti alikua akisema: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* amewaumba Viumbe wake kwa kusema *Kun*, na Vikawa, hivyo kama neno *Kun* ni Kiumbe, basi hii itamaanisha kua Muumba ameuma kiumbe ambacho nacho kikaumba kiumbe chengine, hivyo kama nikikutana na Al Wathiq basi nitamfahamisha ukweli huu ulivyo''

Subhana Allah, ni kutokana na maneno haya basi Imam Al Buwayti alipokamatwa hakua ni mwenye kuepelekwa mbele ya Khalifa Al Wathiq kwani alikua wanajua kua huenda maneno hayo yakaja kuubadilisha mtizamo wa Aqida ya Khalifa Al Wathiq na hivyo Imam Al Buwayti alichukuliwa na kupelekwa moja kwa moja mahkamani kwa Qadhi Mkuu wa Mutazila aitwae Ahmad Ibn Abi Daud ambapo nae aliposikia ujumbe huo basi moja kwa moja akahisi kua Ufahamu na Hoja za Imam Al Buwayti unaweza ukawaharibia malengo yao ya kuungwa mkono na Mamlaka yao na hivyo akamhukumu Imam Al Buwayti kwa kifungo cha miaka minne Jela.

Katika kipindi hiki ambacho Imam Al Buwayti alikua kifungoni basi alikua katika hali mbaya sana kwani alifungiwa kwenye chumba cha chini ya Ardhi na hivyo alikua hajui wakati wa saa, wala siku, wala wiki wala mwezi wala mwaka, hivyo ilikua ni vigumu kwake kufanya Ibada katika wakati husika, kwake yeye alikua anajua wakati wa kupigwa mijeledi tu pale anapoona Mpiga mijeledi anafungua mlango na kuingia ndani kwa ajili ya kumuadhibu ilia badilishe mtizamo wake.

Ambapo hata hivyo Imam Al Buwayti kamwe hakua ni mwenye kuachana na Mtizamo wake wala Ibada zake, kwani alikua akifanya Dhikr, akisoma Qur'an na kusali kimakisio. Imam Al Buwayti aliwaelezea Wanafunzi wake juu ya hili katika barua aliyoiandika kweye kitambaa kwa kutumia wino wa Damu yake na kumpa mmoja kati ya waliomtembelea ambayo ujumbe wake ulikua inasema: '**Hakika mimi nimezuiliwa kutokana na kujitoharisha na kufanya Ibada, hivyo niombeeni kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ili anitafutie njia bora zaid ya kutokana na hili jambo kulingana na udhaifu wangu.**'

Imam Al Buwayti akakumbukia kile ambacho alitabiriwa na Mwalimu wake Imam Muhamamd Idris Al Shafii kua yeye atafariki Kifungoni na kweli hali ilikua hivyo kwani Imam Al Buwayti alifariki mnamo mwaka 231 Al Hijra katika mwezi wa Rajab wakati alipokua gerezani kutokana na kupigania haki za Waislam na kusema kweli, kuamrisha mema na kukataza mabaya mbele ya Watawala, kwani alikua ni mtu ambae asiemuogopa yeyote isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala*, kifo chake Imam Al Buwayti kiliwahuzunisha wengi miongoni mwa Wanazuoni na watu mbali mbali kwani Dunia ilikua imepoteza mmoja kati ya Watu wenye Ilm kubwa sana.

Miongoni mwa vitabu ambavyo aliviandika Imam Al Buwayti kabla ya kufariki kwake ni kile kinachojulikana kama *Al Mukhtasar Al Buwayti*. Hiki ni kitabu ambacho ni miongoni mwa vitabu Mama vya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kwani kilikua ni kitabu ambacho ni chenye mkusanyiko wa Mukhtasar wa Kitabu cha Fiqh cha Imam Al Shafii kiitwacho *Kitab Al Umm* na pia kina mitizamo ya kujitegemea ya Imam Al Buwayti.

Hivyo kitabu hiki cha Imam al Buwayti kiitwacho Mukhtasar Al Buwayti si kama kinavyojielezea katika jina lake kua ni Mukhtasar na hivyo kubainisha mtizamo wa Ufupisho wa Kitabu cha Fiqh ya Imam Al Shafii lakini ukweli ni kua kitabu hiki ni kikubwa kwani kina kurasa 1152, na ni kitabu ambacho si chenye kitumika kwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii tu ambapo miongoni mwao walionukuu ni pamoja na Imaml Juwayni, Imam Abu Is-haq Al Shirazi, Imam Al Ghazali, Imam Al Mawardi, Imam Al Rafi na Imam An Nawawi lakini pia hiki ni kitabu ambacho kimekua kikitumiwa na Wanazuoni wa Madhhab manne tofauti ya *Ahl Sunnah wa Al Jamah,* kwani ni kitabu cha Mwanzo cha Mukhtasar wa Fiqh katika historia ya Kiislam.

Imam Al Buwayti ambae alikua pia akijulikana *Al Shafii Al Awwal* yaani Shafii wa kwanza baada ya Imam Al Shafii mwenyewe kutokana na kua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Fiqh ya Imam Al Shafii na fani nyengine za Ilm ya Dini ya Kiislam alikua pia ni Mcha Mungu na Mwenye Taqwa, mwenye kudumu na Dhikr Allah , ambapo anasema Imam Taqi Ad Din Al Subki kua: ***'Imam Al Buwayti ni mwenye kufikia Darja ya Siddiqin'*** yaani Darja ya pili kwa kua juu baada ya Darja ya Mitume.

IMAM ABU THAWR 170 AH

Imam Abu Abd Allah Ibrahim Ibn Khalid Ibn Abi Al Yamân Abu Thawr Al Kalbi Al Baghdadi alizaliwa mnamo mwaka 170 Al Hijra katika maeneo ya Baghdad nchini Iraq. Imam Abu Thawr alisoma kwa Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Waqi Ibn Jarrah, Imam Al Shafii, Abd Rahman Ibn Mahdi na wengineo wakiwemo Wanafunzi wa Imam Abu Hanifa.

Hivyo Mwanzoni Imam Abu Thawr alikua ni mfuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, lakii baada ya kukutana na Imam Al Shafii na kusoma kwake basi Imam Abu Thawr akahama kutoka kwenye Madhhab ya Imam Abu Hanifa na kuhamia kwenye Madhhab ya Imam Al Shafii.

Ambapo anasema Imam Abu Hatim Ibn Hibban kua: **'Imam Abu Thawr alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa sana katika Ulimwengu huu.'**

Na hii ni kwa sababu tunapomzungumzia Imam Abu Thawr basi hua tunamzungumzia Imam mwenye Ilm kubwa sana, kiasi ya kua alifikia darja ya kua ni *Mujtahid Muntasib,* na hivyo kua ni Imam anaetegemewa mitizamo yake si katika Madhhab ya Imam Al Shafii tu bali pia kwa *Ahl Sunnah wa Al Jamaah* kwa ujumla.

Ambapo tunapozungumzia *Mujtahid Muntasib* basi hua tunazungumzia Mujtahid ambae ni anaefuata Madhhab fulani lakini kutokana na kua na Ilm na ufahamu mkubwa sana basi hua ni mwenye kufanya jitihada katika kutoa Fatwa kulingana na Mtizamo wake lakini kwa kutumia muongozo wa njia ambazo ni zenye kutumiwa na Mujtahid Mkuu wa Madhhab ambapo kwa wake Imam Abu Thawry basi kama tulivyoona kua alikua ni Imam Muhammad Idris Al Shafii. Na hivyo katika baadhi ya Fatwa basi Imam Abu Thawry alikua na mitizamo yake iliyotofautiana na mitizamo ya Imam Al Shafii.

Na ndio maana siku moja Imam Ahmad Ibn Hanbal aliulizwa suali ambapo nae akajibu: '**Ama kuhusiana na suali hili basi waulize wenye kujua zaid kuhusiana na sharia, muulize Abu Thawr.'**
Miongoni mwa Wanafunzi wake Imam Abu Thawr ni Imam Abu Daud, Imam Ibn Majah, Imam Muslim, Imam An Nasai, Imam Al Junayd, Imam Al Baghawi, Imam At Tirmidhi, Imam Ibn Majah na wengineo, ambapo anasema Imam An Nasai kuhusiana na Imam Abu Thawr kua: '**Imam Al Thawr alikua ni Muaminifu na ni mwenye kuaminika na ni Mwanafiqh.**'

IMAM AL HUMAIDI 170 AH

Imam Abd Allah Ibn Az-Zubair Ibn Isa Ibn Ubaid Allaah Ibn Usaamah Ibn 'Abd Allaah Ibn Humaid Ibn Zuhair Ibn Al-Hariths Ibn Asad Ibn' Abdul 'Uza, Abu Bakr Al Humaidiy Al Asadiy Al Quraishi Al Makki alizaliwa katika Mji wa Makkah mnamo mwaka 170 Al Hijra.

Imam Al Humaidi alikua ni mtu mwenye kutokana na kabila la mke wa mwanzo wa R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yaani *Umm Ul Muumini* Khadija Bint Khuwaylid *Radhi Allahu Anha* ambalo ni kabila la Banu Asad, na alisoma chini ya Wanazuoni wengie wakiwemo Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Fudayl Ibn Iyad, Imam Sufyan Ibn Uyaynah ambae alikua na ukaribu mkubwa sana nae, Imam Al Humaidi alihifadhi kutoka kwa Imam Sufyan Ibn Uyaynah takriban hadith 10,000.

Ambapo anasema Imam Abd Rahman Abu Hatim kua: '**Amesema Muuhammad Ibn Abd Rahman Al Harawy kua: 'Mimi niliwasili katika Mji wa Makkah katika**

mwaka 198 Al Hijra ambao ndio aliofariki Ibn Uyaynah mwanzoni mwa mwaka huo, kwani alifariki miezi 7 kabla ya kuwasili kwetu, hivyo tukaulizia kuhusiana na Rafiki wa Ibn Uyaynah na tukaelekezwa kwa Al Humaidy, hivyo tukajifunza kutoka kwake Hadith zake kutoka kwa Ibn Uyaynah.’’

Ambapo baada ya kufariki Imam Sufyan Ibn Uyaynah basi Imam Al Humaidy akahamia kwa kwa Imam Muhamamd Al Shafii kwa ajili ya kujiendeleza kimasomo na hivyo kua na ukaribu Mkubwa sana na Imam Al Shafii kiasi ya kua ilikua kila anapoenda Imam Al Shafii basi na Imam Al Humaidi hua yuko pembeni yake.

Kwani amesema Muhammad Ibn Sahl kua: **‘Amesema Al Rabii Ibn Sulayman kua: ‘Amesema Al Shafii kua: ‘Sijawahi mimi kumuona rafiki yangu wa karibu miongoni mwa waliohifadhi Hadith kama Al Humaidi, kwani amehifadhi Hadith nyingi sana za Sufyan Ibn Uyaynah zifikazo 10,000. ’’’**

Hivyo safari zote zilizobakia za Imam Al Shafii baada ya kukutana na Imam Al Humaidi basi walikua wanaenda pamoja, hadi Imam Al Shafii alipohamia katika ardhi ya nchini Misri basi na Imam Al Humaidi pia alihamia pamoja nae na akaishi Misri hadi mwaka 204 Al Hijra pale Imam Al Shafii alipofariki Dunia basi Imam Al Humaidi ndio akarudi katika Mji wa Makkah ambapo aliishi katika maeneo hayo hadi kufariki kwake.

Imam Al Humaidy alikua na Ilm kubwa sana ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Al Bukhari, Imam Muhammad Ibn Ismaa'il Al-Bukhari, Imam Abu Dawud As-Sijistani, Imam Muhammad Ibn 'Isa At Tirmidhi, Imam Ibn Majah Al-Qazwini, Abu Abd Rahman Ahmad Ibn An-Nasa'i, Muhammad Ibn Yahya Adh-Dhuhliy, Imam Ya'quub Ibn Shaibah, Imam Ya'quub Ibn Sufyan, Imam Abu Hatim Muhammad Ibn Idriis Ar-Razi, Imam Abu Zur'ah 'Ubaid Allah Ibn 'Abdul Kariim Ar-Razi, Imam Muhammad Ibn 'Ali Ibn Maimuun Ar-Raqqiy, Imam Salamah Ibn Shabib, Imam Isma'il Al-Ashbahani, Imam Abul Azhar Ahmad Ibn Al Azhar An Nishapuri, Imam Bishr Ibn Musa Al-Asadi, Imam 'Ubaid Allah Ibn Fadhalah An Nasa'i, Imam Yusuf Ibn Musa Al Qaththan, na wengineo.

Ambapo alisema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: ‘**Al Humaidi yuko pamoja nasi na ni Imam wetu.’**

Imam Abu Hatim nae akasema: ‘**Mtu anaeaminika zaidi katika Hadith za Sufyan Ibn Uyaynah ni Al Humaidi, kwani ni mwenye ukaribu zaidi kwa Sufyan Ibn Uyaynah na ni Mwenye kuaminika.**’

Ambapo kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Is-haq Al Marwazi basi yeye amesema kua: ‘**Hakika mimi nimemsikia Is-haq Ibn Rahawayh akisema kua:** ‘**Maimamu wa wakati wetu ni Al Shafii, Al Humaidi na Abu Ubaid.**’’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Zakariyaa As-Saajiy anasema kua: ‘**Mimi nilimuuliza Abu Daud: ‘Hivi Jee ni nani marafiki wa karibu wa Al Shafii?’ nae akajibu: ‘Wa Mwanzo miongoni mwao ni Al Humaidi, Ahmad Ibn Hanbal na Al Buwaiti, ambae ni Yusuf** Ibn **Yahya Al Misri.’**

Ambapo amesema Abu Al Abbas Al Siraaj kua : ‘**Nimemsikia mimi Muhammad Ibn Isma'il Al Bukhari akisema kua: ‘Al Humaidi ni Imam katika fani ya Hadith.’**

Imam Ibn Hibban nae akasema: ‘**Humaidi ni Mtu wa Sunna na ni Mtu mwenye Hikma na Busara katika Dini.**’

Ambapo kwa Imam Al Hakim basi yeye anathibitisha kwa kusema kua: ‘**Al Bukhari ilikua kama akipata Hadith kutoka kwa Al Humaidi basi hua hatafuti kwa mtu mwengine yeyote.’**

Imam Al-Humaidi alisema kua: ‘**Sunnah kwa upande wetu sisi hua ni Imani ya mtu katika Kuamini Qadar, juu ya Mema na Maovu na Matamu na Machungu, na Imam inajumuisha ndani yake Maneno na Matendo na hua ni yenye kuweza kuzidi na pia kuweza kupungua, na Amali zote hua haziwezi kuhesabika bila ya kushikamanishwa na Nia juu yake amali hizo, na hivyo maneno na vitendo hua havikubaliki kutokana na nia isipokua vinaposhikamanishwa na Sunnah.**’

IMAM AL ANMATI

Imam Abu Al Qasim Uthman Ibn Said Ibn Bashar Al Anmati alizaliwa katika ardhi ya Baghdad nchini Iraq ambapo alijipatia Ilm ya Msingi ya Dini ya Kiislam kabla kuanza safari ya kusafiri katika ardhi tofauti na mwisho wake akamalizia katika maeneo ya ardhi ya Misri ambapo alisoma kwa Wanafunzi wakubwa wa Imam Muhammad Idris Al Shafii, ambao ni Imam Al Muzani na Imam Al Muradi ambao wote walikua ni Maimamu wenye Darja ya Juu katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii, kwani ni miongoni mwa *As-hab Al Wujuh.*

Tunapozungumzia *As-hab Al Wujuh* basi hua tunazungumzia wale Wanazuoni Wakuu wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambao ndio waliyoaeneza na kuyaendeleza Madhhab kuanzia kutoka katika kipindi cha Imam Al Shafii hadi kufikia katika kipindi cha *Hujjat Ul Islami* Imam Al Ghazali, ambapo baada ya hapo ikawa kuna hitajio kubwa la kuzijumuisha pamoja jitihada hizo za mitizamo ya Ilm ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii za Wanazuoni hao na kuziweka katika sehemu moja, hii ni kazi ambayo ilifanywa

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

na Imam Al Rafii na Imam An Nawawi ambao hawa ni wenye kujuliana kama *Shaykhani* yaani Mashaykh wawili wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii.

Hivyo Imam Al Anmati baada ya kumaliza masomo yake katika ardhi ya Misri na kuwiva basi akarudi katika Mji wa Baghdad na kua Mwanazuoni mkubwa sana na anaeaminika na hivyo kuanza kusomesha na kueneza Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii katika maeneo hayo ya ardhi ya Iraq, ambapo anasema Imam Al Subki kua : **'Imam Al Anmati ni sawa na Imam Abu Bakr Al Sibghi alieyaeneza Madhhab ya Imam Al Shafii katika ardhi ya Mji wa Nishapuri.'**

Katika kusomesha kwake katika Mji wa Badghad, Imam Al Anmati alitoa Wanafunzi wengi wa Ilm tofauti kutokana na ufaham wake kwani kuna aliowasomesha, Ilm ya Hadith, Ilm ya Tafsir, Ilm ya Fiqh n.k ambao nao walikua ni Wanazuoni wakubwa sana wakiwemo kina Imam Ibn Surayj, Imam Ibn Khira, Imam Abu Hafs Ibn Wakil, Imam Ibn Khuzaimah, Imam Abu Said Al Istakhari, Imam Ali Ibn Khayran na wengi wengineo.

Imam Al Subki anaendelea kusema kua: '**Ingawa kuhusiana na walio yaenezea Madhhab ya Imam Al Shafii basi katika Ardhi ya Baghdad ni Al Anmati, Katika Ardhi ya Nishapuri ni Imam Al Sibghi, katika ardhi ya Asbahan basi ni Said Ibn Marthad Al Isfahani ambae alikua pia ni Mwanafunzi wa Sufyan Ibn Uyaynah**'

'Lakini hata hivyo Al Sibghi alikua yuko juu Kiilm kuliko Al Anmati, ila kuna kutofautiana kwao kwa upande wa Wanafunzi wao kwani Wanafunzi wa Al Anmati ni wengi na wana athari kubwa zaidi katika kuyaboresha Madhhab ya Imam Al Shafii kuliko Wanafunzi wa Al Sibghi.'

Ambapo anasema Imam Al Khatib Al Baghdad kua: '**Amesema Ibn Al Manaadi kua: 'Al Anmati alikua ni mwenye kunufaisha sana''** na Imam Abu Is-haq Al Shirazi akasema kua: '**Al Anmati ndio sababu ya watu wa Iraq kua ni wenye kuifuatilia na kuihifadhi Fiqh ya Imam Al Shafii.**'

Imam Al Anmati alifariki katika mwezi wa Shawwal ya mwaka 288 Al Hijra.

IMAM IBN SIBGHI AL ZAFARANI 170 AH

Imam Abu Ali Al Hasan Ibn Muhammad Ibn Sibghi Al Baghdad Az Zafarani alizaliwa mnamo mwaka 170 Al Hijra katika maeneo ya ardhi ya Darb Az Zafarani ambayo yapo

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

baina ya Mji wa Baab Sair na Mji wa Karkh, na ndio asili ya kua ni mwenye kuitwa Imam Az Zafarani.

Imam Az Zafarani alikua ni Mwanazuoni mkubwa wa Ilm ya Hadith, Qur'an, Lugha na Fiqh kwani alisoma kutoka kwa Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Waki Ibn Jarrah, Imam Abu Mu'awiyah Adh-Dharir, Imam Isma'il Ibn Ulayya, Imam Ubaidah Ibn Hamid, Imam Abul Wahab ath-Thaqafi, Imam Muhammad Ibn Abi 'Adi, Imam Yazid Ibn Harun, Imam Hajjaj Ibn Muhammad, na wengineo ambapo Mwalimu wake mkuu alikua ni Imam Muhammad Idris Al Shafii, na hivyo alikua ni mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii baada ya kukutana nae wakati Imam Al Shafii alipohamia katika ardhi ya Baghdad.

Imam Az Zafarani alikua ni Mwanafunzi ambae alikua ni mwenye kusoma mbele ya Imam Al Shafii na kumsomea yale aliyoyaandika yeye kwa mkono wake kutoka kwa Imam Al Shafii, na vitabu vyengine ikiwemo Qur'an pia kwani Imam Al Shafii alikua anapenda kusikiliza namna anavyosoma kama anasema Imam Ahmad Ibn Muhammad Ibn Jarah kua: '**Mimi nilimsikia Al Hasan Az Zafarani akisema kua: 'Al Shafii aliniuliza Jee wewe ni Muarabu?' nami nikasema : 'La mimi si Muarabu bali nnatoka tu katika Kijiji cha Zafarani' ambapo nae akasema: 'Basi kwa hakika wewe ndie Chifu wa Kijiji hicho.''**

Na akasema Imam Ibn Hibban kua: '**Safari moja Ahmad Ibn Hanbal na Abu Thawr walikua wamehudhuria Darsa ya Imam Al Shafii, ambapo katika wakati huo Al Hasan Ibn Muhammad Az Zafarani akaaminishwa kuchukua wadhifa wa Imam Al Shafii katika Kisomo.**'

Ambapo Imam Ibn Adi anasema kua: '**Az Zafarani alikua ni mtu ambae mahiri wa Lugha na ufasaha wa kauli.**'

Na hivyo basi Imam Az Zafarani alikua ni Mtu mwenye kujiamini na kuaminika pia kama anavyosema Imam An Nasai kua: '**Az Zafarani ni mtu ambae maneno yake yanaaminika.**'

Imam Abu 'Ali Az-Za'farani alisomesha pia Wanazuoni wengi wakiwemo Imam Bukhari, Imam Abu Daud, Imam An Nasai, Imam Ibn Majah, Imam Ibn Khuzaymah, Imam At Tirmidhi, Imam Awanah Al Isfarini, Imam Abu Qasim Al Baghawi na wengineo.

Siku moja Imam Al Shafii wakati akiwa amekaa yeye na Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Abu Thawr na Imam Al Zafarani ambapo Imam Al Shafi'i alimpa Al Zafarani kitabu cha Al Risala awasomee, na baada ya kuwasomea basi Imam Al Shafii akamuuliza Imam Al Zafarani '**Jee wewe unatokana na kabila la Waarabu gani?'.**

Imam Al Zafarani akajibu : '**Mimi si Muarabu. Mimi natoka katika kijiji cha Zafaraniyyah**'. Imam Al Shafi'i '**Basi wewe ndie Kiongozi wa Kijiji hicho.**'

Anasema Imam Abu Is-haq Al Shirazi kua: **'Katika maeneo ya Ardhi ya Zafarani kuna Msikiti wa Al Shafi, na huo ndio Msikiti niliokua nikisoma katika Darb Al Zafarani.'**

Imam Az Zafarani alifariki katika mwezi wa Ramadhani ya mwaka 260 Al Hijra.

IMAM AL KARABISI

Imam Al Husayn Ibn Ali Ibn Yazid Al Karabisi alizaliwa katika ardhi ya nchi ya Iraq na alikua ni kijana aliejaaliwa ufahamu mkubwa sana na alisoma kwa Wanazuoni wengi sana wa Hadith akiwemo Imam Yazid Ibn Harun, Imam Maan Ibn Isa, Imam Ali Al Madini, Imam Al Shadhakuni, Imam Muhamamd Idris Al Shafii, na wengineo, ambapo mwanzao alikua ni mfuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa labidi baada ya kukutana na Imam A Shafii akabadili Madhhab na kua ni mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii. Anasema Imam Al Karabisi kua:

'Mimi nilikua nautumia Usiku wangu pamoja na Al Shafii, ambae alikua akitumia sehemu moja kati ya tatu za Usiku wake kwa ajili ya kusali, na sikuwahi kumuona akisoma aya zaidi ya 50, na alikua kila akifikia kwenye Aya inayozungumzia Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi nae alikua akiomba aingizwe yeye na Waumini wa Kiislam ndani ya Rehma hizo, na kila akisoma aya inayozunumzia Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi alikua akiomba yeye pamoja na Waislam waepushwe na adhabu hizo kiasi ya kua ilikua nimtu mwenye matumaini na khofu kwa pamoja '

Imam Al Karabisi alikua ni Mwanazuoni mwenye Ilm kubwa sana ya Qur'an, Hadith, Fiqh ya Imam Abu Hanifa na ya Imam Al Shafii na Ilm Al Kalam, ambapo Imam Adh Dhahabi anasema kua: '**Imam Al Karabisi alikua ni Bahari kubwa iliyojaa Ilm.**' Kwani Imam Al Karabisi aliandika vitabu vingi sana vya Ilm ya Fiqh na Usul pia.

Imam Al Karabisi alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa ambao ni Wanafunzi wa Imam Al Shafii katika ardhi ya Baghdad kama walivyokua kina Imam Abu Thawr, Imam Al Humaidi, n.k ambapo yeye Imam Al Karabisi alikua ni mtu mwenye Ilm kubwa sana zaid ya Imam Abu Thawr
Imam Al Karabisi alikua ni mwenye kusema kua; '**Wakati Mwanazuoni wa Hadith anaponukuu hadith basi hua ni mwenye kuhitajika kuonekana juu yake kwa athari ya hadithi hio nje yake na ndani yake Kiilm.**' Na akasemapia kua: '**Kuteleza kwa**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Mwanazuoni mmoja hua kuna madhara makubwa sana kwa Uislam, ambapo kuteleza kwa Wajinga 1000 hua hakuna madhara yeyote. ’

Ambapo kutokana n ucha Mungu wake basi ingawa Imam Al Karabisi alikua ni mtu ambae kamwe hakubali kutoa Fatwa yeyote ambayo ndani yake ina mtizamo unaokubalika kwa Ushahidi wa shahidi mmoja anapokula kiapo kwa mfano kama vile Muawwiyah Ibn Abu Sufyan *Radhi Allahu Anhu* alipokubali Ushahidi wa Umm Salama *Radhi Allahu Anha* peke yake kwa ajili ya Binamu yake, au kama vile alivyokubali Qadhi Al Shuraykh alipokubali ushahidi wa Abu Miljaz.

Kwani anasema Imam Al Karabisi kua: ‘**Kama kuna mtu ambae atasema kua: ‘Ushahidi wa mtu mmoja unakubalika, basi mtu huyo inambidi lazima aombe msamaha kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala*, ama vyenginevyo basi itabidi apewe adhabu ya kifo’**’

Lakini kwa upande mwengine basi Imam Al Karabisi ni Imam ambae mitizamo yake inanukuliwa na kukubalika katika Madhhab ya Imam Al Shafii kwa upande wa Tariqa ya Baghdad, kutokana na umaarufu wake wa Kiilm ambapo amesema Imam Abu Asim Al Abadi kua: ‘**Al Karabisi alikua ni mwneye ufahamu mkubwa sana wa kuhifadhi na alikua na ilm kubwa sana ya Fiqh na ni mwenye kufanya Ijtihad**’

Ambapo anasema Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kuhusiana nae kua: ‘**Imam Al Karabisi alikua ni mwenye utaalamu wa Ilm Al Kalam, Ilm ya Hadith, Ilm ya Fiqh na fani nyenginezo za Ilm, na amenukuliwa kwenye vitabu vingi sana na ni mwenye kuaminika.**’

Imam Al Karabisi alikua na uhusiano wa karibu sana na Imam Ahmad Ibn Hanbal kiurafiki, ambao hata hivyo urafiki huo uligeuka kua ni uadui pale Imam Al Karibisi alipoanza kuzama katika kusomea Ilm Al Kalam, na hivyo ikawa hakuna kufahamiana vizuri baina yao.

Imam Al Karabisi alifariki mnamo mwaka 248 Al Hijra.

IMAM AL RABII IBN AL MURADI 174 AH

Imam Abu Muhammad Al Rabi’ Ibn Sulayman Al Muradi alizaliwa mnamo mwaka 174 Al Hijra katika ardhi ya Mji wa Al Qahira katika nchi ya Misri. Imam Al Rabii alikua ni miongoni mwa Wanazuoni walioanza kusoma kwa Imam Muhamamd Idris Al Shafii tangu walipokua wadogo wakati Imam Al Shafii alipohamia nchini Misri, na alikua ni

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

miongoni wasaidizi wake na ni miongoni mwa watu wanaoandika na kusambaza Vitabu vya Imam Al Shafii, na hivyo alikua ni mwenye ukaribu sana na Imam Al Shafii na kua na Ilm kubwa sana, mbali ya kua alikua na tatizo la kutofahamu haraka.

Kwani anasema Imam Al Bayhaqi katika *Manaqib Al Imam Al Shafii* kua: '**Imam alikua na Mwanafunzi wake ambae alikua ni mzito wa kufahamu, Mwanafunzi huyu alikua akiitwa Al Rabii Ibn Sulayman. Kiasi ya kua iliku ainambidi Imam Al Shafii kurudia mara kadhaa darsa yake kwa Al Rabii Ibn Sulayman kwa kumuuliza: 'Rabii, Jee umefahamu?' na hapo Al Rabii hujibu: 'La bado sijafahamu.'**'

'**Hivyo Imam Al Shafii hua ni mwenye kurudia tena somo hilo huku akiwa amejawa na subra na kisha humuuliza tena: 'Jee umefahamu?' na Al Rabii hujibu : 'La Sijafahamu' kiasi ya kua Imam Al Shafii alikua akimuuliza Al Rabii mara 39 kama amefahamu ama la. Lakini hata hivyo Al Rabii hua bado hajafahamu, na kisha baada ya hapo Al Rabii hua ni mwenye kunyanyuka kutoka kwenye Darsa hio na kuondoka taratibu kutokana na kuona aibu kua amekua ni mwenye kumvunja moyo Mwalimu wake kutokana na kutofanikiwa kufahamu kitu chochote.**'

Na baada ya Darsa hio basi Imam Al Shafii hua ni mwenye kumtafuta Al Rabii na kisha anapomuona basi Imam Al Shafii humwambia Al Rabii: 'Al Rabii twende zetu nyumbani', na hivyo Imam Al Rabii humfuata Imam Al Shafii hadi nyumbani kwake, na kisha humkaribisha na kuanza kumsomesha tena upya kwa utulivu zaidi, lakini hata hivyo Al Rabii Ibn Sulayman hua si mwenye kufahamu pia.

Baada ya kupata matoke hayo basi Imam Al Shafii akamwambia Al Rabii: 'Ewe Mwanafunzi wangu, hakika hadi hapa mimi kwa upande wangu nimejitahidi kutumia jitihada zangu zote kukusomesha, hivyo kama hufahamu, basi la kufanya ni kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akuridhie ili akumwagie Ilm ndani ya ufahamu wako, kwani mimi kazi yangu ni kukupandikizia Ilm, ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie mwenye jukumu la kukupa Ilm, hivyo kama Ilm nnayokupa mimi ni sawa na kukulisha kwa kijiko cha kulia basi bila ya shaka mimi nitaendelea kukulisha wewe.'

Ambapo baada ya kuambiwa maneno haya basi Al Rabii akaanza kumuomba *Allah Subhana wa Ta'ala* kwa ikhlasi kua amjaalie kua ni mwenye Ilm, huku yeye mwenyewe akiwa ni mwenye kuthibitisha hamu yake ya kutaka kujibiwa maombi yake kwa kuendelea kusoma kwa jitihada na Ikhlasi bila ya kuvunjika Moyo.

Ambapo anasema Imam Al Rabii Ibn Sulayman kua: **'Al Shafii alikua ni mwenye kuugawa Usiku wake katika sehemu tatu, sehemu ya kwanza alikua ni mwenye**

kuandika Ilm yake aliyokua nayo, kisha alikua ni mwenye kusali katika sehemu ya pili na kisha alikua ni mwenye kulala katika sehemu ya tatu na ya mwisho.'

Ambapo matokeo yake Imam Al Rabii Ibn Sulayman akawa ni miongoni mwa Wanafunzi bora wa Imam Al Shafii na wanaotegemewa kwa Mitizamo ya Fatwa za *Qawl Jadid* za Madhhab ya Imam Al Shafii na bila ya shaka haishangazi kuona kua Imam An Nawawi amemnukuu mara nyingi sana katika kitabu chake cha *Rawdhah Talibin na Sharh Al Muhadhdhab*. Ambapo Imam Al Rabii ndie alienukuu mtizamo wa Imam Al Shafii kuhusiana na usemao kua: ***'Kuiimba Qur'an ni Makruh'***

Kwani Imam Al Rabii ni Imam anaeaminika sana katika Hadith zake na nukuu zake kiasi ya kua inapotokea kuna kupingana baina ya mitizamo ya Maimamu wengine ambao ni Wanafunzi wa Imam Al Shafii, basi mtizamo unaopewa kipaumbele zaidi miongoni na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Kwani ingawa ukweli ni kua Mitizamo na Nukuu za Imam Al Muzani ambae ni kaka yake Imam Al Rabii wa Kunyonya ina nguvu na kuaminika sana katika Madhhab ya Imam Al Shafii lakini nayo pia inapokua imegongana na kupingana na Mitizamo ya Imam Al Rabii basi Mitizamo ya Imam Al Muzani hua ni yenye kuwekwa pembeni na kutumika mitizamo ya Imam Al Rabii Ibn Sulayman.

Na akasema tena: '**Mimi nilienda kwa Imam Al Shafii wakati akiwa anaumwa na nikamwambia: 'Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akupe nguvu dhidi ya maradhi yako' ambapo nae akasema: 'Kama ikiwa yeye ndie alienipa mimi maradhi basi ndie yeye pia atakaeichukua roho yangu' nami nikasema: 'Wa Allahi sikutakii lolote lile isipokua Jema' ambapo Imam Al Shafii nae akasema: 'Bila ya shaki mimi najua kua wewe hata kama utanikemea mimi basi utakua ni mwenye kufanya hivyo kutokana na kunitakia mema**''

Imam Al Rabii hakusoma kwa Imam Al Shafii tu lakini alisoma pia kwa Imam Abu Muhammad 'Abd Allah Ibn Wahb Al Fihri Al Misri, Imam Bishr Ibn Bakr At-Tunisi, Imam Ayyub Ibn Suwayd Ar-Ramli, Imam Muhammad Ibn Idris Al-Muthlabi, Imam Yahya Ibn Asad, Imam Bukhari, Imam Hasan Ibn Muhammad Az Zafarani, Imam Al Karabisi, Imam Abu Thawr, Imam Al Rahawayh nk

Imam Muhamamd Idris Al Shafii alikua akiipenda sana sauti ya Imam Al Rabii kwani alikua na sauti nzuri sana na ndie aliekua Muadhini wa Msikiti wa Ijumaa wa Amr Ibn Al As *Radhi Allahu Anhu* uliopo katika maeneo ya *Fustat M*jini Al Qahira, ambapo siku moja Imam Al Shafii alimwambia Imam Al Rabii kua: '***Mashaa-Allah*, una sauti ninayovutia vizuri sana, na kwa hakika kama mimi ningekua nnauwezo basi**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ningekulisha Ilm yangu yote kwa kijiko kama vile ambavyo Mama anavyomlisha mtoto wake mchanga kwa Kijiko.’

Imam Al Rabii alisomesha pia Wanazuoni wengie wakubwa wakubwa ambapo miongoni mwao ni pamoja na Imam Abu Daud, Imam an-Nasa'i, Imam Ibn Majah, Imam Abu Zur'ah Ar Razi, Imam At-Tirmidhi, Imam Ibn Al Mundhir, Imam Abu Is-haq Al Marwazi, Imam Abu Hatim Ar Razi, Imam Abd Rahman Ibn Abu Hatim Ar Razi, Imam Zakaria As Saji, Imam Abu Ja'far at-Tahawi, Imam Abu Bakr Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Ziyad An-Nishapuri, Imam Al-Hasan Ibn Habib Al Hashairi, Imam Abu Al Abbas Al Asham, Imam Abu Al Fawaris As Sandi, n.k

Ambapo anasema Imam Al Rabii kua mimi nimemsikia Imam Al Shafii akipenda kurudia kusema mara kwa mara: ‘**Ilm hua sio ile inayosomwa bali hua ni ile inayonufaisha.**’

Imam Al Rabii alifariki mnamo mwaka 270 Al Hijra.

IMAM AL MUZANI 175 AH

Imam Isma’il Ibn Yahya Ibn Isma’il Ibn ‘Amr Ibn Ishaq Ibrahim Al Muzani Al Misri alizaliwa katika maeneo ya Mji wa Al Qahira mnamo mwaka 175 Al Hijr mwaka ambao ndio aliofariki Imam Al Layth Ibn Saad ambapo jina la Muzani linatokana na jina la Mama yake ambae alikua akiitwa Muzaynah Bint Kalb Ibn Wabirah ambae alikua ni Mama wa Kabila maarufu lililokua nchini Misri.

Imam Al Muzani alikua ni mwenye kuhudhuria darsa ya Imam Muhamamd Idris Al Shafii tangu alipokua mtoto mdogo yeye pamoja Dada yake ambae nae pia alikua na ilm kubwa sana ya Madhhab ya Imam Al Shafii ambapo Imam Al Muzani, ambapo kama tulivyoona hapo kabla kua Imam Al Rabii Ibn Sulayman alikua ni kaka yake wa kunyonya ziwa moja. Ambapo dada yake Imam Al Muzani alikua ni Mama yake Imam At Tahawi ambae ni Mwanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa aliendika kitabu cha *Aqidat Tahawwiyah.*

Imam Al Muzani alisoma moja kwa moja kutoka kwa Imam Muhammd Idris Al Shafii kama ilivyokua kwa upande wa Imam Al Rabii Ibn Sulayman. Ambapo anasema Imam Ibn Al Jawzi kua: ‘**Al Muzani alikua ni rafiki yake Al Shafii, na alikua ni Mwanafiqh Mahiri, Thiqah na mcha Mungu na ni mbora miongoni mwa watu na alikua kwenye mstari ulionyooka.**’

Imam Ibn Khallikan alisema kuhusiana nae kua: **‘Al Muzani alikua ni Imam wa wafuasi wa Shafii na alikua ni mwenye kujua zaidi kuhusiana na maana**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

anazozikusudia Al Shafii, njia anazozitumia Al Shafii, Fatwa zake na kile kilichoandikwa nae.'

Kutokana na uwezo wake mkuwa Kiilm basi Imam Al Muzani alikua akijulikana kwa darja ya *Al Imam, Al Allamah, Al Faqih Al Millah* na pia *Alam Al Zahid* kwani Imam Al Shafii alikua akisema kuhusiana na Imam Al Muzani kua: '**Al Muzani ndie mshika kibendera wa Madhhab yangu.**'

Imam Al Muzani alikua ni mwandishi wa Imam Al Shafii pia, na hivyo baada ya kufariki Imam Al Shafii basi nae akaandika kitabu chake cha Fiqh kinachoitwa *Mukhtasar Al Muzani* ambacho amesema Imam Muhammad Ibn Is-haq kua; **'Nimemsikia mimi Al Muzani akisema kua: 'Nimekiandika hiki kitabu kwa mda wa miaka 20, na nilikiandika mara 3 na kisha nikakibadilisha.'**'

Ambapo Imam Al Muzani mwenyewe basi alisema kua: **'Kama Al Shafii angekiwahi kitabu hiki cha Al Mukhtasar basi angekisiliza wakati nikimsomea.**'
Imam Abu Al Abbas Ibn Surayj alisema: '***Mukhtasar Al Muzani* ndio chanzo cha Vitabu vya Madhahab ya Imam Al Shafii, na wamevipangilia vitabu vyao katika mpangilio wa mada maalumu ambao ni wenye maelezo na ufafanuzi wa Madhhab juu ya kila Mada husika.'**

Mbali ya *Mukhtasar Al Muzani* lakini pia Imam Al Muzani aliandika vitabu kadhaa ikiwemo Ufafanuzi wa *Kitab Al Umm* cha Imam Al Shafii, kitabu cha Sharh Al Sunnah, Al Jamii Al Kabir, Al Saghir, Al Targhib fi Al Ilm, Al Masail Al Mutabarah, Al Wathaiq n.k Ambapo ilikua ni kawaida ya Imam Al Muzani kua ni mwenye kusali Rakaa mbili kila baada ya kumaliza kuandika Kitabu.

Imam Al Muzani alikua pia ni mwenye Ujuzi mkubwa wa kufanya mahojiano ya hoja na alikua anapenda kuhojiana na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa katika mambo mbali mbali, ambapo Imam Al Shafii mwenye alisema kuhusiana nae kua: **'Kama Al Muzani angekua ni mwenye kuhojiana kwa hoja na Ibilisi basi angemshinda Ibilisi.'**

Ambapo anasema Imam Ibn Abd Al Barr kua: **'Al Muzani alikua ni Mwanafiqh, Mwanazuoni mwenye uwezo mkubwa sana wa kufanya mahojiano ya hoja miongoni mwa Wanafunzi wa Al Shafii, alikua na uwezo wa kufahamu mambo mengi sana kwa mtizamo wa nguvu ya hoja na ni mwenye kuelezea wazi na kwa kina juu ya kila kitu, alikua yuko juu sana katika Madhhab ya Imam Al Shafii katika ufahamu wake, uhifadhi wake, mitizamo yake na umakini wake, hakuna aliemfikia Darja yake, hata ufahamu wake ni uliojaza mambo mazito tofauti na**

vitabu vyake vimesambaa katika maeneo mbali mbali ya Ardhi kuanzia Mashariki hadi Magharibi, alikua ni Mcha Mungu mwenye Subra na alieachana na Dunia.’

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Yunus basi yeye anasema kua: **‘Al Muzani alikua ni rafiki yake Al Shafii, alikua ni Mcha Mungu, Thiqah katika Hadith na hakuna Mwanazuoni mwenye ujuzi wa Fiqh alietofautiana nae Ilm Yake Juu yake alikua ni mwenye kuachana na Dunia yake, alikua ni kiumbe bora wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* na sifa zake nzuri ni nyingi sana. ’**

Ambapo anasema Amr Ibn Uthman Al Makki kua: **‘Sijawahi mimi kuona mtu mwengine zaidi katika kufanya Ibada kwa wingi miongoni mwa niliokutana nao katika Ardhi ya Makkah, kati ya wale wenyeji na wageni wenye kutembelea Mji huo, na wala wale wenye kutoka kwenye Ardhi ya Sham na wenye kuishi ndani yake na wala watu wa Alexandria wenye kujitahidi zaidi kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kama Al Muzani.’**

‘Na wala sijawahi kumuona mwenye kudumu ndani ya aina hiyo ya jithada ya kiibada zaidi yake, na sijawahi kuona yeyote mwenye Ilm kubwa na ilm juu ya wenye Ilm zaidi yake, na alikua nimtu mkali sana kwa nafsi yake na mtu mlaini sana kwa Nafsi za wenzake, ambapo yeye mwenyewe alikua akisema kua: ‘Mimi ni mfano wa Tabia za Al Shafii mwenyewe.’’

Kwani Imam Al Muzani alikua ni mwenye kudumu katika Sala ya jamaa na kama akiikosa basi alikua akiisali sala yake hio moja peke yake kwa kuirudia mara 25 na alikua akipenda kukosha Maiti kwani alikua anasema kua: **‘Nnakosha Maiti kwa sababu Moyo wangu upate kusafika.’**

Ambapo Imam Abu Said Ibn Sukkari alisema kua: **‘Nilikutana na Al Muzani na sijawahi kuonana na mtu mwengine yeyote yule mwenye kufanya Ibada kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kama Al Muzani na wala sijamuona mtu mwenye umakini kwenye Fiqh kama yeye.**’

Imam Al Abbadi akasema: ‘**Al Muzani alikua ni Mcha Mungu, mwenye kuachana na Dunia, mwenye uzuri wa kauli na muongozo, na mwenye makusudio na malengo katika vitendo vyake.**’

Ambapo kwa upande wa Imam Al Subki amesema kua: **‘Al Muzani ni Imam mwenye Hikma na Busara, Muungaji mkono wa Madhhab, ni Mlima wa Ilm na mwenye mamlaka katika Mahojiano ya nguvu ya Hoja na mcha Mungu alieachana na Dunia, alikua akitosheka na kidogo kutoka ndani ya Dunia hii.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo Imam Al Asnawi anasema kua: **'Imam Al Muzani ni Imam Mcha Mungu, mwenye kuitikia wito wa Mola wake, mwenye kutosheka na kidogo kilichomo Duniani na ni mwenye kutukuzwa miongoni mwa Mashafii.'**

Na Imam Abu 'Asim alisema kua: '**Al Muzani alikua si mwenye kukubali kutia udhu kwenye mtaa wa Ibn Tulun wala kunywa maji kutoka kwenye majagi yake, kwa sababu ya udongo uliokua ukitayarishwa majagi hayo na moto uliokua ukitumika katika kuuoka moto udongo huo ulikua hautoharishi udongo huo, na Wanazuoni kutoka katika sehemu tofauti walikua wanakuja kwa Imam Al Muzani kutoka Khurasani, Iraq na Sham. Ambapo baada ya kuutumikia Uislam na Madhhab ya Mwalimu wake kipenzi Al Shafii basi Al Muzani alirudi kwa Mola wake mnamo mwezi wa Ramadhan ya mwaka 264 Al Hijra.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Khallikan basi yeye anasema kua: **'Imam Al Muzani alifariki siku 6 kabla ya kuwadia kwa mwezi wa Ramadhani wa mwaka 264 Al Hijra na alizikwa katika Makaburi ya Al Qarafat Al Sughra alipozikwa Imam Al Shafii karibu na *Safhul Maqtan.'***

Kutokana na ukubwa wa l'lm yake basi Imam Al Muzani alikua na darja ya Mujtahid na hivyo alikua ni mwenye kua na baadhi ya Mitizamo ambayo ilikua ikitofautiana na Imam Al Shafii katika baadhi ya masuala ya Fiqh ambapo miongoni mwao ni yafuatayo:

1. **Kua na Shaka kuhusiana na utohara wa Maji safi au Mavazi:**

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Kama ikiwa mtu ana debe mbili za maji ambapo moja ni la maji safi na jengine ni la maji yasiyokua safi, na mtu hana uhakika ni lipi ambalo ndio lenye maji yasiyokua tohara, unaokubalika ni ule usemao kua, Hairuhusiki kutumia maji yeyote kati ya haya hadi pale mtu atakapokua na uhakika lipi ni safi na lipi sio safi na huu ndio mtizamo uliopo kwenye *Rawdhat At Talibin.* Ambapo hii pia halkadhalika kwa upande wa nguo au kile kitu kinachotiliwa shaka.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Kama ikiwa mtu ana debe mbili za maji ambapo moja ni la maji safi na jengine ni la maji yasiyokua safi, na mtu hana uhakika ni lipi ambalo ndio lenye maji yasiyokua tohara, basi hua hakuna haja ya kujaribu kuhakikisha lipi lina maji Tohara na lipi lina maji yasiyokua Tohara, bali mtu husika anatakiwa afanye Tayamam na kisha asali, na wala haytokua na haja ya kuirudia Sala hio, na kuhusiana na nguo basi mtu anatakiwa asali na nguo moja kwanza kisha asalie nguo nyengine bila ya kujaribu kuhakikisha ipi ni nguo tohara, ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Abu Thawr.

2. Kujitoharisha baada ya kujisaidia:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Ni wajibu kujitoharisha sehemu za Siri baada ya kujisaidia *(Rawdhat At Talibin)*

Mtizamo wa Imam Al-Muzani.
Sio lazima kujitoharisha kama vile ambavyo ilivyokua sio lazima kuondoa dalili zilizobakia pale mtu anapojitoharisha kwa kutumia Jiwe baada ya kumaliza kujisaidia. (*al-Najm al-Wahhaj*).

3. Kukosha Kichwa katika wakati wa kutia Udhu:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Ni wajibu kukosha sehemu ya kichwa au sehemu ya nywele hata japo unywele mmoja, muhimu ni kua kupangusa kuwe kuko ndani ya mipaka ya kichwa, lakini inapendekezwa zaid kupaka maji kichwa kizima. (*Al Mughni Al Muhtaj* na na *Rawdhat Al Talibin*).

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Ni wajibu kuosha kichwa kizima katika wakati wa kutia Udhu, ambapo huu ni mtizamo wa Imam Malik na Imam Ahmad. Ambapo Imam Al Muzani anasema kua huu pia ndio mtizamo wa Imam Al Shafii katika *Al Mandhur*.

4. Kukosha viungo vya mwili katika Udhu na katika Kukoga Janaba:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni.
Inapendekezwa kupangusa kiungu cha Mwili baada ya kukikosha kama kua na tahadhari, kwa ajili ya kuhakikisha ukamilifu wa ukoshaji, na kujilinda na utofauti wa mtizamo dhidi ya wale ambao wanaosema kua kukosha kiungi ni lazima. *(Al Ghurara Bahiyyah)*

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Ni wajibu kukipangusa kiungo cha mwili katika kutia udhu na kukoga janaba, ambapo huu pia ndi mtizamo wa Imam Malik.

5. Kuchana Ndevu nyingi kwa kuingiza vidole ndani yake katika kutia Udhu:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Kuchana Ndevu nyingi hua ni miongoni mwa mambo yanayopendekezwa katika kutia udhu.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Kuchana Ndevu nyingi hua ni Wajib *(Al Najm Al Wahhaj)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

6. Kutia Udhu kwa Mpangilio wake:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Kutia Udhu kwa mpangilio wake katika kukosha viungo hua ni Nguzo ya Udhu.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Sio Wajibu kutia Udhu kwa mpangilio kwani mpangilio wa udhu hua si Nguzo ya udhu, ambao huu pia ndio mtizamo wa Imam Ibn Al Mundhir, Imam Nasr Ad Din Al Maqdisi, Imam Al Badiji na wengi miongoni mwa Wanazuoni kulingana na Mtizamo wa Imam Al Baghawi

7. Jee Tayammam hua Inaondoa hali ya Janaba, Hedhi, Nifasi n.k?:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Tayammam haiondoi hali ya Janaba, Hedhi, Nifasi, nk.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Tayammum inaondoa hali ya Janaba, Hedhi, Nifasi n.k *(Al Najm al Wahhaj)*

8. **Jee inaruhusika kusali zaidi ya Sala moja ya Fardhi kwa kutumia udhu wa Tayamam ya mara moja?:**

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Hairuhusiki kwa Mtukusali zaidi ya Sala moja ya Fardhi kwa kutumia Tayamam moja.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Inaruhusika kusali Sala za Fardhi unazotaka kwa kutumia Tayamam hiohio moja, na hii ni kwa sababu Tayamum hua inaondoa hali ya Janaba, Hedhi, Nifasi, hivyo inaruhusika kwa mtu kusali Sala kadhaa za Fardh kutokana na Tayamam na huo pia ndio mtizamo wa Imam Ibn Al Mundhir na pia Imam Al Ruwyani. *(Al Najm al Wahhaj)*

9. Kufanya Tayamam Kabla ya Wakati wa Sala:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Mtu anaweza kufanya Tayamam pale mda wa Sala unapoingia.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Mtu anaweza kufanya Tayamam hata kabla ya kuingia wakati wa Sala.

10. Kusali bila ya kua na Udhu pale mtu anapokosa Maji na Udongo pia wa

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

kutayamam:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Mtu anaweza kusali baada ya kukosa maji au udongo wa kutayamam kwa kutumia njia ya kutayamam kukavu bila ya mchanga hii ni kulingana na *Al Qawl Al Jaddid*.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Kama hakuna uwezekano wa kupata maji wala mchanga au udongo basi mtu hua inambidi asali na hakuna ulazima wa kuirudia Sala hio, ambapo huu ni mtizamo wa *Al Qawl Al Qadim* ambao pia ndio mtizamo wa Imam An Nawawi katika Sharh Al Muhadhhab.

11.Urefu wa Mda wa kipindi cha Damu ya Nifas:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Ufupi wa kipindi cha Damu ya Nifasi kwa kawaida hua ni siku 40 na urefu wake hua ni siku 60.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Ufupi wa kipindi cha Damu ya Nifasi ni siku 4 na urefu wake ni siku 40.

12.Mwanzo wa kuingia Sala ya Isha:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Isha huingia baada ya kutoweka kwa mwangaza mwekundu wa kuzama Jua *(Rawdhat Talibin)*

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Sala ya Isha hua inaingia wakati unapotoweka weupe wa kuzama Jua ambao huu pia hua ni mtizamo wa Imam Abu Hanifa.

13. Idadi ya rakaa za Witr:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Wingi wa Idadi wa Rakaa za Witr huanzia na Rakaa moja, ambapo Qadhi Abu Tayyib anasema kua inakirihisha kusali Rakaa moja ya Witri peke yake.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Idadi ndogo kabisa ya Sala ya Witr ni Rakaa tatu, na hii ni kutokana na kauli ya Imam Muhamamd Idris Al Shafii.

14. Awra au Utupu wa Mwanamke aliekua Huru:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Awra au Utupu wa Mwanamke aliekua huru inajumuisha Mwili wake wote isipokua Uso na Mikono.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Awra ya Mwanamke aliekua huru ni Mwili mzima isipokua Uso, Mikono na Miguu.

15. Kuchelewesha Kulipa Ramadhani hadi Ramadhani ya mwaka ujao:

Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.
Kuchelewesha kulipa Ramadhani hadi Ramadhani ya mwaka unaofuatia humuwajibisha mtu husika kulipa kila siku ya ya kufunga na Kibaba kimoja cha chakula.

Mtizamo wa Imam Al Muzani.
Kuchelewesha kulipa Funga za Ramadhani humuwajibisha Mtu kulipa Ramadhani tu bila ya kutoa Kibaba cha chakula.

Ambapo anasema Shaykh Abd Allah Ba Sudan kua: '**Baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii hua wanatumia mitizamo inayojigemea ambayo hua ni tofauti na mitizamo ya Madhhab ya Imam Al Shafii, ambapo hii hua ni mitizamo ambayo ya kibinafsi pale inapokua kuna uzito katika Mtizamo unaokubalika wa Madhhab, ambapo Mitizamo hii ni yenye kujulikana na ipo mingi sana, na hivyo mitizamo hii hua haiwi ni kutoka nje ya Madhhab kwani mitizamo hii hua inategemeana na *Istinbat, Qiyas na Ikhtiyar* zinazolingana na Kanuni za Madhhab ya Imam Al Shafii, na hivyo pia Mwanazuoni anakua na uwezo wa kutumia Mtizamo wa *Al Qawl Al Jadid au Al Qawl Al Qadim* ya Madhhab ya Imam Al Shafii.'**

IMAM AD DARIMI 181 AH

Imam Abd Allah Ibn Abd Rahman Ibn Fadhl Ibn Abd Rahman Ibn Abd Samad At Tamimi Al Samarkandi Ad Darimi ambae ni maarufu kama Imam Ad Darimi alizaliwa katika maeneo ya Darimi nchini Uzbekistan mnamo mwaka 181 Al Hijra.

Imam Ad Darimi alianza kusoma katika ardhi ya Darimi nchini Uzbeksitan ambapo baadae alifunga safari na kuelekea katika maeneo ya Khurasan, Bagdad, Kuffah, Hijaz, Iraq, Sham na Misri na kusoma kwa Wanazuoni mbali mbali wakiwemo Imam Ibn Uwez, Imam Musa Ibn Ismail Al Tabuzaki, Imam Ahmad Ibn Yunus, Imam Nuaym Ibn

Hamamd, Imam Abd ul Ghafar, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Ali Ibn Al Madini, Imam Yahya Ibn Main, n.k.

Imam Ad Darimi alisoma Ilm ya Fiqh kwa Imam Al Buwayti na hivyo alikua ni mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, na alisoma pia Ilm ya Lugha kwa Imam Abu Abd Allah Ibn Al Arabi.

Ambapo Miongoni mwa Wanafunzi aliowasomesha Imam Ad Darimi ni pamoja na Imam Ahmad Ibn Muhammad Ibn Abd Taraifi, Imam Abu Al Abbas Ahmad Ibn Azhar, Imam Muhammad Ibn Al Hassan Ibn Isa, Imam Bukhari, Imam Muslim, Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhii, Imam Hasan Ibn Shabbah Al Bazzar, Imam Abu Zarah, Imam Abd Allah Ibn Ahmad Ibn Hanbal, n.k

Yaqub Ibn Al Qarrab anasema kua: **'Hakika mimi sijawahi kumuona mtu yeyote kama Uthman Ibn Said, na wala yeye mwenye hajawahi kuona mtu yeyote yama alivyo yeye mwenyewe, kwani alisoma Lugha kwa Ibn Arabi, Fiqh kwa Abu Yaqub Al Buwayti, Hadith kwa Yahya Ibn Main na Ali Ibn Al Madini na alikua ni mwenye mafanikio makubwa sana kwenye fani za Ilm hizi, *Allah Subhanah wa Ta'ala* amuingize kwenye Rehma zake'**

Anasema Imam Ibn Hibban kuhusiana nae kua: '**Imam Ad Darimi ni Imam wa Dunia aliesoma kwa Abu Al Walid kutoka kwa watu wa Iraq.'**
Ambapo anasema Imam Abu Zurah Al Razi kua: **'Imam Ad Darimi amewacha zawadi kubwa iliyobora ya maandishi.'**

Na Abu Al Fadhl Al Jarudi anasema kua: **'Imam Ad Darimi alikua ni Imam anaefuatwa katika wakati wa Kipindi cha uhai wake na baada ya kufariki kwake'**

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Daud basi yeye amaesema kua: **'Sisi tumejifunza Hadith kutoka kwake.'**

Na Imam Abu Hamid Al Amash amesema kua: **'Sijawahi kuona Mtu yeyote yule kama Uthman Ibn Said, Muhammad Ibn Yahya na Yaqub Ibn Sufyan miongoni mwa Wanahadith'**

Imam Adh Dhahabi basi nae anasema kua: **'Imam Ad Darimi ni Mwanazuoni mkubwa sana, Al Hafidh, Msahishaji na amesoma Hadith kutoka kwa Ahmad na Yahya Ibn Main. Yeye ni mlinzi wa Sunnah na mwenye uzoefu mkubwa sana katika mahojiano ya kutumia nguvu ya hoja.'**

Na bila ya shaka hili halishangazi kwani kama tulivyoona kua Imam Ad Darimi alisoma kwa Imam Al Buwayti ambae alikua ni mkali sana wa mahojiano ya kutumia nguvu ya

hoja na ndio maana Imam Adh Dhahabi akasema: '**Katika macho ya *Ahl ul Bidaa,* basi Uthman Ad Darimi ni alikua ni gogo kwani ni yeye ndie alienyenyuka na kukabiliana dhidi ya Muhamamd Ibn Karram ambae ndie Mwanzilishi wa Madhhab ya Karramiyyah na ndie aliemfukuza kutoka katika maeneo ya Hirat.'**

Imam Taqi Ad Din Al Subki basi yeye anasema kua: '**Ad Darimi alisafiri sana kwa ajili ya kutafuta Ilm na alikutana na Wanazuoni wakubwa wakubwa, na alikua ni mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa waliotajwa na Al Abbadi katika Tabaqat yake kwa kusema kua: 'Alikua ni Imam wa Fiqh na Hadith.**''

Imam Ibn Abi Hatim Ibn Hibban akasema kua: '**Imam Ad Darimi alikua nini Al Hafidh anaeaminika, Mcha Mungu na Mwenye Ilm kubwa ya Dini, alihifadhi Vitabu vingi na alikua ni mwenye kuikhuisha Sunnah na ni mwenye kupingana na wenye kuchukia Sunnah.'**

Imam Ad Darimi aliandika vitabu vingi sana ikiwemo vya *Musnad, Tafsir na Jami'i.* ambapo tunapozungumzia kuhusiana na *Musnad* basi hua tunazungumzia kuhusiana na Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* ambavyo vinavyoandikwa kuainisha Hadith ambazo zilizopangwa kwa mpangilio maalum kulingana na mada husika Kifiqh, na wala si kulingana na *Sanad* ya mapokezi ya Hadith husika kama wanavyofikiria wengi kutokana na kunasibisha maana ya Jina la *Musnad*, hivyo hadith zinazokuwemo kwenye *Sunan* hua ni *Musnad* pale inapokua ni zenye msingi wake yaani hali ya *Musnadatun.*

Na ndio maana kwa upande wa Kitabu cha Sunan Ad Darimi ambacho ni miongoni mwa Vitabu bora vya Hadith basi akasema Imam Ibn Salah juu yake kua: '***Sunan Ad Darimi* ni *Musnad*'** na Imam Mughkathaya basi amesema kua: '**Wanazuoni wanasema kua *Musnad Ad Darimi* ni Kitabu cha *Hadith Sahih*'** na ndio maana kuna baadhi ya Wanazuoni wakapendekeza kua kitabu cha *Sunan Ad Darimi* kua ni kitabu kinachostahiki kuingizwa kwenye Vitabu ambavyo ni Nguzo Kuu za vitabu vya Hadith.

Na hii ni kwa sababu Wapokezi wake Hadith zake kitabu hicho ni wenye kukubalika na hivyo kua na nguvu zaid na wengi zaida na Sanad zake ni Nzuri na pia kina hadith kidogo sana zenye hali ya kua ni *Munkar*. Ambapo kitabu cha Sunan Ad Darimi kinajumuisha Vitabu viwili vyenye milango 23 ambapo ndani yake mna hadith 3503.

Imam Ad Darimi alifariki mnamo mwezi wa *Dhul Hijja* katika mwaka 280 *Al Hijra.*

SHAYKHA FATIMA AL NISHAPURI

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Fatima Al Nishapuri alikua ni Mwalimu wa Imam Bayazid Al Bistami na pia Mwanafunzi wake, na alikua ni mwanamke mweye Ilm kubwa sana, mwenye Taqwa na pia alijaaliwa kua na Mali nyingi sana, ambazo zolitokana na upande wa Baba yake aliekua ni mtu tajiri katika maeneo ya ardhi ya Balk.

Fatima Al Nishapuri alisoma kwa Wanazuoni tofauti na alikua na Ilm kubwa ya Tafsir ya Quran, Hadith na Tasawwuf aliekua akiishi katika Mji wa Nishapuri. Fatima Al Nishapuri alikua ni Mwalimu wa Imam Abu Hamid Ahmad Ibn Khidruyah, Abu Hafs Al Haddad, Imam Dhun Nun Al Misri, n.k

Kwani lisema Imam Dhu Nun Al Misri kua: **'Fatima Al Nishapuri ni Walii wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ni Mwalimu wangu'**

Imam Dhu Nun Al Misri aliulizwa safari moja: **'Jee kwa mtizamo wako ni nani aliekua juu katika Ilm ya Tasawwuf?'** ambapo nae akajibu: **'Kuna Mwanamke anaitwa Fatima Al Nishapuri ambae huyu ufahamu wake ni wenye kuzama kwenye maana ya ndani kabisa ya Aya za Qur'an jambo ambalo hua ni lenye kumfanya kua ni mwenye kushangaza sana'**

Safari moja walipokutana katika Mji wa Jerusalem Fatima Al Nishapuri alimwambia Dhu Nun Al Misri kua: **'Fuatilia vitendo vyako uwe ni mwenye kuvifanya kwa Ikhasi na mwenye kupingana na Nafsi yako.**'

Fatima Al Nishapuri alipokua tayari kuolewa alimuomba Imam Abu Hamid Ahmad Ibn Khidruyah, kua aende kwa baba yake akampose ili amuoe, ambapo mwanzoni Imam Ahmad Ibn Khidruyah alikataa lakini baadae akabadilisha mtizamo wake huo, na akaamua kumposa Fatima Al Nishapuri na ilipokubaliwa posa hio wakaoana.

Katika wakati wa kipindi cha Uhai wao Imam Yahya Ibn Muadh Al Razi alitembelea maeneo ya Nishapuri alipokua akirudi kutoka katika Mji wa Balkh kuelekea katika Mji wa Ray na hivyo Imam Ahmad Ibn Khidruyah akamualika Nyumbani kwake, lakini kabla ya kumualika kwake basi Imam Ahmad akamwambia Fatima Al Nishapuri: **'Jee akija Nyumbani Yahya Ibn Muadhi tutamtayarishia nini?**'

Ambapo Fatima Al nsihapuri akasema: **'Akija Mtu mkubwa kama huyu Nyumbani kwangu basi hata Mbwa wa jirani nao itabidi wapate sadaqah yao ya chakula'**

Fatima Al Nishapuri alikua ni Mwanamke aliejaaliwa pia kua na utanashati wa kuzungumza kuhusiana na Ilm ya Tasawwuf kiasi ya kua alikua ni mwenye kuwavutia wengi sana katika darsa na mawaidha yake, kwani anasema Imam Abu Hafs Al Haddad kua: **'Mimi nilikua si mwenye kupenda kuwatilia maanani Wanawake na**

kutopenda kuwasikiliza wanapozungumza kuhusiana na Ilm ya Dini lakini baada kukutana na Fatima Al Nishapuri basi niliona na kujua kua bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* humpa Ilm na Ufahamu yeyote ule amridhiae'

Ambapo alisema Imam Bayazid Al Bistami kua: **'Katika Maisha yangu mimi, nimewahi kukutana na Mwanamme halisi mmoja tu na Mwanamke halisi mmoja tu ambae ni Fatima Al Nishapuri, kwani hakuna hali ya darja ya Maqam ambayo niliyokua nikizungumzia nae yeye isipokua alikua tayari ameshaipitia.**'

Na akasema tena kua: '**Yeyote yule anaetaka kupata usafi wa Ilm ya Tasawwuf basi anatakiwa awe ni mwenye kua na ari na jitihada kama za Fatima Al Nishapuri, ambae ni mke wa Ahmad Ibn Khidruyah, hivyo yeyote yule anaetaka kumuona Mwanamme halisi ambae yuko katika maumbile ya Mwanamke basi na aonane na Fatima.'**

Safari moja Fatima Al Nishapuri na Mume wake walitoka na kumtembelea Imam Bayazid Al Bistami ambapo walipofika mbele yake basi Fatima akafungua Niqab yake na hivyo kua ni mwenye kuuwacha wazi uso wake, hili lilikua ni jambo ambalo lililomshangaza sana Mume wake na hivyo baadae akamuuliza: **'Ilikuaje leo ukawa ni mwenye kujivunjia heshima kwa kuuwacha wazi uso wako mbele ya Imam Bayazid?'**

Ambapo Fatima Al Nishapuri akajibu: **'Ni kwa wewe ni kimaumbile ni Mume wangu na yeye kimaumbile Mwalimu wangu wa Dini, kupitia kwako wewe hua natimiza matamanio yangu ya kimwili na kupita kwake hua natimiza matamanio yangu ya kiroho, yaani yeye hua hana uhitaji wangu kijamii wakati wewe ni mwenye kuuhitajia'**

Hali hii ya kumtembelea Imam Bayazid Al Bistami iliendelea katika mazingira kama haya, hadi pale siku moja Imam Bayazid Al Mistami akamuuliza Shaykha Fatima Al Nishapuri: **'Naona mkononi umepaka hina, kwanini'**

Hivyo Shaykha Fatima akasema: **'Ewe Bayazid, pale ulipokua hukua ni mwenye kuiona mikono yangu na hina yangu basi mimi nilikua niko huru mbele yako, lakini sasa hivi hali imebadilika kwani macho yako yameangukia kwenye mikono yangu na kuniona, hivyo mimi nawe kuanzia leo uhusiano wetu umeharamika na kuishia hapa.'**

Na hivyo safari hizo za kutembeleana baina ya Fatima Al Nishapuri na Imam Ahmad Ibn Khidruyha kwa Imam Bayazid Al Bistami zikamalizikia hapo.

Fatima Al Nishapuri alifariki mnamo mwaka 224 Al Hijra wakati akiwa kwenye Ibada ya Hija.

Miongoni mwa wasia wake Shaykha Fatima Al Nishapuri ni kua: **‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* anapomdharau Ibn Adam, basi mtu huyo hua ni mwenye kutokua na muelekeo na hivyo hua ni mwenye kusema mengi asemayo na kwa lugha tofauti. Na *Allah Subhanah wa Ta’ala* asipomdharau mtu basi humjaalia Mtu huyo kua si mwenye kusema kitu isipokua ukweli uliojaa unyenyekevu na Ikhlasi ndani yake.**’

‘**Yeyote yule asiekua pamoja na *Allah Subhanah wa Ta’ala* ndani ya ufahamu wake basi hua ni mwenye kukosea na kupotoka, hata azungumze kwa Lugha gani, na hata awe pamoja na nani, na asiekua pamoja na *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwenye ufahamu wake hua si mwenye kusema isipokua kwa Ikhlasi na mwenye kushikamana na unyenyekevu na kujitolea katika tabia zake’**

‘*Allah Subhanah wa Ta’ala* kutokana na upendo na ukarimu na huruma zake hua ni mwenye kuwaita Ibn Adam kwake ili wapate kuitikia wito wake, na kama wasipomuitikia basi huwaingiza kwenye Mitihani ili wapate kurudi kwake, kutokana na mapenzi yake juu ya Waja wake.’

IMAM DHU NUN AL MISRI 181 AH

Imam Thawban Abu Fadhl Dhu Nun Ibn Ibrahim Al Misri alikua ni Mtu wa Misri aliekua Mtumwa lakini baadae akachiwa huru. Imam Dhu Nun Al Misri alizaliwa kwenye eneo linalojulikana kama Akhmim kutoka katika familia ya watu wenye asili ya Nubah, yaani Wanubi au Waafrika weusi wenye kutoka baina ya ardhi ya Ethiopia na Misri.

Imam Dhu Nun Al Misri alikua ni Mwanafunzi wa Imam Malik Ibn Anas na alikua ni mfuasi wa Madhhab ya Imam Malik. Imam Dhu Nun Al Misri alikua ni muanzilishi wa Ilm ya Tasawwuf nchini Misri.

Ama kuhusiana na Jina lake *Dhu Nun* basi ni neno *Dhu* hua ni lenye kumaanisha Mmiliki, na neno *Nun* lenye kumaanisha Samaki na pia hua linamaanisha Kisima au Kichupa cha Wino ambacho kawaida hua ni chenye kubeba herufi zote zinazoandikwa na Kalamu inayonyonya wino huo, ambapo kwa upande wa Imam Ibn Arabi basi yeye anasema kua: ‘**Herufi Nun ni yenye Siri kubwa sana kwani ndio Mlango wa Rehma na Ukarimu**.’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Dhu Nu Al Misri alikua ni mtu wa mwanzo kuanza kuzungumzia kuhusiana na *Darja Al Munazalat* ambayo ni Daraja ya Kiroho inayozikutanisha Roho za waja wema pamoja Mbele ya Mola wao, hii hua ni kama vile Imam *Dhu Nun Al Misri* alipokutana na *Rabiah Al Adawwiyah*, mbali ya kua watu hawa walikua ni wenye kuishi katika nyakati tofauti hapa Duniani.

Imam Dhu Nun Al Misri alipoulizwa ilikuaje hadi akawa ni mwenye kua na Ilm namna aliyokua nayo basi alisema: '**Nilipokua safarini njia nje ya Mji wa *Al Qakhira* basi usiku ulinikutia Jangwani, hivyo nikala na nilipoamka nikaona Kinda la Ndege ambalo lilikua lilikua liko katika hali ya upofu na lililoanguka kutoka kwenye kiota chake, na kisha hapo hapo pembeni yake ardhi ikapasuka na ndani yake vikatokea vyombo viwili kimoja cha Dhahabu na chengine cha Fedha, ambapo kimoja wapo kikiwa kina chembe za ufuta na chengine kiwa kina maji, hivyo ndege huyo akanza kula huku akinywa maji hayo, hivyo nami nikasema: 'Imetosheleza kwangu mie' na nikaanza kuugonga mlango wa *Allah Subhanah wa Ta'ala hadi* nikafunguliwa Mlango huo'**

Ambapo anasema Imam Muhyi Ad Din Ibn Al Arabi kuhusiana na ukufunguiwa huko mlango kwa Imam Dhu Nun Al Misri kua**: 'Alama kubwa sana na iliyokua wazi ya hali yake ya kiroho ya kukubaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema Dhu Nun Al Misri kua: 'Niliung'ang'ania Mlango huo hadi nikafunguliwa' hivi jee kua Karamah nyengine kubwa zaidi yah ii ya kukubaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*? Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* nasi atujaalie kua ni wenye kupokea habari njema kama walizopokea Mawalii wake.'**

Kwani Imam Muhyi Ad Din Ibn Al Arabi anaendelea kuasema kua: '**Nilikisikia mimi kisa cha Dhu Nun Al Misri na Kinda la ndege nilipotembelea maeneo ya Tunisia mbele ya Muhammad Al Mahdawi ambae alisema kua Kinda hilo la Ndege halikua ni kinda la ndege bali ilikua ni Roho yake mwenyewe Dhu Nun Al Misri, ambayo ilikuja kuwakilisha hali yake aliyokua nayo katika wakati huo.**'

Hivyo hali hii aliyowakilishiwa Imam Dhu Nun Al Misri na Kinda hilo la Ndege, ilikua ni hali aliyokua nayo Imam Dhu Nun Al Misri katika wakati huo ya kutokua na kitu chochote na kutoweza kitu chochote bila ya kuwepo kwa Mola wake yanai *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ambayo ndio hali pia inayotudhihirishia Ibn Adam wote kua si chochote bila ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kua tunamtegemea kwa kila kitu chetu kua ni kutyoka kwake, yeye ni tajiri asiepungukiwa na utajiri wke na sisi ni Masiki wenye kumhitaji yeye katika kila kitu chetu.

Na hivyo hali hi indie iliyompelekea Imam Dhu Nun Al Misri kua ni mwenye kumtegemea kikamilifu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na kujua kua Kila kitu chake kinatoka kwa Mola wake na hivyo kuna Wajibu wa kumuelekea yeye katika kila

kitu na kumuomba kila kitu, ambapo hatua ya mwanzo ya hali hii basi hua ni kama alivyosema mwenyewe Imam Dhu Nun Al Misri kua: '**Mwanzo wa njia ya kumueleeka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni kumpenda, ambapo dalili ya kumpenda huoenekana wazi pale unapokua ni mwenye kujiachia na kujitolea kwa ajili ya kuupata muongozo wake kwa kuikabidhi Roho yako kwake, na hapo utakua ni mweye kuonja raha ya kujiachia mbele yake juu ya kile anachokipenda na kuthibitisha maamuzi yake.**'

Ambapo Imam Dhun Nun Al Misri anaelezea kuhusiana na kumpenda kwake Alah *Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema kua: '**Hakika mimi nnakupenda wewe kwa hali ya mapenzi ya hisia kutamani, na kwa hali ya mapenzi unayostahiki. Ama kuhusiana na na Hisia za Mapenzi ya kutamani basi mimi ni mwenye kukukumbuka katika kila hali yangu bila ya kumkumbuka mwengine yeyote. Ambapo kuhusiana na Mapenzi unayostahiki basi ni kuondolewa Pazia ili nipate kukuona, hakuna kujisifia kwangu mimi juu ya mapenzi yangu mawili haya, bali kuna kusifika kwako wewe ndani yake mapenzi yangu mimi haya juu yako'**

Alisema Imam Dhu Nun Al Misri kua: '**Kama watu wangejua ni vipi wanavyojiona wako chini wale watu wenye Ilm kutokana na unyenyekevu wao basi wangewarushia vumbi kwenye Nyuso zao na vichwa vyao'** ambapo alisema Imam Tahir Al Maqdisi kuhusiana na kauli hii kua: **'Naam Bila ya shaka kwani kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* angedhihirisha Nuru ya watu wenye Ilm kwa wale waliofichikana nayo, basi watu hao wangeungua kutokana na ukali wa Nuru hio na kutoweka kama kwamba hawajawahi kuwepo hapo kabla'**

Ambapo Imam Ahmad A Hawari aliposikia juu ya kauli mbili hizi basi nae akasema: **'Allah amuingize kwenye Rehma zake Dhu Nun Al Misri, kwani aliyasema maneno hayo wakati alipokua akijifikiria nafsi yake, wakati Tahir aliyasema hayo wakati alipokua akimfikiria Mola wake, hivyo waote wawili wkao sahih na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kujua zaidi'**

Anasema Imam Bakr Ibn Abd Rahman kua**: 'Sisi tulikua na Dhu Nun Al Misri katika sehemu ambayo ilikua ni Jangwani, na tukasimama kwenye Mti ambao ulikua umejaa miba, hivyo nami nikasema: 'Ingekua vizuri sana kama huu mtu ungekua ni wenye Tende badala yake' Dhu Nun Al Misri akatabasamu na kisha akasema: 'Inaonekana kua ulikua unatamani kula Tende, enh?' kisha akautikisa Mti huo hukua akisema: 'Nnapa mimi kwa yule ambae amekujaalia na kukudhihirisha wewe kua ni Mti, hivyo jee huwezi kutuzalishia Tende mbivu tukapata kula?'**

Na kisha baada ya hapo haukuchukua mda isipokua Mti huo ukaangusha Tende ambazo zilikua zimpea na tukala hadi tukashiba, kisha tukalala na asubuhi

tulipoamka Dhun Nun alikua hayupo, hivyo nasi tukaenda kuutikisa mti huo tena ili tupate Tende lakini ukatuangushia Miba badala yake.'

Alisema Dhu Nu Al Misri kua: '**Mtu unapoamua kuachana na Dunia basi kimbia kutokana na kila kitu ambacho ni chenye kukusukuma na kukupelekea wewe kua mbali na Mola wako, kwani kila kitu ambacho ni chenye kukukimbiza wewe kutokana na Mola wako hua ni chenye kumilikiwa na Matamanio ya Dunia.'**

Akasema tena Imam Dhu Nun Al Misri kua: '**Yeyote yule ambae ni mwenye kuuangalia Ulimwengu huu bila ya kuona kua ni sehemu ya Kujifunza na kupata Ibra basi Mtu huyo hua ni mwenye Kuua Moyo wake kutokana na athari ya Kua na Dharau juu ya Mola wake.'**

Siku moja wakati Imam Dhu Nun Al Misri alikua akisafiri kwenye Mto Nile pamoja na Wanafunzi wake, na kwa mbali kutoka katika upande mwengine ikatokea Mashua ambayo ilikua ikija kuelekea upande wa Mashua aliyopanda Imam Dhu Nun Al Misri na Wanafunzi wake, ambapo Mashua hio ilikua na Watu wenye kusheherekea jambo fulani kwa ngoma na nyimbo, ambapo hili ni jambo lilikua ni lenye kuwakera Wanafunzi wa Imam Dhu Nun Al Misri, kwa sababu wao walikua ni wenye kuzama kwenye Dhikr Allah.

Hivyo Wanafunzi wa Imam Dhu Nun Al Misri wakamuomba Imam Dhu Nun Al Misri awaombee Dua watu hao kutokana na kero yao, ambapo nae akaomba kwa kusema: '**Ya Allah! Kama vile ambavyo umewajaaliwa kua na maisha yenye Raha watu hawa basi wajaalie kua ni wenye maisha yenye Raha na Akhera pia.'** Ambapo Dua hii iliwastaajabisha sana Wanafunzi hao, kwani waliona kua labda watu hao wataombewa kua Wanyamaze au waadhibiwe lakini imekua kinyume chake kwani wanaombewa Raha zaidi na Akhera pia, lakini hata hivyo nao wakakaa kimya.

Ilipokaribi karibu yao Mashua hio basi Wanafunzi wa Imam Dhu Nun Al Misri wakapigwa na mshangao zaidi, kwani mara tu watu hao walipomuona Imam Dhu Nun Al Misri basi wakaanza kulia na kufanya Toba kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo Imam Dhu Nun Al Misri akasema kuwaambia Wanafunzi wake kua: '**Raha ya Maisha ya Akhera hua ni yenye kupatikana kutokana na Kufanya Istighfar katika Dunia hii, mmeona sasa kua wao na nyinyi nyote mmekua ni wenye kuridhiana bila ya kusababisha Madhara yeyote baina yenu.'**

Imam Dhu Nun Al Misri alisema kua: '**Mahabah hua ni Kupenda kile ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* anakipenda, kukichukia kile ambacho A*llah Subhanah wa Ta'ala* anakichukia, kutafuta Ridhaa yake, kudharau kila kitu ambacho chenye kukuzuia kutokana kumuelekea yeye, kutokua na khofu juu ya wale watakaokuchukia kutokana na mapenzi hayo, kutokua na ubinafsi wa kutojiona**

ndani ya Nafsi yako, kwani Ukuta wa kumuona yeye hua unakua mpana zaidi kutokana na kua ni mwenye kujiona kiwili wili chako peke yake badala yake.'

Safari Moja Imam Dhu Nun Al Misri alikua safarini pia akielekea Misri kutokea katika maeneo ya Jerusalem, ambapo njiani akakutana na Mtu mzima Mwanamke ambae alikua anakuja kutoka Misri kuelekea Jerusalem huku akiwa ameshika Fimbo na Juba. Hivyo Imam Dhu Nun Al Misri akamsalimia na kujitambulisha na kisha akamuuliza Mwanamke huyo: '**Hivi unaelekea wapi? Mbona uko katika hali kama hio ya peke yako?'** yule Mwanamke akajibu: **'Natoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na naelekea kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Hivyo Imam Dhu Nun Al Misri, akaona kua amsaidie Mama huyo kwa chochote kile alichokua nacho na hivyo akingiza mkono wake mfukoni mwake na akatoa vipande vidogo vidogo vya Dhahabu na akampa Mama huyo, ambae nae akakataa kupokea na kisha akaanza kulia huku akisema: '**Ewe Dhu Nun, mtizamo wako juu yangu ni wenye kutokana na ukarimu wa ufahamu wako juu yagu, lakini mimi niko kwa ajili ya *Allah Subhanah Wa Ta'ala* na sipokei chochote kutoka kwa yeyote isipokua yeye, kwani simuabudu yeyoye na hivyo sihitaji chochote kutoka kwa yeyote isipokua yeye.'** Na kisha Mama huyo akaendelea na safari yake.

Ambapo maneno haya yanadhihirisha vile Mama huyo alivyokua ameshikamana na maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo:

﴿إِنْ أَحْسَنْتُمْ أَحْسَنْتُمْ لِأَنْفُسِكُمْ وَإِنْ أَسَأْتُمْ فَلَهَا﴾

In ahsantum ahsantum li-anfusikum wa-in asa/tum falaha *(Surat Al Isra 17:07)*

Tafsir: ***Kama mkifanya Mema basi mnafanya Mema hayo kwa ajili ya Nafsi zenu, na mkiasi basi ni kwa ajili yake pia.***

Na pia yale maneno yasemayo:

﴿وَمَن جَاهَدَ فَإِنَّمَا يُجَاهِدُ لِنَفْسِهِ إِنَّ ٱللَّهَ لَغَنِيٌّ عَنِ ٱلْعَالَمِينَ﴾

Waman jahada fa-innama yujahidu linafsihi inna Allaha laghaniyyun AAani alAAalameena *(Surat Al Anqabut 29:06)*

Tafsir: ***Na yeyote yule anaejitahidi, basi hua ni mwenye kujitahidi kwa Nafsi yake, kwani kwa Hakika Allah ni asiekua na haja ya chochote kutoka kwa Walimwengu wake.***

‘**Mtu mwenye Busara hua ni yule ambae ni mwenye kuthamini ufukara wake, kiasi ya kua Anapotajwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi hua ni mwenye kuona fakhari na anapotajwa yeye hua ni mwenye kujiona kua ni Fakiri.’**

Imam Dhu Nun Al Misri alisema pia kua: **‘Si Mwenye Ilm yule ambae ni mwenye kuikumbatia Dunia yake, na kuichukulia kwa urahisi Akhera yake, na wala si yule ambae ni mwenye kumsahau Mola wake katika utiifu wake juu yake na kumkumbuka katika wakati wa Matatizo yake, na wala si yule ambae ni mwenye kujaza aina tofauti za Ilm kuhusiana na Mola wake lakini akawa ni mwenye kuyatanguliza mbele matamanio yake, na wala sio yule ambae si mwenye kuona haya mbele yake wakati ni Mola wake ndie aliemhifadhia Uchi wake, na wala si yule ambae ni mwenye udhaifu mbele ya Ibilis ambae ni adui yake, na wala si wale ambao wasioweza kuifanya heshima kua ndio Mavazi yao, Tabia njema ndio Ngao yake, na Taqwa ndio pambo lao, na wala si yule anaeifanya Ilm yake kua ni yenye kumpa Kiburi na kujiona.’**

‘Kumpenda *Allah Subhanah wa Ta’ala* huainishwa katika kumfuata *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Nyayo zake iwe kwa ukarimu au kwa vitendo vyake au kwa kutii maamrisho yake na kusita na kubakia ndani ya mipaka ya yale aliyoyakataza.’

‘Ama kuhusiana na Toba basi kuna aina mbili za Toba kuna Toba ya kufanya Istighfar kwa watu wa Kawaida kutokana na Dhambi zao na kuna Toba ya Khawash ambayo ni kutokana na Dharau’

‘Maarifah hunawirisha katika hali zifuatazo: ‘Kunawirika kwa Muumini wa Kawaida, Kunawirika kwa Mwenye kutumia Mutakallimin – Kauli na Kunawirika kwa Hukama (Wanafalsafa) na kunawirika kwa *Walliyu Allah* ambae ni mwenye Ukaribu na *Allah Subhanah wa Ta’ala.’*

‘Ambapo kunawirika kwa Muumini wa Kawaida hua ni kumjua *Allah Subhanah wa Ta’ala* kutokana na mafunzo wanayoyapata, ambapo kunawirika kwa Mutakallimin na Hukama hua ni kutokana na njia ya Ufahamu na Mantiq ambapo kutokana navyo vitu hivyo basi ndio hupata Ladha ya Maarifa. Ambapo kwa upande wa *Muqarrabun* basi wao hua ni wenye Kunawirika kutokana na Muongozo wa *Allah Subhanah wa Ta’ala*, hivyo hua ni wenye kunawirika kutokana

na *Ilham* (ushushio) na *Kashshaf* (ufunuo) na hivyo hapa ufahamu hua haufanyikazi, kwani hua umefikia katika Darja ya juu kabisa.'

Ama kuhusiana na ufafanuzi zaidi wa Mahabah basi hua ni mapenzi yenye majibu na kupokezana ndani yake kutoka kwa Kiumbe juu ya Muumba wake, baina ya anaependa na anaependwa, ambapo mvutano huu wa mapenzi hua mkubwa kuliko mvutano wa Sumaku kwa Chuma, kwani yule anaependa kila anapokua na ukaribu na yule anaempenda basi huvutwa zaidi hadi kufikia hali ya kujumuika na yule ampendae, ambapo mapenzi haya huhisikana baada ya kufikia darja maalaum, na haiwezekani kufundishwa kwani hua ni kitu cha Siri, hususan kutokana na wale wenye kua na hisia za mapenzi kutokana na hisia tano za kimaumbile za Ibn Adam.

Imam Dhu Nun Al Misri alisema kua: **'Nabii Musa alimuuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema: 'Ewe Mola wangu hivi nimimi nikutafutie wapi?' ambapo nae akajibiwa: 'Kwa wale ambao wameshavunjika Nyoyo zao' ambapo nae akasema; 'Ewe Mola wangu bila ya Shaka kwa sasa hivi hakuna mwenye Moyo uliovunjika kama vile ulivyovunjika wangu' ambapo nae akajibiwa: 'Basi tayari mimi niko nawe hapo ulipokuwepo.''**

Imam Dhu Nun Al Misri alifariki mnamo mwaka 248 Al Hijra, ambapo katika usiku wa siku aliyofariki basi kuna watu 70 ndani ya ardhi ya Misri ambao wote waliota ndoto moja ambayo ni yenye kumuonesha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua: **'Nimekuja mimi kukutana na Dhu Nun Al Misri'** na asubuhi yake maneno yasemayo: '**Huyu ni Kipenzi Cha *Allah Subhanah wa Ta'ala*, ambae amefariki kutokana na Mapenzi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*'** yalionekana kwenye paji la uso la Maiti ya Dhu Nun Al Misri.

Ambapo katika Maziko yake basi Ndege walikua ni wenye kuruka kuzunguka Jeneza lake kwa ajili ya kuwafanyia kivuli waliokua wamebeba Jeneza hilo.

Alisema Imam Dhu Nun Al Misri kua: '**Ikhlasi ni Upanga wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hapa Duniani, kwa hua ni wenye kukata kila kitu unachokigusa**.' Yaani Iklhasi hua ni juu yule anaefanyiwa kitu husika ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu, ukifanya kwa ajili ya jambo jengine au kitu chengine basi hua umeshakiamiza kitu hicho Ulichokifanya.

Imam Dhu Nun al Misri aliulizwa: **'Jee ni nini hali ya Mwenye kuachana na Dunia kwa Moyo mkunjufu'** ambapo nae akajibu: **'Huonekana katika hali tatu, anapokua anacho hua ni mwenye kutoa, anapokua hana hua si mwenye kuomba na kuwapendelea wengine pale anapopewa yeye.'**

IMAM AL KIRMANI 190 AH

Imam Abu Muhammad Harb Ibn Ismail Ibn Khalaf Al Hanzali Al Kirmani ambae anatokana na Kabila la Al Hanzali ambalo pia ndio alilotoka Imam Is-haq Ibn Rahawayh linalotokana na Tamim Ibn Murr alizaliwa mnamo mwaka 190 Al Hijra katika maeneo ya ardhi ya Nishapuri katika maeneo yanayojulikana kama Murrab Al Kirmaniyyah ambalo lipo katika maeneo ya Kaskazini Mashariki ya nchi ya Iran baina ya ardhi ya Turkmenistan na Afghanistan.

Imam Abu Muhammad Al Kirmani alikua ni Mwanafunzi wa Imam Al Marwazi ambae nae alisoma moja kwa moja kutoka kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal na hivyo Imam Al Kirmani alikua ni Mwanafiqh mkubwa sana wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na ni mwenye kutegemewa Fatwa zake ndani ya Madhhab hayo.

Kwani anasema Imam Adh Dhahabi kua: **'Kitabu cha Al Masail cha Imam Al Kirmani ni moja kati ya Vitabu mali sana miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Hanbali, ni kitabu kikubwa kina matoleo mawili, na kifo cha ImamAl Kirmani kilikua ni mnamo mwaka 280 Al Hijra na alijaaliwa kua na Maisha marefu kwani aliishi kwa mda wa miaka 90, na kwa hakika sijawahi mimi kusikia malalamiko yeyote juu yake.'**

Katika kutafuta kwake Ilm basi Imam Abu Muhammad Al Kirmani alisoma kwa Maimamu wengine wengi katika kutafuta kwake Ilm akiwemo Imam Abu Al Walid Al Tayalisi, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Abu Bakr Al Humayd, Imam Abu Ubayd Said Al Mansuri, Imam Sulaymān Ibn Ḥarb, Imam Saʿid Ibn Sulaymān An-Nashiṭi, Imam Abdullāh Ibn Sawwār Al Anbarī, Imam Ubayd Allāh Ibn Mūsā Al Absī al-Kūfī , Imam Aḥmad Ibn Al Azhar Al Nīsābūrī, Imam Al Farra Mihammad Ibn Nasr Al Nishapuri, Imam Ibrahīm Ibn Muḥammad Al Maṭlabiyy Al Shafii, n.k

Kwani Imam Al Kirmani alifunga safari kuelekea nchini Iraq mnamo mwaka 213 Al Hijra akiwa na umri wa miaka 23 na kisha miaka 6 baadae akahama kutoka katika ardhi ya Iraq na kuelekea katika Mji Mtakatifu wa Makkah na hivyo kua ni miongoni mwa Maimam waliofunga safari wakiwa wadogo kabisa kwa ajili ya kujitafutia Ilm.

Baada ya Imam Al Kirmani kupata Ilm ya kutosha basi akaawa ni mwenye kuamua kua ni mwenye kujitolea kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kwa ajili ya kujisafisha Nafsi yake.

Baadae Imam Al Kirmani akaelekea Nchini Syria ambapo anasema Imam Abu Zurah Al Dimashq kua: '**Kuna watu wawili tukufu ambao walitutembelea sisi katika Mji wetu ambapo mmoja wao ni Yaqub Ibn Sufyan Al Fasawi ambae kwa watu wa Iraq basi ni ku ahana mfano wake, na mtu wa pili ni Harb Al Kirmani huyu ni miongoni mwa waliosoma kutoka kwangu.**'

Ambapo anasema Imam Abu Hatim Al Razi kua: **'Mwanafunzi mwenzangu katika ardhi ya Mji wa Sham Al Kirmani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amuingize kwenye Rehma zake.**'

Ambapo anasema Imam Ibn Abī Ḥātim kua: **'Al Kirmani alikua ni Mwanafunzi mwenzake Baba wakati walipokua katika ardhi ya Dimashq na Baba yangu alikua akiandika kutoka kwake'**

Hivyo Imam Abu Hatim Al Razi alikutana nae Imam Al Kirmani alipofika katika ardhi ya Dimashq na hivyo wakawa ni wenye kusoma pamoja katika maeneo ya ardhi tofauti na hivyo Imam Al Kirmani kua ni mwenye kua na Walimu wasiopungua 160 na hivyo kua na Ilm kubwa sana..

Imam Al Kirmani alisomesha Wanafunzi wengi pia wakiwemo kina Imam Abu Uthman Al Hiri, Imam Al Qasim Ibn Muhammad Al Kirmani, Imam Abd Allah Ibn Is-haq Al Nahawandi, Imam Abu Hatim Al Razi, Imam Abu Bakr Al Khallal na wengineo.

Ambapo alisema Imam Al Khallal kua: '**Imam Al Kirmani alikua ni mtu mwenye Kuheshimika sana kwa Ilm yake kiasi ya kua Imam Al Marwazi alinishauri mimi kua nisafiri ili niende nikasome kwake.'**

Na kwa upande wa Imam Abu Ya'ala basi yeye anasema kua: '**Amesema Abu Bakr Al Khallah kua, Al Kirmani alikua ni wanafiqh wa Ardhini na Mtawala alimfanya awe juu kuhusiana na kutoa hukumu na mambo mengine ardhini**'

Ambapo anasema Imam Ibn Al Qayyim kua: **'Na mwangalie Harb na Ijmaa alizozonikuu, ni mafanikio makubwa sana kutoka kwa kijana wa Kirmani'**

Na akasema Imam Al Mawardi kua: **'Al Kirmani ni Mkongwe miongoni mwa Wanazuoni wa Hadith'**

Alisema Imam Al Kirmani kua: **'Upukeni Kusoma Uongo, Kughilibu na kusengenya na mkisha weza kufanya hivyo basi mtaweza kufanya kila mnachotaka'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

IMAM BUKHARI 194 AH

Imam Abu Abd Allah Muhamamd Ibn Abu Al Hasan Ismail Ibn Ibrahim Ibn Al Mughira Al Ghafi Al Muhkari Al Bukhari alizaliwa katika sikuya Ijumaa ya Mwezi 13 Shawwal ya mwaka 194 Al Hijra katika Mji wa Bukhara Mjini Uzbekistan Khurasan.

Imam Al Bukhari alitokana na familia yenye watu wenye Ilm na Ucha Mungu, kwani Baba yake Imam Al Bukhari ambae ni mzee Ismail Ibn Ibrahim alifariki miaka michache baada ya kuzaliwa Imam Al Bukhari na hivyo kumuacha Imam Al Bukhari akiwa ni yatima, ambapo mzee Ismail alikua ni Mwanazuoni na mtu mwenye kuthaminika sana katika jamii yake, na alikua ni Tajiri pia, na hivyo alipofariki basi aliwacha Mali kwa ajili ya Watoto wake akiwemo Imam Al Bukhari ambayo ilikua ikisimamiwa na Mama yake ambae nae aliitumia katika kuwatafutia Ilm ya Dini watoto wake.

Imam Al Bukhari alikua ni mwenye kuhifadhi Qur'an wakati akiwa mdogo na hivyo kua ni mwenye hamu sana ya kuijua zaidi Dini yake, kwani Imam Al Bukhari aliulizwa na Wanafunzi wenzake alipoka akisoma Ilm ya Hadhith kwa kuambiwa: '**Jee ulianza lini wewe kutafuta Ilm ya Hadith'** Imam Al Bukhari akajibu: '**Mimi nilijaaliwa kua na ufahamu wa kuhifadhi Hadith tangu katika wakati nilipokua kwenye *Kuttab* nilipokua na umri wa miaka 9-10'**

Imam Al Bukhari alijaaliwa ufaham mzuri sana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambao aliutumia kwa njia sahih ya kuhifadhi Hadith tangu akiwa na umri mdogo huo kwanialikua si mwenye kuandika Hadith bali alikua anahifadhi moja kwa moja kwenye Ufahamu wake bila ya kusahau.

Ambapo anasema Salim Ibn Mujahid kua: **'Mimi nilikua na Muhammad IbnSalim Al Baikandari ambae aliniambia, umechelewa kufika kwani kama ungewahi kidogo tu basi ungekutana na kijana mdogo ambae amehifadhi hadith 70000' hivyo nikaanza kumtafuta kijana huyo hadi nikakutana nae na kumuuliza: 'Wewe ndie unaesema kua umehifadhi hadith 70000?' ambapo nae akasema: 'Naam, kwani mimi sinukuu hadithi kutoka kwa Sahaba au waliofuatia baada yao isipokua ni mwenye kujua kila kitu juu yao kuanzia mwaka waliozaliwa sehemu walizozaliwa na walizoishi na hadi kufariki kwao.''**

Imam Al Bukhari aliendelea kusoma Hadith na alipofikia umri wa miaka 16 alikua tayari ameshazihifadhi Hadith zote za Imam Abd Allah Ibn Mubarak, na Imam Waki Ibn Jarrah kwani alikua ni mwenye kutafuta Ilm ya Hadith katika kila sehemu kuanzia kwenye Mji wake aliokua akiishi wa Bukhara hadi Balkh na Nishapuri na kisha akaelekea katika ardhi takatifu ya Mji wa Makkah ambapo alikaa kwa mda kwa ajili ya

kufanya Ibada ya Hija na kisha kuendelea na Ilm ya Hadith. Na kisha baada ya hapo Imam Al Bukhari akaelekea Misri na kisha akaelekea katika ardhi ya Sham na Baghdad na hivyo kua ni mwenye kusoma kwa Wanazuoni wa Hadith wafikao 1000.

Anasema Imam Bukhari mwenyewe kua: **'Katika kutafuta kwangu Ilm mimi basi nilisafiri kuelekea Misri na Syria mara 2, Basra mara 4 na nilitumia ma wangu katika maeneo ya Hijaz kwa muda wa miaka 6 na kisha nikaondoka na kueleeka Kufah na Baghdad na mara nyingi miongoni mwao nikiwa nimefuatana na Wanazuoni wa Hadith.'**

Ambapo miongoni mwa Walimu wake Imam Al Bukhari ni pamoja na Imam Ahmad Ibn Hanbal,Imam Hammad Ibn Shakir, Imam Makki Ibn Ibrahim, Imam Abu `Asim An Nabil, Imam Ali Ibn Al Madini, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Yahya Ibn Main, Imam Muhammad Ibn Yusuf Al Firyab, Imam Muhamamd Ibn Yusuf Al Baykandi Na wengineo.

Anasema Imam Rashid Ibn Ismail ambae ni kaka yake Imam Al Bukhari kuhusiana na ndugu yake kua: **'Muhammad alikua akitoka pamoja nasi kwa Wanazuoni wa Basra kwa ajili ya kusikiliza Hadith, ambapo sisi sote tulikua tukiziandika Hadith zetu isipokua yeye, na hivyo baada ya siku kadhaa tukaanza kumshambulia Muhammad kwa maneno ya kua amepoteza mda wote bure bila ya kuandika Hadith hata moja, wakati alikua anatakiwa aandike kama tufanyavyo sisi.**

Hivyo Muhammad akasema tuchukue vitabu vyetu tulivyoandika Hadith tulizosoma, na kisha tulipochukua basi akaanza kusoma Hadith kutoka kwenye ufahamu wake, huku sisi tukiangalia kwenye vitabu vyetu. Muhammad alitusomea Hadith hadi zikafikia 15000 kutoka kichwani mwake, na kusikiliza kutoka kwake ilikua ni kama kuzisoma tena hizi hadith mbele ya Mwalim wa Hadith.'

Ambapo anasema Imam Muhammad Ibn Azhar Sijistani kua '**Mimi nilikua nikienda kwa Sulayman Ibn Harab nikiwa ni mwenye kufutana na Al Bukhari kwa ajili ya kusikiliza Hadith, na mimi nilikua nikiandika Hadith lakini yeye Bukhari hakuwahi kua ni mwenye kuandika kile anahokisikiliza, hivyo akaulizwa: 'Kwanini Bukhari haandiki' nami nikasema kua 'Kama ukikosa Hadith yeyote ile katika njia ya Maandishi basi utaipata kwenye ufahamu wa Al Bukhari''**

Safari moja Imam Al Bukhari alienda kwenye mji wa Baghdad, na alipofika basi watu wakawa ni wenye kumzungumzia sana kuhusiana na uwezo wake, hivyo kua baadhi ya Watu wakataka kumuangalia Ufahamu wake, na hivyo wakachagua Hadith 100 tofauti huku wakiwa ni wenye kuzibadilisha Sanad za wapokezi wa Hadith hizo zote, kwa Sanad ya Hadith hii kuiweka kwenye hadith hii au ile n.k na kisha wakakaa mbele ya Imam Al Bukhari na kuanza kusoma hadith hizo katika mparaganyiko wa Sanad na Matn

zake, ambapo Imam Al Bukhari aliposomewa Hadith hizo basi alisema kua Hazijui Hadith hizo hata moja kwa kila aliyosomewa.

Lakini hata hivyo baada ya watu hao kumaliza kusoma Hadith zao na kumuuliza, basi Imam Al Bukhari akazirudia tena upya Hadith hizo kwa kuzinukuu kwa mpangilio wake Sahih wa Sanad na Matn zake kikamilifu tangu mwanzo hadi mwisho, na hivyo kuwaacha watu hao wakiwa hoi, kutokana na uwezo wake kiufahamu.

Mbali ya kua Imam Al Bukhari ni alikua na sifa hizo lakini pia alikua ni Mtu mkarimu sana kwani alikua ni mwenye kutumia Mali aliyoachiwa na Baba yake kwa ajili ya Wasiokua na Uwezo pia, kiasi ya kua sehemu ya Mali yake ilipomalizika basi ilifikia yeye kua ni mwenye kuishi kwa kula Tende moja tu kwa siku, lakini huku akiwa ni mwenye kuwajali wafanyakazi wake, kwa ajili ya mahitajio yao.

Imam Al Bukhari alikua ni Mcha Mungu sana, alikua si mtu mwenye kusimanga, wala kusengenya na alikua ni mwenye ustahmilivu kiasi ya kua alikua si mwenye kuonekana kiwa ni mwenye kukasirika.

Baada ya kumaliza kusoma na kua ni mwenye kuifadhi Hadith nyingi sana basi Imam Al Bukhari alianza kusomesha Ilm ya Hadith na hivyo kua Imam wakati alipotimia umri wa miaka 17 ambapo alikua akisema kua: ‘**Mimi nimehifadhi Hadith Sahih 100000 na hadith zisizokua Sahih 200000’**

Alisema Imam Al Bukhari kua: **‘Mimi sijui kitu chochote kile ambacho watu watakihitaji isipokua watakikuta ndani ya Qur’an na Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam, na* nna matumaini ya kua nitakutana na *Allah Subhanah wa Ta’ala* huku nikiwa si mtu ambae nimemsengenya mtu, kwani sikuanza kusomesha Hadith yeyote ile hadi pale nilipokua nna uhakika wa usahih wa Hadith husika, na nimepitia vitabu vya mitizamo vyote na nimetembelea Mji wa Basr mara 5, na sikuiacha Hadith isipokua nimeiandika isipokua ile niliyokua na shaka nayo, kwa hakika mimi si mwenye kutaka kusema kitu chochote hata mambo ya kidunia bila ya kuanza na kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta’ala*’**

Imam Al Bukhari alisomesha Wanafunzi wengi sana kwani wanafikia idadi ya 9000 ambapo miogoni mwao ni pamoja na Imam Ibn Al-Hajjaj, Imam At-Tirmidhi, Imam An-Nasa’i, Imam Muhammad Ibn Nasr Al-Marwazi, Imam Ibn Khuzaima, Imam Ad Darimi na wengineo.

Ingawa Imam Al Bukhari alikua si Mtu mwenye kuandika Hadith katika kipindi cha Uanafunzi wake lakini hata hivyo mtizamo wake huo ulibadilika baadae kama anavyosema mwenyewe kua: ‘**Mimi nilikua na Is-haq Ibn Rahawayh ambapo nae akasema: ‘Ingekua vizuri sana kama angetokea Mtu akaandika Hadith Sahih za**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*’ hivyo nikaupenda Mtizamo huo na nikaamua kukusanya na kuandika Al *Jamii Al Sahih*’**

Ambapo kabla ya kuandika kitabu hicho basi Imam Al Bukhari alilala kisha akoaota kua amesimama mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, huku akiwa ameshika kipepeo ambacho alikua akimpepelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutokana na Nzi waliokua wapo kwenye eneo hilo, hivyo alipaomka asubuhi yake basi Imam Al Bukhari akaulizia kuhusiana na maana ya Ndoto hio na akaambiwa kua inamaanisha kua: Imam Al Bukhari atakua ni mwenye kuziangamiza Hadith alizozushiwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua alizisema maneno yake, na hivyo hii pia ilimtia ari zaidi ya kuandika Jamii Al Sahih.

Kitabu hiki cha *Jamii Al Sahih* au *Sahih Imam Al Bukhari* ni kitabu chenye Hadithi Sahih 7,275 zilizochaguliwa na Imam Al Bukhari, kutoka katika Hadith 600,000 alizozihifadhi kutoka kwenye Ufahamu wake. Ambapo Imam Al Bukhari alikua haandiki Hadithi kabla ya Kutia Udhu kwanza na kisha Kusali Sala ya Sunnah ya Rakaa 2, kama anavyosema Imam Al Firbari kua: ‘**Alisema Imam Al Bukhari kua: ‘Mimi nilikikusanya kitabu cha Al Jamii Al Sahih wakati nikiwa kwenye Masjid Al Haram, na sikujumuisha Hadith ndani yake isipokua baada ya Kusali Salat Istikhara kwanza, rakaa 2 kwa ajili ya kuomba msaada wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* baada ya kuamini kua Hadith husika ni Sahih.’’**

Tofauti na wanavyojua wengi sana kuhusiana nae Imam Al Bukhari, kua ni Mwanazuoni wa Hadith tu, lakini ukweli ni kua hakua ni mwenye kuandika kuhusiana na Hadith tu, kwani Imam Al Bukhari aliandika pia kuhusiana na fani nyenginezo za Ilm ya Dini alizokua nazo ikiwemo Tafsir, Fiqh na Tarikh.

Ambapo aliasema Imam Naim Ibn Hamamd kua: **‘Imam Al Bukhari alikua ni Al Faqih wa Ummah huu.’**

Miongoni mwa Vitabu alivyoandika ni pamoja na *Tarikh Al Kabir, Tarikh Al Saghir, Tarikh Al Awsat, Khalq Afa la Al Ibada Raf` Al-Yadain fi As-Salah, Adhdhuafaa Al Saghir, Adab Al Mufrad,* n.k.

Ambapo anasema Imam Ibn Khuzaymah kua: **‘Mimi sijawahi kumuona mtu yeyote yule chini ya Mbingu za *Allah Subhanah wa Ta’ala*, mwenye Ilm kubwa na mwenye uwezo wa Kuhifadhi Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama Muhammad Ibn Ismail Al Bukhari’**

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Amr Al Khaffaf basi yeye anasema kua: **‘Muhammad Ibn Ismail ni mwenye Ilm kubwa sana zaidi ya Is-haq Ibn Rahawayh, Ahmad Ibn Hanbal na Wanazuoni wengine kwa Digirii 20 zaidi, hivyo yeyote yule**

atakaemlaani au kumtukana yeye basi mimi namlaani Mtu huyo kwa mara 200 zaidi, kwani Muhamamd Ibn Ismail ni mtu ambae ni Mcha Mungu sana ambae mimi sijawahi kuona mwengine zaidi yake'

Na Abd Allah Ibn Hammad akasema: **'Mimi nilikua natamani niwe Nywele tu kwenye kifua cha Muhamamd Ibn Ismail'**

Baada ya kukaa nje ya ardhi ya Nchi yake kwa mda mrefu basi Imam Al Bukhari akaamua kurudi kwenye maeneo ya Mji wa Bukhara. Ambapo alipokelewa kwa shangwe na furaha, na akaazisha Madrasa yake na kuanza kusomesha watu wake, ambapo kutokana na Ilm yake, Ucha Mungu wake na Uadilifu wake, basi alikua si mtu mwenye kutaka kujulikana na wala kua naukaribu na wenye Mamlaka.

Ambapo baada ya mda kupita basi Gavana wa Mji wa Buhara aitwae Khalid Ibn Ahmad alimwita Imam Al Bukhari nyumbani kwake kwa ajili ya kumsomeshea Mtoto wake. Lakini hata hivyo Imam Al Bukhari akasema: **'Hakika mimi naiheshimu Ilm zaidi ya kuliko nnavyo waheshimu watu, hivyo kama watu watakua ni wenye kuihitaji Ilm basi itawabidi wao waifuate Ilm'**

Ambapo Gavana huyo akasema: **'Sawa lakini Kama Mtoto wangu akija Madrasani kwako basi itabidi umsomeshe peke yake usimsomeshe na Wanafunzi wengine'** hivyo Imam Al Bukhari akasema: **'Hakika mimi siwezi kumzuia mtu kutokana na kutafuta Ilm.'**

Baada ya Majibu hayo basi Gavana Khalid Ibn Ahmad akamfukuza Imam Al Bukhari kutoka kwenye Mji wa Bukhara na hivyo Imam Al Bukhari akahamia katika maeneo ya Khartang ambayo yapo umbali wa kilomita 30 kutoka Samarkand nchini Uzbekistan. Kisha baada ya tukio hilo basi Khalifa wa Baghdad akamfukuza kazi Gavana Khalid Ibn Ahmad na kumuweka ndani jela ambapo alikaa hadi kufariki kwake.

Ambapo Imam Muhamamd Ismali Al Bukhari nae aliishi kwenye eneo hilo la Khartang ambalo ni la kijiji kilichopo bondeni kwa mda na kisha mnamo mwezi mosi wa Shawwal ya mwaka 256 Al Hijra akafariki Dunia katika kijiji hicho.

Imam Al Bukhari hakua Mwanazuoni tu bali pia laikua ni Mtu ambae mwenye umahiri wa kutunga shabah kwa kutumia Upinde na hivyo alikua ni mwenye kujitayarisha kila mara anaposikia kua kuna Vita vya *Jihadi fi Sabili Allah* kwa ajili ya kupigana katika safu ya wapiganajiwanaotumia Upinde.

Alisema Rajaa Al Hafidh kua: '**Al Bukhari alikua ni Dalili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* inayotembea hai Ardhini.'**

Imam Al Husain Al Samarqandi alisema: **‘Muhamamd Ibn Ismail alikua na upekee wa sifa tatu zaidi ya anazosifiwa ambazo ni kua alikua Mtu mkimya na asiesema sana, na mwenye ari kubwa sana ya kutafuta kuhusiana na kile walichokua nacho wengine ambacho yeye hana kuhusiana na Ilm, ambacho yeye hana, na alikua ni mnyenyekevu katika kutafuta kwake Ilm’**

Imam An Najm Ibn Al Fudayl alisema kua: **‘Mimi nilimuona kwenye Ndoto Imam Al Bukhari akiwa anatembea Nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na hivyo kila anaponyanyua mguu wake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Muhamamd Ibn Ismail alikua akiweka mguu wake.’**

Na Imam Yahya Ibn Jafar akasema: **‘Hakika kama mimi ningekua nnao uwezo wa kumpa Muhamamd Ibn Ismail sehemu ya Uhai wangu basi ningefanya hivyo kwa sababu kufariki kwangu hua ni sawa na kufariki kwa Mtu mmoja, lakini kufariki kwa Bukhari kunamaanisha kufariki kwa Ilm.’**

IMAM ABU ZURAH AL RAZI 194 AH

Imam Abu Zurah Ubaid Allah Ibn ‘Abd Al Karîm Ibn Yazîd Ibn Farrūkh Ibn Dâwud ar-Râzî alizaliwa katika ardhi ya Khurasan katika maeneo ya Al Razi mnamo mwaka 194 Al Hijra na anaitwa Imam Abu Zurah ambapo mbali ya kua katika Ulimwengu wa Ilm ya Kiislam kuna Wanazuoni zaidi ya 50 wenye majina ya Abu Zurah, lakini ukisema Abu Zurah bila kutaja jina jengine basi moja kwa moja watu wenye kujua hua wanajua kua ni Imam Abu Zurah Al Razi.

Imam Abd Al Karim ambae ni Baba yake Imam Abu Zurah alikua pia ni mwanazuoni wa Hadith wa Mji wa Al Razi ambae alikua ni maarufu sana. Mara moja Imam Abd Al Karim aliendanae mtoto wake kwenye baraza ya Imam Abd Rahman Ibn Abd Allah Ad Dusytaki, ambapo Imam Abu Zurah kutokana na udogo wake kiumri basi aliingiwa khofu kutokana na ukubwa wa Ilm ya Imam Ad Dusytaki hivyo akawa ni mwenye kujiweka nyuma nyuma.

Mara Imam Ad Duystaki alipomuona Abu Zurah basi alivutiwa nae na hivyo akamuuliza Imam Abd Al Karim kwa kusema: **‘Huyo Kijana mdogo ndio nani?’** Ambapo Imam Abd Al Karim akasema**: ‘Ni Mtoto wangu’** Imam Ad Duystaki akasema: **‘Hebu msogeze hapa Karibu’** na hivyo Imam Abu Zurah akasogezwa karibu, na kisha baada ya kumtizama basi Imam Ad Duystaki akasema: **‘*Ma-shaa Allah* kwa hakika Mtoto wako huyo atakua ni Mtu mkubwa na maarufu sana, atakua ni mweye Ilm kubwa sana ya Hadith, Qur’an Fiqh na Ilm nyenginezo’**

Naam, maneno haya ya Imam Ad Duystaki hayakua ni maneno ya kutupa, kwani Imam Abu Zurah alikua kila anapoenda kusoma basi hua ni mwenye kuwaachia watu mshangao, ndani ya maisha yao kiasi ya kua kila Mwanauzoni wa mji wa Al Ray na Khurasan wakawa ni wenye kutaka kua ni wenye kumsomesha Imam Abu Zurah.

Ambapo Mwalimu wake wa kwanza Imam Abu Zurah baada ya baba yake alikua ni Imam Ibrahim Ibn Musa Al Razi ambapo kutoka kwake tu basi Imam Abu Zurrah alihifadhi hadith 100,000, na kusoma kwa Walimu wengine na kisha baada ya hapo wakati Imam Abu Zurah akiwa na umri wa miaka 13 tu, akafunga safari kwa ajili ya kutafuta Ilm kuelekea katika Miji ya Qazwin, Nishapur, Baghdad, Kufah, Basrah, Wasith, Damascus, 'Asqalan, Beirut, na Misri ambapo hii ilikua ni safari ya misafara ya kutembea kwa miguu ambayo ilikua pia inajulikana kama *Rihla*.

Na anasema mwenye we Imam Abu Zurah kua: ‘**Katika safari yangu ya pili ya Rihla kueleeka Syria, Iraq na Misri nilitumia miaka 4 na miezi 6, ambapo katika wakati huo sikuwahi h ata mara moja kua ni mwenye kupika mwenyewe chakula changu.**’ Imam Abu Zurah Al Razi alipowasili katika ardhi ya nchini Misri na kukaa na kusoma kwa Imam Yahya Ibn Abd Allah, na kisha baada ya kumaliza kusoma na kuamua kurudi nyumbani basi Imam Abu Zurah alimwacha Mwalimu wake huyo akiwa na huzuni sana kuondokewa na Mwanafunzi kama Imam Abu Zurah na hivyo akasema: **‘Namuomba *Allah Subhanah wa Ta’ala* atuletee mtu mwengine kama wewe atunufaishe kutokana na ulivyotunufaisha’**

Imamb Zurah alikua ni Mtu mcha Mungu sana hata katika wakati wa ujana wake na alikua ni mwenye kuachana kabisa na Dunia yake kwani yeye alikua akifikiria kuhusiana na Ilm tu. Ambapo anasema Imam Abu Zurah mwenyewe kua: **‘Kila wakati Masikio yangu yanaposikia kuhusiana na Ilm, basi Moyo wangu hua ni wenye kuitamani sana Ilm hio, kiasi ya kua nilipokua nikipita katika soko kuu la Baghdad ilikua inanibidi nizibe masikio yangu kwa sababu ya kuogopa kua huenda yakasikia I’lm ya nyimbo na Mashairi wanayoimba Wanawake na kisha Moyo wangu ukavutiwa nayo’**

Katika safari zake hizo Imam Abu Zurah alijipatia Ilm yake kutoka kwa Walimu zaidi ya 500 ambapo ndani yake wakiwemo Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Yahya Ibn Ma’în, Imam Abū Nu’aim Al Fadhl Ibn Dukain, Imam Abu Al Walid At Tayalisi, Imam Yahyâ Ibn ‘Abdillah Ibn Bukair, Imam Ahmad Ibn Yūnus, Imam ‘Abd Allah Ibn Sâlih Al ‘Ijlî, Imam Khallâd Ibn Yahyâ, Imam Abu Al Hasan At Tirmidhî, Ahmad Ibn Manî’, Imam Abu Rabî’ Ibn Atki, Imam Abd Allah Ibn Maslamah Ibn Qa’nabî, Imam Mahmūd Ibn Ghailân, na wengineo.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake ni pamoja na Imam Abū Hâtim ar-Râzî, Imam Muslim Ibn al-Hajjâj, Imam Abū ‘Îsâ at-Tirmidhî, Imam Abū ‘Abdir-Rahman an-Nasâ’î, Imam Ibn Mâjah Al Qazwînî, Imam Is·hâq Ibn Mūsâ Al-Ansârî, Imam Ar-Rabî’ Ibn Sulaimân, Imam Yūnus Ibn ‘Abd Al A’lâ, Imam Ibrâhîm al-Harbî, Imam Abū Zur’ah ad-Dimashqî, Imam Abd Allah Ibn Ahmad, Imam ‘Abd Ar-Rahman Ibn Abî Hatim, Imam Abū ‘Awânah Al-Isfarini Imam Abū Bakr Ibn Abî Dâwud, Imam Abū Ya’lâ Al-Mawsilî, Imam Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Wahb Ad Dînawarî, Imam ‘Alî Ibn Al-Hasan Ibn Al-Junaid, na wengineo.

Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema kua: ‘**Hakuna zaidi ya Abu Zurah baada ya kuvuka daraja la Baghdad, kwani kijana huyu amehifadhi hadith 700, 000’** ambapo wakati Imam Abu Zurah alipoenda kusoma kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi siku moja alisema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: **‘Sikusali mimi sala zozote za Sunnah tangu nilipoanza kumsomesha Abu Zurah, kwani nilizama kwenye kuhifadhi kwake hadith na kujikuta nikiwa ni mwenye kuachana na Sala za Sunnah.’**

Ambapo Imam Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Hanbal anasema: **‘Mimi nilimuuliza baba yangu: ‘Ewe Baba je ni nani Mahafidh wa Hadith’ ambapo nae akasema: ‘Ni vijana waliokua pamoja nasi waliokua wakitoka Khurasan, ambao sasa hivi wametawanyika’ nami nikamuliza tena: ‘Ndio kina nani hao?’’**

Ambapo nae akasema: ‘Ni kina Muhammad Ibn Ismâ’îl, ambapo huyu ni Al Bukhârî; , kina Abd Allah Ibn Abd Al Karîm, ambapo huyu ni Al Razi; ‘Abd Allah Ibn ‘Abdir-Rahman, huyu ni Al Samarqandî; na Husain Ibn Shujâ’, huyu ni Al Balkhî.”

Imam Abu Hatim Al Razi nae akasema kua: **‘Abu Zurah alikua akinisomesha mie Hadith, na haukacha mtu mwengine mwenye Ilm Zaidi yake katika Hadith, Fiqh, Ufahamu Kuhifadhi na Ukweli na uaminifu yaani mimi simjui mtu wengine yeyote zaidi yake tangu kuanzia Mashariki hadi Magharibi anaefahamu mambo haya kama yeye.’**

‘Na ukimuona mtu anamchukia Abu Zurah basi fahamu kua mtu huyo ni mpotofu, kwani mimi siwajui watu wacha Mungu isipokua wane hawa nilioonana nao ambao ni Adam, Ahmad Ibn Hanbal, Thabit Ibn Muhammad Az Zahid na Abu Zurar Al Razi.’

Ambapo alisema Imam Al Rabii Ibn Sulayman kua: **‘Hakuna Mwanazuoni ambae mimi niliwahi kukutaa nae kama Abu Zurah.’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Yunus Ibn Abd Allah alisema kuhusiana na Imam Abu Zurah kua: **‘Hakika Abu Zurah ni mwanazuoni maarufu hapa Duniani kama ilivyo Dunia yenyewe kwa umaarufu wake.’**

Imam Abu Zurah anasema kua: **‘Hakika mimi nyumbani kwangu kuna vitabu vingi sana ambavyo niliviandika miaka 50 iliyopita, na hadi hii leo sijavifungua, ambapo hata hivyo ni mwenye kukumbuka kitu gani kipo kimo kwenye kitabu gani, na katika mistari wa ngapi na wa kurasa gani’**

Imam Abu Zurah alisema kua: **‘Mimi nimehifadhi Hadithi 600,000 ambazo ni sahih, ambapo ndani yake zina sanad 14,000 zenye umaalum wa wenye I’lm ya Qiraa na hadith 10,000 ambazo ni za kughushi.’**

Ambapo alisema Imam Abu Musab kua: **‘Hakika mimi sijawah kuona mtu mwenye ukubwa zaidi wa Ilm kama Abu Zurah’**

Ambapo kwa upande wa Imam Ar Rabii Ibn Sulayman basi yeye alisema kua: **‘Abu Zurah ni Dalili ya ukubwa wa *Allah Subhanah wa Ta’ala.’***

Imam Is-haq Ibn Rahawayh nae anasema kua: **‘Hadith isiyojulikana na Abu Zurah hua haina msingi wake katika historia ya Uislam’**

Na amesema Imam Abu Ya’la Al Mosuli kua: ‘**Kila wakati tunaposikia ukubwa wa Ilm ya mtu katika uwezo wake wa kuhifadhi, basi hua kuna kisa ndani yake ambacho ni tofauti na uhalisi ulivyo, isipokua kwa Abu Zurah kwani kuonana nae tu kunatosheleza zaidi kuliko kusikia Jina lake.’**

Safari moja mmoja kati ya Wanafunzi wa Imam Ahmad Ibn Hanbal alitembelea maeneo ya Kuhrasan kwa Imam Abu Zurah na kumwambia kwa kusema kua: **‘Imam Ahmad hua ni mwenye kunyanyua mikono yake juu kukuombea wewe Abu Zurah mara kadha ikiwemo Dua isemayo: ‘Ya Allah, muweke bali kila mtu anaetaka kumsababishia Madhara Abu Zurah, Ya Allah mpe Afya njema Abu Zurah, Ya Allah muepushe na kila shari Abu Zurah’ kiasi ya kua kila siku hua ni mwenye kukumbuka Dua zake juu yako, na hua najisikia raha kutokana na Dua yake hio juu yako, ambapo *Allah Subhanah wa Ta’ala* ameinsaidia mie pia kutokana na dua hio kutokana na mambo mengi’**

Wanazuoni walikua wakiwafananisha watu waliotangulia kabla yao kwa Tabia na ufanyaji waamali njema zao, kwa mfano: Sahaba Abd Allah Ibn Masud Radhi *Allahu Anhu* alikua akifananishwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* ambapo Imam Alqaamah alikua ndie Imam anaefananishwa na Abd Allah Ibn Masud Radhi *Allahu Anhu,* na Imam Ibrahim An Nakhai alikua akifananishwa na Imam Alqamah na Imam

Mansur Ibn Mutamir, na Imam Sufyan Ath Thawry alikua akifananishwa na Imam Mansur Ibn Mutamir, ambapo Imam Waki Ibn Jarrah alikua akifananishwa na Imam Mansur Ibn Mutamir na Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua akifananishwa na Imam Waki Ibn Jarrah na Imam Abu Zurah akawa ni mwenye kufananishwa na Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Imam Abu Zurah pia alikua ni mtaalamu wa fani ya uandishi na hivyo alikua ni mwenye kuandika vitabu vingi sana, kama anavyosema Imam Al Khalil kua: '**Sifa za Abu Zurah nyengi sana hata kuzihesabu, na hakuna mwenye kuweza kushindana nae katika mambo aliyoyafanya na vitabu alivyoandika'**

Ambapo miongoni mwa vitabu vyake ni kama *Fawaid Ar Raziyin, Al Fawaid, Al Fadhail, Dalail Nubuwwah, As Siyar, Al Mukhtashar, Az Zuhd, Al Ath'imah, Al Faraidh, As Saum, Al Adab, Al Wudhu, As Shuf' ah, Al Afrad, Al 'Ilal, Al Jarh wa Ta'dil, At Tafsir, As Sahabah, Al Musnad*, na vyenginevyo.

Siku moja Imam Abu Zurah aliambiwa na Mwanamke mmoja: **'Ewe Abu Zurah! Jee hutaki kupata Malipo ya kumtembelea Muislam Mgonjwa anaeumwa?'** hivyo Imam Abu Zurah akaualiza: **'Yuko wapi huyo Mgonjwa?'** yule Mwanamke akamwambia Imam Abu Zurah **'Twende nikakupeleke, Allah akulipe kwa uakrimu wako'**

Hivyo Imam Abu Zurah akamfuata Mwanamke huyo na alipofika kwenye Nyumba hio basi wakaingia ndani na hapohapo Mwanamke huyo akaufunga Mlango, ambapo Imam Abu Zurah akajua kua kumbe ulikua ni mtego ambao ametegewa, kwani alikua anatakiwa na Mwanamke huyo. Hivyo Imam Abu Zurah akasema: **'Ya Allah Mgeuzie huyu Mwanamke awe Mweusi'** na hapo hapo Mwanamke huyo akawa Mweusi, na akajawa na khofu na kukimbilia katika chumba chengine.

Hivyo Imam Abu Zurah akafungua mlango wa nje na kutoka, kisha njiani akasema: **'Ya Allah Mjaalie yule Mwanamke awe Mweupe kama alivyokua hapo kabla'** na Mwanamke yule akawa mweupe kama alipokua hao kabla.

Mnamo mwaka 264 Al Hijra Imam Abu Zurah alipokua anakaribia kufariki basi alikua akisema: '**Ya Allah kwa hakika mja wako huyu ni mwenye hamu ya kua karibu nawe'** na akasema: **'Kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* akiniuliza imekujae hadi ukawa na hamu na mie kiasi hicho?' basi mimi nitajibu kua: 'Kutokana na kutegemea sana Rehma zako'**

Ulipowadia mda wa kukutana na Mola wake basi wake Imam Abu Zurah akawa ni mwenye kuumwa na tumbo, hivyo wakaja wanazuoni wenzake kumtembelea, Na hivyo Wanazuoni wakataka awasomee Hadith ambapo nae Imam Abu Zurah akasema:

‘Amesema Muadh Ibn Jabal kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Yeyote yule atakaesema *La Ilaha Illa Allah.*’’ ambapo Imam Abu Zurah hakuwahi kumaliza maneno ya Hadith hio yasemayo kua ‘*Ataingia Peponi’* kwani alipofika kwenye maneno hayo ya kushuhudia basi akafariki Dunia huku akiwa ni mwenye kutoa shahada.

IMAM ABU HATIM AL RAZI 195 AH

Imam Abu Hatim Muhammad Ibn Idris Ibn Al Mundhir Ibn Daud Ibn Mahran Al Razi Al Hanzali Al Ghatafan alizaliwa mnamo mwaka 195 Al Hijra katika Ardhi ya Al Razi nchini Iran.

Imam Abu Hatim alikua ni Al Muhaqiq na Al Hafidh mwenye Ilm kubwa sana ya Qur’an, Hadith, Tafsir, Lugha n.k ambapo kwanza alisoma katika mji wa Al Ray alipozaliwa na kisha alipotimia umri wa miaka 18 akaanza safari kutoka katika maeneo mbali mbali ya ardhi za Kiislam kwa ajili ya kujitafutia Ilm kuanzia Khurasan, Iran, Iraq, Yemen, Misri, Hijaz, Sham na Uturuki.

Ambapo mwenyewe anasema kua: **‘Mara ya kwanza mimi kuanza safari ya kutafuta Ilm nilikaa bila ya kurudi nyumbani kwa muda wa miaka 7, tangu nilikua nahesabu maili nilizokua nikisatembea kwa miguu hadi kufikia Farsakh 1000, na baada ya hapo niakaachana na kuhesabu.’**

‘Na sikumbuki ni mara ngapi mimi nilitembea kutoka Kufah kuelekea Baghda, na pia kutoka Makkah kuelekea Madinah, nilienda pia Morroco kutokea Misri na kutoka Misri kuelekea Ramallah, kuelekea Bayt ul Maqdis kuelekea Tabarriyah kuelekea Dimashq, kutoka Dimashq kuelekea Homs kuelekea Antakiyah, na kutoka Antakiyah kuelekea Tarus, na kisha nikarudi Homs.

Na kisha nikaondoka Homs kuelekea Baisan, kueleka Al Raqqa, na kisha nikavuka mto Euphrate kuelekea Baghdad.’

Hii ilikua ni safari yangu niliyoianza kutoka Al Razi mnamo 213 Al Hijra na kurudi nyumbani mnamo mwaka 221 Al Hijra.

Na kisha nilipotimia umri wa miaka 47 nikaanza tena safari mnamo mwaka 242 Al Hijra na kurudi nyumbani mnamo mwaka 245 Al Hijra’

Imam Abu Hatim alisoma kwa Imam Muhammad Ibn Abd Alla Al Ansari, Imam Abu Zaid Al-Nahwi, Imam Uthman Ibn al-Haytham, Imam Hawza Ibn Khalifa, Imam Ubayd Allah Ibn Musa, Imam Ata Ibn Ziyad, Imam Abu Mushar Al Dimashqi, Imam Abu al-Jamahir Muhammad Ibn Uthman Al Tanukhi, Imam Said Ibn Abi Maryam Al-Misry, Imam Abu Al Yaman Al-Homsi Imam Qabisah na wengineo.

Imam Adh Dhahabi anasema kua: **'Imam Abu Hatim alikua ni Bahari ya Ilm alisafiri katika ardhi mbali mbali na hivyo kua ni mwenye kua mbali sana kutokana na Ilm yake ya *Sanad na Matn* za Hadith, ambae alikua ni mwenye kukusanya na kuhakikisha usahih wa Hadith'**

Imam Abu Qasim Al Lalikai kua: **'Abu Hatim alikua ni Imam, Al Hafidh na Al Muhaqiq'**

Ambapo anasema Imam Al Khalili kua: **'Imam Abu Hatim alikua ni Imam wmwenye Ilm kubwa ya tofauti za Mitizamo ya Masahaba,Tabiina na Tabii Tabiina nami nimemsikia Babu yangu akisema kua Imam Ali Ibrahim Al Qattani alisema kua**: **'Hakika mimi sijawahi kumuona mtu kama Abu Hatim' hivyo akaambiwa: 'Lakini umewaona kina Ibrahim Al Harbi na Ismail Al Qadhi' ambapo nae akasema: 'Sijawahi mimi kuona mimi aliemzidi Abu Hatim kwa ucha Mungu.''**

Ambapo anasema Imam Al Khalili kua: **'Abu Hatim Al Labban aliniambia mimi kua: 'Mimi nimekusanya Hadith zilizonukuliwa na Abu Hatim Al Razi na zilifikia 3000''**

Imam Abu Zurah alimwambia Imam Abi Hatim Al Razi kua: **'Hakika mimi sijawahi kuona mtu mwenye nia ya kutafuta Ilm ya Hadith kama uliyokua nayo wewe.'**

Na akasema Yunus Ibn Abd Allah kua: '**Abu Zurah na Abu Hatim ni Maimamu wawili wa Khurasan' na kisha akawaombea Dua kwa kusema: 'Uendelevu wao ni kwa ajili ya kuuboresha Uislam.'**

Ambapo anasema Imam Abd Rahman Ibn Abi Hatim kua: **'Mimi nilimsikia Musa Ibn Is-haq Al Qadhi kua: 'Sijawahi mimi kumuona Mtu yeyote mwenye ufahamu mkubwa kama baba yako''**

Imam Ahmad Ibn Salamah Al Nishapuri kua: **'Sijawahi mimi kumuona mtu yeyote baada Is-haq Ibn Rahawayh na Muhammad Ibn Yahya mwenye uwezo wa kuhifadhi au mwenye Ilm zaidi ya Abi Hatim Al Razi.'**

Na kwa upande wa Uthman Ibn Khurazadh kua: **‘Miongoni mwa wenye ufahamu mkubwa wa kuhifadhi ni wanne ambao ni Muhammad Ibn Al Minhal Ad Darir, Ibrâhîm Ibn ‘Ar’arah, Abū Zur’ah, na Abū Hâtim.’**

Imam Al Baghdadi alisema: **‘Abu Hatim ni Imam wa Hadith anaeaminika’**

Imam Abd Rahman Ibn Abi Hatim anasema kua: **‘Baba yangu aliwasili Basra mnamo mwaka 214, ambapo aliniambia kua: ‘Mnamo mwaka 214 nilikaa Basra kwa mda wa miezi 8 na kisha nikaamua kukaa kwa Mwaka mmoja lakini hata hivyo pesa za matumizi zikanimalizikia. Hivyo nikaanza kuuza Nguo zangu hadi ikawa sina nguo hata moja iliyobakia. Na hivyo kutokua na pesa za matumizi kabisa, lakini hata hivyo nami nikawa ni mwenye kuendelea kuhudhuria kwenye Darsa za Wanazuoni mbali mbali, nikiwa na mmoja kati ya marafiki zangu**’

Hivyo katika siku ya mwanzo baada ya kumalikiwa na matumizi basi nikarudi nyumbani nikiwa sina kitu chochote cha kutia kinywani, isipokua maji ya kunywa tu, na hivyo nikanywa na kulala na siku ya pili asubuhi rafiki yangu akanipitia na kuniambia kua tuende kwenye Darsa lakini nikamwambia kua: ‘Leo haiwezekani kwangu kuhudhuria kwani niko hoi taabani kwa kutokua na nguvu’ hivyo akaniuliza nna tatizo gani?’ nami nikamwambia kua leo ni siku ya tatu ambapo mimi sijatia kitu chochote tumboni mwangu’ hivyo nae akasema kua: ‘Twende zetu mimi nnayo Dinari moja tutatumia pamoja’’ na hivyo ndivyo tulivyoondoka kutoka katika mji wa Basra.

Imam Abd Rahman Ibn Abi Hatim anaendelea kusema kua: **‘Baba aliniambia pia kua: ‘Tulipoondoka katika Mji wa Madina Munawwara na kupanda Jahazi katika maeneo ya Al Jar tulikua watu watatu, yaani mimi, Abu Zuhayr Al Marwazi na Shaykh mmoja wa Nishapur, hivyo wakati tukiwa Baharini Usiku mmoja, nilipolala basi nikaamka huku nikawa katika hali ya kujimwagia Manii, na hivyo asubuhi nikawataarifu wenzangu ambao nao wakaniambia kua nikoge Janaba kwa kuogelea Baharini’**

Lakini mimi nilikua sijui kuogelea, hivyo wakanishauri kua wanifunge kamba na kisha wanitumbukize Baharini kisha wanivute, na hivyo baada ya hapo itakua nimeshakoga Janaba, na tukafanya hivyo.

Baada ya hapo tutakapotea baharini na tukakaa kwa mda wa miezi mitatu na kujikuta tuko kwenye kisiwa ambacho, kilikua hakina watu, hivyo tukashuka natukatembea kwenye kisiwa hicho kwa siku kadhaa hadi chakula chetu kikamalizika, kisha tukatembea kwa siku mbili huku tukiwa na njaa, hadi ilipowadia siku ya tatu, Shaykh Al Marwazi akaanguka na kuzimia, ambapo tukajaribu kumzindua, bila ya mafanikio yeyote’

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na kisha baada ya kutembea baada ya Farsakah 5 nami nikaishiwa na Nguvu na kuanguka pia na kupoteza fahamu. Hivyo Shaykyh wa Nishapuri akaniwacha mimi na yeye akaendelea na safari hadi akakutana na watu, ambao aliwaomba Maji wakamsaidia akanywa na kisha akawaambia watu hao kua: 'Nendeni nilikotoka, kuna wenzangu wawili wameanguka nimewaacha kwani sikuweza kuwachukua.'

'Hivyo baada ya mda nikahisi kuna maji yananimwagikia Usoni, na kisha nikapata fahamu na watu hao wakaninywesha maji, nami nikawaambia kuhusiana na Abu Zuhayr Al Marwazi ambapo nao wakasema kua kuna watu tayari wameshamuona na wanamsaidia, kisha wakanibeba hadi kwenye Meli yao ambayo walituhudumia ndani yake.'

Baada ya hapo tukakaa nao kwa siku kadhaa hadi tuliporudia katika hali zetu za kawaida kiafya, na kisha wakatusaidia kimatumizi na kutupa barua kwa ajili ya Gavana wa mji unaofuatia na kisha wakatushusha na kutuelekeza kwenye mji huo unaoitwa Rayah, hivyo tukatembea hadi tukamalizikiwa na chakula chetu na maji yetu hadi tukakuta Gamba la Kasa ambalo tukalipara nyama iliyomo ndani yake na kula hadi tukaondokewa na njaa na kiu yetu, na kisha tukaendelea na safari yetu hadi tukafika katika Mji wa Rayah, na tukampa barua hio Gavana wa Mji huo ambaae nae akatusaidia kwa kutuchukua kwenye nyumba yake akatupa chakula cha Mikate na Nyama, kisha tukampumzika kwa siku kadhaa na kisha akatupa matumizi na chakula nasi tukaanza safari yetu hadi Misri. *(Shifa Min Sabri al Ulamai)*

IMAM ABU HAFS AL HADDAD

Imam Abu Hafs Amr Ibn Salama Al Haddad Al Nishapuri alizaliwa katika maeneo ya Kurdabaz katika Mji wa Nishapuri. Baba yake Imam Abu Hafs Ibn Salama alikua akiitwa Al Haddad kwa sababu alikua ni mhunzi mwenye kazi ya kutengeneza Vitu ya Chuma ambapo Imam Abu Hafs aliirithi kazi hio pia kutoka kwake.

Imam Abu Hafs Al Haddad alikua ni mwenye Ilm kubwa sana na alisoma pamoja na Imam Ubayd Allah Ibn Mahdi, Imam Ali An Nasrabadi, Imam Shah Ibn Shujaa Al Kirmani, na miongoni mwa Wanafunzi wake ni Imam Al Junayd Al Baghdad, Imam Abu Uthman Al Hiri n.k.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Kutokana na ucha Mungu wake na Ilm aliyokua nayo basi Imam Abu Hafs Al Haddad alikua ni mwenye kuachana na Dunia kabisa na hivyo alikua ni anapotajiwa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi uso wake husawijika kutokana na khofu, na baadhi ya wakati hua ni mweye kuzimia kabisa.

Imam Abu Hafs alikua ni mwenye kujitolea kila kitu chake anachokichuma kwa ajili ya Mayatima na Wajane na Masikini, Ambapo siku moja Imam Abu Hafs alikua akitembea njiani na mara akamuona kijana ambae alikua akilia, na hivyo akamsogelea na kumuuliza: **'Hivi jee una Tatizo gani?'**

Ambapo kijna huyo akasema kua: '**Mimi nilikua sina umiliki wa kitu chochote isipokua Kipando changu, ambacho hata hiyo sasa hivi nacho pia kimenipotea'** Hivyo Imam Abu Hafs akamuombea Dua Mtu huyo na mara atakotekezea Farasi wake mtu huyo.

Imam Abu Hafs alisema kua: **'Kama ingekua Dunia na kila kitu kilichomo ndani yake ingekua vinamilikiwa na wenye kufanya maovu, basi wangeitoa yote na kila kitu chake katika siku ya Malipo kwa ajili ya kujiokoa kutokana na Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yao.**''

Na anasema Imam Abu Uthman Al Hiri kua: **'Mimi nilienda kwa Abu Hafs, na kulikua kna ndizi mbivu mbele yake, hivyo ikachukua Nidizi moja na kuimenya na kisha nikaitia Modmoni na kuila'** ambapo Imam Abu Hafs akaniuliza: **'Kwa haki gani ulizokua nazo ambazo zimaekupelekea kuchukua ndizi zangu kuanza kuzila?' nami nikasema: 'Hakika mimi nnaujua Moyo wako kwa hivyo nakutegemea wewe na Moyo wako, kwani ni mwenye kutoa vile ulivyokua navyo'**

Imam Abu Hafs akasema: **'Kama mimi mwenye ewe sijiamini nafsi yangu jee itakuaje wewe uwe ni mwenye kuniamini mimi? Kwani kwa miaka yote mimi nimekua ni mwenye kuyatumikia matamanio ya nafsi yangu, Hivyo mimi sijui ni nini nnaweza kukifanya hapo baadae kutokana na Nafsi yangu, hivyo jee kama ikiwa mtu hajui kile kitakachotokea Ndani ya Nafsi yake itawezekanaje kwa mwengine kujua kila kitakachomtokea ndani yake?'**

Safari moja Imam Al Junayd alimtembelea Imam Abu Hafs Madrasani mwake, na alipofika alishangaa namna walivyokua wamekaa kwa heshima na adabu Wanafunzi wa Imam Abu Hafs kwani ilikua inapendeza sana, hivyo Imam Al Junayd akamuuliza Imam Abu Hafs: **'Hivi jee uliwafundishaje Wanafunzi wako hali ya kukaa mbele ya Watu wazima?'**

Imam Abu Hafs akasema: '**Ewe Al Junayd, tatizo lako ni kua wewe huangalii darja za waliotangulia, kwani baadhi ya wakati darja za waliotangulia hua ni kwa ajili ya uthibitisho wa Ushahidi wa wanaofuatia baada yao.**'

Imam Al Junayd akawaangalia Wanafunzi hao na kisha akauliza tena: **'Hivi Jee Mwanafunzi huyu amekua nawe kwa mda gani sasa?'** Imam Abu Hafs akamuangalia Mwanafunzi huyo na kisha akasema: **'Kwa mda wa miaka 10' ambapo** Imam Al Junayd akasema: **'*Ma-shaa Allah* naam hata muonekano wake ni wa juu'** ambapo Imam Ab Hafs akasema: **'Naam, Mwanafunzi wetu huyu ameshatumia Dirham 17000 za Dhahabu kwa ajili yetu, na hivyo anatudai lakini hata hivvyo hata hajasema kua anatudai.'**

Ambapo anasema Imam Al Hiri kua: **'Mimi nilikua kwenye nyumba ya Abu Bakr Al Hanafiya ambae alikua ameenda sokoni wakati Abu Hafs akiwepo na kubakia pamoja nami, na tukawa tunakumbushana kuhusiana na marafiki zetu ambapo nami nikasema kua: 'Nnatamani kama na wao wangekuwepo hapa pamoja nami.' Ambapo Imam Abu Hafs akasema: 'Kama tungekua na Kartasi na Kalamu basi tungewaandikia Barua waje' hivyo mimi nikasema kua: 'Nnazo hizi hapa' na Imam Abu Hafs akasema: 'Ila sasa tatizo ni kuwa Mwenye nyumba ameenda sokoni hivyo kama akifariki huko basi, hii nyumba haitokua yake tena itakua ni ya warithi, hivyo haina haja kuwaita''**

Anasema Imam Abu Uthman Al Hiri kua: '**Mimi nilimwambia Abu Hafs kua nnataka kuwausia watu na kuwafundisha Ilm nnayoijua' ambapo nae akaniuliza: 'Kwa nini ukaamua hivyo imekuaje?' nami nikajibu: 'Kwa sababu ya kuwaonea huruma watu' hivyo Abu Hafs akaniuliza: 'Jee unawaonea Huruma watu kwa kiasi gani?'**

Nami nikasema: 'Kiasi ya kua niko tayari kuungua Moto wa Jahannah kwa ajili ya Wenye kufanya dhambi wote.' Hivyo Imam Abu Hafs akaniambia: 'Subiri mimi nikuusie wewe kwanza kua: 'Kwanza iuise Nafsi yako kisha na wale waliokua karibu yako, na usiwaruhusu watu waliokua karibu yake wawe ni wenye kukushughulisha wewe, kwa sababu watu hua wanaonekana kutokana na muonekano wa nje ya miili yao, wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kuangalia ndani yao watu hao.'

Baada ya hapo akatokezea Masikini na mimi nikavua kanzu yangu haraka sana ili niwe wa mwanzo kumpa Maskini huyo, na mara akatokezea Abu Hafs na kuniambia: 'Hakika wewe ni muongo, kwani umekua ukisema kua ni mwenye kua na huruma na watu waliokuzunguka lakini umekua ni mwenye kutoa sadaqa kwa haraka sana ili uwe wa kwanza kupata malipo ya sadaka hio, hivyo kama kweli ungekua na hali kama uliyosema hapo kabla basi unsingefanya hivyo.'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Ambapo anasema Imam Abu Zakarriyah kua: '**Hakika mimi nilikua nnauogopa Umasikini, lakini siku moja Abu Hafs akaniambia kua: '*Kama Allah Subhanah wa Ta'ala* amekuandikia kua uwe Masikini basi bila ya shaka hakuna atakaeweza kukufanya ewe uwe Mtu Tajiri', hivyo nami nikawa si mtu mwenye kuogopa Umasikini tena tangu siku hio.'**

Siku moja aliulizwa Imam Abu Hafs: '**Hivi Jee inawezekana kwa mtu anaedhulumiwa kumsamehe yule anaemdhulumu?'** ambapo nae akajibu kwa kusema kua: **'Naam, kama yule anaedhulumuiwa akiwa anajua kua kudhulumiwa kwake huko ni neema kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake badala yake'.**

Alisema Imam Abu Hafs kua: **'Mwanazuoni wa kweli ni yule mwenye kukhofia siku ya Malipo pale atakapoulizwa :'Hivi wewe ulilipata wapi Jibu la suali hili?' kuhusiana na lile suali aliloulizwa na watu na kisha akalijibu.'**

Na akasema tena kua: 'Hakuna mtu anaekua na haki ya kudai Mamlaka juu ya Waislam wenzake, kwani kila mmoja anatakiwa ajikinge kutokana na kutaka kua na Mamlaka juu ya wengine kwa sababu *Rasul Allah Salllahu Alayhi wa Salam* amesema kua: 'Ogopenikua na Mamlaka juu ya Waislam wenzanu' hii ni kweli kabisa.'

Alisema Imam Abu Hafs kua: **'Jambo bora zaidi ambalo huweza kumkaribisha Mja kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni katika kumtegemea kwake katika kila kitu chako, na kushikamana na Sunnah za Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* katika kila kitu chako na kutafuta riziki ya halali.'**

Imam Abu Hafs alisema: **'Mbakhili ni yule mtu ambae asiemfikiria mtu mwengine yeyote isipokua nafsi yake katika wa shida.'**

Imam Abu Hafs alisema: **'Bidaa ni kuvunja maamrsho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kuzidharau Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kufuata matamanio ya Nafsi yako.'**

Imam Abu Hafs alisema: **'Yeyote yule asiejilaumu Nafsi yake na kutopingana nayo basi ni mwenye kuhadaika, na nyeyote yule mwenye kuridhika kutokana na kujiangalia Nafsi yake basi ameangamia.'**

Imam Abu Hafs alisema: '**Khofu juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni kama tochi iliyomo ndani ya Moyo wa Mtu, na hivyo kila kitu kinachoingia kwenye Moyo kiwe kibaya au kizuri hua ni chenye kuonekana kutokana nayo.'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abu Hafs alisema: **‘Si mwenye kuangamia yule ambae ni mwenye kuziona Rehma na Neema za *Allah Subhanah wa Ta’ala* juu yake.’**

Imam Abu Hafs alisema: **‘Kama ilivyokua Sumu huweza kukupelekea kukuingiza kwenye hali ya kifo basi ndio ilivyo kwa upande wa Dhambi pia kwani nazo huenda zikakuingiza kwenye hali ya kukufuru.’**

Siku moja Imam Abu Hafs alikua amekaa Bustanini na Wanafunzi wake wanamtukuza *Allah Subhanah wa Ta’ala,* katka kuendelea kwao huko *Dhikr Allah* basi mara akatokea Mnyama aina ya Paa akaja moja kwa moja hadi kwenye miguu ya Imam *Abu Hafs* na kukiweka kichwa chake kwenye Mapaja ya Imam Abu Hafs, ambapo nae akamfukuza Paa huyo.

Hivyo baada ya kumaliza Dhikr Allah basi Wanafunzi wake wakamuuliza**: ‘Mbona umemfukuza yule Paa?’**

Ambapo Imam Abu Hafs akasema: **‘Dhikr All ilipozidi kua bora basi nami nikatamani kua angetokea Kondoo ili nikamchinja kisha nikakupeni nyinyi, na hivyo badala yake akatokea yule Paa. Na nilipomuona basi mimi nikakukumbuka kua Fir’awn aliomba dua kwa *Allah Subanah wa Ta’ala* pia kua aufanye Mto Nile ujae Maji ambayo yatakua yanatiririka kwa kinyume chake, na *Allah Subhanah wa Ta’ala* akamkubalia Dua hio ya Firawn.’**
Aliulizwa Imam Abu Hafs: **‘Jee kunyamaza na kusema ni kupi bora zaidi?’** ambapo nae akajibu: ‘**Kama msemaji angejua madhara yaliyomo katika kusema basi hata kama angekua ni mwenye kuishi kama alivyoishi Nabii Nuh basi angekaa kimya tu kwa kadri anavyoweza.’**

Imam Abu Hafs alisema kua: **‘Bila ya shka mtizamo wangu juu yangu baada ya kuiangalia Nafsi yangu kwa mda wa miaka 40, basi naona kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni mwenye kuniangalia kwa jicho la haghabu sana, na hili ni lenye kuonekana kutokana na amali zangu nnazozifanya.’**

Ambapo anasema Murtaish kua**: ‘Mimi nilienda kumtembelea mgonjwa pamoja na Abu Hafs na tulipofika basi mgonjwa huyo akawa amefurahia kutuona, na hivyo baada ya kumsalimia basi Imam Abu Hafs akamuuliza: ‘Jee unaataka upona?’ Mgonjwa huyo akasema : ‘Naam’’ hivyo Imam Abu Hafs akanyanyua mikono na kusema: ‘Ya Allah mponeshe Mgonjwa huyu’ na kisha baada ya maneno hayo basi mgonjwa huyo akawa mzima na kupona.**

Imam Abu Hafs alialikwa kwa Imam Abu Bakr Al Shibli ambae ni mwenye kuishi katika Mji wa Baghdad na hivyo akawa ni mwenye kukaa ndani ya nyumba yake kwa mda wa siku 40 huku akiwa ni mwenye kula vyakula vya aina tofauti ndani yake, na

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

ilipowadia siku ya kuondoka basi Imam Abu Hafs akamwambia Imam Ash Shibli: **'Naondoka mie na nilikua nataka kukuambia kua ukijaaliwa kutembelea maeneo ya Nishapuri basi nitembelee nyumbani kwangu nikuoneshe namna inavyotakiwa kuwahudumia Wageni wako.'**

Imam Al Shibli akauliza: **'Kwani nimefanya nini?'** Imam Abu Hafs akasema: **'Hakuna zaidi ya kile ulichokifanya ambacho ni cha kunitayarishia mimi Vyakula vya aina tofauti, na hivyo kua ni mwenye kujibebesha mzigo mkubwa, jambo ambalo halitakiwi, kwani wanapokuja wageni kwako basi inatakiwa kuwe na wepesi juu yako katika kuwahudumia kwako, na hivyo usiwe na hali ya kujihisi afueni pale wanapoondoka, haitakiwi kuhudumia wageni katika hali kama hio ya kua wanapokuja unakua na uzito na wanapoondoka unakua na wepesi.'**

Na kisha baada ya hapo Maimamu hao wakaagana na baada ya mda Imam Al Shibli akatembelea Nishapuri na hivyo akamtembelea Imam Abu Hafs, na kufikia kwake na ulipoingia wakati wa Usiku basi akaona kua Imam Abu Hafs amewasha Mishumaa 40.

Hivyo Imam Al Shibi akauliza: **'Ndio nini hii? imekuaje'** ambapo Imam Abu Hafs akauliza: **'Ndio nini kitu gani?'** Imam Al Shibli akasema: '**Umesema kua hamna kuhudumia wageni kwa kujipa uzito, sasa mishumaa yote hii 40 ya nini?'**

Imam Abu Hafs Al Haddad akatabasamu na kisha kasema: **'Basi kama unaona kua ni mingi izime'** hivyo Imam Al Shibli akasimama na kuanza kuizima Mishumaa hio mmoja baada ya moja lakini ikawa kila akiizima basi haizimiki isipokua Mshumaa mmoja tu ndio uliozimika.

Hivyo Imam Abu Hafs akasema: **'Mimi niliiwasha Mishumaa 40 makusudi kwa sababu hua ni mwenye kuwasha Mishumaa hio kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na hivyo mmoja tu hua ndio kwa ajili yangu, ambao ndio ulioweza kuuzima wewe. Na hivyo umeshindwa kuizima mishumaa iliyobakia ambayo ni kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Hakika wewe ulifanya kila kitu kwa ajili yangu katika Mji wa Baghdad nilipokutembelea na ndio maana ikawa kuna uzito kwako na uzito kwangu mie pia, lakini hapa kwangu mie kila nilichokifanya nimekifanya kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hivyo kwangu mimi haikua kuna uzito wala israfu.'**

Imam Abu Hafs alisema kua: **'Tabia njema hua ni kua na Adab mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwa kutekeleza majukumu yake kwa Ikhlasi, kutokana na kumuogopa katika Wakati za Matatizo na Wakati wa neema, kua na Ukarimu kwa waja wake na kuwahudumia katika wakati wa Neema, kua na Ukarimu na Nafsi yake mtu, na kutoogopa kuangukia kwenye masikini kutokana na kutoa, kusamehe pale inapowezekana na kuwahurumia watu, kuwatembelea wsiokutembelea,kuwafanyia wema wanaokufanyia maovu na kuwaheshimu**

Waislam wote kwa ujumla kwani Waislam hua ni wenye kua ndani ya Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* '

Wakati Imam Abu Hafs alipokua anakaribia kufariki basi Wanafunzi wake wakamwambia: **'Tunakuomba utuusie'** ambapo nae akasema: '**Kuweni ni wenye huzuni na kukosa utulivu kutokana na makosa mliyoyafanya mbele ya Mola wenu.'**

IMAM HATIM AL ISAM

Imam Abu Abd Rahman Hatim Ibn Anwan IbnYusuf Al Isam alizliwa katika maeneo ya ardh ya Balk nchini Afghanistan na alisoma kwa Imam Shaqiq Al Balkhi ambapo nae akamsomesha Imam Ahmad Al Hadrawayhh.

Siku moja Imam Shaqiqi Al Bakhl alimuuliza Imam Hatim Al Isam: '**Hivi jee wewe tayari umeshasoma kwangu mimi kwa muda wa miaka mingapi?'** ambapo Imam Hatim Al Isam akasema: '**Kwa mda wa miaka 33**' hivyo Imam Shaqiq Al Balkhi akamuuliza tena Imam Hatim Al Isam kwa kusema: **'Na jee ndani ya kipindi chote hicho umejifuza nini kutoka kwangu?'**

Hivyo Imam Hatim Al Isam akasema: **'Nimejifunza mambo manane tu.'**

Ambapo Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Hivi huoni aibu kua kwa mda wote huo wewe umekua ni mwenye kujifunza mambo manane tu?'**

Hivyo Imam Hatim Al Isam akasema: **'Ewe Mwalimu wangu, huo ndio ukweli kutoka kwangu na bila ya shaka mimi sihitajii zaidi ya mambo hayo manane katika maisha yangu ya hapa Duniani na kesho Akhera pia.'**

Hivyo Imam Shaqiq Al Balkhi akauliza: **'Ewe Abu Abd Rahman mbona mimi sijakufaham, hebu nifahamishe vizuri ni vitu gani vinane hivyo ili nami nipate kukuelewa.'**

Imam Hatim Al Isam akasema: **'Ewe Mwalimu wangu, hakika mimi nimekua ni mwenye kuwaangalia watu na nimewaona kua kila mtu hua ni wenye kuchagua kitu chake akipendacho, na hua na ukaribu nacho kitu hicho akipendacho hadi katika wakati anapokaribia kifo chake. Na kisha baada ya hapo Mtu huyo hua ni mwenye kuondoka Duniani na kuachana na kitu chake hicho, na hivyo hua ni mwenye kuingia Kaburini peke yake, kwani hazikwi na kitu chake hicho na wala**

hazikwi na mtu wake huyo anaempenda, kwani kila hua hataki kuingia pamoja nae kaburini kwa ajili ya kuzikwa nae.

Ambapo nami nimetafuta nimpendae ambae atakubali kuingia pamoja nami kaburini lakini, lakini hakuna mtu kama huyo wala kitu kama hicho na hivyo hao wote waliopo na vyote viliopo hua ni kwa ajili ya kuvikumbatia tu hapa Duniani na bila ya shaka hakuna wa kumpenda zaidi isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Ma-shaa Allah, bila ya shaka hilo ni jambo sahih na ni lenye manufaa zaidi, hivyo jambo la pili ni lipi?'**

Imam Hatim Al Isam akasema: **'Ewe Mwalimu wangu, jambo la pili ni kua nimekua ni mwenye kuwaangalia watu na kuwaona kua kila mmoja ni mwenye kukimbilia matamanio ya Dunia yake na hivyo hua ni wenye kuyaweka mbele matamanio yao na wao kua nyuma ya matamanio yao hayo, na hivyo nikafikiria kuhusiana na maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo:**

﴿وَلِمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ جَنَّتَانِ﴾

Waliman kha̲fa maqa̲ma rabbihi jannata̲ni *(Surat Ar Rahman 55:46)*

Tafsir: ***Ama kwa yule (Muumini wa kweli mwenye kupigana jihadi na Nafsi yake kwa kuachana na aliyokatazwa) mwenye kua na khofu kisimamo cha mbele ya Mola wake, basi atalipwa Pepo mbili.***

Ambapo kulingana na Ilm yangu na uzoefu wangu basi najua kua Qur'an ni yenye maneno ya kweli na uhakika, nami naiamini kikamilifu, na kutokana na kuijua Nafsi yangu kua ni Adui yangu, basi nimeamua nisiwe ni mwenye kulaghaiwa nayo Nafsi yangu na hivyo kuamua kua ni mwenye kupingana nayo na hivyo si mwenye kuyaendekeza matamanio ya Nafsi yake, kwani Nafsi iliyoachana na Matamanio hua ni yenye kujisalimisha kwa Mola wake'

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Ma-shaa Allah, bila ya shaka uko sahih, naam, ninufaishe zaidi kwa jambo la tatu, jee ni lipi?'**

Imam Hatim Al Isam akasema: **'Jambo la tatu ni kua mimi nimegundua kua hali za watu wanaingia katika mitihani kutokana na kupenda kukusanya vilivyomo Duniani, hivyo nikafikiria mimi kuhusiana na ile aya isemayo:**

﴿مَا عِندَكُمْ يَنفَدُ وَمَا عِندَ ٱللَّهِ بَاقٍ وَلَنَجْزِيَنَّ ٱلَّذِينَ صَبَرُوٓاْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ﴾

Ma AAindakum yanfadu wama AAinda Allahi baqin walanajziyanna alladheena sabaroo ajrahum bi-ahsani ma kanoo yaAAmaloona *(Surat An Nahl 16:96)*

Tafsir: ***Na chochote kile mlichokua nacho nyie kitaisha, na ama kile kilichopo mbele ya Allah Subhana wa Ta'ala ndio kitakachobakia. Na wale wenye kua na subra basi bila ya shaka tutawalipa kwa ubora kutokana na kila walichokua wakikifanya.***

Ambapo kwa upande wangu mimi basi kile nilicho kikusanya kwa ajili ya Dunia hua ni mwenye kukitumia kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kukigawa kwa masikini, na hivyo kua ni mwenye kumkopesha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kua ni chenye kubakia.

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Ma-shaa Allah, bila ya shaka kwa kufanya hivyo basi inakua ni mwenye unafanya jambo zuri sana, naam, ninufaishe zaidi kwa jambo la nne, jee ni lipi?'**
Imam Hatim Al Isam akasema: **'Jambo la nne ni kua mimi nimewaangalia watu na nikaona kua hakuna hata mmoja anaempenda mwenzake, na hii ni kwa sababu Ibn Adam ni wenye kuoneana wivu na hivyo hua ni wenye kuhasidiana kulingana na Vyeo, Mali, Ilm n.k ambapo mimi nimeiangalia ile aya isemayo:**

﴿أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَةَ رَبِّكَ نَحْنُ قَسَمْنَا بَيْنَهُمْ مَّعِيشَتَهُمْ فِى ٱلْحَيَاةِ ٱلدُّنْيَا وَرَفَعْنَا بَعْضَهُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِّيَتَّخِذَ بَعْضُهُم بَعْضاً سُخْرِيّاً وَرَحْمَةُ رَبِّكَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ﴾

Ahum yaqsimoona rahmata rabbika nahnu qasamna baynahum maAAeeshatahum fee alhayati alddunya warafaAAna baAAdahum fawqa baAAdhin darajatin liyattakhidha baAAdhuhum baAAdhan sukhriyyan warahmatu rabbika khayrun mimma yajmaAAoona *(Surat Az Zikhruf 43:32)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: ***Hivi jee ni wao ndio wanaogawa Rehma ya Mola wao? Ni sisi ndio tunaogawa Rehma ya Maisha yao hapa Duniani, na tumewanyanyua Darja baadhi yao miongoni mwao baadhi yao ili wawe ni wenye kuwaajiri wengine katika ajira zao. Lakini Rehma za Mola wako (Ewe Muhammad) ni bora kuliko kile wanachokikusanya.***

Na hivyo Aya ni yenye kusema kua ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie mwenye kutoa Rehma zake kwa ajili ya Waja wake kwa kuwapa Riziki zao, Ilm, Vyeo, Mali, Watoto n.k ambavyo tayari vimeshakadiriwa kwa kila Mtu hata kabla ya kuumbwa kwake. Na hivyo nimeona kua ingawa hakuna haja ya kufanya kazi, lakini inabidi kufanya kazi kwa ajili ya kutekeleza amrisho lake *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwani hio ndio sababu ya mtu kujipatia riziki yake.

Na hivyo wivu na hua hauna haja kuoneana baina ya watu, kwani unasababisha madhara makubwa, nami nimeridhika na makadirio ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yangu na hivyo hua ni mwenye kufanya kazi kwa ajili ya kujipatia riziki yangu, na hivyo kua ni mwenye kuwapenda Waislam wote nami kua ni mwenye kupendwa na kila Muislam.

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Ma-shaa Allah, una tafakkur nzuri sana, naam, ninufaishe zaidi kwa jambo la tano, jee ni lipi?'**

Imam Hatim Al Isam akasema: **'Jambo la tano ni kua mimi nimewaangalia watu na kuona kua Watu wengi huwanyenyekea watu wengine kutokana na koja kua ni wenye kuwahitaji watu hao, na hivyo watu hao hua ni wenye kuwainamia hao wanaowategemea na kuwanyenyekea, na wanaonyenyekewa nao hua ni wenye kujiona kua wao ni Bora zaid kwa kudhani kua heshima yao hio ni yenye kupatikana kutokana na kua na Mali nyingi au watoto wengi n,k, ambapo baadhi yao hua si wenye kuiheshimu neema ya heshima hio na huifanyia israfu kwa kuitumia sivyo na kwa wasiofaa wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kua:**

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقۡنَٰكُم مِّن ذَكَرٖ وَأُنثَىٰ وَجَعَلۡنَٰكُمۡ شُعُوبٗا وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓاْ

إِنَّ أَكۡرَمَكُمۡ عِندَ ٱللَّهِ أَتۡقَىٰكُمۡ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٞ﴾

Ya ayyuha alnnasu inna khalaqnakum min dhakarin wauntha wajaAAalnakum shuAAooban waqaba-ila litaAAarafoo inna akramakum AAinda Allahi atqakum inna Allaha AAaleemun khabeerun *(Surat Al Hujarat 49:13)*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Tafsir: ***Enyi watu! Hakika sisi tumekuumbeni nyinyi kutokana na Mwanamme Mmoja na Mwanamke mmoja, na tukakufanyeni kua katika mataifa na makabila mbali mbali ili mpate kujuana (na msichukiane). Kwa hakika m-bora wenu mbele ya Allah ni mwenye Taqwa zaid miongoni mwenu. Na Allah ni mjuzi wa kila kitu na ni mwenye habari ya kila mnachokifanya.***

Kwa hivyo watu wamekua ni wenye kuhadaika kutokana na Mali na Vyeo, na watoto na vitu walivyo navyo, hivyo mimi nimeamua kua ni mwenye kushikamana na Taqwa, ili niwe ni mwenye kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala ili* kuupata usamehevu wake, na kua ni mwenye kukaa mbali kutokana na makatazo yake.

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Ma-shaa Allah, hujakosea bila ya shaka, na jambo la sita, jee ni lipi?'**

Imam Hatim Al Isam akasema: **'Jambo la sita ni kua mimi nimekua ni mwenye kuwaangalia watu na kuwaona kua kutokana utofauti wa neema walizoneemeshwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi wamekua wakibaguana na kutengana baina yao, wakati mimi nimeiona ile aya isemayo:**

﴿وَقُل لِّعِبَادِى يَقُولُواْ ٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ إِنَّ ٱلشَّيْطَانَ يَنزَغُ بَيْنَهُمْ إِنَّ ٱلشَّيْطَانَ كَانَ لِلإِنْسَانِ عَدُوّاً مُّبِيناً﴾

Waqul liAAibadee yaqooloo allatee hiya ahsanu inna alshshaytana yanzaghu baynahum inna alshshaytana kana lil-insani AAaduwwan mubeenan *(Surat Al Isra 17:53)*

Tafsir: ***Na waambie Waja wangu (Walioamini) kua wawe ni wenye kusema kile kilichobora tu, kwani kwa hakika Shaytani anatafuta kuwabagua miongoni mwao baina yao, kwani kwa hakika Shaytani kwa Watu ni Adui Mkubwa sana.***

Na hivyo mimi kua ni mwenye kuona na kujua kua Shaytan ndio Adui mkubwa wa Watu kwani ni mwenye kutaka kuwagombanisha watu ili watengane kupingana kutokana na njia ya haki na iliyokua sahih, kwani Qur'an ni yenye kusema kweli hivyo sikua mimi ni mwenye kuwachukulia Waislam kua ni Maadui zangu, bali ni mwenye kuwachukulia wale maadui wa Uislam na Shaytani kua ni maadui zangu, na hivyo si kua ni mwenye kuwafuata wao kwenye njia yao hio na hivyo si mwenye kumuabudu Shaytani bali ni mwenye kuifuata njia ya Wanazuoni wa *Ahl Sunnah,* na naamini juu ya uongofu wao, kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

﴿أَلَمْ أَعْهَدْ إِلَيْكُمْ يَٰبَنِيٓ آدَمَ أَن لاَّ تَعْبُدُواْ ٱلشَّيطَانَ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ﴾

Alam aAAhad ilaykum ya banee adama an la taAAbudoo alshshaytana innahu lakum AAaduwwun mubeenun *(Surat Yasin 36:60)*

Tafsir: ***Hivi jee sikukuambieni mimi kua Enyi Ibn Adam msimuabudu Shaytani kwani yeye ni Adui yenu mkubwa sana.***

Na hivyo mimi sikua ni mwenye kua pamoja na wale wenye kuwalaghai Waislam na kua ni mwenye kutengana nao.

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Ma-shaa Allah, maneno yako matamu sana, na nufaisho la saba, jee ni lipi?'**

Imam Hatim Al Isam akasema: **'Jambo la saba ni kua, mimi nimekua ni mwenye kuwaangalia watu, na kuona kua kila mmoja wao anashughulikia kuhusiana na kula, kunywa, mavazi, makazi na kujitafutia mali na hivyo hua ni wenye kujikusanyia vitu vya haram na vyenye shaka ndani yake na kustahmilia maadhirisho na manyanyaso, wakati amesema** ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **katika Qur'an kua:**

﴿وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِى ٱلأَرْضِ إِلاَّ عَلَى ٱللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِى كِتَابٍ مُّبِينٍ﴾

Wama min dabbatin fee al-ardhi illa AAala Allahi rizquha wayaAAlamu mustaqarraha wamustawdaAAaha kullun fee kitabin mubeenin *(Surat Hud 11:6)*

Tafsir: ***Na hakuna kiumbe hata mmoja Ardhini isipokua ni kutokana na Allah riziki yake na yeye ndie mwenye kujua wapi yalipo makazi yake na malazi yake kwani kila kitu kimo kwenye Kitabu Kilichowazi.***

Hivyo bila ya shaka mimi pia ni mi0ngoni mwa Viumbe wa ***Allah Subhanah wa Ta'ala,*** **na riziki yangu imeshaahidiwa kua itashushwa, na ameamrisha nifanye kazi nami ni mwenye kufanya kazi kama alivyoamrisha, hivyo bila ya shaka naamini kua** ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **atanitumia riziki yangu.**

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Ma-shaa Allah, nipe nufaisho la nane, jee ni lipi?'** Imam Hatim Al Isam akasema: **'Jambo la nane ni kua nimewaangalia watu na kuwaona kua kila mmoja hua ni mwenye kumuamini mwengine na kumtegemea zaidi yule anaemuamini au kutegmea zaidi kile kitu anachokiamini kulingana na thamani yake, hivyo baadhi wanategemea umahiri wao katika kitu husika, wengine wanategemea kipaji chao, wengine mali zao, wengine marafiki zao, vyeo vyao n.k, wakati amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an kua:**

﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّهُۥ مَخۡرَجاً۝وَيَرۡزُقۡهُ مِنۡ حَيۡثُ لاَ يَحۡتَسِبُ وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓ إِنَّ ٱللَّهَ بَٰلِغُ أَمۡرِهِۦ قَدۡ جَعَلَ ٱللَّهُ لِكُلِّ شَيۡءٖ قَدۡراً﴾

Waman yattaqi Allaha yajAAal lahu makhrajan; Wayarzuqhu min haythu la yahtasibu waman yatawakkal AAala Allahi fahuwa hasbuhu inna Allaha balighu amrihi qad jaAAala Allahu likulli shay-in qadran *(Surat At Talaq 65:2-3)*

Tafsir: ***Na wenye kumcha Allah atawajaalia njia ya kutokea; Na atawaruzuku kutokea kule wasikokutegema na wenye kumtegemea Allah basi hua ni mwenye kumtosheleza, kwani kwa hakika Allah hua ni mwenye kukamilisha jambo lake na ni mwenye kukadiria juuya kila kitu.***
Hivyo kwa hakika mimi si mwenye kumhitaia mtu yeyote wala kitu chochote bali ni mwenye kumtumainia *Allah Subhanah wa Ta'ala peke yake tu.*

Imam Shaqiq Al Balkhi akasema: **'Ewe Hatim, namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akunyooshee mambo yako, kwani mimi nimeiangalia *Tawrat* ya Musa na Biblia ya Isa na Zabur ya Daud na Qur'an ya Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* na nimeona kua Vitabu hivi vinne vimefungamana na misingi hii minane, hivyo yeyote yule mwenye kushikamana na misingi hii minane basi hua ni mwenye kushikamana na vitabu vyote hivyo vinne.'**

Siku moja Imam Hatim Ibn Isam alikua yuko kwenye Mkusanyiko wa Watu katika mji wa Balkh ambapo nae akanyanyua mikono na kusema: **'Ya Allah! Hakika mimi nakuomba wewe kua Uwasamehe Waumini wote wale waliofanya dhambi leo hii, wenye vitabu vyeusi na waliothubutu kufanya dhambi.'** Ambapo miongoni mwao watu hao waliokuwepo hapo alikuwemo yule ambae alikua ni mwenye tabia ya kuenda kufufukua Makaburi usiku na kuwaibia maiti wasiokua Waislam wanaozikwa na vitu vya thamani ndani yake, hivyo usiku huo akaenda kama kawaida yake kufukua kaburi na alipoinga ndani yake akasikia sauti ikimwambia: **'Hivi jee wewe huoni haya kua ulia**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

nimiongoni mwa walioombewa Dua leo na Hatim' Hivyo mtu huyo akatoka mbio na kumtafuta Imam Hatim na kuomba msamaha na kisha kutubu baada yake.

Anasema Imam Muhammad Al Razi: '**Hakika mimi nilikaa kwa Hatim Ibn Isam kwa muda wa miaka na miaka, na kamwe sijawahi kumuona akiwa ni mwenye kukasirika isipokua mara moja na hii ilikua ni pale siku moja wakati mmoja kati ya Wasaidizi wa Mlango mmoja wa Duka alipokua akiambiwa Muajiri wake kua: 'Umechukua mzigo wangu hivyo nilipe' ambapo Hatim alipoona hali hio basi akamwambia yule Muajiri kua: 'Ewe Bwana mpe mda usimlazimishe kulipa sasa hivi kama hana' lakini hata hivyo Muajiri huyo akagoma**'

'**Hivyo Hatima ambae alikua amenunua Taula akakasirika na kisha akaipiga na chini, na hapo hapo chini hapo pakajaa Dhahabu na kisha kasema kumwambia Muajiri huyo kua: 'Haya chukua kulingana na thamani ya kile unamchomdai tu kutokana na dhahabu hii kilichobakia kiwachie hapo hapo' hivyo Muajiri huyo ashangaa na kisha akainama na kuchukua thamani ya kile anachodai, lakini tamaa ikamzidi hivyo akaongeza katika kuchukua kwake Dhahabu hio, na hapo hapo mkono wake ukakakamaa, na hivyo ikambidi arudisha kilichozidi'**

Mmoja kati ya Wanafunzi wake Walimuuliza Imam Hatim kwa kusema: **'Ewe Imam Hivi Ukisali hua unakua na hali gani?'**

Imam Hatim akasema: **'Unapoingia wakati wa Sala basi kwanza mimi hua ni mwenye Istighfar na kisha hua ni mwenye kutia Udhu kwa nia njema na safi yenye Ikhlas, Udhu hua ni wenye kuvisafisha Vingo vyangu, hivyo nafanya Istighfar kutoka ndani ya Moyo wangu, kisha naenda Msikitini na ninapoingia ndani yake basi Mbele yangu hua ni mwenye kuiona Masjid Al Haram na hivyo mimi hu ani mwenye kuiweka Maqam Ibrahim baina ya nyusi zangu mbili katika kuiangalia kwangu, na kisha naiweka Pepo katika upande wa kulia kwangu na kisha hua naiweka Jahannam katika upande wa kushotoni mwangun na kuiweka Sirat chini ya Nyayo zangu, na kisha hua namfikiria Malaika wa Kifo akiwa nyuma yangu. Na kuuwakilisha Moyo wangu kwa Mola wangu.**

Kisha nasema Allahu Akbar huku nikiwa na heshima kubwa sana, na mwenye kusuImam kwa utulivu wenye umakini mkubwa sana, nnasoma Qur'an kwa kiraa chenye darja ya usomaji wa mbele ya Mfalme, kisha hua Narukuu, Nasujudu na kwa unyenyekevu mkubwa sana na kukaa *Tahiyyat* kwa hali ya kua ni mwenye kujawa na Shukrani..hio ndio Sala yangu.'

Siku moja pia Imam Hatim Ibn Isam alihudhuria mhadhara ambapo walikua wanazungumaia kuhusiana na Ibada ya Sala na miongoni mwa waliohudhuria alikuwepo Isa Ibn Yusuf ambae alimuuliza Imam Hatim Ibn Isam: '**Ewe Hatim hebu tuelezee**

namna unavyosali ili tupate mfano’ ambapo Imam Hatim akasema: **‘Hakika mimi hua nnanzia kwenye kutembea kuelekea Msikitini kwa khofu upole na unyenyekevu, kisha nnapofika Msikitini huingia msikitini kwa nia yenye Ikhlasi, na nnapofunga Sala husema *Allahu Akbar* huku nikiwa na Ilm yenye kuujua ukubwa wa *Allah Subhanah wa Ta’ala*, na nnaposoma ndani yake hua ni mwenye kusoma kwa kutafakkari, hua nnarukuu kwa heshima na kusjudu kwa unyenyekevu mkubwa, nnapokaa Tahiyyat hutoa salam kulingana na Sunna ya *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* na hutoa salam yangu ya mwisho kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* na hata hivyo baada ya hapo hua ni mwenye kua na khofu kua huenda ikawa sijakubaliwa Sala yangu, na kuomba msamaha kwa Mola wangu na kuiangalia nafsi yangu huku nikiwa nimejawa na khofu ambayo hubakia nao hadi kufariki kwangu’**

Imam Hatim Ibn Isam alisikia kua kuna Mtu ambae ni mwenye Ilm ametembelea katika maeneo anayoishi, lakini ni mwenye kufanya Israfu katika kila kitu, hivyo Imam Hatim Ibn Isam akamtembelea Mtu huyo na kumwambia kua ameenda kwake kwa ajili ya kutaka kujua kuhusiana na Dini yake, ambapo Mtu huyo akamuuliza Imam Hatim Ibn Isam: **‘Jee unataka kuanza kujifunza nini?’**

Imam Hatim Ibn Asim akasema: **‘Nifundishe namna ya kutia udhu kwanza’** ambapo mtu huyo akaanza kumfundisha Imam Hatim Ibn Isam namna ya kutia Udhu na kisha akaanza kutia Udhu mbele yake kwa kila kiungo kukikosha mara 3 kama kawaida, na hivyo alipomaliza basi ikawa ni zamu ya Imam Hatim Ibn Isam ambae akawambia mtu huyo kua: ‘**Niangalie namna nnavyotia Udhu na kama nikikosea basi niambie’**
Hivyo Imam Hatim Ibn Isam akaanza kutia udhu kama kawaida lakin alipofika kwenye kukosha mikono yake basi akakosha mara 4 badala ya mara 3, hivyo mtu huyo akasema: **‘Umekosea, kwani umefanya israfu katika maji’** ambapo Imam Hatim Ibn Isam akauliza kwa kusema: **‘Wapi nilipofanya israfu?’** yule mtu akasema: **‘Mikononi umenawa mara 4 badala ya mara 3.’**

Imam Hatim Ibn Isam akasema: **‘Mimi nilifanya israfu kwenye maji kwa kukosha mkono mara nne lakini wewe mwenzangu hua unafaya Israfu katika mengi sana’** hivyo baada ya kusikia majibu hayo basi Mtu huyo akajua kua Mwanafunzi aliekuja kusoma hakua ni Mwanafunzi bali ni Mwalimu aliekuja kusomesha, hivyo mtu huyo akaingia ndani ya nyumba aliyofikia na kukaa ndani yake bila ya kutoka kwa mda wa siku 40.

Imam Hatim Ibn Isam alisema: **‘Ni vibaya kua na huzuni kwa ajili ya Dunia, na ni Vizuri kua na huzuni kwa ajili ya Akhera’**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

'Toba hua ni kuamka kutokana na mghafiliko, kwa kukumbuka Dhambi zako na kukumbuka Rehma na Makadirio ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie Mola wako'

'Mwenye Kutubu hua ni mwenye sifa nne ambazo ni: Hua ni mwenye kuulinda Ulimi wako kutokana na kusengenya, kusema uongo na kua na husda na maneno yasiyokua na maana. Hua ni mwenye kukumbuka dhambi zake; Hua ni mwenye kujisikia aibu kwa Dhambi zake na kutoona haya katika kumuomba msamaha *Allah Subhanah wa Ta'ala*; Hua ni mwenye kujitayarisha kwa ajili ya Kifo chake.'

'Kama mtu akifiwa na Mtu wa karibu yake, halafu mtu huyo aliefiwa akawa si mwenye kujifunza na kukumbuka Akhera kutokana na Kifo hicho, basi hakuna wasi wala mawaidha yatakayomfaa mtu huyo.'

'Enyi watu fahamuni kua mnapo waasi Ibn Adam wenzenu hua ni kwa sababu ya wao kumuasi Mola wao, na nyinyi mnapomuasi Mola wenu hua ni kwa sababu ya kukosa Rehma za Mola wenu.'

'Enyi watu kuweni na umakini na ndimi zenu ili muwe ni wenye kusema ukweli tu, kuweni makini na macho yenu ili muwe ni wenye kuangalia ya halali yenu tu.'

Kuna mtu aliulizwa: **'Jee uhali gani?'** ambapo nae akasema: **' Mimi ni Mzima na nilie salama'** hivyo Imam Hatim Ibn Isam akajibu: **'Usalama hauwi ni wenye kupatikana hadi pale utakapokua umeshavuka Sirat, na Afya haipatikani hadi pale utakapokua umeshaingia ndani Peponi.'**

Imam Hatim Ibn Isam alisema: **'Jaribu Kutozitamani siku zilizopita kwa sababu huwezi kuongeza Ibada zilizokupita ndani yake na wala huwezi kufanya dhambi ndani yake; Unaweza kua na kisingizio kutokana na yaliyopita, lakini kama ukiwa unatafuta kisingizio kuhusiana na yaliyopita hivi jee utawezaje kutekeleza zile haki za siku ya leo? Hivyo jee itakua na maana kutafuta kisingizio leo hii?' Fikiria kuhusiana na Kesho yake jee utaokoka au utaangamia?'**

Imam Hatim Ibn Isam alisema: **'Jihadhari na kifo ili kisikukute wakati ukiwa katika hali tatu zifuatazo: 'Katika Hali ya Kiburi, Katika hali ya Ubakhili na katika hali ya Kujisifu.'**

'Kuna aina tano za Nyoyo ambazo ni Moyo uliokufa, Moyo wenye Maradhi, Moyo wenye Mghafiliko, Moyo Uliozibwa na Moyo wenye Uiamara. Ambapo Moyo uliokufa hua ni Moyo wa Mtu mwenye Kukufuru, Moyo wenye Maradhi hua ni Moyo wa mwenye Kufanya Dhambi, Moyo wa Masikini hua ni Moyo Ulioghafilika,

Moyo wa mwenye kuasi hua ni Moyo Uliozibwa na Moyo wenye Uimara hua ni Moyo wa yule mwenye Kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

'Moyo wa mtu mwenye kuwasomesha watu Ilm na kisha mtu huyo akawa si mwenye kuifanyia kazi Ilm hio lakini hapo hapo watu wakanufaika na Ilm yake hio kwa kuifanyia kazi utakua ni Moyo wa Mtu atakaekua akijuta katika siku ya Malipo.'

'Yeyote yule anaedai kua ana mambo manne yafuatayo hua ni muongo: Kwanza ni yule anaedai kua anampenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini si mwenye kuachana na Makatazo yake, Pili ni yule ambae ni mwenye kuwadharau masikini halafu akadai kua ni mwenye kumpenda *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*; Tatu ni yule ambae asiewapa Sadaqa masikini mbali ya kua anao uwezo juu ya jambo hilo na kisha akawa anajidai kua anampenda *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Nne ni yule ambae ni mwenye kujidai kua anauogopa Moto wa Jahannam lakini akawa si mwenye kuzikimbia dhambi. '

Imam Hatim Al Asim alimuona Mtu ambae alikua ni mwenye sifa ya ubakhili sana akiwa anatoa sadaqa kwa sababu alikua anaumwa, hivyo akasema: **'Ya Allah mjaalie mtu huyu awe ni mwenye kuendelea Kuumwa kwa sababu kutoa kwake Sadaka hua kua manufaa zaidi kwake kwa ajili ya kufutiwa dhambi zake'**

Na akasema tena kua: **'Lifanye kua ni jukumu lako kujisimamia Nafsi yako katika hali tatu zifuatazo ambazo ni: 'Kukumbuka kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kukuona katika kila kitu unachokifanya, Kukumbuka kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kusikia kila kitu chako unachokisema, Kukumbuka kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kujua hali yako pale unapokua umekaa kimya.''**

Imam Hatim Ibn Asim alialikwa chakula siku moja na mmoja kati ya Wanafunzi wake. Lakini akakataa mualiko huo, na Mwanafunzi huyo akasisitiza juu ya Mualiko huo, hivyo ikabidi Imam Hatim Ibn Asim akubaliane na Mualiko huo na akatoa sharti kwakusema: **'Nitakuja lakini kwa sharti la kua nitakaa katika sehemu nitakayo na nitakula kitu nikitakacho mimi.'**

Mwanafunzi huyo akakubaliana na sharti hilo, na hivyo baada ya kuwasili kwenye mualiko na watu kukaa na chakula kuwekwa basi Imam Hatim Al Isam akanyanyuka na kumuomba mfanyakazi wa mwenyeji wake kua amletee Jiko lenye makaa ya moto na Kikaangio chake, na kisha akaondoka alipokaa akakaa sehemu ya peke yake, na Moto huyo ulipokuja mbele yake akakiweka kikaangio hicho jikoni hadi kikawa kimoto sana,

na kisha akawaambia Wanafunzi wake, kwa kusema kua: '**Hivi jee mnaamini kua katika siku ya Malipo mtasimamishwa na kuhojiwa juu ya kila mlichokila?'**

Wanafunzi wakaitikia: **'Naam tunaamini'** Imam Hatim Ibn Isam akasema: **'Sasa nilikua taka kila mmoja wenu aje mbele yangu hapa kisha aweke miguu yake humu kwenye kikaanggia na kisha aanza kujibu masuali nitakayomuuliza kuhusiana na chakula alichokula hapa katika mualiko huu.'** Wanafunzi wakashangaa na kumuangalia Imam Hatim Ibn Asim bila ya kuamini wanachokisikia, na kisha wakasema: **'La haiweekani kufanya hivyo kwetu sisi'**

Hivyo Imam Hatim Ibn Asim akawauliza Wanafunzi wake hao: **'Kama hamuwezi kufanya hivyo leo hii hapa mbele yangu Duniani, basi mtawezaje kumjibu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kesho akhera katika siku ya Malipo? Katika Ardhi ya shaba imoto pale hali itakavyokua kama inavyosema aya'**

﴿ثُمَّ لَتُسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ ٱلنَّعِيمِ﴾

Thumma latus-alunna yawma-idhin AAani alnnaAAeemi *(Surat Takathur 102:8)*

Tafsir: ***Na kisha katika Siku hio mtaulizwa kuhusiana na kila Neema mlizopewa (Duniani)***

Ambapo maneno hayo yalipelekea Mualiko huo kua wenye kua ni wa vilio kutokana na tukio hilo.

Imam Hatim Ibn Isam alifariki mnamo mwaka 237 Al Hijra.

IMAM ABU BAKR IBN WARRAQ

Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Umar Ibn Warraq alizaliwa katika ardhi ya Tirmidhi ambapo abaadae aliamia katika ardhi ya Balkhi na alisoma kwa Imam Ahmad Ibn Hadrawayhh na Imam Muhammad Ibn Ali Hakim Al Tirmidhi.

Imam Abu Bakar Ibn Warraq alikua ni mtu ambae ni mcha Mungu sana na Mwenye Taqwa, alieachana na Dunia na kila lililokatazwa na hivyo alikua akijulikana kwa jina la *Muaddib Al Awliyah.*

Imam Abu Bakr Al Warraq anasema kua: **'Mwalimu wangu Muhammad Ibn Ali Al Tirmidhii aliniambia mimi kua: 'Nataka kuenda na wewe katika sehemu fulani'**

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

hivyo nami nikamwambia : '*In-shaala Allah* hamna tataizo mimi niko moja nawe' na kisha tukafunga safari na mara tukajikuta kua tumefika katika sehemu ya Jangwa kubwa Sana.

Hili lilikua ni Jangwa ambalo lilikua na Mti mmoja ulionawiri ambao chini yake kulikua na chemchem ya Maji, ambapo pembeni yake tulimuona mtu ambae alikua amekaa kwenye kiti huku pia akiwa amevalia mavazi mazuri sana na ya kupendeza. Tulipomkaribia mtu huyo basi akasimama na kisha tukasalimiana nae na kisha akampisha Mwalimu wangu kwenye kiti chake, na baada yam da wakatokea watu wengie mmoja baada ya mmoja hadi wakafikia watu 40.

Kisha yule mtu tuliemkuta hapo mwanzoni akanyayua mikono yake juu na mara vikashuka vyakula vya aina tofauti mbele yetu kutoka Mbinguni. Kisha tukala na baada ya kumaliza kula basi Mwalimu wangu akamauuliza mtu huyo tuliemkuta baadhi ya masuali, ambapo nae mtu huyo akayajibu kwa ufafanuzi mrefu sana, na ukweli ni kua mimi sikua nikifahamau hata moja kati ya yaliyokua yakiulizwa na kujibiwa. Na baada ya mda Mwalimu wangu akaaga nasi tukaondoka'

Kisha Mwalimu wangu akaniambia: 'Ewe Abu Bakr, bila ya shaka umeshafinikiwa tayari' hivyo nami nikamuuliza: 'Ewe Mwalimu wangu kwani tulikua tumeenda katika sehemu gani mbona mimi sijawahi kuiona sehemu ile, na yule mtu ndie nani?'

Ambapo nae akasema: 'Lile ni Jangwa la Sinai, na mtu tuliekutana nae ni Nguzo ya Mawalii wa eneo hilo.' Nami nikashangaa tumefikaje katika sehemu hio kwani iko mbali sana kutoka katika sehemu tunayoishi hivyo nikamuuliza: 'Ewe Mwalimu wangu tulifikaje sisi katika Jangwa la Sinai kwa mda mfupi kiasi hiki?' ambapo nae akanielezea kilichotokea.

Imam Abu Bakar Al Warraq alikua ni mtu ambae ni mwenye hamu kubwa sana ya kukutana na Al Khidr, hivyo kila siku alikua anaenda Makaburini na kukaa na kutafakari na kisha hua ni mwenye kusoma Qur'an, hivyo moja kati ya siku hizo wakati alipokua akitoka nyumbani kwake kuelekea Makaburini, mara akakutana na Mtu mmoja mzee sana mwenye uso wenye kuvutia akiwa amesimama kwenye mlango wake, hivyo Imam Abu Bakr Al Waraq, akasita kutoka nje na kumuuliza mtu huyo: '***Salaam Alaykum wa Rahmat Allahi Wa Barakatuh*, Vipi unataka kuzungumza na mimi?'**

Mtu huyo akaitikia**: '*Wa Alaykum Salaam wa Rahmat Allahi Wa Barakatuh* naam bila ya shaka'** kisha mzee huyo akapiga hatua kuondoka kwenye Mlango wa nyumba ya Imam Abu Bakr Al Waraq huku akimuashiria kua wafuatane anakoelekea, ambako ni kule kule Mkaburini alikokusudia kuenda Imam Abu Bakr Al Waraq, na walipofika basi mtu huyo akasema: '**Mimi ndie Al Khidr, ambae uliekua na haja ya kujuana**

nae kwa mda mrefu sana, na uliposema kua utazugumza nami basi imebidi ujikoseshe sehemu ya Qur'an leo hii, na kama hii itakua ni kutokana na athari ya kutaka kwako kuzungumza na Al Khidr, hivyo jee utaathirika vipi kama ukiwa unataka kuzungumza na watu wengine wa kawaida?' Imam Abu Bakr Ibn Warraq akakaa kimya huku akiwa amepigwa na bumbuwazi hajui hata aseme nini.

Imam Abu Bakr ibn Warraq alikua na mtoto wa kiume ambae alimpeleka Madrasa kwa ajili ya kusoma Qur'an, ambapo siku moja Mtoto huyo aliporudi Madrasa alikua katika hali mbaya sana. Kwani alikua taabani baada ya kupoteza fahamu, hivyo Imam Abu Bakr Ibn Warraq akamuuliza Mtoto wake huyo ilikuaje hadi akafikia kua na hali hio? Ambapo mtoto huyo nae akasema kua:

'Leo tumesomeshwa aya isemayo:

﴿فَكَيْفَ تَتَّقُونَ إِن كَفَرْتُمْ يَوْماً يَجْعَلُ ٱلْوِلْدَانَ شِيباً﴾

Fakayfa tattaqoona in kafartum yawman yajAAalu alwildana sheeban *(Surat Al Muzamil 73:17)*

Tafsir: ***Hivi mtajilinda vipi, kama mkikufuru katika siku ambayo itawafanya Watoto kua Wazee?***

Hivyo mimi nimejikuta nikiwa na hali kama hii kutokana na maneno ya ayah hii, na kisha baada ya hapo Mtoto wake huyo akafariki Dunia.'

Hivyo Imam Abu Bakr Al Warraq akaanza kulia na kusema: '**Ewe Abu Bakr Mtoto wako ameumwa na amefariki baada ya kuisikia aya hii, wakati wewe mwenyewe umekua ukiisoma Qur'an miaka yote bila ya kuhisi chochote, hivi jee ewe Abu Bakr Una Myo wa jiwe wewe?'**

Imam Abu Bakr Al Warraq ambae alifariki mnamo mwaka 280 Al Hijra, ambapo baada ya kufariki kwake basi Wanafunzi wake Walimuona ndotoni huku akiwa analia, na alipoulizwa kwanini akawa analia basi akasema: **'Miongoni mwa watu wote Waliozikwa karibu yangu pale Makaburini ambao mnasema kua ni Waislam, basi waliokufa wakiwa ni Waislam hawafiki hata kumi'**

Imam Abu Bakr Ibn Warraq alipoulizwa: **'Hivi Jee ulipokewaje baada ya kufariki kwako?'** basi nae akasema: **'Kitabu cha Amali njema na cha Dhambi kilikabidhiwa mikononi mwangu, basi nilikiona Kitabu cha Dhambi kikiwa cheusi sana ndani yake kutokana dhambi nilizozifanya bila ya kujua, na hivyo nikashindwa**

kukisoma vizuri kitabu hicho na mara nikasikia sauti ikisema kwa ukali mkubwa sana: 'Tumeifanya Dhambi hii kua ni iliyofichikana kutokana na fadhila zetu juu yenu mlipokua Duniani, na hivyo haina haja ya kuielezea hapa, kwani tumekusamehe kutokana nayo''

Ambapo anasema Imam Bakr Ibn Sughd kua: **'Abu Bakr Ibn Warraq alikua ni mwenye kufanya Ibada sana kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu bila ya kutegemea malipo yeyote kutoka kwake'**

Alisema Imam Abu Bakr Ibn Warraq kua: '**Matabaka matatu ni bora miongoni mwa Watu: Watawala; Wanazuoni na Wenye kuachana na Dunia. Ambapo Watawala wanapoharibika basi Amani ya watu hutoweka, Wanazuoni wanapopotoka basi Imani ya Dini ya Watu hudhoofika, na pale walioachana na Dunia wanapotoka basi pia Tabia za Watu husika katika Jamii huharibika.**

Ambapo Uharibifu wa Watawala hua ni katika Ukatili wao, Uharibifu wa Wanazuoni hua ni katika Ubakhili wao katika kutoa Ilm na Uharibifu wa wenye kuachana na Dunia hua ni katika Unafiq na Kujionesha.'

'Yeyote yule atakaeridhisha Viungo vyake vya mwili kwa matamanio ya Nafsi yake hua nimwenye kupanda Mti ambao baadae hua ni wenye kuzalisha Majuto kwenye Moyo wake'

'Kuliona jambo jema na kulithamini hua ni kuonesha Heshima juu yake jambo hilo na kuonesha Shukrani kutokana na Neema yake.'

'Mimi hua ni mwenye kusali rakaa mbli kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* halafu nikisha maliza hua ni mwenye kujuta kama anavyojuta mwizi baada ya kuiba kutokana na kujiona kua sikuweza kuabudu Ipasavyo mbele yake *Allah Subhanah wa Ta'ala*'

'Sultan asiechukua malipo kutoka wa Mwanazuoni hapa Duniani hua ni mwenye kusamehewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kesho Akhera'

Jihakikishie Uadilifu baina yako na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Ukarimu na Upole baina yako na Ibn Adam wenzako'

'Kuzama kwenye Ilm Al Kallam bila ya kua na Ilm kubwa na ya kutosha huweza kukupelekea kwenye kufr.'

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

'Kuzama kwenye Tasawwuf bila ya kua na Ilm Ya Fiqh hua ni Upotovu, na kusoma Fiqh bila ya kua na Ilm ya Tassawuf hua ni Uzushi.'

'Waislam wanatakiwa wawe na Nyoyo safi, ndimi safi na kulinda heshima zao, hivyo wale wenye kukosa sifa hizi hua ni wenye kufanya Maovu, na hivyo humruhusu Ibilisi kufany atakavyo juu yao'

'Dini hutoweka pale Wanazuoni wanapokua ni waovu, kwani Wanazuoni ndio wanaoisimamisha Dini, hivyo kama Wanazuoni wakioza basi hakutokua na usimamiaji wa Dini.'

'Matamanio ya Uovu yanapomtawala Mtu basi Moyo wake mtu huyo huingia kiza na Moyo huyo huanza kubana kutokana na kuzungukwa na Kovu za Kiza, na hivyo hasira za mtu huyo hua karibu na kukosa huruma na mapenzi, na hapo mtu huanza kuchukua hatua za kuadhibu, na mtu huyo hutoka kwenye hali ya Ibn Adam na kuingia kwenye hali ya Unyama. Hua ni Ibilisi katika umbo la Ibn Adam'

'Unataka kua na Ikhlas? Basi kwanza itupilie hali ya mbali hali ya matamanio ya mapenzi ya kua kiongozi kutoka ndani ya Moyo wako, na kisha usijihesabu kua wewe uko juu zaidi ya Mtu yeyote.'

'Kinachomkaribisha Mtu kua karibu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni kumuomba kwako kila kitu chako juu yake, na kinachowafanya watu wawe ni wenye kumpenda Mtu hua ni kutohitaji kitu chochote kutoka kwao.'

'Mimi hua ni mwenye kumjua mtu mwenye kula Halali na mwenye kula Haramu kutokana na namna wanavyoamka watu katika wakati wa asubuhi, kwani mwenye kuamkahukua kaiwa na porojo nyingi basi hua ni mwenye kula haramu na mwenye kuamka akiwa na Istighfar na Dhikr Allah hua ni mwenye kula Halali.'

'*Allah Subhanah wa Ta'ala* ameuamrisha Moyo wa Mja wake kua ni wenye kuonesha Heshima kwa Nyumba yake na kua na huruma kwa Viumbe wenzake, na ameuamrisha Ulimi kua ni wenye kutamka Kalimat Tawhid na kuwa na upolle na viube wenzake, na ameuamrisha Mwili Kumuabudia yeye na kuwasadia viumbe wenzake na kua na unyenyekevu juu ya viumbe wengine'

'Fuata Nyayo za wenye Hikma na Busara, kua karibu na wenye kuachana na Dunia na kua na subira na Wajinga.'

'Daima kua makini na mambo matano yafuatayo: '*Allah Subhanah wa Ta'ala*, Nafsi yako, Ibilisi, Dunia na Ibn Adam wenzako, na ukiwa na umakini nayo basi basi utaipata furaha ya Milele, kutokana na kua ni mwenye Kutii maamrisho ya

Mola wakona kuridhia majaaliwa yake juu yako, Kupingana na Nafsi yako, Kua na Uaduia na Ibilisi adui yako, Kuachana na Dunia na kua na Huruma na Ibn Adam wenzako.’

‘Kamwe usiwe ni mwenye kutaka kua karibu na *Allah Subhanah wa Ta’ala* hadi pale utakapokua tayari kuachana na Watu, kamwe usijishughulishe na kutafakkari wakati bado unajishughulisha na Dunia, Kamwe usitake kua na Hikma na Busara wakati Moyo wako hujausafisha kutokana na kua na cheo na Darja mbele ya watu, kwani mambo haya hua hayawezekani kua ni yenye kuwepo sambamba katika sehemu moja’

‘Tabia njema hua ni katika Kuulinda Ulimi wako wakati unapozungumza, Kuulinda Moyo wako unapokua peke yako, kuilinda Koo yako kutokana na kumeza chakula cha Haramu, Kuuzuia mkono wako kutokana na kusababisha madhara, Kuuzuia mguu wako kutokana na kutembea kwako, Kuulinda wakati wako katika kila kitu chako, kwani yeyote yule asievisimamia viungo vyake hua ni mwenye kupoteza wakati wake. Yeyote yule mwenye kuutumia vizuri wakati wake na kujichunga anapokua peke yake na siri zake basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* atampa hifadhi juu ya viungo vyake.’

Alisema Imam Abu Bakr Ibn Warraq kua: **‘Moyo una sifa 6 zifuatazo: Uhai na Kifo, Afya na Maradhi, Kua macho na Kulala. Ambapo hua unakua Hai kutokana na Uogofu, Unakufa kutokana na Upotovu, una Maradhi kutokana na kuikumbatia Dunia na kujaa kiza, Hua na Afya kutokana na Usafi na Ikhlasi, Hua unaamka kutokana na Dhikr na wenye kulala kutokana na Mghafiliko.’**

‘Kufuata Matamanio ya Kidunia hua ni kwenye kusababisha matatizo hapa Duniani na kesho Akhera, hivyo kuachana na Dunia hua ni kuukaribia Ukweli wa Haki unakupelekea kupata utulivu. Mtu anaeachana na matamanio ya Nafsi yake hua ni mwenye kuepukana na matatizo yake.’

Nyoyo za waliochaguliwa hua ni safi na zenye Tabia nzuri hua ndio viongozi wa Watu, kwani huwahimiza watu katika kufanya Mema na kupelekea kuwepo kwa Amani na Usalama katika Jamii kwa kutangazia Maamrisho ya *Allah Subahanh wa Ta’ala* na kukataza makatazo yake.

IMAM ABU UTHMAN AL HIRI

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Imam Abu Uthman Said Ibn Ismail Al Hiri alizaliwa katika ardhi ya Mji wa Ray nchini Iran lakini baadae akahamia katika maeneo ya ardhi ya Nishapuri. Imam Abu Uthman Al Hiri alisoma kwa Imam Yahya Ibn Muadh, Imam Abu Hafs Al Haddad na Maimamu wengineo.

Imam Abu Uthman Al Hiri alikua na Ilm kbwa sana ya Qur'an, Hadith, Tasawwuf na Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii hivyo alikua ni mwenye kua na athari kubwa sana katika kuisambaza Ilm ya Tasawwuf na Madhhab ya Imam Al Shafii katika maeneo ya Nishapuri, na alikua mwenye kua na kiti chake maalum kutokana na Darja yake katika Msikiti mkuu wa mji huo ambacho alikua akikaa kwa ajili ya kutoa darsa zake.

Imam Abu Uthman Al Hiri alianza kujitafutia Ilm yake akiwa bado mdogo kwa kutumia ari, mapenzi na jitihada kubwa sana, na alikua anapenda kuvaa vizuri na kuvutia kila anapokua anatafuta Ilm yake hio ambapo siku moja alipokua anaenda kwenye Darsa pamoja na marafiki zake huku akiwa amevalia Kanzu yake nyeupee na Kilemba chake kipya kizuri sana.

Walipofika basi njiani walipokua wakipita kwenye sehemu ambayo ni yenye mahame ya nyumba ya zamani, walimkuta Punda akiwa amekaa maeneo hayo huku akiwa na kidonda kikubwa kilichokua kinakauka mgongoni mwake lakini hapo hapo kulikua kuna ndege ambao walikua wanamdonoa mgongo wake Punda huyo. Na hivyo kukifanya kidonda hicho kutowezekana kupona haraka badala yake.

Hivyo Imam Abu Uthman Al Hiri akajawa na hali ya kumuonea huruma sana Punda huyo kutokana na hali yake hio, na hivyo akaamua kumsogelea na kisha akavua kilemba chake hicho na kumfunga mgongoni mwake Punda huyo na kukiziba kidonda hicho, na kisha baada ya hapo akajisikia kupungukiwa na uzito wa hisia hizo, kwani tayari ameshampunguzia maumivu na adha hio Punda huyo.

Siku moja wakati Imam Abu Uthman Al Hiri alipokua kwa Imam Yahya Ibn Muadh anasoma mara katika Darsa hio wakaja Watu ambao wakawa wanazungumzia kuhusiana na Mwalimu wao ambae ni mwenye kujulikana kwa jina la Imam Shah Ibn Shujaa Al Kirmani.

Imam Shah Shujaa Al Kirmani alikua ni Mwanazuoni Mcha Mungu sana na alikua na mtoto mmoja wa kike ambae alikua ni mzuri sana, na hivyo Sultan wa Maeneo ya Kirman akawa anataka kumuoa binti yake huyo, hivyo alipoenda kuposa kwa Imam Shah Shujaa Al Kirmani, basi kabla ya kutoa Jawabu akaomba apewe mda wa siku tatu.

Na kisha Imam Al Kirmani akaanza kutembelea Miskiti ya Mji huo yote ndani ya siku tatu hizo hadi akakutana na Kijana ambae alikua akivutiwa sana na namna anavyosali kwa unyenyekevu ndani yake Sala zake, na hivyo akagundua kua huyu Kijana ndie

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

anastahiki kua Mume wa Binti yake, hivyo baada ya kumaliza kumfuatilia akamfuata na kumuuliza kama anayo familia.

Ambapo kijana huyo akasema: **‘La’**

Hivyo Imam Al Kirmani akamuuliza kijana huyo: **‘Jee unataka kuoa nikuozeshe Mtoto wa Shah Shujaa Al Kirmani?’**

Kijana huyo akashtuka na kuuliza: **‘Hivi kwanini Mtu tajiri na Mcha Mungu kama Shah Al Kirmani amuozeshe Binti yake kwa mtu masikini kama mimi nisie kua na kitu? Kwanimimi kitu nnachomiliki ni Dirham 3 tu’**

Hivyo Imam Al Kirmani akasema: ‘Mimi ndie Shah Shujaa Al Kirmani mwenyewe na nitakuozesha Binti yangu. Ambapo hizo Dirham 3 unazomiliki basi moja utaitumia kwa ajili ya Mkate na moja kwa ajili ya Miski na moja itakua ndio mahari utakayotoa’ hivyo wakakubaliana na usiku huo huo Imam Al Kirmani akamuozesha Kijana huyo binti yake.

Ambapo baada ya ndoa hio na Binti wa Imam Al Kirmani alipoingia ndani ya Nyumba ya Mumewe basi akakuta kuna Jagi la Maji na mikate iliyokauka juu ya meza, hivyo akauliza: ‘**Hii mikate imetokea wapi’**

Na kijana akajibu: ‘**Hii niliibakisha tangu jana Usiku niliiwacha kwa ajili ya kula leo’**

Baada ya kupata jibu hilo basi Binti huyo wa Imam Al Kirmani akageuka na kutoka nje, ambapo wakati anafika mlangoni basi kijana yule akasema: **‘Nilijua mimi kua Binti wa Shah Shujaa Al Kirman hatokubali kuolewa nami na hatoweza kuishi nami kutokana na Umasikini wangu.’**

Hivyo Bint huyo wa Imam Al Kirmani akajibu**: ‘Kuondoka kwangu hakuhusianani na umasikini wako, na kutokua na kitu kwako, bali kunahusiana na kukosekana uaminifu wako mbele ya Mola wako kwa kutomuamini kwako, kwani inakuaje unaweka mkate wa Jana kwa ajili ya kula leo, na kuonesha kua wewe si mwenye kuamini katika kuitegemea riziki yako ya kesho kutoka kwake.**

Na hapo hapo namshangaa Baba yangu kwa kunizuia ndani kwa mda wa miaka 20 huku akisema kua ataniozesha kwa mtu alieachana na Dunia yake, na Mcha Mungu na kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kumtegemea yeye tu, lakini badala yake ameniozesha kwa mtu ambae hawezi kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta’ala* hata kwa mkate wake wa kila siku.’

Hivyo Imam Abu Uthman Al Hiri akawa ni mwenye kusikia wanavyomzungumzia na kumsifu Mwalimu wao huyo, hivyo nae akavutiwa na Mwalimu huyo, na hivyo akaamua kuenda kwake kwa ajili ya kuanza kusoma kwake.

Hivyo Imam Abu Uthman Al Hiri akamtafuta Imam Shah Shujaa Al Kirmani na alipokutana nae akamwambia kuhusiana na azma yake ya kutaka kusoma kwake, lakini Imam Al Kirmani akamwambia Imam Al Hiri kua: **'Mimi siwezi kukuchukua na kukusomesha wewe kwa sasa hivi kwa sababu wewe uko chini ya Yahya Ibn Muadh na ndie unae mtegemea, na hivyo kua ni mwenye kulelewa kwenye hali ya mazingira ya kutojituma kwani uko katika mazingira ya kutegemea Mtu, ambapo hakuna aneishi katika hali ya kutegemea atakaeweza kuishi kwenye mazingira ya kujitolea, kwa sababu kutegemea kitu hua kunazalisha uvivu'.**

Ingawa Imam Al Kirmani alisema maneno hayo kumwambia Al Hiri kutokana na kutotaka kuonekana kua ni mwenye kujua zaid au mwenye Ilm zaidi na kumvunja Moyo Imam Al Hiri kua asiachane na Mwalimu wake mkuu hadi atakapowiva lakini Imam Al Hiri akaamua kuchukua maamuzi yake mwenyewe kwani akawa ni mwenye kuenda kwa Imam Al Kirmani kila siku na kuendelea kuomba kua nae ajumuishwe pamoja na Wanafunzi wa Imam Al Kirmani.

Hali hii ilienedelea kwa mda wa mwezi mzima, hivyo Imam Al Kirmani akaona bora amchukue Imam Al Hiri ili awe anasoma pamoja na Mwanafunzi wake, na hivyo wakawa na ukaribu mkubwa sana na urafiki baina yao.

Hivyo siku moja Imam Al Kirmani akamwambia Imam Al Hiri kua anataka atoke nae ili waende kumtembelea Imam Abu Hafs Al Haddad ambae pia ni rafiki yake wa karibu Imam Al Kirmani na anaishi katika mji mwengine ambao ni wa Nishapur.

Hivyo baada ya kukubaliana basi wakatoka wote kwa pamoja hadi kwa Imam Abu Hafs Al Haddad na baada ya kusalimiana nae na kutambulishwa nae na kukaa na kuzungumza nae kwa mda basi Imam Al Hiri, akavutiwa sana na namna anavyoishi na anavyozungumza Imam Abu Hafs Al Haddad na hivyo akataka awe Mwanafunzi wake pia, lakini sasa ikawa anajisikia vibaya kumwambia Mwalimu wake kuhusiana na jambo hilo.

Hivyo Imam Abu Uthman Al Hiri akawa ni mwenye kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kila wakati kua amjaalie kua ni mwenye kubakia katika mji huo pamoja na Imam Abu Hafs Al Haddad ili apate kusoma kutoka kwake. Imam Abu Hafs alikua ni mchangamfu na Mcha Mungu, ambapo nae pia alivutiwa na Imam Al Hiri na hivyo siku moja wakati Imam Al Kirmani na Imam Al Hiri wanakaribia kuondoka basi Imam Abu Hafs akamwambia Imam Al Kirmani kua; **'Mwache huyu kijana wako, abakie nami**

ili nipate kumpatia na Ilm niliyokua nayo mimi pia kama ulivyompatia Ilm uliyokua nayo wewe.'

Na kutokana na kua na ukaribu mkubwa sana wa kirafiki baina ya Imam Abu Hafsa na Imam Al Kirmani basi Imam Al Kirmani akashindwa kumkatalia ombi lake hilo, hususan baada ya Imam Al Hiri kuulizwa kama anataka kubakia ama la, nae akaona kua ile Dua yake aliyoiomba kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi imekubaliwa na ahivyo akajibu kua atabakia ili anufaike zaidi. Hivyo Imam Al Kirmani alipoondoka basi Imam Al Hiri akababakia na kuanza kusoma kwa Imam Abu Hafs Al Haddad.

Imam Abu Uthman Al Hiri alikaa kwa Imam Abu Hafs kwa muda mrefu akiwa anasoma na alikua akimpenda sana Mwalimu wake huyo kiasi ya kua katika Walimu wake wote aliosoma kwao, alikua ni mwenye kua tayari kuachana nao kwa ajili ya kupata Ilm kubwa zaidi kwa Walimu wengine watakaojitokeza katika maisha yake ambapo ilikua ni Imam Abu Hafs tu ndio hataki hata kamwe kuachana nae kwa ajili ya Mwalimu mwengine yeyote kutokana na anavyonufaika nae.

Lakini siku moja Imam Abu Hafs alipowambia Imam Al Hiri kua: **'Ewe Al Hiri kwa hakika sasa hivi umeshawadia wako wewe kuani mwenye kuondoka kutoka kwangu kwani tayari nimekutosheleza kwa kila ulichokua ukikihitajia kutokana na Ilm yangu. Hivyo ondoka nenda nyumbani usije tena karibu yangu.'**

Maneno haya yalimhuzunisha sana Imam Al Hiri kwani alikua akimpenda sana Imam Abu Hafs hivyo bila ya kupinga wala kusema chochote basi akanyanyuka na kuondoka mbele ya Mwalimu wake huyo, kwa kinyume nyume bila ya kumpa mgongo huku akiwa ameuinamisha uso wake chini na machozi yakiwa yanamwagika kutoka machoni mwake, hadi akatoweka mbele ya Imam Abu Hafs.

Halafu baadae usiku akarudi kwenye sehemu hio ya Darsa la Imam Abu Hafs na kuchimbo shimo ambalo aliingia ndani yake na kuhakikisha kua anapokua ndani yake hua haonekani lakini hapo hapo kua ni mwenye kuweza kusikia yanayozungmzwa na watu walio karibu yake, kisha ikawa kila siku anaenda kwenye shimo hilo na kuingia ndani yake na kujificha kabla ya kuwasili mtu yeyote kwenye Darsa hio. Ambapo ingawa alikua akidhania kua hajulikani kua yupo kutokana na kuona kua haonekani, lakini kwa upande wa Imam Abu Hafs alikua akijua na kuhisi kua Al Hiri yupo karibu yake, na baada ya kufuatailia basi akajua sehemu anayojifichia.

Hivyo siku moja baada ya kumalizika Darsa, basi Imam Abu Hafs Al Haddad akanyanyuka na kueleeka kwenye shimo alilolichimba Imam Al Hiri na kisha akafunua ufuniko wake na kisha akamtoa Imam Al Hiri kutoka ndani yake, na kumuonea huruma sana kutokana na namna wanavyopendana mtu na Mwalimu wake na hivyo Imam Abu Hafs akamwambia Imam Al Hiri: **'Basi haina haja ya kujificha wala kufukuzana**

baina yangu na yako, bali itabidi tuwe pamoja kama inavyotakiwa tuwe, hivyo utaendelea kua nami karibu zaidi kwani nimeamua kua nikuozeshe Binti yangu, jee unasemaje?'

Habari hizi zilimfurshisha sana Imam Al Hiri na hivyo hapo hapo akamkumbatia Imam Abu Hafs na kumkubalia kua mtoto wake kupitia kwa njia ya kua Mume wa Binti yake, hivyo ikafanyika harusi kubwa sana, na Imam Al Hiri akawa ni mtu wa karibu sana wa Imam Abu Hafs, kwani hakua rafiki wa karibu na Mwanafunzi tu bali alikua ni mmoja kati ya wana familia ya Imam Abu Hafs, na hivyo Imam Al Hiri akapanda Darja zaidi na kuheshimika zaidi na kua na Ilm kubwa zaidi, kwani hakuna mtu aliefikia darja kama yake katika Ilm ya Fiqh Tasawwuf katika maeneo ya Nishapuri.

Imam Abu Uthman Al Hiri akawa kinara wa Ilm ya Tasawwuf katika maeneo ya Nishapur na Khurasan, akawa na ukaribu na Imam Al Junayd, Imam Al Ruwaym, Imam Muhammad Ibn Fadhl Al Balkhi, Imam Yusuf Ibn Husayn n.k.

Aliusia kwa kusema Imam Al Hiri kua:

'Ucha Mungu wa Moyo hua ni wenye kuonekana katika hali nne zifuatazo; Unyenyekevu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala;* Umasikini mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Khofu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Matumaini mbele ya A*llah Subhanah wa Ta'ala.'*

'Furaha yako hapa Duniani hua ni yenye kukuondoshea Furaha yako pamoja na Mola wako ndani ya Moyo wako, na khofu yako juu ya wengine itakuondolea khofu yako yake kutoka kwenye Moyo wako.'

'Ibn Adam hua hakamiliki hadi pale Moyo wake utakua una usawa katika kutoa na kuzuia na katika kuheshimika na kudharaulika.'

'Rehma huteremshwa pale wanapotajwa waja wema na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndie Bwana wa Waja wema.'

Anasema Abu Husayn Ibn Waraq ambae alikua ni Mwanafunzi wa Imama Al Hiri kua:
'Katika mwaka wetu wa mwanzo wa Ilm ya Tasawuf tulikua tukifuatilia kwa umakini mambo yafuatayo ndani ya Madrasa ya Abu Uthman Al Hiri ambayo ni: Ilikua si wenye kukaa na kitu chochote kwani tunachokipata ilikua ni wenye kuwapa wale wenye shida nacho tuichopata zaidi yetu, tulikua tukilala usiku bila ya kua na chakula chochote wakati wa usiku.

Tulikua si wenye kulipiza kisasi kwa wale waliotufanyia maovu, tulikua ni wenye kuwasamehe na kuwaonesha unyenyekevu na kuwafanyia mema hadi pale hisia mbaya juu yao zitakapoondoka ndani ya nyoyo zetu.'

Anasema pia Abu Amr kua: '**Mimi nilikua namjua Abu Uthman Al Hiri, na nilikua nahudhuria darsa zake na nikawa nimeacha maovu iliyokua nikiyafanya hapo kabla, lakini sasa ikawa narudia maovu hayo hivyo nikaanza kufanya Istighfar, na kisha nikaendelea kufanya tena maovu hayo, hivyo mwisho wake nikaamua kutoenda kwa Mwalimu wangu huyo kutokana na kuona haya kwa maovu yangu hayo na nikawa namkimbia kwani hata kumuona nilikua sitaki kumuona kwa aibu.**

Katika kumkimbia kwangu basi siku moja nikashindwa kumkimbia kwani ghafla nilikumbana nae uso kwa uso, na hivyo akanisalimia na kisha akaniambia: 'Ewe Mtoto wangu usika na watu waovu ambao ni maadui zako hadi pale watu hao watakapokua wako huru na kufanya dhambi, kwani ukikutana nao katika hali ya kufanya dhambi basi wao hua ni wenye kufurahia juu ya jambo hilo, na ukiwa msafi bila ya kufanya dhambi basi wao huhuzunika, hivyo bora njoo kwetu sisi ambao ni wenye kuweza kukustahmilia na hali yako, ili maadui zako wasipate kufurahia matamanio yake.' Ambapo baada ya kuniambia maneno hayo mimi basi nikajisikia wepesi ndani ya Moyo wangu na wazo la kuendelea kufanya dhambi likawa ni lenye kufutika Moyoni mwangu.'

Safari moja Imam Al Hiri alikua akitembea njiani na mara akamuona Mlevi ambae alikua na Firimbi yake mkononi, ambapo mlevi huyo aliomuona Imam Al Hiri basi akaificha Firimbi yake hio ndani a shati lake ili isionekane na Imam Al Hiri kwani Mlevi huvyo alikua akidhania kua Imam Al Hiri akimuona katika hali hio basi atamkemea, lakini hata hivyo Imam Al Hiri alipomkaribia Mlevi huyo basi alimwambia: **'Usiwe na Khofu kwani watu wote ni sawa na Wanafunzi wote ni wamoja.'**

Na kisha akamwambia Mlevi huyo kua akishajitoharisha basi amfuate, hivyo baadae Mlevi huyo akahudhuria darsa ya Imam Al Hiri ambapo Imam Al Hiri akaomba Dua kwa kusema kua: **'Ya Allah hakika mimi nimeshatekeleza jukumu langu hivyo yaliyobakia nakuachia wewe mwenyewe umalizie'** na baada ya dua hio basi Mlevi huyo akawa ni mwenye kuhudhuria Darsa ya Imam Al Hiri na kuachana na ulevi wake.

Kuna mtu mmoja ambae alikua anaishi katika mji wa Furjan ambao upo kaskazini ya Mji wa Nishapuri , na hivyo mtu huyo alikua kila mwaka anaenda katika Ibada ya Hija, na akienda alikua ni lazima apitie kwenye mji wa Nishapuri na alikua akisikia kuhusiana na Imam Al Hiri mbali ya kua hajawahi kuonana nae. Hivyo safari moja akaona bora aende kwenye Madrasa yake akamtembelee ili apate kumjua Imam Al Hiri ndio nani.

Lakini jambo la kushangaza ni kua mtu huyo alipofika kwa Imam Al Hiri na kumsalimia. Basi Imam Al Hiri hakurudisha salamu yake hio, bali alisema: **'Hivi jee kweli kunakua kuna Ibada ya Hija ya kila mwaka kwa yule mtu ambae ni mwenye kuondoka na kumuacha Mama yake akiwa taabani anaumwa na kuondoka bila ya ridhaa yake mama huyo?'**

Baada ya kusikia meneno hayo yule mtu akasitisha safari yake ya Hija ya mwaka huo na kisha akirudi katika mji wa Furjan, ambapo alikaa hadi baada ya mwaka mmoja na kisha akaakmua kufnga tena safari ya Hija, na akampitia tena Imam Al Hiri ambae safari hii baada ya kumsalimia basi Imam Al Hiri alimpokea na kumchangamkia tofauti na hali ilivyokua katika mwaka uliotangulia hapo kabla, ambapo Mtu huyo akasema: **'Mwaka jana nilipokuja nilipokusalimia niligundua kosa langu na hivyo nikarudi kwa Mama yangu na kumsimamia na kumhudumia hadi alipofariki, hivyo naenda kwenye Ibada ya Hija na nikirudi *In-shaa Allah* nitabakia hapa kwa ajili ya kusoma kwako.'**

Hivyo mtu huyo akaenda kwenye Ibada ya Hija na aliporudia akabakia katika Mji wa Nishapuri na kua Mwanafunzi wa Imam Al Hiri.

Kuna Mtu alimwambia Imam Al Hiri kua: '**Ewe Shaykh hakika mimi hua najaribu kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Moyo wangu lakini sifanikiwi zaidi ya kumkumbuka kwenye Ulimi wangu tu.**'

Hivyo Imam Al Hiri akasema: **'Alhamd Lillah shukuru kua angalau kimoja kati ya viungo vyako kimekua na utiifu kwa Mola wako, kwani hii inaonesha kua kuna muelekeo hivyo *In-shaa Allah* viungo vyengine vitafuata muelekeo.'**

Na akasema tena kua: **'Kuipenda Dunia huondoa Mapenzi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutoka ndani ya Moyo, Khofu juu ya Kiumbe mwengine huondoa Khofu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani ya Moyo, Kumuomba mwengine zaidi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* huondoa hali ya kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani ya Moyo.'**

'Kua Mtukufu unapozungumza na Matajiri, na kua Mnyenyekvu unapozungumza na Masikini, na bila ya shaka hua ni heshima unapokua mnyenyekevu mbele ya Matajri na mnyenyekevu mbele ya masikini.'

'Mwenye kukiona kua ni kizuri kile alichokua nacho hua si mwenye kuiona kasoro iliyokua ndani yake.'

'Haiwezekani kwa mtu kua ni mwenye kuziona kasoro zake isipokua yule mwenye kujichunguza nafsi yake.'

Alisema Imam Al Hiri: **‘Jee ni nini kuepukana na yenye shubha?’**

Ambapo Imam Al Hiri akasema: ‘**Salih Ibn Hamdun alikua amesimama mbele ya rafiki yake aliekua anafariki, na rafiki yake huyo alipofariki basi Salih akazima taa iliomo chumbani humo na hivyo mkawa kiza’ hivyo akauliza: ‘Kwanini ukazima taa?’ ambapo nae akajibu: ‘Wakati mtu huyu alipokua hai basi mafuta ya taa hii yalikua yakimilikwa nae, lakini baada ya kufariki kwake basi mafuta haya yamekua yakimilikiwa na Warithi wake, hivyo tafuteni mafuta mengine muiwashe kwa ajili yake.**’

‘Kila aina ya Huzuni inayomfika Muislam hua ni Rehma, lakini Huzuni hio isiwe ni yenye kutokana na mambo ya Dhambi kwani hatakiwi kua na huzuni kutokana na kutowezekana kufanyika dhambi hizo. Hivyo huzuni nyengine zozote zisizotokana na kukosa kufanya maovu hupelekea kufutiwa kwa dhambi kwa Muislam husika na kusamehewa hata kama Huzuni hizo hazitompandisha mtu darja.’

‘Mwenye kusikia jambo jema kisha akalifanyia kazi hua ni mwenye kunufaika nalo mpaka mwisho wa maisha yake, na mwenye kulisikia jambo jema na kisha akaachana nalo hua ni lenye kusahaulika kwake kama inavyosahaulika hadith au kisa ndani ya ufaham wake baada ya mda kupita.’

Mwenye kushikama na Sunnah kwa maneno na vitendo hua ni mwenye kua na Hikma a Busara, ambapo mwenye kushikamana na matamanio ya nafsi yake hua ni mwenye kufanya Bidaa.’

‘Sijawahi mimi kuona Mtu mwenye Darja zaidi ya mwenye Tabia njema, kwani Tabia njema humpandisha Mtu Darja hapa Duniani na Kesho Akhera.’

‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifanya Ibada hadi miguu yake ilikua ikivimba kutokana na kupata Ladha ya kufanya Ibada, Yeyote yule mwenye kuonja ladha ya Ibada hua si mwenye kuchoka kutokana nayo, kwani mwenye kuchoka kutokana na Ibada hua si mwenye kumjua Mola wake isipokua kidogo tu.’

‘Adabu hua na hali mbili, hali ya ndani na hali ya nje, ambapo hali ya ndani hua nikuusafisha Moyo na Hali ya nje hua ni kuvizuia viungo kutokana na kufanya maovu.’

‘Unyenyekevu hutokana na kujijua kutojua kila kitu ndani ya ufahamu wako, kutosahau dhambi zako na kujua kua kila wakati hua unamhitaji Mola wako.’

Amesema Imam Abu Uthman Al Hiri kua: ***'Allah Subhanah wa Ta'ala*** **ni mwenye kutoa msamaha kwa Waja wake waliojidhulumu Nafsi zao kama zilivyosema aya:**

﴿وَإِذَا جَآءَكَ ٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلاَمٌ عَلَيْكُمْ كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ ٱلرَّحْمَةَ أَنَّهُ مَن عَمِلَ مِنكُمْ سُوۤءًا بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابَ مِن بَعْدِهِ وَأَصْلَحَ فَأَنَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

Wa-idha jaaka alladheena yu/minoona bi-ayatina faqul salamun AAalaykum kataba rabbukum AAala nafsihi alrrahmata annahu man AAamila minkum soo-an bijahalatin thumma taba min baAAdihi waaslaha faannahu ghafoorun raheemun *(Surat Al Anaam 6:54)*

Tafsir: ***Na watakapokuja kwenu wale walioamini Aya zetu basi waambieni Salaamun Alaykum; Mola wenu amejiandikia Rehma zake juu yake, hivyo yeyote yule atakaefanya dhambi kwa ujinga wake na kisha akatubu baada yake basi Allah Subhanah wa Ta'ala ni mwingi wa Usamehevu na mwingi wa Rehma.***

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

VYANZO VYA VITABU VILIVYOTUMIKA KWENYE KITABU

***Abjad Al-`Ulum* -** Imam Al-Qanuji.
***Al Bidayah wa An-Nihayah* -** Imam Ibn Kathir.
***Al A`lam* -** Imam Az-Zirkili.
***Al Wafi Bi Al-Wafiyyat* -** Imam As-Safadi.
***Fath Al Bari Sharh Sahih Al Bukhari* -** Imam Ibn Hajar Al `Asqalani.
***Kashf Al Mahjub* -** Imam al Hujwiri.
***Mu`jam Al Buldan* -** Imam Yaqut Al-Hamawi.
***Siyar A`lam An Nubalaa’* -** Imam Adh Dhahabi.
***Tabaqat Al Huffazah* -** Imam Jalaluddin As-Suyuti.
Tabaqat Al Fuqaha Abu Ishaq al-Shirazi.
***Tabaqat Sufiiyah* -** Imam Abd Rahman al Sulami.
Tabaqat Ash Shafi`iyyah Al-Kubrah – Imam Taqi Ad Din As-Subki.
Tabaqat Al Qurra – Imam Adh Dhahabi.
***Tadhkirat Al Huffazh* -** Imam Adh-Dhahabi.
***Tahdhib At Tahdhib* -** Imam Ibn Hajar Al Asqalani.
***Tahdhib Al Kamal* -** Imam Al-Hafizh Al-Mizzi.
***Tahdhib At Tahdhib* -** Imam Ibn Hajar Al Asqalani.
Tarikh Baghdad – Imam Al Khatib Al Baghdadi.
Tarikh Dimashq - Imam Ibn Asakir.
***Tarikh Baghdadi Aw Madinat as-Salam* -** Imam Al Khatib Al Baghdadi.
***Wafiyyat Al A`yan* -** Imam Ibn Khallikan.

VYANZO VYA MTANDAONI VILIVYOTUMIKA KWENYE KITABU

www.ehlisunnetbuyukleri.com
www.eshaykh.com
www.livingislam.org
www.muftiwp.gov.my
www.muslimheritage.com
www.sunnahmuakada.wordpress.com

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH